

# SHUHUDA — KWA — KANISA

2026 Edition

1 ♦ 2 ♦ 3 ♦ 4 ♦ 5 ♦ 6 ♦ 7 ♦ 8 ♦ 9



Uhamisho Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

[MaarifaMtandaoni.com](http://MaarifaMtandaoni.com)

[RohoYaUnabii.Org](http://RohoYaUnabii.Org)

# GOMBO LA 2





KARIBUNI, SAFARI YA KUSIKILIZA NA KUSOMA

SHUHUDA KWA KANISA

Gombo la 2

2026 Edition

New Jersey, Marekani

RohoYaUnabii. Org / RohoYaUnabii.Africa

MaarifaMtandaoni.Com

Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

KARIBUNI katika safari ya KUSIKILIZA NA KUSOMA SHUHUDA  
PAMOJA

MaarifaMtandaoni.Com ROHOyaUNABII.Org RohoYaUnabii.Africa

SHUHUDA KATIKA SAUTI- SIKILIZA SHUHUDA

Shuhuda ni magombo tisa, yenye kurasa 4738 yaliyoanza kuandikwa mwaka  
1855

Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile  
(Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

## **Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4Tsw 472)**

**Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile (Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)**

Miaka 10 iliyopita tulikutana na watu wanaosoma Shuhuda kwa Kingereza kule Dallas, Texas, Marekani, kwenye mkutano wa Vijana wa Marekani uitwao Generation of Youth for Christ -GYC (Testimonies for the Church-Revivalplan.com). Walitueleza umuhimu wa kuyasoma magombo haya na kutuhamasisha kuyasoma, hapo ndipo tulipoanza kuyasoma, tulikuwa tumesikia sura zake chache ila siyo sura zote. Tuling'amua kuwa hayakuwa na tafsiri ya Kiswahili. Nasi Tunashauri kila mtu asome magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua wiki 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com). Ukisoma au kusikiliza nusu saa kwa siku, itakuchukua miezi mine kumaliza magombo yote tisa. Tulianza kuyatafsiri kama marafiki miaka sita iliyopita, na ilituchukua muda wa mwaka, kisha tukaingia uhariri, na uhakiki.

Magombo ya Shuhuda tisa, ni kurasa 4738, ambazo zimetafsiriwa kwa ajili ya kila mwanadamu, na hasa wale watu wanaompenda Mungu na kutamani mabadiliko ya tabia. Habari hizi ni muhimu sana hivyo wewe uko huru kunakili na kusambaza kwa wengine kama zilivyo. Kwa nakala ya kidijitali ya vitabu hivi, tafadhali tembelea ***RohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Africa MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa*** au kwa Kingereza ***WhiteEstate.org***. Kugushi Maandishi ya namna hii au kuyakaba koo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Yeremia 36:27 na Ufunuo 22:18,19 na Kumbukumbu la Torati 4:9.Enendeni Mtandaoni Kote duniani.

### **Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo na kufanya tabia zetu zifae.**

Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...." Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu, na kuishi mtindo wa maisha anayotaka Bwana. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.



-Mkakati wa uamsho au Tumaini linalotiririka ni msaada mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze MUNGU na watu, katika muda ambao maadili yanayomomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili! Mpango huu kwa Kingereza utaupata katika [Revivalplan.Com](http://Revivalplan.Com)

**Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)**

'Maelfu ya watu wataoongoka kwenye ile Kweli, katika saa ya kumi na moja, AMBAO wataupata na kuukubali Ukweli wa injili na Neno la Mungu na KUHUIISHWA KWA harakati za Roho wa Mungu.—EGW'88 755 (1890). – {LDE 212.2}.' Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanamwamini Mwenyezi Mungu na kubatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuongeza ladha bila kupoteza maana, wewe boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Kila Shuhuda imehaririwa mara tano, binafsi nimepitia mara tatu. Tumeweka Pointers (2Tsw 45.5) na kadhalika ili ujhakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Sw inawakilisha, Kiswahili ambacho kinazidi kupanuka na kuwa moja za lugha za Wakristo wengi duniani. Niliona Machapisho ya Nuru kwa Kanisa ambayo sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa yenyewe kabisa kwa uzuri, japo yalichuja kurasa 4738 na kuwa 80 tu!

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. Tuna idadi ya vitabu 130 sasa. Kama umeshiriki hii kazi na jina lako halikuweka, tafadhali tujulishe, Asante

**MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI...**

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni ROHO MTAKATIFU, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika Mashariki wanahitaji pia kusoma Maandishi ya kalamu iliyovuviwa, kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la MUNGU limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 7000 kati ya 14,000, ambayo bado kufikiwa, angalia [Joshuaproject.org](http://Joshuaproject.org) na habari za '1040 window'

'Sambaza Biblia kote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la MUNGU kote.



Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lolote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe chochote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga ufalme wa Mungu, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandao ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu Afrika, basi tunabidishwa pia kuwa waandishi, Watunzi wa nyimbo, na watu wa kuhifadhi kumbukumbu zetu kwa miaka mingi, kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya Ya jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa umakini, nyimbo zilizoimbwa miaka kama 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu vya tenzi na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabuni, nasi hapa tuna nyimbo nzuri, ambazo zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu ya Biblia takatifu, na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto? Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission'-misheni iliyogeuka na kuwa kinyume cha kawaida. Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu. Watoto wetu na sisi mara zingine tunaona pengine tuwe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au tuwe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni ule waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je, viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila maandalizi hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba sio utamaduni wetu kuandika, ila sio utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Sio kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii, kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa muktadha wa Maandiko kwa Waamini ni vizuri tupatie watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti na asili ya kabila la mtu, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili, kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali, nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

## UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Shuhuda ni vitabu vya mashauri na maonyo. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na ROHO MTAKATIFU kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila

hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda [Revivalplan.com](http://Revivalplan.com) kwa lugha ya Kiingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana waamini wengu wanaishi chini ya Sahara, ambao kuna wengi wanaozungumza Kiswahili. Kwa sasa, takwimu zinaonesha kuwa Afrika ina asilimia 50% ya waamini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Miaka kama 10 iliyopita, ni asilimia 3% tu ya Maandishi ya Roho ya Unabii ilikuwa imetafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza 'fluently' katika nchi za Kiswahili ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."
2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la MUNGU
3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania
4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua zama hizo kulikuwa na mambo gani, mfano mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK zilizozungumziwa; zitakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule utakapoingia katika tovuti. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila mtu magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku ([Revivalplan.com](http://Revivalplan.com))



Wenu wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli na ndugu katika safari ya kwenda mbinguni.

Zifuatazo ni sentensi za Kalamu ya matumaini, kalamu iliyovuviwa kwa wamaani, ya Ellen White kuhusu umuhimu wa kuzisoma Shuhuda.

*1. "Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa MUNGU. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na Zao wenyewe. MUNGU ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la MUNGU kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha MUNGU kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa shuhuda rahisi na za moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka. {5T 664.3}*

2. "Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za ROHO WA MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na haya yote yamechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa". 5T 217.2

3. "Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe WAKE. "Kazi yako," Alinielekeza "Ni kubeba Neno Langu... kuchukua Neno Langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kemea kutokana na Neno, matendo ambayo sio sawa ..... Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni... "Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu." RH, Julai 26, 1906

4. Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo

yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao, kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2T 687.2}

5."Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu KUPITIA Shuhuda za ROHO WAKE. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu WAKE kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate..... Acha shuhuda Ipimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani..... Hakuna kazi ambayo ni nusu ya Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa ROHO WA MUNGU, au wa Shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za ROHO WA MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18. Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa Kweli.... FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wa Sabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za ROHO WA MUNGU. Lt156-1903

6."Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5T: 674

7."Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU ... Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ya wengi ni kwamba wanafikiri kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho... 5T: 217

8."Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, na katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, ambazo, huangaza hapa na pale kati ya wingu... RH, Agosti 30,1906

9."Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake maradufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, uasi ambao

huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Shuhuda haipaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili Kwake, ili Ukweli mzuri wa kunyenyesha uweze kuwavutia wote... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU kuwa Somo lako, na hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda.... Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia shuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa, na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili zituamshe na kuvutia akili zetu. Ili sote tusiwe na udhuru FLB: 295

10."Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika Shuhuda.... Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyonenwa kupitia chombo CHAKE alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italetu uharibifu kwa mkosaji. 5T: 678

11."Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linalowabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli.... Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili Yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

12."Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao ..... Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. ....Watunze Watu, HAO kundi la malisho Yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.' SpM: 384

13."Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu WAKE, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye kutoa tahadhari, makaripio, na maonyo..... Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu WAKE wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe KWAKE kwa kila mwale wa nuru ambao umeangazia njia yetu, ikiwa nuru hii imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo." 5T: 681

14."Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Nazijua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, "Tazama, nasimama mlangoni,

nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami..... "Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima yaonekane, na kuamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo zimewaleta watu katika hali mbaya sana, hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Watu Wa laodikia.... RH, Septemba 16, 1873

15."Hatupaswi kuogopa na kuuomba msamaha ulimwengu kwasababu ya kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo. Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi mahitaji ya wanadamu na malaika (1Wakor 4:9) kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wa Sabato hawawezi kufanya mapatano yoyote udunia. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Kweli za msingi za Neno la MUNGU ... Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu wote, Amri za MUNGU na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

16."Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri wanadamu, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa Ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo za kutoa nuru mpya, bali kuisitiza kwa uwazi kwenye moyo, Ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa. Wajibu wa mwanadamu kwa MUNGU na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la MUNGU, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali MUNGU kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa, na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5T 665.1}

17. "Kiburi, kujipenda, ubinafsi, uchoyo, chuki, husuda na wivu vimefunika kwa ukungu, nguvu za ufahamu, na ile Kweli, ambayo ingewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu. Ie Kweli Imepoteza uwezo Wake-Bwana wa kuchangamsha moyo, na kudhibiti akili. Kanuni muhimu sana za ucha Mungu na ibada, hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda hazijaletwa ili kulipuuzia Neno la MUNGU, bali kuliinua juu na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kugusa mioyo ya watu wote. {5T 665.2}

18,"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la MUNGU linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo MUNGU amewawekea hizi kuta kwa ajili ya

maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za MUNGU, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa MUNGU kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo ile nuru ambayo imekwishakutolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini ninyi hamjaithamini, mmeikanyaga, na wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, ni wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo MUNGU ameridhika kuwapatia. {5T 666.1}

Shuhuda zina Kila HALI NA mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake, tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kuziona uso kwa Uso, Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

1. Alex Ngamije -PreciousPresentTruth.org Rwanda
2. Stephen Letta-Masasi, Tanzania
3. Samuel Mhololo -Kigoma, Tanzania
4. Musa Budodi -Shinyanga Tanzania
5. Isack Msusu-Kigoma, Tanzania
6. Mr and Mrs Kumbuka Mlazi Misibo -Kigoma, Tanzania
7. Aimu Abayo –Morogoro, Tanzania
8. Zablon Mgonja -Arusha, Tanzania
9. Mwalimu Peter Marwa -Mwanza, Tanzania
10. Faustine Momadi Mkama -Dar Es Salaam, Tanzania
11. Paul Masaka -Oklahoma, Marekani
12. Ibrahimu Makamba-Tarime, Tanzania
13. Geoffrey Herman -Manyara, Tanzania
14. Pendo Makori -Visiga, Tanzania
15. Judi Mmari Mugane -Siha, Tanzania
16. Kikundi cha Mbaki/Ngulu Maombi -TAUS—USA
17. Women Prayer Warriors WPM -California, Marekani
18. Ezekiel Ojwang -Kiterere, Tanzania
19. John Mugane -Nakuru, Kenya
20. Sandra Barron -Kentucky, Marekani



21. Eliphas Sambeke -Arusha, Tanzania
22. Stefano Kasiri -Kibaha, Tanzania
23. Gideon Christian - Ukerewe, Tanzania
24. Musa Muneja -Bariadi, Tanzania
25. Victoria Swai Mhololo -Arusha, Tanzania
26. Julius Letta -Morogoro, Tanzania
27. John Chilala Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
28. Milinje Bariki Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
29. Mbaraka Hamisi -Kilimanjaro, Tanzania
30. Rachel Akinyi Atandi-Nairobi, Kenya
32. Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania
33. James Ongoro- Mara, Tanzania
34. Basanthi Thavamani-Lazar -Madras, India
35. Ndege Aruya-Rorya, Tanzania
36. Kwandu Kasiri -Pwani, Tanzania
37. Elinath Elisante Kukome -Kilimanjaro, Tanzania
38. Sharifa Athuman Seleman -Dar-es-Salaam, Tanzania
39. Jackson Musa Singano -Dar-es-Salaam, Tanzania
40. Daniel Masaka -Kisii, Kenya
41. Ellen Nyangoye- Nyagori-Rorya, Tanzania
42. Fares Ogilo-Rorya, Tanzania
43. Walter Nehemia -Dar Es Salaam, Tanzania
44. Gerard Nyafanga -Mara, Tanzania
45. Bilionea Wayoga-Rorya, Tanzania
46. Bettie Magesa Muasya-Machakos, Kenya
47. Kilango Makala -Kilimanjaro, Tanzania
48. Loyce Pima -Bunda, Tanzania
49. Niwaeli Mburuja -Hedaru, Tanzania
50. Cindy Tustch -Washington, Marekani
51. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
52. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
53. John Ngasa -Mwanza, Tanzania
54. Methusela Mahumbi-Bariadi, Tanzania
55. Elmad Daudi Ndonga-Mombasa, Kenya
56. Luck Rahim Datoo -Arusha, Tanzania
57. Ruth Lilian Bango -Arusha, Tanzania
58. Mohammed Mboi -Kisii, Kenya
59. William Kalokaza-Rukwa, Tanzania
60. Eline Mrema-Kilimanjaro, Tanzania
61. Obed Lissi-Baraton, Kenya
62. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
63. Emmanuel Oola-Rorya, Tanzania

64. Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
65. Mr and Mrs Weber- Alaska, Marekani
66. Eliakim Mabula-Bariadi, Tanzania
67. Ngusa Mayunga-Rukwa, Tanzania
68. Evans Mobegi-Kisii, Kenya
69. Debbie Bisheli-Nairobi, Kenya
70. Yunus Tiras-Tarime, Tanzania
71. Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
72. Ibrahimu Ibare-Tarime, Tanzania
73. Ghati Matiko-Tarime, Tanzania
74. Haron Wamboa-Machakos, Kenya
75. Timothy Misungwi-Michigan, Marekani
76. Enoc Omosa-North Carolina, Tanzania
77. Filipo Lubua-Pittsburg, Marekani
78. Gibson Mujuni-Kagera, Tanzania
79. Mickey Marr-Scranton, Marekani
80. Lisa Lothian-New York, Marekani
81. Azizi Jacob-Niassa, Mozambique
82. Robert Ndinayo-Goma, Congo
83. Eduardo Punda-Beira, Mozambique
84. Kasereka Mbilika-Goma, Congo
85. Mmaliro Congo-Goma, Congo
86. Yunus Tiras Magira-Tarime, Tanzania
87. Nasra Idrissa Oola-Lushoto, Tanzania
88. Daudi Jabez Masaka-Pennsylvania, Marekani

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa***  
***RohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Net, RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***

Shuhuda zina Kila hali au mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kumwona Mwokozi uso kwa Uso, na kuziona Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. **MARANATHA** Wapendwa wa BWANA! Amina  
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

Wanzilishi wa Huduma Grace Momadi Masaka, Daniel Masaka, Paul Masaka na Daudi Masaka-New Jersey, Marekani

Uhamishoni.Ughaibuni.Mtandaoni.Majumbani

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

**Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)**

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa***  
***RohoYaUnabii.Org RohoYaUnabii.Net, RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***  
Daniel Masaka and Grace Momadi Masaka -New Jersey, Marekani

GOMBO LA 2

Uhamishoni.Ughaibuni.Mtandaoni.Majumbani

2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia tabia, uamsho na matengenezo.

**Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4Tsw 472)**

### YALIYOMO

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI.....

UTANGULIZI.....

KIPINDI CHA GOMBO LA 2.....

UTANGULIZI.....

SURA YA 1

RAMANI YA UZOEFU.....

SURA YA 2

KUTENDA KWA AJILI YA KRISTO.....

SURA YA 3

KUUZA HAKI YA UZALIWA WA KWANZA.....

SURA YA 4

KUNENA MABAYA.....

SURA YA 5

UBINAFSI NA KUPENDA ULIMWENGU.....

SURA YA 6

VYAKULA VYA NYAMA NA VICHOCHEO.....

SURA YA 7

KUPUUZA MATENGENEZO YA AFYA.....

SURA YA 8

UPENDO KWA WAKOSAJI.....

SURA YA 9

DINI YA KILA SIKU.....

SURA YA 10

MATENGENEZO NYUMBANI.....

SURA YA 11

DHAMIRI ILIYOKIUKWA.....

SURA YA 12

MAONYO NA MASHUTUMU.....

SURA YA 13

KUSUDI LA USHUHUDA BINAFSI.....

SURA YA 14

KUHAMIA BATTLE CREEK.....

SURA YA 15

TAHADHARI KWA WAHUBIRI.....

SURA YA 16

MTAZAME YESU.....

SURA YA 17

KUJITENGA NA ULIMWENGU.....

SURA YA 18

UPENDO WA KWELI.....

SURA YA 19

VICHEKESHO KATIKA TAASISI (MABURUDISHO NA HATA  
VITU KAMA KATUNI).....

SURA YA 20

KUUPUZIWA KWA HANNAH MORE.....

SURA YA 21

MAOMBI KWA WAGONJWA.....

SURA YA 22

USHUJAA NDANI YA MTUMISHI.....

SURA YA 23

UDANGANYIFU KATIKA BIASHARA.....

SURA YA 24

KUNYANYASA WAAJIRIWA.....

SURA YA 25

KUGOMBANA KUMEKATAZWA (KUBISHANA).....

SURA YA 26

WACHUKUA MIZIGO KATIKA KANISA.....

SURA YA 27

KIBURI NDANI YA VIJANA.....

SURA YA 28

HALI YA UDUNIA KATIKA KANISA.....

SURA YA 29

MATESO YA KRISTO.....

SURA YA 30

MAONYO KWA KANISA.....

SURA YA 31

KUTAFAKARI NDOA.....

SURA YA 32

HATARI YA UTAJIRI.....

SURA YA 33

ARI YA KIKRISTO (CHRISTIAN ZEAL).....

SURA YA 34

WAJIBU WA VIJANA.....

SURA YA 35

WATUMISHI WA MALI.....

SURA YA 36

KUONGOZWA NA HISIA NA KUENZISHA WENZI.....

SURA YA 37

UKALI KATIKA KUSIMAMIA FAMILIA.....

SURA YA 38

BARUA YA SIKU YA KUZALIWA.....

SURA YA 39

UDANGANYIFU WA UTAJIRI.....

SURA YA 40

VIJANA WANAJOJIDANGANYA WENYEWE.....

SURA 41

WONGOFU WA KWELI.....

SURA YA 42

WAJIBU WA MME NA MKE.....

SURA YA 43

BARUA KWA KIJANA YATIMA.....

SURA YA 44

MWANACHAMA ASİYETAWALIKA.....

SURA YA 45



FARAJA KATIKA MATESO.....  
SURA YA 46  
ROHO YA UBINAFSI NA UDIKTETA.....  
SURA YA 47  
MSIKILIZAJI MSAHAULIFU.....  
SURA YA 48  
TIBA YA HISIA DANGANYIFU.....  
SURA YA 49  
WAJIBU KWA YATIMA.....  
SURA YA 50  
MWITO KWA WACHUNGAJI.....  
SURA YA 51  
KUCHAFUKA KWA MAADILI.....  
SURA YA 52  
KUWA NA KIASI KWA MKRISTO.....  
SURA YA 53  
USHUPAVU ULIOPITILIZA KATIKA MATENGENEZO YA AFYA.....  
SURA YA 54  
HISIA ZA NGONO KWA VIJANA.....  
SURA YA 55  
UPENDO WA KWELI NYUMBANI.....  
SURA YA 56  
UMUHIMU WA KUJITAWALA.....  
SURA YA 57  
STADI ZA KAZI NA UCHUMI.....  
SURA YA 58  
KUCHOCHEA UPINZANI.....

SURA YA 59

WITO KWA KANISA.....

SURA YA 60

MSALABA KATIKA KUIKUBALI KWELI.....

SURA YA 61

HOTUBA KWA WACHUNGAJI.....

SURA YA 62

MAZOEZI NA HEWA.....

SURA YA 63

UBINAFSI WAKARIPIWA.....

SURA YA 64

USHABIKI NA UJINGA.....

SURA YA 65

BINTI ALIYEJIINGIZA KWENYE ANASA.....

SURA YA 66

KWA MKE WA MTENDAKAZI.....

SURA YA 67

UWAKILI USIO NA UAMINIFU.....

SURA 68

MAKOSA YA KUHISIA.....

SURA YA 69

MAKUTANO.....

SURA YA 70

MIKUTANO YA KIJAMII.....

SURA YA 71

JE, TUITUNZEJE SABATO?.....

SURA YA 72

MABURUDISHO YA KIKRISTO.....

SURA YA 73

NDOTO YA KUVUTIA.....

SURA YA 74

MIKUTANO YETU YA MAKAMBI.....

SURA YA 75

NDOTO KUU.....

SURA YA 76

TABIA NA MAVAZI YA WATUMISHI/WACHUNGAJI.....

SURA YA 77

UPENDO WA MALI.....

SURA YA 78

KUSUDI HUKO VERMONT.....

SURA YA 79

KUHAMISHA HAZINA YA KIDUNIA.....

SURA YA 80

HAKUNA REHEMA BAADA YA KRISTO KUJA.....

SURA YA 81

UWAJIBIKAJI KWA NURU ILIYOPOKELEWA.....

## KIPINDI CHA GOMBO LA 2

WAKATI GOMBO LA KWANZA (1) LA SHUHUDA LINAJIKITA KWENYE KUWASILISHA USHAURI AMBAO KWA SEHEMU KUBWA ULIKUWA UNAWEKA MSINGI NA KUENDELEZA MAFUNDISHO, UZOEFU, NA SHUGHULI ZA KANISA JIPYA LA MASALIO LILILOANZISHWA. GOMBO LA 2 KARIBU LOTE LINAJIHUSISHA NA IBADA YA KICHO KWA WAUMINI WAKE. WAKATI WA MIKA KUMI NA TATU ILIYOENDA SAMBAMBA NA MACHAPISHO YA SHUHUDA KUMI NA NNE AMBAZO SASA ZINAENDA KUUNDA GOMBO LA KWANZA (I). KAZI YA UCHAPAJI ILIIMARISHWA, KANISA LILIPANGWA/LILIUNDWA (ORGANIZED), MFUMO WAKE WA FEDHA ULIANZISHWA, NA LILIKUWA LIMEANZA MPANGO IMARA WA AFYA. WAKATI CHAPISHO LA MWISHO LINAANDIKWA, MACHAPISHO YALIKUWA YANAMIMINIKA MFULULIZO KUTOKA KWENYE MITAMBO YAKE YA UCHAPISHAJI YA REVIEW AND HERALD HUKO BATTLE CREEK, MICHIGAN, NA JIRANI PIA, SANITARIUM MPYA ILIYOANZISHWA ILIKUWA INAFANYA KAZI KIKAMILIFU. SIKU ZA GIZA ZA MIKA YA VITA VYA WENYEWE KWA WENYEWE ZILIKUWA ZIMEPITA (1861-1865), NA KWA KANISA ZILIKUWA SIKU ZA FURSA. JUKUMU LILILOKUWEPO MBELE ILIKUWA KUIMARISHA KAZI ILIYOFANYIKA NA KUPANUA MIPAKA ZAIDI. LA MUHIMU KATIKA MAFANIKIO YA KANISA YALİYOKUWA YANAENDELA ILIKUWA UADILIFU WA WASHIRIKI WAKE MMOJA MMOJA.

MAPEMA MWAKA 1868, KAMA ILIVYOELEZWA KATIKA CHAPISHO AMBALO SASA LINAPATIKANA MWISHO WA GOMBO LA KWANZA (1), MAMA ELLEN G. WHITE ALIANZA KUCHAPISHA KWA FAIDA YA KANISA KWA UJUMLA, BAADHI YA SHUHUDA BINAFSI AMBAZO HATA WAKATI HUO ZILIKUWA KIMSINGI HAZIJASAMBAZWA. KUHUSIANA NA HIZI SHUHUDA BINAFSI ALISEMA: "ZOTE ZINA MAONYO NA MAAGIZO ZAIDI AU KIDOGO AMBAYO YANAHUSU MAMIA AU MAELFU YA WENGINE AMBAO WANA HALI ZA KUFANANA NA HIZI. HAWA WANAPASWA KUWA NA NURU AMBAYO MUNGU

AMEONA INAFAA WAPEWE AMBAYO INAKUTANA NA MAHITAJI WALIYO NAYO” GOMBO I, UKURASA. 631.

MAAGIZO HAYO YALILENGA WATU BINAFSI AMBAO WALIKUWA WASHIRIKI WA KANISA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YAANI FEBRUARI, 1868, HADI MEI, 1871, MAAGIZO HAYO YANA KARIBU MAMBO YOTE YALIYOMO KATIKA SHUHUDA NAMBA 15-20, AMBAYO SASA YAPO KATIKA GOMBO LA PILI (2). MAELEKEZO YAKO WAZI, NI YA MOJA KWA MOJA, MAKINI NA RAHISI KUYAFANYIA KAZI, YAMEHUSISHA KILA NYANJA YA UZOEFU BINAFSI NA MIVUTO YA DINI, KUTOKA USENGENYAJI, KUTOKUWA NA KIASI KATIKA ULAJI AU ULAFI, MAHUSIANO YA NDOA HATA BIDII ILIYOPOTOKA, TAMAA YA UTAJIRI, NA USHUPAVU WA DINI. MWANZONI MWA KIPINDI CHA NYAKATI ILIYOHUSIANA NA GOMBO LA PILI (2) MZEE NA MAMA WHITE WALIKUWA KWA KIASI FULANI WAMESTAAFU KWA NAMNA FULANI KULE, GREENVILLE, MICHIGAN, KUTOKANA NA HALI YA AFYA YA MZEE WHITE. PUNDE WALIANZA TENA SHUGHULI YAO KATIKA KUSAFIRI NA KUFANYA MIKUTANO NA WAUMINI KATIKA MAJIMBO YALIYOKABILI JIMBO LA MICHIGAN. MWEZI WA NOVEMBA, 1868, WALIRUDI BATTLE CREEK NA KUFANYA MAKAZI YAO HAPO (UMBALI WA MAKAO HAYA MAWILI ULIKUWA KAMA MAILI 70).

MIEZI MIWILI MAPEMA, SEPTEMBER YA 1868, MKUTANO WA KAMBI ULIFANYIKA WRIGHT, MICHIGAN. KUSANYIKO HILI, LA KWANZA LA AINA YAKE, LILITHIBITISHA BARAKA KUBWA KWA WATU WALIOHUDHURIA KIASI KWAMBA MIAKA ILIYOFUATA ILISHUHUDIA KUENZISHWA KWA MIKUTANO YA KAMBI KAMA SEHEMU YA KAWAIDA YA PROGRAMU ZA KONFERENSI ZA MAJIMBO. UWEPO WA MZEE NA MAMA WHITE ULIHIMIZWA. HIVYO IKATOKEA KWAMBA MIEZI YA JOTO ILIYOFUATA WALIITUMIA ZAIDI KATIKA MIKUTANO HII YA MWAKA. KATIKA SEHEMU YA MWISHO YA GOMBO LA PILI (2) MASHAURI YAHUSUYO MIKUTANO HIYO YA MAKAMBI YANAWENZA KUPATIKANA HUMO.

KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU KILICHOMO KWENYE GOMBO LA PILI (2) KULIKUWA NA MAENDELEO YA KUTIA MOYO KUHUSIANA NA UKWELI WA LEO. TAASISI YA AFYA YA BATTLE CREEK, IKIWA

IMEPITIA KIPINDI CHA KUKATISHA TAMAA KWA KUDONDOKA KWA UCHUMI WA DUNIA, SASA ILIKUWA IMEINGIA KATIKA KIPINDI CHA USTAWI. MWISHONI MWA MWAKA 1868 WAZEE J. N LOUGHBOROUGH NA D. T BOURDEAU WALIWASHA MWENGE WA KAZI YA INJILI KWA WAUMINI WA KANISA LA SEVENTH DAY ADVENTIST HUKO PWANI YA PACIFIC. MWAKA HUO HUO KIKUNDI CHA WATU 50 WANAOTUNZA SABATO HUKO ULAYA WALIANZA KUWASILIANA KWA BARUA NA NDUGU WA MAKAO MAKUU YA KANISA-GENERAL KONFERENSI (GC) HUKO BATTLE CREEK, NA MWAKA ULIOFUATIA WALITUMA MWAKILISHI KUVUKA BAHARI NA KUJA KUSIHI WAMISHENARI WATUMWE KWAO.

LAKINI, PAMOJA NA MAFANIKIO NA JITIHADA ZA MAENDELEO HAYA, ADUI ALIENDELEA KUFANYA KAZI YA KUPUNGUZA UKUAJI WA KIROHO WA WASHIRIKI WA KANISA, ILI KUWAWAFANYA WAPENDE ULIMWENGU NA VIVUTIO VYAKE, KULETA KANISANI CHACHU YA ROHO YA UKOSOAJI, KUKAUSHA CHEMICHEMI YA UKARIMU, NA HASA KUWANASA VIJANA Wawe CHINI YA SAFU YAKE. KUKABILI MIENENDO HII HATARI, MAMA WHITE, KAMA MJUMBE WA MUNGU, ALIKUWA MWAMINIFU NA ALIYEJITOA KULETA JUMBE KWA SAUTI NA KALAMU, AKIWAITA WASHIRIKI WA KANISA KUISHI KWA KIWANGO CHA MUNGU CHA UADILIFU NA HAKI.

KUNA BAADHI YA NYAKATI MAMA/BIBI WHITE ALIPEWA MAFUNUO KUHUSU UZOEFU BINAFSI WA IDADI YA WATU KADHAA KATIKA KANISA MOJA. ALIPOKWISHA KUWAPA WATU HAWA SHUHUDA ZAO BINAFSI KWENYE MIKUTANO, ALIENDA KUANDIKA BAADAYE MAELEZO HAYO NA KUYATUMA KWENYE MAKANISA YAO MAHALIA. MAWASILIANO KADHAA YA NAMNA HII NDIYO YANAYOPATIKANA KWENYE GOMBO LA PILI (2).

MSOMAJI MAKINI WA HILI GOMBO HILI LA KURASA 711 LAZIMA ATAVUTIWA SIYO TU NA MADA TOFAUTI ZINAZOZUNGUMZIWA, ILA PIA WINGI WA MAANDISHI YALIYOTOLEWA YAHUSIANAYO NA SHUHUDA BINAFSI KWA MUDA MFUPI HUU, ILA LAZIMA IKUMBUKWE KWAMBA SHUHUDA HIZI ZILICHOCHAPISHWA ZILIWAKILISHA SEHEMU TU YA MAANDISHI YALIYOANDIKWA NA BIBI

WHITE KWA KIPINDI HIKI. WIKI CHACHE KABLA YA KUONEKANA KWA NAMBA 15. MZEE WHITE ALIWAANDIKIA BARUA REVIEW AND HERALD, AKIWAAMBIA WALE AMBAO WALIPEWA SHUHUDA ZAO KWA MDOMO NA MAMA WHITE WASUBIRI KWA UVUMILIVU MPAKA WAPATE NAKALA ZA MAANDISHI. KUHUSU BIDII NA UVUMILIVU WA MAMA WHITE KATIKA KAZI HII, ALISEMA: "KATIKA SEHEMU HII YA HUDUMA YAKE, ANA KAZI YA MIEZI MIWILI MIKONONI MWAKE. KWENYE ZIARA YAKE YA MASHARIKI ALIBORESHA MUDA WAKE WOTE WA KUPUMZIKA KWA KUANDIKIA SHUHUDA HIZO. HATA MARA ZINGINE ALITUMIA MIDA YA MIKUTANO KUANDIKA, WAKATI WENGINE WALIKUWA WAKIHUBIRI AU KUZUNGUMZA. TANGIA AMERUDI AMEUMIZA AFYA NA NGUVU ZAKE KWA KUWA FARAGHANI PEKE YAKE, KARIBU NA KAZI HII. KWA KAWAIDA ANAANDIKA KUANZIA KURASA ISHIRINI MPAKA AROBAINI KILA SIKU. - REVIEW AND HERALD, MACHI 3, 1868. TUNaweza KUFIKIRIA JINSI AMBAVYO MAMA WHITE ALIVYOKUWA NA AHUENI KWENYE UTOAJI WA USHUHUDA NO. 15 NA SHAUKU YA KUJIPATIA MAPUMZI KO YALIYOHITAJIKA SANA, LAKINI SIKU KUMI BAADAYE ALIKUWA AMESHAJITOSA KATIKA JUKUMU LA KUTAWANYA JUMBE NYINGI ALIZOKABIDHIWA. JIONI YA, JUNI 12, ALIKUWA BATTLE CREEK ANAZUNGUMZA "KWA VIJANA KWA UJUMLA," NA ALIKUWA "AMESHAZUNGUMZA BINAFSI NA WATU KADHAA," MPAKA KARIBU NA SAA NNE USIKU KAMA ILIVYORIPOTIWA NA MZEE WHITE": "ALIPOKUWA ANAZUNGUMZA KWENYE MIMBARI, KWA ADHIMA, UNYENYEKEVU NA KWA KUVUTIA, NGUVU ZA MUNGU ZILIMJIA, NA PAPO HAPO ALIANGUKIA KWENYE ZULIA KWA MAONO. WENGI WALISHUHUDIA JAMBO HILI KWA MARA YA KWANZA, NA KUSHANGAA, NA KWA KURIDHIKA KIKAMILIFU KWAMBA HIYO ILIKUWA NI KAZI YA MUNGU. MAONO YALIDUMU DAKIKA ISHIRINI." - REVIEW NA HERALD, JUNI 16, 1868.

KWA HESABU HALISI KURASA 120 ZA SHUHUDA ZA GOMBO LA PILI (2) ZINAELEZWA WAZI KUWA ZIMEANDIKWA KUTOKANA NA MASHAURI YALIYOTOLEWA KATIKA MAONO HAYA YA JUNI 12, 1868, KWA KANISA AU KWA AJILI YA WATU BINAFSI. KURASA ZAIDI ZILIANDIKWA KUELEZEA MAONO YALIYOTOLEWA MWAKA ULE HUKO PILOT GROVE, IOWA, OKTOBA 2, NA KWENYE KITUO CHA ADAMS,

NEW YORK, OKTOBA 25. MAONO HAYA MENGI YALIPELEKEA MAMA WHITE KUANDIKA BILA KUKOMA. KATIKA KUTOA RIPOTI YA SAFARI YAO KWA BOTI KWENYE MTO WA MISSISSIPPI MNAMO 1870, MZEE WHITE ALIANDIKA MAONI:

"MAMA WHITE ANAANDIKA. MASIKINI HUYU MWANAMKE! ANAANDIKIA BILA KUKOMA KWA HUYU NA KWA YULE, WAKATI AMBAPO ANAPASWA KUPUMZIKA NA KUFURAHIA UZURI WA MAHALI NA JAMII YENYE WATU WA KUPENDEZA, INAONEKANA VIBAYA, LAKINI MUNGU ANABARIKI NA KUSIMAMIA, NA LAZIMA TUCHUKULIANE NALO HIVYO" - REVIEW AND HERALD, JULAI 5, 1870.

NI BARAKA KIASI GANI KWAMBA HIZI SHUHUDA NYINGI KWANZA ZILIZUNGUMZA KWA WATU BINAFSI NA SASA ZIMEKUWA KANISANI. JE, NI MSHIRIKI GANI AMBAYE AKISHAKUSOMA MASHAURI YA TAFAKARI NA MAONYO, HAJAGUNDUA BADO KUWA HAYA MATATIZO, MAJARIBU, NA FURSA ZA WAADVENTISTA WA SABATO WA AWALI NI SHIDA, MAJARIBU, NA FURSA ZAKE LEO PIA. TUNATHAMINI JUMBE HIZI HASWA KWA SABABU MAMA ELLEN G. WHITE MWENYEWEE ANAPOTOA UTAMBULISHO KATIKA UTANGULIZI WAKE UNAOFUNGUA GOMBO LA PILI (2) ANASEMA: "HAKUNA NJIA YA ANA KWA ANA NA YENYE NGUVU YA KUWASILISHA KILE AMBACHO BWANA AMENIONYESHA."

Wadhamini Wa Machapisho Ya Ellen G. White.

## UTANGULIZI

Ndugu na dada zangu hawatatarajia namba hii ya Shuhuda yangu hivi karibuni. Lakini nilikuwa tayari na shuhuda nyingi binafsi, na zingine zimetolewa katika kurasa zinazofuata. Na sijui njia bora ya kuwasilisha maoni yangu juu ya hatari na makosa ya jumla, na wajibu wa wote wanaompenda Mungu na kushika amri Zake, kuliko kwa kutoa shuhuda hizi. Pengine hakuna njia ya moja kwa moja na yenye msisitizo ya kuwasilisha kile ambacho Mungu amekionesha kwangu. {2Tsw 9.1}



Ilionekana ni muhimu kwamba Shuhuda namba 14 inapaswa kuwafikia siku kadhaa kabla ya mkutano wa Halmashauri Kuu (General Conference). Kwa hivyo namba hiyo iliharakishwa kupitia vyombo vya uchapishaji kabla sijapata muda wa kuandaa mambo muhimu yaliyokusudiwa kwa ajili yake. Kwa kweli, hakukuwa na nafasi ya jambo hili katika Namba 14. Kwa kuwa nilikuwa na mambo ya kutosha kwa ajili ya Namba 15, ninawasilisha kwenu kwa maombi kwamba baraka za Mungu zitaambatana nalo kwa faida ya watu Wake wependwa. {2Tsw 9.2}

Trebuchet MS

## **SURA YA 1**

### **RAMANI YA UZOEFU**

Kuanzia Februari 7, 1868, hadi Mei 20, 1868

## **Sura ya Kwanza – Mchoro wa Uzoefu**

Kuanzia Februari 7, 1868, hadi Mei 20, 1868

Baada ya kufika nyumbani kwetu na hisia za safari, na kufanya kazi zilipoisha, tulifikiria kwa busara zaidi kuhusu uchovu wa safari yetu ya mashariki. Wengi walikuwa wakinihimiza kwa barua niandike kile nilichowaambia juu ya kile Bwana alikuwa amenionyesha kuhusu wao. Na kulikuwa na wengine wengi ambao sikuwa nimezungumza nao ambao kesi zao zilikuwa muhimu na za dharura. Lakini katika hali yangu ya uchovu kazi ya uandishi mwingi ilionekana zaidi ya vile mwili wangu ungeweza kustahimili. Hisia ya kuvunjika moyo ilinijia, na nikazama katika hali ya udhaifu na nikakaa hivyo siku kadhaa, nikizimia mara kwa mara. Katika hali hii ya mwili na akili, nilijiuliza kuhusu wajibu wangu kuandika mengi, na kwa watu wengi, ambao wengine wao hawakustahili kabisa. Ilionekana kwangu kuwa hakika kulikuwa na kosa katika jambo hili mahali fulani. {2Tsw 10.1}

Jioni ya Februari 5, Ndugu Andrews alizungumza na watu kwenye nyumba yetu ya ibada. Lakini jioni hiyo muda mwingi nilikuwa katika hali ya kuzimia, na shida ya kupumua, nikiwa nimejieggesha pembeni mwa mume wangu. Wakati Ndugu Andrews aliporudi kutoka kwenye mkutano, watu walikuwa na wasaa maalum wa kuniombea, na nikajisikia kupata nafuu. Usiku huo nililala vizuri, na asubuhi, ingawa nilikuwa dhaifu, nilihisi afueni na kupata faraja ya pekee. Nikawa nimeota kwamba mtu alikuwa ameniletea jora la kitambaa cheupe, na akaniambia nishone nguo kwa watu wa vipimo vya aina yote na ufafanuzi wa kila tabia na hali za maisha mbali mbali. Niliambiwa nizishone na kuzitundika zote, ili ziwe tayari, wakati wake utakapofika. Nilikuwa na mawazo kwamba wengi ambao nilihitajika kuwashonea nguo hawakustahili. Nikauliza ikiwa hicho kilikuwa kipande cha mwisho cha nguo nilichopaswa kushona, na nikaambiwa kwamba sivyo; kwamba mara tu ninapomaliza hiki, kulikuwa na vingine vya kuvifanyia kazi. Nilihisi kukatishwa tamaa na kiwango cha kazi iliyokuwa mbele yangu, na nikasema kwamba nilikuwa nimehusika katika kushona nguo kwa

wengine kwa zaidi ya miaka ishirini, na kazi yangu haikuthaminiwa, na wala sikuona kwamba kazi yangu ilikuwa imetimiza mazuri mengi. Nilizungumza na mtu aliyeniletea kitambaa cha mwanamke mmoja aliyebainishwa haswa, ambaye alikuwa ameniambia nimshonee nguo yake. Nilisema kuwa hataithamini hiyo nguo, na kwamba itakuwa ni kupoteza muda tu, kumpatia kitambaa yeye. Dada huyu alikuwa maskini sana, mwenye akili duni, na mtu asiye nadhifu kwa tabia, na punde ataishia kuichafua tu. {2Tsw 10.2}

Mtu huyo akajibu: "Shona nguo. Huo ni wajibu wako. Hasara sio yako, bali ni yangu. Mungu haoni kama vile mtu anavyoona. Yeye Anaweka wazi kazi, ambayo angependa kuifanya, na wewe haujui ni ipi itakayofanikiwa, hii au ile. Itashangaza kwamba roho nyingi masikini kama hizo, zitaingia katika ufalme, wakati wengine, ambao wamepata upendeleo na baraka zote za maisha, wakiwa na akili mahiri na mazingira mazuri, na kupewa fursa zote za kuweza kuboreshwa zaidi, wataachwa nje. Itadhihirika kuwa hizi nafsi masikini zimeishi kwa nuru dhaifu ambayo walikuwa nayo, na zimefanyika bora zaidi kwa mapendeleo na fedha ndogo walizokuwa nazo, na bado wakaishi maisha yanayokubalika na kupendeza zaidi, kuliko wengine ambao wamefurahia mwangaza kamili na fursa za kutosha kwa maendeleo na uboreshaji wao." {2Tsw 11.1}

Kisha nikanyanyua mikono yangu, iliyopata sugu kwa ajili ya matumizi ya mkasi kwa muda mrefu, na nikasema natamani ningeweza kufanya kitu kingine zaidi ya kudumu katika wazo la kuendelea na aina hii ya kazi. Mtu huyo alirudia tena kusema: {2Tsw 11.2}

"Shona nguo. Muda wako wa kupumzika bado haujafika." {2Tsw 11.3}

Kwa hisia za uchovu mkubwa niliamka ili kuendelea na kazi hiyo. Mbele yangu kulikuwa na mkasi, uliong'aa kwa kusuguliwa, ambao nilianza kuutumia. Mara moja hisia

zangu za uchovu na kukata tamaa ziliniacha; mkasi ulionekana kukata haraka bila ya mimi kutumia juhudi na nikakata nguo baada ya nguo kwa urahisi zaidi. {2Tsw 11.4}

Kwa kutiwa moyo na ndoto hii, niliamua kuandamana na mume wangu na Ndugu Andrews kwenda Gratiot, Saginaw, na wilaya ya Tuscola, na kumtumaini Bwana kunipa nguvu ya kufanya kazi. Kwa hivyo, mnamo 7 Februari, tuliondoka nyumbani, na tukasafiri maili hamsini na tano hadi mahali tulipokuwa tumekubaliana kukutana huko Alma. Hapa nilifanya kazi kama kawaida, nikiwa na kiwango cha kuridhisha cha uhuru na nguvu. Marafiki katika wilaya ya Gratiot walionekana kupenda kusikia ujumbe wetu, lakini wengi wao, wako nyuma sana kuhusiana na matengenezo ya afya na katika kazi ya maandalizi kwa ujumla. Kulionekana kuwa na uhitaji wa utaratibu na ufanisi unaohitajika ili kufanikiwa katika kazi na shauku ya ujumbe kati ya watu hawa. Ndugu Andrews, hata hivyo, aliwatembelea wiki tatu baadaye na akafurahia wakati mzuri wa kuwa nao. Sitasahau jambo la kunitia moyo, kwamba ushuhuda mahususi kabisa ambao nilikuwa nimeandika kwa familia moja ulipokelewa na kuonekana wa manufaa kwa watu waliokusudiwa. Bado tunadumu kuvutiwa kwa dhati na familia hiyo na tunatamani sana kwamba wafurahie kufanikiwa katika Bwana, na ingawa kwa kiasi tunahisi kuvunjika moyo, ila kwa kazi hiyo katika wilaya ya Gratiot tutakuwa na shauku ya kusaidia ndugu zetu, wakati wowote wanapohisi hitaji la kusaidiwa. {2Tsw 12.1}

Kwenye mkutano wa Alma kulikuwa na ndugu waliokuwepo kutoka kwa Mt. Charles na Tittabawassee, wilaya ya Saginaw, ambao walituhimiza tuwatembelee. Hatukuwa tumepanga kuingia wilaya hii kwa wakati huu, isipokuwa kutembelea wilaya ya Tuscola ikiwa njia itafunguliwa. Pasipo na kupata taarifa kutoka Tuscola, tuliamua kutembelea Tittabawassee, na wakati huo huo tuandikie wilaya ya Tuscola na kuulizia kama wanatuhitaji huko. Huko Tittabawassee tulifadhaishwa kwa furaha tuliyoipata baada ya kupata nyumba kubwa ya ibada, iliyojengwa hivi karibuni na watu wetu, iliyojazwa na watunza Sabato. Ndugu walionekana kuwa tayari kwa

ushuhuda wetu, na tulifurahia hali ya uhuru. Kazi kubwa na nzuri ilikuwa imefanywa mahali hapa kupitia kazi ngumu ya Ndugu A. Upinzani mkali na mateso yalikuwa yamefuata, lakini hali hii ilionekana kuyeyuka na wale waliokuja kusikiliza, na kazi zetu zilionekana kuwa nzuri kwa wote. Nilihudhuria mikutano kumi na moja mahali hapa kwa wiki moja, nilizungumza mara kadhaa kutoka saa moja hadi mbili, na kushiriki katika mikutano mingine. Katika mkutano mmoja juhudi ilifanywa kushawishi watu fulani wanaoshika Sabato kusonga mbele na kubeba msalaba. Wajibu mkuu uliokuwa mbele ya wengi wao ulikuwa ubatizo. Katika maono yangu ya mwisho, niliona mahali ambapo Ukweli ungehubiriwa na kuleta makanisa ambayo tunapaswa kutembelea. Hii ilikuwa moja ya maeneo hayo. Nilihisi nia ya kipekee kwa watu hawa. Kesi za watu fulani katika kutaniko zilifunguliwa mbele yangu, na roho ya kazi kwao ilinijia, ambayo sikuweza kuitupa. Kwa muda wa saa tatu niliwafanyia kazi, wakati mwingi nikiwasihi kwa hisia za huruma na kujali. Wote walichukua msalaba katika hafla hiyo na kujitokeza mbele kwa maombi, na karibu wote walizungumza. Siku iliyofuata watu kumi na tano walibatizwa. {2Tsw 12.2}

Hakuna mtu anayeweza kuwatembelea watu hawa bila kuvutiwa na thamani ya bidii ya kazi ya Ndugu A, katika eneo hili. Kazi yake ni kuingia mahali ambapo Ukweli haujatangazwa, na natumai watu wetu wataacha juhudi zao za kumtoa kutoka katika kazi yake hii maalum. Kwa roho ya unyenyekevu anaweza kusonga mbele, akitegemea mkono wa Bwana, na kuokoa roho nyingi kutoka kwa nguvu za giza. Baraka ya Mungu iendeleo kuwa pamoja naye. {2Tsw 13.1}

Kwa kadri ambavyo mfululizo wa mikutano yetu mahali hapa ilikuwa karibu kumalizika, Ndugu Spooner wa Tuscola alikuja kwetu kutembelea wilaya hiyo. Tulikubaliana kukutana naye aliporudi Jumatatu, na tukafuata Alhamisi baada ya ubatizo. Huko Vassart, tulifanya mikutano yetu Sabato na siku ya kwanza kwenye nyumba ya shule ya jimbo kuu. Hapa palikuwa mahali penye uhuru wa kuzungumza, na tukaona matunda mazuri ya kazi zetu. Mchana wa siku ya kwanza

karibu watu thelathini waliorudi nyuma, na watoto ambao walikuwa bado hawajapata taaluma yoyote, walikuja mbele. Huu ulikuwa mkutano wa kuvutia na wenye mafanikio makubwa. Wengine walikuwa wakirudi nyuma na kuiacha kazi, ambao tulihisi tunahitaji kushughulika nao. Lakini wakati ulikuwa mfupi, na ilionekana kwangu kwamba tungeacha kazi haijakamilika. Lakini muda tuliokubaliana kukutana Mt. Charles na Alma ulikuwa umefika, na ili kukutana nao, ilikuwa lazima tufunge kazi zetu huko Vassar Jumatatu. {2Tsw 13.2}

Usiku huo kile nilichokuwa nimeona katika maono juu ya watu fulani katika wilaya ya Tuscola, kilihuishwa katika ndoto tena, na bado nilivutiwa zaidi kuwa kazi yangu kwa watu hao ilikuwa bado haijakamilika. Walakini sikuona njia nyingine zaidi ya kwenda kwenye miadi yetu. Jumanne tulisafiri maili thelathini na mbili kwenda Mt. Charles na tukakaa usiku na Ndugu Griggs. Hapa niliandika kurasa kumi na tano za shuhuda, na nilihudhuria mkutano jioni. Jumatano asubuhi tuliambia kurudi Tuscola ikiwa Ndugu Andrews angeweka miadi huko Alma. Kwa hili alikubali. Asubuhi hiyo niliandika kurasa kumi na tano zaidi, nilihudhuria mkutano na kuzungumza kwa saa moja, na tukasafiri maili thelathini na tatu na Ndugu na Dada Griggs kwenda kwa Ndugu Spooner huko Tuscola. Alhamisi asubuhi tulienda Watrousville, umbali wa maili kumi na sita. Niliandika kurasa kumi na sita, na nilihudhuria mkutano wa jioni, ambapo nilitoa ushuhuda mahususi kwa mtu mmoja aliyekuwepo. Asubuhi iliyofuata niliandika kurasa kumi na mbili kabla ya kifungua kinywa, na kurudi Tuscola, na kuandika kurasa nane zaidi. {2Tsw 14.1} Sabato, mume wangu alizungumza wakati wa mchana, na mimi nilifuata kwa masaa mawili kabla ya kula chakula. Mkutano ulifungwa kwa muda mfupi, na nikala chakula kidogo, na baadaye nikazungumza katika mkutano wa kijamii kwa saa moja, nikitoa ushuhuda ulio wazi kwa watu kadhaa waliokuwepo. Ushuhuda huu kwa ujumla ulipokelewa na hisia za unyenyekevu na shukrani. Hata hivyo, siwezi kusema kwamba wote waliupokea hivyo. {2Tsw 14.2}

Asubuhi iliyofuata, tulipokuwa tunataka kuondoka kwenda kwenye nyumba ya ibada ili kufanya kazi ngumu ya siku hiyo, dada ambaye nilikuwa na Shuhuda kwake kwamba hakuwa na busara na tahadhari, na kwamba hakudhibiti kabisa maneno na matendo yake, aliingia na mumewe na akaonyesha hisia za kutokuwa na maridhiano na fadhaa. Alianza kuzungumza na kulia. Alinung'unika kidogo, na kukiri kidogo, na akajihesabia haki sana. Alikuwa na mtazamo potofu kuhusu mambo mengi ambayo nilikuwa nimemwambia. Kiburi chake kiliguswa wakati nilipoibua makosa yake hadharani. Hapa kulikuwa na tatizo kuu lililo wazi. Lakini kwa nini ahisi hivyo? Ndugu na dada walijua kuwa mambo haya ndivyo yalivyo, kwa hivyo sikuwa nawambia kitu chochote kipya. Lakini sina shaka pia kuwa ilikuwa kitu kipya kwa dada mwenyewe. Hakujitambua mwenyewe, na hakuweza kuyapima vizuri maneno na matendo yake mwenyewe. Hii ni kweli kwa kiwango kikubwa kwa washiriki wote na shuhuda zote, na hiyo hujenga akilini umuhimu wa kuwa na makaripio ya uaminifu ndani ya kanisa, na malezi kwa washiriki wake wote, kuwa na upendo kwa Shuhuda iliyo dhahiri (chuki kwa shuhuda zilizo dhahiri-love of plain testimony). {2Tsw 14.3}

Mumewe alionekana kuhisi kutoafikiana na mimi kwa kuleta makosa yake mbele ya kanisa na akasema kwamba ikiwa Dada White angefuata maagizo ya Bwana wetu katika Mathayo 18:15-17, mkewe asingehisi kuumizwa: "Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye, peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru." {2Tsw 15.1}

Mume wangu baadaye akafafanua kuwa anapaswa kuelewa kwamba maneno haya ya Bwana wetu yalikuwa na rejeleo la visa vya kukoseana kati ya mtu na mtu, na hayangeweza kutumika kwa kesi ya huyu dada. Dada aliyepewa karipio,

hakuwa amemkosea Dada White. Lakini kile kilichokuwa kimekemewa hadharani ni makosa ya wazi ambayo yalitishia ustawi wa kanisa na utume wake. Hapa, ni fungu linalotumika kwa mazingira kama haya ni: 1 Timotheo 5:20: "Wale wadumuo kutenda dhambi wakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope." alisema mume wangu, {2Tsw 15.2} Ndugu alikubali kosa lake kama Mkristo na alionekana kupatanishwa na jambo hilo. Ilikuwa dhahiri kuwa tangu mkutano wa alasiri ya Sabato, walikuwa wamepata vitu vingi juu ya jambo hilo, ambalo lilikuwa limekuzwa na kustaajabisha sana. Kwa hivyo ilipendekezwa kuwa Shuhuda iliyoandikwa isomwe. Wakati hili limeisha, dada ambaye alikemewa na shuhuda hii, aliuliza: "Je! Hivi ndivyo ulivyosema jana?" Nilijibu kwamba ilikuwa hivyo. Alionekana kushangaa na kupatanishwa kabisa na Shuhuda iliyoandikwa. Nilimpa nakala ya hii shuhuda, bila kuhifadhi nakala yoyote kwa kazi yangu. Hapa nilifanya vibaya. Lakini nilimjali sana yeye na mumewe, na nikiwa na shauku kubwa na matumaini katika mafanikio yao, ndiyo maana, katika kesi hii, nilivunja desturi iliyowekwa ya kuhifadhi nakala kwaajili ya uandishi na uchapaji, siku za baadaye. {2Tsw 16.1}

Tayari wakati wa mkutano ulikuwa ukipita, na tukaharakisha kwenda maili moja na nusu kwa kutaniko lililokuwa likingojea. Msomaji anaweza kuamua, baada ya hili tukio, kama eneo la asubuhi hiyo lilitibiwa vizuri kutusaidia katika mkusanyiko wa mawazo na ujasiri unaohitajika ili kusimama mbele ya watu. Lakini ni nani anayefikiria jambo hili? Watu wengine wanaweza kuonyesha huruma kidogo, wakati wale wale wenye misukumo au mihemko, na wasiojali huja na mizigo na majaribu yao kwa ujumla, kabla tu ya kuanza kuzungumza, au wakati tumepata uchovu kabisa kwa kuongea kwa muda. Mume wangu, hata hivyo, alikusanya nguvu zake zote, na kwa kusihi alizungumza kwa uhuru juu ya sheria na injili. Nilikuwa nimepokea mwaliko wa kuongea mchana katika nyumba mpya ya ibada iliyojengwa na kuwekwa wakfu na Wamethodisti. Jengo hili zuri lilikuwa limejaa, na wengi walilazimika kusimama. Nilizungumza kwa uhuru kwa muda



wa saa moja na nusu juu ya amri ya kwanza kati ya amri mbili kuu zilizorudiwa na Bwana wetu, na nilishangaa kujua kuwa ni mada ile-ile ambayo Mchungaji wa Kimethodisti alikuwa amezungumza hapo mchana. Yeye na watu wake walikuwepo kusikia kile nilichokuwa nasema. {2Tsw 16.2} Jioni tulikuwa na mahojiano ya thamani nyumbani kwa Ndugu Spooner na Ndugu Miller, Hatch, na Haskell, na Sisters Sturges, Bliss, Harrison, na Malin. Sasa tulihisi kwamba kazi yetu kwa wakati huu ilikuwa imeisha katika wilaya ya Tuscola. Tulikuwa tumevutiwa sana na watu hawa wapendwa, na bado tukahofia ya kule nyuma, kwamba yule dada anayetajwa, ambaye nilikuwa nina Shuhuda kwake, Je, angemruhusu Shetani kumtumia na kuwaletea shida. Nilihisi moyoni shauku ya dhati kwamba angeweza kuliona jambo hili kwa nuru yake halisi. Mwenendo ambao alikuwa ameufuata, ulikuwa uiharibu mvuto wake ndani na nje ya kanisa. Lakini sasa, ikiwa angepokea karipio linalohitajika, na kwa unyenyekevu kukubali kubadilika, basi kanisa lingempokea upya ndani ya mioyo yao, na watu wangetafakari yaliyo mema zaidi kuhusu Ukristo wake. Na kilicho bora zaidi, angeweza kufurahia tabasamu la kukubalika la Mkombozi wake mpendwa. Je! angeweza kweli kupokea shuhuda yote kwa ukamilifu? Lilikuwa swali lililonipa wasiwasi moyoni. Nilihofia kwamba asingekubali kupokea shuhuda na hivyo kuhuzunisha mioyo ya ndugu katika wilaya hiyo kwasababu ya tukio hili. {2Tsw 16.3} Baada ya kurudi nyumbani, nilimtumia barua ya kumwomba arudishe ile nakala ya Shuhuda niliyompa, na tarehe 15 Aprili nilipokea barua kutoka Denmark, Ikiwa ina maandishi yafuatayo-Toka Denmark, Aprili 11, 1868: "Dada White: rejea barua yako ya tarehe 23 mwezi uliopita. Bado nipo nayo. Nasikitika siwezi kutekeleza ombi lako." {2Tsw 17.1} Mimi binafsi bado nitathamini familia hii kwa hisia nyororo, upendo na kujali, na nita furahi kuwasaidia kadri niwezavyo. Ni kweli kwamba namna hii ya uitikiaji na utendaji kwa wale ambao ninajitolea maisha yangu kwao, inatoa kivuli cha huzuni juu yangu; lakini utume wangu umeainishwa dhahiri

kwangu, kiasi kwamba siwezi kuruhusu vitu kama hivyo kuniondoa katika barabara ya wajibu wangu. Niliporudi kutoka ofisi ya posta na barua hiyo hapo juu, nikihisi kusononeka moyoni, nilichukua Biblia, na kuifungua kwa maombi ili nipate faraja na msaada ndani yake, na jicho langu likatulia moja kwa moja juu ya Maneno yafuatayo ya nabii: "Haya basi wewe jifunge viuno vyako, ukaondoke, na uwaambie maneno yote niliyokuamuru; usifadhaike kwa nyuso zao, nisije nikakufadhaisha wewe mbele yao. Kwa maana, tazama, nimekufanya leo kuwa mji ulio na boma, na nguzo ya chuma, na kuta za shaba juu ya nchi yote, juu ya nchi yote; juu ya wafalme wa Yuda, na juu ya wakuu wake, na juu ya makuhani wake, na juu ya watu wa nchi. Nao watapigana nawe; lakini hawatakushinda; kwa maana Mimi ni pamoja nawe, asema Bwana, ili nikuokoe." Yeremia 1: 17-19. {2Tsw 17.2}

Tulirudi nyumbani kutoka ziara hii kabla tu ya mvua kubwa iliyonyesha ambayo iliondoa theluji yote ardhini. Dhoruba hii ilizuia mkutano wa Sabato uliofuata, na mara moja nilianza kuandaa mambo ya Shuhuda Nambari 14. Pia tulikuwa na fursa ya kumtunza Ndugu King, mpendwa wetu ambaye tulimleta nyumbani kwetu akiwa na jeraha baya kichwani na usoni. Tulimpeleka nyumbani kwetu ili akafie hapo, kwani hatukuweza kufikiria uwezekano wa kupona kwa mtu aliyevunjika fuvu la kichwa kiasi hicho. Lakini kwa baraka ya Mungu kwa kufanya matumizi sahihi ya maji, na chakula kidogo mpaka hatari ya homa ilipokuwa imepita, huku vyumba vyenye hewa safi mchana na usiku vikisaidia, katika wiki tatu tu, aliweza kurudi nyumbani kwake na kuendelea na shughuli zake za kilimo. Hakuwahi kuchukua hata punje moja ya dawa za famasia, toka mwanzo hadi mwisho wa tiba hii rahisi. Ingawa alipungua uzito sana kutokana na kupoteza damu kupitia vidonda vyake na lishe ndogo, lakini punde alipokuwa huru kula chakula aliongezeka uzito kwa haraka. {2Tsw 18.1}

Wakati huu tulianza kazi kwa ndugu zetu na marafiki karibu na Greenville. Kama ilivyo katika maeneo mengi, ndugu zetu walihitaji msaada. Kulikuwa na wengine ambao walishika Sabato, lakini hawakuwa wa kanisa la Waadventista wa Sabato, na pia kulikuwa na wengine ambao walikuwa wameacha Sabato, ambao walihitaji msaada. Tulikuwa na nia moyoni, ya kuzisaidia roho hizi maskini, lakini mienendo ya zamani na nafasi za wakati huu, za washiriki waliokuwa wanaongoza kanisa kwa kuhusiana na watu hawa ilifanya kutowezekana kwetu, kuwafikia ili kuwapa msaada. Katika kufanya kazi na wakosaji, baadhi ya ndugu zetu walikuwa na misimamo migumu, na wenye maneno makali ya kukata-kata, na yenye kuumiza. Na wengine walipofikiria kukataa ushauri wao na kujitenga nao, wangeweza kusema: "Ikiwa kweli, wanataka kwenda, basi waacheni waende." Wakati ambapo huruma, uvumilivu, na upendo mwanana na kujali kwa Yesu kwa huruma nyororo vinakosekana kudhihirishwa na wale wanaojiita kuwa wafuasi Wake, hawa masikini, wakosefu, wasio na uzoefu, waliopigwa-pigwa na Shetani, wanakuwa na uhakika wa kuharibikiwa imani yao. Haijalishi makosa na dhambi za wakosaji zimekuwa kubwa kiasi gani, ndugu zetu lazima wajifunze kudhihirisha sio tu upendo mwanana, huruma, kujali na upole wa Mchungaji Mkuu, lakini pia utunzaji Wake usiokufa na upendo kwa kondoo hawa maskini, wanaopotea-na kutangatanga. Wachungaji au wahudumu wetu, wanafanya kazi kwa bidii na kufundisha wiki baada ya wiki, na wanafurahi kwamba roho chache zinaukubali Ukweli; na bado ndugu wenye uamuzi wa haraka, unaogeza akili, wanaweza kwa dakika tano tu, kuharibu kazi yao kwa kuruhusu hisia ambazo husababisha maneno kama haya: "Ni sawa tu, ikiwa wanataka kutuacha, waacheni waende." {2Tsw 18.2}

Tuligundua kuwa hatuwezi kufanya chochote kwa kondoo waliotawanyika karibu nasi, mpaka kwanza turekebishe makosa miongoni mwa washiriki wengi walio kanisani. Walikuwa wameziacha hizi roho maskini zikitangatanga. Hawakuhisi mzigo kwao. Kwa Kweli, walionekana kujifungia

kwao wenyewe (ubinafsi), na walikuwa wakifa kifo cha kiroho kwa kukosa mazoezi ya kiroho. Bado walipenda kazi ya Mungu kwa ujumla, na walikuwa tayari kusaidia kuitegemeza. Wangewatunza vizuri watumishi wa Mungu. Lakini kulikuwa mapungufu dhahiri katika kuwajali wajane, yatima, na wanyonge wa kundi. Mbali na kuonyesha shauku ya maslahi ka kazi ya Mungu kwa ujumla, kulikuwa na shauku ndogo tu ya kumjali mtu yeyote, zaidi ya familia zao. Kwa dini hii finyu, walikuwa wakifa kifo cha kiroho. {2Tsw 19.1}

Kulikuwa na wengine ambao walitunza/walishika Sabato, na walihudhuria mikutano ya kanisa, na wakatoa zaka na sadaka kwa mpango wa ukarimu, lakini walikuwa nje ya kanisa. Na ni kweli kwamba hawakustahili kuwa katika kanisa lolote. Na japokuwa viongozi wa washiriki wa kanisa, walisimama kama wengine katika kanisa hilo, kama walivyofanya, wakiwatia moyo kidogo ama kutofanya hivyo kabisa, ilikuwa haiwezekani kabisa kwao kuinuka katika nguvu ya Mungu na kufanya vizuri. Tulipoanza kufanya kazi na kanisa, na kuwafundisha kwamba lazima wawe na roho ya kufanya kazi kwa ajili ya wakosaji, mengi ambayo nilikuwa nimeona kwa muktadha wa kazi mahali hapo, yalifunguliwa mbele yangu, na niliandika shuhuda zilizo wazi sio tu kwa wale ambao walikuwa wamekosea sana na walikuwa nje ya kanisa, bali kwa wale washiriki ndani ya kanisa waliokuwa wamefanya kosa kubwa sana, la kutokwenda kuwatafuta kondoo waliopotea. Na kamwe sikuwahi kuvunjika moyo kwa namna ambavyo Shuhuda hizi zilipokelewa. Wakati wale waliokuwa na makosa makubwa walipokemewa na shuhuda nyingi zilizo wazi, na kusomewa hadharani, walizipokea, na kukiri kwa machozi. Lakini baadhi ya wale walio makanisani, ambao walidai kuwa marafiki wakubwa wa kazi ya injili na Shuhuda, hawakudhania kama wao wanaweza kukosea kiasi kile ambacho Shuhuda zilisema. Walipoambiwa kwamba walikuwa wanajali-nafsi zao tu, kwa kushugulikia mahitaji yao tu au kujipenda wenyewe, na wamejifungia wenyewe na familia zao; kwamba walishindwa kuwajali wengine,

walikuwa wabaguzi, na walikuwa wameacha roho za thamani zikiangamia; kwamba walikuwa katika hatari ya kunyanyasa wengine, na kujihesabia haki wenyewe waadilifu, waliletwa katika hali ya fadhaa kubwa kwa kuudhika na majaribu. {2Tsw 19.2}

Lakini uzoefu huu ndio tu walihitaji ili kuwafundisha wengine uvumilivu katika hali kama hiyo ya jaribio. Kuna wengi ambao wanahisi kwa hakika kuwa hawatajaribiwa kuheshimu na kuziamini Shuhuda, na wanaendelea kujisikia hivyo mpaka watakapojaribiwa. Wanafikiria ni jambo la ajabu kwamba mtu yeyote anaweza kutilia shaka Shuhuda. Wanakuwa wakali kwa wale ambao hudhihirisha mashaka, na hukata na kufyeka watu, katika kuonyesha wazi mapenzi yao kwa Shuhuda, wakidhihirisha haki-binafsi kuliko kuwa wanyenyekevu. Lakini wakati Bwana anawakemea kwa makosa yao, wanajikuta ni dhaifu kama maji tu. Basi watu kama hao hawawezi kustahimili kulikabili jaribu. Mambo haya yanapasa kuwafundisha unyenyekevu, kujishusha, kutostahili, upole, kujali, huruma nyororo na upendo mwanana usiokoma kwa wacosaji. {2Tsw 20.1}

Inaonekana kwangu mimi binafsi, kwamba Bwana anawapa wacosaji, walio dhaifu na wanaotetemeka, na hata wale ambao wameasi Ukweli, mwito maalum wa kurejea zizini. Lakini kuna wachache katika makanisa yetu ambao wanahisi kuwa, hivi ndivyo Bwana afanyavyo. Na bado wapo watu wachache tu, wanaosimama upande ambao wanaweza kuwasaidia watu hawa. Wengi, husimama moja kwa moja katika njia za roho hizi ili kuzizuia. Wengi sana, wana roho ya ukali na ni wagumu. Wanataka watimize masharti fulani-fulani, kabla hawajawanyooshea mkono wa msaada. Kwa hivyo huwaepa kwa makusudi, kwa namna fulani, kwa kuondoa ukaribu wa hisia au mahusiano. Hawajajifunza kwamba wana jukumu maalum la kwenda na kuwatafuta kondoo hawa waliopotea. Hawapaswi kusubiri mpaka hawa kondoo waje wenyewe kwao. Soma kisa cha kosisimua cha mwana-kondoo aliyepotea. Luka 15: 1-7: "Basi watoza ushuru na wenye dhambi wote wakamwendea ili wamsikie.

Na Mafarisayo na waandishi wakanung'unika, wakisema, Mtu Huyu Huwapokea wenye dhambi, Naye Hula nao. Akawaambia mfano huu. akisema, Ni mtu gani kati yenu aliye na kondoo mia, akipoteza mmoja wao, asiyewaacha wale tisini na kenda jangwani, aende atafute yule aliyopotea hata ampate? Na kumweka mabegani mwake, akifurahi. Anapofika nyumbani, anaita marafiki na majirani, na kuwaambia, Furahini pamoja nami, kwa sababu nimempata kondoo wangu aliyepotea. Ninawaambia, vivyo hivyo furaha itafanyika kule mbinguni juu ya mwenye dhambi mmoja atubuye, zaidi ya watu waadilifu tisini na tisa [99], ambao hawahitaji toba. " {2Tsw 20.2}

Mafarisayo walinung'unika kwa sababu Yesu aliwapokea watoza ushuru na wenye dhambi wa kawaida, na kula nao. Kwa kujihesabia haki wao wenyewe, waliwadharau wadhambi hawa maskini ambao walisikia Maneno ya Yesu na kushangilia. Kukemea roho hii mbaya ya waandishi na Mafarisayo, huacha somo linalogusa moyo kwa wote, Bwana alitoa mfano wa kondoo aliyepotea. Angalia vipengele mahsusi vifuatavyo: {2Tsw 21.1}

Kondoo tisini na tisa wameachwa, na usakaji/utafutaji wa bidii na uadilifu, unafanywa kwa yule mmoja aliyepotea. Jitihada yote inafanywa kwa kondoo huyu aliyekumbwa na changamoto-bahati mbaya. Vivyo hivyo, ndivyo juhudi ya kanisa inavyopaswa kuelekezwa kwa wale washiriki ambao wanapotea kutoka zizi la Kristo. Na wale ambao wametanga mbali, wewe usingoje mpaka warudi wenyewe kabla ya kujaribu kuwasaidia, lakini nenda kawatafute {2Tsw 21.2}

Kondoo aliyepotea alipopatikana, alichukuliwa nyumbani kwa furaha, na shangwe nyingi zilifuata. Hii inaonyesha kazi yenye baraka, na furaha ya kutumika kwa ajili ya watu waliopotea. Kanisa linaloshiriki kwa mafanikio katika kazi hii ni kanisa lenye furaha. Mwanaume huyo au yule mwanamke ambaye roho yake inavutwa kwa huruma na upendo kwa wale waliopotea, na ambaye hufanya juhudi kuwarejesha katika zizi la Mchungaji Mkuu, anashiriki katika kazi yenye baraka. Na, oh jamani! hilo ni wazo la kuisimua nafsi kwa

kiasi gani! Kwamba mwenye dhambi mmoja anaporudishwa hivyo, kuna furaha zaidi mbinguni kuliko wenye haki tisini na tisa! Wabinafsi, wasioshirikiana na wengine, watu wakali ambao wanaonekana kuogopa kusaidia wale wanaopotea, kana kwamba watachafuliwa kwa kufanya hivyo, hawaoneshi ladha/utamu wa kazi hii ya umishenari; hawahisi ile heri inayojaza mbingu zote na shangwe juu ya uokoaji wa yule mmoja ambaye amepotea. Wamejifungia kwa mtazamo finyu wa hisia zao, na wanakuwa wakavu na wasiozaa matunda kama milima ya Gilboa, ambayo haikuwa na umande wala mvua. Hebu mtu yeyote aliye hodari na mwenye nguvu, afungiwe na asifanye kazi, hakika atadhoofika. Kanisa au wale watu ambao wanajitenga na wengine, na hawataki kushiriki katika kubeba mizigo ya wengine, wanaojitenga na kubaki wenyewe, punde watajikuta dhaifu kiroho. Ni kule kufanya kazi kunamfanya mtu aliye hodari adumu kuwa hodari. Ni kazi ya Kiroho, mateso na kubebeana mizigo tu, ndiyo itakayoliletea kanisa nguvu ya Kristo. {2Tsw 22.1}

Sabato na siku ya kwanza, Aprili 18, 19, tulifurahia wakati mzuri na watu wetu huko Greenville. Ndugu A na B walikuwa pamoja nasi. Mume wangu alibatiza watu nane. Tarehe 25 na 26 tulikuwa pamoja na kanisa huko Wright. Wapendwa hawa wako tayari kutukaribisha. Hapa mume wangu alibatiza watu wanane. {2Tsw 22.2}

Mei 2, tulikutana na kusanyiko kubwa kwenye nyumba ya ibada huko Monterey. Mume wangu alizungumza kwa uwazi na nguvu juu ya mfano wa kondoo aliyepotea. Neno hilo lilikuwa baraka kubwa kwa watu. Kuna watu wengine ambao walikuwa wamerudi nyuma, na walikuwa nje ya kanisa, na hakukuwa na juhudi ya kweli ya kuwasaidia. hakika ni ule ukali, kutokuwa na roho ya kirafiki, masharti magumu, na hisia ya kutojali watu iliyooneshwa na wengine, iliratibiwa namna hiyo, ili kuzuia kurudi kwao wale waliotoka au kurudi nyuma, endapo walitaka kurudi tena. Mada hiyo iligusa

mioyo ya wote, na wote walidhihirisha nia ya kutenda wema, kwa kuweka mambo sawa. Siku ya kwanza tulizungumza mara tatu huko Allegan kwenye kutaniko zuri. Makubaliano yetu yalikuwa kukutana na kanisa huko Battle Creek mnamo tarehe 9, lakini tulihisi kwamba kazi yetu huko Monterey ndiyo tu ilikuwa imeanza, na kwa hivyo tuliamua kurudi Monterey na kufanya kazi na kanisa hilo kwa wiki nyingine. Kazi nzuri iliendelea mbele, zaidi ya tulivyotarajia. Nyumba ilijaa, na hatukuwahi kushuhudia kazi hiyo kufanyika kwa muda mfupi kazi kama ilivyokuwa huko Monterey. Siku ya kwanza, watu hamsini walijitokeza kwa ajili ya maombi. Ndugu waliguswa sana kwa somo la yule kondoo aliyepotea, na wakakiri ubaridi na kutojali kwao, na wakaahidi kufanya mabadiliko. Ndugu GT Lay na S. Rummery walitoa ushuhuda mzuri, na walipokelewa kwa furaha na ndugu zao. Watu kumi na wanne walibatizwa, mmoja wao mtu wa makamo, ambaye alikuwa amehisi kupingana na ile Kweli. Kazi iliendelea kwa kicho, maungamo, na machozi mengi, ikibeba yote mbele yake. Na hatimaye kazi hii ya kuchosha ilihitimisha katika mwaka huu wa Konferensi. Na bado tulihisi kuwa kazi nzuri huko Monterey bado ilikuwa haijamalizika. Tumefanya mipango ya kurudi na kutumia wiki kadhaa katika Wilaya ya Allegan. {2Tsw 22.3}

Mkutano wa Konferensi iliyopita umekuwa msimu wa kupendeza sana. Kazi za mume wangu zimekuwa nzuri sana katika mikutano yake mbalimbali, naye anapaswa kupumzika. Kazi yetu kwa mwaka uliopita ilithaminiwa sana na watu wetu, na kwenye Mkutano wa Halmashauri Kuu (Konferensi), huruma nyororo, kujali, na ukarimu vilidhihirishwa kwetu. Pamoja nao tumefurahia uhuru mkubwa, na tunaachana, tukifurahi kwa kuaminiana na ujasiri na kupendana. {2Tsw 23.1}



## SURA YA 2

### KUTENDA KWA AJILI YA KRISTO

#### Sura ya 2 – Kutenda kwa ajili ya Kristo

Kutoka kwa kile nilichooneshwa, watunza Sabato wanazidi kuwa wabinafsi zaidi kadri wanavyokuwa na utajiri. Upendo wao kwa Kristo na watu wake unaendelea kupungua.

Hawaoni hitaji la kuwasaidia wahitaji, wala hawahisi mateso na huzuni zao. Hawatambui kuwa kwa kuwapuuza masikini na na watu wanaotesekeka, wanampuuza Kristo, na kwamba katika kupunguza uhitaji na mateso ya maskini kwa kadri inavyowezekeka, wanamhudumia Yesu. {2Tsw 24.1}

Kristo anasema kwa watu Wake waliokombolewa: "Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, mrithi ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu; kwa maana nilikuwa na njaa, mkanipa chakula; nilikuwa na kiu, mkaninywesha, Nilikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; nilikuwa mgonjwa, nanyi mlinitembelea; nilikuwa gerezani, mkanijia. {2Tsw 24.2}

"Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulikuona una njaa, na tukakulisha? Au ukiwa na kiu, tukakunywesha? Tulikuona lini wewe ni mgeni tukakukaribisha? Au uchi tukakuvika? Au ni lini tulikuona wewe mgonjwa, au gerezani, tukakujia? Naye Mfalme atajibu na kuwaambia, Amin, nawaambia, Kadri mlivyomtendea

mmoja wa hawa ndugu Zangu hawa walio wadogo,  
mlinitendea Mimi. " {2Tsw 24.3}

Kuwa mchapakazi, kuendelea kutenda kwa subira ambayo huhitaji kujikana nafsi, ni kazi tukufu, ambayo mbingu huitolea tab. Kazi ya uaminifu inakubaliwa na Mungu zaidi, kuliko ibada yenye ari na jitihada na inayodhaniwa kuwa takatifu zaidi. Ni kufanya kazi pamoja na Kristo ndiyo ibada ya kweli. Maombi, maneno ya kutia moyo na kuhamasisha maneno ya mdomoni tu bila matendo, ni matunda ya bei ndogo sana (bei che!), ambayo mara nyingi huambatanishwa na kazi; lakini matunda ambayo hudhihirishwa kwa kutenda matendo mema, katika kuwajali wahitaji, yatima, na wajane, ni matunda yaliyo ya Kweli/dhati, na kwa kawaida/asili huota kwenye mti mzuri.{2Tsw 24.4}

Dini safi na isiyo na waa mbele za Baba ni hii: "kuwatembelea yatima na wajane katika shida zao, na kujilinda bila mawaa na ulimwengu." Matendo mema ni tunda ambalo Kristo anatutaka tuzae: maneno ya upole, matendo ya ukarimu na wema, ya kuwahurumia na kuwajali masikini, wahitaji, na walio na shida. Wakati unapohurumia mioyo iliyolemewa na kukatishwa tamaa kwa huzuni, wakati mkono unanyooshwa kwa wahitaji, wakati walio uchi wanavikwa, na pale mgeni anakaribishwa kwenye kiti sebuleni kwako na anapewa nafasi moyoni mwako, malaika wanasogea karibu zaidi, na kila ombi lililoelekezwa mbinguni hujibiwa. Kila tendo la haki, huruma, na ukarimu hufanya nyimbo zirindime mbinguni. Baba kutoka kwenye kiti Chake cha enzi huwaona wale wanaofanya matendo haya ya huruma, na amewawekea alama kwa ajili ya hazina Zake za thamani zaidi. "Nao watakuwa Wangu, asema Bwana wa majeshi, katika siku ile nitakapotengeneza vito vyangu." Kila tendo la huruma kwa wahitaji, wanaoteswa, huchukuliwa kana kwamba limetendwa kwa Yesu. Unaposaidia maskini, unapohurumia waliotaabika na wanaodhulumwa, na kuwa rafiki wa yatima, unakuwa umejisogeza karibu katika uhusiano na Yesu. {2Tsw 25.1}

"Ndipo atawaambia wale walio mkono wa kushoto, Ondokeni Kwangu, ninyi mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, ulioandaliwa kwa ajili ya Ibilisi na malaika zake. Kwa maana nilikuwa na njaa, nanyi hamkunipa chakula; nilikuwa na kiu, na nilikuwa mgeni, wala hamkunikaribisha; nilikuwa uchi, wala hamunivisha; nilikuwa mgonjwa, na gerezani, nanyi hamkunitembelea. Ndipo watakapomjibu, wakisema, Bwana, lini tulikuona una njaa, au ukiwa na kiu, au mgeni, au uchi, au mgonjwa, au gerezani, na hatukukuhudumia? Ndipo atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kwa vile hamkufanya hivyo kwa mmoja wa wadogo hawa, hamkunifanyia Mimi. Na hawa wataenda katika adhabu ya milele; lakini wenye haki watapata uzima wa milele. " Mathayo 25: 41-46. {2Tsw 25.2}

Hapa Yesu anajitambulisha pamoja na watu Wake wanaoteseka. Ni Mimi niliyekuwa na njaa na kiu. Ni Mimi ambaye nilikuwa mgeni (mtu baki). Ni Mimi niliyekuwa uchi. Ni Mimi ambaye nilikuwa mgonjwa. Ni Mimi nilikuwa gerezani. Wakati ulipokuwa unafurahia vyakula mbalimbali vilivyotandazwa na kusheheni kwenye meza zako za kifahari. Mimi nilikuwa na njaa kwenye kibanda au mtaani karibu na ulipokuwa. Wakati uliponifungia milango yako usoni Pangu, wakati vyumba vyako vilivyojazwa samani/fanicha nzuri havikuwa na mtu wa kuvitumia, Nami sikuwa na hata mahali pa kulaza kichwa Changu kwenye nyumba ya kimasikini. Kabati zako zilijazwa na safu za suti za kubadilisha, kwa vile fedha zilifanyiwa ubaradhifu bila sababu, nguo ambazo ungeweza kuwapatia wahitaji. Nilikuwa na uhitaji wa nguo ya kunisitri. Wakati ulipokuwa unafurahia afya, Mimi nilikuwa mgonjwa. Nilijikuta majanga ya bahati mbaya yamenitupa gerezani na wakanifunga kwa pingu, na roho yangu ikafadhaika, nikinyimwa uhuru na tumaini, wakati ambapo ulikuwa ukitembea kwa uhuru. Ni umoja na ushirika wa ajabu kiasi gani, ambao Yesu anauelezea upo hapa kati Yake na wanafunzi Wake wanaoteseka! Anaifanya shida yao kuwa Yake Mwenyewe. Yeye Anajitambulisha Mwenyewe kuwa nafsi ya mtu huyu anayetaabika. Weka umakini Mkristo mbinafsi: kila tendo la kutowajali wahitaji maskini, yatima,

na watu waliotelekezwa, ni kumpuuza Yesu katika nafsi zao.  
{2Tsw 25.3}

Ninawafahamu watu ambao wanakiri kwa hali ya juu Ukristo, kwa mdomo tu na hufanya hivi kwa bidii kubwa, ambapo mioyo yao imefungwa katika kujipenda-nafsi na ubinafsi kiasi cha kutoheshimu, kuthamini na kufurahia kile ninachokiandika. Mawazo na maisha yao yote yanaitumikia nafsi tu. Kujitoa kafara kwa ajili ya kuwatendea wengine wema, kujinyima ili kuwabariki wengine ni jambo lisilokuwa katika mawazo yao kabisa! Hawana wazo hata kidogo kwamba Mungu anahitaji hili kutoka kwao. Nafsi/Ubinafsi yaani umimi ndiyo sanamu yao. Majuma ya thamani, miezi, na miaka hupita kuelekea kwenye umilele, lakini miaka hiyo haina rekodi/kumbukumbu mbinguni juu ya matendo yao mema, ya kujitolea kwa ajili ya wema kwa wengine, ya kulisha wenye njaa, kuwavika walio uchi, au kumkaribisha mgeni. Hawakubaliani na tendo la kuwakarimu wageni au watu baki. Laiti wangejua kuwa wote waliotaka kushiriki fadhila zao walikuwa wanastahili, basi pengine wangeweza kushawishiwa kufanya kitu katika mwelekeo huu. Lakini kuna heri na fadhila katika kudiriki kukarimu wengine kwani huenda tukawakarimu malaika.{2Tsw 26.1}

Kuna yatima ambao wanapaswa kutunzwa; lakini wengine hawatathubutu kutenda hili, kwani litawaongezea kazi kubwa kuliko ambavyo wangependa kufanya, ikiwachia wakati mdogo wa kujifurahisha na kujiendekeza nafsi zao. Lakini wakati Mfalme atakapofanya uchunguzi, hawa wavivu wasiofanya lolote, wasiojali, wachoyo, wenye ubinafsi, watagundua na kujifunza kwamba mbingu ni kwa wale ambao wamekuwa watendakazi, wale ambao wamejikana wenyewe kwa ajili ya Kristo. Hakuna majaliwa au baraka yeyote iliyoahidiwa kwa wale ambao wanajijali na kujipenda wenyewe tu. Adhabu ya kutisha ambayo Mfalme anawatamkia wale walio mkono Wake wa kushoto, katika muktadha huu, sio kwa sababu ya uhalifu wao mkubwa. Hawahukumiwi kwa mambo ambayo walifanya, lakini kwa yale ambayo hawakuyafanya. Haukufanya mambo yale

ambayo mbingu ilikutuma kufanya. Ulijifurahisha mwenyewe, na sasa chukua sehemu yako pamoja na wale walioishi kwa kujifurahisha tu, nafsi zao wenyewe. {2Tsw 27.1}

Kwa dada zangu ningewaambia: Iweni mabinti wa Fadhili na ukarimu. Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Labda ulifikiri kwamba ikiwa ungeweza kupata mtoto mkamilifu, asiye na hitilafu, basi ungemchukua, na kumtunza; lakini kufadhaisha akili yako na mtoto mkosefu au mwenye makosa, kumrekebisha kwa vitu vingi anavyofanya kwa makosa na kumfundisha upya njia bora, kumfundisha k kuikana nafsi kwa kuwa na kiasi, ni jukumu ambalo wewe unakataa kulibeba. Kuwafundisha wasiojua, kuwahurumia na kuwarekebisha wale ambao wamekuwa daima wakijifunza uovu, sio jukumu rahisi; lakini Mbingu imeliweka jambo hili mikononi mwako. Wao ni mbaraka na japokuwa wanaonekana ni shida, hakika ni mbaraka uliojificha (bila kujua). {2Tsw 27.2}

Miaka kadhaa iliyopita nilioneshwa kuwa watu wa Mungu watapitia jaribu katika suala hili la kuandaa makazi kwa ajili ya wale wasio na makazi; kwamba kutakuwa na wengi watakaokosa makazi kutokana na kuiamini ile Kweli. Upinzani na mateso yatawafanya waumini kupoteza makazi yao, na ilikuwa ni jukumu la wale ambao walikuwa na nyumba kuwakaribisha wale ambao hawakuwa na makazi, kwa kuacha milango yao wazi. Nimeonyeshwa hivi karibuni kwamba Mungu atawajaribu wote wanaodai kuwa watu Wake kuhusiana na jambo hili. Kristo kwa ajili yetu alikuwa maskini ili kwa umaskini Wake, sisi tuweze kufanyika matajiri. Yeye Alijitoa kafara ili aweze kutoa makazi kwa wasafiri na wageni ulimwenguni wanaotafuta nchi bora, Naam, nchi ya mbinguni. Je! Wale ambao wamepokea neema Yake, ambao wanatarajia kuwa warithi wa maisha ya kutokufa, watakataa, au hata kuhisi kusita, kuwakaribisha nyumbani kwao wale wasio na makazi na wahitaji? Je! Sisi, ambao ni wanafunzi wa Yesu, tutawakataa wageni kuingia katika malango yetu kwa sababu hawawezi kuonesha tofauti baina yao na wafungwa? {2Tsw 27.3}

Je! Agizo la mtume halina nguvu katika ulimwengu huu wa leo: "Msisahau kuwakirimu wageni: maana kwa njia hiyo wengine wamewakaribisha malaika bila kujua"? Kila siku ninapata uchungu kutokana na udhihirisho wa uchoyo na ubinafsi miongoni mwa watu wetu. Kuna kiwango cha kutisha cha kupotea kwa upendo na kujali kwa wale wanaostahili kufanyiwa hivyo. Baba yetu wa mbinguni huweka baraka zilizojificha katika njia yetu, lakini wengine hawatawagusa baraka hizi kwa ajili ya hofu ya kupunguza starehe yao. Malaika husubiri kuona ikiwa tutakumbatia fursa zinazotuzunguka kwa ajili ya kutenda wema - wakingojea kuona ikiwa tutawabariki wengine, ili wao pia kwa wakati wao wapate kutubariki sisi. Bwana mwenyewe ametufanya tuwe tofauti, - wengine masikini, wengine matajiri, wengine wenye kukumbana na mateso, - ili wote wapate fursa ya kukuza tabia. Kwa makusudi masikini wameruhusiwa kuwepo kwa mapenzi ya Mungu, ili tujaribiwe na kuthibitishwa, na kukuza kile kilichomo mioyoni mwetu. {2Tsw 28.1}

Nimesikia wengi wakitoa udhuru kwa kushindwa kuwakaribisha watakatifu wa Mungu kwenye nyumba na mioyo yao. "Kwa nini waje kwangu nami sijaandaa chochote, sijapika chochote; watahitajika kwenda mahali pengine." Na huko kwingine kunaweza kuwa na kisingizio zaidi kilichobuniwa ili kutopokea wale wanaohitaji ukarimu na mapokezi yetu (hospitality), na kisha hisia za wageni zinahuzunishwa sana, na huondoka na mtazamo mbaya juu ya ukarimu wa hawa ndugu na dada wanaodai kuwa Wakristo. Ikiwa wewe hauna chakula nyumbani mwako dada, fuata mfano katika kisa hiki cha kwenye Bibilia. Nenda kwa jirani yako na umwambie: Rafiki, nikopeshe mikate mitatu, kwani rafiki yangu aliye safarini amenijia, na sina kitu cha kumpa ale."Hatujawahi kuwa na mfano huu wa kutokuwa na chakula kama kisingizio cha kuwakataa wageni waliotufikia. Wakati Eliya alipoenda kwa mjane wa Sarepta, alishiriki chakula chake kidogo na nabii wa Mungu, naye akafanya muujiza, na akasababisha kwamba katika kitendo hicho cha kumtengenezea mtumishi wake mahali pa kuishi, na kushiriki chakula chake naye, yeye mwenyewe alitegemezwa, na maisha yake na ya mtoto wake yakahifadhiwa. Kwa kufanya hivyo wengi watathibithishwa kwa wema, ikiwa wanafanya hivyo kwa uchangamfu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. {2Tsw 28.2}

Wengine wanasingizia kwamba ni afya zao mbaya - wangependa kufanya ikiwa wangekuwa na nguvu. Hawa wamejifunga katika vifungo vyao wenyewe kwa muda mrefu, na wanafikiria sana kuhusu hisia zao duni, na kuongea sana juu ya mateso, majaribu, na shida zao, kwamba ndio Ukweli wao wa sasa. Hawawezi kufikiria mtu mwingine isipokuwa wao wenyewe, haijalishi ni kwa kiwango gani wengine wanaweza kuwa wahitaji wa huruma na msaada au usaidizi. Wewe ambaye unateseka na afya mbaya, kuna suluhisho kwako. Pale utakapowavisha walio uchi, na kuwakaribisha maskini waliotupwa nje nyumbani kwako, na kuwapa chakula chako wenye njaa, "ndipo nuru yako itakapong'aa kama asubuhi, na afya yako itachomoza upesi. Soma Isaya 58. Kutenda wema ni tiba bora ya magonjwa. Wale ambao hushiriki katika kutenda kazi wanaalikwa kumwita Mungu, Naye ameahidi kuwajibu. Nafsi zao zitashibishwa kipindi cha ukame, nao watakuwa kama bustani inayonyweshewa maji penye kijito, ambayo maji yake hayakauki kamwe. {2Tsw 29.1}

Amkeni ndugu na dada. Msiogope kutenda matendo mema. "Tusichoke katika kutenda mema; kwa maana kwa wakati wake tutavuna, ikiwa hatutazimia." Usisubiri kuambiwa wajibu wako. Fungua macho yako na uone wale wanaokuzunguka; shiriki na tafuta kuwafahamu na kuwa na mahusiano na watu walio dhaifu, wanaoteseka, na wahitaji. Usijifiche kutoka kwao, na usijifanye kana kwamba huoni mahitaji yao, na kuwafungia nje. Ni nani anayetoa uthibitisho uliotajwa katika Yakobo, wa kuwa na dini safi, isiyo na waa wala kunyanzi mbele ya Mungu? Ni nani walio na shauku ya kufanya yote wawezayo kusaidia katika mpango mkuu wa wokovu? {2Tsw 29.2}

Ninamfahamu mjane ambaye ana watoto wawili wadogo wa kuwasaidia, hana kingine cha kumtegemeza isipokuwa kushona kwa sindano yake. Anaonekana mchovu, mwenye mashaka, rangi ya ngozi yake imepauka na aliye dhaifu. Kipindi chote kigumu cha majira ya baridi amepambana kuyakimu mahitaji ya watoto wake. Amepokea msaada mdogo tu, lakini ni nani atapungukiwa kwa kuonyesha shauku kubwa ya kusaidia kesi ya huyu mama? Hapa kuna vijana wake wawili wa kiume, wenye umri wa miaka karibu tisa na kumi na moja, ambao

wanahitaji mahali pa kuishi. Ni nani walio tayari kuwapatia sehemu ya kuishi kwa ajili ya Kristo? Mama anahitajika kupumzishwa jukumu hili la malezi ili abaki na kazi yake ya ufumaji. vijana hawa wako kijijini na mlezi wao afanyaye kazi kwa bidii ni mama yao. Wanahitaji kufundishwa jinsi ya kufanya kazi kwa kadri umri wao utakavyoruhusu. Wanahitaji kufundishwa kwa uvumilivu, kwa upole, na kwa upendo. Wengine wanaweza kusema: "Ah, ndio, nitawachukua na kuwafundisha jinsi ya kufanya kazi." Lakini hawapaswi kusahau mahitaji mengine ambavyo watoto hawa wanahitaji zaidi ya kufundishwa kufanya kazi. Wanahitaji kuelekezwa jinsi watakavyokuza tabia njema ya Kikristo. Wanahitaji upendo, mapenzi na kujaliwa, wanahitaji kuandaliwa vyema ili kufaa kwa maisha haya, na mwishowe waandaliwe kwa ajili ya mbingu. Uvueni ubinafsi, na angalia ikiwa hakuna wengi ambao unaweza kuwasaidia na kuwabariki kwa kutumia nyumba yako, huruma yako, upendo wako, na kwa kuwaelekeza kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Je! Unahitaji kutoa kafara yeyote ili kuokoa roho? Yesu, Mwokozi mpendwa, anaandaa sasa makazi kwa ajili yako; ni kwanini wewe pia kwa upande wako, usiandae mahali kwa ajili ya wahitaji, na kwa kufanya hivyo kuiga mfano wa Bwana wako? Ikiwa hauko tayari kufanya hivyo, wakati utakapohisi kuwa unahitaji makao mbinguni, hakuna atakayekuwa tayari kukupatia. Kwa maana Kristo anatamka: "Kwa vile ambavyo hamkumtendea mmoja wa hawa walio wadogo, hamkunitendea Mimi." Wewe ambaye umekuwa mbinafsi, ukijitafutia unafuu na urahisi wa maisha na mafanikio yako mwenyewe kwa maisha yako yote, muda wako wa rehema unafungwa kwa upesi. Je, unafanya nini ii kukomboa maisha yako ya ubinafsi na kutokuwa manufaa na malengo au maana ya maisha? Amka! Amka!{2Tsw 30}

Mnapozingatia maslahi yenu ya milele, jiamsheni wenyewe, na kuanza kupanda mbegu njema. Kile mkipandacho, ndicho mtakachovuna. Mavuno yanakuja—wakati mkubwa wa kuvuna, wakati tutakapovuna kile tulichokipanda. Hakutakuwa na kushindwa katika kuota kwa yale mazao mliyoyapanda; mavuno ni ya hakika. Sasa ni wakati wa kupanda mbegu. Sasa wewe ufanye bidii ya kujawa na matendo na kazi njema nyingi, "tayari kusambaza, tayari kuwasilisha na kuwasiliana," kujiwekea akiba wenyewe ya msingi mzuri dhidi ya wakati ujao, ili



“mkaushike uzima wa milele.” Ninawasihi, ndugu zangu katika kila sehemu, ondoeni ubaridi wenu unaoganda barafu. Jitieni moyo ndani yenu upendo wa kukaribisha wageni kwa huduma ya ukarimu, upendo wa kusaidia wale wanaohitaji msaada. {2Tsw 31.1}

Unaweza kusema umedanganyika na umewapatia mali zako wale wasiostahili upendo na hisani zako, na kwa hivyo “umevunjika moyo” katika kujaribu kuwasaidia wahitaji. Ninamleta Yesu mbele yako. Yeye Alikuwa kumwokoa mwanadamu aliyeanguka, kuleta wokovu kwa taifa Lake Mwenyewe; lakini hawakumpokea Yeye. Waliichukulia huruma Yake kwa tukano na dharau, na mwishowe, walimwua Yeye aliyekuja kwa kusudi la kuwapa uzima. Je, Bwana wetu aliiacha jamii ya wanadamu iliyoanguka kwa sababu ya hii? Ingawa juhudi zako za kutenda mema hazijafanikiwa mara tisini na tisa, na ulipokea matusi, kejeli, na chuki tu, bado ikiwa ile ya mara mia moja itathibitisha mafanikio, na roho moja ikaokolewa, Oh jamani! Itakuwa ni ushindi mkubwa kiasi gani, uliopatikana! Nafsi moja iliyong’atuliwa toka mikononi mwa Shetani au kifungoni mwake, roho moja iliyofaidika, roho moja iliyohamasishwa kwa kutiwa moyo, hii itakulipa mara elfu moja kwa juhudi zako zote. Kwako Yesu atasema:

“Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi.” Je, hatupaswi kufanya kwa furaha, yote tuwezayo kuiga maisha ya Bwana wetu wa Kiungu? Wengi husinyaa kwa wazo la kutoa kafara yoyote kwa manufaa ya wengine. Hawako tayari kuteseka kwa ajili ya kuwasaidia wengine. Wanajisifu kwa kujidanganya mno wenyewe kwamba hawahitajiki kupata hasara wenyewe kwa faida ya wengine. Kwa watu kama hao tunasema: Yesu Ndiye mfano wetu. {2Tsw 31.2}

Wakati ombi lilipotolewa kwa wana wawili wa Zebedayo kukaa mmoja mkono Wake wa kuume na mwingine mkono Wake wa kushoto katika ufalme Wake, Yesu alijibu: “Hamjui mnaloliomba. Mwaweza kunywa kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao Mimi? Wakamwambia, Twaweza. Yesu akawaambia, Kikombe ninyweacho Mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao Mimi mtabatizwa; lakini habari ya kuketi mkono Wangu wa kuume au mkono Wangu wa

kushoto si Langu kuwapa bali watapewa waliowekewa tayari na Baba Yangu.” Ni wangapi wanaweza kujibu: Tunaweza kunywa kikombe; tunaweza kubatizwa na ubatizo huo; na kutoa jibu kwa ufahamu? Ni wangapi wanamwiga Yeye aliye Mfano Mkuu? Wote waliodai kuwa wafuasi wa Kristo, kwa kuchukua hatua hii, waliahidi wenyewe kutembea kama Yeye alivyotembea. Walakini mwenendo wa wengi, wanaotoa madai ya juu kuhusu Ukweli huonesha kwa kiasi kidogo tu katika mfano wa maisha yao kufanana nayo. Wanatengeneza mwenendo wao kufikia kiwango chao chenye dosari. Hawaigi kujikana nafsi kwa Kristo au maisha Yake ya kujitoa kafara kwa faida ya wengine. {2Tsw 32.1}

Masikini, wale wasio na makazi, na wajane wako miongoni mwetu. Nimesikia mkulima tajiri akielezea hali ya mjane masikini aliye miongoni mwao. Aliomboleza hali yake ya umaskini, na kisha akasema: "Sijui ataishije wakati huu wa majira ya baridi. Ana nyakati ngumu za ufukara sasa." Hao wamesahau Kielelezo, na kwa matendo yao wanasema: "Hapana, Bwana, sisi hatuwezi kunywa kikombe cha kujikana nafsi, fedheha, kunyenyekeshwa na kafara, ambacho ulikinywea, wala kubatizwa na mateso ambayo ulibatizwa nayo. Sisi hatuwezi kuishi kwa kuwatendea mema wengine. Shuguli yetu sisi ni kujitunza wenyewe tu" Nani anapaswa kujua jinsi mjane atakavyoishi isipokuwa ni wale walio na maghala ya nafaka yaliyosheheni vizuri? Mali za kumfanya aishi zipo karibu tu. Na wale ambao Mungu amewafanya mawakili Wake, ambao amewakabidhi mali, wathubutu kuwazuilia wanafunzi wa Kristo wahitaji? Ikiwa ndivyo, wanamzuilia Yesu Mwenyewe. Je, unatarajia Bwana kunyesha nafaka kutoka mbinguni ili kuwapa wahitaji? Je, badala yake, Yeye hakuiweka mikononi mwako, ili kuwasaidia na kuwabariki wahitaji kupitia kwako? Je, Yeye Hakukufanya wewe kuwa chombo Chake katika kazi hii nzuri kukuthibitisha, na kukupa upendeleo wa kuweka hazina mbinguni? {2Tsw 32.2}

Watoto yatima wasio na baba na mama, wametupwa katika jukumu na mikono ya kanisa, na Kristo anawaambia Wafuasi Wake: Wachukueni watoto hawa masikini, waleeni kwa ajili Yangu, nanyi mtapokea ujira wenu. Nimeona ubinafsi mwingi ukidhihirishwa katika mambo haya. Kusipokuwa na ushahidi wa pekee kwamba wao wenyewe watafaidika

kwa kuwaasili katika familia zao wale wanaohitaji mahali pa kuishi, wengine hukataa, na kuondoka, na huku wakijibu hawaonekani kujua au kujali ikiwa watoto wa namna hiyo wanaokolewa au kupotea. Hili wao wanafikiri kuwa siyo wajibu wao. Wanasema pamoja na Kaini: “Je, Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” Hawako tayari kusumbuliwa au kutoa kafara yoyote kwa yatima, na bila kujali huwasukuma watoto kama hao katika mikono ya ulimwengu, ambao wakati mwingine wako tayari kuwapokea kuliko hawa watu wanaodai kuwa Wakristo, kwa mdomo tu. Katika siku ya Mungu, uchunguzi utafanywa kwa wale ambao mbingu iliwapa nafasi ya kuwaokoa. Lakini walitamani kutoa udhuru, na wasingeshiriki katika kazi nzuri, isipokuwa wangeweza kuvifanya kuwa suala la faida kwao. Nimeoneshwa kwamba wale wanaokataa fursa hizi za kutenda mema watasikia toka kwa Yesu: “Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi.” Tafadhali soma Isaya 58: {2Tsw 33.1}

Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua Mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na Bwana? Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” {2Tsw 33.2}

Hii ndiyo kazi maalumu sasa mbele yetu. Kuomba kwetu kote na kuacha kula hakutasaidia chochote isipokuwa tutashikilia kwa uthabiti kazi hii. Wajibu mtakatifu uko juu yetu. Wajibu wetu umetamkwa kwa udhahiri. Bwana amesema nasi kupitia nabii Wake. Mawazo ya Bwana na njia Zake, siyo yale ambayo watu vipofu na wabinafsi, ambao hufa huamini au vile ambavyo wanataka viwe. Bwana huangalia moyo. Ikiwa ubinafsi hukaa humo, Yeye Anajua. Tunaweza kutafuta kuwaficha tabia zetu halisi ndugu na dada zetu, lakini Mungu anajua. Hakuna anachoweza kufichwa Yeye. {2Tsw 34.1}

Mfungo ambao Mungu anaweza kuukubali umeelezewa. Ni kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nyumbani mwako. Usisubiri watu hawa waje kwako. Kazi haiko juu yao kukutafuta/kukuwinda wewe na kukusihi uwapatie mahali pa kukaa. Wewe unapaswa kuwatafuta na kuwaleta katika nyumba yako. Lazima nafsi yako ivutwe nao. Wewe unao mkono mmoja wa kufikia juu na kwa imani shika mkono wenye nguvu uletao wokovu, wakati kwa mkono mwingine wa upendo uwafikie watu walioonewa na kuwafariji kwa kuwapa afueni. Haiwezekani kwako kumshikilia Mungu kwa nguvu, kwa mkono mmoja wakati mkono mwingine unatumika katika kuhudumia anasa zako mwenyewe. {2Tsw 34.2}

Ukishiriki katika kazi hii ya rehema na upendo, je, kazi hiyo itaonekana kuwa ngumu sana kwako? Je, utashindwa na kusetwa chini ya mzigo, na familia yako kunyimwa msaada na mvuto wako? Lo, hapana; Mungu ameondoa kwa uangalifu mashaka yote juu ya hoja hii, kwa kuweka ahadi kwako kwa sharti la utii. Ahadi hii inajumuisha sana yote ambayo wenye kuhitaji zaidi, wenye kusita zaidi, wanaweza kuyatamani. “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara” Wewe Amini tu kwamba Yeye ambaye ameahidi ni Mwaminifu. Mungu anaweza kufanya upya nguvu za kimwili. Na zaidi, anasema Yeye atafanya. Na ahadi hii haikomei hapa. “Na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.” Mungu atajenga ngome kukuzunguka. Ahadi haishii tu hapa. “Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa.” Ikiwa utauacha uonevu na kuondoa maneno ya ubatili, ikiwa utamkunjulia nafsi yako mwenye njaa, “ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa

kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui” {2Tsw 35.1}

Soma Isaya 58, ninyi mnaodai kuwa watoto wa nuru. Hebu muisome kabisa, tena na tena, hasa ninyi mliohisi kusita sana kujisumbua kwa kuwafanyia fadhila wahitaji. Ninyi ambao mioyo na nyumba zenu ni finyu sana, kuwapatia wale wasio na makao, makazi, muisome; wewe unayeweza kuwaona mayatima na wajane wakiteseka kwa mkono wa chuma wa umaskini na kudhalilishwa na walimwengu wasio na huruma, isome. Je, una hofu kwamba mvuto utaingizwa katika familia yako ambao utakugharimu kufanya kazi zaidi, isome. Hofu yako inaweza kuwa haina msingi, na baraka inaweza kuja, inayojulikana na kutambuliwa na wewe kila siku. Lakini ikiwa vinginevyo, ikiwa kazi ya zaidi inahitajika, unaweza kuchota Kwake Yeye aliyeahidi: “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara” Sababu inayowafanya watu wa Mungu kutokuwa na mtazamo imara wa kiroho na kutokuwa na imani zaidi, nimeonyeshwa, ni kwa sababu wamekuwa na akili finyu za ubinafsi. Nabii anazungumza na watunza Sabato, siyo wasioamini, siyo watenda dhambi, bali wale wanaojidai kuwa na uchamungu na utauwa sana. Siyo wingi wa mikutano yako ya ibada ndiyo ambayo Mungu anaikubali. Siyo maombi mengi, lakini kutenda haki, kufanya jambo sahihi na kwa wakati unaofaa. Ni kujijali nafsi kidogo na kuwa mkarimu zaidi. Nafsi zetu lazima zitanuke. Ndipo Mungu atazifanya ziwe kama bustani iliyomwagiliwa maji, ambayo maji yake hayapungui. {2Tsw 35.2}

Soma Isaya 1: “Nanyi mkunjuapo mikono yenu, Mimi nitafigha macho Yangu nisiwaone; naam, mwombapo maombi mengi, Mimi sitasikia; mikono yenu imejaa damu. Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho Yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane. Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi;

bali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga; maana kinywa cha Bwana kimenena haya.-Isaya 1” {2Tsw 36.1}

Dhahabu iliyotajwa na Kristo, Shahidi wa Kweli, ambayo wote lazima wawe nayo, nimeoneshwa kuwa ni imani na upendo kwa pamoja, na upendo huitangulia imani. Shetani daima yuko kazini kuondoa zawadi/vipawa hivi vya thamani toka kwa mioyo ya watu wa Mungu. Wote wanahusika katika mchezo wa Maisha (drama ya Maisha). Shetani anajua vizuri kwamba ikiwa anaweza kuondoa upendo na imani, na kuweka katika pengo hilo ubinafsi na kutokuamini, tabia zote zilizobaki za thamani zitaondolewa haraka kwa ustadi kwa mkono wake wenye udanganyifu, na mtu atashindwa shindano la mchezo huo. {2Tsw 36.2}

Ndugu zangu wapenzi, je, mtamruhusu Shetani atimize kusudi lake? Je, mtajisalimisha ili kupoteza shindano hili ambalo kwalo mnatamani kushinda uzima wa milele? Ikiwa Mungu amewahi kunena kupitia mimi, basi mtashindwa na Shetani, badala ya kuwa washindi, kama vile ambavyo kiti cha enzi cha Mungu kinasimama hakika, hakika mtashindwa, isipokuwa muwe mmebadilishwa kabisa. Upendo na imani lazima vishinde tena na kuletwa maishani mwetu. Je! Utahusika katika mzozo huu upya na ushindwe kurudisha zawadi za thamani ambazo umekaribia kukosa? Utalazimika kufanya juhudi za dhati na bidii zaidi, kuvumilia zaidi na bila ya kuchoka, kuliko vile ambavyo umewahi kufanya. Sio tu kuomba au kufunga, lakini ni kwa kuwa mtiifu, kujitenga na ubinafsi, na kushika mfungo ambao Mungu ameuchagua, atakaokubali. Wengi wanaweza kuhisi huzuni kwa sababu nimesema waziwazi; lakini hii nitaendelea kufanya, ikiwa Mungu ameweka mzigo juu yangu. {2Tsw 37.1}

Mungu anahitaji kwamba wale wanaoshika nafasi za madaraka/uwajibikaji wanapaswa kujiweka wakfu kwa ajili ya kazi hiyo; kwa kuwa wakienenda au kujongea vibaya, watu watahisi kuwa na uhuru wa kufuata nyayo zao. Ikiwa watu wamekosea na viongozi hawapazi sauti dhidi ya huo ubaya, wanaidhinisha ubaya huo, na dhambi hiyo inadaiwa juu yao vile vile kama wacosaji. Wale ambao wanashika nafasi za uwajibikaji/madaraka wanapaswa kuwa watu

wenye kumcha Mungu, ambao daima wanahisi mzigo wa kazi iliyo juu yao. {2Tsw 37.2}

### **SURA YA 3**

#### **KUUZA HAKI YA UZALIWA WA KWANZA**

Ndugu Mpendwa D: Nimekuwa nikipanga kukuandikia kwa muda fulani, lakini kazi zetu zimekuwa endelevu na za kuchosha na hivyo sikupata muda wala nguvu kufanya hivyo. Katika njozi yangu ya mwisho nilioneshwa suala lako. Ulikuwa katika hali mbaya (ya taharuki). Uliijua Kweli, uliuelewa wajibu wako, na ulifurahi katika nuru ya Kweli; lakini kwa sababu viliingiliana na matakwa yako juu ya mambo ya kidunia, ulikuwa unakaribia kuitoa kafara ile Kweli na wajibu kwa manufaa yako mwenyewe. Ulikuwa ukishughulika na manufaa yako, hasa ya kifedha na ukipoteza maono ya utukufu ambao hauna mwisho. Ulikuwa karibu kutoa kafara kubwa sana kwa ajili ya matazamio ya kupendeza ya manufaa ya sasa ya kidunia, yenye udanganyifu. Ulikuwa katika hatua ya kuuza haki yako ya uzaliwa wa kwanza kwa chakula cha dengumwanzo 25. Kama ungegeuka toka katika Kweli kwa ajili ya manufaa ya kidunia, isingekuwa dhambi ya kutojua kwa upande wako, bali uasi wa kukusudia. {2Tsw 37.3}

Esau alitamani chakula apendacho, na akatoa kafara haki yake ya mzaliwa wa kwanza ili kuridhisha hamu ya kula-Mwanzo 25. Baada ya uchu wake wa hamu ya kula uliporidhishwa, akaona upumbavu wake, lakini hakutafuta nafasi ya kutubu ingawa aliitafuta kwa makini na kwa machozi. Kuna wengi sana ambao ni kama Esau. Anawakilisha kundi lililo na baraka maalumu, na ya thamani karibu na ufikiaji wao,—urithi usioharibika, maisha ambayo ni ya kudumu kama maisha ya Mungu (milele), Muumbaji wa ulimwengu, furaha isiyo na kipimo, na uzani wa

milele wa utukufu,—lakini ambao kwa muda mrefu wameendekeza hamu zao za uchu wa chakula, tamaa, mielekeo, na hata uwezo wao wa kutambua na kuthamini ile thamani ya mambo ya milele umehafifishwa. {2Tsw 38.1}

Esau alikuwa na tamaa ya kipekee, yenye nguvu kwa ajili ya chakula fulani bainishi, na kwa muda mrefu alikuwa ameiendekeza nafsi yake, kiasi cha kutohisi umuhimu wa kugeuka toka katika mlo wenye jaribu, alioutamani. Alitafakari juu ya hilo, pasipo kufanya juhudi ya kipekee ya kuzuia hamu yake ya chakula, hadi nguvu ya uchu wa chakula ikaathiri kila fikra nyingine na kumtawala, naye alifikiri kwamba angepata usumbufu mkubwa, na hata kifo, kama asingepata hicho chakula. Alivyozi kukifikiria chakula hicho, ndivyo hamu yake ilivyozi kupata nguvu zaidi, mpaka haki yake ya uzaliwa wa kwanza, iliyokuwa takatifu, ilipoteza thamani yake na utakatifu wake. Alifikiria, Nikiiuza sasa haki ya uzaliwa wangu wa kwanza, ninaweza kuinunua tena kwa urahisi. Alibadilishana haki yake ya uzaliwa wa kwanza kwa chakula akipendacho, akijifurahisha mwenyewe kwamba angeweza kuitupa kwa hiari haki hiyo, na kuinunua tena atakapotaka. Lakini alipotafuta kuinunua tena, hata kwa kafara kubwa sana kwa upande wake, hakuweza kufanya hivyo. Hatimaye alijutia kwa uchungu kukosa kwake subira, upumbavu wake, na wazimu wake. Alilitazama jambo hilo kila upande. Alitafuta kutubu kwa umakini na kwa machozi, lakini yote ilikuwa bure. Alikuwa amedharau baraka yake, na Bwana aliiondoa baraka hiyo kwake, milele. Umefikiri kuwa ikiwa utaitoa kafara ile Kweli sasa, na kuendelea katika mwendo wa uasi wa wazi na kutotii, usingevunja vizuizi vyote na kuwa mtu asiyejali, na ikiwa utasikitishwa na kukatishwa tamaa katika matumaini na matarajio yako ya kupata manufaa ya kidunia, unaweza tena kujitafutia maslahi katika Kweli na kuwa mtaradhia wa uzima wa milele. Lakini wewe umejidanganya mwenyewe katika jambo hili. Kama ungeitoa kafara ile Kweli kwa ajili manufaa ya kidunia, ingegharimu uzima wa milele. {2Tsw 38.2}

Katika mfano wa karamu kuu, Mwokozi wetu anaonesha kwamba wengi watauchagua ulimwengu dhidi Yake Mwenyewe, na kama matokeo, wataipoteza mbingu. Mwaliko wa neema wa Mwokozi wetu ulipuuzwa/ulidharauliwa. Alipitia taabu na gharama kufanya maandalizi



makubwa kwa kafara kubwa. Kisha akatuma mwaliko Wake; lakini “Wote Wakaanza kutoa udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, Nimenunua shamba, sharti niende nikalitazame; tafadhali unisamehe. Mwingine akasema, Nimenunua ng'ombe jozi tano, ninakwenda kuwajaribu; tafadhali unisamehe. Mwingine akasema, Nimeoa mke, na kwa sababu hiyo siwezi kuja.” Kisha Bwana anageuka toka kwa matajiri na wapenda ulimwengu, ambao ardhi na ng'ombe na wake zao vilikuwa vya thamani kubwa katika makadirio yao, kuliko faida ambazo wangepata kwa kukubali mwaliko wa neema aliokuwa amewapa wa kula katika karamu Yake. Bwana mwenye nyumba ana hasira, na anawaacha wale waliodharau zawadi Yake aliyowapa, Naye anaalika watu wa daraja ambalo halina kitu, ambalo halimiliki ardhi na nyumba, lakini ambao ni la watu masikini na wenye njaa, ambao ni vilema na vipofu, na ambao watathamini zawadi iliotolewa, na kwa upande wao watamrudishia Bwana shukrani ya dhati, ibada, upendo wa Kweli (usio bandia) na kujitolea. {2Tsw 39.1}

Bado kuna nafasi. Amri imetolewa: “Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutisha kuingia ndani, nyumba Yangu ipate kujaa. Maana nawaambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu Yangu.” Hapa kuna kundi la watu lililokataliwa na Mungu kwa sababu waliudharau mwaliko wa Bwana. Bwana alimwambia Eli: “Kwa maana wao wanaoniheshimu nitawaheshimu, na wao wanaonidharau watahesabiwa kuwa si kitu.” Kristo anasema: “Mtu akinitumikia, na anifuata; Nami nilipo, ndipo na mtumishi Wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu.” Mungu hatachezewa. Ikiwa wale wenye nuru wanaikataa, au kupuza kuifuata, kwao itakuwa giza. {2Tsw 40.1}

Kafara kubwa ilitolewa kwa upande wa Mwana mpendwa wa Mungu, ili aweze kuwa na nguvu ya kumwokoza mwanadamu aliyeanguka na kumwinua katika mkono Wake wa kuume, kumfanya awe mrithi wa ulimwengu na mmiliki wa uzani wa milele wa utukufu. Lugha haiwezi kueleza thamani ya urithi usioharibika. Utukufu, utajiri, na heshima vinavyotolewa na Mwana wa Mungu ni vya thamani isiyo na kipimo, inayozidi uwezo wa wanadamu au malaika kutoa maoni yoyote yaliyo sahihi juu ya thamani yake, ubora wao, ukuu wao. Ikiwa watu,

waliotumbukia katika dhambi na uharibifu, watakataa manufaa haya ya kimbingu, wanakataa maisha ya utii, wakikanyaga mwaliko wa fadhili ya rehema, na kuchagua vitu dhaifu vya dunia kwa sababu vinaonekana, na ni rahisi kuvifikia kwa vile hawapatwi na usumbufu na kuvifurahia kwa sasa ili kufuata mwendo wa dhambi, Yesu atatoa mfano katika fumbo; hawa hawatauonja utukufu Wake, bali mwaliko huo, watapewa watu wa kundi au daraja jingine. {2Tsw 40.2}

Wale wanaochagua kutoa udhuru na kuendelea katika dhambi na kupatana na ulimwengu, wataachwa katika sanamu zao. Kutakuwa na siku hawataomba kutoa udhuru, wakati hakuna hata mmoja atakayependa kupewa udhuru. Wakati Kristo atakapokuja katika utukufu Wake na utukufu wa Baba Yake, pamoja na malaika wote wa mbinguni -wakimzunguka, wakimsindikiza njiani kwa sauti za ushindi, wakati sauti ya muziki unaorindima na kupendeza unasikika katika katika sikio, ndipo wote watavutiwa; hakutakuwa na hata mtazamaji mmoja asiyejali. Nadharia hazitaijaza roho wakati huu. Rundo la dhahabu ya mtu mwenye choyo na ubahili, lililofurahisha macho yake kama karamu, halina mvuto tena. Miji na majumba ya kifalme ambayo watu wenye kiburi wa dunia wamejenga, na ambayo imekuwa sanamu zao, watayaacha kwa hiari-moyo na kuchukua vitu vyote hivyo. Hakuna mtu anayeitetea ardhi yake, ng'ombe wake, mkewe aliyemwoa, kama sababu ya kutoa udhuru kutoshiriki utukufu wa kushangaza unaotokea ghafla mbele ya macho yake. Wote wanataka kushiriki, lakini wanajua kuwa siyo fungu lao. {2Tsw 41.1}

Kwa maombi ya bidii, na maumivu makali wanamwomba Mungu asiwapite. Wafalme, watu wenye nguvu, wakuu, wenye fahari, wenye kiburi, wenye ubahili na jeuri, wote pamoja wanainama chini ya shinikizo la ole, ukiwa, na taabu isiyoelezeka; maombi ya uchungu mkali wa moyo yanatoka katika midomo yao. Rehema! rehema! Tuokoe na ghadhabu ya Mungu aliyekosewa! Sauti inawajibu kwa udhahiri wa kutisha, ukali, na fahari: “Kwa kuwa nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha Mkono Wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha shauri Langu, Wala hamkutaka maonyo Yangu; Mimi Nami nitacheka siku ya msiba wenu, Nitadhihaki hofu yenu ifikapo.” {2Tsw 41.2}

Ndipo wafalme na wakuu, mtu mwenye nguvu, na maskini, na mtu mwenye choyo, ubahili na jeuri, wote pamoja, watalia hapo kwa uchungu zaidi. Wale ambao katika siku za kufanikiwa kwao walimdharau Kristo na wanyenyekevu waliofuata nyayo Zake, watu ambao hawangenyenyekeza utu wao kumsujudia Kristo, waliouchukia msalaba Wake uliodharauliwa, sasa wamesujudu katika matope ya nchi. Ukuu wao wote umewaacha mara moja, na hawasiti kusujudu hata chini miguuni pa watakatifu. Ndipo wanagundua kwa uchungu wa kutisha kwamba wanakula tunda la njia yao wenyewe, na wamejazwa na mashauri yao wenyewe. Katika hekima yao ya kudhaniwa, waliacha thawabu ya juu, ya milele, walikataa mvuto wa mbinguni, kwa faida ya kidunia. Mng'ao na mapambo ya dunia viliwavutia, na kwa hekima yao ya kudhaniwa, wakawa wapumbavu. Walifurahi katika mafanikio yao ya kidunia kana kwamba faida za kidunia zilikuwa kubwa sana, kiasi kwamba kupitia kwazo wangempendeza Mungu, na hivyo kuipata mbingu. {2Tsw 41.3}

Pesa ilikuwa nguvu miongoni mwa wapumbavu wa dunia, na pesa ilikuwa mungu wao; lakini mafanikio yao yaliwaangamiza. Wakawa wapumbavu machoni pa Mungu na malaika Zake wa mbinguni, wakati watu wenye kutamani makuu ya dunia waliwafikiria kuwa wenye hekima. Sasa hekima yao ya kudhaniwa ni upumbavu, na mafanikio yao ni uharibifu wao. Wanatoa tena mayowe ya huzuni inayovunja moyo: “Wakiiambia milima na miamba, tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; Naye ni nani awezaye kusimama?” Wanayakimbilia mapango ya nchi kama maficho, lakini haya yanashindwa kuwa maficho wakati huo. {2Tsw 42.1}

Ndugu mpendwa, uzima au mauti yako mbele yako. Je, unajua kwa nini hatua zako zimejikwaa? Kwa nini hukuvumilia kwa ujasiri na uthabiti? Umeiharibu dhamiri yako (dhamiri yako imeharibiwa). Taaluma yako ya biashara haijawa nyofu. Unacho kitu cha kufanya hapa. Baba yako hakuangalia kanuni za biashara kwa nuru sahihi. Unaichukulia kama walimwengu wafanyavyo kwa ujumla, lakini sio kama Mungu anavyoiona. “Nawe umpende jirani yako kama nafsi yako.” Je,

umefanya hivi? “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote.” Ikiwa amri hii inatiiwa, inauandaa moyo kutii ya pili, inayofanana nayo: “Mpende jirani yako kama nafsi yako.” Amri zote kumi zinaunganishwa katika hizi mbili zilizoainishwa. Ya kwanza inajumuisha amri nne za kwanza, zinazoonesha wajibu wa mtu kwa Muumba Wake. Ya pili inajumuisha sita za mwisho, zinazoonesha wajibu wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. Ni mikono miwili mikubwa inayotegemeza amri zote kumi, nne za kwanza na sita za mwisho. Hizi ni lazima zifuatwe kwa umakini kabisa. {2Tsw 42.2}

“Ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri.” Wengi sana wanaodai kuwa wanafunzi wa Kristo inavyoonekana watapita bila shida katika ulimwengu huu, na watachukuliwa kama watu wanyofu, wacha Mungu, wakati kuna uharibifu katika kiini hasa, na hii huchafua tabia zao zote na kuharibu uzoefu wao wa dini. “Nawe mpende jirani yako kama nafsi yako.” Hii inatukataza kutumia faida ya wanadamu wenzetu ili kujinufaisha wenyewe. Tumekatazwa kumkosea jirani yetu kwa jambo lolote. Hatupaswi tulitazame jambo hili kwa mtazamo wa watu wa ulimwengu. Kushughulika na wanadamu wenzetu kwa kila kipengele kama tunavyotamani washughulike nasi katika sheria ambayo tunapaswa kuitumia sisi wenyewe kivitendo. Sheria za Mungu zinapaswa kutiiwa katika kila kipengele cha Andiko. Katika mazungumzo yetu yote na kushughulika na wanadamu wenzetu, ikiwa ni waumini au wasioamini, sheria hii inapaswa kutumika: “Mpende jirani yako kama nafsi yako” {2Tsw 43.1}

Hapa wengi wanaodai kuwa Wakristo hawatastahimili kipimo cha Mungu; watakapopimwa katika mizani ya Patakatifu, watakutwa wamepungua. Ndugu mpendwa, “tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na kike, asema Bwana Mwenyezi.” Ni ahadi iliyoje hii! Lakini hatupaswi kupoteza Ukweli kwamba ahadi hii inategemea utii wa amri. Mungu anawaita mjitenge na dunia. Hampaswi kufuata desturi zao, wala kufuatana nao katika vitendo au mwenendo wao kwa namna yoyote.

“Bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” {2Tsw 43.2}

Mungu anatoa mwito kwetu kujitenga na ulimwengu. Je, tutatii? Je, tutatoka kati yao, na kutengwa na kuwa tofauti nao? “Kwa maana kuna uhusiano gani kati ya haki na uovu? Au kuna ushirika gani kati nuru na giza?” Hauwezi kuchangamana na walimwengu, na kushiriki roho yao, na kufuata mfano wao, na kisha kuwa mtoto wa Mungu kwa wakati huo huo. Muumbaji wa ulimwengu anakuita kama Baba Mwenye mapenzi. Ikiwa utajitenga na ulimwengu katika mapenzi yako, na kubaki huru dhidi ya uchafu wake, ukiukimbia ufisadi ulioko ulimwenguni kupitia tamaa, Mungu atakuwa Baba yako, Yeye atakuasili katika familia Yake, nawe utakuwa mrithi Wake. Badala ya ulimwengu, Yeye atakupatia, badala yake, maisha ya utii, ufalme chini ya mbingu zote. Yeye Atakupa uzani wa milele wa utukufu na maisha ambayo ni ya kudumu kama umilele. {2Tsw 44.1}

Baba yako wa mbinguni anapendekeza kukufanya wewe uwe mwanafamilia ya kifalme, kwamba kupitia kwa ahadi Zake kubwa mno na za thamani, uweze kuwa mshiriki wa tabia ya malaika safi wasio na dhambi, na ya Kristo Mwokozi wako, ndivyo utabeba chapa ya Mungu kwa udhahiri zaidi, na ndivyo zaidi kufanana na dunia kutafifia. Ulimwengu na Kristo vinatofautiana sana, kwa sababu ulimwengu hautakuwa na umoja na Kristo. Ulimwengu pia utatofautiana na wafuasi wa Kristo. Katika ombi la Mwokozi wetu kwa Baba Yake, Anasema: "Nimewapa Neno Lako; na ulimwengu umewachukia, kwa sababu wao sio wa ulimwengu, kama vile Mimi nisivyo wa ulimwengu." {2Tsw 44.2}

Wito wako ni mkuu, na ulioinuliwa, kumtukuza Mungu katika mwili na roho yako, ambavyo ni Vyake. Wewe haupaswi kujilinganisha au kujipima na wengine. Neno la Mungu limekupatia wewe kielelezo kisichokosea, mfano usio na dosari. Wewe umeuogopa msalaba. Ni chombo chenye utata kubeba, chombo chenye usumbufu, na kwa sababu msalaba umefunikwa na fedheha na aibu, umeuepuka. Unahitaji kufanya matengenezo ya afya katika maisha yako; kwa

kujikana mwenyewe, na kula na kunywa kwa utukufu wa Mungu. Jiepushe na tamaa za mwili, zipiganazo na roho. Unahitaji kuwa na kiasi katika mambo yote. Hapa kuna msalaba ambao umeuepuka. Kujiwekea mipaka katika lishe rahisi, itakayokuhifadhi katika hali bora ya afya, ni kazi nzito kwako. Kama ungeishi kulingana na nuru ambayo Mbingu iliruhusu iangazee katika njia yako, familia yako ingeokolewa na maumivu mengi. Mwenendo wako mwenyewe umeleta matokeo ya hakika. Unapoendelea na mwenendo huu, Mungu hatakuja katika familia yako na hasa kukubariki na kufanya muujiza kuiokoa familia yako kutokana na mateso/maumivu. Lishe/Chakula cha kawaida kilicho rahisi, kisicho na viungo vyenye kukasirisha tumbo, nyama na shahamu ya kila aina, kingethibitisha baraka kwako na kingemwoko mke wako kwa kiasi kikubwa cha mateso, huzuni, na kukata tamaa. (Chakula rahisi ni kile ambacho ni cha asilia kinachotokana na mbegu za mimea na kinaepuka kadri inavyowezekana chakula kilichosindikwa au kukobolewa-Junkfood/vyakula vilivyo sawa na taka yaani sifuri au makapi, viungo ni vile visivyo na baking soda, pilipili manga, au vyenye kukasirisha tumbo) {2Tsw 45.1}

Hujafuata mwenendo ambao utakuhakikishia baraka za Mungu. Ikiwa unataka baraka Zake zikufuate, na uwepo Wake ukae katika familia yako, ni lazima umtii Bwana, ukifanya mapenzi Yake bila kujali hasara au faida au raha yako mwenyewe. Haupaswi kushauriana na matakwa yako binafsi, wala kibali/idhini ya walimwengu ambao hawamjui Mungu na hawatafuti kumtukuza Yeye. Ukitembea kinyume na Mungu, Yeye atatembea kinyume nawe. Ikiwa una miungu mingine mbele za Bwana, moyo wako utageuzwa toka katika kumtumikia Mungu pekee wa Kweli, na aliye hai, anayehitaji moyo wote, nafsi yote, akili yote na mapenzi yasiyogawanyika. Mungu anahitaji moyo wako wote, roho yote, akili yote, na nguvu zote. Yeye Hatakubali chochote pungufu ya hii. Hakuna kujitenga kunakoruhusiwa hapa; hakuna kazi isiyofanywa kwa moyo wote, itakayokubaliwa. {2Tsw 45.2}

Ili kumtolea Mungu huduma kamilifu, lazima uwe na ufahamu wa wazi kuhusiana na matakwa Yake. Unapaswa kutumia chakula rahisi zaidi, kilichoandaliwa kwa njia rahisi zaidi, ili neva nyeti za ubongo zenye afya zisidhoofishwe, zisihafifishwe, au kupooza, na kufanya iwe vigumu

kwako kutambua mambo matakatifu, na kuthamini upatanisho, naam, damu itakasayo ya Kristo, kama ya thamani kubwa. “Je! Hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.” {2Tsw 46.1}

Ikiwa watu wasio na kusudi la juu zaidi, hushabikia kupata taji la maua au taji iharibikayo kama tuzo ya tamaa zao, wanajitiisha katika kiasi katika mambo yote, ni kwa kiasi gani basi watu wanapaswa kuwa tayari kujikana wenyewe, naam, wale watu wanaodai kuwa wanatafuta, siyo tu taji ya utukufu wa milele, bali maisha ambayo yatadumu milele kama kiti cha enzi cha Yehova, na utajiri ambao ni wa milele, heshima ambazo haziharibiki, uzani wa milele wa utukufu. Je, vivutio vinavyowasilishwa mbele ya wale wanaokimbia katika mbio za Kikristo havitawaongoza kujizoesha katika kujikana nafsi na kiasi katika mambo yote, ili waweze kutiisha hulka zao za mnyama, kuuweka chini mwili kwa nidhamu, na kudhibiti hamu ya kula na tamaa mbaya? Ndipo wanaweza kuwa washiriki asili ya Mbinguni, kwa kuukimbia ufisadi uliomo ulimwenguni kupitia tamaa. {2Tsw 46.2}

Ikiwa thawabu ya thamani kuu na utukufu iliyoahidiwa haitatuongoza kukubali kujinyima mno na kustahimili kujikana nafsi zaidi kuliko watu wa dunia wavyostahimili kwa furaha, wanapotafuta mapambo madogo ya dunia, na taji ya maua iharibikayo, inayoleta heshima toka kwa watu wachache wa kidunia, na chuki toka kwa wengi zaidi,, basi hatustahili uzima wa milele. Katika bidii, udhati na uzito wa kina, ustahimilivu, ujasiri, nguvu, kujikana nafsi, na kafara, hakika tunapaswa kuwazidi wale walioshiriki katika shughuli nyingine yoyote, kwani kitu tunachotafuta kukipata ni cha thamani kubwa kuliko chao. Hazina tunayoitaafuta sio ya kuharibika, ila ya milele, ya kudumu, yenye utukufu sana; wakati ile waitafutayo walimwengu, hudumu kwa siku moja tu;

kwani ni ya kutokomea haraka, inafifia, ni ya kuharibika, na hutokomea kama wingu la asubuhi. {2Tsw 46.3}

Msalaba, msalaba; uinue, Ndugu D, na katika tendo la kuuinua utashangaa kuona kuwa unakuinua wewe, unakusaidia na kukutegemeza wewe mwenyewe. Katika taabu, ufukara, na huzuni nao utakuwa nguvu na fimbo kwako. Utapata yote yametundikwa na rehema, upole, huruma, na upendo usioelezeka. Utathibithishiwa ahadi ya kutokufa. Hebu uweze kusema na Paulo: “Lakini mimi, hashi, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu.” {2Tsw 47.1}

Roho wa Bwana amekuwa akipambana na mke wako kwa muda. Ikiwa ungesalimisha yote kwa Mungu, mke wako angekuwa na nguvu ya kusimama katika nafasi Yake, kutafuta kuuishi Ukweli. Ikiwa unachagua kugeuka kutoka katika Kweli, hautashuka chini peke yako; hautapoteza tu nafsi yako mwenyewe, lakini utakuwa njia ya kuwatoa wengine katika njia, na damu ya roho itakuwa juu ya mavazi yako. Kama ungedumisha uadilifu wako, mama yako, kaka yako E, na yule ambaye sasa anazunguka katika ukingo wa kaburi, sasa wangukuwa wakifurahia faraja ya Roho wa Mungu na kuwa na uzoefu mzuri katika Kweli. Daima tambua kwamba tunawajibika kwa mvuto tunaoutoa. Mvuto wetu hukusanya na Kristo au hutawanya nje. Ama tunazisaidia roho katika njia nyembamba ya utakatifu au sisi ni kikwazo, jiwe la kujikwaa kwao, tukiwatoa nje ya njia. Wewe, ndugu yangu ninayekuheshimu na kukuthamini sana, usiwe na muda wa kupoteza. Kuwa na bidii kuukomboa wakati, kwa sababu siku hizi ni za uovu. Wenzako, wale ambao umechagua ushirika nao, wamekuwa kikwazo kwako. Toka kati yao, ujitenge nao. Mkaribie Mungu; na kuja katika umoja wa karibu na watu Wake. Ruhusu shauku yako na mapenzi yako yajikite katika Kristo na wafuasi Wake. Wapende sana wale wanaompenda Kristo zaidi. Vikate vifungo/viunganishi ambavyo vimekufunga na wale wasiompenda Mungu na Kweli. “Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini? {2Tsw 47.2}



Uko katika hatari inayokaribia kuangamiza meli ya Imani yako (1Tim 1:19). Unahitaji nguvu zote unazoweza kutapata kutoka kwa watu wa Mungu, wale ambao wana tumaini, ujasiri, na imani. Lakini usipuuze maombi, maombi ya siri. Kuwa mwenye utayari na mwepesi katika kuomba; himiza roho ya ibada ya Kweli. Katika kazi yako ya biashara unayo kazi ya kufanya. Ni lipi la kufanya, siwezi kukuambia; lakini kuna kitu hakiko sawa kwako, kuna kosa fulani. Tafuta kwa uangalifu. Sisi tunafanya kazi kwa ajili ya umilele. Matendo yetu yote, maneno yetu yote, yanakwenda kupimwa katika mizani ya Patakatifu. Mungu Mwenye haki na asiye na upendeleo, anaamua kesi zetu zote, kila tukio la historia ya maisha yetu. Yule “Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; naye aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia” {2Tsw 48.1}

Usiruhusu chochote kizuie maendeleo yako katika njia ya kwenda katika uzima wa milele. Masilahi yako ya milele yako hatarini. Lazima kuwe na utendaji wa kazi kamilifu ndani yako. Lazima uwe na uongofu kamili, au utakosa mbingu. Lakini Yesu anakualika wewe umfanye Yeye kuwa nguvu yako, msaada na mhimili wako. Yeye Atakuwa kwako mwamba na msaada ulio karibu katika wakati wa uhitaji. Atakuwa kwako kama kivuli cha mwamba mkubwa wa kukupumzisha wakati wa taabu katika nchi yenye ukame, na uchovu (Zab 63:1). Wasiwasi wako usiwe mkubwa katika kufanikiwa katika ulimwengu huu, bali mzigo wa roho yako uwe: Je, nitaupataje ulimwengu ulio bora? Je, nifanye nini ili niokolewe? Katika kuokoa nafsi yako mwenyewe, unaokoa wengine. Katika kujiinua mwenyewe, unawainua wengine. Katika kukaza ufahamu wako juu ya Kweli na kiti cha enzi cha Mungu, unawasaidia wengine kukaza imani yao inayotetemeka juu ya ahadi Zake, na kiti Chake cha enzi cha milele. Msimamo ambao unapaswa kuwa nao ni kuthamini wokovu zaidi kuliko faida ya kidunia, kwa kuhesabu kila kitu kuwa hasara ili umpate Kristo. Kujiweka wakfu kwa upande wako lazima kuwe kamili. Mungu hatapokea masazo/makombo, dhabihu iliyogawanyika; huwezi kupenda au kuthamini sanamu yoyote. Lazima uifie nafsi na ulimwengu. Fanya upya kujitoa kwako kwa Mungu kila siku. Uzima wa milele unastahili jitihada ya maisha yote, ya kudumu, isiyochoka. {2Tsw 48.2}

Nilioneshwa kwamba kaka yako alikuwa ameshawishika na ile Kweli kwa muda, lakini mivuto ilimzuia. Mkewe alimzuia kutii usadikisho wake. Lakini katika taabu yake alimtafuta Bwana, Naye Bwana alipatikana. Kisha akahisi wasiwasi kwamba mumewe anapaswa kuikubali Kweli; alitubu kwamba alikuwa akimpinga, kwamba kiburi chake na kuupenda ulimwengu vilikuwa vimemzuia kwa muda mrefu kuipokea Kweli. Kama mtoto aliyechoka katika kutafta raha, lakini hakuweza kuipata kwa muda mrefu, aliutii mwaliko wa neema: "Njoo Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha." Nafsi yake iliyochoka na kulemewa ilimtafuta Bwana wake, na kwa toba, kujidhili na maombi ya dhati na bidii, alimtwika mzigo wake Mbeba Mizigo Mkuu, na Kwake akapata raha; alipata ushahidi kwamba unyonge wake na toba ya dhati vilikubaliwa na Mungu, na kwamba kwa ajili ya Kristo alimsamehe dhambi zake. {2Tsw 49.1}

Nilioneshwa, Ndugu D, kwamba una muda mfupi tu wa kufanya kazi. Fanya kazi yako kwa bidii na kikamilifu, uukomboe wakati. Katika shughuli zako za biashara, usiruhusu doa kuchafua tabia yako ya Kikristo. Tunza vazi lako, ili lisichafuliwe na ulimwenguni. Kesha na omba, usije ukaingia majaribuni. Majaribu yanaweza kukuzunguka,, lakini haulazimishwi kuingia kwayo. Unaweza kupata nguvu toka kwa Kristo kusimama bila mawaa katikati ya uchafu wa zama hizi zenye ufiisadi. "Tena kwa hayo Yeye ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." Dumu kukaza macho yako kwa Kristo, juu ya sura ya Mungu. Iga maisha Yake yasiyo na doa, nawe utakuwa mshirika wa utukufu Wake, na kurithi pamoja Naye, ufalme ulioandaliwa kwa ajili yako tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu. {2Tsw 49.2}

## **SURA YA 4**

### **KUNENA MABAYA**

Ndugu F amekuwa na kusudi la Mungu moyoni, lakini amekuwa na hisia za kina sana, na amejitwika mizigo mingi ambayo hakupaswa kuibeba. Ameteseka katika afya kwa njia hii. Wakati mwingine ametazama mambo kwa nuru yenye nguvu, na amekuwa na bidii sana na kusumbuka kuwa wote wayaone haya mambo kwa mtazamo kama wake; na kwa sababu walikuwa nyuma katika kufanya hivyo, amehisi kuvunjika moyo-amesagwa-sagwa. Anahisi mambo kwa kina sana, na yuko katika hatari ya kusesitiza mtazamo wake wa mambo, kwa nguvu sana. {2Tsw 50.1}

Dada F anataka kuwa Mkristo, lakini hakukuza busara, uungwana na adabu ya kweli. Yeye ni mwenye mwelekeo wa matarajio mema, mwenye shauku na kujiamini mwenyewe. Anaonesha upande rafu/mbaya wa tabia yake, na hii haijaonekana kuwa na faida. Anasukumwa na mhemko, akifanya kama vile alivyotaka, na wakati mwingine hisia zake zimesisimshwa sana na kuwa zenye nguvu. Ana mambo anayoyapenda sana kwa nguvu zake zote na ambayo hayapendi kabisa, na ameruhusu hii sifa mbaya kukua katika tabia yake kwa kiasi kikubwa, nayo imeathiri ukuaji wake kiroho na kuwa dhara kwa kanisa. Ameongea sana na bila busara, kwa namna alivyohisi. Hii imekuwa na ushawishi mkubwa kwa mumewe, na wakati mwingine imesababisha mumewe aondoke kwa kuongozwa na msisimko wa hisia, wakati ambapo angesubiri na kutazama mambo kwa utulivu na kuyapima vizuri, ingekuwa na manufaa kwake na kwa kanisa. Hakuna kinachopatikana kwa kwenda haraka, kusukumwa na mhemko, au kwa hisia kali. {2Tsw 50.2}

Dada F anasukumwa na mhemko, na kutafuta makosa, na amekuwa na mengi ya kusema dhidi ya ndugu na dada zake. Hii itasababisha machafuko katika kanisa lolote. Ikiwa angeweza kudhibiti roho yake mwenyewe, ushindi mkubwa ungepatikana. Ikiwa angetafuta mapambo ya mbinguni, naam, mapambo ya roho ya upole na utulivu, ambayo Mungu Mwenyewe, Muumba wa mbingu na dunia, anayaita kuwa ni ya gharama kubwa, basi atakuwa msaada wa Kweli kwa kanisa. Ikiwa angeliwaza na kuilea roho ya Kristo, na kuwa mpatanishi, nafsi yake mwenyewe ingesitawi/ingenawiri, na angekuwa baraka kwa kanisa mahali popote anapoweza kuwepo. Pasipo uongofu na

mabadiliko kamili kufanyika ndani yake, pasipo kujielimisha mwenyewe kutokuwa mwepesi katika kusema na kutokuwa mwepesi katika kugadhabika, na kukuza tabia ya adabu, uungwana na kujistahi kweli kwa Kikristo, ushawishi wake utakuwa wa kuumiza, na furaha ya wengine wanaohusiana naye itateseka. Anadhihirisha uhuru ambao ni uharibifu kwake na kuwatenga marafiki zake. Uhuru huu umemsababishia shida nyingi na umewajeruhi marafiki zake wa karibu. {2Tsw 51.1}

Ikiwa wale waliokuwa na mali walitenda dhuluma katika biashara na mumewe, na hawakumpendelea mumewe zaidi ya walimwengu katika miamala ya biashara, amehisi na kuzungumza, na kuibua hisia za kutoridhika ambazo hazikuwepo hapo awali. Huu ni ulimwengu wa ubinafsi kabisa. Wengi wa wale wanaoikiri Kweli hawajatakaswa nayo, na wanaweza kutokuwa na moyo wa kufanya hata tofauti ndogo katika bei za mazao ya mashambani, wanaposhughulika na ndugu masikini, mapema zaidi kuliko ambavyo wangepanya na walimwengu wenye uwezo. Hawawapendi majirani zao kama nafsi zao. Ingempendeza zaidi, Mungu ikiwa kusingekuwepo ubinafsi mwingi na uwepo ukarimu usio na ubinafsi zaidi. {2Tsw 51.2}

Kama Dada F alivyoona roho ya ubinafsi ikidhihirika katika biashara (dili), ametenda dhambi kubwa zaidi kwa kuhisi na kuzungumza kuhusiana jambo kama alivyofanya. Amekosea katika kuwa na matarajio makubwa zaidi. Hakika ulimi wake umekuwa kiungo kisichotawaliwa kwa hakika, ulimwengu wa uovu, umewasha moto wa jehanamu, haujafugwa, wala haufugiki. Dada F amekuwa na roho ya kulipiza kisasi, akidhihirisha kwa mwenendo wake kwamba aliudhiwa. Hii yote haikuwa sahihi. Amehifadhi hisia za uchungu, ambazo ni ngeni katika roho ya Kristo. Hasira, chuki, na kila aina ya tabia zisizo njema zinaendekezwa kwa kuzungumza kinyume dhidi ya wale wanaotuchukiza, na kwa kurudia-rudia makosa na kasoro na dhambi za majirani. Tamaa mbaya zinarithishwa na kuendekezwa. {2Tsw 51.3}

Dada F, ikiwa umehuzunishwa kwa sababu majirani au marafiki zako wanafanya vibaya kwa maumivu yao, ikiwa wamepatikana na makosa, fuata kanuni ya Biblia. “Enenda ukamwonye, wewe na yeye mkiwa peke

yenu.” Unapomwendea yule unayedhani kuwa amekosea, hakikisha kwamba unazungumza kwa roho ya upole na ya unyenyekevu; kwa kuwa hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. Mkosaji anaweza kurejeshwa sio kwa njia nyingine yoyote isipokuwa kwa roho ya upole, unyenyekevu, na kujali, huruma na upendo mwororo. Kuwa mwangalifu kwa haiba yako. Epuka chochote katika kutazama au ishara, Neno au sauti, au harufu yoyote ya kiburi au kujitosheleza nafsi. Jilinde dhidi ya Neno au kutazama kunakoweza kufanya ujiinue nafsi, au kuweka wema na haki yako kinyume na kisha kuanguka na kushindwa kwao. Jihadhari hata kwa mbali na tabia za kutoheshimu, ukandamizaji, jeuri, chuki au dharau. Kwa uangalifu epuka kila mwonekano wa hasira; na ingawa unatumia usemi wa wazi, hebu kusiwe na shitaka, lawama, kusiwe na ukosoaji wenye shutuma, wala dalili ya hasira au kuudhika bali ya upendo wa dhati. Zaidi ya yote, kusiwepo kivuli cha chuki, hiana au nia mbaya, kusiwe ukali au uchungu wa maneno. Hakuna kitu isipokuwa wema, uungwana na upole vinaweza kutiririka toka katika moyo wa upendo. Walakini haya matunda yote ya thamani yasikuzuie wewe kusema kwa njia ya umakini, adhimu na dhati kabisa, fanya kana kwamba malaika walikuwa wakikuelekezea macho yao kwako, na ulikuwa ukifanya yote kwa kurejelea hukumu inayokuja. Kumbuka kwamba mafanikio ya karipio hutegemea sana roho inayoletwa nayo. Usipuuze maombi ya dhati ili uweze kuwa na roho ya unyenyekevu, na kwamba malaika wa Mungu watangulie mbele yako ili kufanya kazi katika mioyo unayotaribu kuifikia, na kwa hivyo kulainisha kwa mivuto ya kimbingu ili juhudi zako zilete manufaa. Ikiwa wema wowote unatimizwa, wewe usijichukulie sifa kwako mwenyewe. Mungu pekee Yake Ndiye anapaswa kuinuliwa. Mungu pekee Ndiye aliyefanya yote hayo mema. {2Tsw 52.1}

Umetoa udhuru mwenyewe kwa kumsema vibaya ndugu au dada yako au jirani yako kwa wengine kabla ya kumwendea na kuchukua hatua ambazo Mungu ameamuru kabisa. Unasema: "Kwa nini, sikuongea na mtu yeyote hadi nilipolemewa sana hata sikuweza kujizuia." Ni nini kilikulemea wewe? Je, hakukuwa na upuuziaji wa wazi wa wajibu wako mwenyewe, wajibu wa 'hivi ndivyo asemavyo Bwana?' Ulikuwa chini ya hatia ya dhambi kwa sababu haukwenda kumwambia mkosaji kosa lake kati yako na yeye pekee yenu. Ikiwa haukufanya hivi, ikiwa

haukumtii Mungu, unawezaje kuwa vinginevyo, zaidi ya kuwa na mzigo, au moyo wako ulikuwa mgumu wakati ulipokuwa ukikanyaga amri ya Mungu chini ya miguu, na moyoni mwako ukimchukia ndugu au jirani yako? Na ni njia gani umepata ya kujiondolea mzigo? Mungu anakukemea wewe kwa dhambi ya kutotenda (sin of omission) kwa kutokumwambia ndugu kosa lake, nawe unatoa udhuru na kujifariji mwenyewe kwa dhambi ya kutotenda kwa kutomwambia ndugu yako kosa lake, na kutoa udhuru na kujifariji mwenyewe kwa dhambi ya kutenda kwa kusema dhambi za ndugu yako kwa mtu mwingine! Je, hii ndiyo njia sahihi ya kupata amani—kwa kutenda dhambi? {2Tsw 53.1}

Jitihada zako zote za kumwokoza mkosaji zinaweza kuwa za bure. Wanaweza kukulipa mabaya kwa mema. Wanaweza kukasirishwa badala ya kusadikishwa. Je, itakuwaje ikiwa watasikia bila kusudi jema, na wakaendelea kufuata njia mbaya waliyoianza? Hili litatokea mara kwa mara. Wakati mwingine maonyo ya upole zaidi hayatakuwa na matokeo mazuri. Kwa hali hiyo baraka ulizotaka mwingine apate kwa kufuata mwendo wa haki, kuacha kufanya uovu na kujifunza kufanya vyema, zitarudi kifuani mwako mwenyewe. Ikiwa mkosaji anaendelea katika dhambi, mtendee kwa wema, na umwache na Baba yako wa mbinguni. Wewe utakuwa umeikoa roho yako; dhambi yao haiko juu yako tena; sasa wewe sio mshirika wa dhambi yao. Lakini wakipotea/wakiangamia, damu yao iko juu ya vichwa vyao wenyewe. {2Tsw 53.2}

Rafiki mpendwa, mabadiliko kamili lazima yafanyike ndani yako, la sivyo utapimwa katika mizani na kukutwa unapungua. Kanisa katika ---, hasa wanawake wanaozungumza-zungumza, wana somo la kujifunza. “Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai.” Wengi watapimwa katika mizani na kukutwa wanapungua katika jambo hili lenye umuhimu mkubwa. Wako wapi Wakristo wanaotembea kwa kanuni hii? Ni nani atakuwa upande wa Bwana dhidi ya mnema mabaya? Nani atampendeza Mungu, na kuweka ulinzi, ulinzi endelevu, mbele ya kinywa, na kulinda mlango wa midomo? Usinene mabaya juu mtu yeyote. Usisikie mabaya ya mtu yeyote. Ikiwa hakutakuwa na wasikilizaji, hakutakuwa na wanema mabaya. Ikiwa kuna mtu yeyote

ananena mabaya mbele yako, mchunguze. Kataa kumsikiliza, hata kama namna yake ya kusema iwe laini sana na lafudhi yake tamu. Mtu huyu anaweza kuonekana na upendo, na bado akanena maneno ya mafumbo kwa siri na kuichoma kisu tabia ya mhusika gizani. {2Tsw 54.1}

Kataa kabisa kusikia mambo hayo kwa kudhamiria, ingawa mnong'onezaji analalamika juu ya kulemewa mpaka atakaposema. Kulemewa hakika! Na siri iliyolaaniwa inayowatenganisha marafiki wa karibu. Nendeni zenu ninyi mliolemewa, na mjiweke huru na mizigo yenu kwa njia iliyoichagua Mungu. Kwanza nenda umwambie ndugu yako kosa lake kati yako na yeye peke yake. Hii ikishindikana, chukua rafiki yako mmoja au wawili, na umwambie mbele yao. Ikiwa hatua hizi zitashindwa, ndipo uliambie kanisa. Usimwambie mtu asiyeamini, huyu hapaswi kufahamu hata sehemu fulani ndogo ya jambo hilo. Kuliambia kanisa ni hatua ya mwisho kuchukuliwa. Usilitangaze jambo kwa maadui wa imani yetu. Hawana haki ya kujua masuala ya kanisa, udhaifu na makosa ya wafuasi wa Kristo yasije yakafichuliwa. {2Tsw 54.2}

Wale ambao wanajiandaa kwa kuja kwa Kristo wanapaswa kuwa na kiasi na kukesha kwa maombi, kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze; ambaye tunapaswa kumpinga kwa uthabiti katika imani. “Kwa maana, atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme hila. Na aache mabaya, atende mema; Atafute amani, aifuate sana. Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio Yake husikiliza maombi yao.” {2Tsw 54.3}

## SURA YA 5

### UBINAFSI NA KUPENDA ULIMWENGU

Wapendwa ndugu na dada G: Kwa muda nimekusudia kuwaandikia. Kama nuru ambayo Bwana amenipa ilivyokuja kwa wazi mbele yangu, mambo mengine yalisongamana kwa nguvu katika akili yangu nilipokuwa nimesimama mbele ya watu huko ----. Nilitumaini kwamba mtakaa katika mkutano mwingine, na kwamba kazi iliyoanza huko ingeweza kuendelea. Lakini nasikitika kuona kwamba wakati ndugu zetu wanapohudhuria Mkutano, kwa ujumla hawahisi umuhimu wa kujiandaa kwanza kwa ajili mkutano. Badala ya kujiweka wakfu kwa Mungu kabla ya kuja, wanasubiri hadi wafike kwenye mkutano ili kazi ifanyiwe ndani yao huko. Wanaileta nyumba pamoja nao, na vitu ambavyo wanavyoviacha nyuma vinachukuliwa kuwa vya thamani na umuhimu kuliko maandalizi ya moyo kwa ajili kuja Kwake. Kwa hivyo karibu wote wanaondoka wakiwa sio bora kuliko walipokuja. Mikutano kama hiyo inahudhuriwa kwa gharama kubwa, na ikiwa wale wanaokuja hawafaidiki, kuna hasara kwao, na hufanya kazi kuwa ngumu sana kwa wale wanaohisi mzigo wa kazi juu yao. Watu wetu waliondoka kwenye Mkutano huo mapema sana. Labda tungeweza kuona kazi ya pekee zaidi kutoka kwa Mungu ikiwa wote wangebaki na kushiriki katika kazi. {2Tsw 55.1}

Dada G, nina ujumbe kwako. Wewe uko mbali na ufalme. Unaupenda ulimwengu huu, na upendo huu umekufanya upoe na kuwa baridi, mbinafsi, mkali, na bahili. Kitu kikubwa unachokipenda ni dola (\$) yenye thamani kuu. Unajua kwa kiasi kidogo jinsi Mungu anavyomtazama mtu mwenye hali kama yako. Uko katika udanganyifu wa kutisha. Umefanana na ulimwengu badala ya kugeuzwa kwa kufanywa upya nia yako. Ubinafsi na kujipenda mwenyewe vinadhihirishwa katika maisha yako kwa kiwango kikubwa. Hujashinda hii kasoro isiyo nzuri, isiyofurahisha katika tabia yako. Ikiwa hili halitarekebishwa, utapoteza mbingu, na furaha yako hapa itakuwa imeharibiwa sana. Hili limekuwa hivyo tayari. Wingu jeusi lililokufuata,



likifunika maisha yako, litakua kubwa na jeusi mpaka anga lako lote limefunikwa. Unaweza kugeukia kulia, na hakutakuwa na nuru, na kushoto, nawe hutaona mwale. {2Tsw 56.1}

Unajitaabisha mwenyewe mahali ambapo hakuna taabu, kwa sababu hauko sahihi. Haujajiweka wakfu. Roho yako ya kulalamika, ya ubahili inakufanya usifurahi, nayo haimpendezi Mungu. Katika maisha yako umekuwa ukijijali mwenyewe, ukitafta kujifurahisha mwenyewe. Hii ni kazi mbaya masikini, ni biashara isiyo na faida. Kadri unavyozidi kuwekeza hapa ndivyo hasara itazidi kuwa kubwa. Kadri unavyochukua bidhaa kidogo katika biashara hii ya kujihudumia mwenyewe, ndivyo kutakavyokuwa na uwezekano mkubwa sana wa kuokolewa kwa upande wako. Wewe ni mgeni kwa upendo usiojipendelea na kujifikiria, ule usio na ubinafsi, usio na uchoyo, na wakati hauoni dhambi maalum kwa kukosekana kwa tabia hii ya thamani, hautakuwa na bidii/uadilifu ya kupapalilia tabia hii. {2Tsw 56.2}

Ulimpenda mumeo na kuolewa naye. Ulijua kuwa wakati ulipooana naye uliweka agano naye kuwa mama kwa watoto wake. Lakini niliona upungufu kwako katika jambo hili. Kwa kusikitisha mno, wewe umepungua. Huwapendi watoto wa mumeo, na kusipokuwepo mabadiliko kamili, matengenezo kamili kwako, na katika namna yako ya utawala, vito hivi vya thamani vimeharibiwa. Upendo, udhihirisho wa mapenzi, sio sehemu ya nidhamu yako. Je, nikwambie Ukweli na kuwa adui yako kwa kufanya hivyo? Wewe ni mbinafsi sana kuwapenda watoto wa mwingine. Nilioneshwa kuwa matunda ya muungano wenu hayatastawishwa na kubarikiwa na nguvu, uzima, na afya, na Roho wa Mungu angekuacha wewe, ili uwe mwenyewe, usipothibitishwa kabisa na kujaribiwa, na kusahihisha vitu ambavyo unapungukiwa sana. Kama vile ambavyo ubinafsi wako unavyonyausha na kuharibu mioyo michanga inayokuzunguka, ndivyo laana ya Mungu itakavyonyausha na kuharibu ahadi za upendo wako wa ubinafsi na muungano. Na ukiendelea na mwendo wako wa ubinafsi, Mungu atakuja bado karibu nawe na kuondoa sanamu zako, moja baada ya nyingine kutoka mbele ya uso wako mpaka utakaponyenyekesha moyo wako wenye kiburi, ubinafsi, na usiojitiisha, mbele Zake. {2Tsw 56.3}

Niliona kwamba utakuwa na hesabu ya kutoa, inayotisha katika siku ya Mungu kwa sababu ya wajibu wako ambao haukutimizwa. Unafanya maisha ya watoto hao wapendwa kuwa machungu sana, hasa ya mabinti. Yako wapi mapenzi, mpapaso wa upendo, na ustahimilivu wa subira? Chuki inaishi katika moyo ambao haujatakaswa zaidi ya upendo. Lawama na kukosoa, hutoka midomoni mwako zaidi ya sifa na kutia moyo. Tabia zako, njia zako za ukali, asili yako isiyo na huruma, ni kama mvua ya mawe, yenye kuleta uharibufu kwa mche mwororo kwa huyo binti aliye mwepesi kuumia; huiama kwa kila mvua ya mawe kutoka kwako, hadi uhai wake uvunjwe, na kuchubuliwa na kuvunjwa. {2Tsw 57.1}

Uongozi wako unakausha mkondo wa upendo, matumaini, na furaha kwa watoto wako. Huzuni ya kudumu inaonekana katika uso wa msichana, lakini, badala ya kuamsha huruma nyororo na upole ndani yako, hii inaamsha kukosa uvumilivu na chuki ya waziwazi. Unaweza kubadilisha hali hii usoni mwako kwa uchangamfu, utendaji mwema na furaha halisi ukichagua. “Je, Mungu haoni? Je, Hatambui?” yalikuwa maneno ya malaika. Bwana Atakutembelea kwa mambo haya. Ulichukua jukumu hili kwa hiari yako mwenyewe, lakini Shetani ametumia tabia yako ya kukosa ucheshi, kukosa upendo, na kutopendeka, kujipenda mwenye, ubahili, uchoyo, ubinafsi wako kujipatia faida, na sasa inaonekana katika upotovu wake wote, isiyosahihishwa, isiyotawalika, ikikufunga kama mikanda ya chuma. Watoto wanaweza kusoma sura ya mama; wanaelewa ikiwa upendo au chuki inaonyeshwa hapo. Hujui kazi unayoifanya. Je, uso mdogo wenye huzuni, na kushusha pumzi ya afueni kwa moyo uliosongwa kwa matamano, hauamshi upendo wala huruma nyororo moyoni mwako? Hapana, siyo ndani yako. Inamweka mtoto katika umbali kutoka kwako na huongeza chuki yako. {2Tsw 57.2}

Niliona kwamba baba hakuchukua hatua ambayo baba anapaswa. Mungu hafurahishwi na msimamo wake. Mwingine ameiba moyo wa baba toka katika damu ya damu yake na mfupa wa mfupa wake. Ndugu G, umepunguka sana katika utambuzi. Kama kichwa cha nyumba, ungepaswa kuchukua msimamo wako na kutokuruhusu mambo kwenda jinsi yalivyokwenda. Umeona kuwa mambo hayakuwa

sawa na wakati mwingine umehisi mfadhaiko, lakini hofu ya kutompendeza mke wako wa sasa na kuleta ugomvi huondoa furaha katika familia yako, kumefanya ukae kimya wakati ulipaswa kusema. Hauleweki katika suala hili. Watoto wako hawana mama wa kuwaombea, wa kuwalinda dhidi ya lawama kwa maneno yake yasiyopimwa kwa busara. {2Tsw 58.1}

Watoto wako, na watoto wengine wote ambao wamepoteza yule ambaye ndani ya kifua chake upendo wa mama umetiririka, wamekutana na hasara ambayo haiwezi kujazwa. Lakini mtu anapojitokeza kusimama mahali pa mama kwa kundi dogo lililopigwa na shida, utunzaji na mzigo maradufu upo juu yake, hivyo mtu huyu apaswa kuwa mwenye upendo zaidi kadri inavyowezekana, kuwa mwangalifu zaidi katika kukosoa na kutokuwa tishio kuliko mama yao wenyewe angeweza kuwa, na kwa njia hii kujaza hasara ambayo kundi dogo limepata. Wewe, Ndugu G, umekuwa kama mtu aliyelala. Wachukue watoto wako moyoni mwako, wazunguke na mikono yako yenye ulinzi, uwapende kwa moyo mwororo. Ukishindwa kufanya hivi, “Utaonekana kuwa umepungua” itaandikwa dhidi yako. {2Tsw 58.2}

Kuna kazi ya kufanya kwa ajili yenu nyote wawili. Acheni kabisa manung'uniko yenu. Ndugu G, usihangaike na roho ya uchoyo, ubahili, ubinafsi wa roho ya mke wako kutawala matendo yako. Mmekuwa mkinywa katika roho hiyo hiyo, na nyote mmemwibia Mungu. Ombi la umasikini liko katika midomo yenu, lakini Mbingu inajua sio la kweli; ila maneno yenu yatakuwa Kweli yote; mtakuwa maskini kweli kweli, ikiwa mtaendelea kuthamini upendo wa ulimwengu kama manavyofanya. “Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana.” Ondoa na kupangusa laana hii haraka iwezekanavyo. {2Tsw 59.1}

Ndugu G, kama wakili wa Mungu, mtazame Yeye. Ni Kwake ndipo utatoa hesabu ya uwakili wako, sio kwa mke wako. Ni mali ya Mungu ndiyo unashughulika nayo. Yeye Amekuazima kwa kitambo kidogo tu ili kukuthibitisha, kukujaribu, kuona ikiwa utakuwa “tajiri kwa kutenda mema, tayari kutoa mali zako, tayari kuwasiliana na wengine kwa

moyo,” huku ukijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili upate uzima wa milele. Mungu atahitaji mali Yake na riba. Hebu Yeye akusaidie kujiandaa kwa ajili ya hukumu. Hebu nafsi isulubiwe. Hebu neema za thamani za Roho ziishi ndani ya mioyo yenu. Ukataeni ulimwengu na tamaa zake mbaya. “Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.” Ikiwa kukiri kwako kuko juu kama mbingu, walakini wewe ni mbinafsi na mwenye kuipenda dunia, huwezi kuwa na sehemu katika ufalme pamoja na wale waliotakaswa, walio safi na watakatifu. “Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.” Ikiwa hazina yako iko mbinguni, moyo wako utakuwa huko. Utazungumza juu ya mbingu, uzima wa milele, taji isiyoharibika. Ukiweka hazina yako duniani, utazungumzia vitu vya kidunia, ukiwa na hofu juu ya hasara na faida. “Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, na akapata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?” {2Tsw 59.2}

Kuna nuru na wokovu kwa ajili yako, ikiwa utahisi tu kuwa lazima uipate au upotee. Yesu aweza kuwaokoa kwa kiasi cha juu kabisa. Lakini, Dada G, ikiwa Mungu amewahi kusema nami, umedanganywa sana kuhusiana na wewe mwenyewe, na lazima uwe na uongofu kamili, au kamwe hautakuwa mmoja miongoni mwa wale ambao wametoka katika dhiki kuu, baada ya kuosha mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.-{2Tsw 60.1}

## SURA YA 6

### VYAKULA VYA NYAMA NA VICHOCHEO (Flesh meats and stimulants)

Ndugu mpendwa na Dada H: Nilikumbuka nyuso zenu kuwa kati ya watu kadhaa, ambao niliwaona wakihitaji kazi ikamilishwe kwao, kabla ya kutakaswa kupitia Kweli. Uliikumbatia Kweli kwa sababu uliona kuwa Kweli, lakini bado haijaukushikilia wewe. Hujatambua mvuto wake unaotakasa katika maisha. Nuru imekuwa ikiangaza katika njia yako kwa habari ya matengenezo ya afya na wajibu uliopo juu ya watu wa Mungu katika siku hizi za mwisho ili kutenda na kuwa na mazoea kwa mambo yote kwa kiasi. Wewe niliona, ukiwa miongoni mwa idadi ya wale ambao wangekuwa nyuma kuona nuru na kurekebisha namna yako ya kula, kunywa, na kufanya kazi. Kadri Mwanga wa Kweli unapopokelewa na kufuatwa, utafanya matengenezo kamili katika maisha na tabia ya wale wote wanaotakaswa nayo. {2Tsw 60.2}

Biashara yako ni ya tabia ambayo sio rafiki kwa maendeleo ya maisha matakatifu, lakini ni ile ambayo itazuia ukuaji wa neema na ujuzi wa Kweli. Ina tabia ya kupunguza, kushusha thamani ya mtu, na kumfanya mtu kuwa mnyama zaidi kwa tabia yake. Nguvu za juu za akili zinashindwa na zile za chini. Sehemu ya kinyama ya asili yako inatawala ile ya kiroho. Wale wanaodai kuwa wanafaa kutwaliwa mbinguni hawapaswi kuwa wakatili kwa kuchinja wanyama (kuwa watendakazi wa bucha/butchers). {2Tsw 60.3}

Familia yako imeshiriki sana katika ulaji wa vyakula vya nyama, na tabia za kinyama zimeimarishwa, wakati akili imedhoofishwa. Tumejengwa na kile tunachokula, na tukiishi kwa kiasi kikubwa kwa nyama ya wanyama waliokufa, tutashiriki asili yao. Umeendekeza sehemu ya uovu zaidi ya tabia yako wakati ile iliyosafishwa zaidi imekuwa dhaifu. Umesema kwa kurudia-rudia, katika kutetea na kuendekeza kwako ulaji wa nyama: “haijalishi kwamba inaweza

kuwadhuru wengine sana, ila mimi hainidhuru, kwa kuwa nimeitumia maisha yangu yote.” Lakini haujui ni jinsi gani ungekuwa bora, ikiwa ungeepuka matumizi ya vyakula vya nyama. Kama familia, wewe uko mbali na kuwa huru dhidi ya ugonjwa. Umetumia mafuta ya wanyama, ambayo Mungu katika Neno Lake anakataza kabisa: “Neno hili litakuwa amri ya daima, katika vizazi vyenu vyote, ndani ya nyumba zenu zote, ya kwamba hamtakula mafuta wala damu kabisa.” “Tena msile damu yoyote, ama ya ndege, ama ya mnyama, katika nyumba zenu zote.” {2Tsw 60.4}

Una ulaji wa nyama na samaki, lakini sio kitu kizuri. Uko katika hatari kubwa kwa kiasi hiki cha nyama. Ikiwa kila mmoja wenu atafikia kutumia kiasi kidogo cha lishe, ambayo itapunguza kwako pauni ishirini na tano au thelathini ya uzito wako wote, mngepata ugonjwa kwa kiasi kidogo zaidi. Ulaji wa vyakula vya nyama umefanya duni ubora wa damu na mwili. Mifumo yenu iko katika hali ya kuvimba (inflammation), na ina utayari wa kupata magonjwa. Itakuwa rahisi kwenu kupata mashambulio makali sana ya magonjwa na kifo cha ghafla kwa sababu hamna nguvu za mwili ya kushindana na kupinga magonjwa. Utafika wakati nguvu na afya mliyojisifu kwa kujidanganya kwamba mnayo, itaonekana kuwa udhaifu. Siyo kusudi kubwa la mwanadamu kulitukuza tumbo lake. Unajisikia kama vile una hitaji la nyama linalopasa kujaziwa; lakini kwa sababu ya tamaa hii je, mwanadamu atakuwa mnyama kiujumla? [Soma zaidi kuhusu asili ya tabia ya kinyama binadamu anayopata akila-kila nyama (animalize nature), makabila yanayokula sana nyama yanawezekana kuonekana na tabia hizo mara zingine-Meat eating animalizes a person] {2Tsw 61.1}

Umewawekea watoto wako meza ya chakula kisichofaa, kilichokobolewa na kusindikwa, kilichopikwa kwa njia isiyofaa. Umewawekea vyakula vya nyama mbele yao, na matokeo ni nini? Je, wamekuwa safi, wenye akili mahiri, watiifu, waangalifu, na wenye mwelekeo wa kidini? Unajua hii sivyo ilivyo, lakini kinyume kabisa. Mtindo wako wa maisha, umeimarisha asili yako ya unyama na kudhoofisha asili ya kiroho. Umepitisha kwa watoto wako urithi wa kusikitisha, asili iliyo potofu inaongezwa zaidi kuwa potufu kwa tabia

zako mbaya za kula na kunywa kwa ujumla. Meza yako imekamilisha kazi ya kuwafanya vile walivyo. Dhambi iko mlangoni mwako. Unajua kwamba hawana mwelekeo wa kidini au mambo ya kiroho, kwamba hawatakubali vizuizi, lakini watakuwa na mwelekeo wa kutotii na kudharau mamlaka yako. Mwana wako mkubwa hasa ni mpotovu, ana kiwango kikubwa cha ulaji wa unyama. Kwa kiasi kidogo sana, dalili ya utakatifu inaweza kuonekana mwilini mwake. Umewalea watoto wako ili kuendekeza uchu wa chakula, wanapopenda na kama watakavyo. Mfano wako umewafundisha kuwa wao wanaishi ili kula tu, kwamba kuridhisha hamu ya kula ni kila kitu kinachostahili kuishi kwacho. Kuna kazi ya kufanya kwa ajili yako, Ndugu H. Umekuwa kama mtu aliyelala au kupooza kwa kiharusi. Ni wakati sasa ufanye juhudi kubwa kuokoa wanafamilia yako wadogo. Mvuto wa mtoto wako mkubwa ni uovu tu juu yao. Sahihisha meza yako. Chakula kibaya na cha kuisisimua kinaimarisha tamaa za kinyama kwa watoto wako. Kati ya familia zote ninazozifahamu, yako ndiyo inahitaji kuachana na nyama na mafuta ya nyama zaidi, na kujifunza kupika kwa afya, kujikinga na magonjwa na usafi. {2T 61.2}

Dada H ni mwanamke ambaye damu yake imeharibika. Mfumo wake umeharibika kwa uvimbe kwenye mitoki, na kifua kikuu kutokana na ulaji vyakula vya nyama (scrofulous humors). Matumizi ya nyama ya nguruwe katika familia yako imetoa ubora mbaya wa damu. Dada H anahitaji kujifungamanisha na lishe ya nafaka zisizokobolewa, matunda, na mboga, zilizopikwa bila nyama au mafuta mazito kama vile siagi (grease) ya aina yoyote au mafuta ya wanyama. Itachukua muda mrefu kabisa wa kutumia lishe bora kwa umakini sana, ili kukuweka katika hali nzuri ya afya, ambapo utahusiana sawa na maisha. Haiwezekani kwa wale wanaotumia kwa uhuru vyakula vya nyama kuwa na ubongo usiofunikwa na akili yenye utendaji mahiri. {2T 62.1}

Tunakushauri ubadilishe mazoea yako ya kuishi-mtindo wa maisha; lakini wakati unafanya hivi tunakutahadharisha kwenda kwa uelewa. Ninajua familia ambazo zimehama toka lishe ya nyama na kwenda kwenye chakula ambacho lishe yake imepelea sana kwa lishe. Chakula kinaandaliwa vibaya sana, na tumbo hukichukia; na hao wameniambia

kwamba matengenezo ya afya hayakukubaliana nao, kwamba walikuwa wakitindikiwa katika nguvu ya mwili. Hapa kuna sababu moja kwa nini wengine hawajafanikiwa katika juhudi zao za kurahisisha chakula chao. Wana lishe ya kimaskini-duni. Chakula hakiandaliwi kikamilifu au kwa juhudi, na hakibadiliki kwa muda mrefu. Haipaswi kuwa na aina nyingi ya vyakula katika mlo mmoja, lakini milo yote haipaswi kuwa na aina moja ya chakula bila kutofautisha. Chakula kinapaswa kuandaliwa kwa usahili, lakini kwa uzuri ambao utaleta hamu ya kula. Unapaswa kuondoa mafuta mazito (grease) katika chakula chako. Yanaleta shida na kuharibu katika utayarishaji wowote wa chakula unachotengeneza. Kula kwa wingi matunda na mboga za majani. {2T 63.1}

Baada ya kupunguza nguvu zao za mwili kwa kupunguza ujazo na kiwango duni cha chakula, wengine huhitimisha kwamba njia yao ya zamani ya kuishi ndiyo bora zaidi-mtindo wa maisha wa zamani, eti ndio bora. Mfumo lazima upate lishe bora. Hata hivyo hatusiti kusema kwamba vyakula vya nyama siyo lazima kwa afya au nguvu. Ikiwa kinatumiwa ni kwa sababu uchu uliopotoka unatamani chakula hicho. Matumizi yake huchochea tabia za kinyama na kuongeza ukatili na kuimarisha tamaa za kinyama. Wakati tabia za kinyama zinaongezeka, nguvu za kiakili na kimaadili zinapungua. Matumizi ya nyama za wanyama huonekana kusababisha ongezeko la uzito wa mwili na kuhafifisha utendaji wa akili, kwa kuipumbaza. {2Tsw 63.2}

Je, watu wanaojiandaa kuwa watakatifu, safi, na kutakaswa, ili waweze kutambulishwa katika jamii ya malaika wa mbinguni, wataendelea kutoa uhai wa viumbe wa Mungu na kuishi kwa nyama zao na kuzifurahia kama anasa? Kutokana na kile Bwana alichonionesha, utaratibu huu wa mambo utabadilishwa, na watu wa Mungu wa kipekee watakuwa na kiasi katika mambo yote. Wale wanaoishi kwa kiasi kikubwa kwa chakula cha nyama, hawawezi kuepuka kula nyama ya wanyama, ambao kwa kiwango kikubwa au kidogo wana magonjwa. Mchakato wa kuwafanya wanyama wafae kwa soko, huzalisha ndani yao magonjwa; na japo hujaribu kuwekwa tayari kwa namna ya kufaa kadiri inavyowezekana kuwa, wanyama hao hupata joto na magonjwa, wanaposwagwa kabla ya kufika sokoni. Vimiminika na nyama za hawa



wanyama wagonjwa hupokelewa moja kwa moja ndani ya damu ya mwili, na hupita kwenye mzunguko wa mwili wa mwanadamu, na kuwa ugiligili (fluids) na nyama ile ile kwenye mwili wa mwanadamu. Kwa hivyo magonjwa ya uvimbe au kansa na kifua kikuu yanaanza kuingizwa katika mfumo. Na ikiwa mtu huyo tayari ana damu isiyo safi, hali mbaya ya afya inachochewa zaidi na ulaji wa nyama ya wanyama hawa. Dhima ya kupata ugonjwa huongezeka mara kumi kwa kula nyama. Nguvu za kiakili, maadili, na nguvu za mwili zinapungua kwa mazoea ya matumizi ya vyakula vya nyama. Ulaji wa nyama unaharibu mfumo, hutia wingu akili, na kupunguza nguvu za utendaji wa kimaadili. Tunawaambia, wapendwa ndugu na dada, mwenendo wenu salama zaidi ni kuachana na nyama. {2Tsw 63.3}

Matumizi ya chai na kahawa pia huhumiza mfumo. Kwa kiwango fulani, chai huzalisha sumu mwilini. Inaingia kwenye mzunguko na polepole huharibu nguvu ya mwili na akili. Huchochea, husisimua, na kuharakisha mwendo wa utaratibu wa mwili, ikiulazimisha kuchukua hatua isiyo ya asili, na hivyo kumpa mnywaji wa chai hisia kwamba inamfanyia huduma nzuri, kwamba inampa nguvu. Hili ni kosa. Chai huondoa nguvu za neva na kuziacha dhaifu sana. Athari yake inapotoweka na utendaji ulioongezeka unaosababishwa na nguvu yake imepungua, basi matokeo ni nini? Unyong'onyevu na udhaifu unaolingana na nguvu/uchangamfu bandia ulioletwa na chai. Wakati mfumo tayari umezidiwa na unahitaji kupumzika, matumizi ya chai huchochea asili kwa kulisimua kufanya tendo lisilo la kawaida, lisilohitajika, lisilo la asili, na kwa hivyo hupunguza nguvu yake ya kutenda na uwezo wake wa kustahimili; na nguvu zake hukoma muda mrefu kabla ya muda Mbingu iliyopanga zikome. Chai ni sumu kwa mfumo. Wakristo wanapaswa kuachana nayo. Athari ya kahawa ni sawa na chai, lakini athari kwenye mfumo bado ni mbaya zaidi. Athari yake ni kulisimua, na kwa kiwango tu ambacho huinuka juu zaidi ya wastani, itamalizika na kushuka chini ya wastani. Wanywaji wa chai na kahawa hubeba alama usoni mwao. Ngozi hugeuka kuwa rangi ya manjano na kuwa na mwonekano usio na uhai. Mng'ao wa afya hauonekani usoni. {2Tsw 64.1}

Chai na kahawa hazina lishe kwa mfumo. Nafuu inayotokana nazo ni ya ghafla, kabla ya tumbo kuzimeng'anya. Hii inaonesha kuwa kile watumiaji wa vichocheo hivi huita nguvu au nishati, hupokelewa tu kwa kulisimua mishipa ya tumbo, inayopelekea ubongo kuudhika au kusumbuka, na hii kwa upande mwingine inachochewa ili kuleta ongezeko la utendaji katika moyo na nguvu ya muda mfupi katika mfumo mzima. Yote hii ni nguvu ya uongo/bandia ambayo huleta hali kuwa mbaya tu, ingelikuwa heri kama usingelikuwa nayo hii nguvu. Hakika haitoi hata chembe ya nguvu ya asili. {2Tsw 65.1}

Athari ya pili ya kunywa chai ni maumivu ya kichwa, kukosa usingizi, mapigo ya moyo kwenda kasi, tatizo la mmeng'enywa wa chakula, kutetemeka kwa mishipa ya fahamu, na maovu mengine mengi. "Basi ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana." Mungu anataka dhabihu iliyo hai, siyo iliyokufa au inayokufa. Tunapotambua mahitaji ya Mungu, tutaona kwamba Yeye anatumiaji tuwe na kiasi katika kila jambo. Mwisho wa uumbaji wetu ni kumtukiza Mungu katika miili na roho zetu, ambazo ni Zake. Je, tunawezaje kufanya hivyo wakati tunaendelea uchu/ulafi, kwa maumivu ya nguvu za mwili na maadili? Mungu anataka tuitoe miili yetu kuwa dhabihu iliyo hai. Kisha wajibu umeamriwa kwetu kuhifadhi mwili huo katika hali bora kabisa ya afya, ili tuweze kuzingatia matakwa Yake Bwana. "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." {2Tsw 65.2}

Unayo kazi ya kufanya ili kupanga nyumba yako katika utaratibu. Jitakaseni wenyewe toka kwa uchafu wote wa mwili na roho, mkikamilisha utakatifu katika kumcha Mungu. Mnapaswa kufanya bidii kutambua makosa yenu, na katika hofu ya Mungu, mkizitegemea nguvu Zake, yawekeneni mbali. Wapendwa ndugu na dada, mnaumiaji kufanya matengenezo/mageuzi katika suala la utaratibu. Mnapaswa kukua upendo kwa unadhifu na usafi kamili. Mungu ni Mungu wa utaratibu. Yeye Hataruhusu tabia ya ulegevu na isiyofaa kwa yeyote miongoni mwa watu Wake. Katika mavazi yako, ndani ya nyumba yako, katika vitu vyote, onyesha ladha/uzuri na mpangilio. Tunatazamwa kama watu wa pekee. Matengenezo ya mavazi ni kinyume kabisa na

mitindo ya ulimwengu. Wale wanaopokea mavazi haya inawapaswa kuonesha akili ya kupambanua vizuri na utaratibu na usafi kamili katika mavazi yao yote. Mavazi hayapaswi kukubaliwa isipokuwa yametengenezwa vizuri na kupangwa kwa unadhifu. Kwa kuwa hatupaswi kutafuta kuwachukiza watu wasioamini kwa uzembe na kutojali katika mavazi yetu, lakini tunapaswa kuvaa kwa kujistahi, kwa kuzingatia afya na unadhifu, ili mavazi yetu yajiuze yenyewe kwa maamuzi ya akili adilifu. {2Tsw 65.3}

Mnahitaji akili zilizo safi, zenye nguvu, ili kuthamini tabia iliyoinuliwa ya ile Kweli, kuuthamini upatanisho, na kuweka makisio sahihi juu ya vitu vya milele. Ukitembea katika njia mbaya, na kuendekeza tabia mbaya ya kula, na kwa hivyo kudhoofisha nguvu za kiakili, hautaweka makadirio makubwa katika wokovu na uzima wa milele, utakaokutia moyo ili maisha yako yapatane na maisha ya Kristo; hautafanya juhudi hizo za dhati, za kujitoa kafara binafsi kwa kupatana kabisa na mapenzi ya Mungu, ambayo Neno Lake linahitaji, na ambayo ni muhimu kukupa usawa wa maadili katika hatua ya mwisho ya kujipatia kutokufa. {2Tsw 66.1}

## SURA YA 7

### KUPUUZA MATENGENEZO YA AFYA

Wapendwa ndugu na Dada I: Bwana ameonesha mambo kadhaa kuhusiana nanyi ambayo ninahisi ni jukumu langu kuandika. Mlikuwa miongoni mwa idadi ya wale ambao waliowasilishwa mbele yangu, kama watu walio nyuma katika matengenezo ya afya. Nuru imeangaza katika njia ambayo watu wa Mungu wanasafiri, walakini wote hawatembezi katika nuru na kuifuata kwa haraka, kwa kadiri majaliwa ya Mungu yanavyoonesha na kufungua njia mbele yao. Isipokuwa wafanye hivi, watakuwa gizani. Ikiwa Mungu amezungumza na watu Wake, basi Yeye amekusudia watu waisikie na kuitii sauti yake. Sabato iliyopita, nilipokuwa nikizungumza, nyuso zenu zilizokwajuka ziliinuka wazi mbele yangu kama vile nilivyooneshwa. Niliona hali yenu ya afya na maradhi yaliyowatesa kwa muda mrefu. Nilioneshwa kuwa hamjaishi kiafya. Hamu yenu ya chakula imekuwa mbaya, na mmeridhisha ladha na uchu wa chakula kwa gharama ya tumbo. Mmeweka ndani ya matumbo yenu vitu ambavyo haviwezekani kubadilishwa kuwa damu nzuri. Hii imeweka kazi kubwa kwenye ini, kwa sababu viungo vya mmeng'enywa wa chakula vinaharibiwa. Ninyi nyote mna ugonjwa wa ini. Matengenezo ya afya yatakuwa na manufaa makubwa kwenu nyote ikiwa mtayatekeleza kwa umakini. Hili mmeshindwa kulifanya. Uchu wenu ni wa kufisha (morbid), na kwa sababu hamfurahii chakula cha kawaida, na sahili, kilicho na unga wa ngano ambao haujakobolewa, mboga-mboga na matunda yaliyoandaliwa bila viungo (spices) au mafuta, mnaendelea kuasi sheria ambazo Mungu ameziweka katika mfumo wenu daima. Wakati mnaifanya hivi lazima mpate adhabu, kwa maana kila kosa limefungamanishwa na adhabu. Lakini mnashangaa kuhusu hali yenu mbaya ya kiafya. {2Tsw 66.2}

Kuwa na hakika kwamba Mungu hatafanya muujiza kukuokoa kutoka kwa matokeo ya mwenendo wako mwenyewe. Haukuwa na usambazaji wa hewa huria. Ndugu I amefanya kazi katika duka lake, akijitahidi sana kuwa karibu na biashara yake na kujipatia kiasi kidogo tu cha hewa na mazoezi. Mzunguko wake wa damu umedhoofika.

Anapumua tu kutoka juu ya mapafu yake. Ni nadra kwake kuishughulisha misuli ya tumbo katika tendo la kupumua. Tumbo, ini, mapafu, na ubongo vinaumia na kuteseka kwa uhitaji wa uvutaji hewa ndani wa kina, na kamili, ambao ungeitia nguvu damu kama umeme na kuipatia rangi kali ya kung'aa, yenye afya na ambayo hii pekee inaweza kuiweka safi na kutoa siha njema na nguvu kwa kila sehemu ya utendaji hai wa mwili.{2Tsw 67.1}

Nyinyi, wapendwa ndugu na dada, mnaweza kuwa na hali bora zaidi ya afya kuliko mnavyofurahia sasa, na mnaweza kujiepusha na matokeo mengi mabaya, ikiwa mtakuwa na kiasi katika mambo yote—kiasi katika kazi, kiasi katika kula na kunywa. Vinywaji vya moto vinadhoofisha tumbo. Jibini haipaswi kuingia ndani ya tumbo. Mkate wa unga uliokobolewa hauwezi kupatia mfumo chakula ambacho utakipata katika mkate wa ngano ambao haujakobolewa. Matumizi ya kawaida ya mkate wa ngano uliokobolewa hayawezi kuweka mfumo katika hali yenye afya. Ninyi nyote mna maini yasiyo na utendaji mzuri. Matumizi ya unga uliokobolewa huongeza shida ambayo mnajipatia sasa. {2Tsw 68.1}

Hakuna tiba ambayo inaweza kuwaondolea shida zenu za sasa wakati mnakula na kunywa kama mfanyavyo. Mnaweza kujifanyia wenyewe, kile ambacho daktari mzoefu zaidi hawezi kufanya kamwe. ratibuni lishe yenu. Ili kuridhisha ladha au uchu wa chakula, mara nyingi mnashughulisha sana viungo vyenu vinavyomeng'anya chakula kwa kupokea tumboni chakula kisicho bora, na wakati mwingine kwa viwango vilivyokithiri (chakula kingi). Hii huchosha tumbo na kufanya lisifae kupokea hata chakula chenye afya zaidi. Mnafanya matumbo yenu yawe dhaifu daima kwa sababu ya tabia yenu mbaya ya kula. Chakula chako kinafanywa kuwa cha fahari sana (lishe yake ni nyingi mno au kalori- sukari, mafuta mengi, chakula kilichokobolewa na kusindikwa, kukaangwa kama vile keki, maandazi, chips, vitumbua, chapati na hata jamii ya karanga inapaswa kuchukuliwa kwa kipimo cha kiganja cha mkono kwa siku). Chakula chenu hakijaandaliwa kwa njia rahisi, ya asili, lakini haifai kabisa kwa tumbo unapokuwa umekiandaa kwa ajili ya kuipendeza ladha yako. Asili (mwili) inalemewa, na inajitahidi kupingana na juhudi zako za kuilemaza.

Homa zinazofanya mtu asikie baridi kali na homa ni matokeo ya majaribio hayo ya asili/mwili, kujiondolea mzigo mliyouwekea. Ni lazima mpate adhabu ya kuzikiuka sheria za asili (Laws of nature, kama uvutano, afya nk). Mungu ameweka sheria katika mfumo wenu ambazo hamwezi kuzikiuka bila kupata adhabu ya mateso. Mmeshauriana na ladha bila kurejelea afya. Mmefanya mabadiliko kadhaa, lakini mmechukua hatua za kwanza tu katika matengenezo ya lishe. Mungu anahitaji toka kwetu tuwe na kiasi katika kila kitu. “Basi, mlapo, au mnywapo, mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.” {2Tsw 68.2}

Kati ya familia zote ambazo ninafahamiana nazo, hakuna inayohitaji faida ya matengenezo ya kiafya zaidi kuliko yenu. Mnapiga mayowe, miguno na vilio chini ya maumivu na uchovu ambavyo hamwezi kuelezea, na mnajaribu kutii kwa hiari kadri muwezavyo, mkifikiri mateso ni fungu lenu na Majaliwa ya Bwana yameamua iwe hivyo. Ikiwa macho yenu yangefunguka na muone hatua zilizochukuliwa katika maisha yenu kufika katika hali yenu mbaya ya sasa kiafya hakika mngestaajabishwa na upofu wenu kwa kutokuona hali halisi ya jambo kabla. Mmesababisha uchu wa chakula usio wa asili, na hampati hata nusu ya furaha hiyo toka kwa chakula chenu ambayo mngeipata ikiwa msingetumia vibaya hamu yenu ya chakula. Mmeufanyia mwili hiana, na mmekuwa mkikabiliana na matokeo, na hali imekuwa chungu sana. {2Tsw 69.1}

Mwili huwa unavumilia kutumiwa vibaya kwa muda mrefu kadri inavyowezekana bila kupinga, kisha unaamka na kufanya jitihada kubwa ili kujiondoa katika kuelelemewa kwa kutendewa vibaya katika safari yake. Kisha huja maumivu ya kichwa, baridi, homa, woga, kupooza, wasiwasi au magonjwa ya akili na maovu mengine mengi mno kutaja. Mwenendo mbaya wa kula au kunywa hugaribu afya, na utamu wa maisha pamoja nayo. Lo, ni mara ngapi umenunua kile ulichokiita mlo bora au chakula kizuri kwa gharama ya mfumo uliosisimuliwa, kupoteza hamu ya kula, na kukosa usingizi! Kutokuwa na uwezo wa kufurahia chakula, kukosa usingizi usiku, saa za mateso—yote kwa chakula ambacho ladha/uchu ulifurahishwa! Maelfu wameendekeza uroho/ulafi wao mbaya, wamekula chakula kizuri,

kama walivyokiita, na kama matokeo, kimeleta homa, au ugonjwa mwingine mkali, na kifo cha ghafla. Hiyo ilikuwa starehe ya chakula iliyonunuliwa kwa gharama kubwa. Walakini wengi wamefanya hivi, na hawa wanaojiua wenyewe wamekuwa wakisifiwa na marafiki zao na mhubiri wakati wa kusoma tanzia ya mazishi, na hata kubebwa moja kwa moja kwenda mbinguni wakati wa kifo chao. Ni wazo la ajabu iliyoje! Walafi mbinguni! Hapana, hapana; watu kama hao hawataingia kamwe kwenye malango ya lulu ya mji wa dhahabu wa Mungu. Watu kama hao hawatainuliwa kamwe katika mkono wa kuume wa Yesu, Mwokozi wa thamani, Mtu wa Kalvari atesekaye, ambaye maisha Yake daima yalikuwa ya kujikana nafsi na kujitoa kafara. Kuna mahali pameandaliwa kwa watu wote kama hao miongoni mwa wasiostahili, ambao hawawezi kuwa sehemu katika maisha bora ya mbingu, urithi usioharibika. {2Tsw 69.2}

Mungu anawataka watu wote watoe miili yao Kwake kama dhabihu iliyo hai, na sio dhabihu iliyokufa au inayokufa, dhabihu ambayo mwenendo wao wenyewe unadhoofisha, unajaza uchafu na magonjwa. Mungu anataka dhabihu iliyo hai. Mwili, Anatuambia, ni hekalu la Roho Mtakatifu, makao ya Roho Wake, Naye anawataka wote wanaobeba sura Yake kuitunza miili yao kwa kusudi la huduma Yake na utukufu Wake. “Ninyi si mali yenu wenyewe,” anasema mtume aliyevuviwa, “mmenunuliwa kwa thamani;” kwa hivyo “mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika roho, ambavyo ni vya Mungu.” Ili kufanya hivyo, ongeza katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi-2 Petro 1:5-7. Ni wajibu kujua jinsi ya kuutunza mwili katika hali bora kabisa ya afya, na ni jukumu takatifu kuishi kulingana na nuru ambayo Mungu ametoa kwa neema. Tukifunga macho yetu ili tusipate nuru kwa kuogopa, tutayaona makosa yetu, ambayo hatutaki kuyaacha, dhambi zetu hazipungui lakini zinaongezeka. Ikiwa nuru inaachwa katika jambo moja, itapuuzwa katika lingine. Ni dhambi kabisa kuvunja sheria za kuwepo kwetu/mwili, ni sawa tu na kuvunja moja ya zile Amri Kumi, kwani hatuwezi kufanya hivyo bila kuvunja sheria ya Mungu. Hatuwezi kumpenda Bwana kwa moyo wetu wote, akili, roho, na nguvu wakati tunapenda hamu zetu za kula, ladha zetu, bora zaidi kuliko tunavyompenda Bwana. Kila siku tunapunguza nguvu zetu kumtukuza

Mungu, nguvu Zake Yeye. Bwana Anataka nguvu zetu zote, akili zetu zote. Kwa tabia zetu mbaya tunapunguza kushikilia kwetu uzima, huku tukidai kuwa wafuasi wa Kristo, tukijiandaa kwa hatua ya mwisho ya maisha ya kutokufa. {2Tsw 70.1}

Ndugu na dada yangu, mnayo kazi ya kufanya ambayo hakuna mtu anayeweza kuwafanyia. Amkeni toka katika ugoigoi wenu, na Kristo atawapatia uzima. Badilisheni mwenendo wenu wa maisha, kula kwenu, kunywa kwenu, na kufanya kazi kwenu. Wakati mnafuata mwenendo ambao mmekuwa mkifuata kwa miaka mingi, hamuwezi kutambua kwa udhahiri mambo matakatifu na ya milele. Utambuzi wenu, na busara vinafifia na akili zenu zimefunikwa na wingu. Hamjakua katika neema na katika ujuzi wa Kweli kama ilivyokuwa fursa kwenu. Humjakua kiroho, lakini mkiongezeka zaidi na zaidi katika giza. Mmefanya haraka sana kujipatia mali, na mmekuwa katika hatari ya kufanya kazi yenye tamaa ya pesa, mkijitafutia masilahi yenu wenyewe na sio kujali maslahi ya wengine kama ambavyo mngependa wajali maslahi yenu. Mmeendeleza ubinafsi ndani yenu, ambao ni lazima ushindwe. Chunguzeni kwa ukaribu mioyo yenu wenyewe, na maishani mwenu, igeni Mfano usiokosea, na yote yatakuwa sawa kwenu. Hifadhini dhamiri safi mbele za Mungu. Katika yote mnayofanya litukuzeni Jina Lake Mwenyezi Mungu. Vueni ubinafsi na upendo wa kichoyo-kupenda ubinafsi. {2Tsw 71.1}

“Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na kamilifu.” Mila na desturi za wanadamu hazipaswi kuwa kigezo chenu. Hata kama mazingira yenu yanaweza kuwa yenye majaribu, msijiruhusu kamwe kutenda na kuwa na tamaa ya pesa na kuitafuta hata kwa jeuri. Shetani yuko karibu kuwajaribu mfanye hivi, naye hatawaruhusu mpumzike katika jambo hili. Inawezekana kwa mfanya biashara kuwa Mkristo na kuhifadhi uadilifu wake mbele za Mungu. Lakini ili kufanya hivi, uangalifu wa kudumu ni muhimu na kutoa maombi ya dhati na bidii mbele za Mungu ili kulindwa dhidi ya mwelekeo mwovu katika zama hizi zilizoharibika, kujinufaisha nafsi kwa hasara ya wengine. Mko mahali pagumu kukua katika maisha ya utakatifu. Una kanuni, lakini haumtegemei Mungu kwa mambo yote.



Unajiamini sana katika nguvu zako mwenyewe zilizo dhaifu. Una hitaji kubwa la msaada wa Bwana, Lisilopatikana ndani yako. Kuna Mmoja ambaye tunaweza kwenda Kwake kwa ajili ya kupata ushauri, Yule ambaye hekima Yake haina mwisho. Yeye Amekualika wewe uje Kwake, kwa kuwa atakupatia hitaji lako. Ikiwa kwa imani, utamtwika Yeye fadhaa zako zote,, Yeye ajuaye kudondoka kwa shomoro, tegemeo lako halitakuwa bure. Ikiwa utazitumainia ahadi Zake za hakika, na kudumisha uadilifu wako, malaika wa Mungu watakuzunguka. Dumisha matendo mema katika imani mbele za Mungu; ndipo hatua zako zitaongozwa na Bwana, na mkono Wake wenye mafanikio, heri na baraka havitaondolewa kwako. {2Tsw 71.2}

Ikiwa utaachwa kufanya uamuzi wa njia ya mwenendo wako mwenyewe, utafanya kazi duni katika jambo hilo, na ungesababisha kuvunjika kwa imani yako haraka. Peleka taabu na mizigo yako yote kwa Mbeba mzigo. Lakini usije kuacha hata doa moja, kuichafua tabia yako ya Kikristo. Kamwe, kamwe kwa ajili ya faida usiweke muhuri wa rekodi mbaya, ya maisha yako mbinguni, inayotazamwa na jeshi lote la malaika, na Mkombozi wako Mwenye kujikana nafsi, kwa ulafi, ubahili wa kutupwa, uroho wa pesa, ubinafsi, uchoyo au mahusiano au dili ambazo zina udhalimu na uongo. Mwenendo kama huo unaweza kukuletea faida kwa jinsi ulimwengu huu unavyolitazama jambo hilo; lakini, likitazamwa katika nuru ya mbinguni, itathibitisha kuwa ni jambo la hasara kubwa mno, isiyoweza kurekebishika. “Bwana haangalii kama mwanadamu aangaliavyo.” Katika kumtumainia Mungu daima kuna usalama, hakutakuwa na hofu ya kudumu ya uovu wa wakati ujao. Masumbufu, fadhaa na wasiwasi wa kuazima, na wala siyo wetu wanadamu, vitakoma. Sisi tunaye Baba wa mbinguni anayewajali watoto Wake, Naye atafanya na hufanya neema Yake itoshe kila wakati wa hitaji. Tunaposhika hatamu mikononi mwetu wenyewe ili kujiongoza kwa mambo yote yanayotuhusu, na kutegemea hekima yetu wenyewe kwa ajili ya mafanikio, tunaweza kuwa na wasiwasi, fadhaa na kutarajia hatari na hasara, kwa kuwa kwa hakika haya yatatujia. {2Tsw 72.1}

Kujitoa kikamilifu kwa Mungu kunahitajika toka kwetu. Wakati Mkombozi wa wanadamu wenye dhambi na wanaokufa alipokuwa

anafanya kazi ngumu na kuteseka kwa ajili yetu, Alijikana nafsi Yake, na maisha Yake yote yalikuwa ya matukio endelevu ya kazi ngumu na ufukara. Ikiwa hangechagua kufanya hivyo, angeweza kuishi siku Zake duniani katika maisha ya raha, ya mtelemko na yenye kusheheni mema, na kujitwalia raha zote na starehe za maisha haya. Lakini Yeye hakufanya hivyo; Hakujali hali inayofaa au kujifurahisha Mwenyewe. Ila Yeye Hakuishi ili kujifurahisha nafsi Yake Mwenyewe au kuepuka usumbufu, bali kutenda mema na kuokoa wengine toka katika mateso, kusaidia wale wanaohitaji msaada zaidi. Yeye Alivumilia hadi mwisho. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, Naye amebeba muovu yetu sisi sote. Kikombe kichungu kilichokuwa fungu letu kunywa. Kwa vile dhambi zetu zimechanganywa humo. Mwokozi wetu mpendwa alikichukua hicho kikombe kutoka midomoni mwetu na kukinywa Mwenyewe, na badala yake ametupatia kikombe cha rehema, baraka, na wokovu. Ah, hii ni kafara kubwa kiasi gani, kwa watu walioanguka! Ni upendo wa namna gani huu, ni upendo wa ajabu kiasi gani usioweza kuwa na mfanano! Baada ya udhihirisho huu wote wa mateso kuonesha upendo Wake, Je, tutasita au kukimbia majaribu madogo tunayopaswa kuyakabili? Je, tunaweza kumpenda Kristo, na kukataa kuubeba msalaba? Je, tunaweza kupenda kuwa Naye katika utukufu, na kisha tusimfuate toka katika ukumbi wa hukumu hadi Kalvari? Ikiwa Kristo atakuwa kwetu tumaini la utukufu, sisi tutatembea kama Yeye alivyotembea; tutayaiga maisha Yake ya kujitoa kafara, kuwabariki wengine; tutakinywea kikombe, na kubatizwa kwa ubatizo; tutakaribisha maisha ya kujitoa, ibada, maombi, majaribu, na kujikana nafsi, kwa ajili ya Kristo. Mbingu itakuwa rahisi vya kutosha haijalishi ni kafara gani tunayoweza kutoa ili kuipata.-{2Tsw 72.2}

## SURA YA 8

### UPENDO KWA WAKOSAJI

Nilioneshwa kwamba wakati Dada J na Ndugu na Dada K wameona makosa kwa wengine, hawakufanya juhudi za kurekebisha makosa hayo na kuwasaidia wale ambao walipaswa kuwasaidia. Wamewaacha sana peke yao, na kuwa mbali sana nao kwa kutokuwa na roho ya kirafiki au upendo, na kuhisi kwamba hakukuwa na maana kujaribu kufanya chochote kwa ajili yao. Hii siyo sawa. Wanafanya kosa kwa kufanya hivyo. Kristo alisema: “Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi watubu.” Bwana anatutaka tuwasaidie wale wanaohitaji msaada zaidi. Wakati mmeona makosa na mabaya kwa wengine, mmejifungia sana ndani yenu, ninyi wenyewe, na mmekuwa wabinafsi mno katika kuifurahia Kweli. Mungu hakubaliani na huku kuridhika na Kweli na kutotoa kafara yoyote kuwasaidia na kuwaimarisha wale wanaohitaji nguvu. Sote hatujaundwa/hatujapangwa sawa (kila mtu yupo tofauti), na wengi hawajaelimishwa kwa usahihi. Elimu yao imekuwa na umapungufu. Wengine wameambukizwa kuudhika kwa haraka, na elimu yao katika utoto haijawafundisha kuwa na kujitawala nafsi. Kwa hasira hii inayowaka moto, husuda na wivu, hivi viwili mara nyingi huungana. Wengine wana makosa katika mambo mengine. Wengine si waaminifu katika biashara, wadanganyifu katika biashara, wanabamiza wengine ili wapate faida. Wengine ni wadhalimu katika familia zao, wanapenda kutawala (madikteta). Maisha yao yana makosa mengi. Elimu yao yote haikuwa sahihi. Hawakuambiwa dhambi ya kutojisalimisha na tabia hizi mbaya; kwa hivyo dhambi haionekani kwao kuwa mbaya sana. Wengine, ambao elimu yao haijawa na ulema sana, ambao wamekuwa na mafunzo bora, wamekuza tabia isiyo ya kuchukiza sana. Maisha ya Kikristo ya wote yameathiriwa sana kwa mema au kwa ubaya na elimu yao ya awali. {2Tsw 73.1}

Yesu, Wakili wetu, anafahamu mazingira yote yanayotuzunguka na hushughulika nasi kulingana na nuru tuliyokuwa nayo, na mazingira ambayo tumewekwa. Wengine wana utaratibu mzuri zaidi kuliko wengine. Wakati wengine wanaendelea kunyanyaswa, kuteswa, na

katika shida kwa sababu ya sifa za tabia zao zisizofurahisha, wakipigana vita na maadui wa ndani na upotovu wa asili yao, wengine hawana hata nusu ya vita ya kupigana dhidi yao. Wanakaribia kupita njia yote wakiwa huru kutokana na magumu ambayo ndugu na dada zao ambao hawajajipanga vizuri wanayapitia (hawana mpangilio). Katika visa vingi sana hawafanyi kazi kwa bidii sana hata nusu kushinda na kuishi maisha ya Kikristo kama wengine wa wale wasio na bahati niliowataja. Wa mwisho huonekana kuwa duni kila wakati, wakati wale wa awali huonekana bora zaidi kwa sababu ni kawaida kwao kufanya hivyo. Wanaweza wasifanye kazi kwa bidii hata kukesha nusu tu, na kuutiisha mwili, lakini kwa wakati uo huo wanalinganisha maisha yao na ya wengine ambao hawana bahati ya mpangilio mzuri na wameelimishwa vibaya, na kujisifu wenyewe, na hata kujidanganya kwa tofauti hizo. Wanazungumza juu ya kushindwa, makosa, na mabaya ya wale wasio na bahati, lakini hawahisi kuwa wana mzigo wowote katika suala hilo, mbali zaidi ya kuyashikilia hayo makosa na kujitenga na wale wenye hatia ya hayo. {2Tsw 74.1}

Nafasi kubwa sana mliyo nayo kama familia kanisani hufanya iwe muhimu sana kwenu kuwa wabeba mizigo. Sio kwamba mnapaswa kubeba mizigo kwa wale ambao wanaweza kubeba mizigo yao wenyewe, ila pia kusaidia wengine; lakini mnapaswa kuwasaidia wale ambao wanahitaji msaada zaidi, wale ambao wana maisha ya chini, wanaopotoka na wenye makosa, na ambao wanaweza kuwa wamewajeruhi na kuupima uvumilivu wenu kiasi kikubwa. Ni watu wa hivyo ambao Yesu huwasikitikia, kwa sababu Shetani ana nguvu zaidi juu yao naye hudumu kutumia maeneo ya udhaifu wao na kuendesha mishale yake kuwajeruhi mahali walipo na ulinzi kidogo. Yesu hutumia nguvu na rehema Zake kwa visa kama hivyo vya kusikitisha. Yesu Alipouliza ni nani aliyependa zaidi, Simoni akajibu: “Ni yule ambaye amesamehewa vingi.” Ndivyo itakavyokuwa. Yesu hakujitenga na wadhaifu, wasio na bahati, waliopatwa na changamoto, na wanyonge, lakini alisaidia watu kama hao waliohitaji msaada. Hakufanya ziara Zake na kazi kwa daraja la wale wenye akili mahiri zaidi na wenye makosa kidogo, kwa kuwapuuza wale wasio na bahati. Hakuuliza kama ilikubalika Kwake kuwa rafiki wa maskini, wenye mahitaji zaidi.

Hawa ndio alitafuta ushirika nao, kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. {2Tsw 75.1}

Hii ndio kazi mliyoipuuza. Mmejitenga na majukumu yasiyowapendeza na hamjaenda kwa wacosaji na kuwatembelea, na kudhihirisha kujali na upendo kwao, na kufahamiana nao. Hamjawa na roho ya msamaha kama ya Kristo. Mmeonesha mwenendo kama ule tu ambao wote lazima waufikie kabla ya kuwafunika kwa vazi lenu la hisani. Hamtakiwi kufunika dhambi, lakini mwoneshe ule upendo wenye sikitiko na huruma kwa wacosaji ambao Kristo ameonesha kwenu. {2Tsw 75.2}

Mmewekwa katika hali nzuri zaidi kwa ajili ukuzaji wa tabia nzuri za Kikristo. Hamko mahali mnapohisi hitaji la kubana sana, au ambapo roho zenu zimefungwa na kufadhaika na mwenendo wa watoto wasiotii, na waasi. Katika familia yenu hakuna sauti inayopingana. Mnavyo vyote ambavyo moyo unaweza kutamani. Walakini, pamoja na mazingira yenu mazuri, mna makosa mengi, na mengi ya kushinda ili muwe huru na kiburi cha kiroho, ubinafsi, roho ya harara na mihemko, wivu, na kudhania wengine mabaya. {2Tsw 76.1}

Ndugu K hana dhambi ya kusema maovu ya kutubia, kama wengi walivyo nayo, lakini hana utayari wa kuwasaidia wale wenye mahitaji msaada zaidi. Ni mbinafsi. Anaipenda nyumba yake, anapenda utulivu, kupumzika, kutokuwa na taabu, mfadhaiko, na majaribu; kwa hivyo anajipendeza mwenyewe kupita kiasi. Habebi mizigo ambayo Mbingu imempa. Anaepuka majukumu yasiyokubalika, na anajifungia sana katika kupenda kwake utulivu na kutokuwa na makelele. Amekuwa mkarimu sana kwa mali yake, lakini wakati inahitajika kujikana nafsi ili kutenda wema unaohitajika, wakati kafara ya Kweli kwa upande wake inahitajika, ana uzoefu mdogo tu, na lazima aupate huu uzoefu. {2Tsw 76.2}

Anaogopa kwamba atalaumiwa ikiwa atajitosa kusaidia wacosaji. “Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe. Kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake mwenyewe, akajengwe. Kwa maana Kristo Naye hakujipendeza mwenyewe; bali kama ilivyoandikwa, Malaumu yao

waliokulaumu wewe yalinipata Mimi.” Wote walio washiriki wa wokovu huu mkubwa wana jambo la kufanya katika kuwasaidia wale wahitaji wanaochechemea waishike Sayuni. Hawapaswi kuacha kushikilia kwao na kuwafukuza watu mbali, bila ya kufanya juhudi za kuwasaidia kushinda na kujiandaa kwa hukumu. Hapana, kwa kweli! Wakati hawa kondoo wanalia kuzunguka zizi, wanapaswa kutiwa shime na kuimarishwa kwa msaada wote ulio katika uwezo wetu kutoa. Ninyi kama familia mna sheria ngumu sana na mnaweka maoni ambayo hayawezi kuendana kwa kila kesi. Mnakosa upendo, moyo mwororo, upole, wema, uungwana na huruma kwa wale wasio kwenda haraka wanavyostahili. Roho hii imedumu kwa kiwango ambacho mnanyauka kiroho badala ya kufanikiwa katika Bwana. Maslahi yenu, na juhudi, na wasiwasi ni kwa familia yenu na jamaa zenu. Lakini hamjakubali wazo la kuwafikia wengine wanaowazunguka, shindeni kusita-sita kwenu ili mtoe mvuto nje ya mduara huu maalumu. Mnapenda mno mduara wenu na ni kama mnauabudu, na kujifungia ndani yenu wenyewe. Ili Bwana aniokoe ‘mimi na vya kwangu’ ndiyo mzigo wenu mkubwa. Roho hii ni lazima ife kabla ya kufanikiwa katika Bwana na kusonga mbele kiroho, kabla ya kanisa kukua na roho kuongezeka humo kwa wale watakaookolewa. {2Tsw 76.3}

Ninyi nyote mmepungua katika kufanya kazi kwa ajili ya wengine, na lazima mbadilishe msingi wa utendaji wenu wa kazi. Ndugu zenu sio wa thamani sana mbele za Mungu kuliko roho zingine masikini zinazohitaji wokovu. Lazima tuweke nafsi na ubinafsi chini ya miguu yetu, na kuonesha mfano katika maisha yetu roho ya kujitoa kafara binafsi na ukarimu usiojipendelea uliooneshwa na Yesu wakati alipokuwa duniani. Wote wanapaswa kuwajali ndugu zao, lakini hawapaswi kuruhusu kujifungia ndani yao wenyewe kana kwamba ni wao tu ambao Yesu alikuja kuwaokoa. {2Tsw 77.1}

## SURA YA 9

### DINI YA KILA SIKU

Ndugu na Dada L: Nilioneshwa kuwa mna kazi ya kufanya ili kuweka mambo ya mambo ya nyumba yenu sawa. Ndugu L, haujaiwakilisha Kweli vizuri; umeipenda Kweli, lakini haujapata mvuto utakasao katika maisha yako ambayo lazima uwe nayo ikiwa utafaa kuwa katika jamii ya malaika wa mbinguni katika ufalme wa utukufu. Wewe ni fimbo yenye mikwaruzo na unahitaji kuchongwa na kulainishwa sana na unahitaji kubaki kwenye karakana ya Mungu hadi kingo zinazokwaruza ziondolewe, uso usio na msawaziko umelainishwa, nawe utangazwe kufaa kwa ajili ya kuingia kwenye jengo [uwe tofali la kufaa kupachikwa kwenye jengo la Bwana]. {2Tsw 78.1}

Unapaswa kuwa mwangalifu usianzishe mada za Ukweli wa sasa kila mahali. Unaweza kufanya zaidi katika kuiishi ile Kweli kuliko kusema kwa wengine. Unaweza kufanya mambo mengi kwa mfano. Unahitaji kuwa na tahadhari sana katika shughuli zako za biashara, kuziendesha katika kanuni za imani yako. Kuwa mwaminifu katika biashara, Mkweli na mkamilifu katika kazi, ukizingatia kuwa sio jicho la mwajiri wako pekee ambalo linakagua kazi yako, lakini kwamba jicho la Mungu liko juu ya shughuli zote za maisha yako. Malaika wa Mungu wanaangalia kazi yako, na inapaswa kuwa sehemu ya dini yako kuwa kila kipande cha kazi kinachoonessa Ukweli na uaminifu. Yeye “Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; naye aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia.” Mungu anataka kukufanya wewe kuwa sawa/sahihi, mtakatifu, na wa Kweli. {2Tsw 78.2}

Hauzungumzi kwa hekima na busara kwa mke wako na watoto. Unapaswa kukuza wema na upole. Watoto wako hawajapata mvuto bora na mfano mbele yao. Hawapaswi kukutawala wewe, lakini wewe kuwatawala/kuwaongoza wao, si kwa ukali, sio kwa nguvu za ujeuri, lakini kwa uthabiti na uimara wa kusudi. {2Tsw 78.3}

Dada L, una vita kubwa mbele yako ili uwe mshindi. Umeiruhusu nafsi iendelee kushinda. Nia yako shupavu na yenye ukaidi ni adui mkubwa uliye naye. Una na hasira isiyodhibitiwa, na haudhibiti ulimi wako. Ukosefu wa kujidhibiti nafsi, kuwa na kiasi, umekuwa maumivu makubwa kwako mwenyewe na kwa familia yako. Furaha, utulivu, na amani vimetamalaki katika makazi yako kwa muda mfupi tu. Ikiwa mapenzi yako yamechokozwa kidogo tu, unakaudhiwa kwa urahisi sana, na kisha unazungumza na kutenda kana kwamba ulipagawa pepo. Malaika huondoka toka katika eneo lisilo na maelewano ambapo maneno watu wanatupiana maneno ya hasira. Mara nyingi umewafukuza malaika wa thamani, wa mbinguni toka katika familia yako kwa kuendekeza tamaa na mihemko. {2Tsw 78.4}

Mtoto wa nyoka ni nyoka. Roho ile ile unayoidhihirisha inaakisiwa juu yako tena. Watoto wako wameona mapenzi kidogo, wema, kujali, huruma nyororo, upendo mwanana na upole kwamba hawajapata lolote la kuwaongoa katika Kweli au kuwahamasisha kwa heshima kwa mamlaka yako. Kwa muda mrefu wamekula matunda mabaya yaliyozalishwa na wewe, hivi kwamba mwelekeo wao ni uchungu. Hawajapotoka kabisa; imesalia mivuto mizuri, chini ya sehemu za nje ambazo hazijaendelezwa au kupaliliwa vizuri, kuna hisia nzuri za kutenda mema na kufanya yale yaliyo sahihi, na hisia hizi zinaweza kuletwa juu-. Ikiwa maisha yako ya kidini yangekuwa na uwiano zaidi, yakionyesha mfano wa maisha ya Kristo, mambo yangekuwa tofauti katika familia yako. “Kile apandacho mtu, ndicho atakachovuna.” Ile mbegu utakayopanda itakuwa mavuno utakayokusanya. Ikiwa maneno ya upole na yaliyo nyororo ndiyo hutawala katika makazi yako, ungepokea matunda kama hayo. {2Tsw 79.1}

Jukumu zito liko juu yako. Kwa kuzingatia hili, unapaswa kuwa mwangalifu kiasi gani katika maneno yako yote na matendo. Unapanda mbegu ya aina gani mioyoni mwa watoto wako? Wakati wa mavuno—lo! kumbuka, wakati wa mavuno hauko mbali sana. Usipande mbegu mbaya. Shetani yuko tayari kufanya kazi hiyo. Panda mbegu safi, na bora tu. {2Tsw 79.2}



Wewe, dada yangu mpendwa, umekuwa na wivu, mwenye kijicho, na kutafuta makosa. Umedhani ulikuwa umepuuzwa na kudharauliwa. Umepuuzwa sana, lakini unayo kazi ya kufanya kwa ajili yako mwenyewe ambayo hakuna mtu anayeweza kukufanyia wewe. Itahitaji juhudi, uvumilivu, unyofu na bidii ili kupata ushindi dhidi ya tabia zilizojengwa kwa muda mrefu ambazo imekuwa asili ya pili. Tuna hisia nyororo, za kujali na upendo kwa ajili yako, pamoja na makosa yako yote na mapungufu; na wakati tutakuwa uhuru wa kukuambia makosa yako, tunaahidi wenyewe kukusaidia katika kila njia tunayoweza. {2Tsw 79.3}

Nilioneshwa kuwa wewe hauna upendo wa udugu ambao unapaswa kuwa nao. Uovu katika asili yako unatekelezwa kwa njia isiyo ya kawaida. Wewe sio mpole, mwenye upendo, kujali, moyo mwororo na heshima kwa wazazi wako. Haidhuru wana makosa gani, wewe huna udhuru kwa mwenendo uliouonesha kwao. Umekuwa wa moyo mgumu na usio na heshima.

Malaika waligeuka toka kwako kwa huzuni, wakirudia Maneno haya: “Kile apandacho mtu ndicho atakachovuna.” Wakati ukiendelea, nawe utatendewa vivyo hivyo na watoto wako ambavyo wazazi wako wamepokea toka kwako. Hujajifunza jinsi unavyoweza kuwafanya wazazi wako wawe na furaha, na kisha kutoa kafara matakwa yako na anasa yako hadi mwisho huu. Siku zao duniani ni chache kabisa, na zitakuwa zimejaa taabu na shida hata ukifanya kila uwezalo kupunguza makali kaika safari ya kwenda kwao kaburini kwa amani. “Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana Mungu wako.” Hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi. Ni ya lazima, na ina mashiko katika utoto na ujana, katika umri wa kati na utu uzima. Hakuna kipindi maishani ambapo watoto waweza kutoa udhuru au kuwekwa huru wasiwaheshimu wazazi wao. Wajibu huu adhimu ni wajibu kwa kila mwana na binti, na ni moja ya masharti ya kurefusha maisha yao juu ya nchi ambayo Bwana atawapa waaminifu. Hili siyo somo ambalo halistahili kuzingatiwa, lakini ni jambo la muhimu sana. Ahadi imejengwa juu ya sharti la utii. Ukitii, utaishi siku nyingi katika nchi ambayo Bwana Mungu wako anakupa. Ikiwa utaacha kutii amri hii, maisha yako hayatakuwa marefu katika nchi hiyo. {2Tsw 80.1}

Hapa, dada yangu, ni mada ya kuzingatia kwa maombi na kutafakari kwa bidii. Chunguza moyo wako mwenyewe kwa karibu katika nuru ya umilele. Usifiche chochote toka katika uchunguzi wako. Jichunguze, lo! tafuta, kama kwa maisha yako, na kujishutumu mwenyewe, jihukumu mwenyewe, na kisha kwa imani dai damu itakasayo ya Kristo ili kuondoa madoa kutoka kwa tabia yako ya Kikristo. Usijivune, usijidanganye mwenyewe au kujitolea udhuru. Shughulika na roho yako mwenyewe. Na kisha unapojiona mwenye dhambi mwenyewe, anguka, vunjika/pondeka kabisa, chini ya msalaba. Yesu atakupokea wewe, haijalishi kwa jinsi ulivyo mchafu, Naye atakuosha katika damu Yake, na kukutakasa kutokana na uchafuzi wote, na kukufanya ufae kwa jamii ya malaika wa mbinguni, katika mbingu safi na yenye mapatano. Hakuna ukali, na malumbano, hakuna kutoelewana, pale. Yote ni afya, raha, na furaha. {2Tsw 81.1}

Dada L, haujaonesha kutojali wokovu wako. Wakati mwingine umefanya bidii, na umejinyenyekeza mbele ya kanisa na mbele za Mungu; lakini haujapokea faraja na kitia moyo ambacho unahitaji, na ambacho Yesu angekupa bure kama angelikuwepo duniani. Upendo umepungua kanisani, mapenzi yanatakiwa kanisani. Upendo umepungua kanisani. Upendo kwa wakosaji umefunikwa kwa ubinafsi. Kuna ukosefu mkubwa wa neema hii ya thamani miongoni mwa watu wa Mungu. Umefikiria kwamba watu wa Mungu walikuwa hawakujali, na roho yako imeasi dhidi yake. Hawajahisi sawa wala kusema inavyostahili. Hawajafuata njia sahihi. Hawajathibitishwa katika hili. Mbingu haijapendezwa nalo, hakika imekasirishwa. Yesu anakuhurumia wewe, Naye anakualika, uliyechoka, na kulemewa na mizigo, uje Kwake na ujifunze Kwake Yeye aliye mpole na mnyenyekevu wa moyo, nawe utapata raha nafsini mwako. Nira ya Kristo ni laini, na mzigo Wake ni mwepesi. Unapofadhaishwa, ukiwa na wasiwasi, na kukasirishwa, kimbilia kwa Mbeba Mzigo; mwambie Yesu yote. Ndugu na dada zako wanaweza wasithamini juhudi zako, na huenda wasijue jinsi unavyojitahidi sana kupata ushindi; lakini hili lisikukatishe tamaa. Ikiwa Yesu anajua, ikiwa anafahamu juhudi zako za dhati, wewe ridhika. {2Tsw 81.2}

Lazima kuwe na matengenezo kamili katika maisha yako, mabadiliko kwa kufanywa upya nia yako. Mungu anahitaji watu Wake wakusaidie kwa sababu unahitaji msaada, na unapaswa kuwa mnyenyekevu sana ili kusaidiwa na wao. Unapotaribiwa kukiachia hata kitivo chako kimoja kiwe na ukorofi, ah! kumbuka kwamba malaika mwenye kuweka kumbukumbu anaandika kila neno. Yote yameandikwa kitabuni, na, usipooshwa kwa damu ya Kristo, lazima ukutane na rekodi hiyo tena. Sasa una kumbukumbu isiyo safi, yenye doa mbinguni. Toba ya dhati mbele za Mungu itakubaliwa. Unapokaribia kuzungumza kwa jazba, funga kinywa chako. Usitamke hata neno moja. Omba kabla ya kusema, na malaika wa mbinguni watakuja kukusaidia na watawafukuza malaika waovu, ambao wanaweza kukuongoza kumkosea heshima Mungu, kuaibisha kazi Yake, na kudhoofisha nafsi yako mwenyewe. {2Tsw 82.1}

Unayo kazi hasa ya kufanya, kukiri kwa kujidhili mwenendo wako usio na heshima kwa wazazi wako. Hakuna sababu ya udhihirisho huu usiyo wa kawaida kwao. Ni roho ya kishetani kabisa, na umeiendekeza kwa sababu mama yako hajauzuia mwenendo wako. Hisia zako huzalisha sio tu kutopenda waziwazi, kutokuwa na heshima dhahiri, lakini chuki, kijicho, husuda, kudhuru, wivu, zinazodhihirishwa katika matendo yako, na kuwasababishia mateso na ufukara. Hauhisi kama unawafanya wawe na furaha, au hata kuwa na utulivu na faraja. Hisia zako zinabadilika-badilika. Wakati mwingine moyo wako unalainika, kisha unaufunga ukiona kosa kwao, na malaika hawawezi kuugusa moyo wako hata kwa hisia moja ya upendo. Pepo mchafu anakutawala, nawe ni mwenye kinyongo na umejaa chuki. Mungu ameandika maneno yako yasiyo na heshima, matendo yako yasiyo ya wema kwa wazazi wako, aliyokuamuru uwaheshimu, na ukishindwa kuona dhambi hii kubwa, na kuitubu, utazidi kuwa gizani mpaka utaachwa katika njia zako mbaya. {2Tsw 82.2}

Bwana Yu tayari kuwasaidia wote wanaohitaji msaada na kuhisi hitaji hilo. Ukiona umasikini wako na unyonge mbele za Mungu, na kuzishika nguvu Zake kwa bidii, Yeye atasaidia, na kubariki, na kukupatia nguvu, ili kwa matendo yako mema uwaongoze wengine wamtukuze Baba yetu aliye mbinguni. Je, utajiona mwenyewe kama ulivyo? Je,

utasalimisha mapenzi na njia zako kwa Mungu? Je, utatafuta dini iliyo safi na isiyo na taka mbele za Mungu? Lo, itakusaidia nini kupita katika hali hii mbaya ya uharibifu! Huna furaha mwenyewe katika namna hii ya kuishi, na wale walio karibu nawe hawana furaha katika jamii yako. Hakika unajiletea kiasi kikubwa cha taabu na huzuni; na maisha kama hayo uliyoishi hayafai sana. Kwa nini, basi, usipatanishwe na Mungu? Ifie nafsi na ubadilike, ili Yesu akuponye. Yeye Anataka kukuokoa wewe, ikiwa utakubali kuokolewa kwa njia Yake aliyoichagua. Acha Bwana akusaidie kuona na kusahihisha kila kosa, ndilo ombi langu. {2Tsw 83.1}

Ndugu L, unapaswa kuwa mwepesi wa kusikia, si mwepesi wa kusema, si mwepesi wa hasira. Kuwa mwangalifu kwa maneno yako. Usiruhusu Shetani akufanye jiwe la kujikwaa kwa wengine. Kuna kushindwa katika shughuli zako za biashara. Unaibeza kazi yako. Unaimaliza haraka iwezekanavyo, ukifikiri kuwa itatoa kinachohitajika, wakati haijafanywa vizuri. Unakosa ukamilifu katika kazi. Unapaswa kukuza ladha na utaratibu katika yote unayofanya. Chochote kinachostahili kufanywa, kinastahili kufanya vizuri. Ukikosa uaminifu katika maisha yako ya biashara utakosa katika maisha yako ya kidini, na katika siku ya Mungu mizani ya Patakatifu itafunua Ukweli kwamba umepungua. Ukosefu huu ni aibu kwa imani yako. Watu wasioamini wanadai kuwa ni kukosa uaminifu, na kusema: “Ikiwa ni watu kama hawa wanaoshika Sabato, sichagui kuwa mtu wa aina hiyo.” {2Tsw 83.2}

Kama wanadamu wanavyohibitisha kazi yako na kuiona inapungua uimara, uzuri na mpangilio, wanasema wewe ni mdanganyifu, na hotuba nyingi ngumu zimetolewa juu yake. Viapo vingi vimetamkwa juu ya kazi yako, na watu wamemkufuru Mungu. Haumaanishi kutokuwa mwaminifu, lakini kuna uvivu katika kazi zako. Unafikiri waajiri wako wamezidi umakini sana, kwamba unajua nini litakuwa jibu vile vile, kama wao; na kwa hivyo uvivu huu, mtindo ulio huru, ambao haujakamilika huambatana na kazi yako kwa kiwango kikubwa. Unapaswa kupiga hatua katika suala hili na kuboresha kazi yako. Unapaswa kuheshimiwa katika kazi yako yote, na kufunga kazi yako kwa njia ambayo itaonesha kuwa na uthibitisho wa Mungu. Dharau kupuuza kazi yoyote. Kuwa mwaminifu katika lililo dogo. {2Tsw 83.3}

Jaribu kumsaidia mke wako katika mgogoro ulio mbele yake. Kuwa mwangalifu kwa maneno yako, endeleza usafi wa tabia, uungwana, adabu, upole, na utapata thawabu kwa kufanya hivyo. {2Tsw 84.1}

## **SURA YA 10**

### **MATENGENEZO NYUMBANI**

Ndugu M: Kutokana na kile nilichooneshwa, kuna kazi kubwa ya kutimizwa kwako kabla ya kukubalika mbele za Mungu. Nafsi-[Ubinafsi] imetawala sana. Una hasira za haraka na kali, na ni dikteta na dhalimu kwa familia yako. Dada M ni mzembe na sio nadhifu nyumbani kwake. Hana sifa ya utaratibu na unadhifu katika mpangilio wake. Hata hivyo anaweza kupiga hatua katika mambo haya. Ndugu M, unamkaripia mke wako, wewe ni dikteta, na hauna upendo ule unaopaswa kuwa nao. Mke anaiogopa roho yako ya uonevu, lakini haifanyi kile anachoweza kufanya kurekebisha tabia zake mbaya, inayofanya nyumba iwe isiyopendeza na isiyo na mapatano. {2Tsw 84.2}

Ndugu M, haujafuata mwenendo wa busara na familia yako. Watoto wako hawakupendi. Wana chuki zaidi kwako, kuliko upendo. Mkeo hakupendi. Haufuati mwenendo wa kupendwa. Wewe ni shupavu (umepilitiliza kwenye mambo). Wewe ni mkali, unayeshurutisha, dikteta, kwa watoto wako. Unawaambia Ukweli, lakini haubebi kanuni zake katika maisha yako ya kila siku. Wewe sio mvumilivu, mwenye subira, na mwenye kusamehe. Umeendekeza roho yako mwenyewe kwa muda mrefu, nawe uko tayari kuruka kwa jazba ikiwa utachochewa, kiasi cha kuonekana kuwa na shaka kubwa ikiwa utafanya bidii ya kutosha kuifikia nia ya Kristo. Hauna nguvu ya uvumilivu, ustahimilivu, upole, na upendo. Neema hizi za Kikristo lazima uwe nazo kabla ya kuwa Mkristo kweli. Unahifadhi maneno yako ya kutia shime - ili kutia moyo watu wengine baki, na kuwahamasisha, kwa matendo yako ya fadhili, wale wasioyastahili badala ya mke wako mwenyewe na watoto wako. Kuza na kupalilia maneno mazuri, mwonekano mzuri, sifa, na ukubali kwa familia yako mwenyewe, kwa kuwa hii itaathiri furaha yako. Kamwe usiruhusu karipio au maneno mabaya yatoke midomoni mwako. Shinda tamaa hii ya kutawala na kuweka kisigino chako cha chuma, yaani kunyanyasa na kutesa popote unapoweza. Una roho kali ya malumbano, ukosoaji, ubinafsi, na uchoyo. Kwa wengine wewe ni mbinafsi na bahili; kwa wengine unaowafikiria kuwa wa thamani sana kwako, unaweza kutoa kafara ya kitu chochote, hata vitu ambavyo familia yako inahitaji. Wewe ni mkarimu katika mambo haya ili upate sifa na heshima toka kwa wanadamu. Ikiwa ungeweza kuinunua mbingu kwa kafara kubwa kwa wale ambao unachagua kuwa mkarimu kwao, kwa hakika ungeipata. Haukatai kuwekwa katika usumbufu

mkubwa ili kuwafaidisha wengine, ikiwa kwa kufanya hivyo unaweza kujiinua mwenyewe. Katika mambo haya unatoa zaka ya mnanaa na mchicha, na huku ukipuuza mambo mazito, haki na upendo wa Mungu. {2Tsw 84.3}

Haupo tu katika familia yako. Una kazi ya kufanya huko. Mfanye mke wako ajisikie kuwa ana faraja na sio masumbufu, na mwenye furaha kwanza; kisha zingatia hali ya watoto wako. Wapatie chakula kizuri na mavazi. Ndipo ikiwa unaweza, bila kuwawekea mipaka mke wako na watoto, wasaidie wale wanaohitaji msaada zaidi, na uwafanyie hisani zako, pale ambapo zitathaminiwa; itakuwa sifa kwako kuwa mkarimu. Lakini jukumu lako la kwanza na takatifu zaidi ni kwa familia yako. Hawa hawapaswi kunyang'anywa ili wengine wapewe upendeleo. Hebu ukarimu wako, uonekane katika familia yako mwenyewe. Wape uthibitisho unaoonekana wa mapenzi yako, upendeleo, kujali, na upendo. Hii inahusiana sana na furaha yako. Acha kutafuta makosa na kumkemea mkeo, kwa kuwa hili huifanya tu iwe ngumu kwako na kufanya mambo kuwa magumu sana kwake, kama vile kuwa Jehanamu. {2Tsw 85.1}

Malaika wa Mungu hawatakaa katika familia yako mpaka kuwe na mpangilio tofauti wa mambo. Sio mali yako inayohitajika. Walakini unapokaripiwa umedhani ni mali yako kanisa lilitaka. Umedanganyika hapa. Umekuwa mkarimu sana na mali yako, kwa sababu ulidhani hii ilikuwa ni kwa ajili ya kujipatia wokovu na kukununulia cheo kanisani. Hapana, kwa kweli! Ni wewe unayehitajika, si mali kidogo unayomiliki. Ikiwa utabadilishwa kwa kufanywa upya nia yako na kuongoka, shughulika Kweli na nafsi yako mwenyewe. Ndicho kanisa linachohitaji. Umejidanganya mwenyewe. "Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, dini ya mtu huyo ni bure." Itendee familia yako kwa namna ambayo Mbingu inaweza kukubali, na ili kwamba amani iweze kuwa ndani ya makao yako. Kuna haja ya kila kitu kufanywa, kwa familia yako. Watoto wako wamekuwa na mfano wako mbaya mbele yao; umelaumu, na kukaripia, na kudhihirisha roho ya ukali nyumbani, ambapo kwa wakati uo huo, ungeenda mbele ya kiti cha enzi cha neema, kuhudhuria mkutano, na kuishuhudia Kweli. Maonesho haya yamesababisha watoto wako wakudharau na kuchukia

ile Kweli unayoikiri. Hawana imani na ujasiri na Ukristo wako. Wanaamini kuwa wewe ni mnafikiri, na ni kweli kwamba kwa kusikitisha wewe ni mtu aliyedanganyika. Hauwezi kuingia mbinguni bila mabadiliko kamili kuliko Simon Magus aliyedhani kwamba Roho Mtakatifu anaweza kununuliwa kwa pesa-Matendo 8. Familia yako imeiona roho yako ya udanganyifu na kudhulumu wengine, utayari wako wa kuwatendea vibaya wengine ili kujinufaisha, roho yako ya ubahili kwa wale ambao wakati mwingine unashughulika nao, na wanakuchukia na kukudharau kwa hilo; lakini bado kwa hakika wao pia watafuata nyayo zako za kutenda mabaya. {2Tsw 86.1}

Unavyotenda sivyo inavyopaswa kuwa-dili zako ni za uovu. Ni vigumu kwako kutenda kwa haki na kupenda rehema. Umeidharau kazi ya Mungu katika maisha yako. Umepigania Ukweli, lakini si katika roho sahihi. Umezuia watu kuikubali Kweli ambao vinginevyo wangepanya hivyo. Watu wametoa udhuru wenyewe kwa kusonda kidole kwa makosa na mabaya ya watunza Sabato, wakisema: “Hao sio bora kuliko mimi; watasema uongo, na kudanganya, kutia chumvi, kukasirika, na kuzungumza kwa majigambo juu ya sifa zao wenyewe; dini kama hii, mimi siitaki.” Kwa hivyo maisha ambayo hayajawekwa wakfu ya watunza Sabato yenye kasoro huwafanya wawe kikwazo kwa wenye dhambi. {2Tsw 87.1}

Kazi iliyo mbele yako sasa ni lazima ianze katika familia yako. Umejaribu kwa bidii kupiga hatua kwa nje; lakini kazi imekuwa nyingi kwa juu, kazi ya nje na sio kazi ya moyo. Tengeneza moyo wako, jinyenyekeze mbele za Mungu, na omba neema Yake ikusaidie. Usifanye, kama Mafarisayo wanafiki, kufanya mambo ili uonekane mtu wa maombi na mwenye haki machoni pa wengine. Vunja moyo wako mbele za Mungu, na ujue kuwa haiwezekani kwako kuwadanganya malaika watakatifu. Maneno yako na matendo yako, yapo wazi kwa ukaguzi wao. Nia yako na dhamira na makusudi ya moyo yako wazi, katika macho yao. Mambo ya siri zaidi hayajafichwa toka kwao. Ah, basi, rarua moyo wako, na usijisumbue sana kuwafanya ndugu zako wafikiri uko sahihi wakati sio! Kuwa na tahadhari katika familia yako. Unaangalia kuona makosa ya wengine, lakini usifanye hivi tena. Kazi uliyo nayo sasa ya kufanya ni kushinda makosa yako mwenyewe,



kupigana na maadui wako wa ndani wenye nguvu. Mtendee haki mjane na yatima. Usifunike matendo yako kwa kifuniko hafifu cha udanganyifu, ili kushawishi wale ambao unatamani sana wakufikirie kuwa uko sawa, wakati nia na matendo yako hayatakuwa na tafsiri/maana ambayo ungeweka juu yao. {2Tsw 87.2}

Acha ushindani wote na magomvi, na jaribu kuwa mpatanishi. Usipende kwa neno, bali kwa tendo na Kweli. Kazi zako zinapaswa kuwa na uthibitisho wa busara. Je, utashughulika Kweli na roho yako mwenyewe? Usijidanganye mwenyewe. Lo, kumbuka kwamba Mungu hadhihakiwi! Wale walio na uzima wa milele watafanya yote wawezayo ili kuzitengeneza nyumba zao na kuweka mambo sawa. Lazima waanze mioyoni mwao wenyewe na kufuatilia kazi mpaka ushindi, ushindi wa dhati, upatikane. Nafsi lazima ife, na Kristo lazima aishi ndani yako na awe kwako kisima cha maji yanayobubujika uzima wa milele. Sasa, wewe una masaa ya thamani ya majaribio uliyopewa ilikuunda tabia sahihi hata katika uzee wako. Sasa una saa za thamani za rehema ulizopewa kutengeneza tabia sahihi hata katika umri wako uliosonga. Sasa una kipindi ulichopewa cha kuukomboa wakati. Hauwezi kwa nguvu zako mwenyewe kuondoa madhaifu na makosa yako; yamekuwa yakiongezeka juu yako kwa miaka, kwa sababu haujayaona katika ubaya wake, na nguvu ya Mungu kwa uthabiti huyaondoa. Kwa imani hai lazima ushikilie mkono wenye nguvu ya kuokoa. Nyenyekeza moyo wako wenye haki binafsi, masikini, wenye kiburi mbele za Mungu; jinyenyekeze, shuka chini sana, kwa kuvunjika katika hali yako ya dhambi miguuni Pake Bwana. Jitoe kwa kazi ya maandalizi. Usipumzike mpaka utakaposema kwa kweli: Mtetezi wangu Yu hai, na, kwa kuwa Yu hai, nami pia nitaishi. {2Tsw 88.1}

Ukipoteza mbingu, umepoteza vyote; ukipata mbinguni, umepata vyote. Usifanye kosa katika jambo hili, ninakusihi. Maslahi ya milele yanahusika hapa. Fanya kazi kamilifu. Hebu Mungu wa neema yote aangazie ufahamu wako ili upate kutambua mambo ya milele, ili kwamba kwa nuru ya Kweli, makosa yako mwenyewe, ambayo ni mengi, yaweze kudhihirika kwako kama yalivyo, ili uweze kufanya juhudi za lazima kuyaondoa, na badala ya matunda haya mabaya, na machungu upate kuzaa matunda ya thamani kwa uzima wa milele.

“Mtawatambua kwa matunda yao.” Kila mti hujulikana kwa matunda yake. Ni matunda ya aina gani tangu sasa yatapatikana tena juu ya mti huu? Matunda unayozaa yataamua ikiwa wewe ni mti mzuri, au ule ambao Kristo atamwambia malaika Wake: “Ukate; kwa nini unaharibu ardhi?”{2Tsw 88.2}

## SURA YA 11

### DHAMIRI ILIYOKIUKWA

Ndugu mpendwa N: Nahisi kusukumwa na wajibu wa kukuandikia mistari michache. Nimeoneshwa mambo kadhaa kwa habari yako ambayo sithubutu kujizuia. Nilioneshwa kwamba Shetani alikutumia kwa manufaa yake kwa sababu mke wako hakuikubali Kweli. Ulitupwa katika jamii ya mwanamke aliyepotoka/fidhuli, ambaye hatua zake ni za kuelekea Jehanamu. Alidai kuonyesha huruma kubwa kwa ajili yako, kwa sababu ya upinzani ulioupata toka kwa mke wako. Kama nyoka katika Edeni, alifanya tabia zake kuvutia. Aliweka mvuto wake katika akili yako kwamba wewe ni mwanamume ambaye umekuwa ukinyanyaswa vibaya; kwamba mke wako hakuthamini hisia zako na kurudisha mapenzi yako; kwamba kosa lilikuwa limefanywa katika uhusiano wako wa ndoa; hadi ukadhani viapo vya ndoa za kudumu maisha yote kwake ambaye ulimchukua kama mke wako, kuwa kama minyororo inayoumiza. Uliifuata huruma kwa malaika huyu aliye wazi katika usemi. Ulimimina kwake mambo yaliyopaswa kuwa ya mke wako pekee, uliyeapa kumpenda, kumheshimu, na kumtunza kwa muda wote wa maisha yenu. Ulisahau kukesha na kuomba kila wakati ili usije ukaingia majaribuni. Roho yako iliharibiwa na uhalifu. Uliweka muhuri katika kumbukumbu ya maisha yako mbinguni kwa doa na kujutia kwa aibu ya kutisha. Walakini kujidhili kwa kina na toba mbele za Mungu vitakubalika Kwake. Damu ya Kristo inaweza kuziosha dhambi hizi zote. {2Tsw 89.1}

Umeanguka, umeanguka vibaya. Shetani alikutega uingie katika wavu wake, na kisha akakuacha ujifungue mwenyewe na wavu uliojisokotoa nao kwa kadri uwezavyo. Umesumbuliwa na kufadhaishwa, na kujaribiwa kwa kutisha. Dhamiri yenye hatia inakusumbua. Hujiamini

mwenyewe na unafikiria kuwa kila ndugu katika Kristo, hakuamini. Unajionea wivu mwenyewe na kufikiria kwamba wivu upo katika mioyo ya wengine kwako. Haujiamini mwenyewe na unadhani kwamba ndugu zako hawana imani na wewe. Shetani mara nyingi huleta mambo yaliyopita mbele yako na kukuambia kuwa haina tija kwako kujaribu kuiishi Kweli, kwamba njia imenyooka sana kwako. Umeshindwa; sasa Shetani anatumia mwenendo wako wa dhambi, kujinufaisha, kukufanya uamini kwamba siku za ukombozi wako zimekwisha kupita. Uko kwenye uwanja wa vita wa Shetani ukishiriki pambano kali. Boma linalowekwa kuzunguka kila mzunguko wa familia, na kufanya familia iwe takatifu, wewe umelivunja. Na sasa Shetani anakushambulia karibu kila wakati. Hauna raha wala pumziko. Hauna amani, na unatafuta kuwafanya ndugu zako wawajibike kwa hisia zako zinazopingana na mashaka na wivu; unahisi kuwa wana makosa, kwamba hawakupi umakini wao. Tatizo liko kwako mwenyewe. Unataka njia yako mwenyewe, na wala haurarui moyo wako mbele za Mungu, na kwa moyo uliopondeka na uchungu kujitupa kwa udhaifu wote na kupondeka, mwenye dhambi, na mchafu, katika rehema Zake. Jitihada zako za kujiokoa mwenyewe, ikiwa zitaendelea, zitaleta matokeo ya uharibifu wako wa hakika. {2Tsw 89.2}

Acha wivu wako na kutafuta makosa. Geuza usikivu wako kwa habari yako mwenyewe na kwa toba ya unyenyekevu, ukitegemea damu ya Kristo pekee, okoa roho yako mwenyewe. Fanya kazi kamili kwa ajili ya umilele. Ukiacha Kweli utakuwa umekwisha/umeangamia, familia yako imeharibikiwa. Baada ya ngome inayolinda faragha na upendeleo mtakatifu wa uhusiano wa kifamilia umevunjwa mara moja, ni vigumu kujengat ena; lakini kwa uweza wa Mungu, na kwa uweza Wake pekee, wewe unaweza kufanya hivyo. Kweli, Kweli takatifu, ni nanga yako, ambayo itakuokoa kutokana na kuteleza katika mawimbi yaelekeayo chini katika uhalifu na uharibifu. {2Tsw 90.1}

Dhamiri ikikiukwa, hakika inadhoofishwa sana. Inahitaji nguvu ya kudumu ya kukesha na maombi yasiyokoma. Umesimama mahali penye utelezi. Unahitaji nguvu zote ambazo Kweli inaweza kutoa ili kukulinda na kukuokoa toka kwa uvunjikaji wa meli nzima ya imani. Uzima na mauti viko mbele yako; Je, utachagua kipi? Ikiwa ungeona

umuhimu wa kukaa imara juu ya kanuni, pasipo kuendeshwa na mihemko, na kutokatishwa tamaa kwa urahisi, lakini kwa kujiandaa kuvumilia ugumu, usingeshindwa kama ilivyotokea. Umesukumwa na mihemko. Haujawa tayari, kama vile Mfano wetu usio na makosa, kuvumilia ukinzani wa wenye dhambi dhidi yako. Tunashauriwa kumkumbuka Yeye aliyevumilia haya, ili tusije tukachoka na kuzimia katika akili zetu. Umekuwa dhaifu kama mtoto, pasipo na nguvu ya uvumilivu. Hujahisi umuhimu wa kuthibitishwa, kuimarishwa, kutulizwa, kusimikwa, na kujengwa katika imani. {2Tsw 90.2}

Umehisi kuwa inaweza kuwa jukumu lako kuwafundisha wengine ile Kweli badala ya wewe kufundishwa mwenyewe. Lakini lazima uwe tayari kuwa mwanafunzi, kuipokea ile Kweli toka kwa wengine, na lazima uache kutafuta kwako makosa, wivu wako, malalamiko yako, na kwa upole upokee Neno lililopandikizwa, linaloweza kuiokoa roho yako. Ni uamuzi wako ikiwa utakuwa na furaha au huzuni. Ulijisalimisha kwa majaribu na sasa huwezi kuzitumaini nguvu zako mwenyewe. Shetani ana nguvu kubwa juu ya akili yako, na hautakuwa na kitu cha kukushikilia utakapojitenga na mvuto unaozuia wa ile Kweli. Hii imekuwa ulinzi kwako kujizuia na uhalifu na uovu. Tumaini lako pekee ni kutafuta uongofu kamili na kukomboa yaliyopita kwa maisha yako yaliyopangiliwa vizuri na mazungumzo ya kiucha Mungu. {2Tsw 91.1}

Umesukumwa na mihemko. Msisimko umekubaliwa katika utaratibu wako, nawe umependezwa nao. Tumaini lako la pekee kwa sasa ni toba ya dhati ya uasi wako wa zamani wa sheria ya Mungu na kuitakasa nafsi yako kwa kuitii ile Kweli. Kuza usafi wa mawazo na usafi wa maisha. Neema ya Mungu itakuwa nguvu yako ya kuzuia tamaa yako na kudhibiti tamaa zako za mwili na uchu wako wa chakula. Maombi ya dhati na kukesha vitaleta msaada wa Roho Mtakatifu kwako ili kukamilisha kazi na kukufanya upende ule Mfano wako usiokosea. {2Tsw 91.2}

Ukichagua kutupilia mbali mvuto mtakatifu unaodhibiti/unaozuia wa ile Kweli, Shetani atakufanya mateka apendavyo. Utakuwa katika hatari ya kutoa kizuzi kwa hamu yako na uchu, kutotawala tamaa, uovu na tamaa za kuchukiza. Badala ya kuwa na uso wenye amani tulivu katika

jaribu na mateso, kama vile Henoko mwaminifu, ukiwa na uso unaong'aa kwa matumaini na amani inayopita akili zote, utatia muhuri uso wako kwa mawazo ya kimwili, na tamaa mbaya. Utakuwa na mvuto wa kishetani badala ya mvuto wa Mbingu/Mwenyezi Mungu. {2Tsw 92.1}

“Tena kwa hayo Yeye ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani; ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.” Sasa ni upendeleo wako, kwa ungamo la unyenyekevu na toba ya kweli, kuamini Maneno Ya Bwana na kurudi kwa Bwana. Damu ya Kristo ya thamani inaweza kukusafisha na uchafu wote, kuondoa unajisi wako wote, na kukufanya mkamilifu katika Yeye. Rehema za Kristo bado ziko karibu nawe ikiwa utazipokea. Kwa ajili ya mke wako uliyemkosea, na watoto wako, uzao wa mwili wako mwenyewe, acha kufanya uovu, na jifunze kufanya vizuri. Kile ukipandacho, ndicho utakachovuna. Ukipanda kwa mwili utavuna katika mwili, mavuno ya uharibifu. Ukipanda kwa Roho katika Roho utavuna uzima wa milele. {2Tsw 92.2}

Ni lazima ushinde hisia zako nyeti, ambazo zinaumizwa kwa upesi, na kufanya kila kitu kuwa nyeti kwako na kutafuta makosa. Una wivu kwamba wengine hawakupi usikivu wote unaodhani unapaswa kuwa nao. Uzoefu unaojengwa juu ya hisia, na kupendelea ushupavu, havipaswi kutiliwa maanani. Sio salama. Sukumwa na kanuni, na uelewa kamili. Yachunguze Maandiko, na uwe tayari siku zote kumjibu kila mtu akuulizaye habari za tumaini lililo ndani yako, lakini kwa upole na kwa hofu ya Mungu. Hebu kujikweza nafsi kufe. “Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. Huzunikeni, na kuomboleza, na kulia; kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza.” Unaposumbuliwa na majaribu na mawazo mabaya, Yupo Mmoja tu ambaye unaweza kumkimbilia kwa ajili msaada. Mkimbilie Yeye katika udhaifu wako. Ukiwa karibu Naye, mishale ya Shetani inavunjwa na haiwezi kukudhuru. Majaribu yako yakibebwa ndani ya Mungu yatakusafisha na kukunyenyekeza, lakini hayatakuangamiza au kukuhatarisha. {2Tsw 92.3}

## SURA YA 12

### MAONYO NA MASHUTUMU

Ndugu Mpendwa O: Nilioneshwa kuwa ulikuwa umefunikwa na giza, ambalo halikuondolewa na miale ya nuru toka kwa Yesu. Haukuonekana kuitambua hatari yako, lakini ulikuwa katika hali ya kutokujali kabisa, kutohisi na kutojali. Niliuliza sababu ya hali hii ya kutisha, na nikaelekezwa nyuma kwa miaka mingi, na kuoneshwa kuwa tangu ulipoipokea Kweli, haukutakaswa nayo, umeendekeza uchu wako na tamaa zako mbaya kwa kuangamiza hali yako ya kiroho, mwenyewe. Nilioneshwa kuwa Mungu alikuwa ametoa nuru kupitia vipawa vilivyowekwa kanisani, ambavyo vingefundisha, vingeshauri, vingeongoza, vingekaripia, na kuonya. Shuhuda hizi ambazo umekiri kuamini zilitoka kwa Mungu, nae hukuzingatia kuziishi. Kupuuza nuru ni kuikataa. Kukataa nuru kunawaacha watu wakiwa mateka, wakiwa wamefungwa na minyororo ya giza na kutokuamini. {2Tsw 93.1}

Nilioneshwa kwamba umeongeza familia yako bila kutambua jukumu ulilokuwa unalileta juu yako mwenyewe. Imekuwa vigumu kwako kumtendea haki mwenza wako au watoto wako. Mke wako wa kwanza hakupaswa kufa, lakini ulimletea masumbufu na mizigo iliyopelekea kafara ya maisha yake. Mke wako wa sasa ana mengi magumu; uhai wake umekaribia kuchoka. Kwa kuongeza familia yako kwa haraka sana, umedumu katika hali ya umaskini, na mama, aliyeshughulika katika kulea wanafamilia wachanga, hajapata nafasi inayofaa kwa maisha yake. Amewanyonyesha watoto wake katika hali mbaya zaidi, anapopigwa na joto la jiko la kupikia. asingeweza kuwafundisha kama anavyopaswa, wala kudhibiti tabia zao za kulana kufanya kazi. Matokeo ya kula chakula haifai zaidi, na vinginevyo kukiuka sheria ambazo Mungu ameweka katika asili ya miili yetu, kumeleta magonjwa na vifo vya mapema kwa watoto wako wakubwa. Ugonjwa

umeambukizwa kwa watoto wako, na matumizi huru ya chakula cha nyama yameongeza ugumu. Kula nyama ya nguruwe kumeamsha na kuimarisha hali mbaya ya kutisha zaidi iliyokuwa katika vimiminika vya mfumo (damu/mitoki/uvimbe). Wazao wako wamenyang'anywa siha na nguvu ya mwili kabla ya kuzaliwa. Hujaongeza wema katika maarifa, na watoto wako hawajafundishwa jinsi ya kujilinda wenyewe katika hali bora ya afya. Kamwe hata chembe moja ya nyama ya nguruwe isiwekwe juu ya meza yako. {2Tsw 93.2}

Watoto wako wamekua, badala ya kulelewa na kuelimishwa hadi mwisho ili waweze kuwa Wakristo. Katika njia nyingi mifugo yako (ng'ombe) imepata matibabu bora kuliko watoto wako. Haujafanya jukumu lako kwa watoto wako, lakini umewaacha wakue katika ujinga. Haujatambua jukumu uliloliweka juu yako mwenyewe katika kuleta kundi kubwa ulimwenguni la kundi, kwamba kwa kiasi kikubwa ulikuwa unawajibika kwa wokovu wao. Hauwezi kulitupa jukumu hili. Umewanyang'anya watoto wako haki zao kwa kutojali elimu yao na kuwafundisha kwa uvumilivu na uaminifu kwa habari ya kujenga tabia kwa ajili mbinguni. Mwenendo wako kwa kiasi kikubwa umeharibu imani yao kwako. Wewe ni mkali, dhalimu, mkatili; ni msumbufu, unakaripia, na kukemea, na kwa kufanya hivyo unaondoa mapenzi yao kwako. Unawatendea kana kwamba hawakuwa na haki kabisa, kana kwamba walikuwa mashine za kugeuza mikononi mwako kadri upendavyo. Unawakasirisha, na mara nyingi unawavunja moyo. Hauwapi upendo na mapenzi. Upendo huzaa upendo, mapenzi huzaa mapenzi. Roho unayoionesha kwa watoto wako itarudi kwako kwani itaakisiwa. {2Tsw 94.1}

Uko katika hali mbaya, na hauelewi kwa Kweli. Haiwezekani kwa mtu asiye na kiasi kuwa mtu mvumilivu. Kiasi kwanza, kisha uvumilivu. Kwa muda mrefu umeishi kwa ajili ya nafsi yako, na kufuata mawazo ya moyo wako mwenyewe, kiasi kwamba huwezi kutambua mambo matakatifu. Uchu wako mbaya na tamaa vimekutawala. Mpangilio wa vitivo vya juu yaani ogani za akili umedhoofishwa na kutawaliwa na ogani za chini. Mielekeo ya kinyama imekuwa ikipata nguvu. Wakati utambuzi na utendaji wa akili unapoachwa kutawaliwa na uchu wa kula, utambuzi wa juu wa mambo matakatifu umedhoofishwa. Akili

imepungua uwezo, mapenzi hayajatakaswa, na maneno na matendo yanashuhudia kile kilicho moyoni. Mungu amechukizwa na kudharauliwa kwa mazungumzo yako na mwenendo wako. Maneno yako hayajateuliwa na kuchaguliwa vizuri; mazungumzo hafifu, machafu huja kwa kawaida katika midomo yako, hata mbele ya watoto na vijana. Mvuto wako katika suala hili umekuwa mbaya. {2Tsw 95.1}

Mfano wako haujawa sahihi, nawe umekuwa kikwazo kwa watoto wako mwenyewe, na watoto wa watunza Sabato, wanaomtafuta Bwana. Mwenendo wako, katika suala hili, hauwezi kushutumiwa kwa kiasi cha kutosha. "Kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake. Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya. Basi, nawaambia, kila neno lisilo maana watakalolinena watu, watatoa hesabu yake siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa. Moyo wako unahitaji kutakaswa, kusafishwa, kuboreshwa, kwa utii wa kweli. Hakuna kinachoweza kukuokoa isipokuwa uongofu kamili— utambuzi halisi wa njia zako za dhambi na badiliko kamili kwa kufanywa upya nia yako. {2Tsw 95.2}

Umekuwa na usongo/bidii sana kutetea umuhimu wa kutokana imani yetu kwa matendo yetu, na umeifanya imani yako kuwa udhuru wa kutowapa watoto wako fursa ya kupata elimu hata katika matawi ya kawaida. Maarifa kuhusiana na wewe binafsi ndio unaohitaji, na bado utapaswa kuona umuhimu wa kupata. Maarifa ndio watoto wako wanahitaji lakini hawana upendeleo wa kuyapata. Kwa ukosefu huu mkubwa hawawezi kuwa wanajamii wenye manufaa, na watakuwa na upungufu katika elimu yao ya dini. Jukumu zito liko mlangoni pako. Unafupisha maisha ya mkeo. Je, anawezaje kumtukuza Mungu katika mwili na roho ambavyo ni mali Yake Bwana? {2Tsw 96.1}

Mungu amekupa nuru na maarifa, ambayo umekiri kuamini vilitoka moja kwa moja Kwake, vikikuelekeza kukataa uchu wa chakula na tamaa za mwili. Unajua kuwa matumizi ya nyama ya nguruwe ni kinyume na udhihirisho wa amri Yake, haikutolewa kwa sababu alitaka kuonesha hasa mamlaka Yake, lakini kwa sababu itawadhuru wale



watakaoila. Matumizi yake yangesababisha damu kuwa najisi, ili kwamba mafindofindo, kifua kikuu na vimiminika vya mfumo (damu na mfumo wa mitoki), na mwili wote ungetaabika. Hasa mishipa mizuri muhimu na nyeti ya ubongo, hii inakuwa dhaifu na hivyo kufunikwa kiasi kwamba mambo matakatifu hayatatambuliwa, lakini kuwa katika kiwango cha chini na vitu vya kawaida. Nuru kuonyesha kuwa ugonjwa unasababishwa kwa kutumia aina hii mbaya ya chakula, ambayo imekuja mara tu watu wa Mungu walipoweza kuistahimili. Je, umeitii nuru? {2Tsw 96.2}

Umeenda kinyume kabisa na nuru ambayo Mungu amependezwa kuitoa kuhusiana matumizi ya tumbaku. Kuendekeza uchu wa chakula kumeificha nuru iliyotolewa na Mbingu, na umefanya tumbaku kuwa mungu, wakati ni anasa yenye kuumiza. Ni sanamu yako. Umeisujudia sanamu ya chakula badala ya Mungu, wakati huo huo ukikiri imani kubwa katika maono, lakini ukitenda kinyume kabisa nayo. Kwa miaka mingi haujapiga hata hatua moja katika maisha ya utakatifu, lakini umeendelea kuwa dhaifu zaidi, gizani zaidi. Umehisi kuteseka sana kwa kwa ajili ya mwenendo wa Ndugu P kwa kuipinga Kweli kama alivyofanya. Umedhani hali dhaifu naya kukata tamaa ya kanisa ilitokana na upinzani wake. Ni kweli kwamba amekuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya kazi ya Mungu katika ----. Lakini mwenendo uliofuata, wakati unadai kuijua Kweli na kuwa na uzoefu katika kazi ya Mungu, umekuwa kikwazo kikubwa kuliko mwenendo wake. Ikiwa ulisimama katika shauri la Mungu na kutakaswa kupitia ile Kweli uliyodai kuiamini, Ndugu P asingekuwa na mashaka yote aliyokuwa nayo. Nafasi yako kama mtetezi wa njozi imekuwa kikwazo kwa wale waliokuwa hawaamini. Nilioneshwa kuwa kaka yako alijaribu kusimama chini ya mizigo mizito ambayo hali ya kusikitisha ya kanisa ilimletea hadi kukaribia kuangushwa chini kwa uzito aliokuwa ameubeba, na kuidondosha kwa ajili ya maisha yake. Niliona kuwa utunzaji wa Mungu ulikuwa juu ya Ndugu na Dada R, na kama imani yao ingesalia bila kutetereka bado wangeuona wokovu wa Mungu katika nyumba yao wenyewe na kanisani. {2Tsw 96.3}

Nilioneshwa hali ya Ndugu mpendwa na Dada S. Hawa walikuwa wakipita kwenye maji yenye giza, na mawimbi yalikuwa yamekaribia

juu ya vichwa vyao; lakini Mungu aliwapenda, na ikiwa wangezika bidhi tu njia zao Kwake, Yeye angewatoa katika tanuru la mateso wakiwa wametakaswa. Kaka S ametazama upande wa giza, na kutilia shaka ikiwa alikuwa mtoto wa Mungu—alitilia shaka wokovu wake. Nikaona kuwa hapaswi kuhenyeka kwa taabu ili kuamini, lakini anapaswa kumtegemea Mungu kama mtoto anayewatumaini wazazi wake. Ana wasiwasi na mawazo mengi—anajisumbua mwenyewe kutoka nje ya mikono Yesu, na humpa adui nafasi ya kujaribu na kumuudhi. Mungu anajua udhaifu wa mwili na akili, na hatahitaji zaidi kwake kuliko atakavyompa nguvu ya kufanya. Amejaribu kuwa mwaminifu na wa kweli kwa ungamo lake. Ameshindwa katika maisha yake katika mambo kadhaa, yote bila kujua, yaani kwa ujinga tu. Kuhusiana na nidhamu ya watoto wake, amezingatia kama ni jukumu lake kuwa mtu wa kinagaubaga na kuchukulia mambo kwa ukali, na ameipeleka nidhamu hii mbali sana. Ameshughulikia makosa madogo kwa ukali mkubwa mno. Hii imehamasisha kuondoa, kwa kiwango fulani, mapenzi ya mwana toka kwa baba. Wakati wa ugonjwa wake Ndugu S amekuwa na mawazo ya udhaifu. Mfumo wake wa fahamu umeharibiwa wote, naye amedhani kuwa watoto wake hawakuwa na hisia kwake na kumpenda kama wanavyostahili; lakini haya yalikuwa matokeo ya ugonjwa. Shetani alitaka kumwangamiza na kuwavunja moyo na kuwakatisha tamaa watoto wake maskini. Lakini Mungu hajalihesabu hili kuwa kosa lake. Watoto wake wana mizigo mikubwa ya kubeba kuliko wengi walio wazee kuliko wao, na wanastahili nidhamu makini, mafunzo ya busara, yaliyochanganywa na huruma nyororo, upendo, na upole mkubwa. {2Tsw 97.1}

Mama amekuwa na nguvu na hekima ya pekee toka kwa Mungu kwa kumtia shime na kumsaidia mumewe, na kufanya mengi katika kuwafunga watoto wake moyoni wake na kuimarisha mapenzi yao kwa wazazi wao na kwa kila mmoja wao. Niliona kwamba malaika wa rehema walikuwa wakizunguka juu ya familia hii, ingawa matarajio yalionekana kuwa ya giza na mabaya. Wale waliokuwa na matumbo ya huruma kwa Ndugu S hawatakuwa na sababu ya kujutia, kwa kuwa yeye ni mtoto wa Mungu, apendwaye Naye. Hali ya kufadhaisha ya kanisa imeleta madhara sana kwa afya yake. Nilimwona akiangalia upande wa giza, pasipo kujiamini mwenyewe, na kutazama chini

kaburini. Hapaswi kutafakari sana juu ya mambo haya, lakini kumtazama Yesu tu, Mfano usiokosea. Ni lazima aimarishe uchangamfu na ujasiri katika Bwana— akizungumza imani, akizungumza tumaini; pumziko kwa Mungu, na kutohisi kwamba juhudi zinazolemea, zinahitajika kwa upande wake. Yote atakayo Mungu ni kumtumaini Yeye kwa usahili—kujiachilia mikononi Mwake akiwa a udhaifu wake, kuvunjika kwake, na mapungufu yao na Yesu atawasaidia wote wasiojiweza, na kuwatia nguvu na kuwajenga wale wanaohisi kuwa wao ni udhaifu wenyewe. Mungu atatukuzwa katika mateso na dhiki yake, kupitia uvumilivu, imani, na unyenyekevu kwa mfano wake yeye mwenyewe. Ah! hii itathibitisha nguvu ya Kweli tunayoikiri; ni faraja tunapoihitaji; ni msaada wakati kila tegemeo la asili ya kidunia, ambalo limekuwa msaada mkubwa usioweza kuelezeka au kupimika, limeondolewa. {2Tsw 98.1}

Nilioneshwa pia kwa habari ya Ndugu T. Mtu huyu amejikweka katika hali ya utumwa ambayo Mungu hakumwitia. Mungu hapendezwi pale ambapo mababa wazee wanakabidhi uwakili wao mikononi mwa watoto wasiojikweka wakfu, ingawa hawa wazee wanaikiri Kweli. Lakini wakati mali ambazo Bwana amewakabidhi watu Wake zinawekwa mikononi mwa watoto wasioamini ambao ni maadui wa Mungu, Yeye haheshimiwi; kwa kuwa kile kinachopaswa kuwekwa katika mamlaka ya Bwana kinawekwa katika jeshi la adui.{2Tsw 99.1}

Tena, Ndugu T amefanya sehemu ya mtu mdanganyifu. Ametumia tumbaku, lakini anataka ndugu zake wafikirie kwamba hakuitumia. Niliona kuwa dhambi hii imezuia maendeleo yake katika maisha ya utakatifu. Anayo kazi ya kufanya, katika uzee wake, kujiepusha na tamaa za mwili zinazopigana na roho. Ameipenda ile Kweli, na ameteseka kwa ajili ya ile Kweli. Sasa anapaswa kukadiria thawabu ya milele, hazina iliyo mbinguni, urithi usioharibika, taji ya utukufu isioharibika, ili aweze kutoa kafara kwa moyo mkunjufu kuhusiana na kuendekeza uchu mbaya, athari au mateso visije vikawa kubwa zaidi, ili kukamilisha kazi ya utakaso wa mwili na roho. {2Tsw 99.2}

Kisha nikaoneshwa mkamwana wake. Anapendwa na Mungu, lakini ameshikiliwa katika utumwa wa unyonge, hofu, kutetemeka, kukata

tamaa, kuona shaka, na woga mkubwa. Dada huyu hapaswi kuhisi kwamba anapaswa kusalimisha mapenzi yake kwa kijana asiyemcha Mungu ambaye ana miaka michache katika kichwa chake kuliko yeye mwenyewe. Anapaswa kukumbuka kuwa ndoa yake haiharibu utambulisho wake binafsi. Mungu ana madai juu yake kuliko dai lolote la kidunia. Kristo alimnunua kwa damu Yake Mwenyewe. Yeye si mali yake mwenyewe. Kama anashindwa kuweka tumaini lake lote kwa Mungu, na kutiisha usadikisho wake, dhamiri yake, kwa mtu mkali, na dhalimu/dikteta, aliyejazwa na Shetani wakati wowote fahari yake ya kishetani inapoweza kufanya kazi kikamilifu kupitia kwake ili kuitisha hii nafsi inayotetemeka na kusita. Mara nyingi ametupwa katika fadhaa hata mfumo wake wa fahamu umeharibiwa, na yeye ni mtu aliyevunjika -vunjika tu. Je, ni mapenzi ya Bwana kwamba dada huyu awe katika hali hii na Mungu anyang'anywe huduma yake? Hapana. Ndoa yake ilikuwa udanganyifu wa shetani. Walakini sasa anapaswa kuifanya bora zaidi, kumtendea mume wake kwa upole, na kumfurahisha kadiri awezavyo bila kukiuka dhamiri yake; kwa kuwa huyu mume akibaki katika uasi wake, ulimwengu huu utakuwa ndio mbingu yote atakayokuwa nayo. Lakini kujinyima fursa ya mikutano ya ushirika, ili kumfurahisha mume dhalimu mwenye roho ya joka, sio mapenzi ya Mungu. Bwana Anataka roho hii inayotetemeka imkimbilie. Atakuwa maficho Kwake. Atakuwa kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi inayochosha. Kuwa na imani tu, mtumaini Mungu Naye atakuimarisha na kubariki. Watoto wake wote watatu wameathiriwa na mvuto wa Kweli na Roho wa Mungu. Je, watoto hawa wanaweza kuwa na hali nzuri kama watoto wengi wanaotunza Sabato, wote wanaweza kuongoka na kujiandikisha katika Jeshi la Bwana. {2Tsw 99.3}

Kisha nilioneshwa msichana mdogo wa sehemu ile ile, aliyekuwa amemwacha Mungu na alikuwa amefunikwa katika giza. Malaika alisema: "Alipiga mbio vizuri kwa msimu; ni nini kilimzuia?" Nilielekezwa nyuma na kuona kwamba yalikuwa ni mabadiliko ya mazingira. Alikuwa akishirikiana na vijana kama yeye, ambao walijawa furaha na raha, kiburi, na upendo wa ulimwengu. Kama angeyazingatia Maneno ya Kristo, asingehitaji kujisalimisha kwa adui. Kesheni na mwombe, msije mkaingia majaribuni. "Majaribu yanaweza kutuzunguka pote, lakini hii haitusababishi tuingie katika majaribu.

Ukweli unastahili kila kitu. Mvuto wake hauelekei kushusha, lakini kuinua, kusafisha, kutakasa, na kumpandisha juu katika hali ya kutokufa na kiti cha enzi cha Mungu. Malaika alisema: “Je, mtamchukua Kristo, au ulimwengu?” Shetani anauwasilisha ulimwengu pamoja na mvuto wake unaodanganya, unaovutia, kwa wanadamu maskini wenye kufa, nao wanautazama, na mng'ao wake na mapambo hufunika utukufu wa mbinguni na uzima ule unaodumu kama kiti cha enzi cha Mungu. Maisha ya amani, raha, na furaha isiyoelezeka, ambayo hakutakuwa na lolote la sikitiko, huzuni, maumivu, au kifo, yanatolewa kafara kwa maisha mafupi ya dhambi. Wote watakaogeuka toka katika starehe za dunia, pamoja na Musa, kuchagua kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo, wakihesabu aibu ya kushutumiwa Kwake, Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za ulimwengu, pamoja na Musa mwaminifu, watapokea taji isiyoharibika ya kutokufa na uzani uzidio kuwa mwingi sana na utukufu wa milele. {2Tsw 100.1}

Mama wa binti huyu kwa nyakati tofauti amekuwa akiathiriwa na mvuto wa ile Kweli, lakini ameupoteza kwa haraka huu mvuto kwa kutofanya maamuzi. Anakosa uamuzi wa tabia, ni mwenye kusita na kumangamanga sana, na ameathiriwa sana na wasioamini. Anapaswa kuchochea uamuzi, ujasiri, uthabiti wa kusudi, ambao hautapinda kulia au kushoto kutokana na mazingira. Hapaswi kuwa katika hali ya kukosa msimamo na kutangatanga hivyo. Kama hatafanya matengenezo katika suala hili atanaswa kwa urahisi na kuwa mateka wa Shetani kama appendavyo. Atapaswa kuwa na uvumilivu na uthabiti katika kazi ya kushinda, la sivyo atashindwa na kuipoteza nafsi yake. Kazi ya wokovu sio mchezo wa kitoto (lelemama), kushikiliwa kwa nia ya dhati na kuachwa kadri mtu appendavyo. Ni kusudi thabiti, juhudi isiyochoka, itakayopata ushindi hatimaye. Ni yule mwenye kuvumilia mpaka mwisho ndiye atakayeokoka. Ni wale ambao wanaendelea kwa uvumilivu katika kutenda mema ambao watapata uzima wa milele na thawabu isiyoharibika. Ikiwa dada huyu mpendwa angekuwa mkweli kwa usadikisho wake kwa uthabiti na kuwa na utulivu wa kusudi, angeweza kutumia mvuto unaookoa katika familia yake, kwa mume wake, na angeweza kuwa msaada wa pekee kwa binti yake. Wote wanaoshiriki katika vita hii na Shetani na majeshi yake, wana kazi ya

karibu mbele yao. Hawapaswi kuwa wepesi katika kuathiriwa kama nta, ambayo moto huweza kuiyeyusha katika namna yoyote. Lazima wavumilie magumu kama askari waaminifu, wasimame katika kituo cha ulinzi, na kuwa wa Kweli kila wakati. {2Tsw 101.1}

Roho wa Mungu anapambana na familia hii yote. Atawaokoa ikiwa wako tayari kuokolewa kwa njia Yake. Sasa ni saa ya rehema. Sasa ni siku ya wokovu. Sasa, sasa, ni wakati wa Mungu. Kwa niaba ya Kristo tunawasihi wapatanishwe na Mungu wakati wanapoweza, na kwa unyenyekevu, na hofu na kutetemeka, wautimize wokovu wao. Nilioneshwa kwamba ilikuwa kazi ya Shetani kuliweka kanisa katika hali ya kutotambua na kukosa hisia, ili vijana wapate kudumu katika daraja lake mwenyewe. Niliona kwamba vijana walikuwa wanashawishiwa na mvuto wa ile Kweli. Ikiwa wazazi wangejiweka wakfu kwa Mungu na kufanya kazi kwa nia ya uongofu wa watoto wao, Mungu angejifunua kwao na kulitukuza Jina Lake kati yao. {2Tsw 102.1}

Kisha nilioneshwa habari ya Ndugu U, kwamba Shetani alikuwa akimfunga mikanda yake na kumpeleka mbali na Mungu na ndugu zake. Ndugu V amekuwa na ushawishi wa kutia giza sana ufahamu wa ndugu huyu kwa kutokuamini kwake. Nilielekezwa nyuma na kuonyeshwa kuwa njia ya busara zaidi haikufuatwa kwa habari ya ndugu huyu. Hakukuwa na sababu ya kutosha kwanini alipaswa kuachwa nje ya kanisa. Alipaswa kutiwa moyo, hata kuhamasishwa-kusisitiziwa kwa mkazo, kuungana na ndugu zake katika nafasi ya kanisa. Alikuwa katika hali inayofaa zaidi kuingia kanisani kuliko watu kadhaa ambao walikuwa wameungana nalo. Hakuelewa mambo kwa wazi, na adui alitumia kutokuelewa huku kwa madhara yake. Mungu, aonaye mioyo, amefurahishwa zaidi na maisha na mwenendo wa Ndugu U kuliko maisha ya wengine ambao waliungana na kanisa. Ni mapenzi ya Bwana kuwa aje karibu na ndugu zake, ili aweze kuwa nguvu kwao na wao nguvu kwake. {2Tsw 102.2}

Mke wa Ndugu U anaweza kufikiwa na ile Kweli. Katika mambo mengi mwenendo wake hautiliwi shaka kama ile ya wengine wanaodai kuiamini Kweli yote. Walakini hapaswi kuangalia kushindwa na makosa

ya wale wanaodai mambo yaliyo bora, lakini aulize kwa dhati na bidii: Kweli ni nini? Anaweza kutumia mvuto kwa wema kwa muunganiko na mwenza wake. Nafsi hizi, zilizotakaswa kupitia ile Kweli, zinaweza katika nguvu ya Mungu kuwa nguzo katika kanisa na kushinikiza mvuto unaookoa kwa wengine. Roho hizi pendwa zinawajibika kwa Mungu kwa mvuto wanaotoa. Ama wanakusanya pamoja na Kristo au wanatawanya mbali. Mungu anahitaji uzito wa ushawishi wao katika kazi Yake, upande wa ile Kweli. Yesu amewanunua kwa damu Yake Mwenyewe. Wao sio mali zao wenyewe, kwa maana wamenunuliwa kwa thamani/gharama. Kwa hivyo kazi iko mbele yao kumtukiza Mungu katika miili na roho zao, ambazo ni mali Yake. Tunafanya kazi kwa ajili ya umilele. Ni ya umuhimu mkubwa kwamba kila saa itumiwe katika utumishi wa Mungu, na hivyo kujipatia hazina mbinguni. {2Tsw 103.1}

Nilioneshwa swala lako, Ndugu V, kuhusiana na kanisa huko ----, miaka miwili iliyopita. Njozi ilihusiana na wakati uliopita, wa sasa, na ujao. Tunaposafiri na kusimama mbele ya watu katika maeneo tofauti, Roho wa Bwana huleta mbele yangu kwa wazi habari ya mambo niliyooneshwa, hufufua jambo nililopewa hapo awali. Nilioneshwa wewe ukiwa unaipokea Sabato, wakati ukipingana na zile Kweli muhimu zinazohusiana na Sabato. Wewe haukuimarishwa na ile Kweli yote. Kisha niliona akili yako ikielekezwa kwenye mkondo wa kutokuamini, wa mashaka na kutotumaini, na kutafuta kupata vile vitu vilivyokuzwa ili kuimarisha kutokuamini na giza. Badala ya kutafuta ushahidi wa kuimarisha imani, ulifuata mwenendo tofauti kabisa, na Shetani alielekeza akili yako katika mwenendo unaofaa makusudi yake mwenyewe. Unapenda kulumbana/kupigana, na unapoingia kwenye uwanja wa vita, hujui wakati wa kuweka chini silaha zako. Unapenda kubishana, na umeendekeza hii hadi imekutoa katika nuru, imekutoa katika ile Kweli na kwa Mungu, nawe umekwenda mahali ambapo umefunikwa na giza, na kutokuamini kumeitawala akili yako. Wewe umepofushwa na Shetani. {2Tsw 103.2}

Kama Tomaso asiye na imani, umechukulia kuwa ni sifa kuona shaka isipokuwa kama ungekuwa na ushahidi dhahiri, ukiondoa akilini mwako sababu zote za shaka. Je, Yesu alimpongeza Tomaso asiyeamini

wakati akimpa ushahidi ambao alisema angeupata kabla hajaamini? Yesu akamwambia: “usiwe asiyeamini, bali aaminiye.” Tomaso akajibu: “Bwana wangu na Mungu wangu.” Sasa akawa amelazimika kuamini; hakuna nafasi ya shaka. Ndipo Yesu akamwambia: “Tomaso, Wewe kwa kuwa umeniona, umesadiki: wana heri wale wasioona, wakasadiki.” Uliwakilishwa kwangu kama anayeungana na kiongozi wa waasi na jeshi lake katika kuudhi, kusumbua, kufadhaisha, kuvunja moyo, kukatisha tamaa, na kupindua wale wanaoipigania haki, na wanaosimama chini ya bendera yenye damu ya Mfalme Imanueli. Nilioneshwa, mvuto wako umegeuza roho kutoka katika kuitunza Sabato ya amri ya nne. Umetumia talanta zako na ujuzi wako wa kutengeneza silaha ili kuweka katika mikono ya maadui wa Mungu, ili kupigana na wale wanaojaribu kumtii Mungu kwa kuzishika amri Zake. Wakati malaika wameagizwa kuimarisha mambo yaliyosalia, kustahimili na kukabiliana na mvuto wako, wameangalia kwa huzuni kubwa juu ya kazi yako ya kuvunja moyo na kuharibu. Umewasababisha malaika safi, wasio na dhambi, na watakatifu kulia machozi. {2Tsw 104.1}

Wale ambao wanaishi kati ya hatari za siku za mwisho, siku ambazo zinajulikana kwa watu wengi kugeuka toka katika ile Kweli ya Mungu na kwenda katika hadithi za uongo, watakuwa na kazi ya karibu ya kugeuka toka katika hekaya walizoandaliwa kila upande, na kujipatia hamu ya kujilisha katika Kweli, isiyopendwa na wengi. Wale wanaogeuka toka katika hadithi hizi za kubuni ili kwenda katika ile Kweli wanadharauliwa, kuchukiwa, na kuteswa na wale wanaoziwasilisha hekaya hizi kwa watu ili kupokelewa. Shetani anapigana vita na masalia ambao wanajitahidi kuzishika amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu. Malaika waovu wameagizwa kuwatumia watu kama mawakala wao juu ya nchi. Hawa wanaweza kufanikiwa zaidi kutoa ushawishi ili kufanya mashambulio ya Shetani kufanikiwa dhidi ya watu waliosalia ambao Mungu anawaita “Uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, wapate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita watoke gizani wakaingie katika nuru Yake ya ajabu.” Hili, Shetani ameazimia kulizuia. Adui atatumia kila mtu atakayejihusisha na huduma kazi Yake ya kuwazuia wateule wa Mungu kuzitangaza sifa za Yeye aliyewaita watoke gizani



wakaingie katika nuru Yake ya ajabu. Kuficha, na kufunika nuru hii, na kuwasababisha watu wasiitumaini, na kuleta kutoamini, ni kazi ya mwasi mkuu na jeshi lake. Wakati Yesu anawatakasa watu Wake, Kwake Mwenyewe, akiwakomboa toka katika uovu wote, Shetani atayatumia majeshi yake kuzuia kazi na kuzuia ukamilifu wa watakatifu. Adui hatoi nguvu zake kwa wale wote ambao tayari wamefunikwa kwa udanganyifu na wamezingirwa na hadithi za kubuni na makosa, na ambao hawafanyi jitihada kuipokea na kuitii ile Kweli. Adui anajua ana uhakika na hao; lakini wale wanaoitafuta ile Kweli, ili waweze kuitii kwa kuipenda, ndio wanaochochea hasira/uovu wake na hasira yake. Adui hawezi kamwe kuwadhoofisha wakati wanaendelea kuwa karibu na Yesu; kwa hivyo anafurahi anapoweza kuwaongoza katika njia ya kutotii. {2Tsw 105.1}

Tunapomtenda Mungu dhambi, kuna mwelekeo wa kurudi nyuma ya Yesu, kwa kumwacha mwendo wa safari ya umbali wa siku moja; tunatafuta kujitenga na ushirika Wake kwa sababu haitupendezi/tunachukizwa, kwa kila mwanga wa nuru itokayo katika uwepo Wake wa Kiungu, kwa kuwa inaelekeza katika dhambi ambayo tumekuwa na hatia nayo. Shetani anafurahi juu ya dhambi ambazo amezishawishi roho kuzitenda, na anatumia zaidi haya madhaifu na dhambi. Huwa anayarudia-rudia madhaifu haya kwa malaika wa Mungu, na kuwatolea dhahaka za uchokozi zenye maneno ya kuudhi na kuumiza, kuhusiana na madhaifu haya na kushindwa. Kwa kila njia ni mshtaki wa ndugu, na hufurahi juu ya kila dhambi na makosa ambayo watu wa Mungu wanadanganywa kutenda. Wewe, Ndugu V, umeshiriki katika kazi iyo hiyo kwa kiwango kikubwa. Umechukua kile kilichoonekana kwako kama makosa, udhaifu, na mapungufu katika madaraja ya Waadventista wanaoitunza Sabato, na umewaletea maadui wa imani yetu waliokuwa wakipigana vita dhidi ya kundi lile ambalo malaika wa mbinguni walikuwa wakilihudumia, na ambalo shauri lao, Yesu aliyekuwa Wakili wao, alikuwa akisihi mbele za Baba Yake. Akilia, “Uwarehemu/wanusuru, Baba, uwarehemu, nimewanunua kwa damu Yangu,” na kumwinulia Baba Yake mikono Yake iliyojeruhiwa. Umekuwa na hatia mbele za Mungu kwa dhambi kubwa. Umekuwa ukutumia nafasi ya vitu vile vinavyohuzunisha, vinavyoleta uchungu kwa watu wa Mungu wanapowaona baadhi ya wanadamu

wenzao hawajajiweka wakfu na kushindwa mara kwa mara na Shetani. Badala ya kuzisaidia roho hizi zinazokosea ili ziwe zifanye yaliyo haki kwa usahihi, kwa furaha umefanya makosa yao kuwa dhahiri kwa wale waliowachukia kwa sababu walikiri kuzishika amri za Mungu na imani ya Yesu. Umefanya iwe ngumu sana kwa wale waliokuwa wanashiriki katika kazi ya kuokoa wale wanaopotea, kuwasaka kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. {2Tsw 106.1}

Kwa sababu ya kutotii kwa Israeli na kuondoka kwa Mungu, waliruhusiwa kuletwa katika maeneo magumu na kupatwa na mabaya; maadui zao waliruhusiwa kufanya vita nao, kuwanyenyekeza na kuwaongoza kumtafuta Mungu katika shida na taabu zao. “Wakati huo Waamaleki wakatokea, wakapigana na Israeli huko Refidimu.” Hili lilitokea mara tu baada ya wana wa Israeli kutawaliwa na kwa manung'uniko yao ya uasi na malalamiko yasiyo ya haki, yasiyofaa dhidi ya viongozi wao, ambao Mungu aliwastahilisha na kuwateua kuwaongoza jangwani hadi nchi ya Kanaani. Mungu alielekeza njia yao, mahali ambapo hapakuwa na maji, kuwathibitisha, ili aone ikiwa, baada ya kupokea ushuhuda mwingi wa uweza Wake, walikuwa wamejifunza kumgeukia Yeye katika shida zao, na walikuwa wametubu manung'uniko yao ya uasi uliopita dhidi Yake. Waliwashtaki Musa na Haruni kwa misukumo na nia za ubinafsi kwa kuwatoa Misri ili kuwaua wao na watoto wao kwa njaa, ili wapate kujitarisha kwa mali zao. Kwa kufanya hivi Waisraeli walimpa mwanadamu kile walichopokea kama ushahidi wa wazi kwamba kilitoka kwa Mungu peke Yake, ambaye nguvu Zake hazina kikomo. Udhahirisho huu wa miujiza ya kushangaza ya nguvu za Mungu, Yeye angewataka waihusishe na uwezo Wake Yeye peke Yake, na kulitukuza Jina Lake duniani. Mungu aliwaleta juu ya uwanja ule ule wa jaribu mara kwa mara ili kuthibitisha ikiwa bado walikuwa hawajajifunza utendaji Wake na kutubu kutotii kwao na manung'uniko ya uasi. Huko Refidimu, wakati watu walipopatwa na kiu ya maji, walikuwa na kiburi tena, na kuonesha kuwa bado walikuwa na moyo mwovu wa kutokuamini, wa manung'uniko, wa uasi, uliodhahirisha Ukweli kwamba bado isingekuwa salama kuwathibitisha katika nchi ya Kanaani. Ikiwa wasingemtukuza Mungu katika majaribu na shida zao, katika safari zao jangwani hadi Kanaani waliyoitazamia, wakati Mungu daima alikuwa akiwapa ushahidi wa nguvu na utukufu

Wake, na utunzaji Wake kwao, wasingelitukuza Jina Lake na kumtukuza Yeye alipowathibitisha katika nchi ya Kanaani, wakizungukwa na baraka na mafanikio. Kwa sababu watu walikuwa na kiu ya maji, walikasirika, hata Musa akaogopa kwa ajili ya maisha yake. {2Tsw 106.2}

Wakati Israeli waliposhambuliwa na Waamaleki, Musa alimpa Yoshua maagizo ya kupigana na maadui zao wakati akiwa amesimama na fimbo ya Mungu mkononi mwake, na mkono wake ukiinuliwa kuelekea mbinguni machoni pa watu, kuwaonyesha Israeli waasi, wanaonung'unika kwamba nguvu na uwezo wao vilikuwa kwa Mungu. Alikuwa uwezo wao na chanzo cha nguvu zao. Hakukuwa na nguvu katika fimbo ile; Mungu alifanya kazi kupitia Musa. Musa alipaswa kupokea nguvu zake zote toka juu. Alipoinua mikono yake, Israeli walishinda; wakati alipoishusha chini ya mikono yake, Amaleki walishinda. Wakati Musa alipochoka, mikakati ya lazima ilibidi ifanywe ili kuitegemeza mikono yake iliyochoka iendeleo kuinuliwa kuelekea mbinguni. Haruni na Huri walimwandalia Musa kiti, na kisha wote walishiriki katika kuinua mikono yake iliyochoka hadi wakati wa jua kuzama. Kwa hiyo watu hawa waliwaonesha Israeli wajibu wao katika kumtegemeza Musa kwenye kazi yake ngumu wakati alipopaswa kupokea Neno toka kwa Mungu ili awaambie nao. Tendo hili pia lilikuwa likiwaonesha Israeli kwamba Mungu peke Yake Ndiye aliyeshikilia hatima yao mikononi Mwake, kwamba alikuwa kiongozi wao anayetambuliwa. "Bwana akamwambia Musa, Andika habari hii katika kitabu, iwe ukumbusho, kisha ihubiri masikioni mwa Yoshua; ya kuwa nitaufuta ukumbusho wa Amaleki kabisa, usiwe tena chini ya mbingu. . . . Akasema, Bwana ameapa; Bwana atakuwa na vita na Amaleki kizazi baada ya kizazi." Kumbuka aliyokufanyia Amaleki katika njia mlipokuwa mkitoka Misri; jinsi alivyokukuta katika njia, akakupiga katika watu wako walioachwa nyuma, wote waliokuwa wanyonge nyuma yako, ulipokuwa umechoka na kuzimia; wala asimche Mungu. Basi itakuwa, hapo atakapokwisha kukupumzisha Bwana, Mungu wako, katika adui zako wote walio kando-kando, katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi uimiliki, ndipo uufute ukumbusho wa Amaleki chini ya mbingu; usisahau." {2Tsw 107.1}

Malaika wa Mungu alipowasilisha Kweli hizi katika safari na uzoefu wa wana wa Israeli, nilivutiwa sana na jinsi Mungu alivyowajali watu Wake kwa namna ya pekee. Licha ya makosa yao, kutotii kwao, na uasi wao, bado walikuwa wateule wa Mungu. Yeye Alikuwa amewaheshimu sana kwa kushuka toka kwenye makao Yake matakatifu na hata kuja juu ya Mlima Sinai na, kwa ukuu na utukufu na fahari kuu ya kutisha, akazitamka Amri Kumi mbele ya watu wote na kuziandika kwa kidole Chake Mwenyewe katika mbao za mawe. Bwana anasema hivi juu ya watu Wake Israeli: “Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako; Bwana Mungu wako, amekuchagua kuwa watu Wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi. Bwana hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote; bali kwa sababu Bwana anawapenda, na kwa sababu alitaka kutimiza kiapo Chake alichowaapia baba zenu.” {2Tsw 108.1}

Nilioneshwa kuwa wale wanaojaribu kumtii Mungu na kutakasa roho zao kwa kuitii ile Kweli, ni wateule wa Mungu, Israeli Wake wa sasa. Mungu anasema juu yao, kupitia kwa Petro: “Bali ninyi ni uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.” Kama ilivyokuwa kosa kwa Amaleki kutumia udhaifu na uchovu wa Israeli, kuwaudhi, kuwafadhaisha, na kuwavunja moyo, ndivyo haikuwa dhambi ndogo kwako kutazama kwa karibu ili kugundua udhaifu, kusitasita, makosa na dhambi za watu wa Mungu wanaoteseka, na kuzifunua kwa adui zao. Ulikuwa unafanya kazi ya Shetani, na sio kazi ya Mungu. Wengi miongoni mwa Waadventista wanaoishika Sabato huko ----- wamekuwa wadhaifu sana. Wamekuwa wawakilishi wanyonge wa ile Kweli. Hawakuwa na kicho au heshima kwa kazi ya Ukweli wa sasa, na kazi ingekuwa bora zaidi bila wao. Umetumia maisha yasiyowekwa wakfu ya watunza Sabato kama udhuru wa wewe kuchukua msimamo wako wa mashaka na kutokuamini. Umeimarisha pia kutokuamini kwako, kuona kwamba baadhi ya hawa wasiojiweka wakfu wakikiri imani thabiti katika njozi, kuwathibitisha wanapopingwa, na kuwatetea kwa joto-joto (shauku), ambapo, wakati uo huo kwamba walidai juhudi kubwa sana, walikuwa wanapuuza mafundisho yaliyotolewa kupitia maono na walikuwa

wanaenda moja kwa moja kinyume nayo. Kwa jambo hii walikuwa kikwazo kwa Ndugu U, na walikuwa wanasababisha maono kuwa na sifa mbaya kwa mwenendo wao. {2Tsw 109.1}

Ndugu V, nilioneshwa kuwa ulikuwa na moyo wenye kiburi, na ulipofikiri maandishi yako yalipuuzwa katika ofisi ya gazeti la *Review*, kiburi chako kiliguswa, na ukaanza vita ambavyo vimekuwa kama Sauli kuupiga mateke mchoko. Umejiunga na wale wanaogeuzi Kweli ya Mungu kuwa uongo. Umeimarisha mikono ya wenye dhambi na kupinga shauri la Mungu dhidi ya nafsi yako mwenyewe. Umekuwa ukipigana vita dhidi ya kile usichokijua. Hujajua ni kazi gani ulikuwa ukiifanya. Nilimwona mke wako akipambana na Mungu katika maombi, imani yake ikikushika kwa nguvu na kwa wakati uo huo ikitazama katika kiti cha enzi, akiomba ahadi za Mungu zisizoshindwa, kamwe kamwe. Moyo wake umeuma alipokuona ukidumu katika vita vyako dhidi ya ile Kweli. Nilioneshwa kuwa ulikuwa unafanya hivi bila kujua, kwa kupofushwa na Shetani. Wakati unashiriki katika vita hivi, haukuwa ukikua kiroho na kujitoa kwa Mungu. Haukuwa na ushahidi kuwa njia zako zilimpendeza Mungu. Ulikuwa na juhudi, lakini sio kulingana na maarifa. Haukuwa na uzoefu katika wito wangu niliopewa, hakika ulikuwa umeniona kwa nadra sana, na haukuwa na ufahamu wa kazi yangu. {2Tsw 110.1}

Ndugu V, una sifa ambazo zinaweza kukufanya uwe wa huduma maalum katika kanisa lililoko----, au katika kanisa lingine lolote, ikiwa talanta zako zingetolewa kwa ajili ya kutegemeza kazi ya Mungu. Niliona kuwa watoto wako walikuwa sasa katika hali ya kuvutiwa na ile Kweli, na Yesu alikuwa akikuombea, Ndugu V: "Mrehemu kidogo." Nilioneshwa kuwa ikiwa ungeongolewa katika ile Kweli, ungekuwa nguzo katika kanisa, na ungemheshimu Mungu kwa mvuto wako, uliotakaswa kupitia ile Kweli. {2Tsw 110.2}

Niliona malaika wa rehema wakimzunguka Ndugu V. Nilioneshwa kuwa alikuwa amedanganywa sana katika stahiki za maadili na kusimama mbele za Mungu kwa daraja hilo ambao wamejitoa katika mwili. Wachache waaminifu wamo miongoni mwao; hawa wataokolewa; lakini wengi wao kwa muda mrefu hawajajiweka wakfu

katika moyo, na shuhuda za karibu zimekuwa katika njia yao, nira ya utumwa kwao. Wameitupa mbali nira na kubaki na njia zao potovu. Mungu anakuita wewe ujitenge nao. Jitenge na hawa ambao furaha yao ni kupigana vita dhidi ya ile Kweli ya Mungu. Kidogo kutoka kwa hii, tabia ya Kweli itajengwa. Wao ni wa daraja lile linalopenda, linaloishi na kusema uwongo. {2Tsw 111.1}

Ikiwa bidii yako yote iko katika ile Kweli na kazi ya maandalizi kwa ajili wakati huu itatakaswa kupitia ile Kweli utupata stahiki ya maisha ya kutokufa. Upo katika hatari ya kuwa mkali sana kwa watoto wako kwa kila kipengele na unakuwa sio mvumilivu kama inavyohitajika. Kazi kamili ya maandalizi ni lazima iendelee pamoja na wote wanaoikiri ile Kweli, hata tutakaposimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu bila kosa, bila doa, wala kunyanzi, au kitu chochote kama hicho. Mungu atakusafisha ikiwa utajisalimisha kwa mchakato wa utakaso. {2Tsw 111.2}

## **SURA YA 13**

### **KUSUDI LA SHUHUDA BINAFSI**

Wapendwa Ndugu na Dada: Bwana amejidhihirisha tena kwangu. Juni 12, 1868, nilipokuwa nikizungumza na ndugu katika nyumba ya ibada huko Battle Creek, Michigan, Roho wa Mungu alikuja juu yangu, na kwa ghafla nilikuwa katika njozi. Mandhari ilikuwa pana. Nilikuwa nimeanza kuandika Gombo la tano la Vipawa vya Roho (Spiritual Gifts). Iakini nilipokuwa na shuhuda za asili ya kivitendo ambazo unapaswa kuwa nazo mara moja, niliacha chapisho lile ili kuandaa kitabu hiki kidogo. {2Tsw 112.1}

Katika njozi hii ya mwisho nilioneshwa kile kinachothibitisha kabisa mwelekeo wangu katika kuchapisha shuhuda binafsi. Bwana anapochagua masuala ya mtu binafsi na kubainisha makosa yao, wengine, ambao hawajaoneshwa katika njozi, mara nyingi wanachukulia kirahisi kuwa wao wako wakamilifu au wanakaribia kuwa hivyo. Ikiwa mtu anakemewa kwa kosa fulani, ndugu na dada wanapaswa kujichunguza kwa uangalifu ili kuona ni wapi

wameshindwa na wapi wamekuwa na hatia ya dhambi iyo hiyo. Wanapaswa kuwa roho ya ungamo la unyenyekevu. Ikiwa wengine wanawafikiria kuwa wapo sawa, haiwafanyi kuwa hivyo. Mungu huangalia moyo. Yeye huthibitisha na kujaribu mioyo kwa namna hii. Kwa kukemea kosa la mtu mmoja, Yeye anapanga kuwarekebisha wengi. Lakini wakishindwa kubeba mashutumu wenyewe, na kujidanganya kwamba Mungu hajali makosa yao kwa sababu hakuwachagua wao hasa, wanajidanganya nafsi zao wenyewe na watafungiwa gizani na kuachwa katika njia zao wenyewe, kufuata mawazo ya mioyo yao wenyewe. {2Tsw 112.2}

Wengi wanashughulika kwa kujidanganya/uongo na nafsi zao wenyewe na wako katika udanganyifu mkubwa mbele za Mungu. Yeye hutumia njia na mbinu ili kutimiza kusudi Lake na kudhibitisha yaliyo katika mioyo ya wale wanaodai kuwa wafuasi Wake. Yeye Huweka wazi makosa ya wengine ili watu wengine wapate kuonywa, na kuogopa, na kuepuka makosa hayo. Kwa kujichunguza binafsi wanaweza kugundua kuwa wanafanya mambo yale yale ambayo Mungu anayashutumu kwa wengine. Ikiwa kweli wanatamani kumtumikia Mungu, na kuogopa kumkosea, hawatasubiri dhambi zao kuelezwa kwa kubainishwa vibaya kabla hawajaungama, na kwa toba ya unyenyekevu kumgeukia Bwana. Watayaaacha mambo yaliyomchukiza Mungu, kulingana na nuru waliyopewa wengine. Ikiwa, kinyume chake, wale ambao wanatenda yasio haki na wanaona kuwa wana hatia ya dhambi zile zile zilizokemewa kwa wengine, lakini bado wanaendelea katika mwenendo ule ule ambao haujawekwa wakfu kwa sababu tu hawajatajwa kwa kubainishwa majina yao, wanahatarisha nafsi zao wenyewe, nao watafanywa mateka na Shetani apendavyo. {2Tsw 113.1}

## **SURA YA 14**

### **KUHAMIA BATTLE CREEK**

Katika njozi niliyopewa Juni 12, 1868, nilioneshwa kuwa kazi kubwa inaweza kukamilishwa katika kuzileta roho katika ujuzi wa ile Kweli, ikiwa na juhudi sahihi zilizofanywa. Katika kila mji, jiji, na kijiji, kuna watu ambao wangeikubali ile Kweli ikiwa ingeletwa mbele yao kwa njia ya busara. Wamishenari wanahitajika kati yetu, wamishenari wanaojitoa kafara nafsi, ambao, kama Mfano wetu mkuu, hawatajifurahisha wenyewe, lakini wataishi kuwatendea wema wengine. {2Tsw 113.2}

Nilioneshwa kuwa kama watu tuna upungufu. Kazi zetu hazilingani na imani yetu. Imani yetu inashuhudia kwamba tunaishi wakati wa kutangazwa kwa ujumbe mzito na muhimu sana kuwahi kupewa wanadamu wanaokufa. Walakini kwa mtazamo kamili wa Ukweli huu, jitihada zetu, ari yetu, bidii yetu, roho yetu ya kujitoa kafara, havilingani na tabia ya kazi. Tunapaswa kuamka toka kwa wafu, na Kristo atatupatia uzima. {2Tsw 114.1}

Kwa ndugu na dada zetu wengi, kuna mwelekeo wenye nguvu wa kuishi Battle Creek. Familia zimekuwa zikitoka pande zote ili kuishi huko, na wengi zaidi wameelekeza nyuso zao huko. Wengine ambao wamekuja Battle Creek walikuwa na nyadhifa katika makanisa madogo waliyoyahama, na msaada wao na nguvu zilikuwa zinahitajika huko. Watu hao wanapofika Battle Creek, na kukutana na watunza Sabato wengi huko, mara nyingi wanahisi kuwa shuhuda zao hazihitajiki, na kwa hiyo talanta zao huzikwa. {2Tsw 114.2}

Wengine huchagua Battle Creek kwa sababu inatoa fursa au mapendeleo ya kidini/kiroho, ila wanashangaa kwamba hali yao ya kiroho kwanini hupungua baada ya kukaa kwao hapo kwa miezi michache. Je, hakuna sababu ya jambo hili kuwa hivi? Kusudi la wengi limekuwa kujinufaisha wenyewe kifedha-- kushiriki katika biashara ambayo itawazalishia faida kubwa zaidi. Matarajio yao katika hili yanaweza kuwa kweli, wakati wana upungufu wa kiroho na kudumazwa katika mambo ya kiroho. Hawabebi mzigo maalumu kwa sababu wanafikiri hawatajisikia vizuri. Hawajui mahali pa kushikilia ili kutenda kazi katika kanisa kubwa sana, na kwa hivyo huwa wavivu katika shamba la mizabibu la Bwana wao. Wote wanaofuata



mwenendo huu huongeza tu kazi kwa wale walio na mzigo wa kazi kanisani. Wao ni mizigo mkubwa sana. Kuna wengi huko Battle Creek ambao kwa upesi huwa matawi yaliyokauka. {2Tsw 114.3}

Wengine ambao wamekuwa wafanyikazi wale ambao wana uzoefu katika kazi ya Ukweli wa sasa, wanahamia Battle Creek na kutua mzigo wao hapo. Badala ya kuhisi umuhimu wa nguvu maradufu, kukesha, kuomba, na kutekeleza majukumu kwa bidii, wala hawafanyi chochote. Wale ambao wana mizigo ya kubeba ofisini, na hawana muda kwa ajili ya majukumu kando na kazi zao, wanalazimika kujaza nafasi za uwajibikaji kanisani na kufanya kazi muhimu, na nzito ambayo wasipoifanya itabaki bila kufanywa kwa sababu hawa watu wengine, hawataubeba mzigo. {2Tsw 114.4}

Ndugu ambao wanataka kubadilisha eneo la makazi yao, wanaoutazama utukufu wa Mungu, na kuhisi wajibu binafsi upo juu yao kuwatendea mema wengine, kufaidisha na kuokoa roho ambazo Kristo hakuwazuilia maisha Yake ya thamani, wanapaswa kwenda katika miji na vijiji ambako kuna nuru kidogo au hakuna kabisa nuru na pale wanapoweza kutoa huduma ya kweli na kuwabariki wengine kwa bidii na uzoefu wao. Wamishenari wanatakiwa kwenda katika miji na vijiji na kuinua kiwango cha Kweli, ili mashahidi wa Mungu watawanyike kote nchini, ili nuru ya Kweli iweze kupenya kule ambako bado haijafikia, na kiwango cha ile Kweli kiinuliwe ambako hakijulikani bado. Ndugu hawapaswi kukusanyika pamoja kwa sababu tu inawapendeza zaidi, lakini wanapaswa kutafuta kutimiza wito wao mkuu wa kuwatendea wema wengine, watumike katika wokovu angalau wa roho moja. Lakini wengi zaidi waweze kuokolewa kuliko mtu mmoja. {2Tsw 115.1}

Kusudi pekee la kazi hii halipaswi kuwa tu kuongeza thawabu yetu mbinguni. Wengine ni wabinafsi katika suala hili. Kwa mtazamo wa kile Kristo alichotutendea, na kile alichopitia kwa ajili ya wenye dhambi, tunapaswa, kwa upendo safi, usiojifikiria nafsi, kuiga mfano Wake Bwana, kwa kutoa kafara anasa zetu wenyewe na hali inayofaa kwa faida yao. Furaha iliyowekwa mbele ya Kristo, ambayo iliyomtegemeza katika mateso Yake yote, ilikuwa ni wokovu wa wenye dhambi maskini. Hii inapaswa kuwa furaha yetu na kuchochea tamatio letu katika kazi

ya Bwana wetu. Kwa kufanya hivyo tunampendeza Mungu na kuudhihirisha upendo wetu na kujitoa Kwake kama watumishi Wake. Yeye alitupenda kwanza, na hakutuzuilia Mwanawe mpendwa, bali alimtoa toka kifuani Mwake afe ili sisi tuweze kuupata uzima. Upendo, upendo wa Kweli kwa wanadamu wenzetu, hudhihirisha upendo kwa Mungu. Tunaweza kukiri imani ya juu, lakini pasipo upendo huu ni bure tu. Imani yetu inaweza kutuongoza hata kuitoa miili yetu ichomwe moto, lakini bila upendo wa kujitoa kafara, kama uliokuwa katika kifua cha Yesu na kuuonesha kwa mfano katika maisha Yake, sisi ni kama shaba iliayo na upatu uvumao. {2Tsw 115.2}

Kuna familia ambazo hupokea nguvu za kiroho kwa kuhamia Battle Creek. Ni mahali tu pa kuwasaidia wengine, wakati ni mahali pasipokuwa sahihi kwa wengine. Ndugu na Dada A ni mfano wa daraja ambalo wanaweza kunufaika kwa kuhamia mahali hapa. Bwana aliwaelekeza wachukue uelekeo huu. Battle Creek palikuwa tu mahali pa kuwanufaisha, na pameonekana kuwa baraka kwa familia nzima. Wamepata, kwa kuja hapa, nguvu ya kusimama imara katika jukwaa la ile Kweli, na ikiwa wataendelea katika njia ya utii wenye unyenyekevu wanaweza kufurahi kwa msaada walioupokea huko Battle Creek. {2Tsw 116.1}

## SURA YA 15

### TAHADHARI KWA WAHUBIRI.

Katika njozi niliyopewa Juni 12, 1868, niliguswa moyo sana na kazi kubwa inayotakiwa kutimizwa kuwaandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Niliona kwamba mavuno ni mengi, bali watendakazi ni wachache. Wengi ambao kwa wakati huu wako shambani, wakifanya kazi kuokoa roho, ni wadhaifu. Wamebeba mizigo mizito, ambayo imewachosha na kuwalemea. Walakini, nilioneshwa kwa baadhi ya wahubiri wetu kuwa kumekuwa na matumizi makubwa sana ya nguvu ambayo kwa hakika haikuhitajika. Wengine huomba kwa muda mrefu sana na kwa sauti kubwa, ambayo inamaliza nguvu zao

dhaifu na hivyo hutumia pasipo ulazima nguvu zao; wengine mara nyingi huongeza mahubiri yao theluthi moja au nusu zaidi kuliko wanavyopaswa. Kwa kufanya hivyo wanachoka kupita kiasi, mvuto hupungua kwa watu kabla ya mahubiri kufungwa, na mengi hupotea kwao, kwa kuwa hawawezi kuyatunza waliyokwishapokea. Nusu moja tu ya mahubiri, ingekuwa bora kuliko kuendelea mbele zaidi ya hapo. Ingawa mambo yote yanaweza kuwa muhimu, mafanikio yangekuwa makubwa zaidi ikiwa kusali na kuongea kwao kungekuwa kiasi. Matokeo yangefikwa bila uchovu mwingi. Wanamaliza uwezo na nguvu zao, ambazo, kwa manufaa ya kazi, ni muhimu sana kuhifadhi. Ni juhudi ya muda mrefu, baada ya kufanya kazi hadi kufikia uchovu, ambayo hulemea na kuvunja mwili. {2Tsw 116.2}

Niliona kuwa ilikuwa kazi hii ya ziada, wakati mfumo ulipochoka, ndiyo ilimaliza maisha ya Ndugu mpendwa Sperry na kumfanya kwenda kaburini kabla ya wakati. Kama angelifanya kazi kwa kuzingatia afya angeweza kuishi na kufanya kazi mpaka wakati huu wa sasa. Ilikuwa pia, kazi hii ya ziada ambayo ilimaliza nguvu ya uhai ya Ndugu yetu mpendwa Cranson na kusababisha maisha yake ya manufaa kuzimishwa. {2Tsw 117.1}

Uimbaji mwingi, pamoja na kuomba kwa kuinama muda mrefu na kuzungumza, vinachosha sana. Katika visa vingi wahubiri wetu inaonyesha hawapaswi kuendeleza juhudi zao zaidi ya saa moja. Wanapaswa kuacha utangulizi na kuja kwenye somo mara moja, na wanapaswa kujifunza kufunga mahubiri wakati hamu ya watu katika kusikiliza ni kubwa zaidi. Hawapaswi kuendeleza juhudi hadi wasikiaji wao watamani waache kusema. Mengi ya hii kazi ya ziada hupotea kwa watu, ambao mara nyingi wamechoka sana kufaidika na kile wanachosikia; na nani awezaye kujua ni upotevu mkubwa wa kiasi gani unapatikana na wahubiri wanaofanya kazi hivyo? Mwishowe hakuna kinachopatikana kwa kuubebesha nguvu ya mwili kazi hii. {2Tsw 117.2}

Mara kwa mara nguvu inachoka mwanzoni tu mwa juhudi za muda mrefu. Na wakati muafaka kabisa ambapo kuna mengi ya kupata au kupoteza katika mahubiri, mhubiri wa Kristo aliyejitoa, mwenye moyo uliohamasishwa, na mwenye nia ya kufanya kazi, hawezi kutoa nguvu.

Ameitumia katika kuimba, katika maombi marefu na muda mrefu mahubiri marefu, na ushindi unapotea kwa kukosa kazi ya bidii, iliyoongozwa vizuri kwa wakati unaofaa. Wasaa wa thamani umepotea. Maoni yaliyotolewa hayakufuatwa. Ingelikuwa bora kama matamania/shauku isingeamshwa; kwa kuwa usadikisho ukipingwa mara na kushindwa, ni vigumu sana kuvutia akili tena kwa ile Kweli. {2Tsw 117.3}

Nilioneshwa kwamba ikiwa wahubiri wetu wangekuwa na uangalifu katika kutunza nguvu yao, badala ya kuitumia pasipo lazima, kazi yao ya busara, iliyoelekezwa vizuri ingeweza kutimiza mengi zaidi kwa mwaka kuliko inavyoweza kutimizwa kwa kuongea kwa muda mrefu, kuomba, na kuimba, ambazo zinalemea na kuchosha. Katika kisa cha mwisho, watu mara nyingi wananyimwa kazi ambayo wanahitaji sana kwa wakati unaofaa, kwa kuwa mtendakazi anahitaji kupumzika na atahatarisha afya yake na maisha ikiwa ataendeleza juhudi zake. {2Tsw 118.1}

Ndugu zetu wapendwa Matteson na D.T Bourdeau wamefanya makosa hapa, na wanapaswa kufanya matengenezo katika namna yao ya kazi. Wanapaswa kuzungumza kwa ufupi na kuomba kwa ufupi. Wanapaswa kufika kwenye hoja mara moja na kuacha uchovu katika kazi zao. Wanaweza kutimiza mema zaidi kwa kufanya hivi, na kwa wakati uo huo kuhifadhi nguvu ya kuendeleza kazi wanazozipenda, bila kuchakaa na kuvunjika kabisa.-{2Tsw 118.2}

## SURA YA 16

### MTAZAME YESU

Katika njozi niliyopewa mnamo Juni 12, 1868, nilioneshwa hatari ya watu wa Mungu katika kumtazama Ndugu na Dada White na kufikiria kwamba lazima waje kwao na mizigo yao na kutafuta ushauri kwao. Hii halipaswi kuwa hivyo. Wanaalikwa na Mwokozi wao Mwenye huruma na upendo kuja Kwake, wanapokuwa wamechoka na kulemewa na mzigo, Naye atawapumzisha. Kwake watapata pumziko. Katika kupeleka fadhaa na majaribu kwa Yesu, ahadi zao zitatimizwa. Wanapohisi pumziko katika shida zao ambalo hupatikana kwa Yesu pekee wanapata uzoefu ambao ni wa thamani kubwa zaidi kwao. Ndugu na Dada White wanapambania usafi wa maisha, hupambana kuzaa matunda ya utakatifu; lakini wao ni watu wa kufa na wakosefu tu. Wengi huja kwetu na kuuliza: Je, nifanye hivi? Je, nishiriki katika biashara ile? Au, kwa habari ya mavazi, Je, nivae mtindo huu au ule? Ninawajibu: Mnakiri kuwa wanafunzi wa Kristo. Jifunzeni Biblia zenu. Jisomeeni Biblia zenu. Someni kwa makini na kwa maombi mengi maisha ya Mwokozi wetu mpendwa alipokaa kati ya wanadamu duniani. Igeni maisha Yake, na hamtapotea toka katika njia nyembamba. Tunakataa kabisa kuwa dhamiri kwa ajili yenu. Tukiwaambia cha kufanya, mtatutazama tuwaongoze, badala ya kwenda moja kwa moja kwa Yesu kwa ajili yenu wenyewe. Uzoefu wenu utajengwa kwetu. Ni lazima mwe na uzoefu wenu wenyewe, utakaojengwa kwa Mungu. Ndipo mtaweza kusimama katikati ya

hatari za siku za mwisho na kutakaswa na kutoteketezwa na moto wa mateso ambao watakatifu wote lazima waupitie ili uchafu uondolewe katika tabia zao kuandaliwa kwa ajili ya kazi yenye mguso wa mwisho wa maisha ya umilele. {2Tsw 118.3}

Wengi wa ndugu na dada zetu wapendwa wanafikiria kuwa hawawezi kuwa na mkusanyiko mkubwa kama Ndugu na Dada White wasipohudhuria. Katika maeneo mengi wanatambua kwamba lazima jambo fulani lazima lifanyike ili kuwahamisha watu katika bidii zaidi na hatua thabiti katika kazi na kusudi la Kweli. Wamekuwa na wahubiri wafanyao kazi miongoni mwao, lakini wanatambua kuwa kazi kubwa lazima ifanyike, na kuwatazama Ndugu na Dada White kuifanya. Hili, nililiona, halikuwa vile ambavyo Mungu angetaka. Kwanza, kuna upungufu kwa baadhi ya wahubiri wetu. Wanakosa kushugulikia mambo kwa ukamilifu. Hawabebi mzigo wa kazi na kusaidia kuinua pale hasa ambapo watu wanahitaji msaada. Hawana utambuzi wa kuona na kuhisi hasa ambapo watu wanahitaji kurekebishwa, kukaripiwa, kujengwa, na kutiwa nguvu. Baadhi yao hufanya kazi wiki na miezi kadhaa mahali fulani, na kwa kweli kuna mengi ya kufanya wakati wanaondoka kuliko walipoanza. Ukarimu usio na ubinafsi unasua-sua. Ni sehemu moja ya kazi ya mchungaji kuendeleza tawi hili la kazi; lakini, kwa sababu hili halipendezi, wengine hupuuza wajibu wao. Wanazungumza Kweli toka katika Neno la Mungu, lakini hawawavutii watu kwa hitaji la utii. Kwa hiyo wengi ni wasikiaji tu, lakini sio watendaji. Watu wanahisi upungufu. Mambo hayajawekwa katika utaratibu kati yao, na wanawatarajia Ndugu na Dada White wajazie upungufu huo. {2Tsw 119.1}

Baadhi ya ndugu zetu wanaohubiri wameteleza bila kutulia ndani katika kazi na kushikilia mioyo ya watu. Wametoa udhuru kwa mawazo kwamba Ndugu na Dada White wangeleta vitu ambavyo vilikuwa vinapungua; kwamba walikuwa wameizoea kazi kwa kipekee. Hawa watu wamefanya kazi, lakini si kwa njia sahihi. Hawajaubeba mzigo. Hawajasaidia pale ambapo msaada ulihitajika. Hawajasahihisha mapungufu yaliohitaji kusahihishwa. Hawajaingia kwa moyo wote, roho, na nguvu, katika mahitaji ya watu. Wakati umepita, na hawana chochote cha ushahidi wowote wa kuonesha kwa hilo. Mzigo wa

mapungufu yao unatuangukia sisi. Na wanatia moyo watu watuangelie, wakiwasilisha wazo kwamba hakuna kitakachokamilisha kazi isipokuwa Shuhuda yetu mahsusi/maalumu. Mungu hapendezwi na jambo hili. Wahubiri wanapaswa kuchukua majukumu makubwa na sio kuendeleza wazo kwamba hawawezi kuubeba ujumbe huo ambao utawasaidia watu pale wanapohitaji msaada. Kama hawawezi kufanya hivi, wanapaswa kukaa Yerusalemu mpaka watakapopewa nguvu kutoka juu. Hawapaswi kushiriki katika kazi ambayo hawawezi kuifanya. Wanapaswa kwenda wakilia, wakichukua mbegu ya thamani, na kurudi toka katika juhudi yao kwa furaha, wakileta miganda yao pamoja nao. {2Tsw 120.1}

Wahubiri wanapaswa kusesitiza kwa watu umuhimu wa juhudi za mtu mmoja mmoja. Hakuna kanisa linaloweza kustawi isipokuwa washiriki wake ni watendakazi. Lazima watu wainue mahali wanapoinua wahubiri. Niliona kuwa hakuna kitu cha kudumu kinachoweza kutimizwa kwa makanisa katika maeneo tofauti isipokuwa wameamshwa kuhisi kwamba jukumu liko juu yao. Kila kiungo cha mwili kinapaswa kuhisi kwamba wokovu wa roho yake mwenyewe unategemea juhudi yake mwenyewe. Roho haziwezi kuokolewa bila bidii. Mhubiri hawezi kuwaokoa watu. Anaweza kuwa mfereji ambao Mungu atautumia kutoa nuru kwa watu Wake; lakini baada ya taa kutolewa, inabakia kwa watu kujitwalia nuru hiyo, na, kwa upande wao, waingaze kwa wengine. Watu wanapaswa kuhisi kwamba jukumu la mtu binafsi liko juu yao, sio tu kuokoa roho zao wenyewe, bali kushiriki kwa bidii katika wokovu wa wale walio gizani. Badala ya kuwatazamia Ndugu na Dada White kuwasaidia kutoka katika giza lao, wanapaswa kushiriki kwa bidii katika kujisaidia wenyewe. Ikiwa wataanza kuwawinda wale walio wabaya zaidi kuliko wao, ili kujaribu kuwasaidia, wangejisaidia wenyewe kuingia kwenye nuru mapema kuliko njia nyingine yoyote. Ikiwa watu wanawaegemea Ndugu na Dada White, na kuwaamini, Mungu atawanyenyekeza kati yenu au kuwaondoa toka kwenu. Lazima mumtazame Mungu na kumtumainia Yeye. Muegemeeni Yeye, Naye hatawaacha. Hatawaacha mpotee. Neno la Mungu ni la thamani. “Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja Kwangu mpote kuwa na

uzima.” Haya ni Maneno ya Kristo. Maneno ya uvuvio, yakisomwa kwa uangalifu na kwa maombi na kutiiwa kivitendo, yatawafaa kikamilifu katika kila kazi njema. Wahubiri na watu lazima wamtazame Mungu. {2Tsw 120.2}

Tunaishi katika zama za uovu. Hatari za siku za mwisho zinazidi kutuzunguka. Kwa sababu uovu umezidi, upendo wa wengi unapoa. Henoko alitembea na Mungu miaka mia tatu. Ufupi wa wakati kwa sasa unaonekana kusesitizwa kama sababu ya kutafuta haki. Je, ni muhimu kwamba hofu ya siku ya Mungu iwekwe mbele yetu ili kutulazimisha kuchukua hatua sahihi? Kisa cha Henoko kiko mbele yetu. Mamia ya miaka alitembea na Mungu. Aliishi katika zama potovu, wakati uchafuzi wa maadili ulikuwa umejaa pande zote kumzunguka; lakini aliifundisha akili yake katika ibada, kujitoa wakfu, kupenda usafi. Mazungumzo yake yalikuwa juu ya vitu vya mbinguni. Aliielimisha akili yake kufuata mkondo huu, na alikuwa na fikra takatifu. Uso wake uliangaziwa nuru inayong'aa usoni mwa Yesu. Henoko alikuwa na majaribu vile vile kama sisi. Alizungukwa na jamii isiyopenda rafiki kwa haki, kuliko ile ambayo inatuzunguka sisi. Angahewa aliyovuta ilichafuliwa na dhambi na ufisadi, sawa na yetu; lakini aliishi maisha ya utakatifu. Hakuchafuliwa na dhambi zilizotawala katika zama aliyokuwa akiishi. Hivyo ndivyo nasi tunapaswa kubaki safi na bila kupotoka. Alikuwa mwakilishi wa watakatifu wanaoishi katikati ya hatari na upotovu wa siku za mwisho. Kwa sababu ya utii wake wenye uaminifu kwa Mungu, alitwaliwa. Kwa hivyo pia, waaminifu, walio hai na kusalia, watatwaliwa. Wataondolewa kutoka katika ulimwengu wenye dhambi na ufisadi kwenda katika furaha kamili ya mbinguni. {2Tsw 121.1}

Njia ya watu wa Mungu inapaswa kuwa ya kuelekea juu na kwenda mbele katika ushindi. Aliye mkuu kuliko Yoshua anayaongoza majeshi ya Israeli. Mmoja Yuko katikati yetu, tena ni Kiongozi Mkuu wa wokovu wetu, aliyesema kwa ajili ya kutiwa moyo kwetu: “Na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” “Jipe moyo na uwe na uchangamfu; nimeushinda ulimwengu.” Yeye Atatuongoza kwenye ushindi wa hakika. Kile Mungu anachoahidi, Anaweza wakati wowote kukifanya. Na kazi anayowapa watu Wake kuifanya, Yeye



Anaweza kuitimiza kwa wao. Tukiishi katika maisha ya utii mkamilifu, ahadi Zake zitatimizwa kwetu. {2Tsw 122.1}

Mungu anataka watu Wake waangaze kama nuru katika ulimwengu. Sio wahubiri tu wanaohitajika kufanya hivi, lakini kila mwanafunzi wa Kristo. Mazungumzo yao yanapaswa kuwa ya kimbingu. Na wanapofurahia ushirika na Mungu watatamani kuwa na ushirikiano na wanadamu wenzao ili kuonesha kwa maneno yao na vitendo, upendo wa Mungu ambao huhuisha mioyo yao. Kwa njia hii watakuwa nuru katika ulimwengu, na nuru inayopitishwa kwao haitazimika au kuondolewa. Kwa hakika itakuwa giza kwa wale ambao hawatatembea ndani yake, lakini itaangaza kwa mwangaza unaoongezeka katika njia ya wale watakaotii na kutembea katika nuru. {2Tsw 122.2}

Roho, hekima, na wema wa Mungu, unaofunuliwa katika Neno Lake, vinapaswa kudhihirishwa na wanafunzi wa Kristo, na hivyo kuuhukumu au kuusadikisha ulimwengu. Mungu anawajibisha watu Wake kulingana na neema na Kweli waliyopewa. Madai Yake yote ya haki lazima yatimizwe kikamilifu. Viumbe wanaowajibika lazima watembea katika nuru inayowaangazia. Wakishindwa kufanya hivi, nuru yao inakuwa giza, na giza lao ni kubwa kwa kiwango sawa na mwanga wao ulivyokuwa mwingi. Nuru iliyokusanywa imeangaza kwa watu wa Mungu; lakini wengi wamepuuza kuifuata nuru, na kwa sababu hii wako katika hali ya udhaifu wa kiroho. {2Tsw 123.1}

Sio kwa kukosa maarifa kwamba watu wa Mungu wanaangamia sasa. Hawatahukumiwa kwa sababu hawajui Njia, Kweli na Uzima. Ukweli uliufikia uelewa wao, nuru iliyoangaza katika roho, lakini ambayo imepuuzwa au kukataliwa, itawahukumu. Wale ambao kamwe hawakuwa na nuru ya kukataa hawatakuwa katika hukumu. Nini zaidi kingefanyika basi kwa shamba la mizabibu la Mungu kuliko kilichofanyika? Nuru, nuru ya thamani, inaangaza kwa watu wa Mungu; lakini haitawaokoa isipokuwa wamekubali kuokolewa nayo, kuiishi kulingana nayo kikamilifu, na kuisambaza kwa wengine walio gizani. Mungu anatoa wito kwa watu Wake kuchukua hatua. Ni kazi ya mtu binafsi ya kuungama na kuacha dhambi na kumrudia Bwana inayohitajika. Mtu hawezi kufanya kazi hii kwa ajili ya mwingine.

Maarifa ya kidini/kiroho yameongezeka, na hii imeongeza majukumu yanayolingana. Nuru kubwa imekuwa ikiangaza katika kanisa, na kwa hiyo wanahukumiwa kwa sababu wanakataa kutembea ndani yake. Ikiwa wangukuwa vipofu wangukuwa bila dhambi. Lakini wameiona nuru na wamesikia Ukweli mwingi, lakini sio wenye busara na watakatifu. Wengi kwa miaka mingi hawajapiga hatua katika maarifa na utakatifu wa kweli. Wao ni wadumavu wa kiroho. Badala ya kwenda mbele katika ukamilifu, wanarudi nyuma katika giza na utumwa wa Misri. Akili zao hazizoezwi katika utauwa na utakatifu wa kweli. {2Tsw 123.2}

Je, Israeli wa Mungu wataamka? Je, wale wote wanaodai utauwa watatafuta kuondoa kila kosa, kuungama kwa Mungu kila dhambi ya siri, na kuitesa nafsi mbele Yake? Je, watachunguza makusudi ya kila tendo kwa unyenyekevu mkubwa, na kujua kwamba jicho la Mungu linasoma mambo yote, na huchunguza kila kitu kilichofichika? Hebu kazi na iwe kamili, kujiweka wakfu kwa Mungu kuwe kamili. Yeye Anatoa wito wa kusalimisha kikamilifu yote tuliyo nayo na tulivyo. Wachungaji na walei wanahitaji uongofu mpya, mabadiliko ya akili, ambao bila kuwa nayo, sisi sio harufu ya uzima iletayo uzimani, bali ya mauti iletayo mauti. Watu wa Mungu wana upendeleo mkubwa. Wamepewa nuru kubwa, ili waweze kufikia wito wao wa mkuu katika Kristo Yesu; lakini bado hawako vile Mungu angependa wawe na vile anavyopanga watakavyokuwa \*(Wahubiri na washiriki).-{2Tsw 124.1}

## SURA YA 17

### KUJITENGA NA ULIMWENGU

Wapendwa Ndugu na Dada: Mungu alipanga kwamba nuru ya kanisa iweze kuongezeka na kung'aa zaidi hata kufikia siku ile kamilifu. Ahadi za thamani zinatolewa kwa watu wa Mungu kwa sharti la utii. Ikiwa, kama vile Kalebu na Yoshua, mngemfuata Bwana kabisa, Yeye angekuza nguvu Zake katikati yenu. Wenye dhambi wangeongolewa, na waliorudi nyuma wangerudishwa, kwa mvuto wenu; na hata maadui

wa imani yetu, ingawa wangeweza kupinga na kusema kinyume cha ile Kweli, wangeweza kukubali tu kwamba Mungu alikuwa pamoja nanyi. {2Tsw 124.2}

Wengi wa watu wa pekee, wanaomkiri Mungu, wamefuatisha namna ya dunia hata tabia yao ya pekee haitambuliwi, na ni vigumu kutofautisha “kati ya yeye amtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia.” Mungu angefanya mambo makubwa kwa watu Wake ikiwa wangetoka ulimwenguni na kujitenga nao. Ikiwa wangejinyenyekeza kuongozwa na Yeye, Angewafanya kuwa sifa katika dunia yote. Anasema Shahidi wa Kweli: “Nayajua matendo yako.” Malaika wa Mungu wanaowahudumia wale watakaokuwa warithi wa wokovu wanafahamu hali ya wote na wanaelewa kipimo tu cha imani aliyo nayo kila mtu mmoja-mmoja. Kutokuamini, kiburi, tamaa, na kuupenda ulimwengu, vilivyodumu katika mioyo ya watu wanaomkiri Mungu, vimewahuzunisha malaika wasio na dhambi. Malaika hawa wameziona hizo dhambi za kujivuna zikidumu katika mioyo ya wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, na kwamba Mungu hakuheshimiwa kwa mwenendo wao usiofaa, na uliopinda-inda (uovu), na hii imesababishwa wao kulia. Na bado wale wengi wenye makosa zaidi, wale wanaosababisha udhaifu mkubwa katika kanisa na kuleta doa katika imani takatifu, hawaonekani kutahadharishwa au kusadikishwa, lakini wanaonekana kuhisi kuwa wanastawi katika Bwana. {2Tsw 125.1}

Wengi wanaamini kuwa wako juu ya msingi sahihi, kwamba wanayo ile Kweli; wanafurahia uwazi wake na kujivunia hoja zenye nguvu katika uthibitisho wa usahihi wa msimamo wetu. Watu kama hao wanajihesabu kuwa miongoni mwa wateule, watu wa pekee wa Mungu, lakini hawana uzoefu wa uwepo Wake na nguvu kuwaokoa kutokana na kushindwa na majaribu na upumbavu. Hawa wanakiri kumjua Mungu, walakini kwa matendo wanamkana. Giza lao ni kubwa jinsi gani! Kuupenda ulimwengu na wengi, udanganyifu wa utajiri na wengine, vimelisonga Neno, nao wamekuwa wasiozaa matunda. {2Tsw 125.2}

Nilioneshwa kuwa kanisa huko ----- Limeshiriki roho ya ulimwengu na kuwa vuguvugu kwa kiwango cha kutisha. Wakati juhudi zinapofanywa ili kutengeneza mambo katika kanisa na kuwafikisha watu katika nafasi ambayo Mungu angewataka wawe nayo, daraja fulani

litaathiriwa na kazi hiyo, na litafanya juhudi za dhati za kupita katika giza kuingia kwenye nuru. Lakini wengi hawastahimili katika juhudi zao kwa muda mrefu wa kutosha kutambua mvuto utakasao wa Kweli katika mioyo na maisha yao. Masumbufu ya maisha haya yanashughulisha akili kwa kiwango hicho kwamba kujichunguza binafsi na maombi ya siri vinapuuzwa. Silaha imewekwa kando na Shetani anawafikia kwa uhuru, akigandisha utambuzi wao na kuwafanya wasishuku hila zake. {2Tsw 126.1}

Wengine hawaoneshi hamu ya kujua hali yao ya kweli na kuponyoka kutoka katika mitego ya Shetani. Wao ni wagonjwa, wanakufa. Mara kwa mara wanatiwa joto kwa moto la wengine, lakini karibu watiwe ubaridi na desturi, kiburi, urasmi, mapokeo na mvuto wa ulimwengu kiasi kwamba hawana utambuzi wa kuhitaji kwao msaada. {2Tsw 126.2}

Kuna wengi ambao wana upungufu wa kiroho na hisani za Kikristo. Uzito wa wajibu mzito unapaswa kuwa juu yao kila siku wanapoziona nyakati za hatari ambazo tunazoishi na mivuto mibaya inayotuzunguka. Tumaini lao pekee la kuwa washirika wa asili ya mbingu/Mungu ni kuukimbia ufisadi uliopo ulimwenguni. Ndugu hawa wanahitaji uzoefu wa kina na kamili katika mambo ya Mungu, na hili linaweza kupatikana tu kwa juhudi katika upande wao. Msimamo wao unawataka wawe na bidii na juhudi ya kudumu, ili wasipatikane wamelala katika lindo lao. Shetani na malaika zake hawalali. {2Tsw 126.3}

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa vyombo vya haki, watendakazi, mawe yaliyo hai, wakitoa nuru, ili kwamba waweze kuhimiza uwepo wa malaika wa mbinguni. Wanahitajika kuwa mifereji, kama ilivyokuwa, ambayo kupitia hiyo roho ya Kweli na haki itatiririka. Wengi wameshiriki kwa kiasi kikubwa roho na mvuto wa ulimwengu hata wanatenda kama ulimwengu. Wana mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda, na hawatambui ubora wa tabia. Mwenendo wao hautawaliwi na kanuni safi za Ukristo; kwa hivyo wanajifikiria wao tu, anasa na raha zao, kwa kuwapuza wengine. Hawajatakaswa kwa ile Kweli, kwa hivyo hawautambui umoja wa wafuasi wa Kristo ulimwenguni kote. Wale wanaopendwa sana na Mungu ni wale wenye ujasiri binafsi kidogo na

wamepambwa kwa roho ya upole na utulivu; ambao maisha yao ni safi na pasipo ubinafsi, na ambao mioyo yao imeelekezwa, kwa njia ya wingi wa roho ya Kristo, katika utii, haki, usafi, na utakatifu wa kweli. {2Tsw 126.4}

Ikiwa wote walikuwa wamejitolea kwa Mungu, nuru ya thamani ingeangaza kutoka kwao, ambayo ingekuwa na mvuto wa moja kwa moja kwa wote wanaokutana nao. Lakini wote wanahitaji kazi ifanywe kwa ajili yao. Baadhi wako mbali na Mungu, wakibadilika na pasipo uimara kama maji; hawatambui kafara. Wanapotaka upendeleo maalum au anasa, au mtindo wa wote wa mavazi, hawafikirii kama wanaweza au la kuishi bila mtindo huo, au kujinyima hiyo anasa, na kutoa sadaka ya hiari kwa Mungu. Ni wangapi wamefikiria kuwa walikuwa wanahitajika kutoa kafara fulani? Ingawa inaweza kuwa ya thamani ya chini kuliko ile ya tajiri ambaye anamiliki maelfu yake, lakini hiyo inayogharimu kujikana nafsi itakuwa kafara ya thamani, sadaka kwa Mungu. Ingekuwa harufu ya manukato ya kunukia, na kutoka katika madhabahu Yake kama ubani mzuri. {2Tsw 127.1}

Vijana hawaruhusiwi kufanya watakavyo na mali zao, bila kujali matakwa ya Mungu. Pamoja na Daudi wanapaswa kusema: “Wala sitamtotea Bwana, Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa nisizogharimia/zisizonigharimu.” Kiasi cha mali za kubwa kimetumika kuzalisha nakala za picha zao, kama wote wangeweza kuhesabu kiasi cha pesa alichopewa msanii kwa kusudi hili, kingekuwa kiasi kikubwa sana. Na hii ni njia moja tu ambayo mali inatapanywa ovyo, inawekezwa kwa kujifurahisha nafsi, ambayo hakuna faida inayopatikana. Kwa matumizi haya, hawavalishi wala kulisha mjane na yatima hawafarijiwi, wenye njaa hawalishwi, walio uchi hawalishwi. {2Tsw 127.2}

Wakati pesa zinatumiwa kwa kujipendeyesha katika kufurahisha nafsi, sadaka kidogo sana huletwa kwa Mungu karibia kwa moyo usio mkunjufu. Kiasi gani cha mshahara wanaoupata vijana hupelekwa katika hazina ya Mungu ili kusaidia maendeleo ya kazi ya kuokoa roho? Wanatoa kidogo kila wiki na kuhisi kuwa wanafanya kikubwa. Lakini hawatambui kwamba wao ni mawakili tu wa Mungu kwa kidogo

walichonacho kama walivyo matajiri katika mali zao nyingi. Mungu ameibiwa na wao wameendekeza matakwa yao, anasa zao zilishauriwa, ladha yao iliridhishwa, bila kufikiria kwamba Yeye Atafanya uchunguzi wa karibu wa jinsi walivyotumia mali Zake. Wakati hao bila kusita wanafurahisha yanayodhaniwa kuwa matakwa yao na kumzuilia Mungu sadaka wanazopaswa kutoa, Yeye hatakubali tena sadaka kidogo kuliko inavyostahili wanazopeleka kwenye hazina kuliko alivyokubali matoleo ya Anania na mkewe Safira, ambao walikusudia kumwibia katika sadaka zao. {2Tsw 128.1}

Kama jambo la jumla, vijana walio kati yetu wameungana na ulimwengu. Lakini ni wachache wanaodumisha vita maalumu dhidi ya adui wa ndani, wachache sana wana shauku ya kina, ya kutaka sana kujua na kufanya mapenzi ya Mungu. Lakini ni wachache wenye njaa na kiu ya haki, na ni wachache wanaojua chochote kuhusiana na Roho wa Mungu kama mkaripiaji au mfariji. Wamishenari wako wapi? Wako wapi wenye kujikana nafsi, wenye kujitoa kafara? Wako wapi wabeba msalaba? Ubinafsi na masilahi binafsi yamemeza kanuni za juu na bora. Mambo ya umilele yanachukuliwa bila uzito wa pekee katika akili. Mungu anahitaji kila mmoja wao kufikia hatua ya kujisalimisha kabisa. "Hamwezi kumtumikia Mungu na mali." Hamwezi kutumikia nafsi na wakati uo huo kuwa watumishi wa Kristo. Ni lazima kuifia nafsi, kufia kupenda anasa zenu, na kujifunza kuuliza: Je, Mungu atapendezwa na vitu ambayo ninakusudia kutumia mali hii? Je, nitamtukuza Bwana? {2Tsw 128.2}

Tumeamriwa, tulapo, au tunywapo, au tutendapo neno lolote, kufanya yote kwa utukufu wa Mungu. Ni wangapi ambao kwa makini wamesukumwa kwa kanuni badala ya mhemko, na kuitii amri hii kabisa? Ni wanafunzi wangapi vijana huko---- wamemfanya Mungu kuwa tumaini lao na fungu lao, na kwa dhati na bidii wametafuta kujua na kufanya mapenzi Yake? Kuna wengi ambao ni watumishi wa Kristo kwa jina, lakini hawako hivyo katika matendo. Ambapo kanuni za kidini zinatawala, hatari ya kufanya makosa makubwa ni ndogo; kwani ubinafsi, ambao daima hupofusha na kudanganya, unakanyagwa chini. Shauku ya dhati ya kuwatendea wema wengine hutawala kiasi kwamba nafsi inasahaulika. Kuwa na kanuni thabiti za kidini ni hazina isiyoweza

kukadiriwa. Ni mvuto safi zaidi, wa juu zaidi, ulioinuliwa ambao wanadamu wanaokufa wanaweza kuwa nao. Watu wa namna hiyo wana nanga. Kila tendo linazingatiwa vizuri, ili athari yake isije ikawa mbaya kwa mwingine na kuongoza mbali na Kristo. Swali la kudumu la akili ni: Bwana, kwa namna gani nitakutumikia vizuri, na kulitukuza Jina Lako duniani? Je, nitayaendeshaje maisha yangu ili kulifanya Jina lako liwe sifa duniani, na kuwaongoza wengine kukupenda, kukutumikia, na kukuheshimu? Hebu nitamani na kuchagua mapenzi yako tu. Hebu Maneno na mfano wa Mkombozi wangu viwe mwanga na nguvu ya moyo wangu. Ninapomfuata na kumtumainia Bwana, Hataniacha nipotee. Yeye Atakuwa taji yangu ya shangwe. {2Tsw 129.1}

Kama tukikosea tukachukua hekima ya kibinadamu badala ya hekima ya MUNGU tumepotoshwa kwa upuuzi wa hekima ya mwanadamu. Hapa kuna hatari kubwa kwa walio ndani Yake.... Hawana uzoefu kwa ajili yao binafsi. Hawajawa katika tabia ya maombi wakifikiri kwa ajili yao wenyewe, kwa hukumu yenye usawa, isiyobagua, kwa maswali na mada ambazo ni mpya na ambazo mara zote hujitokeza. Wanasubiri kuona kile wengine watafikiri. Kama utata huu, ndiyo yote inayohitajika kuwashawishi kwamba mada inayofikiriwa haina maelezo kabisa. Ingawa daraja hili ni kubwa, haibadilishi ukweli kwamba hawana uzoefu na wana akili dhaifu kupitia kujirahisi kwa muda mrefu kwa adui, na wakati wote watakuwa wasiojiweza, kama watoto, wakitembelea nuru ya wengine, wakiishi kwa uzoefu wa wengine, wakihihi kama wengine wahisivyo, na kufanya kama wengine wafanyavyo. Wanafanya kama vile hawana upekee wao binafsi. Utambulisho wao umezamishwa ndani ya wengine; ni vivuli tu vya wale wanaowadhani wako sahihi. Isipokuwa wameamka kutoka katika tabia yao ya kuyumbayumba na kuisahihisha, wote wataanguka kutoka uzima wa milele; hawataweza kukabili hatari za siku za mwisho. Hawatakuwa na nguvu ya kumpinga Shetani, kwa kuwa hawajui kuwa ndiye mwenyewe. Mtu lazima awepo pembeni yao kuwajulisha kwamba ni adui au rafiki anakuja. Siyo wa kiroho, kwa hiyo mambo ya kiroho hayatambuliwi. Hawana hekima katika mambo yale yalusuyo ufalme wa MUNGU. Wadogo na hata wakubwa hawana udhuru katika kumwamini mwingine kuwa na uzoefu kwa ajili yao. Malaika akasema, "Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, na kumfanya

kiumbe kuwa ngao na tegemeo lake.” Thamani ya kujitegemea inahitajika katika uzoefu wa Kikristo na pambano. {2Tsw 129.2}

Wanaume, wanawake, na vijana, MUNGU anawataka ninyi kuwa na uadilifu wa kishujaa, uimara wa malengo, ustahimilivu na uvumilivu, akili ambazo hazitabeba maoni ya wengine, bali ambazo zitachunguza zenyewe kabla ya kupokea au kukataa, kwamba zitajifunza na kupima ushahidi, na kwa maombi kupeleka kwa BWANA. “Kama mmoja wenu anapungukiwa hekima, aombe kwa MUNGU, ambaye hutoa kwa watu wote kwa ukarimu na wala hakemei naye atapewa. “Sasa, hili ndiyo sharti: lakini aombe kwa Imani, asitilie shaka, maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa BWANA”. Hili hitaji la hekima isiwe ombi lisilo na maana, likipotea akilini mara tu limalizikapo. Ni ombi ambalo huonesha hitaji madhubuti la ndani ya moyo, linaloibuka kutoka utambuzi wa kupungukiwa hekima kupambanua mapenzi ya MUNGU. {2Tsw 130.1}

Baada ya kufanywa ombi, kama jibu halijapatikana haraka, usichoke kusubiri na kutokuwa imara. Usitie shaka, shikilia ahadi, “Mwaminifu ni Yule akuitaye wewe, Yeye ambaye pia atafanya hivyo.” Kama mjane asiyekata tamaa, himiza hitaji lako, kuwa kidete katika lengo lako. Je, ni kitu muhimu na cha matokeo makubwa kwako? Hakika ndivyo. Basi usitie shaka, kwa Imani yako kuweza kujaribiwa. Kama jambo unalohitji ni la thamani, inastahili ukakamavu na bidii ya kazi. Unayo ahadi, kesho na omba. Kuwa imara na ombi litajibiwa; Je, si MUNGU aliyeahidi? Kama Ikikugharimu kitu kukipata utakithamini zaidi ukipatapo. Umeambiwa wazi kwamba ukitilia shaka uhitaji kufikiri kwamba utapata kitu chochote toka kwa BWANA. Angalizo limetolewa hapa ili usijechoka, bali kubaki imara juu ya ahadi. Kama ukiomba, Yeye atakupatia kwa ukarimu na hakemei. {2Tsw 131.1}

Hapa ndipo wengi hufanya kosa. Wanashaka katika lengo lao, na Imani yao hushindwa. Hii ndiyo sababu hawapokei kitutoka kwa BWANA, ambaye ni Chanzo cha nguvu zetu. Hakuna anayehitaji kwenda gizani, akijikwaa kama kipofu; maana BWANA ametoa nuru kama wataikubali katika namna aitoavyo, na siyo kuchagua njia zao wenyewe. Yeye



Anataka bidii katika kufanya wajibu wa kila siku. Hii inahitajika hasa kwa wale wote wanaojihusisha katika kazi pekee, muhimu katika ofisi ya uchapishaji, kwa wote wale ambao juu yao kuna jukumu zito la kazi na wale ambao wanabeba majukumu madogo. Hili linaweza kufanywa kwa kumtafuta MUNGU pekee kuwawezesha kwa uaminifu kufanya lililo sahihi machoni pa mbingu, kufanya mambo yote kwa jinsi ya kuongozwa bila malengo ya ubinafsi, kana kwamba jicho la MUNGU linaonekana kwa wote likiangalia juu ya wote na kuchunguza matendo ya wote. {2Tsw 131.2}

Dhambi ambayo imeharibu kwa kiasi kikubwa, na ambayo inatutenganisha na MUNGU na kuzalisha madhara ya kiroho mengi sana, ni ubinafsi. Hakutakuwa na kumrudia BWANA isipokuwa kwa kujikana nafsi. Peke yetu hatuwezi kitu, lakini, kwa kupitia MUNGU atuwezeshaye, tunaweza kuishi kutenda mema kwa wengine, na kwa njia hii kufukuza uovu wa ubinafsi. Hatuhitaji kwenda nchi za mbali kuonesha nia yetu ya kutoa yote kwa MUNGU katika kuishi maisha yenye manufaa na yasiyo na ubinafsi. Lazima tufanye haya katika mduara wa nyumbani, kanisani miongoni mwa wale tunaohusiana na tunaofanya nao kazi pamoja. Pale palipo na shughuli za kila siku za maisha, ndipo pa kujikana nafsi na kuwekwa katika unyenyekevu. Paulo angesema “nakufa kila siku”. Ni kufa kwa nafsi kila siku katika mambo madogo-madogo ya maisha ambako hutufanya kuwa washindi. Ni lazima tuisahau nafsi katika kutamani kufanya wema kwa wengine. Kwa walio wengi kuna kusudio la upungufu wa upendo kwa wengine. Badala ya uaminifu kutenda wajibu wao, wanatafuta zaidi furaha yao binafsi. {2Tsw 132.1}

MUNGU kwa hakika anaagiza juu ya wafuasi Wake wajibu wa kuwabariki wengine kwa ushawishi wao na vitu vyao, na kuitafuta ile hekima ya Bwana/mbingu ambayo itawawezesha kufanya yote katika uwezo wao kuinua mawazo na hisia za upendo kwa wale wanaokutana nao. Kwa kufanya kwa ajili yawengine, utamu wa kuridhika utapatikana, amani ya ndani ambayo itakuwa zawadi kamilifu. Wakati itakapoamshwa kwa hitaji la juu na heshima kuwafanyia wengine wema, watapata furaha ya kweli katika kufanya kwa uaminifu wajibu mbalimbali wa maisha. Hii huleta zaidi ya zawadi ya kidunia; kwa kila

mwaminifu, utendaji wa wajibu bila ubinafsi unatazamwa na malaika na unang'aa katika kumbukumbu za maisha. Mbinguni hakuna atakayejikiria nafsi yake tu, wala kutafuta furaha yao pekee; lakini wote, kwa usafi (umimi hamna), upendo wa Kweli watatafuta furaha ya viumbe wa mbinguni wanao walio pote karibu yao. Kama tunatamani kufurahia jamii ya mbinguni katika dunia iliyofanywa mpya, lazima tuwe tunaongozwa kwa kanuni za kimbingu hapa. {2Tsw 132.2}

Kila tendo la maisha yetu linaathiri kwa wema ama ubaya. Mvuto wetu unatuongoza juu ama chini; unahisiwa, unafanyiwa kazi, na kwa kiwango cha juu au chini, unazalishwa na wengine. Kama kwa mfano wetu tunawasaidia wengine katika kuendeleza kanuni njema, tunawapa nguvu ya kutenda wema. Na matokeo yake wanaendeleza jitihada ile ile kusaidia kushawishi juu ya wengine, na hivyo mamia na maelfu wanaathiriwa kwa ushawishi wetu bila sisi kujua. Kama sisi kwa matendo tunaimarisha au kusukuma katika utendaji nguvu za uovu zilizoshikiliwa na wale wanaotuzunguka, tunashiriki dhambi yao, na tutatoa hesabu kwa wema ambao tungeweza kuufanya kwao na hatukuufanya, kwa sababu hatukumfanya MUNGU nguvu yetu, kiongozi wetu, na mshauri wetu. {2Tsw 133.1}

## **SURA YA 18**

### **UPENDO WA KWELI**

Upendo wa kweli siyo shauku ya pupa/haraka yenye nguvu inayowaka, yenye harara. Kinyume chake, ni tulivu na yenye kina kirefu kwa asili yake. Huangalia mbali zaidi ya vitu vidogo vya nje na huvutiwa na ubora pekee. Una hekima, huchagua, na kujitoa kwake ni dhahiri na kudumu. MUNGU hutahini na kututhibitisha kwa matukio ya kawaida ya maisha. Ni vitu vidogo vinavyodhihirisha kurasa za moyo. Ni kwa kutilia makini vilivyo vidogo-vidogo, matukio madogo mbalimbali, kujalina na wema katika mambo ya kawaida ya maisha, ndiyo ambako huleta jumla ya maisha ya furaha; Na ni kwa kupuuzia kutia moyo, kutoa maneno ya upendo na kujali wengine katika maisha ndiyo sababu ya huzuni kubwa. Itafahamika mwishoni kuwa kujikana nafsi kwa wema na furaha ya

wale wanaotuzunguka itatengeneza mchango mkubwa wa kumbukumbu mbinguni. Na Ukweli utafunuliwa kuwa kujipenda nafsi bila kujali wema na furaha ya wengine, ipo kwenye uoni wa BABA yetu wa mbinguni. {2Tsw 133.2}

Ndugu B, BWANA anatenda kwa ajili yako, na Yeye atakubariki na kukuimarisha wewe katika njia ya haki. Unaelewa dhana ya Ukweli, na lazima ujipatie ufahamu wote wa mapenzi ya MUNGU na kazi Yake kadri uwezavyo, ili uandaliwe kujaza nafasi ya wajibu wa juu zaidi kama atakuona unaweza kulitukuza Jina Lake vyema zaidi kwa hivyo ufanyavyo. Lazima atake kwako. Lakini hata sasa bado unahitaji kujipatia uzoefu. Una maamuzi ya haraka sana, unaathiriwa kirahisi sana na mazingira. MUNGU anataka kukutegemeza, kukuimarisha, kukutuliza, kwa dhati na unyenyekevu, kama utatafuta hekima Yake Yeye asiyekosea, na ameahidi kuwa ukitafula unapata. {2Tsw 134.1}

Katika kufundisha Ukweli kwa wengine, upo katika hatari ya kuongea kwa kujiamini na kushinikiza kwa nguvu sana, katika namna isiyojali uzoefu wako mdogo. Unaangalia mambo kidogo tu, na una karama ya kupata masomo yote tayari. Sio wote wameumbwa na kuratibiwa kama ulivyo, na hawawezi kufanya hivi. Hutakuwa umeandaliwa kwa subira, kwa upole na utulivu wao, nao wapime ushahidi wale wasioona kwa utayari kama wewe. Utakuwa kwenye hatari ya kuhimiza wengine, kuona mengi mara moja kama uonavyo na kuhisi bidii yote hiyo na ulazima iwe katika hatua ya jinsi unavyohisi. Kama matarajio yako hayajafahamika, upo katika hatari ya kukatishwa tamaa na kutotulia, na kutamani mabadiliko. Lazima uepuke tabia ya kukosoa, jitahidi kuvumilia. Kuwa makini kwa kila kitu kinachoashiria roho ya kuhukumu. Haimpendezi MUNGU kwa roho ya namna hii kuwa ndani ya mtumishi Wake mwenye uzoefu wa muda mrefu. Ni vizuri kwa kijana, kama amebarikiwa unyenyekevu na uzuri wa ndani, kudhihirisha shauku na ari, lakini usongo mihemko na pupa na roho ya kuhukumu vinapooneshwa na kijana ambaye ana miaka michache tu ya uzoefu, haifai kabisa na inachukiza sana. Hakuna kinachoweza kuharibu ushawishi wake haraka sana kama tabia hii. Utulivu, upole, uvumilivu, saburi, kutokukasirishwa mapema, akichukuliana na mambo yote, akitumaini yote, akistahimili yote haya ni matunda yanayokua juu ya

mti wa thamani wa upendo, ambao ni wa ukuaji wa kimbingu. Mti huu ikiwa utatunzwa, utathibitika kuwa wa kijani kibichi wakati wote. Matawi yake hayataoza, majani yake hayatanyauka. Ni wa asili ya kutokufa, wa milele, ukimwagiliwa mara kwa mara na umande wa mbinguni. {2Tsw 134.2}

Upendo ni nguvu. Akili na nguvu ya maadili vinahusishwa katika kanuni hii, na haviwezi kuachanishwa kutoka humo. Nguvu ya utajiri ina tabia ya kupotosha na kuharibu; nguvu ya kulazimisha ni ina nguvu na huumiza; lakini ubora na thamani ya pendo safi ujumuishwa katika ufanisi wa kutenda mema, na kutokufanya kingine chochote zaidi ya wema. Chochote kifanywacho kwa matokeo ya pendo safi kiwe wakati wote kidogo au kudharauliwa machoni mwa wanadamu ni faida yenye matokeo kamili; maana MUNGU anaheshimu zaidi ni kwa upendo kiasi gani mtu amefanya, kuliko ukubwa aliofanya. Pendo ni la MUNGU. Moyo ambao haujaoongoka hauwezi kuwa chimbuko ama kuzalisha mmea huu ukuzwao kimbingu, ambao unaishi na kustawi mahali tu ambapo KRISTO anatawala. {2Tsw 135.1}

Upendo hauwezi kuishi pasipo matendo, na kila tendo huongeza, huimarisha na kuukuza. Upendo utapata ushindi wakati malumbano na mamlaka vinapokosa nguvu. Upendo hufanya kazi siyo kwa faida wala malipo; hata bado MUNGU amepanga kwamba faida kubwa itakuwa matokeo ya hakika ya kila kazi ya upendo. Ni wenye kuenea kwa asili yake na kimya katika utendaji wake, huku ni imara, mkuu na wenye nguvu katika kusudi lake katika kushinda maovu makubwa. Unayeyusha na kubadilisha katika kuhusika kwake, na Utakamata maisha ya wadhambi na kuathiri mioyo yao wakati ambapo nyenzo zingine zimethibitika kutokufanikiwa. Mahali popote nguvu ya elimu, mamlaka, au shinikizo inapotumiwa, na upendo hauonekani kuwepo, mapenzi na nia ya wale ambao tunatafuta kuwafikia huchukuwa hatua ya kujihami, kujibu, na nguvu yao ya kuzuia inaongezeka. YESU alikuwa mfalme wa amani. Alikuwa ulimwenguni kuleta upinzani na mamlaka kujisalimisha Kwake. Hekima na nguvu angeweza kuziamrisha, lakini nyenzo alizotumia kushinda uovu zilikuwa ni hekima na nguvu za upendo. Usijisumbue kugawanya maslahi yako kutoka kazi yako ya sasa mpaka MUNGU atakapoona nafaa kukupa kipande kingine cha

kazi katika eneo lilelile la kazi. Usitafute kwa ajili ya furaha yako mwenyewe, kwa maana kamwe haipatikani kwa kuitafuta. Songa katika wajibu wako. Acha uaminifu uweke alama yote uyafanyayo, na uvikwe unyenyekevu. (2Tsw 135.2)

“Yoyote mtakayo watu wawatendee, nanyi tendeni hayo hayo kwao”. Matokeo ya baraka yataonekana kama matunda ya kazi hiyo. “Kwa kipimo kile mpimiacho, nanyi mtapimiwa” hapa kuna nia zenye nguvu ambazo lazima zitubidishe kupendana kwa moyo safi, kwa bidii. KRISTO ni kielelezo chetu, Yeye alizunguka akitenda mema. Aliishi kubariki wengine. Upendo ulipendezesha na kuongezea alama matendo Yake yote. Hatujaagizwa kujitendea nafsi zetu yale tunayotamani wengine wayatende kwetu; tunatakiwa kuwatendea wengine yale ambayo twatamani wao watutendee sisi chini ya mazingira yafananayo. Kipimo tupimiacho mara zote hupimwa tena kwetu. Upendo safi ni sahili katika utendaji wake, na ni tofauti kutoka kanuni zingine za utendaji. Upendo wa kugusa wengine na nia ya kuwajali wengine inaweza kuzalisha maisha mazuri yaliyopangiliwa vyema na mara kwa mara mazungumzo yasiyo na lawama. Kujiheshimu kutatuongoza kuepuka mwonekano wa uovu. Moyo mbinafsi unaweza kutenda matendo ya ukarimu, ukatambua Ukweli wa leo, na kuonesha unyenyekevu na upendo katika hali ya nje, huku nia yaweza kuwa danganyifu/feki na chafu; matendo yanayomiminika kutoka kwa moyo kama huo yanaweza kuwa na ukosefu wa ladha ya maisha na matunda ya utakatifu wa Kweli, na kuwa maskini wa kanuni za pendo safi. Upendo lazima uthaminiwe na kupaliliwa, maana matokeo yake ni ya Bwana Mwenyewe (Kimbingu). {2Tsw 136.1}

## **SURA YA 19**

### **VICHEKESHO KATIKA TAASISI (MABURUDISHO NA HATA VITU KAMA KATUNI-amusements)**

Wakati vichekesho vilipoingizwa katika taasisi, baadhi huko----- walionesha tabia yao ya hovyoyao na ya juu juu. Walikuwa wameridhishwa na kufurahishwa; fikra zao za kijinga zilizogeuka ziliwafaa wao tu. Vitu vilivyoshauriwa kwa wagonjwa waliolemaa waliona ni vyema kwa ajili yao; na Dkt. C. hawajibilki kwa matokeo yote yanayotokea kutoka kwa ushauri uliotolewa kwa wagonjwa wake. Wale walio katika makanisa mbalimbali nje ya nchi, ambao walikuwa hawajatakaswa, walitekwa juu ya sababu za kwanza za kujiingiza katika anasa, vicheko na upuuzi. Haraka ilipojulikana kwamba madaktari katika taasisi wamependekeza maigizo na vichekesho ili kuhamisha akili za wagonjwa kutoka katika hali zao na kisha kwenda katika kufundisha akili kwa raha zaidi, ilikwenda kama moto ndani ya mabua; wale waliokuwa wapya na makanisa mengine walifikiri kuwa walihitaji mambo kama hayo, na ngao ya haki iliachwa na wengi. Jinsi walivyokuwa wameacha kuongozwa kwa lijamu na hatamu, walijiingiza katika vitu hivi kwa kujitoa zaidi na uvumilivu kana kwamba uzima wa milele ulitegemea juu ya ari yao katika njia hii. Hapa ilikuwepo fursa ya kutambua kati ya wafuasi wa YESU waangalifu na wale ambao waliojidanganya nafsi zao. Baadhi hawakuwa na nia ya MUNGU moyoni. Hawakuwa na kazi ya

utakatifu wa kweli uliotengenezwa nafsini mwao. Walishindwa kumfanya MUNGU tumaini lao, na hawakuwa imara, na walihitaji tu wimbi kuwanyanyua toka katika miguu yao na kuwatupa huku na huku. Watu hawa walionesha kwamba walimiliki uimara kidogo tu na kujitegemea kimaadili. Hawakuwa na uzoefu wao binafsi, na kwa hiyo walitembea katika cheche za mioto/mianga ya wengine. Hawakuwa na KRISTO ndani ya mioyo yao kumkiri kwa ulimwengu. Walijitangaza kuwa wafuasi Wake, lakini vitu vya kidunia na vya muda mfupi viliwashikilia mioyo yao mijinga, na mibinafsi katika utumwa. {2Tsw 137.1}

Kulikuwa na wengine walionekana kutokuwa na wasiwasi juu ya kuzingatia swali la vichekesho na maburudisho. Walihisi kujiamini kwamba MUNGU atafanya yote kuwa sawa ili amani ya akili yao isisumbuliwe. Waliamua kwamba matibabu kwa wagonjwa hayakuwa kwa ajili yao, kwa hiyo wasingesumbuliwa. Chochote wengine katika kanisa ama ulimwengu wawezacho kufanya si kitu kwao; maana walisema, ni nani tumfuate isipokuwa KRISTO? Yeye Ametuachia amri tuenende kama Yeye alivyoenenda. Lazima tuishi kama tunamuona Yeye ambaye haonekani, na kufanya tukifanyacho kwa moyo, kama kwa MUNGU na si kwa wanadamu (2Tsw 138.1)

Wakati mambo kama hayo yanapotokea, tabia inakuzwa. Thamani ya maadili ndipo inapoweza kupimwa kwa kweli. Siyo vigumu kutambua mahali ambapo utawakuta wale wanaoshika utakatifu, huku wakiwa na raha yao na furaha katika ulimwengu huu. Upendo wao haupo juu ya vitu vya juu mbinguni, lakini juu ya vitu vya dunia, mahali Shetani anapomiliki. Wanatembea katika giza, na hawawezi kupenda na kufurahia vitu vya kimbingu kwa sababu hawawezi kuvitambua. Wametengwa kutoka katika maisha ya KRISTO, wakitiwa ufahamu wao giza. Vitu vya ROHO ni upuuzi kwao. Matamania na utendaji wao ni kulingana na njia ya ulimwengu huu. Kama hao wakiweza kuruhusu kuendelea kubeba Jina la KRISTO, huku wakingali wanamtumikia MUNGU na mashetani, wameridhika. Lakini mambo yatatokea kufunua mioyo ya hawa, ambao ni mzigo tu na laana kwa kanisa. {2Tsw 138.2}

Roho iliyopo kanisani ni ile ambayo huwaongoza watu mbali na Mungu na njia ya utakatifu. Wengi katika kanisa wamehusisha hali yao ya upofu wa kiroho na ushawishi unaotokana na kanuni zinazofundishwa katika Taasisi. Hili si sahihi kabisa. Kama kanisa lingesimama katika ushauri wa Mungu, Taasisi hiyo ingekuwa imedhibitiwa. Nuru ya kanisa ingekuwa imeenea kwenye tawi hilo la kazi, na makosa yasingekuwepo hapo. Ilikuwa ni giza la kimaadili la kanisa, ndilo ambalo lilikuwa na ushawishi mkubwa zaidi wa kuunda giza la kimaadili na kifo cha kiroho katika Taasisi hiyo. Kama kanisa lingekuwa katika hali nzuri ya afya, lingeweza kutuma mkondo wa uhai na afya kwenye mkono huu wa mwili. Lakini kanisa lilikuwa gonjwa na halikufurahia kibali cha Mungu wala nuru ya uso Wake. Ushawishi mgonjwa na wa kifo ulisambaa kote katika mwili ulio hai hadi ugonjwa ulipoonekana kila mahali. {2Tsw 138.3}

Daniel na wenzake walikuwa mateka katika nchi ya ugeni, lakini MUNGU hakuhuzunishwa na wivu na chuki za maadui zao kushinda dhidi yao. Wenye haki bila kikomo wameweza kupata msaada toka juu mbinguni. Ni mara mangapi maadui wa MUNGU wameunganisha nguvu zao na hekima kuharibu tabia na ushawishi wa watu wachache wa kawaida ambao walimwamini MUNGU. Lakini kwa sababu BWANA alikuwa upande wao, hakuna ambaye angeweza kushinda dhidi yao. Acha tu wafuasi wa KRISTO wawe wamoja na watashinda. Acha wajitenge na kutoka kwa sanamu zao na kutoka kwa ulimwengu, na ulimwengu hautawatenga wao kutoka kwa MUNGU. KRISTO ni Mwokozi wetu anayejitosheleza hasa wakati wote. Katika Yeye utimilifu wote unakaa. Ni upendeleo kwa Wakristo kujua kwa kweli kwamba Ukweli KRISTO Yu ndani yao. “Huu ni ushindi unashinda ulimwengu, hiyo Imani yetu.” mambo yote yanawezekana kwake aaminiye; mambo yoyote tuyatayo tukiomba, kama tukiamini kwamba tunapokea tutavipata. Imani hii itapenya wingu la giza totoro na kuleta miale ya nuru na matumaini kwa nafsi inayonyong’onyea na kukatatamaa. Ni kukosekana kwa Imani hii na tumaini ambavyo huleta kuchanganyikiwa, misongo ya mawazo na maono ya uovu. MUNGU atafanya mambo makubwa kwa watu Wake pale wanapoweka tumaini lao lote Kwake. “Utauwa na kuridhika ni faida kubwa.” Dini safi na isiyo na taka itaoneshwa katika maisha. KRISTO atathibitisha chanzo cha



nguvu isiyoshindwa, msaada ulio karibu wakati wote wa mateso.  
{2Tsw 139.2}

## **SURA YA 20**

### **KUPUUZIWA KWA HANNAH MORE**

Kuhusu dada Hannah More, nilioneshwa kwamba kumpuuza mama huyu ilikuwa ni kumpuuza KRISTO katika utu wake. Endapo MWANA wa MUNGU angekuja katika unyenyekevu, bila kujifanya, akisafiri mahali-mahali wakati alipokuwa juu ya dunia, hata naye asingekutana na mapokezi yaliyo mazuri. Kinachotakiwa ni kanuni ya kina cha ndani cha upendo, ambao Mtu Mnyenyekevu wa Kalvari, alikuwa nayo. Laiti kanisa lingemthamini huyu mmishenari mpole ambaye maisha yake yote yalikuwa yanaangazia kujihusisha katika huduma ya BWANA Wake. Shauku yake ya dhati ilieleweka vibaya. Mambo yake ya nje hayakuwa yale ambayo yangekidhi ukubali wa hamu ya macho na mitindo, kwani alizoea ukali wa uchumi mgumu na umaskini ulioacha mguso wake juu ya mavazi yake. Vitu vyake alivyovipata kwa shida vimekuwa vikichakazwa haraka, sambamba kama vilivyopatikana kwa kuwanufaisha wengine, kwamba wapate nuru, wale ambao alitumaini kuwaongoza kuelekea msalaba wa Kweli {2Tsw 140.1}

Hata kanisa la KRISTO lililotajwa, kwa vipaumbele vyao vya juu na mafanikio makubwa, hawakutambua sura ya KRISTO katika huyu Mwana wa MUNGU aliyejikana nafsi kwa sababu wao wenyewe walikuwa wameondolewa mbali na KRISTO, kiasi kwamba hawakuakisi sura Yake. Walihukumu kwa mwonekano wake wa nje na hawakuchukua juhudi maalum kutambua uzuri wa ndani. Hapa alikuwepo mwanamke ambaye vyanzo vyake vya ufahamu na uzoefu

wake halisi katika siri na mafumbo ya mambo ya utauwa ulizidi yeyote aliyekuwepo----- na ambaye namna ya ufundishaji wake kwa vijana na Watoto ulikuwa wa kupendanza na kuridhisha, wenye kufunza, kunufaisha na kujenga. Hakuwa mkali, lakini mtu sahihi na mwenye kujali, na angedhihirisha kuwa mmoja wa watendakazi wenye manufaa katika kitengo cha ukufunzi wa vijana na mwenye akili mahiri, rafiki wa manufaa, na mshauri mwenzi kwa kina mama. Angeweza kufikia mioyo kwa kujitoa kwake, kwa jambo la kuonesha matukio katika maisha yake ya dini, ambayo alikuwa amejitolea kwa huduma ya Mwokozi Wake. Ingekuwa kanisa limetokeza kutoka gizani na madanganyo, na kuingia ndani ya nuru halisi, mioyo yao ingevutwa kumwelekea mgeni huyu mpweke. Maombi yake, machozi yake, masumbuko yake, katika kutokuona njia ya manufaa wazi kwake, imeonekana na kusikika mbinguni. BWANA alitoa kwa watu Wake msaada uliobarikiwa na wenye vipaji, lakini walikuwa matajiri waliokuwa na ongezeko la vitu, na hawakuhitaji kitu. Watu waligeuka na kukataa baraka ya thamani, na ya juu zaidi ambayo bado wataendelea kuihitaji. Kama Mzee E angesimama katika nuru sahihi ya MUNGU na angekuwa amejazwa kwa ROHO Wake wakati ambapo huyu mtumishi wa YESU, na mpweke, asiye na makazi, na mwenye kuona kiu kwa ajili ya kufanya kazi kwa BWANA Wake, alipoletwa mbele yake, roho ingejibu roho, kama sura inavyojibu sura katika kioo, moyo wake ungekuwa umevutwa kumwelekea mwanafunzi wa KRISTO, na angemuelewa. Vivyo hivyo pia, kwa kanisa. Watu wamekuwa katika upofu wa kiroho wa namna hiyo, na wamepoteza sauti kamili ya mchungaji wa Kweli na walikuwa wakifuata sauti ya mgeni au mtu baki, ambaye alikuwa akiwaongoza kutoka katika uwepo wa KRISTO. {2Tsw 141.1}

Wengi hutazama juu ya kazi kubwa ya kukamilishwa kwa ajili ya watu wa MUNGU, na maombi yao huenda juu Kwake Bwana kwa msaada katika mavuno makubwa. Lakini, kama msaada hautakuja kwa namna wanavyotaraji, hawataupokea, bali watageuka toka Kwake kama taifa la Wayahudi walivyogeuka toka kwa YESU kwa sababu walikatishwa tamaa katika namna ya kutokea Kwake. Umaskini wa kupindukia na unyenyekevu uliandamana na ujio Wake, na katika kiburi chao walimkataa Yeye aliyekuja kuwapa uzima. Katika hili, MUNGU

angekuwa na kanisa ambalo limejinyenyekeza mioyo yao na kuona hitaji kubwa la kurekebisha njia zao mbele Zake. Asije kuwatembelea na hukumu. Wengi wanaokiri uchaji wa MUNGU, wanafanya kujipamba kwa nje kuwa muhimu zaidi, kuliko kujipamba kwa ndani. Ingekuwa kanisa zima limejinyenyekeza mbele za BWANA na kurekebisha makosa yao yaliyopita kikamilifu kabisa kama njia ya kukutana na mapenzi Yake, wasingekuwa wamepungukiwa katika kukadiria uwezo wa kimaadili wa tabia. {2Tsw 142.1}

Nuru ya dada Hannah More imepotea, ambapo ingeweza kuwa sasa inawaka kwa kung'aa, na kuangaza njia ya wengi ambao wanatembea katika njia za giza za makosa na uasi. MUNGU analiita kanisa Lake kuzinduka kutoka katika usingizi wao na kwa dhati kujiuliza matokeo ya huku kujidanganya kwao. Miongoni mwao ni wakufunzi ambao majina yao yapo kwenye vitabu vya kanisa. Shetani anawapotosha na kuwadanganya katika hofu kubwa ya wokovu. Hakuna kitu kinachohadaa zaidi kuliko udanganyifu wa dhambi. Ni muungu wa ulimwengu huu ambaye hupumbaza, hupofusha na kuongoza katika uharibifu. Shetani haji na lundo la majaribu yake kwa wakati mmoja. Hufunika haya majaribu kwa muonekano wa mema; huchanganya kidogo, baadhi ya maboresho kwa upuuzi na vichekesho na nafsi zilizodanganyika huimiza, kama sababu ya kujiingiza kwayo kwamba thamani kubwa itapatikana. Huu ni upande tu wa udanganyifu, Sanaa ya kuzimu ya Shetani imefunikwa. Nafsi zilizodanganywa zinapiga hatua moja, kisha zinajiandaa kwa nyingine. Ni vyema zaidi kufuata mwelekeo wa mioyo yao binafsi kuliko kusimama katika kujilinda na kupinga manong'onezo ya kwanza ya adui mwerevu, na hivyo kufungia nje biashara yake. Oh, ni kwa namna gani Shetani anakesha kuona chambo chake kimenaswa kwa urahisi na kuona nafsi zikitembea katika njia hasa aliyoandaa! Hataki waache kuomba na kudumisha aina ya wajibu wa kidini, kwa maana wafanyapo hili anaweza kuwafanya kutumika zaidi katika huduma yake. Hujumuisha ustadi na mitego midanganyifu kwa uzoefu wao na taaluma zao, na kwa hivyo kwa ajabu huendeleza kazi yake. Mafarisayo wanafiki waliomba na kufunga, na walishika aina ya utauwa huku wakiwa waovu moyoni. Shetani husimama ili kumdhihaki KRISTO na malaika Zake kwa matusi,

akisema: “Nimewapata! Nimewapata! Nimeandaa hila zangu kwa ajili yao. Damu Yako haina thamani hapa. Maombezi Yako na nguvu na matendo Yako ya ajabu hakika zaweza koma; Ninao kikapuni mwangu! Ni wangu! Hawastahimili ukiri wao kama watu wa KRISTO, hawahimili kwanza walifurahia mwangaza wa uwepo Wake, nitawatunza kwangu katika muonekano hasa wa mbingu, ambao wanauzungumzia. Ni masomo kama haya ambayo ninaweza kuyatumia ili kuwatega wengine.” {2Tsw 142.2}

Sulemani anasema, “yeye autumainiye moyo wake ni mjinga,” na wapo mamia wa namna hiyo ambao wanapatikana miongoni mwa wanaokiri utauwa. Anasema mtume, “sisi siyo wajinga wa hila zake.” Oh, Sanaa ya kushangaza kiasi gani, ujuzi gani, werevu gani, unaofanyika kuwaongoza wafuasi wa KRISTO waliokiri kuungana na ulimwengu kwa kutafuta furaha katika maburudisho ya ulimwengu, chini ya udanganyifu kuwa mazuri yatapatikana! Na hivyo watu wasiojilinda wanaingia kabisa katika nyavu, wakijidanganya wenyewe kwamba hakuna uovu njiani. Upendo na hisia za namna hiyo zinajengwa, na hii huweka msingi mwembamba ambao juu yake wanajenga imani yao kwamba wao ni wa watoto wa MUNGU. Wanajilinganisha na wengine na kutulia chini wameridhika kwamba wao ni bora zaidi ya Wakristo wengi wa Kweli. Lakini uko wapi upendo wa KRISTO wa dhati uking’aa wazi katika maisha yao, miali Yake angavu inabariki wengine? Biblia yao iko wapi? Na inasomwa kwa kiasi gani, mawazo yao yako wapi? Yapo juu ya mbingu na vitu vya mbinguni? Siyo asili kwa akili zao kwenda katika njia hiyo. Somo la Neno la MUNGU halivutii kwao. Halina kile ambacho kinawasisimua na kutamanisha akili, na moyo wa asili ambao haujazaliwa upya unapendelea vitabu vingine kuliko Neno la MUNGU. Umakini wao umemezwa katika ubinafsi. Hawana kina, na hitaji la dhati kwa ajili ya ushawishi wa ROHO wa MUNGU juu ya akili na moyo. MUNGU Hayupo katika mawazo yao yote. {2Tsw 143.1}

Nitawezaje kuvumilia wazo kwamba wengi wa vijana katika zama hizi watakosa uzima wa milele kwani watakuwa wamepungukiwa. Oh, kwamba mlio wa ala za muziki ungeweza kukoma na wasiwe tena wakikaa mbali na kutumia muda wa thamani katika kukidhi wayapendayo. Oh, kwamba wangetoa muda kidogo katika mavazi, na

mazungumzo yasiyo na faida, na kupeleka mbele maombi yao ya dhati ya kuugua kwa MUNGU kwa uzoefu bora.

Kuna ulazima mkubwa kwa ajili ya kujitathmini kwa ukaribu katika nuru ya Neno la MUNGU. Hebu kila mtu ajiulize: “Je nipo vizuri, au nimeoza moyoni? Je nimefanywa upya katika KRISTO, au bado ni muovu moyoni katika vazi jipya linalovaliwa kwa nje? “Jiunganishe mwenyewe mpaka katika mahakama kuu, na katika nuru ya MUNGU jichunguze kuona kama kuna dhambi ya siri ambayo unaithamini, sanamu (idol) yoyote ambayo bado hujaitoa. Omba, ndiyo, omba kama ambavyo hujawahi kuomba kabla, kwamba usije kudanganywa na mipango ya Shetani, kwamba usije kuhafifishwa na roho potovu, isiyozingatia, isiyojali, na kuhudhuria katika wajibu wa kidini kuinyamazisha dhamiri yako. {2Tsw 144.1}

Siyo sahihi kwa Mkristo katika zama yoyote ya ulimwengu kuwa mpenda anasa, lakini ni kiasi gani zaidi sasa, wakati kurasa za historia ya dunia hii zipo karibu kufungwa. Hakika msingi wa tumaini lako la uzima wa milele hauwezi kuwa umewekwa sahihi sana. Mafanikio ya nafsi yako na furaha yako ya milele hutegemea juu ya msingi wako, ambao umejengwa juu ya KRISTO. Wakati wengine wanakimbilia maburudisho ya kidunia na kuhema nayo, wewe uwe unakimbilia ahadi ya hakika ya upendo wa MUNGU, kwa dhati, na kwa ari ukilia: Nani atanionesha jinsi ya kufanya wito wangu na uteule wangu hakika? Moja ya ishara za siku za mwisho ni kwamba Wakristo wanaomkiri Kristo ni wapenda anasa zaidi kuliko wapenda MUNGU. Shugulika na nafsi yako mwenyewe kwa dhati, kwa kweli. Jipeleleze kwa uangalifu. Ni wachache kiasi gani, baada ya tathmini aminifu wanaweza kuangalia juu kuelekea mbinguni na kusema: “mimi siyo mmoja wa wale walioelezewa! Mimi siyo mpenda anasa zaidi ya mpenda MUNGU! Maisha yangu yamefichwa katika KRISTO ndani ya MUNGU, na wakati Yeye aliye uzima wangu atakapotokea, hakika, nami nitatokea hakika na Yeye katika utukufu. “Upendo na neema ya MUNGU! Oh, neema ya thamani! Ya thamani zaidi ya dhahabu safi. Huipandisha na kuiheshimisha roho zaidi ya kanuni zote, na hupangilia mapenzi juu ya mbingu, wakati wale walio karibu nasi waweza kuwa na ubatili na wakijihusisha katika anasa na upuuzi, mazungumzo yetu ni ya mbinguni, mahali tunapomtazamia mwokozi; nafsi ikimtafuta MUNGU

kwa ajili ya msamaha na amani, kwa ajili ya haki na utakatifu wa Kweli. Zungumza na MUNGU na tafakari ya vitu vya juu mbinguni, itabadilisha nafsi katika mfano wa KRISTO. {2Tsw 144.2}

## **SURA YA 21**

### **MAOMBI KWA WAGONJWA**

Kwa suala la dada F, pale inahitajika kuwa kazi kubwa imekamilishwa. Wale walioungana katika kuomba kwa ajili yake walihitaji kazi iliyofanywa kwa ajili yao. Endapo MUNGU angejibu maombi yao, ingethibitisha uharibifu kwao. Katika masuala kama hayo ya ugonjwa au kuteseka, pale ambapo Shetani anatawala akili, kabla ya kujihusisha katika maombi hapo, lazima kuwe na chumba cha faragha cha kujitathmini moyo ili kugundua kama hakuna dhambi inayohitaji kutubiwa, nayo iungamwe, na kuachwa. Unyenyekevu wa dhati na kina, wa nafsi mbele za MUNGU ni wa lazima, na uimara katika unyenyekevu wenye kutegemea juu ya thamani ya damu ya KRISTO pekee. Kufunga

na kuomba hakutakamilisha kitu wakati nafsi imetengwa mbali na MUNGU kwa njia mbaya ya matendo. “Je hii siyo swaumu niliyoichagua? Kufungua vifungo vya uovu, kuacha mizigo mizito na kuwaachilia walioonewa wawe huru, na kwamba mvunje kila nira, Je, sio kuwapatia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta nyumbani kwako maskini waliofukuzwa? Wakati unapomuona mtu aliye uchi, wewe umvike, na usijifiche kutoka kwa ndugu wa damu moja nawe” “ndipo utakapoita, na BWANA atajibu, ndipo utakapolia Naye atasema Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri: Naye BWANA atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako, nawe utakuwa kama bustani iliyomwagiliwa maji na kama chemichemi ambayo maji yake hayapungui.” {2Tsw 145.1}

Ni kazi ya moyo ndiyo BWANA anahitaji, matendo mema, yanayochipua kutoka katika moyo uliojazwa upendo. Wote lazima kwa uangalifu na kwa kuomba wafikirie Maandiko hayo hapo juu (Isaya 58), na wachunguze nia zao na matendo. Ahadi ya MUNGU kwetu ni utii, bila ya kuweka sharti, kukubali na kutekeleza maagizo Yake yote. “Piga kelele” anasema nabii Isaya, “usiache, paza sauti yako kama tarumbeta, na uwaoneshe watu Wangu Wangu kosa lao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao. Huku wakinitafuta Mimi kila siku, na kufurahi kujua njia Zangu, kama vile taifa ambalo limetenda haki, na halijaacha maagizo ya MUNGU wao, wananiuliza Mimi maagizo ya haki; hufurahi kumkaribia MUNGU. Ambapo husema mbona tumefunga, lakini huoni? Mbona tumejitesa nafsi zetu, lakini Wewe huelewi? {2Tsw 146.1}

Hapa kuna watu wanaosemwa kwamba, hukiri kwa mdomo kwa hali ya juu, hawa wapo katika desturi ya kuomba, na ambao wanafurahi katika mafunzo ya dini; lakini bado kuna upungufu. Wanagundua kuwa maombi yao hayajibiwi; usongo/ari zao, juhudi zao za dhati haziangaliwi au kutambuliwa mbinguni, na kwa dhati wanauliza kwanini BWANA hawajibu. Siyo kwa sababu kuna kupuuziwa kokote katika upande wa MUNGU. Ugumu upo kwa watu. Huku wakikiri

utauwa, hawazai matunda kwa utukufu wa MUNGU; kazi zao hazipo kama zilivyotakiwa kuwa. Wanaishi huku wakipuuzia majukumu mema yaliyo chanya na wazi. Isipokuwa haya yamefanywa, MUNGU hawezi kujibu maombi yao kulingana na utukufu Wake. Katika swala la kutoa maombi kwa kwa ajili ya dada F. Kulikuwa na mkanganyiko wa hisia. Baadhi walikuwa washupavu na kuongozwa na msisimko. Walikuwa na ari, lakini siyo katika ufahamu. Baadhi walitazamia vitu vikubwa kufanyika kwa hivyo wakaanza kushangilia ushindi kabla ya ushindi kupatikana. Kulikuwa na onyesho la roho ya Yehu zaidi: “njooni nami, na mtaona ari yangu kwa BWANA.” Badala ya kujitumaini nafsi, na kujipa uhakikisho namna hii, jambo lilitakiwa kupelekwa kwa MUNGU kwa roho upole na kutotumainia nafsi, na kwa moyo wa kuvunjika na toba. {2Tsw 147.1}

Nilioneshwa kwamba kuhusiana na swala la ugonjwa, ambapo njia ipo wazi kwa maombezi kwa ajili mgonjwa, jambo hilo lazima kukabidhiwa kwa MUNGU katika imani tulivu, siyo kwa kimbunga cha msisimko. Yeye peke Yake, Ndiye anajua maisha ya nyuma ya mtu, anajua nini itakuwa hatima yake mbeleni. Yeye ambaye anajua mioyo yote ya watu, anajua endapo mtu kama atanyanyuliwa kutoka kwenye ugonjwa, atalitukuza Jina Lake ama kumuaibisha Bwana kwa kurudi nyuma na uasi. Yote tunayohitajika kufanya ni kumwomba Bwana kuwainua wagonjwa kama kwa kupatana na mapenzi Yake, tukiamini kwamba Yeye anasikia sababu ambayo tunawasilisha na kutoa maombi ya dhati na bidii. Kama BWANA ataona itamtukuza vyema, Yeye atajibu maombi yetu. lakini kuhimiza urejeshwaji wa afya bila kujikabidhi kwa mapenzi Yake siyo sahihi. {2Tsw 147.2}

Kile MUNGU anachoahidi anaweza katika wakati wowote kukifanya, na kazi ambayo huwapa watu Wake kuifanya anaweza kuikamilisha kupitia wao. Kama watu hao wataishi kulingana na kila alilosema, kila Neno zuri na ahadi itakamilishwa kwao. Lakini kama watakosa utii kamili, ahadi kubwa na za thamani zipo mbali, na haziwezi kufikia hatima au utimilifu wake. {2Tsw 148.1}

Yote ambayo yanaweza kufanywa katika kuomba kwa ajili ya wagonjwa ni kumwomba MUNGU kwa dhati kwa niaba yao, na katika



imani kamili kuacha jambo hilo mikononi Mwake. Kama tukiendekeza uovu mioyoni mwetu BWANA hatatusikia. Yeye Anaweza kutenda kile atakacho Mwenyewe na watu Wake. Yeye Atajitukuza Mwenyewe kwa kutenda ndani yao na kupitia wale ambao wanamfuata kwa ukamilifu, ili kwamba ijulikane kwamba ni BWANA, na kazi zao zimetendwa katika Yeye. Alisema KRISTO “kama mtu yoyote atanitumikia Mimi, huyo BABA Yangu atamheshimu” tunapokuja Kwake tunatakiwa kuomba kwamba tuweze kuingia na kukamilisha mapenzi Yake, na kwamba matamano yetu na maslahi yetu yazame katika Yeye. Lazima tutambue ukubali wetu wa mapenzi Yake, na siyo katika kumuomba kukubaliana na yetu. Ni bora kwetu kwamba MUNGU hajibu mara zote maombi yetu wakati tunapotaka, na kwa jinsi tunavyotaka. Yeye Atatufanyia mengi na mema mno kwa ajili yetu tena zaidi ya matamano ya maombi yetu yote, maana hekima yetu, ni upuuzi au ujinga mtupu. {2Tsw 148.2}

Tumeuunganika katika maombi ya dhati karibu na kitanda cha wagonjwa wanaume, wanawake, na watoto, na tumeona kwamba walirejeshwa kwetu kutoka kifoni kama jibu la maombi yetu ya dhati. Katika maombi haya tuliwaza lazima tuwe chanya na kuifanyia kazi Imani yetu, na tusiombe chochote isipokuwa uzima/kupona kwa mgonjwa tu. Hatukuthubutu kusema, “kama itamtukuza MUNGU,” tukihojia kuwa ingekiri kuonesha shaka kwetu. Kwa hamu tumetazama wale ambao wamesharejeshwa kwetu, kama vile kutoka kwa wafu. Tumewaona baadhi ya hawa, hasa vijana, wakirejeshwa katika afya, na wamemsahau MUNGU, wamekuwa chukizo, kwa maadili mabaya katika maisha, wakisababisha huzuni na maumivu kwa wazazi na marafiki, na wamekuwa fedheha kwa wale waliohofu kuomba. Wameishi bila kumheshimu na kumtukuza MUNGU, ila kumkufuru Yeye kwa maisha ya uovu. {2Tsw 148.3}

Hatuwekei alama njia zetu tena kwamba ndio za kufuata, wala kutafuta kumletea BWANA matakwa yetu. Kama maisha ya wagonjwa yataweza kumtukuza Yeye, tunaomba kwamba waweze kuishi; hata hivyo, siyo kama tutakavyo bali kama atakavyo Bwana. Imani yetu yaweza kuwa imara tu, na ya kutegemewa, kwa kukabidhi matamano yetu kwa MUNGU, Mwenye hekima yote, bila joto la mifadhaiko, na katika Imani

timilifu, tukitumaini yote Kwake. Tunayo ahadi. Tunajua Yeye anatusikia kama tukiomba sawasawa na mapenzi Yake. Maombi yetu lazima yasichukue mfumo wa kuamrisha/amri, lakini yawe maombezi Kwake Yeye kufanya mambo tumuombayo. Wakati kanisa linapoungana pamoja, litakuwa na nguvu na uwezo; lakini wakati baadhi yao wanapoungana na ulimwengu, na wengi wanapelekwa katika kutamani, jambo ambalo MUNGU huchukia, Yeye anaweza kufanya kwa ajili yao, ila kwa udogo tu. Kutokuamini na dhambi vinawafungia mbali na MUNGU. Sisi tu wadhaifu sana hata hatuwezi kuhimili mafanikio ya kiroho, tusije tukachukua utukufu, na kujitwalia wema na haki nafsini mwetu wenyewe, kama ndiyo sababu ya ishara ya mbaraka wa MUNGU, wakati yote ilikuwa kwa sababu ya rehema na upendo mkubwa na fadhili za BABA yetu wa mbinguni Mwenye huruma, na sio kwa sababu ya wema wowote ulioonekana ndani yetu. {2Tsw 149.1}

Daima tushinikize mvuto ambao utakuwa ukitakasa wale walio karibu yetu. Huu ubora wa maadili yaokoayo umekuwa dhaifu sana-- wengi wameungana na ulimwengu na wameshiriki roho yake na ushawishi wake, na urafiki wao na dunia umewatenga na MUNGU, YESU ameenda mwendo wa safari ya siku nzima mbele yao. Hawawezi tena kuisikia sauti Yake ya mashauri na maonyo, na wanafuata hekima na maamuzi yao binafsi na hukumu. Wanafuata njia ambayo huonekana njema machoni pao, lakini ambayo baadaye huthibitika kuwa upuuzi/upumbavu. MUNGU hataruhusu kazi Yake, kuchanganywa na sera za kidunia. Watu wajanja, na wapanga njama wa ulimwengu siyo watu wa kuchukua nafasi za uongozi katika kazi hii makini sana na takatifu. Lazima wawe wameongoka, au kujihusisha katika wito ule ambao ni sawa na mapenzi yao ya dunia, ambao hauhusishi hatima ya umilele. MUNGU hataingia katika ubia na walimwengu. KRISTO anampatia kila mtu uchaguzi wake: Je, utakuwa Nami au na ulimwengu? Je, Utavumilia mateso na aibu, kuwa wa pekee, na mwenye ari ya matendo mema, hata kama utachukiwa na ulimwengu, na kuchukua Jina Langu, au utachagua utukufu, heshima, sifa na faida ambazo ulimwengu unatoa, na kutokuwa na sehemu ndani Yangu? "Hamwezi kumtumikia MUNGU na mapepo/mashetani au mali." {2Tsw 149.2}

## SURA YA 22

### USHUJAA NDANI YA MCHUNGAJI/MTUMISHI

Mpendwa ndugu G: nimekuwa nikioneshwa kuwa ulikuwa umepungua sana katika wajibu wako kama Mchungaji/Mtendakazi. Unakosa sifa muhimu. Hauna roho ya kimishenari. Hauna tabia ya kuacha raha na starehe yako ili kuokoa roho. Wapo wanaume, wanawake na vijana wa kuletwa kwa KRISTO ambao wangeshikilia Ukweli endapo nuru ingeangaziwa kwao. Katika ujirani/mazingira yako wapo majirani ambao wana sikio la kusikia {2Tsw 150.1}

Nilikuona ukitafta kuwaelekeza baadhi; lakini katika wakati ambao ulihitaji uvumilivu, ushujaa, na nguvu, ukazimia moyo, ukaingia mashaka, na kukatishwa tamaa, na kutelekeza/kudondosha kazi. Ulitamani raha yako mwenyewe, na ukaruhusu maslahi ambayo yalifanya mambo yaende chini. Pale kungeweza kuwa na mkusanyiko wa watu; lakini fursa ya thamani ilipita kwa wakati huo, kwa sababu ya ukosefu wako wa nguvu. Niliona bila wewe kuamua kujifunga silaha kamili za kivita, na kukubali kuvumilia magumu kama askari mzuri wa msalaba wa KRISTO, na kuona kwamba unaweza kutumika na kutumiwa kuleta watu kwa KRISTO, ni bora kuacha kazi yako kama mchungaji na uchague wito mwingine. {2Tsw 150.2}

Nafsi yako haijatakaswa kwa kazi. Haubebi mzigo wa kazi juu yako. Unachagua sehemu rahisi kuliko ile iliyokabidhiwa kwa mtumishi wa KRISTO. Yeye Hakuhesabu maisha Yake ya thamani Kwake Mwenyewe.

Hakujipendeza Mwenyewe (hakujipandisha juu, au kuonyesha hadhi yake), lakini aliishi kwa mafanikio ya wengine. alijifanya mwenyewe hana heshima, na kuchukua juu ya nafsi Yake namna ya mtumwa. Haitoshi kuwa na uwezo wa kuwasilisha hoja namawazo ya msimamo wetu mbele za watu. Mtumishi wa KRISTO lazima awe na upendo usio na kikomo kwa watu, roho ya kujikana nafsi, ya kujitoa. Lazima awe tayari kutoa maisha yake, kama itakuwa inahitajika, kwa kazi ya kuokoa wanadamu wenzake, ambao KRISTO aliwafia. {2Tsw 151.1}

Unahitaji uongofu kwa kazi ya MUNGU. Unahitaji hekima na maamuzi ya busara katika kuongoza kazi yako. Kazi zako hazihitajiki miongoni mwa makanisa. Lazima uende nje katika maeneo mapya na uthibitishe kazi yako. Nenda na roho ya utumishi ili kuongoa roho ifuate Kweli. Ikiwa unaona thamani ya roho, ishara ndogo kwa ajili ya wema itafurahisha moyo wako na utavumilia, ingawa kutakuwa kazi nyingi na uchovu katika juhudi. Baada kutibua maji kwa kuingiza somo la Ukweli, usihame sehemu hiyo hata kama kuna ishara ndogo ya mafanikio. Je unatarajia mavuno bila mahangaiko? Je Unatarajia kwamba Shetani atakuwa tayari kuruhusu watumwa wake watoke safu au jeshi lake na kuelekea kwenye safu ya KRISTO? Atafanya kila juhudi kuziacha pingu za giza alizowafungia chini ya bendera yake nyeusi. Je unaweza kutarajia kuwa mshindi katika kuleta roho kwa KRISTO bila bidii ya dhati, wakati una adui kama huyo kukutana naye na kupambana? {2Tsw 151.2}

Lazima uwe na ushujaa zaidi, usongo zaidi, na kuweka mbele bidii kubwa, la sivyo utaamini kwamba umekosea wito wako. Mtumishi anayevunjwa moyo kwa urahisi hufanya madhara kwa kazi anayotaka kuikuza, na kujitendea dhuluma mwenyewe. Wote wanaokiri kuwa watumishi wa KRISTO lazima wajifunze hekima kwa kusoma historia ya Mtu wa Nazareti, na pia historia ya Martin Luther na maisha ya wanamatengenezo wengine. Kazi zao zilikuwa ngumu, lakini walistahimili ugumu kama maaskari waaminifu wa msalaba wa KRISTO. Usikwepe majukumu. Kwa unyenyekevu, na uungwana, hebu uwe tayari kushauriwa, kuelekezwa. Baada ya kupokea ushauri kutoka kwa wenye hekima, wenye busara, bado kuna Mshauri ambaye hekima Yake haikosei. Usiache kupeleka mambo yako mbele Zake na tafuta

njia Yake. Amekupa mwaliko kwa ahadi kwamba kama umepungukiwa na hekima na umuombe, atakupatia kwa ukarimu, Naye hakemei. Kazi takatifu na makini ambayo tumeunganishwa nayo inahitaji moyo wote, uongofu kamili, ambao maisha yao yameunganishwa na maisha ya KRISTO. Hawa wanachota rojorojo na lishe kutoka mti wa mzabibu unaoishi (utomvu wa lishe ya mti unaosafirishwa na mabomba ya mmea-sap), na kunawiri katika BWANA. Ingawa wanaona ukubwa wa kazi, na kwa mshangao wanasema, “Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo?” hata hivyo hawatakimbia kazi na taabu, lakini watatumika kwa dhati na bila ubinafsi kuokoa roho. Kama wachungaji wadogo, walio chini ya Kristo Mchungaji Mkuu ni waaminifu katika wajibu wao wote, wataingia katika furaha ya BWANA wao na kupata kuridhika kwa kuona watu waliookolewa mbinguni kupitia juhudi zao zenye uaminifu. {2Tsw 151.3}

## **SURA YA 23**

### **UDANGANYIFU KATIKA BIASHARA**

Mpendwa Ndugu H: nimekuwa nikisubiri fursa kukuandikia, lakini nimekuwa nikizuiwa. Baada ya maono yangu ya mwisho niliona ilikuwa wajibu wangu kufanya haraka kuweka mbele yako kile BWANA alipendezwa kuwasilisha kwangu. Nilielekezwa nyuma na kuoneshwa kwamba miaka mingi ya huko nyuma, hata kabla ya ndoa yako, imekuwepo ndani yako tabia ya udanganyifu katika biashara, kutaka

kujipatia zaidi katika njia isiyo ya uaminifu. Una roho ya tamaa, tabia ya kudanganya katika biashara ambayo ni roho ya uharibifu kwa ukuaji wako kiroho na kwa kiasi kikubwa iliumiza ushawishi wako. Familia ya baba yako waliangalia mambo haya katika mtazamo wa kidunia kuliko katika rejea kiwango cha juu kilichoinuliwa na kutukuzwa na BWANA MUNGU wetu: “Nawe mpende BWANA MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.” Katika hili umeshindwa. Kushughulika kwa njia yoyote ili kujitwalia mali kwa tamaa na bila haki haimpendezi MUNGU. Bwana hatafumbia macho makosa na dhambi zilizo katika mwelekeo huu bila kuzikiri kwa kikamilifu na kuziacha kabisa. {2Tsw 152.1}

Nilielekezwa mbali katika siku za nyuma na kuoneshwa kupuuzia/kulegea kwa namna ambayo ulichukulia haya mambo. BWANA Ameweka alama bidhaa za Wanyama zinazobebwa kwenda sokoni, ule mzigo wa wanyama ambao walikuwa dhaifu kwamba wasingeweza kuwa na faida kuwatunza, hivyo waliandaliwa kwa chakula na kupelekwa sokoni, na hivyo kununuliwa na kuingizwa kwenye matumbo ya watu. Moja ya bidhaa hizi ziliwekwa juu ya meza yetu kwa muda kulisha familia yetu kubwa katika siku za umaskini wetu. Haukuwa peke yako wa kulaumiwa katika hili. Wengine katika familia yako walikuwa na hatia sawa nawe. Haijalishi ikiwa ilipangwa kwamba hao wanyama wanunuliwe na kuliwa na sisi au na walimwengu. Ni kanuni ya vitu ambavyo vinamchukiza MUNGU; umevunja amri Yake. Hukumpenda jirani yako kama ufanyavyo kwa nafsi yako, maana usingetaka kuwa kitu hicho-hicho kufanywa kwako. Ungehesabu umetukanwa/umedhalilishwa. Roho ya ngumu imeongoza katika kuondoka huku toka kanuni ya Kikristo, na ikasababisha wewe kushuka kuelekea aina ya biashara ambayo ilinufaisha nafsi yako kwa hasara ya wengine. {2Tsw 153.1}

Wakati swali la ulaji wa nyama lilipo letwa mbele yangu miaka mitano iliyopita, likionyesha ni kidogo jinsi gani watu walijua kile walichokuwa wanatumia kwa chakula katika mfumo wa nyama, hii biashara yako ilioneshwa. Matokeo ya kula nyama ya wanyama hawa wasio na afya ni damu yenye magonjwa, kuugua, na homa. Matukio ya aina hii mengi

yalioneshwa kwangu kama yafanywavyo kila siku na walimwengu. Wewe, kaka yangu, hujaona kosa hili kwa upande wako kama BWANA alionavyo, hujaona kwamba ilikuwa ni dhambi kubwa kwa upande wako. Mambo mengi ya tabia ya kufanana na hii yamechukua nafasi katika maisha yako, ambayo utakuta kwamba malaika achukuaye kumbukumbu kwa uaminifu ameyaandika, na ambayo utakutana nayo tena isipokuwa kwa kutubu na kukiri na kusahihisha makosa hayo. {2Tsw 153.2}

Niliomba kusubiri na kuona. Nilielekezwa kuongea kwa wazi, kutoa kanuni zenye za kawaida na za jumla, na kukuacha wewe kuzifanyia matumizi mwenyewe. Nilioneshwa kuwa MUNGU hangeonesha makosa yaliyofanywa na watu Wake mara kwa mara, lakini atasababisha kutolewa katika kusikika kanuni Zake za jumla, za karibu, Kweli makini, na wote lazima wawe wazi kushawishiwa kuona, kuhisi, na kuelewa ikiwa wamehukumiwa au la. Haujashughulikia roho yako mwenyewe kwa ukaribu na kwa uaminifu. alisema malaika: "Nitamuonesha, nitamjaribu, nitakwenda kinyume chake, mpaka ametambua Mkono wa MUNGU unashughulika naye." {2Tsw 154.1}

Niliona hilo wakati nikiwa ---- wale waliunganishwa na familia yako hawakwenda sahihi. Ulionesha roho ya tamaa, ukifurahia udanganyifu na kutokuwa mwaminifu, ukitaka kujichumia zaidi mwenyewe. Usingeweza kuwa na ushawishi wa wema mahali pale mpaka umekomboa yaliyopita kwa badiliko la jumla la tabia katika biashara na wanadamu wenzako. Nuru yako ilikuwa giza kwa watu, na ushawishi wako ulikuwa ni maumivu makubwa kwa kazi ya Ukweli wa sasa. Ulileta fedheha juu ya Ukweli, na biashara ya udanganyifu wako, ya kujichumia mwenyewe zaidi, ilisababisha jina lako kuwa msemu miongoni wa watu. Mara nyingi umeanguka chini ya viwango vya walimwengu wengi kuhusiana na uaminifu katika kufanya biashara. Mzee siwezi kufanya wema---. Maneno yake ni kama maji yaliyomwagwa juu ya ardhi, kwa maana alikuwa ameunganishwa nawe na akashiriki katika biashara hii ya udanganyifu. Katika Nyanja nyingi alikuwa kama mlimwengu katika shughuli/dili za biashara. Alikuwa na tamaa na kwa haraka alikuwa anaanza kuwa mbinafsi. Njia yake katika mambo mengi ilipangwa kuharibu ushawishi wake na haikufaa kwa

mchungaji/mtendakazi wa KRISTO. Alisema malaika katika maono yaliyotolewa Rochester, New York, mwaka 1866: “Mkono Wangu utaleta hali ngumu. Anaweza akusanye, lakini nitatawanya mpaka amekomboa yaliyopita na kufanya kazi isiyo na mawaa kwa umilele. “Kila Mkristo wa Kweli lazima awe juu ya kujifedhehesha na kujishusha mpaka chini, na kuchuuza kwa roho ya biashara ya kiulimwengu. {2T 154.2}

Wewe siyo bahili; unapenda kuwa mkarimu, upo tayari kugawa, una moyo uliokunjuka, na U mtoaji; lakini kile ambacho ni kosa kwako ni roho iliyotajwa ndani ya barua hii, ya kutokumpenda jirani yako kama nafsi yako; ni kupuuzia kuona makosa yako na kuyasahihisha wakati nuru ya nguvu yenye Ukweli, imekueleza wazi wajibu wako. Wewe ni mpenzi wa ukarimu, na MUNGU hawezi kukutupa ili udanganywe na mdanganyifu mkubwa wa wanadamu, lakini atakuja moja kwa moja kwako na kukuonesha mahali unapokosea ili uweze kuangalia nyuma hatua zako. Sasa anakuita kukomboa yaliyopita, na kupanda kilele cha juu cha matendo, na acha kumbukumbu ya maisha yako irekodi yale yasiyochafuliwa kwa tamaa au ubinafsi wa kupenda faida. {2Tsw 155.1}

Maamuzi yako katika mambo ya kidunia yatakuwa upuuzi isipokuwa uyatoe yote kwa MUNGU. Wewe na mke wako si wacha Mungu. Ukiroho wenu siyo ule ambao MUNGU angetaka muwe nao. Kupooza kunaonekana kuwa juu yenu; ila wote mna uwezo wa kuweka ushawishi mkubwa kwa ajili ya MUNGU na Ukweli Wake kama mtapamba kukiri kwenu na maisha mazuri yaliyopangiliwa, na yenye mazungumzo ya uchaji Mungu. Mara kwa mara mnaingia katika haraka kubwa, na baadae mnakuwa papara na kukasirishwa, kisha mnaamrisha msaada katika hali ya haraka. Hili ni uharibifu kwa maendeleo yenu ya kiroho. {2Tsw 155.2}

Muda ni mfupi, na hauna muda wa kuchelewesha maandalizi ya moyo yenye ulazima katika kufanya kazi kwa dhati, na uaminifu kwa ajili ya nafsi yako mwenyewe, na kwa wokovu wa rafiki zako na majirani, na wale wote walio chini ya ushawishi wako. Siku zote lenga kuishi zaidi katika nuru ambayo ushawishi wako waweza kuwa unatakasa wale ambao unashirikiana nao katika biashara au mahusiano ya kawaida.



Kuna ukamilifu katika YESU. Unaweza kupata nguvu kutoka Kwake Yeye, ambayo itakuwezesha wewe kuenenda kama Yeye alivyoenenda, lakini lazima pasiwe na kujitenga kwa mapenzi yako Kwake. Yeye Anakuhitaji wewe kikamilifu, nafsi, mwili na roho. Wakati unapofanya yote kwa upande wako ambayo anahitaji, Atafanya kazi kwa ajili yako, na kukubariki na kukuimarisha kwa utajiri wa neema Yake. {2Tsw 155.3}

## **SURA YA 24**

### **KUNYANYASA WAAJIRIWA**

Mpendwa kaka J: uzito mkubwa umekuwa juu ya akili yangu tangu maono niliyopewa ijumaa jioni, Juni 12, 1868. Nilioneshwa kuwa wewe hujitambui. Hujahisi kupatanishwa na Shuhuda iliyotolewa kuhusu jambo lako nawe hujafanya kazi kamili kubadilika. Nilirejeshwa kwa Isaya; “Je, hii siyo swaumu niliyoichagua? Kufungua vifungo vya uovu, kuacha mizigo mizito na kuwaachilia walioonewa wawe huru, na kwamba mvunje kila nira, Je si kuwapatia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta nyumbani kwako maskini waliofukuzwa? Wakati

unapomuona aliye uchi, wewe umvike, na usijifiche na ndugu wa damu moja nawe?”. Utakapofanya mambo haya, utapokea baraka zilizoahidiwa {2Tsw 156.1}

Unaweza kuuliza swali, “mbona tumefunga,” “na wala huoni? Mbona tumejitesa nafsi zetu, na hata Hautambui?” MUNGU ametoa sababu kwa nini maombi yako hayakujibiwa. Umefikiri kwamba umepata sababu ndani ya wengine na umeelekeza makosa mashitaka juu yao. Lakini niliona kuwa kuna sababu za kutosha ndani ya nafsi yako mwenyewe. Una kazi ya kufanya. kuweka moyo wako sawa. Lazima utambue kuwa kazi lazima ianze na nafsi yako. Umewanyanyasa maskini na umefaidika mwenyewe kwa kuchukua faida ya uhitaji wao. Kuhusu mali, umekuwa mdanganyifu na umetenda bila haki. Haujawa na ile roho ya fadhili, adilifu na njema ambayo wakati wote inatambulisha maisha ya wafuasi wa KRISTO. Umemnyanyasa mwanamke mwajiriwa katika ujira wake. Ulimuona amevalia nguo za kimaskini, mfanyakazi mwenye bidii ambaye ulijua alikuwa mwadilifu na mcha MUNGU; bado ulijipatia faida kutoka kwake kwa sababu ulikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo. Niliona upuuziaji wa kuona na kuelewa mahitaji yake, na ujira mdogo uliomlipa, yote yameandikwa mbinguni kana kwamba yamefanywa kwa YESU katika nafsi ya mmoja wa watakatifu Wake. Kama ulivyotenda hili kwa mwanafunzi mdogo wa KRISTO, umemtendea Yeye. Mbingu zimezingatia udanganyifu wako wote kwa wale waliokutumikia ndani ya nyumba yako, rekodi itabaki kwa uaminifu imeandikwa dhidi yako isipokuwa imetubiwa na marejesho yamefanywa. Mjongeo mmoja wa makosa, hufanya madhara zaidi kuliko inavyoweza kuondolewa kwa miaka.; kama mkosaji angeona ukubwa wa uovu, ingekamua kutoka nafsini mwake vilio vya maumivu. Wewe ni mbinafsi kuhusiana na mali. Katika jambo la ndugu K: malaika wa MUNGU alilenga na kusema “kwa kadri ya ulivyotenda hivi kwa mmoja wa wanafunzi wa KRISTO, umetenda hili kwa YESU katika nafsi Yake.” {2Tsw 156.2}

Matukio niliyoorodhesha siyo hayo tu peke yake. Mimi ningetaka uone mambo kama mbingu zilivyofunua mbele yangu. Kuna udanganyifu wa huzuni juu ya fikra. Ni dini ya KRISTO pekee ndiyo unayoihitaji. Yeye Hakujipendeza Mwenyewe, lakini aliishi kuwanufaisha wengine. Una

kazi ya kufanya, na usipoteze muda kunyenyekeza moyo wako mbele za MUNGU, na kwa maungamo yaliyo na unyenyekevu, ondoa mawaa kutoka katika tabia yako ya Kikristo. Hatimaye unaweza kujihusisha katika kazi makini ya kushugulikia wokovu wa wengine bila kufanya makosa mengi. {2Tsw 157.1}

Je, Muda wako umekuwa na faida gani, kwa kutumiwa jinsi ambavyo umekuwa ukitumiwa wakati ukijihusisha katika kazi ambayo MUNGU hakukuweka uifanye? Mivuto imefanywa juu ya akili na uzoefu umepatikana, ambapo itahitaji kazi kubwa kwao kuufuta. Roho zitazunguka katika giza, kwa mifadhaiko na kutoamini, na baadhi hazitapona kamwe. Kwa kufunga na maombi ya dhati, kwa kuchunguza moyo kwa kina, kuchunguza nafsi vikali, kuiweka wazi roho; usiache tendo lolote kutoroka uchunguzi wako mkali. Kisha, kwa kufa nafsi kabisa na maisha yako kufichwa kwa KRISTO katika MUNGU, toa maombi yako manyenyekevu. Kama unanuia maovu moyoni mwako, BWANA hatakusikliza. Endapo Bwanga angesikia maombi yako, wewe ungejitukuza na kujikuza tu. Shetani amesimama tayari, akijiandaa kufanya faida kubwa aliyojipatia. {2Tsw 157.2}

Oh, ni muhimu kiasi gani kuwa mwaminifu katika vitu vidogo unaelezea maisha yetu, kwamba uadilifu wa Kweli unaweka alama njia ya matendo yetu, na daima tuweke mawazoni kwamba malaika wa MUNGU wanachukua kumbukumbu ya kila tendo! Kile ambacho tunawapimia na kuwapa wengine nasi tutapewa. Kicho kiambatane nawe usije ukatenda bila haki na kwa ubinafsi. Kwa ugonjwa na taabu BWANA ataondoa kwetu kingi zaidi kuliko tunachopata kwa kusaga uso wa maskini. MUNGU Mwenye haki anapima nia zetu zote na matendo yetu yote. {2Tsw 158.1}

Nilioneshwa kaka na dada L. Kupenda dunia kumekula sana utauwa wa Kweli na kufisha ganzi nguvu za akili hadi Ukweli unashindwa kuwa na ushawishi ubadilishao juu ya maisha na tabia. Kupenda dunia kumefunga mioyo yao katikakuhurumia na kujali mahitaji ya wengine; roho ya kupenda dunia imewatenganisha kutoka kwa MUNGU. Kaka na dada, ninyi mna kazi ya kufanya kutoka chini ya takataka za ulimwengu; mnahitajika kufanya juhudi za dhati kushinda kupenda kwenu dunia,

ubinafsi wenu, na uchoyo wenu. Hizi ni dhambi zinazolaani watu wa MUNGU. Nilioneshwa nyuma katika jamii ambayo mliishi kabla ya kuhamia ----. Mlikuwa na tamaa na wadanganyifu na wakali katika mikataba ya biashara (dili/deal). Mkichukua faida kila wakati ambapo mngeweza kupata mwanya wa kufanya hivyo. Nilijaribu kutafuta katika matendo ya maisha yenu kanuni ya kujitoa na ukarimu lakini sikuweza kuona, zilikuwa adimu sana. Nuru yenu ilianguza mbele ya wengine katika namna ambayo walihisi kukasirishwa nanyi na imani yenu. Ukweli umelaumiwa kwa tamaa zenu na dhuluma katika uchuuzi. Hebu MUNGU na aweze kuwasaidia kuona yote, na kuwa na chuki kama ile Aliyonayo kwa ajili ya uovu huu. Acheni nuru yenu ianguze ili wengine kwa kuyaona matendo yenu mema waweze kuongozwa kumtukuza BABA yenu aliye mbinguni. MUNGU hajafurahishwa na njia yenu, maana imewekwa alama ya maslahi binafsi. Bado Yeye hajapendezwa nayo, na atashughulika nanyi katika hukumu, isipokuwa mmejiondolea wenyewe hii roho ya udogo, na kutafuta kutakaswa kupitia Ukweli. Imani pasipo matendo imekufa, ikiwa peke yake. Imani haitawaokoa isipokuwa imethibitishwa kwa matendo. MUNGU anahitaji kwenu kuwa matajiri katika kazi njema, tayari kusambaza, tayari kuwasiliana, kuweka ghalani kwa ajili yenu msingi mwema dhidi ya muda ujao, ili muweze kupata uzima wa milele. {2Tsw 158.2}

Nilioneshwa kwamba umenyanyasa waajiriwa wanyonge katika mishahara yao. Umechukulia faida mazingira na kujipatia wafanyakazi kwa gharama ya chini. Hii imekuwa haimpendezi MUNGU. Ungewalipa wafanyakazi wako kwa ukarimu, yote ile waliyoifanyia kazi. MUNGU anaona na anajua. Mchunguzaji wa mioyo anajua mawazo, nia na malengo ya moyo. Kila senti ambayo imetwaliwa nawe kwa njia hii, kama itatunzwa, itatawanywa kupitia taabu na ugonjwa. Ulimwengu, ulimwengu, ulimwengu, umekuwa ni kawaida ya siku kwako. Wokovu wa roho umekuwa si muhimu bali namba mbili. Oh, laiti ungeona, katika nuru ya umilele, jinsi MUNGU aonavyo hivi vitu. Ungestushwa na usingetulia hadi umerekebisha mambo. {2Tsw 159.1}

Mlikuwa na nuru juu ya matengenezo ya afya, lakini hamkuipokea na kuishi kwayo. Mliridhisha hamu ya kula na kumfundisha kijana wenu somo la huzuni kwa kumharibu katika kula wakati wote na chochote

alichochagua. Katika kupenda kwenu dunia mliendelea kufanya kazi juu ya mpango wa shinikizo la juu. Mkono wa MUNGU uliondolewa, na mliachwa katika udhaifu wenu wenyewe. Halafu wote mlijikongoja juu ya ukingo wa kaburi, na bado mlishindwa kujifunza somo katika mambo mengi ambayo MUNGU angepeda mjifunze. Mlidumisha kupenda kwenu dunia. Ubinafsi wenu wa Kupenda faida, udanganyifu wenu mdogo ulikuwa haujaachwa. Hamkuthamini huruma, kujali na huruma nyororo na umakini katika kumjali yule aliyekuwa akiwatunza wakati wa ugonjwa wenu, kama mngekuwa nayo, ingewaongoza ninyi kuonesha roho bora ya ukarimu na uungwana badala ya kushughulika nayekwa unyanganyi wa hali ya chini kwa yule aliyekuwa mkweli kwenu. Umesaga uso wa maskini, umetenda bila haki. “Kuna atapanyaye, na bado huongezeka, na kuna yule azuiaye zaidi lakini huelekea katika umaskini.” {2Tsw 159.2}

Ilionekana kwangu, wakati vitu hivi vilivyooneshwa mbele yangu, kwamba Shetani alikuwa na nguvu kiasi cha kupofusha akili kupitia kuipenda dunia, kwamba hata wale wanaomkiri Kristo walisahau, au kupoteza akili na hisia ya Ukweli kwamba MUNGU anaishi na kwamba malaika Zake wanachukua kumbukumbu ya matendo yote ya watoto wa wanadamu; kwamba kila kitendo cha ubahili, kila uchuuzi mdogo, vinawekwa katika kumbukumbu ya maisha. Kila siku inabeba mzigo wake wa kumbukumbu ya wajibu ambao haujatekelezwa, upuuziaji, ubinafsi, udanganyifu, ulaghai, na hila. Kiasi gani cha kazi uovu kinajikusanya kwa ajili ya hukumu ya mwisho! Wakati KRISTO ajapo, “Ujira Wake upo pamoja Naye, na kazi Yake mbele Yake,” kumlipa kila mtu kulingana na matendo yake yalivyokuwa. Ni ufunuo wa namna gani basi utakuwa umefanywa! Kuchanganyikiwa gani kutaonekana usoni mwa baadhi wakati matendo ya maisha yao yanapofunuliwa juu ya kurasa za historia! {2Tsw 160.1}

“Sikilizeni, ndugu zangu wapendwa, Je, MUNGU hajawachagua maskini wa dunia hii kuwa matajiri wa imani, na warithi wa ufalme ambao Yeye ameahidi kwa wale wampendao? Lakini ninyi mmewadharau maskini. “Itawafaidia nini, ndugu zangu, ingawa mtu atasema anayo imani na hana matendo? Je, imani itamuokoa? kama kaka au dada yupo uchi na maskini wa chakula cha kila siku, na mmoja wenu akawaambia,

nendeni kwa Amani, mkapate joto na kushiba; hata hivyo asiwape vile vitu vnavyohitajika kwa mwili, itamfaidia nini? Hivyo pia imani, ikiwa haina matendo, imekufa, ikiwa peke yake.” Unaweza kuamini Ukweli wote; ila kama bado kanuni zake hazijachukuliwa katika maisha yako, kukiri kwako kwa mdomo hakutakuokoa. Shetani anaamini na kutetemeka. Adui anatenda kazi. Anajua muda wake ni mfupi, na ameshuka chini kwa nguvu kubwa kufanya kazi zake ovu sawasawa na imani yake. Lakini watu wamkirio MUNGU hawaungi mkono imani yao kwa matendo yao. Wanaamini katika ufupi wa wakati, huku bado wanashikilia tu kwa hamu vitu vya ulimwengu huu kana kwamba ulimwengu utakaa miaka elfu kama ulivyo sasa. {2Tsw 160.2}

Ubinafsi unatia dosari katika njia ya wengi. “Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia matumbo yake ya huruma au huruma zake, je upendo wa MUNGU wakaaje ndsni yake huyo? Watoto wadogo tusipende kwa neno wala kwa ulimi; bali kwa tendo na Kweli. Katika hili tutafahamu ya kwamba tu wa Kweli nasi tutaituliza mioyo yetu mbele Zake, ikiwa mioyo yetu inatuhukumu kwa maana MUNGU ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote. Wapenzi mioyo yetu isipotuhukumu tuna ujasiri kwa MUNGU; na lolote tuombalo twalipokea Kwake, kwa kuwa twazishika amri Zake, na kuyatenda yapendezayo machoni Pake.” {2Tsw 161.1}

Jitengeni nafsi zenu na ubinafsi na mfanye kazi kamilifu kwa ajili ya umilele. Mbadili na kukomoba yake yaliyopita na msiwasilishe Ukweli mtakatifu mnaoukiri mahali mnapoishi sasa kama mlivyofanya kule mlipoishi kabla. Acha nuru yenu iangaze zaidi kwamba wengine kwa kuona matendo yenu mazuri waweze kuongozwa kumtukuza BABA yetu wa wa mbinguni. Msimame juu ya jukwaa lililoinuliwa la Ukweli wa milele. Dhibitini shughuli za biashara yenu katika maisha haya thabiti kulingana na Neno la MUNGU. {2Tsw 161.2}

## SURA YA 25

### KUGOMBANA KUMEKATAZWA

(Malumbano, kupigana au Combativeness)

Mpendwa ndugu M: wakati tulipokutana nawe pale ---, tulikuwa na shauku kukusaidia, na tukaogopa usingepokea msaada ambao ulihitaji pale. Nilipendekeza ujio wako katika eneo letu na kujumuika nasi, pamoja watoto wengine wapendwa wa MUNGU, ili uweze kuwa unajifunza masomo muhimu sana ambayo unapaswa kujifunza mbele yako ili uweze kustahimili majaribu na hatari za siku hizi za mwisho. Nilikumbuka uso wako kama yule mmoja ambaye BWANA alinionesha akipambana kushinda juu ya tabia za uovu zenye nguvu, ambazo ziliongoza siyo tu katika uharibifu wa mwili wako lakini kwa uharibifu wa milele baada ya hapo. Umepata ushindi mara nyingi, lakini bado una ushindi mkubwa wa kujipatia; una vita vya kupigana na maadui wa ndani, isipokuwa ushinde, furaha yako mwenyewe itaharibiwa na wale wote wanaohusiana nawe. {2Tsw 162.1}

Chembe za uovu ndani ya tabia yako lazima lazima zishindwe. Lazima ushikilie kazi kwa bidii, maombi ya unyenyekevu kwa MUNGU, na kutambua kutojiweza na udhaifu wako bila neema Yake maalumu. Imani ya ile Kweli tayari imeleta matengenezo katika maisha yako, ila matengenezo haya bado si kamilikama inavyotakiwa ili wewe ufikie kipimo cha MUNGU. Unapenda Ukweli, lakini lazima ushikilie kwa kina zaidi maisha na mvuto wa maneno yako na tabia yako yote. Una somo kubwa la kujifunza, nawe usipoteze muda katika kujifunza. Hujajielimisha mwenyewe kutawala nafsi yako. Huu ni ushindi maalumu kwa ajili yako kuupata. Katika mfumo wako kuna vipengele vya vita zaidi kuliko vya Amani. Unahitaji kukuza adabu/uungwana, staha na upole wa Kweli wa Kikristo. “Katika heshima mkipendana mmoja na mwingine” “Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.” {2T 162.2}

Tabia yako ya ugomvi ni kubwa, na unasimama kwa kujizatiti ‘misuli’, tayari kukataa kila kitu pale upatapo nafasi. Hufanyi kazi kuona ni kwa ukaribu kiasi gani unaweza kufanya mawazo yako na maoni yako kupatana na yale ya wengine, lakini unasimama ukiwa umejitayarisha kutofautiana kama endapo nafasi yoyote itapatikana kwa wewe kufanya hivyo. Hii uharibu nafsi yako mwenyewe hurudisha nyuma maendeleo ya kiroho, na siyo tu uhuzunisha na kujeruhi wale ambao wangukuwa rafiki zako wa dhati, lakini wakati mwingine huwachukiza, kiasi kwamba, jamii yako haikubaliwi na kufurahiwa nao, lakini inaudhi. Ni kama jambo la kawaida kwako, kama vile unavyopumua, kwa wewe kufikiria mtazamo na maoni ya wengine kuwa ni duni kwa ya kwako. Mara kwa mara unakosea hapa, kwa kuwa hauna hekima yote na ufahamu ambao unajipa sifa mwenyewe. Mara kwa mara unaweka maoni yako juu ya wanaume na wanawake ambao wana miaka mingi ya uzoefu kuliko wewe, na ambao wana sifa/stahiki bora zaidi kuongoza na kutoa maneno ya uamuzi wa busara kuliko wewe. Lakini hujaona haya masumbufu yasiyokubalika, na kwa hiyo hujatambua madhara na matunda machungu yaliyozalishwa. Umeendekeza kwa muda roho ya ubishani, ya vita. Ugeukaji wako wa akili wa ajabu hupelekea wewe kufurahia mambo ambayo ni kinyume. {2T 163.1}

Elimu yako imekuwa fedheha, haijawa na faida katika uzoefu wako sahihi wa sasa ulioupata wa kidini. Karibu kila kitu ulichojifunza chapaswa kutupwa nawe ujifunze upya. Una hasira ya haraka, ambayo inahuzunisha rafiki zako na malaika watakatifu, na kujeruhi roho yako mwenyewe. Hii ni kinyume na roho ya Ukweli na utakatifu wa kweli. Lazima ujifunze kukuza adabu, staha na uungwana katika kuzungumza kwa kiasi. Nafsi lazima itiishwe na kuwekwa katika utii. Mkristo hataendelea katika ugomvi na malumbano hata na wale waovu kabisa na wasioamini. Je, ni kosa kubwa kiasi gani kutamani hii roho kwa wale wanaoamini Ukweli na wanaotafuta amani, upendo, na maelewano! Anasema Paulo: “Iweni na amani ninyi kwa ninyi.” Hii roho ya malumbano inapingwa na kanuni zote za kimbingu. Katika hubiri la KRISTO juu ya mlima anasema: ‘Heri wapatanishi maana wataitwa wana wa MUNGU.’ Heri wenye upole maana watairithi nchi.” Wewe utapata shida kila uendapo, isipokuwa umejifunza somo ambalo MUNGU amepanga wewe kujifunza. Jitumaini kidogo na



kutoweka/usiweke mbele maoni yako mwenyewe na umiliki roho inayofundishika, ile ya mwanafunzi. “Yeye ambaye si mwepesi wa hasira ni mwema kuliko shujaa, na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atekaye mji.” “Yeye asiye mwepesi wa hasira ni wa ufahamu mwingi, bali mwenye roho ya hamaki hutukuza upumbavu.” Anasema Yakobo: “Kwa hivyo ndugu zangu wapenzi, kila mtu awe mwepesi wa kusikia, si mwepesi kusema, si mwepesi wa hasira: maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya MUNGU.” {2T 163.2}

Roho ya kujiamini mwenyewe ipo ikidumu katika maisha yako. Endapo ungekuwa na uzoefu hakika zaidi katika mambo ya MUNGU, basi ungetambua kwamba matunda unayozaa ni mabaya. Hayana lishe lakini yanajaza uchungu wale wote ambao huyatumia. Ni lazima ushinde ujeuri wako, roho ya udikteta. Nina matumaini makubwa, kaka yangu mpendwa, kwamba wewe, ambaye umeonesha kuwa na ujasiri wa maadili kumkabili adui ndani yako mwenyewe, utapambana kwa ushujaa na adui wa tamaa/hamu ya chakula na tabia zenye nguvu za uovu ambazo zimekufunga kama kwa kamba za chuma, zitatumika kufanya kazi hapa na kupata ushindi. Umekuwa na roho isiyo na tahadhari, na kutojali, kwani umehisi kwamba hakuna hata mmoja anayekujali, wewe, kwamba karibu kila mtu alikuwa adui yako, na hivyo hukujali kitakachotokea -liwalo na liwe. {2T 164.1}

Ukweli umekukuta ukiwa hauna furaha. Uliona ndani yake nguvu ambayo ingekuina na kukupa nguvu ambayo hukuwa nayo. Ulishika miale ya nuru iliyokuangazia juu yako; na kama sasa utajitoa nafsi yako kwa ukamilifu ili kuongozwa nayo, itakuongoa kabisa na kukutakasa, na kukuandaa kwa hatua za mguso wa mwisho katika safari ya kutokufa. Unazo sifa nyingi za tabia nzuri; una moyo wa ukarimu. MUNGU anakutaka uwe sahihi, yaani sahihi tu. Haupo tayari kuambiwa au kuelekezwa. Unataka uwe ndiwe mtoa amri au dikteta pekee. Lakini lazima uwe mnyenyekevu, mwenye roho ya kufundishika, na mwenye urafiki, mvumilivu, mstahimilivu, aliyejaa upole na rehema. {2T 164.2}

Tuna shauku ya kutaka mema kwako, na tunataka kukusaidia, ninaomba upokee mistari hii kwa moyo sahihi, na uiache kwa uzuri iguse moyo wako na maisha. {2T 165.1}

Mwitikio

Dada White,

Shuhuda Niliyopokea Jana Nauchukulia Kama Karipio Zuri Linalostahili Ambalo Najisikia Kwa Kweli Kukushukuru Kwa Dhati. Natumaini Kuwa Mshindi. Nimetambua Kikamilifu Ukubwa Wa Kazi Ninayotakiwa Kufanya, Ila Naamini Kwamba Kwa Msaada Wa Neema Ya Mungu Nitaweza Kushinda. {2T 165.2}

## SURA YA 26

### WABEBA MIZIGO KATIKA KANISA

Wapendwa kaka na dada N: June 12, 1868, nilioneshwa baadhi ya mambo yakiwarejelea nyie. Mna kazi ya kufanya lakini hamuioni; hamjawa wabeba mizigo. Mnapaswa kuwa na shauku kubwa katika kazi na kusudi la MUNGU kuliko mfanyavyo. Mmepofushwa sana na kupenda dunia hata hamuoni ni ushawishi mkubwa kiasi gani, huu ulimwengu unao juu yenu. Hamuoni kwamba uzito maalumu wa majukumu upo juu yenu, wala hamtambui umuhimu wa muda na kazi inayotakiwa kukamilishwa. Mpo kama watu waliolala usingizi. Umoja ni nguvu. Kuna udhaifu mkubwa katika kanisa kwa sababu ndani yake kuna walio nyuma ambao hawachukui mizigo. Nyie siyo watenda kazi na KRISTO. Roho ya udunia inafungia mioyo yenu mivuto ambayo ile Kweli ingefanya. {2T 165.3}

Ni muhimu kwamba wote sasa waamke na waje kazini na watende kama watu wenye uhai, wakitumika kwa wokovu wa roho zinazopotea. Kama wote ndani ya kanisa wangeamka na kuja kumsaidia BWANA, tungeona vile uamsho wa kazi Yake kama ambavyo hutujapata kuona hata sasa. MUNGU anataka hili kwenu na kwa kila mshiriki wa kanisa. Haijaachwa kwako kuamua ikiwa ni vema kwako kutii wito wa MUNGU. Utii unatakiwa; na isipokuwa umetii utasimama juu pabaya kuliko kutokuwepo upande wowote (neutral). Isipokuwa umependelewa kwa Baraka ya MUNGU, wewe unayo laana Yake. Yeye Anakutaka wewe kuwa tayari na mtii, na asema utakula mema ya nchi. Laana kali imetamkwa juu ya wale ambao hawaji kumsaidia BWANA. "Ulaaniwe Meroz, alisema malaika wa BWANA, walaani kwa uchungu wakazi wake kwa maana hawakuja kumsaidia BWANA, kumsaidia BWANA juu ya wenye nguvu. Waamuzi 5:23-25" Shetani na malaika zake wapo katika uwanja wa pambano kupinga kila hatua ya kwenda mbele ambayo watu wa MUNGU wanachukua, kwa hiyo msaada wa kila mtu unahitajika. {2T 165.4}

Kaka na dada N, ushawishi wa marafiki wasioamini unawaathiri zaidi nyinyi, kuliko mnavyotambua. Hawawaletai nguvu, bali giza na

kutokuamini. Mnayo kazi binafsi kila mmoja katika shamba la BWANA. Mmefikiri na kujijali wenyewe kwa kupitiliza sana, nafsi zenu. wekeni mioyo yenu katika utaratibu, na kisha muwe katika bidii. Jiulize: “BWANA, Je, unataka mimi nifanye nini?” MUNGU anataka toka kwenu bidii ya kumtafuta Yeye. Anawabidisha mjichunguze mioyo yenu wenyewe kwa makini ili kugundua yote yanayozuia uzaaji wenu wa matunda mengi, na kile ambacho kitabakia. Kinachosababisha msiwe na ROHO wa MUNGU zaidi ni kwa kuwa hambebi kwa furaha msalaba wa KRISTO. Katika maono ya mwisho niliona mlidanganywa kutokana na nguvu ya kupenda kwenu dunia. Shughuli na masumbufu ya maisha haya na udanganyifu wa mali vinasonga Neno, na mnakuwa hamzai matunda. MUNGU anatutaka tuzae matunda mengi. Yeye Hatatoa amri pasipo kuzipa nguvu ya kufanya kufanya kazi zake. Yeye Hatafanya sehemu ya kazi yetu, wala Yeye kutaka tufanye Yake. Ni MUNGU afanyaye kazi ndani yetu. Lakini, ni lazima sisi tuufanyie kazi wokovu wetu wenyewe kwa hofu na kutetemeka. “Imani kama haina matendo, imekufa” ikiwa yenyewe, imani lazima itegemezwe kwa matendo; wale watendao, au wenye utendaji, wanahesabiwa haki mbele za MUNGU. Hamumpendezi MUNGU katika kuzungumzia umaskini wenu, ili hali mnavyo tele. Vyote mnavyomiliki ni mali Yake, bado ameona vyema kuwafanya nyie wakili wa hiyo kwa muda mfupi, Yeye anawajaribu na kuwathibitisha, je, mtastahimilije huu mtihani? Yeye Atataka ya Kwake, na faida. {2T 166.1}

Mmekaza macho yenu juu ya kile mlichotoa kwa mipango mbalimbali, na kinaonekana kikubwa kwenu. Lakini mngefanya mengi sana zaidi, kama mngepanua mioyo yenu, na mikono yenu ingetolewa kwa kusudi la MUNGU na kwa wahitaji, mngekuwa msingefanya zaidi ya wajibu wenu, na mngekuwa na furaha zaidi. BWANA ana wito juu yenu kuleta sadaka madhabahuni, na siyo kuishikilia kibindioni ili isifikiwe, lakini iwekwe katika madhabahu. Madhabahu hutakasa sadaka wakati inapowekwa juu yake na siyo kabla. {2T 167.1}

Hamjajitenga na ulimwengu kama MUNGU anavyowataka kuwa, lakini hamuoni na kuelewa hatari yenu. Mnapotoshwa kwa kupenda kwenu dunia. Nyote wawili mnahitaji kuchimba chini katika chemchemi ya Ukweli. Isipokuwa mtafanya kuja katika hali tofauti ambapo

mtamheshimu MUNGU kwa ushawishi wenu na vitu vyenu, vinginevyo laana Yake itakuja juu yenu. Mnaweza kukusanya, lakini Yeye atatapanya. Badala ya afya yenu kuchipua haraka, mtakuwa kama tawi lililonyauka. BWANA anaita watendakazi ---watu ambao wanaweza na watatambua moyoni wokovu wa roho, na watatoa chochote ili waokolewe. Hakuna mwingine yeyote anayeweza kufanya kazi hii kwa ajili yenu, sadaka za wengine, hata kama zitakuwa za ukarimu sana, haziwezi kuchukua nafasi ya za kwenu. Ni kujisalimisha kwa MUNGU ndicho mnachotakiwa kufanya, jambo ambalo, hakuna mwingine anayeweza kufanya kwa ajili yenu. Ni nguvu ya ROHO pekee ikifanya kazi kupitia imani yenye nguvu ambayo inaweza kuwafanya muweze kwa mafanikio kuzuia mitego mingi Shetani aliyoiweka kwa ajili ya miguu yenu. Maneno na mfano wa Mwokozi vitakuwa nuru na nguvu ya mioyo yenu. Kama mtamfuata na kumwamini Yeye, Hatawaacha mpotee. Mnaiogopa mno chuki ya wale ambao hawampendi na kumtumikia MUNGU. Kwa nini mnataka kutunza urafiki wa maadui wa BWANA wenu au kushawishiwa na maoni yao? Je, hamjui kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa MUNGU?" kama mioyo ingekuwa sahihi, kungekuwa na maamuzi zaidi ya kujitenga na ulimwengu. {2T 167.2}

BWANA angefanya kazi kubwa na njema katika eneo hili la karibu, majira ya machipuko yaliyopita ingekuwa wote wameona hitaji la hii kazi na kuja kumsaidia BWANA. Hakukuwa na umoja katika utendaji. Wote hawakuona umuhimu wa kazi na kujihusisha kwayo kwa moyo. Kulikuwa hakuna kuyasalimisha yote kwa MUNGU. Mlioneshwa kwangu kuwa mnasumbuliwa na kufadhaishwa, ukungu wa giza ukikusanyika juu yenu. Mlikuwa mkiuliza na hamkuwa katika nafasi ya kupokea nguvu ninyi wenyewe wala kuitoa kwa wengine. Ni wakati wa kuogofya kabisa. Hakuna muda sasa wa kuthamini sanamu, hakuna sehemu kwa ajili ya mapatano na Beliali au kwa ajili ya urafiki na ulimwengu. Wale ambao MUNGU anawakubali na kuwatakasa kwa ajili Yake wanaitwa kuwa na bidii na uadilifu katika huduma Yake, wakiwa wametakaswa na kujitoa Kwake. Siyo mfano wa utauwa wala jina juu ya kumbukumbu za kanisa, ambayo hufanya "Jiwe lililo hai" katika jengo la ROHO. Ni kufanywa upya katika maarifa na utakatifu wa Kweli, kusulubishwa kwa ulimwengu na kufanywa hai katika KRISTO, ndiko kunakounganisha roho kwa MUNGU. Wafuasi wa KRISTO wana lengo

moja linalowaongoza katika mtazamo, kazi moja kubwa: wokovu wa wanadamu wenzao. Maslahi mengine yoyote, lazima yawe chini/duni kwa hili; inatakiwa kuhusisha bidii kubwa zaidi na nia ya ndani kabisa. {2T 168.1}

MUNGU kwanza anataka moyo, mapenzi. Yeye Anataka wamfuatao wampende na kumtumikia kwa mioyo yao yote, kwa roho zao zote, kwa nguvu zao zote. {2T 168.2}

Amri Zake na neema zinaratibiwa kutokana na mahitaji yetu, na bila hizo, hata tufanye chochote tuwezacho kufanya, hatuwezi kuokolewa. Anataka Utii kamili. Sadaka ya vitu, au huduma yoyote, haitakubaliwa bila moyo. Nia/Mapenzi, ni lazima yasalimishwe. BWANA anataka kutoka kwenu kujiweka wakfu kukubwa Kwake na kujitenga kukubwa kutoka kwa roho na ushawishi wa ulimwengu. {2T 169.1}

“Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya MUNGU, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani, mkaingie katika nuru Yake ya ajabu” KRISTO amewaita ninyi kuwa wafuasi Wake, kuiga maisha Yake ya kujitoa nafsi na kujikana nafsi, na kuvutiwa katika kazi kubwa ya ukombozi wa jamii ya ubinadamu iliyoanguka. Hamjatambua tu kazi ambayo MUNGU anawataka kufanya. KRISTO Ndiye Mfano wetu. Kile ambacho ninyi mmepungukiwa ni upendo. Kanuni hii safi na takatifu inatofautisha tabia na mwenendo wa Wakristo kutoka kwa watu wa ulimwengu. Pendo la MUNGU lina nguvu ya ushawishi utakasao. Unapatikana katika mioyo iliyofanywa upya pekeee, na kwa asili hutiririka nje kwa wanadamu wenzao. {2T 169.2}

“Pendaneni ninyi kwa ninyi,” anasema Mwokozi wetu, “kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna mtu mwenye upendo mkubwa kama huu, kwamba mtu atoe maisha yake kwa ajili ya rafiki yake.” KRISTO ametupa kielelezo safi cha upendo usio na ubinafsi. Hamjaona bado upungufu wenu katika suala hili, na hitaji lenu kubwa kwa hili kufika mbinguni, bila hilo madhumuni yenu yote mazuri, na usongo/ari yenu, hata kama ikiwa ya namna ile kwamba mnetoa mali zenu kuwalisha maskini na miili yenu kuchomwa moto, ni bure tu. Mnahitaji ule upendo

na ukarimu, ambao huvumilia yote, haufanyi haraka kukasirika, hustahimili yote, huamini yote, hutumaini yote, huvumilia yote. Bila roho ya upendo, hakuna anayeweza kuwa kama KRISTO. Kwa hii kanuni iishiyo rohoni, hakuna anayeweza kuwa kama ulimwengu. {2T 169.3}

Mwenendo wa Wakristo ni kama ule wa BWANA wao. Yeye Alisimika kiwango, nacho kimeachwa kwetu kuzungumza, iwapo tutakifuata au hatutakifuata bado tutakuwa nacho daima. BWANA na Mwokozi wetu aliacha pembeni enzi Yake, utajiri na utukufu, na alitutafuta sisi, ili atuokoe kutoka katika taabu na kutufanya sisi kama Yeye. Yeye Alijinyenyekeza na kuchukua asili yetu ili tuweze kujifunza Kwake, na kuiga maisha Yake ya ukarimu na kujikana nafsi, na kumfuata hatua kwa hatua kwenda mbinguni. Hamwezi kuwa sawa na nakala; lakini mnaweza kufanana nayo na kulingana na uwezo wenu, kufanya sawasawa na hiyo. “Mpende BWANA, MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.” Upendo kama huo lazima uishi ndani ya mioyo yenu, ili muwe tayari kutelekeza hazina na heshima za ulimwengu kadri muwezavyo ikiwa itasaidia kushawishi hata roho moja kujihusisha katika huduma ya KRISTO. {2T 169.4}

MUNGU anawaagiza kwa mkono mmoja wa imani, shikilia mkono Wake wenye nguvu, na kwa mkono mwingine, wa upendo, zishikeni roho zinazopotea. KRISTO ni Njia, Kweli, na Uzima. Mfuateni Yeye. Msitembee kwa kufuata mwili, bali kwa kufuata ROHO. Enendeni kama alivyoenenda. Haya ndiyo mapenzi ya MUNGU, hata kutakaswa kwenu. Kazi mtakiwayo kufanya ni kufanya mapenzi Yake Yeye anayetegemeza maisha yenu kwa utukufu Wake. Kama mkifanya kazi kwa ajili ya nafsi zenu, haitawafaidia kitu. Kufanya kazi kwa manufaa ya wengine, kuacha kujijali wenyewe zaidi kwa dhati, kutoa yote kwa MUNGU, kutakubaliwa Kwake na kurejeshwa kwa utajiri wa neema Yake. {2T 170.1}

MUNGU hajawapa/hajawagawia mgawo wenu kwa ajili tu ya kukodolea macho na kujali nafsi zenu. Mnatakiwa kuhudumu, na kuangalia wengine, na katika zoezi hili mtaonesha yale maovu katika tabia

ambayo huhitaji kusahihishwa, na itaimarisha zile sehemu dhaifu zinazohitaji kutegemezwa na kuimarishwa. Hii ni sehemu ya kazi tunayotakiwa kufanya; siyo bila subira, kwa wasiwasi na kuudhika, na kwa kulazimishwa, lakini kwa uchangamfu, furaha, kwa ajili ya kufikia ukamilifu wa Kikristo. Kuondoa kutoka kwetu kila kitu ambacho hatukubaliani nacho au hakitupendezi, siyo kumuiga KRISTO.

Mnatakiwa kuwa na wivu mkubwa kwa ajili ya heshima ya MUNGU. Kwa makini jinsi gani mnatakiwa ninyi kutembea kwa hekima, na tahadhari, pale ambapo sasa njia yenu haipo kama ilivyotakiwa kuwa. Kama mngewaona malaika safi na macho yao ya kung'aa, macho ya kuchunguza kwa umakini yamekazwa juu yenu, wakiangalia kuweka kumbukumbu jinsi Mkristo anavyomtukuza BWANA Wake; au mngeweza kutazama na kufarahia, ushindi wa kejeli wa malaika waovu, wakielezea kila njia iliyopotoka, na wakinukuu Maandiko yaliyokiukwa na kulinganisha maisha kwa Maandiko ambayo mnakiri kuyafuata lakini mnayakiuka, mngeshangazwa na kushtushwa wenyewe. Inachukua mtu mzima kumfanya Mkristo mjasiri. Oh, sisi ni vipofu kwa kiasi gani, viumbe wenye uoni mfupi! Kwa udogo kiasi gani tunatambua vitu vitakatifu, na kwa udhaifu jinsi gani tunaelewa utajiri wa neema Yake! {2Tsw 170.2}

Jambo moja nataka liguse mioyo na akili zenu. Mnao mawakala maalumu wa Shetani ambao wameunganishwa karibu nanyi, na nguvu zao na ushawishi wao una athari inayoonekana juu yenu. Kwa sababu hambaki karibu vya kutosha na MUNGU, kuhakikisha msaada maalum wa malaika wakuu na wenye nguvu. Umoja wenu kwa pamoja una nguvu zaidi na maadui wa BWANA wenu, na hamtambui kuwa mpo katika hatari ya kufanya uharibifu wa imani yenu. Kama mtahimiza, kwa udogo tu, majaribu ya Shetani, basi mtajiweka wenyewe juu ya uwanja wa vita, na kisha pambano litakuwa refu na la kuumiza kabla hamjapata ushindi na shangwe kwa Jina la YESU, ambaye amemshinda Shetani. {2Tsw 171.1}

Shetani ana faida nyingi. Alimiliki nguvu ya akili ya ajabu ya malaika, ambayo wachache tu hujenga wazo lolote. Shetani alijua uwezo wake, ama sivyo, asingejihusisha katika vita na MUNGU Mwenye nguvu,



BABA wa milele, na Mfalme wa Amani. Shetani hutazama kwa karibu matukio, na pindi anapompata mmoja ambaye kwa njia ya kipekee ana nguvu ya roho wa upinzani kwa Ukweli wa MUNGU, atafunua kwake hata matukio ambayo hayajatimizwa, ili aweze zaidi kujihakikishia kiti katika moyo wake. Yeye ambaye hakusita kuthubutu kupambana na Yeye anayeshikilia uumbaji katika kiganja Chake, ana uovu wa kuogofya katika kutesa na kudanganya. Anashikilia watu katika mtego wake wakati wa sasa. Katika uzoefu wake wa karibu miaka elfu sita, adui hajapoteza stadi, ujuzi, hila, ulaghai au hata ujanja wake wowote. Wakati wote huu amekuwa mtazamaji wa karibu wa yote yanayohusu pambano letu sisi, jamii ya wanadamu. {2Tsw 171.2}

Wale ambao wamepinga Ukweli wa MUNGU kwa ukali, Shetani huwatumia kama mawakala wake. Kwa hao atatokea katika mtu dhaniwa na mavazi ya mwingine, yaweza kuwa rafiki wa wakala. Ataongeza imani yao kwa kutumia maneno ya huyu rafiki na kuhusianisha mazingira ambayo yanakaribia kutokea au ambayo kweli yametokea na ambayo wakala hakuyajua. Wakati mwingine kabla ya kifo au ajali anatoa ndoto au, hujifananisha na mtu mwingine, anazungumza na wakala, hata kumfundisha maarifa kwa njia ya mapendekezo yake. Lakini ni hekima kutoka chini (kuzimu) na siyo kutoka juu. Hekima inayofundishwa na Shetani inapingwa na Ukweli, isipokuwa, kutumikia makusudi yake, anaonekana kujivisha yeye mwenyewe kwa nuru ambayo hufunika malaika. Kwa kundi fulani la akili, adui atakuja akiidhinisha sehemu ya kile wafuasi wa KRISTO wanaamini kuwa Ukweli, wakati akiwaonya kukataa sehemu nyingine kama hatari na kosa baya la fundisho la imani (error). {2Tsw 172.1}

Shetani ni gwiji katika kazi. Hekima yake ya kuzimu huitumia kwa mafanikio mazuri. Yupo tayari na anaweza kufundisha wale ambao wanakataa mashauri ya MUNGU dhidi ya roho zao wenyewe. Chambo alichokipata kitafaulu katika kuleta roho ndani ya wavu wake. Ili aweze kukaza ufahamu wake wa kuzimu juu yao, atajivika kwa kila uzuri unaowezekana na kufanya uvutie iwezekanavyo. Kwa hivyo wote ambao wamenaswa, watajifunza kwa gharama kubwa upumbavu wa kuuza mbingu na kutokufa kwa udanganyifu ambao ni mbaya sana katika matokeo yake. Mshitaki wetu, Shetani, siyo mtupu kwa hekima

au nguvu. Huzunguka kama simba aungurumaye, akimtafuta wa kummeza. Atatenda “Katika uwezo wote na ishara na ajabu za uongo, na kwa udanganyifu wote usio haki kwa wanaopotea; kwa sababu hawakupokea kuipenda ile Kweli, ili waweze kuokolewa.” Kwa sababu walikataa Ukweli, “MUNGU ataachilia kwao udanganyifu wenye nguvu, ili wauamini uongo: ili wote waangamizwe ambao hawakuamini Ukweli, lakini walijifurahisha katika udhalimu.” Tuna adui mdanganyifu, mwenye nguvu, wa kupambana naye, na usalama wetu pekee ni katika Yeye ambaye Anakuja, ambaye Atamuangamiza huyu mdanganyifu mkuu kwa uwezo mdomoni Mwake, na kumharibu na mwangaza wa kuja Mwake. {2Tsw 172.2}

Ninawawasilisha hili kwenu katika kicho cha BWANA (hofu ya Mungu), na kuwaomba muamke kutoka katika wafu, na KRISTO atawapa uzima. {2Tsw 173.1}

## SURA YA 27

### KIBURI NDANI YA VIJANA

Mpendwa dada O: ilikuwa nia yangu kuwa na mazungumzo na wewe kabla ya kuondoka---lakini nilizuiwa na vitu vingi. Siandiki kwa hisia za matumaini kwamba barua hii barua inaweza kufanya badiliko lolote maalumu katika mwenendo wa tabia yako kufikia hapa kama uzoefu wa dini yako unavyohusika. {2Tsw 173.2}

Nimejisikia huzuni sana kuhusu wewe. Katika mkutano uliofanyika ----, nilifuata kanuni za jumla, na kufikiri kufikia mioyo kwa kutoa shuhuda ambayo nilitumaini ingeleta badiliko katika maisha yako ya kidini. Nimejaribu kuandika, kama ilivyotolewa katika Shuhuda Na. 12, kuhusu hatari za vijana. Mtazamo huo ulioupata Rochester. Huko nilioneshwa kuwa kosa limefanywa katika mafunzo yako tangu utoto wako na miaka ya kuendelea. Wazazi wako walifikiri, na wamezungumzia hili ukisikia, kwamba ulikuwa Mkristo wa asili. Dada zako walikuwa na upendo kwako, ambao ulipelekea ibada ya sanamu zaidi kuliko utakaso. Wazazi wako wamekuwa na pendo lisilotakaswa kwa watoto wao, ambalo limewapofusha macho yao katika kasoro zao. Wakati mwingine, wanapokuwa wamezinduka kwa kiasi fulani, huwa tofauti. Lakini umekuwa ukidekezwa, ukibembelezwa na kusifiwa kwa udanganyifu mpaka maslahi yako ya umilele yamehatarishwa. {2Tsw 173.3}

Niliona kuwa hujifahamu mwenyewe. Una haki yako binafsi ambayo inakufunga katika udanganyifu kuhusu mafanikio yako ya kiroho. Wakati mwingine umehisi namna ya ushawishi wa ROHO wa MUNGU. Lakini kuhusu mabadiliko yenye kufanya upya akili, wewe ni mgeni. “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya MUNGU yaliyo mema, ya kupendeza, na ukamilifu” haujawa na huu uzoefu, kwa hiyo hauna nanga. Wewe siyo Mkristo, na bado imekuwa ikizungumzwa kwako katika maisha yako yote kwamba ulikuwa Mkristo wa asili. Umelichukulia hili kama jambo la kawaida kwamba wewe ulikuwa sahihi, wakati ulikuwa mbali sana na kukubaliwa na MUNGU. Huu

udanganyifu umekua kimo, na wakati ulipoendelea kukua, na kuimarishwa na nguvu zako, hali hii inatishia kuthibitisha uharibifu wako. Wazazi wako wameona wivu kwa watoto wao, na pale taarifa ya kutoheshimiwa, inapoletwa na watoto wao, wamehisi kuvutwa na kuisimka mara moja, na wamewaonea watoto huruma, na kusimama moja kwa moja katika njia ya mafanikio yao kiroho. {2Tsw 174.1}

Wewe na dada yako P mmekuwa na kiasi kikubwa cha kiburi, ambacho kitakuwa kama mabua tu, katika siku ya MUNGU. Kujipenda nafsi na kiburi cha nafsi, kiburi cha mavazi na kutaka kujionyesha kwa watu, vimewashinda. Ubinafsi umewatenga na wema. Wote wawili lazima muwe na uongofu kamili, upya kamili wa akili, badiliko kamili, la sivyo hamtakuwa na sehemu katika ufalme wa MUNGU. Mwonekano wenu, kupendeza kwenu-uzuri wenu wa sura, mavazi yenu, havitawaletea kibali kwa MUNGU. Ni thamani na sifa ya maadili ambayo MIMI NIKO anatazama. Hakuna uzuri halisi wa mtu au wa tabia nje ya KRISTO, hakuna ukamilifu wa Kweli, adabu au tabia bila neema itakasayo ya roho ya unyenyekevu, huruma, na utakatifu wa kweli. {2Tsw 174.2}

Nimeoneshwa kuwa roho zitapotea kupitia ushawishi na mfano wenu. Mmekuwa na nuru na upendeleo, na kwa hivyo mtatoa hesabu. Ninyi siyo wanadini kwa asili au watu wa ibada, lakini mnatakiwa kufanya juhudi maalum, ili kuweka akilini mwenu vitu vya dini/kiroho. Ubinafsi umewatawala. Kujithamini kwenu ni kukubwa mno (self esteem); lakini kumbukeni kwamba mbingu zinatazama thamani ya maadili, na kupima tabia kama ni njema na ya thamani kwa mapambo ya ndani, na mvuto binafsi, haya yote yanazama chini kwa kutokuwa muhimu katika kujilinganisha kwa yale mafanikio ya thamani, yaani pambo la roho ya upole na utulivu, hakika hayo ndiyo yana thamani kubwa mbele za Mungu. Kupenda kwenu kujifurahisha na kujiridhisha, kukosa kwenu utakaso na uchaji Mungu, kumekuwa uharibifu kwa wengi. Wale waliokuwa wamerudi nyuma hamkuweza kuwafaa, maana maisha yenu yalikuwa kama ya walimwengu kiujumla. {2Tsw 175.1}

Wale wanaotembelea----- wanabeba mvuto uliotengenezwa na ninyi na vijana wengine ambao hawafurahii dini yenye vitendo, kwamba hakuna uhalisia katika dini. Kiburi kinaimarishwa ndani yao; kupenda

kujionesha, kupenda mambo ya upuuzi na anasa vinaongezeka, na mambo matakatifu hayatambuliwi. Wanapokea wazo kwamba wamekuwa waangalifu sana kwamba dhamiri zao zimenolewa mno, wamejali mambo kwa kinagaubaga sana (too particular). Ikiwa wale wanaoishi katikati ya kazi nzito ya utumishi wa Mungu wanashawishiwa kidogo sana na zile Kweli za makini zinazowasilishwa mara kwa mara sana, kwa nini wao basi wawe waangalifu au makini au wajali sana? Kwanini wao waogope kujifurahisha nafsi zao, wakati hii imeonekana kuwa lengo la wale wenye uzoefu mrefu katika-----? {2Tsw 175.2}

Ushawishi wa vijana katika----- unaenea pote kule wanapofahamika, na maisha yao yasiyo na utauwa ni msemu wa huko; na hakuna wale ambao wana ushawishi wenye mwelekeo usio sahihi kuliko ninyi. Mmeidhalilisha Imani kwa kukiri kwenu kwa mdomo na kuwa wawakilishi duni wa ile Kweli. Anasema Shahidi wa Kweli: “Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto, ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi kwa sababu u uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu.” Kama mngekuwa baridi, basi pangekuwa na matumaini kwa kiasi fulani kwamba mngeongoka; lakini wakati ambapo kujihesabia haki kumemfunga mtu kwa mkanda, badala ya haki ya KRISTO, udanganyifu unakuwa mgumu sana kuonekana, na kujihesabia haki ni kugumu sana kuwekwa pembeni, hivyo kwamba ufikiaji kwa mtu, unakuwa ni mgumu mno. Yule asiyeongoka, na asiyemjua MUNGU, anasimama katika hali nzuri zaidi kuliko huyo. {2Tsw 175.3}

Wewe ni kikwazo kwa wadhambi. Kukosa kwako kicho, ibada na kujitoa wakfu, kumewekwa alama. Unatawanya kutoka kwa KRISTO badala ya kukusanya pamoja Naye. Kama MUNGU atanisaidia kupasua mavazi yako ya kujihesabia haki, ningetumaini kwamba bado ungekomboa wakati na kuongoza kwa maisha ya mfano bora. Umekuwa ukipata uamsho wa mara kwa mara, na hakika mara zingi umeshindwa kusimama, na kurudi katika hali yako ya awali ya kutofanya kitu chochote na kujihesabia haki, una jina la kuwa hai wakati umekufa. Kiburi chako kinatishia kuwa uharibifu wako. MUNGU amezungumza na wewe juu ya hii mada. Kama hamfanyi matengenezo,

taabu itakuja juu yenu, na furaha yenu itageuzwa kuwa huzuni, mpaka mnyenyekeze mioyo yenu chini ya mkono wa MUNGU. Maombi yenu MUNGU hayakubali. Yanatoka katika mioyo iliyojaa kiburi na ubinafsi. Wewe, dada yangu mpendwa, unashugulika na vitu batili-vya kipuuzi, unakimbiza upepo tu; umeishi maisha yasiyo na malengo, wakati, ungekuwa mnyenyekevu na kuishi kubariki wengine, ndipo ungekuwa mbaraka kwako mwenyewe na wote karibu yako. Acheni MUNGU awasamehe wazazi wako na dada zako kwa sehemu waliyotenda kukufanya wewe jinsi ulivyo—Vile tu ambavyo MUNGU hawezi kukubali, vile tu ambavyo, kama utabaki hivyo hivyo, utakuwa mabua kwa ajili ya moto, kukuteketeza katika siku ya MUNGU (hukumu). {2Tsw 176.1}

Wakati nilipooneshwa kuhusu roho ya ubinafsi iliyopo ndani ya wale waliokuwa wakifanya kazi latika ofisi, kwamba kulikuwa na baadhi ambao walikuwa wakifanya kazi kwa ajili ya mshahara tu, kana kwamba wanajihusisha katika biashara ya kawaida, wote wawili mlikuwa miongoni mwa idadi hiyo. Wote wawili mlikuwa wabinafsi na kujijali nafsi tu. Hamu yenu ilikuwa kujifurahisha nafsi zenu na kujipatia mshahara mkubwa. Roho hii imelaani ofisi kwa kiwango kikubwa hasa, na mbingu hukunja uso juu yake. Wengi wamekuwa na hamu sana ya kujipatia mali. Haya yote ni makosa. Roho ya udunia imeingia ndani ya moyo, na KRISTO amefungiwa nje, MUNGU awaonee huruma watu Wake. Na natumaini utaoongolewa. . . {2Tsw 176.2}

Mmemiliki roho ya mizaha, na mmekuwa na mazungumzo ya kipuuzi na yasiyo na maana. Oh, ni adimu kiasi gani mmemtaja YESU! Upendo Wake unaookoa haujaleta mwitikio wa shukrani na sifa, na onyesho na maelezo yaliyokusudiwa kulitukuza Jina Lake na upendo wa kujikana nafsi usiokoma. Nini imekuwa mada ya mazungumzo yenu? Mawazo gani yamekuwa yakiwaleteeni furaha kubwa? Katika ukweli yaweza hata hakusemwa kwamba ni YESU na maisha Yake ya kujitoa, neema Yake nyingi ya thamani na ukombozi alioufanya vinakuwa nadra sana mawazoni mwenu. Mapenzi makubwa kwa ajili yako, ni adimu katika mawazo yenu yote; lakini vitu visivyo na maana vinaijaza akili yenu. Kujipendeza nafsi zenu, kukamilisha vitu katika maisha ambavyo vinapatana na anasa zenu, hili ndiyo mzigo wa akili yenu. Nachoweza kufanya ni kutamani tu kwamba ‘msingekiria kuhusu kufufuliwa na

KRISTO', kwa maana hamjakidhi vigezo Vyake. "Basi mkiwa mmefufuliwa na KRISTO, yatafutani yaliyo juu KRISTO aliko, ameketi mkono wa kuume wa MUNGU. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na KRISTO katika MUNGU" Jiulizeni wenyewe maswali: Je, nimetimiza vigezo vilivyowekwa hapa na mtume aliyevuviwa? Je, nimedhihirisha kwa maisha yangu, kifo changu kwa ulimwengu, kwamba maisha yangu yamefichwa na KRISTO katika MUNGU? Je, nimezama ndani ya KRISTO? Je ninajitwalia uzima wangu na msaada kutoka Kwake Yeye aliyeahidi kuwa kwangu msaada wa karibu katika kila wakati wa uhitaji? Ninyi mna dini ya mapokeo, lakini hamna ufahamu maalum wa udhaifu wenu, ufisadi wenu, na uovu wenu kwa asili. {2Tsw 177.1}

"Mkristo wa asili! 'Mkristo wa kuzaliwa' Wazo hili la udanganyifu limesaidia wengi kuwa kama vazi la kujihesabia haki binafsi, na limewaongoza wengi katika tumaini dhanifu katika KRISTO, wale ambao hawakuwa na ufahamu wa kimatendo au uhalisia kuhusu Yeye, ya uzoefu Wake, majaribu Yake, maisha Yake ya kujikana nafsi, na kujitoa nafsi. Haki yao ambayo wanaitegemea sana ni kama tu matambara machafu na mabovu tu. Anasema KRISTO, Mwalimu mpendwa: "Yeyote akitaka kunifuata, na ajikane nafsi, na auchukue msalaba wake, na anifuata." Ndiyo, mfuate Yeye kupitia mabaya, kadhalika kupitia taarifa njema. Mfuate katika kufanya urafiki na walio wahitaji sana na wasio na marafiki. Mfuate katika kuisahau nafsi, kupitia matendo tele ya kujikana nafsi na kujitoa kukana kiburi cha ujana na kuwatendea wengine mema; ukitukanwa, usirudishe tusi, oneshwa upendo na huruma kwa jamii ya ubinadamu, iliyoanguka. Yeye Hakuhesesabu maisha Yake kuwa kitu, lakini aliyatoa kwa ajili yetu sote. Mfuate kutoka horini mpaka msalabani, Yeye Alikuwa mfano wetu, Yeye Anakuambia, ili uwe mwanafunzi Wake, ni lazima ubebe msalaba uliodharauliwa, na umfuate Yeye. Je, unaweza kukinywea kikombe? Je, unaweza ukabatizwa kwa ubatizo? {2Tsw 177.2}

Matendo yenu yanashuhudia kwamba ninyi ni wageni kwa KRISTO (watu baki), "Je chemchemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu? Ndugu zangu, Je, mtini waweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa tini? Kadhalika chemchemi haiwezi kutoa maji ya

chumvi na maji matamu. Nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aoneshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri, katika upole/unyenyekevu wa hekima. Lakini, mkiwa na wivu wenye uchungu na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uongo juu ya ile Kweli. Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia ya tabia ya kibinadamu, yenye tamaa chafu kama za uasherati na Shetani. Maana hapo palipo na wivu na ugomvi ndipo palipo na machafuko, na kila tendo baya. Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ni ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina/ubaguzi, haina unafiki. Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao Amani.” {2T 178.1}

Hapa yameorodheshwa matunda ambayo ni ushahidi uliowekwa alama kuwa mtu ambaye amekuwa akitembea katika nguvu ya maisha, amekutana na badiliko--- badiliko lililowekwa alama kama kuwakilishwa na kifo. Kutoka kuishi, maisha yenye utendaji hai, mpaka kifo! Mtu wa kushangaza namna gani! Hakuna anayehitaji kudanganywa hapa. Kama badiliko hili halijawapata ninyi, basi msitulie. Mtafuteni BWANA kwa mioyo yenu yote. Fanyeni hili kuwa kazi muhimu sana ya maisha yenu. {2T 178.2}

Muna hesabu na maelezo ya kutoa kwa mema mtakayokuwa mmefanya wakati wa maisha yenu, kama mngekuwa katika sehemu ambayo kwayo MUNGU alitaka muwe, na ambayo Yeye amefanya majaliwa ya utoaji wa kutosha ambayo mnaweza kuchukua. Lakini mmeshindwa kumtukiza MUNGU juu ya dunia, na kuokoa roho karibu yenu, kwa sababu hamkutaka kufaidishwa wenyewe kwa neema na nguvu, hekima na ufahamu, ambavyo KRISTO ametoa kwa ajili yenu. Mlijua mapenzi Yake, lakini hamkufanya, hapo itahitajika badiliko kubwa linaloonekana ndani yenu nyote wawili, ama hamtasikia kamwe kutoka kwa YESU: “vema, mtumwa mwema na mwaminifu.” {2T 179.1}

Katika jioni ya Juni 12, baada ya kusoma yaliyotangulia kanisani, nilioneshwa kuwa wakati mkiwa hamjali, wenye kiburi, wenye kujigamba, wabinafsi, na msiojali wokovu wa roho, kifo kinafanya kazi yake. Mmoja baada ya mwingine anawaacha, na kwenda kaburini. Upi, umekuwa ushawishi wenu juu ya wale ambao wamekusanyika katika



makusanyiko yenu ya kijamii? Nini kimekuwa kikizungumzwa au kufanywa ili kuongoza roho kwa KRISTO? Je, mmekuwa tayari kwa wakati unaofaa na usiofaa, kufanya wajibu wenu wote? Je, mpo tayari kukutana katika hukumu ya MUNGU na wale ambao mmehusiana nao katika makusanyiko yenu ya kijamii, hasa lile kundi ambalo limetupwa chini ya ushawishi wenu na ambao wamekufa nje ya KRISTO? Je, mmejiandaa kabisa kusema kwamba majirani zenu hawana damu zao kwenye nguo zenu kama lawama kwenu? Nitaorodhesha tukio moja, lile la Q. Je, lawama haitaanguka juu yenu kutoka Kwake? Juu yenu ninyi mliozungukwa kwa ushawishi mzuri wa nyumbani, nyie ambao mlikuwa na kila fursa ya kufaa kuendeleza tabia nzuri za Kikristo, lakini ambao mmeshindwa kuona mzigo kwa ajili ya roho za watu? Kiburi, ubatili, na kupenda anasa vilikuzwa nanyi, kisha mlifanya sehemu yenu katika kuaibisha kukiri kwenu na kuongoza hii roho maskini, ambayo ilikuwa imetupwa na kubamizwa na Shetani, kutilia shaka uhalisi wa Ukweli na udhati wa dini ya Kikristo. {2T 179.2}

Mazungumzo yenu ya kijinga, sawa na yale ya vijana wengine, yalikuwa yachukizayo. Hakukuwa na maadili bora na kuinuliwa, katika upande ambao akili zenu zilielekea, dhihaka, umbea, ujinga, vichekesho vya bure, futuhi, mzaha, na utani. Malaika wameandika matukio mliyoyafanya tena na tena. Bila kujali kusihiwa kwa miito ya dhati kabisa kulikofanywa kwenu, na mmekuwa mkikemewa, na kuonywa, mnalaumika sana kuliko vijana wengine. Mmekuwa na uzoefu mkubwa na ufahamu mkubwa wa ile Kweli. Mmeishi kwa muda zaidi katika---, mlikuwa miongoni mwa wale wa kwanza kukiri kuamini Ukweli na kuwa wafuasi wa KRISTO, na njia yenu ya ubatili na kiburi imetenda zaidi katika kutengeneza uzoefu wa vijana katika eneo hilo kuliko ilivyo kwa wengine wowote. Wale ambao wameongoka kwa Ukweli mmewashikwa kwa mkono, kama ilivyokuwa, na kuwanganishwa na ulimwengu. {2T180.1}

Hatia kubwa inakaa juu yenu na pia juu ya wazazi wenu, ambao wamewapaka mafuta kwa chupa ya mgongo, wakiwasifia kwa kuwadanganya na kiburi chenu na upumbavu wenu. Wamewahurumia mlipokemewa, na wamewapa ninyi fikra ya kutambua kwamba hamkustahili makemeo hayo. Wewe, dada O, umejifikiria mwenyewe

kuwa u mrembo. Wazazi wako wamekusifia. Umfanya urafiki na wasioamini. Kando na kukiri kwako, matendo yako yamekuwa yasiyomstahili msichana mwenye busara na mnyenyekevu. Lakini inapozingatiwa kwamba unakiri kuwa mfuasi wa KRISTO mpole na mnyenyekevu, umeaibisha ushuhuda wako. O dada yangu, Je ulifikiri wale makarani wasingeweza kuelewa kuhusu rangi ya mdomo uliyopaka au usanii/uigizaji unaofanya? Ulifikiri wamevutiwa na sura yako nzuri kwamba wasingeweza kuona ndani na kusoma Ukweli wa tabia yako bandia/feki? Wakati ulipoweka juu ya kichwa chako mapambo ulioazima kutoka kwa duka la dada R, na kisha kujipitisha-pitisha mwenyewe kama vile upo kwenye maonesho mbele ya wale makarani, ulifikiri hii haikugunduliwa? Je, ulisahau kuwa malaika wa MUNGU walihudhuria, na kwamba macho yao masafi yalikuwa yakisoma mawazo yako, na nia na madhumuni ya moyo? Na kutambua kila tendo, na kuelezea ukweli wako, na tabia ya kijinga? Wakati ulipojichosha na mazungumzo yako yasiyo na maana kwa karani wa kiume ambaye wewe ulivutiwa naye, kwa sababu alitia chumvi kuusifia upuuzi wako, ungeweza kusimama mbele ya kioo cha kujitazama, na kuweza kuona ishara za mikono au kichwa, na kunong'oneza, miongoni mwa wale waliokuwa wanakutazama, na kukucheka kwa sababu ulikuwa ukifanya onesho la kipumbavu. Ulikuwa unatia doa juu ya kazi ya ile Kweli. Laiti ungeweza kuingia hilo duka bila kuonekana, muda mfupi baada kutoka nje, na usikie mazungumzo baada ya kusubiri kwa kadri ustaarabu ungeweza kuruhusu, ungeweza kujifunza vitu fulani ambavyo hukufikiri kamwe hapo kabla. Ungejeruhiwa na kunyenyekezwa kujua jinsi ulivyokuwa ukitazamwa hata na makarani wajinga. Yule yule aliyekusifia usoni pako, alijiunga katika kuangua kicheko na kukung'ong'a kwa rafiki zake juu ya mwenendo wako wa k i p u u z i . { 2 T 1 8 0 . 2 }

Unaweza kuwa na ushawishi wa wema katika---- na kumheshimu Mkombozi wako. Lakini badala ya hili umejifanya mwenyewe kuwa gumzo, kebehi za sifa za uongo kwa makarani ambao ni vijana wadogo, ambao hata hawana ndevu. Mwenendo huu usiofaa umesemwa na wengi sana, na wale waliotambua huku kutofautiana na utata, japokuwa waweza kuwa siyo waumini, na wanaonesha heshima kwako, wanakudharau ndani ya mioyo yao. Unafuata hatua za S, na isipokuwa

wazazi wako wameamka na kufumbua macho yao kuona upumbavu wako, watashiriki hatia yako. Dhambi ipo juu yao na juu ya dada zako kwa njia waliyoichukua katika kukuza kiburi chako na kusifia ubatili wako. Kama wewe na dada zako mngekuwa katika hali ya kuokolewa, wote mngeona hali ya hatari ya watu wasiookoka. Siku inakuja, isipokuwa badiliko kubwa limefanywa ndani yenu, wakati mtakaposikia toka kwa midomo ya wengi. “Nilijihusisha na hawa Wakristo, ila kamwe hawakuniambia hatari yangu. Hawakunionya, niliwaza kwamba kama nilikuwa katika hatari ya kupotea, wasingetulia usiku au mchana bila kuniamsha, ili nione hali yangu ya kupotea. Sasa nimepotea. Kama ningelikuwa katika nafasi yao na ningemuona mmoja katika hali sawa na hii, nisingetulia mpaka nimewafanya waelewe hali yao na kuwaelekeza kwa Yule mmoja pekee anayeweza kuwaokoa. “Mmekuwa watumishi wa Shetani bora na wa kupendeza wakati mmekiri kuwa wafuasi wa KRISTO.” {2T 181.1}

Dada O, umeinuliwa juu sana kwa heshima machoni pako mwenyewe kiasi kwamba hukuwa na busara ya kutathmini watazamaji walivyoweka uduni juu ya tabia yako. Wanakuhesabu wewe ni mtu mwenye kutongoza wanaume na umejipatia kwa haki sifa hii (coquette). Ingekuwa faida kubwa zaidi kwako kusikiliza ushauri wa mtume: “kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje;.... Bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za MUNGU” {2T 182.1}

Wazazi wenu wamefeli mno katika elimu ya watoto wao. Wamewaruhusu kutobeba mizigo ambayo ilikuwa muhimu kwao kubeba. Kwa sababu wameamua kujifurahisha nafsi zao, waliwaruhusu kubaki kitandani, kulala fofofu wakati wa masaa mema na ya kupendeza ya asubuhi, Wakati wazazi kwa uvumilivu walikuwa wameshaamka, wakihenyeka na mihangaiko ya maisha. Hawa watoto hawajajifunza kuzuia vitu vinavyowavutia, kupambana na matamano yao; hawajajifunza kuvumilia ugumu. Wamekuwa wakiachwa kwa kipimo kikubwa kubeba mizigo nyumbani, na hii imekuwa ni jeraha kwao. Hawajajifunza kamwe tendo la kuondoa ubinafsi, kujikana nafsi na kujitoa nafsi.

hawakubali kufanya kazi ambayo hawaipendi, ambayo siyo ya ladha yao. Elimu yao ina mapungufu makubwa. Ila bado wana kiburi---ubatili, kiburi cha majigambo/kujisifu—kinajaza mioyo yao. Dada O amejiona bora kuliko rafiki zake au wenzake, kwamba hawastahili kupewa usikivu, adabu, uungwana na kuheshimiwa nao. Kwa hili ana matakwa ya ukaidi, kufanya kama appendavyo bila kujali matakwa ya wengine, mahitaji ya wengine au hata kwamba anawaletea wengine usumbufu. Mwonekano wa uso wake, siyo wa furaha, tabia ambayo, isipokuwa aishinde, itasababisha vivuli vingi na kutia giza njia yake na hata kudondosha uchungu maishani mwa marafiki zake wakubwa. {2T 182.2}

## **SURA YA 28**

### **HALI YA UDUNIA KATIKA KANISA**

Wapendwa ndugu na dada mnamo juni 12,1868 nilioneshwa kwamba kupenda dunia kulikuwa kwa kiwango kikubwa kunachukua nafasi ya kumpenda MUNGU. Mpo katika nchi ya kupendeza, ambayo ina fursa ya maendeleo ya kidunia. Hii inawaweka mahali palipo na hatari daima, kwa maslahi yenu kumezwa na shauku ya ulimwengu, katika kuweka hazina zenu juu ya dunia. Mioyo yenu itakuwa mahali hazina zenu zilipo. Mmekaa mahali palipo na majaribu na ni rahisi kutumbukia ndani zaidi na zaidi katika ulimwengu, ili muendeleo kujilimbikizia mali; na mnapojishugulisha hivyo, akili hutingwa na pilikapilika za maisha haya , kiasi cha kuufungia nje utauwa wa kweli. Lakini ni wachache tu wanatambua udanganyifu wa mali. Wale ambao wana tamaa ya kupata mali wamejipinda/wamejikita sana juu ya hili jambo moja hata kufanya dini ya KRISTO kuwa jambo lisilo na maana au la pili. Mambo ya kiroho hayathaminiwi na hayatafakariwi, kwa maana kupenda faida kumetia kivuli na hazina ya mbinguni. Kama zawadi ya uzima wa milele ingethaminiwa kwa ari, dhati, uvumilivu, na kwa bidii kuoneshwa na wale wanaokiri kuwa Wakristo, isingekuwa hata na nusu ya

thamani kama mali za kidunia. Linganisha juhudi za dhati zilizofanywa kupata vitu vya dunia kwa ulegevu, na udhaifu, na bidii isiyo fanisi ya kupata hazina ya kiroho na kimbingu. Tusione ajabu basi tunapopata uzoefu mdogo na mvuto wa nuru kutoka hekalu la mbinguni. Matamania yetu hayapo katika huo uelekeo; mara nyingi yamefungiwa katika harakati za kidunia, kutafuta vitu vya kiulimwengu, na kupuuzia vile vya umilele. Mafanikio yanapofusha macho na kudanganya roho. MUNGU anaweza kuzungumza, ila upuuzi na takataka za dunia huzuia sauti Yake kusikiwa. {2T 183.1}

Baba yetu mzee T, mapenzi yake yapo juu ya vitu vya dunia hii wakati yalitakiwa yawe yameondolewa hapa duniani na kuanza kuiva kwa ajili ya mbingu. Maisha ambayo anaishi sasa anatakiwa kuishi kwa imani katika MWANA WA MUNGU; upendo wake unatakiwa kuwa juu ya nchi bora. Anatakiwa kuwa na kiasi kidogo cha hamu katika hazina za dunia ziharibikazo, wakati mambo ya milele, ambayo ni ya matokeo makubwa, yangukuwa maslahi ya kwanza na yote kwake. Siku zake za rehema zipo karibu kuisha. Oh, ni muda mchache kiasi gani umebaki ili kujitoa kwa MUNGU! Nguvu zake zimepungua na uchovu na akili yake imeharibika, na katika ubora wake huduma zake zitakuwa dhaifu; bado kama zitatolewa kwa moyo na ukamilifu, zinakubalika kabisa. Kwa umri wako, kaka T, limekuja ongezeko la ubinafsi na upendo imara na mkali, na kuwa dhati kwa kupenda hazina za ulimwengu huu maskini, kumeongezeka. {2T 184.1}

Dada T. anaupenda huu ulimwengu, kwa asili ni mbinafsi na mchoyo. Ameteseka sana kwa maradhi ya mwili. MUNGU aliruhusu huu ugonjwa kuja juu yake, na bado hajamruhusu Shetani kuchukua maisha yake. MUNGU alipanga kupitia tanuru la maradhi na maumivu kulegeza kushikilia kwake juu ya hazina za kidunia. Kupitia mateso pekee, hili laweza kufanyika. Ni mmoja wa wale ambao mfumo wao umetiwa sumu kwa madawa (ya famasia). Kwa kutumia hizi amejiletea hali yake kuwa hivyo bila kujua, yaani kwa ujinga; bado MUNGU hakuacha maisha yake yachukuliwe, lakini amerefusha miaka ya rehema na kuteseka ili aweze kutakaswa kupitia ile Kweli, afanywe safi, afanywe

mweupe na kujaribiwa/kuthibitishwa, na kupitia tanuru la ugonjwa, basi uchafu uchujwe (taka au kile kisicho chuma kiungue), na awe wa thamani zaidi kuliko dhahabu safi, hata zaidi kuliko kipande cha dhahabu ya ofiri. Kupenda dunia kumeota mizizi katika moyo wa kaka na dada hawa na utahijika mtihani mkubwa kubwa kuondoa hili. Wapendwa kaka na dada, mnapungukiwa na kujitoa wakfu, utauwa, uchaji MUNGU-ibada. Ninyi ni wenda-wazimu kwa mambo ya kidunia. Ulimwengu una nguvu ya kubadilisha akili yenu kwake, wakati ya kiroho na kimbingu hayabebi uzito wa kutosha, kubadili akili zenu. {2T 184.2}

Wanaume na wanawake huko ----- ambao wanakiri kuwa wafuasi wa KRISTO, kwa nini hamumfuati Yeye? Kwa nini mnaonesha ujuha/uwendawazimu, kujitwalia hazina ya kidunia, ambayo majanga yanaweza kuziondoa kwa urahisi, na mnapuuzia utajiri wa mbinguni, ambao ni kutokufa, na hazina isiyoharibika? {2T185.1}

Nilioneshwa tukio la mke wa ndugu U. Ana matamanio ya kufanya kilicho sahihi, lakini ana mapungufu ambayo yanamsababishia yeye na rafiki zake shida nyingi. Anaongea kwa kupitiliza (mno). Hana uzoefu katika mambo ya MUNGU, na isipokuwa ameongoka na kubadilika kwa kufanywa upya akili, hataweza kusimama katikati ya hatari ya siku za mwisho. Kazi ya moyo inahitajika. Kisha ulimi utakuwa umetakaswa. Kuna mazungumzo mengi ambayo ni dhambi na ni lazima yaepukwe. Anatakiwa kuweka ulinzi mkali mbele ya mlango wa midomo yake na kufunga ulimi wake kama kwa lijamu, ili maneno yake yasiweze kutenda uovu. Anatakiwa kuacha kuzungumza makosa ya wengine, kuzungumza kwa muda mrefu upekee wa wengine, na kugundua madhaifu ya wengine. Mazungumzo kama hayo yanakatazwa juu ya mtu yeyote. Hayana faida na ni dhambi kabisa. Huelekea kwenye uovu tu. Adui anajua kwamba kama hii njia itafuatwa na watu waliomkiri KRISTO, inamfungulia mlango kwa ajili yake kutenda kazi. {2T 185.2}

Niliona kwamba wakati kina dada ambao wamepewa kuongea wanapokuwa pamoja, Shetani kwa ujumla yupo, maana hupata kibarua. Husimama karibu ili kulisimua akili na kutumia kwa kiasi kikubwa fursa aliyoipata. Anajua uvumi wote huu, umbea, kusengenya na kufunua siri, na kukata-kata tabia na visu tabia ya mtu, naye

hutenganisha roho toka kwa MUNGU. Huleta kifo cha roho na ushawishi mtulivu wa kidini. Dada U anatenda dhambi sana kwa ulimi wake. Angetakiwa kwa maneno yake kuwa na ushawishi wa wema, lakini mara kwa mara anaongea hovy-hovy. Wakati mwingine maneno yake yameweka au kujenga kwa namna tofauti juu ya vitu kuliko ambavyo hali ilivyo. Wakati mwingine hutia chumvi mambo. Halafu kuna mkanganyiko wa kauli. Hadhamirii kukanganya kauli, lakini tabia ya kuongea sana na kuongea juu ya vitu visivyo na faida kwa muda mrefu kumethaminiwa hata amekuwa hajali na si mwangalifu katika maneno yake, na mara kwa mara yeye mwenyewe hajui anaongea nini. Hii huharibu ushawishi wowote wa wema anaoweza kuwa nao. Ni wakati wa kuwa na matengenezo kamili katika jambo hili. Jamii yake haijathaminiwa kama ambavyo ingeweza kuwa, kama asingeendekeza haya mazungumzo ya dhambi. {2T 185.3}

Wakristo lazima wawe waangalifu kuhusiana na maneno yao. Kamwe wasibebe taarifa mbaya kutoka kwa mmoja wa marafiki na kuzipeleka kwa mwingine, hasa pale wanapotambua kuwa watu hao hawana umoja kati yao. Ni ukatili kudokeza na kusingizia, kana kwamba unajua mambo mengi kuhusu huyu rafiki au yule rafiki ambayo wengine hawajui. Madokezo hayo yanaenda mbali, na kutengeneza mivuto mibaya, zaidi ya kusema kwa uwazi ukweli bila ya kutia chumvi. Ni madhara ya kiasi gani ambayo kanisa la KRISTO limeumizwa kutoka katika vitu hivi! Njia isiyolindwa ya washiriki na isiyo na upatanifu, imelifanya kanisa kuwa dhaifu kama maji. Imani imesalitiwa na washiriki wa kanisa lile-lile, na bado yule mtu aliyekuwa na hatia hakujipanga kifikra kuumiza mtu. Kupungukiwa hekima katika chaguzi za mada za mazungumzo kumeleta maaumivu makubwa. Mazungumzo lazima yawe juu ya mambo ya kiroho na matakatifu; lakini hili limekuwa kinyume chake. Kama mahusiano na marafiki Wakristo yanaelekezwa kuboresha akili na moyo, basi hapo patakuwa hakuna majuto baadaye, na watu wanaweza wakatazama nyuma mahojiano yao kwa roho ya kuridhishwa. Lakini kama masaa yatatumiwa katika mzaha na mazungumzo yasiyokuwa na faida na ubatili tu, ni kupoteza muda bure. Hivyo muda wa thamani unatumiwa kupekua maisha na tabia za wengine, mahusiano ya kirafiki

yataonesha chanzo cha uovu, na ushawishi wenu utakuwa harufu ya kifo hadi kifo. {2T 186.1}

Siwezi kwa hakika kukumbuka watu wote katika kanisa lenu ambao nilioneshwa; lakini niliona kuwa wengi walikuwa na kazi kubwa ya kufanya. Kuna kuzungumza kwa kupindukia, karibu kwa wote, na kiasi kidogo cha tafakari na maombi. Kwa wengi kuna ubinafsi mkubwa. Akili imejitoa kwa nafsi/ubinafsi na siyo kwa faida ya wengine. Nguvu ya Shetani ipo juu yenu kwa kiwango kikubwa. Bado kuna nuru ya thamani miongoni mwenu, na wale ambao wanatafuta kutembea kulingana na mapenzi ya MUNGU. Kiburi na kupenda dunia ni mitego ambayo ni vizuizi vikubwa vya kiroho na kukua katika neema. {2T 187.1}

Ulimwengu huu siyo mbingu ya Wakristo, lakini ni karakana tu ya MUNGU, mahali ambapo tunatengenezwa ili kufaa kuungana na malaika wasio na dhambi katika mbingu takatifu. Tunapaswa mara zote kuzoesha akili katika mambo bora/mema na mawazo yasiyo ya ubinafsi. Elimu hii ni lazima iletwe katika utendaji, uwezo ambao MUNGU ametupa ili Jina Lake liwezwe kutukuzwa juu ya dunia kwa uzuri zaidi. Tunawajibika kwa sifa njema na bora ambazo MUNGU ametupatia sisi, na kuweka uwezo huu katika matumizi ambayo hakuyapanga tufanye, ni kuonesha hali ya kushuka chini na kutoonyesha shukrani Kwake. Huduma ya MUNGU inahitaji uwezo wote wa maisha yetu, na tunashindwa kufikia mpango wa MUNGU isipokuwa tumeleta uwezo huu katika uboreshaji, na kuelimisha akili kupenda kutafakari mambo ya kimbingu, na kuimarisha na kuwezesha nguvu ya nafsi kwa matendo sahihi, ikifanya kazi kwa utukufu wa MUNGU. {2T 187.2}

Wanawake wanaokiri utauwa kwa jumla wanashindwa kuifundisha akili. Wanaicha bila kuitawala, ili iende inapotaka. Hili ni kosa kubwa. Wengi wanaonesha kutokuwa na nguvu ya akili. Hawajaielimisha akili kufikiri; na kwa sababu hawajafanya hili, wanadhani hawawezi. Tafakari ya Maandiko na maombi ni lazima kwa ukuaji katika neema. Kwa nini hakuna uimara zaidi miongoni mwa wanawake, ni kwa sababu ya uchache wa kuifunza-kuipalilia Nidhamu ya akili, uchache wa tafakari na kuakisi. Kuiacha akili katika hali ya kutoshugulishwa (\*kuithibiti akili



kwa kuiadabisha isikae bure, kuipalilia), wanategemea juu ya wengine kufanya kazi yao ya akili, kupanga, kufikiri, na kukumbuka kwa ajili yao, na hivyo wanaendelea zaidi na zaidi kuifanya akili isiwe na ufanisi. Baadhi wanahitaji kufunza akili kwa kuifanyia mazoezi. Wailazimishe akili kufikiri. Wakati wanapomtegemea mtu fulani kufikiri kwa ajili yao, kutatua magumu yao, wakikataa kuishugulisha akili kwa tafakari, kutokuwa na uwezo wa kukumbuka, basi kuangalia mbele ya udunia ndani ya kanisa na kutofautisha kutaendelea. Juhudi lazima ifanywe na kila mmoja kuelimsha akili. {2T 187.3}

Nilioneshwa kaka V unatakiwa kutafuta kuwa wa kiroho zaidi. Hauna tumaini tulivu katika MUNGU ambalo Yeye anataka uwe nalo. Hauifundishi akili yako kupita katika mkondo/chaneli za mambo ya kiroho. Lazima uhimize utulivu na uvumilivu wa akili. Unaendelea mazungumzo mengi yasiyo na maana, yenye ubatili tu, ambayo huumiza roho yako mwenyewe na kuharibu ushawishi wako. Lazima uhimize utulivu na ujasiri wa akili. Unasisimshwa kwa urahisi; una hisia kali, na unaonesha katika msimamo mkali yale uyapendayo na usiyoyapenda. Unahitaji dini nzuri zaidi ili kuwa na ushawishi mtulivu juu yako. Wewe umekaribishwa kujifunza KRISTO, ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo. Funzo la thamani! Kama utajifunza vyema, itabadilisha maisha yote. Upuuzi na mazungumzo yasiyo maana ni uharibifu kwa maendeleo yako ya kiroho. Unatakiwa kutafuta ukamilifu wa tabia na acha mvuto wako umtangaze MUNGU katika maneno na matendo yako. Unahitaji kumtafuta BWANA kwa dhati, na kuchota kwa kina katika chemchemi ya Kweli, ili kwamba mvuto wake utakase maisha yako. Akili yako ipo sana katika dunia. Unatakiwa kuwa na hamu katika maisha bora kuliko haya. Hauna muda wa kupoteza; fanya haraka na uboreshe machache katika masaa haya ya rehema. {2T 188.1}

Mke wako amekuwa na kiburi mno na mbinafsi. MUNGU amekuwa akimleta kupitia tanuru la ugonjwa ili kuondoa haya madoa katika tabia yake. Lazima awe mwangalifu kwamba moto wa ugonjwa usije ukawashwa juu yake bure. Moto unatakiwa uondoe uchafu na kumsogeza karibu na MUNGU, kumfanya awe wa kiroho zaidi.

Kupenda kwake dunia lazima kufe. Kujipenda nafsi lazima kushindwe na mapenzi yake yamezwe ndani ya mapenzi ya MUNGU. {2T 188.2}

Nilioneshwa kuwa kupenda dunia kwa kiasi kikubwa kumemfungia YESU kutoka kanisani. MUNGU anataka mabadiliko, kusalimisha yote Kwake. Isipokuwa akili imeelimishwa kukaa juu ya mandhari ya kidini/kiroho, itakuwa duni na dhaifu katika mwelekeo huu. Lakini wakati inakaa juu ya shuguli za kidunia, itakuwa na nguvu, maana kwa mwelekeo huu imefundishwa, na imejiimarisha kwa kuzoezwa. Sababu ya kuwa vigumu kwa wanawake na wanaume kuishi maisha ya kidini ni kwa sababu hawaizoezi akili katika utauwa. Akili imefundishwa kutenda katika uelekeo kinzani. Isipokuwa akili imezoezwa katika kupata ufahamu wa kiroho na katika kutafuta kuelewa siri ya utauwa, haiwezi kuthamini vitu vya milele kwa sababu haina uzoefu katika uelekeo huo. Hii ni sababu kwa nini karibu wote wanachukulia kuwa ni mpando mgumu kumtumikia BWANA. {2T 189.1}

Wakati moyo unapokuwa umegawanywa, ukikaa zaidi juu ya vitu vya dunia, na kidogo tu juu ya vitu vya MUNGU, hapo hapatakuwa na ongezeko maalumu la nguvu ya kiroho. Mashirika ya kidunia yanadai sehemu kubwa ya akili, yakiita utendaji wa nguvu zake; kwa hiyo katika uelekeo huu kuna nguvu na uwezo wa kutaka zaidi na zaidi shauku na mapenzi, wakati kidogo na kidogo kinatunzwa kwa kutolewa kwa MUNGU. Haiwezekani kwa roho kunawiri wakati maombi siyo zoezi muhimu la akili. Maombi ya familia au jamii pekee hayatoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana, katika faragha, roho inaanikwa wazi kwa jicho la uchunguzi la MUNGU, na kila nia inapekuliwa/inachunguzwa. Ni ya thamani jinsi gani Maombi ya siri! Roho inawasiliana na MUNGU! Ombi la siri lisikiwe tu na MUNGU, Msikia- maombi. Hakuna sikio dadisi linatakiwa kupokea mzigo wa maombi kama hayo. Katika maombi ya faragha roho ipo huru kutoka ushawishi unaozunguka, huru kutoka katika msisimko. Kwa utulivu, ila kwa dhati, maombi yatamfikia MUNGU. Ombi la faragha mara kwa mara linapotoshwa, na madhumuni yake matamu kupotezwa kwa maombi ya sauti ya juu. Badala ya utulivu, ukima na tumaini la kimya na imani katika MUNGU, roho inazamishwa chini, sauti nyenyekevu, sauti inapandishwa katika kiwango cha juu na msisimko unaendekezwa, na kisha ombi la faragha

linapoteza utulivu wake, na mvuto mtakatifu. Kuna tufani ya hisia, tufani ya maneno, inayofanya isiwezekane kutambua sauti tulivu, sauti ndogo ambayo huongea na roho wakati imeshiriki faragha yake, ibada ya moyoni ya Kweli. Ombi la siri likifanyika kwa usahihi lina tija kubwa. Lakini ombi linalofanywa wazi kwa familia yote na majirani, siyo ombi la faragha, hata kama litafikiriwa hivyo, na nguvu ya kimbingu haipokelewi kutoka kwa ombi la namna hiyo. Matokeo mazuri na endelevu yatakuja, yanayotoka kutoka kwa Yeye Aonaye sirini, ambaye sikio Lake lipo wazi kujibu ombi linalokuja kutoka moyoni. Kwa utulivu, imani sahili ishikwayo na roho, huwasiliana na MUNGU na kukusanya Kwake miali ya mwanga wa kimbingu, kuimarisha na kuitegemeza roho kustahimili mapambano ya Shetani. MUNGU ni nguzo/mhimili wa nguvu yetu. {2T 189.2}

YESU ametuachia sisi Neno “Kesheni basi, kwa maana hamjui ajapo bwana wa nyumba, kwamba ni jioni, au kwamba ni usiku wa manane, au awikapo jimbi, au asubuhi, asije akawasili ghafula akawakuta mmelala. Na hilo niwaambialo ninyi, nawaambia wote, kesheni”. Tunasubiri na kutazamia, marejeo ya BWANA, ambaye ataleta mapambazuko, asije kuja kwa ghafula na akatukuta tumelala. Ni muda gani hapa unaorejelewa? Siyo kwa ufunuo wa KRISTO katika mawingu ya mbinguni kuwakuta watu wamelala. Hapana; bali katika kurejea Kwake katika huduma Yake katika Patikatifu mno pa hekalu la mbinguni, wakati anapovua mavazi Yake ya kikuhani na kujivisha Mwenyewe mavazi ya kisasi, na wakati tamko linapotoka: “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu, na mwenye uchafu azidi kuwa mchafu, na mwenye haki azidi kufanya haki, na mtakatifu na azidi kutakaswa.” {2T 190.1}

Wakati YESU atakapokoma kuomba kwa ajili ya watu, mashauri ya watu wote yatakuwa yameamriwa. Huu ni muda wa kutoa hesabu kwa watumishi Wake. Kwa wale ambao wamepuuza matayarisho ya usafi na utakatifu utakaowastahilisha wao kuwa wanaosubiri kumkaribisha BWANA wao, jua linazama katika giza, nalo giza ni nene nalo halichomozi tena. Mlango wa rehema unafungwa na maombezi ya KRISTO yanakoma mbinguni. Muda huu, mwisho huja ghafla juu ya wote na wale ambao wamepuuza kutakasa roho zao kwa kutii Ukweli,

nao wanakutwa wamelala. Walikuwa wamechoka kusubiri na kukesha, wakawa wasiojalii kuhusiana na ujio wa BWANA wao. Hawakutamani kutokea Kwake, na wakafikiri hakukuwa na haja ya kuendelea kuvumilia kwa kiasi hicho na kukesha. Walikuwa wamekatishwa tamaa katika matarajio yao na wakawa wasiojali kuhusu ujio wa Bwana wao tena. Walihitimisha kwamba kulikuwa na muda wa kutosha bado kuamka. Wangehakikisha kutopoteza fursa ya kupata hazina ya kidunia. Ingekuwa salama kupata yote ya ulimwengu huu kadri wawezavyo. Na katika kupata lengo hili, walipoteza shauku yote na matamano katika kutokea kwa BWANA wao. Wakawa wasiozingatia na kutojali kana kwamba ujio Wake ulikuwa bado mbali. Lakini wakati hamu yao ilipozika juu ya faida za kiulimwengu, kazi ilifungwa katika Patakatifu-hekalu la mbinguni na walikuwa hawajajiandaa. {2T 191.1}

Kama hao wangetambua kwamba kazi ya KRISTO katika hekalu la mbinguni ingefungwa mapema sana, ni tofauti kiasi gani wangeenenda, na kwa dhati kiasi gani wangekesha! BWANA akijua kuhusu kutokea kwa haya yote, Anawapa onyo kwa wakati muafaka katika amri ya kukesha. Kwa usahihi anatamka uharaka wa ujio Wake. Hataji muda ili tusije tukapuuzia maandalizi ya wakati uliopo na katika uzembe wetu tukatazama mbele katika muda tunaodhani atakuja na kuhairisha maandalizi. “Kesheni basi: kwa maana hamjui” bado maneno haya yameeleza kutokuwa na uhakika wa siku ya kuja kwa Bwana, na dharura-au jambo la ghafla, na mwishowe kushindwa kutuamsha kutoka ujingani na kukesha kwa dhati na kuboresha kukesha kwetu kwa ajili ya BWANA wetu anayetarajiwa. Wale wasiokutwa wakisubiri na kukesha mwishowe watashangazwa katika kutokuwa waaminifu kwao. BWANA anakuja, na badala ya wao kuwa tayari kumfungulia haraka, wamefungiwa katika usingizi wa kidunia na mwishowe wanapotea. {2T 191.2}

Kuna kundi lililoneshwa mbele yangu tofauti na lile lililoelezewa. Walikuwa wakisubiri na kukesha. Macho yao yalikuwa yameelekezwa Mbinguni, na Maneno ya BWANA wao yalikuwa midomoni mwao. “Niyasemayo kwenu nayasema kwa wote, kesheni” “kesheni basi kwa maana hamjui ajapo bwana wa nyumba kwamba ni jioni au kwamba ni usiku wa manane au awikapo jimbi, au asubuhi. Asiye akawasili ghafla,

akawakuta mmelala” BWANA anataarifu kuchelewa kabla ya asubuhi kucha. Lakini hatawaruhusu kuchoka wala kulegeza kukesha kwao kwa dhati kwa sababu tu asubuhi haifunguki kwao mapema kama walivyotarajia. Watu wanaosubiri walioneshwa kwangu kama wakitazama juu. Walikuwa wakitiana moyo kwa kurudia maneno haya: “kesha la kwanza na la pili yamepita. Tupo katika kesha la tatu, tukisubiri na kukesha kwa ajili ya marejeo ya BWANA. Umebakia muda mchache wa kukesha sasa.” Niliwaona baadhi wakichoka; macho yao yalielekezwa chini na walizingwa na/kwa mambo ya dunia na hawakuwa waaminifu katika kukesha. Walikuwa wakisema: “katika kesha la kwanza tulimtegemea BWANA wetu, lakini tulikatishwa tamaa. Tulidhani hakika atakuja katika kesha la pili, lakini hilo lilipita, Naye hakuja. Tunaweza tena tukakatishwa tamaa. Hatuhitaji kuwa mahsusi/bainishi sana kuhusu saa. Yeye Anaweza asije katika kesha lijalo. Tupo katika mkesha wa tatu na sasa tunafikiri ni vyema kuweka hazina zetu duniani ili tuweze kuwa salama dhidi ya uhitaji” wengi walikuwa wanalala, wakilemewa na masumbufu ya maisha haya na kutekwa na udanganyifu wa mali kutoka katika kusubiri na nafasi ya kukesha kwao (\*Wayahudi waligawa masaa ya usiku katika Mikesha minne -kuanzia saa 12 jioni mpaka saa tatu usiku, mkesha wa kwanza. Kuanza saa tatu ya usiku mpaka saa sita ya usiku mkesha wa pili, kuanza saa sita ya usiku mpaka saa tisa ya usiku, mkesha wa tatu, na kuanzia saa tisa ya usiku mpaka saa kumi na mbili asubuhi, mkesha wa nne). {2T 192.1}

Malaika waliwakilishwa kwangu wakitazama kwa shauku na uangalifu mkali ili kutambua uwepo wa wale waliokuwa wamechoka lakini bado walikuwa wakeshaji waaminifu, wasije wakajaribiwa vikali na kuzama chini ya kazi ngumu na magumu yakazidishwa maradufu kwa sababu ndugu zao wamekengeuka katika kesha lao na kulewa kwa masumbufu, na mafaniko ya ulimwengu. Hawa malaika wa mbinguni walihuzunishwa kwamba wale ambao hapo kwanza walikuwa wakikesha, kwa uzembe na kutokuwa na uaminifu kwao wameongeza majaribu na udunia kwenye mizigo ya kanisa kwa wale ambao kwa dhati na uvumilivu walikuwa wakijitahidi kudumisha subira na kukesha. {2T 193.1}

Niliona kwamba ilikuwa haiwezekani kabisa mtu kuwa na mapenzi na maslahi yaliyokita katika shughuli za kiulimwengu, mambo ya kuongeza mali za kidunia na bado akawa katika kungojea na hali ya kukesha kama Mwokozi wetu alivyoamuru. Alisema malaika. "Wanaweza kupata ulimwengu mmoja tu, lakini ili kupata hazina ya mbinguni, lazima waiache dunia. Hawawezi kuwa na malimwengu yote mawili-They can't have both worlds." Niliona jinsi kuendelea kuwa mwaminifu kulivyo kwa lazima katika kukesha ili kuepuka mitego danganyifu ya Shetani. Adui anawaongoza wale ambao wanapaswa kungoja na kukesha kuchukua hatua mbele, ili kuchukua hatua moja nyingine, kuelekea ulimwenguni; hawana nia ya kwenda mbali lakini ile hatua moja iliyowaondoa mbali zaidi kutoka kwa KRISTO, inafanya iwe rahisi kuchukua hatua nyingine mbali Naye; na hivyo hatua baada ya hatua inachukuliwa kuelekea ulimwenguni, mpaka tofauti zote kati yao na ulimwengu ni tamko la kukiri kwa mdomo tu, jina tu. Wamepoteza upekee wao, tabia takatifu, na hakuna kitu isipokuwa tamko lao la mdomo tu, kuwatofautisha wao kutoka kwa wapenda dunia kati yao. {2T 193.2}

Niliona kwamba mkeshi baada ya mkeshi ulikuwa katika wakati uliopita. Kwa sababu ya hili, Je, pawe na kukosa uangalifu wa kuwa macho? Oh, hapana! Kuna ulazima mkubwa wa kutokukoma ukeshaji, maana sasa wakati ni mchache kuliko kabla ya kupita keshi la kwanza. Sasa kipindi cha kusubiri kwa ulazima ni kifupi kuliko hapo kwanza. Kama tulikesha kwa uangalifu bila kukoma, ni kwa kiasi gani zaidi, hitaji la kuzidisha, [maradifu kwa mkeshi/ukeshaji] katika keshi la pili linahitajika. Kupita kwa keshi la pili kumetuleta katika keshi la tatu, na sasa hatuna udhuru kusitisha ukeshaji wetu. Keshi la tatu linahitaji bidii mara tatu zaidi. Kukosa subira sasa itakuwa ni kupoteza bidii yetu yote ya kuvumilia kukesha hapo awali. Usiku mrefu wa giza unachosha; lakini asubuhi imesubirishwa katika rehema kwa sababu kama BWANA atakuja, wengi wangekutwa hawako tayari. Kutokutaka kwa BWANA watu Wake kuangamia, imekuwa sababu ya kusubiri kwa muda mrefu. Lakini ujio wa asubuhi kwa waaminifu na usiku kwa watu wasio waaminifu, upo hakika juu yetu. kwa kuongojea na kukesha, watu wa MUNGU wanatakiwa kuonesha tabia yao ya kipekee, kujitenga kwao na ulimwengu. Kwa hali yetu ya kukesha tunatakiwa kuonesha kwamba

kweli sisi tu wageni na wapitaji juu ya dunia. Tofauti kati ya wale wanaopenda ulimwengu na wale wanaompenda KRISTO ni dhahiri sana kiasi cha kutokukosewa. Wakati walimwengu wote wana bidii, unyofu katika tamaa ya kupata hazina za kidunia, watu wa MUNGU hawafanani au kufanya maridhiano na ulimwengu, lakini wanaonesha kwa bidii yao ya kukesha katika hali ya kusubiri ambayo inawabadilisha; kwamba makazi yao siyo katika ulimwengu huu lakini kwamba wanatafuta nchi iliyo bora ambayo ni ya kimbingu. {2T 193.3}

Natumaini, ndugu zangu wapendwa na dada zangu, hamtapitisha jicho lenu juu ya Maneno haya bila kufikiria kwa umakini maana yake. Kama watu wa Galilaya walivyosimama wakiangalia kwa uimara kuelekea mbinguni, ikiwezekana waone kidogo, Mwokozi wao anayepaa, watu wawili wenye mavazi meupe, malaika wa mbinguni, walitumwa kuwafariji kwa kupoteza uwepo wa Mwokozi wao, walisimama karibu yao na wakauliza: “Enyi watu wa Galilaya mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu YESU aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mliyomwona akienda Zake mbinguni”. {2T 194.1}

MUNGU amepanga kwamba watu Wake watakaza macho yao kuelekea mbinguni, wakitazama kutokea kwa utukufu kwa BWANA na Mwokozi YESU KRISTO. Wakati umakini wa walimwengu unageuzwa katika shughuli mbalimbali, Umakini wetu lazima uelekee mbingu; imani yetu lazima ifike mbali na kuzunguka kote katika siri ya hazina ya kimbingu tukiteka miale ya nuru ya thamani ya kimbingu kutoka Patakatifu pa mbinguni kung’aa ndani ya mioyo yetu kama inavyong’aa usoni pa YESU. Watu wanaodhihaki wanawabeza wakeshaji wanaosubiri wakidai: “iko wapi ahadi ya kuja Kwake? Mmekatishwa tamaa. Jiungeni nasi na mtafanikiwa katika mambo ya ulimwengu. Pateni mafanikio, pateni pesa na muheshimiwe na ulimwengu” Wale wanaongojea wanatazama juu na kujibu: “tunakesha.” Na kwa kuwa kwao kinyume na anasa za dunia na umaarufu wa kiulimwengu, na udanganyifu wa mali, wanajionesha kuwa katika hiyo hali. kwa kukesha wanakuwa imara; wanashinda uvivu na ubinafsi na kupenda urahisi (maisha bwerere). Moto wa mateso unawaka juu yao na muda wa kusubiri unaonekana kuwa mrefu. Wakati mwingine wanahuzunika na

imani kutetereka lakini wanasonga mbele tena, wanashinda hofu zao na mashaka yao, na wakati macho yao yakielekezwa kuelekea mbinguni, wanasema kwa adui zao “Ninakesha, ninasubiri marejeo ya BWANA wangu. Nitafurahi katika dhiki, mateso na katika uhitaji.” {2Tsw 194.2}

Hamu ya BWANA wetu ni kwamba tuwe tunakesha ili kwamba anapokuja na kugonga tuweze kumfungulia haraka. Baraka inatamkwa juu ya wale watumishi ambao anawaona wakikesha. “Atajifunga na kuwakaribisha chakulani, na atakuja na kuwahudumia.” Ni nani kati yetu katika siku hizi za mwisho atakuwa ameheshimiwa hivyo na BWANA wa kusanyiko? Je, tumejiandaa bila kuchelewa kumfungulia haraka na kumkaribisha ndani? Kesha, kesha, kesha. Karibu wote wamesitisha kukesha kwao na kusubiri; sisi hatupo tayari kumfungulia haraka. Kupenda dunia kumejaza sana fikra zetu, hata macho yetu hayatazami juu lakini chini duniani. Tunaharakisha katika kujishughulisha kwa jitihada kubwa na bidii katika shughuli mbalimbali lakini MUNGU amesahauliwa na hazina ya mbinguni haithaminiwi. Hatupo katika hali ya kungoja na kukesha. Kupenda dunia na udanganyifu wa mali kunatia giza imani yetu na hatutamani na kupenda kuonekana kwa Mwokozi wetu. Tunajaribu kwa nguvu sana na sisi wenyewe kutunza nafsi zetu wenyewe. Hatujatulilia na tunakosa kwa kiasi kikubwa tumaini imara katika MUNGU. Wengi wana wasiwasi na wanafanya kazi, na kuwa na pilikapilika nyingi, wanapotengeneza na kupanga, wanaogopa wanaweza wakaingia uhitaji. Hawawezi kupata muda kuomba au kuhudhuria mikutano ya kidini na katika kujisumbukia wenyewe, hawaachi nafasi kwa ajili ya MUNGU kuwatunza. Na MUNGU hafanyi mengi kwa ajili yao kwa maana hawampi nafasi. Wanafanya mengi sana kwa nafsi zao wenyewe na wanaamini na kutumaini katika MUNGU kiasi kidogo sana. {2Tsw 195.1}

Kupenda dunia kunashikilia kwa hatari juu ya watu ambao BWANA amewaamuru kukesha na kuomba wakati wote, ili asije kwa ghafla akawakuta wamelala. “Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia, mtu akiipenda dunia kumpenda BABA hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani yaani tamaa ya mwili na tamaa ya macho



na kiburi cha uzima havitokani na BABA, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita pamoja na tamaa zake bali yeye afanyaye mapenzi ya MUNGU adumu hata milele.” {2Tsw 196.1}

Nimeoneshwa kwamba watu wa MUNGU ambao wanakiri kuamini Ukweli wa leo hawako katika kungoja na hali ya kukesha. Wanaongezeka katika mali na wanaweka hazina zao juu ya dunia. Wanatajirika katika vitu vya kidunia lakini siyo matajiri kumwelekea MUNGU. Hawaamini katika ufupi wa muda, hawaamini kwamba mwisho wa mambo yote upo karibu, kwamba KRISTO Yu mlangoni. Wanaweza kukiri imani kubwa lakini wanajidanganya roho zao wenyewe maana watatenda kwa imani ambayo wanaimiliki katika ile Kweli. Kazi zao zinaonesha tabia ya imani yao na kushuhudia kwa wale karibu yao kwamba ujio wa KRISTO hautakuwa katika kizazi hiki. Kulingana na imani yao, ndiyo yatakuwa matendo yao. Maandalizi yao yamekuwa yakifanywa katika kubakia katika ulimwengu huu. Wanaongeza nyumba juu ya nyumba, ardhi juu ya ardhi na ni wakazi wa dunia hii tu. {2Tsw 196.2}

Hali ya maskini Lazaro kula makombo kutoka kwenye meza ya mtu tajiri inafaa kuliko ya hawa wanaokiri imani ya mdomo. Kama wangukuwa na imani ya Kweli badala kuongeza hazina zao juu ya dunia, wangukuwa wanasogea mbele na makasia, wakijiweka huru wenyewe kutoka mambo yenye mafundo ya dunia na kuhamishia hazina zao kwenda mbinguni. Hatimaye nia na mioyo itakuwa huko. Maana moyo wa mtu utakuwa mahali hazina yake kubwa ilipo. Wengi wa wale wanaokiri kuamini Ukweli wanashuhudia kwamba kile wanachothamini zaidi kipo katika ulimwengu. Kwa haya wamesumbukia, kwa wasiwasi wa kuchosha na kufanya kazi. Kutunza na kuongeza hazina zao ni somo la maisha yao. Wamehamisha kidogo sana kwenda mbinguni, wamechukua hisa/uwekezaji kidogo ili kuingiza katika hazina ya mbinguni kiasi kwamba akili zao hazijavutiwa kwa upekee kuelekea ile nchi bora. Wamechukua hazina kubwa katika shughuli za dunia hii, na uwekezaji huu kama sumaku, unazivuta chini akili zao kutoka katika vya kimbingu na visivyoharibika, na kwenda vya kidunia na vinavyoharibika. “Mahali hazina yako ilipo ndipo na moyo wako ulipo.” {2Tsw 197.1}

Ubinafsi unawafunga wengi kama vile kamba ya chuma. Ni “Shamba langu,” “bidhaa zangu,” “biashara yangu.” Hata madai ya ubinadamu/utu wa kawaida hayajaliwi nao. Wanaume na Wanawake wanaokiri kuwa wanangoja na kupenda kuonekana kwa BWANA wamefungwa na ubinafsi. wema na utauwa wamejitenga navyo. Kupenda dunia, tamaa ya mwili, tamaa ya macho, kiburi cha uzima vimewafunga sana hata wamepofushwa. Wameharibiwa na ulimwengu nao hawatambui. Wanaongelea upendo kwa MUNGU lakini matunda yao hayaoneshi upendo wanaoelezea. Wanamwibia zaka na sadaka Bwana, nayo laana kali ya MUNGU ipo juu yao. Ukweli umekuwa ukiangaza njia yao kila upande. MUNGU ametenda maajabu katika wokovu wa roho zao ndani ya nyumba zao. lakini ziko wapi sadaka zao zilizoletwa Kwake katika kushukuru kwa ishara Zake za rehema kwao? Wengi wao hawana shukrani kama vile tu wanyama walioumbwa na Mungu walivyo. Kafara kwa ajili ya mtu ilikuwa isiyo na kikomo zaidi ya ufahamu wa akili imara, bado watu wanaodai kuwa washirika wa hizi faida za kimbingu ambazo zililetwa kwao katika gharama kubwa, ni wabinafsi kupindukia kufanya kujitoa kwa ajili ya MUNGU. Akili zao zipo juu ya ulimwengu, ulimwengu, ulimwengu. Katika Zaburi ya arobaini na tisa tunasoma: “Hao wanaozitumainia mali zao na kujisifia wingi wa utajiri wao hakuna mtu anayeweza kumkomboa ndugu yake wala kumpa MUNGU fidia kwa ajili Yake. (Maana fidia ya nafsi zao ina gharama wala hana budi kuiacha hata milele).” Kama wote wangezingatia katika akili zao na wangeweza kwa kiasi kidogo kuthamini kafara kubwa iliyofanywa na KRISTO, wangejihisi kukemewa kwa hofu yao na ubinafsi wao mkubwa. “MUNGU wetu atakuja wala hatanyamaza, moto utakula mbele Zake na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbingu zilizo juu na nchi pia awahukumu watu Wake. Nikusanyieni wacha MUNGU Wangu waliofanya agano nami kwa dhabihu.” Kwa sababu ya ubinafsi na kupenda ulimwengu, MUNGU amesahauliwa na wengi wana ukame wa roho na wanalia “ustawi wangu “ustawi wangu.” BWANA ametoa mali kwa watu Wake kuwathibitisha, kuwajaribu kina cha ukiri wa upendo wao Kwake. Wengine watamuacha na kuiacha hazina yao ya mbinguni kuliko kupunguza mali zao za kidunia na kufanya agano Naye kwa

dhabihu. Bwana Anawaita kujitoa; lakini kupenda ulimwengu kunafunga masikio yao na hawatasikia. {2Tsw 197.2}

Nalitazama kuona nani kati ya wale wanaokiri kuwa wanatazamia ujio wa KRISTO wanamiliki utayari wa kutoa sadaka kwa MUNGU kwa wingi wa vitu vyao. Niliweza kuona maskini wanyenyekevu wachache, kama maskini mjane walikuwa wakikirimu na kutoa vichache vyao. Kila sadaka ya namna hiyo inaandikwa na MUNGU kama hazina ya thamani. Lakini wale wanaojipatia mali na kuongeza utajiri wapo mbali huko nyuma. Hawafanyi kitu kiulinganifu na vile wangeweza. Wanazuia, wakibania na kumwibia MUNGU maana wana hofu wataingia uhitaji. Hawajaribu kumwamini MUNGU. Hii ni moja ya sababu kwamba kama watu tunaumwa na wengi wanaanguka katika makaburi yao. Wenye tamaa wapo kati yetu. Wapenda dunia pia, wamezuia ujira wa waajiriwa waliopo miongoni mwetu. Watu ambao hawana kitu katika ulimwengu huu ambao ni maskini na tegemezi katika kazi yao wameshughulikiwa kwa ukali na bila haki. Wapenda ulimwengu kwa uso mgumu na moyo mgumu zaidi kwa uchoyo umelipa kiasi kidogo kilichopatikana kwa kazi ngumu. Ndivyo wanavyoshughulika na BWANA wao ambaye wanadai kuwa watumwa Wake. Katika uchoyo na kutoa kwa shingo upande kwa namna hii, wanaweka katika hazina ya MUNGU. Mtu yule katika mfano hakuwa na mahali pa kuweka mali zake na MUNGU alikatisha maisha yake yasiyo na faida. Ndivyo atakavyoshughulika na wengi. Ni vigumu kwa kiasi gani katika zama hii ovu, kuepuka ukuzaji wa udunia na uchoyo moyoni. Ni rahisi kiasi gani kuwa mkosefu wa shukrani kwa mtoaji wa rehema zote. Ukeshaji mkubwa unahitajika na maombi mengi ili kuweka roho katika uadilifu wote. “Angalieni, kesheni na ombeni kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo.” {2Tsw 198.1}

## **SURA YA 29**

### **MATESO YA KRISTO**

Ili kutambua thamani kamili ya wokovu, ni lazima kuelewa gharama yake. Katika matokeo ya ufinyu wa mawazo ya mateso ya KRISTO, wengi wanaweka kipimo cha chini kwenye kazi kubwa ya upatanisho (Kati ya Mungu na Mwanadamu, baada ya mwanadamu kuanguka dhambini). Mpango mtukufu wa wokovu wa mwanadamu, uliletwa kwetu kupitia upendo usio kikomo wa MUNGU BABA. Katika mpango huu mtakatifu wa Mungu, unaonekana udhihirisho wa ajabu sana wa upendo wa MUNGU kwa jamii iliyoanguka. Upendo kiasi hicho kama unavyodhihirishwa katika zawadi ya MWANA mpendwa wa MUNGU uliwashangaza/uliwashtua malaika watakatifu. “Kwa maana jinsi hii MUNGU aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanae wa Pekee ili kila amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.” Huyu Mwokozi alikuwa nuru ya utukufu wa BABA Yake na chapa ya nafsi Yake. Alikuwa na utukufu wa Mungu, utakatifu na mamlaka. Alikuwa sawa na MUNGU. Ilimpendeza BABA kwamba katika Yeye utimilifu wote ukae” Yeye ambaye hakuona kule kuwa sawa na MUNGU kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa na mfano wa mwanadamu, tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba.” {2Tsw 200.1}

KRISTO alikubali kufa badala ya mdhambi, ili mtu kwa maisha ya utii, aweze kuepuka adhabu ya sheria ya MUNGU. Kifo Chake hakikufanya sheria isiwe na matokeo, hakikuondoa au kuua sheria, hakikupunguza madai Yake matakatifu wala kuindoa katika hadhi na heshima yake takatifu. Kifo cha KRISTO kilitangaza haki ya sheria ya BABA Yake katika kumuadhibu mdhambi, katika hiyo KRISTO alikubali kubeba adhabu ya sheria Yeye Mwenyewe ili kumwokoia mtu aliyeanguka kutoka katika laana yake. Kifo cha MWANA mpendwa wa MUNGU juu ya msalaba, kinaonesha kutokubadilika kwa sheria ya MUNGU. Kifo Chake kinaitukuza sheria na kuifanya yenye kuheshimika na kutoa ushahidi kwa mtu tabia Yake MUNGU isiyobadilika. Kutoka katika midomo Yake mitakatifu yamesikika Maneno: “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii, la sikuja kutangua bali kutimiliza.” Kifo cha KRISTO kilithibitisha madai ya sheria. {2Tsw 200.2}

Katika KRISTO, aliunganishwa ubinadamu na Uungu. Utume Wake ulikuwa kumpatanisha MUNGU na mtu, kuunganisha mwanadamu mwenye ukomo na umilele Wake. Hii ilikuwa ni njia pekee ambayo wanadamu walioanguka wangeweza kuinuliwa kupitia stahiki na thamani ya damu ya KRISTO kuwa washirika wa asili ya Uungu. Kuchukua asili ya mwanadamu kulimpa/kulimfaa KRISTO kuelewa majaribu na huzuni ya mwanadamu na majaribu yote ambayo aliteswa. Malaika ambao hawakuijua dhambi hawakuweza kuhuzunika na mwanadamu katika majaribu Yake ya pekee. KRISTO alishuka chini kabisa ili kuchukua asili ya mwanadamu na alijaribiwa katika nyanja zote kama sisi ili aweze kujua jinsi ya kuwasaidia wote watakao jaribiwa. {2Tsw 201.1}

Ubinadamu ulipokuwa juu Yake alihisi hitaji Lake la nguvu kutoka kwa BABA. Alikuwa na maeneo pekee aliyoyachagua kwa maombi. Alipenda kufanya ushirika na BABA Yake katika hali ya utulivu ya milimani. Katika zoezi hili nafsi Yake yote takatifu na kamilifu, yenye roho ya ubinadamu iliimarishwa kwa majukumu na majaribu ya siku. Mwokozi wetu anajitambulisha Mwenyewe mahitaji yetu na udhaifu wetu katika hili akawa mtoa dua, Mwombaji akisihi wakati wa usiku akitafuta kutoka kwa BABA Yake mgawo mpya wa nguvu ili akitoka nje, awe ameimarishwa na kufanywa upya, ametayarishwa kwa majukumu na majaribu ya siku. Yeye ni mfano wetu katika mambo yote. Yeye ni kaka/Ndugu katika udhaifu wetu lakini siyo kaka katika shauku na tamaa zetu. Kama Asiye na dhambi asili yake ilijikunja kutoka kwa uovu (alikimbia uovu, hakushiriki uovu). Alihimili mapambano na maumivu ya roho katika ulimwengu wa dhambi. Ubinadamu wake ulifanya maombi kuwa jambo la lazima na fursa yenye kipaumbele. Alihitaji msaada wote wa Kiungu wenye nguvu na faraja ambayo BABA Yake alikuwa tayari kumpa Yeye, Kwake Ambaye kwa manufaa ya mwanadamu, aliaacha furaha ya mbinguni na kuchagua makazi Yake katika ulimwengu wenye ubaridi, usio rafiki na usio na moyo wa shukrani. KRISTO alipata faraja na furaha ya kimbangu katika ushirika na mawasiliano na BABA Yake. Hapa angeweza kutua moyo Wake huzuni ambazo zilikukuwa zikimpondaponda na kumlelea. Alikuwa ni mtu wa sikitiko na aliyejua huzuni. {2Tsw 201.2}

Kutwa nzima alifanya kazi kwa bidii kutenda wema kwa wengine, kuokoa watu kutoka katika uangamivu. Aliponya wagonjwa, alifariji waliomboleza na kuleta furaha na matumaini kwa waliokata tamaa. Aliwafufua wafu wakawa hai tena. Kazi Yake ilipokwisha kwa siku, alitoka jioni baada ya jioni, mbali na machafuko ya mji na mwili Wake uliinama katika bustani ya miti katika dua kwa BABA. Wakati mwingine miale angavu ya mwezi ilianguza juu ya mwili wake ulioinama. Na tena mawingu na giza vikafunga mwanga wote. Umande na vibarafu vyembamba vya usiku vilitulia juu ya kichwa Chake na ndevu wakati wa hali ya maombi. Kwa mfululizo aliendeleza maombi Yake usiku mzima. Yeye ni kielelezo chetu. Kama tungekumbuka hili na kumuiga Yeye, tungekuwa imara zaidi katika MUNGU. {2Tsw 202.1}

Kama Mwokozi wa wanadamu na nguvu Zake za Uungu alihisi uhitaji wa maombi, kiasi gani zaidi basi, wanadamu wadhaifu, wanaokufa na wadhambi wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi yenye umakini, nguvu na ya kudumu! Wakati KRISTO alipokuwa amesumbuliwa vikali na majaribu hakula kitu. Alijikabidhi kwa MUNGU, na kupitia maombi ya dhati na bidii na kujisalimisha kamili katika mapenzi ya BABA Yake, aliibuka kama Mshindi. Wale wanaokiri Ukweli wa siku hizi za mwisho, kutoka katika tabaka zote za watu wanaokiri kuwa Wakristo, lazima wamuige Yeye ambaye Ndiye Kielelezo kikuu katika maombi. {2Tsw 202.2}

"Yatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake." Meza zetu hurundikwa mara kwa mara na vitu vya anasa visivyo vya afya (huchafuliwa na chakula kisichofaa), msaadaa au ulazima, kwa sababu tunapenda mambo hayo kuliko tunavyopenda kujinyima, kuondokana na magonjwa, na kuwa na utimamu wa akili. Yesu aliitafuta kwa bidii nguvu kutoka kwa Baba Yake. Huyu Mwana wa Mungu aliona ni thamani kubwa zaidi, hata Kwake Mwenyewe, kuwa na ushirika na Baba Yake, kuliko kuketi kwenye meza ya anasa/fahari zaidi. Yeye Alitupa uthibitisho kwamba sala ni muhimu ili kupokea nguvu ya kupambana na nguvu za giza na kufanya kazi iliyokabidhiwa kwetu. Nguvu zetu wenyewe ni dhaifu lakini kile ambacho MUNGU anatoa ni kikuu na kitamfanya kila mtu ambaye anakipata awe zaidi ya mshindi. {2Tsw 203.1}

MWANA wa MUNGU alipokuwa akiinama katika hali ya maombi katika bustani ya Gethsemane, uchungu wa roho Yake ulikamua jasho lililokuwa na matone ya damu kutoka kwenye vinyweleo Vyake. Ilikuwa hapa ambapo hofu na kitisho cha giza nene kilimzunguka. Dhambi za ulimwengu zilikuwa juu Yake. Alikuwa akiteseka badala ya mwanadamu kama mvunja sheria ya BABA Yake. Huu ulikuwa ukumbi wa majaribu. Nuru takatifu ya MUNGU ilikuwa ikififia kutoka usoni Mwake na alikuwa akipita katika mikono ya nguvu za giza. Katika roho Yake yenye huzuni, alijilaza kifudifudi juu ya dunia isiyo rafiki. Alikuwa akipitia hasira ya BABA Yake. Alichukua kikombe cha mateso kutoka midomo ya mwanadamu mwenye hatia na kuamua kujitolea kunywa Mwenyewe, na badala yake ampe mwanadamu kikombe cha Baraka. Hasira ambayo ingeanguka juu ya mwanadamu sasa ilikuwa inamiminika/ikimwagika juu ya KRISTO. Ilikuwa hapa ndipo kile kikombe cha fumbo la ajabu, kilitetemeka mikononi Mwake. {2Tsw 203.2}

YESU alipumzika mara kwa mara Gethsemane na wanafunzi Wake kwa ajili ya tafakari na maombi. Wote walijua vyema makao haya matulivu na matakatifu ambayo alikwenda kupumzika na kufanywa upya. Hata Yuda alijua ni wapi pa kuwapeleka umati wa wauaji ili amsaliti YESU katika mikononi yao. Kamwe Mwokozi hakuwahi kutembelea mahali hapo kwa moyo uliojaa huzuni kama siku hiyo. Haikuwa mateso ya mwili ambayo MWANA WA MUNGU alijikunja kwayo, na ambayo yaligandamiza midomoni Yake, kisha mbele ya wanafunzi Wake, Maneno haya ya kuomboleza yalisikia: "Nafsi Yangu ina huzuni kubwa, hata kufa." "Kaeni hapa," alisema, "kesheni pamoja Mimi." {2Tsw 203.3}

Akiwaacha wanafunzi Wake umbali wa kuisikia sauti Yake, akaenda mbali kidogo kutoka kwao na akaanguka kifulifuli akaomba. Nafsi Yake ilifadhaika, akaomba: "Ee BABA Yangu, ikiwezekana, acha kikombe hiki kipite kutoka Kwangu: hata hivyo si kama nitakavyo Mimi, bali utakavyo Wewe." Dhambi za ulimwengu uliopotea zilikuwa juu Yake na kumlelea. Ilikuwa ni hisia za kukunja uso kwa BABA Yake, katika matokeo ya dhambi, ambayo yaliuchana moyo Wake kwa uchungu unaochoma na kukamua kwa nguvu, matone makubwa ya damu

kutoka katika paji la uso Wake, na haya matone, yalishuka kwenye mashavu Yake yaliyokuwa yamebadilika rangi kwa kupauka, na kisha yakaanguka chini, yakilowanisha ardhi. {2Tsw 204.1}

Akiinuka kutoka katika kusujudu, Akaja kwa wanafunzi Wake na kuwakuta wamelala. Akamwambia Petro: "Je! Hamkuweza kukesha pamoja Nami hata saa moja? Kesheni na mkaombe, msiingie majaribuni, roho i iradhi, lakini mwili ni dhaifu. "Wakati muhimu zaidi-wakati ambao YESU aliwasihi kwa ombi maalum la wao kukesha pamoja Naye – wanafunzi walikutwa wamelala. Alijua migogoro mikubwa na majaribu ya kutisha yaliyoko mbele yao. Aliwachukua pamoja Naye ili kwamba waweze kuwa nguvu Kwake (wampe faraja na nguvu), na kwamba matukio ambayo wangeshuhudia usiku huo, na maagizo ya mafundisho wanayopaswa kupokea, wanaweza kuyaweka kabisa kwenye kumbukumbu zao. Hii ilikuwa ni lazima, kusudi imani yao isianguke, bali iimarishwe kwa jaribu lililo mbele yao. {2Tsw 204.2}

Lakini badala ya kukesha na KRISTO, walikuwa wameelemewa na huzuni, na wakalala. Hata Petro ambaye aliyekuwa na usongo/motomoto, ambaye saa chache tu zilizopita, alikuwa ametangaza kwamba atateseka na, ikiwa ni lazima, afe kwa ajili ya BWANA wake, alikuwa amelala. Katika kipindi kizito zaidi, wakati MWANA WA MUNGU alikuwa akihitaji huruma yao na maombi yao ya dhati, wao walikuwa wamelala. Walipoteza vingi kwa kulala kwao. Mwokozi wetu alikusudia kuwatia nguvu kwa majaribu makali ya imani yao ambayo yangewafikia hivi karibuni. Ikiwa wangetumia kipindi hicho cha huzuni kukesha na Mwokozi mpendwa, na maombi kwa MUNGU, Petro hangeachwa kwa nguvu zake dhaifu kumkana BWANA wake wakati wa jaribu. {2Tsw 204.3}

MWANA WA MUNGU akaenda mara ya pili, akaomba, akisema, Ee BABA Yangu, ikiwa kikombe hiki haiwezekani kiniepuke, isipokuwa nikinywe, mapenzi Yako yatendeke. " Akaja tena kwa wanafunzi Wake, akawakuta wao wamelala. Macho yao yalikuwa mazito. Wanafunzi hawa waliolala wanawawakilisha kanisa linalolala, wakati siku ya kujiliwa na Mungu inakaribia. Ni wakati wa utusitusi na giza nene, wakati ambao kukutwa umelala ni hatari ya kufisha zaidi. {2Tsw 205.1}



YESU ametuachia onyo hili: "Kesheni basi, kwa maana hamjui ni lini mkuu wa nyumba atakuja, jioni, au usiku wa manane, au wakati wa kuwika jogoo, au asubuhi: asije akaja ghafla na kuwakuta mumelala." Kanisa la MUNGU linahitajika kutimiza saa ya kukesha ya usiku, kwa vyovyote vile, iwe ni hatari ya kiasi gani, muda mrefu au mfupi. Huzuni sio kisingizio kwa kanisa kutokuwa macho kwa ulinzi. Dhiki au mateso hayapaswi kusababisha uzembe, lakini inapaswa kuwa dokezo la kuwa mwangalifu maradufu zaidi. KRISTO amelielekeza kanisa kwa mfano Wake Mwenyewe kwa Chanzo cha nguvu zao katika nyakati za hitaji, dhiki, na hatari. Mtazamo wa kukesha ni kudhihirisha kama kanisa ni watu wa MUNGU kweli-kweli. Kwa ishara hii wanaosubiri wametofautishwa na ulimwengu na wanaonesha kuwa wao ni wapitaji, wasafiri, mahujaji na wakimbizi, wageni duniani. {2Tsw 205.2}

Kwa mara nyingine tena Mwokozi aliwageukia kwa huzuni wanafunzi Wake waliolala, na akaomba mara ya tatu, akisema Maneno yale yale. Kisha akawajia, akasema, laleni sasa, pumziken; tazama, saa imekaribia; na MWANA WA ADAMU anasalitiwa katika mikono ya wenye dhambi. "Ni ukatili kiasi gani kwa wanafunzi kuruhusu usingizi kufunga macho yao, na kusinzia kuzifunga fahamu zao, wakati BWANA wao alikuwa akivumilia uchungu wa akili usioweza kuelezeka! Ikiwa wangebaki wakikesha wasingelipoteza imani yao wakati walipomwona MWANA WA MUNGU akifa msalabani. Saa hii ya muhimu ya kesho la usiku ilipaswa kuonyeshwa na mapambano bora ya kiakili na maombi, ambayo yangewaitea nguvu ya kushuhudia uchungu usiosemeke wa MWANA WA MUNGU. Saa hii ya kukesha ingewaandaa wao, kama vile watakavyoona mateso Yake msalabani, kuelewa jambo la asili la nguvu ya kuushinda uchungu aliovumilia katika Bustani ya Gethsemane. Na wangeweza kukumbuka vizuri kwa kurejelea Maneno ambayo alikuwa amewaambia akimaanisha mateso Yake, kifo, na ufufuo; na, katikati ya kiza cha nyakati za jaribu la kutisha, miale ya matumaini ingekuwa ikiliangaza giza na kudumisha imani yao. {2Tsw 205.3}

KRISTO alikuwa amewaambia hapo awali kwamba mambo haya yangefanyika, lakini hawakumwelewa. Mandhari ya mateso Yake

yalikuwa ya maumivu makali na ya kutisha kwa wanafunzi Wake, kwa hivyo kulikuwa na umuhimu wa kukesha na kuomba kabla ya haya kutokea. Imani yao ilihitaji kudumishwa na nguvu isiyoonekana kwani walipaswa kupata ushindi wa nguvu za giza. Tunaweza kuwa na mawazo ya mbali sana na duni, juu ya uchungu usioweza kueleweka wa mpendwa MWANA WA MUNGU huko Gethsemane, kama alivyotambua utengano Wake na BABA Yake, ulikuwa matokeo ya kubeba dhambi ya mwanadamu. Akawa dhambi kwa jamii iliyoanguka. Hisia ya kuondolewa kwa upendo wa BABA Yake ilisukuma Maneno haya ya huzuni kutoka Kwake roho iliyomizwa sana: "Nafsi Yangu ina huzuni kubwa, hata kufa." "Ikiwa ni hivyo ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke kutoka Kwangu." Halafu kwa kujitiisha kabisa kwa mapenzi ya BABA Yake, Anaongeza: "Walakini si kama nitakavyo Mimi, bali utakavyo Wewe." {2Tsw 206.1}

MWANA WA MUNGU alikuwa akizimia, akifa. BABA alimtuma mjumbe kutoka Kwake kumuimarisha Mtesekaji wa kimbingu/Kiungu na amtie moyo kukanyaga njia Yake yenye damu. Ikiwa wanadamu wanaokufa wangeweza kutazama kwa mshangao na huzuni jeshi la malaika walipokuwa wakitazama kwa ukimya na kwa huzuni BABA akitenganisha miale Yake ya nuru, upendo, na utukufu kutoka kwa MWANA Wake mpendwa aliye karibu, wao wangeelewa vizuri jinsi dhambi ilivyo ya kuchukiza machoni Pake. Upanga wa haki sasa ulikuwa umeamka dhidi ya Mwanawe mpendwa. Alisalitiwa na busu mikononi mwa maadui Zake, na haraka kupelekwa kwenye ukumbi wa hukumu wa mahakama ya kidunia, na pale kudharauliwa na kuhukumiwa kifo na wanadamu wenye dhambi. Pale MWANA WA MUNGU Mtukufu "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu." Alibeba matusi, kejeli, na dhuluma za aibu, mpaka "Sura Yake ilikuwa imeharibiwa sana kuliko mtu yeyote, na umbo Lake zaidi kuliko wana wa wanadamu." {2T 206.2}

Nani anaweza kuelewa upendo ulioonyeshwa hapa! Jeshi la Malaika watakatifu lilitazama kwa mshangao na kwa huzuni, Yeye ambaye alikuwa Mkuu mbinguni, na ambaye alikuwa amevaa taji ya utukufu, sasa alikuwa amevaa taji ya miiba, mhanga anayetokwa na damu kwa ghadhabu ya umati uliokasirika, uliochochewa katika wenda-wazimu

,na kichaa na hasira ya Shetani. Tazama Mvumilivu mwenye kuteseka! Juu ya kichwa Chake kuna taji ya miiba. Damu Yake ilitiririka, ikitoka kwenye kila mshipa uliotiwa jeraha. Yote haya ni kwa matokeo ya dhambi! Hakuna kitu kinachoweza kumshawishi Kristo aache heshima na enzi mbinguni, na kuja katika ulimwengu wenye dhambi, kupuuzwa, kudharauliwa, na kukataliwa na wale Aliokuja kuwaokoa, na mwishowe kuteseka msalabani, lakini upendo wa milele, wenye kumkomboa mwanadamu, ule ambao milele zote utadumu kuwa fumbo na siri. {2Tsw 207.1}

Shangaeni, enyi mbingu, na Staajabu, Ee dunia! Tazama wanadamu dhalimu waliomtesa Masihi na Mtu aliyeteswa! Umati mkubwa umemfunga Mwokozi wa ulimwengu. Kejeli na kuzomea vimechanganyika na laana za matusi na kufuru. Kuzaliwa Kwake katika maisha ya chini na ya unyenyekevu kunazungumzwa bila kufikiri na kwa jinsi ya hovyoy. Madai Yake kuwa ni MWANA WA MUNGU yanadhihakiwa na makuhani wakuu, na wazee, na mzaha mchafu na kejeli za matusi vilikuwa vikipita kutoka mdomo hadi mdomo. Shetani alikuwa na udhibiti kamili wa akili za watumishi wake. Ili kufanya hivyo kwa ufanisi, anaanza na makuhani wakuu na wazee wa kanisa, na anawajaza hawa na wenda-wazimu wa kidini. Wanasukumwa na roho ile ile ya kishetani ambayo inawapeleka vibaya zaidi kuwa waovu na wenye dhambi, na wenye mioyo migumu. Kuna upatanifu wenye ufidadi katika hisia za wote, kutoka kwa makuhani wanafiki na wazee hadi mtu wa chini kabisa. KRISTO, MWANA WA MUNGU wa thamani, aliongozwa nje, na msalaba ukawekwa juu ya mabega Yake. Katika kila hatua ilibaki damu ambayo ilitiririka kutoka kwa majeraha Yake. Akisongwa na umati mkubwa wa maadui wenye chuki kali/chungu na watazamaji wasio na hisia, Anaongozwa kwenda kusulubiwa. "Alionewa, lakini alinyenyekea, Wala hakufunua kinywa Chake; Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, Na kama vile kondoo anyamazavyo Mbele yao wakatao manyoya Yake; Naam, hakufunua kinywa Chake." {2Tsw 207.2}

Wanafunzi Wake wenye huzuni walimfuata kwa mbali, nyuma ya umati wa wauaji. Alipigiliwa misumari msalabani, na kuning'inizwa kati ya mbingu na ardhi. Mioyo yao ilipasuka na uchungu kwani Mwalimu wao mpendwa anateseka kama mhalifu. Karibu na msalaba kuna vipofu,

wenye misimamo ya ubaguzi na machukizo, makuhani na wazee wasio na imani, wakimdhahi, na kumzomea: "Wewe unayeharibu hekalu na kulijenga ndani ya siku tatu jiokoe Mwenyewe. Ikiwa Wewe ni MWANA WA MUNGU, shuka msalabani. Vivyo hivyo pia wakuu wa Makuhani walimdhahi, pamoja na waandishi na wazee, wakasema, Aliokoa wengine; Mwenyewe Hawezi kujiokoa. Ikiwa Yeye ni Mfalme wa Israeli, na ashuke sasa kutoka msalabani, nasi tutamwamini. Alimtumaini MUNGU; basi amwokoe sasa, ikiwa anampenda: kwa maana alisema, Mimi ni MWANA WA MUNGU." {2Tsw 208.1}

Hakuna neno hata moja ambalo YESU alilijibu kati ya haya yote. Wakati misumari inapigiliwa kwenye mikono Yake, na matone ya jasho la uchungu yalilazimishwa kutoka kwenye vinyweleo Vyake, kutoka kwenye midomo iliyopauka iliyotetemeka ya mtesekaji asiye na hatia, akapumua dua ya msamaha ya upendo kwa ajili ya wauaji Wake: "BABA, wasamehe; kwani wao hawajui walitendalo." Mbingu zote zilikuwa zikitazama kwa shauku kubwa juu ya tukio hilo. Mtukufu Mkombozi wa ulimwengu uliopotea alikuwa akipata adhabu ya mwanadamu kukiuka sheria ya BABA. Alikuwa karibu kuwakomboa watu Wake kwa damu Yake Mwenyewe. Alikuwa analipa madai ya haki ya sheria takatifu ya MUNGU. Hii ilikuwa njia ambayo hatimaye ingepelekea mwisho wa dhambi na Shetani, na jeshi lake lote kuangamizwa. {2Tsw 208.2}

Lo, hapajawahi kutokea mateso na huzuni kama hiyo iliyovumiliwa Mwokozi anayekufa! Ilikuwa ni hisia ya Hasira ya BABA Yake ambayo ilifanya kikombe Chake kiwe kichungu sana. Haikuwa mateso ya mwili ambayo yalimaliza haraka maisha ya Kristo msalabani. Bali ilikuwa ni uzito wa nguvu ya dhambi za ulimwengu uliobamiza, na hisia za Hasira ya BABA Yake. Utukufu wa BABA na uwepo uliodumu wa Babaye, ambao ulikuwa umemwacha, na kukata tamaa kulisisitiza mgandamizo wa uzito wa giza juu Yake na kulazimishwa kutoka kwa midomo Yake iliyopauka na inayotetemeka, kilio cha uchungu: "MUNGU Wangu, MUNGU Wangu, mbona umeniacha?" {2Tsw 209.1}

YESU alikuwa ameungana na BABA katika kuumba ulimwengu. Katikati ya mateso makali ya MWANA WA MUNGU, wanaume vipofu na wenye Imani danganyifu peke yao ndio walibakia bila huruma. Makuhani wakuu na wazee walimtukana na kumkejeli kwa maneno makali MWANA mpendwa wa MUNGU wakati wa mateso Yake, alipolia kwa uchungu katika hatua za mwisho kifoni. Asilia isiyo na uhai inaugua kwa huruma kwa Muumbaji Wake anayetokwa na damu, anayekufa. Ardhi inatetemeka. Jua linakataa kuona tukio. Mbingu zinakusanya weusi. Malaika wameshuhudia tukio la mateso mpaka hawawezi kutazama tena, nao wanaficha nyuso zao kutoka katika eneo la kuchukiza na kutisha. KRISTO Anakufa! Amekata tamaa! Tabasamu la kukubaliwa na BABA Yake limeondolewa, na malaika hawakuruhusiwa kuangaza katika kiza ya masaa ya kuogofya. Wanaweza tu kuona kwa mshangao, Kamanda wao mpendwa, Mkuu wa mbinguni, anateseka na adhabu ya mwanadamu kukiuka sheria ya BABA. {2Tsw 209.2}

Hata mashaka yalimshambulia MWANA WA MUNGU anayekufa. Hakuweza kuona kupitia milango ya kaburi (hakuweza kuona mbele zaidi ya kaburi). Mwanga wa matumaini. Haukuwasilishwa Kwake kuhusiana na kutoka kaburini kama Mshindi na ukubali wa dhabihu wa BABA Yake. Dhambi ya ulimwengu, pamoja na kutisha kwake kabisa, ilihisiwa kwa kina kisichoelezeka na MWANA WA MUNGU. Kuchukizwa kwa dhambi kwa BABA, na adhabu Yake, ambayo ni kifo, ndiyo yote ambayo angeweza kutambua, kupitia giza hili la kushangaza. Alijaribiwa kuogopa kwamba dhambi ilikuwa ya kukera sana mbele ya BABA Yake hata asingeweza kupatanishwa na Mwanawe tena. Jaribu la kutisha ambalo BABA Yake Mwenyewe alikuwa amemwacha milele, kilisababisha mpasuko wa kilio cha maumivu ya uchungu mkali sana msalabani: "MUNGU Wangu, MUNGU Wangu, mbona umeniacha?" {2Tsw 209.3}

KRISTO alihisi kwa ukali sana, kama vile watenda-dhambi watakavyohisi wakati ghadhabu ya MUNGU itakapomwagwa juu yao (adhabu ya mwisho). Giza la Kukata tamaa, kama moshi wa mauti na kifo, vitakapokusanywa juu ya roho zao zenye hatia, na ndipo watakapogundua kwa ukamilifu kabisa, uzito/ukali wa dhambi. Wokovu umenunuliwa kwao kwa mateso na kifo cha MWANA WA

MUNGU. Huu ukombozi unaweza kuwa wao, ikiwa wangeukubali kwa hiari, kwa furaha; lakini hakuna anayelazimishwa kutoa utii kwa sheria ya MUNGU. Ikiwa wanakataa faida ya mbinguni na kuchagua raha na udanganyifu wa dhambi, wana chaguo lao, na mwishowe watapokea mshahara wao, ambao ni ghadhabu ya MUNGU na mauti ya milele. Watatenganishwa milele na uwepo wa YESU, ambaye waliidharau dhabihu Yake. Watakuwa wamepoteza maisha ya furaha na kutoa dhabihu ule utukufu wa milele kwa raha za dhambi za msimu tu. {2T 210.1}

Imani na matumaini yalitetemeka katika mizani, kwa maumivu ya KRISTO aliyekuwa anakufa kwa sababu MUNGU alikuwa ameondoa hakikisho ambalo Hapo awali alikuwa amempa MWANAWA mpendwa wa kudhibitishwa Kwake na kukubalika. Mkombozi wa ulimwengu alitegemea ushahidi uliokuwa umemtia nguvu hata sasa, kwamba BABA Yake alikuwa amekubali Kazi Zake na kufurahishwa nazo. Katika uchungu Wake wa kufa, anapoenda kusalimisha uhai Wake wa thamani, inabidi kwa imani peke yake, amtumaini Yeye ambaye daima amekuwa furaha Yake kumtii. Hakushangiliwa na miale angavu ya matumaini iliyo wazi upande wa kulia wala wa kushoto. Yote yamegubikwa na mgandamizo wa giza. Katikati ya giza la kutisha ambalo linahisiwa na huruma ya nguvu za uasili/nature, Mkombozi alikinywea kikombe cha fumbo/siri hata mpaka machicha/chembe yake yote ya mwisho. Alikataliwa hata matumaini angavu na ujasiri katika ushindi ambao utakuwa Wake katika siku zijazo, Akalia kwa sauti kuu: "BABA, mikononi Mwako naiweka roho Yangu. "Anajua tabia ya BABA Yake, na haki Yake, Rehema Yake, na upendo Wake mkuu, na kwa unyenyekevu na utiii anaanguka mikononi Mwake. Katikati ya ulimwengu wa asili uliochanganyikiwa na kutikiswa, watazamaji walisikia kwa mshangao maneno ya Mtu anayekufa, wa Kalvari. {2T 210.2}

Ulimwengu wa asili ulihurumia mateso ya Muumbaji Wake. Ardhi iliyosukwasukwa, miamba iliyopasuka, ilitangaza kwamba alikuwa MWANA WA MUNGU aliyekufa. Kulikuwa na tetemeko kubwa la ardhi. Pazia la hekalu likapasuka vipande viwili. Hofu iliwakamata wauaji na watazamaji, wakati walipoona jua likifunikwa na gizani, na kuhisi ardhi

ikitetemeka chini yao, wakaona na kusikia miamba ikipasuka. Dhihaka na sauti za kuzomea za makuhani wakuu na wazee zilinyamazishwa wakati KRISTO akiikabidhi roho Yake mikononi mwa BABA Yake. Umati ulioshangaa ulianza kuondoka na kupapasa-papasa njia yao gizani kuelekea mjini. Walijipiga-piga juu ya vifua vyao wakati wakienda kwa hofu, wakiongea kwa kuogopa na kwa kunong'ona, wakisema kati yao wenyewe: "Ni Mtu asiye na hatia ambaye ameuawa. Je! Itakuwaje basi ikiwa ni kweli kwamba YEYE ni MWANA WA MUNGU, kama alivyosisitiza?" {2T 211.1}

Yesu hakusalimisha uhai Wake mpaka alipomaliza kazi aliyokuja kuifanya, na akapaza sauti, kwa pumzi Yake liyokuwa ikififia: na kuondoka "Imekwisha." Shetani wakati alikuwa ameshindwa. Alijua kwamba ufalme Wake ulikuwa umepotea. Malaika walifurahi wakati maneno hayo yalipotamkwa: "Imekwisha." Mpango mkuu wa ukombozi, ambao ulikuwa ukitegemea kifo cha KRISTO, ulikuwa umetekelezwa hadi sasa. Ikawa furaha mbinguni kuwa, wana wa Adamu wangeweza, kupitia maisha ya utii, mwishowe kuinuliwa kwa kiti cha enzi cha MUNGU. Ah, ni upendo wa ajabu kiasi gani! Ni upendo wa ajabu namna gani! ULIOMLETA MWANA WA MUNGU duniani kufanywa dhambi kwa ajili yetu, ili tupatanishwe na MUNGU, na kuinuliwa katika uzima pamoja Naye katika makao Yake ya utukufu. Ah, mtu ni nini, hata gharama kubwa kama hiyo imepaswa kulipia ukombozi wake! {2T 211.2}

Wakati wanaume na wanawake watakapoweza kuelewa kabisa ukubwa wa dhabihu kubwa ambayo imefanywa na Mfalme wa mbinguni kwa kufa badala ya mwanadamu, basi mpango wa wokovu utatukuzwa, na tafakari ya Kalvari itaamsha hisia nyororo na takatifu, upendo mwanana, hisia zenye kupendeza katika moyo wa Mkristo. Sifa kwa MUNGU NA MWANA-KONDOO zitakuwa mioyoni mwao na kwenye midomo yao. Kiburi na kujithamini wenyewe haviwezi kushamiri katika mioyo ambayo huweka kumbukumbu mpya katika matukio ya Kalvari. Ulimwengu huu utaonekana kuwa na thamani kidogo kwa wale ambao wanathamini gharama kubwa ya ukombozi wa mwanadamu, damu ya thamani ya MWANA mpendwa wa MUNGU. Utajiri wote wa ulimwengu hauna thamani ya kutosha kukomboa roho moja inayoangamia. Ni nani

anaweza kupima upendo wa KRISTO aliohisi kwa ulimwengu uliopotea kama alivyoning'inizwa msalabani, akiteseka kwa dhambi za watu wenye hatia? Upendo huu ulikuwa usio na kipimo, usio na mwisho. {2T 212.1}

KRISTO ameonyesha kuwa upendo Wake ulikuwa na nguvu kuliko kifo. Alikuwa akiutumiza wokovu wa mwanadamu; na ingawa alikuwa na mgogoro wa kutisha zaidi na nguvu za giza, lakini, kati ya yote, upendo Wake ulizidi kukua na kuwa imara na imara zaidi. Alivumilia kufichwa kwa uso wa BABA Yake, hadi alipoongozwa kutamka kwa uchungu ndani ya roho Yake: "MUNGU Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Mkono Wake ulileta wokovu. Bei ililipwa kununua ukombozi wa mwanadamu, wakati alikuwa katika mapambano ya nafsi ya mwisho, Maneno yaliyobarikiwa yalitamkwa ambayo yalionekana kusikika tena kupitia uumbaji: "Imekwisha- (Tetelestai!)." {2T 212.2}

Wengi wanaodai kuwa Wakristo wanachangamkia sana biashara za ulimwengu, na shauku zao zinaamshwa kwa burudani/vichekesho/matumbuizo mapya ya kufurahisha, wakati wana mioyo baridi, na huonekana kama imeganda, katika kazi ya MUNGU. Hapa kuna somo, wewe mwana mapokeo yenye ubaridi na urasmi, ambalo lina umuhimu wa kutosha kukuchangamsha wewe. Maslahi ya milele yanahusika hapa. Juu ya somo hili, ni dhambi kuwa mtulivu, usiyeonyesha hisia na asiye na huruma. Matukio ya Kalvari yanaita kutoka ndani yako hisia za ndani kabisa. Juu ya somo hili utapewa udhuru ikiwa utadhihirisha shauku-shangwe, machozi nk. Kwamba KRISTO, ambaye ni bora sana, na asiye na hatia kabisa, alipaswa kufa kifo kichungu, akibeba uzito wa dhambi za ulimwengu, mawazo na fikra zetu haviwezi kuelewa kabisa. Urefu, upana, kimo, kina, wa upendo wa namna ya kushangaza, kiasi kwamba hatuwezi kuelewa. Tafakari ya kina kisichopimika cha upendo wa Mwokozi kinapaswa kujaza akili, kugusa na kuyeyusha moyo, kuboresha na kuinua upendo, na kubadilisha kabisa tabia nzima. Lugha ya mtume aliyotumia ilikuwa ni: "Nilikusudia kutokujua chochote kati yenu, isipokuwa YESU KRISTO, na Yeye aliyesulubiwa. "Sisi pia tunaweza kutazama Kalvari na kwa mshangao kusema: "Hasha mimi si kwamba nitajisifu, isipokuwa



katika msalaba wa BWANA wa YESU KRISTO, ambaye kwa Yeye ulimwengu umesulubiwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu. "{2T 212.3

Kwa kuzingatia ni gharama kubwa kiasi gani wokovu wetu umenunuliwa, ni hatima gani itakuwa kwa wale ambao hupuuza wokovu mkubwa kama huu? Je! nini Itakuwa adhabu ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa KRISTO, lakini wanashindwa kuinama kwa utii mnyenyekevu kwa madai ya Mkombozi wao, na hivyo hawachukui msalaba kama wanafunzi wanyenyekevu wa KRISTO na kumfuata kutoka katika hori hadi Kalvari? "Yeye asiyekusanya Nami, "Asema KRISTO, "hutawanya nje. "{2T 213.1}

Wengine wana maoni finyu juu ya upatanisho. Wanafikiri kwamba KRISTO aliteseka sehemu ndogo tu ya adhabu ya sheria ya MUNGU; wanadhani kwamba, wakati hasira ya MUNGU ilipohisiwa na MWANAWA mpendwa, kupitia mateso yote na maumivu, alikuwa na ushahidi wa upendo wa BABA Yake na kukubalika; na kwamba milango ya kaburi lililokuwa mbele Yake ilianguzwa na tumaini zuri, na kwamba alikuwa na ushahidi wa kudumu wa utukufu Wake wa baadaye. Hapa kuna kosa kubwa. Uchungu mkubwa wa KRISTO ulikuwa hisia ya kuudhiwa kwa BABA Yake. Uchungu wa akili Yake kwa sababu ya hili ulikuwa wa kiwango kile ambacho mwanadamu anaweza kuwa na dhana dhaifu tu kuhusu jambo hili kwani hawezi kuelewa vyema. {2T 213.2}

Kwa wengi kuhusiana na kisa cha kujishusha chini, kunyenyekeka na fedheha na kafara ya BWANA MUNGU wetu, hakiamshi mvuto wa ndani zaidi, na haichochei roho na kuathiri maisha tena, kama vile ambavyo historia ya vifo vya mashahidi wafia dini wa YESU ilivyo kwao. Wengi wamepata kufa kwa kuteswa polepole (tocha); wengine wamepata kufa kwa kusulubiwa. Ni katika nini kifo cha MWANA mpendwa wa MUNGU Kinatofautiana na hivi vifo? Ni Kweli alikufa msalabani kifo cha kikatili zaidi; lakini wengine, kwa ajili ya mpendwa wao, wameteseka vivyo hivyo, kwa jinsi mateso ya mwili yanavyohusika. Kwa nini, basi, mateso ya KRISTO yalikuwa ya kutisha zaidi kuliko yale ya watu wengine ambao wamejitolea maisha yao kwa ajili Yake Bwana? Ikiwa mateso ya KRISTO yalikuwa na maumivu ya

mwili peke Yake, basi kifo Chake hakikuwa tena cha uchungu kuliko ilivyokuwa kwa baadhi ya mashahidi Wake. {2T 214.1}..

Lakini maumivu ya mwili yalikuwa sehemu ndogo tu ya uchungu wa MWANA mpendwa wa MUNGU. Dhambi za ulimwengu zilikuwa juu Yake, pia hisia ya ghadhabu ya BABA Yake wakati alipoteseka kwa adhabu ya kuvunja sheria. Ilikuwa ni haya, ambayo yaliseta roho Yake ya Kiungu. Ilikuwa ni kufichwa kwa uso wa BABA Yake –hisia kwamba BABA Yake mpendwa alikuwa amemwacha- ambayo ilileta kukata tamaa. Utengano ambao dhambi hufanya kati ya MUNGU na mwanadamu ulikuwa umetambuliwa kikamilifu na kuhisiwa kwa nia ya Yule Asiye na hatia, Mtu wa Kalvari Anayeteseka. Alikandamizwa na nguvu za giza. Hakuwa hata na mwale mmoja wa nuru ili kuangaza wakati ujao. Naye alikuwa akipambana na nguvu ya Shetani, ambaye alikuwa akitangaza kwamba alikuwa amemshikilia Kristo kwa nguvu zake, kwamba alikuwa na nguvu kuliko MWANA WA MUNGU, kwamba BABA alikuwa amemkana MWANAWAWE, na kwamba hakuwa tena katika upendeleo wa MUNGU kuliko Yeye Mwenyewe alivyokuwa. Ikiwa kweli alikuwa bado anapendelewa na MUNGU, kwa nini basi alihitaji kufa? MUNGU angeweza kumwokoa kutoka katika mauti. {2T 214.2}

KRISTO hakujisalimisha kwa adui Shetani anayetesa, hata kwa kiwango kidogo (hakumpa mwanya au kujisalimisha kwake), hata katika uchungu Wake mwingi. Majeshi yote ya malaika waovu yalimzunguka MWANA WA MUNGU, ila malaika watakatifu waliagizwa kutovunja safu zao na kujiingiza katika pambano na adui mwenye kudharau, kubamiza kwa maneno na kutukana. Malaika wa mbinguni hawakuruhusiwa kuhudumia roho iliyoteseka ya MWANA WA MUNGU. Ilikuwa katika saa hii mbaya ya giza, sura ya BABA Yake ilifichwa, majeshi ya malaika waovu yakimfunika, dhambi za ulimwengu juu Yake, ndipo Maneno yalifurukuta kutoka midomoni Mwake: “MUNGU Wangu, MUNGU Wangu, mbona umeniacha?” {2T 214.3}

Kifo cha wafia dini hakiwezi kulinganishwa na uchungu aliostahimili MWANA WA MUNGU. Tunatakiwa kuchukua mtazamo mkubwa na wa kina wa maisha, mateso, na kifo cha MWANA mpendwa wa MUNGU. Wakati upatanisho unapotazamwa kwa usahihi, wokovu wa roho

utaeleweka kuwa wa thamani isiyopimika. Katika kulinganisha mpango wa maisha ya milele, mengine yote yanapelea/yanazama katika kutokuwa na umuhimu. Lakini ni kwa namna gani mashauri ya huyu Mwokozi Mwenye upendo yamedharauliwa! Moyo umetolewa kwa ulimwengu na maslahi ya ubinafsi yamefunga mlango dhidi ya MWANA wa MUNGU. Unafiki mtupu na mkubwa na kiburi, ubinafsi na faida, wivu, uovu, kudhuru na tamaa vimeijaza sana mioyo ya wengi kiasi kwamba KRISTO hana nafasi. {2T 215.1}

Alikuwa tajiri milele zote, na bado kwa ajili yetu akawa maskini ili sisi kupitia umaskini Wake tufanywe kuwa matajiri. Alivikwa nuru na utukufu na alizungukwa na majeshi ya malaika wa mbinguni wakisubiri kutekeleza amri Zake. Bado akavaa asili yetu na akaja kuishi miongoni mwa watu wadhambi. Huu ni upendo ambao hakuna lugha inayoweza kuelezea. Upendo unaopita ufahamu. Ni siri kubwa ya utauwa. Roho zetu zinatakiwa kuwa zimetolewa, inuliwa na kuwa na furaha kuu kwa madhari ya upendo wa BABA na MWANA kwa mwanadamu. Wafuasi wa KRISTO hapa wanatakiwa kujifunza kuakisi kwa kiasi fulani upendo wa ajabu na kujiandaa kujiunga na waliokombolewa wote kutoa “Sifa na heshima na utukufu na nguvu .....Kwake Yeye akaaye juu ya kiti cha enzi na kwa MWANA-KONDOO milele na milele.” {2T 215.2}

## **SURA YA 30**

### **MAONYO KWA KANISA**

Ndugu wapendwa hamsimami katika nuru kama MUNGU awatakavyo. Nilielekezwa nyuma katika kusanyiko, wakati majira ya kuchipua yaliyopita, na nilioneshwa kwamba akili zenu hazikuwa zimejiandaa kwa kazi hiyo. Hamkutarajia wala kuamini kwamba kazi kama hiyo ingekamilishwa hatimaye miongoni mwenu. Lakini kazi iliendelea bila kujali kutoamini kwenu na ushirikiano wa wengi miongoni mwenu. {2T 216.1}

Wakati mlikuwa na ushahidi namna hiyo kwamba MUNGU alikuwa anangoja kuwa na rehema kwa watu Wake, kwamba sauti ya rehema ilikuwa ikiwaalika wadhambi na waliorudi nyuma, waelekee msalaba wa KRISTO, kwa nini hamkuungana na wale waliokuwa na mzigo wa kazi juu yao? Kwa nini hamkuja kumsaidia BWANA? Baadhi yenu mlionekana kana kama mmekufa ganzi, mmepigwa butwaa, mmeshangazwa na mlikuwa hamjajiandaa kushiriki kikamilifu katika kazi. Wengi walikubaliwa lakini mioyo yao haikuwa katika hilo. Hii ilikuwa ni ushahidi mkubwa wa hali ya uvuguvugu ya kanisa. {2T 216.2}

Hali yenu ya udunia haitawapa motisha kufungua wazi mlango wa mioyo yenu migumu wakati wa kubisha Kwake YESU, ambaye anatafuta kuingia hapo. BWANA wa utukufu ambaye amewakomboa

ninyi kwa damu Yake Mwenyewe alisubiri mlangoni mwenu kwa ukaribisho lakini hamkusukuma mlango na kufuungua wazi ili kumkaribisha ndani. Baadhi walifungua mlango kidogo na kuruhusu nuru ndogo ya uwepo Wake kuingia lakini hawakumkaribisha Mgeni wa kimbingu ndani. Hakukuwa na chumba/nafasi kwa ajili ya YESU. Mahali ambapo pangetunzwa kwa ajili Yake, palijawa na vitu vingine: “Tazama nasimama mlangoni nabisha mtu akiisikia sauti Yangu na kuufungua mlango nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye na yeye pamoja Nami” kulikuwa na kazi kwa ajili yenu kufanya, kufungua mlango. Kwa muda mlijisikia kukubali kusikia na kufungua mlango lakini hata huo mwelekeo uliondoka, na mlishindwa kushiriki na Mgeni wa mbinguni ambaye ilikuwa upendeleo kumpata. Baadhi hata hivyo walifungua mlango na kwa moyo mkunjufu walimkaribisha Mwokozi wao. {2T 216.3}

YESU hatakulazimisha ufungue mlango. Lazima mfungue wenyewe, na kuonesha mnataka uwepo Wake kwa kumkaribisha kwa dhati. Kama wote wangefanya kazi madhubuti katika kusafisha uchafu wa ulimwengu na kuandaa mahali kwa ajili ya YESU, Yeye angeingia na kukaa nanyi na angefanya kazi kubwa kupitia ninyi kwa ajili ya wokovu wa wengine. Lakini hata hivyo hamkuwa mmejiandaa kwa ajili ya kazi, ambayo ilianza miongoni mwenu kwa nguvu kubwa. Waliorudi nyuma walirejeshwa, wadhambi waliongolewa na sauti ilivuma katika maeneo yaliyozunguka. Jumuiya iliamshwa. Ingekuwa Kanisa limekuja kumsaidia BWANA na njia ingekuwa imefunguliwa kikamilifu kwa kazi zaidi, kazi ingekuwa imekamilishwa ---- na ----- na maeneo yote yanayozunguka, kwa namna ambayo hamjawahi kushuhudia. Lakini akili za ndugu hazikuamshwa na zilikuwa kwa kiasi kikubwa tofauti na swala husika. Baadhi ambao daima wamekuwa wakitafuta faida yao, hawakuweza kufikiri, akili zao kuvutwa kutoka nafsi zao juu ya tukio hili, hata kama wokovu wa roho ungekuwa katika hatari. {2T217.1}

BWANA ameweka mzigo juu yetu. Tulikuwa tayari kuwapa ninyi kile tulichokuwa nacho kwa wakati huo, kama mngekuja pamoja nasi kumsaidia BWANA. Lakini katika hili, kulikuwa na kushindwa kwa wazi. Kukosa shukrani kukubwa kulioneshwa kwa ishara za nguvu za MUNGU miongoni mwenu. Endapo mngepokea ishara za rehema na

wema wa MUNGU kama iwapasavyo kwa mioyo ya shukrani, na kuunganisha shauku kutenda kazi na ROHO wa MUNGU, msingekuwa katika hali yenu ya sasa. Lakini kwa kuwa ile kazi ya thamani ilifanywa miongoni mwenu, mmekuwa mkididimia chini na kunyauka kiroho. {2T 217.2}

Mfano wa kondoo aliyepotea bado hamjauelewa. Hamjajifunza bado somo la Mwalimu wa mbinguni alivyokusudia muelewe. Mmekuwa wanafunzi wasio na wepesi kuelewa masomo-wazito kuelewa mnayofundishwa. Someni mfano katika Luka 15: “Ni nani kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na kenda nyikani, aende akamtafute yule aliyepotea hata amwone? Naye akiisha kumwona, humweka mabegani pake akifurahi. Na afikapo nyumbani kwake huwaita rafiki zake na jirani zake akawaambia, furahini pamoja nami kwa kuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea.” {2T 218.1}

Hapa kuna taarifa za wengi ambao walirudi nyuma kiroho nao walikuwa gizani kwa kuwa walitoka kundini. Lakini kisa mahsusi kilikuwa ni kile maarufu cha ndugu A, juhudi zote hazikufanywa, ambazo zilipaswa kufanya, kwa hekima, ili kumzuia kondoo asitoke kundini na alipotoka nje ya kundi na kutangatanga, juhudi za dhati hazikuwekwa katika kumrudisha. Kulikuwa na umbea mwingi juu ya jambo lake kuliko huzuni ya dhati juu yake. Mambo yote haya yalimzuia kuja

kundini na kufanya moyo wake kutenganishwa mbali zaidi na ndugu zake na kufanya ukombozi wake kuwa mgumu zaidi. Njia hii ni tofauti kwa jinsi gani, kwa kulinganisha na ile iliyofuatwa na mchungaji katika mfano wa Yesu, wakati wa kumtafuta kondoo aliyepotea. Tisini na kenda wote waliachwa katika nyika wajichunge wenyewe, waliachwa katika hatari, bado kondoo mmoja aliyejitenga kutoka katika kundi alikuwa katika hatari kubwa zaidi na kwa kumtafuta mmoja, ilibidi wale tisini na kenda waliachwa. {2Tsw 218.2}

Baadhi ya makanisa hayana shauku ya pekee kuona ndugu A amerudi. Hawajali vya kutosha na kujipinda vya kutosha kutoka katika hadhi yao na kiburi na kufanya juhudi maalumu kumsaidia kuelekea nuruni.

Walisimama nyuma ya nyadhifa zao na kusema: “Hatutakwenda kumtafuta, mwache yeye ndiye aje kwetu.” Akitazama hisia za ndugu zake dhidi yake kama alivyofanya, ilikuwa vigumu kwake kufanya hili. Wangezingatia somo lililofundishwa na KRISTO wangukuwa wapo tayari kuacha heshima na kiburi chao na kwenda kuwatafuta waliopotea. Wangewalilia machozi, wangewaombea, wangewasihi kuwa waaminifu kwa MUNGU na Ukweli na kushikamana na Kanisa. Lakini hisia za wengi zilikuwa: “Kama anataka kwenda, mwache tu aende zake.” {2Tsw 218.3}

Wakati BWANA alipotuma watumishi Wake kufanya kazi kwa ajili ya hawa waliotanga mbali, kazi ambayo mlitakiwa kuwa mmeifanya na hata mlipokuwa na ushahidi kwamba BWANA alikuwa akitoa ujumbe wa rehema kwa hawa maskini waliotanga mbali Naye, bado hamkuwa mmejiandaa kuyaacha maoni yenu. Hamkujisikia kuwaacha tisini na kenda na kumtafuta kondoo aliyepotea mpaka apatikane, hamkufanya hilo. Na wakati kondoo alipopatikana na kurejeshwa kundini kwa furaha, Je mlifurahi? Tulijitahidi kuwaamsha. Tulijaribu kuwaita pamoja kama mchungaji alivyowaita majirani na marafiki zake, mje mfurahi nasi lakini mlionesha kutokuwa tayari. Mlijisikia kwamba kondoo amefanya kosa kubwa kuliacha kundi na badala ya kufurahia kwamba amerejea, mlikuwa na hamu ya kumfanya ajisikie kujuta sana kwa kuondoka na lazima arudi kulingana tu na mawazo yenu. Na tangu kurejea kwake, mmekuwa na hisia za wivu juu yake. Mmekuwa mkichunguza kuona kama kila kitu kipo sawa. Baadhi hawajaridhishwa kabisaj, wamejisikia kutokukubali mambo jinsi yalivyo. {2Tsw 219.1}

Hamjitambui nafsi zenu wenyewe. Baadhi wana ubinafsi ambao unapelekea kufanya ushawishi wao na jitihada zao kuwa finyu. Kuna furaha zaidi mbinguni, kwa mwenye dhambi mmoja atubuye kuliko watu tisini na kenda wenye haki wasiohitaji kutubu. Kanisa lingekuwa limejiandaa kuthamini kazi ambayo BWANA aliyokuwa anafanya miongoni mwao, hatimaye wangukuwa na lile kusanyiko ambalo linakua imara na imara (na nguvu). Lakini badala ya wote kujitosa nafsi zao katika kazi na kuwa na nia maalumu ya dhati katika kufanya yote katika uwezo wao kufuatilia kazi baada ya kuwa tumeiacha, walifanya kana kwamba kazi haikuwahusu wao. Kwamba wao walikuwa

watazamaji tu tayari kuonyesha kutoamini na kutafuta makosa popote palipokuwa na fursa. {2Tsw 219.2}

Nilioneshwa swala la ndugu B. Huwa hana furaha. Haridhishwi na ndugu zake. Akili yake imezoezwa kwa muda kwamba ilikuwa kazi yake kubeba ujumbe. Na Inapohusika uwezo wa ujuzi wake wa Ukweli, anaweza, na anao uwezo huo, lakini anapungukiwa nidhamu na uungwana. Hajajifunza kuitawala nafsi yake. Inahitaji hekima kubwa kushughulika na akili za watu na hajafuzu kwa kazi hii (Hana sifa kwa hiyo kazi). Anaelewa nadharia lakini hajajielimisha mwenyewe katika subira, uvumilivu, upole, wema na adabu ya Kweli (kuheshimu watu). Kama kitu chochote kikiibuka ambacho hakipatani na mawazo yake, hawezi kutulia kwa kujali kama ni hekima kukishughulikia au kukiacha kipite mpaka hapo kitakapokuwa kimecheuliwa/kimefikiriwa kikamilifu. Hujifurukuta mara moja kwa ajili ya vita. Ni mkali, mkorofi, mpenda kulaumu na kama vitu havipatani na mawazo yake anaamsha fujo mara moja. {2Tsw 220.1}

Anashikilia katika tabia ya utu wake vipengele vya vita kuliko vya amani, mapatano na utulivu. Hana hekima ya kuwapa watu wote sehemu yao ya chakula katika wakati husika. “Na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto na wengine wahurumieni kwa hofu mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.” Ndugu B anao ufahamu wa kufanya tofauti hii lakini kwa udogo sana. Ni mshupavu katika tabia yake (rafu) na hajali katika kushughulika kwake na roho za watu. Hili linafanya asiwe na sifa ya kuwa mchungaji mwenye busara na uangalifu. Mchungaji lazima awe na vitu vifuatavyo katika tabia yake; ukarimu mzuri, ujasiri, uvumilivu, upendo na utunzaji wenye huruma nyororo. {2Tsw 220.2}

Ndugu B. atakuwa katika hatari ya kuharibu/kuvunja zaidi kuliko anavyoweza kujenga. Hajakusanya nguvu zake zote na kuzisalimisha katika mapenzi ya MUNGU. Hajabadilishwa bado kwa kufanywa upya akili yake. Anajitegemea mwenyewe na hategemei kikamilifu juu ya neema ya MUNGU, kazi zake hazijengwi katika MUNGU. Kuwa Mchungaji ni kuchukua nafasi muhimu, ya kuwajibika, kulisha kundi la MUNGU ni kazi iliyotukuzwa na takatifu. Ndugu B, BWANA



hakukuhesabu wewe kufaa kuwa mwangalizi wa kundi Lake. Ungekuwa unajifunza somo la kujitawala nafsi katika uzoefu wako wa kidini, serikali yako binafsi na ungehisi ulazima wa kuinua akili na kuutakasa moyo wako kwa utakaso wa ROHO MTAKATIFU, na kuleta nguvu zako zote kuzisalimisha katika mapenzi ya MUNGU, ukitafuta unyenyekevu na upole, ungekuwa sasa kuwa katika nafasi ya kufanya vizuri na kutumia ushawishi ambao ungekuwa unainua na kuokoa. {2Tsw 220.3}

Ndugu na Dada B, mna kazi ya kufanya wenyewe, ambayo hamna mwingine anayeweza kuifanya kwa ajili yenu. Mna tabia ya manung'uniko na malalamiko. Mna jambo la kufanya kushinda hisia zenu za asili. Ishini kwa ajili ya MUNGU wenyewe, mkijua kwamba hamtakiwi kutoa hesabu kwa ajili ya makosa ya wengine. Niliona ndugu B kwamba hakika utashindwa na Shetani na kuvunja Imani kabisa isipokuwa uache tabia ya kutafuta makosa na utafute dini safi isiyo na taka mbele za MUNGU (1 Timotheo 1:19). Unahitaji kuinuliwa katika mawazo yako na maongezi yako, unahitaji uongofu wa dhati na kamili. {2Tsw 221.1}

Uzima au mauti vipo mbele yako. Unatakiwa kuchukulia kwa uzito kwamba unashughulika na MUNGU Mkuu, na daima lazima ukumbuke kwamba Yeye siyo mtoto wa kuchezeza. Huwezi kujihusisha katika huduma Yake kama upendavyo, na kuiacha ukiamua. Nafsi yako kwa ndani kabisa inabidi iongoke. Wote walio kama wewe, ndugu yangu, wameshindwa kukua katika neema ya MUNGU na katika utakatifu kamili katika Jina Lake, katika siku hizi za hatari na majaribu, watakutana na hasara kubwa sana. Msingi wao utadhihirisha kuwa mchanga unaodidimia, badala ya MWAMBA KRISTO YESU. {2Tsw 221.2}

Unakwenda kwa msukumo/mihemko. Unahisi kutokupatanishwa kwa ndugu zako kwa sababu haujatamwa kuhubiri Ukweli. Haufai kuaminiwa katika hili. Zaidi ya mhubiri mmoja aliye mwenye ufanisi atahitajika kufuatilia nyuma pale ulipopita kuamsha watu ili kufunga majeraha na michubuko ambayo kushughulika kwako kwa ukali

kutafanya. MUNGU hapendezwi na wewe na nina hofu kwamba utashindwa kupata uzima wa milele. {2Tsw 221.3}

Hauna muda wa kupoteza. Fanya bidii kubwa kujinusuru nafsi yako kutoka kwenye mtego wa Shetani. Unatakiwa kujifunza kwa YESU ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, ndipo utapata raha. Oh, ni kazi gani unatakiwa kufanya kuelekea utakatifu kamili katika kicho cha MUNGU na kuwa tayari kwa ajili ya jamii ya malaika safi na watakatifu. Unatakiwa kunyenyekeza moyo wako mbele za MUNGU na utafute upole na haki, ili uweze kufichwa katika siku ya hasira ya kutisha ya BWANA. {2Tsw 222.1}

Ndugu B, BWANA aliacha baraka yake itulie juu yako majira yaliyopita ya machipuko lakini haukuona uhusiano ambao kukesha na maombi vinategemeza maendeleo katika maisha matakatifu. Umepuuzia wajibu huu na matokeo ni giza ambalo limekuzingira. Umekuwa katika hali ya mashaka na kutoamini, na mara kwa mara umechagua jamii ya wale walio katika giza, wale ambao Shetani anawatumia kutawanya kutoka kwa KRISTO. Ungeweza kuishi miongoni mwa watu waovu na kubaki bila madoa, mtu safi, usiye na waa kama MUNGU katika hekima Yake ndivyo alivyokuelekeza. Lakini ni hatari kwa wale wanaotaka kumheshimu MUNGU kutafuta furaha yao na maburudisho katika makundi ya wale wasiomcha Yeye. Shetani daima huwazunguka hao kwa giza nene, na kama wale wanaomkiri KRISTO wataenda bila kutumwa ndani ya giza hili, wanamjaribu Shetani kuwajaribu wao. Ili kutenda wema na kulitukuza Jina Lake, BWANA anatutaka sisi tuende miongoni mwa makazi ya roho wachafu, ambako kuna giza jeusi, Yeye atatuzingira na malaika Zake na kututunza tusichafuliwe. Lakini tukitafuta marafiki wadhambi na kufurahishwa kwa utani wao mbaya na kuburudishwa na kuchekeshwa na hadithi zao, michezo na upuuzi, malaika wasafi na watakatifu wanaondoa ulinzi wao na kutuacha katika giza tulilochagua. {2Tsw 222.2}

Ndugu B, ninataka kukutahadharisha, ninataka kukuamsha katika utendaji. Ninataka kukusihi umtafute MUNGU akingali bado anakualika wewe uje Kwake ili uwe na uzima. Kesha, omba, fanya kazi, “Ni kaulimbiu ya Wakristo. Shetani yu macho katika kazi zake, uvumilivu

wake hauchoki, ari yake ni ya dhati na ya kudumu. Hasubiri mawindo yake yaje kwake, anayatafuta mwenyewe. Kupora roho toka katika mkono wa KRISTO ni kusudi lake alilodhamiria, halafu Wakristo wamelala katika upofu wao na wendawazimu katika shughuli zao. MUNGU Hayupo katika mawazo yao. Adui mwangalifu, na anayekesha yupo juu ya njia yao, na bado hawapo katika hatari ikiwa wanamfanya MUNGU tumaini lao. Lakini isipokuwa wametenda hili, nguvu zao zitakuwa udhaifu na watashindwa na Shetani. {2Tsw 222.3}

Ndugu B, ni hatari kwako kuendekeza mashaka. Lazima ujizuie kwenda mbali zaidi katika muelekeo ambao umekuwa ukienda. Upo katika hatari daima. Shetani yuko njiani mwako, akipendekeza mashaka na kusababisha kutoamini. Kama ungesimama imara katika mashauri ya MUNGU, ungeweza kupata ushawishi kwa ajili ya wema juu ya wale wanaopenda jamii yako sasa. {2Tsw 223.1}

Maskini ndugu C alitambua uwepo wa ROHO WA MUNGU, lakini alipungua katika uzoefu. Hakubadilika kikamilifu kutoka kwenye tabia zake za zamani. Alishindwa kumfanya MUNGU nguvu zake daima na miguu yake ikateleza. Hakuna ushirika kati ya KRISTO na Beliali. Ungeweza kumsaidia, kama ungekuwa umeunganishwa na mbingu kama ulivyotakiwa kuwa. Lakini njia yako ya kutojishughulisha, tabia yako ya mazungumzo, na ushawishi wako vimemuimarisha katika kurudi nyuma kwake na kuinyamazisha sauti ya dhamiri ndani yake. Njia yako haikuwa karipio katika njia yake ya kwenda chini (kurudi nyuma). Ungeweza kufanya vyema, kama ungekuwa unaishi kwa ajili ya MUNGU. Nguvu zako ni udhaifu kabisa, hekima yako ni upuuzi tu, lakini wewe haujui hilo. Umekuwa ukiridhishwa sana na nadharia, fundisho sahihi la imani lakini haujatambua ulazima wa nguvu ya MUNGU, umepuuzia upande wa kiroho wa dini. Utu wako wote unatakiwa ulie kwa ajili ya ROHO WA MUNGU, maisha na nguvu ya dini ndani ya nafsi ambayo itaongoza kuelekea kusulubishwa kwa nafsi na tumaini imara kwa Mwokozi wako.{2Tsw 223.2}

Upo katika giza baya na isipokuwa utainuka katika Jina la MUNGU na usambaratishe minyororo ya Shetani, kwa kuivunja na kudai uhuru wako, utaharibu imani. Kwa kiasi kikubwa sana BWANA Hayuko tayari

kukuacha na kwa kiasi hicho ndivyo ulivyo upendo Wake kwako ingawa maisha yako hayajawa yakiendana na mapenzi Yake na kazi zako na njia zako zimekuwa zikimchukiza, Mtukufu wa Mbinguni amejishusha chini ili kukuomba fursa ya kukutembelea na kukuachia Baraka: “Tazama, nasimama mlangoni nabisha” makazi ya utukufu ni Yake, na hiyo furaha inayokaa kwenye nyumba za mbinguni, Naye bado anajinyenyekeza kutafuta kuingia katika mlango wa moyo wako, ili akubariki na nuru Yake na kukufanya wewe ufurahie katika utukufu Wake. Kazi Yake ni kutafuta na kuokoa kile kilichopotea na kipo tayari kuangamia. Yeye Anataka kuwaokoa wengi kadri awezavyo kutoka katika dhambi na kifo, ili awanyanyue katika kiti Chake cha enzi awape uzima wa milele. {2Tsw 224.1}

Ndugu B, nakuomba uamke na kutupilia mbali mashaka yako. Nini kinakufanya wewe uegemee mashaka? Ni maisha yako ya kutangata mbali toka kwa MUNGU, maisha yako ya kutojitoa wakfu, na kutokuwa mcha Mungu, utani wako na mizaha. Kukosa kwako umakini kunahatarisha faida yako milele. KRISTO anakualika wewe kughairi kutoka huu upuuzi. Haukui katika neema na katika ufahamu wa Kweli. Wewe huleti heshima kwenye kazi ya Mungu. Haukui lakini unazama chini na chini katika mizani. Haujengi tabia kwa ajili ya mbinguni na uzima wa milele. {2Tsw 224.2}

Wewe unajipendeza nafsi yako tu, ukipoteza muda katika yasiyo maana na upuuzi, muda ambao ungetumia na familia yako, ukifundisha/ukiwaboresha watoto wako katika njia na maagizo ya MUNGU. Je, ni Hesabu gani utatoa kwa MUNGU kwa kuchezea muda? Je, ni mvuto gani ulio nao juu ya wale ambao hawana kicho cha BWANA mbele yao? “Vivyo hivyo nuru yenu iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema wamtukuze BABA yenu aliye mbinguni.” Hebu MUNGU akutakase macho yako ili uweze kuona hatari. Nafikiri kwa kina kwa ajili yako. Moyo wangu unakuonea huruma kwa kina. Nina hamu ya kukuona unapanda katika viwango vya juu ambavyo ni fursa yako kuvifikia. Unaweza kufanya vyema-mema. Mvuto wako, kama ukitumika katika upande sahihi, utazungumza. Ndugu B, hatua zako zipo katika njia iendayo chini. “Ghairi, ghairi,” mbona unataka kufa?” {2Tsw 224.3}

Kama utaendelea zaidi kufuata njia unayoiendea sasa utakuwa kafiri kulingana na Ukweli na kulingana na Neno la MUNGU. Kesha na uombe daima. Jitoe nafsi yako kikamilifu kwa BWANA, ndipo haitakuwa vigumu kumtumikia. Una moyo uliogawanyika. Hii ndilo sababu giza badala ya nuru linakuzingira. Ujumbe wa mwisho wa rehema sasa unatolewa. Ni ishara ya uvumilivu na huruma ya MUNGU. Njoo! Ndiyo mwaliko unaotolewa sasa. Njooni! kwa maana vitu vyote viko tayari sasa. Huu ni mwito wa mwisho wa rehema. Baadae kitakuja kisasi cha MUNGU Mwenye ghadhabu. {2Tsw 225.1}

Ndugu B, himiza unyenyekevu, upendo, subira na umoja mzuri na ndugu zako. Lakini usi....., oh, usiuze uzima wa milele kirahisi hivyo. Kama utaenda kinyume na Ukweli kamwe hutajua furaha ya kweli utakuwa mwenye kuhuzunika daima hakika. Mbingu ina thamani inayostahili kufanya kila kitu na kwa gharama yoyote. Vunja vifungo vya Shetani. YESU sasa anakualika wewe; Je, utaisikia sauti Yake? Lazima uchukue msimamo wa juu kuliko uliofanya huko nyuma. Fanya iwe ni shuguli yako ya kwanza kupata ufalme wa mbinguni na haki ya KRISTO. Ishi kwa ajili ya MUNGU na mbingu, na zawadi ya milele itakuwa yako mwishoni mwa shindano/pambano. {2Tsw 225.2}

## **SURA YA 31**

### **KUTAFAKARI NDOA**

Nilielekezwa nyuma mwezi wa Mei ambapo BWANA alizuru.....na nilioneshwa jambo la Ndugu D. hakuwa tayari kuchukua sehemu katika kazi hiyo. Mawazo yake na moyo wake vilikuwa mahali pengine. Alikuwa akitafakari ndoa na hakuweza kusikiliza mwaliko wa YESU: "Njooni; kwa maana vitu vyote vimefanywa tayari." Tafakari ya ndoa yake ilizingira umakini wake. Hakuwa na muda au mwelekeo wa kufungua mlango wa moyo wake kwa mgeni mkarimu Mwenye Neema,

ambaye alikuwa anatazamiwa. Angefanya hivi, KRISTO angempa mashauri mazuri ambayo kama yakizingatiwa, yangekuwa ya thamani isiyo na kifani kwake. Angewasilisha mbele yake katika nuru yake ya Kweli hatari ya kusikiliza maagizo ya mwelekeo wa ukaidi na kuacha kando utukufu wa MUNGU na maamuzi ya lengo makini. Angemuagiza kuwa makini jinsi anavyotembea katika hatua za wale ambao wameanguka na wameharibikiwa. Lakini huyu ndugu hakujali kwamba MUNGU ana madai juu yake, kwamba anatakiwa kutofanya lolote bila kumuuliza Yeye ambaye amemnunua. Tunaelekezwa kwamba chochote tufanyacho tunatakiwa kufanya yote kwa utukufu wa MUNGU. {2Tsw 225.3}

Je, wewe Ndugu D, kama mfuasi, mtu anayejifunza, mwanafunzi wa KRISTO ulienda Kwake kwa unyenyekevu, ombi la dhati na kukabidhi njia zako Kwake? Ulishindwa kufanya hili. Hukuchunguza nia yako yote na kwenda kwa uangalifu ili usije ukaleta aibu juu ya kazi ya KRISTO, Mwokozi wako. Hukujali kwamba hii hatua itakuwa na athari ya kuongeza uelewa wako wa kiroho, kuhuisha ari yako, na kuimarisha uaminifu katika Kweli na bidii yako kuikana nafsi. Ulikuwa mjinga wa moyo wako mwenyewe. Kazi ya MUNGU ilionekana ndani ya kanisa, lakini hukuwa na matamania kwa ajili ya ROHO MTAKATIFU. Mambo ya mbinguni yalikuwa hayavutii kwako. Ulipumbazwa na mahaba ya kufikirika na hamu ya matumaini yako mapya ya kuunganisha maslahi yako na yale ya wengine. Hukujali kwamba munganiko wa ndoa lazima utaathiri maslahi yako kwa maisha yote, hata maisha hayo yawe mafupi kiasi gani. {2Tsw 226.1}

Ungetambua kwamba, bila kutiisha moyo wako mwenyewe ulio muovu, usingeweza kuletwa katika muunganiko na ushawishi ambao ungefanya iwe vigumu zaidi kwako kushinda nafsi, na kuifanya njia yako kwenda juu mbinguni kuwa ngumu na yenye mabonde na mawe mengi. Sasa umefanya maendeleo ya dini yako kuwa magumu mara kumi zaidi kuliko uliposimama peke yako. Ni kweli ulikuwa mpweke, kwa sababu ulipoteza kito cha thamani (mke alikufa). Lakini kama ungeshauriwa na ndugu zako na kukabidhi njia zako kwa BWANA, Yeye angefungua njia kwa ajili yako kujiunganisha nafsi yako na mmoja

ambaye angeweza kuwa wa msaada kwako badala ya kikwazo. {2T 226.2}

Kama sasa wewe utamgeukia MUNGU kwa unyenyekevu wa moyo wako wote, Yeye atakuhurumia na kukusaidia. Lakini upo palepale ambapo nguvu zako zimemalizwa na unapanga kuitelekeza imani yako na utii wako kwa MUNGU, ili kumfurahisha mkeo mpya. MUNGU akuhurumie, kwa maana uharibifu upo mbele yako isipokuwa uamke kama askari wa Kweli wa KRISTO na ujihusishe kwa upya katika vita kwa ajili ya uzima wa milele. Usalama wako pekee ni kukaa na ndugu zako na kupata nguvu zote uwezazo kutoka kwao, na kubaki katika Kweli. Upo karibu kutoa kafara ya Ukweli kwa ajili ya amani na raha hapa. Unaiuza roho yako katika soko la bei rahisi. Ni wajibu wako sasa kufanya yote uwezayo kufanya mkeo kuwa mwenye furaha na bado bila kupoteza kanuni ya Ukweli. Lazima ujizoeze uvumilivu, subira na heshima. Kwa kufanya hivyo unaweza kuonesha uwezo wa neema ya Kweli na matokeo ya ile Kweli. {2T 227.1}

Nilioneshwa kwamba kupenda fedha ni mtego kwako. Fedha, mbali na fursa, inapelekea kufanya wema, kubariki wahitaji na kuendeleza kazi ya MUNGU, yenyewe tu ilivyo, ina thamani ndogo. Kidogo unachomiliki ni mtego kwako na isipokuwa ukitumie kama wakili mwenye hekima na mwaminifu katika utumishi wa BWANA wako. itakupatia kidogo tu, lakini zaidi ni kwamba utajipatia taabu tu. Wewe ni mchoyo na mbinafsi. Unahitaji kukuza roho njema yenye ukarimu na kutenganisha mapenzi yako mbali na dunia ama sivyo utashindwa. Madanganyo ya mali yataharibu roho yako hata wema ushindwe na ubaya. Ubinafsi na kupenda mali kutashinda. {2T 227.2}

Kama wewe kaka yangu mpendwa unaokolewa itakuwa hakika ni muujiza wa rehema. Kupenda ulimwengu kunaongezeka juu yako. Kwa ungalifu zingatia Maneno ya KRISTO: “Mpende BWANA MUNGU wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote, na jirani yako kama nafsi yako. Hii ndiyo amri iliyo kuu tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii.” Kaka yangu hujazitii zote, ya kwanza wala ya

pili, ya amri hizi. Hukusita kutoka nje na kujinufaisha mwenyewe ingawa ulijua kwa kiasi kikubwa haitamfaidia kitu jirani yako. Uliangalia faida yako binafsi na kusema: “Je mimi ni mwangalizi wa ndugu yangu?” {2T 228.1}

Hauweki hazina yako mbinguni na kuwa tajiri kumwelekea MUNGU. Nafsi na faida ya kichoyo, maslahi binafsi, hutafuna utauwa wa Kweli kutoka kwa roho yako. Unasujudu kwa muungu wa ulimwengu huu. Moyo wako umetengwa na MUNGU. Mwandishi aliyevuviwa anasema: “Bali njia ya wenye haki ni kama nuru ing’aa ikizidi kung’aa hata mchana mkamilifu.” Hatua za Mkristo zaweza wakati fulani kuonekana dhaifu na kuyumbayumba, ila katika fahamu zake dhaifu, anaegemea/anategemea juu ya Mweza yote, kumsaidia. Anategemezwa na kuendelea mbele kuelekea juu kuelekea utakatifu hakika. Anapata ushindi mpya kila siku na kusogea karibu na karibu zaidi na kiwango kikamilifu cha utakatifu. Jicho lake halitazami chini duniani bali juu, daima anatazama Mfano wa mbinguni (YESU). {2T 228.2}

Ndugu D, kung’aa na kupendeza kwa vitu vya dunia viharibikavyo kumegubika vito vya mbinguni na kufanya maisha ya milele kuwa ya thamani ndogo kwako. Kama mtumishi wa KRISTO, nakusihi uamke ili uione nafsi yako jinsi ulivyo. Faida utayoipata katika njia unayoiendea sasa itakuwa upotevu wa milele. Utatambua mwishoni kwamba umefanya kosa kubwa ambalo halitaweza kuponywa/kusahihishwa. {2T 228.3}

Unaweza kushugulikia hili sasa hivi, ‘Sikia mwito wa rehema ili uishi.’ Furahia kwamba mlango wako wa rehema haujafungwa, ili sasa uweze kwa kuendelea kwa subira katika kutenda vyema, kutafuta utukufu, heshima, kutokufa, na maisha ya milele. Furahia kwamba yeye (mwanamke) ambaye amekuwa rafiki yako mwaminifu kwa miaka mingi ataamka tena wakati wa ufufuo, kile kifo kitamezwa na uzima. Angalia mbele katika asubuhi ya ufufuo wakati yeye (mwanamke) ambaye umeshiriki naye furaha na huzuni zaidi ya miaka 40 ataamka kutoka kwenye nyumba yake ya kifungo. Je, utaacha kukutazamia kwake wewe uliyekuwa mwenzi wake kuwe bure? Je, utakosekana pale



wakati sauti yake itakapopazwa kwa ushindi na furaha: “Ku wapi ewe mauti kushinda kwako? U wapi ewe mauti uchungu wako?” Oh siku hiyo italeta heshima kwa watakatifu! Hakuna aibu, dhihaka, hakuna maumivu, bali amani, furaha, na sifa zisizokoma katika kila ulimi uliokombolewa! Oh, kwamba MUNGU ataongea na moyo wako, na kukushawishi thamani ya uzima wa milele. Na uweze kuongozwa ndugu daima kuwa na tabia ya ukarimu ili ufanye wajibu wako wa uwakili kwa uaminifu na jicho ambalo limekazwa kuelekea utukufu wa MUNGU, ili BWANA aseme kwako: “Vyema mtumwa mwema na mwaminifu.....ingia katika furaha ya BWANA wako.” {2T 229.1}

## **SURA YA 32**

### **HATARI YA UTAJIRI**

Nalioneshwa kuwa baadhi wanajidanganya wenyewe kwa mitazamo yao binafsi. Wanajilinganisha na wale walio na mali nyingi, na kuhisi kuwa hawa ndio pekee wanaoipenda dunia, na wao pekee ndio walio

katika hatari ya tamaa za dunia. Bali hii si sahihi. Wale walio na vingi daima wapo katika hatari, na wanawajibika kwa talanta zote ambazo Mfalme amewakabidhi kuzitunza. Lakini wale walio na vichache vya ulimwengu huu daima wanajitunza kwa kujijali wenyewe vyema, na hawafanyi kile kilicho katika uwezo wao kukifanya, na ambacho Mungu anawahitaji watende. Daima wana fursa za kutenda wema, ila muda mwingi wanajifikiria wenyewe, na wamekariri/wamejifunza kujiridhisha nafsi zao, kiasi kwamba wanafikiri hakuna njia nyingine ya kuweza kufanya. {2T 230.}

Nilioneeshwa kwamba Ndugu na Dada E walikuwa katika hatari ya mawazo yao kuwa muda wote kwenye kujifikiria wenyewe; na zaidi Dada E alikuwa katika kosa zaidi hapa. Ana kiwango kikubwa cha ubinafsi kilichopitiliza, anajipenda mwenyewe kupindukia. Wewe Dada yangu, umejiandaa vibaya kusimama katika siku ya ghadhabu ya Mungu. Haufuati Kielelezo halisi, Yesu. Hakukuwa na hata tendo hata moja la ubinafsi maishani Mwake. Wewe unayo kazi ya kufanya ambayo hakuna mwingine awezaye kuifanya kwa niaba yako. Jitenge mbali na choyo, na jifunze nia na mapenzi ya Mungu. Jifunze kujionesha kukubaliwa mbele ya Mungu. Una papara, mihemko, haupo makini, na una asili ya kukereka kirahisi na kutoridhika na mambo madogo-madogo yasiyo na maana. Unafanya kazi sana kuliko uwezo wako. Hakuna faida katika hili, maana Mungu hahitaji hilo. Msingi wake ni ubinafsi. Dhamiri yako haistahili kupongezwa. Unakwepa majukumu, kazi na uwajibikaji, na unahisi kama unahitaji kupendelewa, kupewa kipaumbele. unapaswa kujutia, kusikitika kwamba tangia utoto wako umekuwa ukidekezwa na kupendelewa, na mapenzi yako yameachwa bila kusalimishwa. Sasa, katika umri mkubwa, unayo kazi ya kufanya ambayo ilipaswa kufanywa katika umri wa utoto. Mume wako amejisalimisha kuendekeza matakwa yako yasiyo ya kawaida na kuruhusu tamaa zako, jambo ambalo linakuletea madhara {2T 230.1}

Ubinafsi, ambao hujidhihirisha wenyewe katika namna mbalimbali kulingana na mazingira, na upekee wa mtu mwenyewe alivyo, lazima ufe. Kama ungekuwa na watoto, na akili yako ingeshawishika kujitenga nawe ili upate kuwalea, kuwaelekeza, na kuwa kielelezo kwao, ingekuwa kwa faida kwako. Umeita umakini na uvumilikvu kuelekea

kwako nyumbani mwako, vitu ambavyo vinapaswa kwenda kwa watoto. Umakini huu unaotaka upewe, ni lazima utaupata. Lakini hujaona kama ni jukumu lako kuwajali wengine, ama kutafuta kuwasaidia wengine. Wewe ni mkaidi, unataka kufanya mapenzi yako tu, na upo tayari kutekeleza mipango yako. Wakati kila kitu kinapokuwa ni rahisi katika njia yako, unadhihirisha matunda ambayo tunatarajia kuona yakizaliwa na Mkristo; lakini unaposukwasukwa au kukasirishwa katika njia yako matokeo yanakuwa kinyume. Kama mtoto aliyedekezwa anayestahili adhabu, una vipindi unavyokuwa na ukaidi wa kudhamiria. Wakati watu wawili wanapoanzisha familia, kama ilivyo katika suala lako, wanakuwa hawana watoto ambao wanaweza wakafunza uvumilivu, wakawaonyesha upendo wa kweli au subira kutokana na utendaji wao wa kitoto, **hawawezi kujitawala na kuwa na mapenzi ya Kweli**, basi kuna haja ya kuwa mlinzi makini ili ubinafsi usije ukajiinua ndani yako wewe mwenyewe kuwa kitovu cha mambo yote, utunzaji, ukiitisha umakini, na kuhitaji kila mtu akuonyeshe usikivu, kujali, na kupendezwa na maslahi yako, wakati ambapo wewe mwenyewe huoni kama una wajibu wowote kwa watu wengine kuwapa haya. Malezi ya watoto katika familia hufanya iwe lazima kwamba sehemu kubwa ya muda itumiwe nyumbani, ili kutoa fursa kwa kufundisha nidhamu na tabia akilini na moyoni kuhusiana na shuguli za kawaida za nyumbani. {2T 230.2}

Unapuza kulinda moyo wako na unapuza kutenda mema kwa mali ambayo Mungu amekupa. Ushawishi wako ungekuwa na faida endapo ungehisi kwamba msaada ulihitajika kwako, kwa wale ambao wanahitaji kutiwa moyo na kuimarishwa. Lakini kwa muda mrefu umejifunza kujifurahisha mwenyewe na kushindwa kuwa msaada kwa wale majirani wanaokuzunguka. Unahitaji nidhamu ya kutawala nafsi yako mwenyewe, ili upendo wako na fikra zako ziwe chini ya udhibiti. Tumia muda kujichunguza binafsi, ili uweze kusalimisha nguvu zako zote na uwezo wako wote kutii na kutenda mapenzi ya Mungu. Umejifungia mwenyewe na ubinafsi. Ni fursa ya kila Mkristo wa Kweli kushinikiza na mvuto wa wema kwa kila mtu atakayehusiana naye katika maisha. {2T 231.1}

Wewe dada yangu, utalipwa kulingana na matendo yako. Chunguza kwa karibu sana nia inayokusukuma kutenda, kisha amua kwa busara, uone kama wewe ni tajiri wa matendo mema au la? Nilirejeshwa nyuma kwenye majira ya kuchipua yaliyopita (April-June) yaliyopita Bwana alipokuwa anafanya kazi nzuri huko na jirani. Malaika wa rehema walikuwa wakizunguka juu ya watu Wake, na mioyo ambayo haikumjua Mungu na Kweli iliguswa moyo sana. Bwana angeliendeleza mbele kazi aliyoianzisha kwa neema, ikiwa ndugu wanalikuwa wanafanya kazi kwa mpango, kama ilivyokuwa inapaswa kuwa. Umeshauriana na mapenzi yako mwenyewe kwa muda mrefu na kufanya kila kitu kuendana na kile ambacho ni rahisi kwako, chochote kilichokugharimu au ilibidi ukifanyie shuguli ulikifungia mlango hata ule mlango ambao ungesaidia kuendeleza kazi ya Mungu. {2T 231.2}

Ulifanya sehemu yako, na watu wengine walihisi kurudi nyuma, wakihofia gharama na kuhesabu kuwa wangelipoteza muda kuhudhuria mikutano ya efoti kama juhudi ingefanywa. Jitihada ya Kikristo ilikosekana. Ulimwengu ulikuwa mbele yetu ukigaragara katika maovu, ukifunuliwa katika hasira/ghadhabu ya Mungu na roho masikini zilizoshikiliwa na mkuu wa giza na bado wale ambao walipaswa kuwa macho na kushirikishwa katika kazi bora kuliko kazi zote, yaani suala la wokovu wa roho zinazoangamia, hawakuwa na shauku ya kutosha kufanya kila juhudi na kutumia kila mali ili kuzungusha wigo na mipaka na hivyo kuziba njia ya uharibifu na kugeuza nyayo za wale wanaoteleza wakielekea njia ya uzima. Uzima wa milele unapaswa kuwa matamania/maslahi ya kina ya kila Mkristo. Kuwa mtenda kazi pamoja na Kristo na malaika wa mbinguni katika mpango mkubwa wa wokovu! Ni kazi gani inayoweza kuwa na uzito kwa kulinganishwa na kazi hii! Kutoka katika kila roho inayookolewa kumjia Mungu ni mapato ya utukufu ya kuakisiwa juu ya yule aliyeokolewa na pia juu ya aliye chombo/njia ya wokovu. {2Tsw 232.1}

## SURA YA 33

### ARI YA KIKRISTO (CHRISTIAN ZEAL)

Kuna ari/usongo wenye kelele, ambao hauna lengo au kusudi, ambao hautokani na maarifa, ambao ni mpofu katika utekelezaji wake na uharibifu katika matokeo yake. Hii sio juhudi (usongo) ya Kikristo. Juhudi ya Kikristo hutawaliwa na kanuni na isiyotokea yenyewe tu bila utaratibu, au ya hapa na pale tu. Ni bidii ya kina na yenye nguvu, huusisha nafsi yote na kuamsha mazoezi ya utii na kimaadili. Wokovu wa roho na shauku ya ufalme wa Mungu ni mambo ya umuhimu wa hali ya juu, kupita yote. Ni Kitu gani kinachohitaji bidii zaidi kuliko kuokoa roho zinazoangamia na utukufu wa Mungu? Kuna mambo ya muhimu ya kuzingatiwa hapa ambayo hayawezi kuchukuliwa kirahisira-hisi! Mambo yenye uzito ni kama suala la umilele. Hatima ya umilele ipo hatarini. Wanaume na wanawake wanaamua kwa uzima wa milele au maafa/ole. Ari ya Kikristo haitojichosha yenyewe katika mazungumzo bali itahisi na kutenda kwa nguvu na ufanisi. Lakini bado juhudi ya Kikristo haitatenda kwaajili tu ya kuonekana. Unyenyekevu utaonekana katika kila hatua na matendo yatakayokuwa yanafanyika. Ari ya Kikristo itapelekea kuwa na maombi ya dhati na bidii, kujinyenyekeza. na maisha ya uaminifu katika shughuli za kawaida za nyumbani. Ndani ya familia kutaonekana upole na upendo, ukarimu na huruma ambayo daima ni matunda ya juhudi na ari ya Kikristo. {2Tsw 232.2}

Nilioneshwa kuwa lazima uchukue hatua ya kusonga mbele. Hazina yako mbinguni, dada E, sio kubwa, wewe si tajiri kwa Mungu. Ni ombi langu kuwa Mungu akufumbue macho yako uone, na moyo wako uhisi ili ikusaidie kudhihirisha ari ya Mkristo. Loo! Ni wachache kwa kiasi gani wanaohisi thamani ya roho! Ni wachache kiasi gani walio tayari kujitoa kikamilifu kuleta roho kwa kweli ya Kristo! Kuna maneno mengi tu, maneno mengi ya kukiri upendo kwa roho zinazopotea; lakini kuzungumza tu bila kutenda si kitu, kwani mazungumzo yasiyo na

thamani kabisa. Ni ari ya Kikristo yenye bidii ndio inayohitajika, ari itakayoonyeshwa kwa kufanya kitu. Wote ni lazima sasa wafanye kazi nafsini mwao wenyewe, na watakapokuwa na Yesu mioyoni mwao, watamdhihirisha na kumshuhudia kwa wengine. Ni hakika kuwa nafsi iliyompokea Yesu haiwezi ikanyamazishwa isitangaze habari za Yesu kwa watu wengine. Hii ni sawa na kutokuweza kuzuia maporomoko ya maji ya mto Niagara Canada, yanapotiririka. {2T 233.1}

Nilioneshwa kuwa ndugu F. amezikwa kwenye takataka za ulimwengu. Hawezi kupata muda wa kumtumikia Mungu, hata ule wa kusoma Neno kwa bidii na kuomba ili kujua ni nini Bwana angemtaka afanye katika maisha yake. Talanta yake imezikwa huko ardhini, mahangaiko ya kila siku ya maisha yamemeza shauku yake ya mambo ya uzima wa milele. Ufalme wa Mungu na haki ya Yesu Kristo sio kipaumbele cha kwanza katika maisha yake, bali cha pili. Anapenda sana biashara yake, lakini niliona ni mpaka abadilishe mwelekeo wake, vinginevyo mkono wa Bwana utakuwa kinyume chake. Anaweza akakusanya vingi lakini Bwana atatapanya. Angeweza kufanya vizuri, lakini wengi wamekuwa na fikra kama watafanikiwa biashara zao, hawawezi kufikiria kufanya chochote kwa ajili ya wokovu wa roho zinazopotea, wala hawafikiri kundeza kazi aliyoianziasha Mwokozi wao. Wanasema hawawezi kufanya mambo nusu-nusu hivyo wameachana na wajibu wao wa mambo ya kidini, na kuzama katika mambo ya dunia. Wanafanya biashara zao kuwa kipaumbele cha kwanza na kumsahau Mungu, na Yeye hafurahishwi nao. Ikiwa kama kuna yeyote anayefanya biashara ambayo haiwezi kumfanya akue kiroho na utakatifu kamili katika kumcha Mungu, inampasa abadili na kufanya biashara ambayo atakuwa na Yesu kila wakati. {2Tsw 233.2}

Ndugu F, hauheshimu kukiri kwako imani, ari uliyo nayo ni bidii ya kidunia na shauku yako ni ya kidunia. Hivyo unakufa kiroho. Hauelewi hali ya hatari uliyonayo, mapenzi yako kwa dunia yanameza maisha yako ya kidini, unapaswa uamke na uchukue hatua ya kumtafuta Mungu na kutubu juu ya kurudi kwako nyuma. Ungama kwa dhati juu ya mambo uliyomuudhi Mungu kisha umrudie Mungu. Wajibu wako wa kidini umekuwa tu wa kimtindo (urasmi). Haufurahii dini, kwa kuwa furaha halisi hutegemea utii wa hiari. Watu walio na utayari wa moyo

na watiifu watakula mema ya nchi. Udhihirisho wako hauonyeshi kuwa utaishi na Mungu katika ufalme Wake. Mara zingine unajihushisha tu na matendo ya nje ya kidini, lakini moyoni mwako sio hivyo. Mara zingine unashusha neno la onyo kwa wadhambi au Neno kwaajili ya Ukweli lakini umekuwa ukifanya huduma kama vile unalazamishwa, kana kwamba imetolewa kwa msimamizi wa kazi ya vibarua, badala ya kuwa huduma ya furaha na upendo wa ndugu. Ikiwa moyoni mwako utakuwa na ari ya Kikristo, majukumu magumu yatakuwa mepesi na ya kufurahisha. {2Tsw 234.1}

Kwa nini maisha ya Mkristo yanaonekana kuwa ni magumu sana kwa wengi, ni kwamba wana mioyo iliyogawanyika-ndumila-kuwili, watu wenye nia mbili, kitu ambacho kinawafanya wasiwe imara katika mapito yao yote. Endapo wangukuwa wamejaa hamasa ya bidii ya Mkristo ambayo daima ni matokeo ya kujitoa na kutakaswa kikamilifu na Mungu, badala ya kilio cha maombolezo. Badala ya kuomboleza ustawi wangu! Ustawi wangu masikini, lugha ya nafsi ingekuwa: "Sikieni kile ambacho Bwana amenitendea" hata kama wewe ungeokolewa, kitu ambacho kinatiliwa shaka katika njia unayopitia, ni kwa namna gani, utakuwa umeweka mipaka ya wema wa kile ulichokikamilisha. Hakuna roho ambayo itakuwa imeokolewa kwa kutumia juhudi zako. Je Bwana atakwambia wewe "Vema mtumwa mwema na mwaminifu?" Hivi ni kitu gani wewe umekuwa ukifanya kwa uaminifu? Kazi ngumu katika biashara na masumbufu ya maisha haya. Je, hili litaleta Maneno ya neema kutoka kwa Bwana "Vyema mtumwa mwema na mwaminifu"? {2T 234.2}

Ndugu yangu, Yesu anakupenda, Naye anakualika ugeuke papo hapo (UTurn) na kuondoa macho kwa dunia na kuyaelekeza juu ya alama ya mwito wako mkuu, ulio katika Yesu Kristo. Acha upuuzi na mizaha. Acha uzani mzito wa wakati tunaoishi ubebwe na wewe mpaka vita iishe. ,Nenda ukafanye kazi; ikiwa umejitoe wakfu kwa Mungu, mvuto wako utasema. {2T 235.1}

Wengi wa wanafamilia ya ndugu G wapo katika barabara ya inoyoshuka chini. H anaishi maisha yasiyo na lengo. Amejaa upumbavu mwingi, ubatili na kiburi. Mvuto wake haukukubaliana na jukumu teule,

haukuelekezi katika wema na utakatifu. Yeye hapendi vizuizi ambavyo dini imeweka; kwa hiyo hatosalimisha moyo wake katika mkondo wake mtakatifu. Anajipenda mwenyewe sana, anapenda raha na starehe na anapenda kujifurahisha mwenyewe. Inasikitisha na inasikitisha kweli jinsi yatakavyokuwa matokeo yake, asipobadilika mara na kuutafuta utakatifu wa Kweli wa Mungu. Anaweza kutafuta kukuza na kuinua uwezo wa mvuto wake kwa ndugu zake. Mungu anawapenda watoto kama hawa, lakini sio Wakristo. Kama wangaliweza kuishi maisha ya unyenyekevu ya Mkristo, wangukuwa wana wa nuru na watenda kazi pamoja na Mungu, wangukuwa wamishenari kwa familia zao na kwa jamii yao. {2T 235.2}



## SURA YA 34

### WAJIBU WA VIJANA

Kama tu, vijana wangeweza kuona mazuri yaliyo kwenye uwezo wao kuyatimiza, ikiwa wangemfanya Mungu kuwa nguvu na hekima yao, wasingefuata tena mwenendo wa kutojali na kupishana Naye Bwana; wasingeyumbishwa tena na ushawishi wa wale ambao hawajajitoa wakfu kwa Mwokozi, badala ya kuhisi kwamba wajibu wa mtu binafsi upo juu yao, kuweka juhudi, na hivyo waweze kutenda mema kwa na kuwaongoza wengine katika haki, wao wanajitoa wenyewe kutafuta mambo ya maburudisho na vichekesho. Wao ni wanajamii wasio na mchango katika jamii yao, na wanaishi maisha yasio na malengo kama vipepeo. Vijana wanaweza kuwa wajuzi wa ile Kweli, na wakaiamini lakini wasiishi. Watu kama hao wanakuwa na imani iliyokufa. Mioyo yao haiguswi na Neno kwa kiwango cha kugeuza mwenendo na tabia zao mbele za Mungu, na hawana hata mwelekeo wa kufanya mapenzi Yake kama wale wasioamini. Mioyo yao haipatani/haiendani na mapenzi ya Mungu; maisha yao yana uadui na Mungu. Wale ambao wamesalimisha maisha yao kwa mambo ya matumbuizo na wanaopenda kujifurahisa kwa anasa za ulimwengu, wanachukia mambo ya kidini. Je, Bwana atawaambia vijana hawa wanaokiri Jina Lake, “Vema mtumwa mwema na mwaminifu,” Isipokuwa wawe wema na waaminifu? {2Tsw 235.3}

Vijana wapo katika hatari kubwa, uovu mkubwa hutokea kutokana na wao kusoma vitu vya kipuuzi. Wanapoteza muda mwingi ambao wangetumia kwa kufanya shuguli/kibarua chenye manufaa. Wengine wanaweza hata kujinyima usingizi ili waweze kumaliza kitabu cha riwaya za mapenzi chenye vichekesho na kupotosha. Dunia imefurika/imejaa riwaya za kila aina, kuna baadhi ambazo hazionyeshi tabia ya hatari kuliko zingine, baadhi maadili yake yako chini, na zina matusi, lugha mbaya, tabia ya kihuni, zingine zimevishwa ubora wa aina fulani ila ushawishi wake ni wa kufisha. Loo! ikiwa vijana wangetafakari juu ya matokeo mabaya yanayosababishwa na ushawishi riwaya za kuisisimua katika akili zao! Je! Baada ya kusoma riwaya hizo, unaweza ukafunua Maandiko Matakatifu na kusoma Maneno ya Uzima na shauku/hamu kubwa. Je! Hauoni kwamba Biblia

haifurahishi baada ya kusoma riwaya hizo? Sumaku ya masimulizi ya kimapenzi yapo akilini, yanaharibu sauti nzuri ya akili, na yanakufanya usiweze kuidhibiti akili yako juu ya mambo ya muhimu katika Maisha, yale ya milele, Kweli makini ambayo inahusu uzima wako wa milele. Unawatendea dhambi wazazi wako unapotumia muda wao kufanya malengo, na mambo duni kama hayo, na pia unamtendea Mungu wako dhambi kwa kutumia muda ambao ugetumia kujitoa kikamilifu kwa ibada Kwake, badala ya mambo yasio na malengo. {2Tsw 236.1}

Ni wajibu wa vijana kuhamasisha unyofu, na mambo adhimu. Uzembe, upuuzi, mizaha na utani utapelekea ukavu/utasa wa kiroho na kukosa kibali cha Mungu. Wengi wenu hufikiri kuwa hamna ushawishi mbaya juu ya wengine na hivyo kuhisi kwa kiwango fulani kuridhia; Lakini Je! Una ushawishi kwa wema? Je! Unajitahidi katika mazungumzo yako na matendo yako unatafuta kuwaongoza wengine kwa Mwokozi au ikiwa wanamkiri Kristo, Je! Unawaongoza katika kutembea karibu Naye zaidi? {2Tsw 236.2}

Vijana wanapaswa kukuza roho ya ibada na uchaji-Mungu. Hawawezi wakamtukuza Mungu isipokuwa daima wanalenga kufikia kimo cha ukamilifu wa Kristo-ukamilifu katika Yesu Kristo. Hebu neema za Kikristo ziwepo na kuzidi, ndani yako (tabia na adabu ya Kikristo). Mpe Mwokozi wako mapenzi yako bora, matakatifu na makamilifu. Salimisha utiifu wako wote kwa mapenzi Yake mema. Yeye Mwokozi, hatapokea kitu chochote isipokuwa utii mkamilifu kwa mapenzi Yake. Usiondolewe katika msimamo wako thabiti kwa dhihaka, kejeli au kuzomewa na wale ambao akilini mwao wamepotoka kwa ubatili. Mfuate Mwokozi wako kwa kutotenda maovu na kwa taarifa ya matendo mema, hesabu kuwa yote ni furaha na heshima kuubeba msalaba wa Kristo. Yesu anakupenda. Yeye Alikufa kwa ajili yako. Usipomtafuta kumtumikia Yeye kwa moyo usiogawanyika, utashindwa kuwa na ukamilifu mbele Zake katika kumcha Yeye, na utalazimika kusikia Maneno ya kutisha wakati wa mwisho "Ondoka". {2Tsw 237.1}

## **SURA YA 35**

### **WATUMISHI WA MALI**

Suala la ndugu I ni la kutisha. Dunia hii ni muungu wake; anaabudu pesa, hajatii onyo alilopewa miaka iliyopita na kushinda upendo wake kwa ulimwengu wakati akiendelea kuvikuza vitivo vyake vyote. Dola/Shilingi ambazo amekusanya tangu wakati huo zimekuwa kama kamba nyingi sana za kunasa roho yake na kumfunga katika mambo ya ulimwengu. Kadri alivyopata mali amekuwa na tamaa ya kupata zaidi. Nguvu zake zote zimeelekezwa katika jambo moja, kupata pesa. Huu umekuwa mzigo wa mawazo yake, wasiwasi wa maisha yake. Ameelekeza nguvu zake zote za nafsi yake, kuwa katika mwelekeo huu mmoja, mpaka nia na madhumuni ya yeye kuwa mwabudu mamoni/pesa. Juu ya jambo hili amekuwa mwendawazimu. Mfano wake kwa familia yake ni kuwaongoza kufikiria kuwa mali inapaswa kuthaminiwa kabla ya kuthamini mbingu na hali ya kutokufa. Amekuwa kwa miaka mingi sasa, akielimisha akili yake juu ya kupata mali.

Ametoa dhabihu maisha yake ya milele kuwa kafara kwa raha ya dunia hii. Anaamini Ukweli, anapenda kanuni za Ukweli, na anapenda kuona wengine wakifanikiwa katika Ukweli; lakini amejifanya mwenyewe kuwa mtumwa wa mamoni (fedha) kabisa mpaka anahisi amefungwa kumtumikia bwana wake kwa maisha yake yote. Lakini kwa kadri anavyoishi kwa muda mrefu ndivyo anavyojisikia zaidi kujitoa katika kupenda kupata, pasipo kutupilia mbali huyu muungu mbaya, pesa. Itakuwa kama anavinyangua viungo vyake vya thamini, lakini ni lazima ifanyike hivyo kama anaithamini mbingu. {2Tsw 237.2}

Haitaji kulaumiwa na yeyote, bali kuhurumiwa zaidi na wote. Maisha yake yamekuwa ni makosa mabaya. Ameteseka kwa uhitaji wa kufikirika, wakati amezungukwa na vingi. Shetani ameteka nyara akili yake na kulisimua mwili wake kutafuta pesa, amemfanya kuwa mwendawazimu wa jambo hili. Uwezo wake wa juu, na bora wa kuishi umeletwa chini ya ubahili, na ana mwelekeo wa ubinafsi. Tumaini lakela Pekee, ni katika kuvunja kamba za ibilisi na kushinda uovu huu katika tabia yake. Amejaribu kufanya hivyo kwa kufanya kitu baada ya dhamiri yake kushugulikiwa, lakini hii haikuwa toshelevu. Huku kufanya bidii kukubwa tu na kuagana na mamoni wake kidogo na kuhisi kuwa wakati wote anaachana na roho yake, sio tunda la dini ya Kweli. Ni lazima aelemishe akili yake katika matendo mema, lazima apinge tabia yake ya kuchuma mali (kujipatia mali au fedha). Ni lazima akuze upendo wenye tabia ya kutenda mema, na kushinda roho ndogo ya umasikini, na udanganyifu katika kujipatia fedha, ambayo ameikuza. {2Tsw 238.1}

Katika kufanya biashara na wafanyabiashara huko.... Ndugu na dada sichukui njia ambayo inamfurahisha Mungu. Wafanyabiashara wengine wanajihusisha na kuchuuza au kubembeleza watu washushe bei za vitu vyao chini sana (bargain) yaani wapunguziwe bei kwa hali ya chini sana, na wanachukua muda mrefu wakiwaambia wawapunguzie visenti vichache tu, na wanazungumza jambo hili kana kwamba pesa ndiyo kila kitu kwao—muungu wao. Laiti wangerudi nyuma kule walipokuwa wakifanyia ‘dili’ zao, bila kuonekana na watu na kuyasikiliza mambo yanayozungumzwa mara baada ya wao kuondoka,

wangeweza kuelewa kwa uwazi mvuto wao wa ubahili na tamaa ya pesa ulivyokuwa. Imani yetu inadharauliwa na Mungu anatukanwa na wengine kwaajili ya uroho na ubahili huu wa tamaa ya hata senti chache. Malaika wanageuka kwa kuchukizwa. Kila kitu mbinguni ni bora na kilichoinuliwa. Wote hutafuta maslahi na furaha ya wengine. Hakuna hata mtu anayejitolea kujishugulikia mambo yake kwa ubinafsi, na kujitunza mwenyewe. Ni furaha kuu ya hawa viumbe watakatifu, kushuhudia furaha hiyo na ucheshi wa wale waliowazunguka. {2Tsw 238.2}

Malaika hawa wanapokuja kuwahudumia wale watakaokuwa warithi wa wakovu na kushuhudia wakionyesha ubinafsi, tamaa ya kuwa tajiri, kudhulumu wengine na kujinufaisha wenyewe kupitia hasara za wengine. Wanarudi kwa huzuni. Wanapowaona wale wanaodai kuwa warithi wa kutokufa wakiwa na ubahili wa kutupwa, wanaposhirikiana na wale ambao hawana matamanio ya juu kuliko kuweka hazina zao hapa duniani, wanarudi wakiwa na aibu; kwa kuwa Ukweli mtakatifu umefedheheshwa. {2Tsw 239.1}

Hakuna njia yoyote ambayo Bwana angeweza kutukuzwa vizuri na Ukweli kuheshimiwa zaidi kuliko wale wasioamini kuona namna Ukweli unavyofanya kazi kubwa na nzuri juu ya binadamu mwenye asili ya tamaa na ubahili. Ikiwa ingeweza kuonekana kuwa imani kama hiyo ina ushawishi wa kutengeneza tabia zao, kuwabadili kutoka uchoyo, ubahili, ubinafsi, tamaa, dhuluma, watu wenye kupenda pesa, waliobadilishwa kuwa watu wanaopenda kutenda mema, wanaotafuta fursa kutumia uwezo wao wenyewe kuwabariki wale wanaohitaji kubarikiwa, wanaowatembelea wajane na wasio na baba katika shida zao, watu wanaojitunza wasipatae mawaa ya ulimwengu, ungelikuwa ushuhuda kuwa dini yao ni ya Kweli. Hao wangekuwa wameruhusu nuru yao kuangaza na watu wangeona matendo yao nayo yangeongoza kumtukuza Baba yao alie mbinguni. Tunda hili lingekuwa utakatifu na wao wangelishi maisha ya uwakilishi wa Kristo hapa duniani. Wadhambi wangeshawishika kuwa kuna nguvu katika Ukweli, nguvu ambayo ni ngeni kwao. Wale wanaodai kungoja na kukesha wakitazamia marejeo ya Mwokozi wao hawapaswi kufedhehesha dai lao kwa kujadili dili la kupunguziwa bei, kwa kubishana na kushugulikia,

ili wapate mpaka senti ya mwisho. Matunda kama hayo hayakui katika mti wa Kikristo. {2Tsw 239.2}

Ndugu I, Bwana hafurahishwi na kuangamia kwako, lakini ingekuwa heri kama ungesimama imara kwa nguvu Zake na kuwa na amani Naye kwa kufanya mapenzi yako, yaendane na mapenzi Yake ya kimbingu. Kama picha yako ya uaminifu wa njia unayoufata katika pesa ingewasilishwa mbele zako, ungeogopa. Ungechukizwa na ubahili wako, na tamaa kupenda kwako pesa. Ungefanya juhudi ya maisha yako kupata neema ya Mungu inayobadilisha, ambayo ingekufanya uwe mtu mpya. Mali ambayo ilikuja kwako toka kwa ndugu ilikuwa laana kwako. Iiongeza tu tabia yako ya kupenda pesa, na ulikuwa uzito wa ziada wa kukuzamisha katika adhabu katika ile siku ya hukumu. {2Tsw 240.1}

“Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani na kujichoma kwa maumivu mengi” wakati watu wanapotumia nguvu ya akili na mwili ili kupata utajiri na kuridhika na raha ya kujiwekea utajiri ambao hawawezi kuutumia kamwe, na ambao utadhihirisha maumivu kwa watoto wao, wanatumia vibaya mamlaka ambayo Mungu amewapa. Wanaonyesha kuwa tabia zao zimefanywa mbaya kwa kukimbizia mali. Badala kutambua furaha, wana huzuni. Wamefunga milango ya roho zao kwa wahitaji, na wameonyesha ushahidi kuwa hawakuwa na huruma kwa wanaoteseka. {2Tsw 240.2}

Ndugu yangu, moyo wako sio sugu kwa mahitaji na mambo ya muhimu ya watu wengine. Una hisia za ukarimu, na unapenda kukaribisha watu. Mara kwa mara upo tayari kutenda tendo la fadhili kwa ndugu au jirani, lakini unafanya pesa kuwa muungu wako, na upo katika hatari ya kuthamini mbingu kwa kiasi kidogo mno kuliko unavyothamini fedha zako. Katika kupata pesa mara nyingi kuna hatari, isipokuwa neema ya Mungu ni kanuni inayotawala roho yako. Wakati Wakristo wanadhibitiwa na kanuni za kimbingu, watasambaza/watagawa kwa mkono mmoja wakati mwingine ukipokea. Hii ndiyo busara na afya ambayo Mkristo anaweza kuchukua wakati akiwa na pesa na akiendelea kutengeneza pesa. Tungelipenda kumuuliza ndugu I;

utafanya nini na pesa zako? Wewe ni msimamizi wa mali za Mungu. Mungu amekupatia talanta nyingi na bado unaweza ukafanya mengi mazuri nazo. Unaweza kuwekeza katika benki ya mbinguni kwa kuwa tajiri wa matendo mema. Bariki watu wengine kwa Maisha yako. “Msijiwekee hazina dunia, nondo na kutu viharibupo na wevi huivunja na kuiba; bali wekeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.” {2Tsw 240.3}

Kumbuka kuwa hazina zilizotunzwa mbinguni hazipotei. Zimehifadhiwa kwa ajili yako mwenyewe kwa maamuzi ya hekima ya mali hizo ambazo mbingu imekufanya kuwa wakili. “Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize” anasema mtume “Wasiwe na majivuno ya juu, wala wasitumainie utajiri usiokuwa na hakika, bali kwa Mungu aliye hai, ambaye ametupatia utajiri wa vitu vyote ilituweza kuvifurahia; kuwa yatende mema, ili wawe matajiri wa matendo mema, wako tayari kusambaza, tayari kuwasiliana; wakijiwekea akiba ya msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate kushikilia uzima wa milele. {2Tsw 241.1}

Kuna hatari ndugu I, ya maisha yako kupotea na zawadi ambazo Mungu amekupa kusalimishwa kwa Shetani, nawe ukafanywa mateka wa mapenzi yake mwenyewe. Je, unaweza kulibeba wazo hilo? Je, kwa maisha haya mafupi unaweza kuchagua kujitumikia mwenyewe na kupenda pesa zako, halafu ukaachana nazo zote, kisha usiwe na sifa ya kwenda mbinguni, usiwe na haki ya kuishi maisha ya umilele? Una pambano kubwa mbele yako la kutenganisha mapenzi yako kutoka katika hazina ya duniani hii. Pale hazina yako ilipo, na moyo wako pia utakuwapo. Kesha, Omba, fanya kazi, ni maneno ya kauli mbiu ya Mkristo anayekesha. Jiamshe mwenyewe nakusihi. Tafuta vitu vinavyodumu. Vitu vya dunia hii lazima vitapita haraka. Je, uko tayari kubadilishana dunia na mbingu, kutoka katika hazina za ulimwengu huu na kupata hazina za mbinguni? Je, unatengeneza tabia kwaajili ya umilele? Ikiwa utapotea hatimaye, utajua ni nini kilithibitisha uharibifu wako—ni kupenda pesa. Utalia kwa uchungu “Jamani, udanganyifu wa utajiri!” Nimepoteza roho yangu. Nimeiuza kwa fedha. Nafsi yangu na mwili niliiuza/nimebadilishana kwa ajili ya kupata pesa. “Nimeitoa mbingu kafara, nikihofia kwamba nitakosa pesa nisipojitoa kuitafuta”.

“Kutoka kwa Bwana sauti itasikika; mchukue huyo mtumishi asiye na faida, mfungeni mikono na miguu na kumtupa kwenye giza nene. Tunatumaini kuwa hii haitakuwa hatima yako. Tunatumaini utapeleka hazina yako mbinguni, na kuhamisha mapenzi yako na kuyafunga juu ya Mungu na hazina isiyokufa. {2T 241.2}

Nimeona kuwa familia nzima ilikuwa katika hatari ya kushiriki kwa kiwango fulani roho ya baba yao. Dada I, tayari umeshachukuwa mwelekeo huo, Mungu akusaidie kuona na kufanyia mabadiliko kamili. Kuza tabia ya kupenda na kutenda mema; tafuta kuwa tajiri wa matendo mema. Katika mambo mengi unaweza kufanya zaidi ya unavyofanya sasa. Una jukumu la kibinafsi mbele za Mungu. Una jukumu la kufanya, ambalo huwezi kutolea udhuru. Dumisha kutembea karibu na Mungu; omba bila kukoma. Utakuwa na kazi ya kufanya kwa ukaribu kama utaokoa nafsi yako. Tafuta kuwa na mvuto kinyume na yale matendo yasiyo sahihi katika familia yako. Chukua msimamo wako bora kwa Mungu. Mwili wako ni tofauti na wa mume wako, hivyo utahukumikiwa na Mungu kwa utofauti usipofanya mabadiliko juu yako mwenyewe. Fanya bidii ya kuokoa roho yako mwenyewe, Jaribu kuweka ushawishi ulio bora wa kuokoa familia yako. Acha mfano wako uonyeshe kuwa hazina yako iko mbinguni, ya kwamba umewekeza yote katika nyumba bora na maisha bora ambayo ni ya milele. Fundisha akili yako kuthamini mambo ya mbinguni, kuinuliwa, kumpenda Mungu na kuonyesha nia ya utii kwa mapenzi Yake. {2T 242.1}

Unaweza kupewa jaribio; unaweza kuthibitishwa jinsi mapenzi yako yalivyo na nguvu kwa mambo ya duniani. Unaweza kufanywa uelewe ukurasa wa moyo wako ambao kwa sasa haujui. Mungu anajua majaribu yako unapona hali ya mumeo na watoto wako, ambao kwa kiasi kikubwa hawana Imani iokoayo. Mengi yanakutegemea wewe kuliko vile unavyoweza kudhani. Unapaswa kuvaa silaha za vita (Efeso 6). Usitumie nguvu zako za thamani katika kazi ambayo mwingine anaweza kuifanya. Mtie moyo binti yako kushiriki kazi yenye manufaa na kukusaidia kubeba mizigo ya maisha. Anahitaji nidhamu. Akili yake ni batili, anashugulikia vitu vya kipuuzi. Anahitaji kumpa Mungu yote;



Kisha anaweza kuwa wa manufaa na kumpendeza Mwokozi wake. {2T 242.2}

Dada yangu, fanya kazi kidogo, na omba na tafakari zaidi. Maslahi ya umilele yanapaswa kuwa ya msingi kwako. Mungu amekataza kuwa watoto wako wafundishwe kuipenda pesa. Uboreshaji wa ukweli na upole wa tabia haviwezi kupatikana katika nyumba ambamo ubinafsi unatawala. Uboreshaji wa Kweli hauridhiki na kujipamba na maonyesho ya mwili. Kutakaswa na ubora wa Kweli utaonekana katika juhudi ya kuwabariki na kuwainua wengine. Umuhimu wa mambo ya umilele upo kwa kiasi kidogo sana kwa watoto wako. Hebu Mungu aweze kuwazindua kabla hawajechelewa na kisha walie kwa uchungu mkubwa: “Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka”. {2T 243.1}

Ndugu J, kesi yako iliwasilishwa mbele yangu. Una nafasi ya kuwajibika. Umekabidhiwa talanta ya pesa na ushawishi. Kwa kila mtu kazi imegawiwa –kitu cha kufanya, sio tu kushirikisha ubongo wako, mifupa na misuli katika kazi ya kawaida; inamaanisha zaidi ya hii. Unaifahamu hii kazi kutoka katika mtazamo wa kidunia, na una uzoefu ndani yake katika uwezo wa kidini. Lakini kwa miaka michache iliyopita umekuwa ukipoteza muda, na sasa utalazimika kufanya kazi haraka ili kukomboa wakati uliopita. Kuwa na talanta tu haitoshi, ni lazima sasa uzitumie sana kwa faida, sio kwako tu ila hata kwa Yule aliyekupa talanta. Yote uliyonayo ni mkopo/amana kutoka kwa Mungu wako. Yeye Atahitaji talanta aliyokupa mkononi mwako ikiwa na faida. {2T 243.2}

Kristo ana haki ya huduma yako. Wewe umekuwa mtumishi Wake kwa neema. Haupaswi kutumikia maslahi yako mwenyewe, bali maslahi ya Yeye Yule aliyekuajiri. Kama mtu anayekiri kuwa Mkristo, unawajibika moja kwa moja kwa Mungu wako. Haukupewa mali yako mwenyewe kama dhamana ya uwekezaji. Ingekuwa hivyo, ungeweza kushauriana na raha yako mwenyewe katika matumizi ya hiyo mali, Mtaji ulio nao katika biashara yako ni wa Bwana, kwa hivyo unaweza kuutumia vizuri au vibaya. Kuna njia ambayo mtaji huo unaweza ukawekezwa--uwekeze kwa wachuuzi--ili kwamba itakuwa ikimpatia Bwana faida.

Ikiwa inaruhusiwa kuzikwa duniani, Bwana wako ama wewe hamtanufaika, na utakuwa umepoteza vyote ambavyo umepewa na Bwana kama wakili. Ni ombi langu kuwa Mungu akusaidie ndugu yangu, kutambua nafasi yako halisi kama mtumishi aliyeaminiwa na kuajiriwa na Mungu. Kwa mateso Yake Mwenyewe na kifo Chake alikununua kwa kulipa fidia ili upate kumtumikia kwa huduma yako na utii ulio tayari. {2T 244.1}

Wakati wa majaribu ya miaka michache iliyopita, akili yako iliteseka na ukaona kuwa ni bora ugeuze usikivu wako kuingia kwa kikamilifu katika mambo ya dunia, kwa makusudi ya kujipatia mali. Mungu katika upendo Wake na neema Yake kuu kwako, kwa mara nyingine tena amekukusanya zizini Mwake. Majukumu mapya na wajibu sasa yamewekwa juu yako. Una mapenzi makubwa kwa hii dunia. Umekuwa ukiwekeza hazina yako duniani. Yesu sasa anakualika uhamishe hazina yako, na uiwekeze mbinguni; kwa kuwa hazina yako ilipo ndipo na moyo wako upo. Katika shughuli zako za biashara na nduguzo na pamoja na wale wasioamini, jilinde mwenyewe. Kuwa mkweli kwa imani yako na udumishe ubora wa Kweli wa roho yako, ambayo itakuwa sifa njema kwa Ukweli/imani unayokiri. {2T 244.2}

Umeshika nafasi nzuri sana ambayo watu wengine wanakutazama. Una akili nyingi zaidi ya kawaida. Wewe ni mtu mwenye utambuzi wa haraka, na hisia za kina. Baadhi ya ndugu hawajafikia kuwa na hekima hiyo. Wamekutazama wewe, na wamepata hisia kuhusu hali yako, na wametamani kwamba ungekuwa mkarimu zaidi wa mali yako. Wamejifanya wenyewe kutokuwa na furaha kwa kadri wanavyojipima na wewe. Haya yote hayawasaidii. Hawa wanapungukiwa na vitu vingi sana, na kama watakuwa wanyenyekevu katika huduma ambayo Bwana anahitaji toka kwao, watakuwa na yote watakayohitajika kwao kuyafanya. Hawawezi kudumu kupoteza muda wao kwa kuhofia kwamba Jirani zao walio na kazi nyingi watashindwa kufanya kazi yao vyema. Wakati wanaweka shauku zao kwenye mambo ya watu wengine, kazi yao wenyewe imepuuzwa na ni watumishi wavivu. Walikuwa na hamu ya kufanya kazi ya majirani zao badala ya kazi walizowajibika kuzifanya wenyewe. {2T 244.3}

Wanafikiri kwamba ikiwa wangekuwa na talanta tano za kushughulikia, wangeweza kufanya vizuri zaidi kuliko yule ambaye alikabidhiwa hizi talanta. Lakini Bwana anafahamu kwa uzuri sana kuliko wao. Hakuna anayehitaji kuomboleza kwamba yeye hawezi kumtukuza Mungu kwa talanta ambazo hakuwahi kuwapewa na ambazo hawawajibiki kwazo. Hawahitajiki kusema “Ikiwa ningekuwa katika nafasi ya mtu mwingine maishani ningefanya mengi mazuri na mtaji wangu.” Mungu hatohitaji zaidi ya kile alichokubariki nacho, kama mawakili wa neema Yake. {2T 245.1}

Talanta moja, huduma ya unyenyekevu, ikiwa imewekwa wakfu kikamilifu, na kutumiwa kukuza utukufu wa Mungu, itakubalika kama uboreshaji wa talanta nzito zaidi. Dhamana anuwai ni kulingana na uwezo wetu ulivyo. Kila mtu amepewa kulingana na uwezo wake. Hakuna anyayepaswa kupuuzia kazi yake, akiangalia kama ni ndogo sana na asiifanyie kazi vizuri. Ikiwa anafanya hivi yeye hujidanganya kwa majukumu yake ya kimaadili na hudharau siku ya vitu vidogo. Mbingu huwagawia kazi zao na inawapasa kuwa na shauku yao kuifanya kazi hiyo vizuri, kulingana na uwezo wao. Mungu anahitaji kuwa wote, wadhaifu na wenye nguvu, na kila mmoja kutimiza kazi yake aliyoteuliwa kuifanya. Riba inayotarajiwa itakuwa kwa uwiano wa kiasi kile ulichokabidhiwa. {2T 245.2}

Kila mmoja kwa uadilifu wa dhati na shauku ya moyo anapaswa kuifanya kazi yake, akiwaacha watu wengine kwa Bwana wao, wakisimama imara au kuanguka. Kuna wengi wenye usengenyaji huko....., ni wengi ambao wanafurahia tu kuwatazama ndugu zao wakifanya kazi, na kwa sababu hiyo wamekuwa dhaifu kila mara. Watatoa ushuhuda katika mkutano na sababu hawana Yesu mioyoni mwao kumkiri, watajaribu kuvutia ndugu zao kwa wajibu wao. Nafsi hizi masikini hazijui wajibu wao wenyewe, na bado wanachukua jukumu la kuwaangazia wengine kuhusu wajibu wao. Ikiwa watu kama hao watajali kazi yao wenyewe, na kupata neema ya Mungu mioyoni mwao, kungekuwa na nguvu katika kanisa ambayo sasa imekosekana. {2T 245.3}

Ndugu J, unaweza kutenda mema. Una maamuzi mazuri na Mungu anakuongoza kutoka gizani kwenda nuruni. Tumia talanta yako kwa utukufu wa Mungu. Ziweke kwa mbadilishanaji/mchuuzi, ili Bwana atakapokuja, atapokea mali Yake na fidia. Kata vishikio vyako kutoka kwa vitu visivyo na thamani vya duniani na vielekeze vimshikilie Mungu. Wokovu wa roho ni kitu cha hatima kubwa kuliko ulimwengu wote. Roho moja inayookolewa, huishi katika zama zote za umilele, kumsifu Mungu na Mwana-Kondoo, hiyo ni ya thamani zaidi kuliko mamilioni ya pesa. Utajiri huzama bila thamani ukilinganisha na thamani ya roho ambayo Kristo alikufa kwa ajili yake. Wewe ni mtu unayechukua tahadhari na husongi mbele kwa pupa. Jitoea muhanga kwa ajili ya Ukweli, na kuwa tajiri kwa Mungu. AchaBwana akusaidie unaposonga mbele haraka iwezekanavyo unapoendelea kuweka thamani inayostahii kuhusiana na mambo ya umilele. {2T 246.1}

Watoto wako wanahitaji kazi ya kina zaidi ya neema ya Mungu katika mioyo yao. Wanahitaji kukuza unyofu, kiasi na uthabiti wa tabia. Ikiwa wamewekwa wakfu kwa Mungu, wanaweza kufanya mema na kutoa ushawishi ambao utaokoa wenzao. {2T 246.2}

Hebu masikini wasifikiri kuwa hakuna kitu ambacho wanaweza kufanya, eti kwa sababu hawana utajiri kama wa ndugu zao. Wanaweza kujitoa kwa njia mbalimbali. Wanaweza kuishi maisha ya kujikana nafsi. Wanaweza kuishi maisha ya uchaji Mungu. Na katika maneno yao na matendo wanaweza kumheshimu Mwokozi wao. Wadada haswa wanaweza kuwa na nguvu ya ushawishi mkubwa ikiwa wataacha kusengenya kwao na kutumia muda wao kukesha na kuomba. Wanaweza kumtukuza/kumheshimu Mungu. Wanaweza kuruhusu nuru yao iangaze ili wengine, kwa kuona matendo yao mema, wataongozwa kumpatia Mungu wetu wa mbinguni utukufu. {2T 246.3}

Kama kielelezo cha kushindwa kwako kuja kumsaidia kazi Mungu, kama ilivyokuwa fursa yako, niliekelezwa katika maneno haya; “Umelaaniwa Merozi, alisema malaika wa Bwana, walaani kwa uchungu wenyeji wake; kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu” Waamuzi 5:23. Je, Merozi alikuwa amefanya nini? Hakuna chochote. Na hii ndiyo ilikuwa dhambi

yao. Wao hawakwenda kuwa msaada kwa Bwana dhidi ya mashujaa (sin of omission-kutofanya). {2T 247.1}

## SURA YA 36

### KUONGOZWA NA HISIA NA KUENZISHA WENZI

(Mwanamume na Mwanamke kwaajili ya ndoa au uhusiano wa kimapenzi)

Mpendwa Dada K, katika maono niliyopewa Juni iliyopita nilioneshwa kuwa una uthabiti wa tabia, utambuzi wa kusudi, ukihifadhi kiasi cha ukaidi. Hutaki kuongozwa, lakini unajisikia mwenye hamu ya kujua na kufanya mapenzi ya Mungu. Umedanganywa ndani yako mwenyewe; haujaelewa moyo wako mwenyewe. Unafikiria kuwa mapenzi yako yalikuwa chini ya mapenzi ya Mungu, lakini katika hili haukuamua vema. Umekutana na majaribu na umeruhusu akili yako kukaa juu ya tumaini linalokatisha tamaa. Kwa miaka kadhaa ya nyuma maisha yako yalikuwa na mwelekeo wa kipekee. Kumeonekana kuwa na roho ya machafuko ndani yako. Haukuwa na furaha, ingawa hakukuwa na kitu katika mazingira yako kilichopelekea kuwe na uvuli wa giza. Haujaelekeza kuadibisha akili yako juu ya mada za kufurahisha au zenye uchangamfu. Una uwezo wa kutoa ushawishi mkubwa katika kupendelea Kweli ikiwa utafundisha tu akili yako kukimbia katika mikondo iliyo sahihi. Maneno na matendo yako yote yanapaswa kuwa heshima kwa Mkombozi wako, kuinua upendo Wake na kukuza zawadi Yake. {2T 247.2}

Umeanguka katika kosa la kusikitisha ambalo limeenea sana katika kizazi hiki kinachoshuka chini kimaadili, hasa kwa wanawake. Unapenda sana jinsia nyingine. Unapenda sana jamii yao; mawazo yako kwao ni ya kujipendelea, na kuwasifia kwa udanganyifu na

unahamasisha au unaruhusu mazoea ambayo hayapatani kabisa na mawaidha ya Mitume, “Kujiepusha na kila aina ya uovu”. {2T 248.1}

Haujajua kuwa haujitambui mwenyewe. Unatembea katika giza. Umekuwa na shuguli ya kumachisha wavulana na wasichana (huyu anamfaa huyu kwa ndoa/mahaba). Hii ni biashara/shuguli isiyo na uhakika; kwa maana haujui moyo wako, au wa wale watu unaowamachisha, hivyo unaweza kufanya kazi mbaya sana, na hivyo basi unachangia kuongezea uasi mkubwa katika kazi ya kumachisha wasichana na wavulana. Adui anajishughulisha na ushawishi wa wale ambao hawafaani kabisa kwa kila mmoja ili kuunganisha maslahi yao kwa mahusiano ya mapenzi/ndoa. Anashangilia katika kazi hii, kwa kuwa kwa hilo yeye anaweza kuleta taabu zaidi na ole isiyo na tumaini kwa familia ya wanadamu kuliko kwa kutumia ustadi wake katika mwelekeo mwingine. {2T 248.2}

Umeandika barua nyingi, ambazo zimeweka madai makubwa juu yako. Barua hizi zilijikita katika mada za imani na tumaini letu; lakini kilichochangwanywa humu ni maswali ya karibu na kubuni katika suala la huyu au yule kama alikuwa karibu kuo, na unatoa mapendekezo yako kuhusu ndoa ifanyike na nani. Unaonekana kujua mengi juu ya ndoa zinazotarajiwa, na kuandika na kuzungumzia juu ya mambo haya. Hii husababisha mapungufu/njaa kwa roho yako. “Kinywa hunena kile kilichojazwa moyoni.” Umefanya jitihada kubwa kwa udhalimu kwako mwenyewe kwa kuruhusu akili yako na mazungumzo yako kujikita katika maswala ya mapenzi na ndoa. Haujawahi kuwa na furaha, na ndio sababu umekuwa ukihangaika kutafuata furaha. Hii siyo biashara yenye faida. Unapotafuta kufanya wajibu wako kwa bidii, na kujiamsha kuwahudumia wengine, ndipo utapata pumziko la nafsi yako. Akili yako inakaa juu yako mwenyewe. Inahitaji kuvutwa mbali na wewe mwenyewe kwa kutafuta nuru ya kuwahudumia watu wengine, kuifanya mizigo yao kuwa miyepesi; na kuwafanya wawe wenye furaha ndipo utakapokuwa na furaha na uchangamfu wa moyoni mwako. {2T 248.3}

Una ugonjwa wa mawazo. Umejifikiria mwenyewe kuwa ni mgonjwa, lakini hii imekuwa ya kufikirika zaidi kuliko ukweli halisi. Umekuwa siyo

mkweli kwako mwenyewe. Umezungumza na vijana wa kiume na umeruhusu kuwepo kwa uhuru mbele zako ambao unapaswa kuruhusiwa kwa kaka (kwa ndugu na si kwa wanaume wengine). Nilioneshwa kuwa ushawishi wako katika..., haukuwa vile ungepaswa kuwa. Umeruhusu akili yako kwenda chini kimaadili. Ungeweza kuzungumza, na kucheka na kuongea mazungumzo ya kipuuzi yasiyostahili mkristo. Tabia yako haikuwa kama ilivyopaswa kuwa. Ulionekana kama mtu asiye na uti wa mgongo. Ulikuwa umeegemea juu ya wengine, ambao ni mkao mbaya kwa binti kuchukua mbele ya watu. Ikiwa ungefikiria hivyo, ungeweza kutembea pia na kukaa wima kama wengine wengi. Hali ya akili yako husababisha uvivu na hofu ya mazoezi, wakati zoezi hili linathibitisha njia moja kubwa ya kupona kwako. Hautawahi kupona isipokuwa utaweka kando huu ulegevu, mawazo yenye ndoto za mchana na ujiamshe ili kufanya kazi kungali bado ni mchana. Fanya na vile vile fikiria na kisha upange. Geuza akili yako mbali na miradi ya kimahaba. unachanganya dini yako na mapenzi yaliyo madanganyifu ya hisia tu kichwani, mahaba ya kupenda ambayo hayainui bali kushusha tu. Sio wewe peke yako ambaye umeathiriwa; wengine wameumizwa na mifano yako, na ushawishi wako. {2T 248.4}

Kwa asili wewe hupenda kuabudu, kama ungaliweza kufunza akili yako juu ya mada zilizoinuliwa ambazo hazina kitu cha kufanya juu yako mwenyewe, lakini zina asili ya mbinguni, bado unaweza kuwa wa manufaa. Lakini sehemu kubwa ya maisha yako umeyapoteza kwa kuota tu kwamba utakuwa na kazi ya kubwa ya kufanya huko baadaye, wakati ungepaswa kuwajibika sasa, wakati kazi za sasa japo zionekane kuwa ndogo, umezipuuzia. Umekuwa sio mwaminifu. Bwana hatakuamini kwa kukupa kazi kubwa mpaka kazi iliyoko mbele yako umeiona na kuifanya kwa utayari na kwa moyo mchangamfu. Isipokuwa moyo umewekwa kwenye kazi, utajivuta polepole sana, haijalishi kazi ile unayoweza kuwa nayo. Bwana anajaribu uwezo wetu kwa kutupatia kwanza majukumu madogo ya kutekeleza. Ikiwa tutageuza mwelekeo wetu na tutoke hapo tukiwa wenye hali ya kutoridhika na kunung'unika, Yeye hatatatupa amana hiyo tena mpaka tutakapokuwa tumetambua na kuwa waaminifu katika majukumu

madogo tuliopewa na kuyatekeleza vyema. Ndipo majukumu makubwa yatawekwa juu yetu. {2T 249.1}

Umekabidhiwa talanta sio kwa kutumia vibaya, lakini zimetolewa ili zikazalishwe kwa wachuuzi, ili wakati Bwana atakapokuja, aweze kupokea mali zilizo Zake na riba. Mungu hajatupatia talanta bila malengo maalumu. Ametoa amana hizi takatifu kulingana na uwezo alio nao kila mja Wake. “Kwa kila mtu na kazi yake.” Yeye hutoa bila upendeleo, na anatarajia kupokea sawa na alivyokupa. Ikiwa wote watafanya wajibu wao kulingana kipimo cha uwajibikaji wao, kiwango walichokabidhiwa, kiwe hicho kiwe kikubwa au kidogo, kitaongezeka mara mbili. Uaminifu wao unajaribiwa na kuthibitishwa na uaminifu wao ni ushahidi mzuri wa uwakili mwaminifu, na kustahili kwao kukabidhiwa amana zenye utajiri wa Kweli, hata ile zawadi ya uzima wa milele. {2T 250.1}

Kwenye mkutano huko New York, Oktoba, 1868, nilioneshwa wengi ambao hawafanyi wajibu wao, watu ambao wangukuwa wanafanya mema. Nilioneshwa tabaka la watu waliokuwa wanafahamu kuwa wana misukumo ya mizuri ukarimu, wenye hisia za uchaji Mungu/ibada, na upendo wa kutenda mema; lakini wakati huo huo wanaishi bila kufanya chochote. Wameridhika kwa njia hasi, wakijipendeza kwamba ikiwa wangukuwa nayo fursa, au upendeleo fulani, basi wangeweza kufanya kazi nzuri sana; ila wamekaa wakisubiri fursa. Wanadharau akili nyembamba ya bahili masikini ambaye anabania visenti vichache kwa ajili ya wahitaji. Wanaona kuwa anaishi kwa ajili ya nafsi yake wenyewe kwa ubahili, kuwa hana wito wa kuwatendea wengine mema, kuwabariki kwa talanta ya ushawishi na mali ambazo zimewekwa kwake azitumie, sio kwa kutumia vibaya, au kuziruhusu kula kutu, au kuzizika chini ardhini. Wale ambao wanajipa wenyewe hali ya ubahili na ubinafsi wanawajibika kwa matendo yao ya uchoyo, wanawajibika kwa talanta walizotumia vibaya. Lakini wale wanaowajibika zaidi ni wale ambao wana misukumo ya ukarimu na kwa kawaida ni wepesi kutambua mambo ya kiroho, ikiwa watabaki bila kufanya kazi, wakingojea fursa waliyokuwa wanaitarajia nayo haikupatikana, na huku wakitofautiana na utayari wao wa kutenda kwa kutokuwa na utayari kama bahili wanayemcheka, na kupuuzia kwao kwamba hali yao ni



nzuri zaidi kuliko ile ya majirani zao wenye roho za ubahili. Hao hujidanganya wenyewe. Umiliki tu wa sifa ambazo hazikutumiwa ni kuongeza majukumu tu; na ikiwa watazitunza talanta za Bwana wao bila kuziendeleza au kuzihifadhi, hali yao haina utofati na ile ya majirani zao ambao wao huwadharau. Kwao wataambiwa, mlijua mapenzi ya Bwana wenu lakini hamkuyatenda. {2T 250.2}

Kama ungefundisha akili yako juu ya masomo yaliyoinuliwa, kutafakari juu ya mada za mbinguni, ungeweza kufanya vizuri sana. Ungekuwa na ushawishi juu ya akili za watu wengine, kugeuza mawazo yao ya ubinafsi na tabia ya kupenda ulimwengu katika mkondo wa kiroho. Kama mapenzi yako na mawazo yaliyoletwa chini ya mapenzi ya Kristo, ungeweza kutenda mema. Fikra zako zina ugonjwa kwa sababu umeziruhusu ziendeshwe kwenye mkondo uliopigwa marufuku, na sasa umekuwa mwota ndoto. Kuota ndoto za mchana na kujenga majumba ya mapenzi kichwani, yamefanya usiwe mtu wa manufaa au msaada. Umeishi katika ulimwengu wa kufikirika; umekuwa mfia dini mawazoni mwako, na Mkristo wa kufikirika. {2T 251.1}

Kuna mengi ya hii hisia ya chini iliyochanganywa na uzoefu wa kidini wa vijana katika enzi hii ya ulimwengu. Dada yangu, Mungu anataka ubadilishwe. Inua mapenzi yako, nakusihi. Tumia nguvu zako za kiakili na za mwili kwa huduma ya Mkombozi wako, ambaye amekununua. Takasa mawazo yako na hisia zako ili kazi zako zote zifanyike katika Mungu. {2T 251.2}

Umekuwa katika udanganyifu wa kuhuzunisha. Mungu angetaka uchunguze kila wazo kwa karibu, na nia ya moyo wako. Shughulikia ipasavyo na nafsi yako mwenyewe. Ikiwa mapenzi yako yangeelekezwa kwa Mungu kama Anavyotaka, ungeweza kushinda majaribu unayopitia. Kuna kiherehere kwenye roho yako ambacho hakitapata afueni mpaka mawazo yako yatakapokuwa yamebadilishwa. Mpaka ndoto za mchana na ujenzi wa majumba makubwa ya fahari kichwani zikome, na utakuwa tayari kufanya wajibu wako wa sasa. {2T 251.3}

Katika uandishi wako wa barua, acha kumachisha watu na kutabiri juu ya ndoa za marafiki zako. Mahusiano ya ndoa ni matakatifu. Lakini katika kizazi hiki kilichoporomoka maadili uovu wa kila namna hufunikwa na ndoa. Imetumiwa vibaya na imekuwa uhalifu ambao umekuwa ni mojawapo ya dalili za siku za mwisho, kama vile ndoa zilivyoendeshwa kwa uhalifu kabla ya mafuriko. Shetani anajishughulika kila wakati kuharakisha vijana wasio na uzoefu katika muungano wa ndoa. Lakini jinsi tunavyotukuza kidogo ndoa zinazofungwa sasa ndivyo itakuwa bora. Wakati utakatifu wa asili na madai wa ndoa na madai yake yatakapokuwa yameeleweka vizuri, itakuwa sasa imepata kibali cha mbingu, na matokeo yake yatakuwa ni furaha kwa pande zote mbili na Mungu atatukuzwa. Hebu Bwana Mungu akuwezeshe kutenda kazi iliyoko mbele yako unayopaswa kuitenda. {2T 252.1}

Nipo karibu kuandika juu ya hili kosa. Udanganyifu unaofanywa chini ya kofia ya dini. Tamaa ya mwili inadhibitiwa na wanaume na wanawake. Akili inapopotoshwa kupitia upotovu wa mawazo na hisia, na bado nguvu ya udanganifu wa Shetani unapofusha macho yao kuwa maskini, nafsi zenye kudanganywa hujipendekeza kwamba zina nia za kiroho, zimejiweka wakfu kwa uchaji, wakati uzoefu wao wa kidini unaundwa na hisia za mapenzi mapotofu kuliko kupenda usafi, wema wa Kweli na unyenyekevu wa roho; akili haijatolewa katika ubinafsi, haitekelezwi na kuinuliwa kwa kuwabariki wengine, na kufanya kazi nzuri. Dini iliyo safi, isiyo na mawaa mbele za Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatembelea yatima na wajane katika taabu zao na kujilinda bila mawaa na ulimwengu. Dini ya Kweli huboresha akili, husafisha ladha/mionjo, hutakasa maamuzi na kumfanya mmiliki wake kushiriki katika usafi na ushawishi wa kimbangu; huleta malaika karibu na hutenganisha zaidi na zaidi kutoka katika ushawishi wa ulimwengu. {2T 252.2}

Battle Creek, Michigan.

## SURA YA 37

### UKALI KATIKA KUSIMAMIA FAMILIA

Ndugu L: Juni ya mwaka jana nilioneshwa kuwa kuna kazi mbele yako ya kurekebisha njia zako. Wewe mwenyewe hauoni hili. Maisha yako yamekuwa makosa. Hautafuti mwenendo wenye hekima na rehema katika familia yako. Umekuwa mkali. Ikiwa utaendelea kufuata njia ambayo umekuwa ukiifuata kwa mke wako na watoto, siku zako zitafupishwa, na watoto wako watakuogopa, lakini hawatakuwa na upendo kwako. Unahisi kuwa njia yako ipo katika hekima ya Kikristo, lakini katika hili, wewe unajidanganya mwenyewe. {2T 253.1}

Una maoni ya kipekee kuhusu kusimamia familia yako. Unatumia uhuru kiholela, nguvu ambayo hairuhusu uhuru wa nia na mapenzi kwa wale walio karibu nawe. Unafikiri mwenyewe unatosha kuwa kichwa katika familia yako, na kuhisi kuwa kichwa chako kinatosha kumhamisha kila mwanafamilia kama vile mashine mkononi mwa anayeitumia. Unaamuru na kujichukulia mamlaka. Hii inachukiza mbingu na kuhuzunisha na kusikitisha malaika. Unajiendesha mwenyewe katika familia yako kana kwamba wewe peke yako una uwezo wa kujitegemea na kuwa na serikali yako mwenyewe. Umeudhika kwamba mke wako amejitosa kupinga maoni yako au kuhoji juu ya maamuzi unayoyafanya. {2T 253.2}

Baada ya maumivu ya muda mrefu kwa mkeo, na kwa subira akingojea matakwa yako, ameamua kuasi dhidi ya mamlaka yako isiyo ya haki, na amekuwa mwenye woga na aliyevurugwa, na ameonyesha chuki na dharau kwa njia zako. Wewe ndiye umepelekea haya juu yake na umemshtaki kwa dhambi ya kuongozwa na roho ya shetani, wakati wewe ndiye uliyekosea. Ulimsukuma katika hali ya kukaribia kukata tamaa na kujilaumu, na baadaye unamchokoza na maneno ya matusi. Ni jinsi gani ingekuwa rahisi kwako kumfanya awe na maisha ya furaha, uchangamfu na kupendeza. Lakini imekuwa kinyume cha hii. {2T 253.3}

Umekuwa mzembe na mvivu sana. Haukuwa na shauku ya kutumia nguvu uliyopewa na Bwana. Huu ni mtaji wako. Matumizi ya busara ya

nguvu, na tabia ya uvumilivu, bidii ya kazi, ingekuwezesha kupata faraja maisha- kuondoa usumbufu. Umekosea, na ukafikiria ni kiburi ndio kinachomfanya mke wako atamani kuwa na vitu vizuri karibu yake. Amekuwa ametendwa kwa ubahili na uchoyo nawe. Anahitaji chakula cha ukarimu zaidi, chakula kingi kwenye meza yake, na katika nyumba yake anahitaji vitu vizuri na vyenye kusaidia maisha kuwa rahisi zaidi (comfortable), vitu vya kumfanya afanye kazi zake kwa urahisi kwa kadri iwezekanavyo. Lakini umekuwa ukiona mambo kwa mtazamo usiofaa. Umekuwa ukifikiria kuwa karibu chochote kilichokuwa kinaliwa kilikuwa kizuri na cha kutosheleza, kama wewe ungeliishi kwa kutumia hicho na kubakia kuwa na nguvu basi hata yeye. Umempa chakula kisichotosha mke wako mdhaifu. Lakini hawezi kutengeneza damu nzuri na seli kwa aina ya chakula ambacho kinafanana na mahitaji ya mwili wako, maana mahitaji yake ili kuweza kunawiri kiafya ni tofauti. Watu wengine hawawezi kuendelea kuishi kwa afya na chakula kile kile ambacho wengine wanaweza kuishi vizuri sana kwa chakula hicho, ingawa kimeandaliwa kwa namna ile ile. {2T 254.1}

Uko katika hatari ya kuwa na msimamo mkali, unaopitiliza. Mfumo wako ungeweza kubadilisha chakula rafu-rafu chenye lishe duni kuwa damu nzuri. Viungo vyako vya kutengeneza damu viko katika hali nzuri. Lakini mke wako anahitaji lishe ya aina maalumu zaidi. Ukimpa chakula hicho hicho ambacho wewe ukila huzalisha damu nzuri katika mwili, mfumo wake hauwezi kuutumia vizuri. Amekosa nguvu, na anahitaji chakula bora, chenye lishe nzuri, na chenye kutia nguvu mwili. Anapaswa kupata matunda ya kutosha na asiwekewe mipaka ya kula chakula hicho hicho siku hata siku. Ameshikilia uzima/maisha kwa udogo, ni mgonjwa, hali yake ya afya si nzuri. Anaumwa, na mahitaji ya mfumo wa mwili wake unatofautiana na wale wenye afya bora. {2T 254.2}

Ndugu L, una hadhi/heshima kubwa, lakini je, kweli umeifanyia kazi hiyo heshima? La! Hapana! Umejitwalia tu. Umependa starehe. Wewe na kazi ngumu hamuendani pamoja. Kama usingekuwa mtu mvivu kwenye biashara, ungeweza kupata unafuu mkubwa katika maisha kitu ambacho huwezi kukipata kwa sasa. Umemkosea mke wako na watoto wako pia kwa tabia yako ya uvivu. Masaa ambayo yangetumiwa

kwa kazi ya bidii, yamekuwa yakipita, wakati wewe ukiwa unapiga magumzo, ukisoma na kuendekeza raha tu. {2T 254.3}

Unawajibika Kwa mtaji wa nguvu zako, kama vile mtu tajiri alivyo kwa mali zake. Wote ninyi ni mawakili. Kila mtu amekabidhiwa jukumu. Usitimie nguvu zako vibaya, bali uzitumie kupata mahitaji ya kutosha na muhimu ya familia yako, na kuwa na sehemu utakayopeleka kwa Mungu, kwa kusudi la kusaidia kusukuma Ukweli wa sasa mbele. Umekuwa ukijua juu ya uwepo wa kiburi, kujionyesha na ubatili katika..... na kuhisi kuwa mfano wako usije ukawa na sura ya kiburi na ubaradhifu. Katika jitihada zako kufanya hivi, umeifanya dhambi yako kubadilika na kuwa kubwa kwa mwelekeo wa upande mwingine (wengine walikuwa wabaradhifu, yeye anaendekeza ubahili) {2T 255.1}

Umekuwa na makosa sana katika uzoefu wako wa kidini. Umesimama upande mmoja kama mtazamaji, mkodoa macho tu, Ukitazama mapungufu na makosa ya wengine, na kujijengea mwenyewe heshima yako, kwa kujivuna kwa sababu unaona makosa yao. Umekuwa mwangalifu na mnyofu katika dili/shughuli, na pale umeona mapungufu katika hili kwa wengine ambao hukiri kwa mdomo kwa hali ya juu, umejilinganisha mwenyewe na makosa yao na kanuni zao katika utendaji/dili, na umesema moyoni mwako, “mimi ni bora kuliko wao”, wakati huo huo ulikuwa umesimama mbali na kanisa, ukiangalia na kutafuta makosa, bila hata ya kufanya chochote, haukuweza kuja kumsaida Bwana, ili kukabiliana na kuponya/kukarabati uovu. Ulikuwa na kiwango ambacho kwacho uliwapima wengine. Ikiwa walishindwa kufikia wazo lako, huruma yako haikuwa pamoja nao, na ulikuwa na hisia za kuridhika kuhusiana na wewe mwenyewe. {2Tsw 255.2}

Umekuwa mkali kwa uzoefu wako wa kidini. Endapo Mungu angekushughulia kama vile ambavyo unawashughulikia wale ambao unadhani wana makosa ndani ya kanisa, na kama ulivyoshughulika na familia yako mwenyewe, hali yako ingekuwa mbaya hakika. Lakini Mungu Mwenye rehema, upendo mwanana, na huruma nyororo iliyopitiliza, ambaye upendo Wake, fadhili Zake hazibadiliki, amekuwa akisamehe na hakukutupa kando wala hakukukatilia mbali kwa sababu

ya dhambi zako, makosa yako mengi na kurudi nyuma kwako. Lo! Hapana! anakupenda bado. {2T 255.3}

Je, umewahi kufikiri kwamba “kwa kipimo kile unachowapimia watu ndicho utakachopimiwa na wewe tena?” Umeona kiburi na ubatili na roho ya kupenda ulimwengu kwa wengine wanaodai kuwa wakristo huko..... Huu ni uovu mkubwa; na kwa sababu roho hii inaendekezwa, malaika wanahuzunika/wanalizwa. Wale wanaofuata mfano wa watu ambao hawajawekwa wakfu wanafanya ushawishi wa kutapanya kutoka kwa Kristo, na wanajikusanyia kwenye nguo zao damu ya roho za watu. Ikiwa wataendelea na njia hiyo hiyo watapoteza roho zao, na siku moja watakuja kujua ni nini maana ya kuhisi uzito wa kutisha wa roho zingine ambazo zimepotoshwa kwa kutokujitoa kwao wakfu kwa Mungu, wakati wakidai kutawaliwa na kanuni za kidini. {2T 256.1}

Una sababu ya kuhuzunika Kwa kiburi chako na ukosefu wa unyenyekevu kwa wale wanaokiri vitu bora. Lakini umewaangalia wengine, na ukazungumzia mapungufu na makosa yao na kupuuzia nafsi yako binafsi. Hauwajibiki kwa dhambi yoyote ya ndugu zako, isipokuwa kama mfano wako uliwasababisha wajikwae, ulisababisha miguu yao kugeuzwa kutoka katika njia nyembamba. Una kazi kubwa na nzito mbele yako ya kujidhibiti na kujitawala mwenyewe, kuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo, kujielimisha kuwa na moyo mwororo, wenye kujali, wenye mahusiano ya karibu, na wa kusikitia familia yako, na kuwa na roho yenye ubora, na ukarimu wa Kweli kwa roho ambayo hudharau kila kitu kinachohusiana na ubahili. {2T 256.2}

Umefikiri kwamba kulikuwa na kazi kubwa iliyowekwa juu ya jumba la mikutano-kanisa na umekuwa ukizungumzia kuhusu matumizi yasiyo ya lazima. Huhitaji kuwa na mashaka ya namna hii, ndani ya moyo wako. Hakuna kitu ndani ya nyumba hiyo ambacho kinaandaliwa kwa uangalifu mwingi, unadhifu, au utaratibu. Kazi au maandilio sio mazuri sana. Mpangilio wa hiyo nyumba, hauna ubaradhifu wowote. Je, wale ambao wako tayari kulalamika juu ya hali ya nyumba ya ibada, wanazingatia kweli kwamba ilijengwa kwa ajili ya Nani? Kwamba ilifanywa kwa kusudi maalumu la kuwa nyumba ya Mungu; Kutolewa wakfu Kwake; kuwa mahali ambapo watu hukusanyika kukutana na

Mungu? Wengi hufanya kana kwamba Muumba wa mbingui na ardhi, Yeye aliyefanya kila kitu kinachopendeza na uzuri katika dunia yetu, atafurahisha kuona nyumba iliyojengwa kwa ajili Yake bila mipango/utaratibu au uzuri. Wengine hujenga nyumba kubwa, kwa ajili ya urahisi/faraja yao wenyewe, wakati huo hawawezi kugharamika sana katika ujenzi wa nyumba iliyowekwa wakfu kwa ajili ya Mungu. Kila senti iliyo mikononi mwa watu ni mali ya Mungu. Yeye Amewakopesha watu kwa muda mfupi,, ili watumie kwa utukufu Wake; ila wao, wanapotumia mali hii kwa maendeleo ya kusudi la Mungu wanatenda kana kwamba kila senti ikitumiwa hivyo itakuwa ni hasara kwa ujumla. {2T 256.3}

Mungu asingependa watu Wake wafuje mali ili kujionyesha au kuwa na mapambo, lakini angependa kuwaona wakiwa na unadhifu, mpangilio, na uzuri katika kumjengea Bwana nyumba ambayo atatumia kukutana na watu Wake. Wale wanaomjengea Mungu nyumba wanapaswa kuonyesha shauku, uangalifu na ladha katika mpangilio wake, kwani kitu ambacho kimeandaliwa ni cha juu na kitakatifu zaidi kuliko nyumba za kawaida tunamoishi. {2T 257.1}

Bwana Mungu husoma nia na makusudi ya wanadamu. Wale wenye mitazamo ya juu kuhusiana na tabia Yake Bwana, watafanya na kuhisi kwamba raha yao ya juu, ni kufanya kila kitu ambacho kimeunganishwa Naye, kuwa kazi yenye ubora zaidi na kikionyesha uzuri na ladha bora zaidi. Lakini wale ambao kwa malalamiko wanajenga nyumba duni ili kuiweka wakfu kwa Mungu, ambao wenyewe wasingekubali kuishi humo, huonyesha kukosa kwao kicho kwa Mungu na vitu vitakatifu. Kazi yao huonyesha mambo ya muda ni ya thamani zaidi machomi pao kuliko mambo yenye asili ya kiroho. Vitu vya milele vimefanywa kuwa namba mbili, yaani havina kipaumbele. Haizingatiwi kuwa muhimu, hii nyumba ya Mungu kuwa na vitu vizuri na vyenye kufanya huduma kuendeshwa kwa ubora, lakini wanachukulia kuwa muhimu sana kuwa na vitu hivi wenyewe katika mambo ya maisha haya. Watu watadhihirisha toni na hisia halisi ya maadili ya kanuni za mioyo yao. {2T 257.2}

Watu wetu wengi wamekuwa na mtazamo finyu. Mpangilio, usafi, uzuri, ladha, faraha na urahisi huitwa kiburi na upendo wa ulimwengu. Kosa

limefanywa hapa. Kiburi cha ubatili, chenye maonyesho ya hovy hovy,na mapambo yasiyofaa havimfurahisi Mungu. Lakini Yeye aliyemuambia mwanadamu dunia yenye uzuri/ladha na kupanda bustani yenye kupendeza katika Eden, ikiwa na jamii ya miti mbali mbali kwaajili ya matunda na uzuri, na aliyeipamba na kuingarisha dunia kwa uzuri wa maua mengi ya kupendeza, ya kila aina zake na rangi, ametupatia ushahidi wenye mashiko kuwa Yeye anapendezwa na uzuri. Pamoja na hayo bado atapokea sadaka ya unyenyekevu kutoka kwa masikini wa hali ya chini, mtoto aliye mdhaifu zaidi, ikiwa hatakuwa na kitu kizuri zaidi cha kumtolea Mungu. Ni moyo mkunjufu, ndio Bwana anapokea. Mtu ambaye Bwana ametakasa moyo wake, anainuliwa juu ya vitu vyote, ataongozwa katika kusalimisha nia yake kwa nia ya Bwana na atajisalimisha yeye mwenyewe chini ya usimamizi na utawala Wake. {2Tsw 258.1}

Mwanadamu asiyeona mbali, anayeweza kufa, hawezi akazielewa vyema njia na kazi za Mungu. Macho yao hayajaelekezwa kwenda juu Kwake kama inavyopaswa kuwa. Hawana maoni yaliyoinuliwa kwa vitu vya umilele. Wanaangalia tu mambo haya na maono yaliyojaa mawingu. Hawafurahii kwa jinsi ya pekee kwa kutafakari upendo wa Mungu, utukufu na uzuri wa mbingu, tabia iliyoinuliwa ya malaika watakatifu, ukuu na upendo usioelezeka wa Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Kwa muda mrefu wameweka vitu vya dunia mbele ya maono yao kiasi kwamba mambo ya umilele hayako wazi kwao na hayaeleweki. Wana mipaka ya uelewa wa Mungu, mbingu, na umilele. {2Tsw 258.2}

Vitu vitakatifu vimeshushwa chini na kuwekwa na vile vya kawaida; kwa hivyo katika kushughulika na Mungu wanadhihirisha roho ile ya ubahili, uchoyo, ubinafsi kama vile ya wanavyoshughulika na wanadamu wenzao. Sadaka zao kwa Bwana ni vilema, gonjwa, au pungufu. Wanaendelea na wizi huo kwa Bwana ambao wanawafanyia wanadamu wenzao. Akili zao hazifikii kiwango cha juu cha maadili, lakini kimedumu kubaki katika viwango vya chini; daima wanapumua hewa isiyo iliyovunda kwa harufu mbaya, ya nyanda za chini ya dunia (miasma). {2Tsw 258.3}



Ndugu L, unatawala kwa fimbo ya chuma katika familia yako. Wewe ni mkali katika serikali ya kuwasimamia watoto wako. Hautapata upendo wao kwako kwa njia hii ya usimamizi. Wewe sio mwenye huruma nyororo, mahusiano ya karibu, upole, kujali, Upendo mwanana, joto, mapenzi, uungwana, na adabu kwa mke wako, bali u jeuri, mkali, na unamtawala kwa mabavu, ukimlaumu na kumshutumu. Familia iliyodhibitiwa vizuri, yenye utaratibu ni jambo la kupendeza mbele za Mungu na malaika wanaohudumu. Ni lazima ujifunze jinsi ya kufanya nyumba iwe na utaratibu, uzuri, na yenye faraja. Kisha ipambe hiyo nyumba na pambo la heshima yenye ladha, na roho hiyo itapokelewa vizuri na watoto; na utaratibu, kanuni na utii utakuwa ukitolewa kirahisi, kwa hiari na kudumishwa na nyote wawili. {2Tsw 259.1}

Ndugu L, umezingatia mtoto ni nani, na anakwenda wapi? Watoto wako ndio washiriki wadogo wa familia ya Mungu.....kaka na dada uliokabidhiwa uwatunze na Baba yako wa mbinguni uwalee na kuwafundisha kwa ajili ya mbingu. Unaposhughulika nao kwa ujeuri na ukali na kuwa rafu-rafu kama vile ambavyo umekuwa ukifanya, je unakumbuka kuwa Mungu atakuwajibisha kwa kutoa hesabu kwa malezi ya namna hii? Haupaswi kuwalea watoto wako kwa ukali na rafu hivi. Kumbuka kuwa mtoto sio farasi au mbwa kuamriwa tu kwa kadri mapenzi yako yanayojeruhi yanavyojisikia, au kuthibitiwa katika hali zote kwa fimbo na mjeledi, au kwa kupigwa makofi na mikono yako. Kuna watoto ambao wana hasira mbaya sana katika haiba yao, kiasi kwamba maumivu ya kiboko ni muhimu, lakini katika kesi nyingi kiboko kimekuwa kikiharibu mambo zaidi, kwa aina hii ya malezi kwa watoto. {2Tsw 259.2}

Unapaswa kujitawala mwenyewe. Kamwe usiwaadhibu watoto ukiwa na umeudhika au ukiwa na ghadhabu nyingi au ukiwa na shauku yenye hasira. Waadhibu kwa upendo, onyesha kuwa haupendi kuwafanya wakose furaha na kuwasababishia maumivu [ila umwonyeshe ubaya wa kosa na kwa sababu ya kosa hilo ndio maana umemuadhibu, hivyo utamsaidia kuchukua hilo kosa na kuliacha]. Usinyoshe mkono wako na kuanza kuwashushia vipigo isipokuwa unaweza ukafanya hivyo ukiwa na dhamiri safi mbele za Bwana Mungu wako, na ukiomba mibaraka Kwake juu ya adhabu unayoenda kutoa ili iweze kumsaidia

kujirekebisha. Hamasisha upendo kwenye mioyo ya Watoto wako. Hata wakati unapomwadhibu umwonyeshe roho ya upendo. Wasilisha kwao malengo ya juu na nia sahihi ya kujikana nafsi/kuwa na kiasi. Usiwaonyeshe hisia zako, kwamba ni lazima uwadhibiti kwa sababu ni uchaguzi wako kuwafanya watii; kwa sababu wao ni wanyonge na wewe una nguvu, kwa kuwa wewe ndiye baba na wao ni watoto. Ikiwa unataka kuiharibu familia yako, wee endelea tu kuitawala familia kwa mabavu, unyama, na nguvu nyingi na hakika utafanikiwa kufanya hivyo. {2Tsw 259.3}

Mke wako ana huruma sana na hujali watu, na huudhika na kupata msongo kirahisi. Anahisi nidhamu yako yenye ujeuri na ukali na hilo humfanya afikirie kinyume ili kupunguza makali. Anatafuta namna ya kukabiliana na kuupunguza ukali wako, na wewe unahukumu hili kuwa kama kosa lake kubwa la kutofanya wajibu wake wa kuwadhibiti watoto. Unafikiria yeye amedekesha watoto, anaonyesha upendo wa kupindukia na moyo ulio teketeki sana. Huwezi kumsaidia katika swala hilo mpaka kwanza, ujisahihishe mwenyewe na kudhihirisha upendo mwanana, kujali na huruma ya mzazi ambayo unapaswa kuwa nayo katika familia yako. Ni usimamizi wako mbaya ndio unasababisha mke wako alegee katika nidhamu yake. Ni lazima upunguze ukali wako, kulainishwa moyo., unahitaji kusafishwa na ushawishi wa Roho wa Mungu. Unahitaji uongofu wa Kweli; ndipo unaweza kufanya kazi ukiwa na mtazamo sahihi. Unahitaji kuruhusu upendo ujae ndani ya moyo na kutawala nafsi yako na kujiruhusu kujaza nafasi ya kujistahi wewe mwenyewe na kujiinua kwa nafsi; yaani ubinafsi, ni lazima ufe. {2Tsw 260.1}

Mke wako anahitaji huruma, upole na upendo wako. Bwana Mungu anampenda. Mke wako yuko karibu sana na ufalme wa Mungu kuliko wewe. Lakini anakufa pole pole na wewe ndiye unayeondoa maisha yake polepole. Unaweza kumfanya awe na furaha ukinuia. Unaweza kumtia moyo aegemee mapenzi yako makubwa kwake, akuweke wewe kuwa msiri wake na kukupenda. Unamfanya moyo wake utoke kwako. Anajikunja kukufungulia hisia za moyo wake, kwa kuwa umedharau hisia zake; umekejeli hofu zake na kwa majivuno umeendeleza maoni yako kana kwamba hakukuwa na maoni mengine isipokuwa yako tu.

Heshima yake kwako hakika itakufa ikiwa utaendelea na njia hiyo. Na heshima inapotoweka, basi mapenzi hayakai hapo tena. {2Tsw 260.2}

Ninakusihi ugeuke, urudie katika njia na ujinyenyekeze na kuungama kwamba umemkosea mke wako. Yeye sio mkamilifu. Ana makosa, lakini anatamani kwa dhati kumtumikia Mungu na kuvumilia hali yako hiyo kwake na kwa watoto wenu. Wewe ni mwepesi sana kugundua kasoro za mke wako na wakati unaweza kuzichambua, wewe hufanya hivyo. Yeye ni dhaifu; lakini hata kwa huo udhaifu wake, yeye anamtukuza Mungu vizuri kuliko wewe unavyofanya licha ya kwamba una nguvu. {2Tsw 261.1}

## **SURA YA 38**

### **BARUA YA SIKU YA KUZALIWA**

Mwanangu Mpendwa: ninakuandikia haya katika siku yako ya kuzaliwa ya kumi na tisa. Imekuwa raha kuwa na wewe katika wiki chache zilizopita. Uko karibu kutuacha, lakini maombi yetu yatakufuata huko uendako. {2Tsw 261.2}

Mwaka mwingine wa maisha yako unafungwa leo. Unaweza kuuangaliaje tena mwaka huu ulioishapita? Je, umepiga hatua katika maisha ya Mbingu (Kanuni za Mwenyezi Mungu?) Je, umesonga mbele katika maisha ya kiroho? Je, umesulubisha nafsi pamoja na mapenzi, na tamaa za mwili? Je, umeongeza shauku ya kusoma Neno la Mungu? Je, umepata ushindi uliodhamiriwa dhidi ya upotovu wako, utukutu na kutotii? Loh! Ni nini imekuwa rekodi ya maisha yako kwa huu mwaka ambao sasa umepita milele, ambao hauwezi kurudishwa nyuma tena? {2Tsw 261.3}

Unapoanza mwaka mwingine mpya tena, hebu uwe na dhamiri dhati ya kuendelea juu na mbele. Acha maisha yako yainuliwe juu zaidi na yawe na utukufu kuliko ilivyokuwa. Ulifanye lengo lako kutotafuta maslahi yako binafsi na anasa zako, lakini kuendeleza kusudi la Mkombozi

wako. Usibaki katika nafasi ya utegemezi ambapo unahitaji watu wakusaidie daima, na ambapo watu wengine itabidi wakulinde ili wakufanye udumu kubaki katika njia nyembamba. Unaweza kuwa na nguvu ya kutumia ushawishi wa utakaso juu ya watu wengine. Unaweza ukawa mahali ambapo mapenzi ya nafsi yako yataamshwa kutenda mema kwa wengine, ili kufariji wenye huzuni, kutia nguvu wanyonge, na kutoa ushuhuda wako kuhusu Kristo wakati wowote fursa inapojitokeza. Nuia kumheshimu Mungu, katika kila kitu, kila wakati na kila mahali. Beba dini yako katika kila nyanja/mahali. Chochote unachokifanya, kifanye kwa ukamilifu unachokifanya. {2Tsw 261.4}

Haujapata uzoefu wa nguvu ya Mungu iokoayo kama fursa yako pekee, ni kwa sababu haujaifanya kuwa lengo kuu la maisha yako kumtukuza Kristo. Hebu kila kusudi unaloliunda, kila shuguli unayojihusisha nayo, na kila burudani unayofurahia, iwe kwa utukufu wa Mungu. Hebu hii iwe lugha ya moyo wako: Ni wako ee Bwana, kuishi kwa ajili yako, kufanya kazi kwa ajili yako, na kuteseka kwaajili yako. {2Tsw 262.1}

Wengi wanakiri kuwa upande wa Bwana, kumbe sivyo; uzito wa matendo yao yote uko juu ya upande wa Shetani. Je, ni kwa njia gani tunaweza kutambua tuko upande wa nani? Ni nani aliye na moyo wetu? Ni nani aliye na mawazo yetu? Ni nani tunayependa kuzungumza Habari zake? Ni nani ana mapenzi yetu ya jotojoto zaidi na nguvu zetu bora? Ikiwa tuko upande wa Bwana, tafakari zetu zitakuwa Kwake na mawazo yetu matamu yatakuwa kuhusu Yeye. Hatuna urafiki na dunia; tumesalimisha yote tuliyo-nayo, na sisi wenyewe na kuviweka hivi vyote wakfu Kwake, na tuna shauku ya kubeba taswira Yake, kupumua Roho Yake, kufanya mapenzi Yake na kumpendeza katika kila kitu. {2Tsw 262.2}

Unapaswa kufuata njia iliyoazimiwa kabisa, ambayo hakuna atakayepotezwa nawe au atakayekufananisha au kukosea. Hauwezi kutoa ushawishi kwa ulimwengu bila maamuzi. Maazimio yako yanaweza kuwa mazuri na ya dhati, lakini yatadhihirisha kushindwa kama hautamfanya Mungu kuwa nguvu zako na kusonga mbele kwa utambuzi wa kusudi uliodhibitishwa. Unapaswa kutoa moyo wako wote

kwa Bwana na kufanya kazi ya Mungu. Unapaswa kuwa na bidii ya kupata uzoefu katika maisha ya Kikristo. Unapaswa kumwonyesha Kristo maishani mwako kwa mfano wako. {2Tsw 262.3}

Huwezi kumtumikia Mungu na mali. Aidha upo upande wa Bwana kabisa au upande wa adui. “Yeye ambaye hayuko pamoja Nami yu kinyume Nami; na yeye asiyekusanya pamoja Nami hutawanya.” Watu wengine hufanya maisha yao ya kidini kushindwa kwa sababu kila wakati wanamangamanga na hawawezi nguvu katika nia zao. Mara nyingi wanasadikishwa na kuja kujitoa kabisa katika hatua ya kusalimisha vyote kwa Mungu; lakini wanashindwa kufikia lengo, kisha wanaanguka tena. Wakati wakiwa katika hali hii dhamira huwa inaendelewa kuwa sugu na dhaifu na kuathiriwa kwa upungufu na ushawishi wa Roho wa Mungu. Roho Wake Ameonya, Amesadikisha, na Amepuuzwa, mpaka Amehuzunishwa na kwenda mbali. Mungu hatachezewa. Yeye anaonyesha wajibu wazi na ikiwa kuna kupuuza kufuata nuru, inakuwa giza. {2Tsw 263.1}

Mungu anakuagiza wewe uwe mtenda kazi pamoja Naye katika shamba Lake la mizabibu. Anzia tu hapo ulipo. Njoo msalabani, na hapo ujikane nafsi, ulimwengu, na kila sanamu. Mchukue Yesu moyoni mwako kikamilifu. Upo mahali pagumu kuhifadhi utakatifu/uchaji Mungu na kutumia ushawishi utakaowaongoza wengine kutoka dhambini na furaha za nafsi na anasa na kuelekea katika njia nyembamba, tengeneza njia kwa waliokombolewa na Bwana ili watembee ndani. {2Tsw 263.2}

Jisalimishe kikamilifu kwa Mungu. Salimisha kila kitu kwake bila kizuizi, na kisha tafuta amani inayopita akili zote za kibinadamu. Hauwezi ukapata lishe nzuri ya kiroho kutoka kwa Kristo kama haumo ndani Yake. Kama haumo ndani Yake wewe ni tawi lililonyauka. Hauhisi matakwa yako ya usafi na utakatifu wa Kweli. Inakupasa kuhisi shauku yenye bidii ya kupata Roho Mtakatifu na kuomba kwa dhati ili kuweza kumpata. Hauwezi kutazamia mibaraka ya Mungu pasipo kuitafuta. Kama ukitumia mali zilizo ndani ya uwezo wako ungeona ukuaji wa neema na ungepiga hatua kuelekea Maisha ya juu. {2Tsw 263.3}

Sio asili yako kupenda vitu vya kiroho; lakini unaweza kupata upendo huo kwa kuifanyisha akili yako mazoezi, nguvu ya uwepo wako, katika mwelekeo huo. Uwezo wa kutenda ndiyo unaohitaji. Elimu ya Kweli ni uwezo wa kutumia vitivo vyetu ili kuweza kufikia matokeo yenye manufaa. Ni kwa nini mambo ya dini huchukua sehemu ndogo sana ya umakini wetu, wakati ulimwengu una nguvu ya akili, mifupa na misuli? Ni kwa sababu msukumo wote wa uwepo wetu umepindishwa katika mwelekeo huo. Tumejielelemisha wenyewe katika kujihusisha kwa bidii na nguvu katika biashara za duniani, mpaka imekuwa rahisi kwa akili kuchukua mwelekeo huo. Hii ndio sababu Wakristo wanaona Ukristo kuwa ni mgumu kwao, na mambo ya dunia ni rahisi sana. Vitivo vyetu vimeelimishwa kutumia uwezo wao katika mwelekeo huo. Katika maisha ya kiroho/kidini kumekuwa na uthibithisho wa Ukweli wa Neno la Mungu, lakini bila kielelezo kwa vitendo kwao katika maisha. {2Tsw 263.4}

Kukuza fikra za kidini na hisia za uchaji Mungu na ibada haikufanywi kuwa sehemu ya elimu. Haya yanahitaji kushawishi na kumiliki mwili wote. Kuna mapungufu katika desturi ya kutenda kile kilicho sahihi. Kuna vitendo vya msimu, hapa na pale, wakati mambo yanaenda kwa urahisi, lakini kuwa na asili ya kufikiria mambo ya Mbingu hiyo siyo kanuni inayotawala ya akili.{2Tsw 264.1}

Hakuna haja ya kuwa mbilikimo wa kiroho, kama akili itaendelea kuzoezwa katika mambo ya kiroho. Lakini kuomba tu peke yake kwaajili ya hili, na kuhusu hili, haitakidhi hitaji la tatizo hili. Ni lazima uzoeze akili yako kujali na kuzingatia mambo ya kiroho. Ni lazima uwe na mazoea kwenye ubongo wako kuwekea umakini mzito mambo ya kiroho. Mazoezi yataleta nguvu. Wakristo wengi wapo katika njia iliyo wazi kupoteza ulimwengu zote (dunia na mbingu). Kuwa mkristo nusu na mtu wa dunia nusu, hukufanya uwe sehemu moja ya mia Mkristo na iliyobakia mtu wa dunia (1/100 Mkristo vs(dhidi) 99/100 Mtu wa dunia). {2Tsw 264.2}

Kuishi maisha ya kiroho ndiyo Mungu anahitaji, ila maelfu wanalia nje: “sijui tatizo ni nini; sina nguvu za kiroho, sifurahi roho wa Mungu” hata hivyo mtu huyo huyo atakuwa amechangamka na kuwa mwongaji

sana na kwa ufasaha wakati wa kuzumgumzia juu ya mambo ya kidunia. Sikiliza watu kama hao kwenye mkutano. Dazeni (12) ya maneno inazungumzwa na sauti ambayo haisikiki vizuri Wao ni wanaume na wanawake wa ulimwengu. Wamekuza tabia za kidunia mpaka vitivo vyao vimekuwa imara katiaka mwelekeo huo. Walakini wamekuwa wadhaifu kama watoto katika mambo ya kiroho, wakati wanapaswa kuwa imara na wenye utashi mahiri. Hawapendi kukaa katika siri ya utauwa wa Mungu. Hawajui lugha ya mbinguni na hawajafundisha akili zao ili ziandaliwe kuimba nyimbo za mbinguni au kufurahia katika mazoezi ya kiroho ambayo yatajumuisha umakini wa wote. {2Tsw 264.3}

Wale wanaodai kuwa Wakristo wa mdomo tu, Wakristo wenye udunia, hawayafahamu mambo ya mbingu. Hawataletwa katika geti la Yerusalemu mpya kushiriki katika mazoezi ambayo hayakuwafurahisha au kuwapendeza. Hawakufundisha akili zao kufurahia ibada/uchaji Mungu na katika kutafakari mambo ya Mungu na mbingu. Je, wanawezaje kushiriki vipi katika huduma za ibada za mbinguni? Watafurahiaje Anga hewa lenye mambo ya kiroho, safi na takatifu, wakati halikuwa jambo la furaha wakiwa duniani. Angahewa hilo likutakuwa usafi wenyewe-takatifu. Lakini angahewa hilo halikujulikana kwao. Walipokuwa duniani walikuwa wakitafuta stadi na mtindo wa maisha wa kidunia. Walijua mahali pa kushika na jambo la kufanya. Vitivo vya stadi za kuelekea chini kimaadili vilivyotumiwa navyo vilipata mazoezi na kukua, wakati uwezo bora zaidi na wa juu wa akili ambao haukuimarishwa kwa kutumiwa, haukuwa na uwezo wa kuamka mara moja katika zoezi la kiroho kwani havikuwa naa nguvu. Mambo ya kiroho hayatambuliwi, kwa sababu yanatazamwa kwa macho yenye mapenzi ya dunia, ambayo hayawezi kukadiria thamani na utukufu wa Kiungu/Uungu juu ya vitu vya muda na kitambo. {2Tsw 265.1}

Akili sharti ielemishwe na kuadibishwa kupenda usafi. Upendo kwa vitu vya kiroho unapaswa kuhamasishwa; ndio, lazima utiwe moyo, kama ungelikua katika neema na katika ujuzi wa Ukweli. Shauku kwa wema na utakatifu wa Kweli ni sahihi kwenda mbele kama ilivyo mpaka mwisho, lakini ukiishia hapa, itakuwa sawa-sawa na bure. Kusudi jema ni sahihi, lakini itathibitisha kuwa haina faida yoyote kama

halitatekelezwa. Wengi watapotea wakiwa wanatumainia na kutamani kuwa wakristo; lakini hawakufanya jitihada za dhati, hivyo basi watapimwa katika mizani na kukutwa wamepungua. Nia lazima izoeshwe katika mwelekeo sahihi. Nitakuwa Mkristo kwa moyo wangu wote. Nitajua urefu na upana, urefu na kina cha upendo mkamilifu. Sikiliza maneno ya Yesu: “Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana watashibishwa” Majaliwa na mipango ya kutosha yametolewa na Kristo ili kushibisha na kuridhisha roho ambayo ina njaa na kiu ya haki. {2Tsw 265.2}

Kipengele safi cha upendo kitatanua/kitafafanua nafsi kwa mafanikio ya juu, kwa maarifa yaliyoongezwa kwa mambo ya kimbingu, ili yatosheleze kwa ukamilifu. Wengi wanaojiita Wakristo hawana hisia ya nguvu ya kiroho ambayo wangeweza kuwa kama wangukuwa na matamano, ari na uvumilivu wa kupata ujuzi wa mambo ya mbingu/Mungu kama vile wanavyopata vitu visivyokuwa na maana na vinavyoharibika vya maisha haya. Umati unaodai kuwa Wakristo wameridhika kuwa mbilikimo wa kiroho. Hawana tabia ya kujijengea kutafuata kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake; hivyo utauwa ni siri na fumbo lililofichika kwao, hawawezi kulielewa. Hawamjui Kristo kwa ujuzi binafsi na uzoefu wa maisha halisi. {2Tsw 266.1}

Waache wanaume na wanawake walioridhika kwa hali zao za umbilikimo, na ulema katika mambo ya kimbingu, wasafirishwe ghafla na kisha wafike mbinguni kushuhudia papo hapo juu, hali takatifu ya ukamilifu ambayo hudumu hapo kila wakati-- kila nafsi iliyojazwa kwa upendo, kila uso ukiangaza kwa furaha; muziki wa kupendeza wenye sauti nzuri ya nyuzi/kinubi ukiinuka kwa heshima kwa Mungu na Mwana-Kondoo; na mikondo isiyokoma ya nuru ikitiririka juu ya watakatifu kutoka katika uso Wake Yeye aketie juu ya kiti cha enzi, na kutoka kwa Mwana-Kondoo; na waache watambue kuwa kuna uzoefu wa furaha kuu na ea juu zaidi unaopatikana, na kadiri ya wingi wa furaha unavyopokelewa kutoka kwa Mungu, ndivyo uwezo wao unavyoongezeka kupanda juu kwenye furaha ya milele isiyoelezeka, na hivyo kuendelea kupokea furaha mpya na ugavi mkubwa zaidi kutoka kwenye chanzo cha utukufu usiokoma wa mbinguni --Je, watu kama hao, nauliza, wanaweza kujichanganya na umati wa watu wa mbinguni,



na kushiriki katika nyimbo zao, na kustahimili usafi wao, uliotukuka, unaosafirisha utukufu unaotoka kwa Mungu na Mwana-Kondoo? Lo! Hapana Mlango wao wa rehema ulikuwa wazi kwa miaka mingi ili wapate kujifunza lugha ya mbinguni, ili waweze “kuwa washirika wa tabia ya Uungu, wakiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.” Lakini walikuwa na shuguli zao zenye ubinafsi, zenye kushirikisha nguvu za akili zao na nguvu za miili yao. Wasingeweza kumudu kumtumikia Mungu bila ya kutoa kila kitu na kufanya hii biashara. Biashara za kidunia lazima zije kwanza na kuchukua nguvu zao bora na wazo lao la muda mfupi ndiyo linatolewa kwa Mungu. Je, hao watabadilishwa baada ya uamuzi wa mwisho: “yeye aliye mtakatifu, na azidi kuwa mtakatifu” “yule aliye mchafu na azidi kuwa mchafu”? Wakati kama huo unakuja mbele. {2Tsw 266.2}

Wale ambao wameelimisha akili zao kufurahia mazoezi ya kiroho ndio wanaoweza kuchukuliwa juu mbinguni, na wasilemewe na mshtuko wa mshangao kwaajili usafi na utukufu wa juu mbinguni. Unaweza kuwa na ujuzi mzuri wa sanaa, unaweza kuwa na ujuzi wa sayansi, unaweza kushinda katika muziki na katika uandishi, tabia yako inaweza kufurahisha wenzi wako, lakini mambo haya yana uhusiano gani na maandalizi ya kuingia mbinguni? Yamefanya nini kukuandaa kusimama mbele ya mahakama ya mbinguni? {2Tsw 267.1}

Usidanganywe Mungu hadhihakiwi. Hakuna chochote isipokuwa utakatifu ndiyo utakuandaa kwenda mbinguni. Ni uchaji-Mungu ulio dhati, wenye vitendo na moyo ulio safi, wenye tabia iliyoinuliwa na kukuwezesha kuingia katika uwepo wa Mungu, “Anayeishi katika nuru isiyoweza kukaribiwa”. Tabia ya mbinguni lazima tuipe hapa duniani au hatuwezi kuipata kabisa. Basi anza mara moja. Usijidanganye mwenyewe kwamba wakati utakuja ambapo unaweza kuwa na jitihada za dhati kwa urahisi kuliko sasa. Kila siku unaongeza umbali na Mungu. Jiandae kwa ajili ya umilele kwa shauku ambayo haujawahi kuionyesha. Elimisha akili yako kuipenda Biblia, kupenda mikutano ya maombi, kupenda muda wa tafakari na zaidi ya yote muda ambayo nafsi inafanya ushirika na Mungu. Uwe mtu ambaye ana akili ya mbinguni kama utaunganishwa na kwaya katika hekalu la juu mbinguni. {2Tsw 267.2}

Mwaka mapya wa maisha yako umeanza sasa. Ukurasa mpya umefunguliwa katika kitabu cha kumbukumbu cha malaika. Nini itakuwa kumbukumbu katika kurasa zake? Je! Itajaa madoa ya wino wa kumpuuzia Mungu, na majukumu yasiyotimizwa? Hasha isiwe hivyo, Mungu asiruhusu! Hebu kumbukumbu inayopigwa na muhuri iwe ile ambayo wewe hutaibishwa nayo kama itafunuliwa na kutazamwa na macho ya wanadamu. {2Tsw 268.1}

## SURA YA 39

### UDANGANYIFU WA UTAJIRI-madanganyo ya utajiri

Dada mpendwa M: wakati Bwana aliponionyesha swala lako, nilioneshwa miaka mingi iliyopita, ulipokuwa mwongofu katika kuja Kwake Yesu hivi karibuni. Ulitazamia, na ulipenda, kuonekana Kwake Masihi. {2Tsw 268.2}

Mume wako kwa asili alikuwa mtu mwenye upendo, na ubora wa akili; lakini alitegemea nguvu zake mwenyewe, ambazo zilikuwa udhaifu tu. Hakuhi hitaji la kumfanya Mungu kuwa nguvu yake. Vinywaji vya kulevya vilipumbaza akili yake na mwishowe kupozesha uwezo wa ubongo wake. Sura yake ambayo ni ya mfano wa Mungu ilitolewa kafara ili kuendekeza kiu ya unywaji wake wa vileo vikali. {2Tsw 268.3}

Ulikabiliana na upinzani na unyanyasaji, lakini Mungu bado alibaki kuwa chanzo cha nguvu yako. Wakati uliendelea kumwamini, Yeye alikutegemeza. Katika majaribu yako yote haukuruhusiwa kuzidiwa nguvu. Ni mara ngapi malaika wa mbinguni walikuimarisha wakati ulipokuwa unakata tamaa, kwa kuwasilisha wazi wazi mafungu ya Maandiko matakatifu katika akili yako yakikuelezea, upendo wa Mungu usioshindwa, na kukupatia ushahidi kuwa fadhili Zake zenye upendo hazibadiliki, roho yako ilimtumainia Mungu. Kufanya mapenzi ya Baba yako wa mbinguni, ilikuwa chakula chako na kinywaji chako. Wakati mwingine ulikuwa na imani thabiti juu ya ahadi za Mungu, na tena, imani yako iliweza kujaribiwa kwa hali ya juu kabisa. Majaliwa ya Mungu yalikuwa fumbo kwako, hata hivyo muda mwingi ulikuwa na

ushahidi kuwa Yeye alikuwa anatazama mateso yako na hakuweza kufanya mzigo wako kuwa mzito kiasi cha kukushinda kuubeba. {2Tsw 268.4}

Bwana aliona kuwa unahitaji uimara wa ufalme Wake wa mbinguni. Hakukuacha wewe katika tanuru la moto mateso likuteketeze. Bali Kama mtakasaji na msafishaji wa fedha, Jicho Lake daima lilikuwa kwako, akitazama mchakato mzima wa utakaso, mpaka hapo atakapokuwa ameona umeakisi sura Yake ndani yako. Ingawa mara nyingi umehisi miale ya mateso inawaka juu yako, na wakati mwingine umefikiri itakuteketeza, lakini bado fadhili za upendo wa Mungu umekuwa mwingi zimekuwa juu yako katika nyakati hizi, kama vile ulivyokuwa na furaha na huru katika roho na ushindi katika Yeye. Tanuru lilikuwa kwaajili ya kusafisha na kutakasa, lakini sio kuteketeza na kuharibu. {2Tsw 269.1}

Nilikuona unapambana na umaskini, ukitafula kujikimu kimaisha wewe na watoto wako. Mara nyingi haukujua nini cha kufanya; siku za mbeleni zilionekana kuwa za giza kwako na zisizo na uhakika. Katika shida yako ulimlilia Bwana, na alikufariji na kukusaidia na miale ya matumaini ilikuangazia, ikikikuzunguka. Mungu amekuwa wa thamani kwako kwa kiasi gani kwa nyakati kama hizo! Upendo Wake unaofariji ni mtamu namna gani! Ulihisi kuwa una hazina ya thamani iliyotunzwa mbinguni. Kwa kadiri Unavyoangalia thawabu ya watoto wa Mungu wanaoteswa, ni faraja ya kiasi gani kuhisi kwamba wewe unaweza kudai kwamba Yeye ni Baba yako! {2Tsw 269.2}

Kesi yako, kwa kweli ilikuwa mbaya zaidi kuliko kama ungelikuwa ni mjane. Moyo wako ulihuzunishwa na mwenendo mbaya wa mumeo. Lakini mateso yake, ukatili wake, vitisho vyake na ukatili/vurugu, havikuongoza ujitegemee hekima yako mwenyewe, na kumsahau Mungu. Hilo lilikuwa mbali; kwa hekima ulihisi udhaifu wako na kwamba hukuweza kubeba mzigo wako, na katika udhaifu wako wa ufahamu ulifarijika kwa kuleta mzigo wako kwa Yesu, Mbeba Mizigo mkubwa. Jinsi ulivyothamini kila mwale ya nuru kutoka kwenye uwepo Wake! Na kwa uimara jinsi gani ulihisi uwepo wa nguvu Zake mara kwa mara! Wakati dhoruba ya mateso na ukatili ilipotokea juu yako bila

kutarajia, Bwana hakukuacha uzidiwe; lakini katika nyakati hizo za majaribu uligundua nguvu, utulivu, na amani ambazo zilikuwa za ajabu kwako. {2Tsw 269.3}

Wakati shutuma na kejeli kali zaidi kuliko mikuki na mishale zilipokuangukia, ushawishi wa Roho wa Mungu katika moyo wako ulikuongoza kusema kwa utulivu, bila jazba. Kwani haikuwa asili yako kufanya hivyo. Lilikuwa ni tunda la Roho wa Mungu. Ilikuwa neema ya Mungu iliyoimarisha imani yako katikati ya “Kilichotarajiwa kukawia kuja, moyo huugua”. Neema ilikufanya imara kwa vita na taabu na kukupitisha ili kujipatia ushindi. Neema ilikufundisha kuomba, kupenda na kutumaini, bila kujali mazingira yako yasiyofaa. Kwa kadri unavyokumbuka mara kwa mara kuwa maombi yako yalijibiwa kwa namna ya pekee, haukuhisi ni kwa sababu ya haki/sifa yoyote kwako mwenyewe, lakini ni kwa sababu la hitaji lako kubwa. Uhitaji wako ulikuwa ni fursa kwa Mungu. Maisha yako katika vipindi vya majaribu yalikuwa ni kumtegemea Mungu tu. Na udhihirisho wa ukombozi Wake maalum wakati ulipokuwa kwenye majaribu, ulikuwa kama chemichemi katikati ya Jangwa kwa msafiri dhaifu na aliyechoka (oasis). {2Tsw 270.1}

Mungu hakukuacha uangamie. Mara kwa mara aliinua marafiki kukusaidia, wakati ambao hukutarajia kitu. Malaika wa Mungu walikuhudumia hatua kwa hatua, walikuongoza wewe hata katika njia iliyo na mawe, mwinuko na mashimo mashimo. Ulishinikizwa na umaskini, lakini hii ilikuwa changamoto ndogo ambayo ilihitajika ukabilianenayo. Wakati N alipotumia mamlaka yake kukunyanyasa na kukudhuru, ulihisi kuwa kikombe unachokinywea ni kichungu kweli kweli; na alipojidhalilisha kufuata njia ya uovu, kwamba unakasirishwa na kutukanwa katika nyumba yako mwenyewe, alitengeneza bonde kati yake na wewe ambalo halikuweza kuvukwa kamwe. Halafu katika maumivu ya shida yako na kuchanganyikiwa Bwana Mungu aliweza kuwainua marafiki. Hakukuacha peke yako; lakini nguvu Zake zilikuwezesha, na ungeweza kusema “Bwana ni msaada wangu”. {2Tsw 270.2}

Katika majaribu yako yote, ambayo hayakuweza kufunuliwa katika uhalisi wake kwa watu wengine, kamwe haujawahi kukosa rafiki, anayesema: “Niko pamoja nanyi siku zote, hadi ukamilifu wa dahari.” Yeye Alipokuwa duniani, aliguswa sana na kilio cha mwanadamu. Ingawa sasa amepaa kwenda kwa Baba Yake, na anaabudiwa na malaika wanaozitii amri Zake kwa haraka, moyo Wake ambao unaopenda wanadamu, unaoona sikitiko na kuhurumia, haujapata badiliko lolote. Unabaki moyo wa huruma isiyobadilika bado. Yesu huyo huyo anayejua majaribu yako yote, hakukuacha wewe peke yako, upambane na majaribu, kupigana na uovu na mwishowe kupondwa kwa mizigo na lawama. Kupitia kwa malaika wake alikuningoneza, “Usiogope kwa maana Mimi Niko pamoja nawe: “ni hai, na aliyekufa, na tazama sasa ni hai hata milele. Najua huzuni yako; nimevumilia yote, nazijua changamoto zako; Nayajua majaribu yako, Nimekabiliana nayo. Nimeyaona machozi yako. Nami pia nililia. Matumaini yako ya duniani yamevunjika, lakini inua macho yako ya imani juu na tazama ndani ya pazia na hapo ndipo kuna nanga ya matumaini yako. Uhakikisho wa milele utakuwa wako, kwamba unaye Rafiki anayeshikamana kwa karibu kuliko ndugu. {2Tsw 271.1}

Oh! Dada yangu mpendwa, kama ungeona, kama nilivyoona, njia na kazi za Mungu zilivyodhihirishwa kupitia shida na majaribu yako yote katika uzoefu wa nyuma, ulipokuwa umekandamizwa na mkono wa umaskini, usingezewa kamwe kumsahau Bwana, bali upendo wako ungeongezeka, na bidii yako ya kukuza utukufu Wake isingekuwa ya kukuchosha. {2Tsw 271.2}

Kwa ajili ya mateso na majaribu yako ya kipekee, afya yako haikuweza kustahimili na ikafeli. Marafiki wanaofanya kazi ya Mungu walikuwepo lakini wachache, na wengi wao walikuwa ni maskini; na ukaona tumaini dogo sana kwa upande wa kulia kwako au kushoto. Uliwatizama watoto wako na hali yao duni, ya umasikini, ya kukosa msaada, na moyo wako karibu uzimie. Katika wakati huu, kupitia ushawishi wa Waadventisata wa Sabato ambao walikuwa wameungana na kanisa la Shakers, ambao ulikuwa ukiwaamini kwa sababu walikuwa marafiki wako wakati wa shida, ulishawishika kwenda katika dhehebu lao kwa muda, lakini malaika wa Mungu hawakukuacha. Walikuhudumia na

walikuwa kama ukuta wa moto kukuzunguka. Malaika hawa walikulinda haswa kuhusiana na ushawishi wa udanganyifu kutoka kwa watu hao. Shakers waliamini kuwa ungeweza kuungana nao katika mwelekeo wao; na walidhani ya kuwa ikiwa watakushawishi uwe mmoja wao, ungelikuwa msaada mkubwa sana kwao kwa kusudi au misheni yao; kwa sababu ungekuwa mwanachama wa nguvu wa dhehebu lao. Wangekupatia nafasi ya juu mno ya uongozi kati yao. Shakers wengine walikuwa wamepata mafunuo fulani ya kiroho, wakiwaambia kuwa uliandaliwa na Mungu kuwa mshiriki wao mashuhuri katika jamii yao; kwamba ulikuwa miongoni mwa watu ambao huwezi kuletwa kwa hoja au ushawishi wa maneno; kwamba wema wao ungekuwa na ushawishi mkubwa kwani nguvu au shinikizo ingeweza kutofaulu kwa matumaini yao. {2Tsw 271.3}

Sumaku (magnetism kama tiba) ilitumiwa miongoni mwao kwa namna ya nguvu ya ushawishi. Kupitia nguvu hii walidanganyika kuwa ungefanywa kutazama mambo kwa nuru ile ile waliyoitumia. Haukujua mbinu zote za sanaa hii na udanganyifu waliyotumia kufanikisha madhumuni yao. Bwana alikuhiifadhi. Mduara wenye mwanga ulionekana ukikuzunguka, kutoka kwa malaika wanaohudumia, ili kwamba giza lililokuwa limetanda kwako lisifunike kwa wingu wa lile duara la nuru lililokuwa likikuaangazia. Bwana aliifungua njia, nawe ukaondokana na jamii hiyo ya udanganyifu, na ukaondoka bila wao kukudhuru, kanuni ya imani yako zilikuwa safi kama vile hukuwa kati yao. {2Tsw 272.1}

Ugonjwa wa mkono wako ulileta mateso makubwa. Uligeukia Upande wa kulia na kushoto kwa ajilli ya msaada. Ulikubali mwanamke mganga ajaribu kujisifia ustadi wake juu yako. Huyu mwanamke alikuwa wakala maalum wa Shetani, kupitia majaribio yake, karibu upoteze maisha yako. Sumu aliyoingiza kwenye mfumo wako ilitosha kumua mtu mwenye mwili ulio na afya na nguvu. Hapa tena Mungu aliingilia kati, la sivyo maisha yako yangetolewa kafara. {2Tsw 272.2}

Kila njia uliyokuwa umeamua kutumia ili kurejesha afya ya mwili wako haikufanikiwa. Sio mkono wako tu, bali pia mfumo wako wote ulitiwa ugonjwa. Mapafu yako yaliathiriwa, na ulikuwa unakwenda kufa haraka

sana. Katika wakati kama huu ulihisi kuwa Mungu pekee Yake Ndiye anayeweza kuokoa. Ungeweza kufanya jambo moja zaidi; ungeweza kufuata mwelekeo wa mtume katika sura ya tano ya Yakobo. Hapo ulifanya agano na Mungu, kwamba ikiwa angeokoa maisha yako bado ungeweza kuwahudumia watoto wako mahitaji yao, ungelikuwa kwa Mungu, na Yeye peke Yake ungelimtumikia; ungeyatoa maisha yako wakfu kwa ajili ya utukufu Wake, ungetumia nguvu zako kufanya kazi Yake na kutenda mema duniani. Malaika wanaandika kumbukumbu ya ahadi iliyotolewa kwa Mungu. {2Tsw 273.1}

Tulikuja kwako wakati wa mateso yako makubwa na tukadai ahadi ya Mungu kwa niaba yako. Hatukuthubutu kuangalia mwonekano wa nje; kwa kuwa kwa kufanya hivyo tungekuwa kama Petro, ambaye Bwana alimwambia aje Kwake juu ya maji. Alipaswa kukaza macho yake juu kwa Kristo; lakini aliangalia chini mawimbi yalivyokuwa yamechafuka. na imani yake ilishindwa. Kwa unyenyekevu na uthabiti tulidai ahadi ya Mungu peke, bila kujali mwonekano, na kwa imani tuliomba Baraka. Nilioneshwa kwa upekee kuwa Mungu alifanya kazi ya ajabu, na uliokolewa kwa miujiza ya huruma Yake, na kuwa mnara hai/unaoishi kwa uweza wa Bwana wa uponyaji, kushuhudia matendo Yake ya ajabu kwa wana wa wanadamu. {2Tsw 273.2}

Wakati huo ulihisi mabadiliko makubwa, mtazamo wa akili yako uligeuzwa, na furaha na raha ilichukua nafasi ya mashaka na dhiki iliyokuwa imejaza moyo wako. Sifa za Mungu zilikuwa moyoni mwako na kwenye kinywa chako. “Ah! Ni ajabu hii Bwana ametenda!” ilikuwa hisia ya moyo wako. Bwana alisikia maombi ya watumishi Wake, na kukuinua juu mpaka sasa unaishi na kuvumilia majaribu, ukitazamia na kungojea kuonekana Kwake, na kulitukuza Jina Lake. Umaskini na masumbufu vilishinikiza kwa kiasi kikubwa. Wakati mwingine wingu jeusi lilikufunika, ukashindwa kuvumilia kuuliza. “Ee Mungu, umeniacha?” Lakini hakuachwa, ingawa hukuweza kuona njia wazi mbele yako. Bwana angependa wewe utumainie upendo na rehema Zake katikati ya wingu na giza, na vile vile ukiwa kwenye jua. Wakati mwingine mawingu yaliondoka, na nguzo ya nuru ingekuangazia daima kuimarisha moyo wako uliokata tamaa na kukuongezea ujasiri na ungeweza tena kuweka imani yako inayoyumba-yumba juu ya ahadi za

uhahika wa Baba yako wa mbinguni. Uliweza kulia bila kupanga- Ee, Mungu, ninakuamini; ninakutumainia. Hata sasa umekuwa msaada wangu, wala haujaniacha hata sasa. {2Tsw 273.3}

Jinsi ulivyopata ushindi, na nuru ikakuangazia tena, hukuweza kupata lugha ya kuelezea shukrani zako za dhati kwa Baba yako wa mbinguni kwa neema yake; na ulidhani kuwa hautakuwa na mashaka tena na upendo Wake na utunzaji Wake. Haukutafta maisha rahisi. Haukuchukulia kama kazi nzito zinazohitaji bidii kama ikiwa njia ingefunguka wazi ili kwamba uweze kuwatunza watoto wako na kuwalinda dhidi ya uovu ulioshamiri katika zama hizi ulimwenguni. Ulikuwa mzigo wa moyo wako kuwaona watoto wako wakimgeukia Bwana. Ulimwomba Mungu kwa kulia sana na kwa majonzi makubwa kwa ajili ya watoto wako. Ulikuwa na shauku kubwa ya uongofu wao. Wakati mwingine moyo wako ulikata tamaa na kuzimia, na ukahofu kuwa maombi yako hayataweza kujibiwa; uliwaweka tena wakfu watoto wako kwa Mungu upya, na matamania ya moyoni mwako yakawaweka mbele ya madhabahu. {2Tsw 274.1}

Walipoingia jeshini, maombi yako yaliwafuata huko. Walitunzwa kwa namna ya ajabu, kutoka katika hatari. Wakaita kuwa ni bahati yao nzuri; lakini maombi ya mama yaliyotoka kwenye moyo wenye fadhaa/wasiwasi, moyo uliolemewa na mzigo, kama alivyohisi hatari kwa watoto wake na kukatwa kwa maisha yao ujanani bila kuwa na matumaini kwa Mungu, ndio, ulikuwa na mengi ya kufanya kwa utunzaji wao. Ni maombi mangapi yalipelekwa mbinguni ili kwamba watoto hawa wafundishwe kumtii Mungu, kutoa maisha yao wakfu kwa utukufu wa Mungu! Katika mfadhaiko wako ulimwomba Mungu akurudishie watoto wako tena kwako, na ungetafuta kwa bidii kuwaongoza katika haki. Ulifikiri kuwa ungeweza kufanya kazi kwa uaminifu wa ziada kuliko vile uliyokwisha kuifanya kwao. {2Tsw 275.1}

Mungu alikuruhusu uweze kufundishwa katika shule ya shida na mateso yako, ili kwamba uweze kupata uzoefu ambao utakuwa wa thamini kwako na kwa wengine. Katika siku za umaskini wako na majaribio ulimpenda sana Mungu, na ulipenda fursa ya mambo ya dini. Ujio wa Yesu uliokuwa karibu ulikuwa faraja kwako. Lilikuwa tumaini



lako lililo hai kwamba hivi karibuni ungeweza kupata kupumzika kutokana na kazi, na kuhitimisha changamoto na majaribu yako yote; Ulipogundua kuwa haujafanya kazi au kuteteseka sana; kwani mtume Paulo anatangaza “Mateso tunayoyapa ni ya kitambo tu, hutufanya tuzidi sana kuyapatia uzito mambo ya umilele” {2Tsw 275.2}

Kukutana na watu wa Mungu kwako kulionekana kama kuitembelea mbingu. Vigingi havikuweza kukuzuia. Ungeweza kuvumilia kupata uchovu na njaa ya chakula ya muda mfupi, lakini hakutaka kunyimwa chakula cha kiroho. Uliitafuta neema ya Mungu kwa bidii, nawe hukutoka bure. Ushirika na watu wa Mungu vilikuwa mbaraka wenye utajiri ambao uliweza kufurahia.{2Tsw 275.3}

Katika uzoefu wa Kikristo nafsi yako ilichukia, ubatili, kiburi na kujionyesha. Uliposhuhudia mwenendo wa wale waliodai kuwa ni Wakristo walikuwa ni watu wa kujionyesha na kuchochea kiburi, moyo wako na mdomo wako ulisema; “Laiti kama mimi peke yangu ningepata mali ya watu ambao sio waaminifu katika uwakili wao, ningehisi kama fursa ya pekee ya kuwasaidia wahitaji na kusaida maendeleo ya kazi ya Mungu!” {2Tsw 275.4}

Mara nyingi ulitambua uwepo wa Mungu unapomtafuta kwa njia ya unyenyekevu kuwaangazia wengine kulingana na Ukweli katika siku hizi za mwisho. Ulikuwa umejionea Ukweli mwenyewe. Yale ambayo ulikuwa umeyaona, umeyasikia, umeyapitia na kuyashudia, ulijua kuwa sio riwaya/hekaya za uongo. Ulifurahia kuwasilisha mbele ya watu wengine, katika mazungunzo ya faragha, njia za ajabu ambazo Bwana alikuwa amewaongoza watu Wake. Ulisimulia kushughulika Kwake na matumaini hata ukaleta usadikisho kwenye mioyo ya wale waliokusikiliza. Ulongea kana kwamba una ujuzi wa mambo ambayo umethibitisha. Wakati wa kuzungumza kwa wengine kwa Ukweli wa Sasa, ulitamani fursa kubwa zaidi na ushawishi uliopanuliwa zaidi, ili uweze kuwajulisha wengi walio katika giza, waingie kwenye nuru iliyoangaza katika njia yako. Wakati mwingine uliangalia umaskini wako, ushawishi wako uliokuwa na mipaka, na bidii zako, ambao mara

kwa mara ulitafsiriwa vibaya na wale wanaodai kuwa marafiki wa Ukweli, na ulikuwa karibu kuvunjika moyo. {2Tsw 276.1}

Wakati mwingine katika hali yako ya kutokuwa na utulivu ulikosea katika maamuzi, na kulikuwa na wale ambao walipaswa kuwa na upendo ambao haufikirii ubaya, waliotazama, na kushuku mabaya na wakayakuza zaidi makosa waliyofikiri walikuwa wakiyaona toka kwako. Lakini upendo na huruma nyororo ya Yesu havikuondolewa; vilikuwa ni msaada kwako katikati ya majaribu na mateso ya maisha yako. Ufalme wa mbinguni na haki ya Yesu Kristo vilikuwa msingi wako. Maisha yako yalikuwa na makovu ya kutokuwa na ukamilifu, kwa sababu u binadamu ambaye hajakamilika na hivyo hukosea, lakini kutoka kwa kile ambacho Mungu amekuwa akifurahishwa kunionyesha kwenye maisha yako ya kukatisha tamaa yaliyokuwa yanakuzunguka katika siku zako za majaribu na umaskini, simjui mtu ambaye angeweza kuwa na uhuru zaidi yako kutenda makosa kuliko wewe ulivyotenda, kama wangukuwa na mazingira kama yako yalivyokuwa, katika umaskini na majaribu yenye aibu. Ni rahisi kwa wale ambao wameepushwa na majaribu mazito ambayo wengine wanakabiliwa nayo, kutazama na kuhoji na kushuku uovu na kutafuta makosa. Wengine wako tayari kuwakosoa wengine kwa kufuata njia tofauti kuliko kuchukua jukumu la kusema nini kifanyike, au kuonyesha njia sahihi zaidi. {2Tsw 276.2}

Ulichanganyikiwa. Hukujua ni wapi pa kutumainia. Kulikuwa na watunza Sabato wachache katika...na jirani ambao walitoa ushawishi unaoookoa. Wengine ambao walidai kuwa na imani hawakuwa na heshima ya Ukweli wa Sasa. Hawakukusanya pamoja na Kristo, lakini walitapanya mbali. Walikuwa wanazungumza kwa sauti kubwa na muda mrefu; Lakini mioyo yao haikuwa katika kazi hiyo. Hawakutakaswa na Ukweli waliokuwa wanaukiri. Hawa ambao hakuwa na mizizi ndani yao wenyewe, hivyo waliacha imani. Kama wagelifanya hili katika kipindi cha mwanzo kabisa, ingekuwa vizuri kwa ajili ya maslahi ya Ukweli wa Neno la Mungu. Katika matokeo ya mambo hayo Shetani alijipatia faida kwako na kuandaa njia kwa ajili ya kurudi kwako nyuma. {2Tsw 277.1}

Umakini wangu uliitwa katika shauku yako ya kutaka kumiliki mali. Hisia ya moyo wako ilikuwa: Ah! Ikiwa ngingekuwa na fedha/mali, nisingekuwa mbaradhifu! Ngingekuwa mfano kwa wale ambao ni mabahili na wanaotubu. Ningewaonyesha mbaraka mkubwa unaopokelewa kwa kutenda mema. Nafsi yako inachukia tamaa. Jinsi ulivyoona wale ambao walikuwa na mali nyingi za ulimwengu huu wakifunga mioyo yao kwa kilio cha wahitaji ulisema; “Mungu atawatembelea; atawalipa ujira kulingana na kazi zao”. Kama ulivyoona matajiri wanavyotembea kwa kiburi chao, mioyo yao imezungukwa na ubinafsi, kama kamba za chuma unahisi kuwa walikuwa maskini kuliko wewe, ingawa ulikuwa mhitaji na mwenye kuteseka kuliko wao. Ulipowaona hawa wanaume wenye kiburi wakijiinua kwa sababu ya nguvu za pesa, uliwasikitikia, na usingependa kubadilisha nafasi nao. Japo ulitamani kuwa na mali ambayo ungetumia kama karipio au kuwasuta wale wenye tamaa. {2Tsw 277.2}

Bwana akamwambia Malaika Wake ambaye amekuhudumia hata sasa: “nimemthibitisha katika umaskini wake na mateso yake hajajitenga mbali Nami, wala hata kuniasi. Sasa nitamthibithisa na ustawi, na mafaniko. Nitamfunulia ukurasa wa moyo wa binadamu ambao haufahamu. Nitamwonyesha kuwa pesa ni adui hatari zaidi aliyewahi kukutana naye. Nitamfunulia udanganyifu wa utajiri; kwamba ni mtego, hata kwa wale ambao wanahisi kuwa wako salama kutokana na ubinafsi, na hata kuona kwamba wamethibitishwa kuwa imara kwa kutukuzwa, ubaradhifu, kiburi na kupenda kusifiwa na mwanadamu.” {2Tsw 278.1}

Kisha nikaonyeshwa kuwa njia ilifunguliwa kwa ajili yako kuboresha hali ya maisha yako na kwa urefu ili uweze kupata mali ambazo ulifikiria utatumia kwa hekima na kwa utukufu wa Mungu. Je, ni kwa wasiwasi kiasi gani Malaika anayekuhudumia alikuwa akikutazama katika majaribu yako mapya na kuona ni msimamo gani utakaokuwa nao katika mtihani huo. Kwa kadri ulivyopata mali mkononi kwako, nilikuona taratibu na kwa uhakika ukijitenga mbali na Mungu. Mali uliyokabidhiwa ulitumia kwa faida yako binafsi, ukijizungushia vitu vizuri ya maisha haya. Niliwaona Malaika wakikuangalia kwa shauku, wakiwa na huzuni, nyuso zao zikiwa zimefunikwa nusu, wakisikitika

kukuacha. ila uwepo wao haukuonekana kwako, na ulifuata mwendo wako mwenyewe bila ya kuwa na kumbukumbu kuwa una Malaika anayekulinda. {2Tsw 278.2}

Biashara na masumbufu ya cheo nafasi yako mpya vilichukuwa muda wako mwingi na umakini wala hakujali wajibu wako kwa Mungu. Yesu alikuwa amekununua kwa damu Yake Yeye Mwenyewe. Wewe sio mali yako mwenyewe. Muda wako unaotumia kushugulikia vitu, uwezo wako, nguvu na mali unazozitumia, yote haya ni mali ya Mkombozi wako. Yeye Amedumu kuwa Rafiki yako, uwezo na msaada wako wakati ambapo marafiki wote walipokuacha. Umelipa upendo na neema ya Mungu kwa kutokuwa na shukrani na usahaulifu. {2Tsw 278.3}

Usalama wako pekee ulikuwa tu ni kumtumainia Kristo Mwokozi wako. Hakukuwa na usalama kwako mbali na msalaba wa Kalvari. Ni kwa namma gani uwezo wa kibinadamu ni dhaifu kama ilivyoonekana katika tukio hili! Ah! Ni dhahiri jinsi gani kuona Ukweli kuwa mwanadamu hana uwezo kabisa isipokuwa ule ambao Mungu anatoa kwa wale wanaomtegemea na kumtumainia! Ombi moja tu linalotolewa kwa Mungu kwa imani ya dhati lina nguvu zaidi kuliko utajiri wa akili ya mwanadamu. {2Tsw 279.1}

Katika mafanikio yako haukutekeleza maazimio uliyokuwa umekusudia katika shida yako. Udanganyifu wa utajiri ulikugeuza kutoka kwenye malengo yako. Masumbufu ya maisha yaliongezeka kwako. Ushawishi wako uliongezeka. Wenye dhiki na waliosumbuka waligundua unafuu kutoka kwenye mateso yao, wakakutukuza wewe, nawe ukajifunza kupenda kupokea sifa kutoka kwenye midomo ya binadamu maskini anayekufa. Ulikuwa katika jiji maarufu, na ulifikiri ni muhimu kuwa hapo ili kufanikisha biashara yako, na kutunza ushawishi wako, kwa mazingira yako kuwa yalingane na hali ya biashara yako. Lakini ulichukua mambo na kuyapeleka mbali sana. Ulisukumwa sana na maoni na maamuzi ya watu wengine. Ulitumia mali kwa namna isiyo ya lazima, ili tu kuridhisha tu tamaa ya jicho lako na kiburi cha maisha yako. Ulisahau kuwa u wakili wa pesa za Bwana wako. Wakati mali zilitumika kwa kuhimiza ubatili tu, hukuzingatia kuwa malaika

wanaweka kumbukumbu ya uliyokuwa unatenda ambayo kwa mshangao na aibu haukujua utakuja kukutana nayo tena. Alisema malaikia huku akikunyoshea kidole “Ulijitukuza wewe mwenyewe, lakini haukuweza kumtukuza Mungu”. Hata ulijiinua katika kudhani ya kuwa uwezo wako wa kununua vitu ulitoka kwako mwenyewe. {2Tsw 279.2}

Sehemu kubwa ya pesa imetumiwa kwa vitu visivyo na maana ambavyo vingeweza kusemwa kuwa vilifanywa tu kwa kujionyesha, kuhimiza moyo wa ubatili na kiburi kitakacho kuletea kujuta na aibu. Ikiwa ungekuwa unazingatia madai ya mbingu juu yako na uweke mwelekeo sahihi wa mali uliyopewa mamlaka kuiangalia, kwa kuwasaidia wahitaji na kuendeleza Ukweli wa Sasa, ungekuwa umeweka hazina mbinguni na ungeweza kuwa tajiri kwa Mungu. Fikiria ni kiasi gani cha pesa umewekeza ambapo hakuna mtu aliyefaidika, hakuna aliyelishwa au kuvishwa, na hakuna mtu aliyesaidiwa kuona makosa ya njia zake ili amgeukie Kristo na kuishi. {2Tsw 279.3}

Umefanya uwekezaji mkubwa katika biashara zisizo na uhakika. Shetani alipofusha macho yako ili usiweze kuona kuwa biashara hizi hazitakupatia faida yoyote. Biashara ya kujipatia uzima wa milele haikuweza kuamsha shauku yako. Hapa ungetumia mal ibila hatari yote hii, bila riski, bila kukatishwa tamaa, na mwisho ungeweza kupata faida tele. Hapa ungeweza kuwekeza katika benki isiyoshindwa kamwe, benki ya mbinguni. Hapa ungeweza kutoa hazina zako ambapo hakuna mwizi anayeweza kukaribia wala kutu kuharibu. Biashara hii ni ya milele na ni bora zaidi kuliko biashara yoyote ya kidunia, kama vile mbingu zilivyo juu kuliko dunia. {2Tsw 280.1}

Watoto wako hawakuwa wanafunzi wa Kristo. Walikuwa katika urafiki na dunia na moyo wao wa asili ulitamani kuwa kama walimwengu. Tamaa ya macho na kiburi cha maisha iliwatawala na watu waliweza kukushawishi kwa kiasi fulani. Umetafuta kwa bidii zaidi kuwapendeza na kuwaridhisha watoto wako kuliko kumpendeza na kumtukuza Mungu. Umesahau madai ya Mungu juu yako, na mahitaji ya kazi Yake. Ubinafsi umekufanya utumie pesa kwa mapambo na kujifurahisha mwenyewe na watoto wako. Haukufikiria kuwa pesa hizi sio zako; kwamba ulikopeshwa tu, ili kukujaribu na kuthibitisha wewe, kuona

kama utajua na kuepuka maovu uliyoyathibitisha kwa watu wengine. Mungu amekufanya wewe kuwa wakili Wake na atakaporudi na kukuhesabu na watumishi Wake, ni hesabu gani utakayoitoa kama wakili? {2Tsw 280.2}

Imani yako na kumtegemea kwa unyenyekevu ilianza kupotea pole pole kwa hakika pale, mali ilipoanza kutiririka kwako. Haukumwacha Mungu ghafla au mara moja. Kurudi kwako nyuma kulikuwa taratibu. Uliacha ibada ya asubuhi na jioni kwa sababu haikufanya taratibu zako ziende unavyotaka-ilikuwa usumbufu. Mke wa mtoto wako (mkamwana) alikusababishia jaribio la kipekee, wa tabia ya ujeuri, iliyoonekana kukatisha tamaa kuendelea na maombi ya familia. Nyumba yako ikawa nyumba isiyo na maombi. Biashara yako uliifanya kuwa ya kwanza, na Bwana na Ukweli Wake vilifanywa kuwa namba mbili. Tazama nyuma uone uzoefu wako wa mwanzo; Je, majaribu haya wakati ule yangeliweza kuondoa familia yako kutoka kwenye maombi? {2Tsw 280.3}

Hapa, kwa kupuuza maombi ya sauti, ulipoteza ushawishi katika nyumba yako ambayo ungeweza kuudumisha. Ilikuwa jukumu lako kumtambua na kumkiri Mungu katika familia yako, bila kujali matokeo. Maombi yako yalipaswa yawasilishwe mbele za Mungu asubuhi na jioni. Ungekuwa kama kuhani wa Bwana katika familia yako, ukiungama dhambi zako na za watoto wako. Kama ungekuwa mwaminifu, Mungu, Ndiye ambaye angekuwa kiongozi wako, usingemwacha na kufuata hekima yako mwenyewe. {2Tsw 281.1}

Mali zilitumiwa isivyo lazima ila kwa kujionyesha. Juu ya dhambi hii kwa wengine ungehisi huzuni kubwa. Na wakati wewe unatumia mali hiyo hiyo, ulikuwa unamwibia Mungu. Kisha Bwana akasema: "nitatawanya. Nitamruhusu kwa wakati, atembee katika njia ya hiari yake mwenyewe. Nitapofusha hukumu na kuondoa hekima. Nitamwonyesha kwamba nguvu zake ni dhaifu, na hekima yake ni upumbavu. Nitamshusha na kumfumbua macho yake ili aone ni mbali kwa kiasi gani ameniacha. Ikiwa kama hatanigeukia kwa moyo wake wote, na katika njia zake zote kunikiri Mimi, Mkono Wangu utatawanya, na kiburi cha mama na watoto wake kitaangushwa chini, na umaskini

utakuwa tena fungu lao. Jina langu litatukuzwa. Kujivuna kwa mwanadamu kutaweza kushushwa chini, na kiburi cha mwanadamu kitashushwa pia. {2Tsw 281.2}

Mtazamo huo hapo juu ulitolewa mnamo tarehe 25 mwezi 12 1865, katika jiji la Rochester, New York. Mwezi wa Juni uliopita nilioneshwa kuwa Bwana alikuwa akikushughulikia kwa upendo, na sasa anakualika umrudie Yeye ili uweze kuishi. Nilioneshwa kuwa kwa miaka mingi sasa umehisi kuwa umekuwa katika hali ya kurudi nyuma kiroho. Ikiwa uliwekwa wakfu kwa Mungu unaweza kuwa umefanya kazi nzuri na kubwa katika kuruhusu nuru yako iangaze kwa wengine. Kwa kila mtu kazi ya kufanya kwa Bwana imetolewa. Kwa kila mmoja wa waja Wake Bwana, ametoa karama maalum, au talanta. “Akampa mmoja talanta tano, na mwingine mbili, na mwingine talanta moja; kwa kila kulingana na uwezo wake/anuwai.” Kila mtumishi ameaminiwa kwa kupewa karama/talanta fulani ambayo atawajibika kwayo; na amana hizi tofauti zinaendana na uwezo wa kila mtumishi. Katika kutoa hizi talanta Zake, Mungu hajaonyesha upendeleo/ubaguzi. Amegawanya talanta kulingana na uwezo wa kila mtenda kazi Wake, Naye anatarajia mrejesho kwa kila alichokupa. {2Tsw 281.3}

Katika uzoefu wako wa awali Bwana alikupa talanta za ushawishi, lakini hakukupa talanta ya mali, hivyo hakukutarajia wewe utoe katika umaskini wako kiwango ambacho hakukupa. Kama mama mjane, ungetoa kile unachoweza, ingawa kama umezingatia mazingara yako mwenyewe, ungehisi udhuru kutokana na kufanya hata vile ulivyofanya. Katika ugonjwa, Mungu hakuhitaji kutoka kwako hiyo nguvu ya utendaji inayotumika pale ambapo ugonjwa ulikuwa umekunyima. Ingawa ulikuwa umezuiliwa katika ushawishi na uwezo wako, lakini Mungu alikubali juhudi zako za kufanya mema na kuendeleza kazi yake kulingana na kile ulichonacho, sio kulingana na kile usichokuwa nacho. Bwana hadharau sadaka iliyotolewa kwa unyenyekevu, hiari moyo na kwa dhati. {2Tsw 282.1}

Una uchangamfu na ari. Bidii na kuwa dhati katika jambo jema ni sifa nzuri. Katika majaribu yako ya awali na kuchanganyikiwa, ulikuwa unapata uzoefu ambao ulikuwa wa faida kwa watu wengine. Ulikuwa

na bidii na ari ya kumtumikia Mungu. Ulikuwa unapenda kuwasilisha ushaidi wa msimamo wetu kwa wale ambao hawaamini Ukweli wa Sasa. Uliweza kusema kwa uhakika, kwa sababu mambo haya yalikuwa uhalisia kwako. Ukweli ulikuwa ni sehemu ya kiini cha maisha yako; na wale waliousikiliza wito wako wa bidii na dhati hawakuwa na shaka kwa uaminifu wako, bali walisadikishwa kwamba mambo haya yalikuwa Kweli. {2Tsw 282.2}

Katika majaliwa ya Mungu ushawishi wako umetanuka; nikiongezea na hili, Mungu ameona kuwa inafaa kukuthibitisha kwa kukupatia talanta ya mali. Kwa hivyo umewekwa chini ya uwajibikaji mara mbiili. Hali yako ya kimaisha ilipoimarika, ulisema “Mara tu nitakapopata nyumba basi nitachangia kazi ya Mungu” Lakini mara ulipokuwa na nyumba ndipo ulipoanza kuona mambo mengi ya kuyafanyia maboresho kama vile ulivyoona inakufaa na kukufurahisa kiasi kwamba ulimsahau Mungu na madai Yake kwako, na kwa kiasi kidogo sana ulipenda kusaidia kazi ya Mungu kuliko siku zako za umaskini na mateso yako. {2Tsw 283.1}

Ulikuwa unautafuta urafiki na ulimwengu, na kujitenga zaidi na zaidi kutoka kwa Mungu. Ulisahau agizo/himizo la Kristo: “jihadharini ninyi wenyewe, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi na ulevi na wasiwasi wa maisha haya, na hivyo siku hiyo ije juu yenu bila kujua.” “Ajidhanie amesimama aangalie asianguke.” {2Tsw 283.2}

Kuna maneno matatu katika kauli-mbiu ya maisha ya Kikristo, ambayo yanapaswa kuzingatiwa ikiwa hatungetaka Shetani afanye jitihada za kutunyemelea bila ya sisi kung’amua; yaani, *Kesha, omba, fanya kazi*. Maombi na kukesha ni muhimu ili kusonga katika maisha ya Kiroho/Kiungu. Kamwe hakukuwa na wakati muhimu zaidi katika historia yako kama sasa. Usalama wako pekee ni kuishi kama mlinzi. Kesha na kuomba daima. Ah! Ni kinga ya ajabu kiasi gani dhidi ya kuingia majaribuni na kuanguka katika mitego ya ulimwengu! Je! Unapaswa kuwa na bidii kiasi gani katika kazi miaka hii michache iliyopita, wakati ushawishi wako ulikuwa mpana. {2Tsw 283.3}



Dada mpendwa, sifa za mwanadamu na mkondo wa kusifiwa kwa udangayifu na ulimwenguni umekuwa na ushawishi mkubwa kwako kuliko vile ulivyokuwa unajua. Haukuwa ukiboresha karama zako-ukizitoa nje kwa kuzichuuza kwa wafanyabiashara. Kwa asili yako una mapenzi na u mkarimu. Tatizo ni kwamba tabia hizi zimekuwa kwenye utendaji kwa kiwango kikubwa, lakini sio kama vile Mungu anavyohitaji zitumiwe. Kumiliki tu hizi karama bora, haitoshi; Mungu anahitaji ziendele kutumiwa daima, kwa maana kupitia karama hizo, Yeye atawabariki wale wanaohitaji kusaidia kuendeleza kazi Yake kwaajili ya wokovu wa mwanadamu. {2Tsw 283.4}

Bwana hatategemea roho zenye ubinafsi na ubahili kuwatunza maskini wanaostahili, wala kuendeleza kusudi la kazi Yake. Hao ni watu wenye akili finyu mno; wangelalamika tu, huku wakiwa na kinyongo kwa kuwahurumia kidogo tu wale walio wahitaji na wenye dhiki. Pia wangetaka huduma hiyo ya kazi ya Mungu ipunguzwe kulingana na akili zao finyu. Kutunza mali ndiyo wazo lao kuu. Mbinu za kupunguza utoaji wa huduma kwao ni wazo linalojitokeza sana. Fedha zao ndiyo zenye thamani zaidi kwao kuliko hata roho ambazo Kristo alizifia. Maisha kama hayo, ni mabaya zaidi kuliko sifuri (tupu) kwa kadri Mungu na mbingu inavyohusika. Mungu hatakabidhi kazi Yake muhimu mikononi mwao. {2T 284.1}

“Ulaaniwe Merozi, akasema malaika wa Bwana, ulaaniwe vikali katika maisha yako hayo; kwa sababu haukuja kwa msaada wa Mungu, kwa msaada wa Mungu dhidi ya wenye nguvu kubwa.” Merozi alikuwa amefanya nini? Hakuna lolote alilofanya. Ila hii ndiyo ilikuwa dhambi yao. Laana ya Mungu ilikuja juu yao kwa sababu ya yale ambayo hawakuyafanya (omission). Mtu mwenye akili ya ubinafsi, na finyu, anawajibika kwa ubahili/uchoyo wake, lakini wale walio na mapenzi kwa watu, wenye hisia za huruma, msukumo wa ukarimu na upendo kwa roho zilizo chini ya wajibu wao mzito, wanaweka kwenye wajibu mzito, unaowakandamiza; kwa maana wakiruhusu karama hizi zikabaki bila kutumiwa na kupotea watajumuishwa na watumwa wasio waaminifu. Kuwa na hizi karama pekee haitoshi. Wale walio nazo wanapaswa watambue kuwa majukumu na wajibu wao unaongezeka. {2T 284.2}

Bwana atahitaji kila wakili Wake kutoa hesabu ya uwakili wake, kuonyesha kile alichozalisha kwa karama/amana alizopewa. Wale ambao watapewa tunu hawatajisifia wenyewe kustahili kwao na uadilifu walioiufanya kwenye biashara; watampa Mungu utukufu wote. Wanasema juu ya kile walichopewa, kuwa “Talanta Yako” na wala siyo yao wenyewe au yetu sisi. Wanapozungumzia juu ya kufanikiwa kwao au ongezeko, wote wanakuwa waangalifu katika kuelezea, ni wapi ilipotoka. Mitaji yao ilitolewa na kukuzwa na Bwana wao. Waliifanya biashara Yake kwa mafanikio makubwa, na kurudisha mtaji na faida, kwa Mpaji. Yeye Alizawadia jitihada zao za dhati kana kwamba sifa zote hizo ni za kwao wenyewe, wakati wana deni la neema na rehema nyingi za Mtoaji. Maneno Yake katika kuwazaidia na kuwapongeza wale wasiostahili yanaanguka masikioni mwao: “Vema mtumwa mwema na mwaminifu: ulikuwa mwaminifu kwa machache, Nitakufanya uwe mwaminifu kwa mengi; ingia katika furaha yya Bwana wako. {2T 284.3}

Kwako, wewe Dada yangu, umekabidhiwa karama ya ushawishi na karama ya kuwa fedha; na wajibu wako ni mkubwa. Inakupasa utembeke kwa umakini na hofu ya Mungu. Hekima yako ni dhaifu, lakini hekima itokayo juu ni imara na ina nguvu. Bwana amekusudia kukuangazia katika giza lako na kukudokeza kidogo, mwonekano wa mambo ya hazina ya mbinguni, ili uweze kuwa na uelewa wa kulingananisha mambo ya dunia na mbingu, na kisha akuache uchague kati ya dunia na maisha ya uzima wa milele. Niliona kuwa bado una fursa ya kurudi kundini. Yesu amekukomboa kwa damu Yake Yeye mwenyewe, na anakuhitaji utumie karama zako katika huduma Yake. Moyo wako haujafanywa mgumu kiasi cha Roho Mtakatifu kushindwa kukufikia. Wakati Ukweli wa Neno la Mungu unapowasilishwa, hukutana na mwitikio wa moyo wako. {2T 285.1}

Niliona kuwa unapaswa kutafakari na kujifunza kuhusiana na kila hatua. Haupaswi kufanya chochote kwa harara. Acha Mungu awe mshauri wako. Yeye Anawapenda watoto wako, na ni sahihi wewe nawe uwapende; lakini sio sahihi kuwapa sehemu ya upendo unaopaswa kumpa Mungu, ambao Yeye anadai. Wana misukumo ya wema, huruma na ukarimu. Wana sifa nzuri ya tabia. Ikiwa wangeona hitaji lao

pekee la Mwokozi na kusujudu chini ya msalaba, wangeweza kupata ushawishi wa kutenda mazuri. Kwa sasa wana mapenzi na mambo yanayowafurahisha ya anasa kuliko kumpenda Mungu. Kwa sasa wamesimama upande kwenye safu ya adui, na chini ya bendera nyeusi ya Shetani. Yesu anawaalika waje Kwake, kuacha kuwa upande wa adui, na kusimama chini ya bendera ya damu ya msalaba wa Kristo. {2T 285.2}

Hii inaoneka kwao kama kazi ambayo hawawezi kuifanya, kwa kuwa itawalazimu kujikana nafsi mno. Hawana maarifa ya vitendo kwenye njia. Wale waliojikusisha na vita vya nchi, na wamekuwa katika hali ngumu, taabu na hatari za maisha ya kiaskari, wanapaswa kuwa wa mwisho katika kusita na kudhihirisha woga katika vita hivi vikubwa vya uzima wa milele. Katika kesi hii watapigania taji ya maisha na urithi wa kutokufa. Mshahara wao utakuwa wenye uhakika na mkamilifu, na vita vitakapomalizika faida yao itakuwa uzima wa milele, furaha isiyo na kazi, na uzito wa milele wa utukufu. {2T 286.1}

Shetani atapinga kila hatua watakayokuwa wanaifanya. Atawasilisha ulimwengu mbele yao kwa upeo wake wote wa kuvutia, kama alivyofanya kwa Mwokozi wa ulimwengu wakati alipomjaribu siku arobaini jangwani. Kristo alishinda majaribu yote ya Shetani, na ndivyo pia inapaswa iwe kwa watoto wako. Wanamtumikia bwana mgumu. Mshahara wa dhambi ni mauti. Dhambi inagharimu mno, hawawezi kulipia gharama zake-[kifo na uzima wa milele ndiyo gharama-deni la dhambi, hakuna mwanadamu aweza kulilipia isipokuwa Yesu]. Wataiona kuwa ni biashara yenye gharama kubwa- ngumu. Watakutana na hasara ya milele mwishoni. Watapoteza majumba ambayo Yesu amekwenda kuwaandalia wale wanaompenda, na watapoteza uzima ambao ungelingana na maisha ya Mungu (umilele). Na hii sio yote. Lazima wanywee kikombe cha ghadhabu kwa kumkosea Mungu kwa kusitisha huduma yao Kwake na kusalimisha maisha yao yote kwa adui mbaya. Watoto wako bado hawajapata nuru halisi vizuri, na hukumu hufuata tu kukataa kwao nuru. {2T 286.2}

Ikiwa wale wanaodai kuwa Wakristo wote walikuwa wanyofu na dhati na wenye bidii katika juhudi zao za kukuza utukufu wa Mungu, Je, ni

machafuko ya kiasi gani yangeelekezwa katika safu ya adui. Shetani ana bidii na ni mkweli katika kazi yake. Hataki roho ziokolewe. Hataki nguvu zake juu yao waliovunjika. Shetani hana masihara na wala hajifanyi (siyo feki). Ni Mwenye bidii kali. Anaona Kristo anaalika roho kuja Kwake ili kupata uzima, na anafanya juhudi na ari kubwa katika jitihada zake za kuwazuia watu wasiukubali wito. Hakuna njia ambayo hataiacha bila ya kuijaribu kuitumia kuwazuia kutoka chini ya jeshi lake na kuwa chini ya safu ya Kristo. Je! Ni kwa nini wale wanaojiita wafuasi wa Kristo hawawezi kuwajibika kwa juhudi sana Kwake, kama ambavyo maadui Wake hufanya juhudi dhidi Yake? Kwa nini wasifanye klile wawezalo? Shetani hufanya kila awezalo kuzihifadhi roho zisiwe upande wa Kristo. Alikuwa wakati mmoja malaika aliyeheshimika Mbinguni, na ingawa ameshapoteza utakatifu wake, hajapoteza nguvu zake. Anabamiza nguvu zake zenye matokeo ya kutisha. Hasuburi mawindo yake kumjia. Anawinda-huyafuata mawindo. Huenda huku kule duniani kama simba angurumaye, akitafuta mtu ammeze. Siku zote havai sura ya ukali wa simba, lakini wakati anapooni atafanya kazi nzuri na kupata ufanisi bora kwa kujigeuza kuwa kama malaika wa nuru, basi hufanya hivyo. Anaweza kubadilisha ngurumo ya simba kwa urahisi kwa hoja zenye ushawishi zaidi au kwa mnong'ono laini. Ana vikosi vya Malaika kumsaidia katika kazi yake-mapepo. Mara nyingi huficha mitego yake na vishawishi vyenye udanganyifu wa kuvutia. Yeye huvutia na kuwadanganya wengi kwa kusifia ubatili wao, yaani kuwapaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Kupitia wakala wake huwasilisha raha za ulimwengu kwa nuru ya kuvutia, akisambaza njia ya kuzimu kwa maua yenye majaribu, na hivyo ndivyo roho hulogwa, huvutwa na kuharibiwa. Baada ya kila hatua yenye kusonga mbele katika barabara ya kushuka chini, Shetani ana majaribu maalum ya kuwaongoza watu mbali zaidi kwenye njia isiyofaa. {2T 286.3}

Ikawa watoto wako walidhibitiwa na kanuni za kidini, wangeimarishwa dhidi ya uovu na ufisadi uliowazunguka katika kizazi hiki kilichopotoka. Mungu atakuwa kwao mnara wa nguvu ikiwa watataka kumtumainia yeye. "Hebu na ashike nguvu Zangu, ili afanye amani na Mimi; naye atafanya amani na Mimi. Bwana atakuwa kiongozi wa ujana wao ikiwa watamwamini na kumtumaini. {2Tsw 287.1}

Dada yangu mpendwa, Bwana amekuhurumia sana wewe na familia yako. Umewekwa chini ya wajibu kwa Baba yako wa mbinguni kulisifu na kulitukuza Jina Lake takatifu duniani. Ili kuendelea katika upendo Wake Bwana, unapaswa kufanya kazi kila wakati kwa unyenyekevu, wa nia/akili, upole na roho ile tulivu iliyo ya thamani kubwa machoni pa Mungu. Nguvu zako katika Mungu zitaongezeka huku ukitoa Kwake yote wakfu; ili kwa hilo uweze kusema kwa ujasiri: “Ni nani atakayetutenganisha na upendo wa Kristo? Je, ni shida? Au taabu? Au mateso? Au njaa? Au umaskini? Au hatari? Au Kifo? Hapana. “Kwa maana nina hakika kwamba kifo, wala uzima wala malaika wala enzi au mamlaka, wala vitu vilivyopo, wala mambo yanayokuja, wala urefu, wala kina, au kiumbe kingine chochote, kitaweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio ndani ya Kristo Yesu Bwana wetu.” {2Tsw 288.1}

## **SURA YA 40**

### **VIJANA WANAOJIDANGANYA WENYEWE**

Kaka O; nimeonyeshwa katika maono hatari ya vijana. Kesi yako ililetwa mbele yangu. Niliona kuwa haukupamba taaluma yako.

Unaweza kuwa ulifanya vizuri na mfano wako unaweza kuwa ulikuwa mbaraka kwa vijana ambao mmeshiriki pamoja; lakini jamani! nafsi yako ya ndani haijageuzwa kwa Mungu. Kama ungekuwa na mwenendo wa kudumu kama impasavyo Mkristo, ndugu zako na marafiki zako wangeshawishiwa na mwenendo wako na kufuata hatua zako. Ndugu yangu moyo wako hauko sawa na Mungu; mawazo yako hayajainuliwa kwa Mungu; unaruhusu akili yako kutembea katika mkondo usio sahihi. Maadili yako sio safi, hayana sauti iliyoinuliwa. Tabia zako zimekuwa zinadhuru afya yako ya kimwili na kuleta mauti ya kiroho. Hauwezi kustawi katika mambo ya kiroho mpaka utakapokuwa umeongoka. {2Tsw 288.2}

Unapogundua ushawishi wa nguvu ya Mungu juu ya moyo wako, itaonekana katika maisha yako. Umekosa uzoefu wa kidini, lakini bado haujachelewa sana kumtafuta Mungu kwa bidii na moyo wa kulia na toba sasa; “Je, nifanye nini ili niokolewe?” hauwezi kuwa mkristo wa Kweli mpaka utapokuwa mwongofu wa dhati. Umekuwa na mpenzi katika mambo ya anasa kuliko kuwa na upendo kwa Mungu. umekuwa ukitafta anasa, Je, umewahi kupata furaha ya Kweli katika njia hiyo? Umetafuta kukubalika kwa mabinti wadogo wasio na uzoefu. Umekuwa na mawazo mengi juu yao kiasi kwamba haukuweza kuelekeza akili yako juu kwa Mungu na mbingu. Safisheni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na itakaseni mioyo yenu, ninyi wenye nia mbili.” Agizo/Ushauri huu unakuhusu wewe. Unahitajika ujifunze njia, mapenzi na kazi za Mungu. unahitaji dini safi na isiyo na unajisi; unahitaji kukuza hisia za ibada/uchaji. Acha kufanya maovu, na ujifunze kufanya vizuri. Baraka ya Mungu haziwezi kukaa juu yako mpaka uwe umekuwa kama Kristo. {2Tsw 289.1}

Ninaumia sana ninapooni ukosefu mkubwa wa uchaji wa Mungu kwa vijana. Shetani anachukua akili zao na kuzigeuza kwenye mkondo wa ufiisadi. Udanganyifu wa nafsi upo kwa vijana wengi-kujidanganya wenyewe. Wanafikiri wao ni Wakristo, lakini hawajawahi kuongoka. Hadi kazi hii itakapokuwa imetekelezwa ndani yao, hawataelewa siri hii ya utauwa. Hakuna amani kwa waovu. Mungu anahitaji Ukweli na kuwa dhati moyoni-unyofu wa moyo. Anakuona na kukusikitikia, na vijana wote ambao wanafuata kwa bidii vitu vya kitoto vya kuchezea

(toys-vitu vya dunia au miungu), hao hupoteza muda wa thamani na kupungukiwa kwaajili ya vitu visivyo na thamani. Kristo amekununua kwa gharama ya thamani, na kukuzawadia neema na utukufu kama utavipokea; lakini ulizipa kisogo ahadi za thamani, karama za uzima wa milele, na kujiingiza kwenye mambo duni yasiyotosheleza ya anasa za dunia hii. {2Tsw 289.2}

Kazi yako katika mwelekeo huu haitakuletea faida yoyote. Mshahara wa dhambi ni mauti. Uzima na mbingu vipo mbele yako, lakini umeonekana kutojua thamani yake. Haujatafakari vitu vya thamani vya mbinguni. Kama umegeuka na kuuacha upendo wa Kristo ulio na thamani isiyopimika-usio na kifani, kama mbingu, utukufu na maisha ya milele yamezingatiwa kwa thamani ndogo, ni msukumo gani tunaoweza kuwasilisha ili utupe kusonga mbele na kichocheo kipi kitakachotupa raha? Je, ni michezo ya kipumbavu, na anasa zinazosisimua akili, ndivyo vitatavutia, na kisha vitutenganishe na Mungu, na kuifisha mioyo yetu ili tusimheshimu na kumcha? {2Tsw 289.3}

Oh! Nakusihi wewe ambaye una matamanio madogo sana ya vitu vitakatifu, uchunguze moyo wako mwenyewe kwa ukaribu. Ni ombi gani utafanya mbele ya Mungu kwa maisha yako ya udunia, maisha yasiyowekwa wakfu? Katika siku hiyo ya kutisha hautakuwa na ombi la kufanya. Maneno yatakuishia. Fikiria, oh! Fikiria. Katika masaa yako ya unayotafuta anasa, kwamba haya mambo yote yana mwisho. Kama ungalikuwa na mtazamo sahihi wa maisha, maisha yasiyo na mwisho na Mungu, na vitu vya mbinguni, hakika ungegeuza maisha yako ya starehe, anasa na dhambi, kwa kasi sana. Je, ni kwa kasi kiasi gani, wewe ungebadilisha nia, akili, mwenendo na washirika wako, na kugeuza nguvu za mapenzi yako kuelekea kwa Mungu na vitu vya mbinguni. Je, ungekudharau kwa kudhamiria kiasi gani, kule kuanguka kwako majaribuni, ambako kumekudanganya na kukuvuta utumbukie. Je, ni kiasi gani cha bidii na ari kingetekelezwa kwa juhudi zako kwaajili ya maisha haya yenye mbaraka; Je, utaomba kwa dhati na bidii na uvumilivu kiasi gani kwa Mungu kwaajili ya neema Yake asimame juu yako, ili nguvu Zake zikudumishe na kukusaidia kumshinda Shetani. Je, ungekuwa na uadilifu jinsi gani, katika kuboresha kila fursa ya kidini ya kujifunza njia na mapenzi ya Mungu. Je, Ungekuwa mwangalifu jinsi

gani katika kutafakari sheria ya Mungu, na kulinganisha maisha yako na madai Yake. Je, unachukuaje tahadhari -kwa uangalifu, ili usije ukatenda dhambi kwa neno au tendo, na kuwa na bidii ya kukua katika neema na utakatifu wa kweli. Mazungumzo yako yasingekuwa juu ya vitu vya upuuzi, isipokuwa ya mbingu. Hapo ndipo Utukufu na mambo ya umilele yangewekwa wazi kwako, na usingeweza kupumzika mpaka umejibidisha kukua kiroho zaidi na zaidi. Lakini vitu vya dunia viliteka umakini na Mungu akasahaulika. Nakusihi ugeuze uso wako, na ufikirie vizuri kumtafuta Bwana, ili aweze kupatikana kwako; mwite maadam Yu karibu. {2Tsw 290.1}

## SURA 41

### WONGOFU WA KWELI.

Mpendwa kaka P: Tulipokuwa kule... ....mwaka mmoja uliopita, tulifanya kazi kwa ajili ya maslahi yako. Nilioneshwa hatari yako na tulikuwa katika matamanio ya kukuokoa; lakini tunakuona haukuwa na nguvu ya kutekeleza maazimio yaliyofanywa. Nina wasiwasi juu ya jambo hilo, na hofu kwamba sikuwa mwaminifu kama nilivyokuwa ninapaswa, katika kukuletea mbele yako yote niliyokuwa nikijua kuhusu kesi yako. Vitu vingine nilivihifadhi, sikukwambia. Wakati nilipokuwa Battle Creek mnamo Juni, nilioneshwa tena kuwa haukufanya maboresho ya namna yoyote, na sababu hiyo ilitokana na kutokuwa na njia kamilifu nyuma yako. Haufurahii dini. Ulimwacha Mungu na haki Yake. Umekuwa ukitafula furaha katika njia mbaya, katika anasa zilizokatazwa na hauna ujasiri wa kimaadili wa kukiri na kuacha dhambi zako ili upate rehema.{2T 291.1}

Haukuitazama dhambi kama uovu mbaya na uhalifu mbele za Mungu, na kuiweka mbali; umeshindwa kufanikisha kazi kamilifu; na wakati adui alipokujia na majaribu yake haukumpinga. Laiti ungejua jinsi



dhambi ilivyo chukizo machoni pa Mungu, usingejiingiza majaribuni kirahisi hivyo. Haukuwa umeongoka kweli kweli na kuchukia maisha yako ya dhambi na upumbavu. Dhambi bado ilionekana kupendeza kwako, ulikuwa unatamani matokeo ya raha zake za udanganyifu. Haukuwa na uongofu wa dhati ndani ya moyo wako na hivyo ulipoteza kwa haraka ule uongofu ulioupata. {2T 291.2}

Ubatili wa kibinafsi katika kesi yako, kama vile ilivyo kwa watu wengine, imekuwa kizuizi kikuu kwako. Umekuwa ukipenda kusifiwa. Huu umekuwa mtego kwako. Marafiki zako wanaodai wakristo wameonyesha furaha ya peke katika kushirikiana nawe, na hii imekufurahisha. Akili dhaifu, wanawake wenye kukuhurumia wamekusifu na wameonekana kupendezwa wakiwa nawe kama vile wamevutiwa; na umehisi kuwa ni nguvu ya kuvutia juu yako katika ushirika wao. Haukutambua, wakati ulipokuwa unajifurahisha katika anasa zako ukitaifuta masaa ambayo ni ya familia yako, kwamba Shetani alikuwa akisuka wavu wake ili anase miguu yako. {2T 291.3}

Shetani ameweka majaribu kwa kila hatua maishani mwako. Haukutumia mali zako kwa busara ya kiuchumi kama vile ulivyo paswa kuwa. Unachukia ubahili. Hii ni sawa; lakini unakwenda kinyume kabisa, na njia yako imewekwa kwa alama ya upotevu (mwana mpotevu). Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake somo la kuwalisha watu elfu tano. Alifanya muujiza mkubwa wa kuwalisha umati ule mkubwa kwa mikate mitano na samaki wawili wadogo. Baada ya wote kutosheka, Yeye hakuangalia vipande vya mabaki kwa kuvipuuzia, kama vile vilikuwa chini ya hadhi Yake kuviangalia. Yeye ambaye alikuwa na nguvu ya kufanya muujiza mkubwa sana wenye kutambulika, na kuwapa chakula kundi kubwa, aliwaambia wanafunzi Wake: "Kusanyeni vipande vilivyobaki, kwamba hakuna cha kupotea". Hili ni fundisho kwetu sote, na ambalo hatupaswi kulipuuza. {2T 292.1}

Una kazi kubwa mbele yako, na hauwezi kupoteza tena muda mwingine bila kuushikilia. Ndugu P, ninashtushwa na wewe; lakini ninajua kuwa Mungu anakupenda bado, ingawa njia yako imekuwa ya upotofu. Kama asingekuwa na upendo wa dhati kwako asingenionyesha hatari yako mbele yangu kama alivyofanya. Wewe

umekuwa ukijishugulisha na mizaha na kucheza na wanaume na wanawake ambao hawana hofu ya Mungu mbele yao. Wanawake wenye vichwa dhaifu na wasio na maadili wamekuweka kikapuni mwao, na ulikuwa kama ndege mwenye uliyevutwa na uliyelogwa kwao, ukiwatumbuiza. Ulionekana kuvutiwa na hawa watu hovyoy na wa mambo ya juu juu tu. Malaika wa Bwana walikuwa juu yako wakifuatilia na kuweka kumbukumbu kwa uaminifu kwa kila tendo baya, kila tukio lililoacha njia ya wema. {2T 292.2}

Ndio, kila tendo, liwe la siri ambalo ulifungwa nalo, liko wazi mbele ya Mungu, Kristo na kwa malaika watakatifu. Kitabu kinaandikwa cha matendo yote ya watoto wa wanadamu. Hakuna kipengele cha rekodi hii kinachoweza kufichwa. Kuna tiba moja tunayopewa kama wanadamu wakosefu. Toba ya dhati na ungamo la dhambi, na imani katika damu ya Kristo inayotakasa, italeta msamaha, na msamaha utaandikwa kando ya Jina Lake. {2T 292.3}

Oh ndugu yangu, ikiwa ungefanya kazi kamili mwaka mmoja uliopita, mwaka wa thamani uliopita haukuhitaji kuwa kwako mwaka mbaya kama Sifuri tu. Ulijua mapenzi ya Bwana kwako, lakini haukufanya hayo. Uko katika hali ya hatari. Hisia zako zimekuwa butu katika mambo ya kiroho; una dhamiri iliyokiukwa. ushawishi wako haukusanyi bali hutawanya. Hauna hamu ya mazoezi ya kiroho-kidini, wewe sio mtu mwenye furaha. Mke wako angeunganisha mapenzi yake na watu wa Mungu ikiwa utatoka katika njia yake. Anahitaji msaada wako. Je, mnaweza kushika kazi hii na kuifanya pamoja? {2T 293.1}

Mwezi wa Juni uliyopita niliona kuwa tumaini lako pekee la kuvunja kongwa la utumwa wako, ulikuwa kutoka kwa wale ulioshirikiana nao. Ulikuwa umejitolea kwa majaribu ya Shetani hadi umekuwa mtu dhaifu. Ulikuwa mpenzi wa anasa zaidi kuliko kumpenda Mungu, na ulikuwa ukiporomoka kuelekea chini kwa haraka sana. Nimekatishwa tamaa kuona umedumaa na kuendelea katika njia hiyo ya kutojali ambayo umekuwa kwa miaka mingi. Umejua na kupata uzoefu wa upendo wa Mungu; na imekuwa furaha yako kufanya mapenzi Yake. Umekuwa ukifurahia usomaji wa Neno la Mungu. Umekuwa makini kuhudhuria kwa muda wake mikutano ya maombi. Ushuhuda wako umekuwa

ukitoka katika moyo ulioguswa na ushawishi wa upendo wa Kristo. Lakini umepoteza upendo wako wa kwanza. {2T 293.2}

Mungu sasa anakuita wewe ili utubu, kuwa na usongo/ari katika kazi. Hatima ya furaha yako ya milele itabainishwa na njia unayoiendea sasa. Je, unaweza kukataa mwaliko wa neema inayopatika sasa? Je, unaweza kuchagua njia zako mwenyewe? Je, unaweza kufurahia kiburi na ubatili, na mwishowe kupoteza roho yako? Neno la Mungu linatuambia wazi kuwa ni wachache watakaokolewa, na kwamba idadi kubwa ya hata wale walioitwa itathibitishwa kuwa haistahili uzima wa milele. Hawatakuwa na sehemu mbinguni, lakini watapata sehemu yao na Shetani, na kupata mauti ya pili. {2T 293.3}

Wanaume na wanawake wanaweza kutoroka huzuni, ole na hukumu hii ya kutisha ikiwa wataamua. Ni kweli kuwa Shetani ndiye mwanzilishi mkuu wa dhambi; lakini hii haimpi mtu udhuru wa kutenda dhambi; kwani Sherani hawezi kulazimisha watu wafanye maovu. Adui huwajaribu tu wafanye dhambi, na kufanya dhambi ionekane kuwa ya kuvutia na kupendeza; lakini anaiacha kwa maamuzi yao ikiwa wataifanya au la. Hawalazimishi watu kulewa, wala hawalazimishi kukaa mbali na mkutano wa dini; lakini yeye huwasilisha majaribu kwa njia ya kushawishi mtu afanye uovu, na mtu ana utashi na uhuru wa maadaili, kukubali au kukataa. {2T 294.1}

Wongofu ni kazi ambayo wengi hawaithamini. Sio jambo rahisi kubadilisha akili za mpenda dhambi au ulimwengu, na kuzileta zielewe upendo wa Kristo usioneneka, tunu za neema Yake, na utukufu wa Mungu, ili roho iwe imejaa upendo wa Mungu na kuvutiwa na siri za ajabu za mbingu. Anapoelewa mambo haya, maisha yake ya zamani yanaonekana kuwa ya kuchukiza na ya kukimbiwa. Anachukia dhambi na kulainisha moyo wake kwa Mungu na kumpokea Kristo katika maisha yake na furaha ya roho wake. Anaacha anasa zake za zamani. Anakuwa na akili mpya na mapenzi mapya, shauku mpya, nia mpya; huzuni zake na tamaa, na upendo, vyote hivi huwa vipya. Tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima, ambavyo hapo awali kabla ya Kristo vilipendwa, sasa vinaachwa, na Kristo ni sumaku ya maisha yake, na taji ya furaha yake. Mbingu, ambayo hapo awali mtu hak, na

uona inavutia, sasa inatazamwa katika utajiri wa utukufu Wake; na anaifikiria kama makazi yake ya baadaye, ambapo ataona, atapenda na kumsifu Yule aliyemkomboa kwa damu Yake ya thamani. {2T 294.2}

Matendo ya utakatifu, ambayo yalioneka ya kuchosha, sasa anayafurahia. Neno la Mungu, ambalo lilikuwa duni, butu na lisilovutia, sasa ni chaguo la masomo yake, mshauri wake. Ni barua iliyoandikiwa kwake kutoka kwa Mungu, iliyo na Maandishi ya Yule wa Milele. Mawazo yake, maneno yake na matendo yake yanapimwa katika sheria hii na kujaribiwa. Anatetemeka kwa amri na vitisho vilivyomo ndani yake, wakati anashikilia ahadi Zake na kuimarisha roho yake kwa kula hizi ahadi mwenyewe. Jamii ya wacha Mungu zaidi sasa inachaguliwa Naye, na waovu, ambao kundi lao alilipenda, sasa hafurahishwi nao tena. Anatoa machozi kwa dhambi ambazo zamani alizichekea. Kujipenda mwenyewe na ubatili vinaachwa, na anaishi kwa Mungu, na ni tajiri wa matendo mema. Huu ni utakaso ambao Mungu anahuitaji. Hakuna pungufu ya hili Atakalokubali Yeye. {2Tsw 294.3}

Ninakusihi ndugu yangu, uuchunguze moyo wako kwa bidii na kujiuliza: “Ninasafiri katika barabara ipi, na ni wapi itakapoishia?” unayo sababu ya kufurahi kwamba maisha yako hakukatiliwa mbali wakati ulikuwa hauna tumaini lenye uhakika la uzima wa milele. Mungu akusaidie ili kwamba usipuuzie kazi hii na uangamie katika dhambi zako. Usiidanganye roho yako kwa matumaini ya uwongo. Huoni njia ya kushika tena mambo ya kiroho, lakini uwe mnyenyekevu na kukubali kwamba huwezi, na kupokea msaada. Kristo anawasilisha kwako, hata kwako wewe ndugu yangu mkosaji, ujumbe wa rehema: “Njoo; kwa maana vitu vyote viko tayari sasa.” Mungu Yuko tayari kukukubali na kukusamehe makosa yako yote, ikiwa utakuja tu. Ingawa umekuwa mwana mpotevu na umejitenga na Mungu na kukaa mbali Naye kwa muda mrefu, Yeye atakutana nawe hata sasa. Ndio; Mkuu wa mbinguni unakualika kuja Kwake, ili upate uzima. Kristo Yupo tayari kukusafisha kutoka kwa dhambi kama utamshikilia- utamwamini. Je, umepata faida gani katika kuitumikia dhambi? Kuna faida gani ya kutumikia dhambi na kumtumikia Shetani? Je, sio mshahara duni unaopokea? Ah! Geukeni, geukeni; kwa nini uje ufe? {2Tsw 295.1}

Umepata usadikisho mwingi, maumivu mengi ya dhamiri. Umekuwa na malengo mengi na kuweka ahadi nyingi, na bado unakawia na hautaki kuja kwa Kristo ili upate uzima. Loo, laiti moyo wako ungeweza kuvutiwa na hisia za wakati tunaoishi, ili ugeuke na kuishi! Je, hauwezi kusikia sauti ya mchungaji mwema na wa Kweli katika ujumbe huu? Unawezaje kuacha kutii-kukaidi? Usimchezee Mungu, asije akaondoka na akuache katika njia zako zilizopotoka. Ni uzima au mauti vilivyo mbele yako, utachagua kipi? Ni jambo la kutisha kushindana na Mungu na kukataa kusikia sauti Yake ya upendo unaokusii. Unaweza kuwa na upendo wa Mungu unaowaka juu ya madhabau ya moyo wako kama ulivyohisi wakati huo. Unaweza kuzungumza na Mungu kama ulivyofanya nyakati zilizopita. Ikiwa utaacha matendo safi nyuma yako unaweza tena kupata utajiri wa neema Yake na uso wako kudhihirisha tena upendo Wake. {2Tsw 296.1}

Haupaswi kuungama kwa watu ambao hawajui dhambi zako na makosa yako. Sio wajibu wako kutangaza ungamo lako, kitu ambacho kitapelekea wasioamini kushangilia; bali kwa wale ambao ni sahihi, ambao hawatachukua makosa yako kuwa faida, ungama sawa sawa na Neno la Mungu, na waache wakuombe, na Mungu atakubali kazi yako, Naye atakuponya. Kwa ajili ya nafsi yako, kwa ajili ya faida ya nafsi yako, fanya kazi kamili kwaajili ya umilele. Weka kando kiburi chako, ubatili wako na ufanye kazi iliyonyoka. Rudi tena zizini. Mchungaji anasubiri kukupokea. Tubu na fanya sehemu yako kwanza, kisha uje tena katika uhusiano na Mungu. {2Tsw 296.2}

## **SURA YA 42**

### **WAJIBU WA MUME NA MKE**

Ndugu R, mwezi Juni uliopita swala lako lililetwa mbele yangu katika njozi. Lakini nimedumu katika shinikizo a kazi kiasi kwamba nilishindwa kuandika vitu nilivyoonyeshwa katika kesi za kila mtu. Nilitamami niandike kile nilichopaswa kuandika, kabla sijasikia jambo lolote kuhusu wewe; kwa kuwa Shetani angeweza kupendekeza shaka katika akili yako. Hii ndiyo kazi yake. {2T 296.3}

Nilioneshwa maisha yako ya nyuma na nilioneshwa kuwa Mungu amekuwa mwema na mwenye rehema sana kwako katika kukuangazia macho yako kuona Ukweli Wake, katika kukuokoa kutoka katika hali yako ya hatari ya mashaka, kutoamini na kutokuwa na uhakika na katika kusimika imani yako na kuweka akili yako juu ya Ukweli wa milele wa Neno Lake. Yeye Alisimamisha miguu yako juu ya mwamba. Kwa sababu kipindi fulani, wewe ulijawa shukrani na unyenyekevu, lakini kwa wakati mwingine umekuwa ukijitenga mwenyewe kutoka kwa Mungu. Ulipokuwa mdogo katika upeo wa macho yako, ndipo ulipokuwa kipenzi cha Mungu. {2T 297.1}

Muziki umekuwa mtego kwako. Unasumbuliwa na kujitathmini nafsi yako kwa uhalisia-self esteem; ni kawaida kwako kuwa na mawazo yaliyoinuliwa kuhusiana na uwezo wako. Kufundisha muziki kumekuwa jeraha kwako. Wanawake wengi wamekufunulia siri ya changamoto za familia zao kwako. Hii nayo imekuwa jeraha kwako. Imekufanya uote pembe na kuitukuza nafsi sana-high self esteem-unajipima nafsi yako kwamba u mtu wa juu sana. {2T 297.2}

Katika familia yako mwenyewe umeshika nafasi ya heshima na yenye majivuno. Kuna kasoro kwa mkeo, ambazo unazifahamu. Mambo haya Yamesababisha matokeo mabaya. Kwa kawaida yeye si mtunzaji mzuri wa nyumba. Inabidi apate elimu juu ya mambo haya. Amefanya maboresho katika baadhi ya mambo, na anapaswa kujitahidi sana kufanya maboresho makubwa. Hana utaratibu, ladha na unadhifu katika utunzaji wa nyumba na pia katika mavazi. Itakuwa inampendeza Mungu ikiwa angeelimisha akili yake juu ya vitu hivi ambavyo amepungukiwa. Hana serikali nzuri katika familia yake. Anakubaliana na vitu kupita kiasi, na anashindwa kudumisha maamuzi yake. Yeye ndiye anavutwa na shauku na madai ya watoto wake, na kuchukua

maamuzi yao badala ya wao kuchukua yake. Badala ya kujaribu kufanya maboresho katika mambo hayo, ambalo ni jukumu lake kuyafanya, anafurahia kupata nafasi ili kutoa udhuru na yeye mwenyewe kujiondoa katika shuguli za nyumbani na majukumu, na kuwaruhusu watu wengine kutekeleza majukumu katika familia yake ambayo anapaswa ajifunze kuyapenda, kufanya. Hawezi kufanya wajibu/sehemu yake kama mke na mama mpaka ajifunze katika mwelekeo huu. Anakosa kujiamini yeye mwenyewe. Yeye ni mwoga na hapendi kuonekana, na hajiamini. Ana mawazo dhaifu sana kwa kile anachokifanya, na hii inamkatisha tamaa kufanya zaidi. Anahitaji kutiwa moyo; anahitaji maneno ya kujali, upendo mwanana, huruma nyororo na mapenzi. Ana roho nzuri. Ni mpole, mnyenyekevu na mtulivu, Bwana anampenda; lakini anapaswa kuwa na juhudi ya dhati kusahihisha makosa yake ambayo yanafanya familia yake isiwe na furaha. Kufanya mazoezi katika haya itamfanya awe na ujasiri katika uwezo wake wa kufanya wajibu wake vizuri. {2T 297.3}

Wewe na mke wako mnatofautina katika mipangilio yenu. Wewe unapenda utaratibu na unadhifu, na una ladha na serikali/uongozi mzuri kabisa. Kama mume umekauka, haunyumbuliki na ni mkali. Ulishindwa kuchukua hatua kuhimiza ujasiri na kumfanya mke wako akuzoe. Upungufu wake umesababisha umchukulie kama duni kwako, na pia umemfanya ahisi kuwa unamchukulia yeye hivyo. Mungu anamthamini zaidi sana yeye kuliko wewe; kwa maana njia zako zimepotoka mbele Zake. Kwa ajili ya mumewe na watoto, na kwa sababu zingine, anapaswa kutafuta kurekebisha upungufu wake na kufanya maboresho katika mambo hayo ambayo sasa anashindwa. Anaweza kufanya ikiwa atajaribu kwa bidii ya kutosha. {2T 298.1}

Mungu hafurahii mambo yaliyovurugika, yasiyo na mpango, ya uzembe, ya uvivu, na ukosefu wa ukamilifu, kwa mtu yeyote. Mapungufu haya ni maovu makubwa na huwa yanadhoofisha mapenzi ya mume kwa mkewe wakati mume anapenda utaratibu, watoto wenye nidhamu nzuri, na nyumba inayoratibiwa vizuri. Mke na mama hawawezi kufanya nyumbani kuwa ya furaha na amani mpaka awe mtu anayependa utaratibu, anayelinda hadhi yake, na ana serikali nzuri; hivyo wote wanaoshindwa katika haya wanapaswa kuanza mara moja kujifunza

wenyewe katika mwelekeo huu na kukuza haya ambayo kwayo wanapungua sana. Nidhamu itafanya makubwa kwa wale ambao wanaokosa sifa hizi muhimu. Dada R anahusika kwenye kasoro hizi, na anafikiria kuwa hawezi kufanya zaidi kuliko anavyofanya. Baada ya yeye kujaribu na kushindwa kuona mabadiliko yanayoonekana kwake mwenyewe, anakatishwa tamaa. Hii haipaswi kuwa hivi. Furaha yake yeye mwenyewe na familia yake hutegemea na kujizindua kwake mwenyewe, na kufanya kazi kwa kuazimia kwa bidii na ari kufanya matengenezo katika haya. Ni lazima awe na ujasiri na maamuzi; avae ujasiri wa kike. Asili yake ni kuepuka vile ambavyo hajavijaribisha bado. Hakuna mtu yeyote anayepaswa kuwa na utayari na kupenda kutenda hili kuliko yeye, ambapo anaweza kufikiri anaweza kufaulu. Ikiwa atashindwa katika juhudi zake mpya, anapaswa kujaribu, na kujaribu tena. Anaweza kupata heshima kutoka kwa mumewe na watoto. {2T 298.2}

Nilioneshwa kuwa kujitukuza kwako mwenyewe kumesababisha ndugu R kujikwaa. Ametumia hadhi fulani, yenye ladha ya ukali katika familia yake na kwa mke wake. Hii imemfanya mke wake ajikunje na amemfungia mke wake nje kwa jinsi hii. Alihisi kuwa asingeweza kumwendea, na imekuwa hivyo katika maisha yake ya ndoa, kama vile mtoto anayeogopa ukali wa baba mwenye hadhi ya juu na kumbe huyu ni mkewe. Mke anampenda, anamheshimu na kumwona mume wake ni wa wadhifa wa juu sana licha ya mume kukosa kumtia moyo ajiadini. Ndugu yangu, inakupasa uchukue hatua zitakazomtia moyo mke wako mwoga, anayejikunja kugemea mapenzi yako, na hii itakupa nafasi kwa njia ambayo ni nyeti na ya mapenzi kusahihisha dosari zinazojitokeza kwake, kwa jinsi unavyoweza kufanya hivyo, na kumtia moyo aweze kujiamini mwenyewe. {2T 299.1}

Nilioneshwa kwamba hauna ule upendo kwa mke wako ambao unapaswa kuwa nao. Shetani ametumia kwa faida kasoro zake na makosa yako, kuharibu familia yako. Unaona aibu mke wako kuingia moyoni mwako, na heshima yako imepungua chini na chini kwake yeye ambaye ulichukua kiapo cha nadhiri kumpenda na kumtunza mpaka kifo kitakapowatenganisha. {2T 299.2}



## Hatari Ya Kueleza Siri Ya Familia

Tarehe 25, Octoba ya 1868, kesi yako iliwasilishwa tena mbele yangu. Nilioneshwa mawazo hayo mabaya na matakwa haramu yamesababisha matendo yasiyofaa na ukiukaji wa amri za Mungu. Umejishushia heshima wewe mwenyewe, mke wako na kusudi la Mungu. Ungeweza kuwa na ushawisi mzuri kwa kazi ya Mungu. Lakini ulifuata mwenendo usiofaa katika maswala ambayo ulidhani kuwa matokeo yake ni madogo ila yamesababisha maovu makubwa. {2T 300.1}

Ndugu R, sasa upo kwenye hatari ya kuvunjikiwa imani yako kabisa. Umetenda dhambi sana. Lakini unatafuta kufunika makosa yako, na kupofusha macho ya wale ambao wanakushuku kwa mabaya uliyotenda, basi hiyo imekuwa mbaya sana mara kumi. Wote hawakutenda kwa busara na kwa upendo na umakini mwingi kama Bwana angefurahiswa iweze kuwa, ili kukunusuru-kukuokoa. Lakini ulipojaribu kujifanya kuwa u mkosefu asiye na hatia, Je, ulidhani kuwa Mungu asingeweza kuona mwenendo wako mpotovu? Je, ulidhani kuwa Yeye aliyemuumba mwanadamu kutoka mavumbi ya ardhi, na kumpulizia pumzi ya uhai katika mianzi miwili ya pua, asingejua kusudi na nia ya moyo? Ulidhani kuwa ukiungama dhambi yako ungepoteza heshima, na hadhi yako .... Maisha yako, kama ulivyodhani. Ulidhani kuwa ndugu zako wasingekuwa na imani na wewe. Haukulitazama jambo katika nuru sahihi. Ni aibu kutenda dhambi, lakini siku zote ni heshima kuungama dhambi. {2T 300.2}

Malaika wa Mungu wameweka kumbukumbu sahihi kwa kila tendo, hata kama unadhani ulilitenda kwa siri ya kiasi gani. Mungu anaangalia kusudi la mwanadamu na matendo yake yote. Kila mtu atapewa ujira wake kulingana na jumla ya matendo yake, yawe mema au mabaya. Kile apandacho mtu ndicho atakacho kivuna. Hakutakuwa na pando litakaloshindwa kuleta matunda. Mavuno ni ya uhakika na mengi. Umejaribu kuwaficha ndugu zako mwenendo wako. Uliwezaje kufanya hivyo, wakati ulijua kuwa una hatia mbele ya Mungu? Kama unathamini wokovu wa nafsi yako. Ufanye kazi ya dhati kwaajili uzima wa milele. {2T 300.3}

Utapaswa kusafisha njia yako nyuma yako kwa toba ya dhati. Unahitaji uongofu wa kweli.....badiliko la nafsi kwa kufanywa upya nia yako. Lazima ushinde kuithamini nafsi yako kuliko unavyopaswa kufanya (high self-esteem). Lazima ujifunze kuwathamini wengine kuwa bora zaidi kuliko wewe. Maoni yako yaliyoinuliwa kuhusiana na sifa zako lazima yadondoshwe chini, na lazima uwe mpole, mnyenyekevu na mwenye roho ya kutulia, ambayo mbele za Mungu ni vyenye thamani kuu. {2T 301.1}

Unamiliki roho ambayo imekuongoza kutoka kwenye njia ya haki-unyofu, na sasa unataabika. Mashaka, hofu na kukata tamaa vimekuingia. Una njia moja tu ya kutoka hapo, nayo ni njia ya kukiri na toba. Tumaini lako pekee ni kuanguka juu ya mwamba na kuvunjika vipande vipande; usipofanya hivyo, hakika mwamba utakuanguka na kukusaga-saga kuwa unga. Sasa unaweza kurekebisha makosa yako; sasa unaweza kukomboa yaliyopita. Kwa maisha ya wema na unyenyekevu. wa kweli bado unaweza kutembea na kukubalika mbele za Mungu katika familia yako. Ni ombi langu kuwa Bwana atakusaidia, ukiwa na mtazamo wa hukumu inayokuja, kufanya kazi kwa kuthamini kama maisha yako. Ndugu mpendwa, ninakiri kupendezwa na wewe sana, umekuwa ukitembea gizani kwa muda. Haujafika kwenye hali yako ya sasa ya giza mara moja. Umekuwa ukiacha nuru pole pole. Kwanza uliinuliwa, halafu ukahisi kujitosheleza kwa nguvu zako mwenyewe, kisha Bwana aliondoa nguvu Zake kwako. {2T 301.2}

Umekuwa na shauku ya muziki. Hili limewapa wanawake wasio na tahadhari na busara safi fursa ya wao kukuambia mambo ya siri yanayowatatiza. Hii imekuza kiburi chako, lakini limekuwa mtego kwako. Limefungua milango ya mapendekozo ya Shetani kwako. Haujafanya ilivyostahili. Hauna shuguli au haki ya kusikiliza changamoto za hizo familia. Mawasiliano haya yameharibu akili yako, yameongeza kujiona wewe ni bora na wa thamani zaidi, na kusababisha mawazo mabaya. Umejiruhusu mwenyewe kuwa kuhani anayesikia vitubio vya wanawake wanaoongozwa na hisia zisizo sawa, ambao walihitaji huruma na kupenda waegemee kwako. Endapo walikuwa na maamuzi mazuri na kusimama wakijitegemea wenyewe,

wakiwa na lengo katika maisha, wakupenda kuwatendea wengine mema, wasingeweza kuwa katika mazingiira ambayo walihitaji kwenda kwa mtu yeyote kwa huruma. {2T 301.3}

Haujajua bado udanganyifu wa moyo wa mwanadamu. Haujajua bado zana za Shetani. Baadhi ya watu waliokuwa wakipokea kwa wingi huruma zako ni wahanga, wana maradhi ya mafikara, ni wagonjwa wa mapenzi (lovesick), hisia zao zina mawazo ya kufikirika kuhusu udanganyifu wa mapenzi, daima wanahisi kusukumwa na hisia na kisha wanafurukuta kwa vitu ambavyo si muhimu. Wengine hawaridhishwi na maisha yao ya ndoa. Kwamba hayana mahaba ya kutosha. Usomaji wa riwaya umepotosha hisia zao nzuri walizowahi kuwa nazo. Wanaishi katika ulimwengu wa kufikirika. Katika mawazo yao wanakuwa na aina ya waume wanaowataka, wenye mahaba wanaofanana na wale waliosoma habari zao katika riwaya. Wanazungumzia juu ya mapenzi yao yasiyopokelewa na kurudishwa ipasavyo. Hawaridhiki kamwe au kufurahi. Kwa sababu wana picha mawazoni za maisha ambayo si halisi. Wanapokabiliana na uhalisia, na washuke chini kwa unyenyekevu kwenye maisha halisi na kuchukua mizigo ya maisha yao katika familia zao, kama ilivyo nafasi ya mwanamke, ndipo watapata kuridhika na kufurahi. {2T 302.1}

Umeendekeza mawazo ambayo hayakuwa sahihi/sawa. Mawazo haya yamezaa matunda. “Katika wingi uliojaza moyo kinywa hunena.” maneno yako siyo safi kila wakati, yaliyotakaswa na kuinuliwa. Hila imeonekana kwenye midomo yako mara kwa mara..... mazungumzo ya chini yanayotoka kwenye moyo unaohusudu mawazo ya ufisadi, tamaa mbaya na uovu. {2T 302.2}

Kwa muda sasa miguu yako imegeuzwa kutoka katika njia ya haki na usafi. Unajua kwamba njia zako hazikumpendeza Mungu, kwamba unazikiuka sheria Zake takatifu; Unajua kwamba mambo haya hayawezi kufichwa. Mungu hatoruhusu watu Wake wadanganywe katika kesi yako. Dhambi yako kubwa ni kutafuta huruma za watu ambao hawajui njia zako zilizopinda. Na kwa kufanya hivyo unatenga maamuzi ya wale wanaokiri Ukweli. Tunakusikitikia. Moyo wangu unaugua kwa ajili yako. Sioni kitu chochote mbele yako isipokuwa

upotevu, sioni chochote mbele yako isipokuwa uasi, hakuna lolote isipokuwa kuvunjikiwa kwa imani kabisa. {2T 302.3}

Je, utaficha dhambi zako na kuwa jasiri na kifua mbele tu? Mungu anasema hautafanikiwa. Lakini mtu aungamaye na kuiacha dhambi yake atapata rehema. Je, utachagua mauti? Je utajifungia mlango wa mbinguni mwenyewe kwa sababu hautaki kusalimisha uovu wa kiburi chako? Tumaini lako pekee ni katika kukiri kurudi kwako nyuma. Mungu ameruhusu nuru Yake ikuangazie, katika njia yako. Je, utaichagua njia yako ya ufisadi? Je, utautupa Ukweli nyuma yako kwa sababu hautasapoti/hautaendana na njia yako ya uovu? Loh! omba kwa bidii “rarua moyo wako, na wala sio mavazi yako, ukamrudie Bwana, Mungu wako.” Fanya kazi kamilifu kwa ajili ya umilele. Mungu atakuhurumia. Yeye Atakutendea na kukutafuta kwa dhati kwa niaba yako. Yeye Hatodharau roho iliyovunjika na kupondeka. Je, utageuka? Je, unataka kuishi? Ishi! Nafsi yako inastahili kuokolewa; ni ya thamani. Tunapenda kukusaidia. {2Tsw 303.1}

Niliona kuwa hauna furaha. Roho yako haijatulia. Unajisikia kufadhaika, na na bado unakataa kuchukua njia pekee ambayo itakuletea unafuu na matumaini. Yeye anayeungama na kuziacha dhambi zake atapata rehema. Hali yako ni ya kusikitisha, na unajeruhi sana kazi ya Mungu. Ushawishi wako utawaharibu wengine walio karibu, pamoja na wewe mwenyewe. {2Tsw 303.2}

Kama utakataa kumrudia Mungu na kuungama kurudi kwako nyuma ili aweze kukuponya, hakuna kitu cha kutumainiwa kwako au familia yako masikini ya wakati ujao. Taabu itafuata njia ya mdhambi. Mkono wa Mungu utakuwa kinyume chako. Naye atakuacha utawaliwe na Shetani, kupelekwa kuwa mtumwa wake kwa mapenzi yake. Haujui bado utakwenda mbali kiasi gani. Utakuwa kama mtu aliye baharini na chombo kisicho na nanga. Ukweli wa Mungu ndiyo nanga. Unakwenda mbali sana na nanga. Mapenzi yako ya mambo ya milele yametolewa kafara kwa tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha maisha yako. Upo katika hatua ya kuvunja kifungo kitakachokuokoa na uharibifu mkubwa. Katika kutafuta kuokoa maisha yako kwa kuficha mabaya yako, unajipatia hasara. Ikiwa sasa utanyenyekesha mbele za Mungu, na kuungama makosa yako, na kumrudia kwa nia ya moyo

wako wote, unaweza kuwa bado kuwa na familia yenye furaha. Kama hautafanya hivi, lakini ukaishia kuchagua njia yako mwenyewe, furaha yako ipo ukingoni. {2T 303.3}

Una kazi kubwa ya kufanya. Umekuwa mzembe sana katika mwenendo wako. Maneno yako hayakuwa yameinuliwa, yamekuwa yasiyo na kiasi na usafi. Umekuwa ukijitenga kutoka kwa Mungu, na kukuza tamaa za chini kimaadili. Vitivo vyako vya akili na bora vya nia yako vimesukumwa kwenye mapenzi ya kinyama. Haukuwa na njia sahihi kwa muda mrefu. Haujajitenga na kila mwonekano wa uovu. Sio salama kwako kuendelea na njia hii zaidi. {2T 304.1}

Haukumpenda mke wako kama ulivyopaswa. Yeye ni mwanamke mwema. Ameona kwa kiwango kidogo hatari yako. Lakini wewe umeziba masikio yako kusikiliza tahadhari zake. Umefikiria ni wivu wake tu, lakini hii siyo asili yake. Mkeo anakupenda, na atachukuliana na wewe, na atakusamehe na kukupenda, licha ya kina cha urefu wa makosa uliyomtendea, ikiwa utasogea kwenye nuru na kusahihisha makosa ya matendo yako ya nyuma kuwa safi. Unapaswa kuwa na uongofu kamili. Isipokuwa umefanya hivyo, juhudi zako zote za zamani za kutii Ukweli hazitakuokoa wala kufunika makosa yako ya zamani. Yesu anahitaji kutoka kwako matengenezo ya dhati; ndipo atakusaidia na kukubariki, na kukupenda, na kufuta dhambi zako kwa damu Yake Mwenyewe ya thamani sana. Unaweza kukomboa yaliyokwisha kupita. Unaweza kusahihisha njia zao na bado ukawa na heshima kwa kazi ya Mungu. Unaweza kutenda mema kwa kutumainia nguvu za Mungu na kwa Jina Lake—fanyia kazi wokovu wako mwenyewe na kwa faida ya wengine. {2T 304.2}

Bado unaweza kuwa na familia yenye furaha. Mke wako anahitaji msaada wako. Yeye ni kama vishikio vya mzabibu vinavyong'ang'ania kwenye shina la mzabibu; anataka kuegemea nguvu zako. Unaweza kumsaidia na kumwongoza. Haupaswi kamwe kumlaumu. Kamwe usimkeme kama jitihada zake haziendani kama ulivyokusudia kuwa. Ni bora umtie moyo kwa maneno yenye huruma na upendo. Unaweza kumsaidia mke wako kwa kulinda hadhi yake na kujiheshimu mwenyewe. Kamwe usisifu kazi au matendo ya watu wengine mbele

yake na kumfanya ahisi mapungufu yake. Umekuwa mkali na asiye na hisia za kujali katika swala hili. Umeonyesha heshima kubwa na uungwana kwa vibarua wako kuliko mke wako na umewathamini sana zaidi yake ndani ya nyumba. {2T 305.1}

Mungu anampenda mke wako. Ameteseka. Lakini Mungu ameona yote, ameyawekea alama yote, na hatakuacha bila kukuhesabia hatia kwa maumivu uliyomsababishia. Sio utajiri wala akili inayoleta furaha. Ni uthamani wa maadili. Wema wa Kweli unathaminiwa mbinguni kama ukuu wa kweli. Hali ya mapenzi ya maadili huamua thamani ya mtu. Mtu anaweza kuwa na mali na akili, na bado akawa hana thamani, kwa sababu moto unaowaka wa wema haujawahi kuwaka juu ya madhabahu ya moyo wake, kwa sababu dhamiri yake imechomwa moto, imetiwa giza, na kutokoswa kwenye ubinafsi na dhambi. Wakati tamaa ya mwili inapomtawala mtu, na tamaa ya dhambi ya matendo ya mwili wa asili ya mwanadamu inapochukua nafasi na kutawala, udhanifu, na kutilia shaka kuhusiana uhalisia wa dini ya Kikristo unahimizwa, na mashaka yanazunguzwa kama vile ni fadhila kubwa kuwa na mashaka. {2T 305.2}

Maisha ya Sulemani yangeweza kuwa ya kukumbukwa na ya ajabu hadi mwisho wake ikiwa wema ulihifadhiwa. Lakini aliisalimisha neema hii maalum kwa shauku ya tamaa mbaya za mwili. Katika ujana wake alimtafuta Mungu ili kuongozwa Naye, na alimwamini, na Mungu alimchagulia na akampa hekima iliyoshangaza ulimwengu. Nguvu zake na hekima ilitukuzwa katika nchi yote. Lakini upendo wake kwa wanawake ndiyo ilikuwa dhambi yake. Tamaa hii hakuidhibiti katika utu uzima wake, na ilithibitika kuwa mtego kwake. Wake zake walimpeleka kwenye ibada ya sanamu, na alipoanza kushuka chini katika maisha, hekima ambayo Mungu alikuwa amempa iliondolewa; alipoteza uthabiti wake wa tabia na kuwa kama vijana wahuni wasio na akili njema, akiyumba-yumba kati ya wema na uovu. Akisalimisha kanuni za Bwana, alijiweka mwenyewe katika mkondo wa uovu na hatimaye akajitenga mbali na Mungu, aliye msingi na chanzo cha nguvu zake. Alitoka katika kanuni. Hekima kwake ilikuwa ya thamani machoni pake kuliko dhahabu ya ofiri. Lakini, ole! Shauku ya tamaa ilichukua ushindi dhidi yake. Alidanganywa, akaharibiwa na kurubuniwa na wanawake. Ni

somo la pekee kiasi gani, kuhusu ushahidi wa kuweka umakini na kukesha! Ni ushuhuda ya namna gani kutufanya tuhitaji nguvu kutoka kwa Mungu mpaka mwisho. {2T 305.3}

Katika kupambana na ufigadi wa ndani na majaribu ya nje, hata Sulemani mwenye hekima na mwenye uwezo alishindwa. Sio salama kuruhusu kutoka nje hata kidogo uadilifu mkamilifu. “Jiepushe na hali yoyote yenye mwonekano wa uovu.” Wakati mwanamke anapokuelezea shida ya familia yake, au analalamika juu ya mumewe, kwa mwanamume mwingine, anakiuka kiapo chake cha ndoa; anamvunjia mume wake heshima na anavunja ukuta uliowekwa kutunza heshima na utakatifu wa mahusiano ya ndoa; anafungua mlango wazi kabisa, ili kumwalika Shetani kuleta majaribu yake yenye sumu kali. Hivi ndivyo Shetani angetaka iwe. Kama mwanamke atakuja kwa ndugu Mkristo na mlolongo wa hadithi za ole yake, kukatishwa kwake tamaa na majaribu, daima ungepaswa kumshauri, kama ni lazima kumwambia mtu siri na shida yake, basi amchague mwanamke mwenye kuaminika na hapo hakutakuwa na mwonekano wa uovu, mahali ambapo kazi ya Mungu inaweza kuaibishwa. {2T 306.1}

Mkumbuke Sulemani, katika mataifa mengi hakukuwa na mfalme kama yeye, kipenzi cha Mungu wake. Lakini alianguka. Aliongozwa kutoka kwa Mungu na kuwa mwovu kupitia kuendekeza tamaa za mwili. Hii ndio dhambi inayovuma katika kizazi hiki, na mwendelezo wake unatia hofu. Watu wanaodai kuwa ni watunza Sabato sio wasafi. Kuna wale wanaodai kuwa wanaamini Ukweli ambao ni waovu katika mioyo yao. Mungu atawathibitisha, na upumbavu wao na dhambi yao itaanikwa wazi. Hakuna atakayesimama katika uwepo Wake isipokuwa wale walio safi na wapole. “Ni nani atakayesimama katika mlima wa Bwana? Au ni nani atakayesimama katika Patakatifu Pake? Yule ambaye mikono yake ni misafi na mwenye moyo safi; ambaye hajainua nafsi yake kwa ubatili, wala hajashindwa na udanganyifu.” “Bwana, ni nani atakaye kaa katika hema lako? Nani atakayeishi juu ya mlima wako mtakatifu? Ni mtu aishiye bila lawama, atendaye daima yaliyo mema, asemaye Ukweli kutoka moyoni; ni mtu asiyesengenya watu, asiyemtendea uovu rafiki yake, wala kumfitini jirani yake; ni mtu anayewadharau wafisadi, lakini huwaheshimu wamchao Mwenyezi-

Mungu; ni mtu asiyegeuza kiapo chake hata kikimtia hasara; asiyeopesha fedha yake kwa riba, wala kupokea rushwa kumdhulumu mtu asiye na hatia. Mtu atendaye hayo, kamwe hatatikisika..” {2T 306.2}

## **SURA YA 43**

### **BARUA KWA KIJANA YATIMA**

Rafiki mpendwa: katika maono ya mwisho niliyopewa, niliona kuwa ulikuwa na makosa ya kurekebisha. Ni muhimu kwako kuangalia haya kabla ya kufanya jitihada zinazohitajika ili kuyasahihisha. Una mengi ya kujifunza kabla haujachukua hatua ya kutengeneza tabia nzuri, ya Kikristo ambayo Mungu anaweza kuithibithisha. Tangu udogo wako umekuwa mvulana mpotovu, anayependa kuwa na njia yake mwenyewe na kufuata akili yake mwenyewe. Haukupenda kusalimisha mapenzi yako na nia yako kwa waliokuwa wanakulea. Huu ndio uzoefu ambayo unapaswa kuupata. {2T 307.1}

Hatari yako inazidi kuongezwa na roho ya uhuru ulionao na kujiamini mwenyewe – hili zimeshikana, na kutokuwa na uzoefu wako--ambao vijana wengi wa umri wako wanaweza kufikiria wakati hawana wazazi wao wapenzi wa kuwalea, kuwaangalia kuwaongoza, kuchochea mioyo yao kwa mapenzi mwanana, kujali, huruma nyororo kwenye nafsi zao. Unahisi kuwa ni wakati wako sasa kufikiri na kutenda vile inavyokufaa.



“Mimi ni kijana sasa na wala sio mtoto. Nina uwezo wa kutofautisha jema na baya. Nani ana mamlaka au haki ya kuniingilia? Nina uwezo wa kuwa mipango yangu. Ni nani ana mamlaka ya kuiningilia? Haya yamekuwa ni sehemu ya mawazo yako na unajitia moyo katika hayo kwa vijana wa rika yako. {2T 307.2}

Unahisi kuwa ukilazimisha kudai uhuru wako na kutenda kama kijana wa kiume. Hisia hizi na mawazo haya huongoza katika matendo mabaya. Huna roho ya kunyenyekea na kutii. Ni mwenye busara na aliyebarikiwa sana, yule kijana ambaye anajua kuwa ni wajibu wake, ikiwa ana wazazi ambao atajifunza kutoka kwao awatazame na ikiwa hana wazazi, ana walezi, au wale anaoishi nao, anaowachukulia kama washauri wake, wafariji, na kwa njia zingine kama viongozi wake, na ambao wanafanya taratibu zao za nyumbani na mipaka imhusu yeye pia. Uhuru wa aina moja ni wa kusifiwa. Kutamani kubeba mizigo na majukumu yako mwenyewe, na sio kula chakula cha utegemezi, uhuru huo ni sawa. Ni matamanio bora na shauku ya ukarimu ambapo mtu anaamua kujitegemea. Tabia ya kujibidisha na kazi, kutofuja mali, kutunza vitu ni muhimu. {2T 308.1}

Uliwekwa katika mazingira ambayo sio rafiki kwa ajili ya kukuza tabia nzuri ya Kikristo; lakini sasa umewekwa mahali ambapo unaweza kujijengea sifa au kuibomoa. Hatuamini kwamba utabomoa. Lakini hauko salama dhidi ya majaribu. Katika saa moja tu unaweza kuchagua njia ambayo baadaye itakuletea toba ya majonzi machungu. Kwa kujisalimisha kwa majaribu, kwa kukabiliana na jaribu, unaweza kufanya moyo wako kuwa mbali na watu, kupoteza heshima na kujiamini ambako umekuwa unapata kutoka kwa wale watu waliokuwa wanakuzunguka na pia kuchafua tabia yako ya Kikristo. Una somo la unyenyekuvu la kujifunza. Unachukulia kufanya majukumu ya nyumbani ni jambo duni sana kwako....kazi za nyumbani na majukumu madogo-madogo na kutumwa hapa na pale. Una mtazamo ulio wazi wa kutokupenda kwa majukumu haya madogo lakini unapaswa kukuza upendo wa hivi vitu ambavyo unavichukia sana. Mpaka ufanye hivi, hautakubalika mahali popote. Unapojishughulisha na vitu vidogo muhimu, unafanya huduma ya Kweli zaidi kuliko wakati wa kufanya biashara kubwa na kazi nzito {2T 308.2}

Sasa nina kesi akilini juu ya yule aliyeletwa mbele yangu katika maono ambaye aliyepuuzia hizi kazi ndogo na hakuweza kujishughulisha na mambo haya madogo, kutafuta kupunguza kazi za ndani za wale watu wa nyumbani; lilikuwa jambo dogo kwake. Sasa ana familia, lakini bado ana ile hali ya kutojisikia kujihusisha na mambo haya madogo wakati ni ya muhimu. Matokeo yake ni, kazi ya masumbufu mengi na mzigo umelala kwa mkewe. Mke wake analazimmika kufanya vitu vingi au vitaachwa bila kutekelezwa; na kiwango cha shuguli kinachomjia kwa sababu ya ukosefu wa mumewe kimeanza kuvunja mwili wake. Mume hawezi sasa kuushinda uovu huu kwa urahisi iwezekanavyo kama ilivyokuwa ujanani mwake. Anapuza majukumu madogo na anashindwa kuweka kila kitu sawa, safi na vizuri, hivyo hawezi kuwa mkulima mwenye mafanikio. Yule “Aliye mwaminifu katika lililo dogo zaidi atakuwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; naye aliye mdhalimu kwa machache atakuwa mdhalimu katika mengi pia.” {2T 309.1}

Naamani Mshami alimwendea nabii wa Mungu kwaajili ya matibabu yake kutokana na ugonjwa wa kuchukiza, yaani ukoma. Aliagizwa akaoge katika mto Yordani mara saba. Ni kwa nini hakufuata maelekezo ya Elisha nabii wa Mungu mara moja kwa kadiri alivyoambiwa? Ni kwa nini alikataa kufanya kama nabii alivyomwagiza? Aliwaendea watumishi wake, akiwa ananung'unika. Katika hali yake ya kuona kuwa anaaibishwa, anadhalilishwa na kukatishwa tamaa akawa mwenye mihemko, na kwa hasira alikataa kufuata maagizo ya unyenyekevu aliyoambiwa na nabii wa Mungu. “Nilifikiri” alisema, hakika atanijia na kusimama, na kuita Jina la Bwana Mungu wake, na kunyosha mkono wake juu ya mahali penye ukoma, na kuuponya ukoma wangu. Mbona kuna Abana, na Farpari, mito ya Dameski, bora kuliko maji yote ya Israel? Je! Mimi siwezi kujiosha ndani yake na, na kuwa safi? Basi akageuka na kwenda zake kwa hasira, “mtumishi wake akamkaribia, na akamwambia: “Baba yangu, ikiwa nabii amekuamuru utende jambo kubwa, usingelifanya? Je! Si zaidi basi, akikuambia jioshe, uwe safi?” hapo ndiyo huyu mheshimiwa alizingatia ushauri wa watumishi walio chini yake akaenda kujizamisha katika maji ya mto Yordani, na kuoga. Mito aliyokuwa anaitaja na kutumainia ilikuwa mizuri na kuzungukwa na miti na vinyago, na sanamu ilisimikwa katika

miti ya matunda karibu na mto. Ndiyo, watu wengi walikuwa wakimiminika kwa wingi kuabudu miungu yao ya sanamu katika mito hii; hivyo isingelimgharimu, maana angekosa unyenyekevu. Lakini ilikuwa ni kwa kufuata maagizo

Bainishi/elekezi ya nabii wa Mungu ambayo ingeshusha umaarufu wake na roho ya kiburi aliyokuwa nayo. Utii wa hiari ungeleta matokeo yanayotarajiwa. Alijiosha na kufanywa mkamilifu. {2T 309.2}

Kesi yako kwa namna, naam inafanana na hii ya Naamani. Haujafikiri kwamba ili kukamilisha tabia ya Kikristo, ni lazima ujishushe na kuwa mwaminifu katika yaliyo madogo. Ingawa vitu/mambo unayoitwa kufanya yanaweza kuonekana ni madogo/vidogo katika upeo wa macho yako, ila ndiyo majukumu unayopaswa kuyafanya kwa kadri unavyoendelea kuishi. Kupuuza mambo haya kutakufanya uwe na mapungufu katika tabia yako. Wewe kijana wangu mpendwa, unapaswa kujielimisha kuwa mwaminifu katika vitu vidogo. Huwezi kumpendeza Mungu usipofanya hivyo. Huwezi kupokea upendo na mapenzi isipokuwa umefanya kama unavyopaswa, kwa hiari na furaha. Ikiwa unataka wale unaoishi nao wakupende, ni lazima uonyeshe upendo na heshima kwao. {2T 310.1}

Ni wajibu wako kufanya yote katika uwezo wako, kupunguza uzito wa majukumu ya mdada unayeishi naye. Unamwona, rangi ya uso inapauka/hanawiri, na dhaifu, kwa kupikia familia kubwa. Kila kazi ya ziada anayopaswa kufanya, humchakaza na kupunguza nguvu zake. Hana mikono na miguu ya kijana kufanya vishuguli hivi vidogo vidogo. Walikupokea wewe katika familia yao, kama walivyokuambia na sisi kwa wakati huo ili ufanye kazi haraka 'chap chap'. Sasa kama utapuuzia kufanya hivi vitu wanavyofikiri vitawasaidia zaidi, na kuchagua kufuata mapenzi yako katika kazi, ili kufuata chaguo lako mwenyewe kwamba uwe huru, ni lazima upoteze nafasi yako, na ni lazima watafute mtu atakayefanya vile vitu unavyoviona kuwa ni vidogo kwako kufanya. Kwa sasa unafanya kazi kubwa na nzito kuliko nguvu yako inavyokiri kuweza. Unapenda kufanya kazi za mwanaume. Umeweka mapenzi yako mwenyewe, kwa njia ambayo hutaki kubadilika, ambayo ni lazima uyaache. Ni lazima ufie nafsi, usulubishe

nafsi, pata ushindi juu ya nafsi. Hauwezi kuwa mfuasi wa Kweli wa Kristo isipokuwa unashikilia kazi hii kwa uthabiti. {2T 310.2}

Niliona kuwa kwa asili hauna heshima na adabu kwa wale walio wakubwa zaidi yako. Unapaswa kuwa mwaminifu katika vishuguli vidogo na majukumu unayotakiwa kutekeleza, na sio kwenda ukinung'unika kuhusu hayo kana kwamba ulikuwa unakunywa dawa chungu. Huwezi kuona jinsi usivyofurahisha na kuonekana vibaya. Kwa hivyo hauwezi kuwa na furaha mwenyewe, wala huwezi kuwapa furaha wale walio karibu na wewe. Unapaswa kuweka akilini kuwa Mungu ana madai kwako, kama mtumishi Wake, kuwa mwaminifu, mvumilivu, mwema, mwenye upendo, mtiifu na anayejiheshimu na kuheshimu watu. Hauwezi kufikiria ukamilifu wa Kikristo isipokuwa uwe na udhibiti kamili wa roho yako mwenyewe. Unaruhusu hisia kujitokeza moyoni mwako ambazo ni za dhambi, ambazo ni majeraha makubwa kwako, na ambayo huamsha moyo mgumu, wa ukaidi, tofauti na roho ya Kristo, ambaye unapaswa kuakisi maisha yake. {2T 311.1}

Ni kijana wangu mpendwa, anza upya, udhamirie kwa msaada wa Mungu kufuata vitu ambavyo ni vya Ukweli, vya kupendeza, na vya habari njema. Acha uchaji wa Mungu, uunganishwe na upendo na mapenzi kwa wote wanaokuzunguka, uonekane katika matendo yako yote. Uwe mwaminifu na kamilifu katika utendaji kazi; ondoa kila kitu kilicho na uvivu. Uwe na sehemu ya kila kitu na weka kila kitu mahali pake. Kuwa mtu mwenye kuchukuliana na watu, mwema, mkarimu, mchangamfu na anayepatana na watu-mwenye moyo wa urafiki. Ndipo unapoweza ukapata mioyo ya wale ambao unashirikiana nao. Jambo moja unalopaswa kuzingatia daima: hakuna kijana ambaye anaweza kuwa na roho iliyo sawa kama hawaheshimu wanawake na kutafuta kurahisisha shughuli zao. Ni ishara mbaya sana ambayo inaweza kuonekana kwa vijana wa kiume wanapoona wako juu ya jukumu la kusaidia kazi nzito za wanawake au kutafuta kurahisisha shughuli zao. Mtu kama huyo anatambulika. Hakuna mwanamke yeyote ambaye angeruhusu kusalimisha maisha yake kwa mwanaume kama huyo; kwa maana hatakuwa na huruma, hatokuwa mwangalifu naye atakuwa mtu wa kutojali. {2T 311.2}

Mvulana ni mfano wa mwanamume. Ninakusihi ukabiliane na hilo vizuri. Fanya kila kitu kinachohitajika kufanyika katika mwonekano wa majukumu madogo, hata yakiwa hayakupendezi kwa jinsi gani. Kisha unaweza kupata kibali cha wale wanaokuzunguka, na cha kuthaminiwa zaidi, utakuwa na ukubali wa Mungu. Hauwezi kuwa Mkristo usipokuwa mwaminifu katika jambo dogo. Ikiwa unaomba na unajitahidi kufanya wajibu wako kwa kadri uwezavyo, Mungu atakubariki na kukusaidia. Wakati Yesu atakapokuja kuwachukuwa waaminifu Wake, je! Unatamani akuambie: “Vema mtumishi mwema na mwaminifu”? Je, unatamani kuondoa kasoro zote katika tabia yako, ili upatikane bila kosa mbele ya kiti cha enzi cha Mungu? Ikiwa ni hivyo, basi una kazi ya kufanya kwako mwenyewe ambayo hakuna mwingine anaweza kukufanyia isipokuwa wewe mwenyewe tu. Una wajibu binafsi mbele za Mungu. Unaweza kutembea katika nuru, na kila siku utapokea nguvu kutoka kwa Mungu hadi kushinda kila udhaifu, na hatimaye unakuwa miongoni mwa waaminifu, wa Kweli, na watakatifu katika ufalme wa Mungu. Usikubali kushindwa na majaribu. Shetani atakukwaza kwa kukuchukiza na kutafuata kudhibiti akili yako, ili akuongoze kwenye dhamabi. “Mpinge Shetani naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu, Naye atawakaribia.” {2T 312.1}

Kumbuka kwamba jicho la Mungu lipo juu yako kila wakati. Unapojibu bila adabu, Mungu anakuona na anakusikia. Wakati unakuja ambapo wote watahukumiwa kulingana na matendo yao ya kimwili. Utakuwa na sehemu ya kutenda-kujibu katika hukumu. Je, Yesu atakupokea au atakukataa. Mkimbilie Yesu akutie nguvu na neema. Yeye Anatamani kukusaidia, kuwa kiongozi wa ujana wako, na kukuimarisha ili uweze kuwabariki wengine kwa ushawishi wako. Mungu anakupenda na atakuokoa ikiwa utakuja Kwake kwa njia aliyowekwa kwako; lakini ukiasi na kuchagua njia yako mwenyewe, itakuwa kwa hasara yako milele. Omba sana kwani maombi ni moja ya wajibu muhimu wa muumini. Bila maombi hauwezi kudumisha safari ya Kikristo. Hayo yanakuinua juu kwa Mungu, yanakutia nguvu za kiroho, na kukuwezesha; ni kitendo cha nafsi kuzungumza na Mungu. {2T 312.2}

Usifikiri kuwa unaweza sitisha juhudi zako au kukesha kwako kwa muda hata mfupi; huwezi. Ujifunze Neno la Mungu kwa uaminifu, ili

kwamba usiwe mjinga wa hila za Shetani, kisha upate kujifunza njia za wokovu kikamilifu zaidi. Mapenzi yako lazima yasalimishwe katika mapenzi ya Mungu. Usitafute raha yako mwenyewe, bali ya wale watu wanaokuzunguka; na kwa kufanya hivyo hauwezi kupata kine isipokuwa furaha. Njoo kwa Yesu na mahitaji yako yote na matakwa, na kwa ujasiri utamani baraka Zake. Mtumaini Mungu na tafuta kutembea katika kanuni, na kuimarishwa na kuwezesha kwa maazimio ya hali ya juu na dhamira yenye kusudi linalotokana na Mungu tu. {2T 313.1}.

Haupaswi kukasirika kwa urahisi. Moyo wako usiwe na ubinafsi, lakini upanuke kwa kuwa na upendo. Unayo kazi ya kufanya ambayo haupaswi kuipuuza. Vumilia shida kama askari mzuri. Yesu anafahamu kila mgogoro uliopo, kila jaribu na kila maumivu ya uchungu. Yeye Atakusaidia; kwa maana alijaribiwa katika yote kama sisi, lakini hakutenda dhambi. Nenda Kwake, kijana mpendwa na mizigo yako. Usimtumainie mtu yeyote kwa kumfanya msiri wako, na usimweleze mtu yeyote magumu yako, ila sisi. Umfanye Yesu kuwa mbeba mizigo yako, na utafute uzoefu kamili katika mambo ya kidini/kiroho. Mungu akusaidie na kukubariki, ni ombi langu la dhati. {2T 313.2}

Huruma zangu za dhati na nyororo zinaamshwa kwaajili ya yatima. Kwa hakika hauna nyumba. Kaburi limemchukua baba yako na mama yako, na nyumba uliyoishi utotoni mwako inaishi familia nyingine. Hauwezi kuwa na kumbukumbu makini za baba yako mcha Mungu na mama yako. Unakumbuka kuwa wakati mwingine ulimhuzunisha. Ulikuwa Hujajifunza kujisalimisha na kutii bado; umejifunza sasa somo hili kwa kiasi fulani. Lakini maombi ya wazazi wako yalikuwa kwamba uweze kuwa kati ya wale wanaompenda na kumcha Mungu, watakaopata makao mbinguni. {2T 313.3}

Lo! Huu ni ulimwengu baridi na wa uchoyo/ubinafsi! Ndugu zako, ambao walipaswa wakupende na kuwa marafiki zako kwa niaba ya wazazi wako kama si kwa ajili yako mwenyewe, wamejifungia wenyewe kwa ubinafsi, na hawana shauku maalum kwako. Lakini Mungu atakuwa karibu na mpendwa wako zaidi kuliko jamaa zako wowote wa duniani unaoweza kuwa nao. Yeye Atakuwa rafiki yako na

hatakuacha kamwe. Yeye ni baba wa wasio na baba. Urafiki Wake utathibitika amani tamu kwako na itakusaidia kubeba hasara yako kubwa kwa ujasiri. Tafuta kumfanya Mungu kuwa baba yako, na hautakuwa na haja ya kuwa na rafiki mwingine. Utaanikwa katika majaribu; lakini utasimama imara, ila jitahidi kufanya imani yako imara. Utahitaji neema kusimama imara, lakini Jicho la Mungu lenye huruma litakuwa juu yako. Omba sana na kwa bidii, ukiamini kwamba Mungu atakusaidia. Jilinde dhidi ya vihasira na kuzira kwa kitoto na roho ya mizaha ya kwamba ni lazima upate kitu fulani, au mtu fulani afikie kitu fulani (tantalizing). nilivu ni fadhila ambayo unahitaji kuhimiza. Tafuta uchaji Mungu wa moyoni. Kuwa Mkristo thabiti. Uwe na usafi wa upendo na unyenyekevu wa kujishusha, na kisha haya yasukwe katika maisha yako. {2T 314.1}

Kwa kujielimisha kumcha Mungu, na kuwapenda wote wakuzungukao, Maisha yako yanaweza kuwa yenye faida, yenye furaha, mfano wako kuongoza wengine kwenye njia ya unyenyekevu ya utakatifu. Uwe na ujasiri wa maadili mema kila wakati kutenda mema na kumpa Mwokozi wako utukufu. Ninakusihi, kijana mpendwa, utafute utakatifu wa Kweli. {2T 314.2}

## **SURA YA 44**

### **MWANACHAMA ASİYETAWALIKA**

Dada mpendwa S: baadhi ya mambo nimeonyeshwa yakikurejelea wewe. Hauna ufahamu wa hali yako halisi. Unahitaji kazi ya kina na ya bidii ya neema moyoni mwako. Unahitaji kuweka moyo wako sawa na nyumba yako katika utaratibu. Mfano wako katika familia yako haustahili kuigwa. Umekuwa chini ya viwango, lakini pia ukashindwa kufikia kiwango cha kuinuliwa na Bwana wetu mtakatifu. Unapenda kutembelea watu na kuzungumza mambo mengi ambayo hayamstahili Mkristo. Maneno yako yametiwa chumvi na mara nyingi huwa mbali na Ukweli. Maneno na matendo yako yatakuhukumu siku ya mwisho. Kwa hayo utahesabiwa haki au utahukumiwa. Elimu yako bado haijawa ya

tabia bora, kwa hiyo sasa unayo kazi kubwa na muhimu ya kujielimisha na kujifunza mwenyewe kusafisha mawazo na matendo. Fundisha akili yako ili kwamba itakuwa rahisi kwayo kuishi maisha ya usafi na matakatifu. Kuza mapenzi kwa mambo ya kiroho na utauwa wa Kweli. {2T 314.3}

Mazungumzo yako mara nyingi huwa ya hali ya chini. Unajidanganya nafsini mwako mwenyewe, na uongo huu utathibitisha mauti usipoamka na kujitazama mwenyewe jinsi ulivyo na kumrudia Mungu kwa unyenyekevu wa akili/nia. Una mwelekeo wa kudanganya. Kijana wako hana ujuzi wa majaribio kwa Mungu au wa madai ya Ukweli mtakatifu. Anasifiwa na kudanganywa na wazazi wake kuwa yeye ni Mkristo bila kujengewa msingi wake, lakini ana uwakilishi mbaya zaidi wa Mkristo mtunza Sabato. Mungu atuepushe kufikiria kwamba huo ni Ukristo. Haumuadibishi kijana wako. Anafanya kwa namna anavyojisikia mwenyewe na ana maoni yake yenye ubaguzi. Ana hisia kidogo za adabu ya Kweli, utu wema, na uungwana wa kawaida. Ni mwenye mkorofi/rafu na ambaye hajakuza elimu ya maadili mema, asiyependa wala kupendeka. Unamwasilisha kwa wengine kuwa ni Mkristo, na kwa kufanya hivyo unadhalilisha kazi ya Kristo. Huyu mvulana yupo katika njia mbaya ya kuwa mnafiki aliyeelimika. Hana ile hali ya kujitawala mwenyewe, na kisha unamsifu huku ukimdanganya kwamba yeye ni Mkristo {2T 315.1}

Kazi ya matengenezo ni lazima ianze na wewe. Unapaswa kuwa na mazunguzo masafi na mlinzi wa nyumba, kupenda majukumu ya nyumbani, kumpenda mume wako na mtoto. Unapaswa kujifunza kutumia muda wako vizuri ili usilemee nguvu zako. Majukumu mepesi ya nyumbani unayopaswa kufanya, unaweza kuyabeba pasipo kulemewa, ikiwa utafanya kwa uvumilivu na uadilifu unaofaa.

Lakini una kazi ya kufanya ya kudhibiti ulimi. Hiki ni kiungo kidogo na hunena vitu vikubwa, lakini kinahitaji kuunganishwa na neema na kujitawala kwa kiasi ili kuzuia kisiende huku na kule bila mpango. Mazungumzo yako ni ya hali ya chini, unajiendekeza katika mazungumzo ya kipuuzi na ya hali ya chini. “Maneno yoyote ya ufisadi yasitoke kinywani mwako, isipokuwa yale maneno mazuri yanayoweza



kutumiwa kukuza, ambayo yanaweza kuwasilisha huduma ya neema kwa wasikilizaji. {2T 315.2}

Hebu Bwana apate kukusadikisha katika mambo haya kwa kadri unavyosoma mistari hii. Ninawasihi mvae upole wenye utu wa mwanamke na mama. Kuna wajibu unaomhusu baba. Jitihada zako zinapaswa ziunganishwe ili muweze kumwongoza na kumdhibiti kijana wenu, ambaye anasafiri kwa haraka katika barabara ya upotevuni. Unapaswa kutafuta kwa bidii ibada ya ndani ya moyo, hata mapambo ya roho ya upole na utulivu, ambayo machoni pa Mungu ni ya kutukuzwa, kwa uvumilivu, neema, na unyenyekevu mzuri, unaweza kumfundisha kijana wako maskini, mvulana aliyedanganywa kuhusu kanuni za kwanza za Ukristo, na upole au adabu ya Kikristo. Wewe ni mwenye harara na mwenye kelele. Ah! Ni muhimu kiasi gani uone kazi ya kufanywa kwako, kabla haujachelewa sana! Sasa Yesu anakualika uje Kwake, na ujifunze Kwake, kwa kuwa Yeye ni mpole na Mnyeyekevu wa moyo. Ahadi aliyokupa ni ya uhakika, kwamba utapata pumziko Kwake. Unayo kazi kubwa ya kufanya. Usidanganye nafsi yako mwenyewe, lakini jichunguze mwenyewe kwa nuru ya umilele. Haiwezekani wewe kuokolewa kama vile ulivyo. {2T 316.1}

Dada S, mume wako anaweza kuwa mwenye manufaa kanisani kama ushawishi wako ungekuwa kama ulivyopaswa kuwa. Lakini mfano wako na ushawishi wako unamfanya asiwe na sifa ya kuweka ushawishi unaotakasa hapo kanisani. Ushawishi wa nyumbani una unapikua/unapindua nguvu juhudi zake nzuri. Wewe haustahili kabisa kuwa mke wa mzee wa kanisa. Mungu anakuita kufanya matengenezo. Mume wako anayo kazi ya kufanya, kuweka moyo wake sawa na nyumba katika utaratibu. Atakapoongoka ndipo atakapowaimarisha ndugu zake. {2T 316.2}

Kama familia, mnahitaji kutakaswa kupitia Kweli. Dada mpendwa, Je, unaweza kuangalia kazi unayopaswa kuifanya na kuanza pasipo kuchelewa, Ili ushawishi wako uweze kuwa wa kuokoa? Shughulikia wokovu wako kwa hofu na kutetemeka. Enendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati. “Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu.”

Yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya heshima, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yaliyo ya kupendeza, yoyote yaliyo mazuri, ikiwa kuna wema wowote, na ikiwa kuna sifa yoyote, yatafakarini mambo hayo.” {2T 317.1}

Kuna masomo mengi yenye faida ambayo ni ya kutafakari na kuzungumzia. Mazungumzo ya Mkristo yanapaswa kuwa mbinguni, ambapo tunamtafuta Mwokozi. Kutafakari juu ya vitu vya mbinguni jambo la faida, na daima itaambatana na amani na faraja ya Roho Mtakatifu. Wito wetu ni mtakatifu, imani yetu tunayoikiri imetukuka. Mungu anawatakasa watu kwa ajili Yake Mwenyewe, watu wa kipekee, watu wenye bidii ya matendo mema. Yeye amekuwa kama msafishaji na mtakasaji wa fedha. Wakati taka na chuma zinaondolewa, basi taswira Yake itakisiwa kikamilifu ndani yetu. Ndipo maombi ya Kristo kwa wanafunzi Wake yatajibiwa ndani yetu: “Uwatakase kwa ile Kweli, Neno Lako ndio Kweli” wakati Ukweli una ushawishi wa kutakasa mioyoni mwetu na maishani, tunaweza kumtolea Mungu huduma inayokubalika na tunaweza kumtukuza hapa duniani, tukishiriki asili ya Uungu na kuokoka na ufisadi uliopo ulimwenguni kupitia tamaa. {2T 317.2}

Ah! Ni watu wangapi watakaokutwa hawako tayari wakati Bwana atakapokuja kuhesabu watu Wake! Wengi wana maoni machache juu ya kile kinachomfanya mtu kuwa Mkristo. Kujihesabia haki wenyewe kutakuwa hakuna faida yoyote. Ni wale tu watakaoweza kustahimili majaribu ndio wataokutwa na haki ya Kristo, wale waliojazwa na Roho Wake, na wanaotembea kama vile Yeye alivyotembea, katika usafi wa moyo na maisha. Mazungumzo lazima yawe matakatifu, na kisha maneno yataungwa kwa neema. {2T 317.3}

Bwana awasaidie kama familia kuweka mambo kwa usahihi, kuinuliwa katika maisha, na katika matendo yako yote kuheshimu madai yako, au kile unachokiri. {2T 318.1}

## **SURA YA 45**

### **FARAJA KATIKA MATEO**

Dada Mpendwa T: nimesikia juu ya mateso yako, na nimeharakisha kuandika mistari michache. Dada yangu mpendwa, ninao ushuhuda mzuri sana kwamba Bwana anakupenda. Katika maono ya mwisho niliyopewa, nilioneshwa kesi yako kati ya nyingine nyingi. Niliona kuwa uliathiriwa hapo zamani na njia iliyokuwa makosa, ambayo watu wengine walikuwa wakiyafanya. Lakini kwa umakini ulikuwa mwangalifu sana, na ukiwa na dhamiri na tashwishwi ya kujua kilicho sahihi, ulichukulia jambo hili kwa unyeti sana na kuona kuwa hali yako ilikuwa ni mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa. {2T 318.2}

Umekuwa ukisumbuliwa na ugonjwa kwa muda mrefu sasa. Una athari ya neva (mfumo wa fahamu), wasiwasi na ugonjwa wa tumbo la kuvimbiwa (dyspeptic, tumbo ni ubongo wa pili, una mishipa ya fahamu

mengi). Ubongo umeunganishwa kwa karibu na tumbo, na nguvu yake ya utendaji imekuwa ikiitwa mara nyingi kusaidia viungo dhaifu vya mmeng'enywa wa chakula, ili kurejeshea uhai wa viungo ambavyo vimeathiriwa na udhaifu, vimehuzunishwa na kusongwa sana. Wakati ukiwa katika hali hii, akili yako ina huzuni, na kwa kawaida inaegemea upande wa giza, ukifikiri kuwa uso wa Mungu umekasirika juu yako. Umefikiria kuwa maisha yako hayana maana yoyote, kwamba yamejazwa na makosa na harakati mbaya. Dada mpendwa, kuugua kwako na shida ya kiafya, imepelekea hali hii ya kukosa matumaini na kukata tamaa. Mungu hajakuacha wewe; upendo Wake bado upo kwako, niliona kuwa unapaswa kumtumainia kama mtoto anavyojiamini akiwa katika mikono ya mama yake. Mungu ni mwenye huruma na mwema, Naye amejaa upendo mwingi na huruma. Yeye Hajaondoa uso Wake kutoka kwako. {2T 318.3}

Wewe umekuwa unachukulia vitu kwa unyeti sana. Unafikiria kwa kina sana na hauna uwezo kuacha masumbufu ya maisha, kufadhaika na kukata tamaa kwa akili. Niliona kwamba Mungu ni msaada wako wa sasa ikiwa ungemwamini Yeye tu. Lakini umekuwa na mashaka yanayokutoa kutoka mikononi mwa Mpendwa wako, Mwokozi mwenye upendo. "Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?" Ni ahadi ya pekee ya namna gani! Tunaweza kudai mengi kutoka kwa Baba yetu wa mbinguni Mwenye fadhili. Mibaraka mikubwa imewekwa kwa ajili yetu. Tunaweza kumwamini Mungu, tunaweza kumtumaini Yeye, na kwa kufanya hivyo, tulitukuze Jina Lake. Hata kama tumeshindwa na adui, bado hatujatupiliwa mbali, hatujaachwa na kukataliwa na Mungu. Hapana; Kristo Yupo mkono wa kuume wa Mungu, ambaye pia anatuombea. "Ikiwa kama mtu atatenda dhambi, tunaye Mwombezi mbele ya Baba. Yesu Kristo Mwenye haki." {2T 319.1}

Nataka niseme, dada yangu, wewe usiutupe ujasiri wako. Roho yako masikini yenye kufadhaika, Isimamishe katika ahadi za Mungu. Kwa kufanya hivyo, pingu za adui zitavunjwa, mapendekezo yake hayatakuwa na nguvu. Usisikilize minongono ya adui. Kuwa huru, nafsi iliyomizwa. Kuwa na ujasiri. Uambie moyo wako masikini na

uliofadhaika: “mtumaini Mungu: kwa maana nitamsifu tena, aliye afya ya uso wangu, na Mungu wangu.” Najua Mungu anakupenda. Weka tumaini lako Kwake Bwana. Usifikirie kuhusu vitu vinavyoleta huzuni na msongo, hamisha akili yako kutoka kwenye mawazo yasiyokubalika, yasiyopendeza na umfikirie Yesu aliye wa thamani. Kaa katika nguvu Zake zinazookoa, upendo Wake usikoma, upendo Wake usio na kifani kwako, ndiyo, hata kwako. Ninajua kuwa Mungu anakupenda. Ikiwa hauwezi kutegemea imani yako mwenyewe, basi tegemea imani ya watu wengine. Tunaamini na kutumaini kwaajili yako. Mungu anapokea imani yetu kwa niaba yako. {2T 319.2}

Umejaribu kutenda kwa usahihi, na Mungu anakusikitikia kwa huruma. Uwe na moyo uliochangamka, uiambie huzuni na mashaka yako kwaheri. Kwa kuruhusu au kuendekeza hali ya mashaka, unamvunjia Mungu heshima. Kuna amani katika kuamini na furaha katika Roho mtakatifu. Kuamini huleta amani, na kumtegemea Mungu huleta furaha. Amini, amini! Roho yangu inasema amini. Tulia kwa Mungu. Sadiki ya kwamba, Yeye Ana uwezo kukilinda kile ulichokiweka amana Kwake hata siku ile. Yeye Atakufanya wewe kuwa zaidi ya mshindi kupitia Yeye ambaye anakupenda. Mungu akubariki na kuimarisha imani yako inayoyumba-yumba, ndio ombi letu. Tunakupa hii mistari michache, tukiamini inaweza kukusaidia. {2T 319.3}

## SURA YA 46

### ROHO YA UBINAFSI NA UDIKTETA

Ndugu mpendwa U: nilioneshwa katika maono ya mwisho kwamba utahitaji kujichunguza mwenyewe kwa uangalifu, na kwa wivu, au tabia yako ya kipekee ingeweza kukutawala. Ulikosea ulipokuwa ukimwomba Dada V, na ukachukua roho ile ile ya udikteta, yenye nguvu, ambayo imekuwa laana katika maisha yako. Ulimshinikiza ndugu W, wakati ukizingatia kufeli kwako hapo zamani, ulipaswa kuwa mtu asiyejivuna na mwenye kiasi. Itakuja kuwa vigumu sana kwako kushinda tabia ya kuwaangalia wengine, na kugundua vitu vidogo, na kuzungumza kwa kuazimia, na kukosoa. Yote haya hayakuhusu. Unapofikiria umefaulu kwa kiwango kidogo katika mwelekeo huu, mlango uko wazi kwa ukubwa zaidi kwenye kutofaulu. Hakuna usalama kwako isipokuwa kujidhibiti kwa kila wakati na kuwa na roho ya uvumilivu. Huwezi kukamilisha kazi yoyote kubwa, lakini ukiwa sawa, unaweza kufanya kazi ya Mungu vizuri kidogo. Lakini ushawishi wako hauhitaji kuwa na jeraha; ikiwa umelindwa na umetakaswa kwa Mungu, unaweza kuzungumza neno la amani, la faraja na kutoa ushuhuda kuhusu utajiri mkuu wa Mungu na upendo usio na kikomo wa Yesu. {2T 320.1}

Acha moyo wako ulainishwe na kuyeyushwa chini ya ushawishi wa Roho ya Mungu. Haupaswi kuzungumza sana kuhusu wewe mwenyewe, kwani hii haitamuimarisha mtu yeyote. hupaswi kujifanya mwenyewe kuwa kiini, na kufikiria kwamba ni lazima ujitunze/ujaliwe/utumikiwe kila wakati na kuwaongoza wengine kukujali wewe. Ondoa mawazo yako kutoka kwako mwenyewe na kuyapeleka kwenye mkondo wenye afya zaidi. Zungumza juu ya Yesu na acha ubinafsi uende; wewe uwe umezama ndani ya Kristo, na hii iwe lugha ya moyo wako: “Tazama ni hai, lakini sio mimi, bali ni Kristo anaishi ndani yangu.” Yesu atakuwa msaada wako kila wakati kwa mahitaji yako. Yeye Hatakuacha wewe mwenyewe upigane na nguvu za giza peke yako. Lo! Hapana, ameweka msaada kwa Yule Aliye hodari wa kuokoa kabisa wote wamjiao Yeye. {2T 320.2}

Usijipendeleee. Shinda mawazo yako, upekee wako mdogo, na utafute kumwakilisha Yesu tu. Wakati wa kuzungumza au kuomba katika mkutano, usizungumze kwa kirefu sana. Umeshindwa hapa. Hili unaweza kulirekebisha. Kuhubiri/kuzungumza kwa muda mrefu na kuomba ni kujidhuru afya yako na sio faida kwa wale wanaosikia. Utakuwa na kazi karibuni kuishinda. Walakini unaweza kuifanya ukiwa unashiriki katika kazi hiyo kwa utulivu. Hapa unahitaji kujilinda. Unasita, una haraka, una wasiwasi. Hii unaweza pia kuishinda. {2T 321.1}

Una hamu ya dhati, tamanio la kufanya haki na kufikia ukubali wa Mungu. Endeleza bidii yako ya dhati, juhudi za kudumu, na usife moyo. Uwe mvumilivu. Kamwe usiwe mtu wa lawama. Kamwe usimruhusu adui akudanganye kutoka katika ulinzi wako. Kesha na omba pia. Baada ya kuomba, kesha hapo. Jitihada ni zako mwenyewe; hakuna mtu anayeweza kukufanyia kazi hii. Shikilia nguvu za Mungu, na haraka sana unapona makosa yako ya hapo zamani, ukomboe wakati. {2Tsw 321.2}

## SURA YA 47

### MSIKILIZAJI MSAHAULIFU

Ndugu Mpendwa Y: Kwa maono ya mwisho niliyopewa, nilioneshwa kuwa haujielewi mwenyewe. Una kazi ya kufanya ambayo hakuna anayeweza kukufanyia. Uzoefu wako katika ile Kweli ni mfupi, nawe haujaongoka kikamilifu. Unaweka makadirio ya juu kuhusu wewe mwenyewe kuliko vile unavyoweza kubeba. Nilielekezwa nyuma kwa maisha yako ya zamani. Akili yako ilikuwa haijainuliwa, lakini imekaa juu ya masomo ambayo hayajapangwa kusababisha usafi wa matendo. Umekuwa na tabia za uovu, na ambazo zimechafua maadili yako. Umekuwa karibu sana na jinsia nyingine, na hujawa na mwenendo wa kiasi na staha. Ingekufurahisha zaidi kama kungekuwa na mahusiano ya karibu zaidi kati ya wanaume na wanawake, hasa baada ya nadharia ya Dk. A. mvuto wako kwa----- haukuwa mzuri. Haukuwa mtu sahihi wa mahali hapo; mazungumzo yako ya kijinga na ya upuuzi yalikukosesha sifa ya kuwa na mvuto mzuri. Tabia ya muziki wako haikuwa ya kuhamasisha mawazo au hisia zilizoinuliwa, lakini badala yake ilikuwa ni kuzorotesha. {2T 321.3}

Kwa wiki kadhaa huko nyuma mvuto wako umekuwa ukiimarika; lakini unakosa la uthabiti wa kanuni. Una mapungufu kwa mambo mengi, na katika mambo hayo lazima ujue ni wapi unashindwa. Upumbavu wa ujana wako umeacha alama juu yako; huwezi kamwe kupata kile ulichopoteza kupitia tabia mbaya. Vitu hivi vimekupa ganzi, busara zako kwamba vitu vitakatifu havijatambuliki au kubainishwa wazi. Kwa uzoefu wako wa sasa, huwezi kupinga majaribu. Huwezi kuvumilia majaribu. Haukutakaswa kupitia ile Kweli. Umeshika Kweli, lakini haijakushikilia kwa kukugeuza kwa kufanywa upya nia yako. Wewe ni mtu wa kujidanganya. Ooh, usikubali, nakusihi, usibaki katika udanganyifu, kuhusu hali yako halisi! Hujahisi usadikisho kwa kina kwa sababu ya dhambi zako, na kwa unyenyekevu umtafute Bwana kwa uchungu wa moyo ili makosa yako yafutwe. Usingeweza kuona kwamba njia zako zilikuwa za dhambi sana mbele za Mungu. Kwa hivyo kazi ya matengenezo haijafanywa rohoni mwako. {2T 322.1}



Umejivika mavazi ya kujiona mwenye haki yako mwenyewe, mavazi ya kufunika ulemavu wa dhambi; lakini hii sio dawa. Hujui uongofu wa Kweli ni nini. Mtu wa kale hajafa ndani yako. Una sura ya utauwa, lakini huna nguvu ya utakaso ya Mungu. Unaweza na unaongea na kuandika vizuri, na kwa kadiri maneno yako yanavyokwenda, yanaweza kuwa sahihi; lakini lugha ya Kweli ya moyoni haijazungumzwa. Unajitambua vya kutosha kujua hili. Kesi yako ni hatari; lakini Mungu anakuonea huruma, na atakuokoa ikiwa utaanguka na kuvunjika miguuni Pake, ukijihisi kuwa unajisi wako, uovu, na uozo wako wa rohoni, bila nguvu ya Mungu inayobadilisha. {2T 322.2}

Ndugu yangu, sitaki kukukatisha tamaa, bali kukuongoza kuchunguza nia yako na kutenda kama kwa nuru ya umilele. Achana na mtego wa Shetani. Usikubali, nakusihi, usiongoze mtu yeyote akufikirie wewe katika nuru iliyoinuliwa zaidi kuliko vile unavyoweza kuibeba, kwani wakati huu udanganyifu utakapoondolewa, na ukweli wako kudhihirika kama jinsi ulivyo, kutakuwa na athari. Una usadikisho kwa Roho wa Mungu na unahisi nguvu ya Ukweli, unapoisikiliza; lakini hisia hizi takatifu, nyepesi huondoka, na wewe ni msikiaji msahaulifu. Haujasimikwa, haujaimarishwa, na kutulia katika Ukweli, hujapata uzoefu wa ushawishi Wake Bwana wa utakaso. Umefikiria ni bora kwa shauku yako kuukubali Ukweli, lakini bado haujapata mvuto wake wa kutakasa. Sasa tungekusihi, usidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Hujachelewa kuwa Mkristo; lakini usiende kwa msukumo. Pima kila hatua vizuri, na usidanganye nafsi yako mwenyewe. {2T 323.1}

## SURA YA 48

### TIBA YA HISIA DANGANYIFU

Mpendwa Dada B: Katika maono niliyopewa Juni 12, nilioneshwa kesi yako. Uko katika hali ya kusikitisha, siyo kwa sababu ya ugonjwa halisi, ingawa wewe sio mzima, lakini kwa sababu ya kuyafanya mawazo yako kufikiria kwamba hayawezi kufanya kazi. Miaka kadhaa iliyopita nilioneshwa kwamba umetaabisha akili yako kukaa zaidi juu ya wavulana. Mara nyingi umewafanya kuwa mada ya mazungumzo, na akili yako imekimbilia njia isiyo na faida kwa maendeleo yako ya kiroho. Umeanguka kwenye njia ya kufikiri ambao imesababisha mawazo maovu. Umejeruhi na kuunyanyasa mwili wako mwenyewe, na kujiletea hali ya ujinga akilini. Umeendekeza kwenye msururu wa kupenda fikira na hisia za ‘ugonjwa wa mapenzi-lovesick’ kufikia kuharibikiwa roho na mwili. Ugonjwa huu wa kutofanya mazoezi ni mbaya kwako. Ajira yenye manufaa katika kubeba mizigo ya nyumbani, na kushiriki katika kazi zenye kunufaisha, ingeshinda hali hii mbaya, ingetoa ugonjwa wa hisia hizi za mapenzi zilizo danganyifu na za kufikirika tu, mapema zaidi kuliko njia nyingine yoyote. {2T 323.2}

Umehurumiwa kupita kiasi. Kupunguziwa kila jukumu, imekuwa kosa kubwa sana. Karibu mawazo yako yote sasa ni juu yako mwenyewe. Wewe unaudhiwa kirahisi, huridhiki, na akili yako inakaa juu ya mambo ya kusikitisha, na inatoa picha halisi ya hali yako kuwa mbaya sana, na hata unaweka akilini mwako kuwa kamwe hutaweza kuwa sawa isipokuwa umeolewa. Katika hali yako ya ufahamu wa sasa hufai kuoa/kuolewa. Hakuna mtu ambaye angekutamani wewe katika hali yako ya sasa ya kinyonge, ya kutojiweza, isiyo na manufaa. Ikiwa mtu angevutiwa na kujidai anakupenda, angelikuwa mtu asiye na thamani; kwani hakuna mwanamume mwenye busara anayeweza kufikiria kwa hata sekunde moja kuweka upendo wake, juu ya kitu bure. {2T 324.1}

Hali ya kusikitisha, ya huzuni ya akili yako, ambayo imekuongoza kulialia na kuhisi kuwa maisha hayatamaniki, ni matokeo ya kuruhusu mawazo yako kukimbia kwenye mkondo wa mawazo machafu, juu ya mada zilizokatazwa, huku ukiendekeza tabia ambazo zinadhoofisha

uthabiti, na afya ya mwili wako na kukutayarisha kwa uozo wa mwili wa mapema. Ingekuwa bora kwako kama hujawahi kwenda \_\_\_\_\_. Kukaa kwako hapo kumekujeruhi. Ulikita akili yako juu ya udhaifu wako, na kujichanganya na jamii ambayo ilikuwa ina uharibifu na uovu kwenye ushawishi wake. Bi C alikuwa mwanamke fisadi, mwenye nia mbaya ya uovu. Ushirikiano wake nawe ulizidisha uovu ambao tayari ulikuwa juu yako kwa kiasi fulani. “Mazungumzo mabaya huharibu wema na adabu.” Kwa sasa hali yako haikubaliki ndani ya macho ya Mungu; lakini unafikiri kwamba huna shauku ya kuishi. Lakini ikiwa matakwa yako yatafuatwa kama yalivyo wazi, na kisha maisha yako yakome, kesi yako itakuwa ya kukatisha tamaa kweli-kweli. Hauko tayari kwa dunia hii, wala ijayo ile ya mbingu. {2T 324.2}

Unafikiria kuwa huwezi kutembea, au kupanda farasi, au hata kufanya mazoezi, na unaamua kukaa katika roho ya ubaridi ya kutojali. Umekuwa huzuni na wasiwasi kwa wazazi wako wanaokuendekeza na kukudekesha, na wewe sio faraja kwako mwenyewe. Unaweza kujikakamua na kufanya juhudi mpya, unaweza kazi, unaweza kujikwamua kutoka hali hii ya kutojali iliyo mbaya. Mama yako anahitaji msaada wako; na baba yako anahitaji faraja ambayo unaweza kumpa; kaka zako wanahitaji utunzaji mzuri kutoka kwa dada yao mkubwa; na dada zako wadogo wanahitaji mafundisho yako. Lakini katika kigoda hiki cha uvivu, kama vile umejikalisia juu ya kinyesi cha uvivu, ukiota jua la upendo ambao haujapewa. Umeifanyia nafsi yako mwenyewe upumbavu huu. Soma Biblia yako kama vile ambavyo hujawahi kuisoma hapo awali. Shiriki majukumu ya nyumbani, na punguza uzito kwa wazazi wako walio na mzigo mzito, wanaofanya kazi nyingi. Unapoanza, unaweza usifanye kazi nyingi kwanza ila kila siku ongeza kazi kidogo zaidi ya kufanya na ongeza bidii uliyojiwekea. Hii ndio suluhisho la uhakika kwa akili inayougua na mwili ulionyanyaswa. {2T 325.1}

Ikiwa una bidii na uthabiti wa kusudi, ukiendelea mbele daima, akili yako itarudi, kwa kiwango, cha kukaa juu ya masomo ya afya nzuri, na safi. Kuridhisha ubinafsi kumepunguza kwa kiasi kikubwa nia ya kujali na kufikiria wengine na sasa unapenda kujipendeza mwenyewe tu. Badala ya kudhibiti matendo yako kwa kutenda na kanuni, na hekima,

unajitesa mwenyewe kuongozwa na kila msukumo mdogo ulio wa kitambo. Hii inakufanya ubadilike-badilike na kutokuwa na msimamo au uthabiti. Ni bure kwa wengine kutafuta kukupendeza wewe, kwani haujaweza kujipendeza wewe mwenyewe, hata pale ambapo matakwa yako yote yalitekelezwa. Wewe **ni mtoto** anayebadilika ghafla kila mara bila hata sababu na umekuwa mgonjwa kwaajili yako wewe mwenyewe kupitia ubinafsi wako uliokithiri. {2T 325.2}

Hali hii ya moyo uliopondeka, hali mbaya ni matokeo ya huruma isiyo ya busara na kusifiwa kwa udanganyifu. Umekuwa na akili nzuri sana, lakini haijawa na uwiano sawa kwa sababu imeelekezwa katika mkondo usio sahihi. Umekuwa na thamani kidogo katika jumuiya kuliko sifuri au jedwali lililo tupu. Haipaswi kuwa hivi. Unaweza kujifanyia mwenyewe mambo ambayo hakuna mtu mwingine anaweza kukufanyia wewe. Una majukumu ya kuyafanya, lakini umetoa muda wako mwingi katika vitu visivyokuwa na msaada na matumaini ambavyo unafikiri hauwezi ukafanya. Nia ipo katika kosa, unao uwezo, ila huna nia. {2T 326.1}

Una moyo uliovunjika. Yesu anahitaji mapenzi yako, ikiwa utayasalimisha Kwake Bwana, Yeye atakuondolea maradhi ya mahaba, hisia ya ugonjwa wa mapenzi, upendo usio safi, unaopatikana katika ukurasa za riwaya (novel). Katika Yesu unaweza kupenda kwa moyo wa dhati, na kwa bidii. Upendo huu unaweza kuongezeka kwa kina na kupanuka bila kikomo, na sio kuhatarisha afya ya mwili au nguvu ya akili. Unahitaji upendo kwa Mungu na kwa jirani zako. Ni lazima uamke, na kung'uta udanganyifu huu unaokujia, na kutafuta mapenzi masafi. {2T 326.2}

Tumaini lako la pekee la maisha haya na maisha bora ni kutafuta kwa dhati dini ya Kweli ya Yesu. Usiwe na dini ya mazoea. Unahitaji kuongoka. Ulegevu, uvivu, ubinafsi wenye huzuni hatimaye utakupatia nafasi ya uchangamfu, ambayo itakuwa ya faida kwa mwili na akili. Upendo kwa Mungu utahakikisha upendo kwa majirani zako, na utashiriki katika majukumu ya maisha na shauku kubwa, isiyo na ubinafsi. Kanuni safi ni lazima iendane na matendo yako. Amani ya ndani ya moyo inaleta hata mawazo yako kwenye mkondo wenye afya. Ujitoe kwa Mungu, la sivyo hautapata maisha bora. {2T 326.3}

Una jukumu la kufanya kwa wazazi wako. Haupaswi kukata tamaa utakapokuwa umechoka kwanza. Litathibithisha kuwa jereha la kudumu. Mara nyingi wazazi wako wanachoka sana. Haitakuwa na nusu ya maumivu kwako, kiasi cha wewe kuchoka sana kutumika kikamilifu kwa kazi zenye kunufaisha kama akili yako itavyokuwa kwako mwenyewe, itakuza mazoea ya madhaifu madogo madogo na kuleta matokeo ya kukata tamaa. Kufanya kazi za nyumbani kwa uaminifu, kujaza nafasi ambayo unaweza ukafanya kwa faida kubwa, hata iwe ni rahisi sana na nyenyekevu, ni jambo la kuinuliwa kabisa kwa dhati. Huu ushawishi wa mbingu/Kiungu unahitajika. Katika hili kuna amani na furaha takatifu. Inayo nguvu ya uponyaji. Itafanya kwa siri na taratibu bila ya kujulikana na kutuliza maumivu ya roho, hata mateso ya mwili. Amani ya akili, ambayo hutoka kwenye nia safi na matendo na nia takatifu, itatoa bure chemchemi yenye nguvu kwa viungo vyote vya mwili.

{2T 326.4}

Amani ya dhati na dhamiri isiyokuwa na kosa mbele ya Mungu itahuisha na kutia nguvu akili kama vile umande umwagikao juu ya mimea miyororo. Basi nia inaelekezwa na kudhibitiwa sawa, na yanakuwa na uamuzi, ambao ni huru na upotovu. Tafakari hizi zinapendeza kwa sababu zimetakaswa. Utulivu wa akili ambao unaweza kuwa nao utawabariki wote unaoshirikiana nao. Amani hii na utulivu kwa wakati, itakuwa ya asili, na itaonyesha miale Yake ya thamani juu ya wote wanaokuzunguka, ili kuakisi tena juu yako. Kadri unavyoonja amani hii ya mbinguni na utulivu wa akili, ndivyo itakavyoongezeka zaidi. Ni hai, furaha inayoishi, ambayo haitoi nguvu zote za maadili katika usingizi, lakini inaamsha kwa utendaji ulioongezeka. Amani kamili ni sifa ya mbinguni ambayo Malaika wamamiliki. Mungu aweze kukusaidia ili upate kumiliki amani hii. {2T 327.1}

## SURA YA 49

### WAJIBU KWA YATIMA

Ndugu na dada D wapendwa: ziara yako ya mwisho kwetu na mazungumzo na sisi, imependekeza maoni mengi, ambayo siwezi kuvumilia kuweka machache kwenye karatasi. Nilisikitika sana kwamba mwenendo wa E haukuwa na uaminifu nyakati zote; ila unapotafakari haya, utagundua kwamba hauwezi kutarajia ukamilifu kwa vijana wa rika lake. Watoto wana madhaifu yao, na wanahitaji kufundishwa, na kuelekezwa na uvumilivu mkubwa. {2T 327.2}

Kwamba anazo hisia zisizo sahihi wakati mwingine, ni jambo ambalo linatarajiwa kwa kijana wa umri wake. Ni lazima ukumbuke kuwa kijana huyu, hana Baba wala mama, hana mtu ambaye anaweza kumweleza hisia zake, huzuni zake na majaribu kwa faragha. Kila mwanadamu anahisi kuwa ni lazima awe na mtu fulani wa kumhurumia, mvulana huyu amekuwa akipelekwa kutoka kwa nyumba ya mtu fulani, na kwenda ya mtu mwingine. Huyu kijana amehamishwa kutoka huku na kule ambayo imekuwa changamoto isiyo na tija kwake (from pillar to post), na anaweza kuwa na makosa mengi, na njia nyingi za upuuzi, kwasababu ya uhuru alio nao, na anaweza akawa anakosa adabu/staha. Lakini amekuwa akionyesha jitihada za kufanya kazi/ujasiliamali, na akiwa na maelekezo sahihi na kushughulikiwa kwa upole na upendo, nina hakika kuwa hataweza kutuvunja moyo au kudondosha matumaini yetu, bali angeweza kuleta matunda ya juhudi ambazo watu wamewekeza kwake. Kwa kuzingatia changamoto zake, nadhani ni kijana mzuri sana. {2T 328.1}

Tulipokusihi umchukue tulifanya hivyo kwa sababu tuliamini kabisa kuwa ni jukumu lako na kuwa kumchukua, kungekuletea Baraka. Hatukutarajia kwamba ungefanya hivi ili kufaidika mwenyewe tu kwa msaada ambao utapokea kutoka kwa huyu kijana, lakini kumnufaisha, kufanya jukumu kwa yatima – ni jukumu ambalo kila mkristo wa Kweli anapaswa kulitafuta na kulichukulia kwa shauku na kulitekeleza; ni wajibu, wajibu wa kujitoa dhabihu, ambalo tuliamini kuwa lingekuwa jambo zuri kwako kulifanya, ikiwa ungekifanya kwa moyo mkunjufu,

kwa mtazamo wa kuwa chombo mikononi mwa Mungu, cha kuokoa roho kutoka kwenye mitego ya Shetani, kuokoa mwana ambaye baba yake alijitolea maisha yake ya thamani kuelekeza roho za watu kwa Mwana-Kondoo wa Mungu ambaye anaichukua dhambi ya ulimwengu. {2T 328.2}

Kutoka kwa kile nilichoonyeshwa, Waadventista wa Sabato wana hisia dhaifu tu ya ukubwa ambao ulimwengu na ubinafsi hushikilia mioyo yao. Kama unakusudia kutenda mema na kumtukuza Mungu, kuna njia nyingi unazoweza kuzitumia. Lakini haukuweza kujua kuwa hili ni matokeo ya dini ya Kweli. Hili ni tunda ambalo kila mti mzuri utazaa. Haujahisi kuwa ilihitajika kwako kuwa na shauku kuhusu wengine, kufanya kesi zao kuwa zako, na kudhihirisha Maslahi yasiyo na ubinafsi kwa wale ambao wanasimama zaidi wakihitaji msaada. Haujafikia hatua ya kuwasaidia wale walio na uhitaji zaidi, watu wasio na msaada na wanyonge zaidi. Kama mngekuwa na watoto wenu wa kuzaa wenyewe watoto wenu katika zoezi la kujali, mapenzi, na upendo, ungekuwa haujachukulia swala hili kuwa lako mwenyewe na kwa manufaa yako mwenyewe. Laiti wale ambao hawana watoto, na ambao Mungu amewafanya kuwa mawakili Wake wa mali, wangetanua mioyo yao katika kuwajali watoto wanaohitaji upendo, kujaliwa, na mapenzi na kusaidiwa na mahitaji ya duniani hapa, wangelikuwa na furaha sana kuliko vile walivyo leo. Maadamu vijana ambao hawana utunzaji wa baba wa kuwahurumia na kuwajali wala mapenzi yenye huruma nyororo, wema na upendo mwanana wa mama zao, wanaanikwa katika mazingira hatarishi ya kukumbwa na ushawishi mbaya wa siku za mwisho, ni wajibu wa mtu fulani kuwa mbadala, naam kuchukua nafasi ya baba na mama kwa baadhi yao. Jifunzeni Kuwaonyesha na kuwapa upendo, mapenzi, rehema na huruma. Watu wote wanaokiri kuwa na Baba wa mbinguni, ambaye wanamtumainia kuwa atawajali na kuwatunza, na hatimaye kuwapeleka katika mji aliowaandalia, wanapaswa kuhisi hili jukumu takatifu, la kusimama na kubeba wajibu huu muhimu na wa pekee ulio katika mabega yao kwa kuwa marafiki wa watu wasio na marafiki na kuwa baba kwa yatima na kusaidia wajane, na kuwa na utendaji wenye msaada halisi katika mambo ya kila siku ya dunia hii. Msaada utakaosaidia maslahi ya jamii ya wanadamu. Wengi hawajalitazama jambo hili katika mtazamo wa

nuru ya Kweli. Ikiwa wanaishi kwaajili yao wenyewe tu, hawatakuwa na nguvu kubwa, kuliko ile inayoitajika katika kusaidia . {2T 328.3}

Vijana wanaokua sasa kati yetu hawajaliwi na kutunzwa kama inavyostahili. Ndugu wengine inawapasa wawe na majukumu ambayo hawayafurahii na hawako tayari kuyaona na kuyatekeleza. Hofu ya kujisumbua wenyewe ni udhuru wa watu wengi. Siku ya Bwana, yaani ya hukumu, itafichua majukumu ambayo hayakutimizwa – roho zilipotea kwa sababu ubinafsi hautauki kupata shida au maumivu, ya kutamani na kujishugulisha katika kusaidia wenye shida kwa niaba yao. {2T 329.1}

Nilioneshwa kuwa wale wanaodai kuwa wakristo wanapaswa kukuza mapenzi na fadhili zaidi katika kuwajali wengine, wangelipwa mara nne. Mungu huweka alama. Yeye Anajua sisi tunaishi tukiwa na malengo gani, na huenda kuishi kwetu kupo katika ubora wa kuweza kuwajali maskini, ubinadamu ulioanguka, au kama macho yetu hayakuweza kuona kila kitu lakini mapenzi yetu, na hatukuweza kumwona mtu yoyote isipokuwa sisi wenyewe masikini. Ninakusihi, kwa ajili ya Kristo, na kwaajili ya nafsi yako mwenyewe, na kwa ajili ya vijana, usichukulie swala hili kwa wepesi kama wengi wanavyofikiri. Ni jambo la kuogofya/kufisha, la muhimu linaloathiri shauku yako kwa ufalme wa Kristo, kwa vile wokovu wa roho za thamani unahusika. Kwa nini isiwe jukumu ambalo Mungu ameweka juu ya watu walio na uwezo, kutoa kwa ajili ya faida ya watu wasio na makazi, ingawa wanaweza wakawa wajinga na wasio na nidhamu?

Je, utajifunza kufanya kazi katika mwelekeo wa kupata starehe zenye ubinafsi na kujipatia faida tu? Haifai kwa wewe kupuuza neema na ukubali wa Mungu ambao mbingu inakupa ikiwa utawahudumia wale wanaohitaji utunzaji wako, na kwa hiyo, ili Mungu asibishe hodi bure kwenye mlango wako. Yeye husimama hapo nje ya mlango, kama mtu ambaye ni maskini, yatima wasio na makazi, na wajane wanaoteseka, ambao wanaohitaji upendo, huruma, mapenzi na kutiwa moyo. Usipomfanyia mmoja wa hawa, usingeweza kumfanyia Kristo kama angekuwa hapa duniani. {2T 329.2}



Kukumbuka unyonge wako wa zamani, upofu wako wa kiroho, na giza ambalo lilikuzingira mbele ya Kristo, Mwokozi mpole, mwenye upendo mwanana, kujali, na huruma nyororo, alipokuja kukusaidia na kukukuta pale ulipokuwa. Ikiwa utaruhusu nyakati hizi zipite bila ya kutoa ushahidi dhahiri wa shukrani yako kwa upendo huu wa pekee na wa kushangaza ambao ulitolewa kwako na Mwokozi Mwenye huruma, ninyi ambao mlikuwa wageni katika jamii ya kawaida ya Israeli, kuna sababu ya kuwa na hofu, kuwa bado giza kuu na taabu itakujia. Sasa ni wakati wako wa kupanda. Utavuna kile ulichopanda. Jitolee mwenyewe kwa kadri uwezavyo kwa kila fursa ya kutenda mema. Fursa hizi zinapoboreshwa ni kama neema ya mvua inayopita, ambayo

hukunyweshea maji na kukuhuisha. Ng'ang'ania kila nafasi ndani ya uwezo wako wa kutenda mema. Mikono milegevu itavuna mavuno kidogo. Kwani mtu mzima anaishi kwa ajili gani zaidi ya kuwatunza walio wadogo na kuwasaidia wasiojiweza? Mungu amewakabidhi kwetu sisi ambao tu wazee na wenye uzoefu, Naye atatutaka kutoa hesabu kama majukumu yetu katika mwelekeo huu yamepuuzwa. Haijalishi kama kazi yetu inaweza kutothaminiwa! Haijalishi kama itathibitisha kushindwa mara nyingi, na kufanikiwa mara moja tu! Hii mara moja itatusahaulisha kukatishwa tamaa kote tulikopitia awali. {2T 330.1}

Lakini wachache wana uelewa wa Kweli wa kile kilicho kinachomaanisha Neno Mkristo. Ni kuwa kama Kristo. kuwatendea wengine mema, kutengwa na ubinafsi, usiojifikiria, na maisha yetu kuwa na matendo ya ukarimu usio na ubinafsi. Mkombozi wetu anaziweka nafsi katika uangalizi wa kanisa, kwa wao kuwatunza pasipo na ubinafsi na kuwafunza kwa ajili ya mbingu, na hivyo kuwa watenda kazi pamoja Naye. Lakini kanisa mara nyingi huwatupilia mbali, kwenye uwanda wa vita wa Shetani. Muumini mmoja atasema, "sio jukumu langu," na kisha kutoa udhuru fulani usio na maana. "Naam" anasema mwingine, "hata mimi sio kazi yangu," na hatimaye sio kazi ya mtu yeyote, na roho inaachwa bila kujaliwa na kupotea. Ni wajibu wa kila Mkristo kujihusisha katika shughuli ya kujikana nafsi, ya kujitolea. Je! Mungu hawezi kurudi katika ghala zao na kuongeza makundi yao, ili kwamba badala ya kupoteza waongezewe? "Kuna

atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; na kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji.” {2T 331.1}

Lakini kazi ya kila mtu inapaswa kujaribiwa, na kuletwa hukumuni, na kulipwa sawasawa na kazi yake ilivyokuwa. “Mheshimu BWANA kwa mali yako, na kwa malimbuko ya mazao yako yote. Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi.” “Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Sio kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta masikini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?” Soma fungu linalofuata, na ugundue zawadi kubwa iliyoahidiwa kwa wale wanaofanya hivyo. “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara.” Hapa kuna ahadi kubwa ya thamani kwa wale wote watakaovutiwa na kushugulikia mambo ya wale wanaohitaji msaada. Mungu anawezaje kuingia ndani na kubariki na kufanikisha wale ambao hawajitolei kuwatunza wengine isipokuwa wao wenyewe, na ambao

hawatumii kile ambacho amewakabidhi, kwa ajili ya utukufu Wake duniani? {2T 331.2}

Dada Hannah More amefariki, na alifariki kama mhanga-shahidi- mfiadini kwa ubinafsi wa watu wanaokiri kutafuta utukufu, heshima, kutokufa na uzima wa milele. Akiwa amefukuzwa na waumini wakati wa kipindi kilichopita cha baridi kali, mmishenari huyu wa kujitolea alikufa kwa sababu hakukuwa na moyo uliokuwa na ukarimu wa kutosha kumpokea (alilazimishwa kuondoka kwaajili ya tabia za watu za kutotaka kupokea wageni-exiled). Simlaumu mtu yeyote. Mimi sio hakimumu. Lakini pale Mhukumu wa ulimwengu wote atakapofanya upelelezi, atapatikana mtu fulani wa kulaumiwa. Wote tumekuwa na ufinyu wa mawazo na kumezwa na ubinafsi wetu. Hebu Mungu atuondolee mbali laana hii ya unafiki, iliyotufunika na kutupatia matumbo ya huruma, mioyo ya nyama, upendo mwanana, huruma nyororo, vifungo vya mahusiano ya wema na kujali, ndilo ombi langu, lililotolewa kwa moyo unaosumbuka na kusikia uchungu. Nina uhakika kwamba kazi inapaswa kufanywa kwetu, vinginevyo tutaonekana tumepungua katika siku ya Mungu. {2T 332.1}

Kuhusiana na E, usisahau, nakusihi, kuwa yeye ni mtoto, mwenye uzoefu wa kitoto tu. Usimpime kijana huyu masikini, mnyonge na dhaifu kwa viwango vyako na, kumtegemea awe kama wewe. Ninaamini kikamilifu kuwa una uwezo wa kufanya jambo sahihi kwa mtoto huyu yatima. Unaweza kumpongeza kwa vivutio/zawadi ili kwamba asijihisi kuwa kazi yake haina furaha, isiyopata afueni kwa miale ya matumaini. Ninyi, kaka na dada zangu, mnaweza kufurahiana kwa ujasiri wa kila mmoja wenu, mnaweza kuhurumiana, kushirikiana na kuburudishana, na kuambiana majaribu na mizigo yenu. Mna kitu cha kuwafurahisha ninyi, wakati yeye yuko peke yake. Yeye ni kijana mwenye mawazo mengi, lakini yeye hana mtu yeyote wa kumwamini na kumwambia anayopitia, au wa kumpatia maneno ya kutia moyo katikati ya kukata tamaa kwake na majaribu makali, ambayo najua anayo kama wale ambao umri umekwenda zaidi. {2Tsw 332.2}

Ikiwa mnajifikiria ninyi wenyewe, huo ni upendo wa ubinafsi, usiojazwa kwa baraka za Mbinguni. Nina tumaini kubwa kuwa mtampenda mtoto yatima kwa ajili ya Kristo, kwamba utahisi kuwa mali zako hazina thamani isipokuwa zinatumiwa katika kufanya mema.

Tenda wema; uwe tajiri wa kutenda mema, tayari kutoa mali tayari zao, washirikiane na wengine kwa moyo, huku mkijiwekea akiba dhidi ya wakati ujao, ili kwamba mpate uzima wa milele ulio kweli kweli (1Timotheo 6:17-19). Hakuna atakayevuna thawabu ya uzima wa milele bila kujitoa dhabihu nafsi. Baba na mama waliokuwa wanakaribia kufa waliacha watoto wao, ambao ndivyo vito vyao vya thamani chini ya uangalizi wa kanisa ili wafundishwe mambo ya Mungu na kustahili kwa ajili ya kuingia mbinguni. Wakati wazazi hawa watakapowatafuta wapendwa wao, na mmoja akosekane kwa sababu ya kutojali, Kanisa litajibu nini? Kwa kiwango kikubwa kanisa lina wajibu mkubwa sana kwa ajili ya wokovu wa watoto hawa yatima. {2Tsw 333.1}

Katika uwezekano wote, ninyi mmeshindwa kupata imani, ujasiri na mapenzi ya huyu kijana, kwa kutompatia uthibitisho dhahiri zaidi wa upendo wenu kwa kubania fadhila zenu-vivutio. Kama msingeweza kutumia pesa basi mngeweza kumtia moyo angalau kwa njia fulani kwa kumfanya atambue kuwa hamkuwa msiojali katika shida yake. Kwamba upendo na huruma zitokapo upande mmoja tu ni kosa. Je,

mmejifunza kuonyesha upendo kwa kiasi gani? Ninyi mmejipenda sana wenyewe, na hamhisi umuhimu wa kujizungushia wigo wa mazingira ya upendo mwanana, huruma nyororo, kujali, vifungo vya wema na upole, ambao hutoka katika ubora na uadilifu wa kweli wa moyo. Kaka na dada F waliwaacha watoto wao chini ya uangalizi wa kanisa wakati wa kufa kwao. Walikuwa na ndugu wengi matajiri waliotaka kuwachukua watoto; lakini walikuwa watu wasioamini, na kama wangeruhusiwa kuwatunza, au kuwa walezi, wa watoto hawa, wangeiongoza mioyo yao mbali na Ukweli na kuingia katika mafundisho yenye makosa, na kuhatarisha wokovu wao. Kwa sababu ndugu hawa hawakuruhusiwa kuwachukua watoto, hawakufurahishwa, na hawajawafanya chochote kwaajili ya watoto hawa. Imani ya wazazi katika kanisa inapaswa kuzingatiwa, na isije kusahauliwa kwa sababu ya ubinafsi. {2Tsw 333.2}

Tunayo shauku kubwa kwa watoto hawa. Mmoja tayari ameshakuza tabia nzuri ya Kikristo na ameolewa na mchungaji anayehubiri injili. Na sasa, kwa kurudisha hisani za utunzaji na mizigo iliyobebwa kwa ajili yake, amekuwa mmbeba mizigo wa Kweli katika kanisa. Anatafutwa kwa ushauri na wosia na wale wasio na uzoefu, na huwapa ushauri wautafutao, hakika hawatoki bure. Anao unyenyekevu wa kweli wa Kikristo, na kuwa na heshima, ambayo inaweza kuhamasisha heshima na ujasiri kwa wote wanaomjua. Watoto hawa wako karibu sana na mimi kama watoto wangu tu. Sitawapoteza machoni, wala sitakoma kuwatunza. Nawapenda kwa dhati, kwa wema, kwa upendo. {2Tsw 334.1}

## SURA YA 50

### MWITO KWA WACHUNGAJI

Oktoba 2, 1868, nilioneshwa kazi kubwa na adhimu/nzito sana mbele yetu ya kuuonya ulimwengu kwa hukumu inayokuja. Mfano wetu, ukiwa ni kwa mujibu wa Ukweli tunaoukiri, utaokoa wachache, na kuwahukumu wengi, ukiwaacha bila kisingizio katika siku ambayo kesi za watu wote zitaamuliwa. Wenye haki wanapaswa kuandaliwa kwa uzima wa milele, na wadhambi, ambao hawatakuwa wamejifahamisha na kujizoeza na mapenzi na njia za Mungu, wamepangiwa uharibifu. {2Tsw 334.2}

Sio wote wanaohubiri Ukweli kwa wengine wametakaswa nao. Wengine wana maoni dhaifu ya tabia takatifu ya kazi. Wanashindwa kumtegemea Mungu na kufanya kazi zao zote zifanyike ndani Yake. Utu wao wa ndani haujaongoka. Hawajapata katika maisha yao ya kila siku siri ya utauwa. Wanashughulikia Ukweli usioharibika, wenye uzito wa milele, lakini hawajali, hawana bidii, wala unyofu, kukazana kuwa na Ukweli huu mioyoni mwao, ufanywe sehemu yao, ili kwamba uwe na ushawishi kwao kwa kila kitu wafanyacho. Hawajaunganishwa kweli kweli katika kanuni ambazo Ukweli huu unasisitiza kiasi kwamba haitowezekana kutenganisha sehemu yeyote ya Ukweli na wao wenyewe. {2Tsw 334.3}

Utakaso wa moyo na maisha ndio pekee unaokubalika kwa Mungu. Alisema malaika, alipokuwa amewasonda kidole wachungaji ambao sio waaminifu: “Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi; na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili.” “Iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya BWANA.” Mungu anataka uadilifu wa roho, kwa ile Kweli kuwa ndani kwa kina, ikimbadilisha mtu kabisa kwa nia kufanywa upya kupitia kwa mvuto wa Roho wa Mungu. Sio wachungaji wote ni waaminifu kwa kazi; sio wote wameiweka mioyo yao kwa ajili ya kazi. Wanasonga mbele kiulegevu kana kwamba wana milenia ya

muda itakayowaruhusu kufanya kazi hii ya kuokoa roho. Wanakwepa mizigo na majukumu, kujishughulisha na dhiki. Kujikana nafsi, mateso, na uchovu sio mazuri wala rahisi. Wengine wanajifunza ili kujiokoa kutoka kwa kazi ya kuchosha. Wanajifunza kujipatia urahisi wao wenyewe katika maisha na namna ya kujipendeza wao wenyewe, wake zao, na watoto wao, na kazi ambayo kwayo wamejiingiza inakaribia kupotezwa machoni pao. {2Tsw 335.1}

Mungu anataka roho iliyopondeka na toba ya unyenyekevu kutoka kwa wachungaji ambao kazi zao hazijafanyika ndani Yake. Nilioneshwa watu wanaojishughulisha na mambo ya kiulimwengu. Wanatambua kuwa ikiwa watatimiza malengo yao basi ni lazima watahisi uchovu. Wanaacha raha zao na ile kufurahia kukaa nyumbani, hukubali dhiki; wanavumilia, wana nguvu, na wana shauku. Wachungaji wetu wote hawaoneshi hata nusu ya ari inayooneshwa na wale ambao wanapata faida ya kidunia. Hawana nia wala udhati kwa kusudi lao, wala hawana shauku katika juhudi zao; sio wavumilivu, na hawako tayari kujikana nafsi, kama wale wanaojishughulisha na shughuli za kidunia. {2Tsw 335.2}

God calls for humiliation of soul and humble confessions from the ministers whose works have not been wrought in Him. I was cited to men who engage in worldly enterprises. They know that if they would gain their object they must suffer fatigue. They sacrifice ease and love of home, and endure privations; they are persevering, energetic, and ardent. Our ministers do not all manifest half the zeal shown by those who are securing earthly gain. They are not as intent upon their purpose, nor as earnest in their efforts; they are not as persevering, and are not as willing to deny themselves, as those who engage in worldly pursuits.

Compare these two enterprises. One is certain, eternal, enduring as the life of God; the other is a thing of this life, changeable, perishable, and if men succeed in their ambitious pursuits, that which they gain frequently stings like an adder, and drowns them in perdition. Oh, why should there be so great a contrast in the efforts of those who are engaged—the one class in a worldly enterprise, the other in a heavenly? the one laboring for a treasure here that is perishable, and in the effort suffering much pain for that which is frequently a source of great evil, the other putting forth efforts for the salvation of precious souls, which will be approved of Heaven and rewarded with heavenly riches. There are no risks to run here, no losses to be sustained, the profits are sure and immense.

Linganisha biashara hizi mbili au shughuli hizi mbili. Moja ni Kweli, halisi, la milele, la kudumu kama maisha ya Mungu; jingine ni jambo la maisha haya, linaloweza kubadilika, kuharibika, na ikiwa watu watafaulu katika harakati za tamaa zao, kile wanachokipata mara kwa mara huuma kama nyoka, na kuwazamisha katika upotevu. Lo, kwa nini kuwe na tofauti kubwa katika juhudi za wale wanaojishughulisha—kundi moja katika mambo ya ulimwengu, na jingine mbinguni? Yule anayefanya kazi kwa ajili ya hazina hapa ambazo zinaweza kuharibika, na kwa bidii anateseka kwa maumivu mengi kwa kile ambacho mara

kwa mara ni chanzo cha uovu mkubwa, mwingine hufanya juhudi kwa wokovu wa roho za thamani, ambazo atakubaliwa Mbingu na atalipwa utajiri wa mbinguni. Hakuna hatari za kukimbia hapa, hakuna kudumishwa hasara, faida ni za Kweli na kubwa. {2Tsw 335.3}

Wale ambao wako badala ya Kristo, wakisihi roho zipatanishwe na Mungu wanapaswa kwa amri/kanuni na mfano kudhihirisha nia ya kutoshindwa ili kuokoa roho. Bidii yao, udhati, uvumilivu, kujikana nafsi, na roho ya kujitoa dhabihu inapaswa kuzidi uadilifu na bidii ya wale wanaojipatia faida ya kidunia kwa kuwa nafsi ni ya thamani zaidi kuliko takataka za dunia na mhusika ameinuliwa zaidi kuliko shughuli za kidunia. Mambo yote ya kidunia yana umuhimu mdogo ikilinganishwa na kazi ya kuokoa roho. Vitu vyote vya kidunia sio vya kudumu, vinagharimu sana, ijapokuwa vinagharimu sana. Lakini roho moja iliyoongolewa itang'aa katika ufalme wa mbinguni katika nyakati za umilele. {2Tsw 336.1}

Wachungaji wengine wamesinzia, na watu pia wamesinzia; lakini Shetani ameamka kabisa. Kuna kujitoa muhanga kidogo kwa ajili ya Mungu au kwa Ukweli. Wachungaji lazima waonyeshe mfano. Katika kazi zao wanapaswa kuonesha kuwa wanachukulia vitu vya milele vya thamani isiyo na kipimo na vitu vya kidunia kama vitu ambavyo havina ulinganano na vile vya milele. Kuna wachungaji wanaohubiri Ukweli wa leo ambao wanapaswa kuongoka. Uelewa wao lazima uimarishwe, mioyo yao isafishwe, na mapenzi yao yasalimishwe na kukita kwa Mungu. Wanapaswa kuwasilisha Ukweli katika namna ambayo itaamsha akili kufahamu ubora Wake, usafi, na utakatifu. Ili kuweza kufanya hivi, wanapaswa kuweka mbele ya akili zao kupenda vitu ambavyo vimeinuliwa na ambavyo vinatakasa, vina uhuishaji, na ushawishi mkubwa katika akili. Lazima wawe nao moto wa utakaso wa Kweli unaowaka juu ya madhabahu ya mioyo yao, kushawishi na kupambanua maisha yao; kisha, kwenda watakakokwenda, katikati ya giza, huzuni na ukungu, watawaangazia wale walio gizani na nuru ikaayo ndani yao na kuwaangazia pande zote. {2Tsw 336.2}

Wachungaji lazima wajazwe na roho ile ile kama ya Bwana wao wakati alipokuwa hapa duniani. Yeye alienda akifanya mema, akibariki wengine kwa ushawishi Wake. Yeye Alikuwa mtu wa huzuni na aliyejua majonzi. Wachungaji wanapaswa kuwa na dhana dhahiri ya vitu vya milele na madai ya Mungu dhidi yao; kisha wanaweza kuvutia mioyo ya wengine na kulisimua ndani yao upendo wa kutafakari vitu vya mbinguni. {2Tsw 337.1}

Wachungaji wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia. Je! Zile Kweli ambazo wanazishughulikia zina nguvu? Kama ni hivyo, wanapaswa kutafuta kuzishughulikia kwa ustadi. Mawazo yao yanapaswa kuwa wazi na yenye nguvu, na roho zao zenye bidii/ari, vinginevyo watadhoofisha nguvu ya Ukweli wanaoshughulikia. Kwa kuwasilisha Ukweli kwa woga, na bila ari, kurudia tu nadharia bila kuchochewa wao wenyewe, hawataweza kamwe kuwaongoa watu. Hata wama wangeishi kwa muda mrefu kama alivyoishi Nuhu, juhudi zao hazingeweza kutekelezwa. Upendo wao kwa roho lazima uwe na nguvu kali na bidii yao imara. Njia yao ya ulegevu, isiyo na hisia ya kuwasilisha Ukweli kamwe haitawaamsha wanaume na wanawake kutoka katika usingizi wao kama mauti. Lazima waonyeshe kwa tabia zao, kwa matendo na maneno yao, na kwa kuhubiri na kuomba kwao, kwamba wanaamini kuwa Kristo Yuko mlangoni. Wanaume na wanawake wako katika masaa ya mwisho ya kufungwa kwa mlango wa rehema, na bado ni wazembe na wajinga/wapumbavu, na wachungaji hawana nguvu ya kuwaamsha; wao wenyewe wamelala. Wahubiri waliolala wakiwahubiria watu waliolala! {2Tsw 337.2}

Kazi kubwa lazima itimizwe kwa wachungaji ili waweze kufanya kufanikiwa kwa mahubiri ya Ukweli. Neno la Mungu linapaswa kujifunzwa vizuri-kikamilifu. Usomaji mwingine wote ni duni kuliko hii. Kujifunza Biblia kwa uangalifu sio lazima kuzuie usomaji mwingine wote wa machapisho yenye asili ya kidini; lakini ikiwa Neno la Mungu linasomwa kwa maombi, usomaji wote ambao utakuwa na mwelekeo wa kugeuza akili kutoka kwa Neno La Mungu, huo utaondolewa. Ikiwa tunajifunza Neno la Mungu kwa hamu, na kuomba ili kulielewa, uzuri mpya utaonekana katika kila mstari. Mungu atafunua Ukweli wa



thamani wazi kabisa ili akili ipate raha ya dhati na kuwa na karamu endelevu wakati Ukweli Wake wa kufariji na wa hali ya juu unapofunuliwa. {2Tsw 337.3}

Kutembelea nyumba kwa nyumba ni sehemu muhimu ya kazi ya mchungaji. Anapaswa kulenga kuzungumza na watu wote wa familia, ikiwa wanaukiri Ukweli au la. Ni jukumu lake kugundua hali ya kiroho ya wote; na anapaswa kuwa karibu sana na Mungu ili aweze kushauri, kuhimiza, na kukaripia, kwa uangalifu na kwa hekima. Anapaswa kuwa na neema ya Mungu moyoni mwake na utukufu wa Mungu daima katika mtazamo wake. Kuchukulia vitu kirahisi kwa mizaha ni marufuku kabisa katika Neno la Mungu. Mazungumzo yake yanapaswa kuwa mbinguni, maneno yake yamepikwa na viungo vya neema. Sifa zote zinatotolewa bila kutoka moyoni, bali kwa kujikomba tu, zinapaswa kutupiliwa mbali, kwa kuwa ni kazi ya Shetani kumsifu mtu kwa udanganyifu. Wanadamu walioanguka masikini, na wadhaifu, kwa ujumla wanajidhania wametoshika na hujifikiria wenyewe na hivy hawahitaji msaada katika mwelekeo huu (wa kutukuzwa). Kuwasifu mno wachungaji wako hakustahili. Kunapotosha akili na hakuongozi katika upole na unyenyekevu; lakini bado wanaume na wanawake wanapenda kusifiwa, na ni mara nyingi sana wachungaji wanalipenda hilo. Ubatili wao unafurahishwa na hilo, lakini limethibitisha laana kwa wengi. Kukaripia kunastahili kuthaminiwa kuliko kusifiwa. {2Tsw 338.1}

Sio wote wanaohubiri Ukweli wanagundua kuwa ushuhuda na mfano wao vinaamua hatima ya roho. Ikiwa hawana uaminifu katika utume wao, na kuwa wazembe katika kazi zao, roho zitapotea kama matokeo yake. Ikiwa wanajitoa mhanga na kuwa waaminifu katika kazi ambayo Bwana amewapa kufanya, watakuwa vyombo muhimu katika wokovu wa wengi. Baadhi wanaruhusu mambo madogo-madogo kuwahamisha kutoka katika kazi. Barabara mbovu, hali ya hewa ya mvua, au mambo madogo nyumbani ni udhuru wa kutosha kwao kuacha kazi ya kushughulikia roho. Na mara nyingi hii hufanyika katika wakati muhimu zaidi katika kazi. Wakati watu wamevutiwa zaidi na akili za watu zimechangamshwa na somo, moyo wa shauku unaachwa kufa kwa sababu mchungaji anachagua vitu vinavyomfurahisha na eneo rahisi, na linalompendeza zaidi. Wale ambao hufuata njia hii wanaonesha

wazi kwamba hawana mzigo kwa kazi iliyo juu yao. Wanatamani kubebwa na washiriki. Hawako tayari kuvumilia dhiki na shida ambayo daima ndilo fungu la mchungaji wa kweli. {2Tsw 338.2}

Wengine hawana uzoefu wa kushikilia kazi hiyo na kuona kwamba ilikuwa ya umuhimu mkubwa sana. Hawaingii katika kazi hiyo kwa unyofu, ari na bidii ambayo ingeonesha kuwa wanafanya kazi ambayo itapimwa siku ya hukumu. Wanafanya kazi sana kwa nguvu zao. Hawaweki imani yao kwa Mungu-hawamtegemei Mungu, na kwa hivyo makosa na kutokamilika huashiria juhudi zao zote. Hawampi Bwana nafasi ya kuwafanyia chochote. Hawatembei kwa imani, bali kwa kuona na macho ya mwili. Hawatakwenda haraka au zaidi ya vile wanavyoweza kuona. Hawaonekani kuelewa kwamba kujitosa katika kitu kwa ajili ya Ukweli kuna sehemu yoyote katika uzoefu wao wa kidini. {2Tsw 339.1}

Wengine wanatoka katika nyumba zao kwenda kufanya kazi katika uwanja wa injili, lakini hawatendi kana kwamba Ukweli ambao wanausema ulikuwa Ukweli kwao. Matendo yao yanaonesha kuwa wao wenyewe hawajapata uzoefu wa nguvu iokoayo ya Ukweli. Wakati wanapokuwa nje ya kibweta, wanaonekana kutokuwa na mzigo wa Ukweli. Inaonekana wakati mwingine wanafanya kazi ili kupata faida, lakini mara nyingi bila faida. Wanahisi kama wana haki ya kupata mishahara wanayopokea kana kwamba wameistahili kwa kuifanyia kazi; bila kujali kwamba kutojitoa kwao wakfu, kumeigharimu kazi zaidi, wasiwasi, na maumivu ya moyo kwa wafanya kazi ambao wana mzigo wa kazi juu yao kuliko zile juhudi zao zote kufanya mema. Hao sio watendakazi wenye faida. Lakini watalazimika kubeba wajibu huu wenyewe. {2Tsw 339.2}

Mara nyingi ni kwamba wachungaji wamependa kutembelea karibu makanisa yote, wakiutoa wakati wao na nguvu zao ambapo kazi yao haitafaidia chochote. Mara kwa mara makanisa yamewatangulia wachungaji wanaofanya kazi kati yao, na watakuwa katika hali ya kufanikiwa zaidi ikiwa wachungaji hao wangewapisha njia yao na kuwapatia nafasi Washiriki/Walei kufanya kazi. Jitihada za wachungaji wa namna hiyo kujenga makanisa ni za kubomoa tu. Nadharia ya

Ukweli imewasilishwa tena na tena, lakini haikuongozwa na nguvu ya Mungu itiayo nguvu. Wanaonyesha kupooza kabisa kuhusiana na yanayoendelea; roho hiyo huambukiza, na makanisa hupoteza mapenzi na mzigo wa wokovu kwa wengine. Hivyo basi kwa kuhubiri na mfano wao, wachungaji huwaliwaza watu kwa usalama wa kimwili. Ikiwa wangeyaacha makanisa, na kwenda nje katika maeneo mapya, na kufanya kazi ya kupanda makanisa, wangeelewa uwezo wao na nini ndiyo gharama za kuleta roho kuchukua msimamo wao katika Ukweli. Na hapo wangependa jinsi gani wanapaswa kuwa waangalifu kwamba mfano na ushawishi wao usiweze kamwe kuwavunja moyo au kuwadhoofisha wale ambao imewagharimu sana, katika bidii na maombi kubadilishwa na Ukweli. Hebu “Kila mtu na aipime kazi yake mwenyewe, ndipo atakapokuwa na sababu ya kujisifu ndani yake tu, wala si kwa mwenzake.” {2Tsw 340.1}

Makanisa hutoa mali zao kuwasaidia wachungaji katika kazi zao. Je! Wana nini cha kuwatia moyo katika ukarimu wao? Wachungaji wengine hufanya kazi mwezi hadi mwezi na wanatimiza kidogo sana kiasi kwamba makanisa yanavunjika moyo; hawawezi kuona kuwa kuna kitu chochote kinachofanywa ili kuongoa roho kuufuata Ukweli ama kuwafanya wale ambao ni washiriki wa kanisa kuwa watu wa kiroho zaidi au wenye bidii katika upendo wao kwa Mungu na Ukweli Wake. Wale wanaoshughulikia vitu vitakatifu wanapaswa kujiweka wakfu kabisa kwa kazi hiyo. Wanapaswa kuwa na shauku isiyo na ubinafsi ndani yake na upendo wa dhati kwa roho zinazoangamia. Ikiwa hawana hili wamekosea utume wao na wanapaswa kusitisha kazi yao ya kufundisha wengine, kwa maana wanafanya uharibifu zaidi kuliko wanavyoweza kufanya vyema. Baadhi ya wachungaji wanapenda kujionyesha, lakini hawayalishi makundi ambayo yanaangamia kwa chakula kwa wakati ufaao. {2Tsw 340.2}

Kuna tabia ihusuyo wengine ya kukwepa upinzani. Wanaogopa kwenda katika maeneo mapya kwa sababu ya giza na mizozo ambayo wanatarajia kukutana nayo. Huu ni woga. Watu wanapaswa kufikiwa pale walipo. Wanahitaji miito ya kuwahamasisha na vitendo, na pia mafundisho, na mahubiri. Agizo lililoungwa mkono na mfano litakuwa na ushawishi mkubwa. {2Tsw 341.1}

Mchungaji mwaminifu hatajifunza kushughulikia raha na urahisi wake, lakini atafanya kazi kwa manufaa ya kondoo. Katika kazi hii kubwa, atasahau ubinafsi; katika kutafuta kwake kondoo aliyepotea hatagundua kuwa yeye mwenyewe amechoka, mwenye baridi, na mwenye njaa. Anakuwa na lengo moja tu: kuokoa kondoo aliyepotea na anayetangatanga kwa gharama yoyote inayoweza kumgharimu yeye mwenyewe. Mshahara wake hautamshawishi katika kazi yake wala kumgeuza kuacha wajibu wake. Amepokea utume wake kutoka kwa MFALME wa mbinguni, na anatarajia tuzo Yake wakati kazi aliyokabidhiwa imefanyika. {2Tsw 341.2}

Wale ambao hushiriki katika shughuli ya ualimu wa shule, hujiandaa kwa kazi hiyo. Wanahitimu wenyewe kwa kuhudhuria shule na kuburudisha akili zao katika masomo. Hawaruhusiwi kufundisha watoto na vijana katika masomo ya sayansi isipokuwa wana uwezo wa kuwafundisha. Baada ya kuomba kazi kama mwalimu, wanapaswa kufaulu mtihani chini ya usimamizi wa watu wenye uwezo. Ni kazi muhimu kushughulika na akili changa na kuwafundisha kwa usahihi katika sayansi. Lakini je, kazi ya huduma ni ya muhimu kiasi gani! Walakini wengi wanajihusisha na shughuli muhimu ya kuwavutia wanaume na wanawake kuingia katika shule ya Kristo, ambapo watajifunza jinsi ya kutengeneza tabia kwa ajili ya mbinguni, ambao wanahitaji kuwa wanafunzi wao wenyewe. Wengine wanaoingia kwenye huduma hawahisi mzigo wa kazi juu wao. Wamepokea maoni yasiyo sahihi ya sifa za mchungaji. Wamefikiria kuwa ilihitaji utafiti wa karibu kidogo sana katika sayansi au katika Neno la Mungu ili kuwa mchungaji. Baadhi ambao wanafundisha Ukweli wa sasa hawazifahamu Biblia zao. Wana upungufu wa maarifa ya Biblia kiasi kwamba ni vigumu kwao kunukuu fungu la Maandiko kwa usahihi kutoka katika kumbukumbu ya vichwani mwao. Kwa kuboronga kijinga kwa namna isiyo ya kawaida, kama wanavyofanya, wanatenda dhambi dhidi ya Mungu. Wanabonda-bonda Maandiko, na kuifanya Biblia iseme mambo ambayo hayajaandikwa humo. {2Tsw 341.3}

Wengine ambao maisha yao yote wameongozwa na hisia wamefikiria kuwa elimu au maarifa kamili ya Maandiko hayakuwa na maana kama

tu walikuwa na Roho. Lakini Mungu kamwe hatumi Roho Wake kuidhinisha ujinga. Wale ambao hawana ufahamu, na ambao wako katika hali ambayo haiwezekani kwao kuipata, Bwana anaweza, na hufanya, huruma na kubariki, na wakati mwingine hujishusha kukamilisha nguvu Zake katika udhaifu wao. Lakini Yeye hufanya kuwa jukumu lao kujifunza Neno Lake. Kukosa maarifa katika sayansi sio kisingizio cha kupuuza kujifunza Biblia; kwa maana Maneno ya uvuvio yako wazi ili wasio na kisomo cha madarasani waweze kuyaelewa. {2Tsw 342.1}

Kati ya watu wote walio juu ya uso wa dunia, wale ambao wanashughulikia Ukweli thabiti kwa nyakati hizi za hatari, wanalazimika kuzielewa Biblia zao na kujizoeza na ushahidi wa imani yetu. Isipokuwa wana ujuzi wa Neno la uzima, hawana haki ya kufanya kazi ya kufundisha wengine njia ya uzima. Wachungaji wanapaswa kutia bidii yote kutia “fadhila ya imani yenu tieni na wema; na katika wema wenu maarifa; na katika maarifa yenu kiasi; na katika kiasi chenu saburi; na katika saburi yenu utauwa; na katika utauwa wenu upendano wa ndugu; na katika upendo wa ndugu upendo.” Baadhi ya wachungaji wetu huhitimu wakati hawajajifunza kanuni ya kwanza ya mafundisho ya Kristo. Wale ambao ni mabalozi wa Kristo, ambao wanasimama kwa niaba Yake, wakiomba sana roho zipatanishwe na Mungu, wanapaswa kuwa na sifa ya kuwasilisha imani yetu kwa akili na kuweza kutoa sababu za tumaini lao kwa upole na hofu. Kristo alisema: “Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” {2Tsw 342.2}

Wachungaji wanaofundisha Ukweli usiopendwa na watu, na ambao ni maarufu, watasumbuliwa na watu ambao wanasukumwa na Shetani na ambao, kama bwana wao, wanaweza kunukuu Maandiko kwa urahisi; na Je, watumishi wa Mungu hawatakuwa sawa na watumishi wa Shetani katika kushughulikia maneno ya Uvuvio? Wanapaswa, kama Kristo, kulinganisha Andiko kwa Andiko. Lo! Walau, kwamba wale wanaohudumu katika vitu vitakatifu wangeamka, na, kama Waberoya waungwana, wayachunguze Maandiko kila siku! Ndugu zangu katika huduma, ninawasihi mjifunze Maandiko kwa maombi ya unyenyekevu

kwa moyo ulio na ufahamu, ili mpate kufundisha njia ya uzima kwa ukamilifu zaidi. Ushauri, sala, na mfano wako lazima uwe harufu ya maisha kwa uzima, vinginevyo huna sifa ya kuwaonyesha wengine njia ya uzima. {2Tsw 343.1}

Bwana anahitaji watumishi Wake wote kuboresha talanta alizowapatia. Lakini je, atahitaji kiasi gani zaidi, kwa wale wanaodai kuielewa njia ya uzima, na ambao huchukua wenyewe jukumu la kuwaongoza wengine humo. Mtume Paulo alimhimiza Timotheo hivi: “Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu, watakaofaa kuwafundisha na wengine.” {2Tsw 343.2}

Matokeo mazuri yenye utukufu, yaliyoambatana na huduma ya wanafunzi waliochaguliwa wa Kristo yalikuwa matokeo ya kuchukua katika miili yao kufa kwa Bwana Yesu. Baadhi ya wale walioshuhudia juu ya Kristo walikuwa watu wasio na elimu na wajinga; lakini neema na Ukweli vilitawala mioyoni mwao, vikiwahamasisha na kuwatakasa maisha, na kudhibiti matendo yao. Walikuwa wawakilishi walio hai wa Akili na Roho ya Kristo. Walikuwa nyaraka zilizo hai, zilizojulikana na kusomwa na watu wote. Walichukiwa na kuteswa na wote ambao hawakupokea Kweli waliyoihubiri, na ambao waliudharau msalaba wa Kristo. {2Tsw 343.3}

Watu waovu hawatapinga aina ya utauwa wala kukataa huduma maarufu ambayo haiwapatii kuubeba msalaba. Moyo wa asili hautaleta pingamizi kubwa katika dini ambayo hakuna kitu cha kumfanya mhalifu wa sheria kutetemeka au kuleta juu ya moyo na dhamiri mbaya, hali halisi ya kuogfya, kuhusu hukumu ijayo. Ni onesho la Roho na nguvu ya Mungu, ambayo huinua upinzani na kusababisha moyo wa asili kuasi. Ukweli unaokoa roho sio tu lazima utoke kwa Mungu; lakini pia Roho Wake lazima ahudhurie kuwasilishwa kwake kwa wengine, vinginevyo huanguka bila nguvu mbele ya ushawishi wa upinzani. Laiti, kama kwamba Ukweli ungeshuka kutoka midomoni mwa watumishi wa Mungu kwa nguvu ile kama ya kuichoma njia yake kuingia kwenye mioyo ya watu! {2Tsw 344.1}

Wachungaji lazima wapatiwe nguvu kutoka juu. Wakati Ukweli katika unyenyekevu wake na nguvu, kama ilivyo katika Yesu, umeletwa dhidi ya roho ya ulimwengu, ukilaani raha zake za kosisimua na mivuto inayoharibu, kisha ndipo itaonekana wazi kuwa hakuna maelewano kati ya Kristo na Shetani. Moyo wa asili hauwezi kutambua mambo ya Roho wa Mungu. Mchungaji asiyejitoa wakfu, akiwasilisha Ukweli kwa njia isiyo na subira, nafsi yake mwenyewe isipoguswa na Ukweli anaouzungumza kwa wengine, itafanya tu madhara. Kila juhudi anayoifanya inashusha kiwango tu. {2Tsw 344.2}

Masilahi ya ubinafsi lazima yamezwe katika shauku kubwa kwa wokovu wa roho. Wachungaji wengine wamewahi kufanya kazi kwa bidii, sio kwa sababu hawakuthubutu kufanya vinginevyo, sio kwa sababu ole ulikuwa juu yao, lakini wakiwa na mtazamo wa mshahara ambao wangepokea. Malaika akasema, “<sup>10</sup>Laiti angekuwapo kwenu mtu mmoja wa kuifunga milango; msije mkawasha moto bure madhabahuni pangu! Sina furaha kwenu, asema Bwana wa majeshi, wala sitakubali dhabihu yoyote mikononi mwenu. <sup>11</sup>Kwa maana tokea maawio ya jua hata machweo yake Jina Langu ni kuu katika Mataifa; na katika kila mahali unatolewa uvumba na dhabihu safi kwa Jina Langu; maana Jina Langu ni kuu katika Mataifa, asema Bwana wa majeshi.” Malaki 1:10 {2Tsw 344.3}

Ni makosa kabisa kujihusisha na kila kibarua kinachofanywa kwa ajili ya Bwana. Hazina ya Bwana imefilisiwa/imekaushwa na wale ambao wamekuwa tu madhara kwa kazi hiyo. Ikiwa wachungaji watajitolea kabisa kwa kazi ya Mungu, na kutumia nguvu zao zote kuijenga kazi Yake, hawatapungukiwa. Kuhusiana na mambo ya kidunia, wana fungu zuri kuliko Bwana wao na bora kuliko wanafunzi wake wateule ambao aliwatuma kumwokoia mtu anayeangamia. Mfano wetu Mkuu, Ambaye alikuwa katika mwangaza wa utukufu wa Baba Yake, alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu. Laana na uwongo vilimfuata. Wanafunzi Wake wateule walikuwa mifano hai ya maisha na roho ya Mwalimu wao. Waliheshimiwa kwa kupigwa viboko na kufungwa; na mwishowe ilikuwa ni sehemu yao kuifunga huduma yao kwa damu yao. {2Tsw 345.1}

Wakati wachungaji wanapopendezwa sana katika kazi wanayoipenda kana kwamba ni sehemu ya kuishi wao, basi wanaweza kusema: “Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa, ya kwamba Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa; tumehesabiwa kama

kondoo wa kuchinjwa. Lakini, katika mambo hayo yote tunashinda na zaidi ya kushindi kwa Yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua kwa hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopita, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kingine chochote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.” {2Tsw 345.2}

“Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtapokea taji ya utukufu, ile isiyokauka.” {2Tsw 345.3}

## SURA YA 51

### KUCHAFUKA KWA MAADILI

Nimeonyeshwa kuwa tunaishi katikati ya hatari za siku za mwisho. Kwa sababu uovu umejaa, upendo wa wengi umepoa. Neno "wengi" linamaanisha wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Wanaathiriwa na uovu unaotawala na wanarudi nyuma kutoka kwa Mungu, lakini sio lazima kwamba waathiriwe kwa namna hii. Sababu ya uharibifu huu ni kwamba hawajasimama wazi, kinyume na uovu huu. Ukweli kwamba upendo wao kwa Mungu unapoa kwa sababu uovu uliokithiri unaonesha kuwa, kwa namna fulani, wanashiriki katika uovu huu, vinginevyo usingeathiri upendo wao kwa Mungu na ari na bidii yao katika kusudi Lake. {2Tsw 346.1}

Picha mbaya ya hali ya ulimwengu imewasilishwa mbele yangu. Uovu umejaa kila mahali. Uchafu wa ngono ndiyo dhambi maalum ya zama hizi. Kamwe uovu haukuinua kichwa chake kilichoharibiwa na ujasiri kama sasa. Watu wanaonekana kufa ganzi, na wapenda ubinadamu na wema wa Kweli wanakaribia kukatishwa tamaa na ujasiri wake, nguvu,



na kuenea kwake. Uovu ambao umeenea sio tu kuwa umefungwa kwa asiyeamini na mwenye dhihaka. Kama mambo yangelikuwa hivyo, ingekuwa nafuu, lakini sivyo. Wanaume na wanawake wengi wanaokiri dini ya Kristo wana hatia. Hata wengine wanaodai kusubiria ujio Wake, hawajajiandaa kwa tukio hilo kuliko hata Shetani mwenyewe. Hawajisafi wenyewe kutokana na uharibifu huo. Kwa muda mrefu wamehudumia tamaa zao kiasi kwamba ni kawaida kwa mawazo yao kuwa najisi na fikra zao huharibika-huwa na ufisadi. Haiwezekani kusababisha akili zao kukaa juu ya mambo safi na matakatifu kama ambavyo ingekuwa kazi kugeuza mkondo wa Maporomoko ya maji ya mto Niagara yanayoshuka chini huko Canada, yageuke na kupeleka maji yake kwenda juu. {2Tsw 346.2}

Vijana na watoto wa jinsia zote mbili, wanajihusisha na uchafuzi wa maadili, na hufanya machukizo haya, maovu yaharibuyo roho—na—mwili (masturbation vice-punyeto, ponografia nk). Wengi wanaodai kuwa Wakristo wamepumbazwa sana na mazoea yale yale kiasi kwamba busara za maadili yao haziwezi kuamshwa kuelewa kuwa ni dhambi, na kwamba ikiwa itaendelezwa, matokeo yake ya uhakika yatakuwa ni uharibifu kabisa wa mwili na akili. Mwanadamu, kiumbe bora zaidi duniani, aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, anajigeuza kabisa na kuwa mnyama! Anajifanya mwenyewe kuwa mbaya zaidi na fisadi. Kila Mkristo atalazimika kujifunza kuzuia tamaa zake na kudhibitiwa na kanuni. Asipofanya hivi hastahili kuitwa kwa Jina la Mkristo/Kikristo. {2Tsw 347.1}

Wengine ambao hukiri kwa ukuu kuhusu Imani, hawaelewi dhambi ya kupiga punyeto, kujinyanyasa wenyewe (masturbation) na matokeo yake ya uhakika. Tabia iliyoanzishwa muda mrefu imepofusha ufahamu wao. Hawatambui uzito mkubwa wa dhambi hii, dhambi inayodhalilisha, ambayo inanyonya nguvu kwenye mfumo na kuharibu nguvu zao za neva za ubongo. Kanuni za maadili ni dhaifu sana wakati zinapopambana na tabia iliyoanzishwa na kuimarishwa. Ujumbe maalum kutoka mbinguni hauwezi kulazimisha moyo kwa nguvu ambao haujaimarishwa dhidi ya uovu wa tabia hii mbaya. Mishipa muhimu ya ubongo imepoteza afya/tuni yao nzuri na msisimko mbaya ili kukidhi hamu isiyo ya asili ya ashiki ya mwili. Mishipa ya fahamu ya

ubongo ambayo huwasiliana na mfumo mzima ndio chombo pekee ambacho Mbingu zinaweza kuwasiliana na mwanadamu na kuathiri maisha yake ya ndani. Chochote kinachosumbua mzunguko wa mikondo ya umeme katika mfumo wa neva, hupunguza nguvu za uwezo muhimu sana, na matokeo yake ni kuangamiza hisia za akili. Kwa kuzingatia ukweli huu, ni muhimu kwa kiasi gani basi, kwamba wachungaji na watu wanaokiri utauwa, wanapaswa kusimama wazi na bila mawaa kutoka kwa roho ya uovu idhalilishayo! {2Tsw 347.2}

Nafsi yangu imeinama chini kwa uchungu kwani nimeonyeshwa hali dhaifu ya watu wanaomkiri Mungu. Uovu umeenea, na upendo wa wengi unapoa. Kuna Wakristo wachache tu wanaolichukulia hili jambo kwa nuru sahihi na ambao wanafanya usimamizi mzuri juu yao wenyewe wakati maoni ya umma na desturi hayawahukumu. Ni wachache kiasi gani, wanaozuia tamaa zao kwa sababu wanahisi wanawajibika kufanya hivyo na kwa sababu hofu ya Mungu ipo mbele ya macho yao! Vitivo vya juu vya mwanadamu vimetawaliwa na hamu ya vyakula na tamaa mbaya. {2Tsw 347.3}

Wengine watatambua uovu wa kuendekeza dhambi, lakini bado watajitetea na kutoa udhuru kwa kusema kwamba hawawezi kushinda tamaa zao. Huu ni ukubali mbaya sana kwa mtu yeyote kufanya ambaye anamtaja Kristo. Hebu “Kila mtu alitajaye Jina la Bwana na auache uovu.” Kwanini udhaifu huu? Ni kwa sababu mwelekeo wa tamaa wanyama umeimarishwa kwa kujizoesha hivi mpaka umepata kuongezeka dhidi ya mamlaka ya juu. Wanaume na wanawake hawana kanuni. Wanakufa kiroho kwa sababu kwa muda mrefu wamekuwa wakiendekeza shauku zao za asili kiasi kwamba nguvu zao za kujitawala zinaonekana zimehama. Tamaa za chini za asili yao zimeshika hatamu, na kile kinachopaswa kuwa nguvu ya kutawala kimekuwa mtumishi wa shauku ya ufisadi. Nafsi inashikiliwa katika utumwa wa chini kabisa. Kupenda anasa zihusianazo na ngono chafu kumezima hamu ya utakatifu na kufanya mafanikio ya kiroho kunyauka. {2Tsw 348.1}

Nafsi yangu inaomboleza kwa ajili ya vijana ambao wanajifunza tabia katika kizazi hiki kilichopotoka. Natetemeka kwa ajili yao wazazi pia;

kwani nimeonyeshwa kama jambo la jumla kuwa hawaelewi majukumu yao ya kuwalea watoto wao katika njia iwapasayo. Mila na mitindo hupewa kipaumbele, na watoto hawachukui muda kujifunza, nao kuyumbishwa na haya na kuharibiwa; wakati wazazi wao wanaojifurahisha wao wenyewe wamepoozeshwa na wamelala kwa hatari yao. Lakini ni vijana wachache sana walio huru dhidi ya tabia mbaya. Wanatolewa udhuru wasifanye mazoezi ya mwili kwa kiwango kikubwa kwa hofu kuwa watafanya kazi kupita kiasi. Wazazi hubeba mzigo wao wenyewe ambao watoto wao wanapaswa kuubeba. Kufanya kazi kupita kiasi ni vibaya, lakini matokeo ya uvivu ni ya kutisha zaidi ya kazi zinazopitiliza. Uvivu husababisha kupendelea tabia mbaya. Kuwa na bidii katika kazi hakuchoshi na kumaliza hata sehemu ya moja ya tano [1/5] kama vile tabia mbaya ya kujinyanyasa. Ikiwa kazi rahisi, iliyoratibiwa vizuri huwachosha watoto wako, kwa uhakika, wazazi, kuna kitu, kando na kazi yao, ambacho hudhoofisha mifumo yao na kutoa hali ya kuchoka kila wakati. Wape watoto wako kazi za mikono ambazo zitawasaidia kufanyia mazoezi ya mishipa na misuli. Uchovu utakaotokana na kazi kama hiyo utapunguza mwelekeo wao wa kujiingiza katika tabia za uovu. Uvivu ni laana. Unazalisha tabia za ngono chafu na haramu, ulevu na ufisadi [licentiousness-ukosefu maadili, kujizuia tabia chafu, mwenendo usio na aibu, na kutotii sheria za Mungu kimakusudi, ambazo mara nyingi hujulikana kwa kujifurahisha kingono bila kizuizi, uasherati, na uasi-sheria.]. {2Tsw 348.2}

Kesi nyingi zimewasilishwa mbele yangu, na kwa kuwa nimekuwa na fununu ya maisha yao ya ndani, roho yangu imekuwa ikiumizwa na kuchukizwa na mioyo iliyooza ya wanadamu wanaokiri utauwa na wanazungumzia kuhamishiwa kwenda mbinguni siku moja. Nimekuwa nikijiuliza mara kwa mara: Je, ni nani ninayeweza kumwamini? Ni nani asiye na uovu? {2Tsw 349.1}

Mimi na mume wangu tumewahi kuhudhuria mkutano ambapo huruma zetu ziliguswa kwa ajili ya ndugu ambaye alikuwa mgonjwa sana wa mapafu, kifua kikuu [phthisic]. Alikuwa amebadilika ngozi na aliyekonda. Akasihi watu wa Mungu wamwombee. Alisema kuwa familia yake ilikuwa inaumwa na kwamba alikuwa amefiwa na mtoto. Alizungumza

kwa hisia za kufiwa. Akasema kuwa alikuwa akingojea kwa muda kuonana na Ndugu na Dada White. Alikuwa akiamini kwamba ikiwa wangemwombea atapona. Baada ya mkutano kufungwa, ndugu walitutaka tulizingatie ombi hilo. Walisema kwamba kanisa lilikuwa likiwasaidia; kwamba mkewe alikuwa mgonjwa, na mtoto wake alikuwa amekufa. Ndugu walikuwa wamekutana nyumbani kwake, na waliungana katika kuiombea familia iliyokuwa inataabika. Sisi tulikuwa tumechoka sana, na tulikuwa na mzigo wa kazi juu yetu wakati wa mkutano, na tulitoa udhuru kwamba hatungeweza kuunga nao. {2Tsw 349.2}

Nilikuwa nimeamua kutokujihusisha katika kumwombea mtu yeyote isipokuwa pale tu Roho wa Bwana aagize jambo hilo. Nilikuwa nimeonyeshwa kuwa kulikuwa na uovu mwingi umeenea, hata kati ya wale wanaodai kuwa watunza Sabato, kiasi kwamba sikutaka kuungana katika maombi kwa ajili ya wale wale ambao sikuijua historia yao. Nilieleza sababu yangu. Nilihakikishiwa na ndugu kwamba, kwa kadiri ya walivyomjua mtu huyu, alikuwa ndugu anayetstahili. Nilizungumza maneno machache na yule ambaye alikuwa ametoa maombi kwa niaba yetu ili apate kuponywa, lakini sikuweza kujisikia huru. Yule ndugu aliyeugua alilia, na akasema kwamba alikuwa akitungojea tuje, na alihisi kuwa na hakika kwamba ikiwa tutamuombea basi atapona. Tulimwambia kuwa sisi hatukuwa tukiyajua maisha yake, kwamba tungependa wale wanaomjua wamuombee. Yeye alituomba sana kwa bidii sana kiasi kwamba tuliambia kuzingatia suala lake na kuahidi kuliwasilisha mbele ya Bwana usiku ule; na kama njia itafunguliwa, tutalichukua ombi lake. {2Tsw 349.3}

Usiku huo tulipiga magoti kuomba na tuliwakilisha hoja yake mbele za Bwana. Tuliomba kwamba tuweze kujua mapenzi ya Mungu kumhusu. Yote tuliyotamani ni kwamba Mungu atukuzwe. Je! Bwana angependa tumuombee mtu huyu aliyesumbuliwa? Tuliacha mzigo kwa Bwana na tulienda kupumzika. Katika ndoto suala la mtu huyo liliwasilishwa wazi. Mambo yake kutoka utoto wake yalionyeshwa, na kuwa ikiwa sisi tutaomba Bwana hatatusikia; kwa maana aliwaza uovu moyoni mwake. Asubuhi iliyofuata yule mtu alikuja tumuombee. Tulimchukua kando na

kumwambia tunasikitika kulazimishwa kukataa ombi lake. Nilielezea ndoto yangu, ambayo alikubali kuwa ni kweli. Alikuwa akipiga ponografia/punyeto kutoka utoto wake, na alikuwa akiendelea na mazoea hayo wakati wa maisha yake ya ndoa, lakini akasema atajaribu kujikwamua dhidi ya hili. {2Tsw 350.1}

Mtu huyu alikuwa na tabia ya muda mrefu aliyohitaji kuishinda. Alikuwa katika umri wa kati wa utu uzima. Viwango vyake vya kimaadili vilikuwa dhaifu sana kiasi kwamba wakati vilipoletwa kupambana na tabia kuendekeza nafsi vilivyowekwa zamani, naye aliendelea kushindwa na hii dhambi. Tamaa mbovu za maadili za kuelekea chini, zilikuwa zimechukua nafasi ya juu zaidi ya asili ya utu-wema. Nilimuuliza kuhusiana na matengenezo ya kiafya. Alisema hawezi kuyaishi. Mkewe alitupa unga usiokobolewa nje ya milango ya nyumba, ikiwa ungeletwa ndani ya nyumba. Familia hii ilikuwa imesaidiwa na kanisa. Maombi yalikuwa pia yakitolewa kwa niaba yao. Mtoto wao alikuwa amekufa na mkewe alikuwa mgonjwa, na mume na baba wakaacha kesi yake juu yetu ili tumlete mbele ya Mungu Aliye safi na Mtakatifu, ili aweze kufanya muujiza na amponye. Hisia za maadili za mtu huyu zilikuwa zimekufa ganzi. {2Tsw 350.2}

Wakati vijana wanachukua mazoea mabaya wakati roho ni laini, hawatawahi kupata nguvu kabisa na kwa usahihi kukuza tabia ya kimwili, kiakili, na kimaadili. Hapa kulikuwa na mtu aliyejidhalilisha kila siku (punyeto/ponografia), na bado akathubutu kujitosa mbele za Mungu na kuomba nyongeza ya nguvu ambayo alikuwa nayo na kuitumia ovyo ovyo, na ambayo, ikiwa atapewa, ataitumia katika tamaa yake. Uvumilivu gani anao Mungu! Ikiwa Yeye anapaswa kumshughulikia mwanadamu kulingana na njia zake mbaya, ni nani angeweza kuishi mbele zake? Je! Ingekuwaje kama tungekuwa hatuna tahadhari na kubeba kesi ya mtu huyu mbele ya Mungu wakati alikuwa akifanya uovu, je, Bwana angesikia? Je, Angekuwa amejibu? “Maana Wewe si Mungu upendezwaye na mabaya; Mtu mwovu hatakaa Kwako; Wajivunao hawatasimama mbele ya macho Yako; Unawachukia wote watendao ubatili.” “Kama ningaliwaza uovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia.” {2Tsw 351.1}

Hii sio kesi moja peke yake. Hata uhusiano wa ndoa haukutosha kumlinda mtu huyu kutoka kwa tabia za uovu za ujana wake. Natamani ningeshawishiwa kuwa kesi kama hizi nilizowasilisha ni nadra, lakini najua ni za mara kwa mara. Watoto wanaozaliwa na wazazi ambao wanatawaliwa na tamaa mbaya hawana thamani. Ni nini kinachoweza kutarajiwa kwa watoto kama hao isipokuwa kushuka chini kwa kiwango kuliko wazazi wao? Je, ni nini kinachoweza kutarajiwa kwa kizazi kinachoinuka? Maelfu hawana kanuni. Hawa ndio hasa huwaambukiza watoto wao tamaa zao zenye kusikitisha, zenye ufidadi. Urithi ulioje! Maelfu huburuza nje maisha yao yasiyokuwa na maadili, na kanuni, yakichafua washirika wao, na kuendeleza tamaa zao mbaya na kuambukiza/kurithisha kwa watoto wao. Wanachukua jukumu la kuwapatia watoto, muhuri wa tabia yao wenyewe. {2Tsw 351.2}

Ninakuja tena kwa Wakristo. Ikiwa wote wanaokiri kuitii sheria ya Mungu, watakuwa huru kutokana na uovu, roho yangu ingefarijika na kupata afueni kutoka kwa kifungo; lakini sio. Hata wengine wanaodai kuzishika amri zote za Mungu wana hatia ya dhambi ya uzinzi/ngono. Je, ninaweza kusema nini kuamsha hisia zao zilizopooza? Kanuni za maadili, zinazotendwa kwa uangalifu, zinakuwa kinga ya pekee ya roho. Ikiwa kuna wakati ambao chakula kilipaswa kuwa cha aina rahisi zaidi, ni sasa. Nyama haipaswi kuwekwa mbele ya watoto wetu. Ushawishi wake ni kulisimua na kuimarisha mazoea mabaya, maadili yaendayo chini, na ina tabia ya kuua nguvu za maadili. Nafaka na matunda yaliyotengenezwa bila mafuta ya wanyama, na katika hali ya asili iwezekanavyo, vyapaswa kuwa chakula cha meza za wote wanaodai wanajiandaa kwa kubadilishwa kwenda mbinguni. Chakula kisichotiwa vitu vingi vya kulisimua mwili, kinasaidia zaidi kwa tamaa kuweza kudhibitiwa kwa urahisi. Kuridhisha ulimi kwa utamu wa ladha hakupaswi kuzingatiwa bila kujali afya ya mwili, akili, au maadili. {2Tsw 352.1}

Kuendekeza mazoea mabaya kutaongoza wengi kufunga macho yao katika nuru, kwani wanaogopa kuwa wataona dhambi ambazo hawako tayari kuziacha. Wote wanaweza kuona ikiwa watafanya hivyo. Ikiwa watachagua giza badala ya nuru, uhalifu wao hautakuwa mdogo. Kwa nini wanaume na wanawake wasisome, na kujipatia akili mahiri juu ya

vitu hivi vinavyoathiri sana nguvu zao za kimwili, kiakili na za kimaadili kimakusudi hivi? Mungu amekupa wewe makao ya kutunza na kuhifadhi katika hali bora kwa huduma na utukufu Wake. Miili yenu sio yenu wenyewe. “Au Hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika roho zenu, ambazo ni mali ya Mungu.” “Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.” {2Tsw 352.2}

## **SURA YA 52**

### **KUWA NA KIASI KWA MKRISTO**

(Imewasilishwa Katika Mji Wa Battle Creek, Machi 6, 1869 Na Kuripotiwa na Uirah Smith)

“Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, Mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu” 1 Wakorintho 6:19, 20. {2Tsw 354.1}

Sisi sio mali yetu wenyewe. Tumenunuliwa kwa thamani kubwa, hata kudhihirishwa kwa mateso na kifo cha Mwana wa Mungu. Ikiwa tungeweza kuelewa hili, na kulitambua kikamilifu, tungepata hisia ya majukumu muhimu yaliyo juu yetu yanayotuhitaji kujiweka katika hali bora kabisa ya afya, ili tuweze kumpa Mungu huduma kamilifu. Lakini tunapochukua njia yoyote tu ambayo inapunguza nguvu zetu, au inadhofisha nguvu zetu, na kuleta ukungu akilini mwetu, basi hatumtukuzi katika miili na roho zetu ambazo ni Zake, bali tunafanya kosa kubwa mbele Zake. {2Tsw 354.2}

Je! Yesu amejitoa kwa ajili yetu? Je! Gharama kubwa imelipwa ili kutukomboa sisi? Je, si hivyo basi, kwamba sisi sio mali yetu wenyewe? Je! Ni kweli kwamba nguvu zote za uhai wetu, miili yetu, roho zetu, vyote tulivyo navyo na tulivyo, ni mali ya Mungu? Kwa kweli ni hivyo. Na tunapogundua hili, ni wajibu mkubwa kiasi gani unaotuangukia kujinyekekeza kwa Mungu ili Aweze kutuhifadhi katika hali hiyo ili tumtukuze Yeye hapa duniani kwa miili yetu na katika roho zetu ambazo ni Zake. {2Tsw 354.3}

Tunaamini pasipo shaka, kwamba Kristo anakuja hivi karibuni. Hii sio hekaya kwetu; ni jambo halisi. Hatuna shaka, wala hatukuwa na shaka kwa miaka, Mafundisho ambayo tunayo leo ni Ukweli wa leo na kwamba tunakaribia hukumu. Tunajiandaa kukutana na Yeye ambaye, atasindikizwa na mkusanyiko wa malaika watakatifu, akitokea katika mawingu kutoka mbinguni kuwapa waaminifu na wenye haki mguso wa kutokufa. Anapokuja haji kutusafisha dhambi zetu na kuondoa mapungufu yetu, kutuponya udhaifu wa hasira na tabia zetu. Ikiwa imefanyika kwetu hakika, basi kazi hii yote itamalizika kabla ya wakati huo. Wakati Bwana atakapokuja, wale walio watakatifu watakuwa watakatifu bado. Wale ambao wamehifadhi miili yao na roho zao katika utakatifu, utakaso na heshima, basi watapokea mguso huo wa mwisho wa kutokufa. Lakini wale wasio na haki, wasiotakaswa, na wachafu watabaki hivyo milele. Hakuna kazi itakayofanyika kwao ili kuondoa mapungufu yao na kuwapa tabia takatifu. Msafishaji basi hakai kufuata mchakato wake wa kusafisha na kuondoa dhambi zao na ufisadi wao. Haya yote yanapaswa kufanyika katika kipindi hiki cha rehema. Ni Sasa hivi ambapo kazi hii inapaswa kutimizwa kwetu. {2Tsw 355.1}

Tunakumbatia Ukweli wa Mungu kwa mitizamo yetu tofauti, na tunapokuwa chini ya ushawishi wa Ukweli huo, itatimiza kazi hiyo kwetu ambayo ni muhimu kutupatia usawa wa maadili kwa ufalme wa utukufu na jamii ya malaika mbinguni. Sasa tuko kwenye karakana ya Mungu. Wengi wetu ni mawe yasiyo laini kutoka kwenye machimbo. Lakini tunaposhikilia Ukweli wa Mungu, mvuto Wake unatuathiri. Ukweli unatuinua na unatuondolea kila dhambi na kutostahili kwetu kwa aina yeyote. Hivyo tunaandaliwa kumwona Mfalme katika uzuri



Wake, na mwishowe kuungana na malaika wakamilifu wa mbinguni katika ufalme wa utukufu. Ni hapa duniani, ndiyo kazi hii inapaswa kutimizwa kwa ajili yetu, hapa ndiyo miili na roho zetu zinajitayarisha kuvalishwa kutokufa. {2Tsw 355.2}

Tuko katika ulimwengu ambao unapingana na haki na usafi wa tabia, na ukuaji wa neema. Popote tunapoangalia tunaona ufisadi na unajisi, ulemavu na dhambi. Je! Ni kazi gani tunayopaswa kufanya kabla ya kuvishwa kutokufa? Ni kuhifadhi miili yetu kwa utakatifu, usafi wa roho, ili tuweze kusimama bila mawaa mahali ambapo panafuka uharibifu uliokithiri karibu nasi katika siku hizi za mwisho. Na ikiwa kazi hii haijamalizika tunahitajika kuifanya mara moja, kwa moyo wote na kwa uelewa. Ubinafsi haupaswi kuja hapa kutushawishi. Roho wa Mungu anapaswa kuwa na udhibiti kamili juu yetu, akiwa mshawishi wa matendo yetu yote. Ikiwa tunapata mguso wa mbingu inavyotakiwa, na kushika nguvu inayotakiwa ya kutoka juu mbinguni, tutahisi ushawishi wa utakaso wa Roho wa Mungu juu ya mioyo yetu. {2Tsw 356.1}

Wakati tumejaribu kuwasilisha matengenezo ya afya kwa ndugu na dada zetu, na tumezungumza nao juu ya umuhimu wa kula na kunywa na kufanya yote wanayofanya kwa utukufu wa Mungu, wengi kwa matendo yao wamesema: "Sio shuguli yako kunipangia kwamba nile hivi au vile. Chochote tutakachofanya ni sisi wenyewe tutabeba athari zake." (msituingilie, ninyi sio mabosi wetu) Wapendwa, mmekosea sana. Sio nyinyi tu mnaoumia mkienda njia isiyo sahihi. Jamii mnayoishi inabeba matokeo ya makosa yenu, kwa kiwango kikubwa, na vile vile ninyi wenyewe. Ikiwa unateseka na kutokuwa na kiasi kwako kwa kula au kunywa, sisi ambao tuko karibu nawe au tunaoshirikiana nawe tunashiriki nawe na tunaathiriwa na udhaifu wako pia. Tunalazimika kuteseka kwa sababu ya mwenendo wako mbaya. Ikiwa ipo hali inayopunguza nguvu zako za akili au mwili, wakati tupo katika jamii yako, nasi tunaathiriwa nayo. Ikiwa, badala ya kuwa na uchangamfu wa roho, wewe ni mwenye huzuni, unawapa wengine kivuli cha roho hiyo wale wanaokuzunguka. Ikiwa tuna huzuni, sonona, na wenye matatizo nawe u katika hali nzuri kiafya, utakuwa na akili zako shwari za kutuonyesha njia ya kutoka shimo hilo kwa kuzungumza maneno ya kutufariji. Lakini ikiwa ubongo wako

umesumbuliwa na kutiwa ganzi sana na njia zako mbaya ya maisha kiasi kwamba huwezi kutupa ushauri mzuri, Je! Hatupotezi nasi hapo? Je, Ushawishi wako hautuathiri sana? Tunaweza kuwa na kiwango kizuri cha kujiamini katika maamuzi yetu wenyewe, lakini tunataka kuwa na washauri; kwani "washauri wengi hufanya ushindi uwe wa hakika." Tunatamani mienendo yetu ionekane yenye mwendelezo kwa wale tunaowapenda, na tunataka kutafuta ushauri wao na kuwa na uwezo wa kuwapa mawazo yetu kwa uwazi. Lakini tunajali nini kupata uamuzi wako, ikiwa nguvu yako ya neva ya ubongo imechoshwa sana, na nguvu zimeondolewa kutoka kwa ubongo ili kushugulikia chakula kibaya kilichowekwa ndani ya tumbo lako, au hata kushugulikia chakula kilichorundikana na chenye afya? Tutajali nini kwa mashauri ya watu kama hawa? Wanaona kupitia mrundikano wa chakula kisichoyeyushwa. Kwa hivyo mtindo wako wa maisha unatuathiri. Haiwezekani kwako wewe kufuata mwenendo wowote mbaya bila kusababisha wengine kuteseka. {2Tsw 356.2}

"Je, hamjui kwamba katika mashindano ya mbio wote wanaoshindana hukimbia, lakini ni mmoja wao tu apewaye tuzo? Kwa hiyo kimbieni katika mashindano kwa jinsi ambavyo mtapata tuzo. Kila mmoja anayeshiriki katika mashindano hufanya mazoezi makali. Wao hufanya hivyo ili wapokee taji isiyodumu, lakini sisi tunafanya hivyo ili kupata taji idumuyo milele. Kwa hiyo mimi sikimbii kama mtu akimbiaye bila lengo, sipigani kama mtu anayepiga hewa, la, bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha ili nikiisha kuwahubiria wengine, mimi nisiwe mtu wa kukataliwa." Wale ambao walishiriki mbio ili kupata tuzo ya maua ambayo ilichukuliwa kuwa na heshima maalum walikuwa wenye kiasi katika mambo yote ili misuli yao, akili zao, na kila sehemu yao iwe katika hali nzuri zaidi kwa kukimbia. Ikiwa hawangekuwa na kiasi katika vitu vyote, wasingekuwa na unyumbulifu huo ambao walipaswa kuwa nao kama wangekuwa bila kiasi. Wakiwa na kiasi, wangeweza kukimbia mbio hizo kwa mafanikio zaidi; walikuwa na hakika zaidi ya kupokea taji.{2Tsw 357.1}

Lakini pamoja na kujizuia kwao, - juhudi zao zote za kujipatia lishe bora ili kuwa katika hali nzuri, wale waliokimbia mbio za kidunia walikimbia ili mradi tu. Wangeweza kufanya kadri wawezavyo, na hata hivyo baada

ya yote kutopokea tuzo ya heshima; kwani mwingine anaweza kuwa mbele yao kidogo, na achukue tuzo. Ni mmoja tu aliyepokea tuzo. Lakini katika mbio za mbinguni tunaweza sote kukimbia na wote kupata tuzo. Hakuna kutokuwa na uhakika, hakuna hatari ya kutoweza, katika suala hilo. Lazima tuvae neema za mbinguni, na, jicho kuelekezwa juu kwenye taji ya kutokufa, daima tuweke mfano huu mbele yetu. Yeye Alikuwa mtu wa huzuni na anayejua masikitiko. Maisha ya unyenyekevu, ya kujikana-nafsi ya Bwana wetu wa mbinguni tunapaswa kuyatilia maanani kila wakati. Halafu tunapotafuta kufanana Naye, tukikazia macho alama ya ushindi, tunaweza kukimbia mbio hii kwa hakika, tukijua kwamba ikiwa tutafanya kadiri tuwezavyo, hakika tutapata tuzo. {2Tsw 358.1}

Watu wanaweza kujikana nafsi na kuwa na nidhamu ili kukimbia na kupata taji inayoharibika, ile ambayo ingeangamia kwa siku moja (taji la maua-laurel), na ambayo ilikuwa tu ishara ya heshima kutoka kwa wanadamu hapa. Lakini tunapaswa kukimbia mbio, ambayo mwisho wake ni taji la kutokufa na uzima wa milele. Ndio, inapita yote na uzito wa utukufu wa milele utatunukiwa kwetu kama tuzo wakati mbio zimeendeshwa. "Sisi," anasema mtume, "tutakuwa tusioharibika." Na ikiwa wale walioshiriki katika mbio hizi hapa duniani kwa taji ya kidunia wanaweza kuwa na kiasi katika mambo yote, sisi Je? ambao tunaona taji isiyoweza kuharibika, uzani wa milele wa utukufu, na maisha ambayo yanalingana na maisha ya Mungu? Tunapokuwa na motisha hii kuu mbele yetu, je! Hatuwezi "kukimbia kwa uvumilivu mbio iliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu aliye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu"? Yeye Ametuelekeza njia, na akaiwekea alama kote kwa nyayo Zake Mwenyewe. Ni njia ambayo Alisafiri, na tunaweza pia, pamoja Naye, kupata uzoefu wa kukana nafsi na kuteseka, na kutembea katika njia hii iliyo na nyayo za damu Yake Mwenyewe. {2Tsw 358.2}

"Mimi sikimbii pasipo kuwa na lengo. Sipigani kama mtu anayepiga hewa; lakini nauimarisha mwili wangu na kuutawala." Kuna kazi hapa kwa kila mwanamume, mwanamke na mtoto ya kufanya. Shetani anatafuta kila mara kupata udhibiti wa miili yenu na roho zenu. Lakini Kristo amekununua, na wewe ni mali Yake Mwenyewe. Na sasa ni

kwako kufanya kazi kwa umoja na Kristo, kwa umoja na malaika watakatifu wanaokuhudumia. Ni wajibu wako kuuweka mwili wako chini, na kuuleta kujisalimisha kwa utii. Isipokuwa utafanya hivi hakika utapoteza uzima wa milele na taji ya kutokufa. Na bado wengine watasema: "Je! Inamhusu nini mtu mwingine yeyote kile ninachokula au kile ninachokunywa?" Nimekuonyesha jinsi gani njia zako zilivyo na mahusiano na wengine. Umeona kuwa inahusiana sana na ushawishi unaotoa katika familia zenu. Inahusiana sana na kujenga tabia za watoto wako. {2Tsw 359.1}

Kama nilivyosema hapo awali, tunaishi katika kizazi kilichopotoka. Ni wakati ambapo Shetani anaonekana kuwa na udhibiti kamili juu ya akili ambazo hazijawekwa wakfu kwa Mungu. Kwa hivyo kuna jukumu kubwa sana juu ya wazazi na walezi ambao wana watoto wa kuwakuza. Wazazi wamechukua jukumu la kuleta watoto hawa duniani; na sasa wajibu wao ni nini? Je! Ni kuwaruhusu wafanye wanayoweza, na kama vile watakavyotaka? Wacha nikuambie, jukumu zito liko juu ya walezi na wazazi hawa." Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." Je! Unafanya hivi unapoandaa chakula mezani na kuita familia yako kushiriki? Je! Unaweka mbele ya watoto wako chakula kile ambacho unajua tu, kitatengeneza damu bora zaidi? Je! Ni chakula hicho ambacho kitahifadhi mifumo yao ili ipunguze hali za homa homa? Je! Ndio ambayo itawaweka katika uhusiano mzuri sana wa maisha na afya? Je! Hiki ndicho chakula ambacho unajifunza kuweka mbele ya watoto wako? Au wewe, bila kujali faida yao ya baadaye, unawapa chakula kisicho na afya, kinachosisimua na kinachokera? {2Tsw 359.2}

Wacha nikuambie kuwa watoto huzaliwa kwa uovu. Shetani anaonekana kuwa na udhibiti wao. Yeye humiliki akili zao changa wakiwa wadogo, na uharibika. Kwa nini baba na mama hufanya kana kwamba wana uchovu juu yao? Hawaamini kwamba Shetani anapanda mbegu mbaya katika familia zao. Wao ni vipofu na wazembe kuhusu mambo haya kama inavyowezekana kuwa. Kwa nini hawaamki, na kusoma juu ya masomo haya? Anasema mtume Petro: "Jitahidini sana katika imani yenu kuongeza wema; na katika wema, maarifa; katika maarifa, kiasi; katika kiasi, saburi," nk. Hapa kuna kazi ambayo

inayompasa kila mtu anayedai kumfuata Kristo; ni kuishi juu kwa mpango wa kuongezeka. {2Tsw 360.1}

Sura baada ya sura imefunguliwa kwangu. Ninaweza kuchagua familia baada ya familia ya watoto katika nyumba hii, kila mmoja ambaye ni mwovu kama kuzimu yenyewe. Wengine wao hudai kuwa wafuasi wa Kristo, na ninyi, wazazi wao, ni watu wasiojali kana kwamba mmekuwa na mshtuko wa kupooza. {2Tsw 360.2}

Nimesema kwamba wengi wenu ni wabinafsi. Hamjaelewa nilichomaanisha. Mmejifunza ni chakula gani kitakuwa na ladha bora kwenu. Ladha na starehe, badala ya utukufu wa Mungu, na hamu ya kusonga mbele katika maisha ya kiroho, na kukamilisha utakatifu katika kumcha Mungu, vimetawala. Umeshauriana na raha yako mwenyewe, hamu yako mwenyewe; na wakati umekuwa ukifanya hivi, Shetani amekuwa akikuandama juu yako na, kama ilivyo kawaida, amekukatisha tamaa katika juhudi zako kila wakati. {2Tsw 360.3}

Baadhi yenu wakina baba mmewapeleka watoto wenu kwa tabibu ili aone wana shida gani. Ningekuambia katika dakika mbili shida ni nini. Watoto wako wamepotoka. Shetani amepata udhibiti wao. Amekuja nyuma yako, wakati wewe, ambaye ni kama Mungu kwao, wa kuwalinda, ulikuwa umejisahau, umeshikwa na usingizi, na umelala. Mungu amekuamuru wewe kuwalea katika hofu na malezi ya Bwana. Lakini Shetani amepita mbele yako kabisa na amewafunga kwa kamba ngumu kuwazunguka. Na bado wewe unalala. Hebu Mbingu na ikuhurumie wewe na watoto wako, kwani kila mmoja wenu anahitaji huruma Yake Bwana. {2Tsw 360.4}

Ikiwa ungechukua msimamo wako juu ya matengenezo ya afya; kama ungeongeza imani yako, wema kwa wema, maarifa kwa maarifa, kiasi, mambo yangukuwa tofauti. Lakini mmeamshwa kwa sehemu tu kuhusiana uovu na ufiadini ulio ndani ya nyumba zenu. Umefungua macho yako kidogo kisha ukajitayarisha kulala tena. Je! Unafikiri malaika wanaweza kuja katika makao yako? Je! Unafikiri watoto wako wanaegemea kuelekea ushawishi mtakatifu kukiwa na vitu hivi kati yenu? Ninaweza kuhesabu familia baada ya familia ambazo ziko karibu

kabisa chini ya udhibiti wa Shetani. Najua vitu hivi ni Kweli, na ninataka watu waamke kabla ya kuchelewa milele, na damu ya roho, na hata damu ya roho za watoto wao wenyewe, ipatikane kwenye mavazi yao. {2Tsw 361.1}

Akili za baadhi ya watoto hawa zimedhoofika kiasi kwamba wana nusu tu [ $\frac{1}{2}$ ] au theluthi moja [ $\frac{1}{3}$ ] ya busara na akili mahiri, ambayo wangukuwa nayo ikiwa wangukuwa wema na safi. Wameitupa mbali akili kwa kujidhulumu (dhambi za punyeto na ngono chafu). Hapa hapa katika kanisa hili, ufisadi umejaa kila upande. hapa na pale na kuna kuimba, au mkusanyiko fulani wa anasa. Kila wakati ninaposikia juu ya haya, najisikia kama vile nimevaa nguo za magunia. "Laiti kichwa changu kingekuwa maji, na macho yangu kuwa chemchemi ya machozi!" "Waachilie watu Wako, Ee Bwana." Nasikia mfidhaiko. Nina uchungu wa roho ambao unazidi kitu chochote ambacho ninaweza kukuelezea. Umelala fo! fo! fo! Kama umeme na radi za mlima Sinai zingenguruma, Je, zingeliamsha kanisa hili? [Kutoka 19 na 20] Je! Wangewaamsha ninyi, akina baba na mama, kuanza kazi ya matengenezo katika nyumba zenu wenyewe? Mnapaswa kuwa kuwafundisha watoto wako. Unapaswa kuwafundisha jinsi ya kujiepusha na maovu na ufisadi wa wakati huu. Badala ya hivi, wengi wanasoma jinsi ya kupata chakula kizuri. Unaweka mezani mwako siagi, mayai, na nyama, na watoto wako wanakula. Wanalishwa na vitu vile ambavyo vitasisimua tamaa zao za wanyama, halafu mnakuja kwenye mikutano na kumwomba Mungu awabariki na kuokoa watoto wako. Je! Maombi yako yanapaa kwenda juu kwa kiasi gani? Una kazi ya kufanya kwanza. Unaposhugulika kwa watoto wako katika yote yale ambayo Mungu amekukabidhi ufanye, basi unaweza kwa ujasiri kudai msaada maalum ambao Mungu ameahidi kukupa. {2Tsw 361.2}

Unapaswa kujifunza kuhusu kiasi katika mambo yote. Lazima ujifunze juu ya kile unachokula na kile unachokunywa. Na bado unasema: "Haimuhusu mtu yeyote kile ninachokula, au kile ninachokunywa, au kile nachoweka juu ya meza yangu." (it is nobody business what my kids eat) Ni suala linalomhusu mtu mwingine, labda uwachukue watoto wako na kuwafungia ndani, au uende jangwani ambapo hautakuwa mzigo kwa wengine, na ambapo watoto wako wasiotii,

wanaokataa usimamizi na wabaya, hawataharibu jamii wanayojichanganya nayo. {2Tsw 362.1}

Wengi ambao wamepokea matengenezo ya afya, wameacha kila kitu kinachowaumiza, ila kinachofuata kwa sababu wameacha vitu hivi je! sasa wanaweza kula kadri watakavyo? Wao huketi mezani, na badala ya kuzingatia ni kiasi gani wanapaswa kula, wanajitoa kwa hamu ya uroho wa chakula na kula kupita kiasi. Na tumbo halina mpaka wa linaloweza kufanya, au yote inalopaswa kufanya, siku hiyo basi, litakuwa na wasiwasi kuhusu mzigo uliowekwa ndani yake. Chakula chote kinachowekwa ndani ya tumbo, ambacho mfumo hauwezi kuchakata faida, ni mzigo kwa viungo katika kazi yake. Kinapunguza ufanisi wa mashine hii hai. Mfumo umeshindiliwa na unaziba na hauwezi kufanikiwa kutekeleza kazi yake kwa mafanikio. Viungo muhimu vinachoshwa bila ya sababu, na nguvu ya neva ya ubongo huitwa tumboni kusaidia viungo vya mmeng'enyo kuendelea na kazi yao ya kujaribu kukitoa chakula ambacho hakina manufaa kwenye mwili. {2Tsw 362.2}

Kwa hivyo nguvu ya ubongo hupunguzwa kwa kuchoka sana kwa ajili ya kusaidia tumbo lililolemewa na mzigo wake mzito. Na baada ya kumaliza kazi, ni hisia gani zinazopatikana kama matokeo ya matumizi haya ya lazima ya nguvu hizi muhimu? Hisia ya mchoko wa njaa, kuzimia, na kujihisi kwamba ni lazima ule zaidi. Pengine hisia hii inakuja kabla tu ya wakati wa chakula. Ni kwasababu gani hii huja? Mwili unakuwa na wasiwasi kulingana na kazi yake na unakuwa umechoka kabisa. Nawe unafikiria kuwa tumbo linasema, "Nataka chakula zaidi," wakati, katika kuzimia kwake linasema wazi, "Naomba kupumzika." {2T 363.1}

Tumbo linahitaji kupumzika ili kukusanya nguvu zake zilizochoka kwa kazi nyingine. Lakini, badala ya kuliruhusu kipindi chote cha kupumzika, unafikiri linahitaji chakula zaidi, na kwa hivyo unaongeza mzigo mwingine kwenye mwili, na kulikatalia mapumziko yanayohitajika. Ni kama mtu anayefanya kazi shambani mwanzoni mwa siku mpaka anachoka. Anarudi saa sita mchana na kusema kuwa amechoka na ana uchovu, lakini wewe unamwambia aende kufanya kazi tena na

atapata afueni. Hivi ndivyo unalitendea tumbo lako. Limechoka kabisa. Lakini badala ya kuliruhusu lipumzike, unalipa chakula zaidi, na kisha unaita nguvu kutoka mifumo mingine kwenda kwenye tumbo, kusaidia katika kazi ya mmeng'enywa wa chakula. {2T 363.2}

Wengi wenu wakati mwingine mmehisi ganzi kwenye bongo zenu. Mmejisiikia kutopendelea kuchukua kazi yoyote ambayo inahitaji bidii ya akili au ya mwili, mpaka mtakapopumzika kutoka mzigo huu uliowekwa kwenye mfumo. Halafu, tena, kuna hali hii ya mchoko mkali (goneness). Lakini mnasema ni chakula zaidi kinachotakiwa, kisha mnaweka mzigo maradufu kwenye tumbo ili lishugulikie. Hata kama uko makini katika ubora wa chakula chako, Je! Unamtukuza Mungu katika mwili wako na roho yako, ambazo ni Zake, kwa kula chakula kingi hivyo? Wale ambao huweka chakula kingi tumboni, na hivyo kuvishikiza viungo, hawangeweza kufahamu Ukweli ikiwa wangesikia haya juu yao. Hawakuweza kuamsha hisia za ubongo ili kutambua thamani ya upatanisho na dhabihu kubwa ambayo imetolewa kwa binadamu aliyeanguka. Haiwezekani kwao kufahamu tuzo kubwa, ya thamani, na utajiri unaopita kiasi ambao umehifadhiwa kwa washindi waaminifu. Sehemu yetu ya “unyama” wa maumbile yetu haipaswi kamwe kuachwa itawale maadili na akili. {2T 363.3}

Je! Kula kupita kiasi kuna athari gani kwa tumbo? Tumbo linakuwa dhaifu, viungo vya mmeng'enywa vinadhooifika, na magonjwa, pamoja na mtiririko wa uovu huletwa kama matokeo. Ikiwa watu walikuwa na ugonjwa hapo awali, huongeza shida juu yao na hupunguza nguvu zao, kila siku wanayoishi. Wanatumia nguvu zao muhimu katika hatua isiyo ya lazima kushugulikia chakula wanachoweka matumboni mwao. Hii ni hali mbaya sana! Tunajua hali inayoitwa kuvimbiwa kwa uzoefu wetu (dyspepsia). Tumekuwa nayo katika familia yetu, na tunahisi kuwa ni ugonjwa wa kuogopwa sana. Wakati mtu anakuwa amevembewa hasa, anakuwa kwenye shida zaidi, kiakili na kimwili; na marafiki zake lazima pia watateseka na kuhangaika, isipokuwa kama hawajali au wasio na ubinadamu. Na je! Utasema: "Nachokula au njia gani nafuata sio suala linalokuhusu wewe"? Je! Kuna mtu yeyote karibu na mtu aliyevimbiwa sana anayeumia? Chukua tu jinsi ambayo itawakera kwa namna fulani. Utaona jinsi walisivyotulia kwa hasira! Wanajisiikia vibaya, na



inaonekana kwao kuwa watoto wao ni wabaya sana. Hawawezi kuzungumza nao kwa utulivu, au, kwa huruma/neema maalum, wafanye vitu kwa utulivu katika familia zao. Wote wanaowazunguka wanaathiriwa na ugonjwa walio nao; wote wanapaswa kuhangaika kutokana na udhaifu wao. Wanaleta vivuli vyenye giza kwa wengine. Basi, Je! Mazoea yako ya kula na kunywa hayaathiri wengine? Hakika yanaathiri. Nawe unapaswa kuwa mwangalifu sana katika kuhifadhi hali bora ya afya ambayo unaweza kumtolea Mungu huduma kamilifu na kufanya jukumu lako katika jamii na kwa familia yako. {2T 364.1}

Lakini hata wanamatengenezo wa afya wanaweza kukosea kwa wingi wa chakula. Wanaweza kula chakula bora kisicho na kipimo. Wengine katika nyumba hii hukosa ubora. Hawajawahi kuchukua hatua thabiti juu ya matengenezo ya afya. Wamechagua kula na kunywa kile walichopenda na wakati walipenda. Wanaumiza mifumo yao kwa njia hii. Sio hivyo tu, bali wanajeruhi familia zao kwa kuweka mezani mwao vyakula vyenye kosisimua mwili ambayo vinaongeza hamu ya kinyama kwa watoto wao na kuwaongoza kutojali sana vitu vya mbinguni. Kwa hivyo wazazi wanaimarisha tabia ya kupenda vyakula vitokanavyo na wanyama, na wanapunguza nguvu za kiroho za watoto wao. Je! Watalazimika kwa kiasi gani kulipa adhabu nzito mwishowe! Na kisha wanashangaa kwamba watoto wao ni dhaifu sana kimaadili! {2T 365.1}

Wazazi hawajawapa watoto wao elimu sahihi. Mara kwa mara hudhihirisha udhaifu uleule unaoonekana kwa watoto. Wanakula vibaya, na hii huwafanya muda wote kulifikiria tumbo na mfumo wa neva kuathirika, na hawana nguvu za kutumia katika mwelekeo mwingine. Hawawezi kudhibiti watoto wao vizuri kwa sababu ya kutokuwa na uvumilivu kwao wenyewe, wala hawawezi kuwafundisha njia sahihi. Mara zingine huwashika kwa ukali na kuwaadhibu kwa kuwapiga makofi kwa hasira. Nimesema kwamba kumtingisha-tingisha mtoto kwa hasira, kutatingisha mapepo wachafu wawili waingie ndani, na kumfukuza pepo mmoja atoke nje. Ikiwa mtoto amekosea, kumtikisatikisa kunazidi kuongezea mambo kuwa mabaya zaidi. Hakumsaidii kujirekebisha au kujisalimisha. Wakati mwili hauko katika hali nzuri, wakati mzunguko umekatika, na mfumo wa nguvu za neva umefanya yote ambayo unaweza ili kushugulikia chakula kibovu au chakula kingi

mno hata kizuri kimeng'enywe vyema, wazazi hawana usimamizi mzuri tena. Hawawezi kuona kitendo na matokeo yake. Hii ndio sababu - katika kila hatua wanayochukua katika familia zao wanaunda shida zaidi kuliko kuponya. Hawaonekani kuelewa na kutafakari madhara na kisababishi chake, na wanaenda kufanya kazi kama vipofu. Wanaonekana kutenda mambo kana kwamba wangemtukuza Mungu haswa kama wangepanya vitu kama watu wasio na ustarabu, wakorofi au washenzi (wildmen), na ikiwa kuna jambo baya litatokea katika familia zao, wangelishugulikia ili kulizima kwa ukali, ujeuri na vurugu. {2T 365.2}

Watoto wetu ni akina nani? Hao ni kaka na dada zetu wadogo tu katika familia ambayo Mungu anaitambua kuwa Yake. Tunashughulika na washiriki wa familia ya Bwana. Na wakati uangalizi wao umewekwa kwetu, tunapaswa kuwa waangalifu kwa kiasi gani katika kuwalea kwa ajili ya Bwana, ili kwamba wakati Bwana atakapokuja tuweze kusema: "Hapa, Bwana, tupo, sisi na watoto ambao umetupa. "Je! Basi tutaweza kusema: Tumejaribu kufanya kazi yetu, na tumejaribu kuifanya vizuri "? {2T 366.1}

Nimewaona akina mama wenye familia kubwa, ambao hawakuweza kuona kazi iliyokuwa karibu tu na njia yao, mbele yao tu hapo, katika familia zao. Walitaka kuwa wamishenari na kufanya kazi kubwa mbali. Walikuwa wakijitafutia nafasi ya juu kwaajili yao wenyewe, ila walipuuzia kushughulika na kazi ya majumbani mwao ambayo Bwana alikuwa amewaachia wafanye. Ni muhimu kiasi gani, kwamba ubongo uwe wazi! Ni muhimu kiasi gani, kwamba mwili uwe huru kwa kadri iwezekanavyo kutokana na magonjwa, ili tuweze kufanya kazi ambayo Mbingu ametuachia tufanye, na kuifanya kwa njia ambayo Mwalimu anaweza kusema: 'Vema, mtumishi mwema na mwaminifu. Umekuwa mwaminifu katika mambo madogo, nitakukabidhi makubwa. Njoo ufurahi pamoja na Bwana wako" Dada zangu, msidharau vitu vichache ambavyo Bwana amewaachia mfanye. Wacha vile mnavyofanya kila siku viwe vitendo vile ambavyo katika siku ya usuluhishi wa mwisho wa hesabu, yaani katika siku ile ya hukumu, hautaajibika kukutana na rekodi iliyowekwa na malaika anayerekodi. {2T 366.2}

Lakini vipi kuhusu lishe duni? Nimezungumzia juu ya umuhimu wa kiwango cha chakula na ubora, kuzingatia sana uwiano wa kanuni za afya. Lakini hatupendekezi chakula chenye lishe haba. Nimeonyeshwa kuwa wengi huchukua maoni yasiyofaa kuhusu matengenezo ya afya na wanatumia lishe duni sana. Wanajikkimu kwa lishe ya bei rahisi, na duni, iliyoandaliwa bila uangalifu au kuzingania lishe ya mfumo wa mwili. Ni muhimu kwamba chakula kiandaliwe kwa uangalifu, ili hamu, isiyopotoka, iweze kufurahia. Kwa sababu sisi kutokana na kanuni tumeacha utumiaji wa nyama, siagi, mikate yenye matunda na viungo (mince pies), viungo (chunguza viungo gani vya kuacha mifano itakuwa siki, pilipili manga, nutmeg, na aina zingine za viungo vinavyokasirisha tumbo), mafuta ya nguruwe, na yale ambayo yanakera tumbo na kuharibu afya, Kamwe isifikiriwe kuwa kile tunachokula kina madhara madogo tu. {2T 367.1}

Kuna wengine wanapitiliza katika lishe yao. Lazima wale kiasi kama hicho na ubora kama huo, na wakite kwa vitu viwili au vitatu. Wanaruhusu vitu vichache tu kuwekwa mbele yao au familia zao kula. Katika kula chakula kidogo, na ambacho sio bora, hawaingizi ndani ya tumbo kile ambacho kitafaa kuujenga mwili. Chakula duni hakiwezi kutengeneza damu nzuri. Mlo usio kamili/duni utaleta upungufu wa chembechembe za kwenye damu. Nitataja kesi ya Dada A. Kesi hiyo iliwasilishwa kwangu kuonyesha ushupavu kupitiliza. Aina mbili za watu ziliwasilishwa mbele yangu: Kwanza, ni wale ambao hawakuishi kutokana na nuru ambayo Mungu alikuwa amewapa. Hawa walianza matengenezo kwa sababu mtu mwingine alifanya hivyo. Hawakuelewa mfumo wao wenyewe binafsi. Kuna wengi wenu ambao hukiri Ukweli, ambao wameupokea kwa sababu mtu mwingine aliupokea, na kwa maisha yao wasingeweza kutoa sababu mwingine alifanya hivyo. Hii ndiyo sababu mtu huyo hawezi kuwa na msimamo, anakuwa dhaifu kama maji. Badala ya kupima nia zako kwa mwangaza wa umilele, badala ya kuwa na maarifa ya kiutendaji ya kanuni zinazosimamia matendo yako yote, badala ya kuchimba chini na kujijengea msingi sahihi, wewe unatembea katika cheche za moto zilizowashwa na mtu mwingine. Na utashindwa katika hili, kwani umeshindwa katika matengenezo ya afya. Sasa, ikiwa ungekuwa unatenda kwa kufuata kanuni, usingefanya hivi. {2T 367.2}

Wengine hawawezi kuguswa moyo na umuhimu wa kula na kunywa kwa utukufu wa Mungu. Kuendekeza hamu ya chakula huathiri katika mahusiano yote ya maisha. Inaonekana katika familia zao, makanisani mwao, katika mikutano ya maombi, na katika mwenendo wa watoto wao. Imekuwa laana ya maisha yao. Huwezi kuwafanya waelewe Ukweli wa siku hizi za mwisho. Mungu ametoa kwa ukarimu riziki na furaha kwa viumbe vyake vyote; na ikiwa sheria Zake hazingevunjwa kamwe, na zote zikitendwa sawasawa na mapenzi ya Mbingu, afya, amani, na furaha ndiyo utakuwa uzoefu, badala ya shida na uovu unaoendelea. {2T 368.1}

Kundi lingine ambalo limeshikilia matengenezo ya afya lina ukali sana. Wanachukua msimamo, kisha husimama kwa ukaidi katika nafasi hiyo, na hutenda karibu kila kitu kwa kupitiliza kiasi/kiwango. Dada A alikuwa mmoja wa hawa. Hakuwa na huruma, upendo na mapenzi kama Bwana wetu wa mbinguni. Haki ndiyo ilikuwa karibia kila kitu ambacho angeweza kuona. Alibeba mzigo zaidi ya Dk Trall. Wagonjwa wake walilazimika hata kumwacha kwa sababu hawakuweza kupata chakula cha kutosha. Mlo wake usio duni, ulio na mapungufu, ulimfanya kupungukiwa damu. {2T 368.2}

Ulaji wa nyama unapunguza ubora wa damu. Pika nyama na viungo, kisha ule na keki na mikate ya kuoka yenye nyama (minced pies) na utakuwa na damu isiyo na ubora. Mwili huwa unachoshwa sana katika kuyeyusha au kukiondoa chakula cha aina hii. Sambusa za nyama (minced pies) ambayo ndani yana vitu kama matunda, nyama za kusaga na siki/achari (pies and pickles), ambazo hazipaswi kupata nafasi ndani ya tumbo la mwanadamu, zitatoa damu duni ya kusikitisha. Na chakula duni, kilichopikwa kwa njia isiyofaa, na kichache, hakiwezi kutengeneza damu nzuri. Nyama na vyakula vya kukaanga kwa mafuta na lishe duni, itatoa matokeo sawa. Minced pies are generally small, baked pastries filled with spiced, dried fruit ("mincemeat") or savory meat in a thick crust, originating from European traditions. Samosas are traditionally deep-fried, triangular pastries with spicy savory fillings (potatoes, meat, peas) originating from South/Western Asia, offering a lighter, crispier texture often accompanied by chutneys {2T 368.3}

Sasa kuhusiana na maziwa na sukari: Ninajua watu ambao wameogopa matengenezo ya afya, na wakasema sitaki kuhusiana na hili jambo, kwa sababu linazungumzia dhidi ya matumizi yaliyopitiliza ya vitu hivi. Mabadiliko yanapaswa kufanywa kwa uangalifu mkubwa, na tunapaswa kusonga kwa uangalifu na kwa busara. Tunataka kuchukua njia hiyo ambayo inakubalika, kwa wanaume na wanawake wenye akili mahiri kote. Kutumia maziwa na sukari kwa kiasi kikubwa ni jambo lenye madhara. Zinaleta uchafu na sumu kwenye mwili. Maziwa hupatikana kutoka kwa Wanyama ambao mara nyingi hawana afya. Wanaweza kuwa na maradhi. Ngombe anaweza kuwa mzima kabisa asubuhi na akafa kabla ya usiku. Hiyo yaonyesha alikuwa mgonjwa asubuhi na maziwa yake yalikuwa na ugonjwa; ila wewe haukujua tu. Ulimwengu wa mifugo waweza kuwa na maradhi. Nyama zina magonjwa. Je! Tunaweza kweli kujua kwamba wanyama walikuwa na afya kamilifu, ningependekeza watu waache maziwa na sukari tele wanazotumia mapema kabla ya nyama. Nyama haileti uharibifu kama ule ambao maziwa na sukari hufanya. Sukari huziba mfumo. Inazuia ufanyaji kazi wa mwili wa mwanadamu. {2T 368.4}

Kulikuwa na kesi moja katika Wilaya ya Montcalm, Michigan, ambayo nitazungumzia. Mtu huyo alionekana vizuri. Mrefu wa futi sita na alikuwa na sura nzuri. Niliitwa kumtembelea katika ugonjwa wake. Nilikuwa nimezungumza naye hapo awali kuhusu mtindo wa maisha yake. "Sipendi macho yako yanavyonitazama," Nilimwambia. Alikuwa akila sukari nyingi. Nikamuuliza kwanini alifanya hivi. Alisema kuwa alikuwa ameacha nyama, na hakujua ni nini kitatoa mbadala wa nyama na sukari. Hakuridhika na chakula chake, kwa sababu tu mkewe hakujua kupika. Baadhi yenu mnawapeleka binti zenu, ambao wamekaribia kuwa wanawake shuleni kujifunza sayansi kabla ya kujua kupika, hili linapaswa kufanywa kwa umuhimu wa kwanza. Hapa kulikuwa na mwanamke ambaye hakujua kupika; hakuwa amejifunza jinsi ya kuandaa chakula chenye afya. Mke na mama huyu alikuwa na upungufu katika nyanja hii muhimu ya elimu; na kwa sababu hiyo, chakula kilichopikwa vibaya, kisichotosheleza na kisicho bora kwa mahitaji ya mwili, kilifanya sukari iliwe bila kipimo, ambayo ilileta hali ya ugonjwa kwenye mwili mzima. Maisha ya mtu huyu yalitolewa

kafara bila sababu kwa upishi mbaya. Nilipokwenda kumwona huyu mgonjwa nilijaribu kuwaambia kwa kadri nilivyoweza kuratibu hali hii, na haikuchukua muda akaanza kupona taratibu. Lakini kwa ujinga alitumia nguvu zake wakati alikuwa dhaifu, alikula kiasi kidogo kisicho na ubora unaofaa, na akaugua tena. Wakati huu hakukuwa na msaada kwake. Mwili wake ulionekana kuwa na mifumo mingi iliyoharibika. Alikufa akiwa mwathirika wa mapishi mabaya. Alijaribu kufanya utumiaji wa sukari uchukue nafasi ya mapishi bora, jambo lililofanya hali kuwa mbaya zaidi. {2T 369.1}

Mara nyingi mimi huketi kwenye meza za ndugu na dada, na huona kwamba wanatumia kiasi kikubwa cha maziwa na sukari. Hizi huziba mfumo wa mwili, hukera viungo vya kumengenywa, na kuathiri ubongo. Chochote kinachozuia mwendo unaotakiwa wa mitambo hai ya mwanadamu, huathiri ubongo moja kwa moja. Na kutokana na nuru niliyopewa, sukari, ikitumiwa sana, ni mbaya zaidi kuliko nyama. Mabadiliko haya yanapaswa kufanywa kwa uangalifu, na mhusika anapaswa kusaidiwa kwa njia ambayo haijaratibiwa kuchukiza na ili kuwafanya wale ambao tungewafundisha na kuwasaidia wasiikatae. {2T 370.1}

Dada zetu mara nyingi hawajui kupika. Kwa wale ningesema: Ningeenda kwa mpishi bora kabisa ambaye angeweza kupatikana nchini, na kubaki pale ikiwa ni lazima kwa wiki kadhaa, hadi nitakapokuwa nimebobeza sanaa hii ya upishi, kuwa mpishi mwenye akili mahiri na mjuzi. Ningesomea hii kozi hata ningekuwa na umri wa miaka arobaini. Ni jukumu lako kujua kupika, na ni jukumu lako kuwafundisha binti zako kupika. Unapowafundisha sanaa ya upishi unawajengea kizuizi ambacho kitawahifadhi na upumbavu na uovu ambao wanaweza kushawishiwa kushiriki. Ninamthamini mshonaji wangu, namthamini mwandishi wangu; lakini mpishi wangu, ambaye anajua vizuri jinsi ya kuandaa chakula kinachodumisha maisha na kulisha ubongo, mifupa, na misuli, anachukua nafasi muhimu zaidi kati ya wasaidizi katika familia yangu. {2T 370.2}

Akina mama, hakuna kitu kinachosababisha maovu kama vile kuwaondolewa majukumu mabinti zako, na usiwape kazi yoyote

maalum ya kufanya, ukiwaacha wachague lolote wanalotaka kufanya wenyewe, labda kushona vitambaa kidogo, kutarizi au kazi nyingine ya kupendeza iwashugulishe. Wacha wawe na mazoezi ya viungo na misuli. Ikiwa watachoshwa, kuna nini basi? Je, ninyi hamchoki katika kazi yenu? Je! Uchovu utawaumiza watoto wako, labda iwe wanafanya kazi kupita kiasi, zaidi ya vile inavyokuumiza? Hapana, kabisa. Wanaweza kupona kutokana na uchovu wao katika kupumzika usiku vizuri, na kuwa tayari kushiriki katika kazi siku inayofuata. Ni dhambi kuwaacha wakue katika uvivu. Dhambi na uharibifu wa Sodoma ilikuwa chakula tele na uvivu. {2T 371.1}

Tunataka kufanya kazi kwa kuzingatia mtazamo sahihi. Tunataka kuenenda kama wanaume na wanawake ambao wataletwa katika hukumu. Na tunapopokea matengenezo ya afya tunapaswa kuyapokea katika hali ya wajibu, na sio kwa sababu mtu mwingine ameanza kuyafanya. Sijabadilisha msimamo wangu hata chembe toka nilipoanza matengenezo ya afya. Sijarudi hata hatua moja nyuma tangu nuru kutoka mbinguni juu ya mada hii ilipoangaza njia yangu. Niliachana na kila kitu mara moja, - kuanzia nyama na siagi, na kutoka kula milo mitatu, - na wakati nilikuwa nikijishughulisha na kazi nzito ya ubongo, kwa kuandika kutoka asubuhi hadi jua lituapo. Nilikula chakula mara mbili kwa siku bila kubadilisha kazi yangu. Nimeteseka sana na magonjwa, nilipata mishtuko mitano ya kupooza. Mkono wangu wa kushoto umekuwa umefungwa begani kwasababu ya maumivu makubwa ya moyo kwa miezi kadhaa. Wakati nilipofanya mabadiliko haya katika lishe yangu, nilikataa kuiruhusu ladha ya chakula kunitawala. Je! Hiyo itanizuia katika njia ya kupata nguvu zaidi, ili nipate kumtukuza Bwana wangu? Je! Hiyo itanizuia njia yangu kwa muda mfupi? Kamwe! Nilipata njaa kali. Nilikuwa mlaji mkubwa wa nyama. Lakini nilipozimia, niliweka mikono yangu juu ya tumbo langu na nikasema: "Sitaonja hata kipande kidogo. Nitakula chakula rahisi, au sitakula kabisa." Mkate haukuwa wa kupendeza kwangu. Kwa Nadra sana niliweza kula kipande kikubwa kuzidi sarafu ya dola. Vitu vingine katika matengenezo havikuwa shida sana, lakini nilipokuja kwa mkate nilikuwa na mtihani kiasi. Wakati nilifanya mabadiliko haya nilikuwa na vita maalum vya kupigana. Milo miwili au mitatu ya kwanza, sikuweza kula. Nikaliambia tumbo langu: "unaweza kungoja hadi utakapoweza

kula mkate." Baada muda kidogo niliweza kula mkate, na mkate wa ngano isiyokobolewa, pia. Huu sikuweza kula kabla; lakini sasa una ladha nzuri, na hamu ya chakula haijanipotea. {2T 371.2}

Wakati wa kuandika kitabu cha Karama za Kiroho (Spiritual Gifts), Gombo la tatu na nne, ningechoka kwa wingi wa kazi. Hapo nikaona kwamba ni lazima nibadilishe maisha yangu, na kwa kupumzika siku chache nikawa sawa tena. Nilichukua msimamo wangu wa matengenezo ya afya kutokana na kanuni. Na tangu wakati huo, ndugu, hamjanisikia kuelezea suala la matengenezo ya afya ya kupitiiliza ambayo imenilazimu kuachana nayo. Sijaongeza mengine ila nayayosimamia hadi leo. Ninapendekeza kwako mlo wenye afya na ulio kamili. {2T 372.1}

Sioni kama ni adhabu kubwa kuacha kutumia vitu hivyo ambavyo vinatoa harufu mbaya nikipumua na kuleta ladha mbaya mdomoni. Je! Ni kujikana nafsi kuacha vitu hivi na kuingia katika hali ambayo kila kitu ni kitamu kama asali; na ambapo hakuna ladha mbaya iliyoachwa kinywani na hakuna hisia ya kuchoka ndani ya tumbo? Hivi vilikuwa vikinipata wakati mwingi. Nimezimia wakati mtoto wangu akiwa mikononi mwangu tena na tena. Haya yote sina sasa, Je! Nitaita hii ni adhabu wakati naweza kusimama mbele yenu kama ninavyofanya leo? Hakuna mwanamke mmoja katika mia ambaye angeweza kuvumilia wingi wa kazi ninayofanya mimi leo. Ninafanya mambo kwa kanuni sasa na sio kwa mihemuko. Ninasonga mbele kwa sababu niliamini Mbingu itakubali njia niliyokuwa nikichukua kujileta katika hali bora kabisa ya afya, ili nipate kumtukuza Mungu katika mwili na roho yangu, ambavyo ni Vyake. {2T 372.2}

Tunaweza kuwa na aina ya chakula kizuri, kisichokobolewa au kusindikwa, kilichopikwa kwa njia ya afya, ili kiweze kupendeza kwa wote. Na ikiwa ninyi, dada zangu, hamjui kupika, niwashauri mjifunze. Ni muhimu sana kwenu kujua jinsi ya kupika. Kuna roho nyingi zilizopotea kutokana na upishi duni kuliko mnavyofikiria [watu wamekufa kwa upishi mbaya]. Upishi mbaya husababisha magonjwa, maradhi, na hasira mbaya na hulka zingine za kupitiliza (tempers); mwili unakuwa unatatanishwa, na vitu vya mbinguni haviwezi



kutambuliwa. Kuna mafundisho tele ya kiroho katika upishi mzuri wa chakula kuliko wengi mnavyofikiria (alisema katika kupika mkate, sisi tutasema katika kupika ugali au nafaka tunazotumia). Kuna mafundisho tele ya kiroho/Neno la Mungu katika upishi mzuri kuliko vile mnavyofikiria. Tunataka mjifunze dini nzuri ni nini, na muitende katika familia zenu. Wakati nimekuwa niko nje ya nyumbani kwangu wakati mwingine, nimejua kuwa mkate uliopo mezani, na chakula kwa ujumla, vingeniumiza; lakini ningelazimika kula kidogo kudumisha maisha. Ni dhambi mbele ya Mbingu kuwa na chakula kama hicho. Nimeteseka kwa kukosa chakula kizuri. Kwa tumbo la kuvimbiwa, unaweza kuweka kwenye meza yako matunda ya aina tofauti, lakini sio mengi kwenye mlo mmoja. Kwa njia hii unaweza kuwa na aina tofauti, na utakuwa na ladha nzuri, na baada ya kula milo yako utahisi vizuri. {2T 373.1}

Nimeshangazwa kujua kwamba, hata baada ya nuru yote ambayo mmepewa mahali hapa, wengi wenu hula katikati ya milo! Haupaswi kamwe kuruhusu hata kipande kidogo kupita midomoni mwako kati ya milo yako ya kawaida. Kula unachostahili, lakini kula katika mlo mmoja, na kisha subiri hadi mlo mwingine. Ninakula vya kutosha kukidhi matakwa ya maumbile; lakini ninapoinuka kutoka mezani, hamu yangu inalingana tu na wakati niliketi kula. Na mlo mwingine ukija, niko tayari kuchukua sehemu yangu ya chakula, na sio zaidi. Je! Nile maradufu sasa kwa sababu ya ladha nzuri, ningewezaje kuinama na kumwomba Mungu anisaidie katika kazi yangu ya uandishi, wakati sikuweza kupata wazo kwa sababu ya ulafi wangu? Je! Ninaweza kumwuliza Mungu ashugulikie mzigo huo wa chakula usiofaa kwenye tumbo langu? Hiyo itakuwa ni kumvunjia heshima Yeye. Hiyo itakuwa kumwulizia aendekeze tamaa yangu. Sasa nakula tu ninachofikiria ni sahihi, hivyo nitamwomba Yeye Kristo anipatie nguvu ya kufanya kazi Yake aliyonituma. Na nimejua kuwa Mbingu imesikia na kujibu maombi yangu wakati nitatoa ombi hili. {2T 373.2}

Tena, tunapokula pasipo kuwa na kiasi, tunatenda dhambi dhidi ya miili yetu wenyewe. Siku ya Sabato, ndani ya nyumba ya Mungu, walafi watakaa na kulala ndani ya nyumba ya Mungu pasipo kupata Kweli ya Neno la MUNGU inayochoma mioyo na kuangaza. Hawawezi kuweka

macho yao wazi, wala kuelewa mazungumzo mazito yaliyotolewa (hotuba takatifu). Je! Unafikiri kwamba hao wanamtukuza Mungu katika miili na roho zao, ambazo ni Zake? Hapana; Hawamrudishii Bwana utukufu Yeye. Na wale wanaotumikisha matumbo na kuvimbiwa – Jambo lililosababisha hii hali inaendelea tumboni (dyspepsia). Badala ya kuzingatia taratibu, ameruhusu hamu ya kula iweze kumwendesha, na kula katikati ya milo. Kama amekuwa ni mwenye kukaa tu, atakuwa hajapata hewa kutoka mbinguni inayosaidia katika kazi ya kumengenga chakula; atakuwa hana mazoezi ya kutosha kwa afya yake. {2T 374.1}

Baadhi yenu mnajisikia kana kwamba mngenda mtu awaambie ni kiasi gani cha chakula mle. Haipaswi kuwa hivi. Tunapaswa kutenda kutoka kwa maoni ya kimaadili na kidini. Tunapaswa kuwa na kiasi katika kila kitu, kwa sababu taji isiyoweza kuharibika, hazina ya mbinguni, iko mbele yetu. Na sasa nataka kusema kwa kaka na dada zangu, nitakuwa na ujasiri wa kimaadili kuchukua msimamo wangu na kujitawala mimi binafsi. Nisingependa kuweka hilo kwa mtu mwingine. Unakula sana, halafu unajuta, na kwa hivyo unaendelea kufikiria juu ya kile unachokula na kunywa. Wewe kula tu kile kilicho bora, na fanya hivi mara moja, ukijisikia uko wazi machoni pa Mbingu, na bila majuto ya dhamiri. Hatuamini katika kuondoa vishawishi mbali kabisa na watoto au watu wazima. Sisi sote tuna vita mbele yetu na lazima tusimame katika nafasi ya kupinga vishawishi vya Shetani, na tunataka kujua kuwa tunayo nguvu ndani yetu kufanya hili. {2T 374.2}

Na wakati tunataka kukuonya usile kupita kiasi, hata kile chakula bora zaidi, pia tunaonya wale ambao ni wenye msimamo mkali wasiinue kiwango cha uwongo na kisha wajitahidi kumleta kila mtu kufikia hapo. Kuna wengine ambao wanaanza kama wanamatengenezo wa afya ambao hawastahili kushiriki katika shuguli yoyote, na ambao hawana ufahamu wa kutosha hata kutunza familia zao wenyewe, au kuweka nafasi zao kanisani sahihi. Na wanafanya nini basi? Hawa Huwa wanafanya kazi kama madaktari wa matengenezo ya afya, kana kwamba wanaweza kufanikisha hilo. Wanachukua majukumu ya kazi hiyo ya taaluma ya afya, na kubeba maisha ya wanaume na wanawake

wanayaweka mikononi mwao, wakati hawajui chochote juu ya taaluma hiyo. {2T 374.3}

Sauti yangu itainuliwa dhidi ya watu wanaofanya kazi ya kutibu wagonjwa bila uzoefu kulingana na kanuni za matengenezo ya afya. Mungu apishe mbali kwamba tusiwe majaribio yao! Tu wachache sana kuwa majaribio. Ni vita vya aibu kabisa kwetu kufa. Mungu atuokoe na hatari kama hiyo! Hatuhitaji walimu na matabibu kama hao. Wacha wale wanaojaribu kutibu magonjwa, wawe ambao wanajua yahusuyo mfumo wa kibinadamu. Tabibu wa mbinguni alikuwa amejaa huruma. Roho hii inahitajika kwa wale wanaoshughulika na wagonjwa. Wengine ambao huamua kuwa matabibu ni watu wenye msimamo mkali, wenye ubinafsi, wabaguzi na wenye shingo ngumu. Huwezi kuwafundisha chochote. Labda hawajawahi kufanya chochote kinachostahili kufanywa. Huenda hawakufanikiwa kimaisha. Hawajui chochote kinachostahili kujua, na bado wameanza kufanya matengenezo ya afya. Hatuwezi kumruhusu mtu kama huyo kumuua huyu na yule. Hapana; hatuwezi kuchukuliana nalo hilo, kwani lina gharama kubwa! {2T 375.1}

Tunataka kuwa sawa kila wakati. Tunataka kuwaleta watu wetu kwenye msimamo sahihi juu ya matengenezo ya afya. "Acheni sisi," asema mtume, "tujitakase na uchafu wote wa mwili na roho, tukikamilisha utakatifu katika kumcha Mungu." Lazima tuwe sahihi ili kusimama katika siku za mwisho. Tunahitaji utimamu wa ubongo, wenye akili zenye uwezo mzuri wa kuchanganua mambo vyema na miili yenye afya. Tunapaswa kuanza kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watoto wetu, kwa kila mshiriki wa familia zetu. Je! Tunashikilia na kufanya kazi kutoka kwa mtazamo sahihi? Yesu anakuja; Ikiwa tutafuata njia ya kutupotosha kwenye Ukweli wa leo unaoinua roho wa siku hizi za mwisho, tunawezaje kutakaswa kupitia Kweli? Je! Tunawezaje kuwa tayari kwa kutokufa? Bwana atusaidie ili tuanze kufanya kazi hapa kuliko hapo awali. {2T 375.2}

Tumezungumza juu ya kuwa na mfululizo wa mikutano mahali hapa, na kushikilia kufanya kazi kwa watu. Lakini hatuthubutu kuweka mikono yetu chini, ili kuwainua ninyi. Tunataka ninyi muanze kazi hii ya matengenezo katika nyumba zenu wenyewe. Tunataka wale ambao

wamekuwa nyuma waje. Lazima muanze kufanya kazi. Na tutakapoona kwamba mmeanza kujitahidi, tutakuja na kuinua hii kazi. Tunaamini mtaenda kuwasaidia watoto wenu katika matengenezo wenu, ili wamgeukie Kristo, na kwamba roho ya matengenezo ienee katikati yako. Lakini unapoonekana umekufa maradufu, na uko tayari kung'olewa na mizizi, hatuthubutu kufanya kazi hiyo. Bora twende kwa kusanyiko la wasioamini ambapo kuna mioyo ya kupokea Kweli. Mzigo wa Ukweli uko juu yetu. Kuna watu wa kutosha kusikia Ukweli; na tunatamani kuwa mahali ambapo tunaweza kuzungumza nao. Je! Mtatusaidia kwenda kuifanya hii kazi, mkianzia kwenu? {2T 376.1}

Bwana awasaidie kuweza kupata mguso ambao hamjawahi kupata awali. Pia awasaidie kuifia nafsi, na mpate roho ya matengenezo ndani ya nyumba zenu, ili malaika wa Mungu waingie katikati yenu, kukuhudumieni, na muweze kufaa kwa safari ya mbinguni. {2T 376.2}

\*Soma zaidi Mashauri ya lishe na chakula (Counsels on Diet and Foods)  
- Viungo vya kukasirisha ukuta wa tumbo kama vile pilipili manga, haradali, allspice, siki, baking soda n.k, anasema viepukwe. Na vingine kama mdalasini, pilipili ya cayenne, karafuu vitumike kwa udogo/uangalifu. Ila viungo kama manjano, tangawizi, vitunguu saumu, vitunguu, pilipili hoho n.k ni sawa, ila katika kila kitu kiasi, maana kama vina ukali fulani, na kukwangua tumbo siyo vizuri.

## **SURA YA 53**

### **USHUPAVU ULIOPITILIZA KATIKA MATENGENEZO YA AFYA**

Wakati wa mkutano wa kila mwaka katika Kituo cha Adams, New York, Oktoba 25, 1868, nilioneshwa kwamba ndugu huko ----- walikuwa katika mshangao na fadhaa/dhiki kubwa kwa sababu ya mwenendo uliofuatwa na B na C. Wale ambao wanapenda kazi ya Mungu mioyoni mwao hawawezi kuvumilia kutokuwa na wivu wa kazi ya MUNGU kwenda mbele. Nilioneshwa kuwa wanaume hawa hawakuwa wa

kutegemewa. Walikuwa wenye msimamo mkali, unaopilitiza na wangeangusha kazi ya matengenezo ya afya chini. Hawakuwa wakifuata mwenendo ambao ungeweza kuwasahihisha au kuwarekebisha wale ambao walikuwa hawana kiasi katika lishe yao; lakini ushawishi wao ungewachukiza waumini na wasioamini, na ungewafukuza mbali na matengenezo, badala ya kuwaleta karibu nayo. {2T 377.1}

Maoni yetu yanatofautiana sana na yale ya ulimwengu kwa ujumla. Sio maarufu, hayapendwi na watu. Walio wengi watakataa nadharia yoyote, hata iwe ya busara kiasi gani, ikiwa itaweka kizuizi juu ya hamu ya kula. Ladha inazingatiwa kuliko busara na afya. Wote ambao huacha njia ya kawaida ya mapokeo, na kutetea matengenezo, watapingwa, watahesabiwa wana wazimu, wenye msimamo mkali, daima waendeleo kufuata wanachokisimamia bila kukata tamaa. Lakini wakati watu wanaotetea matengenezo wanapokuwa washupavu wa mafundisho, wakibadilika-badilika kwenye wanachokiamini, watu hawatalaumiwa ikiwa watachukizwa na matengenezo ya afya. Hawa wenye misimamo mkali wanajeruhi zaidi katika miezi michache kuliko wanavyoweza kurekebisha katika maisha yao yote. Kwaajili yao, nadharia nzima ya imani yetu imeshutumiwa, na hawawezi kamwe kuwaleta wale wanaoshuhudia maonyesho kama hayo ya kile kinachoitwa matengenezo ya afya wafikirie kuwa kuna jambo zuri ndani humo. Watu hawa wanafanya kazi ambayo Shetani anapenda kuona ikiendelea. {2T 377.2}

Wale wanaotetea Ukweli usiopendwa wanapaswa kusimamia kile wanachokiamini katika maisha yao, na wanapaswa kuwa makini kufanya kazi kama wale wenye misimamo migumu. Hawapaswi kufanya kazi ili waone ni kwa kiasi gani wanaweza kuwa tofauti na watu wengine, bali kinyume chake yaani kuona ni karibu kiasi gani waweze kwenda ili kuwafikia wale ambao wanataka kufanya matengenezo, ili waweze kuwasaidia kufikia msimamo ambao wao wenyewe wanauthamini sana. Ikiwa wanafikiria hivyo, watafuata njia ambayo itapendekeza Ukweli wanaotetea, kulingana na mtazamo bora wa wanaume na wanawake wenye busara. Hawa watalazimika

kukiri kuwa kuna msimamo katika somo la matengenezo ya afya. {2T 377.3}

Nilioneshwa mwenendo wa B katika familia yake mwenyewe. Amekuwa mkali, dikteta na asiyeshaurika. Alipokea matengenezo ya afya kama alivyoshauriwa na Ndugu C, na, kama yeye, alichukua msimamo mbaya juu ya somo hilo; na kwa kuwa hakuwa mtu mwenye kuchanganua mambo, amefanya makosa makubwa, ambayo matokeo yake hayawezi kufutika. Akisaidiwa na vitu vilivyokusanywa kutoka vitabuni, alianza kutekeleza nadharia aliyosikia ikitetewa na Ndugu C, na, kama yeye, alifanya hoja ya kuleta yote kwa kiwango alichokijenga/alichokisimika. Alileta familia yake mwenyewe kwa sheria zake ngumu, lakini alishindwa kudhibiti tabia zake zenye tamaa za kinyama. Alishindwa kujileta kwenye viwango, na kuweka mwili wake chini. Kama angekuwa na maarifa sahihi ya mfumo wa matengenezo ya afya angejua kwamba mkewe hakuwa katika hali ya kuzaa watoto wenye afya. Tamaa/shauku zake ambazo hazikutawaliwa zilikuwa zikiyumba bila busara kutoka sababu hadi athari. {2T 378.1}

Kabla ya kuzaliwa kwa watoto wake hakumtendea mkewe kama mwanamke aliye katika hali inayopasa kujaliwa. Alitumia sheria zake ngumu, kulingana na maoni ya Ndugu C, ambayo yalithibitisha kuwa maumivu makubwa kwa mkewe. Hakutoa ubora na kiwango cha chakula ambacho kilikuwa cha lazima kulisha maisha ya watu wawili, yaani mtoto na mama. Maisha ya mtoto tumboni yalikuwa yakimtegemea mama, na mfumo wake haukupokea chakula chenye lishe na afya bora, kizuri kinachohitajika kudumisha nguvu zake. Kulikuwa na upungufu katika wingi na ubora-kisichokobolewa au kusindikwa. Mfumo wake ulihitaji mabadiliko, aina tofauti na ubora wa chakula ambao ulikuwa wa lishe zaidi. Watoto wake walizaliwa wakiwa na nguvu dhaifu ya umengenyaji wa chakula na damu duni. Kutokana na chakula mama alilazimishwa kutumia, hakuweza kuwa nadamu bora, na kwa hivyo alizaa watoto waliojaa dhihaka. {2T 378.2}

Njia inayofuatwa na mume, baba wa watoto hawa, inastahili adhabu kali. Mkewe aliteswa kwa kukosa chakula bora, chenye lishe. Hakuwa

na chakula au mavazi ya kutosha ya kumfanya aishi kwa faraja, na bila usumbufu. Amebeba mzigo ambao umekuwa na **usumbufu na uchungu kubeba. Mume huyu akawa muungu, dhamiri, na matakwa ya mke. Kuna asili** ndani ya mwanadamu ambazo zitaasi dhidi ya mamlaka hii inayodhaniwa. Haitakubaliana kwa ufuatiliaji kama huo. Kutakuwa na shinikizo hilo na kupinga mamlaka hayo. Lakini haikuwa hivyo katika kesi hii. Mke alivumilia mume kuwa dhamiri yake na kujaribu kuona pengine itakuwa bora kwake. Lakini mwili/asili ya hasira haikuweza kutawaliwa kwa urahisi. Madai yake yalikuwa ya dhati. Kutamani lishe bora kwa maumbile kulimwongoza kuomba asaidiwe, lakini hakukuwa na mwitikio. Matakwa yake yalikuwa machache, lakini hayakuzingatiwa. Watoto wawili wametolewa kafara kwa makosa yake ya kutokujua na ushabiki wa kijinga. Ikiwa wanaume wenye akili timamu watawatendea wanyama wasiozungumza kama vile alivyomtendea mkewe kuhusu chakula, jamii ingejichukulia suala hilo mikononi mwao na kumfikisha mbele ya sheria. {2T 379.1}

Kwanza, B hakupaswa kufanya uhalifu mkubwa sana wa kuwaleta watoto duniani kwa kuwa sababu zilikuwa tosha kumwonyesha kwamba lazima watakuwa wagonjwa kwani watapata urithi mbaya kutoka kwa wazazi wao. Lazima wangepata urithi mbaya. Damu yao lazima ina uvimbe kwenye tezi za shingo usio mzuri kutoka kwa wazazi wote wawili, haswa baba, ambaye tabia zake zimekuwa haribifu kwa damu na kuchochea mfumo wake wote. Sio tu watoto hawa masikini watapata tabia inayohusiana na maambukizo ya mfumo wa kupumua (scrofulous), lakini mbaya zaidi chembe cha ugonjwa mbaya utakuwa unatoka pande zote mbili; watabeba upungufu wa akili na maadili kutoka kwa baba, na kutoka kwa mama ukosefu wa uhuru wa maamuzi, ujasiri wa maadili, na nguvu mwilini. Ulimwengu tayari umelaaniwa na ongezeko la watu wa aina hii, ambao ilibidi viwango vyao vya mwili vishuke chini, pia viwango vya nguvu ya akili, na maadili vilikuwa pungufu na vile vya wazazi wao; kwa vile hali yao na mazingira yao yalikuwa hafifu ukilinganisha na ya wazazi wao. {2T 379.2}

B hana uwezo wa kutunza familia. Hawezi kumtunza hata mtu mmoja kama inavyopaswa, na hakupaswa kuwa na hata mmoja anayemtegemea. Ndoa yake ilikuwa makosa. Amefanya maisha ya

mkewe kuwa ya huzuni na ameongeza shida kwa kuleta watoto duniani. Wanaishi, na hiyo ndiyo yote. {2T 380.1}

Wale wanaodai kuwa Wakristo hawapaswi kuingia kwenye uhusiano wa ndoa mpaka jambo hilo lizingatiwe kwa uangalifu na kwa maombi kutoka kwa msimamo ulioinuliwa ili kuona ikiwa Mungu anaweza kutukuzwa na umoja huo. Halafu wanapaswa kuzingatia vizuri matokeo ya kila upendeleo wa uhusiano wa ndoa, na kanuni iliyotakaswa inapaswa kuwa msingi wa kila tendo. Kabla ya kuongeza familia zao, wanapaswa kuzingatia ikiwa Mungu atatukuzwa au kudharauliwa kwa kuwaleta watoto ulimwenguni. Wanapaswa kutafuta kumtukuza Mungu kwa umoja wao tangu mwanzo, na kila mwaka wa maisha yao ya ndoa. Wanapaswa kuzingatia kwa utulivu ni mpango gani unaweza kufanywa kwa maslahi ya watoto wao. Hawana haki ya kuleta watoto ulimwenguni kuwa mzigo kwa wengine. Je! Wana biashara ambayo wanaweza kutegemea kuikumu familia ili wasihitaji kuwa mzigo kwa wengine? Ikiwa hawajafanya hivyo, wanafanya uhalifu kwa kuwaleta watoto ulimwenguni kuteseka kwa kukosa utunzaji mzuri, chakula, na mavazi. Katika enzi hii ya kasi na ufisadi/uovu, mambo haya hayazingatiwi. Tamaa na shauku inachukua mvuto na haitasalimu amri, japo udhaifu, taabu, na kifo ni matokeo ya utawala wake. Wanawake wanalazimika kuishi maisha ya shida, maumivu, na mateso kwa sababu ya tamaa zisizoweza kudhibitiwa za wanaume walio na jina la mume - kwa haki wangeweza kuitwa wanyama. Akina mama wanaburuzana na maisha mabaya, na watoto mikononi mwao karibu muda wote, wakijitahidi kwa kila njia kuweka mkate vinywani mwao na nguo mwilini mwao. Majanga/Misiba hiyo iliyojilimbikiza imejaa ulimwenguni. {2T 380.2}

Kuna upendo mdogo tu wa Kweli, usio na hila, wa kujitolea, na safi. Karama hii ya thamani yaani upendo ni ya nadra sana. Tamaa inaitwa upendo. Wanawake wengi wapole na wenye sifa njema wamekasirika sana, kwa sababu uhusiano wa ndoa ulimruhusu yule ambaye alimwita mume kuwa mkatili katika mahusiano yao. Upendo wake aliona kuwa wa chini sana hivi kwamba alichukizwa. {2T 381.1}



Familia nyingi sana zinaishi katika hali isiyo na furaha sana kwa sababu mume na baba huruhusu hisia za kinyama katika maumbile yake kutawala akili na maadili. Matokeo yake ni kwamba hisia za unyonge na huzuni huja mara kwa mara, lakini ni nadra wanagundua kwamba haya ni matokeo ya mwenendo wao usiofaa. Tuko chini ya majukumu mazito kwa Mungu ya kuweka usafi wa roho na ukamilifu wa mwili, ili tupate kuwa faida kwa wanadamu, na kumtolea Mungu huduma kamilifu. Mtume anatoa maneno haya ya onyo:" Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake." Anatuhimiza kuendelea kwa kutuambia kwamba "Wanariadha hujipa mazoezi na nidhamu kali; hufanya hivyo ili wajipatie taji iharibikayo! Lakini sisi twafanya hivyo tupate taji ya kudumu daima" Anawahimiza wote wanaojiita Wakristo kutoa miili yao "dhabihu iliyo hai, takatifu, inayokubalika mbele za Mungu." Anasema: " lakini nauimarisha mwili wangu na kuutawala, ili baada ya kuwahubiria wengine, mimi mwenyewe nisije nikakataliwa." {2T 381.2}

Ni kosa linafanywa kwa ujumla la kutoleta tofauti katika maisha ya mwanamke kabla ya kuzaliwa kwa watoto wake. Katika kipindi hiki muhimu kazi za mama zinapaswa kupunguzwa. Mabadiliko makubwa yanaendelea katika mfumo wake. Anahitaji kiwango kikubwa cha damu, na kwa hivyo ongezeko la chakula chenye lishe zaidi ili kutengeneza damu. Asipokuwa na chakula cha kutosha chenye lishe, hawezi kuhifadhi nguvu zake za mwili, na watoto watakuwa wameibiwa nguvu. Mavazi yake pia yanahitaji umakini. Uangalizi unapaswa kuchukuliwa ili kulinda mwili kutoka kwa hisia ya baridi. Haipaswi kuita nguvu za uhai juu kwenye Ngozi ili kusambaza joto kwaajili ya uhaba wa nguo za kutosha. Ikiwa mama atanyimwa chakula kizuri na chenye lishe, atakosa wingi na ubora wa damu. Mzunguko wake utakuwa duni, na mtoto wake watakosa vitu hivyo hivyo. Kutakuwa na kutowezekana kwa watoto kupata chakula kinachofaa ambacho kinaweza kubadilishwa kuwa damu nzuri ili kulisha mfumo. Ustawi wa mama na mtoto hutegemea sana juu ya mavazi mazuri, ya joto na usambazaji wa chakula chenye lishe. Baridi ya upepo wa ziada kwa uhai wa mama lazima uzingatiwe na kushugulikiwa. {2T 381.3}

Lakini, kwa upande mwingine, wazo kwamba wanawake, kwa sababu ya hali yao maalum ya ujauzito, wanaweza kuruhusu hamu ya kula iwe

bila kuthibiti, ni kosa linatokana na mila, lakini sio busara. Hamu ya chakula ya wanawake katika hali hii inaweza kuwa ya kutofautiana, inayofaa, na ngumu kutosheleza; na desturi hufikiria kwamba anaruhusiwa kuwa na chochote anachopenda, bila kufikiri kwa busara ikiwa chakula hicho kinaweza kutoa lishe kwa mwili wake na ukuaji wa mtoto wake ipasavyo. Chakula kinapaswa kuwa na lishe, lakini hakipaswi kulisimua mwili. Desturi inasema kwamba ikiwa anataka nyama, mboga mboga zenye siki, chakula kilichotiwa viungo (jifunze zaidi viungo gani ni vibaya kwa mwili), au mikate inayookwa na nyama au mabaki ya chakula, wacha apewe tu; hamu ya kula pekee ndiyo iwe mshauri. Hili ni kosa kubwa, na linaumiza sana. Madhara hayawezi kukadiriwa. Kama kuna kuna kipindi ambacho lishe rahisi na utunzaji maalum juu ya ubora wa chakula kinacholiwa unahitajika, ni katika kipindi hiki muhimu. {2T 382.1}

Wanawake ambao wana kanuni, na ambao wamefundishwa vizuri, hawataacha lishe rahisi, mida hii kulinganisha na wakati mwingine wa Maisha yao. Watazingatia kuwa maisha mengine yanawategemea wao, na watakuwa waangalifu katika tabia zao zote, na haswa katika lishe. Hawapaswi kula chakula kisicho na lishe bora na cha kujifurahisha, kwa sababu tu kina ladha nzuri tu. Kuna washauri wengi mno walio tayari kuwashawishi wafanye mambo ambayo busara ingewaambia hawapaswi kuyafanya. {2T 382.2}

Watoto wenye magonjwa huzaliwa kwa sababu ya kuridhisha hamu ya kula kwa wazazi. Mfumo haukutaka aina ya chakula ambacho akili ilipenda. Kwa sababu kipo mawazoni, basi ni lazima kiwe ndani ya tumbo, ni kosa kubwa, ambalo wanawake wa Kikristo wanapaswa kukataa. Mawazo hayapaswi kuruhusiwa kutawala mahitaji ya mfumo wa mwili. Wale ambao huruhusu ladha itawale, watapata adhabu ya kukiuka sheria za maisha yao. Na jambo hilo haliishii hapa; watoto wao wasio na hatia pia watakuwa watesekaji/wanaougua. {2T 383.1}

Viungo vya mwili vinavyotengeneza damu haviwezi kubadilisha viungo vya chakula, mikate iliyoweka matunda na nyama za kusaga, mboga-mboga zenye siki, na nyama zilizo na ugonjwa kuwa damu nzuri. Na ikiwa chakula kingi kinapelekwa ndani ya tumbo, hivi viungo vya

mmeng'enyo vinalazimika kufanya kazi kupita kiasi ili kuyeyusha na kuvitoa tumboni ili kufanya mfumo uachane na vitu vyenye kuukasirisha, mama hujidhulumu mwenyewe na huweka msingi wa magonjwa kwa watoto wake. Ikiwa atachagua kula apendavyo, na kile anachopenda kwenye fikra zake, bila kujali matokeo, atajipatia adhabu, lakini sio peke yake. Mtoto wake asiye na hatia lazima ateseke kwa sababu ya ujinga wake. {2T 383.2}

Uangalifu mkubwa unapaswa kutekelezwa ili kuwa na mazingira ya mama yenye kupendeza na ya kufurahisha. Mume na baba yuko chini ya jukumu maalum la kufanya yote kwa uwezo wake, kupunguza mzigo wa mke na mama. Anapaswa kubeba, kadiri iwezekanavyo, mzigo wa hali yake. Anapaswa kuwa mtu mzuri, mwenye adabu, mkarimu, na mpole, na haswa kuwa mwangalifu kwa matakwa yake yote. Utunzaji wanaopata wanawake wengine wajawazito ni mdogo sana na haufikii nusu ya ule wanaopewa wanyama zizini {2T 383.3}

B amekuwa na upungufu sana. Alipokuwa katika hali bora ya afya, mkewe hakupewa chakula kingi kizuri na mavazi sahihi. Halafu, wakati alipohitaji mavazi ya ziada na chakula cha ziada, na chakula rahisi na chenye ya ubora lakini chenye lishe, hakuruhusiwa. Mfumo wake ulitamani chakul/nyenzo za kugeuzwa kuwa damu, lakini hakutaka kumpatia. Maziwa kidogo na sukari, na chumvi kidogo, mkate mweupe ulioumuka kwa mabadiliko ya lishe, unga wa graham (usiokobolewa) ulioandaliwa kwa njia tofauti na mikono yake mwenyewe, keki ya zabibu, uji wa mchele, matunda damu (plum), na tini, mara kwa mara, na vyakula vingine vingi ambavyo ningeweza kutaja, vingejibu mahitaji ya hamu ya kula. Ikiwa hangeweza kuleta baadhi ya vitu hivi, maji ya zabibu kidogo hayangemdhuru; ingekuwa bora kwake kuwa nayo kuliko kutokuwa nayo. Na wakati mwingine, hata kiwango kidogo cha nyama isiyoumiza ingekuwa bora kuliko kuwa na hamu kali aliyokuwa nayo ya chakula cha aina fulani. {2T 383.4}

Nilioneshwa kuwa wote B na C wamedharau kusudi la Mungu. Wameiletea doa ambalo halitafutwa kabisa. Nilioneshwa familia ya Ndugu yetu mpendwa D. Ikiwa ndugu huyu angepata msaada unaofaa kwa wakati unaofaa, kila mshiriki wa familia yake angekuwa hai leo. Ni

jambo la kushangaza kwamba sheria za nchi hazikumshugulikia kwa ukali, wakati huu wa unyanyasaji. Familia hiyo ilikuwa ikiangamia kwa kukosa chakula, chakula kilicho cha kawaida, na rahisi zaidi. Walikuwa na njaa katika nchi ya vyakula vingi. Kukosa maarifa ndicho kilikuwa kinaendelea. Kijana huyo hakufa kwa ugonjwa, lakini kwa njaa. Chakula kingeimarisha mfumo na kuweka mitambo ya mwili katika mwendo. {2T 384.1}

Katika hali ya homa kali, kujinyima chakula kwa muda mfupi kutapunguza homa na kufanya matumizi ya maji kuwa na ufanisi zaidi. Lakini daktari anayehusika, anahitaji kuelewa hali halisi ya mgonjwa na asiruhusu kuzuiliwa kwa lishe kwa muda mrefu sana hadi mfumo wake utakapokuwa na nguvu. Wakati homa inaendelea, chakula kinaweza kuchochea na kulisimua damu; lakini mara tu nguvu ya homa inapotoka, lishe inapaswa kutolewa kwa uangalifu, kwa busara. Ikiwa chakula kinazuiliwa kwa muda mrefu sana, hamu ya tumbo italeti homa, ambayo itaondolewa na posho ya chakula yenye ubora unaofaa. Inaupia mwili kitu cha kufanyia kazi. Ikiwa kuna hamu kubwa inayoonyeshwa kwa chakula, hata wakati wa homa basi kutosheleza hamu hiyo na kiwango cha wastani cha chakula rahisi, itakuwa bora kuliko mgonjwa anyimwe. Wakati anaweza kupata mawazo yake juu ya kitu kingine chochote, maumbile hayatazidiwa na sehemu ndogo ya chakula rahisi. {2T 384.2}

Wale ambao huchukua maisha ya wengine mikononi mwao, lazima wawe wanaume ambao wamewekwa alama kama ndio ambao hufanya maisha kufanikiwa. Lazima wawe wanaume wa maamuzi na hekima, watu ambao wanaweza kuhurumia na kuhisi kwa kina kirefu, wanaume ambao mwili wao wote unasisimka wanaposhuhudia mateso ya wanadamu. Wanaume wengine ambao hawajafanikiwa katika biashara yoyote maishani huchukua taaluma ya udaktari. Wanayatwaa maisha ya wanaume na wanawake mikononi mwao, wakati hawana uzoefu kabisa. Walisoma mpango ambao mtu aliufuata kwa mafanikio, na kuupitisha, na kisha kufanyia mazoezi juu ya wale ambao wana imani nao, kwa kweli huharibu cheche ya mwisho ya maisha ya watu; lakini baada ya yote hawajifunzi chochote, lakini wanaendelea tu kwa furaha na matumaini katika kesi inayofuata,

wakizingatia matibabu yale yale bila kubadilisha. Watu wengine wanaweza kuwa na nguvu ya mwili ya kutosha kuhimili ubaya huu uliowekwa juu yao, na kuishi. Kisha hawa wanafunzi wa miili ya watu huchukua utukufu kwao, wakati hakuna anayestahili. Kila sifa inatokana na Mungu na maumbile yenye nguvu. {2T 385.1}

Ndugu C amekuwa akichukua nafasi isiyostahili katika kusimama kama msaada wa B. Amekuwa akili kwake, na amesimama karibu na kumsaidia na kumfanya asimame. Wanaume hawa wawili ni shupavu, watu waliopitiliza juu ya ujumbe wa matengenezo ya afya. Ndugu C anajua kidogo sana kuliko vile anavyofikiria anajua. Anajidanganya mwenyewe. Yeye ni mbinafsi, mwenye ubaguzi na mwenye msimamo mkali katika kutekeleza maoni yake; hafundishiki. Hajasalimisha mapenzi yake. Yeye sio mtu wa akili nyenyekevu. Mtu kama huyo hapaswi kuwa katika shuguli ya udaktari. Anaweza kuwa alipata ujuzi mdogo kwa kusoma, lakini hii haitoshi. Uzoefu ni muhimu. Watu wetu ni wachache sana kuweza kutolewa dhabihu kwa bei rahisi na bila heshima kwa kukubali kufanyiwa majaribio na wanaume kama hao. Jumla ya watu wengi wa thamani wangetolewa kuwa mhanga kwa maoni yao magumu na wanachoamini kabla ya matabibu hawa kukata tamaa, kukiri makosa yao, na kujifunza hekima kwa uzoefu. {2T 385.2}

Ndugu C mtu ambaye ana msimamo usiobadilika na nia iliyokaza, na hafundishiki ili Bwana Aweze kumtumia kufanya kazi yoyote maalum katika kusudi Lake. Yeye ni mkaidi sana kiasi kwamba hata watu wanaokufa kwa maoni yake hawambadilishi anachonuia. Anaweza kudumisha maoni na anachoamini kwa dhati na bidii sana. Wanaume hawa bado inabidi wajifunze kwa masikitiko yao ili waweze kufundishwa vizuri, na wasiendeshe maoni yao yaliyopitiliza, Haijalishi matokeo yatakavyokuwa. Jamii itakuwa na nafuu, na itakuwa salama kiasi kwa ujumla, ikiwa wanaume hawa wote watapata ajira katika shuguli nyingine ambayo maisha na afya za watu havitahatarishwa na mwenendo wao. {2T 386.1}

Ni jukumu kubwa kwa mwanadamu kuchukua maisha ya mwingine mikononi mwake. Na kupata maisha hayo ya thamani yanatolewa mhanga kwa njia ya usimamizi mbaya ni jambo la kutisha. Kesi ya

familia ya Ndugu D ni mbaya. Wanaume hawa wanaweza kutetea mwenendo wao; lakini hiyo haitaokoa kazi ya Mungu kushutumiwa, wala kumrudisha yule mwana aliyeteseka na kufa kwa kukosa chakula. Maji ya zabibu kidogo na chakula vingemwinua kutoka katika kitanda cha mauti na kumrudisha kwa familia yake. Baba ya marehemu pia hivi karibuni angehesabiwa na wafu ikiwa njia hiyo hiyo ingeendelea ambayo ilikuwa ikifuatwa kumtibu mwana wake, lakini uwepo na ushauri kwa wakati unaofaa wa daktari kutoka Taasisi ya Afya ulimwoko. {2T 386.2}

Ni wakati ambapo lazima kitu kifanywe ili kuzuia wanafunzi, au wale wasiokuwa na ujuzi wa kutosha, wasichukue fani hii na kutetea matengenezo ya afya. Kazi zao na maneno yao yanaweza kuepukwa; kwani wanaleta maumivu zaidi kuliko watu wenye hekima na akili zaidi, na ushawishi bora wanaoweza kutumia, wanaoweza kukabiliana nao au kuupinga. Haiwezekani kwa watetezi waliohitimu vizuri matengenezo ya afya, kuondoa kabisa kwenye akili za umma chuki hizo au kazi mbovu inayopokelewa kupitia njia mbaya ya hawa watu wenye misimamo mikali na kuweka somo kubwa la matengenezo ya afya kwenye msingi mzuri katika jamii ambapo watu hawa wamefikiria. Mlango pia umefungwa kwa kiwango kikubwa, hivyo wasioamini hawawezi kufikiwa na Ukweli wa sasa juu ya Sabato na kuja kwa Mwokozi wetu hivi karibuni. Ukweli wa thamani zaidi hutupwa kando na watu kama haustahili kusikilizwa. Wanaume hawa wanarejelewa kama wawakilishi wa warekebishaji wa afya na watunza Sabato kwa ujumla. Jukumu kubwa liko juu ya wale ambao wameonekana kuwa kikwazo kwa wasioamini. {2T 386.3}

Ndugu C anahitaji uongofu kamili. Hajioni mwenyewe alivyo. Ikiwa alikuwa na kujithamini kidogo na unyenyekevu zaidi wa akili, maarifa yake yangeweza kutumiwa kwa vitendo. Ana kazi ya kufanya mwenyewe ambayo hakuna mtu mwingine anayeweza kumfanyia. Hatatoa maoni yake au hukumu kwa mtu yeyote aliye hai, isipokuwa atalazimika kufanya hivyo. Ana tabia ambazo ni mbaya sana na ambazo zinapaswa kushinda. Anawajibika zaidi kuliko B, na kesi yake ni mbaya kuliko yake; kwani anayo akili na maarifa zaidi. B amekuwa kivuli cha akili yake. {2T 387.1}

Ndugu C ana msimamo usiobadilishwa; Ana msimamo mkali sana kwa vile anavyopenda na asivyovipenda, Anapoanza njia mbaya, na kufuata mwelekeo uliopotoka na kupinda wa akili yake, bila kuelekea upande wa hekima, na kosa lake liwasilishwe mbele yake, hata ikiwa anajua kuwa hayuko sawa, anasita sana kukiri kwamba amekosea na amefuata njia mbaya hivyo ataunda udhuru wa aina fulani na kuwafanya wengine waamini kwamba yeye hata hivyo yuko sawa. Hii ndio sababu ameachwa kufuata uamuzi hekima yake mwenyewe, ambayo ni upumbavu. {2T 387.2}

Katika familia ya baba yake, hakuwa baraka, lakini sababu ya kuleta wasiwasi na huzuni. Mapenzi yake hayakusalimishwa toka utoto. Alikuwa na tabia ya kusita kukiri na kusema ukweli kwamba alikuwa amefanya makosa na alifanya baya lile, ili kujiondoa shidani, angeweka nguvu za akili yake kazini kubuni visingizio ambavyo alijisifu mwenyewe kwa kujidanganya, kwamba si uongo wa moja kwa moja, badala ya kujinyenyekeza vya kutosha kukiri makosa yake. Tabia hii imeletwa mpaka kwenye uzoefu wake wa kidini. Ana tabia ya kipekee ya kugeuza hoja kwa kusingizia usahaulifu, wakati, mara nyingi, anachagua tu mwenyewe kusahau. {2T 387.3}

Ndugu na marafiki zake wangeweza kuletwa katika Kweli ikiwa angekuwa jinsi Mungu angependa awe. Lakini njia zake asizotaka kubadilisha zimemfanya asikubaliwe. Ametumia Kweli kama mada ya kugombana. Licha ya upinzani wa baba yake amezungumza masomo ya Biblia katika familia ya baba yake, na ametumia masomo yenye utata zaidi ili alete ugomvi, badala ya kutafuta roho kwa unyenyekevu wote wa akili, na kwa upendo usiokwisha, kuwavuta kwenye Kweli na kuwaleta kwenye nuru. {2T 388.1}

Wakati amefuata njia mbaya, ni kwa dhahiri amekuwa mwanafunzi asiyefaa wa Yesu ambaye ni mpole na mnyenyekevu, na amejua kwamba maneno na matendo yake hayakuwa kulingana na ushawishi wa kweli inayotakasa, kwa ukaidi amesimama kwa kujitetea mwenyewe, mpaka uaminifu wake umehojiwa. Ameufanya Ukweli wa thamani zaidi wa siku hizi za mwisho kuwa chukizo kwa marafiki na

jamaa zake; ameonekana kuwa kikwazo kwao. Ukwepaji wake, ushabiki wake, na maoni ya kupitiliza aliyochukua yamegeuza roho nyingi mbali na Kweli kuliko bidii yake aliyoileta. {2T 388.2}

Kupenda kulumbana/magomvi, ukaidi, na kujithamini kupita Kiasi ndiyo tabia yake. Hii haiwezi kubariki kanisa lolote na ushawishi wake mpaka atakapoongoka. Anaweza kuona makosa ya wengine, na atauliza mwenendo wa huyu na wa yule ikiwa hawakubaliani kabisa na kile anachowasilisha; lakini ikiwa mtu yeyote anapokea kile anachotetea, hawezi na hataona makosa yao. Hii sio sawa. Anaweza kuwa sahihi katika mambo mengi, lakini hana nia iliyokaa ndani ya Kristo. Wakati atakapojiona jinsi alivyo, na kusahihisha kasoro katika tabia yake, basi atakuwa katika nafasi ya kuangaza nuru yake mbele ya watu, ili watu, kwa kuona matendo yake mema, wataongozwe kumtukuza Baba yetu aliye mbinguni. Nuru yake imeangaza kwa namna ambayo watu wameichukulia kuwa giza na kugeuka kwa kuchukizwa. Lazima aifie nafsi mwenyewe, na ni lazima awe na roho inayoweza kufundishika, au ataachwa afuate njia zake mwenyewe na kujazwa na matendo yake mwenyewe. {2T 388.3}

"Mtumishi wa Mungu hapaswi kubishana; bali awe mpole kwa watu wote, akiwafundisha, kwa subira, kwa upole akiwaelekeza wale wanaowapinga; kwa matumaini kwamba Mungu anaweza kuwajalia watubu na kuifahamu Kweli." "Wasizungumze ubaya wa mtu yeyote; bali waishi kwa amani na masikizano, [wasiseme Ukweli kwa kujisifu, kwa njia ya kuonyesha wananyakua ushindi], wawe daima wapole kwa kila mtu." "Bali mtakaseni Kristo kuwa Bwana mioyoni mwenu. Siku zote muwe tayari kumjibu mtu yeyote atakayewauliza kuhusu sababu ya tumaini lililomo ndani yenu. Lakini fanyeni hivyo kwa upole na kwa heshima." {2T 389.1}

Ndugu C anataka akili yake iwadhibiti wengine, na isipokuwa anaweza kupata fursa hii hajaridhika. Yeye sio mtunza amani. Njia yake itasababisha mkanganyiko zaidi na kutoamini katika kanisa kuliko ambavyo watu 10 wangeweza kuzuia jambo hilo. Tabia yake ya kipekee ni kupenda kudonoa kasoro, na kutafuta makosa kwa wote isipokuwa yeye mwenyewe. Hatafanikiwa mpaka ajifunze somo



ambalo alipaswa kujifunza miaka iliyopita, unyenyekevu wa akili. Katika umri wake atajifunza somo hili kwa gharama kubwa kwake. Katika maisha yake yote amekuwa akijaribu kujijenga, kujiokoa, kuhifadhi maisha yake mwenyewe; na amepoteza juhudi zake za kuongoa watu kila wakati. {2T 389.2}

Kile ambacho Ndugu C anachohitaji ni kuondolewa utando wa udanganyifu kutoka kwa macho yake, ili aweze kuangalia, na macho yanayoangazwa na Roho wa Mungu, ndani ya moyo wake mwenyewe, na ajaribu na kuipima kila nia, na asimruhusu Shetani aweke rangi ya uongo kwenye safari na katika utendaji. Msimamo wake ni wa hatari sana. Karibuni tu uamuzi wake utageukia upande wa kulia, au ataendelea kuwadanganya wengine na kujidanganya mwenyewe. Roho yake ya ndani inahitaji wongofu, na kutiishwa na kubadilishwa, kwa kufanywa upya nia yake. Hapo ndipo ataweza kufanya mema. Lakini kamwe hawezi kuja kwenye nuru mpaka ahimize roho ya ungamo la unyenyekevu na kushikilia uamuzi wa kurekebisha makosa yake na, kwa kadiri awezavyo, kuondoa aibu aliyoleta juu ya kazi ya Mungu. {2T 389.3}

## **SURA YA 54**

### **HISIA ZA NGONO KWA VIJANA**

Ndugu mpendwa na Dada E: Imekuwa muda tangu nilipochukua kalamu yangu kuandika chochote isipokuwa barua za dharura ambazo hazingeweza kusubiri. Nimekuwa na uzito moyoni, ulionikatisha tamaa juu ya nafsi yangu kwa miezi, ambayo ilikaribia kuniangamiza. Jambo ambalo linanivunja moyo zaidi ni hofu kwamba yote ninayoweza

kuandika hayatakuwa na faida yoyote kama vile bidii yetu, wasiwasi, na kazi ya kuchosha ilivyokuwa katika ----- majira ya baridi na majira ya kuchipua mimea. Maoni yasiyo na matumaini niliyoyachukua ya mambo na vitu vya mahali hapo yamefanya kalamu yangu ikaribie kuacha kuandika na sauti yangu ikaribie kunyamaza. Mikono yangu imedhoofishwa, na moyo wangu umekuwa na huzuni, kuona hakuna kitu kilichopata mafanikio kwa juhudi za muda mrefu hapo. Sina matumaini kabisa kuhusu juhudi zetu kufanikiwa kuamsha hisia za watu wetu wanaotunza Sabato kuona nafasi iliyoinuka ambayo Mungu anawataka wachukue. Hawaoni mambo ya kidini kwa mtazamo wa juu. Hii ndiyo hali yako tu. {2T 390.1}

Bwana amenipa maoni ya baadhi ya uchafu uliopo kila mahali. Uovu, uhalifu, na tamaa zipo hata katika maeneo ya juu. Hata katika makanisa yanayodai kushika amri za Mungu kuna wenye dhambi na wanafiki. Ni dhambi, sio majaribu na mateso, ambayo hutenganisha Mungu na watu Wake na kuifanya roho isiweze kufurahia na kumtukuza Yeye. Ni dhambi inayoangamiza roho. Dhambi na uovu vipo katika familia za watunza Sabato. Uchafuzi wa maadili umefanywa zaidi kuliko maovu yote na kusababisha jamii ya binadamu kuzorota. Inafanywa kwa kiwango cha kutisha na huleta magonjwa ya karibu kila aina. Hata watoto wadogo sana, watoto wachanga, wanaozaliwa wakiwa na maudhi ya asili ya viungo vya ngono (irritability), hupata afueni ya kitambo katika kuvishika viungo hivyo vya uzazi, ambayo huongeza tu muwasho, na husababisha kurudia kwa kitendo hicho, hadi hapo tabia inapoengeka ambayo inaongezeka na wanapoendelea kukua. Watoto hawa, kwa ujumla huwa wadogo na dhaifu, wanaandikiwa dawa na matabibu na kukandikwa na madawa ya famasia (drugged); lakini uovu huu hauondolewi. Kwa sababu kiini chake hakijaondolewa. {2T 390.2}

Kwa ujumla Wazazi hawashuku kuwa watoto wao wanaelewa chochote juu ya uovu huu (vice/punyeto). Katika kesi nyingi wazazi ndio wenye dhambi halisi. Wametumia vibaya haki zao za ndoa, na kwa kujifurahisha wameimarisha tamaa zao za kinyama. Na kadiri hizi zinavyoimarika, vitivo vya kimaadili na kiakili vimekuwa dhaifu. Yale ya

kiroho yamezidiwa na za mwili haribifu. Watoto huzaliwa na tabia ya wanyama iliyokuzwa kwa kiasi kikubwa, Watoto wamepewa muhuri wa tabia ya wazazi. Kitendo kisicho cha asili cha viungo nyeti vya siri hutoa muwasho. Wanasisimuka kwa urahisi, na kupata unafuu wa kitambo wakivishika viungo hivi vya uzazi. Lakini uovu huongezeka kila wakati. Kupungukiwa nguvu kwenye mfumo kunahisiwa. Nguvu ya ubongo imedhoofika, na kumbukumbu hupunguka. Watoto waliozaliwa na wazazi hawa, karibu kila wakati watachukua kawaida ya tabia za kuchukiza za uovu wa huu wa siri, unaojulikana kama punyeto. Agano la ndoa ni takatifu, lakini ni kiasi gani cha tamaa na uhalifu inashughulikia! Wale ambao wanahisi wako huru, kwa sababu wameolewa/oa, hivyo wanaweza kudhalilisha miili yao kwa kutosheleza tamaa za kinyama, mwendo wao uliodhalilika utaendelezwa kwa watoto wao. Dhambi za wazazi zitatembelewa juu ya watoto wao kwa sababu wazazi wamewapa muhuri wa tabia zao zenye tamaa za mwili mbaya. {2T 391.1}

Wale ambao wamejiimarisha kabisa katika uovu huu wa kuharibu roho na mwili kawaida hupumzika mara chache mpaka mzigo wao wa uovu wa siri upelekwe kwa wale ambao wanashirikiana nao. Udadisi unaamshwa mara moja, na maarifa ya uovu hupitishwa kutoka kwa kijana mmoja mpaka mwingine, kutoka kwa mtoto hadi mtoto, mpaka inakuwa ni nadra kumpata mmoja ambaye hajui mazoea ya dhambi hii ya kudhalilisha. {2T 392.1}

Watoto wako wamefanya vitendo vya kujichua mpaka rasimu juu ya ubongo imekuwa kubwa sana, haswa kwa kisa cha mtoto wako mkubwa, kiasi kwamba akili zao zimejeruhiwa vibaya. Nuru ya akili ya ujana wao imepunguzwa. Nuru za akili za ujanani zimedhoofika, wakati sehemu ya mambo ya maadili ya chini imekuwa ikiongezeka. Kwa sababu hii mwanao anageuka na kuchukia mambo ya kidini. Amekuwa akipoteza nguvu yake ya kuwa na kiasi, na ana kicho kidogo kuhusiana na vitu vitakatifu, na heshima ndogo kwa jambo lolote lenye mionjo ya kiroho. Umesema hili llinatokana na mazingira yako, lakini haujajua sababu halisi. Mwana wako anaweza kusemwa kwamba amebeba mvuto wa kishetani badala ya wa Mungu. Anapenda dhambi na uovu kuliko wema wa kweli, usafi, na haki. Ni picha ya kusikitisha. {2T 392.2}

Athari za tabia mbaya kama hizo sio sawa kwa akili zote. Kuna watoto wengine ambao wana nguvu za maadili zilizokuzwa kwa kiasi kikubwa, ambao, kwa kushirikiana na watoto ambao wanajichua, wanaanzishwa katika uovu huu. Athari juu ya vile, itakuwa mara nyingi sana kuwafanya wawe na huzuni, hasira, na wivu; lakini hawa wanaweza wasipoteze heshima yao kwa ibada ya dini, na hawawezi kuonyesha uovu maalum kwa mambo ya kiroho. Wakati mwingine watateseka sana kutokana na hisia za majuto, na watajisikia kudhalilika machoni mwao, na kupoteza heshima kwao wenyewe. {2T 392.3}

Ndugu na dada, hamueleweki mbele za Mungu. Mmeshindwa kutekeleza wajibu wako nyumbani, katika familia yako mwenyewe. Hamkuwadhibiti watoto wako. Umeshindwa sana kujua na kuyafanya mapenzi ya Mungu, na baraka Yake haijaegemea familia yako. Ndugu E, umekuwa mbinafsi. Umekuwa na kujithamini kukubwa. Umedhani kwamba una kiwango kizuri cha unyenyekevu, lakini haujajielewa. Njia zako si sawa mbele za Mungu. Ushawishi wako na mfano haujalingana na maneno yako. Unatafuta makosa mengi waliyo nayo wengine; unaona wanapotoka na hawako sawa, lakini wewe ni kipofu kwa kosa hilo hilo, hakika lipo kwako mwenyewe. {2T 392.4}

Dada E amekuwa mbali na Mungu. Moyo wake haujatiishwa na neema. Upendo wake kwa ulimwengu, na wa vitu vilivyo katika ulimwengu, umefunga moyo wake kwa upendo wa Mungu. Upendo wa mavazi na muonekano umemzuia asiwe mzuri, na umemwongoza kuweka akili yake na mapenzi juu ya vitu hivi vya kijinga. Kutoamini kumekuwa kukiimarika moyoni mwake, na amekuwa akipenda kweli kidogo, na anaona kivutio kidogo katika unyenyekevu wa utauwa wa kweli. Hajahimiza ukuaji wa neema za Kikristo. Hajapenda unyenyekevu au kujitoa wakfu kwa ibada. Amechukua makosa ya wale waliodai kuwa wamejitolea kwa ile Kweli, na akafanya ukosefu wao wa kiroho, makosa yao, na dhambi zao kuwa kisingizio kwa tabia yake ya kupenda ulimwengu. Ametazama mwendo wa wale ambao walikuwa wameunganishwa na ----, na ambao walikuwa mbele kuchukua juu yao mizigo ya kanisa, na amehusisha kufeli kwake kwa makosa yao, akisema kwamba yeye hakuwa mbaya zaidi kuliko wao. Watu kama

hao na wenye msimamo mzuri walifanya hivi au vile, na alikuwa na haki kufanya hayo, kama wao. Vile vile hawakuishi wakifanya matengenezo ya afya bora kuliko yeye; walinunua na kula nyama, na walikuwa wana nafasi za juu kanisani, na hivyo alikuwa na udhuru, kwa kweli, na mfano kama huo, ikiwa angefanya vivyo hivyo. {2T 393.1}

Hii sio kesi pekee ambapo kupuuza kufuata nuru ambayo Bwana ametoa kumefunikwa nyuma ya makosa ya wengine. Ni kwa aibu ya wanaume na wanawake wenye akili mahiri, kwamba hawana kiwango cha juu zaidi kuliko kile cha wanadamu wasio wakamilifu. Mwenendo wa wale wanaowazunguka, hata kama hawajakamilika, huchukuliwa na wengine kama kisingizio cha kutosha kwao, kufuata njia ile ile. Wengi watayumbishwa na ushawishi wa ndugu fulani anayeongoza. Ikiwa huyo ndugu ataacha shauri la Mungu, mfano wake unashikwa kwa furaha na wale ambao hawajajiwekwa wakfu, ambao sasa wanahisi kuwa wako huru na kizuizi. Sasa wana udhuru; na mioyo yao isiyojitakaswa hujisifu katika fursa ya kupendeza matamania yao na kuchukua hatua karibu na ushirika na roho ya ulimwengu, ambapo wanaweza kufurahia anasa zake na kuridhisha hamu yao. Kwa hivyo huweka juu ya meza zao, vitu ambavyo sio vya afya sana, na ambavyo wamefundishwa kuacha, ili kuhifadhi hali bora zaidi ya afya. {2T 393.2}

Kumekuwa na vita mioyoni mwa wengine, tangu matengenezo ya afya yalipoanzishwa. Wamehisi uasi ule ule kama wana wa Israeli wakati hamu zao za chakula zilipozuiliwa katika safari yao kutoka Misri kwenda Kanaani. Wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, ambao maisha yao yote waliendekeza raha zao na masilahi yao wenyewe, kujifurahisha kwao wenyewe, urahisi wa maisha na matamania yao wenyewe, hawako tayari kubadilisha mwenendo wao na kuishi kwa utukufu wa Mungu, wakiiga maisha ya kujitolea yasiyo na mifano ya makosa. Mfano kamili umetolewa kwa Wakristo kuiga. Maneno na kazi za wafuasi wa Kristo ni njia ambayo kanuni safi za Ukweli na utakatifu zinawasilishwa kwa ulimwengu. Wafuasi wake ni chumvi ya dunia, na nuru ya ulimwengu. {2T 394.1}

Dada E, huwezi kutambua baraka nyingi ulizopoteza kwa kufanya mapungufu ya wengine kuwa dawa ya kutuliza dhamiri yako kwa

kupuuza wajibu wako. Umekuwa ukijilinganisha na wengine. Njia zao zilizopotoka, kushindwa kwao, imekuwa kitabu chako cha kiada. Lakini makosa yao, ujinga wao na dhambi, haufanyi kutomtii kwako MUNGU kwako kuwa sio dhambi kubwa. Tunasikitika kwamba wale ambao wanapaswa kuwa msaada kwako katika juhudi zako za kushinda kujipenda nafsi, kiburi cha moyo wako, ubatili wako na kupenda kukubali vya ulimwengu, vimekuwa kikwazo tu kwako kwasababu ya upungufu wa viwango vya kiroho na utauwa wa Kweli . Hatuwezi kukuambia ni kwa kiasi gani tunajuta kwamba wale ambao wanapaswa kuwa Wakristo ambao wanapaswa kujikana nafsi, bado wako mbali sana kufikia kiwango hicho. Wale ambao wanapaswa kuwa thabiti, wanaoendelea na bidii katika kazi ya Mungu, wanadhoofishwa na Shetani kwa sababu wanakaa mbali sana na Mungu. Wanashindwa kupata nguvu ya neema Yake, ambayo kwayo wanaweza kushinda udhaifu wa asili yao, na, kwa kupata ushindi katika ishara kwa Mungu, waonyeshe wale walio na imani dhaifu njia, Ukweli, na uzima. {2T 394.2}

Jambo ambalo limetukatisha tamaa kiasi kikubwa limekuwa kuwaona wale walio ---- ambao wamekuwa na uzoefu wa miaka katika huduma na kazi ya Mungu, na nguvu zao, zimepunguzwa kwa kutokuwa na uaminifu kwao. Wamekuwa wakishindwa katika kila pigano na adui wakati wanashambuliwa. Mungu angewafanya watu hawa kuwa na nguvu, kama walinzi waaminifu katika kazi yao ya kulinda ngome, ikiwa wangetembea katika nuru aliyowapa na kubaki imara kwa jukumu, wakitafuta kujua na kuyafanya mapenzi ya Mungu yote. Shetani, bila shaka, kupitia udanganyifu wake, atazidanganya hizi roho zenye mapungufu/uovu, na kuzifanya ziamini kwamba ziko sawa kila wakati. Hawajatenda dhambi mbaya, hawajaangukia katika uovu, na lazima, baada ya yote, wapo tu kwenye msingi wa Kweli, na kwamba Mungu atakubali kazi zao. Hawaoni dhambi maalum wanazopaswa kutubu, hakuna dhambi ambazo zinahitaji udhalilishaji maalum, ungamo la unyenyekevu, na kujitoa moyo. Udanganyifu wa namna hii ni wenye nguvu kweli wakati wanakosea sura ya utauwa kwa nguvu yake, watu wenye kumcha Mungu, lakini wataikana nguvu Yake, na wanajidanganya kwamba wao ni matajiri na hawahitaji chochote. Laana ya Merozi iko juu yao: "Ulaaniwe Merozi, alisema malaika wa

Bwana, Walaanini kwa uchungu wenyeji wake; kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu "{2T 395.1}

Dada yangu, usisingizie kasoro zako kwa sababu eti wengine wanakosea. Katika siku ya BWANA hautathubutu kuomba hiki kiwe kisingizio cha kupuuza kwako kuunda tabia ya mbinguni, yaani wengine hawakuonyesha kujiweka wakfu kwa mambo ya kiroho. Upungufu huo huo ambao uliugundua kwa wengine ulikuwa ndani yako mwenyewe. Na ukweli ni kwamba japo wengine walikuwa wenye dhambi, hiyo haifanyi dhambi zako kuwa si mbaya. Wote ninyi, wao na wewe, ikiwa mtaendelea katika hali yenu ya sasa ya kutokamilika, mtatenganishwa na Kristo, na kuwa pamoja na Shetani na malaika zake, na mtaadhibiwa na uharibifu wa milele kutoka kwa uwepo wa Bwana na kutoka kwa utukufu wa nguvu Yake. {2T 396.1}

Bwana aliandaa majaliwa/nafasi ya kutosha, kwamba ikiwa utamtafuta, na kufuata nuru atakayokupa, basi hutaanguka njiani. Neno la Mungu ulipewa wewe kama taa ya miguu yako, Mwanga wa njia yako. Ikiwa utajikwaa, itakuwa kwa sababu hujawasiliana na Mwongozi wako, yaani Neno la Mungu, na kulifanya Neno hilo la thamani kuwa kanuni ya maisha yako. Mungu hakukupa kama mfano maisha ya mwanadamu mwingine yeyote, hata maisha ya huyo mwanadamu yawe mazuri na kudhihirishwa kutokuwa na mawaa. Ikiwa utafanya kama wengine na kuenenda kama wengine wanavyoenenda, mwishowe utaachwa nje ya Jiji Takatifu, na umati mkubwa ambao pia umefanya kama vile vile wewe ulivyofanya, wakifuata mfano ambao Bwana hakuwaachia, hwa watapotea kama wewe utakakavyopotea. {2T 396.2}

Yale ambayo wengine wamefanya, au wanaweza kufanya siku za usoni, hayatapunguza jukumu lako au hatia. Wewe umepewa kielelezo, maisha yasiyo na makosa yenye sifa ya kujinyima na ukarimu usio na ubinafsi. Ukiacha mfano huu sahihi, mfano huu mzuri, na kuchukua ile isiyo sahihi, ambayo imewasilishwa wazi katika Neno la Mungu kama ile ambayo unapaswa kuachana nayo, hatua yako itapata mshahara unaostahili; maisha yako yatakuwa bila mafanikio. {2T 396.3}

Moja ya sababu kubwa za kudidimia kwa kanisa huko ----- ni kujipima wao wenyewe kwa wenyewe na kujilinganisha wao kwa wao. Ni wachache tu ambao wana kanuni hai katika nafsi na wanaomtumikia Mungu kwa jicho moja tu yaani wakiangalia utukufu Wake tu. Wengi katika ----- hawakubali kuokolewa kwa njia iliyochaguliwa na Mungu. Hawachukulii kwa umakini kushugulikia wokovu wao wenyewe kwa hofu na kutetemeka. Mwishowe hawaoni; na, badala yake huwa na shida ya kupata uzoefu kupitia juhudi za kibinafsi, watakuwa na hatari ya kuegemea wengine na kuamini uzoefu wao. Hawawezi kukubali kukesha na kuomba, kuishi kwa ajili ya Mungu, na Yeye tu. Inapendeza zaidi kuishi kwa kujitii mwenyewe kuliko BWANA. {2T 396.4}

Kanisa huko ----- wamejazwa na kurudi nyuma kwao wenyewe, na hawahitaji kuwa na ndoto za mafanikio, hadi wale wanaliotaja jina la Kristo watakapokuwa waangalifu kutoka katika uovu wote, hadi watakapojifunza kukataa uovu na kuchagua mema. Tunatakiwa kukesha na kuomba bila kukoma; kwa kuwa mtego umewekwa njiani mwetu, na tutapata majaribu yake Shetani wakati ambapo hatutegemei. Ikiwa wakati huo hatutazingatia maombi, basi tutabebwa na adui na tutapata hasara iliyokusudiwa. {2T 397.1}

Ni jukumu zito kiasi gani limepewa wazazi! Kwa udogo wa kiasi gani umepata hisia juu ya uzito wa mzigo huu! Kiburi cha moyo, kupenda kujionyesha, na kutotawala hamu ya kula vimezishika akili zako. Vitu hivi vimekuwa vya kipaumbele kwako, na ujio wa adui haukutambuliwa. Adui amepanda Viwango vyake ndani ya nyumba yako na kutia muhuri wa sanamu yake ya kuchukiza juu ya tabia za watoto wako. Lakini ulikuwa umepofushwa sana na muungu wa ulimwengu huu, ulikuwa mfu sana kwa mambo ya kiroho na ya mbingu, hata usingeweza kugundua faida ambayo Shetani alikuwa ameipata au utendaji kazi wake, hapo katika familia yako. {2T 397.2}

Umewaleta watoto ulimwenguni ambao hawakuwa na sauti kuhusu kuzaliwa kwao. Mmekuwa mawakili na kuwajibika kwa kiwango kikubwa kwa furaha yao ya baadaye, na ustawi wao wa milele. Mzigo uko juu yako, uwe una busara au la bado upo tu, kufundisha watoto



hawa kwa Mungu, kuwaangalia kwa uangalifu na wivu mara tu anapokuja adui mjanja na uwe tayari kuinua kiwango dhidi yake. Jenga ukuzaji wa sala na imani juu ya watoto wako, na fanya mazoezi ya kukesha kwa bidii na uadilifu. Hauko salama hata kidogo dhidi ya mashambulio ya Shetani. Huna wakati wa kupumzika kutoka kwa shuguli ya kukesha kwa bidii kwenye kituo chako. Haupaswi kulala hata muda kidogo kwenye kituo chako cha ulinzi. Hii ni vita muhimu zaidi. Matokeo ya milele yanahusika. Ni kufa na kupona, kwako wewe na familia yako. Usalama wako pekee ni moyo wako upondeke mbele za Mungu na kuutafuta ufalme wa mbinguni kama mtoto wadogo. Hauwezi kuwa mshindi katika vita hivi ikiwa utaendelea kufuata mwenendo uliofuatila awali. Haujakaribia karibu na ufalme wa mbinguni. {2T 397.3}

Wengine ambao hawajamkiri Kristo, wako karibu na ufalme wa Mungu kuliko vile wanavyodai watunza Sabato katika ----. Humkujiweka ndani ya upendo wa Mungu na kuwafundisha watoto wenu kumcha Bwana. Hamkuwafundisha Ukweli kwa bidii na uadilifu, mliposimama, na mlipoketi, na mlipotoka, na mlipoingia. Hamkuwazuia. Mnaangalia watoto wa wengine na kujifariji kwa kusema: "Watoto wangu sio wabaya kushinda watoto wao." Hii inaweza kuwa kweli, lakini je! Kutotelekeza majukumu kwa wengine kunafanya wajibu wako kupungua nguvu kwa maagizo ambayo Mungu ameamuru wewe kama mzazi? Kwako yamewekwa majukumu ya kulea watoto hawa kwa ajili Yake, na wokovu wao unategemea kwa kiwango kikubwa juu ya elimu wanayopata katika utoto wao. Wajibu huu wengine hawawezi kuuchukua; ni wako, peke yako, kama mzazi. Unaweza ukatumia misaada yote unayoweza kupata ili kufanikisha hii kazi kuu na muhimu; lakini baada ya kufanya yote haya, kuna nguvu juu ya kila wakala wa kibinadamu, ambao itafanya kazi nawe kupitia njia ambayo ni fursa yako kuitumia. Mungu Atakusaidia, na kwa uwezo Wake unaweza kumtegemea. Uwezo Wake hauna kikomo. Wakala za kibinadamu zinaweza zisifanikiwe, lakini Mungu anaweza kuwaongezea matunda kwa kufanya kazi ndani yenu na kupitia kwenu. {2T 398.1}

Una kazi ya kufanya, kuiweka nyumba yako sawa ili iwe na utaratibu. Malaika safi, wasio na dhambi hawawezi kufurahi kuvinjari katika

makao ambayo uovu mwingi unafanywa. Umelala kwenye kituo chako cha ulinzi. Vitu visivyo na umuhimu vimechukua akili zako badala ya mambo mazito zaidi. Inapaswa kuwa shuguli ya kwanza maishani mwako kuutafuta ufalme wa mbinguni na haki Yake; ndipo una ahadi kwamba vitu vyote vingine utazidishiwa. Hapa ndipo umeshindwa katika familia yako. Endapo ungekuwa unateseka moyoni kwamba wewe na familia yako mnawezaje kuingia katika lango jembamba, mngokusanya kwa bidii kila mwale wa nuru ambayo Bwana ameruhusu kuangazia njia yenu, na mngependa kutembea katika hiyo. {2T 399.1}

Hujazingatia nuru ambayo Bwana amekupa kwa neema juu ya matengenezo ya afya. Umejisia kuinuka dhidi yake. Hujaona umuhimu wake, hakuna sababu inayokufanya usiupokee ujumbe huu. Hujajisia kuzuia hamu/tamaa yako ya kula. Hujaona hekima ya Mungu katika kupewa nuru kuhusu kizuizi cha hamu ya kula. Yote ambayo uliweza kutambua ni usumbufu uliokufikia wa kutawala hamu ya chakula. Bwana ameacha nuru Yake ituangazie katika siku hizi za mwisho, ili utusitusi na giza ambalo limekuwa likikusanyika katika vizazi vilivyopita kwa sababu ya dhambi ya ulafi iweze kufutiliwa mbali kwa kiasi fulani. Na kwamba mlolongo wa maovu ambayo yamesababishwa kwa sababu ya kula sana na kunywa iweze kupunguzwa. {2T 399.2}

Bwana kwa hekima amekusudia kuwaleta watu Wake katika nafasi ambayo wangejitenga na ulimwengu kiroho na kiutendaji, ili watoto wao wasiweze kuongozwa kwa urahisi katika ibada ya sanamu na wachafuliwe na uharibifu wa zama hizi. Ni mpango wa Mungu kwamba wazazi waaminio na watoto wao wasimame kama mawakili hai wa Kristo, raia mbinguni wanaotarajiwa. Wote ambao ni washirika wa tabia ya Uungu, wataokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa zake. Haiwezekani kwa wale ambao huendekeza na tamaa ya chakula kufikia ukamilifu wa Kikristo. Hauwezi kuamsha hisia za maadili za watoto wako wakati wewe sio mwangalifu katika uteuzi wa chakula chao. Meza ambazo, kwa kawaida wazazi huandaa kwa watoto wao ni mtego kwao. Lishe yao sio rahisi, na haijaandaliwa kwa njia ya kiafya. Chakula hiki mara nyingi kina mafuta na sukari nyingi na husababisha homa, huwa na tabia ya kuchochea na kusiimua sehemu

laini ya juu ya tumbo (ukuta wa tumbo-lining). Tabia za kinyama huimarishwa na kutawala, wakati nguvu za kimaadili na kiakili zimedhoofishwa na mtu kuzitumikia tamaa za mwili. Unapaswa kujifunza kuandaa chakula rahisi lakini chenye lishe kamili. Nyama, na keki zenye sukari nyingi, na mikate iliyoandaliwa na viungo vya aina yoyote, sio lishe yenye afya wala mlo ulio kamili. Mayai hayapaswi kuwekwa juu ya meza yako. [*Tazama Kiambatisho*]. Ni jeraha kwa watoto wako. Matunda na nafaka, yaliyoandaliwa kwa njia rahisi zaidi, ndio yenye afya zaidi, na yatatoa lishe kubwa kwa mwili, na, wakati huo huo, hayatadhuru akili. (Ushauri wa mayai sio wa jumla, ila kwa kesi ya mtu katika 7Shuhuda uk, 135, MH320, na 9T162 ) {2T 399.3}

Kula kwa mpango au masaa maalum ni muhimu sana kwa afya ya mwili na utulivu wa akili. Watoto wako wanapaswa kula tu wakati wa milo ya kawaida. Hawapaswi kuruhusiwa kutoka nje ya sheria hii iliyowekwa. Wakati wewe, Dada E, unapokosekana nyumbani, huwezi kudhibiti mambo haya muhimu. Tayari mwana wako mkubwa amepunguza nguvu ya mfumo wake wote na kuweka msingi wa ugonjwa wa kudumu. Mtoto wako wa pili anafuata kwa kasi katika hatua zake, na hakuna hata mmoja wa watoto wako aliye salama kutoka kwa uovu huu. {2T 400.1}

Unaweza usipate ukweli kutoka kwa watoto wako kuhusu tabia zao. Wale ambao hufanya uovu huu kwa kujificha wakifanya punyeto, watasema uongo na kudanganya. Watoto wako unaweza kukudanganya, kwani hauko katika hali ambayo unaweza kujua ikiwa watajaribu kukupotosha. Kwa muda mrefu umepofushwa na adui hivi kwamba unakuwa na nuru ndogo ya mwangaza wa kutambua giza. Kuna kazi kubwa, nzito, na muhimu kwako kuifanya mara moja, kuweka mioyo yenu na nyumba kwenye utaratibu. Njia yako salama ni kujitoa na kufanya hii kazi inavyotakiwa. Usijidanganye na ukaamini kwamba, hata hivyo, jambo hili limewasilishwa mbele yako kwa lugha ya kutia chumvi sana. Sijafunika chochote. Nimesema Ukweli ambao utakupa mtihamu wa kuamua. Amkeni! amkeni! Niwasihi, kabla ya hamjachelewa kurekebisha makosa, na wewe na watoto wako mkaangamia katika uharibifu wa jumla. Shika kazi nzito ya wakfu, na ulete msaada wa kila mwale wa nuru kwako ambao unaweza

kuukusanya ambao ilianguza kwenye njia yako ila hukuwa umeithamini na kwa pamoja ongeza na msaada wa nuru inayoanguza sasa, anza uchunguzi wa maisha yako na tabia, kana kwamba kama upo mbele ya mahakama kuu ya Mungu. "Jiepusheni na tamaa za mwili, ambazo zinapingana na roho," ni himizo la mtume. Ufisadi na rushwa vimeshamiri kila upande, na usipokuwa na nguvu zisizo za kibinadamu za kutegemea kusimama dhidi ya nguvu ya uovu, utashindwa na kuanguushwa chini na upotevu wa sasa. Bila utakatifu hakuna mtu atakayemwona Mungu. {2T 400.2}

Bwana anawajaribu na kuwathibitisha watu Wake, Malaika wa Mungu wanaangalia ukuaji wa tabia na kupima thamani ya maadili. Mlango wa rehema unakaribia kufungwa, nawe haujawa tayari. Laiti neno la onyo lingeweza kuwaka mioyoni mwenu! Uwe tayari! Jitayarishe! Jitayarishe! Fanyeni kazi zenu mchana ukiwepo, maana usiku unakuja ambapo hakuna mtu awezaye kufanya kazi. Agizo litatoka: mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu. Hatima ya wote itaamuliwa. Wachache, ndio, ni wachache tu, katika idadi kubwa ya watu ambao wapo duniani, watakaokolewa na kupata uzima wa milele, wakati umati ambao haujakamilisha utakaso wa roho zao katika kutii Ukweli watateuliwa kwa kifo cha pili. Ee Mwokozi, tunza ununuzi wa damu Yako, ndicho kilio cha moyo wangu wenye uchungu. {2T 401.1}

Nina hofu sana kwako na kwa wengi wanaodai kuamini Ukweli katika ---. O, chunguza, chunguza kwa uadilifu na bidii mioyo yenu wenyewe, na mfanye kazi kamilifu kwaajili ya hukumu! Nina uchungu moyoni ninapokumbuka ni watoto wangapi wa wazazi wanaotunza Sabato wanaoharibu roho na miili kwa uovu wa siri (punyeto). Karibu na wewe kuna familia inayoonyesha tabia zao mbaya katika miili yao na akili zao pia. Watoto hawa wako kwenye barabara ya moja kwa moja, kuelekea upotevuni. Wamejidhalilisha, na wamewafundisha wengine wengi katika uovu huu. Mvulana mkubwa amekuwa mbilikimo, kimwili na kiakili, kwa kujiingiza katika mazoezi ya punyeto. Akili ndogo aliyosalia nayo ni ya hali ya chini. Ikiwa ataendelea na tabia hii mbaya mwishowe atakuwa zezeta. Kila kutokuwa na kiasi kwa watoto ambao wamekua, ni uovu mbaya na utatoa matokeo mabaya, kuupungizia nguvu mfumo

na kudhoofisha akili. Lakini kwa wale ambao wanajiingiza kwenye tabia hii mbaya kabla ya kukua kwao, athari mbaya zinawekwa wazi zaidi, na kupona kutokana na athari zake ni kunazidi kupoteza tumaini. Mwili ni dhaifu na umedumaa; misuli imetepeta; macho huwa madogo, na wakati mwingine huonekana kuvimba; kumbukumbu siyo salama, na inakuwa kama chujio; kwa kutokuwa na uwezo wa kutilia makini mambo na mafunzo yanapongezeka. {2T 402.1}

Kwa wazazi wa watoto hawa ningesema: Mmeleta watoto ulimwenguni kuwa laana tu kwa jamii. Ni watu wasiotii, wenye hasira, wagomvi, na wabaya. Ushawishi wao kwa wengine unaharibu. Wanabeba muhuri wa tabia ya baba, ya tamaa zake za mwili. Hasira yake ya haraka na kikatili inaakisiwa ndani yao. Wazazi hawa walipaswa kwenda mashambani zamani, na hivyo kujitenga na jamii ya watoto wale ambao hawangeweza kunufaika nao, bali kuwadhuru tu. Sekta thabiti za stadi shambani, zingekuwa baraka kwa watoto hawa, na ajira ya kila wakati, kama nguvu zao zingeweza kuvumilia, hili lingewapatia nafasi ndogo ya kuharibu miili yao kwa kujichua, na ingewazuia kuwafundisha idadi kubwa ya wengine katika tabia hii ya kuzimu. Kazi ni baraka kubwa kwa watoto wote, haswa kwa daraja hilo ambalo akili zao zina mwelekeo wa uovu (vice) na upotovu. {2T 402.2}

Watoto hawa wamewasiliana na maarifa zaidi ya uovu katika ---- Hata Juhudi zote za umoja za wahudumu na watu wanaodai utauwa zingefanya wasingeweza kuwabadilisha. Wengi ambao wamejifunza kutoka kwa watoto wako wataenda kwenye upotevu badala ya kudhibiti tamaa zao na kuacha utovu wa dhambi hii. Akili moja yenye uovu inaweza kupanda mbegu mbaya kwa kipindi kifupi kuliko vile watu wengi wanavyoweza kung'oa ufidia huo, hata kama wangetumia muda wa maisha yao yote. Watoto wako ni 'usemi/msemo wa mfano' katika vinywa vya wale wanaoutukana Ukweli. Hawa ni watoto wa watunza Sabato, lakini wao ni wabaya kuliko watoto wa watu wa mataifa kwa ujumla. Wanamiliki ubora mdogo, hawajiheshimu wenyewe. Ndugu F amekuwa hana heshima katika kazi ya Mungu. Hasira yake ya haraka na ushawishi wa jumla haukuwa na mwelekeo wa kuinua, lakini kushuka kwa kiwango cha chini. Kazi ya Mungu imetukanwa vibaya kwa kukosa kwake maamuzi na

uboresaji/utakaso. Ingekuwa bora zaidi kwaajili ya kulinda Kweli ikiwa familia hii ingeondolewa zamani katika nafasi waliyopewa kusimamia, na wawe ambapo pamejitenga zaidi ili ushawishi wao usisikike au kuonekana sana. Watoto wao wameishi katika nuru ya Ukweli na wamekuwa na fursa ambazo ni watoto wachache tu wamezipata; lakini wakati huu wote hawajafaidika, lakini wamekuwa wakikua zaidi na zaidi katika upotovu huu mgumu. Kuondolewa kwao hapo kungekuwa baraka kwa kanisa na kwa jamii, na kwa familia nzima. Ajira thabiti inayohusiana na ardhi itakuwa mbaraka kwa baba na watoto, wangeweza kufaidika na kilimo. {2T 403.1}

Niliona kwamba familia ya Ndugu G inahitaji kazi kubwa kufanywa kwao. H na I wameenda mbali katika uhalifu huu wa kujichua; haswa hii ni kweli kwa H, ambaye amekwenda mbali katika mazoezi ya dhambi hii, kiasi kwamba akili yake imeathiriwa, macho yake yamedhoofika, na ugonjwa umemfunga. Shetani ana udhibiti kamili wa akili ya kijana huyu masikini, lakini wazazi wake hawako macho kuona uovu na matokeo yake. Akili yake imefanywa duni, dhamiri yake imepata sugu, hisia zake za maadili zimepungua, na atakuwa mwathirika tayari wa kushirikiana na marafiki waovu kutenda dhambi na uhalifu. Ndugu na Dada G, amkeni, nawasihi sana. Hamjapokea nuru ya matengenezo ya afya na kuifanyia kazi. Ikiwa mngezuia tamaa ya chakula mngeokoa muda wa kazi na fedha; na, kilicho cha matokeo makubwa zaidi, ni kwamba ungekuwa umehifadhi kwako hali bora ya afya ya mwili na kiwango kikubwa cha nguvu ya kiakili kufahamu Ukweli wa milele; ungekuwa na ubongo ulio wazi kupima ushahidi wa Ukweli na ungekuwa tayari zaidi kuwapa wengine sababu ya tumaini lililo ndani yako. Chakula chako sio sahili, na chenye afya ambacho kitatengeneza damu bora. Damu yenye uchafu hakika itaficha nguvu za maadili na kiakili, na kuamsha na kuimarisha tamaa za asili yako. Hakuna yeyote kati yenu anayeweza kumudu chakula kinacholeta homa na msisimko, kwa sababu ni kwa gharama ya afya ya mwili na ustawi wa nafsi zako na roho za watoto wako. {2T 404.1}

Unaweka mezani chakula ambacho kinachosha viungo vya kumengenya, husisimua tamaa za kinyama, na kudhoofisha nguvu za kimaadili na kiakili. Chakula chenye lishe tajiri kama mafuta na sukari

nyingi, na vyakula vilivyokobolewa na kusindikwa na nyama havina faida kwako. Laiti ungejua asili ya nyama unayokula, je! Ungewajua Wanyama hawa ambao nyama hizi zilichukuliwa kabla hawajafa, ungegeuka na kuchukia nyama yako. Wanyama wale ambao nyama yao unakula huwa na magonjwa, na mara nyingi hivi kwamba, wangeacha bila kuchinjwa, wangekufa wenyewe; lakini wakati pumzi ya uhai iko ndani yao, wanauawa na kuletwa sokoni. Unachukua moja kwa moja kwenye mfumo wako hisia zao na sumu ya aina mbaya zaidi, na bado haujatambua. Unapenda kuendekeza tamaa ya chakula. Una somo hapa la kujifunza: Kwa hiyo, ulapo, au unywapo, au ufanyapo kitu chochote, fanya yote kwa utukufu wa Mungu. "{2T 404.2}

Nakusihi, kwa ajili ya Kristo, uweke nyumba yako na mioyo sawa - katika utaratibu. Ruhusu Ukweli wa asili ya mbinguni kukuinua na kukutakasa, nafsi, mwili, na roho. "Jiepusheni na tamaa za mwili, ambazo zinapingana na roho." Ndugu G, kula kwako kuna tabia ya kuimarisha tamaa mbaya za maadili mabovu. Haudhibiti mwili wako kama wajibu wako unavyopasa kufanywa ili kukamilisha utakatifu katika hofu ya Mungu. Kiasi katika kula lazima kufanyike kabla hujapata tabia ya uvumilivu. Kumbuka kwamba umewapa watoto wako, kwa kiwango kikubwa, muhuri wa tabia yako mwenyewe. Unapaswa kujilinda, na usiwe mkali, jeuri au mwenye papara. Shughulika nao kwa uamuzi thabiti, lakini kwa uvumilivu, kwa upendo, kwa huruma, kama vile Yesu anavyokushughulikia. Kuwa mwangalifu jinsi unavyokemea. Uwe mvumilivu kwa watoto wako, lakini usiwaachie kufanya wanavyotaka. Hii umepuuza sana. Hujawarekebisha kwa njia inayofaa, kwa vile wewe binafsi hujaithibiti kikamilifu roho yako. Kazi kubwa lazima ifanyike kwenu nyinyi wawili. {2T 405.1}

Ndugu G, kama ungeendelea kutoka nguvu hadi nguvu, kuifuata nuru ambayo Bwana ametoa, Yeye angekuchagua sasa uwe kama chombo cha haki. Una talanta; una uwezo; unaweza kufanya kazi kwa utukufu wa Mungu; lakini haujajisalimisha kikamilifu kwa Mungu. Laiti ungetafuta kuwa naupole, utafute haki ya Kristo, ili ufichwe siku ya ghadhabu kali ya Bwana! {2T 405.2}

Ndugu na dada mpendwa, mnapaswa kushikiana kwa umoja na kwa uvumilivu kurekebisha haki yako ya usimamizi wa watoto wako. Dada G umekuwa hauna kiasi; bado mkiungana, pamoja na kwa upendo mnaweza kufanya mengi, hata sasa, kuweka mioyo ya watoto wako kwako na kuwafundisha njia nzuri na sahihi. Mna kazi ya kufanya katika kuweka mioyo yenu na ya nyumba yako kwenye utaratibu. Unapaswa kukuza utendaji wenye maelewano. Ushawishi wa kubadilishwa na Roho wa Mungu unaweza kufanya kazi kubwa kwenu ninyi nyote wawili, na mtaunganisha mioyo yenu na juhudi katika kazi ya matengenezo katika familia yenu. Kuudhika kote, Kutoridhika, manung'uniko, na kuwaka hasira kwa haraka kunapaswa kukoma. Athari zake ni kuwadhoofisha niinyi wawili na kuharibu ushawishi ambao lazima utumiwe ikiwa mnataka mfanikiwe kuwafundisha watoto wenu kuingia mbinguni. {2T 405.3}

Shetani sasa ana kiwanja. Watoto wako maskini ni mateka wake; adui ana udhibiti wa akili zao na huwafanya wachukue mwelekeo wa kwenda chini. Hisia zao za maadili zinaonekana kupooza. Wamejichua na kujisifu katika maovu yao. Wavulana kama hao wana uwezo wa kueneza sumu katika mtaa mzima, kwa majirani au jamii, na ushawishi wao kufisha utahatarisha wote wanaowasiliana nao katika mazingira ya shule. Watoto wako wameharibika katika mwili na akili. Uovu umeweka alama kwa watoto wako wakubwa. Wamechafuliwa, wamechafuliwa sana, na dhambi. Tabia za wanyama zinawatawala, wakati uwezo wa maadili na akili ni dhaifu sana. Tamaa za tabia mbovu, zinazoelekea chini zimepata nguvu kwa kuzifanyia mazoezi, wakati dhamiri imekuwa ngumu na kuunguzwa. Huu ndio ushawishi ambao ufisadi (vice) utaweka kwenye nguvu za akili. Wale wanaojitolea kufanya kazi ya uharibifu wa miili yao na akili zao hawaishii hapa. Hatimaye watapatikana wapo tayari kujiingiza kwenye uhalifu wa karibia aina yoyote, kwa kuwa dhamiri zao zimeungua. Wazazi hawajaamshwa hata nusu, kuhusu kutambua jukumu lao la kuwa wazazi. Wao wamechukua likizo kutoka kwa wajibu wao. Hawafundishi watoto wao uovu wa tabia hizi hatarishi, zinazoharibu wema. Mpaka wazazi waamke, hakuna tumaini kwa watoto wao. {2T 406.1}



Naweza kutaja kesi za wengine wengi, lakini nitaacha, isipokuwa katika visa vichache. J ni mshirika hatari. Yeye ni mhusika wa somo la uovu huu. Ushawishi wake ni mbaya. Neema ya Mungu haina ushawishi juu ya moyo wake. Ana akili nzuri, na baba yake ameamini sana kwamba hilo litamsaidia kusawazisha mambo; lakini nguvu ya akili peke yake sio dhamana ya ubora wa wema. Kukosekana kwa kanuni ya kidini humfanya fisadi moyoni na mjanja katika maovu yake. Ushawishi wake ni mbaya kila mahali. Yeye ni kafiri katika kanuni zake na anajisifu katika kutomwamini MUNGU. Wakati akiwa na wale wa rika lake, au wale walio wadogo kuliko yeye, anazungumza kwa kujua juu ya mambo ya kidini kwa mzaha na anadhihaki Ukweli na Biblia. Ujuzi huu wa kujifanya una ushawishi kwa akili zilizopotoka na kusababisha vijana wa kiume waonee aibu Ukweli. Wenzi wa aina hiyo wanapaswa kuepukwa kabisa, kwani hii ndiyo njia pekee ya uhakika kwa usalama. Mabinti wadogo wanapendezwa kuhusiana na huyu kijana; hata wengine wanaodai kuwa Wakristo wanapendela kuwa naye. {2T 406.2}

K ni mvulana ambaye anaweza kujenga tabia njema ikiwa amezungukwa na ushawishi sahihi. Anahitaji mfano sahihi. Ikiwa vijana wanaomkiri Kristo wangemheshimu Yeye maishani mwao, wangeweza kutoa ushawishi ambao unaweza kupinga ushawishi mbaya wa vijana kama ule wa J. Lakini vijana kwa ujumla hawana dini zaidi ya wale ambao hawajawahi kutamka jina la Kristo. Hawaachani na uovu. Mvulana mwerevu, mwenye akili, kama J, anaweza kuwa na ushawishi mkubwa wa uovu. Ikiwa akili hizi nyingi zingedhibitiwa kwa uzuri na kupenda haki, zingekuwa na nguvu kwa mema; lakini ikiwa itapindishwa kwenye upotovu, ushawishi wake mbaya kwa washirika wake hauwezi kukadiriwa, na hakika utamtumbukiza katika upotevu. Akili nzuri iliyoharibiwa na uovu hufanya moyo kuwa mbaya sana. Akili mahiri iliyotakaswa na Roho wa Mungu ina nguvu iliyofichwa na inasambaza nuru na usafi kwa wote ambao mmiliki mwenye furaha anahusiana nao. {2Tsw 407.1}

Ikiwa mvulana mwenye uwezo wa akili mkubwa kama J angekabidhi moyo wake kwa Kristo, ingekuwa wokovu wake. Kwa njia ya dini safi akili yake ingeletwa kwenye njia ya afya; nguvu zake za kiakili na kimaadili zingekuwa zenye imara kwa uwezo na zenye usawa; dhamiri,

iliyoangaziwa na neema ya BWANA, ingefanya kazi kwa wepesi na usafi, kudhibiti mapenzi yake na matakwa, na kusababisha Ukweli na unyofu katika kila tendo la maisha. Bila kanuni za dini, kijana huyu atakuwa mjanja mjanja, asiye mkweli, feki na msanii, katika njia mbaya, na atawatia sumu wale wote anaoshirikiana nao. Ninawaonya vijana wote wajihadhari na kijana huyu ikiwa ataendelea na kupotosha dini na Biblia. Hamuwezi kuwa kujilinda vya kutosha mkiwa mnahusiana naye. {2T 407.2}

Kwa kushirikiana na wale wavulana ambao hawana ushawishi mzuri, L pia anaharibiwa. J na K sio washirika wenye faida kwake, kwani hushawishiwa kwa urahisi katika mwelekeo mbaya. ----- sio mahali bora kwake. Tabia zake sio safi; anajichua. Kwa sababu ya hili na upendo wake kwa kikundi cha washirika waovu, shauku ile mbayo husaidia kuunda tabia nzuri na kupata mbingu mwishowe zitadhoofika. Vijana wanaotamani kutokufa lazima wasimame hapo walipo na wasiruhusu fikira au vitendo vibaya. Mawazo machafu husababisha matendo machafu. Ikiwa Kristo atakuwa mada ya kutafakari, mawazo yatatengwa mbali kutoka kwa kila mada ambayo inapelekea kwenye matendo machafu. Akili itaimarishwa kwa kukaa juu ya mada za kuinua. Ikiwa imefundishwa kuwa na wepesi wa kupitia kwenye njia ya usafi wa moyo na na utakatifu, itakuwa na afya na nguvu. Ikiwa amefunzwa kukita kwenye mada za kiroho, itakuwa na kawaida kuchukua nafasi hiyo. Lakini mvuto huu wa mawazo kwa vitu vya mbinguni hauwezi kupatikana bila zoezi la imani kwa Mungu na bidii, unyofu na unyenyekevu katika kumtegemea Yeye kwa nguvu hiyo na neema ambayo itatosha kwa kila dharura. {2T 408.1}

Usafi wa maisha na tabia iliyoumbwa kwa mfano wa Kristo haipatikani bila bidii na kanuni zisizoyumba. Mtu anayemanga-manga huku na kule hatafanikiwa kufikia ukamilifu wa Kikristo. Hao watapimwa katika mizani na kupatikana wamepunguka. Kama simba anayeunguruma, Shetani anatafuta mawindo yake. Yeye hujaribu hila zake kwa kila kijana aliyejiziuka; kuna usalama tu katika Kristo. Ni kupitia neema Yake pekee, ndipo Shetani anaweza kushindwa na kurudishwa nyuma. Shetani huwaambia vijana kuwa kuna wakati wa kutosha bado, ili waweze kujiendekeza katika dhambi na uovu wa punyeto mara moja

na wasirudie tena; lakini anasa au tamaa hiyo moja itahatarisha maisha yao yote. Usijitose mahali ambapo Mungu amekataza. Katika siku hizi za hatari ya uovu, wakati vishawishi vya uovu na ufisadi viko kila upande, kilio cha dhati na bidii, cha moyo wa vijana kiinuliwe kwenda mbinguni: "Jinsi gani! Kijana aisafishe njia yake?" Na hebu masikio yake na yawe tayari kusikia na moyo wake uweze kutii maagizo yaliyotolewa katika jibu: "Ni kwa kutii maagizo ya MUNGU." Usalama pekee kwa vijana katika wakati huu wa uchafuzi ni kumfanya Mungu kuwa tegemeo lao. Bila msaada wa MUNGU, hawataweza kudhibiti tamaa na hamu za kibinadamu. Katika Kristo ndiko msaada unaohitajika upo, lakini ni wachache kiasi gani, watakaokuja Kwake kwa msaada huo. Yesu alisema wakati alikuwa duniani: "Wala hamtaki kuja Kwangu mpate kuwa na uzima." Katika Kristo wote wanaweza kushinda. Unaweza kusema pamoja na mtume: "Lakini katika mambo hayo yote sisi ni zaidi ya washindi, kupitia Kwake Yeye Aliyetupenda." Tena: "bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha." {2T 408.2}

Nimeandika kabisa kisa cha Ndugu E na familia, kwa sababu kesii hii moja, inaonyesha hali halisi ya familia nyingi, na Mungu angetaka familia hizi kuchukua hili kana kwamba limeandikwa maalum kwa faida yao. Kuna kesi nyingi zaidi ambazo ninaweza kuteua, lakini nimetaja ya kutosha tayari. Kwa Jumla kwa wasichana wadogo jambo la uovu wa kujichua sio la kawaida kwao. Wanaofanya hivyo afya huharibiwa kabisa. Wengine wanapoingia umri wa wanawake wako katika hatari ya kupooza ubongo kutokana na athari ya uovu huu. Tayari nguvu za kiadili na kiakili zimedhoofishwa na kupooza, na tamaa za kinyama, zinapata kuongezeka na kuharibu mwili na roho. Vijana, iwe wa kiume au wa kike, hawawezi kuwa Wakristo isipokuwa wataacha kabisa kufanya tabia hii mbaya ya kuzimu, ya kuharibu roho na mwili. {2T 409.1}

Wengi wa vijana wana hamu ya vitabu. Wanasoma kila kitu wanachoweza kukipata. Hadithi za kisisimua za mapenzi na picha zisizo safi zina ushawishi mbaya. Riwaya zinasomwa kwa hamu na wengi, na, kama matokeo, mawazo yao yanachafuliwa. Kwenye magari, picha za wanawake walio uchi husambazwa mara nyingi kwaajili ya kuuzwa. Picha hizi zenye kuchukiza pia zinapatikana katika saloons za

Daguerrean na zimetundikwa kwenye kuta za wale ambao huhusika na uchoraji. Huu ni wakati ambao ufiisadi umejaa kila mahali. (Haya ni ya miaka 1800- ila leo kuna mtandao ambao ni hatari zaidi ya vitabu, na pia kujichukua picha ili kujionyesha au kujitazama tazama ni fursa ya mabilioni, hatujitaji Studio! Hebu tusome haya kwa hofu kisha yatusaidie leo) Tamaa ya jicho na tamaa mbaya zinaamshwa kwa kutazama na kwa kusoma. Moyo umeharibiwa kupitia mawazo. Akili hufurahia kutafakari matukio ambayo huamsha tamaa za kuelekea chini, yaani za uovu. Picha hizi mbaya, zinazoonekana kupitia mawazo yaliyotiwa unajisi, zinaharibu maadili na kuandaa watu waliopotoshwa, wanaofikiria ni mapenzi na kumbe sio, basi waongozwa kirahisi na tamaa mbaya. Kisha hufuata dhambi na uhalifu ambao huvuta viumbe vilivyoumbwa kwa mfano wa Mungu hadi kiwango sawa na wanyama, na kuzama nao katika upotevu. Epuka kusoma na kutazama vitu ambavyo vitapendekeza mawazo machafu. Kuza nguvu za kimaadili na kiakili. Wacha nguvu hizi adhimu zisiwe dhaifu na kupotoshwa na usomaji mwingi wa hata vitabu vya hadithi. Ninajua akili zenye nguvu ambazo zimekuwa zisizo na usawa na zenye kupooza, au kudumazwa, kwa kutokuwa na kiasi katika kusoma (kutochagua vitu bora vya kusoma au hata kuangalia). {2T 410.1}

Natoa wito kwa wazazi kudhibiti kile watoto wao wanachokisoma. Kusoma sana kunawadhuru tu. Haswa usiruhusu kwenye meza zako magazeti ambayo hupatikana hadithi za mapenzi (love stories, romantic stories). Haiwezekani kwa vijana kuwa na mawazo mema akilini na kanuni za kiroho isipokuwa watafurahia kusoma kutoka kwenye Neno la Mungu. Kitabu hiki (Biblia) kina historia ya kufurahisha na kuisimua zaidi, kinaonyesha njia ya wokovu kupitia Kristo, na ndio mwongozo wao kwa maisha ya ufanisi na bora. Wao wote wangesema kuwa hiki, ndicho kitabu hiki ni cha kupendeza zaidi kati ya vile walivyowahi kuvisoma, ikiwa mawazo yao hayangepotoshwa na hadithi za kuisimua za mhusika wa uongo. Ninyi mnaomtazamia Bwana wenu aje kwa mara ya pili kuibadilisha miili yenu inayokufa, na kuifanya kama mwili Wake mtukufu sana, lazima mpande juu kwa hatua kubwa zaidi. Lazima ufanye kazi kutoka kwenye hali ya juu kuliko ulivyofanya kabla ya sasa, la sivyo hautakuwa kwenye nambari hiyo ambayo itapokea mguso wa kutokufa. {2T 410.2}

## SURA YA 55

### UPENDO WA KWELI NYUMBANI

Ndugu M: Katika Kituo cha Adams nilioneshwa kwamba ulikosa roho ya kujitolea wakati ulikuwa kwenye Taasisi; haukutumia ushawishi ambao unapaswa. Ungeweza kuangaza nuru yako hapo, lakini haukufanya hivyo. Mara nyingi ulipuuza jukumu lako kwaajili ya burudani. Umeshindwa kutunza na kubeba majukumu. Haufurahii mazoezi ya mwili. Unapenda raha yako mwenyewe; wewe na kazi yenye kutoa jasho ni tofauti. Huu ni ubinafsi. Uliruhusu mali ya taasisi izeeke na iharibiwe, wakati ilikuwa shuguli yako kuona kuwa imehifadhiwa, na kwamba kila kitu kiko sawa, na kimetunzwa kwa shauku kubwa na uangalifu kuliko ingekuwa ni mali yako mwenyewe. Ulikuwa msimamizi asiye mwaminifu. Kila wakati uliamua kujiingiza katika burudani, kucheza croquet\* au kitu chochote cha aina hiyo, ulikuwa unatumia wakati ambao ulilipwa na ambao haukuwa wako. Ni kama usamehewe wakati unachukua pesa ambazo haukuzifanyia kazi na kuzitumia mwenyewe. {2T 411.1}

\*Croquet ni mchezo unaohusisha kupiga mipira ya mbao au plastiki na gongo kupitia magoli.

Ndugu Loughborough, Andrews, Aldrich, na wengine hawakujua. Walikukadiria kwa viwango vya juu sana. Hungeweza kujaza waliyokuajiri kujaza. Walikosea katika uamuzi walipokulipa mshahara mkubwa sana kwa kazi yako. Haukutolea jasho pesa uliyopokea. Ulikuwa unazorota/unazembea sana kazini na ulikuwa goi goi sana (mtegeaji/mvivu). Haukupenda kufanya kazi hii kiasi cha kutosha na haukuwa macho kuona mambo yanavyokwenda na kuwajibika katika utendaji, ulipuuzia mambo sana. {2T 411.2}

Ndugu yangu, uko mbali na Mungu; umerudi nyuma. Hauna ujasiri mzuri wa maadili. Unajisalimisha kwa tamaa zako mwenyewe badala ya kujikana nafsi. Katika kutafuta furaha, umehudhuria sehemu za burudani ambazo Mungu hakubaliani nazo, na kwa kufanya hivyo umedhoofisha roho yako mwenyewe. Ndugu yangu, una mengi ya kujifunza. Unaendekeza uchu wa chakula, kwa kula chakula kingi kuliko mfumo wako unavyoweza kubadilisha kuwa damu nzuri. Ni dhambi ya kutokuwa na kiasi katika wingi wa chakula kinacholiwa, hata ikiwa ubora wake hauna maswali. Wengi wanahisi kwamba, ikiwa hawali nyama na vitu vingine ambavyo ni vya mazoea, wanaweza kula chakula rahisi kingi kadri wanavyotaka hata wasiweze kula zaidi. Hili ni kosa. Wengi wanaodai kuwa watu wa matengenezo ya afya hawana lolote isipokuwa ulafi tu. Wanaweka mzigo kwenye viungo vya kumengenya kiasi kwamba nguvu ya mfumo inachoka katika juhudi za kuyeyusha chakula. Pia hilo lina ushawishi wa kukatisha tamaa akili, kwani nguvu ya neva ya ubongo inaitwa kusaidia tumbo katika kazi yake. Kula kupita kiasi, hata kwa chakula kizuri na rahisi, hupooza neva nyeti za ubongo na kudhoofisha nguvu yake. Kula kupita kiasi kuna athari mbaya kwa mfumo kuliko kufanya kazi bila kiasi; nguvu za kiroho huangushwa kikamilifu zaidi kwa kula bila kiasi kuliko kwa kufanya kazi kupita kiasi. {2T 412.1}

Kamwe viungo vya kumengenya havipaswi kubebeshwa chakula bora na kingi ambacho kitatoza mfumo kufanya kazi kwa usahihi. Yote ambayo huchukuliwa ndani ya tumbo kwa kile mfumo unaweza kutumia kugeuza damu nzuri, huziba mashine/mitambo ya mwili; kwani hakiwezi kufanywa kuwa nyama au damu, na uwepo wake hulemea ini na hutoa hali mbaya ya mfumo. Tumbo linafanya kazi

kupita kiasi katika juhudi zake za kuyeyusha chakula kitoke, na kisha kuna hali ya shida, ambayo inatafsiriwa kumaanisha ni njaa; na bila kuruhusu viungo vya mmeng'enyoo kupata muda wa kupumzika kutokana na kazi yao kali, Ili nguvu zilizopo zisaidie kuratibu kazi hiyo, kiasi kingine kisicho na kipimo kinaingizwa ndani ya tumbo, na kuifanya mashine iliyochoka ianze kazi tena. Mfumo hupokea lishe kidogo kutoka kwa chakula kingi sana, hata kikiwa bora na kinachofaa, ukilinganisha na kiwango cha wastani kinachochukuliwa kwa vipindi vya milo vya kawaida. {2T 412.2}

Ndugu yangu, ubongo wako umepumbazwa. Mwanamume anayekula kiwango cha chakula unachokula anapaswa kuwa mtu anayefanya kazi ya nguvu, ya mikono. Mazoezi ni muhimu kwa mmeng'enyoo na kwa hali nzuri ya afya ya mwili na akili. Unahitaji mazoezi ya mwili. Unatembea na kufanya vitu kama vile mwili wako ni mbao iliyogang'amaa, kana kwamba mwili wako hauwezi kunyumbulika. Zoezi la afya la kuchangamsha ndilo unalohitaji. Hii itaimarisha akili. Usisome wala kufanya mazoezi makali mara baada ya mlo; hii itakuwa ukiukaji wa sheria za mfumo. Mara tu baada ya kula kuna hali ya dharura sana kwenye nishati ya neva. Nguvu ya ubongo inaitwa kuingia katika mazoezi ya kusaidia tumbo; kwa hivyo, wakati akili au mwili inachoshwa na kuwekwa chini sana baada ya kula, mchakato wa mmeng'enyoo wa chakula unazuiliwa. Nguvu ya mfumo, ambayo inahitajika kuendelea na kazi kwa mwelekeo mmoja, inaitwa itoke na kufanya kazi pahali pengine. {2T 413.1}

Unahitaji kuwa na kiasi katika mambo yote. Kukuza nguvu za juu za akili, na kutakuwa na nguvu ndogo ya ukuaji wa tabia ya mnyama. Haiwezekani kwako kuongeza nguvu za kiroho wakati hamu yako ya chakula na matakwa yako hayana udhibiti kamili. Anasema mtume aliyevuviwa: "lakini nauimarisha mwili wangu na kuutawala, ili baada ya kuwahubiria wengine, mimi mwenyewe nisije nikakataliwa." {2T 413.2}

Ndugu yangu, amka/zinduka mwenyewe, nakuomba, na acha kazi ya Roho wa Mungu ifike ndani zaidi kuliko juu juu; wacha ifikie chemichemi za ndani za kila tendo. Ni kanuni inayotakiwa, kanuni thabiti, na nguvu ya kutenda katika mambo ya kiroho na ya kidunia.

Jitihada zako zinakosa bidii. Lo! ni wangapi walio chini katika kiwango cha kiroho kwa sababu hawatawali hamu yao ya kula! Nishati ya neva ya ubongo vina ukungu na karibu kupooza kwa kula kupita kiasi. Watu kama hao wakienda nyumba ya Mungu siku ya Sabato, hawawezi kujikaza wasilale- hawawezi kufungua macho yao. Miito itolewayo ya dhati zaidi haiwezi kuamsha hisia au akili zao zilizopungua na kuzembea. Ukweli unaweza kuwasilishwa kwa hisia za kina, lakini hauamshi hisia za maadili au kuangaza ufahamu. Je! Hawa wamejifunza kumtukuza Mungu katika kwa kila jambo? {2T 414.1}

Haiwezekani kuwa na dhana wazi ya vitu vya milele isipokuwa akili imefundishwa kukaa juu ya mada zilizoinuliwa. Mapenzi yote lazima yaletwe chini ya utii kamili wa nguvu za maadili. Wakati wanaume na wanawake wanapokiri imani thabiti na bidii ya kiroho, najua kuwa maneno yao ni ya uwongo ikiwa hawajadhibiti tamaa zao zote. Mungu anahitaji hili. Sababu ya kushinda kwa giza la kiroho kama hilo ni kwamba akili inaridhika kuchukua kiwango cha chini na haielekezwi kuelekea juu kwenye njia safi, takatifu, na ya mbinguni. {2T 414.2}

Niliona kuhusu familia yako, Ndugu M, kwamba haukufurahi. Mke wako amekata tamaa, na wewe umekata tamaa. Mke wako alitarajia kupata ndani yako mtu mwungwana zaidi, bora, wa mipangilio bora zaidi iliyosafishwa. Amekuwa hana furaha sana. Ana kiasi kikubwa cha kiburi. Jamaa wa familia yake upande wa mama yake ni watu wenye dhamiri makini, lakini wana kiburi na pia ni mashuhuri. Amechukua urithi wa tabia hizi sana. Ila hana hulka ya kuzionyesha kirahisi. Sio kawaida kwake kutangulia kuonyesha au kudhihirisha mapenzi/mahaba (affection). Anaangalia udhihirisho wa mapenzi kati ya mume na mke kama udhaifu na jambo la kitoto. Amehisi kuwa ikiwa atashawishi mapenzi, pengine hayangejibiwa kwa mwitikio wenye upendo mzuri, bora na ulioinuliwa, lakini kwa tabia isiyo njema duni na ya tamaa; kwamba hizo ndiyo zingeimarishwa, lakini sio upendo safi, wa kina, na mtakatifu. {2T 414.3}

Mke wako anapaswa kufanya bidii kutoka kwenye kutojihusisha, kutunza hadhi yake, na kukuza unyenyekevu katika vitendo vyake vyote. Na wakati kiwango cha juu cha tabia kimeamshwa ndani yako, na



kuimarishwa na mazoezi, utaelewa vizuri matamano ya wanawake; utaelewa kuwa roho inatamani upendo wa hali ya juu, safi kuliko ilivyo katika hali ya chini ya tamaa za wanyama. Hamu hizi zimeimarishwa ndani yako kwa kuziendekeza na kuzifanyia mazoezi. Ikiwa sasa kwa kumcha Mungu unaweka mwili wako ukiuthibiti, na unatafuta kukutana na mke wako kwa mapenzi safi, yaliyoinuliwa, matakwa ya asili yake yatatimizwa. Mchukue na mweke moyoni mwako; mthamini kwa hali ya juu. {2T 415.1}

Umeinuliwa na umechukua msimamo wa juu ya mke wako. Hujajielewa. Umepokea shukrani za juu kuhusiana na uzoefu wako wa kidini na maendeleo katika maisha ya kiroho. Vitu hivi vimekurudisha nyuma, badala ya kumsaidia, mke wako. ake amekuogopa, ameogopa kwamba hakujielewa mwenyewe, na kwamba ungeenda kwa mwendo wa haraka. Ndoa yako haina furaha. Hamfaani. Mkeo ana asili ya kuona woga, haya, hofu, na kujikunja. Umeshindwa kabisa kumuelewa mkeo. Yeye anasita na anaogopa kusogea kwa sababu anaogopa kwenda haraka sana. Anahitaji kujiamini na anapaswa kuhimizwa kujitegemea. {2T 415.2}

Ndugu M, unashindwa kumsaidia mke wako awe na ujasiri. Unakosa adabu/uungwana na kumjali kila wakati na wema. Wakati mwingine hudhihirisha upendo, lakini ni upendo wa ubinafsi. Upendo sio kanuni kwako inayofika chini kabisa na kuwa msingi wa vitendo vyako vyote. Sio upendo wenye ubinafsi unaohimiza kufikiria maslahi yake na utunzaji wake, ukipenda kuwa naye karibu, ukimuonyesha kuwa unapendelea awe mwenzi wako, ukimwonyesha unapenda uwepo wake au tuongeze Je! siyo upendo usio na ubinafsi unaohimiza kufikiria maslahi yake na utunzaji wake daima zaidi ya wengine wote. Umetafuta starehe zako mwenyewe, ukimwacha mkeo nyumbani akiwa mpweke na mara nyingi mwenye huzuni. Umekuwa ukifuata mwenendo potofu kabla ya kuhamia mahali hapa na kuendelea kufanya hivyo tangu hapo, kwa kiwango kidogo kwa kukosa fursa na udhuru kufanya hivyo. {2T 415.3}

Mke wako alitoa dhihaka kukuashiria kwamba alipata viashiria dhidi ya mapungufu yako. Yeye anakuogopa. Ungekuwa na upendo wa dhati,

ambao mtu mwenye tabia kama yake anauhitaji, ingelikupa njia ya kupata mwitikio wa moyo wake. Moyo wako una ubaridi na ugumu sana. Wakati mwingine umeonyesha mapenzi, lakini hayajaamsha upendo kwa sababu haujawa mwenye uungwana na umakini, na kuonyesha kumthamini mke wako kwa kushugulikia furaha yake. Umejisikia mara nyingi kuwa na uhuru kujiondokea taratibu kwa kufuata raha zako mwenyewe, bila kushauriana naye juu ya raha yake au furaha yake hata kidogo. {2T 416.1}

Upendo wa kweli na safi ni wa thamani. Una mvuto wa kutoka mbinguni. Una kina na unadumu. Hauna harara katika udhihirisho wake, wala kuwepo na kutoweka hapa na pale. Hauna tamaa za kibinafsi. Unazaa matunda. Utakuongoza uwe na bidii ya kila wakati kumfurahisha mke wako. Ikiwa una upendo huu, hautatoka jasho kufanya kazi hii. Haitaonekana unalazimishwa. Ukienda kutembea au kuhudhuria mkutano, itakuwa jambo la kawaida kama kuvuta pumzi, kumwambia mke wako aandamane nawe, na utatafuta jinsi ya kumfurahisha kwenye jumuiya yako. Unachukulia mafanikio yake ya kiroho kama duni kuliko yako, lakini niliona kuwa Mungu alifurahishwa zaidi na roho yake kuliko yako. Haumstahili mke wako. Yeye ni bora sana kwako. Yeye ni mmea dhaifu, nyeti; mkeo anahitaji kutunzwa kwa upole. Anatamani sana kufanya mapenzi ya Mungu. Lakini ana roho ya majivuno, na ni mwoga, anayejikunja akigombezwa. Ni kama kifo kwake watu wakizungumza kuhusu yeye au kumwangalia kwa kumchunguza. Mruhusu mke wako apendwe, aheshimiwe, na athaminiwe, kwa kutimiza nadhiri ya ndoa, na atatoka katika msimamo huo wa woga, na wa kuona haya kirahisi ambao ni wa asili kwake. {2T 416.2}

Hebu mwanamke atambue kwamba anapendwa na mumewe na ni wa thamani kwake, sio kwa sababu tu analeta manufaa katika nyumba yake, lakini kwa sababu yeye ni sehemu ya nafsi yake, na ataitikia mapenzi ya mume na kuakisi upendo aliopokea. Hebu mke wako awe mtu wa pekee kwako na wa kujaliwa na moyo wako. Ungeangalia mambo kama vile Mungu atakavyo uone, ungehisi kupotea bila kuwa na mke wako maishani mwako. Wewe unafikiri imani yake haifai kuwa

nayo, lakini hii Imani yake, italeta majibu mapema kuliko imani yako. {2T 416.3}

Ndugu M, unashindwa kuelewa moyo wa mwanamke. Hufikiri kuhusu yale tunayotenda huleta matokeo. Unajua kwamba mke wako sio mchangamfu na mwenye furaha, kama unavyotaka kumuona, lakini hauchunguzi sababu. Hauchambui/haudadavui mwenendo wako ili uone kama ugumu upo ndani yako. Mpende mkeo. Ana njaa ya upendo wa kina, wa kweli, unaoinua. Mruhusu awe na uthibitisho unaoonekana kwamba kujali kwake na shauku yake kwako, inavyoonyeshwa na kupendezwa kwake nawe, inathaminiwa na kupata mrejesho. Tafuta maoni na idhini yake kwa yale unayoenda kufanya. Heshimu uamuzi wake. Usihisi kuwa unajua yote ambayo ni muhimu kujua. {2T 417.1}

Nyumba iliyo na upendo ndani, ambapo upendo huonyeshwa kwa maneno na uso na matendo, ni mahali ambapo malaika wanapenda kudhihirisha uwepo wao, na kutakasa eneo hilo kwa miale ya nuru kutoka kwenye utukufu. Huko majukumu ya unyenyekevu ya nyumbani yanavutia. Hakuna jukumu la maisha ambalo mkeo hatapendezwa hali ikiwa hivyo. Atafanya kazi hizo kwa moyo mkunjufu na atakuwa kama mwale wa jua kwa wote wanaomzunguka, na atakuwa akimwimbia Bwana moyoni mwake. Kwa sasa anahisi kuwa huna mapenzi ya moyo wako. Umempa yeye sababu za kujisikia hivi. Unafanya majukumu muhimu uliyokabidhiwa kama kichwa cha familia, lakini kuna mapungufu. Kuna ukosefu mkubwa wa ushawishi wa upendo ambao unaleta mawazo ya kutakiana mema. Upendo unapaswa kuonekana katika sura na tabia, na kusikika kwenye sauti zetu. {2T 417.2}

Mke wako anaogopa kukufungulia moyo wake; kwani mara tu atakaposema maoni tofauti na wewe, unayapuuzia. Unazungumza kwa nguvu na mkazo sana kiasi kwamba hana ujasiri wa kusema neno lingine. Mioyo yenu haipo pamoja. Msimamo wako unakuwa juu yake na unadumisha kukandamiza uamuzi na maoni yake kama vile hayana maana. Unafikiria kwamba mafanikio yako yana maendeleo makubwa sana kuliko yake. Ndugu yangu, haujijui mwenyewe. Mungu huangalia moyo, sio maneno au kauli zako. Mambo ya nje hayapimwi kwa uzito na Mungu kama watu. Moyo mnyenyekevu na roho iliyopondeka

Mungu huthamini. Mwokozi wetu anajua migogoro ya maisha ya kila mtu. Yeye Hauhukumu kulingana na mwonekano, bali kwa haki. {2T 418.1}

Roho yako ina nguvu. Unapochukua msimamo haupimi jambo hilo vizuri na kufikiria ni nini itakuwa athari ya kudumisha maoni yako na kwa njia ya kujitegemea unayaweka katika sala na mazungumzo yako, wakati unajua kuwa mke wako hashikilii maoni sawa na hayo uliyonayo. Badala ya kuheshimu hisia za mke wako, na kwa upole kuepuka hizo mada, kama mume muungwana angelifanya, mada ambazo unajua mnatofautiana, na zinaleta upinzani moyoni, wewe umekuwa ukizikazania na kupendelea kuzizungumzia, na umeonyesha msimamo wa kutoa maoni yako bila kujali mtu yeyote aliye karibu nawe. Umehisi kuwa wengine hawakuwa na haki ya kuona mambo tofauti na wewe. Matunda haya hayakui kwenye mti wa Kikristo. {2T 418.2}

Kwa upande wa Dada N, haukuona mambo kwa nuru yake halisi. Ikiwa angeponywa katika kujibu maombi yako mwenyewe na ya wengine, ingethibitisha uharibifu kwa zaidi ya watu wawili au watatu kati yenu. Mungu mwenye busara alikuwa na usimamizi wa jambo hili. Yeye Anasoma nia na madhumuni ya moyo. {2T 418.3}

Mke wako ana haki sawa kuwa na maoni yake kama wewe ulivyo na haki kuwa na maoni. Uhusiano wake wa ndoa hauharibu utu wake. Ana jukumu la kibinafsi. Hautakuwa salama mpaka uondoe vizuizi hivi katika yake nawe udhihirishe kwake roho ya hisani zaidi, Roho kama ya Kristo ya uvumilivu, na kujali wengine kwa nuru ambayo unataka wengine wakutendee vile vile. Bado haujajifunza" Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. "Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana;" {2T 418.4}

**Kuendesha Mikutano Ya Kijamii**

Nilioneshwa, Ndugu M, kwamba unahitaji kazi kubwa ifanyike kwako kabla ya kuwa na ushawishi kanisani, kurekebisha makosa yao au kuwainua juu. Hauna unyenyekevu huo wa nia ambao unaweza kufikia mioyo ya watu wa Mungu. Umejiinua. Unahitaji kuchunguza nia yako na matendo yako kuona kwamba macho yako yanatazama kwaajili ya utukufu MUNGU tu. Ndugu O au wewe hampo kukidhi mahitaji ya vijana na kanisa kwa ujumla. Hamshuki chini kwa urahisi ili kuelewa njia bora ya kuwasaidia. Haina ushawishi bora kwako na Ndugu O kuacha viti vya washiriki wa kawaida na kukaa kwenye mimbari mbele ya watu. Mnapochukua nafasi hiyo, mnahisi kwamba ni lazima msembe au mfanye kitu kulingana nafasi ya jukwaa mliyochukua, badala ya kunyanyuka na kusema maneno machache kwa uhakika, ninyi mara nyingi mnatoa maoni marefu, ambayo yanaumiza sana mionjo ya kiroho ya mkutano. Wengi hufurahi mkikaa chini. Mngekuwa mahali ambapo kulikuwa na watu wachache tu kama vijijini, na watu wanaoboresha wakati, basi maneno marefu kama hayo yangefaa zaidi huko. {2T 419.1}

Kazi ya Bwana ni kazi kubwa, na watu wenye busara wanahitajika kuifanya. Wanahitaji Watu ambao wanaweza kuchukuliana na mahitaji ya watu. Ikiwa unatarajia kusaidia watu haupaswi kuchukua msimamo ambao unaonyesha uko juu yao, bali chini pamoja nao. Hili ni kosa kubwa la Ndugu O. Yeye ni amekakamaa, yaani hanyumbuliki kirahisi. Sio kawaida yake kurahisha mambo kwa unyenyekevu Hauishi vitendo na matokeo yake. Hawezi kupewa mapenzi na upendo wa watu. Hashuki chini ili aweze kuwaelewa watoto na kuzungumza kwa mguso ambao utayeyusha mioyo yao. Anasimama na kuzungumza na watoto kwa njia ya busara, lakini haina msaada kwao. Mazungumzo yake kwa kawaida ni marefu na ya kuchosha. Wakati mwingine angezungumza robo tu ya yale anayozungumza, mkazo ungeachwa akilini mwa watu. {2T 419.2}

Wale ambao hufundisha watoto wanapaswa kuepuka maneno ya kuchosha. Maneno mafupi na ya uhakika yatakuwa na ushawishi mzuri. Ikiwa kuna mengi ya kusemwa, tengeneza muhtasari na vipindi tofauti. Maneno machache ya kupendeza leo na siku nyingine, yatakuwa na faida zaidi kuliko kuwa nayo yote mara moja. Hotuba ndefu hulemea

akili ndogo za watoto. Mafundisho marefu sana hufanya watu wachukie hata mafundisho ya kiroho, kama vile kula kupita kiasi kunavyolemea tumbo na kupunguza hamu ya kula, na kusababisha hata kuchukia chakula. Akili za watu zinaweza kuvimbiwa kwa hotuba nyingi sana. Fanya kazi kwaajili ya kanisa, lakini haswa kwa vijana, Kwa maana ni amri juu ya amri;; kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo. Zipe akili muda wa kuyeyusha Ukweli unaowalisha. Watoto lazima wavutwe kuelekea mbinguni, sio kwa haraka, lakini kwa upole sana. Battle Creek, Michigan, Oktoba 2, 1868. {2T 420.1}

## **SURA YA 56**

### **UMUHIMU WA KUJITAWALA**

Ndugu Mpendwa P: Nimejaribu mara kadhaa kukuandikia, lakini nimekuwa nikizuiliwa mara nyingi. Sitachelewesha tena. Nimehisi kwa siku chache zilizopita haswa wasiwasi juu yako. Juni iliyopita mambo kadhaa yalionyeshwa kwangu yakuhusuyo. Nilibebwa kurudi nyuma na kuonyeshwa maisha yako yasiyotulia, na ya kutanga-tanga. Ulikuwa bila Mungu. Maisha yako yamekuwa maisha magumu, ya ovyo na hatari. Walakini nikaona kwamba kwa rehema Mungu ameyaokoa maisha yako mara nyingi wakati ilionekana kuwa hakuna nguvu ya binadamu au hekima inayoweza kuyahifadhi. Wewe umesimama kama mwujiza wa rehema ya MUNGU. Wakati maisha yako yamekuwa karibu na hatari, Kristo, Wakili wako, amesihi kwa niaba yako: "Baba, tunza maisha yake kwa muda kidogo. Yeye amekuwa mti usiozaa matunda, ambao umesumbua ardhi, lakini usiukate. Nitasubiri kwa uvumilivu

kwa muda kidogo, na kuona ikiwa hautazaa matunda. Nitaugusa moyo wake na Kweli. Nitaonyesha moyo wake dhambi zilizomo." {2T 421.1}

Nilioneshwa kwamba Bwana alikuwekea wazi njia ya kumtii na kumtumikia. Hatua zako zilielekezwa Magharibi, ambapo mazingira yako yatapendezewa zaidi na ukuaji wa neema, na ambapo itakuwa rahisi kwako kujenga tabia ya mbinguni. Ulikuwa katika familia yetu na ukapokelewa ndani ya mioyo yetu. Haya yote yaliagizwa na Bwana. Haukuwa na uzoefu ambao ulikuwa ni muhimu kuishi maisha ambayo Mungu angeyakubali. Ulikuwa mahali ambapo kwa miezi michache tu ungeweza kupata nuru na maarifa sahihi zaidi ya Ukweli wa Leo, kuliko vile ambavyo ungeweza kupata kwa miaka mingi endapo ungeendelea kukaa Mashariki. {2T 421.2}

Kuhani wetu Mkuu mwenye huruma alikuwa akijua udhaifu wako na makosa yako, hakukuacha katika uzoefu wako wa kupigana na adui mkubwa katikati ya mazingira mabaya. Laiti ungalibaki ----- Usingebaki na Ukweli. Upinzani ambao ungekuwa umepokea huko ungeamsha mapigano kwako, na ungedharau Ukweli kwa roho ya harara na hasira; na kisha, kadri vizuizi vilipotokea katika safari yako ya Kikristo, ungekuwa umekata tamaa na kuuacha Ukweli. Una mengi ya kushukuru. Moyo wako unapaswa kujazwa na shukrani kwa Mwokozi wako Mwenye upendo kwa huruma Yake kwako, kwako wewe ambaye kwa muda mrefu umeutumia vibaya upendo Wake. {2T 421.3}

Nilioneshwa kuwa wewe ulikuwa jiwe lisilo laini kutoka kwenye machimbo hayo, ambayo lilihitaji kuchongwa sana, mraba, kulainishwa na kulifanya lingae kabla ya kuliweka kwenye nafasi yake kwenye jengo la mbinguni. Baadhi ya kazi hii imefanywa kwa ajili yako; lakini, oh, kuna kazi kubwa zaidi bado ya kufanywa! Umekuwa na roho isiyo na furaha, umekutana na ugumu wa maisha (maisha rafu), hujakuwa na maisha yenye furaha; lakini wewe ndiye uliyesimama katikati ya nuru yako mwenyewe, ukajizuia mema yasije kwako. Katika ujana wako uliendekeza roho ya kutoridhika; hukutaka kuongozwa; ulichagua kutembea njia unayotaka mwenyewe, bila kujali uamuzi au ushauri wa wengine. Haungekubali kudhibitiwa na baba yako wa kambo, kwa sababu ulitaka kufuata njia yako mwenyewe. Hakuelewa njia bora ya

kukusimamia, na uliazimia kutokuheshimu mamlaka yake. Mara tu anapoanza kuzungumza nawe, ulianza kujihami. Malumbano yako yalikuwa makubwa, na ungepambana na kila kitu na kila mtu aliyepinga mipango yako. Hata wakati mapendekezo yalipotolewa kwa njia bora ya kufuata katika mipango yako na kazi, ungeweza kuhamaki papo hapo (uliruka). Ukafikiri unalaumiwa, ukafikiri unasingiziwa, na ulihisi kuhuzunishwa na wale ambao walikuwa marafiki zako wa kweli. Mawazo yako yalikuwa na ugonjwa. Ulifikiri kwamba kila mtu alikuwa dhidi yako na kwamba Maisha yako yalikuwa magumu sana. Ni kweli yamekuwa magumu, ila ni wewe umeyafanya hivyo. {2T 422.1}

Mwenendo wako kwa baba yako wa kambo ulikuwa mbaya. Hakustahili kutendewa na wewe ulivyofanya. Alikuwa na mapungufu na alikuwa na makosa, lakini wakati ulikuwa umeanza kuyaona haya kwa mwangaza wa mashindano, haukuona makosa yako mwenyewe. Katika majaliwa ya Mungu, mke wako aliugua. Alikuwa mwanamke mwenye roho ya kujivuna; lakini aliungama dhambi zake, na toba yake ilikubaliwa na Mungu. {2T 422.2}

Njia yako imezungushiwa wigo, upande wa kulia na kushoto, kukuzuia usiende mbele na kudidimia upotevuni. Bwana ameleta roho yako isiyodhibitiwa, isiyofundishika, iweze kunyenyekea Kwakwe. Hukumu na rehema pamoja, zimekuleta kwenye toba. Kama Yona, ulikimbia jukumu lako la sasa hadi baharini. Mungu aliziba njia yako kwa kutembelewa na rehema Zake. Usingeweza kufanikiwa au kuwa na furaha, kwa sababu hutaki kujishusha. Ulibeba ubinafsi na kujitendea dhambi na kwenda navyo. Uliendekeza roho ya kutoridhika, isiyotulia na hukukabiliana na majukumu kwenye njia yako. Ulitaka mabadiliko, kazi kubwa zaidi. Ukawa na msimamo wa kutangatanga. {2T 423.1}

Jicho la Mwokozi mpendwa limekuwa limekuwa likikuangalia, la sivyo ungeachwa katika hali yako ya mahangaiko, na katika dhambi zako, na kuachwa kuendelea tabia hiyo na kwenye mazingira ya kukosa furaha. Ukiwa ugenini na mgonjwa, kwa masikitiko umehisi hali yako ya huzuni, na ukiwa. Umepitia siku ambazo usiku ulionekana mrefu na siku wa kuchosha, kutotulia na maumivu, mbali na mama yako na dada zako,



ukiwa na wale usiowajua pekee kukusaidia katika mahitaji yako, na bila matumaini ya Kikristo kukutegemeza. {2T 423.2}

Ulikuwa ukitaafuta furaha, lakini haukuipata. Ulikuwa umepuuza ushauri wa mama yako na kukusihi kwake usivunje amri za Mungu. Wakati mwingine upuuzaji huu umesababisha kwako uchungu wa moyo. Lakini siwezi kuingia katika kila jambo, kwani sina nguvu. Nitakita kwenye vitu vya muhimu zaidi nilivyoonyeshwa. {2T 423.3}

Niliona kuwa kuna kazi iko mbele yako ambayo hauielewi. Ni kufisha nafsi yako, kujisulubisha mwenyewe. Una wepesi wa hasira, tabia ambayo ni lazima uishinde. Unavyo viwango vya tabia njema, hivi ni ambavyo vitakufanya uwe na marafiki ikiwa roho yako ya hasira haitajeruhi wengine. Una kiambatisho chenye nguvu kwa wale wanaoonyesha kupendezwa nawe. Unapoelewa mambo kwa usahihi wewe ni mwangalifu; lakini mara nyingi unafanya vitu kutoka kwa msukumo, bila kuangalia na kutafakari. {2T 423.4}

Unatoa hukumu kwa watu, na kutoa maoni kuhusu njia zao na tabia zao, wakati hauelewi msimamo wao au kazi yao. Unaangalia vitu kwa mtazamo wako na kisha uko tayari kuhoji au kushutumu mwenendo wanaoufuata, bila kutazama kwa uwazi, na busara mambo kila upande. Huna ujuzi wa majukumu ya wengine na haupaswi kuhisi kuwajibika kwa matendo yao, lakini fanya jukumu lako, ukiwaacha wengine na Bwana. Uwe na roho ya uvumilivu, dumisha amani na utulivu wa akili, na uwe mwenye shukrani. {2T 424.1}

Niliona kwamba Bwana alikuwa amekupa nuru na uzoefu, ili uweze kuona dhambi ya roho ya harara na jazba na kudhibiti tamaa zako. Hakika ukishindwa kufanya hivi, ndivyo utakavyoshindwa kwa uzima wa milele. Lazima ushinde ugonjwa huu wa mawazo. Wewe u nyeti, unaumizwa haraka sana, na ikiwa neno linasemwa linalopelekea njia tofauti na ile ambayo umekuwa ukifuata, unaumizwa. Unahisi unalaumiwa, na kwamba lazima ujitetee mwenyewe, na kuokoa maisha yako; na katika bidii yako kuokoa maisha yako, unayapoteza. Una kazi ya kufanya ya kufisha nafsi yako na kukuza roho ya kuchukuliana na watu na uvumilivu. Acha mawazo ya kufikiri kwamba hautumiwi sawa,

kwamba umetendewa vibaya, kwamba watu wanataka kukuzingira wakudhuru. Macho yako yanakuambia yasiyo kweli. Shetani anakuongoza kuchukua maoni haya yaliyopotoka ya vitu. {2T 424.2}

Ndugu Ndugu P, katika Kituo cha Adams kesi yako ilioneshwa tena kwangu. Niliona kuwa daima umeshindwa kujitawala. Umefanya juhudi; lakini juhudi hizi zimefika nje-nje tu, hazijagusa chemchemi au kiinicha utendaji. Hasira yako ya haraka mara nyingi husababisha majuto na maumivu ya dhati na kujilaani. Roho hii ya kutokuwa na kiasi au shauku inayopitiliza aidha kwa furaha sana au hasira sana, isipotiishwa, itaoongezeka na kuleta kutotulia, kuudhika, kukosoa wengine; kwa kweli, hii tayari unayo kwa kiwango fulani (passionate spirit). Utakuwa tayari kukasirika kwa kila kitu. Ikiwa umepata kikumbo barabarani, utakwazwa, na neno la malalamiko litatiririka kwenye midomo yako. Wakati wa kuendesha gari barabarani, ikiwa huna nusu ya barabara, hasira itapanda kwa muda mfupi tu. Ukiulizwa kuacha unachofanya ili usaidie au kuchukuliana na wengine, utasumbuka, utaudhika kuhangaika, na kuhisi kuwa hadhi yako imeshushwa. Utaanika dhambi zako zinazokuzinga kwa upesi, kwa wote. Uso wako utaonyesha roho isiyo na subira, na kinywa chako kitaonekana kuwa tayari kila wakati kutamka neno la hasira. Katika tabia hii, kama katika utumiaji wa tumbaku, kuacha kabisa ni suluhisho pekee la uhakika. Mabadiliko kamili lazima yatendeke ndani yako. Mara nyingi unahisi lazima ulindwe zaidi. Unasema kwa uthabiti, "nitakuwa mtulivu zaidi na mvumilivu;" lakini kwa kufanya hivi unagusa uovu kwa nje tu; unakubali kubaki na simba ndani na kumlinda/kumtazama. Lazima uende mbele zaidi ya hivi. Nguvu ya kanuni peke yake ndiyo inaweza kuondoa adui huyu anayeangamiza na kukuletea amani na furaha. {2T 424.3}

Umesema mara kadhaa: "Siwezi kumiliki hasira yangu." "Lazima niongee." Unakosa roho ya upole na unyenyekevu. Ubinafsi/umimi uko hai, na unasimama kila wakati kuulinda ili usife au usitukanwe. Anasema mtume: "Kwa maana ninyi mmekufa, na maisha yenu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Wale ambao wamekufa nafsi hawatakuwa wepesi kulinda nafsi sana na hawatakuwa tayari kushugulikia kila kitu ambacho kinaweza kukasirisha. Wafu hawana hisia. Wewe hujafa. Kama ungekufa, na maisha yako yafichwe ndani ya

Kristo, mambo elfu moja ambayo sasa unaona, na ambayo yanakusumbua, usingeyatilia maanani; ungekuwa unashikilia yale ya milele na ungeyashinda majaribu madogo madogo ya maisha haya. {2T 425.1}

"Ulimi pia ni kama moto. Ulimi ni ulimwengu wa uovu "Busara ya mtu huiahirisha hasira yake; Nayo ni fahari yake kusamehe makosa." "Asiye mwepesi wa hasira ana fahamu nyingi; Bali mwenye roho ya hamaki hutukuza upumbavu." "Asiye mwepesi wa hasira ni mwema kuliko shujaa; Na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atekaye mji" "Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu." "Azuiaye maneno yake ni mwenye maarifa; Na mwenye roho ya utulivu ana busara." -- "roho ya utulivu." {2T 426.1}

Aliye Mfano wetu Mkuu, aliinuliwa kuwa sawa na Mungu. Alikuwa Kamanda Mkuu mbinguni. Malaika wote watakatifu walifurahi kusujudu mbele Yake." Hata tena, amletapo Mzaliwa wa Kwanza ulimwenguni, asema, "Na wamsujudu malaika wote wa Mungu." Yesu alijichukulia asili yetu, akaweka kando utukufu Wake, ukuu Wake, na utajiri Wake ili kufanya utume Wake, kuokoa kile kilichopotea. Yeye hakuja kuhudumiwa, bali kuhudumia wengine. Yesu, alipotukanwa, kunyanyaswa, na kutukanwa, hakujilipiza kisasi. Yeye "Ambaye, alipotukanwa, hakutukana tena." Wakati ukatili wa mwanadamu ulipomsababisha ateseke kupigwa na majeraha maumivu, hakutoa tishio kwa watu, lakini alijitoa na kujikabidhi kwa Yeye anayehukumu kwa haki. Mtume Paulo aliwahimiza ndugu zake Wafilipi: "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye Yeye mwanzo alikuwa Yuna namna ya Mungu, Naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa Hana utukufu, Akatwaa namna ya mtumwa, Akawa Ana mfano wa wanadamu." Je! Mtumwa ni mkuu kuliko Bwana wake? Kristo ametupa maisha Yake kama kielelezo, na tunamvunjia heshima tunapokuwa na wivu kwa kila jambo dogo, na tuko tayari kukasirika kila tunapoumizwa, jeraha la kudhania au la kweli. Sio ushahidi wa akili nzuri na uungwana kila mara kukazana kujitetea, na kuhifadhi heshima

yetu. Bora tuteseke vibaya mara mia moja kuliko kuumiza roho ya mtu kwa kuwa na moyo wa kulipiza kisasi, au kutoa hasira. Kuna nguvu inayopatikana kwa Mungu. Yeye Anaweza kusaidia. Yeye Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Ukiuliza kwa imani, utapokea; lakini lazima ukeshe ukiomba. Kesha, omba, fanya kazi, inapaswa kuwa kauli mbiu yako ya Ulinzi. {2T 426.2}

Mke wako aweza kuwa mbaraka ikiwa angechukua tu jukumu ambalo ni wajibu wake kuchukua. Lakini ameeepuka majukumu, maisha yake yote, na sasa yuko katika hatari ya kushawishiwa, badala ya kukushawishi wewe. Badala ya kuwa na ushawishi wa upole, unaokuinua, kuna hatari ya yeye kufikiria jinsi unavyofikiria, na kutenda unavyotenda, bila kuangalia kwa kina kabisa na kuongozwa na kanuni katika vitendo vyake vyote. Mnahurumiana, na, kwa bahati mbaya, mnasaidiana kuona mambo isivyo. Anaweza kuwa na ushawishi mzuri, lakini ana roho ambayo ina ladha ya uvivu wa kiroho na kuonea aibu kazi. Yeye husita kushiriki katika kazi yoyote nzuri ikiwa haifurahishi, na haikubaliki kwake. Dhambi ya Merozi ilikuwa nini? Kutofanya chochote. Sio kwa sababu ya uhalifu ambao ulikuwa mkubwa walihukumikiwa, lakini kwa sababu hawakuja kumsaidia Bwana. {2T 427.1}

Nilioneshwa kuwa mke wako hajielewi mwenyewe. Alijiepusha na kazi za utunzaji/shuguli katika ujana wake na hajawahi kuhusika nazo hata sasa. Anapenda kuwaegemea wengine, badala ya kutumia nguvu zake mwenyewe. Hajajihamasisha kujitegemea kwa njia nzuri. Angepaswa, katika miaka ya nyuma, kujifunza kubeba majukumu. Hana hali ya afya nzuri. Yeye ana asili ya ugonjwa wa ini kutofanya kazi yake vizuri, na hana mwelekeo wa kupenda kufanya mazoezi. Hana maamuzi ya kujishugulisha na kazi isipokuwa iwe lazima. Yeye hula karibu mara mbili ya kiwango ambacho anapaswa kula. Chakula chote zaidi ya kile kinachotakiwa kutengeneza damu nzuri, akikiweka tumboni mwake kinakuwa hakina faida kama takataka, na kinakuwa mzigo kwa viungo kutafuta jinsi ya kukiondoa, mfumo wake umezibwa na vitu vingi ambavyo vinafanya mambo yaende pole pole katika kazi yake, huziba mashine za mwili, na kudhoofisha nguvu za uhai. {2T 427.2}

Kuchukua chakula zaidi kwenye mfumo kuliko unavyoweza kubadilisha kuwa damu nzuri, husababisha ubora mbaya wa damu na huchosha nguvu kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko kazi au mazoezi ya mwili. Ulaji kupita kiasi husababisha akili kuwa duni na kuzembea. Mishipa ya ubongo huombwa kusaidia viungo vya mmeng'enyoy, na hivyo huongezewa mzigo mwingi, kudhoofishwa, na kusumbuliwa. Hii inaacha hisia za kuwa duni kiakili, na inamfanya mke wako awe na hatari ya kupatwa na mshtuko wa kupooza wakati wowote. Anachohitaji sio kutiwa moyo kuacha kufanya mazoezi. Hakuna kitu cha hatari kwake kama kubakia hivyo yaani nguvu zake za mwili hazishugulishwi kwa mazoezi yanayochangamsha. Mazoezi ya mwili ni muhimu sana. Haya yataimarisha mwili na akili yake. Wakati atakapoamka na kuwajibika kwa kuwa na msimamo, na aone faida inayotokana na kuwa na malengo maishani, hatakuwa na mwelekeo wa kuzama kwenye uvivu na kukimbia kazi ngumu. Haweki moyo wake katika kile anachofanya; kwa hivyo yeye huzunguka-zunguka akifanya vitu kama mashine, akihisi kuwa kazi ni mzigo. Hawezi,, wakati anahisi hivyo, kutambua kwamba aweza kufanya maisha yawe mapya na kwamba kuwa na nguvu ni fursa kubwa sana. Anakosa ujasiri na nguvu za mwili. Anapenda kujipoteza kwenye vitu duni na visivyo na maana au uchangamfu. Uchovu mzito anaohisi unaweza kuondoka tu kwa kula kwa kiasi, udhibiti kamili juu ya hamu yake ya kula na tamaa zake zote, na kwa kutumia utashi wake kuamua na kumsaidia, kufanya mazoezi. Anahitaji maamuzi yake kuupa nguvu ubongo wake ili kumwezesha kupinga uvivu. {2T 428.1}

Dada P, kamwe hauwezi kuwa mbaraka ulimwenguni, isipokuwa umenuia na nguvu ya kutosha kukuwezesha kushinda hali ya kutojali na kutotaka kubeba majukumu. Unapotumia kila siku nguvu zilizo ndani yako, changamoto hii itapungua, hadi hapo itakapokuwa rahisi kama asili yako ya pili kutimiza majukumu, kuwa mwangalifu na mwenye bidii. Unaweza kujizoeza kufikiria, unapolipunguzia mzigo tumbo lako. Mzigo huu unachosha ubongo. {2T 428.2}

Unapaswa pia kuishi kwa malengo, na madhumuni, katika maisha. Mtu anayeishi bila makusudi, atakuwa na mwelekeo wa uvivu, lakini pale ambapo kwenye mtazamo kuna kitu muhimu cha kutosha mbele,

nguvu zote za akili zitakuja kwa shughuli mara moja. Ili kufanikiwa kimaisha, mawazo lazima yaelekezwe kwa uendelevu na uthabiti kwenye utulivu juu ya malengo ya maisha, na yasiachwe kutangatanga na kushughulika na vitu visivyo vya maana, au kuridhika na kukaa kufikiria fikiria mambo ya upuuzi, ambayo ni matunda ya kukwepa uwajibikaji. Kuota ndoto za mchana, na kujenga magorofa hewani namna hiyo kunafanya akili iwe finyu. {2T 429.1}

Chukua jukumu la sasa. Fanya kwa mapenzi, kwa moyo wote. Unapaswa kuamua kufanya kitu ambacho kitahitaji juhudi za akili na nguvu za mwili. Moyo wako unapaswa kuwa katika kazi yako ya sasa. Wajibu uliopo mbele ya uso wako, sasa ndiyo kazi yenyewe ambayo Mbingu inataka ufanye. Kuota kuhusu kazi za mbali, na kufikiria na kupanga kuhusu siku zijazo, itathibitika kuwa haina faida, na haitakufanya uweze kufanya kazi hiyo, ingawa kazi hiyo ambayo Mbingu sasa inaweka mbele yako inaweza kuwa ndogo, Mbingu sasa inaweka mbele yako. Haupaswi kunuia kujifunza kufanya huduma au kazi kubwa, lakini kufanya kwa moyo mkunjufu na vizuri, kazi unayoiona kuifanya leo. Vipaji vimekabidhiwa mikoni mwako, ili vizae maradufu. Unawajibika kuvitumia kwa usahihi au vibaya. Haupaswi kutamani vitu vikuu ili ufanye huduma nzuri, lakini ufanye kazi yako ndogo uliyopewa. Boresha talanta zako, ingawa ni chache, na acha hisia ya uwajibikaji wako kwa Mungu kwa matumizi ya hizi talanta iwe sahihi kwako. {2T 429.2}

Haupaswi kutarajia kuepuka maumivu na uchovu katika taabu na majaribu ya maisha. Mwana wa Mungu Alichukua mwili wa binadamu. Alichoka mara kwa mara kimwili na kiroho. Alisema: "Lazima nizifanye kazi Zake Yeye aliyenituma, wakati bado ni mchana; usiku unakuja, ambao hakuna mtu awezaye kufanya kazi." Unapaswa kusitisha ndoto zako za mbali, na ulete akili yako katika majukumu ya karibu nawe, na uyatekeleze kwa furaha. {2T 429.3}

Ulimwengu huu sio mbingu ya Mkristo. Ni mahali pa majaribio tu, pa kuthibitishwa ili kuonekana tunafaa kuingia mbinguni. Ni eneo la vita vya maisha yetu, mizozo yetu na huzuni; na ni muhimu kwamba sisi sote tuwe na ufahamu thabiti wa ulimwengu bora unaokuja, ambao

utakuja, vita vitakapomalizika, amani, furaha, na raha, kufurahiwa milele. Niliona kwamba nyinyi wawili mtakuwa katika hatari kubwa ya kuharibikiwa na imani ikiwa mmeungana, kwa sababu mtaangalia mambo katika nuru isiyo ya kweli. Ninyi wawili mna kazi kubwa ya kujifanyia wenyewe, lakini mko katika hatari ya kuwa vipofu msione kosa alilo nalo mmoja wenu {2T 430.1}

Dada P anapaswa kulindwa ili asichochee roho ya harara ya mumewe kwa kumwelezea malalamiko yake anayodhanja, ili kupata huruma. Anaona vitu kwa msimamo wa nguvu na anahisi sana juu ya mambo ambayo hayastahili hata kutiliwa maanani. Atalazimika kujifunza hii na kuelewa kuwa ni busara kunyamaza. Anahitaji nguvu ya uvumilivu. Ni rahisi sana kuviingiza vitu akilini kuliko kuvitoa, wakati vimewasili humo. Ni rahisi kukazia makosa tunayofikiri tumefanyiwa kuliko kutuliza au kudhibiti hasira zinapoamshwa. {2T 430.2}

Ndugu P ana sifa ambazo zingekuwa bora ikiwa zingesafishwa na ushawishi wa dini safi. Anaweza kuwa mbaraka. Uchamungu wa dhati peke yake, unaweza kumstahikisha kutekeleza majukumu yake vizuri katika ulimwengu huu na kumpa kustahili mbingu. Tabia ya mbinguni lazima ipatikane duniani, ndugu yangu, la sivyo hautawahi kuimiliki; kwa hivyo unapaswa kuanza kushiriki mara moja katika kazi ambayo unapaswa kufanya. Unapaswa kufanya kazi kwa bidii ili upate kustahili mbingu. Ishi kwaajili mbingu. Ishi kwa imani. {2T 430.3}

Ndugu P, wewe ni jiwe lisilo laini-jiwe rafurafu; lakini mkono wa fundi stadi uko juu yako. Je! Utamwacha akuchonge na kukupa umbo linalofaa, na akupe mngao wa jengo lile linalojengwa bila sauti ya shoka au nyundo? Hakuna pigo linalopaswa kupigwa kwenye jiwe, baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema. Lazima ufanyiwe kazi sasa, wakati mlango wa rehema haujafungwa bado, shinda hasira yako yenye nguvu sasa, au ujitenge na Mungu hatimaye. {2T 430.4}

Yesu anawapenda nyinyi wawili na atawaokoa ikiwa mtaokolewa kwa njia Yake aliyoiteua Bwana. Unaweza kuwa na dini ya Kweli ikiwa una njaa na kiu nayo. Nenda kwa Mungu kwa imani na unyenyekevu, na uombe, nawe utapokea; lakini kumbuka kwamba mwanafunzi hayuko

juu ya Mwalimu wake wala mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake. Unahitaji kuthamini kujishusha chini na unyenyekevu wa akili uliokaa ndani ya Kristo.

Battle Creek, Michigan,  
Februari 9, 1869.{2T 431.1}

## SURA YA 57

### STADI ZA KAZI NA UCHUMI

Ndugu mpendwa na Dada R: Nimekuwa nikitafuta nafasi ya kukuandikia, lakini nimekuwa mgonjwa, na sikuweza kumwandikia mtu yeyote. Lakini nitajaribu kuandika mistari michache asubuhi ya leo. {2T 431.2}

Wakati nilioneshwa majukumu juu ya watu wa Mungu kwa masikini, haswa wajane na yatima, nilioneshwa kwamba mimi na mume wangu tulikuwa hatarini kuchukua mizigo ambayo Mungu hakutupa, na hivyo kupunguza ujasiri na nguvu kwa kuongeza shuguli nyingi na wasiwasi wetu. Niliona kwamba mume wangu alienda mbali zaidi katika kesi yako kuliko ilivyokuwa jukumu lake kwenda. Kupendezwa nawe kwako kulimpelekea kuchukua mzigo ambao ulikuwa zaidi ya wajibu wake, na ambayo haikuwa na msaada kwako, lakini umekuhimiza ndani yako wewe, tabia ya kuwategemea watenda kazi wenzako katika Bwana. Unawaangalia wakusaidie na kukufanyia upendeleo, wakati haufanyi kazi kwa bidii kama wao, na wala hautumii fedha kwa uangalifu mara zingine kama wanavyohisi ni jukumu lako kufanya. {2T 431.3}

Nilioneshwa kwamba wewe, ndugu yangu na dada yangu, una mengi ya kujifunza. Hujaishi kulingana na uwezo wako kiuchumi. Hujajifunza kutumia fedha unavyopaswa. Unapopata mshahara mkubwa, haujui jinsi ya kufanya au kutumia kwa uangalifu ili uweze kukupeleka kwa siku nyingi. Unafikiria mambo ya ladha au hamu ya chakula badala ya



busara. Wakati mwingine unatumia pesa kununua aina ya chakula ambacho ndugu zako hawawezi kumudu bei yake. Dola zinahama mfukoni mwako kwa wepesi/urahisi sana. {2T 431.4}

Dada R ana afya mbaya. Anaendekeza hamu ya chakula na kulipa kazi nzito tumbo lake. Analemea tumbo lake kwa kula kupita kiasi na kwa kuweka ndani ya tumbo lake aina ya chakula ambacho hakihesabiwi kuwa bora kulisha mwili wake. Chakula chake huchukuliwa kwa kiasi kisicho na kipimo, na anafanya mazoezi kidogo tu; kwa hivyo mwili wake unachoshwa sana. Kulingana na nuru ambayo Bwana ametupatia, chakula rahisi ni bora kwa kuhakikisha afya na nguvu. Mazoezi ni muhimu kwa afya yake. {2T 432.1}

Kujikana ni somo ambalo nyinyi wawili bado hamjapata kujifunza. Tawaleni hamu yenu ya kula, Ndugu R. Mungu amekupa wewe mtaji wa nguvu kubwa. Hii ni ya thamani kubwa kwako kuliko pesa na inapaswa kuthaminiwa zaidi. Nguvu haiwezi kununuliwa na dhahabu au fedha, nyumba au ardhi. Ni rasilimali kubwa ambayo unayo. Mungu anahitaji utumie kwa busara mtaji wa nguvu ambazo amekubariki nazo. Wewe ni wakili Wake kama vile yule mtu ambaye ana mtaji wa pesa. Ni vibaya kwako kushindwa kutumia nguvu zako kwa faida nzuri, kama ilivyo kwa tajiri kuhifadhi utajiri wake kwa tamaa kwa sababu inakubalika kufanya hivyo. Hauna bidii ya kuitunza familia yako. Unaweza kufanya kazi ikiwa kazi imeandaliwa kwa urahisi, lakini haujitahidi kujiongeza kazini na kufanya kazi kwa kuhisi kuwa ni jukumu lako kutumia wakati na nguvu zako kwa faida nzuri na kwa hofu ya Mungu. {2T 432.2}

Umekuwa katika biashara ambayo wakati mwingine inaweza kukupa faida kubwa mara moja. Baada ya kupata mshahara hujajifunza kujiwekea akiba ukifikiria kwamba wakati mwingine fedha hazingeweza kupatikana kwa urahisi, lakini umefuja pesa sana kwa mahitaji ya kufikirika. Laiti wewe na mkeo mngeelewa kuwa ni jukumu ambalo Mungu amewaamuru, jukumu la kupinga ladha ya chakula na matamano yenu, na muweke akiba kwaajili ya siku zijazo badala ya kuishi kwa sasa tu, sasa mnekuwa mmejiwezea, na familia yako ingekuwa ina mahitaji muhimu ya maisha ambayo ingekuwa hali ya

faraja. Una somo la kujifunza ambalo haupaswi kurudi nyuma katika kujifunza. Ni kufanya kidogo unachopokea, kiende mbali. {2T 432.3}

Dada R anamwegemea sana mumewe. Maisha yake yote amekuwa akitegemea huruma za wengine, akijifikiria mwenyewe, akitaka wote wamwangelie yeye kama kitovu cha yote. Amekuwa akibembelezwa sana-akidekeshwa, na hajajifunza kujitegemea. Hajakuwa msaada kwa mumewe ambavyoangepaswa katika mambo ya kidunia au ya kiroho. Lazima ajifunze kuchukuliana na udhaifu wa mwili na asikazie hilo kama yeye anavyofanya. Lazima apigane vita vya maisha mwenyewe; jukumu la kibinafsi liko juu yake. {2T 433.1}

Dada R, maisha yako yamekuwa makosa. Umejiingiza kusoma chochote na kila kitu. Akili yako haijafaidika na kusoma huko kwingi. Mishipa yako imekuwa ikisisimka wakati ikifuatilia kwa haraka hadithi hiyo. Ikiwa watoto wako wanakukatiza ukiwa unasoma, unazungumza kwa ukali, bila subira. Huna kujizuia au kuthibiti nafsi, na kwa hivyo unashindwa kuwalea watoto wako kwa mkono thabiti, usioyumba. Unafanya vitu kutokana na msukumo. Unawadekeza na kuwafurahisha, halafu unakuwa na wasiwasi na kuwakemea, na kuwa mkali. Njia hii inayobadilika-badilika inawaumiza sana. Wanahitaji nidhamu endelevu, na thabiti, isioyumba; maana wamepotoka. Wanahitaji nidhamu ya kawaida, yenye busara na pia nidhamu yenye hekima. {2T 433.2}

Unaweza ukajiepusha na wasiwasi na kuwa mwanamke haswa, na kutenda kutokana na kanuni, na sio kutokana na msukumo. Umefikiria kuwa lazima mume wako awe na wewe, kwamba huwezi kukaa peke yako. Unapaswa kuona kwamba jukumu lake ni kufanya kazi ili kutunza familia yake. Unapaswa kujifunza kukana matakwa na mapenzi yako, na usimwongoze ahisi kwamba lazima afanye wewe utakavyo, na kuratibu mambo yote kukuelekea wewe. Unahusika katika kubeba mizigo ya maisha. Lazima uweke ujasiri na nguvu kwenye akili yako. Hebu uwe mwanamke, na sio mtoto asiye na mashiko ya maisha. Umekuwa ukibembelezwa, na mizigo yako umekuwa ukibebewa kwa muda mrefu. Sasa ni jukumu lako kutafuta kukana matakwa na mapenzi yako, na kutenda kutoka kwa kanuni, kwa faida ya sasa na ya baadaye ya familia yako. Hauko sawa; lakini ikiwa unapaswa kukuza

akili iliyoridhika, yenye uchangamfu, itakusaidia kushikilia vizuri katika maisha haya, na pia maisha yanayokuja. {2T 433.3}

Ndugu R, ni wajibu wako kutumia kwa uangalifu na kwa busara matumizi ya mtaji wa nguvu ambao Mungu amekupa. {2T 434.1}

Dada R, ubongo wako umechoka na unakosa nguvu kwa kusoma. Unapaswa kuepuka tabia ya kusonga akili yako na kila kitu kinachoweza kuingizwa humo. Maisha yako hayajatumika kwa njia bora. Hujajinufaisha mwenyewe, wala wale walio karibu nawe. Umemegegemea mama yako ambaye siyo kwa faida yako. Kama ungetegemea zaidi nguvu zilizo ndani yako, ikiwa ungejitegemea zaidi, ungekuwa na furaha zaidi. Sasa unapaswa kubeba mizigo yako mwenyewe kadiri uwezavyo, na umtie moyo mumeo kubeba yake katika kufanya kazi yake. {2T 434.2}

Endapo haukuendekeza tamaa yako ya kusoma na kutafuta kujifurahisha mwenyewe, ungetumia wakati mwingi kufanya mazoezi ya mwili kwa busara, na ungekula kwa uangalifu chakula kinachofaa, chenye afya, ungeepuka matatizo mengi. Sehemu ya mateso haya imekuwa ya kufikirika ubongoni. Endapo ungekuwa umeweka akili yako ipinge mwelekeo wa kuondokana na udhaifu, usingekuwa na mshtuko wa neva. Akili yako inapaswa ipelekwe mbali na wewe mwenyewe kwenda kwenye majukumu ya kazi za nyumbani, kuiweka nyumba yako kwenye utaratibu, unadhifu, na ladha. Usomaji mwingi, na kuruhusu akili yako ibadilishwe na vitu vidogo, imesababisha kupuuzwa kwa watoto wako na majukumu yako ya nyumbani. Haya ndiyo majukumu ambayo Mungu amekupa ufanye. {2T 434.3}

Umejihurumia mwenyewe sana. Umeiita akili yako kwako mwenyewe na umekaa juu ya hisia zako duni. Dada yangu, punguza kula-kula chakula kidogo. Shiriki katika kazi ya mikono, na weka akili yako kwenye vitu vya kiroho. Fanya akili yako kuacha kujifikiria mwenyewe. Kukuza roho yenye kuridhika, changamfu unazungumza sana juu ya vitu visivyo vya maana. Hupati nguvu ya kiroho kutoka kwa hili. Ikiwa nguvu uliyotumia katika kuongea ilitumika kwa maombi, ungepokea

nguvu za kiroho na ungeimba nyimbo za furaha moyoni mwako kwa Mungu. {2T 434.4}

Umedhibitiwa na hisia, sio kwa wajibu na kanuni. Umejishugulisha na hisia za kukumbuka nyumbani (homesick) na kuumiza afya yako kwa kuingiza roho ya machafuko. Tabia zako za maisha hazina afya. Unahitaji kufanya matengenezo. Hakuna yeyote kati yenu aliye tayari kufanya kazi kama wengine wanavyofanya kazi, au kula kama ndugu zenu wanavyokula. Ikiwa iko katika uwezo wako kupata vitu, utakuwa navyo. Ni jukumu lako kufanya mambo kwa kujali uchumi. {2Tsw 435.1}

Kesi nyingine ambayo ilikuwa tofauti na yako iliwasilishwa ile ya Dada S. Ana afya dhaifu, na ana watoto wawili wa kutunza, na kazi yake ya kushona inalipa malipo madogo sana. Kwa miaka mingi alipata shida kidogo ya msaada wa pesa. Aliteswa na afya mbaya, lakini alibeba shida zake mwenyewe. Hapa kulikuwa na mtu aliyehitaji kusaidiwa. Sasa angalia kesi yako. Mtu uliye na familia ndogo na mtaji mzuri wa nguvu, lakini daima unakuwa katika deni na kuwategemea wengine. Haya yote ni makosa. Una masomo ya kujifunza. Pamoja na Dada S, uchumi ndio vita ya maisha. Hapa upo mwanamume, mwenye nguvu nyingi, na bado ni tegemezi na haujiongezi. Una kazi ya kufanya. Unapaswa kuwa na usawa wa lishe. Ishi wakati wote maisha rahisi tu kama ndugu zako wanavyoishi. Ishi kwa matendo ya matengenezo ya kiafya. {2Tsw 435.2}

Yesu alifanya muujiza na kuwalisha watu elfu tano, na kisha akafundisha somo muhimu la uchumi: "Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote." Wajibu, na majukumu muhimu, yapo juu yako. "Msiwiwe na mtu yeyote, isipokuwa upendo." Ikiwa ungekuwa dhaifu, endapo usingeweza kufanya kazi, basi ndugu zako watakuwa na jukumu la kukusaidia. Jambo kama lilivyo sasa, kile ulichohitaji kutoka kwa ndugu zako sasa ni wakati ulipokuwa unahama mwanzo ni kukusaidia kuanza maisha pale tu. Kama ungekuwa na ari inayostahili, na wewe na mke wako mkakubali kuishi kulingana na mapato yenu, mngeondokana na aibu. Mtalazimika kufanya kazi kwa mshahara mdogo na hata mkubwa pia. Kazi na uchumi vingeweka familia yako, kabla ya hii, katika hali nzuri zaidi. Mungu anataka wewe uwe wakili

mwaminifu wa nguvu zako. Yeye Anataka uutumie uwakili kuweka familia yako sawa ili isiwe na uhitaji na utegemezi. {2Tsw 435.3}

Battle Creek, Michigan,  
Machi 22, 1869

## SURA YA 58

### KUCHOCHEA UPINZANI

Dada mpendwa T: Nimeonyeshwa kuwa kumekuwa na hitilafu katika maisha yako ya kiroho. Una roho ya malumbano sana. Ingawa ni fursa yako kufikiria na kutenda kwaajili yako mwenyewe, umelibeba jambo hilo kupita kiasi. Umekuwa na uhuru zaidi ya unyenyekevu. Umefuata njia ya kukasirika badala ya kutulia. Imekuwa muhimu kwako kumiliki uthabiti ili kusimama kutetea Ukweli; lakini umekosea mara kwa mara kwa kutokuwa na roho hiyo ya upole na utulivu ambayo Mungu anaiona kuwa ya thamani kubwa. Katika familia yako umekutana na upinzani dhahiri kwa wale wasiopenda Ukweli, lakini umeshindwa kuyakabili majaribu haya kwa njia bora zaidi. Umezungumza sana na umepitiliza kwa kuwa chanya sana. Umechanganya upendo na upole kidogo tu katika juhudi zako kwa familia yako, haswa kwa mumeo. Uko katika hatari ya kubeba hoja kwa kupitiliza katika jambo hilo, na kuumiza badala ya uponyaji. Mahali popote ambapo unaweza kusalimisha uamuzi wako na usitoe mhanga kanuni za Ukweli, ni bora kwako kufanya hivyo, hata ikiwa unafikiria uko sawa. Una jukumu, kitambulisho, ambacho hakiwezi kuunganishwa kwa mumeo. Walakini kuna vifungu ambavyo vnakufanya uwe mmoja naye, na katika mambo mengi, ikiwa ungekuwa mwenye kukubaliana zaidi, ingekuwa bora zaidi

kwa mume wako, watoto wako, na wewe mwenyewe. Wewe ni una misimamo mikali. Hautafuti kuwavuta kwa BWANA wale wanaotofautiana nawe. Wewe ni mwepesi kugundua wakati utafaidika, na unafanyia hilo kazi kwa kuvutia upande wako. Ungekuwa na uvumilivu zaidi uliochanganywa na upendo wenye ladha nzuri, na kama kwa ajili ya Kristo unaacha mambo mengine yapite bila ya kubishana-bishana na watu na kuyaleta kwao ili wapate kuchukua mawazo Yake. Kupitisha vitu vingi bila kuvichukua na kuvisukuma nyumbani, na hivyo kuunda hisia zisizo na ucheshi, ushawishi, utakuwa bora, na wa kuokoa zaidi. Unahitaji upendo mwanana, huruma nyororo, kujali na mapenzi. {2T 436.1}

Unaona Ukweli, halafu unafikiria jinsi huyu au yule anapaswa kufanya; na ikiwa wanashindwa kufikia alama uliyoweka, unahisi kujiondoa kutoka kwao. Hauwezi kushirikiana nao, na upendo hufa kutoka moyoni mwako kwa ajili yao, wakati kwa kweli wako sawa kama wewe tu kwenye jambo mlilotofautiana. Unajitengenezea maadui wakati unaweza kuwa na marafiki. Wewe una usongo mkali na mtazamo chanya, na unapoonza Ukweli, unabeba mambo na kupitiliza. Kwa hivyo unawafukuza watu, badala ya kuwaleta kwako na kuwakumbatia moyoni mwako. Unaangalia sifa zisizofaa/zinazochukiza katika tabia ya wale unaoshirikiana nao, na unakita juu ya **kuonekana kwao tofauti nawe na makosa, badala ya kuona tabia zao za ukombozi. Niliielekezwa kwa Andiko** hili: "Hatimaye, ndugu zangu, mambo yote yaliyo ya Kweli, yoyote yaliyo na sifa njema, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote ya kupendeza, yoyote yenye staha, ukiwepo uzuri wowote, pakiwepo chochote kinachostahili kusifiwa, tafakarini mambo hayo. "Hapa, dada mpendwa, unaweza kutafakari na kubashiri ukapata faida. Zingatia sifa nzuri za wale unaoshirikiana nao, na uone makosa na mapungufu yao kidogo iwezekanavyo. Una roho ya vita kupita kiasi, na unavuruga vitu na kuleta machafuko. Lazima ubadilishe maisha yako na tabia yako ikiwa utawahi kuorodheshwa na wale wanaosikia maneno haya: "Heri wapatanishi; maana hao wataitwa watoto wa Mungu." Usiruhusu maneno yoyote, ila yale ya wema fadhili, upendo yaanguke kutoka midomoni mwako kuhusu watu wa familia yako au kanisa. {2T 437.1}

Unahitaji kufungua moyo wako ili upendo uingie, ule upendo unaokaa kifuani mwa Yesu. Ikiwa Mwokozi wako atakutendea wewe kama unavyowatendea wale ambao mnatofautiana, bila shaka utakuwa katika hali ya kufadhaika. Kesi yako karibu tu ikose tumaini. Lakini namshukuru Bwana kwamba tuna kuhani mkuu mwenye huruma ambaye anaweza kuguswa na hisia za udhaifu wetu. Umejaribiwa na wengine, na umefuata njia kuelekea kule ambapo Mbingu haikubaliani. Una kazi ya kufanya ili kuruhusu ushawishi laini wa neema ya Mungu uingie moyoni mwako; tafuta upole, itafute haki. {2T 438.1}

Wewe ni mwenye bidii na ile Kweli. Unaipenda na unatamani kuwekeza kitu ndani yake. Hii ni sawa, lakini kuwa mwangalifu kwamba maagizo unayowapa wengine yanaungwa mkono na mfano. Lazima utafute amani. Unaweza kutafuta amani bila kudondosha hata kanuni moja ya Kweli. Umepandwa na hasira, umeshambulia, na kupigania njia yako unayotaka, na sasa unahitaji kulainisha ushawishi wako, kupendeza, kutuliza, badala ya kuchochea upinzani. Umekuwa na kujiamini na kujithamini kwingi, na umejiinua mwenyewe. Sasa unahitaji kumuinua Yesu na kuiga maisha Yake yasiyoumiza, Yeye ambaye amani ilimfuata kila mahali. {2T 438.2}

Wewe, dada yangu, utathibitisha kuwa jaribu/mtihani kwa watu wa Mungu isipokuwa utakuwa tayari kujifunza, na uko tayari kushauriwa. Haupaswi kuendelea kuhisi kuwa unajua yote. Una mengi bado ya kujifunza kabla ya kufikia ukamilifu mbele za Mungu. Somo tamu na bora zaidi litakalopatikana litakuwa lile la unyenyekevu. "Jifunze kutoka Kwangu," anasema Mnazareti Mnyenyekevu; "kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsiini mwenu." Somo hili la upole, kuchukuliana, uvumilivu, na upendo wewe bado, haujajifunza na kuwa mtendaji. Unaweza kuwa baraka. Unaweza kusaidia kama vile inavyowezekana; lakini lazima uweke vipimo vyako (rula) chini kwani wewe haupaswi kuvitumia hivyo vipimo (measuring tape). YEYE asiyekosea katika hukumu, ambaye anaelewa udhaifu wa tabia zetu zilizoanguka, zenye ufisadi, Anashikilia kiwango Mwenyewe. Yeye hupima katika mizani ya Patakatifu, na Kipimo Chake cha haki sisi sote, tutakubaliana nacho. {2T 438.3}

Unakosea katika mwenendo wako kwa mumeo. Unahitaji kukuza upole zaidi na heshima kwake. Wewe ni mkali. Unabeba mambo kupita kiasi na unadhuru nafsi yako mwenyewe na Kweli. Unafanya Ukweli uchukize na kusababisha watu waogope. Ruhusu upendo ulainishe maneno yako na uonyeshe kwenye matendo yako na mtindo wa maisha, kisha utapata mabadiliko kwa wale unaoshirikiana nao. Kutakuwa na amani, umoja, na maelewano, badala ya ugomvi, wivu, na mafarakano. Acha upendo na upole utekelezwe, haswa katika familia yako, na utapokea baraka. {2T 439.1}

## **SURA YA 59**

### **WITO KWA KANISA**

Oktoba 2, 1868, nilioneshwa hali ya wale wanaodai kuwa watu wa MUNGU. Wengi wao walikuwa katika giza kuu, lakini walionekana kutojali hali yao halisi. Hisia za idadi kubwa zilionekana kuwa na ganzi kuhusiana na mambo ya kiroho na ya milele, wakati akili zao zilionekana kuwa na macho maang'avu kwa masilahi yao ya kidunia. Wengi walikuwa wakipenda sanamu mioyoni mwao na walikuwa wakifanya uovu uliowatenganisha na Mungu na kuwafanya kuwa miili ya giza kwa wengine. Niliona ni watu wachache tu waliosimama kwenye nuru, na kuwa na utambuzi wa hali ya kiroho, kugundua vizuizi hivi na kuviondoa njiani. Watu ambao wamesimama katika nafasi za uwajibikaji sana kwenye moyo wa kazi wamelala. Shetani amewapooza ili mipango na hila zake zisigundulike, wakati anafanya kazi ya kunasa, kudanganya, na kuharibu. {2T 439.2}

Wengine ambao huchukua nafasi ya walinzi kuonya watu hatari, wameacha kulinda zamu na wameketi kwa utulivu. Ni walinzi wasio waaminifu. Wanabaki kutofanya kazi, wakati adui yao mjanja anaingia kwenye ngome na anafanya kazi kwa mafanikio kando yao kubomoa kile ambacho Mungu ameamuru kijengwe. Wanaona kwamba Shetani anawadanganya wale wasio na uzoefu na wasio na tahadhari; lakini wanayaona haya na kuyakalia kimya, kana kwamba hawakuwa na shauku maalum ya kazi, kana kwamba mambo haya hayawahusu. Hawaoni hatari yoyote maalum; hawaoni sababu ya kupiga mbiu. Kwao



kila kitu kinaonekana kuwa kiko sawa tu, na hawaoni umuhimu wa kuinua sauti za uaminifu za onyo kwa tarumbeta ambazo zinaambatana na ushuhuda ulio wazi, kuwaonyesha watu makosa yao na nyumba ya Israeli dhambi zao. Makaripio na maonyo haya husumbua utulivu wa walinzi hawa wanaolala, wapenda raha, na hawafurahishwi. Wanasema moyoni mwao, ikiwa sio kwa maneno: "Hii haipaswi kuwa hivi. Ni hali kali sana, katili sana. Watu hawa wametusumbua na kutupa mihemko bila sababu, na wanaonekana kutotaka kutupumzisha au kunyamaza. 'Ninyi inawatosha, kwa kuwa mkutano wote ni mtakatifu, kila mmoja miongoni mwao, BWANA Naye Yuko kati yao.' Hawako tayari kwamba tuwe na faraja yoyote, amani, au furaha. Ni kazi ya bidii, kazi ngumu, na umakini usiokoma pekee ambao itawaridhisha walinzi hawa wasio na busara, ambao ni wagumu kufanya nao kazi. Kwa nini hawatabiri mambo laini, na kulia: Amani, amani? Kila kitu kitaendelea vizuri. " {2T 440.1}

Hizi ni hisia za kweli za watu wetu wengi. Na Shetani anafurahi kwa kufanikiwa kwake kudhibiti akili za watu wengi wanaodai kuwa Wakristo. Adui amewadanganya, amezipa ganzi bongo zao na akapanda bendera yake ya kuzimu katikati yao, na wamedanganywa kabisa, ila hata hawajui kuwa ndiye yeye. Watu hawa hawajaweka sanamu za kuchonga, lakini dhambi yao sio kidogo machoni pa Mungu. Wanaabudu pesa. Wanapenda faida ya kidunia. Wengine watatoa mhanga dhamiri kwa lolote ili wapate wanachotaka. Watu wanaomkiri MUNGU ni wabinafsi na wanajishugulikia na kujitunza wenyewe. Wanapenda mambo ya ulimwengu huu, na wana ushirika na kazi za giza. Wanafurahia udhalimu. Hawana upendo kwa Mungu wala upendo kwa jirani zao. Wao ni waabudu sanamu, na ni mbaya, na mbaya zaidi, mbele za Mungu kuliko wapagani, wanaoabudu sanamu ambao hawajui njia bora. {2T 440.2}

Wafuasi wa Kristo wanatakiwa kutoka ulimwenguni, na kujitenga, na wasiguse kilicho najisi, na wana ahadi ya kuwa Wana na Mabinti wa YEYE Aliye Juu, washiriki wa familia ya kifalme. Lakini ikiwa hali hazizingatiwi kwa upande wao, hawatatambua, na hawawezi kutimiza ahadi. Kukiri kwamba ni Wakristo sio kitu mbele za Mungu; lakini utii wa Kweli, unyenyekevu, na wawe hiari kwa matwaka yake ndipo

wanapaswa kuwa watoto wa MUNGU, wapokeaji wa neema Yake, washiriki wa wokovu Wake mkuu. Hao watakuwa wa kipekee, tamasha kwa ulimwengu, kwa malaika, na kwa wanadamu. Tabia yao ya kipekee, na takatifu itaonekana, na itawatenganisha kabisa na ulimwengu, itawatoa toka kwenye mapenzi na tamaa zake. {2T 441.1}

Niliona hilo lakini ni wachache kati yetu wanatimiza sifa hizi. Upendo wao kwa Mungu uko kwenye maneno mdomoni, sio kwa matendo na kwa Ukweli. Utaratibu wa mwenendo wao, matendo yao, yanawashuhudia kwamba wao sio watoto wa nuru bali wa giza. Matendo yao hayakufanywa kwa Mungu, lakini kwa ubinafsi, katika udhalimu. Mioyo yao ni migeni kwa neema Yake inayofanya upya. Hawajapata uzoefu wa nguvu inayobadilisha, inayowaongoza kutembea hata kama Kristo alivyotembea. Wale ambao ni matawi yaliyo hai ya Mzabibu wa mbinguni watakula kupitia mirija yake na utomvu/lishe ya Mzabibu (sap). Hawatakauka na hawatakosa matunda kwenye matawi yake, wataonyesha uzima na nguvu, na watafanikiwa na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Watakuwa waangalifu kukimbia uovu wote na kukamilisha utakatifu katika kumcha Mungu. {2T 441.2}

Kama Israeli ya zamani kanisa limemvunjia Mungu heshima kwa Kuondoka toka kwenye nuru, kupuuzia majukumu Yake, na kutumia vibaya upendeleo Wake wa juu na uliotukuka wa kuwa wa kipekee na tabia takatifu. Washiriki wake wamekiuka agano lao kuishi kwa Mungu na Yeye peke Yake. Wamejiunga na wenye ubinafsi na wapendao ulimwengu. Kiburi, upendo wa raha, na dhambi vimependwa, na Kristo ameondoka. Roho Wake amezimwa kanisani. Shetani hufanya kazi bega kwa bega na watu wanaojiita Wakristo; walakini wamekosa ufahamu wa kiroho kiasi kwamba hawamtambui wala kumwona. Hawana mzigo wa kazi. Kweli nzito wanazodai kuamini, hazina uhalisia kwao. Hawana imani ya Kweli. Wanaume na wanawake watatenda maigizo ya imani yote ambayo kwa kweli wanayo. Kwa matunda yao mtawatambua. Sio kukiri tu, lakini matunda wanayozaa, yanaonyesha tabia ya mti. Wengi wana mfano wa utauwa, majina yao yako kwenye vitabu vya ushirika vya kanisa; lakini wana rekodi yenye mawaa mbinguni. Malaika wa kurekodi ameandika kwa uaminifu matendo yao.

Kila tendo la ubinafsi, kila neno baya, kila jukumu lisilotekelezwa, na kila dhambi ya siri, na kila aina ya ulaghai na ujanja, imeandikwa kwa uaminifu katika kitabu cha kumbukumbu kilichohifadhiwa na malaika wa kurekodi. {2T 441.3}

Wengi sana wanaodai kuwa watumishi wa Kristo, sio Wake. Wanadanganya nafsi zao kwa uharibifu wao wenyewe. Wakati wanakiri kuwa ni watumishi wa Kristo, hawaishi kwa kutii mapenzi Yake. "Hamjui ya kuwa Kwake Yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa Wake katika kumtii, mmekuwa watumwa Wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki?" Wengi, wakati wanakiri kuwa ni watumishi wa Kristo, wanamtii bwana mwingine, wakifanya kazi kila siku dhidi ya Bwana ambaye wanakiri kumtumikia. "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili: kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyo mwingine; au sivyo atamshikilia huyu, na kumdharau yule mwingine. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali." {2T 442.1}

Masilahi ya kidunia na ya ubinafsi hushirikisha roho, akili, na nguvu ya wanaojiita wafuasi wa Mungu. Kwa makusudi yote wao ni watumishi wa fedha/mali. Hawajapata kusulubiwa kwa ulimwengu, na mapenzi na tamaa zake. Lakini ni wachache kati ya wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanaoweza kusema kwa lugha ya mtume: "Lakini mimi kamwe sitajivunia kitu chochote isipokuwa msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo; kwa maana kwa njia ya msalaba, ulimwengu umesulubiwa kwangu, na mimi nimesulubiwa kwa ulimwengu." "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini naishi; lakini sio mimi, bali Kristo anaishi ndani yangu; na maisha ambayo ninaishi sasa katika mwili, naishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, na akajitoa Mwenyewe kwa ajili yake mimi. " Ikiwa utii wa hiari na upendo wa Kweli ni tabia ya maisha ya watu wa Mungu, nuru yao itaangaza na mwangaza mtakatifu kwa ulimwengu. {2T 442.2}

Maneno ambayo Kristo aliwaambia wanafunzi Wake yalichongwa kwa wote ambao wangeamini Jina Lake: "Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini ikiwa chumvi imepoteza ladha yake, itakolezwa na nini? Haifai tena; bali kutupwa nje, na kukanyagwa na watu." Taaluma ya utauwa bila

kanuni ya maisha haina maana kabisa kama chumvi bila sifa/tabia yake ya kuhifadhi vitu. Mkristo asiye na kanuni anayedaiwa na utunzaji wa kanuni ni dharau, aibu kwa Kristo, ni fedheha kwa Jina Lake. "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliowekwa juu ya mlima hauwezi kufichika. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, lakini juu ya kinara; nayo inawapa nuru wote waliomo ndani ya kilima. Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni. " {2T 443.1}

Matendo mema ya watu wa Mungu yana ushawishi mkubwa kuliko maneno. Kwa maisha yao ya adili na vitendo visivyo vya ubinafsi mtazamaji huongozwa kutamani haki ile ile iliyozaa matunda mazuri sana. Anavutiwa na nguvu hiyo kutoka kwa Mungu inayobadilisha, wanadamu wenye ubinafsi kuwa mfano wa Mungu, na Mungu anaheshimiwa, Jina Lake limetukuzwa. Lakini Bwana hutukanwana kazi Yake kulaumiwa na watu Wake walio watumwa wa ulimwengu. Wako kwenye urafiki na ulimwengu, maadui wa Mungu. Tumaini lao pekee la wokovu ni kujitenga na ulimwengu na kwa sti/bidii kudumisha tabia yao tofauti, takatifu, na ya kipekee. Ah! kwanini watu wa Mungu hawatazingatia masharti yaliyowekwa katika Neno Lake? Ikiwa wangefanya hivi wasingeshindwa kutambua baraka bora zilizotolewa bure kutoka kwa Mungu kwa wanyenyekevu na watiifu. {2T 443.2}

Nilishangaa wakati niliona giza la kutisha la washiriki wengi wa makanisa yetu. Ukosefu wa utauwa wa Kweli uliwafanya wawe kama miili ya giza na mauti, badala ya kuwa nuru ya ulimwengu. Wengi walidai kumpenda Mungu, lakini kwa matendo walimkana Yeye. Hawakumpenda, hawakumtumikia, wala kumtii Bwana. Masilahi yao wenyewe ndiyo yalikuwa kipaumbele. Idadi kubwa ilionekana kuwa na ukosefu wa kanuni wa kutisha. Walisukumwa huko na kule na ushawishi usiotakaswa na walionekana hawana mizizi ndani yao. Nikauliza mambo haya yanamaanisha nini. Kwa nini kulikuwa na hali duni ya kiroho, ni wachache sana ambao walikuwa na uzoefu wa kuishi katika mambo ya kidini? Nilielekezwa kwa maneno ya nabii: "Mwanadamu, watu hawa wameweka sanamu zao mioyoni mwao, na wameweka kikwazo cha uovu wao mbele ya uso wao: Je! Nitaulizwa nao kabisa? Kwa hivyo sema uwaambie, na kuwaambia, Bwana

MUNGU asema hivi; Kila mtu wa nyumba ya Israeli, ambaye huweka sanamu zake moyoni mwake, na kuweka kikwazo cha uovu wake mbele ya uso wake, na kumjia nabii; Bwana atamjibu yeye ajaye kwa kadiri ya wingi wa sanamu zake, ili niwachukue nyumba ya Israeli mioyoni mwao, kwa sababu wote wametengwa na Mimi kwa sanamu zao." {2T 444.1}

Watu wa Mungu waliwakilishwa kwangu kama wapo katika hali ya kurudi nyuma. Jicho lao halijakita kutazama kwa utukufu wa Mungu peke yake. Utukufu wao wenyewe ndiyo una sauti zaidi. Wanatafuta kujitukuza na bado wanajiita Wakristo. Utakatifu wa moyo na usafi wa maisha lilikuwa somo kuu la mafundisho ya Kristo. Katika Mahubiri Yake ya Mlimani, baada ya kubainisha ni nini lazima kifanyike ili kubarikiwa, na nini kisifanyike, anasema: "Basi ninyi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." {2T 444.2}

Ukamilifu, utakatifu, hakuna pungufu ya hili, ingewapa mafanikio katika kutekeleza kanuni ambazo alikuwa amewapa. Bila utakatifu huu moyo wa mwanadamu una ubinafsi, una dhambi, na ni mbaya. Utakatifu utamwongoza yule alie nao kuzaa na kuzidi daima katika kazi zote njema. Hatachoka kamwe katika kutenda mema, wala hatatafuta vyeo vya ulimwengu huu. Atatazamia kupandishwa juu wakati ambapo Mkuu wa mbinguni utawainua waliotakaswa kwenye kiti chake cha enzi. Ndipo atakapowaambia: "Njoni, mmebarikiwa na Baba Yangu, mrithi ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu." Kisha Bwana anaorodhesha kazi za kujikana nafsi na rehema, huruma na haki, ambazo walikuwa wamefanya. Utakatifu wa moyo, utazaa/utatoa matendo mema. Ni kukosekana kwa hali ya kiroho, kukosekana kwa utakatifu, ndiyo inapelekea vitendo visivyo vya haki, kijicho, chuki, kushuku watu, wivu, maneno mabaya kwa wengine, na kila dhambi ya kuchukiza na iliyo mbaya zaidi. {2Tsw 445.1}

Nimejaribu kwa hofu ya Mungu kuweka mbele ya watu Wake hatari na dhambi zao, na nimejitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu dhaifu, kuwaamsha. Nimesema mambo ya kushangaza, ambayo, ikiwa wangeamini, yangewasababishia mahangaiko na woga, na kuwafanya wawe na usongo katika kutubu dhambi na maovu yao. Nimesema

mbele yao kwamba, kutokana na kile nilichoonyeshwa, ni idadi ndogo ya wale wanaodai kuamini Ukweli mwishowe wataokolewa - sio kwa sababu hawawezi kuokolewa, lakini kwa sababu hawangeokolewa katika njia teule ambayo Mungu Mwenyewe ameichagua. Njia iliyoonyeshwa na Bwana wetu wa MUNGU ni nyembamba sana na lango ni nyofu sana kuweza kuwaingiza wakati wanashikilia ulimwengu au wakati wanathamini ubinafsi au dhambi ya aina yoyote. Hakuna nafasi ya mambo haya; ila bado kuna wachache watakaokubali kuachana na mambo haya, ili wapate kupita njia nyembamba na kuingia kwenye lango nyofu. {2Tsw 445.2}

Maneno ya Kristo yapo wazi: "Jitahidini (akimaanisha henyeka kwa maumivu mengi) kuingia kwa mlango mwembamba; kwa maana, nawaambia, wengi watatafuta kuingia, lakini hawataweza." Sio wote wanaojiita Wakristo ni/walio Wakristo moyoni. Kuna watenda dhambi katika Sayuni sasa, kama ilivyokuwa zamani. Isaya anazungumza juu yao akimaanisha siku ya BWANA: "Wenye dhambi walio katika Sayuni wanaogopa; tetemeko [hofu] limewashika wasiomcha Mungu [wanafiki]; Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao; ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele? Ni yeye aendaye kwa haki, anenaye maneno ya adili; ni yeye anayedharau faida ipatikanayo kwa dhuluma; akung'utaye mikono yake asipokee rushwa; azibaye masikio yake asisikie habari za damu; afumbaye macho yake asitazame uovu. Huyu ndiye atakayekaa juu; majabali ni ngome yake; atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma." {2Tsw 446.1}

Kuna wanafiki sasa ambao watatetemeka watakapojua jinsi walivyo. Uovu wao wenyewe utawatia hofu na mshtuko, katika siku hiyo ambayo itatupata hivi karibuni, siku ambayo "Bwana atatoka mahali Pake kuwaadhibu wakaazi wa dunia kwa uovu wao." Lo, kwamba mambo haya ya kutisha yasiweze kuwapata, ili wawe na hisia za wazi za kujua hali yao na waweze kuamka wakati bado kuna rehema na matumaini, wakiri dhambi zao, na wanyenyekeze roho zao mbele za Mungu, ili awasamehe makosa yao, na kuponya kurudi nyuma kwao! Watu wa Mungu hawako tayari kwa matukio ya kutisha na yanayotaribu mbele yetu, hawako tayari kusimama safi kutoka kwenye uovu na tamaa katikati ya hatari na uharibifu wa enzi hii mbaya ya

uharibifu. Hawana silaha za haki, na hawajajiandaa kupigana na uovu ulioshamiri. Wengi hawatii amri za Mungu, lakini wanakiri kufanya hivyo. Ikiwa wangekuwa waaminifu, kutii amri zote za Mungu wangekuwa na nguvu ambayo ingeleta kuamini kwenye mioyo ya wasioamini. {2Tsw 446.2}

Nimejaribu kutekeleza wajibu wangu. Nimeelezea dhambi maalum za wengine. Nilioneshwa kuwa katika hekima ya Mungu dhambi na makosa ya wote hayangefunuliwa. Ila wote wangekuwa na mwangaza wa kutosha kuona dhambi zao na makosa yao, ikiwa wangependa kufanya hivyo na kwa bidii wapende kuachana nazo, na kukamilisha utakatifu katika kumcha Bwana. Wangeweza kuona ni dhambi gani ambazo Mungu aliziwekea alama na pia kukemea kwa wengine. Ikiwa hizi zilikuwa zikipendwa na wao wenyewe, wangepaswa kujua kwamba zilimchukiza Mungu na walikuwa wametenganishwa Naye; na kwamba wasipoanza kwa bidii na kwa usongo kazi ya kuziondoa wataachwa kwenye giza. Mungu ni Mtakatifu mno kuchukuliana na uovu. Dhambi ni mbaya sana machoni Pake katika kesi hii kama zilivyo kesi nyingine. Hakuna udhuru utakaofanywa na Mungu asiye na upendeleo. Wote walio na hatia hushughulikiwa katika shuhuda hizi za kibinafsi, ingawa majina yao hayawezi kuambatanishwa na ushuhuda maalum uliotolewa; na ikiwa watu binafsi watapitia na kufunika dhambi zao wenyewe kwa sababu majina yao haswa hayajatajwa, hawapewa mafanikio na Mungu. Hawawezi kusonga mbele katika maisha ya kiroho, lakini watazidi kuwa na giza na giza tele, mpaka nuru ya mbinguni itaondolewa kabisa. {2Tsw 447.1}

Wale wanaodai utauwa, lakini hawajatakaswa na Ukweli ambao wanakiri, ila hawatabadilisha mwenendo wao wa vitendo, ambao wanajua ni wa kuchukiza mbele za Mungu, kwa sababu hawajakabiliwa na jaribio la kukemewa mmoja mmoja kwa dhambi zao. Ila Wanaona, kwa shuhuda za wengine, basi kesi yao wenyewe imesondwa kidole kwa uaminifu mbele yao. Wanathamini uovu ule ule. Kwa kuendelea na mwenendo wao wa dhambi, wanakiuka dhamiri zao, wakifanya mioyo yao kuwa migumu, na kuzifanya shingo zao kuwa ngumu, sawa tu na wale ambao shuhuda ilikuwa imetolewa kwao moja kwa moja. Katika kupitia hizo na kisha wakatae kuacha dhambi zao na kurekebisha

makosa yao kwa ungamo la unyenyekevu, toba, na kujidhadhalisha, wanachagua njia yao wenyewe, na wamepewa matokeo sawa, na mwishowe wanaongozwa kuwa mateka na Shetani, kutenda mapenzi yake. Wanaweza kuwa na ujasiri kwa sababu wanaweza kuficha dhambi zao wengine wasizijuie na kwa sababu hukumu za Mungu haziji kwa njia inayoonekana juu yao. Wanaweza kuwa na mafanikio katika ulimwengu huu. Wanaweza kuwadanganya wanadamu maskini, wasioweza kuona vizuri na wakachukuliwa kama mifano ya uchaji Mungu, wakati wako katika dhambi zao. Lakini Mungu hawezi kudanganywa."Kwa sababu hukumu juu ya tendo baya haitekelezwi upesi, mioyo ya wanadamu huthibitishwa ndani yao ili kutenda mabaya. Ijapokuwa mwenye dhambi amefanya maovu mara mia, akazidisha siku zake; lakini hata hivyo najua hakika ya kwamba itakuwa heri kwao wamchao Mungu, wenye kicho mbele Zake; walakini haitakuwa heri kwa mwovu, wala hatazidisha siku zake, zilizo kama kivuli; kwa sababu hana kicho mbele za Mungu." Ingawa maisha ya mwenye dhambi yanaweza kurefushwa humu duniani, lakini sio katika nchi mpya. Atakuwa kama yule ambaye Daudi anamtaja katika Wimbo wa Zaburi:"Kwa maana bado kitambo kidogo, na mtu mwovu hatakuwapo; Naam, utafikiria kwa makini mahali pake, wala hapatakuwapo. Bali wapole watairithi nchi." {2Tsw 447.2}

Rehema na Ukweli huahidiwa kwa watu wanyenyekevu na wanaotubu, lakini hukumu zimeandaliwa kwa wenye dhambi na waasi. "Haki na hukumu ndio makao ya kiti chako cha enzi." Watu waovu na wazinzi hawataepuka hasira ya Mungu na adhabu waliyoipata kwa haki. Mwanadamu ameanguka; na itakuwa kazi ya maisha yote, iwe ndefu au fupi, kupona kutoka kwa anguko hilo, na kupitia Kristo, kurudisha tena sura ya Mungu, ambayo aliipoteza kwa dhambi na kuendelea kwa uovu. Mungu anahitaji mabadiliko kamili ya nafsi, mwili, na roho ili kupata tena hali iliyopotea kupitia Adamu. Bwana kwa huruma hutuma miale ya nuru kumwonyesha mwanadamu Ukweli wa hali yake. Ikiwa hatatembea katika nuru, anaonyesha furaha akiwa gizani. Hatakuja kwenye nuru ili asiye akakemewa na matendo yake. {2Tsw 448.1}

Kesi ya N. Fuller imenisababishia huzuni nyingi na uchungu wa roho. Kwamba amejitoa chini ya udhibiti wa Shetani, kufanya uovu kama



alivyofanya ni jambo la kutisha sana. Ninaamini kwamba Mungu alipanga kwamba kesi hii ya unafiki na uovu, iwekwe wazi kwa njia ambayo imefanyika, ili iweze kuthibitisha onyo kwa wengine. Hapa ni kisa cha mtu ambaye alikuwa anafahamu mafundisho ya Biblia, na ambaye alikuwa amesikiliza shuhuda zilizobebwa nami mbele yake, dhidi ya dhambi alizokuwa akifanya. Zaidi ya mara moja alikuwa amenisikia nikisema kwa hakika juu ya dhambi zilizopo za kizazi hiki, kwamba ufisadi ulikuwa umeenea kila mahali, kwamba tamaa mbaya ilidhibiti wanaume na wanawake kwa ujumla, kwamba miongoni mwao kulikuwa na rundo la uhalifu wenye giza jeusi ulioendelea kufanywa kila wakati, na walikuwa wakipata harufu mbaya ya uharibifu wao wenyewe. Mekanisa ya majina na si matendo yamejaa uasherati na uzinzi, uhalifu na mauaji, matokeo ya tamaa mbaya, tamaa ya zinaa; lakini vitu hivi hufichwa. Wahudumu katika ngazi za juu wana hatia; lakini mavazi ya utauwa hufunika matendo yao ya giza, na huendelea mwaka hadi mwaka katika mwenendo wao wa unafiki. Dhambi za makanisa'yenye jina' zimefika mbinguni, na waaminifu mioyoni wataletwa kwenye nuru na kutoka huko. {2Tsw 449.1}

Kutokana na nuru ambayo Mungu amenipa, uasherati na uzinzi unachukuliwa na idadi kubwa ya wanamarejeo wanaotunza siku ya kwanza kama dhambi ambazo Mungu hazitilii maanani, anazifumbia macho tu. Dhambi hizi zinafanywa kwa kiwango kikubwa. Hawatambui madai ya sheria ya Mungu juu yao. Wamevunja amri za YEHOVA Mkuu na kwa bidii hufundisha wasikilizaji wao kufanya vivyo hivyo, wakitangaza kwamba sheria ya Mungu imefutwa na haina nguvu yoyote juu yao. Kwa mujibu wa hali hii ya uhuru wa mambo, dhambi haionekani kuwa mbaya sana; "kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria."Tunaweza kutarajia kupata katika kikundi hiki, wanaume ambao watadanganya, na kusema uwongo, na kujiachilia kwa tamaa mbaya. Lakini wanaume na wanawake wanaotambua Amri Kumi zina mashiko bado, ambao wanashika amri ya nne ya sheria kumi za MUNGU. Wanapaswa kutekeleza maishani mwao kanuni za maagizo yote kumi, yaliyotolewa kwa ukuu wa kutisha kutoka Mlima Sinai. {2Tsw 449.2}

Waadventista Wasabato, ambao wanadai kuwa wanangojea na kupenda ujio wa Kristo, hawapaswi kufuata mwenendo wa watu wa dunia. Hao sio kigezo cha watunza amri. Wala hawapaswi kuiga mfano wa wanamarejeo wanaotunza siku ya kwanza, ambao wanakataa kukubali madai ya sheria ya Mungu na kuikanyaga chini ya miguu yao. Kundi hili halipaswi kuwa kigezo kwao. Waadventista wanaoshika amri wanachukua nafasi ya pekee, iliyoinuliwa. Yohana aliwaona katika maono matakatifu na kwa hivyo aliwaelezea: "Hawa ndio wale wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." {2Tsw 450.1}

Bwana alifanya agano maalum na Israeli ya kale: "Basi sasa, ikiwa mtasikiliza sauti Yangu, na kulishika agano Langu, basi mtakuwa hazina ya kipekee Kwangu kuliko watu wote; kwa maana dunia yote ni Yangu. Nanyi Mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu." Anawahutubia watu Wake wanaoshika amri katika siku hizi za mwisho: "Bali ninyi ni kizazi kiteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa pekee; ili mpate kumwonyesha Yeye aliyewaita kutoka gizani na kuingia katika mwanga wa ajabu." "Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho." {2Tsw 450.2}

Sio wote wanaodai kuzishika amri za Mungu wanatawala miili yao katika utakaso na heshima. Ujumbe makini na mzito kabisa kuwahi kutolewa kwa bin-Adamu umekabidhiwa watu hawa wanaokufa, na wanaweza kuwa na ushawishi mkubwa ikiwa watatakaswa na huo ujumbe. Wanakiri kwa midomo kusimama juu ya jukwaa lililoinuliwa la Ukweli wa milele, wakishika amri zote za Mungu; kwa hivyo, ikiwa wanajiingiza katika dhambi, ikiwa wanafanya uasherati na uzinzi, kosa lao ni kubwa zaidi ya mara kumi, kuliko yale makundi niliyoyataja, ambayo hayakubali sheria ya Mungu kuwa ina mashiko. Kwa namna ya pekee wale wanaodai kushika sheria ya Mungu wanamvunjia heshima na kuishutumu Kweli kwa kuvunja maagizo Yake. {2Tsw 450.3}

Ilikuwa katika kuenea kwa dhambi hiyo hiyo, uasherati, kati ya Israeli ya kale, ambayo ilileta juu yao dhihirisho la ishara ya kuchukizwa kwa Mungu. Hukumu Zake zilifuata kwa karibu dhambi yao hiyo mbaya; maelfu walianguka, na miili yao iliyooza, iliachwa kuleta uchafuzi jangwani. "Lakini Mungu hakufurahishwa na wengi wao; maana

waliafia nyikani. Sasa mambo haya yalikuwa mifano yetu, ili tusiwe na tamaa ya mambo mabaya, kama vile wao pia walivyoyatamani. Wala msiwe waabudu sanamu, kama vile wengine wao walivyokuwa, kama ilivyoandikwa, Watu walikaa chini kula na kunywa, wakainuka kucheza. Wala tusizini, kama wengine wao walivyozeni, na wakaanguka kwa siku moja elfu ishirini na tatu. Wala tusijaribu Kristo, kama wengine wao walivyomjaribu, na waliangamizwa na nyoka. Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika, na kuangamizwa na Mwangamizi. Sasa mambo haya yote yaliwapata kuwa mifano, na yameandikwa ili kutuonya, ambaye mwisho wa ulimwengu umemjia. Kwa hivyo yeye anayedhani anasimama aangalie asianguke. " {2Tsw 451.1}

Waadventista Wasabato, kuzidi watu wengine wote ulimwenguni, wanapaswa kuwa mifano ya uchaji, utakatifu wa moyo na mazungumzo. Nilielezea mbele ya N. Fuller kwamba watu ambao Mungu alikuwa amewachagua kama hazina Yake ya kipekee walitakiwa kuinuliwa, kusafishwa, kutakaswa, washiriki wa tabia ya Mungu, wakiwa wameepuka uharibifu uliopo ulimwenguni kupitia tamaa. Je! Wale ambao wamemkiri MUNGU kwa hali ya juu wajiingize katika dhambi na uovu, hatia yao itakuwa kubwa sana. Bwana hukemea dhambi za mtu mmoja, ili wengine wachukue hilo onyo na wapate woga (hofu). {2Tsw 451.2}

Maonyo na karipio hayatolewi kwa Waadventista Wasabato wenye makosa kwa sababu maisha yao ni ya kulaumiwa zaidi kuliko maisha ya wanaojiita Wakristo wa makanisa ya 'jina tu', wala sio kwamba matendo yao ni mabaya kuliko Wasabato wale ambao hawakubali utii kwa madai ya sheria ya Mungu, lakini kwa sababu wao wana nuru kubwa, na kwa kukiri kwao wamechukua msimamo wao kama watu maalum wa Mungu, wateule, wenye sheria ya Mungu iliyoandikwa mioyoni mwao. Wanaashiria uaminifu wao kwa Mungu wa mbinguni kwa kujitolea kutii sheria za serikali Yake. Wao ni wawakilishi wa Mungu duniani. Dhambi yoyote ndani yao inawatenganisha na Mungu na, kwa namna ya pekee, inalitikana Jina Lake kwa kuwapa maadui wa sheria Yake takatifu, nafasi ya kulaumu kusudi na hoja Yake na watu Wake, ambao amewaita "mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa

takatifu, watu wa pekee, "ili waonyeshe sifa za Yeye aliyewaita watoke gizani na kuingia katika nuru Yake ya ajabu. {2Tsw 452.1}

Watu ambao wanafanya vita na sheria ya YEHOVA Mkuu, ambao wanaona jambo jema kuzungumza, kuandika, na kutenda mambo ya kuleta uchungu na ya kuchukiza zaidi kuonyesha dharau yao ya sheria hiyo, wanaweza kufanya taaluma iliyoinuliwa ya upendo kwa Mungu, na ikaonekana wana bidii kubwa ya kidini, kama walivyokuwa makuhani wakuu wa Kiyahudi na wazee; lakini, katika siku ya BWANA, "Watapatikana wamepungukiwa" Itasemwa juu yao na Mtukufu wa mbinguni. "Kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria." Kioo ambacho kingewasaidia kugundua kasoro za wahusika wao, hukasirikiwa, kwa sababu kinaonyesha dhambi zao. Waadventista wanaoongoza ambao wameikataa nuru wamepata moto wa wazimu dhidi ya sheria takatifu ya Mungu, kama vile taifa la Kiyahudi lilivyokuwa dhidi ya Mwana wa Mungu. Wako katika udanganyifu wa kutisha, wakidanganya wengine na kudanganywa wenyewe. Hawataifikia nuru, matendo yao yasipate kukemewa. Hao hawawezi kufundishwa. Lakini Bwana huwakemea na kuwasahihisha watu wanaodai kutii sheria Zake. Yeye Anaonyesha dhambi zao na kuweka wazi uovu wao, kwa sababu Yeye anataka kuwatenganisha na dhambi zote na uovu, ili waweze kuukamilisha utakatifu katika hofu Yake na wawe tayari kufa katika Bwana au kuchukuliwa mbinguni Ajapo mara ya pili. Mungu huwakemea, huwakaripia, na kuwasahihisha, ili waweze kusafishwa, kutakaswa, kuinuliwa, na mwishowe kuinuliwa kwenye kiti Chake cha enzi. {2Tsw 452.2}

Mzee Fuller amesikia ushuhuda unaotolewa hadharani, kwamba watu waliodai ni wa Mungu siyo wote ni watakatifu, na kwamba wengine walikuwa wafisadi. Mungu alitaka kuwainua, lakini walikataa kupanda kwenye nyanda za juu kwenye utekelezaji. Hasira mbaya za kinyama ziliwafanya wayumbe-yumbe, na nguvu za maadili na akili zilishindwa na kuwafanya wawe watumishi wa tamaa hizo mbaya. Wale ambao hawadhibiti tamaa zao za msingi hawawezi kufahamu upatanisho au kuweka thamani sahihi juu ya roho. Hawana uzoefu wa wokovu na hata hawauelewi. Kuridhisha shauku ya kinyama ni matamanio yao makubwa zaidi ya maisha yao. Mungu hatakubali chochote isipokuwa

usafi na utakatifu; doa moja, kunyanzi moja, kasoro moja katika tabia, itawazuia milele kutoka mbinguni, na utukufu na hazina Zake zote. {2Tsw 453.1}

Majaliwa ya kutosha ya Mungu yametolewa kwa wote ambao kwa dhati, kwa bidii, na kwa kufikiria, wanaanza kazi ya kukamilisha utakatifu katika hofu ya Mungu. Nguvu, neema, na utukufu vimetolewa kupitia Kristo, ili ziletwe na malaika wanaohudumia warithi wa wokovu. Hakuna aliye chini sana, aliye fisadi na mbaya, hivi kwamba hawawezi kupokea kwa Yesu aliyekufa kwa ajili yao, nguvu, usafi, na haki, ikiwa wataondoa dhambi zao, wataacha mwenendo wao wa uovu, na watageuka na kusudi kamili la moyo. kwa Mungu aliye hai. Bwana Anasubiri kuwavua nguo zao, zenye madoa na kuchafuliwa na dhambi, na kuwavika mavazi meupe, yangaayo haki; Naye Anawaamuru waishi na wasife. Katika Yeye wanaweza kushamiri. Matawi yao hayatanyauka wala kuacha kuzaa matunda. Ikiwa wanakaa ndani Yake, wanaweza kupata maji na lishe kutoka Kwake, kujazwa na Roho Wake, kutembea hata kama Yeye alivyotembea, kushinda kama Alivyoshinda, na kuinuliwa kwa mkono Wake wa kulia. {2Tsw 453.2}

Mzee Fuller ameonywa. Maonyo waliyopewa wengine yalimhukumu. Dhambi zilizoshutumiwa kwa wengine zilimkemea na kumpa nuru ya kutosha kuona jinsi Mungu anavyochukulia uhalifu wa mhusika kama vile alikuwa akifanya, lakini hakuacha njia yake mbaya. Aliendelea kufuata njia yake za kutisha, zisizo za utauwa na mbovu, akiharibu miili na roho za kundi lake. Shetani alikuwa ameimarisha tamaa mbaya ambazo mtu huyu hakuzitiisha, na akazishirikisha katika kazi yake ya kuongoza roho za watu kifoni. {2Tsw 454.1}

Wakati alikiri kushika sheria ya Mungu, alikuwa, kwa njia ya kujipendeza zaidi, akikiuka maagizo yake yaliyo wazi. Alijitoa mwenyewe kwa kuridhia kwa anasa za kidunia. Amejiuza kufanya uovu. Je! Mshahara wa mtu kama huyo utakuwa nini? Hasira na ghadhabu ya Mungu itamwadhibu kwa dhambi. Kisasi cha Mungu kitaamshwa dhidi ya wale wote ambao tamaa zao mbaya za mwili zimefichwa chini ya mavazi ya kichungaji. Wakati alikiri kuwa mchungaji wa kundi, alikuwa akiongoza kundi kwenye uharibifu wa uhakika. Matokeo haya ya

kutisha ni matunda ya tamaa za mwili, ambayo "ni uadui dhidi ya Mungu; kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi." {2Tsw 454.2}

Nilirejelewa kwa Andiko hili: "Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki." Waliodai kuwa Wakristo, ikiwa hakuna nuru zaidi, mmepewa ile Iliyomo katika fungu hili, hamtakuwa na udhuru ikiwa mtakubali kudhibitiwa na tamaa mbaya. {2Tsw 454.3}

Neno la Mungu linatosha kuangazia akili iliyo na ukungu na linaweza kueleweka na wale ambao wana hamu yoyote ya kulielewa. Lakini pamoja na hayo yote, wengine wanaodai kusoma Neno la Mungu hupatikana wakiishi kinyume kabisa na mafundisho Yake yaliyo wazi. kisha, huwaacha wanaume na wanawake bila udhuru, Mungu anatoa ushuhuda ulio rahisi na wazi, akiwarejesha kwenye Neno ambalo wamepuuza kufuata. Walakini wale wanaotumikia matamania yao wanaacha mwangaza huu wote. Hawataacha mwendo wao wa dhambi, lakini wataendelea kufurahia udhalimu mbele ya vitisho na kisasi cha Mungu dhidi ya wale wanaofanya mambo kama hayo. {2Tsw 454.4}

Kwa muda mrefu nimekuwa nikitaka kuongea na dada zangu na kuwaambia hivyo, kutokana na kile Bwana amekuwa radhi kunionyesha mara kwa mara, kuna kosa kubwa miongoni mwao. Hawajali kujiepusha na mionekano yote ya uovu. Sio wote wenye uangalifu katika mwenendo wao, kama inavyofaa wanawake wanaodai ni watauwa. Maneno yao hayachambuliwi na kuchaguliwa vizuri kama wale ya wanawake ambao wamepokea neema ya Mungu. Wanajiweka karibu sana na wanaume. Wanakaa karibu nao, huelekea kwao, na wanaonekana kuchagua jamii yao. Wanaridhishwa sana na kutaka kupata umakini na usikivu wa wanaume. {2Tsw 455.1}

Kutoka kwa nuru ambayo Bwana amenipa, dada zetu wanapaswa kufuata njia tofauti. Wanapaswa kujihadhi (kuwa na soni-reserved) zaidi, waonyeshe ujasiri mdogo, na wajihimize ndani yao faraja "kuwa na haya usoni/soni na kiasi." Wote kaka na dada huendekeza a

mazungumzo mengi sana ya urafiki na kuchangamkiana mno wakati wakiwa pamoja. Wanawake wanaodai utauwa huendekeza mzaha mwingi, futuhi, na kucheka. Hii haifai, ni kutokuwa na staha na inamhuzunisha Roho wa Mungu. Maonyesho haya yanaonyesha ukosefu wa usafishwaji/uboreshaji wa Kweli wa Kikristo. Hayatii nguvu roho ndani ya Mungu, lakini huleta giza kuu; wanawafukuza malaika safi, waliosafishwa (wasio na mawaa), wa mbinguni na huwashusha chini wale wanaojihusisha nao makosa haya, kwa kiwango cha chini. {2T 455.2}

Dada zetu wanapaswa kuhimiza upole, unyenyekevu wa Kweli; hawapaswi kuwa mstari wa mbele, kuzungumza, kuwa wenye ujasiri, kimbelembele, lakini wanyenyekevu na wasio na kiburi, wepesi wa kusema. Wanapaswa kuthamini kujistahi, adabu, na uungwana. Kuwa mkarimu, wapole, wenye huruma, wenye kusamehe, na wanyenyekevu, hii itakuwa inampendeza Mungu. Ikiwa watachukua nafasi hii hawatalemewa na macho/umakini usiofaa kutoka kwa wanaume ndani ya kanisa au nje. Wote watahisi kuwa kuna duara takatifu la usafi karibu na wanawake hawa wanaomcha Mungu, ambalo linawalinda kutokana na uhuru wowote usiofaa. {2Tsw 456.1}

Pamoja na wanawake wengine wanaodai utauwa, kuna uhuru wa ovyo, wa kihuni, mbaya wa njia ambayo husababisha uovu na makosa. Lakini wale wanawake wacha Mungu ambao akili na mioyo yao inashiriki katika kutafakari juu ya mada ambazo zinaimarisha usafi wa maisha, na yale ambayo huinua roho kuzungumza na Mungu, hawatapotoshwa kwa urahisi kutoka kwa njia ya haki na wema. Hao wataimarishwa dhidi ya udanganyifu na ustadi wa Shetani; watakuwa tayari kuhimili sanaa yake ya kutongoza jinsia nyingine. {2T 456.2}

Ubatili na upuuzi, mitindo au fasheni ya ulimwengu, tamaa ya jicho, na tamaa ya mwili, zimeunganishwa na anguko la wenye bahati mbaya. Yale yanayopendeza moyo wa asili na akili ya mwili hupendwa. Ikiwa mizizi ya tamaa ya mwili ingeng'olewa mioyoni mwao wasingekuwa dhaifu sana [kimaadili]. Ikiwa dada zetu wangehisi umuhimu wa kutakasa mawazo yao, kamwe hawangeteseka kwa uzembe wa tabia ambao unasababisha matendo yasiyofaa, hawahitaji kabisa kuchafua

usafi wao wa moyo hata kidogo. Ikiwa wangeona jambo hili kama vile Mungu amewasilisha kwangu, wangukuwa na chuki kubwa ya vitendo vichafu hivi kwamba wasingepatikana kati ya wale ambao wataanguka kupitia majaribu ya Shetani, bila kujali ni nini kitakachochaguliwa kama chombo cha kuwasilisha makwazo hayo. {2T 456.3}

Mhubiri anaweza kuwa anashughulika na vitu vitakatifu, vilivyowekwa wakfu, na bado asiwe mtakatifu moyoni. Anaweza kujitoa kwa Shetani kufanya uovu na kuharibu roho na miili ya kundi lake. Walakini ikiwa akili za wanawake na vijana wanaodai kumpenda na kumcha Mungu zingeimarishwa na Roho Wake, ikiwa wangezifundisha akili zao usafi wa mawazo na kujielimisha ili kuepuka mwonekano wowote wa uovu, wangukuwa salama kutokana na utongozaji wowote usiofaa na kuwa salama kutokana na ufisadi uliowazunguka. Mtume Paulo aliandika juu yake mwenyewe: "Naupa mwili wangu mazoezi magumu na kuutia katika nidhamu kamili, nisije mimi mwenyewe nikakataliwa baada ya kuwahubiria wengine." {2T 456.4}

Ikiwa mhudumu wa injili hathibiti matamanio yake ya chini, ikiwa anashindwa kufuata mfano wa mtume na hivyo avunja heshima taaluma yake na imani yake hata kutaja jina la tamaa ya dhambi, dada zetu wanaokiri utauwa hawapaswi kwa kujidanganya hata mara moja wenyewe, kwamba dhambi au uhalifu hupoteza uzito wake kwa sababu mchungaji wao pia anathubutu kuifanya. Ikiwa wanaume wanaowajibika wanaonekana kuipenda na kuikaribia dhambi, hii haipaswi kupunguza hatia na ukubwa wa dhambi hiyo akilini mwa mtu yeyote. Dhambi inapaswa kuonekana kama dhambi daima, inapaswa ionekane ni ya kuchukiza, kama ilivyokuwa ikizingatiwa hapo awali; na akili za walio safi na walioinuliwa zinapaswa kumchukia na kumkwepa yule anayejiingiza katika dhambi, kama vile wangemkimbia nyoka ambaye uchungu wake ulikuwa mbaya. {2T 457.1}

Ikiwa akina dada wangeinuliwa na wakawa na usafi wa moyo, utongozaji wowote wa ufisadi, hata kutoka kwa wahudumu wao, ungepingwa kwa njia nzuri na usingerudiwa tena kamwe. Akili lazima ziwe na ukungu mwingi wa Shetani ikiwa wanaweza kusikiliza sauti ya yule anayetongoza eti sababu yeye ni mchungaji, na kwa hivyo huvunja



amri za Mungu zilizo wazi na nzuri na kujidanganya kwamba hawatendi dhambi. Je! Hatuna Maneno ya Yohana: "Yeye asemaye, Ninamjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, na Ukweli haumo ndani yake"? Je, Sheria inasema nini? "Usizini." Wakati mtu anayedai kushika sheria takatifu ya Mungu, na kuhudumu katika kwenye vitu vitakatifu, hutumia fursa ya ujasiri aliopewa wa mamlaka yake na anatafuta jinsi ya kutosheleza tamaa zake za mwili za msingi, Ukweli huu wenyewe tu unapaswa kuwa tosha kumwezesha mwanamke anayedai kumcha Mungu kuona kwamba, ingawa mwanamume huyu ana nafasi iliyoinuliwa kama mbingu, pendekezo lisilo safi kama la utongozaji kutoka kwake hutoka kwa Shetani aliyejifanya malaika wa nuru. Nashindwa kuamini kwamba Neno la Mungu linakaa ndani ya mioyo ya wale ambao hujitoa kwa urahisi kutelekeza usafi wao wa moyo na wema uchafuliwe juu ya madhabahu ya tamaa mbaya. {2T 457.2}

Dada zangu, epukeni hata mwonekano wa uovu. Katika enzi hizi za kasi, zenye harufu ya ufisadi unaotokota, hatuko salama bila kuwa macho kwa ulinzi. Wema na adabu ni nadra. Ninawasihi kama wafuasi wa Kristo, ambao mmekiri kuhusu Imani yenu kwa hali ya kuinuliwa, kuthamini vito vya thamani, na vya bei ya juu vya staha na adabu ya Mkristo. Hii italinda maadili mema. Ikiwa una tumaini lolote a kuinuliwa mbinguni mwishowe ili ujiunge na kikundi cha malaika safi, wasio na dhambi, na kuishi katika mazingira ambayo hakuna hata doa la uchafu mdogo wa dhambi, thamini kujistahi, uungwana, unyenyekevu na wema. Hakuna kitu isipokuwa usafi, usafi mtakatifu, utasimama uhakiki mzuri, huo utastahimili siku ya BWANA, na kupokelewa katika mbingu safi na takatifu. {2T 458.1}

Kishawishi kidogo tu, kutoka chanzo chochote kinachoweza kuja, kikikukaribisha kuendekeza dhambi au kuruhusu kujianika kwenye uhuru usiofaa kwako, kinapaswa kuchukiwa kama dharau mbaya zaidi kwa utu wako wenye heshima (dignified womanhood). Busu kwenye shavu lako, wakati na mahali pasipo sahihi, linapaswa kukufanya ukatae kumfukuza mjumbe wa Shetani kwa kuchukizwa. Ikiwa ni kutoka kwa mtu aliye katika kazi za juu zihusuzo mambo matakatifu, dhambi hiyo ni kubwa zaidi ya mara kumi, na inapaswa kumwongoza

mwanamke au kijana aliye na hofu ya Mungu kupatwa na woga/hofu, sio tu kutokana na dhambi ambayo angekufanya utende, lakini pia kutokana na unafiki na kucheza na uovu kwa mtu ambaye watu wanamheshimu na kumheshimu kama mtumishi wa Mungu. Anashughulikia vitu vitakatifu, lakini anaficha Ukweli wa moyo wake chini ya vazi la uchungaji. Epuka aina yoyote ya mahusiano ya namna hiyo. Kujihusisha na uovu huu hata kwa njia ndogo sana ni ushahidi wa kutosha wa ubongo wenye uovu unaohusiana na ngono na jicho lenye tamaa. Ikiwa kitia-moyo kidogo kimetolewa katika mwelekeo huu, ikiwa kutongozwa kwa aina iliyotajwa kunavumiliwa, hakuna ushahidi bora zaidi unaoweza kutolewa kwamba akili yako sio safi na salama kama inavyopaswa kuwa, na kwamba dhambi na uhalifu vina mvuto kwako. Unashusha kiwango cha hadhi yako ya mwanamke na uadilifu, na unatoa ushahidi bila kuacha mashaka kwamba shauku ya chini, ya kinyama, ya kawaida na tamaa imeruhusiwa kubaki hai moyoni mwako na haijawahi kusulubishwa. {2Tsw 458.2}

Kama nilivyoonyeshwa hatari za wale wanaodai mambo bora, na dhambi ambazo ziko kati yao, - -kikundi ambacho hakuna aliyekishuku kuwa katika hatari yoyote kutokana na dhambi hizi zinazochafua, - - nimeongozwa kuuliza: Je, ni Nani, Ee Bwana, Atakayekuwa tayari kusimama utakapotokea? Ni wale tu walio na mikono safi na mioyo safi, watasimama siku ya kuja Kwake. {2Tsw 459.1}

Ninahisi kusukumwa na Roho wa Bwana kuwahimiza dada zangu ambao wanadai utauwa kuchangamkia mwenendo wa adabu usio wa kujianika (kutojiheshimu), kuonea haya uovu na kuwa na kiasi. Uhuru uliochukuliwa katika enzi hii ya uovu/ufisadi haupaswi kuwa kigezo kwa wafuasi wa Kristo. Maonyesho haya ya mitindo ya kufahamiana hayapaswi kuwepo kati ya Wakristo wanaoenda kuvikwa kutokufa. Ikiwa uasherati, uchafuzi, uzinzi, uhalifu, na mauaji ni utaratibu wa kila siku kati ya wale ambao hawajui ile Kweli, na ambao wanakataa kudhibitiwa na kanuni za Neno la Mungu, ni muhimu kwa kiasi gani, kwamba kundi linalodai kuwa wafuasi wa Kristo, washirika wa karibu na Mungu na malaika, kupaswa kuonyesha njia/mfano bora na wa kiungwana zaidi. Ni muhimu kiasi gani kwamba kwa usafi wao na

fadhila yao wasimame tofauti kabisa na kundi lile ambalo linadhibitiwa na tamaa mbaya za wanyama. {2Tsw 459.2}

Nimeuliza: Je! Ni lini wadada katika ujana wao watajistahi kwa usahihi? Ninajua kuwa hakutakuweco na mabadiliko yoyote ya maamuzi hadi wazazi watakapoona umuhimu kwa kuwa na uangalifu zaidi katika kuwafundisha watoto wao kwa usahihi. Wafundishe kutenda kwa kujistahi na unyenyekevu. Waelimishe wawe na manufaa, na msaada, kuhudumia wengine kuliko kushugulikiwa na kuhudumiwa. {2Tsw 459.3}

Shetani anatawala akili za vijana kwa ujumla. Binti zako hawafundishwi kujikana nafsi na kujikana nafsi. Wanabembelezwa, wanaendekezwa na kiburi chao kinakuzwa. Wanaruhusiwa kujifanyia wanavyotaka hadi wanakuwa wakaidi na wenye kujipendeza wenyewe, na akili yako inashugulishwa na kuchanganyikiwa kujua ni njia gani ufuata ili uwaokoe kutoka kwa uharibifu. Shetani anawaongoza kuwa mithali/msemo katika vinywa vya wasioamini kwa sababu ya ujasiri wao, kutokuwa na aibu na staha na unyenyekevu wa kike. Wavulana wadogo vile vile wameachwa kuwa na njia yao wenyewe. Kabla ya kuingia ujana tu, au miaka ya kumi + au kubalehe, wameshaanza kuwa karibu na wasichana wadogo wa rika lao, wakiandamana nao nyumbani na kufanya nao mapenzi. Na wazazi wamo kifungoni kabisa kupitia tamaa zao wenyewe na mapenzi potofu kwa watoto wao hivi kwamba hawathubutu kufuata mwendo ulioazimiwa katika kuamua kufanya mabadiliko na kuwazuia watoto wao wenye kasi sana katika umri huu wa haraka. {2T 460.1}

Kwa wasichana wengi wadogo wavulana ndio mada ya mazungumzo yao; Na kwa upande wa vijana wa kiume, ni wasichana ndiyo somo la mazungumzo yao. "Kwa maana mtu huongea kutokana na yale yaliyojaa moyoni mwake." Wanazungumza juu ya mada ambazo akili zao hutembelea zaidi. Malaika wa anayefanya kazi ya kurekodi maisha, anaandika maneno ya wavulana na wasichana wanaodai kuwa Wakristo. Je! Watachanganyikiwa na kuona aibu kwa kiasi gani watakapokutana nayo tena katika siku ya BWANA! Watoto wengi ni wanafiki wacha Mungu. Vijana ambao hawajakiri mambo ya Mungu

bado hukwazwa na hawa wanafiki, na mioyo yao kufanywa migumu kwa kila juhudi zinazoweza kufanywa na wale wanaopenda wokovu wao. {2Tsw 460.2}

Lazima kuwe na watu wanaochaguliwa katikati ya kazi, wanaume ambao katika kila dharura wanaweza kutegemewa kutunza ngome, wanaume wasio na ubinafsi, walio na ukarimu mwingi na kazi zote nzuri, ambao maisha yao yamefichwa ndani ya Mungu, na wanaofikiria maisha bora yenye thamani kuliko chakula na mavazi. "Je! maisha si zaidi ya chakula, na mwili ni zaidi ya mavazi?" Mungu anawaita walinzi waaminifu kwenye moyo wa kazi, ni nani atakayependa roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake, na ni nani atakayechukua mzigo wa roho zinazoangamia, akitazamia malipo hayo ya thawabu ambayo yatakuwa yao watakapoingia kwenye furaha ya Bwana wao, na kuona roho zilizookolewa kupitia juhudi zao na kuishi kwa muda milele kama vile Mungu aishivyo, na kuwa na furaha, furaha ya milele, katika ufalme Wake mtukufu. Oh jamani, kama tungewaamsha akina baba na akina mama kwa busara na wajibu wao! Laiti wangehisi kwa uzito mkubwa wa jukumu ambalo liko juu yao! Basi wangeweza kumzuia adui na kupata ushindi wa thamani kwa Yesu. Wazazi hawaelewi kikamilifu jambo hili. Wanapaswa kuchunguza kwa karibu maisha yao, kuchambua mawazo na nia zao, na waone ikiwa wamekuwa waangalifu katika mwenendo wao. Wanapaswa kuangalia kwa karibu kuona ikiwa mfano wao katika mazungumzo na mwenendo, umekuwa vile wangetamani watoto wao kuiga. Usafi na fadhili zinapaswa kung'aa katika maneno na matendo yao mbele ya watoto wao. {2Tsw 460.3}

Nimeonyeshwa familia ambazo mume na baba hajakuwa na staha hiyo na kujihadhi ule utu wenye heshima, mfano wa Mungu, anaopaswa kuvaa mfuasi wa Kristo haukuwepo. Ameshindwa kufanya matendo mema ya upole, upendo mwanana, huruma nyororo, uungwana, na adabu anayopasa kumtendea mkewe, ambaye ameahidi mbele za Mungu na malaika kumpenda, kumheshimu, na kumjali wakati wote wanapoishi pamoja. Msichana aliyeajiriwa kufanya kazi ndiyo amekuwa huru na kwenda mbele kidogo ya wajibu wake, kwa kutengeneza nywele zake na kuwa makini kwa upendo wake, na huyu

baba anafurahi, huku ni kufurahishwa kwa kijinga. Amepunguka katika uonyeshaji wa upendo wake na umakini kwa mkewe kama alivyokuwa zamani. Ni hakika kwamba Shetani anafanya kazi hapa. Heshimu wafanyakazi ulioajiri wakusaidie, uwatendee fadhili, kwa uangalifu, lakini usiende zaidi ya hapo. Ruhusu mwenendo wako usiwe wa kuwatongoza au kuwa na mazoea nao. Ikiwa una maneno ya fadhili na matendo ya adabu ya kutoa kwao, ni salama kila wakati kumwambia mke wako ayapeleke kwao. Itakuwa baraka kubwa kwake, na italeta furaha katika moyo wake, na hii itaakisiwa kwako tena. {2T 461.1}

Nimeonyeshwa pia kwamba mke ameruhusu huruma zake na shauku na mapenzi yake kwenda kwa wanaume wengine, ambao wanaweza kuwa washiriki wa familia. Yeye huwafanya kuwa wasiri wake, anaonyesha upendeleo wa kuwa nao, na huwaelezea shida zake na labda maswala yake ya kibinafsi ya familia. {2T 462.1}

Haya yote ni makosa. Shetani yuko chini yake; na usipotishika na kuachia haya hapo ulipo, adui atakuongoza kwenye uharibifu. Huwezi kuzingatia tahadhari ya kutosha na kuhimiza hifadhi ya kutosha katika suala hili. Ikiwa una maneno ya kujali, ya upendo na umakini ya kutoa, hebu mpe yule ambaye uliahidi mbele za Mungu na malaika kumpenda, kumheshimu, na kumjali wakati wote mtakapokuwa hai. Ah, ni Maisha mangapi yamefanywa machungu kwa kuvunjika kwa kuta ambazo zinafunga siri za kila familia na ambazo zimeratibiwa kuhifadhi usafi na utakatifu Wake! Mtu wa tatu anapelekewa siri na mke, na mambo yake binafsi ya familia huwekwa wazi mbele ya rafiki huyo maalum. Hiki ni kifaa cha Shetani kutenganisha mioyo ya mume na mke. Laiti hii ingekoma! Mashida ya ulimwengu mengi yangeondoka! Fungeni ndani ya mioyo yenu Habari za makosa ya mwenzi. Mwambie Mungu shida zako peke yako (E). Yeye Anaweza kukupa ushauri sahihi na faraja ya uhakika, ambayo itakuwa safi, bila uchungu ndani yake. {2Tsw 462.2}

Ninafahamiana na wanawake kadhaa ambao wamefikiria ndoa zao zilikuwa makosa. Wamesoma riwaya za mapenzi mpaka mawazo yao yamekuwa ya ugonjwa, na wanaishi katika ulimwengu wa ubunifu wao wenyewe. Wanajifikiria kuwa wao ni wanawake wenye akili nyeti, wa hali ya juu, iliyosafishwa, na wanafikiria kwamba waume zao si watu

wa kisasa na maendeleo sana (washamba), kwamba hawana sifa hizi za hali ya juu, na kwa hivyo hawawezi kufahamu tabia zao za juu (wanafikiria wao wenyewe ni za juu!), zilizosafishwa. Kwa hivyo wanawake hawa wanajiona kuwa ni wa hali ya juu katika wanaoteseka, na wafia maadili. Wamezungumza juu ya hili na kulifikiria mpaka wamekuwa karibu na kuwa na wenda-wazimu juu ya mada hii. Wanafikiria kuwa na thamani kubwa kuliko ile ya wanadamu wengine, na haikubaliki kwa hisia zao 'nzuri' kushirikiana na ubinadamu wa kawaida. Wanawake hawa wamejifanya kuwa wapumbavu; na waume zao wako katika hatari ya kufikiria kwamba wanawake hawa wanayo akili ya hali ya juu. {2Tsw 462.3}

Kutokana na kile Bwana amenionyeshea, wanawake wa namna hii wamepotosha mawazo yao kwa kusoma riwaya, kuota ndoto za mchana, na kujenga magorofa hewani, wakiishi katika ulimwengu wa kufikirika. Hawaleti akili zao wenyewe kwenye majukumu ya kawaida yaliyo muhimu kwa Maisha ya kila siku. Hawachukui mizigo ya maisha ambayo ipo katika njia yao na watafute kujenga nyumba yenye furaha na ucheshi kwa waume zao. Wanaweka uzito wao wote juu yao, bila kubeba mizigo yao wenyewe. Wanategemea wengine wajue matakwa yao na kuwafanyia, na wakati huo wako huru kukosoa na kuuliza maswali watakavyo. Wanawake hawa wana ugonjwa wa mapenzi mawazoni (lovesick), wakifikiria kila wakati kuwa hawapendwi, kwamba waume zao hawawapi umakini wote wanaostahili. Wanajifikiria wenyewe kama wafia dini. {2Tsw 463.1}

Ukweli wa mambo ni kwamba, ikiwa wangejionyesha kuwa na faida, thamani yao ingeweza kuongezeka; lakini wakati wanafuata njia ya kuvuta wengine kila mara wawaonee huruma na umakini, wakati wanahisi hawana jukumu kufanya hivyo kwa wengine, wanapitia maisha wakiwa wamejitenga, wenye ubaridi, na wasioweza kukaribiwa, wasiobeba mizigo ya wengine na wasiojua huzuni na shida za wengine. Kunaweza kuwa kidogo sana chenye thamani katika maisha yao. Wanawake hawa wamejelimisha kufikiria na kutenda kana kwamba ilikuwa kwao kujishusha kuolewa na wanaume walioolewa nao, na kwa hivyo mipangilio yao mizuri ya maisha haitathaminiwa kabisa. Wameona mambo yote kuwa makosa. Wanafikiri waume zao

hawawastahili. Daima wao huwachosha waume zao kwa utunzaji, uvumilivu, wakati ambapo wangeweza kuwa msaada, kunyanyua mizigo ya maisha pamoja nao, badala ya kuota ndoto hewani kuhusu maisha yasiyo halisi yanayopatikana kwenye vitabu vya mapenzi na mahaba ya mapenzi. Bwana na awahurumie wanaume ambao wamefungwa kwa wake wa namna hii ambao ni vyombo visivyo na faida (useless machines), wanaofaa kusubiriwa tu, kupumua, kula na kuvaa tu. {2Tsw 463.2}

Wanawake hawa wanaodhani wameumbwa kwa maumbile nyeti na ya pekee huwa wake na mama wasio na maana (useless mothers). Mara nyingi huwa wanaondoa mapenzi yao kutoka kwa waume zao, ambao ni watu muhimu na wenye manufaa, wenye utendaji wenye msaada, na huonyesha umakini kwa wanaume wengine, na kwa kupumbazwa na hisia za mapenzi hupenda kuvuta huruma za wengine, wakiwaambia majaribu yao, shida zao, matamanio yao ya ukuu, matarajio ya kufanya kazi zenye heshima, na kufunua Ukweli kwamba maisha yao ya ndoa ni ya kukatisha tamaa, na kikwazo kwao kufanya kazi waliyotarajia kuifanya. {2T 464.1} Ah, ni shida iliyoje katika familia ambazo zingeweza kuwa na furaha! Wanawake hawa ni laana kwao wenyewe na laana kwa waume zao. Kwa kudhani wao ni malaika, wanajifanya wapumbavu, na wao sio lolote isipokuwa mizigo mizito. Wajibu wa kawaida wa maisha ambao Bwana amewaachia wafanye, wanaubwaga hapo njiani mwao, na hawana utulivu na daima hulalalamika, kila wakati wanatafuta kazi rahisi, iliyoinuliwa zaidi, rahisi na inayokubalika zaidi. Wakidhani kuwa malaika, wanapatikana kuwa ni wanadamu tu baada ya yote. Wao ni wenye kujihuzunisha, kuudhika kirahisi, kujifadhaisha, wasioridhika, wanawaonea waume zao wivu kwa sababu sehemu kubwa ya muda wao hawaitumii kuwasubiri hawa wake. Wanalalamika kutelekezwa wakati waume zao wanafanya kazi ambayo wanapaswa kufanya. Shetani hupata ufikiaji rahisi wa kundi hili. Hawana upendo wa kweli kwa mtu yeyote ila kwao wenyewe. Walakini Shetani anawaambia kwamba kama mtu huyu au yule angalikuwa mume wao, wangepurahi kweli kweli. Wao wateja wa Shetani kirahisi sana, wakiongozwa kwa urahisi kuwakosea heshima waume zao wenyewe na kuvunja sheria ya Mungu. {2T 464.2}

Napenda kuwaambia wanawake wa aina hii: Unaweza kutengeneza au kuharibu furaha yako mwenyewe. Unaweza kufanya nafasi yako kuwa yenye furaha na uridhike au kutokuweza kuridhika. Njia ambayo unafuata itaumba furaha au shida kwako. Je! Hawa watu hawajawahi kufikiria kwamba waume zao wamewachoka kutokana na kutokuwa na faida kwao, mihemuko ya harara, kuudhika-udhika, kutafuta kwao makosa, vilio vyao vya hisia kali, wakifikiria kwamba kesi yao ni ya huzuni sana? Tabia yao ya kukasirika-kasirika, ya kipuuzi, kwa kweli inapunguza mapenzi ya waume zao na kuwafukuza kutafuta huruma, na amani, na faraja mahali pengine kuliko nyumbani. Mazingira yenye sumu yapo hapo wanapoishi, na nyumba yao kwao ina maana zote isipokuwa mahali pa mapumziko, amani, au furaha. Mume yuko chini ya majaribu ya Shetani, na mapenzi yake huwekwa kwenye yale yaliyokatazwa, na hushawishiwa kwa uhalifu na mwishowe atapotea. {2T 464.3}

Wanawake wana kazi kubwa ya utume, haswa wale ambao ni wake na mama. Wanaweza kuwa baraka kwa wote wanaowazunguka. Wanaweza kuwa na ushawishi wenye nguvu kwa mema ikiwa wataacha nuru yao iangaze ili wengine waongozwe kumtukuza Baba yetu wa mbinguni. Wanawake wanaweza kuwa na ushawishi wa kubadilisha ikiwa watakubali tu kutoa njia yao na mapenzi yao kwa Mungu, na wamuache Yeye kudhibiti akili zao, mapenzi, na maisha yao. Wanaweza kuwa na ushawishi ambao utaelekea kuboresha na kuwainua wale wanaoshirikiana nao. Lakini kundi hili kwa ujumla halijui nguvu waliyo nayo. Wanatoa ushawishi bila ufahamu wao ambao unaonekana kufanya kazi kiasilia kutoka kwa maisha yaliyotakaswa, moyo uliofanywa upya. Ni matunda ambayo hukua kwa asili juu ya mti mzuri wa upandaji wa Bwana. Ubinafsi umesahaulika, wameunganishwa na maisha ya Kristo. Kuwa tajiri wa matendo mema ni kawaida kwao kama kuvuta pumzi kwao. Wanaishi kuwatendea wengine mema na bado wako tayari kusema: Sisi ni watumishi wasio na faida. {2Tsw 465.1}

Mungu amempa mwanamke utume wake; na ikiwa yeye, kwa njia yake ya unyenyekevu, lakini kwa kadiri ya uwezo wake, hufanya nyumba yake kuwa mbingu, kwa uaminifu na kwa upendo akifanya majukumu



yake kwa mumewe na watoto, akitafuta kila wakati kuruhusu Nuru Takatifu iangaze kutoka kwa maisha yenye faida, usafi, na maadili ili kuangaza karibu naye, anafanya kazi aliyoachiwa na Mwalimu, na atasikia kutoka midomo Yake ya BWANA Maneno haya: “Vema, mtumishi mwema na mwaminifu. Njoo ufurahi pamoja na Bwana wako.” Wanawake hawa ambao wanafanya kwa utayari yale ambayo mikono yao hupata kufanya, kwa uchangamfu wa roho ya kuwasaidia waume zao kubeba mizigo yao, na kuwalea/kuwafundisha watoto wao kwa Mungu, ni wamishenari wa hali ya juu. Wanajishughulisha na idara muhimu ya kazi kubwa inayofanyika duniani kuandaa wanadamu kwa maisha ya juu mbinguni, na watapata thawabu yao. Watoto wanapaswa kufundishwa kwa ajili ya mbingu na kuwekwa kuangaza katika nyua za ufalme wa Bwana. Wazazi, haswa akina mama, wanapokuwa na maoni ya Kweli juu ya kazi muhimu wanayowajibika ambayo Mungu amewaachia wafanye, hawatajishughulisha sana na yale yanayowahusu majirani zao, ambayo hayawahusu. Hawatakwenda nyumba kwa nyumba kushiriki katika umbeya wa mitindo, wakiangalia makosa ya wengine, ubaya wao, na mapungufu ya majirani zao. Watahisi mzigo mkubwa ulio wajibu wao kwa watoto wao wenyewe, hivyo hawataweza kupata wakati wa kukosoa majirani zao. Wambeya na wasambazaji wa habari ni laana mbaya kwenye vitongoji na makanisa. Theluthi mbili ya shida zote za kanisa huibuka kutokana na chanzo hiki 2/3 . {2Tsw 465.2}

Mungu anahitaji wote kutenda kwa uaminifu majukumu ya leo. Hii imepuuzwa sana na sehemu kubwa ya watu wanaojiita Wakristo. Jukumu la leo limepotezwa haswa na kikundi hichi ambacho nimekitaja, ambao wanafikiria kuwa wao ni wa hali ya kiungwana ya juu zaidi kuliko viumbe vingine, kuliko wanadamu wenzao wanaowazunguka. Kwamba akili zao zinageukia kituo hiki cha mafikara, ni uthibitisho wa kweli kwamba wao ni duni, wanyonge, wenye kiburi, na wabinafsi. Wanajisikia wapo juu ya maskini wa hali ya chini na wanyenyekevu, wale ambao Yesu anasema amewaita. Daima Wanajaribu kutafuta nafasi ya kupigiwa makofi, kupongezwa na kupata sifa kwa kufanya kazi kubwa ambayo wengine hawawezi kufanya. Lakini inasumbua mioyo yao ya ndani wanayosema imetakaswa, kushirikiana na wanyenyekevu, na watu waliopata shida na majanga.

Wanakosea sababu halisi kabisa. Sababu ya wao kuachana na moja ya majukumu haya ambayo hayakubaliki sana inapatikana katika ubinafsi wao mkuu. Kujipenda wenyewe ndiyo kitovu cha vitendo na nia zao zote (dear self, me, myself and I). {2T 466.1}

Nilielekezwa kwa Mkuu wa mbinguni. Wakati YEYE ambaye malaika walimwabudu, Yeye ambaye alikuwa tajiri wa heshima, mwenye ukuu usio na kifani, na utukufu, alipokuja duniani, na akajikuta katika umbo kama mwanadamu, Yeye hakuomba asili Yake iliyosafishwa kama kisingizio cha kujiondoa mbali na wenye shida. Katika kazi Yake Alipatikana kati ya wanaoteseka, wenye shida, maskini, na wahitaji. Kristo alikuwa mfano wa uboreshaji na usafi; Maisha na tabia Yake yaliinuliwa; lakini katika kazi Yake hakupatikana kati ya watu wenye vyeo vya hali ya juu, wala kati ya watu wenye heshima zaidi wa ulimwengu huu, lakini pamoja na waliodharauliwa na wahitaji. Nilikuja, anasema Mwalimu wa mbinguni, "kuokoa kile kilichopotea." Ndio; Mkuu na Mtukufu wa mbinguni alipatikana akifanya kazi kuwasaidia wale ambao wanahitaji msaada zaidi. Naomba mfano wa Kristo uviaibishe visingizio vya kundi hilo ambalo limevutiwa sana na nafsi zao zilizo maskini, hivi kwamba wachukue ladha yao iliyosafishwa na wito wao wa juu kusaidia wasiojiweza. Hao wamechukua nafasi ya juu kuliko Bwana wao, na mwishowe watashangaa kujikuta wakiwa chini kuliko wale wa chini kabisa wa kundi ambalo tabia zao zilizosafishwa, wenye asili nyeti walishtuka kuchangamana nao na kuwafanyia kazi. Ni kweli, inaweza kuwa haikubaliki kila wakati kuungana na Mwalimu na kufanya Naye kazi katika kusaidia kundi linalohitaji msaada zaidi; lakini hii ndiyo kazi ambayo Kristo alijinyenyekeza kuifanya. Je! Mtumwa ni mkuu kuliko Bwana wake? Yeye Ametoa mfano, na anatuamrisha kuuiga. Inaweza kuwa haikubaliki kwetu, lakini jukumu linabidisha kwamba kazi kama hiyo ifanyike. {2T 467.1}

Wanaume waaminifu na waliochaguliwa wanahitajika kuwa vichwa vya kazi (kuongoza). Wale ambao hawana uzoefu wa kubeba mizigo, na ambao hawataki kuwa na uzoefu huo, hawapaswi, kwa sababu yoyote, kukaa hapo. Wanaume wanatafutwa ambao watakaolinda roho kama wale ambao wanapaswa kutoa hesabu. Baba na mama katika Israeli wanatafutwa katika Kituo hiki cha ulinzi muhimu. Hebu watu wenye

ubinafsi na wanaojijali, bahili, wenye tamaa, wapate mahali ambapo tabia zao mbaya hazitaonekana sana. Jinsi wanavyokuwa mbali watu hawa na wapweke, ndivyo inakuwa bora kwa kazi ya Mungu. Ninatoa wito kwa watu wa Mungu, popote wanapopatikana: Amka ushike jukumu lako. Zingatia kwamba hakika tunaishi kati ya hatari za siku za mwisho. {2T 467.2}

Natumahi kuwa kesi ya N. Fuller itawaamsha ninyi, baba na mama, kuona umuhimu wa kazi kamilifu majumbani mwenu, kati yenu na watoto wenu, ili kwamba hakuna hata mmoja wenu atakayedanganywa na Shetani, hata kuiona dhambi kama mtu huyu masikini, anayesikitikisha sana kwa kile alichofanya. Wale walioshiriki pamoja naye katika uhalifu wasingedanganywa na kuharibiwa ikiwa wangekuwa na hali ya juu ya utu wema na usafi, na kuthamini daima kuona hofu na uovu wa dhambi katika mwenendo wao. Wakati wanaishi chini ya utangazaji wa ujumbe mzito kabisa kuwahi kutolewa kwa wanadamu, wakiwasilisha sheria ya Mungu kama mtihani wa tabia na kama muhuri wa Mungu aliye hai, wanakiuka maagizo Yake matakatifu. Dhamiri za wale wanaofanya hivi zimechomwa na kuwa ngumu sana. Wamepinga ushawishi wa Roho wa Mungu mpaka wameweza kutumia Ukweli mtakatifu kama vazi kuficha kilema cha roho zao zilizoharibika na uovu. Mtu huyu amedanganywa sana na Shetani. Amekuwa akihudumia tamaa mbaya wakati akidai kuwa amejitolea kwa kazi ya Mungu, akihudumu katika vitu vitakatifu. Anajiona kuwa mzima wakati hakukuwa na utimilifu ndani yake. {2T 468.1}

Nimefikiria hili kwa uzito sana kwani nimeona ushawishi wenye nguvu wa tamaa za kinyama katika kudhibiti wanaume na wanawake wasio na akili na uwezo wa kawaida. Wangekuwa na uwezo wa kushiriki katika kazi nzuri, ya kutumia mvuto mkubwa, ikiwa hawangekuwa watumwa wa tamaa za mwili mbaya. Kuamini kwangu ubinadamu kumetetemeshwa sana. Nimeonyeshwa kuwa watu wa mwenendo mzuri, wasiochukua uhuru usiofaa na jinsia nyingine, walikuwa na hatia ya kufanya dhambi ya punyeto kila siku ya maisha yao. Hawajajizuia na dhambi hii mbaya hata wakati mikutano ya ibada imekuwa ikiendelea. Wamesikiliza mazungumzo mazito ya wakfu na yenye mvuto juu ya

hukumu hiyo, ambayo ilionekana kuwaleta mbele ya mahakama ya Mungu, ikiwasababisha kuogopa na kutetemeka; lakini haikupita hata saa moja kabla hawajashughulika na dhambi yao wanayoipenda, inayowavutia, wakichafua miili yao wenyewe. Walikuwa watumwa wa uhalifu huu mbaya sana hivi kwamba walionekana hawana nguvu ya kudhibiti tamaa zao. Tumejitahidi kusaidia wengine kwa dhati na bidii, tumewasihi, tumelia na kuwaombea; lakini tunajua kwamba hata kati ya bidii yetu yote na dhiki, nguvu ya tabia ya dhambi imepata ushindi, na dhambi hizi zimetendwa. {2T 468.2}

Kupitia mashambulio makali ya ugonjwa au kwa usadikisho wa nguvu za dhamiri za wengine waliokuwa na hatia kuamshwa na kuwachoma sana mpaka kusababisha kukiri mambo haya kwa aibu kubwa. Wengine wana hatia sawa. Wamefanya dhambi hii karibu maisha yao yote na, katika miili yao iliyo na kuugua na kumbukumbu zinazopoteza mambo, wanavuna matokeo ya tabia hii mbaya; lakini wana kiburi sana kukiri. Wao ni wasiri, na hawajaonyesha dhamiri zao kujutia kwa dhambi hii kubwa. Ujasiri wangu kuhusu uzoefu wao wa Kikristo ni mdogo sana. Wanaonekana kuwa hawajali ushawishi wa Roho wa Mungu. Vitu vitakatifu na vile vya kawaida ni sawa kwao. Mazoea ya kawaida ya uovu huu unaodhalilisha kwa kuchafua miili yao wenyewe haujasababisha machozi machungu na toba ya kutoka moyoni. Wanahisi kuwa dhambi yao ni dhidi yao peke yao. Hapa wanakosea. Je! Wana ugonjwa mwilini au akilini tu, wengine huhisi pia, wengine wanateseka pia. Mawazo yao yana makosa, kumbukumbu ni duni, hapa makosa hufanywa, na kuna upungufu kila mahali ambayo huathiri sana wale ambao wanaishi nao na wanaoshirikiana nao. Mabadiliko na majuto huhisiwa kwa sababu vitu hivi vinajulikana na wengine. {2T 469.1}

Nimezitaja kesi hizi kuonyesha nguvu ya uovu huu wa kuharibu roho na mwili. Akili nzima hutolewa kwa mapenzi ya chini. Kitivo cha maadili na kiakili kinachukuliwa na nguvu za chini. Mwili unapunguzwa nguvu, ubongo umedhoofika. Nyenzo zilizowekwa hapo kulisha mfumo zinaharibiwa. Kuna uvujaji mwingi kwenye mfumo wa ubongo. Mishipa mizuri ya ubongo, inaamshwa na kitendo kisicho cha asili, hufa ganzi na ugonjwa na kupooza (kujichua). Nguvu za kimaadili na kiakili

zinadhoofika, wakati hamu ya kinyama zinaimarika na kukua zaidi na mazoezi. Hamu ya chakula kisicho na afya inapiga yowe kwa tamaa. Wakati watu wamezoea tabia ya kujinyanyasa, haiwezekani kuamsha hisia zao za maadili kuthamini vitu vya milele au kufurahia mazoezi ya kiroho. Mawazo machafu hushika na kudhibiti mafikara na kufurahisha akili, na kinachofuatia ni hamu isiyoweza kudhibitiwa ya utendaji wa vitendo vichafu. Ikiwa akili ingeelimishwa kutafakari masomo ya kuinua, mawazo yafunzwe kutafakari juu ya vitu safi na vitakatifu, ingeimarishwa dhidi ya uovu huu mbaya unaoshusha roho na mwili. Kwa kufunzwa itazoea kukaa juu, kwenye vitu vya mbinguni, safi, na vitakatifu, na haitaweza kuvutiwa na msingi huu, wa ufisadi, na uovu mbaya. {2T 470.1}

Tunaweza kusema nini juu ya wale ambao wanaishi katika mwanga mkali wa Ukweli, lakini kila siku hufuata na kutenda dhambi na uhalifu? Starehe zilizopigwa marufuku, zenye kosisimua zina sumaku kwao na hushikilia na kudhibiti utu wao wote. Watu kama hao hupendezwa na udhalimu na uovu, na lazima waangamie nje ya mji wa Mungu, na kila kitu chenye kuchukiza. {2T 470.2}

Nimetafuta kuwaamsha wazazi kwa jukumu lao, lakini wanalala. Watoto wako wanafanya uovu wa punyeto, na wanakudanganya. Unawaamini kiasi kwamba unafikiria kuwa ni wazuri sana na wasio na hatia kuweza kufanya uovu kwa siri. Wazazi huwafurahisha, huwaendekeza na kuwabembebeza watoto wao, na kuwaingiza katika kiburi, lakini hawawazuii kwa uthabiti na maamuzi. Wanaogopa sana mapenzi na ukaidi wa Watoto wao, wenye makusudi kiasi kwamba wanaogopa kuzungumza nao uso kwa uso; dhambi ya uzembe, ambayo ilirekodiwa dhidi ya Eli, itakuwa dhambi yao. Ushauri wa Petro ni wa thamani ya juu zaidi kwa wote ambao wanajitahidi siku moja wapate tuzo ya kutokufa. Anawahutubia wale walio na imani sawa, Imani ile ya thamani: {2T 471.1}

"Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika hali ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo. Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. Kwa kuwa uweza Wake wa

Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake na wema Wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, ukarimu/upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiye kuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu, kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo. "{2T 471.2}

Tuko katika ulimwengu ambao nuru na maarifa vimejaa, lakini wengi wanaodai kuwa na imani sawa, Imani ile yenye thamani ambayo wengi wameamua kuwa wajinga kwa kudhamiria wasiijue. Nuru iko karibu nao, lakini hawajitwalii wenyewe. Wazazi hawaoni umuhimu wa kujielimisha wenyewe, kupata maarifa, na kuyaweka kwenye vitendo katika maisha yao ya ndoa. Ikiwa wangepuata himizo la mtume, na kuishi kwa mpango wa kujiongeza, hawangukuwa wasio na matunda katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Lakini wengi hawaelewi kazi ya utakaso. Wanafikiria wamefikia utimilifu wa maarifa, wakati wamejifunza masomo ya kwanza tu kwenye kuongeza. Utakaso ni kazi inayoendelea-yenye mwendelezo; haupatikani kwa saa moja au siku, na kisha kudumishwa bila juhudi yoyote maalum kwa upande wetu. {2T 472.1}

Wazazi wengi hawapati maarifa ambayo wanapaswa katika maisha ya ndoa. Hawajiwekei ulinzi ili Shetani asiwachukue na kudhibiti akili zao na maisha yao. Hawaoni kwamba Mungu anawataka kudhibiti maisha yao ya ndoa yasiwe ya kupitiliza, bali yawe na kiasi. Lakini ni wachache sana wanaoona kuwa ni wajibu wao wa kidini kutawala tamaa zao.

Wamejiunganisha katika ndoa na kile ambacho ni chaguo lao, na kwa hivyo wanafikiria kuwa ndoa hutakasa utoshelevu wa tamaa mbaya za chini. Hata wanaume na wanawake wanaodai utauwa huachia tamaa zao mbaya za kimwili, na hawafikirii kwamba wanawajibika kwa Mungu kwa matumizi ya nguvu zao muhimu, ambazo zinadhoofisha maisha yao na hupunguza nguvu ya mfumo mzima. {2T 472.2}

Agano la ndoa takatifu linafunika dhambi zenye giza jeusi sana. Wanaume na wanawake wanaodai utauwa huidhalilisha miili yao wenyewe kwa kuendekeza tamaa mbaya, na hivyo kujishusha chini ya tamaa mbaya zisizo za kibinadamu. Wanatumia vibaya nguvu ambazo Mungu amewapa kuhifadhiwa kwaajili ya utakaso na heshima. Afya na maisha hutolewa dhabihu juu ya madhabahu ya tamaa mbaya za mwili. Nguvu za juu na bora huletwa chini ya tabia za wanyama. Wale ambao hufanya hivyo hawajui matokeo ya mwenendo wao. Laiti wote wangeweza kuona kiwango cha mateso wanayojiletea wao wenyewe kwa anasa zao za dhambi, wangeshtuka, na wengine, angalau, wangeepuka mwendo wa dhambi ambao huleta ujira ulio wa kutisha. Wana maisha ya huzuni sana katika kundi hili kubwa na ingekuwa bora kwao kufa kuliko kuishi; na wengi hufa kabla ya muda wao, maisha yao yametolewa dhabihu katika kazi ya aibu ya kuendekeza sana tamaa za kinyama. Walakini kwa sababu wameoa wanafikiria hawatendi dhambi (kwa ngono inayopitiliza). {2T 472.3}

Wanaume na wanawake, siku moja mtajifunza tamaa ni nini na matokeo ya kuiendekeza kwake. Shauku za chini za tamaa za mwili kama hizo zinaweza kupatikana katika uhusiano wa ndani ya ndoa kama vile zinavyopatikana nje yake. Mtume Paulo anawahimiza waume kuwapenda wake zao "kama vile Kristo pia alilipenda kanisa, na akajitoa mwenyewe kwa ajili yake." "Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo Naye anavyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili Wake. "Sio upendo safi ule ambao humshawishi mwanamume kumfanya mkewe chombo cha kuhudumia tamaa yake. Ni tamaa za wanyama ambazo zinaashiria kwa mayowe na kelele ili ziendekezwe. Ni wanaume

wachache kiasi gani ambao wanaonyesha upendo wao kwa njia iliyoainishwa na mtume: "ili ajipatie kanisa linalong'aa, lisilo na doa wala kunjamano wala kitu kingine cho chote kama hicho; liwe takatifu na bila kasoro. ili [asilichafue, bali] alitakase na kulisafisha; liwe takatifu na bila mawaa." Hii ndio sifa ya upendo katika uhusiano wa ndoa ambao Mungu anautambua kuwa mtakatifu. Upendo ni kanuni safi na takatifu; lakini shauku ya matamania haitakubali kizuizi, na haitaamriwa au kudhibitiwa kwa busara. Ina upofu wa matokeo; haiongozwi na/au kutibithiwa na busara. Wanawake wengi wanasumbuliwa na shida kubwa za unyonge na ugonjwa uliomo ndani yao kwa sababu sheria za miili yao zimekuwa zikipuuzwa; sheria za asili zimekanyagwa. Nguvu ya ujasiri wa ubongo huharibiwa na wanaume na wanawake, ikiitwa katika hatua isiyo ya asili ili kuridhisha tamaa za kimwili ; na zimwi hili baya la tamaa, la shauku ya chini, huchukua jina maridadi na nyeti la mapenzi. {2T 473.1}

Watu wengi waliodai kuwa Wakristo waliopitishwa mbele yangu walionekana kukosa msaada wa maadili. Walikuwa wanyama zaidi ya wacha Mungu. Kwa kweli, walikuwa na silika ya unyama wote. Wanaume wa aina hii humdhalilisha mke ambaye wameahidi kumlisha na kumtunza. Wamefanywa kuwa chombo cha kuhudumia, kuridhisha tamaa ya chini, ya kujipendzesha. Na wanawake wengi hujisalimisha kuwa watumwa wa matamania yasiyo na kiasi; hawamiliki miili yao katika utakaso na heshima. Mke hahifadhi hadhi na heshima aliyokuwa nayo kabla ya ndoa. Taasisi hii takatifu ilipaswa kuhifadhi na kuongeza heshima yake ya kike na hadhi takatifu; lakini usafi wake wa kike, wenye heshima ya Bwana umetumalizwa juu ya madhabahu ya tamaa ya mwili ya hali ya chini; Umetolewa kafara ili kumpendeza mumewe. Haitachukua muda kupoteza heshima kwa mumewe, ambaye hajali sheria ambazo hata wanyama wa Mungu walioumbwa hutoa utii kwazo. Maisha ya ndoa huwa nira yenye uchungu; kwani upendo hufa, na mara nyingi kutokuaminiana, wivu, na chuki huchukua nafasi yake. {2T 474.1}

Hakuna mwanamume anayeweza kumpenda kweli mke wake wakati mke atanyenyekea kwa subira kuwa mtumwa wake, wa kuhudumia tamaa zake mbaya (za kupitiliza kwa ngono). Katika unyenyekevu



wake, mke hupoteza thamani aliyokuwa nayo machoni pa mumewe. Anamuona ameshuka chini, na si mtu wa kuheshimiwa, ni wa kiwango cha chini; na muda si mrefu atamshuku kuwa yeye atakubali kujishusha kirahisi kwa mwanamume mwingine kumfanyia kama yeye mwenyewe. Atashuku uthabiti wake na usafi, atamchoka, na kutafuta vitu vipya ili kuamsha na kuimarisha tamaa zake za kuzimu. Sheria ya Mungu haizingatiwi. Wanaume hawa ni wabaya kuliko wanyama; ni mashetani walio katika umbile la binadamu. Hawajui kanuni za kuinua, za kuvutia, za upendo wa kweli, uliotakaswa.{2T 474.2}

Mke pia humwonea wivu mume na anashuku kwamba ikiwa nafasi itatokea, atamwendea mwingine kirahisi na kufanya hivyo kwa mwingine kama alivyofanya kwake yeye. Anaona kwamba hadhibitwi na dhamiri au hofu ya Mungu; vizuizi hivi vyote vilivyotakaswa vimebomolewa na tamaa mbaya; Tabia ya mume ambayo inafananishwa na tabia ya Mungu hufanywa kuwa mtumwa wa tamaa ya chini, ya kinyama. {2T 475.1}

Ulimwengu umejaa wanaume na wanawake wa utaratibu huu; na nyumba nadhifu, zenye ladha nzuri, naam, wamo ndani ya nyumba za bei ghali ila zenye jehanamu ndani yake. Fikiria, ikiwa unaweza, watoto wa wazazi kama hao watakuwaje. Je! Watoto hawatazama chini kwenye mizani? Wazazi hutoa muhuri wa tabia kwa watoto wao. Kwa hivyo watoto ambao wamezaliwa na wazazi hawa hurithi kutoka kwao sifa za akili ambazo ni za tamaa za chini. Na Shetani hupalilia chochote kinachoelekea kwenye ufisadi na maangamizi. Jambo ambalo sasa linapaswa kuamuliwa ni: Je! Mke atajisikia amefungwa kabisa kushugulikia mahitaji ya mumewe, wakati anaona kuwa hakuna chochote kwa mumewe isipokuwa tamaa za chini zinazomdhibiti, na wakati busara yake inamsadikisha kuwa anachofanya kwa mumewe huumiza mwili wake, ambao Mungu ameamuru juu yake aumiliki katika utakaso na heshima, kuuhifadhi kama dhabihu iliyo hai kwa Mungu? {2T 475.2}

Sio mapenzi safi, na matakatifu ambayo husababisha mke kutosheleza tabia za kinyama za mumewe kwa gharama ya afya na maisha. Ikiwa ana upendo wa Kweli na hekima, atatafuta kugeuza akili yake

kuachana na kuridhisha matamano yake na kwenda kwenye mada za juu na za kiroho kwa kukaa juu ya masomo ya kiroho ya kupendeza. Inaweza kuwa muhimu kushawishi kwa unyenyekevu na kwa upendo, hata kwa hatari ya kukasirika kwake, kwamba asiweze kudhalilisha mwili wake kwa kujitolea kupita kiasi, kwa ngono. Anapaswa, kwa upole, upendo, na kwa fadhili, kumkumbusha kwamba Mungu Ndiye Mwenye madai ya kwanza na ya hali ya juu. juu ya mwili wake wote, na kwamba hawezi kupuuza madai haya, kwani atawajibika katika siku kuu ya Mungu. "Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu, na nyinyi si mali yenu? Kwa maana mmenunuliwa kwa bei ya thamani; kwa hivyo mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na kwa roho zenu, ambazo ni za Mungu. "Mlinunuliwa kwa gharama; msiwe watumwa wa wanadamu. "{2T 475.3}

Ikiwa atainua mapenzi yake, na katika utakaso na heshima ahifadhi utu wake uliosafishwa, wa kike, mwanamke anaweza kufanya mengi kwa ushawishi wake wa busara kumtakasa mumewe, na hivyo kutimiza utume wake wa hali ya juu. Kwa kufanya hivyo, anaweza kumwokoza mumewe na yeye mwenyewe, na hivyo kufanya kazi maradufu. Katika suala hili, nyeti na gumu sana kulisimamia, hekima nyingi na uvumilivu ni muhimu, pamoja na ujasiri wa maadili na ushujaa. Nguvu na neema zinaweza kupatikana katika maombi. Upendo wa dhati unapaswa kuwa kanuni inayotawala moyo. Upendo kwa Mungu na upendo kwa mume ndiyo tu msingi sahihi wa vitendo. {2T 476.1}

Endapo mke ataamua kuwa ni haki ya mume kuwa na udhibiti kamili wa mwili wake, na kuunda akili yake ili iendane na ya mume wake kwa kila jambo, kuenenda kwenye mkondo ule ule kama ya mume, basi yeye amesalimisha utu wake; utambulisho wake utapotea, utaunganishwa na ule wa mumewe. Yeye ni mashine tu kwa mapenzi yake, kuendeshwa na kudhibitiwa, kiumbe cha raha na anasa yake. Anafikiria kwa niaba yake, anaamua kwaajili yake, na anatenda kwa niaba yake. Yeye humvunjia Mungu heshima kwa kuchukua nafasi hii ya ukimya. Ana wajibu mbele ya Mungu ambao ni kuhifadhi jukumu lake. {2T 476.2}

Wakati mke anajitolea mwili na akili yake kwa udhibiti wa mumewe, akiwa kimya/passive katika mambo yote, akitoa kafara dhamiri yake, utu wake, na hata utambulisho wake, anapoteza nafasi ya kutumia ushawishi huo mkubwa kwa mema, ambao amepewa kuwa nayo ili amwinue mumewe. Angeweza kulainisha tabia yake ya ukali, na ushawishi wake utakasao ungeweza kutendwa kwa njia ya kusafisha na kutakasa, ukimwongoza mume kujitahidi kwa bidii kutawala tamaa zake na kuwa na nia ya mionjo ya kiroho zaidi, ili wote waweze kuwa washiriki pamoja wa tabia Mungu, kwa kuepukana na ufisadi ulioko ulimwenguni kupitia tamaa. Nguvu ya ushawishi inaweza kuwa nzuri kuongoza akili kwenye mada ya juu na yenye ubora na uungwana, kuliko ya kupenda mambo yaliyo ya chini, tamaa za ngono ambazo moyo usiofanywa upya kwa neema kawaida huzitafuta. Ikiwa mke anahisi kuwa ili kumpendeza mumewe lazima ashuke kwa kiwango chake, wakati shauku ya kinyama ni msingi mkuu wa upendo wake na hudhibiti matendo yake, humchukiza Mungu; kwani anashindwa kuwa na ushawishi wa kumtakasa mumewe. Ikiwa anahisi kuwa lazima atii tamaa zake za kinyamaa bila ya kuwa na neno la kupinga, haelewi wajibu wake kwake wala kwa Mungu wake. Ngono iliyopindukia itaangamiza kupenda mazoezi ya ibada/uchaji, itachukua kutoka kwa ubongo lishe inayohitajika kulisha mfumo, na itamaliza kabisa nguvu. Mwanamke yoyote hapaswi kumsaidia mumewe katika kazi hii ya kujiangamiza. Hatafanya hivi ikiwa amepewa nuru, na ana mapenzi ya kweli kwa mumewe. {2T 476.3}

Kadiri tamaa za kinyama zinavyoendekezwa, ndivyo zinavyozidi kuwa na nguvu, na vurugu zake zitakuwa na mayowe/kelele zaidi kuendekezwa. Hebu wanaume na wanawake wanaomcha Mungu waamke kwa wajibu wao. Wengi wanaojiita Wakristo wanakabiliwa na kupooza kwa neva na ubongo kwa sababu ya kutokuwa na msimamo wa kuikana nafsi, katika mwelekeo huu. Uozo upo katika mifupa na mafuta yake kwa watu wengi wanaochukuliwa kama watu wazuri, ambao husali na kulia, na ambao husimama katika ngazi za juu, lakini ambao mizoga yao michafu haitapita kamwe milango ya jiji la mbinguni. {2T 477.1}

Laiti ningewafanya wote waelewe wajibu wao kwa Mungu kuhifadhi viungo vyao vya kiakili na kimwili katika hali bora ya kumtolea Muumba wao huduma kamilifu! Hebu mke Mkristo ajizuie, kwa maneno na matendo, kutoka kwa kuamsha shauku za kinyama za mumewe. Wengi hawana nguvu kabisa ya kupoteza katika mwelekeo huu. Kuanzia ujana wao wamepunguza nguvu za ubongo na kuharibu mwili kwa kuridhisha tamaa za wanyama. Kujikana nafsi na kiasi lazima ziwe kauli mbiu na mwongozo katika maisha yao ya ndoa; ndipo watoto wanaozaliwa kwao, hawatadidimia sana kimaadili, kwa kuwa na viungo vya maadili na akili dhaifu, na nguvu za kinyama. Uovu wa punyeto upo kwa watoto karibu ulimwengu wote. Je! Nini sababu yake? Je, ni nani amewapa muhuri wa tabia? Bwana afungue macho ya wote kuona kwamba wamesimama katika sehemu zenye utelezi! {2T 477.2}

Kutoka kwa picha ambayo imewasilishwa mbele yangu juu ya ufiadini wa wanaume na wanawake wanaodai utauwa, nimeogopa kwamba itabidi nipoteze kabisa matumaini yangu kwa wanadamu. Nimeona kwamba usingizi wa kutisha uko karibu kwa kila mtu. Ni ngumu sana kuwaamsha wale ambao wanapaswa kuwa macho ili kuwa na hisia yoyote ya haki, ambayo Shetani ameshikilia akili. Hawajui ufiadini uliojaa kila mahali. Shetani amewapofusha akili zao na kuwalaza katika usalama wa tamaa za kimwili. Kushindwa kwa juhudi zetu za kuwaleta wengine waelewe hatari kubwa zinazozikumba roho wakati mwingine hunisababisha kuogopa kwamba maoni yangu ya upotovu wa moyo wa mwanadamu yametiwa chumvi. Lakini wakati Ukweli unaletwa kwetu kwa kuonyesha ulemavu wa kusikitisha wa yule aliyethubutu kuhudumu katika vitu vitakatifu huku akiwa na moyo mchafu, ambaye mikono yake imetia madoa ya dhambi na kuchafua vyombo vya Bwana, nina hakika kwamba sijaliweka hili jambo kwa kutia chumvi sana-sijachora picha kwa mkazo kuliko ilivyo. {2T 478.1}

Nimekuwa nikibeba shuhuda wyenye nguvu sana, kwa maandishi na kwa kuongea, nikitumaini kuwaamsha watu wa Mungu kuelewa kwamba wameangukia nyakati za hatari. Nimejisikia mgonjwa moyoni kwa kutokujali kunakoonyeshwa kwa wale ambao wanapaswa kuelewa utendaji wa Shetani, na ambao wanapaswa kuwa macho na kulindwa. Nimeona kwamba Shetani anaongoza akili za hata wale wanaokiri

Ukweli kujiingiza katika dhambi mbaya ya uasherati. Akili ya mwanamume au mwanamke haishuki chini kwa hatua moja tu yaani kutoka usafi na utakatifu hadi upotovu, ufisadi, na uhalifu. Inachukua muda kumbadilisha mtu mwenye tabia ya kawaida afikie kuwa na tabia ya Mungu, au kuwashusha wale waliokuwa na mfano wa Mungu katika tabia zao kuwa wanyama au shetani. Kwa kutazama tunabadilishwa. Japo ameumbwa kwa mfano wa Muumba Wake, mwanadamu anaweza kuelimisha akili yake kiasi kwamba dhambi ambayo hapo awali aliichukia itakuwa ya kupendeza kwake. Anapoacha kukaa macho katika kituo cha ulinzi na kuomba, huacha kulinda ngome, moyo, na kujiingiza katika dhambi na uhalifu. Akili inashushwa, na haiwezekani kuiinua kutoka kwenye ufisadi wakati inaelimishwa kutumikisha nguvu za kimaadili na kiakili, na kuzileta chini ya tamaa mbaya za mwili. Vita vya mara kwa mara dhidi ya nia ya mwili lazima idumishwe; na lazima tusaidiwe na ushawishi safi wa neema ya Mungu, ambao utavutia akili juu na kuizoesha kutafakari juu ya vitu safi na vitakatifu. {2T 478.2}

Matakwa ya mwili hayawekwi na wanaodai kutunza Sabato. Wengine wameipokea Sabato ambao akili zao zimewahi kuwa na ufisadi. Na walipokubali Ukweli hawakuhisi umuhimu wa kugeuka kabisa (nyuzi 180) kutoka njia za zamani na kubadilisha mwenendo wao wote. Wamekuwa kwa miaka kadhaa wakifuata mielekeo ya moyo ambayo haijapata kuzaliwa upya, na wamevutwa na tamaa mbaya za tabia zao za mwili, ambazo zilikuwa zimeharibu sura ya Mungu ndani yao na kuchafua kila kitu walichogusa; kwa hivyo maisha yao yote ya baadaye yatakuwa mafupi sana, ikiwa yatakuwa marefu, basi wapande ngazi ya Petro ya ukamilifu wa Kikristo, kwa matayarisho ya kuingia katika ufalme wa Mungu. Lakini wapo wachache ambao wanahisi kuwa hawawezi kuokolewa kwa kuikiri ile Kweli peke yake, isipokuwa watakaswe kupitia Kweli, kwa kujibu maombi ya Bwana wetu wa Yesu kwa Baba Yake: "Uwatakase kwa ile Kweli Yako. Neno Lako ndiyo Kweli." {2T 479.1}

Wanaume na wanawake wanaodai kuwa wanafunzi wa Kristo na kuzishika amri zote za Mungu watalazimika kuwa na roho ya kuugua katika maisha yao ya kila siku, kuugua kuingia katika mlango

mwembamba (Ezekieli 9). Wanaougua kwa maumivu ndio pekee watakaohamasisha kupita kwao kwenye lango jembamba na njia nyembamba ambayo inaingia kwenye uzima wa milele, kwenye utimilifu wa furaha tele na kwenye mema ya milele. Wale ambao hawana jitihada hawataweza kamwe kuingia. Maisha yote ya Wakristo wengi hayatatumika kwa juhudi kubwa zaidi kutafuta kuingia mle, na hivyo thawabu yao pekee itakuwa kugundua kwamba haiwezekani kwao kamwe kuingia katika lango hilo nyembamba. {2T 479.2}

Nimekuwa nikishangaa kuona ni familia ngapi zimepofushwa na Shetani, ili wasiwe na ufahamu wa utendaji kazi wake, hila na udanganyifu wake, unaofanywa katikati yao. Wazazi wanaonekana kubabaishwa, na kupumbazwa na ushawishi wa kupooza wa yule mwovu, na bado wanadhani wako sawa. Nimeonyeshwa kuwa Shetani anatafuta kudhalilisha akili za wale ambao wanaungana katika ndoa, ili aweze kupiga muhuri wa taswira yake ya chuki juu ya watoto wao. Kwa sababu wameingia kwenye uhusiano wa ndoa, wengi wanafikiria kwamba wanaweza kujiruhusu kudhibitiwa na tamaa za wanyama. Wanaongozwa na Shetani, ambaye huwadanganya na kuwaongoza kupotosha taasisi hii takatifu. Adui anafurahishwa na kiwango cha chini ambacho akili zao huchukua; kwani ana mengi ya kupata katika mwelekeo huu. Anajua kwamba ikiwa anaweza kulisimua tamaa za chini, na kuziweka katika hali ya kupendeza, hana chochote cha kusumbuka katika uzoefu wao wa Kikristo; kwa kuwa vitivo vya kimaadili na kiakili vitakuwa chini, wakati tabia za kinyama zitatawala na kushika nafasi ya juu; na tamaa hizi za chini zitaimarishwa na mazoezi, wakati sifa nzuri zaidi zitakuwa dhaifu na dhaifu zaidi. {2T 480.1}

Adui anaweza kuunda tabia/kizazi chao watoto kwa urahisi zaidi kuliko vile angeweza kwa wazazi, kwani anaweza kudhibiti akili za wazazi ili kupitia wao awape muhuri wa tabia yake kwa watoto wao. Kwa hivyo watoto wengi huzaliwa na tamaa za wanyama kwa kiwango kikubwa na zikiendelea kukuzwa, wakati nguvu za maadili mema zimekuzwa kidogo tu. Watoto hawa wanahitaji mafunzo ya umakini ili kuleta, kuimarisha, na kukuza nguvu za kimaadili na kiakili, hili hizi zipate kuongoza/kutawala. Lakini mipango ya Shetani haitambuliki; hila zake

hazieleweki. Watoto hawafundishwi kwaajili ya Mungu. Elimu yao ya maadili na dini imetelekezwa. Tamaa za kinyama zinaimarishwa kila wakati, wakati vitivo vya maadili vinadhoofishwa. {2T 480.2}

Watoto wengine huanza kujichua katika utoto wao; na kadri wanavyozidi kuongezeka miaka, hamu ya tamaa hukua nao na kupata nguvu wanapoimarika nguvu zao za mwili. Akili zao hazijatulia. Wasichana wanatamani kukaa pamoja na wavulana, na wavulana pia wanataka wakae kwenye vikundi vya wasichana. Mwenendo wao hauna soni na kiasi. Wana ujasiri na kimbelembele, na wanajichukulia uhuru usiofaa. Tabia ya kujichua imepunguza akili zao na kuchafua roho zao. Mawazo maovu, na usomaji wa riwaya, hadithi za mapenzi, na vitabu viovu husisimua mawazo yao, na hivi ndivyo hupelekana na mawazo hayo potovu. Hawapendi kazi, na wanapofanya kazi hulalamika juu ya uchovu; migongo yao inauma; vichwa vyao vinauma. Je! Hakuna sababu ya kutosha? Je! Wamechoka kwa sababu ya kazi yao? Hapana, hapana! Walakini wazazi huwadekeza watoto hawa wanapolalamika, na kuwaachilia wasifanye kazi au kuwajibika. Hili ndilo jambo baya sana ambalo wanaweza kuwafanyia. Kilichotokea ni kwamba wameondoa karibu kizuizi pekee ambacho kinamzuia Shetani kupata ufikiaji wa rahisi kwenye akili zao dhaifu. Kazi muhimu ingesaidia kwa njia fulani kuwa kinga kutoka kwa udhibiti wake Shetani ulioazimiwa. {2T 481.1}

Tuna ujuzi wa kiasi fulani, jinsi Shetani anavyofanya kazi na jinsi anavyofanikiwa katika hilo. Kutoka kwa kile ambacho nimeonyeshwa, amepumbaza akili za wazazi. Wao hawashuku kwa haraka kwamba watoto wao wenyewe wanaweza kuwa na makosa na wenye dhambi. Baadhi ya watoto hawa, hudai kuwa Wakristo, na wazazi hulala, hawaogopi hatari, wakati akili na miili ya watoto wao zinaharibiwa. Wazazi wengine hawajali hata kuweka watoto wao pamoja nao wanapokuwa katika nyumba ya Mungu. Wasichana wadogo huhudhuria mikutano na hukaa kwenye viti vyao, inaweza kuwana wazazi wao, lakini mara nyingi hukaa wenyewe nyuma ya kanisa. Wana tabia ya kutoa udhuru na kutoka nje ya kanisa. Wavulana wanaelewa hili, na kwenda nje kabla au baada ya wasichana, na kisha, wakati mkutano unafungwa, wanaongozana nao kwenda nyumbani. Wazazi

hawana busara katika hili, hawajui kinachoendelea. Tena, visingizio vinafanywa vya kutembea, na wavulana na wasichana hukusanyika katika uwanja wa maonyesho, au mahali pengine pa faragha, na hapo hucheza na kuwa na wakati wa hali ya juu, bila jicho la uzoefu juu yao kuwaonya. Wanaiga wanaume na wanawake ambao ni watu wazima. {2T 481.2}

Hizi ni zama za mambo yanayokwenda haraka. Wavulana na wasichana wadogo huanza kuangaliana kwa makini wakati ndiyo tu wapo umri wa chekechea, wakichukua mafunzo kuhusu heshima kwa kuonyesha mwenendo wao. Je! Ni nini athari ya mchanganyiko wa jinsia hizi mbili? Je! Inaongeza usafi kwa vijana ambao hukusanyika pamoja? Hapana! Kwa kweli inaongeza tamaa za kwanza za mwili; baada ya mikutano kama hiyo vijana hutiwa wazimu na Shetani na hujitolea kwa mazoea yao mabaya. {2T 482.1}

Wazazi wamelala, na hawajui kwamba Shetani ameweka bango lake la kuzimu ndani ya nyumba zao. Niliongozwa kuuliza, mambo yatakuwaje kwa vijana katika wakati huu wa uovu? Narudia, Wazazi wamelala. Watoto wanapendezwa na 'hisia za mapenzi' na Kweli haina nguvu ya kurekebisha makosa. Je! Ni nini kifanyike kuzuia wimbi la uovu? Wazazi wanaweza kufanya mengi ikiwa wataamua kufanya hivyo. Ikiwa msichana mchanga anayeingia tu katika ujana wake amevutiwa na kuhusiana karibu na mvulana wa rika lake, au zaidi, anapaswa kufundishwa, kumwonyesha hasira yule mvulana hivi kwamba hakuna maendeleo au utongozaji kama huo utakaorudiwa tena. Wakati wavulana au vijana wanamtafuta msichana mara kwa mara kuna kitu kibaya. Binti huyo anahitaji mama kumuonyesha nafasi anayopaswa kushika, kumzuia, na kumfundisha kile kinachompasa kufanya msichana wa umri wake. {2T 482.2}

Mafundisho ya imani mabaya ambayo yameshinda, yanasema kwamba, kama inavyoonekana kutoka kwa mtazamo wa kiafya, jinsia mbili lazima zichanganyike pamoja, imefanya kazi yake mbaya. Wakati wazazi na walezi wanajua asilimia kumi tu ya ujanja ambao Shetani anao, basi, yawezekanaje ushirika huu wa jinsia uweze kuwa hauna hatia? Kwa hali ilivyo, Shetani amefanikiwa zaidi katika juhudi zake za



kuziroga akili za vijana; na kujichanganya kwa wavulana na wasichana huongeza tu uovu mara ishirini x20. Hebu wavulana na wasichana waajiriwe katika kazi muhimu. Wakichoka, watakuwa na mwelekeo mdogo wa kuharibu miili yao wenyewe. Hakuna kitu cha kutumainiwa kwa upande wa vijana, isipokuwa kuna mabadiliko kamili katika akili za wale walio watu wazima kwao. Punyeto imepigwa muhuri juu ya huduma za wavulana na wasichana, na nini kinafanywa kurudisha nyuma maendeleo ya uovu huu? Wavulana na vijana wanaruhusiwa na kuhimizwa kuchukua uhuru kuwafuata mabinti au wanawake wanaowaita (wanaowatongoza wavulana). Acha Mungu awaamshe akina baba na mama wafanye kazi kwa bidii ili kubadilisha hali hii mbaya ya mambo, ndiyo maombi yangu. {2T 482.3}

Nimekuwa nikiangalia shuhuda zilizotolewa kwa watunza Sabato na nimeshangazwa na huruma za Mungu na utunzaji Wake kwa watu Wake kwa kuwapa maonyo mengi, akionyesha hatari zao, na kuwasilisha mbele yao nafasi ya juu, ambayo angewataka wachukue. Ikiwa wangejiweka katika upendo Wake na kujitenga na ulimwengu, Yeye angeleta baraka Zake maalum kukaa juu yao, na nuru Yake iwaangaze. Mvuto wao kwa mema unaweza kuhisiwa katika kila Idara ya kazi na katika kila sehemu ya uwanja wa injili. Lakini ikiwa watahindwa kufikia akili ya Mungu, ikiwa wataendelea kuwa na hisia kidogo juu ya tabia iliyoinuliwa ya kazi kama walivyokuwa nayo zamani, ushawishi wao na mfano wao utathibitisha laana mbaya. Watafanya mabaya/maumivu na mabaya tu. Damu ya roho za thamani zitapatikana kwenye mavazi yao. {2T 483.1}

Ushuhuda wa onyo umerudiwa. Nauliza: Ni nani ameyasikliza maonyo? Nani ambao wamekuwa na bidii katika kutubu dhambi zao na ibada ya sanamu, na wamekuwa wakikaza mwendo kwa bidii, kufikia mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu? Ni nani wameonyesha kazi ya ndani ya Mungu, inayoongoza kwa kujikana na kujitoa dhabihu kwa unyenyekevu? Ni nani ambao wameonywa na wakajitenga mbali na ulimwengu, kutoka kwa mapenzi na tamaa zake, hata wameonyesha kukua kila siku katika neema na katika kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo? Je! Tunapata nani kati ya wale wenye utendaji hai wa kazi, ambao wanahisi mzigo kwa kanisa? Je!

Tunaona wakina nani ambao Mungu anawatumia haswa, akifanya kazi nao na kupitia kwao kuinua kiwango, na kulileta kanisa juu kwa viwango, ili wamjaribu Bwana na kuona ikiwa hatawamwagia baraka? {2T 483.2}

Nimesubiri kwa tashwishwi, nikitumaini kwamba Mungu angeweke Roho Wake juu ya wengine na kuwatumia kama vifaa vya haki kuamsha na kuweka utaratibu kwa kanisa Lake. Karibu nimekata tamaa kama nilivyoona, mwaka baada ya mwaka, kumekuwa na kutoka nje ya njia ya unyenyekevu ambako Mungu amenionyesha lazima uwe tabia ya maisha ya wafuasi Wake. Kumekuwa na shauku ndogo na ndogo zaidi, kwa kujitolea, kufanya kazi ya Mungu. Ninauliza: Je! Wale ambao wanakiri imani yao kwa shuhuda wamejaribu kuishi kulingana na nuru iliyotolewa ndani yao? Je! Wamezingatia maonyo yaliyotolewa? Je! Wamezingatia maagizo waliyopokea? {2T 484.1}

Niliona kwamba mabadiliko makubwa lazima yafanyike katika mioyo na maisha ya wengi sana, kabla ya Mungu kufanya kazi ndani yao kwa nguvu Yake kwa wokovu wa wengine. Lazima wafanywe upya kwa sura/mfano wa Mungu, katika haki na utakatifu wa kweli. Ndipo upendo wa ulimwengu, kujipenda mwenyewe, na kila tamaa ya maisha iliyohesabiwa kujiinua itabadilishwa na neema ya Mungu na kuajiriwa katika kazi maalum ya kuokoa roho ambazo Kristo alikufa kuzikomboa. Unyenyekevu utachukua mahali pa kiburi, na majivuno na ubinafsi kwa nafasi ya unyenyekevu na upole. Kila nguvu ya moyo itadhibitiwa na upendo usio na ubinafsi kwa wanadamu wote. Shetani, niliona, ataamka kwa haraka watakapoanza kwa bidii kazi ya matengenezo ndani yao. Adui anajua kwamba watu hawa, ikiwa wamewekwa wakfu kwa Mungu, wangeweza kuthibitisha nguvu za ahadi Zake Mungu na kutambua nguvu inayofanya kazi nao, ambayo mpinzani hataweza kuipinga au kuikanyaga. Wangegundua maisha ya Mungu katika roho zao. {2T 484.2}

Familia moja haswa, imehitaji faida zote ambazo wangeweza kupata kutoka kwa matengenezo katika lishe, lakini hawa ndio wamerudi nyuma kabisa. Nyama na siagi zimetumiwa nao kwa uhuru kabisa, na viungo vibaya havijatupwa kabisa (pilipili, baking soda, siki nk Spices).

Familia hii ingeweza kupata faida kubwa kutoka kwa chakula chenye lishe, iliyosimamiwa vizuri. Kiongozi wa familia alihitaji chakula rahisi cha kawaida na chenye lishe. T Ni mtu wa kukaa kitini tu, na damu yake ililitembea kwa uvivu kupitia mfumo huo. Hakuweza, kama wengine, kupata faida ya mazoezi kwa afya yake; kwa hivyo chakula chake kinapaswa kuwa cha ubora na kiasi kinachofaa. Familia hii haikuwa na usimamizi mzuri kuhusu lishe; kumekuwa na kasoro. Inapaswa kuwa na wakati maalum kwa kila mlo, na chakula kinapaswa kutayarishwa kwa njia rahisi na bila mafuta mazito (grisi); lakini muda na maarifa yalipaswa kuchukuliwa kwenye matayarisho ya lishe, afya, na kufanya kivutie. Katika familia hii, na pia kwa wengine wengi, mlolongo maalum wa chakula umekuwa ukitengenezwa kwa wageni, sahani nyingi zimetayarishwa zenye lishe nyingi yaani vyakula vilivyo na mafuta na sukari nyingi, ili wale wanaoketi mezani wajaribiwe kula kupita kiasi. Halafu kwa wageni wasipokuwepo, kulikuwa mwikikio wenye athari kubwa katika kukosekana kwa maandalizi ya chakula kinacholetwa. Chakula hicho kilikuwa kidogo na kilikosa lishe. Waliona sio jambo la maana sana "kwa sisi wenyewe." Wenyeji. Chakula kililiwa mara kwa mara, na wakati wa kawaida wa mlo haukuzingatiwa. Kila mwanachama wa familia alijeruhiwa na usimamizi kama huo. Ni dhambi kwa dada yetu yeyote kufanya maandalizi mazuri kwa wageni, na kudhulumu familia zao kwa lishe ndogo ambayo itashindwa kutosheleza/kulisha mwili. {2T 485.1}

Ndugu aliyezungumzwa hapa alihisi upungufu katika mfumo wake; hakupata lishe ya kutosha, na alidhani kwamba nyama ingempa nguvu aliyohitaji. Angekuwa ametunzwa ipasavyo, meza yake ingetengwa kwa wakati unaofaa na chakula chenye lishe bora, mahitaji yote ya mwili yangepatikana vyema. Siagi na nyama huchochea mwili. Hivi vimejeruhi tumbo na kupotosha ladha. Mishipa nyeti ya ubongo imepumbazwa, na hamu ya wanyama imeimarishwa kwa gharama ya vitivo vya kimaadili na kiakili. Nguvu hizi za juu, ambazo zinapaswa kudhibiti mtu, zimekuwa zikidhoofika, hivi kwamba mambo ya milele hayajaweza kutambuliwa. Kupooza kumepunguza mionjo ya kiroho, ibada na uchaji. Shetani amefurahi kwa kushinda na ameona ni jinsi gani anaweza kuingia kwa urahisi kupitia hamu ya chakula na kudhibiti

akili za wanaume na wanawake, ambazo Mungu Muunba ameziratibu/amezihesabia kufanya kazi nzuri na kubwa. {2T 485.2}

Kesi iliyotajwa hapo juu sio ya pekee; kama ingekuwa, nisingeileta hapa. Wakati Shetani anamiliki akili, inachukua muda mfupi sana na nuru na maagizo ambayo Bwana ametoa kwa neema, hupotea na hayana nguvu! Ni visingizio vingapi vinaundwa na hubuni mahitaji ambayo hayapo, ili mradi, vibebe mwenendo wao wa makosa katika kuweka kando taa na kuikanyaga chini ya miguu yao! Ninasema kwa uhakika. Pingamizi kubwa kwa matengenezo ya afya ni kwamba watu hawa hawaishi huu ujumbe; na bado watasema vibaya kwamba hawawezi kuishi haya matengenezo ya afya na kutunza nguvu zao. {2T 486.1}

Kila tunapoenda tunapata hali kama hiyo ya watu wanaotoa udhuru mzuri “kwa nini hawawezi kuishi nje ya matengenezo ya kiafya”. Hawajaishi ujumbe huu, na hawaujaufuata kwa umakini, kwa hivyo hawawezi kufaidika nao. Wengine huanguka katika kosa kwasababu huacha nyama na wanaona hawana haja ya kutumia matunda na mboga bora mahali pake, yaliyoandiliwa katika hali yao ya asili, bila mafuta na viungo. Ikiwa wangukuwa na ustadi wa kupanga vile ambavyo Muumba amewazunguka navyo, wazazi na watoto wenye dhamiri safi wakishirikiana kwa pamoja katika kazi hiyo, wangepurahia chakula rahisi, na kisha wataweza kuzungumzia kwa uelewa juu ya matengenezo ya afya. Wale ambao hawajabadilishwa na matengenezo ya afya, na hawajawahi kuyapokea kabisa, sio mahakimu wazuri wa faida zake. Wale ambao huchepuka mara kwa mara ili kuridhisha hamu zao za chakula kwa kula bata mzinga aliye na mafuta mengi na nyama zingine, hupotosha hamu zao, na hawa hawapaswi kuwa mashahidi wa faida za mfumo wa matengenezo ya afya kwani Wanatawaliwa na ladha ya chakula, na sio kanuni. {2T 486.2}

Nina meza iliyoandaliwa vizuri wakati wote. Sifanyi mabadiliko yoyote wageni wakitokea, wawe waumini au wasioamini. Ninakusudia kutoshangazwa, kwa kutokuwa tayari kukaribisha mgeni mmoja au 12 kwenye meza yangu, wale wote watakaokuja kunitembelea, wanaweza kupata nafasi ya kuhudumiwa. Nina chakula rahisi cha kutosha, chenye

afya na cha kukidhi njaa na kulisha mfumo. Ikiwa wapo wanaotaka zaidi ya hivi navyowapa, wako huru kutafuta mahali pengine. Hakuna siagi au nyama ya aina yoyote inayokuja kwenye meza yangu. Keki huonekana hapo kwa nadra sana. Kwa ujumla nina matunda mengi, mkate mzuri, na mboga. Meza yetu daima ina wema na msaada kwa watu, na wote wanaokula chakula huboreshwa na afya yao inakusaidiwa. Wote huketi bila hamu hasi ya chakula, na hula na kufurahia ukarimu na fadhila zinazotolewa na Muumba wetu. {2T 487.1}

Kutojali kwa ajabu kumedhihirishwa juu ya somo hili muhimu na wale walio watenda kazi. Ukosefu wa utulivu wa kuzingatia kanuni za matengenezo ya afya ni kiashiria halisi cha tabia na nguvu zao za kiroho. Wana upungufu katika uzoefu wao wa Kikristo. Dhamiri haizingatiwi. Msingi au sababu ya kila tendo sahihi lililopo na linalofanya kazi katika moyo huboreshwa hupata utii bila kuathiriwa na mambo ya nje au yale ya ubinafsi. Roho ya kweli na dhamiri njema zinatoshia kuhamasisha na kudhibiti nia na mwenendo wa wale wanaojifunza juu ya Kristo na wanaofanana naye. Wale ambao hawana nguvu ya kanuni ya kidini ndani yao huyumbishwa kwa urahisi, na mifano ya wengine, katika mwelekeo mbaya. Wale ambao hawajawahi kujifunza wajibu wao kutoka kwa Mungu, na kujifahamisha na makusudi Yake juu yao, hawaaminiki wakati wa vita kali na nguvu za giza. Wanapindishwa na muonekano wa nje wa mambo na mwonekano wa sasa hivi. Wanaume wa kidunia wanatawaliwa na kanuni za kidunia; hawaoni baraka ya kengine. Lakini Wakristo hawapaswi kutawaliwa na kanuni hizi. Hawapaswi kutafuta kujiimarisha katika utekelezaji wa wajibu kwa sababu nyingine yoyote isipokuwa upendo wa kutii kila sharti la Mungu linalopatikana katika Neno Lake na kuamriwa na dhamiri iliyoangaziwa. {2T 487.2}

Katika moyo uliofanywa upya kutakuwa na kanuni iliyowekwa ya kutii mapenzi ya Mungu, kwa sababu kuna upendo kwa yaliyo ya haki, mema, na matakatifu. Hakutakuwa na kusita, kushauriana na ladha, au kusoma kwa sababu zisizo njema kama vile kupunguza upungufu au maisha rahisi, au kuchukua mwelekeo fulani eti kwa sababu wengine hufanya hivyo. Kila mtu anapaswa kufanya maamuzi ya kuishi kwaajili yake mwenyewe. Akili za wote ambao hufanywa upya kwa neema

zitakuwa njia wazi, daima zikipokea nuru, neema, na Ukweli kutoka juu, na kupeleka kwa wengine haya. Kazi zao zina matunda. Matunda yao ni kwa utakatifu, na mwisho uzima wa milele. {2T 488.1}

Lakini ni wachache sana walio na maarifa yenye vitendo ya utakaso wa Kweli wanayodai. Utiifu wao na uchaji haujapatana na nuru waliyopendelewa. Hawana hisia halisi ya wajibu ulio juu yao kutembea kama wana wa nuru, na wala si kama wana wa giza. Ikiwa nuru ambayo wamepewa hao wangukuwa wamepewa Sodoma na Gomora, wangetubu kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu, na wangepanya hivyo ili kuepuka ishara ya ghadhabu ya Mungu. Itakuwa rahisi zaidi kwa Sodoma na Gomora kuikabili siku ya hukumu kuliko wale waliokuwa wamebahatika kupata nuru iliyo wazi, na wamefanyiwa kazi nyingi sana. lakini hawakufaidika kwayo. Wamepuuzia wokovu mkuu ambao Mwenyezi Mungu kwa rehema alikuwa tayari kuutoa. Walipofushwa sana na Shetani kiasi kwamba wakajifikiria kuwa wao ni matajiri na wana upendeleo wa Mungu tele, wakati Shahidi wa Kweli anawatangazia kuwa wao ni wanyonge, maskini, na vipofu, na uchi. {2T 488.2}

## **SURA YA 60**

### **MSALABA KATIKA KUIKUBALI KWELI**

Mpendwa Dada U: Kwa kiasi Fulani nimejua upekee wa shauku/hulka yako, tahadhari yako, hofu yako, ukosefu wako wa matumaini na ujasiri. Ninakuhurumia katika mateso yako ya akili, kwani hauwezi kuona kila

kitu wazi wazi kwa kuzingatia msimamo wetu na imani kama unavyoweza kutamani. Tunakujua wewe dhamira yako ni makini sana, na bila shaka kwamba, ungeweza kupata fursa ya kusikia juu ya hoja zote za Ukweli wa sasa, na kupima ushahidi wewe mwenyewe, basi ungesimikwa, ungeimarishwa, ungetulia katika hiyo kweli, ili kwamba upinzani au malaumu yasingekusogeza kutoka katika msingi wa uhakika. Kwa kuwa haujapata fursa kama wengine wengi kuhudhuria mikutano na kujionea mwenyewe ushahidi unaoambatana na uwasilishaji wa Ukweli tunaoushikilia kuwa mtakatifu, tunahisi kuwa na ushawishi zaidi kwako. Mioyo yetu inavutwa kwa ajili yako, na upendo wetu kwako ni wa dhati na wa uhakika. Tunahofu kwamba kati ya hatari za siku hizi za mwisho unaweza kuvunjikiwa na imani. Usihuzunishwe na mimi kwa kuandika hivi. Hauwezi kuwa na ufahamu kamili, kama nilio nao, wa hila na udanganyifu wa Shetani. Udanganyifu wake ni mwingi; mitego yake ni makini na kwa ujanja, amejiaandaa kuwateka waliojiziuka na wasiomshuku. Tunataka wewe uukwepe ujanja wake; tunataka uwe upande wa Bwana kikamilifu, ukimpenda, na kumngojea na kutamani sana kutokezea Kwake Mwokozi wetu katika mawingu ya mbinguni. {2T 489.1}

Tangu juhudi zako za mwanzo za kuitunza Sabato, mambo mengi yameibuka kukukatisha tamaa; lakini tunatumaini kwamba vitu hivi havitahamisha mawazo yako kutoka katika Kweli muhimu katika siku hizi za mwisho. Ingawaje watetezi wa Ukweli sio wote ambao hufanya kama inavyostahili, kwa sababu hawajatakaswa na Ukweli wanaoukiri, Ukweli ni ule ule; mng'ao wake haujapunguzwa. Ingawa hawa wanaweza kusimama kati ya Ukweli na wale ambao hawajapata kuushikilia kabisa, na kivuli cha giza lao kinaweza kuonekana kwa muda kama kinaufunika mng'ao wake mkali, lakini hakika haiwezekani; Ukweli wenye asili ya mbinguni hauwezi kuhafifishwa. Usafi wake na tabia iliyoinuliwa havibadiliki. Unaishi; kwa kuwa ni wa milele. {2T 489.2}

Dada yangu mpendwa, shikamana na Ukweli. Jipatie uzoefu wako mwenyewe. Una upekee wako binafsi. Wewe unawajibika tu kwa njia ambayo, bila utegemezi wa wengine wote, utatumia nuru inayoangaza juu ya njia yako. Ukosefu wa kujiweka wakfu kwa wengine hautakuwa kisingizio kwako. Ukweli kwamba wanapotosha Ukweli kwa njia yao ya

matendo mabaya, kwa sababu hawajatakaswa nayo, hautakupunguzia wewe uwajibikaji hata kidogo. Wajibu mzito uko juu yako kuinua kiwango cha Ukweli, kuubeba juu sana. Hata kama yule mbeba-viwango atazimia na kuanguka, usiache kiwango cha thamani kuburuzika mavumbini. Kichukue na kukibeba juu, hata kwa kuhatarisha jina lako zuri, heshima yako ulimwenguni, na maisha yako, ikiwa inahitajika. Dada yangu wa kuheshimiwa sana, ninakusihi utazame juu. Shikamana sana na mkono wa Baba yako wa mbinguni. Yesu, Wakili wetu, Yeye anaishi kutuombea. Yeyote yule akikana imani kwa maisha yake machafu, hawezi kuubadilisha Ukweli kuwa uongo. “Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri huu, Bwana awajua walio Wake.” “Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni.” Wakati mwingine ninaogopa hiyo miguu yako itateleza, kwamba utakataa kutembea katika njia ya unyenyekevu, iliyonyooka na nyembamba ambayo inaongoza katika uzima wa milele katika ufalme wa utukufu. {2T 490.1}

Ninawasilisha mbele yako maisha ya kujikana nafsi, unyenyekevu, na kujitolea kwa Bwana wetu wa mbinguni. Mungu wa mbinguni, Mfalme wa utukufu, aliacha utajiri Wake, fahari Yake, heshima Yake na utukufu, na, ili kumuokoa mwanadamu mwenye dhambi, alijishusha katika maisha ya unyenyekevu, umaskini, na aibu; “ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba, akidharau aibu.” Loo, kwa nini tunakereka sana na kushtuka kwa majaribio na shutuma, na aibu na kuteseka, wakati Bwana wetu ametupatia mfano kama huo? Nani wangependa kuingia kwenye furaha ya Bwana wao wakati hawakuwa tayari kushiriki mateso Yake? Ni Nani! Mtumishi asiye tayari kubeba unyenyekevu na aibu na lawama ambazo Mwalimu alizibeba bila ubinafsi kwa ajili yake! Mtumishi anayekwepa maisha ya unyenyekevu na kujitolea ambayo ni kwa ajili ya furaha yake ya milele, ambayo anaweza hatimaye kuipata thawabu kubwa sana, ya milele! Lugha ya moyo wangu ni: Wacha mimi nishiriki na Kristo kwa mateso Yake, ili hatimaye nishiriki pamoja Naye utukufu. {2T 490.2}

Ukweli wa Mungu haujawahi kupendwa na kuwa maarufu ulimwenguni. Moyo wa asili huwa unachukia Ukweli. Ninamshukuru Mungu kwamba lazima tuachane na upendo wa ulimwengu, na kiburi cha moyo, na kila



kitu ambacho huelekea kuabudu sanamu, ili kuwa Wafuasi wa Mtu wa Kalvari. Wale wanaoutii Ukweli, kamwe hawataweza kupendwa na kuheshimiwa na ulimwengu. Kutoka katika midomo ya Mwalimu wa mbinguni, alipokuwa akitembea kwa unyenyekevu kati ya wana wa wanadamu, yalisikika Maneno haya: Yeyote anayetaka kuwa mwanafunzi Wangu, na auchukue msalaba wake, na kisha anifuate. Ndio, fuata Mfano wetu. Je! Yeye Alikuwa akitafuta sifa na heshima ya wanadamu? La, hapana! Haya sasa Je, sisi tutafute heshima au sifa kutoka kwa walimwengu? {2T 491.1}

Wale ambao hawana upendo kwa Mungu hawatawapenda watoto wa Mungu. Sikiza Maneno ya maelekezo ya mbinguni: “Ole wenu ninyi watu watakapowasifu.” “Heri ninyi watu watakapowachukia, na kuwatenga, na kuwashutumu, na kulitupa nje jina lenu kama neno ovu, kwa ajili ya Mwana wa Adamu. Furahini siku ile, na kurukaruka, kwa kuwa, tazama, thawabu yenu ni kubwa mbinguni.” “Lakini ole wenu ninyi mlio na mali! Kwa kuwa faraja yenu mmekwisha kuipata.” Katika injili ya Yohana tena tunapata Maneno ya Kristo: “Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana. Iwapo ulimwengu unawachukia, mwajua ya kuwa umenichukia Mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali Mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile Neno nililowaambia, Mtumwa sio mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi Mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika Neno Langu watalishika na lenu.” “Mimi nimewapa Neno Lako; na ulimwengu umewachukia, kwa kuwa wao si wa ulimwengu. Kama Nami nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu. Wao sio wa ulimwengu, kama Mimi nisivyo wa ulimwengu.” {2T 491.2}

Katika Yohana wa Kwanza tunasoma: “Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo duniani.” Katika Waraka wa Paulo kwa Warumi anawasihi, kwa rehema Zake Mungu, kwamba waitoe miili yao iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yao yenye maana. “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya

kumpendeza, na ukamilifu.” Na Yakobo anatangaza: “Hamjui ya kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.” {2T 492.1}

Ninakuomba utafakari kwa uangalifu maagizo katika Waraka wa Paulo kwa Wagalatia: “Maana, sasa Je! Ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.” Ninaogopa kuwa uko katika hatari kubwa ya kuharibikiwa na imani. Unafikiria kwamba inabidi ujitoe mhanga kwa mambo fulani haswa ili uweze kuitii Kweli. Tunaamini kwamba umejitoa mhanga kiasi fulani, lakini ungekuwa umejitolea kikamilifu zaidi katika kufanya kazi hii kikamilifu, miguu yako sasa isingekuwa inajikwaa, imani yako ikiyumba. Simaanishi sasa kuhusu kutoa mali zako, lakini kwa kile kinachokaribia zaidi ya hiki, kwa kile ambacho kitasababisha mzozo unaoumiza kuliko kutoa vitu vyako, yale yanayokugusa haswa kibinafsi. Hujasalimisha kiburi chako, upendo wako wa kutaka kukubaliwa na ulimwengu usioamini. Unapenda watu wazungumze mazuri juu yako. {2T 492.2}

Haujapokea na kuutekeleza Ukweli kwa unyenyekevu wake. Naogopa, kusema kuwa, umekuwa ukihisi kama vile ulikuwa unajishusha chini kwa kukubali kupokea Ukweli usiopendwa kama ulivyotetewa na watunza Sabato wa Kiadventista. Umetafuta, kwa kiwango kikubwa, kudumisha roho ya ulimwengu na bado upokee Ukweli. Hii haiwezekani. Kristo hatakubali chochote isipokuwa moyo wote, mapenzi yote. Kuwa na urafiki na dunia ni uadui kwa Mungu. Unapotamani kuishi ili kuepukana na fedheha, unatafuta nafasi ya juu kuliko Bwana wako Anayeteseka; na wakati unashiriki katika hili, unatengana na Baba yako aliye mbinguni, ukibadili upendo Wake kwa yale ambayo haifai kuyapata. {2T 493.1}

Nimehisi kushinikizwa rohoni juu yako dada yangu, na pia kwa mume wako. Nilivyochukua kalamu yangu kuandika, kesi zako zimeletwa wazi mbele yangu. Ninajua kabisa hatari zako, za hali ya kufadhaika na mashaka yenu. Kila kitu kimekuwa kibaya kwako, Dada U, tangu ulipotafuta kuitii sheria ya Mungu. Lakini hakuna kitu kimekuwa kikwazo kikubwa kwenu ninyi nyote kama kiburi chenu. Ninyi wawili

wote mnapenda kujionyesha; hii haina sehemu katika dini nzuri, yenye unyenyekevu. Niliona kwamba ninyi nyote wawili mlikuwa mkipambana na maumivu makali, mtajaribiwa na kuthibitishwa. Katika pambano hili, Shetani angejitahidi sana kupofusha macho yenu yasione mambo yenu ya milele, na angewasilisha faida za wakati huu wa sasa, maisha haya mafupi ya kitambo ambayo hayaaminiki. Mngeona vitu vya kuvutia vya maisha haya, na isipokuwa mmeachana na kupenda kwenu kujionesha na kupenda ulimwengu hamngeweza kudumisha upendo wa Mungu. Yesu aliwasilishwa kwangu, akionesha uzuri na vivutio vya mbinguni, akitafuta kuvutia macho yako kutoka ulimwenguni, na akasema: “Je! mtachagua kipi, Mimi, au ulimwengu? Hawawezi kuwa na Mimi na kuwa na upendo kwa ulimwengu, pia. Je! Utamtoa dhabihu Yule aliyekufia kwa ajili ya kiburi cha uzima, kwa hazina za ulimwengu? Chagueni kati Yangu Mimi na ulimwengu; ulimwengu hauna nafasi Kwangu.” {2T 493.2}

Niliona miguu yako ikiyumba-yumba, imani yako ikitetereka. Shaka na kutokuamini vilikuwa vimekuzingira, na nuru ya Yesu ilikuwa ikiondoka. Ubatili ni mojawapo ya kanuni zenye nguvu za asili zetu zilizopotoka, na Shetani ataivutia kila wakati kwa mafanikio. Watu wamekuwa wakitafutwa ambao walikuwa tayari kumsaidia Shetani kazi yake—kukurubuni na kukudanganya, kuwasilisha uwezo wako na mvuto ambao unaweza kuwa nao katika jamii, wakikuhimiza kuwa utakuwa wa kuhurumiwa sana endapo utaunganisha mapenzi yako na watu wa imani nyenyekevu na kuchanganyika katika daraja la wanajamii hao, kama wanavyolichukulia kuwa, wako chini yako kitabaka. Imekana kwako kuwa ulikuwa ukijitahidi sana kujitolea kwa ajili ya Ukweli. Ni kweli kwamba watu wengi walio na ushawishi hawachagui kutoa kafara tamaa zao za kidunia, kutenganisha mapenzi yao kutoka kwa ulimwengu, na kugeuza nyayo zao katika njia nyembamba, njia ya unyenyekevu iliyopitiwa na Mtu wa mateso wa Kalvari. Wanazichukulia talanta na mvuto wao kuwa za thamani sana kutoweza kutumiwa kwa kazi ya Mungu, za thamani sana kutoweza kurudishwa kumtukuza Mpaji aliyewakopesha talanta hizi ili kuweza kuboreshwa na kurudishwa Kwake zote, rasilimali na faida iliyopatikana. Kwa faida za muda mfupi wanazotarajia kuzipata watatoa mhanga umilele. Kwa kusifiwa kwa kutia chumvi kwa

wanadamu, watageuka kutoka katika ukubali wa Bwana, Muumba wa mbingu na nchi, na watapoteza haki zote za heshima itokayo juu. Ni wachache sana wanajua kipi ni kwa faida yao! Hamthamini hili. Yesu, kupitia maisha ya mateso yasiyo na mfano na kifo cha aibu, amefungua njia ambayo mwanadamu anaweza kufuata nyayo Zake, na mwishowe Atukuzwe katika kiti Chake cha enzi, na apokee thawabu ya kutokufa na uzima wa milele. Kwa maisha ya utii, atapokea urithi wa milele, hazina isiyo najisi, isiyochuja au kutokomea. {2T 494.1}

Katika Waraka wa Kwanza wa Paulo kwa Wakorintho tunasoma: “Kwa sababu Neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa.” “Maana ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, na vitu ambavyo haviko, avibatilishe vile vilivyoko; ili mwenye mwili awaye yote asiye akajisifu mbele za Mungu.” Unao Mfano wa Kristo, maisha Yake asiyejifanya, asiyejidai, bila kujionesha au kujikweza. Je! mtumwa yuko juu ya Bwana wake? {2T 495.1}

Mpendwa dada, una akili nzuri na unaweza kufanya vizuri. Unaweza kuwa kama nanga kwa mumeo na nguvu kwa wengine wengi. Lakini ikiwa unasimama ukisitasita kati ya mawazo mawili, ukiwa haujapatanishwa katika kazi ya Mungu ya unyenyekevu, mvuto wako katika mwunganiko na mume wako utatekelezwa kwa njia isiyofaa. Je! Neno la Mungu linasemaje? Geuka kutoka katika maoni ya watu kwenda katika Sheria na Ushuhuda. Zima kila fikra za ulimwengu. Fanya uamuzi wako kwa ajili ya umilele. Pima ushahidi katika wakati huu muhimu. Hakika hatupaswi kutarajia kuyakwepa majaribu na mateso katika kumfuata Mwokozi wetu; kwa kuwa huu ndio mshahara wa wale wanao--Mfuata. Anatangaza wazi kwamba tutapata mateso. Mapenzi yetu ya kidunia lazima yatiishwe kwa yale ya milele. Sikiliza maneno ya Kristo: “Petro akaanza kumwambia, Tazama, sisi tumeacha

vyote tukakufuata Wewe. Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili Yangu na kwa ajili ya injili, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele.” Faida za milele zinahusika hapa. {2T 495.2}

Msijidanganye kwamba kama mkiuacha Ukweli vizuizi vyote katika kupata mali vitaondolewa. Shetani anakwambia hivi; huo ni udanganyifu wake. Ikiwa baraka ya Mungu inakaa juu yako kwa sababu unakabidhi vyote Kwake, utafanikiwa. Ukimwacha Mungu, Naye atakuacha. Mkono Wake unaweza kutawanya haraka kuliko unavyoweza kukusanya. “Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake?” {2T 496.1}

Wewe, dada yangu mpendwa, unahitaji uongofu kamili katika Ukweli, ambao utaua nafsi. Je! Huwezi kumwamini Mungu? Tafadhali soma Mathayo 10: 25-40. Tafadhali soma pia, kwa moyo wa kuomba, Mathayo 6: 24-34. Hebu Maneno haya na yauguse moyo wako: “Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha, Je! Sio zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Maisha bora hapa yanawasilishwa na. Kwa mwili inamaanisha mapambo ya ndani, ambayo hufanya wanadamu wadhambi, wenye upole na haki ya Kristo, wenye thamani machoni Pake, kama vile Henoko, na inawapa haki ya kupokea mguso wa mwisho wa kutokufa. Mwokozi wetu anatuelekeza kwa ndege wa angani, ambao hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi katika ghala, lakini Baba yao wa mbinguni huwalisha. Kisha Yeye Anasema: “Ninyi Je! Si bora kupita hao?..... Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti; Nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo.” Mayungiyungi haya (maua mazuri yaotayo kwenye maji), kwa utulivu na kutokuwa na hatia, hugusa akili ya Mungu vyema kuliko Sulemani katika mapambo yake ya gharama kubwa, lakini alikuwa na umaskini wa mapambo ya mbinguni. “Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo

leo, na kesho hutupwa kalibuni, Je! Yeye hatazidi kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?” Je! Hamuwezi kumwamini Baba yenu wa mbinguni? Je! Wewe Huwezi kuzitumainia ahadi Zake za thamani? “Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na Haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.” Ahadi ya thamani! Je! hatuwezi kuitegemea hii ahadi Yake? Je! Hatuwezi kuwa na imani kamili, tukijua kwamba Yeye aliyeahidi ni Mwaminifu? Ninakuomba uiache imani yako inayotetemeka, na zichukue tena ahadi za Mungu. Weka uzito wako wote juu ya hizo na imani isiyoyumba; kwa kuwa hazitashindwa, haziwezi, kushindwa kwamwe. {2T 496.2}

## **SURA YA 61**

### **HOTUBA KWA WACHUNGAJI**

Ndugu Wapendwa: Oktoba 25, 1868, nilioneshwa kuwa sio wote wanaodai wameitwa kufundisha Ukweli wana sifa/stahiki kwa kazi hii takatifu. Wengine wako mbali kufikia akili na mapenzi ya Mungu. Wengine huendekeza uvivu kwenye mambo ya muda mfupi, na kisha hata maisha yao ya kidini yana alama ya uvivu wa kiroho. Ambapo kuna ukosefu wa nguvu ya ustahimilivu kwenye mambo ya kitambo na shughuli za biashara, upungufu huo utaonekana katika mambo ya kiroho pia. {2T 498.1}

Baadhi yenu ni viongozi wa familia, na mfano na ushawishi wenu unaunda tabia za watoto wenu. Mfano wako utafuatwa nao kwa

kiwango kikubwa au kidogo, na ukosefu wako wa ukamilifu, unaweka mfano mbaya kwa wengine. Lakini upungufu wako unahisiwa kwa mambo mazito zaidi, katika kusudi na kazi ya Mungu. Familia zenu zimehisi upungufu huu, na kuteseka kwa matokeo yake; wamekosa vitu vingi ambavyo uchapaji kazi kwa bidii na uvumilivu vingeweza kuleta. Lakini upungufu huu umeonekana na kuhisiwa katika kusudi na kazi ya Mungu katika kiwango kikubwa, na kazi ya Mungu muhimu, zaidi kuliko vitu vinavyohusu maisha haya. {2T 498.2}

Ushawishi wa wachungaji wengine sio mzuri. Hawajalinda kwa uangalifu muda na matukio yao, na hivyo kuwapa watu mfano wa bidii ya kazi. Wao hutumia wakati kwa uvivu na masaa ambayo, yanapoendelea kupita milele, ndivyo rekodi yao ya matokeo yake, haiwezi kukumbukwa kamwe. Wengine ni wavivu kwa asili, hili linafanya kuwe na ugumu katika kufanikisha shuguli au jambo lolote wanalofanya. Upungufu huu umeonekana na kuhisiwa kote kote katika uzoefu wao wa kidini. Wale walio na makosa sio pekee yao wanaoshindwa au wanaopoteza; wengine hufanywa kuteseka kutokana na upungufu wao. Katika kipindi hiki cha mwisho, wengi wana mafunzo ya kujifunza ambayo yangepaswa kujifunzwa katika za tarehe za mapema zaidi. {2T 498.3}

Wengine sio wanafunzi wa karibu wa Biblia. Wameshindwa kujituma wenyewe kwa uadilifu na bidii katika masomo ya Neno la Mungu. Kwa sababu ya kupuuza hili, wamefanya kazi kwa hasara kubwa na hawajawahi katika juhudi zao za kichungaji kutimiza sehemu moja ya kumi ya kazi, 1/10- ambayo wangeweza kufanya ikiwa wangeona umuhimu wa kutumia kwa karibu akili zao katika kusoma Neno. Wangeza kuwa wanaojua Maandiko, wenye nguvu na hoja za Biblia, kiasi kwamba wangeweza kukabiliana na wapinzani na kwa hivyo wangewasilisha sababu za imani yetu kiasi kwamba Ukweli ungeweza kushinda na kunyamazisha upinzani wao. {2T 499.1}

Wale wanaohudumu katika Neno, lazima wawe na ujuzi kamili wa Neno hilo kama inavyowezekana kwao kulipata. Lazima waendeleo kutafuta, kuomba, na kujifunza, au watu wa Mungu wataendelea mbele katika ujuzi wa Neno Lake na mapenzi Yake, na kuwaacha mbali sana hawa

wanaodai kuwa walimu. Je! Ni nani atakayewafundisha watu wanapokuwa wamejua zaidi ya waalimu wao? Jitihada zote za wachungaji hao hazina matunda. Kuna haja kwamba watu wawafundishe Neno la Mungu kwa ukamilifu zaidi, kabla ya wao kuweza kuwafundisha wengine. {2T 499.2}

Wengine labda sasa wangukuwa watendakazi kamili ikiwa wangetumia vizuri muda wao, wakihihi kwamba watalazimika kutoa hesabu kwa Mungu kwa wakati wao uliotumiwa vibaya. Wamemchukiza Mungu kwa sababu hawajafanya bidii. Kuridhisha nafsi, kujipenda wenyewe, na kupenda raha na maisha rahisi, vimewazuia wengine katika mema, viliwazuia kupata maarifa ya Maandiko ili waweze kuwa wamekamilihwa katika matendo yote mema. Wengine hawana thamani ya muda na wameutumia kwa uzembe/uvivu kitandani, masaa ambayo yangeweza kutumiwa katika kusoma Biblia. Kuna masomo machache ambayo wamekuwa wakiyashugulikia zaidi, ambayo wanayajua, na katika hayo wanaweza kuzungumza na kukubalika; lakini kwa kiasi kikubwa wamepumzisha mambo hapa. Hawajajisikia kabisa kuridhika na wao wenyewe, na wakati mwingine wamegundua upungufu wao; na bado hawajaamshwa vya kutosha katika uhalifu wa kupuuzia kushugulika kusoma Neno la Mungu, ambalo wanakiri kulifundisha. Kwa sababu ya ujinga wao, watu wamekata tamaa; hawapokei ujuzi mahiri, ambao wangeweza kuupata kutoka kwao na ambao wanatarajia kuupata kutoka kwa wachungaji wa Kristo. {2T 499.3}

Kwa kuamka mapema na kutumia vizuri muda wao, wachungaji wanaweza kupata wasaa wa uchunguzi wa karibu wa Maandiko. Lazima wawe na uvumilivu, na wasizuiliwe katika lengo hilo, bali watumie muda wao katika kusoma Neno, wakiwasaidia wengine Ukweli ambao akili zingine, kupitia kazi ya kuchosha, wamefanya Ukweli utolewe nje kwao, na kwa bidii na juhudi madhubuti zitayarishwe mikononi mwao. Kuna wachungaji ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa miaka mingi, wakifundisha wengine Ukweli, wakati wao wenyewe hawana ujuzi wa mambo madhubuti ya msimamo wetu. Ninawaomba hao kuachana na uvivu wao. Ni laana kwao daima. Mungu anawataka kutumia kila wakati kuzaa matunda mema kwao



wenyewe au kwa wengine. “Sio walegevu katika kazi; mkiwa na juhudi katika roho zenu, mkimtumikia Bwana.” “Yeye naye aliye mvivu katika kazi yake, Ni ndugu yake aliye mharabu.” {2Tsw 500.1}

Ni muhimu kwa wachungaji wa Kristo kuona umuhimu wa utamaduni wa kibinafsi, ili kuipamba taaluma na kudumisha heshima. Bila mafunzo ya akili hakika watashindwa katika kila wanachokifanya. Nimeonyeshwa kuwa kuna ukosefu wa makusudi kwa baadhi ambao wanalihubiri neno. Mungu hafurahishwi na njia na mawazo yao. Njia yao ya hovy ovyo ya kunukuu Maandiko ni aibu kwa taaluma yao. Wanadai kuwa waalimu wa Neno, na bado wanashindwa kurudia Maandiko kwa usahihi. Wale wanaojitolea kabisa kuhubiri Neno hawapaswi kuwa na hatia ya kunukuu Andiko hata moja vibaya. Mungu anahitaji utimilifu wa watumishi Wake wote. {2Tsw 500.2}

Dini ya Kristo itaonyeshwa mfano na mmiliki wake maishani, katika mazungumzo, na kazi. Kanuni zake zenye nguvu zitaithibitisha nanga. Wale ambao ni waalimu wa Neno wanapaswa kuwa kielelezo cha uchaji, mifano kwa kundi. Mfano wao unapaswa kukemea uvivu, ulegevu, ukosefu wa juhudi katika uzalishaji na uchumi. Kanuni za dini zinadai bidii, uadilifu, uzalishaji, na uchumi. Sentesi “Toa hesabu ya uwakili wako” hivi karibuni itasikiwa na wote. Ndugu zangu, je! Ni hesabu gani ambayo mnaweza kutoa ikiwa Mwalimu sasa ataonekana? Haujawa tayari. Bila shaka ungehesabiwa pamoja na watumishi wavivu wakati wanalipo. Wakati muhimu bado umeachiwa. Nakusihi ukomboe wakati. {2Tsw 501.1}

Paulo alimhimiza Timotheo: “Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtendazi kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la kweli.” “Walakini uyakatae maswali ya upumbavu na yasiyo na elimu, ukijua ya kuwa huzaa ugomvi wa kijinsia. Na tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu, akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua Kweli; wapate tena fahamu zao, kutoka katika mtego wa ibilisi, ambao hao wametegwa naye, hata kufanya mapenzi yake.” {2Tsw 501.2}

Ili kutimiza kazi ambayo Mungu anahitaji kutoka kwao, wachungaji wanahitaji kufanywa wafae kwa nafasi yao-wawe na stahiki/sifa. Mtume Paulo, katika barua yake kwa Wakolosai, anasema hivi kuhusu huduma yake: “Ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawasawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu, nilitimize Neno la Mungu; siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu Wake; ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa; nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu; ambaye tunamhubiri habari Zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote; tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu. Nami najitaabisha kwa Neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendayo kazi ndani yangu kwa nguvu.” {2Tsw 501.3}

Bwana hahitaji kuthamini utakatifu na kujitolea kwa udogo, kazi ya huduma ambayo watumishi Wake wanaoishi karibu na mwisho wa mambo yote wanaifanya. Yeye Hawezi kukubali kazi ya wafanyakazi isipokuwa wanatambua ndani ya mioyo yao wenyewe uzima na nguvu ya Ukweli ambao huwasilishwa kwa wengine. Yeye hatakubali chochote kisichokuwa na bidii, kisichoshugulikiwa kwa nguvu na ari ya moyo wa kazi. Kuwa macho na kuzaa matunda kunahitajika kwa kazi hii kubwa. Mungu anataka watendakazi wasio na ubinafsi, wale ambao watafanya kazi kwa ukarimu usio na ubinafsi na kutoa mapenzi yao yasiyogawanyika kwa kazi hiyo. {2Tsw 502.1}

Ndugu zangu, mnakosa kujitolea na kujiweka wakfu kwa kazi hiyo. Mioyo yenu ni ya ubinafsi. Mapungufu ndani yenu lazima yajazwe, vinginevyo kabla ya muda mrefu mtakutana na kukatishwa tamaa kubaya—mtapoteza mbingu. Mungu hachukulii kwa urahisi kupuuzwa kwa utendaji wenye uaminifu, wa kazi ambayo amewaachia watumishi Wake kuifanya. Nguvu ya kudumu na kumtegemea Mungu mara kwa mara vinakosekana kwa wengi wanaofanya kazi katika huduma. Matokeo ya ukosefu huu, huleta mizigo mikubwa kwa wachache ambao wana sifa hizi, na hao wanaohitajika kurekebisha upungufu ulio wazi kwa wale ambao wanaweza kuwa watenda kazi ikiwa watataka kuwa hivyo. Kuna wachache ambao wanafanya kazi mchana na usiku,

wakijinyima wenyewe pumziko na maburudiko ya kijamii, wakiutumikisha ubongo zaidi, kila mmoja akifanya kazi ya watu watatu, wakiyachakaza maisha yao ya thamani kufanya kazi ambayo wengine wanaweza kufanya, lakini wameipuuza. Wengine ni wavivu sana kutekeleza sehemu yao; wachungaji wengi wanajihifadhi wenyewe kwa uangalifu, kwa kujiepusha na mizigo, wakibaki katika hali ya kutokuwa na ufanisi, na kutofanikisha chochote. Kwa hivyo wale wanaotambua thamani ya roho, ambao wanathamini utakatifu wa kazi na wanahisi kwamba lazima iende mbele, wanafanya kazi ya ziada, wakitenda kwa bidii kali, isiyo ya kibinadamu, na kutumia nguvu zao za ubongo kufanya kazi iendeleo kusonga. Je! Mvuto wa kazi na kujitolea kwake viligawanywa sawa?, Je, wale wote ambao hudai kuwa wachungaji walikuwa na bidii katika kuyasalimisha mapenzi yao kwa kazi, bila kujali maslahi yao wenyewe?; wafanyikazi wachache wenye bidii, wanaomcha Mungu ambao wamejichosha maisha yao wangeweza kuhuishwa kwa kuondolewa shinikizo hili kubwa juu yao, na nguvu zao zingeweza kuhifadhiwa ili kwamba, wakati zinapohitajika zinaweza kusema kwa nguvu maradufu, na kutoa matokeo makubwa zaidi kuliko inavyoweza kuonekana wakati huu zikiwa chini ya shinikizo la utisho mkubwa na wasiwasi. Bwana hafurahishwi na kutokuwa uwiano huku (hamna balance). {2Tsw 502.2}

Wengi wanaodai wameitwa na Mungu kuhudumu katika Neno na mafundisho hawahisi kutokuwa na haki ya kudai kuwa waalimu isipokuwa wamefanywa kamili kwa bidii wakijifunza Neno la Mungu. Wengine wamepuuza kupata ujuzi wa fani rahisi za elimu (3R-Reading, 'Rithmetic, 'Riting kusoma, kuandika na kuhesabu). Wengine hawawezi hata kusoma kwa usahihi; wengine wananukuu Maandiko vibaya; na wengine, kwa ukosefu wa sifa za kufaaa kwa kazi wanayojaribu kufanya, huathiri kazi ya Mungu na kuufanya Ukweli kutokuwa na manufaa au kudharauliwa. Hawa hawaoni umuhimu wa kukuza akili, hasa kwa kuhimiza uboreshaji bila kuathiri udhati, na kuinua tabia ya Kweli ya Kikristo. Njia yenye ufanisi na inayofaa ya kufikia hili ni kuselimisha nafsi kwa Mungu. Yeye Ataelekeza akili na mapenzi ili yajikite juu ya Uungu na umilele, na kisha watamiliki nguvu bila harara, kwa kuwa nguvu zote za akili na za mwili wote zitainuliwa, zitasafishwa, na kuelekezwa katika kituo cha juu kabisa, mkondo

mtakatifu. Kutoka kwa midomo ya Mwalimu wa mbinguni yalisikika Maneno haya: “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote, na nguvu zako zote.” Wakati huu utii na kujisalimisha kunafanywa kwa Mungu, unyenyekevu wa Kweli utajaza neema kila tendo, wakati huo huo wale ambao ni washirika wa Mungu na malaika Zake wa mbinguni watamiliki heshima ya mbinguni. {2Tsw 503.1}

Bwana anahitaji watumishi Wake kuwa wenye nguvu. Haimpendezi Yeye kuwaona hawana waleguvu na wavivu. Wanakiri kuwa na ushahidi kwamba Mungu amewachagua kikamilifu kuwafundisha watu njia ya uzima; lakini mara nyingi mazungumzo yao hayana faida, na wanaonesha kuwa hawana mzigo wa kazi juu yao. Nafsi zao hazijatiwa nguvu na Kweli kuu ambazo wao huwasilisha kwa wengine. Wengine huhubiri Kweli hizi, za umuhimu mkubwa, kwa njia ya ulegevu sana kiasi kwamba hawawezi kuwaathiri watu. “Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako.” Wanadamu ambao Mungu amewaita lazima wafunzwe kufanya bidii, kufanya kazi kwa bidii na kwa ari bila kuchoka kwa ajili Yake, ili kuzivuta roho kutoka motoni. Wakati wachungaji wanahisi nguvu ya Ukweli katika nafsi zao, wakiufurahia katika nafsi zao wenyewe, ndipo watapata nguvu ya kuathiri mioyo, na kuonesha kwamba wanaamini kabisa Ukweli wanaouhubiri kwa wengine. Wanapaswa kuweka mbele ya akili zao thamani ya roho, na kina kisicho na mfanano cha upendo wa Mwokozi. Hii itaamsha roho ili kwamba pamoja na Daudi waseme: Moyo wangu ukawa moto ndani yangu, na katika kuwaza kwangu moto ukawaka.” {2Tsw 504.1}

Paulo alimhimiza Timotheo: Hebu “Mtu awaye yote asiudharau ujana wako; bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo, katika imani na usafi. Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kuonya na kufundisha.” “Uyatafakari hayo; ukae katika hayo, ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo, maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.” Uzito ulio muhimu sana hapa umeambatanishwa na maisha ya Kikristo ya mchungaji/mtumishi wa Mungu! Anahitajika sana kujifunza Neno kwa

uaminifu, ili yeye mwenyewe aweze kutakaswa na Ukweli na aweze kuwa na sifa ya kufundisha wengine. {2Tsw 504.2}

Ndugu, mnatakiwa kuonesha mfano wa Ukweli katika maisha yenu. Lakini wale ambao wanadhani kuwa wana kazi ya kufanya kufundisha wengine Ukweli sio wote wameongoka, na kutakaswa na Ukweli. Wengine wana maoni potofu juu ya vile Mkristo anavyopaswa kuwa na njia ambayo uzoefu wa dini thabiti unavyopatikana; na kwa uchache sana, wanaelewa sifa ambazo Mungu anahitaji kwa watumishi Wake kuwa nazo. Watu hawa hawajatakaswa. Wakati mwingine huwa na hisia zinazopaa-paa (zenye mori mori), ambazo huwapatia fikra kwamba kwa kweli ni watoto wa Mungu. Utegemezi huu juu ya hisia ni moja ya udanganyifu maalum wa Shetani. Wale ambao wanajishugulisha, hivyo hufanya dini yao kuwa jambo la hali ilivyo. Kanuni imara inapungua. Hakuna wawezao kuwa Wakristo walio hai isipokuwa wana uzoefu wa kila siku katika mambo ya Mungu na mazoea ya kujikana nafsi kila siku, wakibeba kwa moyo mkunjufu msalaba na kumfuata Kristo. Kila Mkristo aliye hai ataongezeka kila siku katika maisha ya Uungu. Anapoendelea kuuelekea ukamilifu, anapata uzoefu wa uongofu kwa Mungu kila siku; na uongofu huu haukamiliki mpaka afikie ukamilifu wa tabia ya Kikristo, maandalizi kamili ya mguso wa mwisho wa kutokufa. {2T 505.1}

Mungu anapaswa kuwa jambo la juu zaidi cha mawazo yetu. Kumtafakari Yeye na kumsihi kwa maombi, kunainua roho na kuhuisha mapenzi. Kupuuza kutafakari na maombi hakika kutasababisha kupungua kwa upendo wa kidini. Halafu kutaonekana uzembe na uvivu. Dini sio mhemko tu ya hisia. Ni kanuni ambayo imeunganishwa na majukumu yote ya kila siku na shughuli za maisha. Hakuna kitakachochukua mawazo sana au kuyatumbuiza zaidi, hakuna kazi inayohusishwa, ambayo itazuia kuambatanishwa na kanuni hii. Ili kudumisha dini safi na isiyo na mawaa, ni muhimu kuwa watendakazi wanaodumu katika jitihada. Lazima tufanye kitu sisi wenyewe. Hakuna mtu mwingine anayeweza kufanya kazi yetu. Hakuna yeyote anayeweza kufanya kazi yetu, hakuna anayeweza kuufanyia kazi wokovu wetu kwa hofu na kutetemeka. Hii ndiyo kazi haswa ambayo Bwana ametuachia sisi kuifanya. {2T 505.2}

Wachungaji wengine wanaodai kuitwa na Mungu wana damu ya roho kwenye mavazi yao. Wamezungukwa na watu waliorudi nyuma na wenye dhambi, na bado hawahisi mzigo kwa roho zao; wanaonesha kutojali kuhusu wokovu wao. Wengine wamekaribia kulala kiasi kwamba wanaonekana hawana ufahamu wa kazi ya mtumishi wa injili. Hawazingatii kuwa wao kama madaktari wa kiroho wanahitajika kuwa na ustadi wa kushughulikia roho zilizougua kwa dhambi. Kazi ya kuwaonya wenye dhambi, ya kuwalilia na kuwasihi, imepuuzwa mpaka roho nyingi zimeshatanga-tanga mbali sana kiasi cha kutoweza kutibiwa. Wengine wamekufa katika dhambi zao, na katika hukumu watakabiliana na lawama za hatia yao dhidi ya wale ambao wangeweza kuwaokoa, lakini ambao hawakufanya hivyo. Wachungaji wasio waaminifu, ni adhabu ya jinsi gani inayowasubiri! {2Tsw 506.1}

Watumishi wa Kristo wanahitaji uvuvio mpya, ili waweze kutambua wazi-wazi zaidi mambo matakatifu, na kuwa na dhana wazi ya tabia takatifu, isiyo na lawama ambayo wao wenyewe lazima waiunde ili waweze kuwa mifano kwa kundi. Hakuna kitu ambacho tunaweza kufanya sisi wenyewe ambacho kitatuleta kwenye hali ya juu ambapo Mungu anaweza kutukubali kama mabalozi Wake. Ni kumtegemea Mungu kabisa tu, na imani thabiti na inayofanya kazi, ndiyo itakayokamilisha kazi ambayo Yeye anahitaji kufanywa ndani yetu. Mungu anaita watu wanaotaka kufanya kazi. Ni mwendelezo katika kutenda mema ndio utaunda tabia za mbinguni. Kwa uwazi, kwa uaminifu na upendo, lazima tuwavutie watu na kuwaita kujiandaa kwa siku ya Mungu. Wengine watahitaji kusihiwa kwa bidii kabla ya kuweza kushawishiwa. Hebu kazi ijulikane kwa upole na unyenyekevu, lakini kwa bidii ambayo itawafanya kuelewa kuwa mambo haya ni ya uhalisi-Ukweli, na kwamba uzima na kifo vipo mbele yao kwa uchaguzi. Wokovu wa roho sio jambo la kuchezewa. Mwenendo wa mtendakazi kwa Mungu unapaswa kuwekewa uzito na umakini, na kujawa na sifa ya unyenyekevu na adabu ya kweli ya Kikristo, lakini bado bidii inapaswa kufanywa katika kazi ambayo Mwalimu amemwachia afanye. Uvumilivu wa njia katika jambo la haki, kuifundisha/kunidhamisha akili kwa kufanyia kazi mazoezi ya kidini- kupenda Ibada/uchaji na vitu vya mbinguni, kutaleta kiwango kikubwa zaidi cha furaha. {2T 506.2}

Ikiwa tunamfanya Mungu kuwa tumaini letu, tunao uwezo wa kudhibiti akili katika vitu hivi. Kupitia mazoezi endelevu kutakuwa na nguvu ya kupigana na maadui wa ndani na kujitiisha nafsi, mpaka kutakapokuwa na badiliko kamili, na shauku, hamu, na mapenzi vitaletwa katika utii kamili. Ndipo kutakuwa na uchaji Mungu wa kila siku nyumbani na ugenini (utauwa), na tunaposhiriki katika kazi kwa ajili ya roho, nguvu itaambatana na juhudi zetu. Mkristo mnyenyekevu atakuwa na vipindi vya ibada ambavyo sio vya misimu isiyotabirika ya hapa na pale (spasmodic), siyo ya vipindi, au vya ushirikina, bali tulivu na mwanana, vya kina, vya daima na vya bidii. Upendo kwa Mungu, kujizoesha utauwa, vitapendeza wakati kuna kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu. {2T 507.1}

Sababu ambayo wachungaji wa Kristo hawafanikiwi tena katika kazi zao ni kwa sababu hawajajitolea bila ubinafsi kwa kazi. Shauku ya wengine imegawanyika; wana nia mbili. Wasiwasi wa maisha haya huchukua umakini wao, na hawatambui jinsi kazi ya mchungaji ilivyo takatifu. Hao wanaweza kulalamikia kuhusu giza, kutokuamini kukubwa, na kukosa uaminifu. Sababu ya hii ni kutoweka mambo sawa na Mungu; hawaoni umuhimu wa kujitoa wakfu kabisa na kwa ukamilifu Kwake. Wanamtumikia Mungu kidogo, lakini wao wenyewe zaidi. Wanasali, lakini kidogo tu. {2T 507.2}

Mwalimu wa mbinguni, alipokuwa akijihusisha katika huduma Yake ya kidunia, aliomba sana kwa Baba Yake. Mara nyingi alikuwa akipiga magoti usiku kucha katika maombi. Roho Yake mara nyingi ilikuwa na huzuni wakati Alipohisi nguvu za giza za ulimwengu huu, na aliuacha mji ulio na shughuli nyingi na umati wa watu wenye kelele, ili kutafuta mahali pa utulivu kufanya maombezi Yake. Mlima wa Mizeituni ulikuwa ni kituo alichokipendelea Mwana wa Mungu kwa ibada Zake. Mara kwa mara baada ya umati kumwacha kwa pumziko la usiku, hakupumzika, ingawa alikuwa amechoka kwa kazi za siku hiyo. Katika Injili ya Yohana tunasoma: “Walikwenda kila mtu nyumbani kwake. Naye Yesu akaenda mpaka Mlima wa Mizeituni.” Wakati mji ulinyamaza kimya, na wanafunzi walikuwa wamerudi nyumbani kwao kupata pumziko katika usingizi, Yesu hakulala. Maombi yake ya Kiungu yalikuwa yakipanda

kwenda kwa Baba Yake kutoka Mlima wa Mizeituni ili wanafunzi Wake waepushwe na ushawishi wa uovu ambao wangeweza kukutana nao kila siku ulimwenguni, na ili roho Yake Mwenyewe ipate kuimarishwa, kutayarishwa na kutegemezwa kwa majukumu na majaribio/changamoto ya siku inayofuaia. Usiku wote, wakati wafuasi Wake walikuwa wamelala, Mwalimu wao wa kimbingu alikuwa akiomba. Umande na utando wa barafu ndogo-ndogo za usiku vilianguka juu ya kichwa Chake, akiwa amepiga magoti kwa maombi. Mfano Wake umeachwa kwa wafuasi Wake. {2T 508.1}

Mwalimu na Mkuu wa mbinguni, wakati alipokuwa akishughulika katika utume Wake, mara nyingi alikuwa akiomba kwa bidii. Hakutembelea kila wakati Mizeituni, kwa maana wanafunzi Wake walikuwa wamegundua mahali Pake pa pumziko alipopapenda, na mara nyingi walimfuata. Alichagua utulivu wa usiku, wakati ambapo hakutakuwa na usumbufu. Yesu angeweza kuponya wagonjwa na kufufua wafu. Yeye Mwenyewe alikuwa chanzo cha baraka na nguvu. Aliamuru hata dhoruba, na zilimtii Yeye. Yeye hakuwa amechafuliwa na ufigadi, hakuizoea dhambi-mgeni kwa dhambi; lakini aliomba, na mara nyingi kwa kilio cha nguvu na machozi. Aliwaombea wanafunzi Wake na Yeye Mwenyewe, na hivyo akijifunganisha na mahitaji yetu, udhaifu wetu, na mapungufu yetu, ambayo ni ya kawaida sana kwa ubinadamu. Alikuwa Mwombaji/Mwombezi Mwenye nguvu, hakuwa na tamaa za asili ya ubinadamu wetu, asili zilizoanguka, lakini alizungukwa na udhaifu kama huo, bali Yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote. Yesu alivumilia uchungu ambao ulihitaji msaada/usaidizi kutoka kwa Baba Yake. {2T 508.2}

Kristo Ndiye mfano wetu. Je! Watumishi wa Kristo wamejaribiwa na kuumizwa vibaya na Shetani? Ndivyo ilivyokuwa Kwake pia Yeye ambaye hakuijua dhambi. Alimgeukia Baba Yake katika masaa haya ya dhiki. Alikuwa duniani ili Aweze kutoa njia ambayo sisi wanadamu tunaweza kupata neema na nguvu za kusaidia katika kila wakati wa uhitaji, kwa kufuata mfano Wake katika maombi ya mara kwa mara ya dhati na bidii. Ikiwa watumishi wa Kristo wataiga mfano huu, watajazwa na Roho Wake, na malaika watawahudumia. {2T 509.1}



Malaika walimhudumia Yesu, Ila uwepo wao haukufanya maisha Yake kuwa ya raha na uhuru kutoka mzozo mkali na majaribu makali. Alijaribiwa katika mambo yote kama sisi, lakini hakutenda dhambi. Ikiwa wachungaji, wakati wanajihusisha katika kazi ambayo Mwalimu amewateua kuifanya, wana majaribu, mifadhaiko na mashaka na vishawishi, Je! wangevunjika moyo, wakati wanajua kwamba kuna Yule aliyekwisha kuvumilia haya yote mbele yao? Je! Watupilie mbali ujasiri wao kwa sababu hawatambui yote ambayo wanatarajia kutoka katika kazi zao? Kristo alifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya taifa Lake Mwenyewe; lakini juhudi Zake zilidharauliwa na hao hao aliokuja kuwaokoa, na wakamuua Yule aliyekuwa kuwapatia uzima. {2T 509.2}

Kuna idadi ya kutosha ya wachungaji, lakini kuna ukosefu mkubwa wa watendakazi. Watendakazi, wafanyao kazi pamoja na Mungu (walei), walio na ufahamu wa utakatifu wa kazi na mizozo mikali ambayo lazima wakutane nayo ili kuipeleka kazi mbele kwa mafanikio. Wafanyakazi hawatazimia na kukata tamaa kwa sababu ya kazi, hata iwe ngumu kiasi gani. Katika Waraka kwa Warumi Paulo anasema: “Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo: ambaye kwa Yeye tumepata kwa njia ya imani kufikia neema hii ambayo mnasimama ndani Yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. Wala si hivyo tu, ila twafurahia katika dhiki pia; tukijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayari; Kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi” Ambaye Katika Yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika. Hatuna udhuru ikiwa tutashindwa wenyewe kujichotea majaliwa ya neema makubwa yaliyofanywa kwa ajili yetu ili tusipate kupungukiwa chochote. Kusita na kukwepa kazi kwaajili ya dhiki, kulalamika katika shida, huwafanya watumishi wa Mungu kuwa wadhaifu na kutokuwa na uwezo wa kubeba majukumu na mizigo. {2T 509.3}.

Wote wanaosimama bila kutahayari mbele ya vita lazima wahisi vita maalum vya Shetani dhidi yao. Wanapotambua mashambulio yake, watakimbia kwenye Ngome imara. Wanahisi hitaji lao maalum la

nguvu kutoka kwa Mungu, na wanafanya kazi kwa nguvu Zake; kwa hivyo ushindi wanaoupata hauwainui wao, bali huwaongoza kwa imani kutegemea zaidi usalama kutoka kwa Mwenye Nguvu. Shukrani kubwa na ya dhati kwa Mungu imeamshwa mioyoni mwao, na wanafurahi katika dhiki ambayo wanapata wakati wa kushinikizwa na adui. Watumishi hawa wa kujitolea wanapata uzoefu na kuunda tabia ambayo italeti heshima kwa kazi ya Mungu. {2T 510.1}

Wakati wa sasa ni msimu wa upendeleo wa pekee na dhamana takatifu kwa watumishi wa Mungu. Ikiwa amana hizi zitatunzwa kwa uaminifu, kutakuwa na thawabu kubwa kwa mtumwa mwaminifu wakati Bwana atasema: “Toa hesabu ya uwakili wako.” Kazi ya dhati na bidii na taabu, kazi isiyo na ubinafsi, uvumilivu, juhudi ya kudumu, itakuwa ya thawabu kubwa; Yesu atasema: Tangu sasa siwaiti tena watumwa, lakini marafiki, wageni. Idhini ya Mwalimu haitolewi kwa sababu ya ukubwa wa kazi iliyofanywa, au kwa sababu vitu vingi vilivyopatikana, bali kwasababu ya uaminifu/uadilifu, katika hata vitu vichache. Sio kwa matokeo makubwa tunayopata, bali kwa nia ambazo tunazo katika kile tunachotenda, hizo zina uzito kwa Mungu. Yeye Anathamini wema na uaminifu kuliko ukubwa wa kazi iliyokamilishwa. {2T 510.2}

Nimeonyeshwa kuwa wengi wako katika hatari kubwa ya kushindwa kukamilisha utakatifu katika kumcha Bwana. Wachungaji wako katika hatari ya kupoteza roho zao. Baadhi ambao wamehubiri wengine, wao wenyewe watakatiliwa mbali kwa sababu hawakukamilisha tabia ya Kikristo. Katika kazi yao hawaokoi roho, na wanashindwa hata kuokoa roho zao wenyewe. Hawaoni umuhimu wa kujitambua wenyewe na kujidhibiti nafsi zao. Hawakeshi na kuomba, ili wasije wakaingia majaribuni. Ikiwa wangekesha, wangeweza kujua mazoea yao dhaifu, pale walipo na uwezekano mkubwa wa kushambuliwa vibaya na majaribu. Kwa kukesha na kuomba, maeneo yao ya udhaifu yanaweza kulindwa hata kuwa maeneo ya nguvu yao, na wanaweza kukabiliana na majaribu bila kushindwa. Kila mfuasi wa Kristo anapaswa kujichunguza kila siku, ili apate kufahamu kabisa mwenendo wake mwenyewe. Kwa wengi kuna kupuuza uchunguzi wa nafsi (uchunguzi binafsi haupo). Kupuuza huku daima ni hatari kwa mtu anayekiri kuwa

mnenaji wa Mungu, akichukua nafasi ya kutisha, ya uwajibikaji wa kupokea Maneno kutoka kwa Mungu na kwenda kuwapa watu Wake. Mwenendo wa kila siku wa mtu kama huyo una ushawishi mkubwa kwa wengine. Ikiwa ana mafanikio yoyote katika kazi, yeye huleta waongofu wake katika kiwango chake cha chini, na ni nadra kuweza kuinuka juu. Njia za mchungaji wao, maneno yake, ishara na tabia zake, imani yake, na utauwa wake, huchukuliwa kama mfano kwa wale wote ambao ni watunza Sabato wanaongojea Ujio wa Yesu (Waadventista wa Sabato); na ikiwa wanamfuata yule aliyewafundisha Ukweli, wanadhani wanafanya wajibu wao wote. {2T 511.1}

Kuna mengi katika mwenendo wa mchungaji ambayo anaweza kuboresha. Wengi wanaona na kuhisi upungufu wao, lakini wanaonekana kutojua ushawishi wanaotoa. Wanajua matendo yao wanayoyafanya, lakini huyaacha kutoka katika kumbukumbu zao, na hivyo basi hawabadilishwi. Ikiwa wachungaji wangepanya matendo ya kila siku kuwa mada ya kutafakari kwa uangalifu na kujikagua kwa kukusudia, na kwa kitu hicho wazitambue tabia za maisha yao wenyewe, basi wangejifahamu vizuri. Kwa uchunguzi wa karibu wa maisha yao ya kila siku katika hali zote wangejua nia zao wenyewe, kanuni zinazowasukuma. Uchunguzi huu wa matendo yetu kila siku, ili kuona ikiwa dhamiri inayakubali au inayalaani, ni muhimu kwa wote wanaotaka kufikia ukamilifu wa tabia ya Kikristo. Vitendo vingi ambavyo hupita kama kazi njema, hata vitendo vya ukarimu, na nia njema, vikichunguzwa kwa ukaribu, vitapatikana vikichochewa na nia mbaya. Wengi hupokea sifa kwa pongezi, na makofi kwa fadhila ambazo hawana. Mchunguza mioyo hukagua nia ya kufanya jambo, na mara nyingi vitendo ambavyo vinashangiliwa sana na watu vinarekodiwa na Bwana kama vinavyotoka katika nia za ubinafsi na misingi ya unafiki. Kila tendo la maisha yetu, liwe bora na la kusifiwa au linalostahili karipio, linahuhukumiwa na Mchunguza mioyo kulingana na nia ambayo iliyochochea. {2T 511.2}

Hata wachungaji wengine wanaotetea sheria ya Mungu, wana ujuzi mdogo, kuhusiana na wao wenyewe. Hawatafakari, na kuchunguza nia zao. Hawaoni makosa na dhambi zao, kwa sababu hawatendi, kwa uaminifu, unyofu na kwa bidii, kuchunguza maisha yao, matendo yao,

na tabia zao tofauti na kwa ujumla, na kuzilinganisha na sheria takatifu na safi ya Mungu. Madai ya sheria ya Mungu hayajaeleweka vizuri kwao, na wanaishi kila siku kwa kukiuka roho ya sheria hiyo ambayo wao wanakiri kuiheshimu. “Kwa sheria,” anasema Paulo, “kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria.” “Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria: kwa maana singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani.” Wengine ambao hufanya kazi katika Neno na mafundisho hawana uelewa halisi wa sheria ya Mungu na madai Yake matakatifu, au ya upatanisho wa Kristo. Wao wenyewe wanahitaji kuongoka kabla ya kuweza kuongoa wenye dhambi. {2T 512.1}

Kioo cha uaminifu ambacho kingefunua kasoro katika tabia kimepuuzwa; kwa hivyo ulemavu na dhambi vimo, na huonekana kwa uwazi na wengine, ikiwa wale walio katika makosa hawaelewi hili. Dhambi ya kuchukiza ya ubinafsi ipo kwa kiwango kikubwa miongoni mwa watu, hata kwa baadhi ambao wanakiri kuwa wamejitoe kwa kazi ya Mungu. Ikiwa wangelinganisha tabia zao na mahitaji Yake, haswa na Kiwango kile kikubwa, sheria Yake takatifu, ya haki, na njema, wagegundua, ikiwa wangetafiti kwa bidii, kwa uaminifu, kwamba ni wahitaji wa kuogofya, wamepunguka. Lakini wengine hawako tayari kuangalia mbali vya kutosha au kwa kina kiasi cha kutosha, kuona uovu wa mioyo yao. Wamepungua katika mambo mengi sana; lakini bado wanabaki katika ujinga wa hatia yao kwa kupenda, na wana nia ya kujali matakwa yao ambayo Mungu hayajali. {2T 512.2}

Baadhi kwa asili sio watu wa kujitoe kumcha Mungu kwa ibada, na kwa hivyo wanapaswa kuhimizwa na kutiwa moyo kukuza tabia ya uchunguzi wa karibu wa maisha yao wenyewe na nia zao, na wanapaswa sana kutunza upendo wa mazoezi ya kidini na maombi ya siri. Mara nyingi husikika wakiongea juu ya mashaka na kutokuamini, na kukaa juu ya changamoto za ajabu ambazo wamekuwa nazo kuhusiana na hisia za kikafiri. Wanakaa katika ushawishi wa kukatishwa tamaa na hivyo kuathiri imani yao, tumaini, na ujasiri katika Ukweli na katika mafanikio ya mwisho ya kazi na utumishi katika yale ambayo wanahusika nayo, na hata kuonyesha ni jambo la ubora maalum au la tabia njema kuonyesha mashaka. Wakati mwingine wanaonekana kufurahi sana kushugulikia juu ya misimamo ya makafiri

na kuimarisha kutokuamini kwao na kila hali wanayoweza kuikusanya kama kisingizio cha giza lao. Kwa hao tunaweza kusema: Ingekuwa bora mng'atuke mara moja, na muache kuta za Sayuni mpaka mtakapokuwa watu waongofu na Wakristo wazuri. Kabla ya kuchukua jukumu la kuwa wachungaji, mnatakiwa na Mungu mjitenge ninyi wenyewe kutoka katika kuupenda ulimwengu huu. Thawabu ya wale wanaoendelea katika nafasi hii ya kutilia mashaka itakuwa ile wanayopewa waoga na wasioamini. {2T 513.1}

Lakini je! Ni nini sababu ya mashaka haya, giza hili na kutokuamini? Ninajibu: Hawa watu hawako sawa na Mungu. Hawazishughulikii nafsi zao kwa uaminifu na Kweli. Wamepuuzia kukuza uchaji Mungu wa binafsi (utauwa). Hawajajitenga wao wenyewe kutoka katika ubinafsi na kutoka dhambini na kwa wenye dhambi. Wameshindwa kujifunza maisha ya kujikana nafsi, ya kujitoa kafara kwa Bwana wetu na wameshindwa kuiga mfano Wake wa usafi, kujitolea, na kujitoa mhanga. Dhambi ambayo inawazinga kwa urahisi, imeimarishwa kwa kuiendekeza. Kwa uzembe wao wenyewe na dhambi, wamejitenga wenyewe kutoka katika uwepo wa Mwalimu wa mbinguni, na Yeye amesafiri kwa umbali wa siku moja mbele yao. Wanao pamoja nao watu wavivu, walegevu, waliorudi nyuma, wasioamini, wasio na heshima, wasio na shukrani, wasio watakatifu, na wahudumu wao ni, malaika waovu. Kwanini ushangae kwamba hao wako gizani, au kwamba wana mashaka na mafundisho ya Imani ya Biblia? "Mtu akitaka kuyatenda mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafunzo." Atajua kwa hakika kuhusiana na jambo hili. Ahadi hii inapaswa kukimbiza mashaka yote na maswali. Ni kujitenga na Kristo ambako huleta mashaka. Yeye Anafuatwa na mwenye bidii, mnyofu, mkweli, mwaminifu, mpole, mnyenyekevu, na msafi, ambaye malaika watakatifu, waliovaa mavazi maridadi ya mbinguni, huwatakasa, huwaangazia, huwasafisha, na kuwalinda; kwani wanasafiri kwenda mbinguni. {2T 513.2}

Hakuna ushahidi mkubwa unaohitajika kuulizwa ili kujua kuwa mtu yuko mbali sana na Yesu, na anaishi huku akipuuzia kufanya maombi ya siri, kupuuzia ucha Mungu binafsi, pia ni kweli kwamba huzungumza mashaka na kutokuamini, kwa sababu mazingira yake hayapendezi.

Watu kama hao hawana dini safi, ya kweli, isiyo na mawaa ya Kristo. Wana maisha bandia/feki ambayo mchakato wa kusafisha utateketeza kabisa kama pumba. Punde tu Mungu anapowathibitisha, na kuwajaribu imani zao, wanayumba, wanasimama kiudhaifu, wakipepesuka kwanza kuelekea upande mmoja na, kisha mwingine. Hawana nakala halisi ambayo Paulo alikuwa nayo, ambayo inaweza kutoa utukufu katika dhiki kwa sababu “mkijua ya kuwa dhiki kazi yake ni kuleta saburi, na kazi ya saburi ni kuleta uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu.” Wana dini ya matukio/hali ya hewa/mazingira. Ikiwa kote wale wanaowazunguka wana nguvu katika imani na ujasiri katika mafanikio ya mwisho ya ujumbe wa malaika wa tatu, na hakuna mvuto maalum uletwao kushuhudia dhidi yao, basi wanaonekana kuwa na imani kwa kiasi fulani. Lakini mara tu shida inapoonekana kuja katika utumishi wao, na kazi inaenda pole pole sana, na msaada wa kila mtu unahitajika, hizi roho maskini, ingawa zinaweza kushuhudiwa kuwa watumishi wa injili, wanatarajia kila kitu kuwa sifuri. Hawa wanazuia kazi badala ya kusaidia. {2T 514.1}

Uasi ukitokea, na uasi ukadhihirika, hauwasikii wakisema, kwa maneno ya kutia moyo na kushangilia kwa juu: Ndugu, msizimie; iweni hodari. “Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii, Bwana awajua walio Wake.” Watu ambao wanaathiriwa na hali ya hewa au mazingira wanapaswa kubaki majumbani mwao na kutumia nguvu zao za mwili na akili katika nafasi za kuwajibika kidogo ambapo hawatawajibika kukutana na upinzani mkali kama huo. Ikiwa kila kitu kinaendelea vizuri, wanaweza kupasi na kuonekana watu wazuri sana, wenye kujitoa kwa ibada. Lakini hawa sio wale ambao Mwalimu atawatuma kufanya kazi Yake, kwa maana hawa wanapingwa na wajumbe wa Shetani. Pia shetani, na jeshi la malaika zake wabaya, watajipanga dhidi yao. Mungu amewaandalia uwezekano watu aliowaita kufanya kazi Yake, ili waweze kuwa washindi katika kila shindano. Wale wanaofuata mwelekeo Wake hawatakutana na kushindwa. {2T 515.1}

Bwana, akiongea kupitia Paulo, Waefeso 6:10-18, anatuambia jinsi ya kujiimarisha dhidi ya Shetani na wajumbe wake. “Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uweza wa nguvu Zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi haya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga Kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani; na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote, mkitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.” {2T 515.2}

Tunashiriki katika kazi iliyoinuliwa, na takatifu. Wale wanaokiri kuwa wameitwa kufundisha Ukweli kwa wale wanaokaa gizani, hawapaswi kuwa miili ya kutokuamini na giza wao wenyewe. Wanapaswa kuishi karibu na Mungu, ambapo wanaweza kuwa nuru yote katika Bwana. Sababu inayowafanya kutokuwa hivyo ni kwamba hawalitii Neno la Mungu wao wenyewe; kwa hivyo mashaka na kukatishwa tamaa huoneshwa na kutamkwa, wakati maneno ya imani na furaha takatifu tu ndiyo yanapaswa kusikiwa. {2T 516.1}

Ni dini, ndiyo ambayo wachungaji wanaihitaji; uongofu wa kila siku kwa Mungu, maslahi na shauku isiyogawanyika, isiyo na ubinafsi kwa kusudi na kazi Yake. Lazima kuwe na kujidhili, na kuondoa wivu wote, kufikiria mabaya kuhusiana na wengine, husuda, chuki, uovu, na kutokuamini. Mabadiliko kamili yanahitajika. Wengine wamepoteza mtizamo wa Mfano wetu, Mtu wa mateso wa Kalvari. Katika huduma Yake hatuhitaji kutarajia urahisi, heshima, na ukuu katika maisha haya; kwa kuwa Yeye, Mkuu wa mbinguni, haku hayapokea hayo. “Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko.” “Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu: adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; Na kwa kupigwa kwake

sisi tumepona.” Tukiwa na Mfano huu mbele yetu, Je, tutachagua kuachana na msalaba, na kuyumbishwa na mazingira yetu/matukio Je! Bidii yetu, ari yetu, inaamshwa tu wakati tukiwa tunazungukwa na wale ambao wanakesha na wana bidii katika kazi na kusudi la Mungu? {2T 516.2}

Je! Hatuwezi kusimama kwa Mungu, hata mazingira yetu yawe mabaya na ya kukatisha tamaa? “Basi tuseme nini kwa mambo haya? Ikiwa Mungu Yuko upande wetu, ni nani anayeweza kuwa kinyume chetu? Yeye ambaye hakumwachilia Mwanawe Mwenyewe, lakini alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, itawezekanaje Yeye kupitia kwa Mwanaye ashindwe kutupatia vitu vyote bure? Ni nani atakayewashtaki wateule wa Mungu? Mungu Ndiye anayehesabia haki. Ni nani anayehukumu? Ni Kristo aliyekufa, naam, akafufuka tena, ambaye Yuko mkono wa kuume wa Mungu, ambaye pia anatuombea. Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je, ni dhiki, au taabu, au mateso, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa, Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa; tunahesabiwa kama kondoo kwa yule aliyechinjwa. La, katika mambo haya yote sisi ni zaidi ya washindi kupitia Yeye aliyetupenda. Kwa maana nina uhakika, ya kuwa wala mauti, wala uhai, wala malaika, wala enzi, wala mamlaka, wala vitu vilivyopo, wala vitu vijavyo, wala urefu, wala kina, wala kiumbe kingine chochote, hakitaweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.” {2T 517.1}

Wahudumu wengi hawana nia isiyogawanywa katika kazi ya Mungu. Wamewekeza lakini kidogo katika kusudi Lake, na kwa sababu wamewekeza hisa ndogo sana katika kukuza Ukweli, wanajaribiwa kwa urahisi kuihusu na kuhama kutoka kwayo. Hawajathibitishwa, kuimarishwa, na kukaa. Yeye ambaye anayeelewa vizuri tabia yake mwenyewe, ambaye anafahamu dhambi ambayo inatuzinga kwa wepesi, na majaribu ambayo yataweza kumshinda kwa urahisi, hapaswi kujianika bila ya ulazima na kukaribisha majaribu kwa kujiweka chini ya ardhi ya adui. Hata hivyo ikiwa jukumu linamwita mahali ambapo hali sio nzuri, atapata msaada maalum kutoka kwa Mungu, na kwa hivyo atajifunga kwa utayari kwa vita na adui. Ujuzi wa nafsi ya mtu, utawaokoa wengi wasiingie katika vishawishi vikali, na



kuzuia wengi kushindwa vibaya. Ili kujitambua sisi wenyewe, ni muhimu tuchunguze kwa uaminifu nia na kanuni za mwenendo wetu, tukilinganisha matendo yetu na kiwango cha wajibu kinachofunuliwa katika Neno la Mungu. Wachungaji wanapaswa kuhimiza utoaji kwa ukarimu. {2T 517.2}

Nilioneshwa kuwa baadhi ya watu ambao wamekuwa wakifanya kazi katika ofisi zetu za uchapishaji, katika Taasisi zetu za Afya, na katika huduma ya kichungaji, wanafanya kazi kwa ujira tu. Kuna wengine sio watu wa ujira pekee yake; sio wote wana hatia katika suala hili, lakini ni wachache wameonekana kutambua kwamba lazima watoe hesabu ya uwakili wao. Mali ambazo zimewekwa wakfu, ili kusukuma kazi ya Mungu zimefanyiwa ubadhirifu. Familia zilizo katika umaskini, ambazo zilikuwa zimejionea ushawishi wa Ukweli unaotakasa na kwa hiyo waliuthamini na kujisikia wenye shukrani kwa Mungu kwa ajili yake, wamefikiria kwamba wangeweza na wanapaswa kujinyima hata mahitaji ya maisha ili kuleta matoleo yao kwa hazina ya Bwana. Wengine wamejinyima hata mahitaji ya nguo ambazo walihitaji sana ili kujisitiri. Wengine wameuza ng'ombe wao wa pekee na wametoa wakfu kwa Mungu pesa yote waliyoipokea. Kwa uaminifu wa roho zao, na machozi mengi ya shukrani kwa sababu ilikuwa fursa yao kufanya hivyo kwa kazi ya Mungu, wameinama mbele za Bwana na sadaka yao. wakiomba baraka Zake juu yake kama walivyotoa, kuomba kwamba iweze kuwa njia ya kuleta ujuzi wa Kweli kwa roho zilizo gizani. Mali ambazo zimetolewa wakfu kwa namna hii, hazijatumiwa kila wakati kama wafadhili wa kujitolea walivyoniua zitumike. Watu wenye tamaa, wenye ubinafsi, wasio na roho ya kujinyima au kujitolea wenyewe, wameshughulikia pesa hizi kwa njia zisizo za uaminifu zilipoletwa kwenye hazina, na wameiba hazina ya Mungu kwa kupokea mali au fedha ambazo hawakuwa wamepata kwa haki. Usimamizi wao usiotakaswa, uzembe, ufujaji, ubaradhifu na kutawanya mali ambazo zilikuwa zimewekwa wakfu kwa Mungu kwa maombi na machozi. {2T 518.1}

Nilioneshwa kuwa malaika wa kurekodi hufanya rekodi ya uaminifu ya kila toleo la sadaka lililowekwa wakfu kwa Mungu na kuwekwa kwenye hazina, na mwisho wa hazina hizo zilizotolewa. Jicho la Mungu

hutambua kila senti iliyotolewa kwa kazi Yake, na utayari au kusita kwa mtoaji. Nia ya kutoa pia huandikwa. Hao wanaojitoa mhanga, wanaojitolea kumrudishia Mungu vitu ambavyo ni Vyake, kama Yeye anavyotaka kwao, watalipwa kulingana na matendo yao. Ingawa mali zilizowekwa wakfu zitatumiwa vibaya, na hivyo zisitimize lengo ambalo Mtoaji alikuwa nalo kichwani. ---utukufu wa Mungu na wokovu wa roho -- Wale ambao walitoa dhabihu hiyo kwa uaminifu na unyofu wa moyo, na jicho likiwa limekita kwaajili ya utukufu wa Mungu, hawatapoteza thawabu yao. {2T 518.2}

Wale wote ambao wametumia vibaya mali zilizowekwa wakfu kwa Mungu watahitajika kutoa hesabu ya uwakili wao. Baadhi kwa ajili ya ubinafsi wamejichotea ili kukidhi tamaa yao ya kupenda mali. Wengine hawana dhamira yenye kujali; dhamira imeota sugu kutokana na muda mrefu wa kuendekeza uchoyo. Wanavitazama vitu vitakatifu na vyenye umilele kwa mtazamo hafifu. Kutokana na mazoea ya muda mrefu ya kuendekeza uovu, hisia zao za kimaadili zaonekana kupooza. Inaonekana haiwezekani kwao kuinua maoni na hisia zao kwa kiwango kilichoinuliwa kilichoonyeshwa wazi katika Neno la Mungu. Isipokuwa kuna mabadiliko kamili kwa kufanywa upya akili, kundi hili halitapata nafasi mbinguni. Wale ambao wanafuata njia ya ubinafsi na dhambi, bila kuzingatia hata hazina ya Mungu kama takatifu, hawangeweza kuthamini usafi na utakatifu wa utakaso katika ufalme wa mbinguni au thamani ya utukufu mkuu, tuzo ya milele, iliyohifadhiwa kwa washindi waaminifu. Akili zao kwa muda mrefu zimeendeshwa kwa kiwango cha chini cha ubinafsi, hata hawawezi kufahamu vitu vya milele. Hawauthamini wokovu. Inaonekana haiwezekani kuinua akili zao ili kukadiria kwa usahihi mpango wa wokovu au thamani ya upatanisho. Masilahi ya ubinafsi yamegubika mwili wote; kama jiwe la sumaku, limeshikilia akili na mapenzi, likiwafunga kwenda chini. Baadhi ya watu hawa, hawatawahi kufikia ukamilifu wa tabia ya Kikristo kwa sababu hawaoni thamani na umuhimu wa kuwa na ukamilifu huo. Akili zao haziwezi kuinuliwa, ili waweze kushangilia na kuvutiwa na utakatifu huo. Kujipenda na masilahi ya ubinafsi yamepotosha tabia hiyo kiasi kwamba haiwezi kufanywa kutofautisha utakatifu wa milele na maisha ya kawaida. Kazi ya Mungu na hazina Yake sio takatifu kwao kuliko

biashara ya kawaida au mali zilizotolewa kwa malengo ya kidunia. {2T 519.1}

Wajibu katika mwelekeo huu una mashiko kwa wote wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Sheria ya Mungu inabainisha wajibu wao kwa wenzao: "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Kwa kupuuza haki, rehema, na ukarimu kwa jirani zao, wengine wameufanya moyo kuwa mgumu, kiasi kwamba wanaweza kwenda mbali zaidi na hata kumwibia Mungu bila hofu ya dhamiri. Je! Watu hao Wanafunga macho yao na ufahamu wao kwa Ukweli kwamba Mungu anajua, kwamba anasoma kila kitendo na nia iliyowasukuma? Thawabu Yake iko pamoja Naye, na kazi Yake mbele Yake, kumpa kila mtu kadiri ya kazi yake. Kila tendo jema na kila tendo lisilofaa, na ushawishi wake kwa wengine, hufuatwa na Mchunguzaji wa mioyo, ambaye kila siri hufunuliwa. Na thawabu itakuwa kulingana na nia ambayo iliwafanya kutenda {2T 520.1}

Bila kujali maonyo na kurudiwa mara kwa mara ambayo Bwana ameyatuma, wale ambao wamechukua nafasi za uwajibikaji wamefuata njia zao wenyewe na kuongozwa na uamuzi wao wenyewe ambao haujatakaswa, na, kwa sababu hiyo, kazi ya Mungu imeumizwa, na roho zimegeuzwa, kutoka kwenye ile Kweli. Wale wote ambao wana hatia, watakuwa na rekodi ya kuogopesha kukutana nayo katika siku ya malipo ya mwisho. Ikiwa wataokolewa, haitakuwa kwa juhudi yoyote ya kawaida; maisha yao ya zamani, lazima yaonekane kwao na kukombolewa. Ikiwa kazi hii itafanywa kwa uaminifu, na ikifuatiwa kwa uvumilivu na bidii isiyochoka, itafanikiwa kabisa. Lakini wengi hawatafanikiwa kwa sababu unyofu na bidii ambayo wanaanza nayo kazi, inakufa kwasababu ya uvivu na kutojali. Juhudi zao ni sahihi mwanzoni, kwasababu wanakuwa na hekima ya hali zao halisi; lakini wanatafuta kusahau yaliyopita, na kuyapitisha bila kuchukua vizuizi na kufanya kazi kamili. Toba yao sio ya huzuni ya kweli kwamba kupitia ushawishi wao, Mungu amedhalilishwa na roho ambazo Kristo alifia zimepotea. Wanafanya juhudi kwa msimu na wakionyesha hisia kubwa hapa na pale; lakini juhudi hizi zinakoma, na kisha hisia hizi zinakoma, na kisha hufuata ulegevu, na kutojali ambayo huonyesha kwamba Mungu hakuwepo kikamilifu kwenye hii shuguli, hisia zilikuja juu tu kwa

muda, ila kulikuwa hakuna kazi ya kina cha kutosha kubadilisha kanuni ambazo zilitawala matendo yao, wanashawishiwa kuongozwa tena katika njia ile ile mbaya kama walivyokuwa mwanzoni; kwani hawana nguvu ya kuhimili ujanja wa Shetani, bali, wanakuwa watumwa wa hila zake. {2T 520.2}

Maisha ya Mkristo wa Kweli huwa endelevu. Hakuna kusimama au kurudi nyuma. Ni haki yako “Kujazwa maarifa ya mapenzi Yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; mkiwezesha kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu Wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha; mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru” {2T 521.1}

Ninawasihi wote, haswa wale wanaohudumu kwa Neno na mafundisho, kujitolea kikamilifu kwa Mungu. Jitoeni wakfu maisha yenu Kwake, na kwa kweli muwe mfano kwa kundi. Usiridhike tena kukaa mbilikimo katika vitu vya kiroho. Hebu lengo lako lisiwe pungufu ya ukamilifu wa tabia ya Kikristo. Hebu maisha yenu yasiwe ya ubinafsi na yasiyo na lawama, ili yaweze kuwa karipio hai kwa wale ambao wana ubinafsi na ambao mapenzi yao yanaonekana kuwa juu ya hazina yao ya kidunia. Mungu Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, kufanywa imara “Kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo Wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu” {2T 521.2}

## **SURA YA 62**

### **MAZOEZI NA HEWA**

Katika uumbaji wa mwanadamu Bwana Mungu alipanga kwamba anapaswa kuwa mwenye kujishughulisha, utendaji hai na mwenye

manufaa. Walakini wengi wanaishi katika ulimwengu huu kama mashine zisizo na faida, kana kwamba ni wafu. Hawaangazii njia za wengine, si mbaraka kwa yoyote. Wanaishi tu kuwaletea wengine mizigo. Kwa kadiri ushawishi wao kwenye upande wa wema unavyohusika, wao ni kama sufuri tu; lakini wana uzito upande usiofaa. Kwa kuchunguza maisha yao kwa ukaribu sana, ni kwa nadra sana utapata wamevutiwa na tendo la ukarimu usio na ubinafsi. Wanapokufa, kumbukumbu zao hufa nao. Majina yao hufutika haraka sana; kwani hayawezi kuishi, hata katika mapenzi mazuri ya marafiki zao, kwa njia ya wema wa kweli na matendo mema. Kwa watu kama hao, maisha yamekuwa makosa-bahati mbaya. Hawakuwa mawakili waaminifu. Wamesahau kuwa Muumba wao, Naye ana madai juu yao na kwamba Yeye Aliwaumba kuwa hai katika kutenda mema na katika kuwabariki wengine kwa mivuto yao. Masilahi ya ubinafsi huvutia akili na husababisha kumsahau Mungu na kusudi la Muumba wao. Wote wanaokiri kuwa wafuasi wa Yesu, wanapaswa kujua kwamba jukumu liko juu yao kuhifadhi miili yao katika hali bora ya afya, ili akili zao ziwe wazi kuelewa vitu vya mbinguni. Akili inahitaji kudhibitiwa, kwani ina ushawishi mkubwa juu ya afya. Fikra mara nyingi hupotosha, na zikiendekezwa, huleta aina kali za ugonjwa kwa muathiriwa. Wengi hufa kwa magonjwa ambayo ni ya kufikiria tu. Ninawajua watu kadhaa ambao wamejiletea magonjwa halisi na ushawishi wa mawazo. {2T 522.2}

Dada mmoja alibebwa na mumewe kutoka kitini hadi kitandani, na kutoka chumba hadi chumba, kwa sababu alifikiri kuwa alikuwa dhaifu sana kuweza kutembea. Lakini kesi hiyo ilipowasilishwa kwangu baadaye, aliweza kutembea kama mimi mwenyewe ikiwa angefikiria hivyo. Ikiwa ajali ingelitokea, --- ikiwa nyumba ilishika moto na kuungua, au mmoja wa watoto wake angekuwa katika hatari ya kupoteza maisha kwa kuanguka, - mwanamke huyu angeamshwa na nguvu ya 'hali halisi', na angeweza kutembea kwa utayari na kwa haraka; Angeweza kutembea, kwa kadiri nguvu ya mwili ilivyohusika; lakini mawazo yenye kuugua, yalimpelekea kuhitimisha kuwa hakuweza, na hakuamsha nguvu ya hisia kupinga udanganyifu huu. Mawazo yalisema 'Hauwezi kutembea, na ingekuwa bora usijaribu'. Kaa kimya; viungo vyako ni dhaifu hata huwezi kusimama. Laiti dada huyu

angekuwa ametumia nguvu yake ya dhamiri na kuamsha ari yake na nguvu zake zilizodhoofu, udanganyifu huu ungefichuliwa. Kwa sababu ya kujitoa kwa mawazo, labda anafikiria, hadi leo, kwamba wakati alikuwa mnyonge alikuwa wa muhimu sana; lakini hii ilikuwa kituko cha mawazo, ambayo wakati mwingine hucheza kwa ujanja wa ajabu juu ya binadamu wagonjwa, wasio na umilele. {2T 523.1}

Wengine wanaogopa sana hewa kiasi kwamba wanajigubika nguo nyingi vichwani na miilini mwao hadi waonekane kama miili yenye sanda za mafarao wa Misri waliokuwa wanawekwa kwenye makaburi yao ya mapiramidi (mummies). Wanakaa ndani ya nyumba, kwa ujumla hawafanyi kazi, wakiogopa watajichosha na kuugua ikiwa watafanya mazoezi iwe ndani au nje kwenye hewa safi. Wangeweza kufanya mazoezi kama mazoea ya kawaida, katika hewa ya wazi kila siku ya kupendeza, ikiwa wangedhani tu hivyo. Kuendelea kutokuwa na mazoezi ni moja wapo ya sababu kubwa za kudhoofika kwa mwili na udhaifu wa akili. Wengi ni wagonjwa ambao wanapaswa kuwa na afya nzuri sana na kumiliki baraka moja tajiri zaidi ambayo wangeweza kufurahia. {2T 523.2}

Nimeonyeshwa kuwa wengi ambao ni dhaifu, na wanaolalamika kila wakati, hawana hali mbaya sana kama wanavyofikiria wenyewe. Baadhi yao wana nia ya nguvu, ambayo, ikitumika katika mwelekeo sahihi, itakuwa njia nzuri ya kudhibiti mawazo na hivyo kuzuia magonjwa. Lakini hutokea mara kwa mara kwa mapenzi kuelekezwa katika upande usio sahihi na kwa ukaidi, wao hukataa kutenda kwa hekima. Yale mapenzi/nia ndiyo yanayofanya maamuzi. Wanakuwa vilema na dhaifu, na umakini wa watu wadhaifu ndiyo wanapewa, hata bila kujali maoni ya watu wengine. {2T 524.1}

Nimeonyeshwa akina mama ambao wanatawaliwa na mawazo ya ugonjwa, ushawishi wake pia huwa juu ya mume na watoto. Madirisha lazima yafungwe, kwa sababu mama anahisi baridi. Kama yeye anahisi baridi hata kidogo tu, na mabadiliko yamefanywa katika mavazi yake, anafikiria watoto wake lazima wafanyiwe vivyo hivyo, na kwa hivyo familia nzima hunyanganywa nguvu, na hivyo hudhoofu katika nguvu

ya mwili. Wote wameathiriwa na akili moja, wameathiriwa kimwili na kiakili kupitia mawazo ya magonjwa ya mwanamke mmoja, ambaye anajiona ni kigezo au kipimo cha familia nzima. Mwili umevikwa kulingana na mambo ya mawazoni tu ya 'ugonjwa' na hushindiliwa juu yake na manguo mengi ambayo hudhoofisha mfumo wa mwili. Ngozi haiwezi kutekeleza kazi yake; tabia aliyojifunza ya kukwepa hewa na kuepuka mazoezi, hufunga vitundu vyake vya ngozi. Vijitundu hivyo vidogo ambavyo mwili hupumua, - hufanya kuwe na ugumu wa kutoa uchafu kupitia vitundu hivyo. Mzigo wa kazi hutupwa kwenye ini, mapafu, figo, nk, na hivi viungo vya ndani vinalazimika kufanya kazi ya ngozi. Kwa hivyo watu hujiletea magonjwa kwa mazoea yao mbaya; Walakini, mbele ya nuru na maarifa, wanazingatia mwenendo wao wenyewe. Wanawaza hivi: 'Je! Hatujajaribu jambo hili? Na je, hatulielewi hili kwa uzoefu?' Lakini uzoefu wa mtu ambaye mafikra yake ni makosa, haupaswi kuwa na uzito sana kwa mtu yeyote. {2Tsw 524.2}

Msimu unaohofiwa zaidi na mtu anayeenda kati ya wadhoofu hawa ni msimu wa baridi na barafu. Ni majira ya baridi kweli kweli, siyo nje tu, lakini ndani, kwa wale ambao wanalazimika kuishi katika nyumba moja na kulala katika chumba kimoja. Waathiriwa hawa kwa mawazo ya ugonjwa, hujifungia wenyewe ndani na kufunga madirisha, kwa kufikiri hewa iliyomo ndani huathiri mapafu yao na vichwa vyao. Fikra zinafanya kazi; wanatarajia kupata magonjwa ya baridi kama mafua, na kikohozi na flu, basi watakuwa nayo. Hakuna idadi ya hoja inayoweza kuwafanya waamini kwamba hawaelewi falsafa ya jambo zima. Je! Hawajathibitisha? Watabishana kwa hoja hiyo. Ni kweli kwamba wamethibitisha upande mmoja wa swali, - kwa kuendelea katika msimamo wao wenyewe, - na bado wanapata magonjwa ya baridi ikiwa mwili umepata hewa kidogo tu. Mwili wao teke teke kama watoto wachanga, hawawezi kuvumilia chochote; ila bado wanaishi, na wanaendelea kufunga madirisha na milango, na kukaa kwa bidii karibu na jiko ili waote moto, wa kufurahia shida yao. Hakika wamethibitisha kwamba mwenendo wao haujasaidia wapone, lakini umeongeza shida zao. Kwa nini hawataruhusu busara kushawishi maamuzi yao na kudhibiti mawazo? Kwa nini sasa usijaribu njia tofauti, na kwa njia ya busara upate mazoezi na hewa nje ya jengo, badala ya kukaa ndani ya

nyumba siku hadi siku, kama kifungu cha bidhaa kavu kuliko kiumbe hai? {2Tsw 525.1}

Sababu kuu, kama sio sababu ya pekee, ya kwa nini wengi huathiriwa na kuwa na ulema, ni kwamba damu haizunguki kwa urahisi, na mabadiliko katika mfumo wa damu, mitoki na maji, ambayo ni muhimu kwa maisha na afya, Havifanyiki. Hawaipei miili yao mazoezi au mapafu chakula, ambayo ni, hewa safi; kwa hivyo haiwezekani kwa damu kuwa na nguvu, na hivyo hupita kwa unyonge kwenye mfumo. Kadri tunavyofanya mazoezi, ndivyo tunafanya mzunguko mzuri wa damu. Watu wengi hufa kwa kukosa mazoezi, kuliko kwa kuwa na uchovu wa kupita kiasi; wengi zaidi miili yao hula kutu kuliko kuchakaa. Wale ambao wamezoea kujifanyia mazoezi katika hewa ya wazi kwa ujumla wanakuwa na mzunguko wa damu mzuri na wenye nguvu. Sisi ni tegemezi zaidi juu ya hewa tunayopumua kuliko juu ya chakula tunachokula. Wanaume na wanawake, vijana kwa wazee, ambao wanatamani afya, na ambao watafurahia maisha ya kazi, wanapaswa kukumbuka kuwa hawawezi kuwa nayo haya, bila kuwa na mzunguko mzuri wa damu. Shuguli yoyote wanayoifanya na mwelekeo wao, wanapaswa kuamua kufanya mazoezi katika hewa ya wazi kadri wawezavyo. Wanapaswa kuhisi ni jukumu la kidini kushinda hali mbovu za kiafya ambazo zimewafanya wazuiliwe ndani ya nyumba, kunyimwa mazoezi nje ya uwanja wenye hewa huru. {2Tsw 525.2}.

Baadhi ya watu walioathirika na baridi huwa wanashindwa kusadikishwa umuhimu mkubwa wa mazoezi ya kila siku ya nje, ambapo wanaweza kupata hewa safi ya kutosha. Kwa kuhofia kupata mafua au kikohozi, hukaa bila mazoezi, wakikazana mwaka hadi mwaka, katika njia yao wenyewe na kuishi katika mazingira ya kuwa na afya mbaya na kukosa nguvu. Haiwezekani kwa watu hawa kuwa na mzunguko mzuri wa damu. Mfumo mzima hudhoofu kwa kukosa mazoezi na hewa safi. Ngozi inakuwa dhaifu na huhisi zaidi mabadiliko yoyote katika mazingira. Mavazi ya ziada huvaliwa, na joto la chumba huongezwa. Siku inayofuata wanahitaji kuongeza joto kidogo, na mavazi kidogo ili kuhisi joto kabisa, na kwa hivyo huwa wanaendekeza kila hisia inayobadilika hadi huwa na nguvu kidogo ya kuvumilia baridi yoyote. Wengine wangeweza kujiuliza: "Je! tufanyaje? Je! Ungetaka sisi tuendelee kuwa na baridi?" Ukiongeza mavazi, hebu yawe kidogo tu, na



ufanye mazoezi, ikiwa inawezekana, ili kupata tena joto unalohitaji. Ikiwa hamuwezi kushiriki katika mazoezi makali, kokeni moto; lakini mara tu mnapopata joto, vueni mavazi yenu ya ziada na ondokeni kwenye moto. Ikiwa wale wanaoweza, watashiriki katika kazi fulani kuchukua mawazo kutoka kwao, kwa jumla wangesahau kuwa walikuwa wanasikia baridi na hawatapata madhara. Unapaswa kupunguza joto la chumba chako mara tu unapopata joto lako la asili. Kwa watu ambao wana mapafu dhaifu na ulema, hakuna kitu kinachoweza kuwa kibaya kuliko mazingira yenye joto kali. {2Tsw 526.1}

Walemavu wasiofuata kanuni za afya mara nyingi hujinyima mwanga wa jua. Hii ni moja ya mawakala wazuri sana wa uponyaji wa asili. Ni tiba rahisi sana, kwa hivyo haipo kwenye fasheni kwao kuizoea na kuipenda, kuifurahia miale ya jua la Mungu na kuipamba nyumba yetu na uwepo wake. Fasheni au mitindo huchukua usumbufu mkubwa zaidi kuwatenga watu na nuru ya jua sebuleni na vyumbani mwa kulala kwa kushusha mapazia na kufunga shata za madirisha, kana kwamba miale yake ni mibaya kwa maisha na afya. Sio Mungu ambaye ametuletea ole nyingi ambazo wanadamu tunazirithi. Upumbavu wetu wenyewe umesababisha sisi kujinyima vitu vyenye thamani, baraka ambazo Mungu ametoa na ambazo, ikiwa zinatumwa vizuri, zina thamani isiyo na kifani katika kurejesha afya. Ikiwa mngependa nyumba zenu kuwa nzuri na za kuvutia, mzifanye ziwe zenye kung'aa na hewa na mwangaza wa jua. Ondoa mapazia yako mazito, fungua madirisha, ondoa vidhibiti mwanga, na ufurahie mwangaza wa jua, hata ikiwa ni kwa gharama ya mwanga wa jua kupausha rangi ya mazulia yako. Jua la thamani linaweza kufifisha rangi ya mazulia yako, lakini litatoa rangi yenye afya kwenye mashavu ya watoto wako. Ikiwa mna uwepo wa Mungu na mna mioyo yenye bidii, yenye upendo, nyumba ya unyenyekevu iliyong'arishwa na hewa na mwangaza wa jua, na ucheshi unaokaribisha ukarimu usio na ubinafsi, mtakuwa katika familia yenu, na kwa msafiri aliyechoka, mbingu ya hapa duniani. {2Tsw 527.1}

Wengi wamefundishwa tangu utoto kuwa hewa ya usiku ni mbaya kwa afya na hivyo ni lazima wasiingize kwenye vyumba vyao. Kwa kujiumiza kwao wenyewe hufunga madirisha na milango yao ya

vyumba vya kulala, kujikinga na hewa ya usiku ambayo wanasema ni hatari sana kwa afya. Katika hili wamedajinganya. Wakati wa baridi ya jioni, inaweza kuwa muhimu kujilinda kutokana na ubaridi kwa mavazi ya ziada, lakini wanapaswa kuyapa mapafu yao hewa. {2Tsw 527.2}

Jioni moja ya vuli, wakati mmoja tulikuwa tukisafiri katika gari iliyojaa, ambapo hewa iliyokuwa inasambaa ilikuwa mbaya sana kutokana na kuchanganyika kwa pumzi nyingi. Pumzi kutoka kwa mapafu na miili ilisababisha hisia mbaya zaidi kuja juu yangu. Nilifungua dirisha langu na nilikuwa nikifurahia hewa safi, wakati mwanamke mmoja kwa dhati na bidii, alisihi kwa sauti, akisema: "Usifungue dirisha hilo. Utapata baridi na kuwa mgonjwa, kwani hewa ya usiku si nzuri kiafya. "Nilimjibu:" mama, hatuna hewa nyingine, ndani ya gari hili au nje yake, isipokuwa hewa ya usiku. Ukikataa kuvuta hewa ya usiku, basi bora uache kupumua. Mungu amewapatia viumbe wake hewa ya kupumua mchana, na hiyo hiyo hewa, ilifanyika baridi kidogo, kwa usiku. Usiku haiwezekani kwako kupumua chochote isipokuwa hewa ya usiku. Swali ni: Je! Hewa ya usiku tunayopumua itakuwa safi, au imeboreshwa baada ya kuwa imepumuliwa toka puani mwetu tena na tena? Je! Ni kwa afya yetu kupumua hewa ya usiku iliyochafuliwa ya gari hili? Pumzi zilizotolewa nje na mapafu na miili ya wanaume waliojiloeka kwenye tumbaku na pombe, huchafua hewa na kuhatarisha afya. Na bado karibu abiria wote huketi kama wasiojali kana kwamba wanavuta pumzi safi zaidi ya mazingira. Mungu ametupatia busara, kwamba usiku tupumue hewa ya usiku, na jua lichwapo, hewa ya siku. Ikiwa tunashindwa kufuata mpango wa Mungu, na damu ikawa isiyo safi, makosa ni yetu na mazoea yetu mabaya yameifanya hali iwe hivi. Lakini hewa ya usiku, inayovutwa usiku, yenyewe tu pekee, haitaleta sumu kwa maisha ya mwanadamu. Wengi wanaugua magonjwa kwa sababu wanakataa kupokea ndani ya vyumba vyao usiku, hewa safi ya usiku. Hewa ya bure, safi ya mbinguni ni moja wapo ya baraka tajiri zaidi tunazoweza kufurahia. {2Tsw 527.3}

Baraka nyingine ya thamani ni mazoezi sahihi. Kuna watu wengi wasio na nguvu, na wavivu, wasio na kazi ambao hawapendi shughuli za mwili au mazoezi kwa sababu yanawachosha. Je, inakuwaje mazoezi yanawachosha? Sababu mazoezi kuwachosha ni kwamba

hawaimarishi misuli yao kwa kufanya mazoezi, kwa hivyo huwa na nguvu kidogo. Wanawake na wasichana walemavu wanafurahi zaidi kujishughulisha na kazi ndogondogo kama kushona, au kutarizi, au kuweka mapambo, kuliko kufanya kazi za kuchosha mwili. Ikiwa watakuwa na afya, hawapaswi kuacha mazoezi ya mwili; kwani kwa hilo wataongeza udhaifu wa misuli na unyonge. Ufungue au ubane mkono wako mmoja na ubaki bila kazi, hata kwa wiki chache, kisha uuachilie, na utagundua kuwa ni mdhaifu kuliko ule ambao umekuwa ukiutumia wakati ule mwingine ulipokuwa umefungwa. Kutokuwa na shughuli hutoa athari sawa kwenye mfumo mzima wa misuli. Damu haiwezi kuwa na nguvu kuweza kuondoa uchafu kama ambavyo ingekuwa mzunguko wa kazi yake ungehamasishwa na mazoezi. {2Tsw 528.1}

Pale hali ya hewa inaporuhusu, wote wanaoweza kufanya mazoezi wanapaswa kutembea uwanjani kila siku kwenye hewa iliyo wazi, majira ya joto na majira ya baridi. Lakini mavazi yanapaswa kufaa kwa mazoezi, na miguu inapaswa kulindwa vizuri. Kutembea, hata iwe ni wakati wa msimu wa baridi ya theluji, kutaleta faida zaidi kwa afya kuliko dawa yoyote ile madaktari wanayoweza kuagiza. Kwa wale ambao wanaweza kutembea, kutembea ni bora kuliko kuendesha farasi/gari. Misuli na mishipa ya damu huwezesha kutekeleza kazi yao vizuri. Kutakuwa na nguvu iliyoongezeka, ambayo ni muhimu sana kwa afya. Mapafu yatakuwa na kazi inayohitajika, kwani haiwezekani kwenda nje katika hewa ya kupunga ya msimu wa baridi asubuhi, bila kuchochea mapafu kufanya kazi yanavyotakiwa. {2Tsw 529.1}

Utajiri na uvivu au kukaa bila kazi, hufikiriwa na wengine kuwa baraka za kweli. Lakini wakati watu wengine wamepata utajiri, au kuurithi bila kuutarajia, tabia zao utendaji hai wa kazi zimeachwa, hawashuguliki na chochote katika muda waliopewa, wanaishi maisha ya kivivu, na faida au manufaa yao yanaonekana yamekoma; wanakuwa wasio na utulivu, wenye wasiwasi, na wasio na furaha, na maisha yao hivi karibuni yanaisha. Wale ambao huwa na shughuli nyingi, na huenda kwa ucheshi kuyafanya majukumu yao ya kila siku, ndio wenye furaha na afya zaidi. Mapumziko na utulivu wa usiku huleta kwenye miili yao iliyochoka, usingizi mzito. Bwana alijua ni kipi kilikuwa bora kwa furaha

ya mwanadamu wakati akimpa kazi ya kufanya. Adhabu ambayo ilitajwa kwamba lazima mwanadamu atolee jasho mkate wake, na ahadi ya furaha ya baadaye na utukufu, ilikuja kutoka kiti hicho hicho cha enzi. Zote ni baraka. Wanawake wa mitindo hawana thamani kwa kila mwisho mzuri wa maisha ya mwanadamu. Wana mwamko kidogo wa tabia bora, wana ujasiri mdogo wa maadili au nguvu za mwili. Lengo lao kubwa ni kuangaliwa, kwamba watu washangae kuhusu wao na kusifiwa. Wanakufa mapema na hakuna anayewakumbuka, (au kuwamiss/kuwakosa/kuwatafuta) kwa maana hawajambariki mtu yeyote. {2Tsw 529.2}

Mazoezi husaidia kazi ya umeng'enywaji wa chakula. Kwa kutembea nje baada ya kula, nyoosha kichwa chako kwa kuinua shingo, rudisha nyuma mabega, na fanya mazoezi ya wastani, itakuwa faida kubwa kubwa. Akili itaelekezwa kutoka kwa ubinafsi, na kwenda kwenye uzuri wa asili. Akili ikiwa na umakini mdogo kwa tumbo baada ya kula, ni bora zaidi. Ikiwa una hofu ya kila wakati kwamba chakula chako kitakuumiza, hakika itakuwa hivyo. Sahau nafsi yako au ubinafsi, na fikiria kitu cha kuchangamsha. {2Tsw 530.1}

Wengi hufanyia kazi wazo potofu kwamba ikiwa wamepata baridi au magonjwa ya baridi kama vile kikohozi, au mafua, basi ni lazima waachane na hewa ya nje kwa uangalifu na kuongeza joto la chumba chao mpaka kiwe na joto la kupita kiasi. Mfumo unaweza kuharibika kwa kuondoka nje ya utendani kazi wa kawaida, vitundu-hewa hufunikwa na taka, na viungo vya ndani vinateseka zaidi au kwa uchache kwa joto na kukereka, kwa sababu damu imepata baridi na kumwagwa chini zaidi ya Ngozi. Kwa wakati huu ukilinganisha na mida yote, mapafu hayapaswi kunyimwa hewa safi na nzuri. Kama hewa safi inapaswa kuhitajika basi ni wakati sehemu yoyote ya mfumo wa mwili kama mapafu au tumbo umepata shida. Mazoezi yaliyofanyiwa maamuzi vizuri huchochea damu juu ya viungo hivi na kuvipa ahueni. Mazoezi ya kasi, lakini sio ya kuumiza mwili, kwenye hewa ya nje na uchangamfu wa roho, yatakuza mzunguko wa damu, yakifanya ngozi inawiri/kung'aa, na kutuma damu iliyoimarishwa na hewa safi, hadi miisho ya viungo-miguu na mikono. Tumbo lenye magonjwa litapata unafuu kwa mazoezi. Madaktari mara kwa mara wanashauri watu

wanaohisi kuumwa na wadhoofu kutembelea nchi za kigeni, kwenda kwenye chemchemi au kutembea baharini, ili kurejesha afya. Wakati ambapo, katika kesi tisa kati ya kumi- 9/10, endapo wangekula kwa kiasi na kushiriki mazoezi ya afya na roho iliyochangamka, wangeweza kurudisha tena afya na kuokoa muda na pesa [nchini mwao!] Mazoezi, na matumizi ya bure na mengi ya hewa na jua, --- ni baraka ambazo Mbingu zimewapa wanadamu wote bure, - hutoa uhai na nguvu kwa wadhaifu waliokonda. {2Tsw 530.2}

Idadi kubwa la wanawake wameridhika kuzunguka-zunguka kwa muda mrefu karibu na jiko, wakivuta hewa isiyo safi kwa nusu au robo tatu ya wakati, hadi ubongo unapopata moto, na nusu yake kuathirika kwa kupumbazwa. Wanahitaji kwenda nje, na kufanya mazoezi hata ingawa shuguli zingine ndani ya nyumba zitapuuzwa. Wanahitaji hewa baridi ili kutuliza akili zilizovurugwa. Hawana haja ya kwenda kwa majirani zao kusengenywa, lakini wanapaswa kuwa na malengo ya kufanya mambo mema, kufanya yale ambayo mwisho wa siku yanakuwa na faida kwa wengine. Kisha watakuwa mfano kwa wengine na kupokea faida halisi wao wenyewe. {2Tsw 531.1}

Afya kamili inategemea mzunguko mzuri wa damu. Tahadhari maalum inapaswa kutolewa kwa viungo vilivyo mwisho mwa mwili, yaani miguu na mikono (ivikwe vizuri katika maeneo ya kifuani na viungo vya mbali/juu ya moyo-mikono, miguu, kichwa) kiasi kikubwa cha joto huwemo. Wazazi wanaowavalisha watoto wao nguo fupi au zinazokaribiana na hivyo, wanatoa kafara afya na maisha ya watoto wao katika mitindo ya maisha isiyofaa. Ikiwa sehemu hizi hazipati joto kama lililo mwilini, mzunguko wa damu hautokuwa sawa. Kama viungo hivi vya mwishoni, ambavyo viko mbali na viungo muhimu visipovikwa vizuri, damu huelekea kichwani, na kusababisha maumivu ya kichwa au kutokwa na damu puani, au kubana kwa kifua, kutoa kikohozi au mapigo ya moyo kwenda mbio, kwa sababu ya damu nyingi ndani ya maeneo husika; au tumbo lina damu nyingi, na kusababisha mmeng'enyo mbovu wa chakula. {2Tsw 531.2}

Ili kufuata mitindo, akina mama huvalisha watoto wao magauni mafupi na miguu inakuwa karibu uchi; na damu hupozwa kutoka kwenye asili

yake na kumwagwa kwenye viungo vya ndani, kuathiri mzunguko na kuzalisha magonjwa ndani ya mwili. Miguu haikuumbwa na Muumba wetu kuvumilia kuwa wazi, kama ulivyo uso. Bwana Mungu aliupa uso mfumo wa mzunguko wa damu ulio mkubwa sana, kwa sababu lazima uwe wazi. Yeye Alitoa, pia, mishipa mikubwa na neva kubwa za miguu na nyayo, kuwa na kiasi kikubwa cha kubeba mkondo wa maisha ya mwanadamu, ili miguu iweze kuwa sawa na joto kama la mwili. Vinapaswa kuvikwa vizuri sana ili kupeleka damu kwenye viungo vya mwishoni mwa mwili-miguu na mikono. Shetani amevumbua na kubuni mitindo ya mavazi, ambayo huiacha miguu baridi na wazi, na kuleta ubaridi kwenye mkondo wa maisha tofauti na uasili wake. Na wazazi wanasujudu kwenye hekalu la mitindo na kuwavika watoto wao hivi kwamba misuli na mishipa husinyaa na kufanya kazi kwa utofauti na kusudi la Mungu alivyoiumba. Matokeo yake ni miguu na mikono kuwa daima huwa na baridi sana. Wazazi wote ambao hufuata mitindo badala ya busara watatoa hesabu kwa Mungu kwa kuwanyang'anya watoto wao afya. Hata maisha yenyewe hutolewa dhabihu kwa muungu wa mitindo. {2Tsw 531.3}

Watoto ambao wamevikwa kulingana na mitindo hawawezi kuvumilia kukaa katika mazingira ya wazi isipokuwa kama hali ya hewa sio kali. Kwa hivyo wazazi na watoto hubaki kwenye vyumba vyenye hewa isiyo safi, wakiogopa mazingira nje ya nyumba; kwasababu ya mitindo yao ya mavazi. Ikiwa wangevaa wenyewe kwa busara, na kuwa na ujasiri wa kimaadili kuchukua msimamo wao upande wa haki, wasingetahatarisha afya kwa kwenda nje, katika majira ya joto na majira ya baridi, na kufanya mazoezi kwa uhuru uwanjani kwenye hewa huru. Lakini ikiwa wataachwa bila kusumbuliwa katika maisha yao, wengi hivi karibuni wangekamilisha mchakato wa kujitoa kafara kwa maisha yao wenyewe, na ya watoto wao. Na wale ambao wanalazimika kuwauguza huwa wagonjwa na kuteseka. Mlemavu ambaye anatawaliwa na mawazo anapaswa kuogopwa. Wote wanaoishi katika nyumba pamoja naye wanakuwa dhaifu. Mume hupoteza nguvu zake za neva, na kuwa mgonjwa kwa sababu, kwa wakati mwingi, ameporwa na mkewe, hewa muhimu ya mbinguni. Maskini watoto! Hawa ndio wanaoteseka zaidi, maana wanafikiri kwamba mama anajua vyema kilicho sahihi. Njia mbaya ya mama imemdhoofisha mwenyewe, na,

akiisikia baridi, yeye hujirundikia mitandio zaidi, na hufanya hivyo kwa watoto pia, akidhani kwamba lazima pia wao wawe na baridi. Milango na madirisha vimefungwa, na joto la chumba limeongezeka.

Watoto mara nyingi wamekonda na dhaifu, na hawana kiwango cha juu cha maadili. Mume na watoto wamefungwa kwa msimu wa baridi, watumwa wa dhana za mwanamke anayedhibitiwa na mawazo ya kufikirika, na wakati mwingine anakuwa na msimamo usiotaka kubadilika. Wanafamilia kama hawa ni wafia dini wa kila siku. Wameitoa afya mhanga, kwa kuitikia mabadiliko katika mawazo ya mwanamke mlalamishi, na mwenye kunung'unika. Wananyimwa, kwa kiwango kikubwa, hewa, ambayo itawapa nguvu na kuwapa nishati na uhai. {2Tsw 532.1}

Wale ambao hawatumii mikono na miguu yao kila siku wataona udhaifu wakati watakapojaribu kufanya mazoezi. Mishipa ya damu na misuli haviko katika hali ya kufanya kazi yao na kuweka mwili wote hai katika hatua ya kiafya, ili kila kiungo kiweze kufanya kazi katika mfumo wake. Miguu huwa imara na yenye nguvu inapofanya kazi. Mazoezi ya wastani kila siku yataipa uimara misuli ambayo bila mazoezi huwa legelege, hutepeta na kudhoofika. Kwa kufanya mazoezi kila siku katika maeneo ya wazi yenye hewa ya kutosha, ini, figo na mapafu pia vitakuwa imara katika kufanya kazi zao. Usaidie mwili wako kukuza uwezo wa maamuzi, utakaoweza kukabili baridi na kutoa nguvu kwa mfumo wa fahamu. Kwa muda mfupi utatambua manufaa ya mibaraka ya kufanya mazoezi na hewa safi ambapo huwezi kuishi bila kuwa nayo. Mapafu yako, yakikosa hewa yatakuwa kama mtu aliye na njaa ya chakula. Hakika, tunaweza kuishi kwa muda mrefu bila chakula, kuliko bila hewa, ambacho ndicho chakula MUNGU alichotoa kwa mapafu yetu. Hivyo usichukulie hewa kama adui yako, bali mbaraka wa thamani kutoka kwa MUNGU. {2Tsw 533.1}

Ikiwa walemavu wanakubali kujifariji kuwa ni wagonjwa mawazoni mwao, hawatapoteza tu nguvu yao wenyewe, lakini watawavunja moyo wale ambao wanawatunza. Nawashauri wanawake walemavu wenye mazoea ya kuvaa nguo nyingi kuzipunguza taratibu, pale inapobidi, ili mwili upate hewa. Wengi kati yenu mnaishi kwaajili ya kula na kupumua tu na kufeli kusudi la Mungu la kuwaumba. Mnapaswa kuwa

na lengo Madhubuti lililoinuiliwa katika maisha yenu na kutafuta kuwa wa manufaa na kuwa wa kutegemeka katika familia yako na kuwa wenye manufaa kwa jumua, kwa ujumla. Haupaswi kuhitaji umakini wa familia kukuangalia wewe tu, wala wewe kupenda kukaribisha huruma za wengine. Fanya sehemu yako katika kutoa upendo na huruma kwa wahitaji, ukikumbuka kwamba wao pia wana huzuni na majaribu yao wenyewe. Angalia haya, na ikiwa huwezi kuyafanya, basi kwa maneno ya huruma na upendo, punguza mizigo yao. Kwa kuwabariki wengine, utagundua unapata baraka wewe mwenyewe pia. {2Tsw 533.2}

Kwa wale ambao kwa kadiri iwezekanavyo, wanajishughulisha na kazi njema kwa wengine, kwa kuwasaidia wengine kwa shauku, na upendo kwa vitendo, hii siyo tu itawaondolea magonjwa katika maisha ya bindamu wenzao tu, na kuwapunguzia mizigo ya maisha, lakini pia itawaponya na kurudisha afya ya mioyo, roho na miili yao wenyewe.. Kutenda wema ni kazi yenye faida kwa wote, mtoaji na mpokeaji. Ukisahau umimi/ubinafsi wa maslahi yako kwaajili ya wengine, wewe utapata ushindi juu ya udhaifu wako. Kuridhika utakakopata katika kutenda mema kwa wengine kutakusaidia kwa kiasi kikubwa katika kurejesha akili yako kutoka katika fikira za ugonjwa. Raha ya kufanya mema huleta uhai kwenye akili na mwangwi huu huenda kwenye mwili mzima. Wakati nyuso za watu wema zikiangazwa na uchangamfu, na sura zao zikionyesha mwinuko wa maadili ya akili, wale watu wabinafsi, bahili na wachoyo watakata tamaa, watainama chini, na watakuwa na huzuni. Kasoro zao za kimaadili zitaonekana katika nyuso zao. Ubinafsi na kujipenda wenyewe kutaonekana kwa muhuri wa matendo yao ya nje. Mtu huyo ambaye anashawishiwa na ukarimu usio na ubinafsi wa kweli, ni mshiriki wa asili ya Kiungu, akiwa ameokoka kutoka katika ufisadi ulio katika ulimwengu kupitia tamaa, wakati wenye ubinafsi na wenye uchoyo wameutunza ubinafsi wao mpaka umekausha huruma zao za kijamii, na nyuso zao zinaonyesha picha ya adui aliyeanguka, badala ya ule usafi na utakatifu. {2Tsw 534.1}

Watu wenye walemavu na wagonjwa, ninawashauri kujitosa kwa jambo hili. Kuza uwezo wako wa kufanya maamuzi, na angalau fanya jaribio la jambo hili. Ondoa mawazo yako kutoka kujipenda mwenyewe. Tembea nje kwa imani. Je! Una mwelekeo wa kuweka mawazo yako juu yako,



kuogopa kufanya mazoezi, na kuogopa kwamba ukitoka nje katika hewa utapoteza maisha yako; pinga mawazo haya na hisia. Usikubali kujisalimisha kwa mawazo yako ya ugonjwa. Kama ukishindwa katika jaribu hili, kinachoweza kutokea ni kufa tu. Na itakuwaje kama Ukifa? Heri Maisha ya mtu mmoja yapotee kuliko wengi watolewe kafara. Matakwa na maoni ambayo wewe huthamini, sio tu huharibu maisha yako mwenyewe, lakini huumiza wale ambao maisha yao ni ya thamani zaidi kuliko yako. Lakini njia tunayopendekeza kwenu, haitawanyima kufurahia maisha au kuwadhuru. Mtapata faida kutoka kwake. Hampaswi kuwa wenye harara au wazembe; anzeni kwa wastani mwanzoni kuwa na hewa zaidi, na mazoezi, na endeleeni kupata nguvu hadi mtakapokuwa wenye manufaa, na mbaraka kwa familia zenu na kwa wote wanaowazunguka. Ruhusu uamuzi wako usadiki kuwa mazoezi, mwanga wa jua, na hewa ni baraka ambazo Mbingu imetoa kuwafanya wagonjwa wawe wazima na kutunza afya wale ambao sio wagonjwa. Mungu hakunyimi hizi baraka za bure, ulizopewa na Mbingu, lakini wewe umejiadhibu kwa kufunga milango yako dhidi yake. Zikitumiwa vizuri, mawakala hawa rahisi lakini wenye nguvu, watasaidia mwili kushinda shida za kweli, ikiwa zipo, na zitatoa mionjo mizuriya afya, kwa akili na nguvu kwa mwili. {2Tsw 534.2}

Katika zama hizi za ulimwengu, ambazo wanaume na wanawake wanadhibitiwa na uovu na mitindo, Wakristo wanapaswa kuwa wahusika wema na sehemu kubwa ya busara. Ikiwa ndivyo ilivyokuwa, sura ambazo sasa zimejaa huzuni, zenye alama za ugonjwa na ufisadi, zitakuwa na matumaini na uchangamfu, zikiangazwa na wema wa kweli na dhamiri safi. {2Tsw 535.1}

Mfumo wa kukaa bila kufanya chochote ni laana kubwa zaidi ambayo imeangukia kwa jamii yetu ya wanadamu. Watoto walio na bahati mbaya ya kulelewa na kuelimishwa na akina mama ambao hawana maadili ya kweli, lakini ambao wana mawazo ya kuugua na wanaugua magonjwa ya kufikiria, wanahitaji huruma, maagizo ya uvumilivu, na utunzaji mzuri wa wote wanaoweza kuwasaidia. Matakwa ya watoto hawa hayatimizwi, na elimu yao haiwastahilishi kuwa wanajamii wanaofaa maishani mwao, na huwaleta kaburini mapema. Ikiwa maisha yao ni marefu, hawatasahau masomo waliyofundishwa na

mama. Makosa ya maisha yake yamevutiwa kwao na maneno yake na matendo yake, na mara nyingi watafuata nyayo zake. Mavazi yake huanguka kama ngozi nyeusi kwa watoto wake maskini. Mienendo yake isiyofaaa ya tabia yake huigwa na watoto katika maisha yao, na hawawezi kushinda masomo ya utoto wao kwa urahisi-unakuwa kama muhuri katika maisha yao. {2Tsw 535.2}

Mahusiano nyororo ya kidunia, yenye huruma, vifungo vya kujali na upendo mwanana, ni yale kati ya mama na mtoto wake (tender relationship). Mtoto huvutiwa kwa urahisi na maisha na mfano wa mama kuliko ule wa baba; kwa kuwa kifungo chenye nguvu cha kujali, huruma, na upendo mwororo, huwaungaisha kuwa na umoja. Akina mama wana jukumu zito. Ikiwa ningeweza kuwavutia kazi ambayo wanaweza kufanya katika kufinyanga akili za watoto wao ningelikuwa na furaha. {2Tsw 536.1}

Ikiwa wazazi wenyewe wangepata maarifa, na kuhisi umuhimu wa kuyatumia maarifa kwa vitendo katika elimu ya watoto wao wapendwa, tungepaswa kuona mpangilio tofauti wa mambo kati ya vijana na watoto. Watoto wanahitaji kufundishwa juu ya miili yao wenyewe. Kuna vijana wachache tu ambao wana ujuzi wowote dhahiri wa mafumbo ya maisha ya mwanadamu. Wanajua lakini kidogo juu ya mwili ulio hai. Daudi anasema: "Nitakusifu; kwa maana nimeumbwa kwa kutisha na kwa kustaajabisha." Wafundishe watoto wako kujifunza kutoka kwa sababu hadi athari; waonyeshe kwamba ikiwa watakiuka sheria za mwili wao, lazima walipe adhabu kwa kuugua magonjwa. Ikiwa katika juhudi yako huwezi kuona maboresho maalum kwao, usivunjike moyo; kwa subira na upole waelekeze, mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo. Ikiwa kwa njia hii umefanikiwa kujisahau mwenyewe, bai umechukua hatua moja katika mwelekeo sahihi. Endelea mbele hadi ushindi upatikane. Endelea kufundisha watoto wako juu ya miili yao wenyewe na jinsi ya kuitunza. Uzembe kuhusu afya ya mwili huwa na uzembe katika tabia ya maadili. {2Tsw 536.2}

Usipuuze kufundisha watoto wako jinsi ya kupika. Kwa kufanya hivyo, unawapa kanuni ambazo lazima wawe nazo katika elimu yao ya kiroho/kidini. Katika kuwapa watoto wako masomo katika fiziolojia, na

kuwafundisha kupika kwa urahisi na bado kwa ustadi, unaweka msingi wa matawi muhimu zaidi ya elimu. Ujuzi unahitajika kutengeneza ugali/mkate mwepesi na mzuri. Kuna dini tele katika kupika vizuri mkate au chochote cha afya, na ninahoji dini ya kikundi kile ambacho ni wajinga sana na wazembe sana kuweza kujifunza kupika. {2Tsw 537.1}

Tunaona Ngozi zilizosinyaa na za manjano, na vilio vya maumivu ya kuvimbiwa kila mahali tuendako. Tunapokaa kwenye meza, na kula chakula kilichopikwa kwa njia ile ile kwa miezi kadhaa, na labda miaka, nashangaa kwamba, hawa watu wako bado hai. Mkate na biskuti vimetiwa baking soda (saleratus). Matumizi ya baking soda yalikuwa ni kusaidia usumbufu uwe mdogo; kwa sababu ya usahaulifu, mkate mara nyingi huruhusiwa kuwa na uchachu kabla ya kuoka, na kurekebisha uovu, kiasi kikubwa cha baking soda kinaongezwa kuokea ambayo huifanya kuwa isiyofaa kwa tumbo la mwanadamu. Baking soda haipaswi kuletwa ndani ya tumbo kwa namna yoyote, kwani athari ni ya kutisha. Inakula ukuta wa tumbo, husababisha kuvimba, na mara nyingi husumisha mfumo mzima. Wengine husihi: "Siwezi kutengeneza mkate mzuri au wa thamani isipokuwa nitatumia baking soda, au 'sodium bicarbonate' seleratus Kwa kweli unaweza ikiwa unakuwa mwanafunzi, nawe utajifunza. Je! Afya ya familia yako haitoshi kukuhimiza hili na hamu ya kujifunza kupika na jinsi ya kula? {2Tsw 537.2}

Kile tunachokula hakiwezi kubadilishwa kuwa damu nzuri isipokuwa kina ubora mzuri, rahisi na chenye lishe. Tumbo kamwe haliwezi kubadilisha mkate mchachu kuwa mtamu. Chakula kilichotayarishwa vibaya hakina lishe na hakiwezi kutengeneza damu nzuri. Vitu hivi vinavyohangaisha na kutibua tumbo vitakuwa na ushawishi mbaya juu ya hisia nzuri za moyo, na kutia ganzi. Wengi wanaojiunga na matengenezo ya kiafya wanalalamika kwamba hayakubaliani nao; lakini, baada ya kukaa kwenye meza zao, ninafikia uamuzi kwamba sio matengenezo ya kiafya ambayo ni makosa, lakini chakula kilichoandaliwa vibaya. Wanamatengenezo wa afya, zaidi ya wengine wote, wanapaswa kuwa waangalifu na kujiepusha kuwa watu wanapilitiza kwa pande zote. Mwili lazima uwe na lishe ya kutosha. Hatuwezi kuishi kwa hewa tu; wala hatuwezi kuhifadhi afya isipokuwa

tuwe na chakula chenye lishe. Chakula kinapaswa kuandaliwa kwa mpangilio mzuri ili kiweze kupendeza na kuwa ladha nzuri pia. Akina mama wanapaswa kuwa wataalamu wa fiziolojia ya vitendo, ili waweze kuwafundisha watoto wao kujitambua na kujua miili yao, na kuwa na ujasiri wa kimaadili kutekeleza kanuni sahihi ili kupinga mitindo ya kuangamiza afya na maisha. Kuvunja sheria za uhai wetu bila sababu, ni ukiukaji wa sheria ya Mungu. {2Tsw 537.3}

Upishi duni polepole huondoa nguvu za maisha ya maelfu. Ni hatari kwa afya na maisha kula kwenye meza za watu wengine, mikate iliyochachuka isiyomuka vizuri na iliyochacha na chakula kingine kilichoandaliwa kwa kuzingatia hayo mawili (mkate unakuwa mzito, na pia una ugwadu sana). Akina mama, badala ya kutafuta kuwapa binti zako elimu ya muziki, wahekimishe katika mafundisho ya matawi haya yenye faida ambayo yana uhusiano wa karibu zaidi na maisha na afya. Wafundishe mafumbo/siri zote ya kupika. Waonyeshe kwamba hii ni sehemu ya elimu yao na ni muhimu kwao ili kuwa Wakristo. Isipokuwa chakula kimeandaliwa kwa njia kamilifu na ladha nzuri kwenye mdomo, hakiwezi kubadilishwa kuwa damu nzuri ili kujenga seli (tishu) zinazopotea. Binti zako wanaweza kupenda muziki, na hii inaweza kuwa sawa; inaweza kuongeza furaha ya familia; lakini ujuzi wa muziki bila ujuzi wa kupika sio jambo la thamani sana. Wakati binti zako watakapokuwa na familia zao wenyewe, uelewa wa muziki na kazi za ufahari wa kidunia havitaweza kuleta mezani chakula cha jioni kilichopikwa vizuri, kilichoandaliwa kwa umaridadi, ili wasione haya kukiweka mbele ya marafiki zao, wanaoheshimiwa sana. Akina mama, kazi yenu ni takatifu. Hebu Mungu awasaidie kuichukua kwa mtazamo wa utukufu Wake na fanya kazi kwa bidii, uvumilivu, na upendo kwa faida ya sasa na ya baadaye ya watoto wako, ukiwa na jicho lililokita kwa utukufu wa Mungu tu. {2Tsw 538.1}

## SURA YA 63

### UBINAFSI WAKARIPIWA

Ndugu yangu A:

Tangu mkutano wa kambi ya Illinois, kesi yako imesisitizwa kwa uzito kwenye akili yangu. Ninapokumbuka mambo kadhaa yaliyonyeshwa kuhusu wahudumu/wachungaji, haswa wewe mwenyewe, nina wasiwasi sana. Kwenye mkutano huko Illinois nilizungumza haswa juu ya sifa za mhudumu wa injili. Nilipowasilisha mbele ya watu sifa za mtumishi aliye na ujumbe adhimu/mzito kwa siku hizi za mwisho, mengi ambayo nilisema yalikuhusu, na nilitarajia kusikia utambuzi kutoka kwako. Kabla ya kuongea kwangu, mke wako alizungumza na Dada Hall juu ya kukatishwa tamaa kwako. Alisema kuwa wewe ulikuwa hajui kama ni jukumu lako kuhubiri; ulikuwa bado una mashaka moyoni, kuhusiana na wajibu wako wa kuhubiri, na ulivunjika moyo, na haukuingia katika kazi hiyo kama ambavyo ungepaswa kufanya kama ungehisi moyoni umetulia, na huna mashaka na kazi hii. Dada Hall aliniambia kwamba ikiwa ningekuwa na neno la kutia moyo kwako, mke wako angefurahi kuniambia. Nilimwambia Dada Hall kwamba sikuwa na neno la kuongea la kutia moyo, na kwamba ikiwa hauna uhakika na jukumu lako, basi ungingojea hadi ujue wajibu wako mwenyewe. Kisha nikazungumza juu ya sifa za mchungaji/mhudumu wa Kristo; na, ikiwa ningekuwa nimetimiza wajibu wangu kikamilifu, ningepaswa kusema nawe dhahiri nilipokuwa kituo cha treni. Ila uwepo wa wasioamini pale stendi ya treni, ndio sababu pekee ambayo ilinizuia. {2Tsw 539.1}

Huko Minnesota nilikuwa tena na mzigo mzito kuhusu mwenendo wa watendakazi wetu, kwa kumuona Ndugu B na kuzungumza naye kuhusu kasoro zake za kujali za mambo ya maisha haya ambazo zilisimama katika njia yake ya uongoaji wa roho na kuwa kizuizi.

Mwenendo na kasoro yake ya mambo ya maisha haya, ilileta tena kesi yako waziwazi mbele yangu kwamba, ikiwa ningekuwa katika hali ya kawaida, ningepaswa kukuandikia kabla ya kuondoka kwenye uwanja wa kambi. Hatukuwa na wakati wa kupumzika, lakini tulikuja moja kwa moja Wisconsin. Nilikuwa mgonjwa, lakini Mungu aliniimarisha kufanya wajibu wangu mbele ya watu. Niliposimama mbele ya hadhira/umma niligundua sura ambazo sikuwa na ufahamu wa kuziona hapo awali. Tena kesi yako, kuhusiana na wengine, ilikuja wazi mbele yangu. Hapa ndipo hali/mahali ambapo ushawishi wako ulikuwa laana mbaya badala ya baraka. Ilikuwa pia mahali ambapo mema mengi yangeweza kutimizwa hata na wewe tu. Ungekuwa umewekwa wakfu kwa Mungu, na kujitolea kufanya kazi kwa wokovu wa roho ambao Kristo alikufa kwa ajili yao, kazi yako ingefanikiwa kabisa. Uliielewa hoja za msimamo wetu. Sababu za imani yetu, zilizoletwa mbele ya akili za wale ambao hawajaangaziwa juu yao bado, hizo hufanya maoni yenye kuazimiwa, kama akili ambazo hazikujazwa na ubaguzi ili wasipate ushahidi uliopewa. Niliona nyenzo bora zaidi, za kuwaunda/kuwafanya Wakristo bora wa utunzaji wa Sabato karibu na ---- na ----; Japo wengine walipendezwa na mlolongo mzuri wa Ukweli, na walikuwa karibu tayari kuamua juu yake, uliacha uwanja wa kazi bila kumaliza kazi uliyokuwa umefanya. Hii ilikuwa mbaya zaidi kuliko ambavyo usingewahi kuingia mahali hapo. Shauku hiyo ya watu haiwezi kuinuliwa tena. {2Tsw 539.2}

Kwa miaka nuru imekuwa ikitolewa juu ya hatua hii, ikionyesha umuhimu wa kufuatilia shauku/maslahi ambayo yamekuzwa baada ya kufikia watu, na bila kuacha mpaka wote waamue kuegemea kwenye uUkweli na wamepata uongofu unaohitajika kwa ubatizo na kuungana na washiriki wengine walio na kanisa tayari au wapande kanisa lao wenyewe. Hakuna mazingira au hali iliyo na umuhimu wa kutosha kumwita mchungaji, au kumtoa kutoka pale ambapo shauku ya watu imeundwa, baada ya kufundisha/uwasilishaji wa ile Kweli. Hata magonjwa na kifo havina matokeo makubwa (ya umilele) kuliko wokovu wa roho ambazo Kristo alitoa dhabihu kubwa sana kwa ajili yao. Wale ambao wanaohisi umuhimu wa Ukweli, na thamani ya roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yao, hawataacha watu wenye shauku au hamu ya Neno la Mungu, na kuondoka kwaajili ya zingatia lolote lile au sababu yoyote ile. Watasema: Waache wafu wazike wafu wao.

Masilahi ya nyumbani, maslahi aardhi na nyumba, hayapaswi kuwa na hata nguvu ndogo ya kumvuta mtu kutoka uwanja wa kazi. Ikiwa wachungaji wataruhusu mambo haya ya kidunia kuwaondoa kwenye kazi, jukumu pekee lao kufuata ni kuacha vyote, kutokuwa na ardhi au masilahi ya muda ambayo yatakuwa na ushawishi wa kuwavuta kutoka kwa kazi hii ya wakfu, katika siku hizi za mwisho. Nafsi moja ina thamani zaidi kuliko ulimwengu wote. Je! inakuwaje kwamba wanaume wanaodai wamejitolea kwa kazi takatifu ya kuokoa Roho za watu, waruhusu mali zao ndogo za muda, kushugulisha akili na mioyo yao, na kuwazuia kutoka kwa wito wao wa juu ambao wanadai kuwa wamepokea kutoka kwa Mungu? {2Tsw 540.1}

Niliona, Ndugu A, kwamba ushawishi wako katika maeneo ya karibu na ---- na ---- umefanya uharibifu mkubwa kwa kusudi la kazi Mungu. Nilijua ushawishi huo ulikuwa nini wakati ulikuwa huko Battle Creek mwisho. Kama nilivyoandika jambo muhimu kwa watendakazi, kesi yako imeletwa mbele yangu, na nilikusudia hii iwe imeandikwa kabla; lakini haikuwezekana. Kwa usiku-tatu nimelala kidogo tu. Kesi yako imekuwa juu ya akili yangu karibu kila wakati. Nilikuwa nakuandikia akilini mwangu, nilipokuwa usingizini, na pia wakati nilikuwa macho. Wakati nilitambua kutaniko la wale watu bainishi waliojeruhiwa na ushawishi wako, ningepaswa kulileta jambo hilo nje, kama ungekuwepo. Hakuna neno hata moja kutoka kwa mwenye mwili anayekufa, aliyenipa umbeya kuhusiana na mwenendo wako. Nilijisikia kulazimika kuzungumza na mmoja au wawili kwa kuzingatia jambo hilo, nikiwaambia kwamba nilikumbuka sura zao kuhusiana na mambo kadhaa ambayo nilioneshwa kuhusiana nawe. Halafu, kwa kusita sana, ukweli uliohusiana na jambo husika, nawe ulithibitishwa na watu, kwamba yote niliyowaambia yalikuwa kweli. Nimesema tu kile niliamini ni lazima niseme kwa hofu ya Mungu, nikitimiza wajibu wangu kama mtumishi Wake. {2Tsw 541.1}

Miaka miwili iliyopita niliona kuwa wewe na mke wako wote wawili mlikuwa watu wenye ubinafsi, wenye tamaa ya mali/vitu, watu wachoyo. Masilahi yako ya kibinafsi yalipendwa kwako kuliko roho ambazo Kristo alikufa. Nilioneshwa kuwa, kwa ujumla haukuwa na mafanikio katika kazi zako. Una uwezo wa kuwasilisha Ukweli; una akili

ya uchunguzi; na kama sio kwa kasoro nyingi katika tabia yako ya Kikristo, unaweza kufanikisha mema. Lakini, kwa sababu nyingi, haujaweza kufanikiwa katika kuhubiri Ukweli. Mojawapo ya laana kuu za maisha yako, Ndugu A, umekuwa mbinafsi wa kupindukia-mbinafsi mkubwa. Umekuwa ukifikiria na kufanya mahesabu kichwani, kwa faida yako mwenyewe. Ninyi wawili mmejifanya kituo cha huruma na umakini. Unapoenda mahali na kuingia kwenye familia, unatupa uzito wako wote kwao, ukiwaacha wakupikie, wakutumikie na wakusubiri; na hakuna hata mmoja wenu kati ya ninyi wawili anayetafuta kufanya kazi nyingi kama mnavyoonyesha watu mnafanya. Familia inaweza kuwa inafanya kazi ngumu, ikibeba mizigo yao na yako; lakini nyinyi wawili mna ubinafsi mkubwa, hata hamuwezi kuona kuwa wamechoshwa na kwamba nyinyi wawili mna uwezo wa mwili kuliko wao kufanya kazi wanazowafanyia. Ndugu A, wewe ni mvivu sana kumpendeza Mungu. Wakati kuni au maji yanahitajika, haujui, na mnaruhusu vitu hivi viletwe na wale ambao tayari wamefanya kazi nyingi, na mara nyingi ni wanawake ambao huwafanyia kazi, wakati shuguli hizi ndogo, uungwana na adabu katika maisha ndio vinavyohitajika wewe kufanya kwa faida ya afya yako. Umejaa nyama na damu, na hufanyi mazoezi ya kutosha kwa faida yako mwenyewe. Uvivu unaodhihirisha, na tabia ya tamaa ya kujitwalia vitu na kubania kila kitu ambacho unaweza kufaidisha wengine, imekuwa ni aibu kwa ile Kweli na kikwazo kwa wasioamini. {2Tsw 542.1}

Mke wako, pamoja na wewe, mna maisha ya kivivu na bwerere. Wakati wako umetumika kitandani wakati ambapo uliweza kuamka kwa bidii ukionyesha ucheshi maalum kwa familia uliyokuwa ukiilemea. Umefikiria kuwa, kwa sababu ulikuwa mchungaji, wanapaswa kuzingatia uwepo wako kama vile ni fadhila au upendeleo hivi, na wanapaswa kukusubiri, kukutumikia na kukupendelea, wakati huna la kufanya ila kujali masilahi yako binafsi. Tabia ambayo umeionyesha imekuwa mabaya sana. Ninyi wawili mmezingatiwa kama wawakilishi wa wachungaji na wake zao ambao wanahusika katika kuwasilisha kwa ulimwengu Sabato na kuja kwa Bwana wetu hivi karibuni. {2Tsw 542.2}



Wale ambao wanafahamu maisha yako watasema kuwa kukiri kwako, mafundisho yako, na maisha yako hayaendani pamoja. Wanaona kuwa matunda yako sio mazuri, na wanaamua kuwa wewe hauamini vitu unavyofundisha wengine. Wanahitimisha kuwa wachungaji-wahudumu wote ni kama wewe mwenyewe ulivyo, na Ukweli mtakatifu na wa milele baada ya yote, ni udanganyifu tu. Je, ni nani atakayewajibika kwa maoni kama haya na matokeo mabaya kama hayo? Naomba uone uzito ulio juu yako kutokana na ubinafsi wako, ambao ni laana kwako mwenyewe, na kwa wale wote wanaokuzunguka. {2Tsw 543.1}

Tena, Ndugu A, unasumbuliwa na hisia na maoni ambayo ni matunda ya asili ya ubinafsi. Unafikiria kwamba wengine hawathamini kazi yako. Unajiona una uwezo wa kufanikisha kazi kubwa, lakini unatoa udhuru kwa kushindwa kwako kuifanya, kwa sababu wengine hawakupi nafasi na sifa kulingana na uwezo wako. Una wivu kwa wengine na umezuia maendeleo ya kazi katika Illinois na Wisconsin, ukifanya kazi kidogo tu, na kuwazuia wale ambao wangependa kazi ikiwa ungetoka njiani mwao. Kujihisi kwako kwingi na wivu umedhoofisha mikono ya wale ambao wangeweka vitu kwa mpango na kuvileta kwenye mikutano hii. Ikiwa uboreshaji wowote unaonekana katika majimbo haya [konferensi], unaelekea kufikiria kuwa inahusika kwa kiwango kikubwa na wewe mwenyewe, wakati ni ukweli kwamba ikiwa mambo au konferensi viliachwa kwako kusimamia au kuongoza, kila kitu kingeenda chini ardhini kwa kasi sana. Katika mahubiri yako kwa ujumla wewe ni mkavu sana, baridi na hauonyeshi hisia. Hausuki mafundisho ya Biblia na matendo pamoja, katika vitendo na mafundisho. Unaongea kwa muda mrefu na kuwachosha watu. Badala ya kukaa tu juu ya sehemu hiyo ya mada yako ambayo unaweza kuiweka wazi kabisa kwa uelewa wa wote, wewe unazunguka na kuja kwa maelezo madogo madogo ambayo hayasaidii mhusika na ambayo yanaweza yakaachwa na hakuna litakaloharibika. Wakati mambo mengi ambayo sio ya lazima kabisa yanaletwa, msikiaji hupoteza mlolongo wa hoja na hawezi kuzingatia somo husika. Wakati mchungaji anapata usikivu wa watu, anapaswa kuenenda kutoka pointi kwa pointi (vipengele), kwa kadri inavyowezekana na kuacha kuongea vitu visivyo na maana na pointi zilizozongwa-zongwa. Anapaswa kuacha maoniyake mbele ya watu kwa kutofautisha hoja zenye (vipengele) kama vigingi vya maili vya

umbali barabarani. Kufunika vidokezo muhimu, na safu ya maneno mengi-mengi, huku ukikokota kila kitu kilicho na uhusiano wa mbali na somo husika, huharibu nguvu yake na kuficha mlolongo mzuri wa Ukweli. Unahubiri kwa kujivuta na kuboresha watu kwenye kuhubiri na pia kwenye kila kitu unachofanya. Wewe ndiye mhitaji haswa, ikiwa mtu yeyote alihitaji kupata nguvu na Roho wa Ukweli. Unahitaji Kristo aliyeumbwa ndani yako tumaini la utukufu. Unahitaji dini, nakala halisi. {2Tsw 543.2}

Nilielekezwa kwa maneno yafuatayo ya uvuvio: "Ni nani mtu mwenye busara na aliye na ujuzi kati yenu? Na aonyeshe kutoka kwa mazungumzo mazuri matendo yake kwa upole wa hekima." Lakini hekima itokayo juu kwanza ni safi, kisha yenye amani, mpole, na rahisi kusikilizwa, imejaa rehema na matunda mema, bila ubaguzi, na haina unafiki. Na matunda ya haki hupandwa ndani amani ya wale wanaofanya amani." "Wanaume ambao Mungu amewaita katika kazi ya kuokoa roho watahisi mzigo kwa watu. Masilahi ya ubinafsi yatamezwa kwa kujali kwao kwa wokovu wa roho ambazo Kristo alikufa. Watahisi nguvu ya himizo la Petro: "Wazee walio kati yenu nawasihi, ambaye pia ni mzee, na shahidi wa mateso ya Kristo, na pia mshiriki wa utukufu utakaofunuliwa: Lisha kundi la Mungu ambalo liko kati yenu, mkichukua usimamizi wake, si kwa kubanwa, bali kwa hiari; si kwa faida ya uchafu, lakini kwa nia tayari; wala si kama mabwana juu ya urithi wa Mungu, bali kwa mfano wa kundi. Na Mchungaji Mkuu Atakapotokea, mtapokea taji ya utukufu isiyokauka." {2Tsw 544.1}

Wewe ni mkaidi kwa asili. Wivu na ukaidi ni matunda ya asili ya ubinafsi. Umefanya maboresho kadhaa; lakini niliona mengi bado yanahitaji kufanywa, niliona waziwazi ushawishi wa kutisha wa maisha yako ya ubinafsi, yasiyotolewa wakfu, naogopa kwamba kamwe hutaona jinsi tabia hizi zinavyokuwa za kuchukiza mbele za Mungu. Ninaogopa kwamba hautagundua hii vya kutosha, ili kuyaweka haya mbali na kuwa kama Mkombozi wako Anayejikana Mwenyewe, Safi na Asiye na ubinafsi, maisha yako yapaswa kuwa yenye sifa ya ukarimu usio na ubinafsi. Ushawishi wako na mfano unasababisha wengine wanaopenda Ukweli na kazi ya Mungu, na wale ambao wanathamini imani yetu, kupoteza roho yao ya kujitolea na nia yao katika Ukweli wa

leo. Mwendo wako wa ubinafsi na uchoyo huzaa roho ile ile ndani yao; na tabia yako ya ubahili, tamaa ya mali na kujinufaisha mwenyewe, wakati unakiri kuwa mhudumu wa haki, tabia hiyo imefunga mioyo ya wengi sana dhidi ya kutoa mali zao ili kuendeleza huduma ya Ukweli (injili/Neno Takatifu). Ikiwa wachungaji watawawekea watu mfano wa kuwa wabinafsi, Mifano hiyo itaelezea juu ya kazi ya Mungu kwa nguvu kubwa mara kumi kuliko mahubiri yao yote. {2Tsw 545.1}

Mungu amedharauliwa na vitu vya kipuuzi unavyofanya. Shuguli zako zina ladha ya kutokuwa na uaminifu (dili zako ni za udanganyifu). Haujaacha nyayo za ukamilifu nyuma yako, na mpaka kuwe na mabadiliko kamilifu katika maisha yako, utakuwa laana hai kwa kanisa mahalia, popote ulipo. Wewe ni mtumishi wa mshahara tu, na hauwashi moto juu ya madhabahu ya Mungu, au kufunga milango bure -Malaki 1:10. Utapowawekea watu mfano wa kujitoa nafsi na wa kujiweka wakfu kwa ibada kwa kazi ya Mungu, ukifanya Ukweli na wokovu wa roho kuwa kipaumbele, basi ushawishi wako utawaleta wengine katika nafasi ile ile ya kujitoa nafsi na kujiweka wakfu kwa ibada, na kuufanya ufalme wa mbinguni na haki ya Kristo kwanza. Unajiona kama umeruhusiwa kujinufaisha mwenyewe na kazi ya MUNGU. Ndugu zako, kutokana na ukarimu wa roho zao, wanakupa upendeleo na kukusaidia kwa njia mbali mbali, nawe unapokea misaada yao kama jambo la kawaida, lisilo na shaka, kama vile ni haki yako. Na ikiwa kuna yoyote ambaye hayuko huru nawe kwa kikamilifu, na hakupi upendeleo, una wivu, na hausiti kuwajulisha wengine waelewe kuwa hauthaminiwi, na kwamba watu hao ni wabinafsi. Mara nyingi unawataja majina wengine ambao wamehusiana hivi na wewe [kwa kukupa vitu nk], kama mifano ambayo wanapaswa kuiga. Hawa ambao wamekupa upendeleo kwa ukamilifu haswa, nao wameenda mbele zaidi ya wajibu wao. Hujaufanyia kazi imani yao au ukarimu wao. Hukuwa na mizigo mizito ya kubeba kwa kazi hii ya Mungu, na umewatupia wengine mizigo mingi zaidi ya uliyosaidia kuiinua; lakini umekuwa ukiendelea kupata mali, na kupata vitu vizuri vya maisha haya, na umeyachukulia yote haya kama haki yako. Ingawa umepokea mshahara wako wa kila wiki, daima hukuridhika. Pamoja na malipo uliyopokea, umekuwa ukisimamia mambo kila wakati ili ujinufaishe mwenyewe. Kazi ya Mungu imekulipa. bila kujali ikiwa ulifanya kwa

wingi au kwa uchache kazi hiyo. Haujatolea jasho mali ambazo umepokea. {2Tsw 545.2}

Mke wako ameendekezwa/amedekeshwa na wazazi wake na mumewe kiasi kwamba amekuwa mtu mwenye msaada mdogo sana au mwenye faida ndogo tu. Nyote wawili mmeona wale ambao wamelemewa na mizigo na hamjawasaidia kuiinua mizigo, pamoja nao. Mkeo amejipumzisha kama mzigo mnyonge kwa familia, akijiumiza mwenyewe vikali, na wengine pia, wakati, katika hali ya afya, alikuwa na uwezo mzuri wa kufanya kuliko wengine ambao walikuwa wakibeba mizigo yake na yako. Walakini hakufikiria hili. Nyote wawili hamkuweza kuona Ukweli katika kesi hiyo na kuwahurumia wengine. Wengine ambao mmepokea msaada kwao ili mjitunze ninyi mwenyewe na mtoto wenu, hawakujiweza kifedha, kufanya kile walichofanya; lakini walidhani walikuwa wakiwahudumia watumishi wa Kristo wanaojitolea nafsi zao; kwa hivyo walijinyima nafsi zao na kuvumilia usumbufu na shida, ili tu wabebe mizigo ambayo mliweza kujibebwa wenyewe kuliko hata wao wanalivyowezwa kuibeba kwa ajili yenu. {2Tsw 546.1}

Mke wako amekuwa hataki kuchukua mizigo ya maisha yake. Anataka wito wa juu, na anapuuza majukumu ya rahisi ya leo. Hakuna kati yenu anayetii amri ya Mungu: Mpende jirani yako kama nafsi yako. Ubinafsi na uchoyo unafanya msishugulikie mahitaji ya majirani zenu. Roho zenu ndogo, roho za usaliti zinaambukiza. Mfano wako umechochea zaidi kuupenda ulimwengu, na roho ya ubahili, na roho ya umasikini, kuliko kitu kingine chochote kilichotokea Wisconsin na Illinois. Kama usingefanya chochote isipokuwa kuzingatia masilahi yako ya kidunia, kazi ya Mungu katika majimbo haya mawili ingekuwa katika hali nzuri zaidi kuliko ilivyo leo. Mafanikio uliyopata hayakaribii kabisa majeraha uliyoleta. Kazi ya Mungu imeangushwa chini ardhini. Hisia zako zinazochomwa kirahisi na wivu, nazo zimekuwa mfano kwa wengine. Tulikutana na roho hii huko Illinois na huko Wisconsin. Hali ya makanisa katika ---- na maeneo ya jirani imekuwa ya kuaibisha. Ukosefu wa upendo na umoja, kufikira watu maovu, wivu, na ukaidi, vinavyoonekana katika makanisa haya, vimeundwa kwa kiasi kikubwa kutokana na tabia yako. Nafasi uliyokuwa nayo baada ya ushabiki huko ----, ukisimama juu ya hadhi yako, ukitofautisha vitu vidogo

vidogo, ukigawanya mambo kwa unafiki na wale ambao Mungu alikuwa amekutuma na ujumbe maalum, ilisimama moja kwa moja kwa njia ya wengine, kuona na kurekebisha makosa yao. Kozi/mwenendo wako wakati huo, kwa kushindwa kushikilia na kufanya kazi upande sahihi katika kusahihisha ushabiki huo mkali, ilitoa sura kwa hali ya kukatisha tamaa ya mambo ambayo imekua nje ya utawala huo wa giza wa ushabiki. Ndugu C na D, na kanisa lote huko ----, na watu huko ----, hawakuletwa nje kwa nafasi sahihi, kama vile wangukuwa wanyenyekevu na wanaoweza kufundishwa, wakifanya kazi kwa umoja kama watumishi wa Mungu. {2Tsw 546.2}

Wakati mtu anayedai kuwa mwalimu, kiongozi, anajitosa katika mwenendo ambao umefuatwa nawe wewe kwa sababu ya ukaidi wako, atakuwa na mzigo mzito wa jukumu la kubeba roho ambazo amezikwaza na zikaangamia milele. Mtendakazi hawezi kuwa mwangalifu sana juu ya mvuto wake. Ukaidi, wivu, na ubinafsi havipaswi kuwa sehemu ya nafsi yake; kwani, hivi vikiendekezwa, ataharibu roho nyingi zaidi ya zile ambazo anaweza kuziokoa. Ikiwa hatashinda mambo haya hatari katika tabia yake, ingelikuwa bora kwake kama asingelikuwa na uhusiano wowote na kazi ya Mungu. Kuendekeza kwa tabia hizi, ambazo zinaweza kuonekana kwamba sio mbaya sana kwake, kutaziweka roho za watu mbali naye, naye atashindwa kuzifikia, na hata watu wengine pia wataashindwa kuzifikia. Ikiwa wahudumu kama hao wangeacha mambo yajiendeshe yenyewe, roho zinazohusika na ushawishi wa Roho wa Mungu zinaweza kufikiwa na wale ambao wanaweza kuwapa mfano unaofaa kuigwa, kulingana na Ukweli wanaofundisha. Kwa maisha thabiti mchungaji atabaki na imani/ujasiri wa wale wanaoutafuta Ukweli, hadi hapo atakapoweza kuwasaidia kushikilia ufahamu/ujuzi wao juu ya Mwamba wa Kale; na baadaye, ikiwa watajaribiwa, ushawishi huo utamwezesha kuwaonya, kuwasihia, kuwakaripia, na kuwashauri kwa mafanikio. {2Tsw 547.1}

Juu ya watu wengine wote, wahudumu wa Kristo, wanaobeba Ukweli mzito wa siku hizi za mwisho, wanapaswa kuwa huru kutokana na ubinafsi. Ukarimu usio na ubinafsi unapaswa kuwa kwao kitu cha kawaida Wanapaswa kuona aibu kwa matendo wanayowatendea ndugu zao ambayo yana alama za ubinafsi. Wanapaswa kuwa mifano

ya uchaji, nyaraka zinazoishi, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Matunda yao yanapaswa kuwa ya utakatifu. Roho wanayonapaswa kuwa nayo ni kinyume na ile inayodhihirishwa na walimwengu. Kwa kukubali Ukweli wa Bwana/mbingu wanakuwa watumishi wa Mungu, na si watoto wa giza tena na watumwa wa ulimwengu. Kristo amewachagua kutoka ulimwenguni. Ulimwengu hauelewi siri ya utauwa, kwa hivyo haijui nia au madhumuni yale ambayo yanashawishi. Ila Roho na uzima ulio ndani yao, ambayo hudhihirishwa katika mazungumzo yao ya kimbingu, maisha yao ya kujikana, kujitolea dhabihu, maisha yasiyo na lawama, huwa na nguvu ya kushawishi ambayo itawaongoza wasioamini katika Ukweli wote, kuwaongoza kumtii Kristo. Wao ni mifano hai kwa sababu wao ni kama Kristo. Wao ni nuru ya ulimwengu, chumvi ya dunia, na ushawishi wao kwa wengine unaokoa. Wao ni wawakilishi wa Kristo duniani. Malengo yao na matamanio yao hayavuviwi na vitu vya kidunia, wala hawawezi kufanya kazi kwaajili ya kujipatia faida wenyewe au kufurahia upendo wa kichoyo Kwa kuwa mazingatio ya umilele yanatosha kupikua/kupindua chini kila kivutio cha kidunia. Mkristo wa kweli atafanya kazi ili ampendeze Mungu tu, akiwa na jicho lililokita kwaajili ya utukufu Wake tu na hufurahia tuzo ya kufanya mapenzi Yake. {2Tsw 548.1}

Wachungaji haswa wanapaswa kujua tabia na kazi za Kristo, ili waweze kumuiga Yeye Bwana; kwani tabia na kazi za Mkristo wa kweli ni kama Zake. Yeye Aliacha utukufu Wake, Mamlaka Yake, utajiri Wake, ili kuwatafuta wale ambao walikuwa wakiangamia katika dhambi. Alijishusha kwa mahitaji yetu, ili apate kutuina mbinguni. Kujitolea dhabihu, kukana nafsi, na ukarimu usio na ubinafsi uliashiria maisha Yake. Yeye Ndiye kielelezo chetu. Je! Wewe, Ndugu A, umeiga Mfano? Ninajibu: Hapana. Yeye Ndiye mfano mkamilifu na mtakatifu, tuliopewa sisi binadamu kuuiga. Hatuwezi kujilinganisha na Mfano huu; lakini hatutakubaliwa na Mungu ikiwa hatutauiga na, kulingana na uwezo ambao Mungu ametupatia, kufanana nao Mfano huu. Upendo kwa roho ambazo Kristo alikufa kwazo itapelekea ninyi kujikana wenyewe na utayari wa kujitolea ili kuwa watenda kazi pamoja na Kristo katika wokovu wa roho. {2Tsw 549.1}

Kazi za watumishi waliochaguliwa na Mungu zitazaa matunda zikifanywa Ndani Yake. Maneno na matendo yao ni mifereji ambayo

kanuni safi za Ukweli na utakatifu zinawasilishwa ulimwenguni. Maisha yao ya mfano huwafanya kuwa nuru ya ulimwengu na chumvi ya dunia. Watumishi wa Mungu wanapaswa, kwa mkono wa imani, kuushika Mkono Wenye nguvu na kukusanya miale ya mbingu ya nuru kutoka juu, na wakati huo huo kwa mkono wa pili wa upendo, kuzifikia roho zinazopotea. Bidii na uadilifu ni muhimu katika kazi hii. Uvivu utaruhusu roho ambazo zinaweza kuokolewa, kuteleza mbali ambapo itakuwa ni vigumu kuzifikia. Mungu anataka katika Huduma Yake wahudumu walio macho, wenye nguvu na wavumilivu, ambao ni walinzi waaminifu juu ya kuta za Sayuni, wakisikiliza ili kusikia Maneno kutoka kwa Mwalimu mbinguni na kwa uaminifu wakitangaza maneno waliyoyasikia kwa Mwalimu wa mbinguni kwa watu wengine {2Tsw 549.2}

Umefanana sana na Merozi. Una bidii kabisa wakati kile unachofanya kitaleta faida kwako mwenyewe, lakini hauna motisha ya kuwa na bidii maalum isipokuwa pale utakapofaidika. Hakika wewe ni mtu uliyeazimia kuwa mvivu. Unaweza kula posho (mgawo) wako mara kwa mara kwa uthabiti, lakini hauna upendo maalum kwa kazi za mikono. Hakuna mtu apaswaye kushika nafasi ya mchungaji asipokuwa na bidii katika kazi za mikono, bidii katika biashara, na mwaminifu katika utekelezaji wa majukumu yote ya maisha ya kijamii na ya umma. Mungu ametuchagua sisi, kama watumishi Yake, ambayo inahitaji uvumilivu wenye nguvu. Hatupaswi kudeka kama wanyama wa kufugwa wanaoepuka kazi ngumu (pets), ugumu wa maisha, na ukinzani. {2Tsw 550.1}

Nilielekezwa kwa maneno yafuatayo yaliyovuviwa: Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, Ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo. Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe

katika miili yetu." Kujitosheleza kwa mtume hakukuwa ndani yake mwenyewe, lakini kwa uwepo na nguvu ya Roho Mtakatifu, ambaye ushawishi wake wa neema ulijaza roho yake, ukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo. Huduma yake ilizaa matunda. {2Tsw 550.2}

Amri kuu ya kwanza ni: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote." "Na ya pili yafanana nayo, Mpende jirani yako kama nafsi yako." Juu ya amri hizi mbili, hutegemea maslahi yote na wajibu wa viumbe vyenye maadili. Wale ambao hufanya wajibu wa kuwatendea wengine kama vile wengine wangewatendea wanaletwa katika nafasi ambao Mungu anaweza kujifunua kwao. Watakubaliwa Naye. Wamefanywa wakamilifu katika upendo, na matendo, na maombi yao hayatakuwa ya bure. Wanaendelea daima kupokea neema na kweli kutoka katika kichwa cha chemchemi, na wanapeleka kwa ukarimu kwa wengine nuru ya mbingu na wokovu wanaoupokea. Ndani yao imetimia lugha ya Maandiko: "Mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele." {2Tsw 550.3}

Ubinafsi ni chukizo mbele za Mungu na malaika watakatifu. Kwa sababu ya dhambi hii, wengi wanashindwa kupata mema ambayo wana uwezo wa kuyafurahiya. Wanaangalia kwa macho ya ubinafsi juu ya mambo yao wenyewe, na hawapendi na kutafuta masilahi ya wengine kama wanavyofanya ya kwao wenyewe. Wanabadilisha utaratibu wa Mungu, na kurudi nyuma. Badala ya kufanya kwa wengine kile wanachotaka wengine wawafanyie, wanajifanyia wenyewe kile wanachotaka wengine wawafanyie wao, na kuwafanyia wengine kile ambacho hawataki kabisa kirejeshwe kwao. Hapa ndipo unahitaji kujifunza. Upendo ni wa Mungu. Huna upendo uliokaa kifuni mwa Kristo. Moyo usiowekwa wakfu, hauwezi kuwa chanzo, au hauwezi kutoa, mmea huu wa asili ya mbinguni, ambao, ili kushamiri, lazima unyweshewe maji kila wakati na umande wa mbinguni. Huu mmea unaweza kushamiri tu, moyoni ambamo Kristo Anatawala. Upendo huu hauwezi kuishi na kushamiri bila matendo; na hauwezi kutendwa bila kuongezeka kwa juhudi, na kutapakaa ukieneza asili yake kwa wengine. Kanuni hii, wewe umepungukiwa nayo sana, na kwa hivyo yote yamekuwa giza wakati ambapo uwepo wake ungefanya yote kuwa nuru. {2Tsw 551.1}



Ndugu yangu, unahitaji mabadiliko ya jumla, uongofu kamili. Bila hii wewe ni kiongozi ambaye ni kipofu tu. Ushawishi wako hauongezi upendo na umoja kwa wale ambao upo nao. Badala kujenga, wewe una ushawishi wa kutapanya. Umelaani Magharibi na mapungufu yako. Wakati ambapo umepungukiwa sana na neema ya Mungu, na umetekwa sana na ubinafsi, huwezi kulileta kanisa kwenye msimamo ambao Mungu analitaka lichukue. "Ambayo nimefanywa mhudumu, kwa kadiri ya uweza wa Mungu niliopewa kwa ajili yenu, ili kulitimiza Neno la Mungu; hata ile siri iliyokuwa imefichika tangu zamani na tangu vizazi vyote, lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu Wake: ambaye kwao Mungu alitaka kujulisha utajiri wa utukufu wa siri hii kati ya Mataifa ni nini, ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu; ambaye tunamhubiri, tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu kwa hekima yote; nipate kumleta kila mtu mkamilifu katika Kristo Yesu; na kwa hiyo nafanya kazi kwa bidii, nikijitahidi kadiri ya matendo Yake, yafanyayo kazi ndani yangu kwa nguvu. "{2Tsw 551.2}

Watendakazi wa Mungu lazima wawe na Ukweli mioyoni mwao ili kufanikisha kuiwasilisha hii Kweli kwa wengine. Lazima watakaswe na huu Ukweli wanaohubiri la sivyo watakuwa kikwazo tu kwa wenye dhambi. Wale walioitwa na Mungu kuhudumu katika vitu vitakatifu wameitwa kuwa na mioyo safi na kuishi maisha ya utakatifu. "Iweni safi, ninyi mnaobeba vyombo vya Bwana." Ikiwa Mungu anatamka ole juu ya wale walioitwa kuhubiri Ukweli na kukataa kuitii, ole nzito zaidi ni juu ya wale wanaochukua kazi hii takatifu pasipo kuwa na mikono safi na mioyo safi. Kwa kuwa kuna ole kwa wale wanaohubiri Ukweli na huku hawajatakaswa mioyoni na maishani mwao, hivyo basi kuna ole kwa wale ambao hupokea na kudumisha hali ya kutotakaswa katika nafasi ambayo hawawezi kuijaza. Ikiwa Roho wa Mungu hajatakaswa na kusafisha mikono na mioyo ya wale wanaohudumu katika vitu vitakatifu, watazungumza kulingana na uzoefu wao usio mkamilifu, uzoefu wenye mapungufu, na mashauri yao yatapotosha watu kwenda mbali na Mungu, wale watu ambao wanawaangalia watendakazi kwa matumaini katika hukumu zao na uzoefu wao. Mungu awasaidie wachungaji kutii mawaidha ya Paulo kwa Wakorintho: "Jichunguzeni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au

hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo Yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa?" Kuna kazi ya kufanya, ndugu yangu, ikiwa utapata uzima wa milele. Mungu akusaidie kuifanya kazi hii kikamilifu, ili upate kuwa mkamilifu/kamili, na asiyepungukiwa na lolote. Chicago, Illinois, Massasoit House, July 6, 1870. {2Tsw 552.1}

## **SURA YA 64**

### **USHABIKI NA UJINGA**

Ndugu E: Nikiwa Rochester, New York, Desemba 25, 1865, kabla ya kutembelea Jimbo la Maine, niliona mambo kadhaa kuhusiana na hali ya kutatanisha na kukatisha tamaa katika jimbo hilo. Nilioneshwa kwamba idadi kadhaa ya watendakazi ambao walikuwa wakifikiri ni

jukumu lao kufundisha Neno la Mungu hadharani, waliona kuwa wamekosea kuhusika na kazi waliyokuwa wakiifanya. Hawakuwa na wito wa kujiweka wakfu kuhusiana na wajibu wa kazi hii nzito na ya wakfu. Hawakuwa na sifa kwa kazi ya huduma, kwa sababu hawangeweza kuwafundisha/kuwaelekeza wengine jinsi inavyotakiwa. {2Tsw 553.1}

Uzoefu wa wengine ulikuwa umepatikana kutoka kwenye kikundi cha mashabiki wa kidini, watu waliopitiliza, ambao hawakuwa na hisia za Kweli juu ya tabia ya kazi iliyoinuliwa kama hiyo. Uzoefu wa kidini wa kikundi cha wale wanaojiita Waadventista Wasabato haukuaminika. Hawakuwa na kanuni thabiti zilizosimamia matendo yao yote. Walijiamini wenyewe, na kujisifu. Dini yao haikujumuisha matendo ya haki, unyenyekevu wa kweli wa roho, na kujitolea kwa dhati kwa Mungu, lakini ilikuwa na msukumo, makelele na mkanganyiko/kuchanganyikiwa, yaliyo na ladha mbaya na isiyo ya kawaida. Hawakuwa wamehisi, wala hawakuweza kuhisi, umuhimu wa kuvikwa haki ya Kristo. Walikuwa na haki yao wenyewe, ambayo ilikuwa kama matambara machafu, na ambayo kwa vyovyote vile Mungu hawezi kukubali. Watu hawa hawakuwa na upendo kwa umoja na maelewano katika utendaji wao. Walifurahia machafuko. mkanganyiko, usumbufu, na pia utofauti wa maoni ndiyo ulikuwa chaguo lao. Walikuwa hawawezi kuongozwa, kutiishwa, kuzaliwa upya, na pia walikuwa hawajawekwa wakfu, na jambo hili la mkanganyiko liliendana sana na akili zao zisizo na nidhamu. Walikuwa laana kwa kusudi ya kazi ya Mungu na walileta jina la Waadventista Wasabato katika sifa mbaya au ladha mbaya. {2Tsw 553.2}

Watu hawa walikuwa hawajapata uzoefu wa kazi ya matengenezo, au utakaso kupitia Ukweli. Walikuwa wana mikwaruzo (rafu) na wasioboreshwa. Walikuwa hawajawahi kuonja utamu/uzuri, na utakaso wa ulimwengu unaokuja. Hawakuwa wamepata uzoefu, wala mioyo yao haikustajabishwa na siri ya utauwa. Waliweka vitu vya mbingu na vya milele sawa sawa na vitu vya kawaida, na wangezungumza juu ya mbingu na kuja Kwake Yesu kama vile wangepanya wanapozungumzia kuhusu farasi. Walikuwa na maarifa ya juu juu au nadharia ya Ukweli tu, lakini zaidi ya haya yote walikuwa wajinga. Kanuni zake hazikuwa

zimeshika maisha yao na kuwaongoza kuchukia nafsi zao. Hawakuwa wamejiona wenyewe katika nuru ambayo Paulo alijitazama mwenyewe katika hiyo, ambayo ilimwongoza aone kasoro za maadili katika tabia yake. Hawakuwa wamefishwa kamwe na sheria ya Mungu, na hawakujitenga na uchafu wao na unajisi. Ni kazi inayopendwa na wengine wa kundi hili ni kushiriki katika mazungumzo ya kipuuzi na futuhi. Tabia hii waliipata, na wakajiingiza kwenye shuguli ambazo zinapaswa kuwa na sifa ya kutafakari kwa kicho na kujitoa wakfu. Kwa kufanya hivyo, walidhihirisha ukosefu wa adabu/hadhi ya kweli na uboreshaji/usafishwaji, na walipoteza heshima ya watu wenye busara ambao hawakuwa na elimu kuhusu Ukweli. Kundi hiki lilijitupa kwenye mkondo wa majaribu na kujiweka mahali ambapo adui aliwaongoza kwa mafanikio, na amedhibiti akili zao kwa urahisi na kuharibu uzoefu wao wote kiasi kwamba watakosa uwezekano wa kujiokoa kutoka kwenye mtego wake adui, na kupata uzoefu mzuri. {2Tsw 554.1}

Moto wa siku ya Mungu utateketeza makapi na mabaki, na hakutabaki chochote cha wale wanaoendelea katika mwenendo usiomcha Mungu ambao wameupenda kwa muda mrefu. Kundi hili lina ladha/sifa mbaya kwa jamii ya wale ambao Mungu Yuko pamoja nao kweli. Uzoefu wao wa kidini ni wa hali ya chini sana hivi kwamba hawana sehemu, wala fungu katika uzoefu wa busara, wenye akili wa kidini; kwa hivyo wamedharau jamii ya wale ambao Mungu anaongoza na anafundisha. Kejeli yenye dharau, kushushua na kejeli inayohusiana na mategemeo halisi imeng'ang'aninia akili za kipekee za kundi hili. Wana ujasiri na jeuri, na hawajali tabia njema. Hawana huduma ya kubagua na kutoa heshima kwa yule anayestahili heshima. Wanaonyesha roho ya kiburi, ya uasi, na ya ukaidi dhidi ya wale ambao wana tofauti na maoni waliyo nayo. Tabia zao zenye machafuko na mwenendo mbaya humpelekea mtumishi wa Kweli wa Mungu kuhisi kwamba wamepinga juhudi zilizofanywa kwao, naye hukatishwa tamaa kufanya kazi zaidi kwa niaba yao. Wanajiunga na ushindi uliodharauliwa wa asili inayofanana haswa na ile ambayo Shetani na malaika wabaya hujihusisha juu ya roho ambazo wamejitwalia na kujihifadhia. Shetani na malaika wabaya wapo upande wao kufurahi pamoja nao- na kujiinua nao. Kesi za watu ambao tabia hii imeundwa kwa namna ya kipekee na imekua kwa kushangaza haina tumaini. Wamewekwa katika kujiona kuwa ni

waadilifu, na kila kitu kama uboreshaji na mwinuko wa tabia ambao wanawasiliana nao huitwa na wao 'kiburi na ukosefu wa unyenyekevu'. Mikwaruzo ya Ukali na ujinga huchukuliwa kama unyenyekevu. {2Tsw 554.2}

Ndani ya kundi hili ndimo umepata sehemu kubwa ya uzoefu wako wa kidini; kwa hivyo huna stahiki kazi ya kufundisha ujumbe wa makini zaidi, uliosafishwa, wenye kuinua, na unaobeba ujumbe wenye mtihamu zaidi kuliko jumbe zozote kwa wanadamu. Unaweza kufikia kundi la daraja hili la akili, lakini sehemu ile ya watu, wenye akili zaidi ya jamii itakimbia mbali na utumishi wako. Huna maarifa ya kutosha hata katika fani za kawaida za elimu, kuwa mwalimu wa wanaume na wanawake ambao wana Shetani mjanja kwa upande mwingine anayewapendekezea na kuwabunia njia na mbinu za kuwaongoza kutoka nje ya Ukweli. {2Tsw 555.1}

Walimu wa shule za kawaida wanatakiwa kuwa mabwana waliobobea shughuli zao. Wanachunguzwa kwa ukaribu ili kubaini ikiwa watoto wanaweza kuaminiwa vizuri kwa utunzaji wao. Kwa uchunguzi mkamilifu wa sifa zao, hujaribiwa kulingana na umuhimu wa nafasi ambayo wanahitajika kuishika. Niliona kwamba kazi ya Mungu ni ya tabia iliyoinuliwa zaidi, na ya kupendeza zaidi, yenye maslahi, kama ile ya milele ilivyo juu ya vile vya muda. Kosa lililofanywa hapa haliwezi kutengenezwa. Ni la umuhimu usio na kikomo kwamba wote wanaokwenda kufundisha Ukweli wanapaswa kuwa na sifa stahiki kwa kazi yao. Hakuna uchunguzi mkali zaidi unapaswa kuwekwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kufundisha Ukweli kuliko kwa wale wanaofundisha shule zetu. Kazi ya Mungu imedharauliwa na ulegevu, mwenendo mwepesi unaofuatwa na wale wanaojiita wahudumu wa Kristo. {2Tsw 555.2}

Nilioneshwa kuwa wahudumu lazima watakaswe na utakatifu, na lazima wawe na ujuzi wa Neno la Mungu. Wanapaswa kufahamu vizuri hoja za Biblia na kujitayarisha kutoa sababu ya tumaini lao, au wanapaswa kusitisha kazi zao na kushiriki katika wito ambapo upungufu hautahusisha athari kubwa kama hizo. Wachungaji wa madhehebu maarufu wa siku hizi ni wahubiri wanaokubalika ikiwa wanaweza kuzungumza juu ya vidokezo vichache rahisi vya Biblia;

lakini watendakazi ambao wanaeneza Ukweli usiopendwa kwa siku hizi za mwisho, ambao wanapaswa kukutana na wanaume wenye elimu, watu wenye akili kali, na wenye upinzani wa kila aina, wanapaswa kujua ni jambo gani wanalohusika nalo. Hawapaswi kuchukua jukumu la kufundisha Ukweli isipokuwa wanapohitimu/kuwa na sifa za kazi hiyo. Kabla ya kushiriki, au kujitoa kwa kikamilifu kwa kazi hii wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia. Ikiwa hawana elimu ili waweze kuzungumza hadharani kwa kukubalika, na kutendea haki Ukweli, na kumheshimu Bwana ambaye wanayekiri kumtumikia, wanapaswa kusubiri hadi wafae kupata stahiki ya nafasi hiyo. {2Tsw 556.1}

Ndugu E, huwezi kujaza nafasi ya mchungaji/mhudumu wa Kristo. Niliona kuwa umekosa uzoefu sahihi wa kidini. Huna ujuzi kuhusu wewe mwenyewe. Huwezi hata kusoma kwa usahihi, au kutumia lugha ambayo inaweza kufikisha Ukweli kwa uelewa wa jamii yenye akili mahiri. Huwezi kutofautisha na kuweza kufanya maaumuzi sahihi. Haujui ni wakati gani sahihi wewe kuzungumza, au wakati gani uwe na busara kunyamaza. Umefikiria sana, kuhusu kundi la daraja la kipekee nililolitaja kwamba ulijua yote yanayohusika; kwamba hautaona mapungufu yako wakati wanawasilishwa mbele yako. Una tabia ya kujithamini kwa hali ya juu, na uzoefu wako umejulikana na kujiamini mwenyewe na kujigamba. {2Tsw 556.2}

Haufundishiki, kwa hivyo kazi ya Mungu isingefanikiwa mikononi mwako. Ungeshindwa kutambua kushindwa wakati utakapokutana nako. Kazi ya Mungu ingeletwa kwenye aibu na kuvunjiwa heshima na kazi yako, na utashindwa kugundua Ukweli. Kikundi cha daraja fulani kinaweza kusadiki Ukweli wako; lakini wengi zaidi wangegeuzwa na kuwekwa mahali ambapo hawangeweza kufikiwa na kazi inayofaa, ya busara. Kilichosukwa na uzoefu wako ni vitu ambavyo vitakavyohibitisha maumivu kwenye Ukweli. Mungu hawezi kukuidhinisha wewe kama mwakilishi wa Ukweli. {2T 557.1}

Tabia zako hazijasafishwa na kuinuliwa. Mwenendo wako haukumpendeza Mungu. Maneno yako yamekuwa ya hovyo na ya kutojali. Unakosa uchamungu na kujitoa kwa ibada. Hujapata uzoefu katika maisha ya kiroho. Unashindwa kuelewa jinsi ya

kutumia/kugawia watu kwa halali Neno la kweli, ukimpa kila mmoja sehemu yake ya chakula kwa wakati wake unaofaa. Umependelea kushindana na kugombea vipengele/pointi, wakati ulikuwa nje ya nafasi yako na ungeweza kushindwa tu. Hii ndio roho ya kikundi cha huko Maine ambacho nimekitaja. Ni furaha yao kushiriki kwenye shindano na kushugulika nalo kwa ujasiri. Usingeweza kuonyesha upole katika kuwafundisha wale wanaojipinga wenyewe. Daima utakuwa na ulema, kwa kiwango fulani, na uzoefu wako mbaya. Unakosa utamaduni wa kibinafsi na upole. Una masomo muhimu ya kujifunza kabla ya kuwa mfuasi wa Kristo asiyejisifu, anayekubalika, hata katika hali ya binafsi na faragha. {2Tsw 557.2}

## SURA YA 65

### BINTI ALIYEJIINGIZA KWENYE ANASA

Rafiki Mpendwa F: Nilioneshwa kuwa ulikuwa katika hatari ya kuwa chini ya udhibiti kamili wa adui mkubwa wa roho. Uzoefu wako katika --- haukuwa mzuri kwako. Kukaa kwako huko----- kulikumiza; ukawa na kiburi na ubatili. Watu walipungukiwa, wale ambao walikuwa wakikudekesha bila busara na kukusifu mpaka ukawa na ubatili, mpumbavu, na mjinga. Umekuwa ukipinga vizuizi, umekuwa na kichwa kigumu, mwenye kukusudia/makusudi, na mkaidi, na umewasumbua wazazi wako. Wamekosea. Baba yako amekudekesha bila busara. Umechukua fursa hii na kuwa mdanganyifu. Umepokea uthibitisho wa kukubaliwa ambako haukustahili. {2Tsw 558.1}

Ulikuwa na kichwa chako mwenyewe katika ----- na ukachukua uhuru ambao haupaswi kuruhusiwa kwa muda ule. Wakati wewe au dada zako mlipokemewa, mlihisi kutukanwa na kuripoti jambo hilo kwa mama yenu kana kwamba mmetendwa mabaya. Ulitia chumvi, na alikuwa na wasiwasi na alisisimka kwa urahisi na kukasirika ikiwa alifikiri msimamo wake na hadhi yake haikuheshimiwa. Alikasirishwa na mtu yeyote aliyewaamuru watoto wake, na hakuficha kukasirika kwake. Aliongea visivyo kwa wale ambao alipaswa kuonyesha heshima yake kwao. Mama yako alionyesha ukosefu mkubwa wa hekima katika kushiriki kwake mawazo yako na kuwalaumu wale ambao alipaswa kuwashukuru badala ya kuwalaumu. Alikuumiza wewe na akakufanyia kazi ambayo hawezi kuikarabati kabisa. Ulishinda kwa sababu ulijiona uko salama kutokana na lawama, ulidhani kuwa unaweza kufanya upendavyo. Jicho la mama yako halikuwa juu yako kila wakati; na hata kama lingekuwa, asingaliweza kugundua mielekeo yako mibaya. {2Tsw 558.2}

Shuleni ulikuwa na mwalimu mzuri na bora, lakini ulihisi kukasirika kwa sababu ulizuiliwa. Ulifikiri kwamba kwa sababu ulikuwa binti ya G, basi mwalimu wako anapaswa kuonyesha upendeleo kwako na haipaswi achukue uhuru wa mamlaka yake kukurekebisha na kukukemea. Dada zako pia walishiriki roho ile ile. Ulibeba malalamiko yako kwa wazazi



wako; walisikia toleo la upande wako wa mambo na wakakuhurumia zaidi au kidogo, na hisia zao zikachochea na ripoti zako za kutia chumvi. Walikujeruhi. Haujaadabishwa kwa ukali kama ulivyostahili. Hata hivyo ulikasirika kwa sababu haukuweza kuwa na njia yako mwenyewe, lakini ulilazimishwa kukubali kufuata njia kamili iliyowekwa na maagizo ya Ndugu H. Wakati ulikuwa shuleni, wakati mwingine ulikuwa ukileta matata, msumbufu, usiye na heshima, na mwenye kudharau, na kukosa sana adabu na nidhamu. Ulikuwa jasiri, mbinafsi, na ulijiinua, na ulihitaji nidhamu thabiti nyumbani na pia shuleni. {2Tsw 558.3}

Akili yako si safi. Ulipumzishwa kutoka kwenye usumbufu na utumishi kwa muda mrefu sana. Wajibu wa nyumbani ungekuwa moja wapo ya baraka tajiri zaidi ambazo ungekuwa nazo. Uchovu haungekuumiza hata moja ya kumi kama vile mawazo yako machafu ya tamaa za ngono, katika mwenendo wako. Umepokea maoni yasiyo sahihi kuhusu kujumuika pamoja kwa wasichana na wavulana, na imekuwa akilini mwako kuwa katika kikundi cha wavulana. Wewe sio safi moyoni na akilini. Umejeruhiwa na kusoma hadithi za mapenzi na mahaba, na akili yako imekuwa ikivutiwa na mawazo machafu. Mawazo yako yamekuwa mafisadi, mpaka unaonekana hauna nguvu ya kudhibiti mawazo yako. Shetani anakuongoza wewe kuwa mateka/msukule apendavyo. Huna furaha. Humpendi Mungu au watu Wake. Una roho ya uchungu kwa wale ambao wanaona tabia yako ya kweli. Unaonekana kuwalaumu kwa maoni wanayochukua kuhusiana na kesi yako, lakini wewe ndiye wa kulaumiwa. Mwenendo wako umekuwa ule unaopaswa kupewa tahadhari na maonyo. Una wewe tu wa kujilaumu katika hili. {2Tsw 559.1}

Wewe ni mtu wa hatari kuhusiana na wengine, na umefanya mabaya mengi kwa ushawishi wako katika ----. Umeongoza badala ya kuongozwa. Umemvunjia Mungu heshima na unawajibika Kwake kwa kazi ya uovu ambayo umetenda kwa ushawishi wako. Mwenendo wako haukuwa safi, wenye kiasi, au staha na uzuri wa kuvutia. Hujakuwa na hofu ya Mungu mbele ya macho yako. Umekuwa ukijificha mara nyingi ili kutimiza mipango yako kwamba unabeba dhamiri iliyovunjwa. Msichana wangu mpendwa, isipokuwa utasitisha unayofanya tu mahali

ulipo, hakika uharibifu uko mbele yako. Acha kuota ndoto zako ya mchana, na kujenga magorofa hewani. Zuia mawazo yako yasikimbie kwenye mfereji wa upumbavu na ufisadi. Huwezi kushirikiana kwa usalama na wavulana. Wimbi la majaribu linaamshwa na kuongezeka ndani ya kifua chako, na huwa na tabia ya kung'oa kanuni, wema wa kike, na unyenyekevu wa Kweli. Ikiwa utaendelea katika mwenendo wako wa kukusudia, na kichwa kigumu, hatima yako ni nini? {2Tsw 559.2}

Mwaka mpya umetujia. Umenuia kufanya nini? Je! Umeamua nini kuwa kumbukumbu inayoletwa kwa Mungu na malaika wanaohudumu wa kazi yako siku hadi siku? Je, ni maneno gani ambayo umetamka yatakayotokea kwenye ukurasa wa kitabu cha kumbukumbu? Je! Ni mawazo gani ambayo Mchunguzaji wa mioyo atayapata kuwa yanapendwa nawe? Yeye ni mtambuzi wa mawazo, nia na makusudi ya moyo. Una rekodi ya kutisha ya mwaka uliopita, ambayo imewekwa wazi kwa Mtukufu wa mbinguni na mamilioni ya malaika safi, wasio na dhambi. Mawazo yako na matendo, hisia zako za kukatisha tamaa na zisizotakaswa, zinaweza kuwa zimefichwa kwa wanadamu; lakini kumbuka, matendo madogo sana katika maisha yako, yako wazi kwa Mungu. Una rekodi yenye mawaa, iliyoonekana mbinguni. Dhambi ambazo umetenda zote zimesajiliwa hapo. {2Tsw 560.1}

Uso wa Mungu uliokunjwa wa Mungu U juu yako, na bado unaonekana ni maskini wa hisia; hutambui hali yako ya kupotea na kuangamia. Wakati mwingine unakuwa na hisia za kujuta; lakini roho yako ya kiburi, na ya kujitegemea haraka inainuka juu ya hii, na kuzuia sauti ya dhamiri. Haufurahi, lakini unafikiria kwamba ikiwa ungekuwa na njia yako mwenyewe isiyozuiliwa ungefurahi. Mtoto masikini jamani! Unashikilia nafasi sawa na ile ya Hawa katika Edeni. Alifikiri kwamba angeinuliwa sana ikiwa angeweza kula tu tunda la mti ambalo Mungu alikuwa amemkataza hata kuugusa, asije akafa. Alikula, na kupoteza utukufu wote wa Edeni. {2Tsw 560.2}

Unapaswa kudhibiti mawazo yako. Hii haitakuwa kazi rahisi; huwezi kuikamilisha bila juhudi za karibu na hata kali. Lakini Mungu anataka hili kwako; ni wajibu unaotua kwa kila mtu anayewajibika. Unawajibika

kwa Mungu kwa mawazo yako. Ukiendekeza mawazo ya kipuuzi, ukiruhusu akili yako kukaa juu ya masomo machafu, wewe, kwa kiwango fulani, una hatia mbele za Mungu kana kwamba mawazo yako yalitekelezwa tayari. Kile tu kinachozuia hatua ya utekelezaji ni ukosefu wa fursa. Kuota ndoto za mchana na usiku, na kujenga majumba makubwa kwenye mafikara ni tabia mbaya na ya hatari sana. Wakati zinapoanzishwa, ni ngumu sana, ni kama haiwezekani kabisa kuvunja tabia kama hizo, na kuelekeza mawazo kwenye mada safi, takatifu, iliyoinuliwa. Unapaswa kuwa mlinzi mwaminifu juu ya macho yako, masikio yako, na akili zako zote ikiwa ungetawala akili yako na kuzuia mawazo yasiyo na maana na mabaya ili yasichafue roho yako. Nguvu ya neema pekee ndiyo inaweza kutimiza kazi hii inayotamanika zaidi. Wewe ni dhaifu katika mwelekeo huu. {2Tsw 561.1}

Umekuwa mpotovu, jasiri, na unayediriki. Neema ya Mungu haina nafasi moyoni mwako. Kwa nguvu ya Mungu peke Yake ndiyo unaweza kujileta mwenyewe ambapo unaweza kuwa mpokeaji wa neema Yake, chombo cha haki. Sio tu kwamba Mungu anakuhitaji wewe kudhibiti mawazo yako, lakini pia tamaa zako na mapenzi yako. Wokovu wako unategemea kujitawala kwako katika mambo haya. Shauku na mapenzi ni mawakala wenye nguvu. Endapo vitatumiwa vibaya, ikiwa vimewekwa kwa nia mbaya, ikiwa vitu hivi vimewekwa isivyo, vina nguvu kutimiza ajali ya uharibifu kwako na kukuachia uvunjifu mbaya na wenye huzuni, bila Mungu na bila tumaini. {2Tsw 561.2}

Mawazo yanapaswa kudhibitiwa vizuri daima na kwa juhudi ikiwa tamaa na mapenzi, dhamiri na tabia vitatiishwa. Uko hatarini, kwani uko juu ya hatua ya kutoa kafara, yale yahusuyo umilele kwenye madhabahu ya shauku. Shauku inapata udhibiti mzuri wa nafsi yako yote - shauku yenye ubora wa aina gani? Ya msingi wa chini, ya tamaa za mwili, yenye asili ya uharibifu. Kwa kuipa nafasi, utafanya maisha ya wazazi wako kuwa na uchungu, utaleta huzuni na aibu kwa dada zako, Hebu toa kafara ya tabia yako mwenyewe, na kisha upoteze mbingu na maisha matukufu ya kutokufa. Je! Uko tayari kufanya hivi? Nakusihi uachie hapo hapo ulipo. Usiendeleze hatua nyingine katika ukaidi, na ubaya; kwani mbele yako kuna taabu na mauti. Isipokuwa wewe utajidhibiti nafsi juu ya shauku na mapenzi yako, hakika utajiletea

mwenyewe sifa mbaya na wote wanaokuzunguka, na utajiletea aibu juu ya tabia yako ambayo itadumu maisha yako yote. {2Tsw 562.1}

Wewe Hautii wazazi wako, si mpole, huna shukrani, na sio mtakatifu. Tabia hizi duni ni matunda ya mti wa ufisadi. Wewe una kimbelembele. Unawapenda wavulana, na unapenda kuwafanya kuwa mada ya mazungumzo yenu. "Kinywa kinasema yatokayo katika moyo." Vitabia vimekuwa na nguvu kukudhibiti; na umejifunza kudanganya ili kutekeleza malengo yako na kutimiza tamaa zako. {2Tsw 562.2}

Sifikirii kuwa kesi yako haina tumaini; ikiwa ningefikiria hivyo, kalamu yangu haingekuwa inaandika kwenye mistari hii. Kwa uweza wa Mungu unaweza kukomboa yaliyopita. Jina lako tayari ni neno maarufu katika ----; lakini unaweza kubadilisha hili kwa kutumia uwezo ambao Mungu amekupa. Unaweza hata sasa kupata ubora wa maadili, ili jina lako lihusishwe na vitu safi na vitakatifu. Unaweza kuinuliwa. Mungu amekupa wewe msaada wa muhimu. Amekualika uje Kwake, na Ameahidi kubeba mizigo yako na kukupa raha ya roho. "Jifunzeni kutoka Kwangu," anasema Mwalimu wa mbinguni/Kiungu, "Kwa kuwa Mimi ni mpole na Mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha kwa roho zenu." Kwa muda mrefu umekuwa juu ya unyenyekevu huu na upole. Itabidi ujifunze somo hili muhimu la Mwalimu wa mbinguni kabla ya kupata lile pumziko lililoahidiwa. Umejifikiria sana wewe mwenyewe, juu ya busara na akili zako mwenyewe kwamba u mwerevu sana, kiasi kwamba imekuongoza kwa athari na ubatili na hata kukufanya ukaribie kuwa mpumbavu. Una ulimi wa udanganyifu, ambao umejiingiza katika upotoshaji na uwongo. Ah, msichana wangu mpendwa, ikiwa ungeweza kuamka tu, ikiwa dhamiri yako iliyolala, na iliyokufa ingewezwa kuamshwa, na uweze kuthamini maoni ya uwepo wa Mungu wa daima, na kujiweka chini ya udhibiti wa dhamiri iliyoangazwa, iliyoamka, ungelikuwa mwenye furaha mwenyewe na mbaraka kwa wazazi wako, ambao mioyo yao sasa unaiumiza. Unaweza kuwa chombo cha haki kwa wenzako unaoshirikiana nao. Unahitaji wongofu kamili, na bila hiyo uko katika uchungu kama wa nyongo na katika vifungo vya uovu. Unaweza kujiwazia uko huru ukifuata mwongozo wa akili yako mbaya, akili itakayoleta maumivu na hata kifo; lakini wewe u katika utumwa wa kudhalilisha zaidi. Bila

kanuni za dini, unaweza kujiona kuwa u mtu wa kuonewa wivu; lakini wote walio wema na waadilifu wataangalia tabia yako kwa huruma na mwenendo wako kwa kuchukizwa. Unaweza kuwa mshiriki wa tabia ya Uungu ikiwa utatoroka uharibifu uliomo duniani, kwa sababu ya tamaa; au kuchagua kwa kuwa mshiriki wake, unaweza kuzama katika ufisadi huu na kubeba mvuto wa kishetani. {2Tsw 562.3}

Una dada wadogo ambao wanaweza kubarikiwa na ushawishi wako. Unaweza kuangazia nuru tamu, ya thamani, katika familia ya baba yako na kuufurahisha moyo wake; au unaweza kuwa kivuli chenye giza, wingu, dhoruba ambayo litaleta uharibifu. Shauku yako ya kusoma ni ya tabia ambayo ikiendekezwa itapotosha mawazo na itathibitisha uharibifu wako. Isipokuwa unazuia mawazo yako, usomaji wako, na maneno yako, mawazo yako yatakuwa magonjwa bila matumaini. Soma Biblia yako kwa umakini, kwa maombi, na uwe ukiongozwa na mafundisho yake. Hili ndilo usalama wako. {2Tsw 563.1}

Achana na mambo ya wavulana. Katika jamii yao vishawishi vyako vinakuwa vya bidii na nguvu. Weka ndoa nje ya kichwa cha usichana wako. Haufai kwa hili kwa namna yoyote. Unahitaji uzoefu wa miaka kabla ya kuwa na sifa ya kuelewa majukumu, na kuchukua mizigo, ya maisha ya ndoa. Linda mawazo yako kwa hali chanya, shauku zako, na mapenzi yako. Usishushe hadhi hizi ili kuhudumu tamaa. Ziinue kwa usafi, uzitoe wakfu kwa MUNGU. {2Tsw 564.1}

Unaweza kuwa msichana mwenye busara, mnyenyekevu, mwema, lakini haliwezi hili kufanyika bila ya bidii. Lazima ukeshe, lazima uombe, lazima utafakari, lazima uchunguze nia yako na matendo yako. Chambua kwa ukaribu hisia zako na matendo yako. Je! Wewe, mbele ya baba yako, unaweza kufanya kitendo kibaya? Hapana, Hakika. Lakini unafanya hivi mbele ya Baba yako wa mbinguni, Aliye juu sana, mtakatifu sana, safi sana. Ndio; unauharibu mwili wako mwenyewe mbele ya malaika safi, wasio na dhambi, na mbele ya Kristo; na unaendelea kufanya hivi bila kujali dhamiri, bila kujali nuru na maonyo uliyopewa. {2Tsw 564.2}

Kumbuka, rekodi imeandikwa juu ya matendo yako yote. Lazima ukutane tena na mambo ya siri zaidi ya maisha yako. Utahukumiwa kulingana na matendo yaliyofanywa mwilini. Je, uko tayari kwa hili? Unajijeruhi mwenyewe kimwili na kimaadili. Mungu amekuamuru uhifadhi mwili wako katika utakatifu. " Je, hamjui kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu ..... nanyi si mali yenu wenyewe? Kwa maana mmenunuliwa kwa bei ya thamani kubwa; kwa hivyo mtukuzeni Mungu katika na miili yenu, na kwa roho zenu, ambazo ni za Mungu. Je, Mungu hatahukumu kwa kujidhalilisha kwako, kwa tamaa na shauku mbaya, na mapenzi yasiyofaa, pale atakapodai utajiri wa mapenzi na nafsi yako yote, kujitolea kwa huduma Yake? [ibada Kwake] {2Tsw 564.3}

Tena nakuonya kama mtu ambaye lazima akutane na mistari hii siku ile wakati kesi ya kila mtu itakapoamuliwa. Jitoe kwa Kristo bila kuchelewa; Yeye peke Yake, kwa nguvu ya neema Yake, anaweza kukukomboa kutoka kwa uharibifu. Yeye peke Yake Ndiye anayeweza kuleta nguvu zako za kimaadili na kiakili katika hali ya afya. Moyo wako unaweza kuwa na joto na upendo wa Mungu; uelewa wako, wazi na kukomaa; dhamiri yako, iliyoangaziwa, yenye wepesi, na safi; mapenzi yako, yaliyonyooka wima na yaliyotakaswa, chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu. Unaweza kuwa kile ambacho unachagua kuwa. Ikiwa sasa utakabilina na mabadiliko na kugeuka kabisa nyuzi 180 (180 degrees), Acha! kufanya uovu na ujifunze kutenda mema, basi utakuwa na furaha kweli kweli; utafanikiwa mapambano ya maisha, na utainuka kwa utukufu na heshima katika maisha yaliyo bora kuliko haya. "Chagua leo utakayemtumikia." {2Tsw 564.4}

## **SURA YA 66**

### **KWA MKE WA MTENDAKAZI**

Dada Mpendwa I: Jana nilikuwa na wakati wa kutafakari, na sasa nina mawazo machache ambayo ningetaka kuwasilisha kwako. Sikuweza

kujibu swali lako kwa urahisi kuhusu wajibu wako wa kusafiri na mume wako. Sikuwa bado nimejifunza matokeo ya kuandamana naye; kwa hivyo sikuweza kuzungumza kwa uelewa kana kwamba nilikuwa najua ushawishi uliokuwa umetoa kwa watu. Siwezi kutoa shauri gizani. Lazima nijue ushauri wangu ni sahihi katika nuru. Faida kubwa inachukuliwa kwa maneno yangu, kwa hivyo lazima nienende kwa uangalifu sana. Baada ya kutafakari kwa uangalifu, kutafuta kuita vitu ambavyo vimekuwa vikionyeshwa kwangu kuhusiana na kesi yako, sasa niko tayari kukuandikia. {2Tsw 565.1}

Kutoka katika barua ulizoniandikia mimi zikimlenga Kaka J, nina hofu kwamba una chuki na wivu juu yake. Nina matumaini kuwa hii sio shida ya jambo lenyewe, lakini nina hofu ndiyo kesi ilivyo. Wewe na mume wako mna fikra za wivu sana, kwahiyo mnahitaji kujilinda katika mwelekeo huu. Hatuhisi kuwa Kaka J anaonekana kuwa sawa kwa mambo yote. Tunafikiri kuwa mke wake yuko mbali kutoka katika haki na ana ushawishi mkubwa juu yake; ila bado tuna tumaini kuwa kama mambo yote yataenda kwa hekima kuhusiana na yeye, na kisha atarejea mwenyewe kutoka katika mtego wa shetani na kuona vitu vyote kwa usahihi.(2Tsw 565.2)

Mpendwa Dada, tumeamua kutokuwa na upendeleo na bila kuwa na maneno yetu au matendo yetu katika namna yoyote ile kushawishika kwa kusikia tu, kwamba fulani kasema hivi au vile. Hatuna tunaowaweka karibu na kuwabembeleza au kuwadekesha-pets. Acha Bwana atupe hekima ya kimbingu, kwamba tutende kwa haki na bila ya upendeleo, na hivyo tukutane na akili ya Roho Wake. Hatuhitaji kazi zetu zifanywe kwa ubinafsi. Hatuhitaji hisia za mtu binafsi. Kama tunafikiri kuwa sisi sio maalum kuhusishwa, au kama tunaona au kudhani kuwa tunaona kutelekezwa ambako ni chanya, basi tunahitaji roho ya msamaha ya Bwana wetu. Watu waliodai kuwa wafuasi Wake hawakumpokea, kwa sababu alikaza uso kuelekea Yerusalemu, na hakutoa ishara yoyote maalum kwamba angekaa pamoja nao. Hawakufungua milango yao kwa Mgeni huyu wa Mbingu, na hawakuona hitaji la Yeye kushikamana nao, ingawa walimuona mwenye kuchoshwa na safari, na usiku ulikuwa unakaribia. Hawakutoa ishara yoyote kuwa kwa hakika wanamhitaji Yesu. Wanafunzi walijua

kuwa Yesu alipanga kukaa pale usiku ule, na hivyo walihisi kwa umakini kile alichofanyiwa Bwana wao na hivyo walikuwa wenye hasira, na walimuomba Yesu aonyeshe hasira na aite moto kutoka mbinguni ili kuwaangamiza hao ambao wamembeza au kumnyanyasa. Lakini Yesu alikemea ghadhabu na shauku yao kwa uadilifu, na akawaambia sikuja kuhukumu bali kuonyesha rehema. (2Tsw 566.1)

Somo hili la Mwokozi wetu ni kwa ajili yako wewe na mimi. Chuki haipaswi itawale mioyo yetu hata, tukitukanwa hatupaswi kurudisha matusi. Ooh hisia za wivu na kushuku watu bila hata ushahidi, ni tabia mbovu kiasi gani umeleta! Ni kwa kiasi gani umeugeuza urafiki na upendo kuwa uchungu na chuki! Hatupaswi kujikweza, kujiona kuwa bora, kujipenda nafsi, na kufa katika maslahi yetu wenyewe. Ni lazima mivuto yetu izamishwe katika Kristo na ndipo tutaweza kusema: "Ninaishi; lakini si mimi bali Kristo ndani yangu." Kristo ametuambia namna ya kufanya kila kitu kuwa rahisi na furaha tupitiapo Kwake.' "Njooni Kwangu ninyi vyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu." Ugumu mkubwa ni kuna kiasi kidogo sana cha upole na unyenyekevu kiasi kwamba nira ni chungu na mzungu ni mzito. Tunapomiliki upole wa Kweli na unyenyekevu tutakuwa tumezama kabisa katika Kristo hatutabeza au kupuuza moyoni; sisi ni viziwi kwa malaumu na vipofu kwa dharau na matukano. (2Tsw 566.2)

Dada I, kama upekee wa kesi yako ulivyonijia kwa usahihi mbele zangu, ninaona pingamizi zito la safari yako. Hukuchua mizigo ambayo unayostahili kuchukua. Wewe unahitaji watu wengine wakuhurumie, bali wewe huwa hauwahurumii wao. Umeweka uzito pale ulipo, na mara nyingi ulisubiri juu ya wale wenye kubeba mizigo yao wenyewe na wewe mwenyewe ukishindwa kufanya hivyo peke yako. Huna msaada kabisa kwa faida yako mwenyewe, na ushawishi wako sio kama wa mke wa mchugaji anavyopasa awe. Unahitaji kazi za mikono zaidi ya ulizo nazo na kulingana na vile nilivyoonyeshwa ninafikiri ungekuwa zaidi katika mstari wa jukumu lako kushiriki kwa furaha katika kazi ya kumwelimisha msichana wako, na kuhimiza upendo wa majukumu ya nyumbani. Hukupokea elimu katika mwelekeo huu katika usichana



wako, na hii imeyafanya maisha yako kutokuwa na furaha kuliko ambavyo ingekuwa. Hupendi kazi za mikono; na unaposafiri unahisi unakuwa kama mlema, na kushindwa kuwa msaada na kufanya uwezavyo ili kuangazia mizigo uliyoitengeneza mwenyewe. Umeshindwa kutambua kuwa mara nyingi wale wanaokusubiri wewe, hawawezi kufanya kazi ya ziada kama wewe usivyoweza, unawaegemea wengine, na unaweka uzito wako wote juu yao. Sina ushahidi kuwa Mungu alikuwa kufanya kazi maalumu katika kusafiri. (2Tsw 567.1)

Unayo elimu ya kujifunza ambayo bado hujaimiliki. Ni nani awezaye kumfundisha mtoto vizuri kama mama? Ni mwanamke gani awezaye kujifunza kasoro zake katika taasisi yake mwenyewe na kwa watoto wake kama mama katika utendaji wake wa majukumu ambayo mbingu imempa? Uhalisia wa kwamba hupendi hii kazi siyo ushahidi kuwa hii sio kazi ambayo Bwana alikuteulia wewe. Huna nguvu za kimwili na kiakili kutosheleza kukufanya wewe kusafiri. Unataka kutumikiwa/kuhudumiwa, badala ya wewe kutumikia wengine. Wewe bado hujawa mtu wa kusaidia vya kutosha, ili kukomesha mzigo ulio nao kwa mume wako na wale wakuzungukao. (2Tsw 567.2)

Wale ambao hawawezi kusimamia mtoto/watoto wao kwa busara, hawana sifa za kufanya mambo kwa hekima katika mambo ya kikanisa au kujihusisha na ushupavu wa akili itawaliwayo na Shetani kwa njia ya majaribu, kama wangeweza kwa furaha na upendo kufanya sehemu ya matakwa yao kama wazazi, ndipo wangeelewa kwa uzuri namna ya kubeba mizigo ndani ya kanisa. Mpendwa Dada, Nakushauri uwe mke mwema kwa mume wako na nyumbani kwa ajili yake. Tegemea rasilimali zako mwenyewe, na punguza kuelemea sana juu yake. Simama wewe mwenyewe kwa ile kazi ambayo Bwana angekupa kuifanya. Mwelekeo wako ni kuwa na kiherehere kufanya kazi kubwa, ili kutimiza utume mkubwa, na kupuuza au kubeza kazi ndogo ndogo njiani mwako, ambazo zina umuhimu sawa kukamilishwa kama zile kubwa. Hebu matamanio yako yaamshwe ili kutumika, kuwa mtenda kazi badala ya kuwa mtazamaji. (2Tsw 568.1)

Dada yangu mpendwa, Mimi ninasema waziwazi na sithubutu kusema vinginevyo. Ninakuomba sana uichukue mizigo ya maisha badala ya kuikwepa. Msaidie mume wako kwa kujisaidia mwenyewe. Fikra ambazo mmezishikilia kuhusiana na heshima ya wachungaji inavyopasa kuhifadhiwa, haiendani na mujibu wa mfano wa Bwana wetu. Mtumishi wa Kristo lazima aonyeshe kuwa na utulivu, upole, upendo, uvumilivu, kujizuia, huruma, kujistahi na adabu. Mchungaji lazima achukue tahadhari kwa hekima, mazungumzo na mawazo mapana, na mwenendo usiolaumika. Hii ndio hadhi ya injili. Lakini kama mchungaji akija katika familia ambapo ataweza kujihudumia mwenyewe, kwa namna yoyote basi afanye hivyo, na kwa mfano wake ahimise ufanyaji wa shuguli/kazi kwa kujihusisha na kazi za mikono wakati akiwa bado hana wingi wa mizigo na majukumu mengine. Mchungaji hatajiondolea heshima yake, na kwa ubora atajihusisha katika afya na uzima akijihusisha katika kazi muhimu. Mzunguko wa damu utakuwa wa ulinganifu, kazi za mikono, zitapunguza msongo wa ubongo, na zitaleta damu kutoka kwenye ubongo. Ni muhimu kwa mume wako kuwa na kazi za mikono zaidi ili kuupa ubongo nafuu (kupumzisha). Mazoezi ya mwili yatausaidia mmeng'enywa wa chakula. Kama angetumia sehemu ya muda wa kila siku kwa mazoezi, wakati sio vyema kusisitiza kwa juhudi ya muda mrefu kwa sababu ya vikao, ingekuwa ni faida kwake, na asingejiondolea heshima kutoka katika huduma yake. Mfano ungekuwa kwa mujibu wa ule wa Bwana wetu. (2Tsw 568.2)

Tunawapenda na tunataka mfanikiwe katika jitihada zenu za kunuia kupata Maisha bora Steamer ``Keokuk, Mto mississippi``, Sept 30, 1869. (2Tsw 569.1)

## SURA YA 67

### UWAKILI USIO NA UAMINIFU

Mpendwa kaka K, Vitu vichache vinanishinikiza akilini mwangu, ninahisi jukumu la kuandika kwa Kaka L na kwako. Nimehusianisha kiini cha jambo lako; lakini kama nilivyo na mzigo akilini mwangu; nitaandika. Nilioneshwa kwamba kuhusiana nawe, ubinafsi umekuwa wa kwanza kwako (Mimi na Yangu imetangulia). Umekuwa na kujijali sana mwenyewe, kiasi kwamba Bwana hana sehemu ya kufanya kwako. Hujampa Yeye nafasi yoyote. Kwa kiasi kikubwa, Amempa Ndugu L na wewe mwenyewe kazi kulingana na maamuzi yenu mwenyewe, ili muweze kusadiki kuwa hekima yenu ni upumbavu. Hujafanya kazi kwa masilahi ya wajane na Yatima, kama Bwana alivyoamuru juu ya wafuasi Wake; wala hujafanya shauri la masikini wa Bwana kuwa lako, kwa kutekeleza maslahi yao mapana, wala hujatafuta kumpa Mungu utukufu na kulitukuza Jina lake; kwahiyo sasa Bwana amekupa mateso wewe na Ndugu L kufuatana na sababu ya chaguzi zenu wenyewe. Yeye Ameruhusu mjichunguze ninyi wenyewe. Maslahi yenu ya ubinafsi yamekuwa ni msingi wa matendo yenu, na mtavuna kwa kile mlichopanda wenyewe. Nalionyeshwa kuwa hakika mtapokea tuzo mapema au baadae kufuatia huduma za maslahi yenu binafsi. ``Toa hesabu ya wakili wako`` lazima isikike kwako. Mnawajibika kwa Mungu kwa kazi mliyopewa ambayo kwa fedheha imeipuuza, ili kujitumikia wenyewe. (2Tsw 569.3)

Kama mngelikuwa mkitafuta kujionyesha kuwa mmekubaliwa na Mungu, huku mkitafuta ufalme wa Mungu na haki ya Kristo, mngekuwa mnaifanya kazi za Kristo. Masikini, wajane, na yatima wangeita kutoka kwenu, huruma nyororo, kujali, upendo sikitiko na utu wema, ungelikuwa na shauku nao na kuwatendea kama vile ambavyo ungetaka mkeo na watoto wako watendewe mema endapo wangeachwa kuwa tegemezi na wenye mateso kutoka ulimwengu wa wasio na huruma, hisia baridi, au Wakristo wasio na moyo wa huruma.

Katika upande wako kumekuwa na sehemu ya huzuni, ya kutohisi shida za watu, na moyo uliopuuza wasio na bahati, moyo usio na upendo kwa watu wenye majanga. Umetumikia maslahi yako mwenyewe, bila kujali mahitaji yao makuu. Mungu hawezi kukubariki mpaka uone dhambi yako juu ya mambo haya. (2Tsw 570.1)

Niliona kuwa kazi ya Bwana, haina utukufu katika macho yako kuliko bishara zako mwenyewe. Mambo ya umilele hayajatambulika. Bwana ametoa maonyo na mashutumu ili kukuamsha katika ufahamu wa jukumu lako, kwa kukufanya ujue ni nini kinachotarajiwa toka kwako. Lakini hukuyatilia maanani maonyo haya. Bado hujatambua kuwa unashughulika na Mungu. Mmemuibia Mungu na kujihudumia ninyi wenyewe. (2Tsw 570.2)

Wapo wengi katika imani njema, wamejitoa mhanga kwa kutoa fedha katika ofisi ili kuwapata wengine. Baadhi ya wanaume na wanawake, wamefanya kazi kwa bidii na kuweka wakfu fedha kwa Bwana, mapato haya ya kazi ngumu na ya uchumi wao na wametoa kwaajili ya ofisi ili kuendeleza kazi. Wajane na masikini wametoa karibu kila kitu wanachokitegemea katika kujikimu, kwa kumwamini Mungu kuwa atawatunza, na pia wamejiweka wakfu kwa Bwana kwa njia ya maombi na machozi, na bado wamejitoa kwa furaha wakijihisi kuwa walikuwa wanasaidia kazi kubwa ya kuokoa roho. Familia masikini wameuza ng'ombe wao wa pekee, wakijikana nafsi zao na za watoto wao wadogo, wasinywe maziwa, wakihisi pia kuwa wanamtolea Mungu sadaka. Wameweka mali zao kwenye ofisi kwa imani thabiti. Ubinafsi na usimamizi mbaya umesaidia ubadhirifu kwa njia hii. Mungu anawashikilia wale ambao wanawajibika kutunza mali hii kwa ajili Yake. Mungu huwawajibisha wale ambao wameshughulikia; "Toa hesabu ya uwakili wako" itasikika haraka sana. Hebu Bwana akusaidie ujiweke huru kutoka katika kila laumu. (2Tsw 571.1)

Battle Creek, Michigan,  
Jan 17, 1870

## MAKOSA YA KUHISIA

Mpendwa Dada M: Shauri lako liko katika akili yangu, na siwezi kuepuka kukuandikia dhamira yangu kutokana na nilichokiona kwako. Nimeridhishwa mawazoni kwamba unasafiri katika ukungu na giza. Hauoni vitu katika nuru sahihi. Umepofusha macho yako katika shauri lako mwenyewe kwa kujitetea hivi: “Nisingefanya hivi au vile kama kusingekuwa na ushawishi wa wengine ambao umeniongoza kwa hatua hiyo. {2Tsw 571.2}

Unaendelea kutafuta makosa kwa hali yoyote, Kitu ambacho ni kutafuta makosa kuhusiana na riziki ya Mungu. Umeendelea kujitolea kwa watu fulani au vitu kujibu nafasi ya Mbuzi wa Azazeli, pale ambapo unaweza kuweka lawama ya kukuleta wewe katika nafasi ya kujihisi na kuongea yasiyostahili kwa Mkristo. Badala tu ya kujilaumu mwenyewe, kwa kasoro zako, unalaumu hali ya mambo, matukio na mazingira ambayo yamekupelekea kuwa na tabia ambayo imelala au iliyojificha chini ya uso, isipokuwa kitu fulani kiinuke kwa kusumbua na kuamsha tabia hizo kuwa hai na kuwa katika utendaji. Basi zitaonekana katika ulemavu na nguvu zake zote. (2Tsw 571.3)

Unajidanganya mwenyewe katika dhana hii kwamba hazipo tabia ambazo hazipendezi kwako, mpaka uletwe katika nafasi ambazo zitakufanya utende na kuongea katika namna ambayo itazifunua kwa wote. Hauko tayari kuona na kuungama kwamba ni asili yako ya matendo ya mwili ambayo bado haijabadilishwa na kutiishwa kwa Kristo. Bado haujaisulubisha nafsi yako. (2Tsw 572.1)

Mara zingine siku na wiki hupita bila kuendeleza roho za uovu ambazo nimezitaja kama, kukosa subira, roho ya kidkteta, na shauku ya kumtawala mumeo. Kupenda kutawala wengine na kuwaleta katika kwenye maoni yako, kumekaribia kukuharibu wewe na mumeo. Unapenda kupendekeza na kuamuru wengine. Unapenda watu

wadhanie na kuona kuwa kwako kuna nuru bora zaidi, na kwamba una uongozi maalumu kutoka kwa Mungu. Na kama wasingefanya hivyo, unaanza kuwashuku, kuwa na wivu, kuhisi roho ya machafuko; huridhiki na kwa kiwango kikubwa huna furaha kabisa. {2Tsw 572.2}

Hakuna kitu kinachoamsha kwa urahisi sifa mbaya katika tabia yako kama, kupingwa kwa hekima yako na maamuzi yako kwa kutumia mamlaka yako. Roho yako yenye nguvu ya kutawala na kujiona wewe ndiye bora, ambayo ilionekana kusinzia, inaamshwa katika nguvu kamili. Ubinafsi unakutawala na huongozwi tena kwa mawazo ya wazi na hekima, na maamuzi ya utulivu kuliko mtu mwenda-wazimu. Ubinafsi katika nguvu zake zote hushindana kwa ustadi, na itachukua akili imara kuweza kukuzuia. Baada ya wazimu wako kupita, hapo ndipo unaweza kuvumilia, njia zako kuulizwa. Lakini unasimama tayari kujihesabia haki kwa kusihi kwamba wewe huchukulia mambo kwa njia nyeti sana; una hisia zenye kina; unateseka sana. Niliona ya kuwa haya yote hayatakupa udhuru wewe, mbele za Mungu. Unachanganya kiburi na hisia nyeti. Ubinafsi unajiinua kwako. Wakati ubinafsi unaposulubiwa, ndipo hisia hizi nyeti au kiburi zitakufa; vinginevyo wewe sio Mkristo. Kuwa Mkristo ni kuwa kama Kristo Mwenyewe, kuwa mnyenyekevu, mpole, na roho tulivu, vitabeba ukinzani bila ya kukasirika na kuwa kama mwendawazimu. Ikiwa udanganyifu uliofunikwa utararuliwa vipande vipande, ili kwamba uweze kujiona mwenyewe kama vile Mungu akuonavyo, hutatafuta tena kujihesabia haki mwenyewe, lakini utaanguka kabisa kwa Kristo na kuvunjikavunjika, Yeye pekee tu, Ambaye ndiye anaweza kuondoa kasoro zako katika tabia yako, na kukuganga wewe kwa kukufanya uwe mzima. {2Tsw 572.3}

## SURA YA 69

### MAKUTANO

Mungu alitoa mwongozo kwa Waisraeli kukusanyika mbele Zake kwa vipindi maalumu vilivyowekwa, mahali ambapo Yeye angepachagua kuzitunza siku maalumu ambazo hakuna kazi isiyo ya lazima inapaswa kufanywa, bali muda wa kujitolea kwa kuzingatia Baraka ambazo Mungu ametoa. Katika misimu hii maalumu walipaswa kuleta zawadi, sadaka za hiari, na sadaka za shukrani kwa Bwana, kwa kulingana na alivyokuwa amewabariki. Mtumwa na mjakazi, mgeni, yatima na mjane walielekezwa kufurahi kwamba kwa nguvu Zake Mungu na kwa mkono hodari, Yeye aliwatoa katika kifungo cha utumwa hadi furaha ya uhuru. Nao waliamriwa wasijihudhurisha mbele za Bwana mikono mitupu. Walitakiwa kuleta zawadi zao za shukrani kwa Mungu kwa rehema Zake za daima na baraka walizopewa. Sadaka hizi zilitofautiana kulingana na baraka za mtoaji alizoweka juu yao na hivyo walikuwa na fursa ya kufurahi. Hivyo tabia za watu kwa uwazi ziliendelezwa na kukua. Wale ambao waliweka thamani kubwa juu ya Baraka hizi ambazo wamepewa na Mungu, walileta matoleo yao kulingana na thamani ya Baraka hizo. Wale ambao nguvu zao za kimaadili zilipumbazwa na kufa ganzi kwa ubinafsi na ibada ya sanamu, wapendao kupokea fadhila, badala ya kusukumwa na upendo wa dhati kwa Mtoaji wao mkarimu, walileta matoleo kidogo. Kwahiyo mioyo yao ilifichuliwa. Licha ya siku hizi maalumu za sherehe za kidini za furaha na shangwe, pasaka ya kila mwaka ilipaswa kukumbukwa na taifa hili la Kiyahudi. Bwana aliweka agano kwamba ikiwa wangekuwa waaminifu katika kuyashika maagizo Yake, Yeye angewabariki katika maongezeko yao yote na kwa kila kazi zao zote za mikono. {2Tsw 573.1}

Mungu hajataka pungufu ya kile cha taifa la Israeli kwa watu Wake katika kipindi hiki cha mwisho, katika kafara na dhabihu. Wale ambao Yeye amewabariki kwa uwezo, na hata mjane na yatima, hawapaswi kusahau Baraka Zake. Hasa wale ambao Mungu amewafanikisha na kuwapa vitu ambavyo ni Vyake, hawa wanapaswa kujihudhurisha mbele Zake, wakiwa na roho ya kujitolea na kuleta sadaka kulingana na

baraka ambazo Bwana amewapa. Lakini wengi ambao Mungu amewafanikisha wameonyesha kutokuwa na shukrani Kwake. Ikiwa Baraka Zake zipo juu yao, na Yeye huwaongezea utajiri wao, wanafanya fadhila hizi kuwa kama kamba za kuwafunga kwa kupenda mali zao; wanaruhusu bishara ya kidunia kuchukua mapenzi yao na utu wao wote, na kupuuzia ibada na haki ya Kidini. Hawana uwezo wa kuacha bishara zao na kuja mbele za Mungu hata mara moja kwa mwaka. Wanageuza Baraka za Mungu kuwa laana. Wanatumikia maslahi yao ya muda kwa kupuuzia matakwa ya Mungu. {2Tsw 574.1}

Wanaume wamilikio maelfu hubaki nyumbani mwaka baada ya mwaka, wakijishughulisha kwa bidii sana, shughuli zao za kiulimwengu na mivuto yake, na hujihisi kuwa hawawezi kutoa kafara ndogo ya kuhudhuria mikutano ya kila mwaka ya kumwabudu Mungu-makambi. Yeye Amewabariki katika vikapu na ghala zao na kuwazunguka kwa faida Zake upande wa kulia na wa kushoto, lakini wanamzuia matoleo madogo ambayo Yeye ameyataka kutoka kwao. Wanapenda kujitumikia. Nafsi zao zitakuwa kama jangwa lisilosafishwa na umande au mvua ya mbinguni. Bwana amewaitea Baraka ya thamani ya neema Yake. Yeye amewaokoa kutoka katika utumwa wa dhambi na utumwa wa makosa, na kuwafungulia katika giza lao ufahamu wa nuru ya utukufu wa Ukweli wa sasa. Na Je, ushuhuda huu wa upendo na rehema za Mungu hautoi mwito wa kurudisha shukrani? Je! Wale wale wanaodai kuamini kuwa mwisho wa vitu vyote umekaribia watakuwa vipofu kwa maslahi yao ya kiroho na kuishi kwa ulimwengu huu na maisha haya peke yake? Je! Wanatarajia kuwa maslahi yao ya milele yatajishugulikia wenyewe? Nguvu za kiroho hazitakuja bila juhudi yoyote kutoka kwao. {2Tsw 574.2}

Wengi wanaodai kutazamia kutokea kwa Bwana wetu wana wasiwasi, ni watafutaji wa mizigo kwa faida ya kidunia. Wamekuwa vipofu kwa maslahi ya milele. Wanafanyia kazi kile ambacho hakiwatoshelezi. Wanatumia pesa zao kwa kile ambacho si mkate/chakula. Wanajitahidi kujiridhisha kwa hazina walizo nazo zilizowekwa juu ya ardhi, ambayo lazima iangamie. Nao wanapuuza maandalizi ya umilele, ambayo yanapaswa kuwa kazi ya kwanza na ya Kweli katika maisha. {2Tsw 575.1}



Hebu wale wote wanaoweza, wahudhurie mikutano hii ya kila mwaka. Wote wanapaswa kuhisi kuwa Mungu anataka hili kwao. Ikiwa hawatachangamkia upendeleo ambao Yeye ameutoa ili kwamba wawe imara ndani na nguvu ya neema Yake, watadhoofika na kudhoofika zaidi, na watapungukiwa zaidi na zaidi shauku yao yote ya kujiwekwa wakfu kwa Mungu. Njooi Ndugu na Dada kwenye mikutano hii mitakatifu ili kumtafuta Yesu (convocations). Yeye Atakuja kwenye sikukuu. Atakuwepo na atafanya kwa ajili yako yale yote ambayo unataka yafanywe. Mashamba yako hayapaswi kuzingatiwa kwa uthamani mkubwa kuliko maslahi ya roho. Hazina zote ulizo nazo, , hata ziwe za thamani kiasi gani, hazitaweza kukununulia amani na matumaini, ambayo itakuwa faida isiyo na kikomo, ikiwa itakugharimu yote uliyonayo na taabu na mateso ya maisha. Hisia imara ya mambo ya umilele na moyo ulio tayari kutoa vyote kwa Kristo ni baraka za thamani zaidi kuliko utajiri na raha zote na utukufu wa ulimwengu huu. {2Tsw 575.2}

Mikutano hii ya makambi ni ya umuhimu. Inagharimu kitu. Watumishi wa Mungu wameyatoa maisha yao na kupata uchovu, kwa kuwasaidia watu, ambapo wengi wao wameonekana kana kwamba hawahitaji msaada. Kwa hofu ya kupoteza kidogo faida yao ya ulimwengu huu, baadhi wameacha fursa hizi za thamani kuja na kwenda kana kwamba zilikuwa na umuhimu mdogo. Hebu wale wote wanaodai kuuamini Ukweli, waheshimu kila fursa ambayo Mungu huwapa ili kupata kuona vema juu ya Kweli Yake, vigezo Vyake, na matayarisho muhimu kuhusiana na ujio Wake. Upole, furaha, utii na uaminifu kwa Mungu, hivi ndivyo anavyohitaji. {2Tsw 576.1}

Haupaswi kujichosha na mahangaiko na shughuli nyingi zisizo na lazima. Kwa uaminifu fanya kazi ambayo kwa majaliwa ya Mungu, Yeye amekupatia, Naye Mungu atakujali. Yesu atazidisha na kupanua Baraka zako. Lazima ufanye kwa bidii ikiwa kuna wokovu mwishoni. Njoo katika mikutano hii, tayari kuifanya kazi. Acha wasiwasi wako wa nyumbani na uje kumtafuta Yesu, Naye atapatikana kwako. Njoo na sadaka zako kama vile Mungu alivyokubariki. Onyesha shukrani kwa sadaka yako ya hiari kwa Muumba wako, mtoaji wa fadhila zote.

Asiwepo yeyote atakayekuja mikono mitupu. “Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mibinguni, na kuwafungulieni Baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la.” {2Tsw 576.2}

## SURA YA 70

### MIKUTANO YA KIJAMII

Hivi majuzi nilipokea barua kutoka kwa ndugu ambaye ninamheshimu sana, akiuliza kuhusu ni jinsi gani mikutano inapaswa kufanywa. Aliuliza ikiwa kuna maombi mengi yatakayotolewa mfululizo, na kisha pumziko la muda mchache na maombi kadhaa tena. {2Tsw 577.1}

Kutokana na nuru niliyokuwa nayo juu ya mada hii mimi nimeamua kuwa Mungu hahitaji sisi tunapokusanyika kwa ajili ya ibada Yake, kufanya hivi vipindi viwe vya kutaabisha na vya kuchosha kwa kubaki kusujudu kwa muda mrefu kabisa (sana), tukisikiliza maombi kadhaa ya muda mrefu. Wale walio na afya dhaifu hawawezi kuvumilia kutumia nguvu kwa njia hii na kuuchosha mwili sana. Mwili unachoka kwa kubaki umeinana hivyo muda mrefu; na kibaya zaidi, akili inachoka sana kwa kuendeleza zoezi hili la maombi ambapo hakuna burudiko la kiroho linalopatikana, na mkutano unakuwa mbaya kwao zaidi ya kupoteza. Watu wamechoka kimwili na kiakili na hawajapata nguvu za Kiroho. {2Tsw 577.2}

Mikutano ya Konferensi na sala haipaswi kufanywa kuwa ya kuchosha. Ikiwezekana yote ifanyike kwa muda uliopangwa, na ikiwa kuna mmoja

anayechelewa, kwa nusu saa au hata dakika kumi na tano, kusiwe na kusubiri. Hata ikiwa wapo watu wawili tu, wanaweza kudai ahadi hiyo. Mkutano unapaswa kufunguliwa kwa muda ule uliopangwa ikiwa inawezekana, kukiwa na watu wachache au wengi. Kaida na ushupavu baridi vinapasawa kuwekwa kando, na wote wanapaswa kuchochewa kwa jukumu la kutunza muda. Katika matukio ya kawaida hakupaswi kuwa na maombi ya zaidi ya dakika kumi. Baada ya kuwa na mabadiliko ya ratiba au mkao, na zoezi la kuimba au kuhimizana au kutiana moyo, ili kuondoa yale yenye desturi za ratiba zenye kuchosha watu au kuboeshia na kufanya watu wapungukiwe na shauku, basi, ikiwa yeyote anahisi kuwa na mzigo wa maombi, hebu na waombe. {2Tsw 577.3}

Wote wanapaswa kuhisi kuwa ni jukumu la Mkristo kuomba kwa ufupi. Mwambie Bwana kile unachotaka, bila ya kuzunguka-zunguka ulimwengu mzima. Katika maombi ya faragha wote wana fursa/nafasi ya kuomba kadiri ya wanavyotamani na kujieleza jinsi watakavyo. Wanaweza kuwaombea ndugu zao na marafiki. Katika chumba cha faragha ndio mahali pa kusemea shida zao binafsi, mitihani na majaribu yao. Mkutano wa kawaida wa wote, ni wa kumwabudu Mungu na sio sehemu ya kufungua siri za moyoni. {2Tsw 578.1}

Ni nini lengo la kukusanyika pamoja? Je! Ni kumfahamisha Mungu, na kumfundisha/kumuelekeza kwa kumwambia yote tuyajuayo kwa maombi? Tunakutana pamoja ili kujengana na kubadilishana mawazo na hisia, kukusanya nguvu, nuru, na ujasiri kwa kufahamishana na wengine matumaini na matamano; na kwa sala zetu za dhati za kutoka moyoni na bidii, zinazotolewa kwa imani, tunapata burudiko na nguvu kutoka kwa Chanzo cha nguvu zetu. Mikutano hii inapaswa kuwa misimu yenye thamani zaidi na inapaswa kufanywa kuwa ya kuvutia kwa wote ambao wanapendezwa, na kuwa na ladha na mambo yoyote ya kidini. {2Tsw 578.2}

Kuna wengine, ninaogopa, ambao hawachukui changamoto/masumbufu yao kwa Mungu kwa maombi ya faragha, lakini wanayahifadhi hadi kwenye mkutano wa maombi, na huko hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Hivyo hao wanaweza kuitwa

kama wauaji wa mkutano wa maombi (prayer killers). Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao yenye ubaridi ulioganda, shuhuda refu za kurudi nyuma hutupa kivuli. Watu wote wanashangilia wanapokamilisha, na haiwezekani kutupa fadhaa, ubaridi na giza ambalo sala zao na miito yao ya kuhimiza, huleta kwenye mkutano. Kutoka katika nuru ambayo nimeipokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na kijamii, na isiyo mirefu sana. Kujihifadhi, kutoonyesha moyo wa kirafiki, kiburi, ubatili, na hofu juu ya mwanadamu yapaswa kuachwa nyumbani. Kutofautiana kudogo na chuki havipaswi kuchukuliwa nasi kwenye mikutano hii. Kama familia yenye umoja, unyenyekevu, usahili upole, ujasiri, na upendo, hivi vinapaswa kuwepo mioyoni mwa ndugu na dada wanaokutana ili kuburudishwa na kuimarishwa kwa kuleta nuru/mianga yao pamoja. {2Tsw 578.3}

“Ninyi ni nuru ya ulimwengu,” anasema Mwalimu wa Mbinguni. Wote hawana uzoefu sawa katika maisha yao ya kidini. Lakini wale walio na uzoefu tofauti-tofauti huja kwa pamoja na kwa usahili na unyenyekevu wa akili, na kuongea juu ya uzoefu wao. Wote wanaokazana kupata mwenendo wa kusonga mbele wa Kikristo wanapaswa kuwa, na watakuwa na uzoefu ambao unaishi, ambao ni mpya na wa kuvutia. Uzoefu hai umeundwa na mitihani ya kila siku, migogoro, na majaribu, juhudi kubwa na ushindi, na amani kubwa na furaha inapatikana kupitia kwa Yesu. Uhusiano rahisi wa uzoefu kama huu unatoa nuru, nguvu, na maarifa ambayo yatasaidia wengine katika maendeleo ya maisha ya kimbingu/Kiungu. Ibada kwa Mungu inapaswa kuwa ya kupendeza na kufundisha kwa wale ambao wana mapenzi yoyote ya mambo ya Kiungu na ya kimbingu. {2Tsw 579.1}

Yesu Mwalimu (Rabi) wa kimbingu, hakujitenga mbali na wana wa Adamu na kutoonyesha urafiki, bali ili awafaidishe watu, alitoka mbinguni na kuja duniani, ambapo wapo, kwamba usafi na utakatifu wa maisha Yake uweze kuangaza juu ya njia zote na kuangaza njia ya mbinguni. Mkombozi wa ulimwengu alifikiri kufanya maelekezo ya mafundisho Yake kuwa wazi na rahisi, ili wote waweze kuyaelewa. Kwa ujumla alichagua sehemu ya wazi kwa mazungumzo Yake. Hakuna kuta ambazo zingezuia makutano yaliyomfuata; lakini alikuwa na sababu maalumu za kukimbilia mashambani na kando ya bahari ili

kutoa masomo ya mafundisho Yake. Pale kwenye uwazi aliweza kuwa na uthibiti wa mazingira na kuyatumia kama vielelezo na picha ambazo watu wa maisha ya kawaida waliweza, kutambua vyema, na hivyo kuwa vielelezo vya Kweli muhimu ambavyo aliwajulisha. Pamoja na masomo Yake ya maelekezo, alihusisha kazi za Mungu katika asili. Ndege ambao walikuwa wakiimba nyimbo zao kwa furaha bila ya kujali masumbufu, maua ya kondeni yaking'aa kwa uzuri, yungiyungi maua ya majini ambayo yalitulia kwa usafi wake katika ziwa, miti mirefu, ardhi iliyolimwa, nafaka inayopeperushwa, udongo tasa, miti isiyozaa matunda, milima ya milele, chemichemi ibubujikayo, jua linalozama, linalofikia rangi na kupaka rangi mbingu kwa rangi ya dhahabu—yote haya aliyatumia kuwavutia wasikilizaji Wake kwa Ukweli wa mbinguni. Aliunganisha kazi za vidole vya Mungu mbinguni na juu ya dunia kwa Maneno ya uzima aliyokusudia kutia akilini mwao kwamba wanapaswa kuangalia kazi za Mungu za ajabu kwenye vitu vya asilia (nature), masomo Yake yanaweza kuwa mapya katika kumbukumbu zao. {2Tsw 579.2}

Katika juhudi Zake zote Kristo alitaka kufanya mafundisho Yake yavutie. Alijua kuwa umati wa watu waliochoka, na wenye njaa wasingeweza kupokea manufaa ya kiroho, na hakusahau mahitaji yao ya kimwili. Katika tukio moja Yesu alifanya muujiza mmoja wa kuwalisha watu zaidi ya elfu tano ambao walikuwa wamekusanyika kusikiliza maneno ya uzima ambayo yalikuwa yakitoka midomoni Mwake. Yesu alizingatia mazingira wakati wa kutoa Ukweli Wake wa thamani kwa umati. Mandhari ilikuwa ya kuvutia macho na ya kuamsha kuvutiwa/kuthamini vifuani na mioyoni mwa wapenzi wa urembo na yote yaliyo mazuri. Angeweza kutukuza Hekima ya Mungu katika ubunifu wa kazi Zake, na kuyafungamanisha masomo Yake matakatifu kwa kuelekeza akili zao kupitia asili hadi kwa Mungu aliyeumba asili. {2Tsw 580.1}

Kwa hiyo mandhari, miti, ndege, maua ya kondeni, vilima, ziwa na uzuri wa mbingu vilihusishwa katika akili zao na Kweli takatifu ambazo zingewafanya kumtukuza kwa kumbukumbu watakapovitazama baada ya Kristo kupaa mbinguni. {2Tsw 580.2}

Wakati Kristo alipokuwa akiwafundisha watu, hakutumia muda huo kwa maombi. Hakuwashurutisha, kama vile mafarisayo walivyofanya katika ibada na sala zao ndefu na zenye kuchosha. Aliwafundisha wanafunzi Wake namna ya kuomba: “Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao hupenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, wamekwisha pata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba Yako aliye sirini; na Baba Yako aonaye sirini atakujazi. Nanyi mkiwa katika kusali msipayuke payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwasabu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayo ahitaji kabla ninyi hamjamwomba. Basi ombeni hivi.” {2Tsw 580.3}

Kristo alisisitiza juu ya wanafunzi Wake wazo kwamba maombi yao yanapaswa kuwa mafupi, wakieleza ni nini wanachotaka na si zaidi. Akitoa urefu na kiini cha maombi yao, wakielezea matakwa yao kwa mahitaji ya muda mfupi na baraka za kiroho, na kwa shukrani zao kwa pamoja. Ulikuwa ni ujumuishaji wa kiasi gani sampo (mfano) ambao maombi haya yameshugulikia! Yameshughulikia mahitaji halisi ya wote. Dakika moja au mbili inatosha kwa sala yoyote ya kawaida. Kunaweza kuwa na matukio ambapo maombi yapo kwa njia maalum iliyochochewa na Roho wa Mungu, ambapo ombi la ibada hufanywa kwa Roho. Nafsi yenye kiu inakuwa na uchungu na kuugua mbele za Mungu kwa matamano. Roho inashindana kama alivyofanya Yakobo na haitatulia bila ya udhihirisho maalum wa nguvu za Mungu. Hii ni kama vile ambavyo Mungu anavyohitaji iwe. {2Tsw 581.1}

Lakini wengi hutoa maombi kwa njia kavu, ya mahubiri (wanamhubiri Mungu?). Hawa husali kwa wanadamu, sio kwa Mungu, kama wangelikuwa wanaomba kwa Mungu, na kweli wanaelewa walichokuwa wanakifanya, wangelitishwa katika ushupavu wao; kwani wanatoa hotuba kwa Bwana kwa njia ya maombi, kana kwamba Muumba wa ulimwengu alihitaji habari maalum juu ya maswali ya jumla kuhusiana na mambo yanayotendeka ulimwenguni. Maombi

hayo yote ni kama shaba iliayo na upatu uvumao. Hayahesabiki mbinguni. Malaika wa Mungu wamechoka na maombi hayo, hata wanadamu wanaosikiliza nao pia wamechoshwa. {2Tsw 581.2}

Mara nyingi Yesu alipatikana katika maombi mara nyingi. Aliamua kwenda mahali pa upweke penye miti au milimani ili kufanya dua Yake ifahamike mbele za Baba Yake. Wakati masumbufu na shughuli za siku zilipomalizika, na wenye uchovu wakitafuta kupumzika, Yesu alitumia muda huo kwa maombi. Tusingepuuzia maombi, kwani kuna kuomba kidogo na kukesha kudogo sana. Na bado kuna kuomba kwa Roho na kwa ufahamu kudogo sana. Maombi ya bidii, ya unyofu, na shukrani, yanayofaa kila wakati hayachoshi kamwe. Maombi ya namna hii huwavutia na kuwaburudisha wale walio na upendo kwa ibada. {2Tsw 582.1}

Maombi ya faragha yanapuuziwa, na ndio sababu wengi hutoa sala ndefu zenye kuchosha, maombi yaliyorudi nyuma, wakati wanapokusanyika kumwabudu Mungu. Wanaenda katika maombi baada ya juma ambalo majukumu ya kuomba yalipuuzwa, na wanaomba wakizunguka-zunguka, wakitumaini kujazia au kulipizia pale walipokuwa hawaombi na kutuliza dhamiri zao zinazowahukumu, ambazo ni kama zinawapiga mijeledi. Wanatumaini kwamba kuomba kwao ndiyo kutawapa kibali cha Mungu. Na maombi hayo pamoja na kulazimika kuwasikiliza wanadamu wenye kufa (mortal). {2Tsw 581.2}.

Wana matumaini kwa kuomba kwao sala refu, watawapa upendeleo wa Mungu. Lakini maombi haya mara nyingi yameleta matokeo ya kushusha akili za wengine kufikia kiwango chao cha chini sana, cha giza la kiroho. Kama Wakristo wangelichukua nyumbani mafundisho ya Yesu kuhusiana na kukesha na kuomba, hapo ndipo wangekuwa na akili mahiri zaidi katika kumwabudu kwao Mungu. {2Tsw 582. 2}

## SURA YA 71

### JE, TUITUNZEJE SABATO?

Je! Tunaitunzaje Sabato? Mungu ni Mwenye huruma. Matakwa Yake ni ya busara, kulingana na wema na tabia Yake ya ukarimu. Lengo la Sabato lilikuwa wanadamu wote wapate kufaidika. Mtu hakufanywa ili kuitosheleza/kuinufaisha Sabato; kwani Sabato iliumbwa baada ya uumbaji wa mwanadamu, ili kukidhi mahitaji yake. Baada ya Mungu kuumba dunia kwa siku sita, alipumzika na kuitakasa na kuibariki siku ambayo alipumzika kutoka kwa kazi Yake ambayo alikuwa ameiumba na kuifanya. Yeye Alitenga siku hiyo maalum kwa mwanadamu kupumzika kutoka katika kazi zake, kwamba anapotazama dunia chini na juu mbinguni, atatafakari kwamba Mungu aliumba haya yote kwa siku sita na kupumzika siku ya saba; na kwamba anapaswa kuona udhibitisho Dhahiri wa hekima ya Mungu isiyo na mwisho, basi moyo wake unaweza kujazwa na upendo na kicho kwa Muumba Wake.{2Tsw 582.3}

Ili kuishika Sabato kuwa takatifu, sio lazima tujizungushie kuta, tujifungie kutoka katika mandhari nzuri za asili na kutoka kwenye hewa ya bure na iliyosheheni, yenye nguvu ya mbinguni. Hatupaswi kwa vyovyote vile kuruhusu mizigo na shughuli za biashara kugeuza mawazo yetu juu ya Sabato ya Bwana, ambayo Yeye aliitakasa. Hatupaswi kuruhusu akili zetu ziwe juu ya vitu vya kidunia na hata tabia zake. Lakini akili haiwezi kuburudishwa, kuhuishwa, na kuinuliwa kwa kuzuiliwa karibu masaa yote yote ya Sabato ndani ya kuta, tukisikiliza mahubiri marefu na ya kuchosha, ya desturi/kaida na maombi ya kawaida. Sabato ya Bwana itakuwa imewekwa kwa matumizi mabaya ikiwa itasherehekewa hivyo. Lengo la kuanzisha Sabato halitatimizwa. Sabato iliumbwa kwaajili ya mwanadamu, kuwa mbaraka kwake kwa kuziita akili zake kutoka katika kazi za kidunia ili kutafakari uzuri na utukufu wa Mungu. Ni muhimu kwamba watu wa Mungu wakusanyike kuzungumza juu Yake, kubadilishana mawazo na maoni kuhusu Ukweli uliopo katika Neno Lake, na kutoa sehemu kwa maombi sahihi. Lakini nyakati hizi, hata siku za Sabato zisifanywe za kuchosha kwa urefu na kukosa hamu. {2Tsw 583.1}



Sehemu ya siku ya Sabato, wote wanapaswa kuwa na fursa ya kuwa nje ya nyumba. Ni kwa jinsi gani watoto wanaweza kupokea ufahamu sahihi kuhusiana na Mungu, na akili zao zikavutiwa zaidi, kuliko kutumia wakati wao nje, sio kwa kucheza, lakini kwa kushirikiana na wazazi wao? Hebu akili zao changa zihusishwe na Mungu katika mandhari nzuri ya asili, hebu umakini wao uitwe kwa ishara za upendo wa Mungu kwa mtu katika kazi Zake za uumbaji, nao wataavutiwa na kupendezwa. Hawatakuwa katika hatari ya kuhusisha tabia ya Mungu kwa kila kitu ambacho kina ukali na ugumu; lakini watakapoona vitu vizuri ambavyo Yeye ameviumba kwaajili ya furaha ya mwanadamu, wataongozwa kumuona kama Baba mpole, Mwenye upendo mwanana, huruma nyororo na kujali. Wataona kwamba makatazo na maagizo Yake hayakufanywa ili kuonyesha nguvu Zake na mamlaka, lakini kwamba Yeye ana matazamo wa furaha kwa watoto Wake. Kama tabia ya Mungu inavyovaa kipengele cha upendo, ukarimu, Uzuri, na mvuto, wataavutiwa kumpenda. Unaweza kuelekeza akili zao kwa ndege wazuri wanaotunga muziki angani kwa nyimbo zao za kufurahisha, katika minara ya nyasi na maua yenye rangi nzuri katika ukamilifu wao unaopeleka manutako angani. Yote hayo yanatangaza upendo na ustadi wa Msanii wa mbinguni, na kuonyesha utukufu wa Mungu. {2Tsw 583.2}

Wazazi kwanini msitumie masomo ya thamani ambayo Mungu ametupa katika kitabu cha asili, kwa kuwapa watoto wetu wazo sahihi la tabia Yake? Wale wanaojitoa mhanga kwa kuacha usahili na kushugulikia fasheni, kutokuwa wanyenyekevu na kujifungia wenyewe mbali na uzuri wa asili, hawataweza kuwa na nia ya kiroho. Hawawezi kuelewa ustadi na nguvu ya Mungu kama inavyoonyeshwa katika kazi Zake za uumbaji; kwahiyo mioyo yao haiwezi kuhuishwa na kudunda kwa upendo mpya na mvuto, na hawatajazwa na kicho na kustaajabu na heshima wamuonapo Mungu katika asili. {2Tsw 584.1}

Wote wanaompenda Mungu wanapaswa kufanya wawezavyo ili kuifanya Sabato kuwa siku ya furaha, takatifu na ya kuheshimiwa. Hawawezi kufanya hivi kwa kutafuta anasa zao katika dhambi, na maburudisho yaliyokatazwa. Walakini wanaweza kufanya mengi kwa

kuitukuza Sabato katika familia zao na kuifanya kuwa siku ya kuvutia zaidi ya juma. Tunapaswa kutoa muda wetu ili kuwavutia watoto wetu. Mabadiliko yatakuwa ya ushawishi mzuri juu yao. Tunaweza kutembea nao nje ya anga-hewa; twaweza kukaa nao mashambani na kwenye mwanga wa jua., na kuzipa akili zao zisizotulia kitu cha kuwashibisha kwa kuzungumza nao juu ya kazi za Mungu, na itawahamasisha kwa upendo na heshima kwa kuwaelekeza kwenye vitu vyema katika asili. {2Tsw 584.2}

Sabato inapaswa kufanywa iwe ya kufurahisha sana kwa familia zetu kiasi kwamba kurudi kwake kila wiki kutasifiwa sana kwa furaha. Hakuna njia bora zaidi ambayo wazazi wanaweza kuitukuza na kuiheshimu Sabato kuliko mbinu ya kutoa mafundisho sahihi katika familia zao na kuwafurahisha katika mambo ya kiroho, kuwapa maoni sahihi juu ya tabia ya Mungu na kile anachotaka kwetu ili kukamilisha tabia sahihi ya Kikristo na kufikia uzima wa milele. Wazazi fanyeni Sabato kuwa ya kufurahisha, ili watoto wenu wawe wanaitazamia na wawe wanaikaribisha mioyoni mwao. {2Tsw 585.1}

## **SURA YA 72**

### **MABURUDISHO YA KIKRISTO**

[Imeripotiwa kama ilivyozungumzwa mbele ya kundi La watu zaidi ya mia mbili waliokuwa wakifurahia msimu aa burudani katika ziwa la Goguac, karibu na mji Wa Battle Creek, Michigan, Mei, 1870.]

Nimekuwa nikifikiria ni tofauti gani itaonekana kati ya mkutano wetu hapa leo na yale makusanyiko yanayoendeshwa na watu wasioamini. Badala ya kuomba, na kumtaja Kristo na mambo ya kidini, vingesikika vicheko vya kijinga na mazungumzo ya ujinga yasiyo na maana. Lengo lao lingekuwa ni kujifurahisha kwa kuwa na wakati mzuri kiujumla. Wangeanza kwa upumbavu na kuishia katika ubatili. Tunahitaji kuwa na mikusanyiko itakayoongozwa vizuri, na kwa mwenendo wetu,

tuweze kurudi majumbani mwetu tukiwa na dhamiri isiyo na kosa mbele za Mungu na wanadamu; dhamira ambayo hatujawaumiza wala kuwajeruhi kwa namna yoyote wale ambao tumeshirikiana nao, au kuwa na mvuto mbaya juu yao. {2Tsw 585.2}

Hapo ndipo wengi wanaanguka. Hawazingatii hili kwamba wanawajibika kwa ushawishi wanaouweka kila siku; kwamba lazima watoe hesabu kwa Mungu kwa msukumo wanaofanya, na ushawishi wanaotupa katika miunganiko yao yote maishani. Ikiwa ushawishi huu utakuwa na kawaida ya kuvuta mawazo ya wengine mbali na Mungu na kuwavutia katika mkondo wa ubatili na upumbavu, ukiwaongoza kutafuta raha yao wenyewe katika burudani na kuendekeza upumbavu, ni lazima wataitoa hesabu kwa hili. Na ikiwa watu hawa ni wanaume na wanawake wenye ushawishi, ikiwa nafasi zao ni kwamba mfano wao utawaathiri wengine, basi dhambi kubwa zaidi itakuwa juu yao kwa kupuuza kudhibiti mwenendo wao kwa kiwango cha Biblia. {2Tsw 585.3}

Tukio ambalo tunafurahiya leo ni kulingana tu na maoni yangu juu ya burudani. Nimejaribu kutoa mtazamo wangu juu ya mada hii, lakini mtu anaweza kuelewa vyema kwa vielelezo kama vya kuona kwa kwa macho nauzoefu, kuliko kuzungumza. Nilikuwa kwenye uwanja huu karibu mwaka mmoja uliopita wakati kulipokuwa na mkusanyiko unaofanana na huu (kwenye njozi). Karibu kila kitu kilipita kwa kupendeza sana wakati huo, lakini bado mambo mengine yalikuwa ya kutiliwa shaka au kuchukiza. Futuhi na utani wa kutosha viliendekezwa na baadhi ya watu. Watu wote hawakuwa watunza Sabato, na ushawishi ambao ulidhihirika, kwamba haukuwa wa kupendeza kama tulivyotaka uwe. {2Tsw 586.1}

Lakini naamini kwamba, wakati tunatafuta kuziburudisha roho zetu, kuzifanya upya na kuimarisha miili yetu, tunahitajika kwa Mungu kutumia nguvu zetu zote kwa wakati wote kwa kusudi bora. Tunaweza kushirikiana pamoja kama tufanyavyo hapa leo, na kufanya yote kwa utukufu wa Mungu. Tunaweza, na tunapaswa kufanya burudani zetu kwa jinsi hii kwamba tutaweza kuwa na stahiki za kutekeleza yale majukumu tunayopewa kwa mafanikio zaidi, na kwamba ushawishi

wetu utakuwa wa faida zaidi kwa wale ambao tunahusiana nao. Hasa ingekuwa jambo muhimu juu ya hafla kama hii, ambayo inapaswa kutuchangamsha sisi sote. Tutaweza kurudi majumbani mwetu tukiwa na tumeboreshwa kiakili na mwili ulioburudika, na kuandaliwa kushugulikia kazi katika upya, na tukiwa wenye matumaini bora na ujasiri bora. {2Tsw 586.2}

Tunaamini kwamba ni upendeleo wetu kila siku katika maisha yetu kumtukuza Mungu duniani; kwamba hatuishi katika ulimwengu huu kwa kujifurahisha wenyewe tu, wala kujipendeyesha wenyewe tu. Tuko hapa kwaajili kunufaisha jamii ya ubinadamu, kuwa baraka kwa jamii. Na ikiwa tutaacha akili zetu zijiendeshe kwenye mkondo huo wa chini ambao wengi wanatafuta ubatili tu na upumbavu kwa kuruhusu akili zao kuendesha, tunawezaje basi kuwa baraka kwa jamii, faida kwa jamii ya binadamu wenzetu na kizazi chetu? Hatuwezi kuendekeza matumbuizo au burudani ya aina yoyote bila hatia ambayo itatufanya tusiwe na sifa/stahiki au kutofaa kutekeleza kwa uaminifu zaidi kwa majukumu ya kawaida ya maisha. {2Tsw 587.1}

Tunataka kutafuta kilichoinulia na cha kupendeza. Tunataka kuelekeza akili mbali na vitu hivyo ambavyo ni vya juujuu na visivyo na umuhimu wowote, ambavyo havina uimara. Tunachotamani ni, kukusanya nguvu mpya kutoka kwa yote tunayojihusisha nayo. Kutoka kwa mikusanyiko hii yote kwa kusudi la burudani, kutoka kwa jumuiya hii ya kupendeza, tunataka kukusanya uwezo/nguvu mpya ili kuwa wanaume na wanawake bora. Kutoka kwa kila chanzo kinachowezekana, tunataka kukusanya ujasiri mpya, uwezo mpya, nguvu mpya, nguvu mpya, ili tuweze kuinua maisha yetu kwa usafi na utakatifu, na sio kushuka kwenye kiwango cha chini cha ulimwengu huu. Tunasikia wengi wanaodai kuwa na dini ya Kristo mara nyingi wakiongea hivi: "Lazima sote tushuke kwa kiwango fulani cha chini." Hakuna kitu kama hicho cha Wakristo kushuka chini ya kiwango. Kukubali Ukweli wa Mungu na dini ya Biblia sio kushuka chini, ni kuja juu, juu ya kiwango kilichonyanyuliwa juu zaidi, ambapo tunaweza kuwasiliana/kuzungumza na Mungu. {2Tsw 587.2}

Kwa sababu hii-hii Kristo alijinyenyekeza na hata akachukua asili yetu juu Yake, kwamba kwa fedheha Yake Mwenyewe na kwa mateso na kafara Yake, Aweza kuwa jiwe la kukanyaga kwa watu walioanguka, ili

waweze kupanda juu sababu ya sifa na kustahili Kwake, na kwamba kwa ubora na wema Wake, juhudi zao za kushika sheria ya Mungu ziweze kukubalika Kwake. Hakuna kitu kama hicho hapa cha kushuka kwa kiwango. Tunatafuta kuipandisha miguu yetu, na kuiweka juu ya jukwaa lililoinuliwa na kutukuzwa la Ukweli wa milele. Tunatafuta zaidi kuwa kama malaika wa mbinguni, wenye mioyo iliyo safi zaidi, wasio na dhambi, wasio na hatia, na wasio na unajisi. {2Tsw 587.3}

Tunatafuta usafi na utakatifu wa maisha, ili mwishowe tuweze kufaa kwenye jamii ya mbinguni katika Utukufu wa Kifalme; na njia pekee ya kufikia mwinuko huu wa tabia ya Kikristo ni kupitia Yesu Kristo. Hakuna njia nyingine ya kuinuliwa kwa familia ya wanadamu. Baadhi huzungumzia aibu waliyovumilia na walivyojitoa sadaka, kwa sababu walitwaa Ukweli wa asili ya mbinguni! Ni kweli kwamba ulimwengu haukubali Ukweli; watu wasioamini hawaupokei. Wanaweza kuzungumza juu ya wale ambao wamekubali Ukweli na kumtafuta Mwokozi, na kuwawakilisha huku wakiwa wanaacha kila kitu, wakitoa kila kitu, na kutoa dhabihu ya kila kitu ambacho kinastahili kuhifadhiwa. Lakini usiniambie mimi hivi. Ninafahamu zaidi ya hayo. Uzoefu wangu unathibitisha kuwa vinginevyo. Usiniambie kwamba ni lazima sisi tutoe hazina zetu za thamani zaidi na kisha tusipokee baraka sawia. Hapana, kwa kweli! Muumba Huyo ambaye aliiweka Edeni nzuri kwa wazazi wetu wa kwanza, na ambaye amepanda kwa ajili yetu miti na maua mazuri, na kutoa kila kitu kilicho kizuri na tukufu wa asili kwa jamii ya wanadamu kufurahiya, aliunda/aliumba kwamba wafurahie. Hivyo usifikirie kwamba Mungu anatutaka sisi tutoe kila kitu ambacho ni furaha yetu kubaki nacho hapa. Yeye anahitaji tuachane na yale tu ambayo hayatakuwa mema kwetu na kuzuia furaha yetu. {2Tsw 588.1}

Mungu yule ambaye amepanda miti hii mizuri na kuifunika kwa utajiri wa majani yake, ambaye ametupatia sisi vivuli angavu na maridadi vya maua mazuri, na ambaye kazi Yake ya mikono ya kupendeza tunaiona katika ulimwengu wote wa asili, hakubuni haya ili tusiwe na furaha; Hakuibuni dunia ili kwamba tusiwe na ladha nayo, na tusifurahie mambo haya. Ni kwa ubunifu Wake tuvifurahie na kuwa na raha katika haiba changamfu ya asili, ambayo ni ya uumbaji Wake Mwenyewe. {2Tsw 588.2}

Ni sawa kwamba tunapaswa kuchagua maeneo kama haya, yenye miti shamba au miti kwa misimu ya kupumzika na burudani. Lakini wakati tukiwa hapa katika burudani ya Kikristo hatupaswi kutoa usikivu kwa kwaajili ya sisi wenyewe tu, na kufanya muda wa thamani uyoyome katika burudani ambazo zitatoa mivuto ya ladha zisizo kwenye vitu vitakatifu. Hatujaja hapa kujishughulisha na masihara na mzaha, kwa mazungumzo ya kipumbavu na vicheko visivyo na maana. Tupo hapa kutazama uzuri wa asili. Ni nini basi tufanye? Je! Tuanguke na kuabudu asili? Hapana, kwa kweli. Lakini tunapoendelea kutazama kazi hizi za asili tunapaswa kuruhusu akili kuchukuliwa juu zaidi, kwa Mungu aliyeumba asili; hebu basi akili na iinuliwe kwa Muumbaji wa ulimwengu, na kisha kumwabudu Muumba ambaye amefanya vitu hivi vyote vizuri kwa ajili ya faida na furaha yetu. {2Tsw 589.1}

Wengi wanafurahiya sanaa/michoro mizuri na wako tayari kuabudu talanta ambazo zinaleta huo mchoro mzuri, lakini ni wapi ambapo wale wanaojitolea maisha yao kwa kazi hii wanapata usanifu wao? Ni wapi wasanii hawa huyapata maoni yao ya vitu vya kuweka kwenye maonyesho ili kuuza? Kutoka kwa mandhari nzuri ya asili - kutoka kwa uzuri wa asili, kutoka tu kwa asili (wanaiga ubunifu wa Mungu). Watu binafsi hutumia uwezo wao wote, na kutoa mapenzi yao yote juu ya vionjo kwa mwelekeo huu. Wengi huziondoa akili zao kutoka katika uzuri na utukufu wa asili ambao Muumba wetu amewaandalia ili kufurahia, na kutoa nguvu zao zote kwa utimilifu wa sanaa; lakini vitu hivi vyote ni nakala zisizo kamilifu kutoka kwa vitu vya asili. Sanaa haiwezi kufikia ukamilifu unaoonekana wa asili. {2Tsw 589.2}

Muumbaji wa vitu vyote vizuri vya asili amesahaulika. Naliona wengi ambao wangechangamkia sana kuhusiana na picha ya machweo ya jua, kisha wakati huo huo wangeweza kupata fursa ya kuona machweo ya jua halisi na tukufu, karibu kila jioni kwa mwaka. Wanaweza kuona rangi nzuri ambazo Msanii mkuu wa asili asiyeonekana, akiwa na ustadi wa Kimbingu, aliyepaka rangi pazia tukufu kwenye mawingu yanayosafiri mbinguni, na bado wanageuka bila ya kujali kutoka katika picha iliyotengenezwa na Mbingu na kwenda kwenye uchoraji wa sanaa, kwa kutumia vidole visivyo kamilifu, na hukaribia kuinama chini ili wazisujudie. Sababu ya hii ni nini? Ni kwa sababu adui karibu kila

wakati anatafuta kugeuza akili kutoka kwa Mungu. he, tunapomwasilisha Mungu na dini ya Kristo, watampokea? Kwa kweli, hapana. Hawataweza kumkubali Kristo. Jamani ni Nini! Je! wao hufanya dhabihu ambayo wangepaswa kutoa kumpokea? Hapana kabisa! Lakini ni nini kinachohitajika? Upendo bora na utakatifu wa moyo Kwake ambaye aliacha utukufu wa Baba na akashuka kufa kwa jamii ya waasi. Aliacha utajiri Wake, enzi Yake, na mamlaka Yake ya juu, na kuchukua asili yetu, ili aweze kutengeneza njia ya kutunusuru au tuweze kutoroka – kufanya nini basi? Kukufedhehesha wewe? kukushusha hadhi wewe? Hapana, hakika. Ili kukutengenezea njia ya kukunusuru kutoka katika kutokuwa na tumaini na huzuni kuu-[kukusaidia utoroke kutoka katika hali ya kutisha], ili kukuinua hata mwisho katika ufalme Wake kwa mkono Wake wa kuume. Kwa ajili hii kuu, dhabihu kuu, ilitolewa. Na ni nani anayeweza kutambua dhabihu hii kubwa? Ni nani anayeweza kuithami hii dhabihu? Hakuna ila hao ambao wanaelewa siri ya utauwa, ambao wameonja nguvu za ulimwengu ujao, na ambao wamekunywa kutoka katika kikombe cha wokovu ambacho kimewasilishwa kwetu. Kikombe hiki cha wokovu, Bwana hutupatia, ambapo kwa midomo Yake Mwenyewe alikunywa, badala yetu, kikombe chenye uchungu ambacho dhambi zetu zilikuwa zimekiandaa, na ambacho tulipewa/kiligawanywa kwetu ili kukinywa. Walakini bado tunazungumza kana kwamba Kristo, ambaye ametoa dhabihu kama hiyo, na kuudhihirisha upendo kama huo kwetu, angeweza kutunyima kila kitu ambacho ni cha thamani kuwa nacho.{2Tsw 589.3}

Je! Yeye Angetunyima ili kuwe na faida ya aina fulani? Hapana! Sio mambo mazuri angetunyima, Isipokuwa angeweza kutunyima fursa ya kujitoa kutumikia tamaa za asili ya mwilini na tamaa mbaya za moyoni. Hatuwezi kukasirika tu wakati ambapo tunapenda, na kudumisha dhamiri safi na kibali cha Mungu. Lakini Je! hatuko tayari kuliacha hili? Je! Kuendekeza kwa tamaa mbaya kwaweza kutufanya tuwe na furaha yoyote? (hapana) Ni kwa sababu haitatupa furaha ndiyo sababu vizuizi hivi vimewekwa juu yetu kwa hili jambo. , Haitaongeza starehe/raha yetu kukasirika na kuendekeza/kupalilia mwenendo mbaya. Kwa kweli haitakuwa kwa furaha yetu kufuata uongozi wa moyo wa asilia. Je! Tutafanywa kuwa bora kwa kuzifurahisha au kuziendekeza tamaa?

Hapana!; Hizo zitatoa kivuli katika miji yetu na kututupia dhiki na uchovu juu ya furaha yetu. Tukitoa nafasi kwa mwenendo wa uchu wa asili tutaumiza tu mwili na kuvunja mfumo vipande vipande. Kwa hivyo Mungu angetutaka tuzuie hamu ya chakula, na tutawale tamaa, na kufanya mwili wote mzima uwe chini ya utii. Na Yeye ameahidi kutupatia nguvu ikiwa tutashiriki katika kazi hii. {2Tsw 590.1}

Dhambi ya Adamu na Hawa ilisababisha hofu ya utengano kati ya Mungu na mwanadamu. Na Kristo akaingia kati ya mwanadamu aliyeanguka na Mungu, na kumwambia mwanadamu: "Unaweza bado kuja kwa Baba; kuna mpango uliopangwa kwa njia ambayo Mungu anaweza kupatanishwa na mwanadamu, na mwanadamu na Mungu; kwa kupitia mwombezi/mpatanishi unaweza kumkaribia Mungu. "Na sasa anasimama kukupatanisha. Yeye Ndiye Kuhani Mkuu mtetezi/mpatanishi kwa niaba yako; na wewe unapaswa kuja kutoa hoja yako kwa Baba kupitia kwa Yesu Kristo. Kwa hivyo unaweza kupata njia ya kufika kwa Mungu; na ingawa umetenda dhambi, kesi yako ina matumaini. "Mtu yeyote akifanya dhambi, tunaye wakili pamoja na Baba, Yesu Kristo Mwenye haki." {2Tsw 591.1}

Ninamshukuru Mungu kwa kuwa tunaye Mwokozi. Na hakuna njia ambayo tunaweza kuinuliwa, isipokuwa kupitia Kristo. Basi mtu yeyote asifikirie kuwa ni fedheha kubwa kwake kumpokea Kristo; kwani wakati tunapochukua hatua hiyo, tunashika kamba ya dhahabu inayomwunganisha mtu mwenye ukomo na Mungu asiye na mwisho (Yule wa milele); tunachukua hatua ya kwanza kuelekea furaha ya Kweli (kuinuliwa kwa Kweli), ili tuweze kutosheleza jamii kwa usafi na malaika wa mbinguni katika ufalme wa utukufu. {2Tsw 591.2}

Usivunjike moyo; usizimie moyo. Ingawa unaweza kuwa na majaribu, ingawa unaweza kuwa umezungukwa na adui mjanja, lakini ikiwa una hofu ya Mungu mbele yako, malaika ambao wana nguvu zaidi watatumwa kuwa msaada wako, na unaweza kuwa zaidi ya mshindani kwa nguvu za giza. Yesu Yu hai. Yeye Alikufa ili kutengeneza njia ya kutokea kwa jamii iliyoanguka, na Yu hai leo kutuombea, ili kwamba tuinuliwe kwa mkono Wake wa kuume. Mtumaini Mungu. Ulimwengu unasafiri kwa njia pana; nawe unaposafiri katika njia nyembamba, na



kuwa na ushindani na viongozi wenye kushikilia misingi yao madhubuti na mamlaka, na kukabiliana na upinzani wa maadui, kumbuka kuwa majaliwa na njia imefanywa kwa ajili yako. Msaada umewekwa juu ya Yule aliye Hodari, na kupitia Yeye utaweza kushinda. {2Tsw 591.3}

Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, Nami nitawapokea, nanyi mtakuwa wana na binti za Bwana Mwenyezi. Ahadi ya ajabu namna gani hii! Ni ahadi kwako kwamba utakuwa mshirika wa familia ya kifalme, warithi wa ufalme wa mbinguni. Ikiwa mtu anaheshimiwa, au kuwa na muunganiko na moja ya wafalme wa dunia, ni kwa jinsi gani avyozunguka pande zote za majarida ya siku na kuchochea wivu wa wale ambao wanajiona wana bahati ndogo. Lakini hapa kuna Mmoja aliye Mfalme juu ya wote, mfalme wa ulimwengu, Mwanzilishi wa kila jambo jema; Naye anatuambia: Nitawafanya Wanangu wa kiume na wa kike-wana na mabinti; Nitakuunganisha Kwangu; mtakuwa watu wa jamaa ya kifalme na watoto wa Mfalme wa mbinguni. {2Tsw 592.1}

Paulo anasema: "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu." Kwa nini tusifanye hivi, wakati tuna vivutio vya namna hii, fursa ya kuwa watoto wa Yule Aliye juu, upendeleo wa kumwita Mungu wa mbinguni Baba yetu?

Je! Hii Haitoshi? Na Je! Unakuita huku ni kunyimwa kwa kila kitu cha thamani ambacho unastahili kuwa nacho? Je! Hii ni kutoa kila kitu cha thamani ambacho unastahili kuwa nacho? Acha mimi niungane na Mungu na malaika watakatifu, kwa maana haya ndiyo matamanio yangu makubwa. Unaweza kuwa na mali zote za ulimwengu huu; lakini mimi ni lazima niwe na Yesu; Lazima niwe na haki ya urithi wa milele, mali ya milele. Ngoja nifurahiye uzuri wa ufalme wa Mungu. Acha nifurahie rangi na michoro Yake ambayo vidole Vyake Mwenyewe imevipaka rangi (uumbaji). Nitazifurahiya. Unaweza nawe kuzifurahia. Hivi hatuviabudu ila kupitia hivyo tunaweza kuelekezwa Kwake na tazama utukufu Wake, Yeye ambaye alifanya vitu hivi vyote ili tufurahie. {2Tsw 592.2}

Tena nasema: Uwe na ujasiri na moyo mkuu. Mtumaini Bwana. Hebu adui asikunyang'anye ahadi Zake. Ikiwa mmejitenga na ulimwengu, Mungu amesema kwamba atakuwa Baba yenu, nanyi mtakuwa wana na binti Zake. Je! hii Haitoshi? Je! Ni ushawishi gani mkubwa zaidi unaweza kuwasilishwa mbele yako? Je! Kuna jambo lolote la maana kuwa kama kipepeo na bila ya kuwa na kiini au lengo maishani? Ah! Wacha mii nisimame katika jukwaa la Ukweli wa milele. Nipe thamani ya kutokufa. Acha nishike mnyororo wa dhahabu ambao umeshushwa kutoka mbinguni hadi duniani, na ngoja univute kwa Mungu na kwa utukufu. Hili ndilo tamanio langu kuu; hili ndilo lengo langu. Kama wengine hawana kitu cha juu kuliko mavazi, ikiwa wanaweza kufurahiya maonyesho ya nje na kuridhisha roho zao kwa lesi na riboni na vitu vya kupendeza, wacha wafurahie haya. Hebu niache mimi nipate mapambo ya ndani. Acha nivae roho hiyo ya upole na utulivu ambayo ina thamani kubwa machoni pa Mungu. Nami ninawapendekezea kwenu, vijana wa kiume na wa wake, kwa maana ni ya thamani machoni pake kuliko dhahabu ya Ofiri. Hii ndio inayomfanya mtu kuwa wa thamani kuliko dhahabu safi, kuliko kabari ya dhahabu ya Ofiri. Dada zangu, na ninyi vijana, itawafanya kuwa wa thamani mbele ya Mbingu kuliko dhahabu, naam, kuliko kabari ya dhahabu ya Ofiri. Ninampendekeza kwako Yesu, Mwokozi wangu Aliyebarikiwa. Ninamwabudu-nitamthamini; Ninamtukuza. Laiti ningekuwa na Kinywa kisichoweza kufa, ili nimsifu kama vile ninavyotamani! Kwamba ningeweza kusimama mbele ya ulimwengu uliokusanyika na kusema kwa sifa ya sumaku Zake zisizo na mfanano! {2Tsw 593.1}

Na wakati ninamuabudu na kumtukuza, nataka umtukuze pamoja nami. Msifu Bwana hata wakati Unapoanguka gizani. Msifu hata katika majaribu. "Furahini katika Bwana siku zote," anasema mtume; "tena nasema, Furahini. "Je! hiyo italeta utusitusi na giza katika familia zenu? Hapana, kwa kweli; italeta mwale wa jua. Kwa hivyo utakusanya miale ya nuru ya milele kutoka kiti cha enzi cha utukufu na kuwatawanya kwako. Wacha niwasihi kushiriki katika kazi hii, kutawanya nuru hii na uzima kote kukuzunguka, sio tu katika njia yako mwenyewe, bali katika njia za wale unaoshirikiana nao. Acha lengo lako liwe kuwafanya wanadamu walio karibu nawe kuwa bora, kuwainua, kuwaelekeza

mbinguni na kwa utukufu, na kuwaongoza kutafuta, vitu vilivyo juu ya vyote duniani, mali ya milele, urithi wa milele, utajiri ambao ni wa kutokuharibika. -{2Tsw 593.2}

## SURA YA 73

### NDOTO YA KUVUTIA

Nilipokuwa Battle Creek mnamo Agosti, 1868, niliota kuwa nipo na kundi kubwa la watu. Sehemu ya mkutano huu ulianza kujiandaa tayari kwa safari. Tulikuwa na mabehewa makubwa yaliyojaa mizigo. Na tulipokuwa tukisafiri, barabara ilionekana kupanda. Upande mmoja wa barabara hii kulikuwa na bonde refu; upande wa pili ulikuwa na ukuta wa juu laini na mweupe, kama uliomaliziwa (finishing) kwa kupakwa plasta rafu kwenye vyumba vilivyopakwa chokaa. {2Tsw 594.1}

Tulipokuwa tukisafiri, barabara ilizidi kupungua na kuwa na mpando mkali. Katika maeneo mengine ilionekana kuwa nyembamba sana kwamba tulihitimisha kuwa hatuwezi kusafiri tena na mabehewa yaliyosheheni. Kisha tukayatoa/tukayafungua mabehewa kutoka katika farasi, tukachukua sehemu ya mzigo kutoka kwa magari na kuiweka juu ya farasi, na kusafiri juu ya farasi. {2Tsw 594.2}

Tulipoendelea, njia bado iliendelea kuwa finyu. Tulilazimika kujibana karibu na ukuta ili kujiokoa tusidondoke kwenye barabara nyembamba chini ya bonde. Tulipofanya hivyo, ile mizigo juu ya farasi ilikandamizwa ukutani na kutusababisha kuyumba kuelekea kwenye maporomoko makali. Tuliogopa kwamba tutaanguka na kupondwa vipande-vipande kwenye miamba. Kisha tukakata mizigo kutoka kwa farasi, na ilianguka juu ya maporomoko/bonde. Tuliendelea kupanda farasi, tukiogopa sana, tulivyokuwa tunakuja kwenye maeneo

membamba barabarani, kwamba tunaweza kupoteza balansi/msawaziko wetu na kuanguka. Kwa nyakati kama hizo mkono ulionekana kuchukua hatamu na kutuongoza juu ya njia hatari. {2Tsw 594.3}

Kwa kuwa njia ilizidi kuwa nyembamba, tuliamua kuwa hatuwezi tena kwenda kwa usalama, huku tukiwa juu ya farasi, hivyo tuliacha farasi na tukaenda kwa miguu, tukiongozana, kama kwa mnyororo wa mtu mmoja mmoja, kila mmoja akifuata nyayo za mwingine. Kwa wakati huu kamba ndogo zilishushwa kutoka juu ya ukuta mweupe safi; hizi tulizishika kwa bidii/ari na uchangamfu, ili kutusaidia kuweka usawa (balansi) wetu juu ya njia. Tulipokuwa tukisafiri, kamba hiyo ilisogea pamoja nasi. Njia hatimaye ilikuwa nyembamba sana hivyo tukaazimu kwamba tunaweza kusafiri salama zaidi bila viatu vyetu, kwa hivyo tukavua viatu toka miguu mwetu na kwenda mbali bila ya viatu. Muda mchache iliamuliwa kuwa tunaweza kusafiri kwa usalama zaidi bila soksi zetu; hivyo ziliondolewa, na tukaendelea tukiwa peku miguuni. {2Tsw 595.1}

Kisha tukawafikiria wale ambao hawakuwa wamezoea umasikini na shida. Je, wapo wapi sasa? Hawakuwa katika kundi hili. Katika kila mabadiliko wengine waliachwa nyuma, walibaki wale tu ambao walikuwa wamezoea kuvumilia shida. Taabu za njiani ziliongeza shauku ya kuendelea hadi mwisho. {2Tsw 595.2}

Hatari yetu ya kuanguka kutoka kwenye njia iliongezeka. Tulijibanza karibu na ukuta mweupe, lakini bado hatukuweza kuweka kabisa miguu yetu juu ya njia, kwani ilikuwa nyembamba sana. Kisha tukaning'iniza karibu uzito wetu wote juu ya kamba, tukisema: "Tunashikilia kutoka juu! Tunashikilia kutoka juu!" Maneno yale yale yalitamkwa na kundi lote katika njia nyembamba. Tuliposikia sauti za siku kuu na shangwe ambazo zilionekana kutoka kwenye shimo chini, tulitetemeka. Tulisikia viapo vya dharau, matusi, mzaha mchafu, na nyimbo mbaya. Tulisikia wimbo wa vita na wimbo wa densi. Tulisikia ala za muziki na sauti kubwa za vicheko, vilivyochanganyika, matusi, na laana na vilio vya uchungu na maombolezo machungu, na walikuwa na fadhaa na mihangaiko zaidi kuliko hapo awali kwenye njia nyembamba

na ngumu. Wakati mwingi tulilazimika kuweka uzito wetu wote juu ya kamba, ambazo ziliongezeka kwa ukubwa tulipokuwa tukiendelea. {2Tsw 595.3}

Niligundua kuwa ukuta mzuri mweupe, ulikuwa umetapakaa damu. Ilisababisha hisia za majuto kuona ukuta ulivyobadilika hivi. Hisia hii, hata hivyo, ilidumu lakini kwa muda mfupi, kwani karibuni nilidhani kuwa ilikuwa inapaswa kuwa hivyo. Wale ambao wangefuata watajua kuwa wengine wamepita katika njia ngumu na nyembamba mbele yao, na kuhitimisha kuwa ikiwa wengine waliweza kuendeleza mwendo wao, hata wao wanaweza kufanya hivyo. Na damu itokapo kwa taabu kutoka kwa miguu yao inayouma, hawatazimia kwa kuvunjika moyo; lakini, wakiona damu ukutani, watajua kuwa wengine wamevumilia maumivu yale yale. {2Tsw 596.1}

Mwishowe tulifika kwenye korongo/shimo kubwa, ambalo njia yetu iliishia. Hakukuwa na kitu sasa cha kuongoza miguu, wala kitu cha kupumzikia miguu. Utegemezi wetu wote lazima uwe juu ya kamba, ambazo zilikuwa zimeongezeka kwa ukubwa, kubwa sawa na miili yetu. Hapa kwa kitambo tulitupwa kwa mshangao na kwa dhiki. Tuliulizana kwa minong'ono ya hofu: "Je! Hiyo kamba imeunganishwa na nini?" Mume wangu alikuwa mbele yangu. Matone makubwa ya jasho yalikuwa yakidondoka kutoka paji la uso wake, mishipa kwenye shingo yake na mapigo yaliongezeka hadi mara mbili ya ukubwa wake ya kawaida, na kukandamizwa, kuugua kwa maumivu kulitoka kwanye midomo yake. Jasho lilikuwa likidondoka kutoka usoni mwangu, na nilihisi fadhaa na uchungu kama vile sikuwahi kuhisi hapo awali. Mapambano ya kutisha yalikuwa mbele yetu. Tukishindwa hapa, shida zote za safari yetu zilikuwa zimepatikana bure. {2Tsw 596.2}

Mbele yetu, upande wa pili wa shimo hilo, kulikuwa na uwanja mzuri wa nyasi za kijani kibichi, karibu urefu wa inchi sita. Mimi sikuweza kuona jua; lakini miangaza myeupe, laini ya nuru, inayofanana na dhahabu safi na fedha, ilikuwa imekaa juu ya uwanja huu. Hakuna kitu ambacho nilikuwa nimekiona hapa duniani kinachoweza kulinganishwa uzuri na utukufu wa uwanja huu. Lakini Je! tungeweza kufanikiwa kuufikia? Tuliuliza kwa wasiwasi. Kamba ikikatika, lazima tuangamie. Kwa

kunong'ona, tena kwa uchungu, maneno yalitolewa: "Ni nini kinashikilia kamba?" Kwa muda tulisita kujitosa. Basi tukapaza sauti: "Matumaini yetu tu ni kuiamini kamba kabisa. Imekuwa ni utegemezi wetu kwa kila njia ngumu. Hata sasa haitatuangusha. "Bado tulikuwa tukisita na kufadhaika. Maneno hayo yalinenwa wakati huu:" Mungu anashikilia kamba. Hatupaswi kuogopa. "Maneno haya yalirudiwa na wale walio nyuma yetu, wakiongozana nasi: "Yeye Hatatuangusha sasa. Ametuleta salama mpaka sasa." {2Tsw 596.3}

Kisha mume wangu akajitupa juu ya dimbwi la kutisha hadi kwenye uwanja mzuri zaidi mbele. Mara moja nikimfuatia. Oh, ni hali gani ya utulivu, unafuu na shukrani kwa Mungu tulihisi! Nikasikia sauti zikipazwa za ushindi wa sifa kwa Mungu. Nilikuwa mwenye furaha, mwenye furaha kamilifu kabisa. {2Tsw 597.1}

Niliamka, na kugundua kuwa kutokana na wasiwasi niliokuwa nimeupata kupita uzoefu wa ile njia ngumu, kila neva ya fahamu katika mwili wangu zilionekana kutetemeka. Ndoto hii haihitaji ufafanuzi wowote au maoni. Ilifanya hisia kama hiyo juu ya akili yangu kuwa kila kitu ndani yake, nayo itakuwa wazi mbele yangu wakati kumbukumbu zangu zikiendelea. {2Tsw 597.2}

## SURA YA 74

### MIKUTANO YETU YA MAKAMBI

Hakuwezi kukawa na ushawishi wenye madhara kwa mkutano wa makambi, au mkutano mwingine wowote wa kidini, kama kutembeleana na mazungumzo/magumzo mengi yasiyohusiana na mkutano au kuwa na maana na mkutano. Mara kwa mara wanaume na wanawake hukusanyika kwenye makundi, na kushiriki mazungumzo juu ya masomo ya kawaida ambayo hayahusiani na mkutano. Wengine wameleta mashamba yao, wengine wameleta nyumba zao, na wanaweka mipango yao ya kujenga. Wengine wanachambua tabia za wengine, na kuwakatakata na hawana muda au utaratibu wa kupeleleza mioyo yao, kugundua kasoro za tabia zao ili waweze kurekebisha makosa yao katika utakatifu kamili wa hofu ya Mungu. Ikiwa wote wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wangepanya kuboresha muda wa mkutano katika kuzungumza juu ya Ukweli, kwa kukaa juu ya tumaini la Kristo, wakichunguza mioyo yao wenyewe, na kwa maombi ya dhati mbele za Mungu, wakiomba baraka Zake, kazi kubwa zaidi ingefanikiwa kuliko vile ambavyo bado hatujaona. Wale Wasioamini, ambao huwatuhumu kwa uwongo wale wanaoamini Ukweli, wangesadikishwa kwa sababu ya "mazungumzo yao mazuri katika Kristo." Maneno na matendo yetu ni matunda tuzaayo; "kwa sababu hiyo kwa matunda yao mtawatambua." {2Tsw 597.3}

Mungu alitoa mwongozo kwa Waisraeli kukusanyika mbele Zake kwa vipindi maalumu vilivyowekwa, mahali ambapo Mungu atapachagua na kuziadhimisha siku hizi maalumu ambazo hakuna kazi isiyo ya lazima inapaswa kufanywa, bali muda wa utolewe katika kutafakari Baraka ambazo Mungu amewapa. Katika misimu hii maalumu, mtumwa na mjakazi, mgeni, yatima na mjane walielekezwa kufurahi kwamba kwa nguvu Zake Mungu na kwa mkono hodari aliwatoa katika kifungo cha utumwa hadi furaha ya uhuru. Nao waliamriwa wasijihudhurishe mbele za Bwana mikono mitupu. Walitakiwa kuleta zawadi zao za shukrani

kwa Mungu, kwa rehema Zake za daima na Baraka walizotunukiwa. Sadaka na zawadi za hiari kulingana na baraka za mtoaji alizoweka juu ya hizo na hivyo walikuwa na nafasi ya kufurahi. Hivyo tabia za watu, ziliendelea kukua kwa uwazi. Wale ambao waliweka uthamani mkubwa juu ya baraka hizi ambazo wamepewa na Mungu, walileta matoleo yao kulingana na thamani ya shukrani na baraka hizo. Wale ambao nguvu zao za kimaadili zilipumbazwa na kufa ganzi kwa ubinafsi na kupenda ibada ya sanamu kwa kibali na baraka walizopewa, wapendao kupokea fadhila, badala ya kusukumwa na upendo wa dhati kwa Mpaji wao mkarimu, walileta matoleo kidogo. Kwa hiyo mioyo yao ilifichuliwa. Licha ya siku hizi maalumu za sherehe za kidini za furaha na shangwe, pasaka ya kila mwaka ilipaswa kukumbukwa na taifa hili la Kiyahudi. Bwana aliweka agano kwamba ikiwa wangekuwa waaminifu katika kuyashika maagizo Yake angewabariki katika maongezeko yao yote na kwa kila kazi zao zote za mikono. {2Tsw 598.1}

Mungu hajataka pungufu ya hili kwa watu Wake katika kipindi hiki cha mwisho, katika Kutoa sadaka na dhabihu kama alivyofanya katika taifa la Israel. Wale ambao amewabariki kwa mali, na hata mjane na yatima, hawapaswi kusahau baraka Zake. Hasa wale ambao Mungu amewafanikisha na wamrudishie vitu ambavyo ni Vyake, wanapaswa kujihudhurisha mbele Zake wakiwa na roho ya kujitolea nafsi na kuleta sadaka kulingana na baraka ambazo Bwana amewapa. Lakini wengi ambao Mungu amewafanikisha wameonyesha kutokuwa na shukrani Kwake. Ikiwa Baraka Zake zipo juu yao, na Yeye kawaongezea utajiri wao, wanafanya fadhila hizi kuwa kama kamba za kuwafunga kwa kuipenda mali zao; wanaruhusu bishara ya kidunia kuchukua mapenzi yao na utu wao wote, na kupuuzia ibada na upendeleo wa Kidini-fursa za kiroho. Hawana uwezo wa kuacha bishara zao na kuja mbele za Mungu hata mara moja kwa mwaka. Wanageuza baraka za Mungu kuwa laana. Wanatumikia maslahi yao ya muda kwa kupuuzia matakwa ya Mungu. {2Tsw 599.1}

Watu wamilikio maelfu hubaki nyumbani mwaka baada ya mwaka, wakijishughulisha kwa bidii na shughuli zao za kiulimwengu na mivuto yake, na hujihisi kuwa hawawezi kutoa kafara ndogo ya kuhudhuria mikutano ya kila mwaka ya ili kumwabudu Mungu. Yeye Amewabariki katika marobota/vikapu vya vyakula wanavyotumia sasa na ghala zao



na kuwazunguka kwa faida Zake upande wa kulia na wa kushoto, lakini bado wanamzuia matoleo madogo ambayo Yeye ameyataka kutoka kwao, Wanapenda kujitumikia wenyewe. Roho zao zitakuwa kama jangwa lisilosafishwa na umande au mvua ya mbinguni. Bwana amewaitea baraka ya thamani ya neema Yake. Yeye amewaokoa kutoka katika utumwa wa dhambi na utumwa wa makosa, na kuwafungulia katika giza lao ufahamu wa nuru ya utukufu wa Ukweli wa sasa (leo). Na Je, ushuhuda huu wa upendo na rehema za Mungu hautoi mwito kwao wa kurudisha shukrani? Je! Wale wale wanaodai kuamini kuwa mwisho wa vitu vyote umekaribia watakuwa vipofu kwa maslahi yao ya Kiroho, na kuishi kwa ulimwengu huu na maisha haya peke yake? Je! Wanatarajia kuwa mivuto/maslahi yao ya milele kujishugulikia yenyewe? Hawawezi kupata nguvu za kiroho hazitakuja bila juhudi yoyote kutoka kwao. {2Tsw 599.2}

Wengi wanaodai kutazamia kutokezea kwa Bwana wetu, wana wasiwasi na mahangaiko, nao ni watafutaji wa mizigo kwa faida ya kidunia. Wamekuwa vipofu kwa maslahi ya milele. Wanafanyia kazi kile ambacho hakiwatoshelezi. Wanatumia pesa zao kwa kile ambacho si mkate. Wanajitahidi kujiridhisha kwa hazina walizo nazo zilizowekwa juu ya dunia, ambazo lazima ziangamie. Nao wanapuuza maandalizi ya umilele, ambayo yanapaswa tu kuwa kazi ya kwanza na ya Kweli katika maisha. {2Tsw 600.1}

Hebu wale wote wanaoweza, wahudhurie mikutano hii ya kila mwaka. Wote wanapaswa kuhisi kuwa Mungu anataka hili kwao. Ikiwa hawatachangamkia upendeleo huu ambao ameutoa ili kwamba wawe imara ndani Yake na katika nguvu ya neema Yake, watadhoofika na kudhoofika zaidi, na watapungukiwa na kupungiwa zaidi, shauku yao yote ya kuweka wakfu vyote kwa Mungu. Njooi Ndugu na Dada kwenye mikutano hii mitakatifu ili kumtafuta Yesu. Yeye Atakuja kwenye sikukuu. Atakuwepo na atafanya kwa ajili yako yale yote ambayo unataka kuyafanya. Mashamba yako hayapaswi kuzingatiwa kwa uthamani mkubwa kuliko maslahi makuu ya roho. Hazina zote ulizo nazo, ziwe za thamani kiasi gani, hazitaweza kukununulia amani na matumaini, ambayo itakuwa faida isiyo na kikomo, ikiwa itakugharimu yote uliyo nayo na taabu na mateso ya maisha. Hisia

imara ya mambo ya umilele na moyo ulio tayari kutoa vyote kwa Kristo ni baraka za thamani zaidi kuliko utajiri wote na raha zote na utukufu wa ulimwengu huu. {2Tsw 600.2}

Mikutano hii ya makambi ni ya umuhimu. Inagharimu kitu. Watumishi wa Mungu wameyatoa maisha yao wakijichosha kuwasaidia watu, ambapo wengi wao wameonekana kana kwamba hawahitaji msaada. Kwa hofu ya kupoteza kidogo, faida yao ya ulimwengu huu, baadhi wameacha fursa hizi za thamani kuja na kwenda kana kwamba zilikuwa na umuhimu mdogo. Hebu wale wote wanaodai kuuamini Ukweli waheshimu kila upendeleo/fursa ambayo Mungu huwapa ili kupata kuona vema juu ya kweli Yake, Matakwa Yake, na matayarisho muhimu kwa marejeo Yake. Roho iliyotulia, yenye uchangamfu, na utii wenye uaminifu kwa Mungu, ndivyo anavyohitaji. {2Tsw 601.1}

Haupaswi kujichosha na mahangaiko, wasiwasi na shughuli nyingi zizohitajika. Siku moja uliyopewa, hiyo ndiyo kwa uaminifu ufanye kazi ambayo kwa majaliwa ya Mungu, Yeye amekupatia, Naye Mungu atakujali. Yesu atakuzidishia kwa kina na kupanua baraka zako. Lazima ufanye kwa bidii ikiwa kuna wokovu mwishoni. Njoo katika mikutano hii tayari kuifanya kazi. Acha mifadhaiko yako ya nyumbani na uje kumtafuta Yesu, naye atapatikana kwako. Njoo na sadaka zako kama vile Mungu alivyokubariki. Onyesha shukrani kwa sadaka yako ya hiari kwa Muumba wako, mtoaji wa fadhila zote. Asiwepo yeyote atakayekuja mikono mitupu. "Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mibinguni, na kuwafungulieni Baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la." {2Tsw 601.2}

Lengo la mkutano wa makambi ni kuwaongoza wote, kujitenga na maswala ya biashara na mizigo, na kujitoa kwa siku chache kumtafuta Bwana. Tunapaswa kuchukua muda wetu katika kujichunguza, kuchunguza kwa ukaribu mioyo yetu, ungamo la toba la dhambi, na kufanya upya nadhiri zetu Kwake Aliye Juu. Ikiwa yeyote atakuja kwenye mikutano hii kwa malengo yasiyostahili, na ya chini, tuna

matumaini kuwa tabia ya mikutano itakuwa ya kuleta akili zao kwa malengo sahihi. {2Tsw 601.3}

Wengine wanateseka sana kwa kupitia kazi za ziada katika kuandaa mkutano wa makambi. Wao ni watu walio na roho ya ukarimu, na hawataki chochote kifanyike kwa ubahili. Wengine hufanya ubanifu mkubwa na wamechoka kabisa wanapokuja kwenye mikutano, na mara tu wanapokuwa wanaachiliwa kutoka katika shinikizo la kazi, asili iliyochoka huwafanya wahisi kwamba wamedhulumiwa. Baadhi ya watu hawa huenda hawajawahi kuhudhuria mikutano ya makambi hapo kabla, na hawakujulishwa kuhusu maandalizi ambayo wanapaswa kuyafanya. Wanapoteza mikutano mingine mizuri ambayo ni lazima kuhudhuria. Sasa makosa haya yalifanywa kwa maandalizi makubwa sana. Hakuna kitu kinachopaswa kupelekwa kwenye mkutano wa makambi isipokuwa vitu vyenye afya zaidi, vilivyopikwa kwa njia rahisi, bila ya viungo na grisi (mafuta mazito kama margarine, kimbo, mafuta ya kuku, mafuta ya wanyama nk Usikose mikutano ukienda makambi, kwa kulala chumbani au kujiipikilisha sana!) {2Tsw 601.4}

Ninashawishika kwamba hakuna haja ya kujiletea ugonjwa kwaajili ya kuandaa mkutano wa makambi, ikiwa watashika sheria za afya katika kupika kwao. Ikiwa hawatetengeneza keki, au keki zenye kuwekwa vitu ndani (Pies) lakini kupika mkate rahisi wa ngano isiyokobolewa (graham bread), kutegemea matunda yaliyosindikwa, au yaliyochemshwa na kuhifadhiwa au makavu, hawahitaji kuugua wakati wa kuandaa mkutano, na hawahitaji kuwa mgonjwa wakati wa mkutano. Hakuna anayepaswa kuhudhuria mkutano mzima bila ya kuwa na chakula chenye joto. Daima kuna majiko ya kupika juu ya kwenye kambi, ambayo yanaweza kupatikana. {2Tsw 602.1}

Ndugu na dada lazima wasiwe wagonjwa wakati wa ukambikaji. Ikiwa watavaa mavazi ya baridi asubuhi na usiku, na ni muhimu kutofautisha mavazi yao kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa, ili kuhifadhi mzunguko mzuri (wa damu na mfumo wa mitoki), na kuzingatia utaratibu katika kulala, na kula chakula rahisi, bila kuchukua chochote katikati ya milo, hawana haja ya kuwa wagonjwa. Wanaweza kuwa na

afya nzuri wakati wa mkutano, akili zao zinaweza kuwa safi na kuweza kupendezwa, kuthamini na Ukweli, na wanaweza kurudi majumbani mwao wakiwa wameburudishwa katika mwili na roho. Wale ambao wamekuwa wakifanya kazi ngumu siku hadi siku sasa wanaacha zoezi lao; kwa hivyo wasingekula ule wastani wao wa chakula. Ikiwa watafanya hivyo, matumbo yao yatachoshwa kupita kiasi. Tunataka kuwa na nguvu ya ubongo ziongezeke haswa kwenye hii mikutano na katika hali ya afya zaidi kwa kusikia Kweli, kuithamini, na kuihifadhi, ili wote wapate kuifanyia/kuitendea mazoezi baada ya kurudi kutoka kwenye mkutano. Ikiwa tumbo limelemewa na chakula kingi sana, hata kile sahili, nguvu ya ubongo inaitwa kusaidia viungo vya mmeng'enyoy. Kuna kufa ganzi kwa hisia juu ya ubongo. Haiwezekani kabisa kuyafungua macho. Kweli ambazo zinapaswa kusikilizwa, kueleweka, na kutekelezwa, hupotea kabisa kupitia shida, au kwa sababu ubongo uko karibu kupooza kwa sababu ya kiwango cha chakula kinacholiwa. {2Tsw 602.2}

Ningeshauri wote kutumia kitu cha vuguvugu ndani ya tumbo angalau kila asubuhi. Unaweza kufanya hivi bila kazi nyingi. Unaweza kufanya uji wa ngano isiyokobolewa. Ikiwa unga usiokobolewa una chenga chenga, upepete, na wakati uji ni wa moto, ongeza maziwa. Hii itafanya uji kuwa tamu na nzuri na yenye afya katika uwanja wa makambi. Na ikiwa mikate yako ni mikavu, fikicha ndani ya uji, na utafurahia. Sikubaliani na kula chakula kingi cha baridi, kwa sababu nguvu ya uhai lazima itolewe kutoka kwa mfumo ili kupasha chakula hadi kiwe cha joto sawa na tumbo kabla ya kazi ya kumeng'anya kuendelea. Chakula kingine rahisi sana ni mlo mzuri wa maharagwe ya kuchemshwa au kuokwa. Changanya sehemu ya maharagwe na maji, ongeza maziwa au krimu (cream), na tengeneza mchuzi; mkate unaweza kutumika kama katika uji wa graham (unga usiokobolewa). {2Tsw 603.1}

Nimefurahishwa kuona maendeleo ambayo wengi wamefanya katika mageuzi/matengenezo ya afya, lakini nasikitika kuona pia wengi wakiwa nyuma. Ikiwa mtu yeyote atakuwa mgonjwa katika ukambikaji wetu, uchunguzi unapaswa kufanywa juu ya sababu ya ugonjwa, na hatua zinapaswa kuchukuliwa juu ya kesi hiyo, na rekodi kuwekwa. Siko tayari kwamba sifa ya mikutano yetu ya makambi iwe mbaya

kwamba ndiyo sababu ya kuwafanya watu waugue. Ikiwa sababu inayofaa itafuatwa kwa hii mikutano muhimu, inaweza kufanywa kuwa baraka kwa afya ya mwili na kwa afya ya roho pia. {2Tsw 603.2}

## **SURA YA 75**

### **NDOTO KUU**

Usiku wa Aprili 30, 1871, Nilienda kupumzika kwa huzuni sana katika roho. Kwa miezi mitatu nilikuwa nimekuwa katika hali ya kukata tamaa sana. Nilikuwa nimeomba mara kwa mara kwa uchungu wa roho kwa ajili ya kupata nafuu. Nilikuwa nimeomba msaada na nguvu kutoka kwa Mungu, ili nipate kushinda, na kuinuliwa juu ya kukatishwa tamaa kuzito kulikokuwa kumeipoozesha imani na matumaini yangu, na kunifanya kutokufaa kwa chochote. Usiku huo nilikuwa na ndoto ambayo ilifurahisha sana hisia za akili yangu. Niliota kwamba nilikuwa nahudhuria mkutano muhimu ambao kundi kubwa lilikusanyika. Wengi walikuwa wameinama mbele za Mungu kwa maombi ya dhati, na bidii na walionekana kulemewa. Walikuwa wakimsihi Bwana kwa nuru maalum. Wachache walionekana kuwa na uchungu wa roho; hisia zao zilikuwa kali; walilia kwa machozi na kwa sauti, wakaomba msaada na nuru. Ndugu zetu mashuhuri walikuwa wakishiriki katika tukio hili la kushangaza zaidi. Ndugu A alikuwa amesujudu chini, akionekana kwa wazi, yu katika shida kubwa. Mkewe alikuwa amekaa kati ya makundi ya dhihaka na wasiojali. Alionekana kama anatamani wote kuelewa kwamba aliwadharau wale ambao walikuwa wakijidhalilisha wenyewe. {2Tsw 604.1}

Niliota kwamba Roho wa Bwana Aliku juu yangu, nikainuka katikati ya kilio na sala, nikasema: Roho wa Bwana Mungu Yu juu yangu. Ninajisikia kuhimizwa kusema kwako kwamba lazima uanze kufanya kazi binafsi kwa ajili yako mwenyewe. Unamtazama Mungu na unatamani afanye kazi kwa ajili yako ambayo alikuachia wewe uifanye. Ikiwa mtafanya kazi yenu wenyewe, ambayo mnajua kwamba mnapaswa kuifanya, basi Mungu atawasaidia wakati mnahitaji msaada. Umeacha bila ya kutenda, mambo yale ambayo Mungu amekuachia kuyafanya. Umekuwa ukimwita Mungu akufanyie kazi yako. Na lau ungefuata nuru aliyokupa, basi angekuangazia nuru zaidi juu yako; lakini wakati unapopuuza mashauri, maonyo, na makemeo ambayo yametolewa, unawezaje kumtarajia Mungu kukupa nuru zaidi na baraka katika kupuuza na kudharau? Mungu sio kama mwanadamu; Yeye hatachezewa na kukosewa heshima. {2Tsw 604.2}

Nilichukua Biblia ya thamani na ikizungukwa na shuhuda kadhaa za Kanisa, zilizotolewa kwa watu wa Mungu. Hapa, nilisema mimi, kesi karibu za wote zimetimizwa (kwenye hizi shuhuda). Dhambi ambazo wanapaswa kuachana nazo zilionyesha. Ushauri ambao wanautaka unaweza kupatikana hapa, umetolewa kwa kesi zingine zilizo sawa na za kwao wenyewe. Mungu amekuwa radhi kukupa mstari juu ya mstari na amri juu ya amri. Lakini sio wengi wenu mnaojua hakika yaliyomo kwenye shuhuda. Hamyajui Maandiko. Kama ingelikuwa umelifanya Neno la Mungu kuwa somo lako, na shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kristo, usingekuwa na haja ya kuhitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuzia kujifungamanisha ninyi wenyewe na Kitabu cha Mungu kilichovuviwa ambacho ametaka kukufikia kirahisi kwa Shuhuda za moja kwa moja, zikiita usikivu wako kwa maneno yaliyovuviwa ambayo uliyapuuzia kuyatii, na kukuhimiza wewe kuyaratibu maisha yako kulingana na mafundisho Shuhuda zilizotolewa, na kukuvutia akili zako kwa umuhimu wa Kweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa si kwaajili ya kutoa nuru mpya, lakini kutia kwa dhahiri juu ya moyo, Ukweli wa uvuvio uliofunuliwa tayari. Wajibu wa mwanadamu kwa Mungu na kwa mwenzake umeainishwa wazi katika Neno la Mungu; lakini ni wachache tu kati yenu wanaomtii Bwana kwa nuru waliyopewa. Ukweli wa ziada haukuletwa nje; lakini Mungu kupitia Shuhuda, amerahisisha Kweli kuu zilizotolewa tayari na

kwa njia Yake Mwenyewe aliyoichagua ili kuleta mbele ya watu, kuwaamsha na kuzivutia akili kwa hizi, ili wote waachwe bila ya kuwa na udhuru. {2Tsw 605.2}

Kiburi, kujipenda, ubinafsi, chuki, husuda, na wivu vimefunika nguvu za ufahamu, na Ukweli, ambao ungekufanya uwe na busara kwa wokovu, umepoteza nguvu yake kwa kuvutia na kudhibiti akili. Kanuni Muhimu sana za utauwa hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya maarifa ya Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda hazipaswi kudharau Neno la Mungu, lakini kulikweza na kuvutia akili kwa Neno la Mumgu, ili unyenyekevu mzuri wa ukweli uweze kuwavutia wote. {2Tsw 605.3}

Nikasema zaidi: Kama Neno la Mungu lilivyozungukwa na hivi vitabu na majarida, ndivyo Mungu amekuzingira wewe ndani kwa kukukaripia, ushauri, maonyo, na kukutia moyo. Hapa mnalia mbele za Mungu, katika uchungu wa roho zenu, kwa nuru zaidi. Nimeidhinishwa na Mungu kukuambia kuwa hakuna mwangaza mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utang'aa kwenye njia zenu mpaka myafanyie kazi matumizi ya nuru mliyopewa tayari. Bwana amewazungushia wigo kwa nuru; lakini hamjaithamini nuru; mmeikanyaga juu yake. Wakati wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza, au wameifuata lakini bila kuijali au bila shauku. Wachache wameweka mioyo yao kutii nuru ambayo imempendeza Mungu kuwapa. {2Tsw 606.1}

Wengine ambao wamepokea maonyo maalum kupitia shuhuda wamesahau katika wiki chache karipio lililotolewa. Shuhuda kwa wengine zimerudiwa mara kadhaa, lakini hawajazifikiria kuwa zina umuhimu wa kutosha, kuzingatiwa kwa uangalifu. Imekuwa kwao kama hekaya zisizo na maana. Kama wangelikuwa wamezingatia nuru waliyopewa wangeepuka hasara na majaribu ambayo wanafikiria ni magumu na makali. Wanapaswa kujilaumu wenyewe tu. Wameweka nira juu ya shingo zao wenyewe, ambazo zinahuzunisha kubeba. Sio nira ambayo Kristo amewafungia. Kujali kwa Mungu na upendo Wake vilikuwa vikitekelezwa kwa niaba yao; lakini ubinafsi wao, mabaya yao, roho zisizoamini hazikuweza kutambua wema na rehema Zake. Wanakwenda mbio kwa hekima zao wenyewe, wakashikwa na majaribu

na kuchanganyikiwa kwa mashaka, wamewekewa mtego na Shetani. Mtakapokusanya miale ya nuru ambayo Mungu ametoa huko nyuma, ndipo atakapoongeza zaidi kutoa nuru.{2Tsw 606.2}

Niliwaelekeza kwa Israeli ya kale. Mungu aliwapa sheria Yake, lakini hawakutii. Kisha akawapa sikukuu na maagizo, ambayo, katika kuyatekeleza, Mungu angeweza kuwekwa ndani ya kumbukumbu zao. Walikuwa wameelekea kumsahau Yeye na madai Yake juu yao, kwamba ilikuwa ni lazima waweke akili zao zikichochewa kutambua majukumu yao ya kumtii na kumheshimu Muumba wao. Laiti wangukuwa watiifu, na kupenda kushika amri za Mungu, wingi wa siku kuu, kaida na ibada zingehitajika. {2Tsw 607.1}

Ikiwa watu ambao sasa wanadai kuwa hazina ya kipekee ya Mungu, wangetii matakwa Yake, kama Yalivyoainishwa katika Neno Lake, Shuhuda maalum zisingetolewa kuwaamsha kwa majukumu yao na kuwakumbusha dhambi zao na hatari zao za kutisha kwa kupuuza kutii Neno la Mungu. Dhamiri zimekuwa butu kwa sababu nuru imewekwa kando, imepuuzwa, na kudharauliwa. Na Mungu ataondoa Shuhuda hizi kutoka kwa watu, na kuwanyang'anya nguvu, na kuwanyenyekesha. {2Tsw 607.2}

Niliota kwamba, wakati nilipokuwa nikisema, nguvu ya Mungu iliniangukia kwa njia ya kushangaza sana, na nilinyimwa nguvu zote, lakini sikuwa na maono. Nilidhani kwamba mume wangu alisimama mbele ya watu akasema, "Hii ni nguvu ya ajabu ya Mungu. Yeye Amezifanya Shuhuda hizi kuwa njia kuu ya kufikia roho, na atafanya kazi kwa nguvu zaidi kupitia Shuhuda hizi kuliko vile alivyofanya hata sasa. Nani atakuwa upande wa Bwana?" {2Tsw 607.3}

Nilipata ndoto kwamba idadi kubwa ya watu, walinyanyuka papo hapo, kwa kuitikia wito. Wengine walikaa kimya, na sura zilionyesha chuki au hasira, wengine walidhihaki, wakadharau na kukejeli, na wachache walionekana kutokuguswa kabisa. Mmoja alisimama kando yangu akasema, Mungu amekuinua, amekupa maneno ya kuongea na watu, na kufikia mioyo yao na hajampa mwingine yeyote. Amezitengeneza Shuhuda zako ili kukutana na mioyo ambayo inahitaji msaada. Lazima



wewe usiendeshwe na dharau, kejeli, lawama, na kulaani. Ili kuwa chombo maalum cha Mungu, haupaswi kutegemea mtu yeyote, bali umtegemee Yeye peke Yake, na, kama mzabibu unavyong'ang'ania, acha vishikio vyako vitambae juu Yake Bwama (tendrils). Atafanya njia kupitia wewe ili kuwasilisha nuru Yake kwa watu. Lazima ukusanye nguvu kutoka kwa Mungu, kila siku, ili uweze kuimarishwa, ili mazingira yako yasihafifike au kupoteza nuru ambayo Bwana ameruhusu kuangaza juu watu Wake kupitia kwako. Ni mpango maalum wa Shetani kuzuia nuru hii isije kwa watu wa Mungu, ambao wanaihitaji sana wakati huu wa hatari za siku hizi za mwisho. {2Tsw 607.4}

"Mafanikio yako yapo katika unyenyekevu na usahili wako. Mara tu utakapojiondoa kwenye hili, na kutengeneza Ushuhuda upendeze akili za mtu fulani, nguvu yako itakuwa imeondoka. Karibu kila kitu katika enzi hizi kimekewa mngao na hakina uhalisi. Ulimwengu umejaa shuhuda zinazotolewa kwa kupendeza na haiba kwa muda mfupi, na kujiinua yenyewe. Ushuhuda wako ni wa tabia tofauti. Unapaswa j kuja chini kwenye mambo madogo madogo ya maisha, ukiweka imani dhaifu kutoka katika kufa, na kuwakumbusha waumini binafsi umuhimu wa kuangaza kama nuru ulimwenguni. {2Tsw 608.1}

Mungu amekupa Shuhuda zako, ili uweke mbele ya yule anayerudi nyuma na mwenye dhambi hali yake halisi, na hasara kubwa anayoipoteza kwa kuendelea na maisha ya dhambi. Mungu amekupa hili juu yako kwa kufungua mbele ya maono yako kama asiye na mtu mwingine yeyote anayeishi kwa sasa, na kulingana na nuru aliyokupa, Yeye atakuwajibisha kwa hiyo. 'Sio kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa majeshi.' Paza sauti yako kama tarumbeta, ukawaonyeshe watu Wangu makosa yao, na nyumba ya Israeli dhambi zao." {2Tsw 608.2}

Ndoto hii ilikuwa na ushawishi mkubwa juu yangu. Nilipoamka, mfadhaiko na huzuni/sonona yangu ilikuwa imekwisha, roho yangu ilikuwa changamfu, na nilitambua amani kubwa. Udhaifu ambao ulikuwa haunistahilishi katika kazi uliondolewa, nami nilitambua nguvu na wepesi ambao ulikuwa mgeni kwa miezi kadhaa. Ilionekana kwangu kwamba malaika wa Mungu walikuwa wameagizwa kuniletea unafuu.

Shukrani isiyoelezeka iliujaza moyo wangu kwa mabadiliko haya makubwa kutoka kwenye kukata tamaa hadi nuru na furaha. Nilijua kuwa msaada huo umetoka kwa Mungu. Udhahirisho huu ulionekana kwangu kama muujiza wa rehema za Mungu, nami sitaacha kamwe kuwa mwenye shukrani kwa fadhili Zake za upendo. {2Tsw 608.3}

## **SURA YA 76**

### **TABIA NA MAVAZI YA WATUMISHI/WACHUNGAJI**

[Imeripotiwa kama ilivyozungumzwa mbele ya Mkutano Mkuu Wa 1871.]

Waefeso 3: 6, 7: "Ya kwamba Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa Ahadi Yake iliyopo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili; Injili hiyo ambayo nimefanywa mhudumu wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadri ya uweza wa utendaji Wake." {2Tsw 609.1}

"Ambayo nilifanywa kuwa mhudumu," sio tu kuwasilisha Ukweli kwa watu, bali kuutimiza maishani. {2Tsw 609.2}

"Na kuwafanya watu wote waone ushirika wa siri, ambao tangu mwanzo wa ulimwengu umesitirika kwa Mungu. "Mstari wa 3: 9. Hii haimaanishi tu Maneno yanayotiririka kinywani; sio tu kuwa na ufasaha

katika kusema na kuomba; lakini katika kumfanya Kristo afahamike na, kuwa na Kristo ndani yetu, na kumfanya ajulikane na wale wanaosikia. {2Tsw 609.3}

Yeye "Ambaye sisi tunamhubiri, tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu kwa hekima yote," sio kama wasio na ujuzi, sio katika ujinga," ili tuweze kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu; kulingana na kazi Yake, itendayo kazi ndani yangu kwa nguvu." Wakolosai 1:28, 29. Ni kazi ya Mungu, neema kutoka kwa Mungu, kutambua na kuhisi, kukarimu maisha na matendo, ambayo yanavutia juu ya wale wasikiao. {2Tsw 609.4}

Lakini sio hili tu. Kuna mambo mengine ya kuzingatiwa, ambayo wengine wamekuwa wazembe, na kuyapuuzi, lakini ambayo yana matokeo yake, kwa nuru ambayo kwayo imewasilishwa mbele yangu. Mguso moyoni unafanywa kwa watu kwa mwenendo wa mzungumzaji katika mimbari, kwa mtazamo wake, na kwa njia yake ya kuongea. Ikiwa mambo haya ni kama vile Mungu angefanya kuwa yao, msukumo ambao watatoa utapendelea Ukweli; haswa hilo kundi litapendelewa kwa kushawishi ambao wamekuwa wakisikiliza hekaya za kubuni. Ni muhimu kwamba mtindo wa wahudumu uwe wa kiasi na wenye hadhi, kwa kufuata Ukweli mtakatifu, uliotukuka anaofundisha, ili maoni mazuri yapatikane juu ya wale ambao hawapendelei mambo ya dini kwa asili yao. {2Tsw 609.5}

Uangalifu katika mavazi ni kitu muhimu. Kumekuwa na ukosefu hapa kwa wachungaji ambao wanaamini Ukweli wa leo. Mavazi ya wengine hata yamekuwa machafu. Sio tu kumekuwa na ukosefu wa ladha na utaratibu katika kupanga mavazi kwa njia inayofaa juu ya mtu, na kuwa na rangi inayofaa na kupendeza kwa mtumishi wa Kristo, lakini mavazi ya wengine yamekuwa ya hovy hovy. Wachungaji wengine huvaa Vesti ya rangi nyepesi, wakati suruali zao zikiwa nyeusi, au fulana nyeusi na suruali ya rangi nyepesi, bila ladha au utaratibu na mpangilio wa mavazi wanapokuja mbele za watu. Vitu hivi ni mahubiri kwa watu. Mhudumu anawapa watu mfano wa utaratibu, na anaweka mbele yao unadhifu wa umaridadi na ladha katika mavazi yao, au anawapa

masomo kwa ulegevu na ukosefu wa ladha ambayo watakuwa katika hatari ya kufuata. {2Tsw 610.1}

Kitambaa cha rangi ambazo ni nyeusi-nyeusi au za giza [dark] hufaa zaidi kwa mhudumu katika mimbari na itafanya hisia nzuri juu ya watu kuliko inavyotengenezwa na mchanganyiko wa rangi mbili au tatu tofauti katika mavazi yake. {2Tsw 610.2}

Nilielekezwa kwa wana wa Israeli zamani, na nilioneshwa kuwa Mungu alikuwa ametoa maelekezo maalum kuhusu mavazi na mtindo wa mavazi utakaovaliwa na wale waliohudumu mbele Zake. Mungu wa mbinguni, ambaye Mkono Wake unafanya ulimwengu uendele, ambaye hututegemeza na kutupatia maisha na afya, ametupa ushahidi kwamba Yeye anaweza kuheshimiwa au kudharauliwa kwa mavazi ya wale wanaomtumikia. Alitoa maelekezo maalumu kwa Musa kwa kuzingatia kila kitu kinachohusiana na huduma Yake. Alitoa maagizo hata kwa habari ya mpangilio wa nyumba zao na kubainisha mavazi kwa wale ambao wanaopaswa kuyavaa ambao wangehudumu katika huduma Yake. Walipaswa kudumisha mpangilio katika kila kitu na haswa kuhifadhi usafi. {2Tsw 610.3}

Soma maagizo ambayo Musa alipewa ili kuwajulisha wana wa Israeli, wakati Mungu alipokuwa akishuka juu ya mlima kuzungumza katika masikio yao sheria Yake takatifu. Je, alimwamuru nini Musa awaambie watu wakifanye? Kuwa tayari siku ya tatu; kwa maana siku ya tatu alisema, Bwana atashuka juu ya mlima mbele ya macho ya watu wote. Walipaswa kuweka mipaka juu ya mlima. "Bwana akamwambia Musa, Enenda kwa watu, ukawatakase leo na kesho, na wafue nguo zao." Mungu Huyu mkubwa na hodari, Aliyeumba Edeni nzuri na kila kitu chenye kupendeza ndani yake ni Mungu wa utaratibu, na Anataka utaratibu na usafi kwa watu Wake. Mungu Huyu Mwenye nguvu alimwagiza Musa kuwaambia watu wafue nguo zao isije kukawa na uchafu katika mavazi yao na juu ya nafsi zao walipokuwa wakipanda mbele za Bwana. Musa akashuka kutoka mlimani kwenda kwa watu, na wakafua nguo zao, kulingana na amri ya Mungu. {2Tsw 611.1}

Na kuonyesha jinsi walivyokuwa waangalifu kuhusu usafi, Musa alipaswa kuweka birika la maji kati hema ya kukutania na madhabahu,

"na uweke maji hapo, kwa kunawa." Musa na Haruni, na wana wa Haruni waliomtumikia Bwana, walipaswa kunawa mikono yao na miguu yao, wakati walipoingia ndani ya hema ya kukutania, na walipoingia mbele za Bwana. {2Tsw 611.2}

Hii ilikuwa amri ya Mungu Mkuu na Mwenyezi. Hakukuwa na kitu cha kizembe na kisicho safi kuhusiana na wale ambao walionekana mbele Zake wakati walipokuja katika uwepo Wake mtakatifu. Na kwa nini ilikuwa hivi? Je, malengo ya uangalifu huu wote? Je. Ilikuwa tu kukabidhi watu kwa Mungu? Je, Ilikuwa tu kwa kupata idhini Yake? Sababu ambayo nilipewa ilikuwa hii, ili mguso na mvuto sahihi uweze kufanywa juu ya watu. Ikiwa wale waliohudumu katika ofisi takatifu watahindwa kudhihirisha kujali, na heshima kwa Mungu, katika mavazi yao na mwenendo wao, watu wangepoteza kicho na heshima yao kwa Mungu na huduma Yake takatifu. Ikiwa makuhani walionyesha kumcha Mungu sana kwa kuwa waangalifu sana na makini sana hasa walipokuja katika uwepo Wake, iliwapa watu wazo lililoinuliwa juu ya Mungu na mahitaji Yake. Iliwaonyesha kuwa Mungu alikuwa mtakatifu, na kazi Yake ilikuwa takatifu, na kwamba kila kitu kihusianacho na kazi Yake lazima kiwe kitakatifu; kwamba lazima kiwe huru kila kitu au chochote chenye unajisi na uchafu; na kwamba unajisi wote lazima uwekwe mbali na wale wanaomkaribia Mungu. {2Tsw 612.1}

Kutoka kwa nuru ambayo nimepewa, kumekuwa na uzembe katika suala hili. Naweza kusema kama vile Paulo anavyowasilisha. Inafanywa katika ibada ya kujifanyia mtu anachotaka na kupuuza mwili. Lakini uhiari huu katika unyenyekevu, hii ibada ya kujifanyia mtu anavyotaka na kupuuza mwili, sio unyenyekevu ambao una ladha ya mbinguni. Ule unyenyekevu utakuwa mahsusi kuwa nao, kwa matendo na mavazi ya wote wanaohubiri Ukweli mtakatifu wa Mungu, sawa na sahihi kabisa, ili kila kitu kilichounganishwa nasi kitaendana na dini yetu takatifu. Mavazi yenyewe yatakuwa pendekezo la Ukweli kwa wasioamini. Haya yenyewe, yatakuwa ni mahubiri. {2Tsw 612.2}

Lakini vitu ambavyo ni makosa mara nyingi hupita kwenye mimbari takatifu. Mhudumu mmoja akiongea na mwingine katika mimbari mbele ya mkutano, akicheka na kuonekana kana kwamba hana mzigo

wa kazi, au kukosa hisia kuu ya wito wake mtakatifu, hudharau Ukweli na huleta mambo matakatifu kwa kiwango cha chini cha vitu vya kawaida na vya tamaa za kimwili. Mfano unaelekea kuondoa hofu na uchaji wa Mungu kutoka kwa watu na kuondoa hadhi takatifu ya injili ambayo Kristo alikufa ili kuitukuza. Kulingana na nuru ambayo nimepewa, ingempendeza Mungu kwa wahudumu Wake kuinama kwa kupiga magoti mara tu watakapoingia kwenye mimbari, na kuomba msaada kwa kicho kutoka kwa Mungu. Ni hisia ya ajabu kwa kiasi gani ingefanywa? Kutakuwa na umakini na hofu juu ya watu. Mhudumu/mchungaji wao anawasiliana na Mungu; anajitoa kwa Mungu kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kinakaa juu ya watu, na malaika wa Mungu wanaletwa karibu sana. Wachungaji wanapaswa kumwangalia Mungu kuwa kitu cha kwanza wanapoingia kwenye mimbari, na hivyo kuwaambia wote: Mungu Ndiye chanzo cha nguvu zangu. {2Tsw 612.3}

Mhudumu ambaye ni mzembe katika mavazi yake mara nyingi huwajeruhi wale walio na ladha nzuri na busara iliyosafishwa. Wale ambao wana makosa katika suala hili wanapaswa kurekebisha makosa yao na kuwa waangalifu zaidi na wenye busara. Kupotea kwa roho zingine mwishowe kutafuatiliwa na kuonekana kulihusana na ukosefu wa mpangilio, unadhifu na mavazi ya mhudumu kutokuwa safi. Mwonekano wa kwanza uliathiri watu vibaya kwa sababu hawakuweza kwa njia yoyote kuhusisha kuonekana kwake na Ukweli aliouwasilisha. Mavazi yake yalikuwa kinyume dhidi yake; na ushawishi uliotolewa ni kwa watu ambao aliwawakilisha, alikuwa ambaye hakujali chochote juu ya mavazi yake, na wasikilizaji wake hawakutaka uhusiano wowote na kundi la watu wa aina hiyo. {2Tsw 613.1}

Hapa, kulingana na nuru ambayo nimepewa, kumekuwa na kupuuza dhahiri miongoni mwa watu wetu. Wahudumu wakati mwingine husimama kwenye mimbari na nywele zao zikiwa zimetimka/rafu, zikionekana kana kwamba zilikuwa hazijaguswa na brashi na kitana kwa wiki nzima. Mungu huvunjiwa heshima wakati wale wanaojihusisha na huduma Yake takatifu wanapuuzia muonekano wao. Zamani makuhani walihitajika kuwa na mavazi yao kwa pateni/mtindo maalum kwa kufanya huduma mahali Patakatifu na kuhudumu katika

ofisi za makuhani. Walipaswa kuwa na mavazi yanayolingana na kazi yao, na Mungu alibainisha wazi wazi ni kwa namna gani hili linapaswa kuwa. Birika liliwekwa kati ya madhabahu na makutano, kwamba kabla ya kuja katika uwepo wa Mungu, mbele ya macho ya mkutano, wanaweza kunawa mikono na miguu yao. Je! Hili lilifanya hisia gani kwa watu? Iliwaonyesha kwamba kila chembe ya vumbi lazima iondolewe kabla ya kwenda mbele za Mungu; kwa kuwa Alikuwa Mkuu sana na mtakatifu sana na ikiwa wasingefuata masharti haya, kifo kingefuata. {2Tsw 613.2}

Lakini angalia mtindo wa mavazi ambayo huvaliwa na baadhi ya wahudumu wetu katika siku za leo. Baadhi ya wanaohudumu katika mambo matakatifu hupanga mavazi yao juu ya miili yao, na hivyo kwa kiasi fulani, huharibu ushawishi wa kazi yao. Kuna ukosefu wa ladha katika rangi na unadhifu wa kufaa. Je! Ni hisia/mwonekano gani unaotolewa na namna hii ya mavazi? Je, sababu ni kwamba kazi ambayo wanajihusisha inachukuliwa kama sio takatifu au iliyotukuka kuliko kazi za kawaida, kama kulima shambani. Mhudumu kwa mfano wake anashusha chini vitu vitakatifu kuwa sawa na vitu vya kawaida. {2Tsw 614.1}

Mvuto wa wahubiri hao haumpendezi Mungu. Ikiwa yoyote ameletwa ili kupokea Ukweli kutoka kwa kazi zao, mara nyingi huiga wahubiri wao na kushuka kwa kiwango cha chini sawa na wao. Itakuwa ngumu zaidi kuwarekebisha hawa na kuwaleta katika nafasi nzuri, na kuwafundisha utaratibu wa kweli na upendo kwa nidhamu, kuliko kufanya kazi ili kuwabadili katika Ukweli, wanaume na wanawake ambao hawajawahi kusikia. Bwana anawataka wahudumu Wake kuwa safi na watakatifu, ili kuwakilisha ipasavyo kanuni za Ukweli katika maisha yao wenyewe, na kwa mfano wao kuwaleta wengine katika kiwango cha juu. 2Tsw 614.2}

Mungu anawataka wote wanaodai kuwa watu Wake wateule, japo sio waalimu wa kufundisha ile Kweli, wawe wanalifu kuhifadhi usafi wa kibinafsi na utakatifu, pia usafi na mpangilio katika nyumba zao na mazingira yao. Sisi ni mifano kwa ulimwengu, barua zilizo hai zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Mungu anataka wote

wanaodai utauwa, na haswa wale wanaofundisha Ukweli kwa wengine, kujiepusha na kila aina ya uovu. {2Tsw 614.3}

Kutoka katika nuru ambayo nimekuwa nayo, huduma ni ofisi takatifu na iliyoinuliwa, na wale wanaokubali hii Nafasi wanapaswa kuwa na Kristo mioyoni mwao na kuonyesha hamu/shauku ya dhati ya kumwakilisha Yeye inavyostahili mbele ya watu katika matendo yao yote, katika mavazi yao, katika kusema kwao, na hata kwa namna ya kuongea kwao. Wanapaswa kuzungumza kwa heshima/kicho. Wengine huharibu hisia nzito ambayo wanaweza kuwa wameifanya juu ya watu, kwa kupaza sauti zao juu sana na kupiga kelele na kupiga yowe katika kuwasilisha Ukweli [hallooing and screaming]. Wanapowasilishwa kwa njia hii, Ukweli hupoteza utamu wake mwingi, nguvu yake na umuhimu. Lakini ikiwa sauti itatumiwa kwa usahihi, ikiwa ina kicho na wadhifa wake, na ikiwa inaweka kuwa na uwiano na hata kuonesha masikitiko, utatoa hisia bora zaidi. Hii ndiyo sauti ambayo Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake. Aliwavutia kwa kicho na uzito; Aliongea kwa njia ya kusikitisha. Lakini kelele kubwa hizi zinafanya nini? [ hallooing and screaming ] Hizo Haziwapi watu chochote kuhusiana na maoni yaliyoinuliwa zaidi ya Kweli na haziwavutii watu kwa undani zaidi. Zinasababisha tu hisia zisizokubaliwa au za kukasirisha kwa wasikilizaji na huchosha viungo vya sauti vya mhubiri. Sauti itokavyo nje ya mdomo ina mengi ya kufanya katika kuathiri mioyo ya wale wanaosikia. {2Tsw 615.1}

Wengi ambao wanaweza kuwa wanaume wenye faida/wanaofaa wanatumia nguvu zao muhimu na kuharibu mapafu yao na viungo vya sauti kwa tabia yao ya kuzungumza. Wahudumu wengine wana tabia ya kuwa na haraka wakitetemesha sauti na maneno kutoka kwa kasi kwa wanachokisema kana kwamba walikuwa na somo la kurudia na walikuwa wakifanya haraka iwezekanavyo [rattling]. Hii sio njia bora ya kuongea. Kwa kutumia utunzaji mzuri, kila mhudumu anaweza kujielimisha mwenyewe kusema waziwazi na kwa kuvutia, sio kurundika maneno pamoja kwa haraka bila kuchukua muda kupumua. Anapaswa kuzungumza namna ya wastani, ili watu waweze kupata mawazo na kuyaweka akilini mwao wakati anapopita. Lakini wakati jambo hilo linapokimbizwa haraka sana, watu hawawezi kupata



vipengele/pointi kwenye akili zao, na hawana muda wa kupokea maoni ambayo ni muhimu kwao kuwa nayo; na wala hakuna wakati wa kweli kuwaathiri/kuwachoma kama ingelipaswa kuwa. {2Tsw 615.2}

Kuzungumza kutoka kooni, kuruhusu maneno kutoka kwa sehemu ya juu ya viungo vya sauti, wakati wote huvisikitisha na huvikasirisha viungo, sio njia bora ya kuhifadhi afya au kuongeza ufanisi wa viungo hivyo. Unapaswa kuivuta hewa iingine ndani kwa ukamilifu na acha tendo/kazi kubwa ya kuvuta hewa, ifanyike kutoka kwenye misuli ya tumbo. Wacha mapafu yawe ni kituo tu, lakini usiyategemee kufanya kazi hiyo. Ukiruhusu maneno yako kutoka kina cha chini kabisa, ukitumia misuli ya tumbo, unaweza kuzungumza na maelfu kwa urahisi kama ilivyo katika kusema na makumi. {2Tsw 616.1}

Baadhi ya wahubiri wetu wanajiua wenyewe kwa kuomba kwa muda mrefu, kwa kujichosha na sauti kubwa, wakati sauti ya chini ingefanya hisia nzuri na kuokoa nguvu zao wenyewe. Sasa, wakati unaendelea bila kujali sheria za uhai na afya, na kufuata msukumo wa wakati huu, usimlaumu Mungu, ukiharibikiwa na afya. Wengi wenu hupoteza wakati na nguvu katika utangulizi mrefu na udhuru muanzapo kuzungumza. Badala ya kuomba msamaha kwa sababu uko karibu kuwahubiria watu, unapaswa kuanza kazi yako kana kwamba Mungu alikuwa na kitu cha kusema nao. Wengine hutumia karibu nusu saa ya kuomba msamaha; kwa hivyo muda unapotea, na wanapofika kwenye mada yao, wakati wanatamani kukazia mada za Kweli, watu wanakuwa wameshachoka tayari, na hawana nguvu au hawavutiwi na ile Kweli. Unapaswa kuzifanya hoja muhimu za Ukweli wa sasa kuwa dhahiri kama vigingi vya umbali (milestone) vilivyo barabarani ili watu waelewe. Hapo ndipo wataona hoja ambazo unataka kuwasilisha na mafundisho unayotaka kukazia ili wayashike. {2Tsw 616.2}

Kuna daraja lingine ambalo uhutubia watu kwa sauti ya kunung'unika. Mioyo yao haijalainishwa na Roho wa Mungu, na wanafikiri ni lazima wafanye hisia za kuonekana kwamba wana unyenyekevu. Sababu hii haitukuzi huduma ya injili, lakini huileta chini na kuishusha hadhi. Wachungaji wanapaswa kuwasilisha joto la Ukweli kutoka kwenye utukufu. Wanapaswa kuongea kwa namna ambayo inastahili

kumwakilisha Kristo na kuhifadhi hadhi inayofaa wahudumu Wake.  
{2Tsw 617.1}

Maombi marefu yanayofanywa na baadhi ya wahudumu yamekuwa ya kushindwa sana. Kuomba kwa urefu mkubwa, kama wengine wafanyavyo, haifai kwenye nyumba ya Mungu. Wanaumiza koo na viungo vya sauti, na kisha wanazungumzia juu ya kuharibikiwa afya kwaajili ya kazi zao ngumu. Wanajijeruhi wenyewe wakati hawakuitwa kwa hilo. Wengi wanahisi kwamba kuomba kunawaumiza viungo vyao vya sauti kuliko kuzungumza. Hii ni kwa sababu ya hali mkao (position) usio asili ya mwili, na namna ya kichwa kinavyosimama. Wanaweza kusimama na kuzungumza, na wasijisikie kujeruhiwa. Mkao katika maombi unapaswa kuwa wa asili kabisa (natural). Kuomba kwa muda mrefu huchosha, na hakulingani na injili ya Kristo. Nusu au hata robo saa ni ndefu kabisa. Muda wa dakika chache ni wa kutosha kuleta hoja yako mbele za Mungu na kumwambia unataka nini; na unaweza kuchukua watu pamoja nawe na usiwachoshe na kupunguza hamu yao ya kujitoa wakfu na sala. Wanaweza kuburudishwa na kuimarishwa, badala ya kuchoshwa. {2Tsw 617.2}

Makosa yamefanywa na wengi katika mazoezi yao ya kidini katika kuomba kwa muda mrefu na kuhubiri kwa muda mrefu, kwa ufunguo wa juu wa sauti, na sauti ya kulazimishwa, kwa mkazo usio wa asili na sauti isiyo ya asili. Mhudumu amejichosha mwenyewe bila pasipo lazima na kuwafadhaisha sana watu kwa mazoezi magumu ya kuchosha, ambayo yote hayo siyo ya lazima. Wachungaji wanapaswa kuzungumza kwa adabu ili kuwafikia na kuwavutia watu. Mafundisho ya Kristo yalikuwa ya kuvutia na makini; Sauti Yake ilikuwa ya kupendeza. Na Je! haifai sisi, kama ilivyo kwa Kristo, kujifunza kuwa na tuni nzuri kama ya nyimbo katika sauti zetu? Bwana Alikuwa na ushawishi mkubwa, kwa maana Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Sisi tupo chini sana Kwake na kwa sasa tumepungukiwa mno, na hata tungefanya kwa kadiri tuwezavyo, bado juhudi zetu zitakuwa duni. Hatuwezi kupata na kumiliki mvuto aliokuwa nao Yeye; lakini kwa nini hatupaswi kujielimisha tuje karibu na Kielelezo kama inavyowezekana kwetu kufanya, ili tuweze kuwa na ushawishi mkubwa zaidi juu ya watu? Maneno yetu, matendo yetu, mwenendo wetu, hulka yetu, mavazi yetu,

kila kitu, kinapaswa kuhubiri. Sio tu kwa maneno yetu tunapaswa kusema kwa watu, lakini kila kitu kinachohusiana na nafsi yetu kinapaswa kuwa mahubiri kwao, ili maoni sahihi yaweze kufanywa juu yao, na kwamba Ukweli uliosema uchukuliwe nao kwenda nyumbani kwao. Hivyo imani yetu itasimama katika mwanga bora mbele ya jamii. {2Tsw 617.3}

Sikuwahi kuelewa zaidi kuliko nilivyoelewa leo tabia iliyoinuliwa ya kazi, kuheshimika kwake, utakatifu wake, na umuhimu wetu katika kuistahili/stahiki. Ninaona hitaji ndani yangu. Lazima nipate ustahili mpya unaofaa, mpako mtakatifu, au sitaweza kuendelea kuwafundisha wengine. Lazima nijue kwamba ninatembea na Mungu. Lazima nijue kwamba ninaelewa siri ya utauwa. Lazima nijue kwamba neema ya Mungu iko ndani ya moyo wangu, kwamba maisha yangu yanaendana na mapenzi Yake, kwamba ninatembea katika nyayo Zake. Kisha maneno yangu yatakuwa kweli na matendo yangu yatakuwa sawa. {2Tsw 618.1}

Lakini kuna jambo lingine ambalo nilikuwa karibu nimesahau. Ni ushawishi ambao mhubiri anapaswa kujitahidi kuuishi katika huduma yake. Kazi yake sio tu kusimama kwenye mimbari tu. Kwenye mimbari ndipo tu inaanza kazi. Anapaswa kuingia katika familia tofauti, na kumbeba Kristo huko, na kubeba mahubiri yake huko, na utekelezaji kwa matendo yake na maneno yake. Anapotembelea familia anapaswa kuuliza hali zao. Je! Yeye ndiye mchungaji wa kundi? Kazi ya mchungaji haifanyiki kwenye mimbari tu. Anapaswa kuzungumza na washiriki wote wa kundi, pamoja na wazazi ili kujifunza misimamo yao, na vivyo hivyo na watoto kujifunza yao. Mchungaji anapaswa kulilisha kundi ambalo Mungu amemfanya kuwa mwangalizi. Itakubalika kwenda nyumbani na kujifunza nao; lakini ukifanya hivi kwa kupuuzia kazi ambayo Mungu amekuamuru uifanye, unafanya vibaya. Kamwe usiingie katika familia bila kuwaalika kwa pamoja, na kusujudu na kuomba nao kabla ya kuondoka. Uliza afya ya roho zao. Je! Daktari stadi hufanya nini? Anauliza juu ya maelezo ya kesi hiyo, kisha anatafuta kutoa tiba. Vivyo hivyo daktari wa roho anapaswa kuuliza juu ya magonjwa ya kiroho ambayo washiriki wa kundi lake wanaugua, kisha aende kazini kutoa tiba sahihi, na amuulize Tabibu Mkuu aje

amsaidie. Wape msaada ambao wanahitaji. Wahudumu wa namna hiyo watapokea utukufu na heshima yote wanayostahili kama wahudumu wa Kristo. Na kwa kuwafanyia wengine hivyo nafsi zao zitahuishwa na kuwa hai. Lazima wawe wanapata nguvu kutoka kwa Mungu ili kuwapa nguvu wale ambao watawahudumia. {2Tsw 618.2}

Hebu Bwana atusaidie kumtafuta kwa moyo wote; Ninataka kujua kwamba kila siku nakusanya mionzi ya Bwana kutoka kwa utukufu, ambayo hutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu na kuangaza kutoka kwenye uso wa Yesu Kristo, na kutawanyika katika njia kunizunguka mimi. Ninataka kuwa nuru tu katika Bwana. {2Tsw 619.1}

## **SURA YA 77**

### **UPENDO WA MALI**

Ndugu Mpendwa B: Nimeanza kuandika ushuhuda kwako mara mbili, lakini nimeshindwa kuukamilisha kwa kupungukiwa muda. Sipaswi kuchelewesha tena, kwa maana ninahisi huzuni ya mzigo mzito juu ya kesi yako. Nimeandika ushuhuda kwa wahudumu kadhaa, na kesi zao zinapojirudia akilini mwangu, ninatambua kabisa kuwa hali zao za ni za kuhuzunisha. Kesi yako sio ya kipekee. Upendo wa faida, upendo wa pesa, vimekuwa maarufu kwa wahudumu wetu wengi wanaodai kuwa wawakilishi wa Kristo. Mifano ya baadhi ya hawa wahudumu imewafanya watu wakate tamaa. {2Tsw 619.2}

Baadhi ya wachungaji wetu wamesimama moja kwa moja katika njia ya maendeleo ya kazi ya Mungu, na watu ambao wanawatazama kama mfano wanarudi nyuma kutoka kwa Mungu. Karibu miaka miwili iliyopita nilioneshwa hatari za wachungaji wetu na matokeo ya

mwenendo wao kuhusiana na kazi ya Mungu. Nimesema kwa jumla kwa kuzingatia mambo haya, lakini wale walio na makosa zaidi ndio wanaokuwa wa mwisho kutumia shuhuda kwenye maisha yao wenyewe. Wengine wamepofushwa na masilahi yao ya ubinafsi kiasi kwamba hupoteza mtazamo wa tabia iliyoinuliwa ya kazi ya Mungu. {2Tsw 620.1}

Ndugu B, maisha yako yamekuwa karibu kutofaulu. Ulikuwa na talanta za ushawishi, lakini huna iliyoboreshwa kwa akaunti bora. Umeshindwa katika familia yako; umeacha mambo yaende huria mwishoni, na upungufu huo unaonekana kanisani. Bwana amekupa nuru ya kuzingatia katika kupuuza wajibu katika familia yako na njia ambayo unapaswa kufuata ili kukomboa yaliyopita. Upungufu wako ulielezwa, lakini haukuhisi dhambi ya kuleta watoto ulimwenguni bila mafunzo sahihi. Umetoa udhuru kwa makosa yao, dhambi zao, kupotoka kwao, kutochukua tahadhari, njia hatarishi na njia mbovu, na kujidanganya kwamba watakuwa sawa/sahihi siku zinapoendelea. {2Tsw 620.2}

Eli kwa hakika anawakilisha kesi yako. Mara kwa mara umejadiliana na watoto wako, ukisema: Kwanini mnafanya maovu kiasi hiki? lakini hukutumia mamlaka yako kama baba, kama kuhani wa nyumba hiyo, kwamba maneno yako yawe sheria katika familia yako. Upendo wako na wa mkeo ulio na makosa kwa watoto wako umewaongoza kupuuza jukumu la dhati la kuwajibika kwenu kama wazazi. {2Tsw 620.3}

Wajibu maradufu ulikuwa juu yako, Ndugu B, kama mhudumu wa Mungu, kutawala na kusimamia vizuri nyumba yako mwenyewe na kuwaleta watoto wako chini ya utii. Lakini umefurahishwa na uhodari wao na umesamehe makosa yao. Dhambi ndani yao haikuonekana kuwa kama ina uzito wa dhambi. Umemchukiza Mungu na karibu uwaharibu watoto wako kwa kutowajibika kwako, na umeendelea kupuuza hata baada ya Bwana kukukemea na kukushauri. Jeraha limefanyika katika kusudi la Mungu kwa ushawishi wako kama familia katika maeneo tofauti ambayo umeishi, limekuwa kubwa kuliko mema uliyoyakamilisha. Umepofushwa na kudanganywa na Shetani kuhusu familia yako. Wewe na mke wako mmewafanya watoto wenu kuwa kama rika lenu-[equals]. Wamefanya mambo kama walivyopenda. Kwa

huzuni hili limerudisha nyuma kazi yako kama mhudumu wa Kristo, na kupuuzia jukumu lako la kuleta watoto wako kwa utii kumesababisha uovu mkubwa zaidi, jambo ambalo linatishia kuharibu utumishi wako. Ulikuwa kwa uwazi ukimtumikia Mungu katika kazi Yake, wakati huo huo umekuwa ukijitumikia mwenyewe zaidi. Kazi ya Mungu imekuwa dhaifu na kudidimia; lakini umekuwa ukifikiria kwa bidii na kupanga jinsi ya kujinufaisha mwenyewe, na roho zimepotea kwa kupuuzia kwako majukumu. Wakati wa huduma yako, ungekuwa na nafasi ya kuijenga kazi hii, ikiwa ungeweka mfano kwa kutumikia kusudi la Mungu bila kujali maslahi yako mwenyewe, na kuchakaa kwaajili ya kujitolea kwako, mambo yako yangeweza kuangaliwa kwa udhuru, ingawa hata hivyo isingekubaliwa na Mungu. Lakini wakati upungufu wako umeonekana sana, katika mambo mengine, na kazi ya Mungu imeteseka sana kwa sababu ya mfano ambao umetoa kwa kupuuzia kwako jukumu la familia yako, ni jambo la kusikitisha machoni pa Mungu kwa wewe kudai unatumika kwa kusudi Lake, lakini ukifanya maslahi yako ya ubinafsi kuwa maarufu. {2Tsw 620.4}

Katika kazi zako umeamsha maslahi mara nyingi, na wakati ambao ungeweza kufanya kazi kwa faida bora, umeruhusu masilahi ya nyumbani kukuvuta mbali na kazi ya Mungu. Mara nyingi haujakuwa na uvumilivu na kufanya juhudi zako zote mpaka uridhike kwamba wote walikuwa wameamua kupokea ile Kweli au wapo dhidi ya Ukweli. Sio uongozi wa busara, kuanza vita dhidi ya nguvu za Shetani na kujitoa kwenye vita bila ushindi uwanjani wakati wa kilele cha mapigano, na hivyo kumpa adui nafasi ya kuwafunga zaidi kwa salama wale ambao walikuwa kwenye hatua ya kuondoka katika safu yake na kuchukua msimamo wao upande wa Kristo. Nia hiyo chanya ya hayo maslahi ikiisha kuvunjika, haiwezi tena kuinuliwa. Wachache wanaweza kufikiwa, lakini sehemu kubwa zaidi ya watu, haiwezi kuathiriwa na mioyo yao kulainishwa kwa uwasilishwaji wa Ukweli. {2Tsw 621.1}

Mzee C alipoteza ushawishi wake na nguvu ya Ukweli kwa kujihusisha na dhana za mashaka (speculations), kuhusiana na ndugu zake. Hili lilikuwa jambo la pekee la kuchukiza kwa Mungu kwa mhudumu wa Kristo. Lakini wewe umefanya vivyo hivyo. Wewe umefanya kusudi la Mzee C kuwa kisingizio kwa upendo wa magendo yako.

Umejihalalishia kusudi lako kwa kujifaidisha, kwa sababu wahudumu wengine wamefuata njia hii. Wahudumu wengine hawana vigezo kwa ajili yako. Ikiwa watajeruhi mvuto wao, na kujinyima idhini ya Mungu na matumaini ya ndugu zao, mwenendo wao unapaswa kuepukwa. Kristo Ndiye Mfano wako, na wewe huna kisingizio cha kufuata nyayo za wanaume wadhambi, wanaokosea kuwa mfano isipokuwa maisha yao yawe sawa na maisha ya Kristo. Mvuto wako utakuwa kifo katika kusudi la Mungu ikiwa utaendelea kufuata njia ambayo umeifuata kwa miaka michache iliyopita. Magendo yako na biashara yako, na kukusanya kutoka kwa ndugu zako mali ambayo hujachuma, ni dhambi kubwa mbele za Mungu. {2Tsw 622.1}

Wengine wamejinyima wenyewe vitu muhimu kwa faraja ya familia zao (comfort), na wengine hata mahitaji ya lazima ya maisha, ili kukusaidia wewe, nawe umepokea. Paulo anaandika kwa ndugu zake wafilipi: "Iweni na nia hiyo hiyo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu." " Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine. "Anawaandikia pia ndugu zake wa Korintho:" Mtu asitafute faida yake mwenyewe, bali ya mwenzake."Tena, anasema kwa huzuni: "Kwa maana wote hutafuta vyao wenyewe, wala si vya Kristo Yesu." {2Tsw 622.2}

Roho unayothamini, ya kutazama masilahi yako ya ubinafsi, inaongezeka juu yako, na mazungumzo yako yamekuwa na tamaa. Paulo anawahimiza ndugu zake Waebrania: "Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa Yeye Mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wa sitakuacha kabisa." Unatoa sifa yako kama kafara na ushawishi wako, kwa roho mbaya. Makusudi ya thamani ya Mungu yanashutumiwa kwa sababu ya roho hii ambayo imeshika wachungaji/wahudumu Wake. Umepofushwa na hauoni jinsi mambo haya kwa namna ya pekee yanavyomchukiza Mungu. Ikiwa umeamua kuingia na kuupata ulimwengu wote unaoweza, fanya hivyo; lakini usifanye chini ya mwavuli wa kumhubiri Kristo. Muda wako aidha umejitolea kwa kusudi la Mungu au la. Maslahi yako mwenyewe yamekuwa makubwa. Muda ambao ulipaswa kujitolea kwa kusudi la Mungu, wewe umejitolea zaidi kwa masuala yako ya kibinafsi, na unapokea, kutoka katika hazina ya Mungu, fedha

ambazo hustahili kupokea. Uko tayari kupokea fedha kutoka kwa wale ambao hawana hali nzuri kama wewe mwenyewe. Hauangalii upande wao na kuwa na matumbo ya huruma na kuwasikitikia. Huchunguzi kwa karibu kuona ikiwa wale wanaokusaidia wanaweza kumudu kufanya hivyo. Mara kwa mara inakuwa katika nafasi yako zaidi kuwasaidia wale ambao unapokea msaada kutoka kwao. Unahitaji kuwa mtu wa aliyebadilishwa kabla ya kazi ya Mungu kufanikiwa mikononi mwako. Kujali nyumba yako na shamba vimeishika akili yako. Hujajitoa kikamilifu katika kazi. Kama kisingizio cha kuwa sana nyumbani, umesema kuwa watoto wako wanahitaji uwepo wako na utunzaji, na kwamba lazima uwe pamoja nao ili kutekeleza nuru uliyopewa katika maono. Lakini, Ndugu B, je! umefanya hivi? Unatoa udhuru mwenyewe kwa kusema kuwa watoto wako sasa wako nje ya uwezo wako, ni wakubwa sana hivyo washindwa kuwaamuru kuwasimamia. Katika hili unakosea. Hakuna miongoni mwa watoto wako aliye mkubwa sana na hivyo kushindwa kuheshimu mamlaka yako na kutii amri zako, wakati bado makazi yao yapo chini ya paa lako. Je, wana wa Eli walikuwa na umri gani? Walikuwa wanaume waliooa; na Eli, kama baba na kuhani wa Mungu, alihitajika kuwazuia/kuwanidhamisha. {2Tsw 623.1}

Lakini kuruhusu mawazo yako kuona kwamba watoto wakubwa wawili sasa wako nje ya uwezo wako, na kuwa hawakuwepo wakati Mungu alipokutumia nuru kwamba ulikuwa ukiwaendekeza kwa uharibifu wao; kwamba unapaswa kuwaadabisha. Lakini una watoto wadogo watatu wanaotembea katika njia ya wenye dhambi, wasiotii, wasio na shukrani, wasio watakatifu, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu. Mwanao mdogo anafuata nyayo za kaka yake. Ni kusudi gani unatalifuta juu yake? Je! Unamfundisha mazoea ya bidii ya kazi na faida? Je! Unakuchukua kazi yako iliyopuuzwa kwa hofu na kukomboa yaliyopita? Je! Unatetemeka kwa Neno la Mungu? {2Tsw 624.1}

Kupuuza kwako nyumba yako, ni kwa ajabu kwa namna moja ambayo imeandikwa na Mungu katika Neno Lake na pia haswa shuhuda maalum ulizopewa, ukionyesha kupuuza kwako. Kijana wako hufanya vile atakavyo. Haumzuii. Hukumuelimisha na kumfundisha kubeba sehemu ya mizigo ya maisha yake. Yeye ni mvulana mbaya kwa



sababu ya kupuuza kwako. Maisha yake ni laumu kwa baba yake. Ulijua wajibu wako, lakini haukufanya hivyo. Hashawishiwi na ile Kweli. Anajua anaweza kufanya atakavyo, na Shetani kaidhibiti akili yake. Umefanya watoto wako kuwa kisingizio cha kukuweka wewe nyumbani; lakini, Ndugu B, vitu vya ulimwengu huu vimekuwa kipaumbele. {2Tsw 624.2}

Kusudi la kazi ya Mungu haipo karibu na roho yako, na mfano ambao umewapa watu wa Mungu haustahili kuigwa. Minnesota wanahitaji watendakazi, sio wachungaji tu ambao huenda mahali hapa na pale ambapo wanaona panawafaa. Kusudi la Mungu lazima liwe na wanamgambo wenye utayari, ambao hawatazuiliwa kutoka kwa kazi ya Mungu au wito wa wajibu kwa masilahi yoyote ya ubinafsi au ya kidunia. Minnesota ni shamba kubwa la Bwana, na wengi wameathirika kwa ushawishi na Kweli. Pale Makanisa yangaliweza kuletwa kwa utaratibu wa kufanya kazi, kwa nidhamu kabisa, nuru ingeangaza kutoka kwao ambayo ingewaambia wote jimboni. Ungefanya mara kumi zaidi huko Minnesota kuliko ulivyofanya. Lakini Ulimwengu umekuja kati yako na kazi ya Mungu, na kugawanya shauku/nia yako. Masilahi binafsi yanaingia moyoni mwako, na nguvu ya Ukweli imekuwa ikizimwa. Kuna haja ya mabadiliko makubwa kwako, ili uweze kuletwa katika utaratibu wa kufanya kazi. Umetimiza kidogo kazi halisi ndogo tu, kazi ya dhati na bidii. Walakini umekuwa katika bidii kupata mali yote unayoweza kuipata kama haki yako. Umekuwa mjanja katika kujinyakulia fedha; umeangalia maslahi yako mwenyewe, na umejifaidisha mwenyewe kwa hasara ya wengine. Kwa muda mrefu umekuwa ukienda katika mwelekeo huu; na usipoangaliwa kwa hili, ushawishi wako umefikia mwisho. Moses Hull alienda kwa mwelekeo huu. Mazungumzo yake yalikuwa ya kutamani, na alikusanya mali zote alizoweza kupata. Kushikilia kwake Ukweli hakukuwa na nguvu ya kutosha kuushinda ubinafsi wake. {2Tsw 624.3}

BF Snook alipokubali Ukweli, alikuwa maskini sana. Nafsi zenye ukarimu zilizinyima mahitaji yao, na hata baadhi ya mahitaji muhimu ya maisha, kumsaidia mchungaji huyu, ambaye walimwamini kuwa mtumishi mwaminifu wa Kristo. Walifanya haya yote kwa nia njema, wakimsaidia kama vile wangewasaidia Mwokozi wao. Lakini ilikuwa

njia ya kumharibu mtu huyo. Moyo wake haukuwa sawa na Mungu; alikosa kanuni. Hakuwa mtu aliyeongoka kweli. Kadiri alivyopokea, ndivyo hamu yake ya kutafuta pesa ilivyokuwa kubwa. Yeye alikusanya kila alichoweza kutoka kwa ndugu zake, mpaka aliposaidiwa, kupitia ukarimu wao, kwa nyumba yenye thamani; kisha akaasi imani, na kuwa adui mchungu zaidi kwa wale ambao walikuwa wakarimu sana kwake. Mtu huyu atalazimika kutoa hesabu kwa mali ambazo amechukua kutoka kwa waumini walio wakweli wa moyo, katika ile Kweli. Hakuwaibia wao, bali aliibia hazina ya Mungu. Hatumtakii yeye mabaya; kwa maana "Mungu ataleta hukumuni kila kazi, na kila tendo la siri, ikiwa ni jema au ni baya. "Ametembea katika njia za moyo wake na machoni pake mwenyewe, lakini kwa mambo haya yote Mungu atamleta katika hukumu. Mambo yote yaliyofichika ya giza, yataletwa nuruni, na mashauri ya sirini ya moyo yatadhihirishwa. {2Tsw 625.1}

Ndugu B, wewe sio kama wanaume hawa. Hatungekulinganisha na wao, lakini tungenesema: Jihadhari kutembea katika nyayo zao na kuwa na mazungumzo yenye tamaa za mali au fedha. Tamanio hili kwa upande wa wahudumu kupata mali kwa sababu za ubinafsi ni mtego. Na ikiwa wataendelea, watathibitisha maanguko yao. Wanapojiangalia wenyewe kwa ubinafsi, shauku/nia zao katika kufanikiwa kwa kazi ya Mungu, na upendo wao kwa roho maskini, unazidi kupungua na kupungua. Hawapotezi upendo na shauku katika Kweli mara moja. Kuondoka kwao kutoka kwa kusudi la haki hunyemelea polepole na hivyo kwamba mara nyingi inakuwa vigumu kujua ni muda gani mabadiliko haya yalifanyika. {2Tsw 626.1}

Nadhani njia yako ni ya hatari sana. Hujahisi ulazima wa kuzingatia nuru ambayo Mungu amekupatia, na kukuamsha mwenyewe kuokoa familia yako, ukishugulika kama baba na kuhani wa familia/kaya yako. Hukukana nuru iliyotolewa, hukuinuka kinyume chake; lakini umepuuzia kuibeba nje, kwa sababu hukuwa na nafasi nayo, uliona usumbufu, haikiwa rahisi kwako na hisia zako hazikupendezwa kufanya hivyo. Kwa hiyo ulikuwa kama Merozi. Kwa maana hukuja kumsaidia Bwana, ingawa jambo hilo lilikuwa na matokeo muhimu sana kuathiri masilahi ya milele ya watoto wako -Waamuzi 5:23. Ulipuuza jukumu lako. Katika suala hili ulikuwa mtumwa mvivu. Una utambuzi mchache tu wa jinsi

Mungu anavyoona kupuuza kwa wazazi kuwaadhibu watoto wao. Kama ungefanya matengenezo hapa, ungeona umuhimu wa juhudi zile zile za kudumisha nidhamu na utulivu katika kanisa. Ulegevu wako katika familia yako umeonekana pia katika kazi zako kanisani. Hauwezi kujenga kanisa, mpaka uwe mtu aliyebadilishwa. {2Tsw 626.2}

Kupuuzwa kwa nuru ambayo Mungu amekupa, kwa kiwango fulani, kumekufanya kwa kiwango cha juu wewe kuwa mateka, chombo chini ya Shetani; kwa hivyo mlango umeachwa wazi kwa ajili yake kupata kufika kwako kwa njia zingine na kukufanya wewe kuwa mtu dhaifu. Adui anaona kwamba amefanikiwa kupofusha macho yako kwa masilahi ya familia yako kwa kukuongoza kupuuzia nuru ambayo Bwana ameitoa. Ndipo Shetani amekuzunguka katika mwelekeo mwingine. Amesimua upendo wa magendo na uchuuzi wako, upendo wako wa faida; na kwa hivyo hamu yako imegawanywa kutoka kwa kusudi na kazi ya Mungu. Upendo wa Mungu na Ukweli unazidi kuwa na maana kidogo. Nafsi ambazo Kristo alizifia hazina thamani kwako kuliko masilahi yako ya kidunia ambayo ni ya muda mfupi. Ikiwa utaendelea kufuata kusudi hili, karibuni utakuwa na wivu, mwepesi kuhisi, na mwenye tamaa, na utaondoka kwenye Ukweli, kama wengine walivyoondoka. {2Tsw 627.1}

Una mashaka kuhusiana na kupata kazi karibu na unapoishi, ukitumaini kwamba kitu kinaweza kusemwa au kufanywa ili kuamsha watoto wako. Umepuuza wajibu wako. Unapochukua kazi iliyopuuzwa kwa muda mrefu ambayo Bwana amekuachia uifanye; wakati wewe, pamoja na roho ya Kristo, unapoamka kwa uthabiti kuweka nyumba yako katika utaratibu, basi unaweza kutumaini kwamba Mungu atasaidia juhudi zako na kuvuta mioyo ya familia yako. Wakati wewe umewafanya watoto wako kuwa kisingizio cha kubaki nyumbani kwako, haujafanya kazi ambayo uliomba ubaki nyumbani ili kuifanya. Hujawaadabisha watoto wako. Mkeo ana upungufu katika Nyanja hii, kwa hivyo kuna haja kubwa ya wewe kuwa katika nafasi ya kutekeleza wajibu wako. Upendo wake ni wa aina hiyo ambayo utamfanya awaendekeze/awadekeshe katika kufanya watakavyo na kuwaachia wachague marafiki zao, ambayo itasababisha uharibifu wao. Uwepo wako nyumbani, wakati unawaruhusu watoto wako kufanya watakavyo,

ni mbaya zaidi kwa familia yako, kuliko ikiwa ungekuwa mbali nao; na ina mvuto/ushawishi mbaya zaidi juu ya Ukweli. {2Tsw 627.2}

Mungu anaita watu dhati na bidii, wasio na ubinafsi, watendakazi wasiojipendelea wenyewe katika kusudi Lake ambao wataendelea na matawi mbalimbali ya kazi, kama vile kupata wanachama wa majarida/machapisho, ili kuwafundisha haraka katika kulipa ada yao, na kuhimiza ndugu kuendelea na utoaji wa mpango kwa ukarimu. Dhabihu, kujikana nafsi, suluba, na ukarimu usio na ubinafsi, ulibainishwa katika maisha ya Kristo, ambaye ni Mfano wetu kwa vitu vyote. Kazi na tabia ya mchungaji wa Kweli zitakuwa kulingana na maisha ya Kristo. Aliweka kando utukufu Wake, Nafasi Yake ya Mamlaka, heshima Yake, na utajiri Wake, na kujinyenyekesha kwa mahitaji yetu. Hatuwezi kuwa sawa na Mfano, lakini tunapaswa kuiga. Upendo kwa roho ambazo Kristo alifanya dhabihu hii kubwa unapaswa kuwachochea wahudumu Wake kujitahidi, kujikana nafsi, kuwa na bidii, ili waweze kuwa watendakazi pamoja Naye katika wokovu wa roho. Ndipo kazi za watumishi wa Mungu zitazaa matunda, kwa kuwa watakuwa vyombo Vyake haswa. Nguvu ya Mungu itaonekana juu yao katika ushawishi wa neema ya Roho Wake. Mungu angependa wewe uamke na upate nguvu ya kushinda vizuizi; Usiwe mwenye kukata tamaa kirahisi; ukihitaika, fanya bidii, kama vile mtume Paulo, kwa uchovu, kwa uchungu, kwa kukesha, kusahau udhaifu katika masilahi ya kina yaliyohisiwa kwa roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yao. {2Tsw 628.1}

Baadhi ya wahudumu/wachungaji wetu wanatumia fursa za ukarimu wa ndugu zetu kufaidika wenyewe; na kwa kufanya hivyo wanapoteza ushawishi/mvuto wao hatua kwa hatua; mfano wao katika mambo haya unaharibu imani ya ndugu zao juu yao. Na wanafunga mlango kwa ufanisi kwa wale ambao kwa hakika wanahitaji msaada na hata wale wanaostahili hawawezi kupata. Pia wanafunga mlango pale ambapo kuna mategemeo ya kupata msaada wa kuendeleza kazi ya Mungu. Watu wengi wanavunjwa moyo wawaonapo wahudumu wengine waliowaajiri wakionyesha nia ndogo sana kwa mafanikio juu ya kazi ya Mungu. Hawaoni kujitolea kwao katika kazi. Watu wamepuuzwa, na kazi ya Mungu inasimama, na kuondokewa furaha,

kwasababu ya ukosefu wa mwelekeo mzuri, usimamizi na ufanisi wa kazi ambao walikuwa na haki kuutarajia kutoka kwa wahudumu wao. {2Tsw 628.2}

Katika kukatishwa kwao tamaa baadhi ya ndugu huingiza hisia za kukosa subira na matumaini na huzuni kadiri wanavyoona ubinafsi na tamaa zikidhihirishwa na waalimu wao. Watu wengi wako mbele ya wachungaji wao (kiroho, uaminifu nk). Ikiwa wahudumu wataonyesha roho ya kujitolea na upendo kwa roho, mali haitazuiliwa kwa kazi. Wacha wachungaji wafikie kiwango cha juu kama wawakilishi wa Kristo na tutaona utukufu wa Mungu ukihudhuria uwasilishaji wa Ukweli, na roho zitaletwa kutambua uwazi na nguvu Zake. Kusudi la kazi ya Mungu lazima liwe msingi. {2Tsw 629.1}

Ndugu yangu, unaweza kufanya kazi nzuri. Una ujuzi wa ile Kweli na unaweza kuwa baraka kwa sababu ya Ukweli wa sasa ikiwa umewekwa wakfu na kutakaswa kwa kazi hiyo, ukifanya bila masilahi ya kibinafsi badala yake. Mungu amekupa dhamana takatifu, talanta za thamani; na ikiwa wewe utapatikana kuwa ni mwaminifu, ukiboresha talanta zako kwa uaminifu, hautaibika wakati Mwalimu atakuja, akihitaji mtaji na riba Yake. Sio salama kufanya nuru ionekane haina thamani, au kwa maana yoyote kupuuza nuru ambayo Mungu amekuwa radhi kukupatia. Una kitu cha kufanya ili kujiletea msimamo ambapo Mungu anaweza hasa kukufanyia kazi. {2Tsw 629.2}

Ustawi wa kazi ya Mungu huko Minnesota unatokana zaidi na kazi ya Ndugu Pierce kuliko juhudi zako mwenyewe. Kazi yake imekuwa baraka maalum kwa jimbo hilo. Ni mtu mwenye dhamiri yenye maadili yaliyo mema, uwezo wa kutofautisha jema na baya kwa haraka. Hofu ya Mungu iko mbele yake. Udhaifu umemlelea sana, na hii imemwongoza ajiulize kama alikuwa katika jukumu la wajibu wake na kuogopa kwamba Mungu hakuwa akipendelea juhudi zake. Mungu anampenda Ndugu Pierce. Ana kujithamini kudogo, anaogopa, na ana mashaka na anaogopa kazi; mawazo yake kila wakati akilini mwake ni kwamba hastahili au hana uwezo wa kusaidia wengine. Ikiwa angeshinda woga na kuwa na ujasiri zaidi kwamba Mungu atakuwa pamoja naye na kumtia nguvu angekuwa na furaha zaidi na baraka

kubwa kwa wengine. Katika maisha ya Ndugu Pierce kumekuwa na kushindwa kusoma tabia. Yeye aliamini wengine kuwa waaminifu kama alivyo yeye mwenyewe, na wakati mwingine amedanganywa. Yeye hana utambuzi ambao wengine wanao. Wewe pia umeshindwa, katika maisha yako, kusoma tabia. Umenena amani kwa wale ambao Mungu ametangaza uovu/mabaya juu yao. Katika umri wake na udhaifu Ndugu Pierce anaweza kutindikiwa, lakini wote wanapaswa kumthamini sana kwa sababu ya kazi yake. Anastahili upendo na huruma laini za ndugu zake, kwa kuwa ni mtu mwangalifu, mwenye dhamiri njema, anayemcha Mungu. {2Tsw 629.3}

Mungu anampenda Dada Pierce. Yeye ni mmoja wa watu wenye wasiwasi, woga, na mwangalifu katika wajibu wa utendaji wake, mtu ambaye dhamiri yake inamwongoza kuepuka uovu,; na atapokea tuzo wakati Yesu atakapokuja ikiwa atadumu kuwa mwaminifu hadi mwisho. Hajafanya kwa kujionyesha wema/fadhila zake, ni mtu mkimya zaidi, hapendi umakini uje kwake (reserved and timid); lakini bado maisha yake yamekuwa ya manufaa; yeye amebariki wengi kwa ushawishi wake. Dada Pierce hajitukuzi na kujiamini. Ana hofu nyingi, lakini hajiweki chini ya uongozi wa waoga na wasioamini, ambao hawatapata nafasi ya ufalme wa Mungu. Wale walio nje ya jiji ni miongoni mwa watu wanaojiamini, wenye kujisifu, na inaonekana wenye usongo, wanaopenda kwa maneno tu, lakini si kwa matendo na Kweli. Mioyo yao haiko sawa na Mungu. Hofu Yake haiko mbele yao. Waoga na wasioamini, wale ambao wanaadhibiwa na mauti ya pili, ni wale wa tabaka ambalo wanamwonea aibu Kristo katika ulimwengu huu. Wanaogopa kutenda sawa na kumfuata Kristo, wasije wakakutana na upotevu wa kifedha. Wanapuza wajibu wao, ili kuepukana na lawama na majaribu, na kuikimbia hatari. Wale ambao hawathubutu kufanya haki kwa sababu watajiweka wazi kwenye majaribu, hasara, taabu na mateso ni waoga, pamoja na waabudu sanamu, waongo, na wenye dhambi wote, wanaiva kwaajili ya mauti ya pili. {2Tsw 630.1}

Mahubiri ya Kristo ya Mlimani yatangaza ni nani waliobarikiwa kweli: "Heri walio maskini wa roho [wale wasiojikweza, bali wanyoofu, na wenye tabia ya unyenyekevu, wasio na kiburi kufundishika, si watu wa upuuzi na wenye kutaka makuu kwa ajili ya heshima za ulimwengu]:

kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri walio na huzuni, wale walio na toba/kutubu, wanyenyekevu, na wanaohuzunika kwa sababu ya kushindwa na makosa yao na kwa sababu Roho wa Mungu amehuzunishwa]; kwa maana hao watafarijiwa. Heri wenye upole, wale walio wapole na wenye kusamehe, ambao, wakitukanwa, hawatatukana tena, bali wadhihirishao roho ya kufundishika, na wasiojiweka juu sana]; kwa maana hao watairithi nchi.” Wale walio na sifa zilizo rodheshwa hapa hawatabarikiwa tu na Mungu hapa katika maisha haya, bali watavikwa taji ya utukufu, heshima, na kutokufa katika ufalme Wake. {2Tsw 630.2}

## **SURA YA 78**

### **KUSUDI LA KAZI YA MUNGU HUKO VERMONT**

Nimeonyeshwa kuwa wanafunzi wa Kristo ni wawakilishi Wake duniani; na Mungu amekusudia kuwa watakuwa taa katika giza la kimaadili la ulimwengu huu, lililotawanyika kote nchini, mijini, vijiji, na miji mikuu, "Tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu." Kama watatii Mafundisho ya Kristo katika Mahubiri Yake ya Mlimani, watakuwa wakitafuta daima ukamilifu wa tabia ya Kikristo, na watakuwa nuru ya Kweli ya ulimwengu, mifereji ambayo Mungu atawasilisha makusudi Yake ya Kiungu, Ukweli wa asili ya mbinguni, kwa wale wanaokaa gizani na ambao hawana ujuzi wa njia ya uzima na wokovu. {2Tsw 631.2}

Mungu hawezi kuonyesha ujuzi wa mapenzi Yake, na maajabu ya neema Yake kati ya watu wasioamini duniani asipokuwa ana mashahidi waliotawanyika kote duniani. Ni mpango Wake kwamba hao ambao ni washiriki wa wokovu huu mkuu kupitia Yesu Kristo wanapaswa kuwa wamishenari Wake, miili ya nuru ulimwenguni kote, kuwa ishara kwa watu, barua zilizo hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote, imani yao na matendo yao hushuhudia ukaribu kuhusu

Mwokozi anayekuja na kuonyesha kwamba hawakupokea neema ya Mungu bure. Watu lazima waonywe ili kujiandaa na hukumu inayokuja. Kwa wale ambao wamekuwa wakisikiliza hekaya tu, Mungu atawapa fursa ya kusikia Neno la hakika la unabii, ambao watafanya vizuri kwa kuzingatia kama taa inayoangaza mahali penye giza. Yeye atawasilisha Neno la Ukweli na la hakika kwa uelewa wa wote watakaozingatia; wote wataweza kutofautisha Ukweli na hadithi zilizowasilishwa kwao na watu wanaodai kuelewa Neno la Mungu na kustahili kuwafundisha walio gizani. {2Tsw 631.3}

Ili kuongeza idadi huko Bordoville, ndugu wameondoka huko, wakiacha maeneo walikotoka yakiwa masikini kwa kukosa nguvu na ushawishi wa kudumisha mikutano. Hii imefurahisha maadui wa Mungu na Ukweli. Ndugu hao walipaswa kubaki kama mashahidi waaminifu, matendo yao mema yakishuhudia Ukweli wa imani yao, kwa kuonyesha maisha yao safi na nguvu ya Ukweli. Ushawishi wao ungeshawishi na kuongoa, au ungewahukumu. {2Tsw 632.1}

Kila mfuasi wa Yesu ana kazi ya kufanya kama mmishenari wa Kristo katika familia, kwa majirani anapoishi, katika mji au jiji analoishi. Wote ambao wamewekwa wakfu kwa Mungu ni mifereji ya nuru. Mungu huwafanya kuwa vyombo vya haki kuwasilisha kwa wengine nuru ya Ukweli, na utajiri wa neema Yake. Wasioamini wanaweza kuonekana wasiojali na wazembe; lakini Mungu anawavuta na kusadikisha mioyo yao kuwa kuna uhalisia katika Ukweli. Lakini ndugu zetu wanapoondoka shambani, kuondoka katika mapambano, na kuruhusu kazi ya Mungu kudhoofika, kabla ya Mungu kusema, "Waacheni," watakuwa tu mzigo kwa kanisa lolote ambalo wanaweza kuhamia. Wale ambao wameondoka, ambao walivuviwa, mara nyingi walinyamazisha dhamiri zao kwa kufikiria kwamba, baada ya yote, walikuwa na wasiwasi wa bure tu; wanakata shauri kuwa hakuna ukweli katika taaluma iliyofanywa na Waadventista Wasabato. Shetani hushinda akiona mzabibu uliopandwa na Mungu uking'olewa kabisa au ukiachwa udhoofike. Sio kusudi la Mungu kwamba watu Wake wajikusanye katika vikundi na kulimbikizia ushawishi wao katika eneo mahalia. {2Tsw 632.2}



Jitihada za Ndugu D kuhamasisha ndugu kuhamia mahali pao zilifanywa kwa nia njema, lakini sio kulingana na mapenzi ya Mungu. Njia za Mungu sio kama njia zetu. Yeye Haoni kama vile mtu aonavyo. Makusudi yalikuwa mazuri; lakini, kwa kufanya hivyo, makusudi ya Mungu kuhusu wokovu wa roho hayangeweza kutekelezwa. {2Tsw 633.1}

Mungu anapanga kwamba watu Wake watakuwa nuru ya ulimwengu, chumvi ya dunia. Mpango wa kukusanyika pamoja kwa idadi kubwa, kusimika kanisa kubwa, kumepunguza ushawishi wao na kufanya manufaa kuwa duru ya ushawishi wao kuwa finyu, na kwa kweli wameweka nuru yao chini ya pishi. Ni muundo wa Mungu kwamba ujuzi wa Ukweli uwafikie wote, ili kwamba asiwepo yeyote anayeweza kukaa gizani, bila kujua kanuni; lakini kwamba wote wajaribiwe juu yake na waamue au wapinge, ili wote waonywe na kuachwa bila udhuru. Mpango wa kufanya koloni, au kuhamia kutoka maeneo tofauti ambapo kuna nguvu kidogo au ushawishi kidogo, na kurundika ushawishi wa watu wengi katika eneo moja, ni kuondoa taa kutoka mahali ambapo Mungu angeitaka iangaze. {2Tsw 633.2}

Wafuasi wa Kristo waliotawanyika ulimwenguni kote, hawana kiwango cha juu cha uwajibikaji wao na wajibu uliopo juu yao kuiruhusu nuru yao iwaangazie wengine. Ikiwa kuna mmoja tu au wawili mahali, ingawa wachache kwa idadi wanaweza, kujiendesha mbele ya ulimwengu nak uwa na ushawishi ambao utawavutia wasioamini na Ukweli juu ya imani yao. Wafuasi wa Yesu hawatakutana na akili na mapenzi ya Mungu ikiwa wanaridhika kukaa katika kutokujua Neno Lake. Wote wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia. Kristo aliwaamuru wafuasi Wake: "Mwayachunguza Maandiko, kwa maana mnadhanja mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndio yanayonishuhudia Mimi. Petro anatuhimiza: "Bali mtakaseni Bwana Mungu mioyoni mwenu; muwe tayari daima kumjibu kila mtu anayekuuliza sababu ya tumaini lililo ndani yako kwa upole na kwa hofu." {2Tsw 633.3}

Wengi wanaodai kuamini Ukweli wa siku hizi za mwisho watakutwa wakiwa wamepunguka. Wamepuuza mambo mazito. Uongofu wao ni wa juu juu tu, sio wa kina, sio wa bidii, na sio kamili. Hawajui kwanini

wanaamini Ukweli, wanaamini sababu tu wengine wameuamini, na wanauchukulia Ukweli kuwa wa kawaida tu. Hawawezi kutoa sababu yenye busra au akili mahiri, kwamba ni kwanini wanaamini. Wengi wameruhusu akili zao kujazwa na vitu vya umuhimu mdogo, na masilahi yao ya milele hufanywa kuwa namba mbili. Roho zao zimedumaa na kulemaa katika kukua kiroho. Wengine hawaangaziwi au kujengwa na uzoefu wao au kwa maarifa ambayo ilikuwa fursa yao na wajibu wao kupata. Nguvu na utulivu vipo pamoja na wanaokiri kwa mioyo ya Kweli. {2Tsw 634.1}

Kristo na Yule aliyesulubiwa Anapaswa kuwa mada ya mawazo yetu na kuchochea hisia za ndani kabisa za roho zetu. Wafuasi wa ile Kweli wa Kristo watatoa shukurani kwa wokovu mkuu ambao wamefanyiwa; na popote atakapoongoza njia Yeye, watafuata. Watachukulia kama ni upendeleo kubeba mizigo yoyote ambayo Kristo anaweza kuweka juu yao. Ni kwa njia ya msalaba pekee, tunaweza kukadiria thamani ya nafsi ya mwanadamu. Hiyo ndiyo thamani ya watu ambao Kristo alikufa kwa ajili yao, kwamba Baba huridhika na gharama isiyo na kikomo ambayo amelipa kwa wokovu wa mwanadamu, kwa kumtoa Mwanawe Mwenyewe afe kwa ukombozi wao. Hekima, rehema na upendo ulioje katika utimilifu Wake umeonyeshwa hapa! Thamani ya mwanadamu inajulikana tu kwa kwenda hadi Kalvari. Katika siri na fumbo la msalaba wa Kristo, tunaweza kuweka makadirio juu ya thamani ya mwanadamu. {2Tsw 634.2}

Ni nafasi ya kuwajibika iliyoje, kuungana na Mkombozi wa ulimwengu katika wokovu wa watu! Hii kazi inahitaji kujikana, kujitolea, na ukarimu, kwa uvumilivu, ujasiri, na imani. Lakini wale ambao wanahudumu kwa Neno na mafundisho na hawana matunda ya neema ya Mungu mioyoni mwao na katika maisha yao; hawana imani. Hii ndio sababu kuna matokeo madogo sana kutoka kwa kazi yao. Wengi wanaodai kuwa watumishi wa Kristo, wanaonyesha hujisalimisha vizuri wanapowaona wasioongoka wote wanaowazunguka wakienda upotevuni. Mtumishi wa Kristo hana haki ya kupumzika na kukaa chini kwa unyonge, kwa mtazamo kuwa uwasilishaji wake wa Ukweli hauna nguvu na roho haziamshwi. Anapaswa kuomba, na anapaswa kufanya kazi na kuomba bila kukoma. Wale ambao hujisalimisha kubaki kuwa masikini

na bila baraka za kiroho, bila kupigana kwa bidii kwa ajili ya baraka hizo, huruhusu Shetani ashinde. Imani ya kudumu, na isiyochoka, iliyopo ni jambo la lazima. Watumishi wa Mungu lazima waingie katika ushirika wa karibu na Kristo na kufuata mfano Wake katika mambo yote, katika usafi wa maisha, uadilifu katika kujikana nafsi, kwa fadhili, kwa bidii, na katika uvumilivu. Wanapaswa kukumbuka kuwa siku moja rekodi itaonekana kama ushahidi dhidi yao kwa kuacha wajibu wao, hata ule ulio mdogo kabisa. {2Tsw 635.1}

Ndugu D hakutambua kuwa kwa kuwahimiza ndugu kuhamia kwake, alikuwa akileta mizigo juu yake na kwa kanisa; hakuona kwamba itahitaji muda mwingi na bidii ya kazi, kwa kuwaweka katika hali ambayo wanaweza kuwa msaada badala ya kikwazo. Alifikiri kwamba ikiwa angeweza kukusanya familia mahali pake wangesaidia kuanzisha kanisa, na wangemsaidia yeye kwa huduma na kubeba mizigo. Lakini imethibitishwa huko Bordoville kama huko Battle Creek; kadiri ndugu walivyohamia huko, ndivyo wanavyozidi kuwa mizigo mizito ambayo huwaangukia wafanyakazi ambao walikuwa na kusudi la kazi ya Mungu mioyoni mwao. Ikiwa wanaume na wanawake walio na akili anuwai na mashirika tofauti wanaweza kukusanyika pamoja na kuishi kwa uelewano mzuri, ikiwa wangepanya hivyo kwa kuheshimu wengine na kuwaona kuwa bora kuliko wao wenyewe, ikiwa wangewapenda jirani zao kama wao wenyewe, kama Kristo alivyowaamuru. {2Tsw 635.2}

Lakini ni ngumu sana kushughulika na akili za wanadamu ambazo haziko chini ya udhibiti maalum wa Roho wa Mungu na ambazo zimeanikwa katika udhibiti wa Shetani. Ubinafsi umetawala mioyo ya wanaume na wanawake, na uovu unapendwa sana, hata na wengine wanaodai kuwa na utauwa, kwamba kujumuika pamoja kunapaswa kuepukwa; kwa kuwa hawatakuwa na furaha. {2Tsw 636.1}

Wale ambao Ndugu D alitaka sana waje Bordoville walikuwa wale ambao aliwaona kuwa bora kwa jamii, wenye kutoa ushawishi mzuri. Ni wanaume na wanawake kama hao ndio wanaotakiwa kusimama juu ya ulimwengu kama walinzi waaminifu, ili wale ambao wako nje ya Mungu wasadikishwe kwamba kuna nguvu katika dini ya Kristo. Watu

hao wa ushawishi kwa kweli ni chumvi ya dunia. Mungu asingefurahi kama wangekusanyika pamoja na kupunguza nyanja/duru zao za manufaa. Wanaume wa kuaminika ni adimu sana kwa sababu mioyo ya watu imejitoa sana kwa ubinafsi na masilahi kiasi kwamba hawatambui wengine au mengine. {2Tsw 636.2}

Ikiwa kunaweza kuwa na idadi ya wanaume waliochaguliwa kwenye kituo muhimu huko Battle Creek, Mungu angekuwa radhi; na ikiwa wangejitoa mhanga kwa masilahi yao binafsi kwa ajili ya mateso, wangekuwa tu wakifuata nyayo za Mkombozi wao, aliyeuacha utukufu Wake, enzi Yake na mamlaka ya juu, na kwa ajili yetu akawa masikini, ili sisi, kwa umaskini Wake, tupate kutajirika. Kristo alijitoa dhabihu kwa ajili ya mwanadamu; lakini mwanadamu, kwa zamu yake, hatoi dhabihu kwa hiari na kwa furaha kwa ajili Kristo. Ikiwa idadi ya wanaume na wanawake wanaowajibika, wenye moyo wa Kweli, wanaobeba mzigo ambao, wangetegemewa kama wanamgambo walio na utayari (watu wanaosonga mbele kwa haraka -minuteman), ambao wangejibu mara moja kwa wito na kutoa msaada wakati ambapo msaada unahitajika, wangehamia Battle Creek, Mungu angetukuzwa. Mungu anataka wanaume huko Creek ambao wanaweza kutegemewa; ambao watapatikana wakati wote upande sahihi katika nyakati za hatari; ambao watapigana vita kwa uaminifu dhidi ya adui, badala ya kuchukua nafasi zao na wale ambao wanasumbua Israeli wa Mungu, na kusimama kuwatetea wale wanaodhoofisha mikono ya watumishi wa Mungu, kugeuza silaha zao dhidi ya wale ambao Mungu amewaamuru waendeleo kutegemeza kazi. Ili kufanikiwa, kila kanisa lazima liwe na wanaume ambao linaweza kuwategemea wakati wa hatari, wanaume ambao ni wa Kweli kama chuma, wanaume wasio na ubinafsi, ambao wana nia, maslahi na kusudi la Mungu, likiwa limelala katika mioyo kuliko kitu chochote ambacho kinahusu maoni yao wenyewe au masilahi yao ya kidunia. {2Tsw 636.3}

Makanisa hayajabeba Wakristo walio safi na wa kweli pekee. Sio majina yote yaliyosajiliwa kwenye vitabu vya kanisa yanastahili kuwapo. Maisha na tabia ya baadhi ikilinganishwa pamoja na wengine ni kama dhahabu iliyo na taka isiyofaa. Haifai kuwa hivyo. Wale ambao wana thamani katika maisha na ushawishi wamejihisi umuhimu wa kumfuata Yesu kwa karibu, kufanya maisha ya Kristo kuwa somo lao

na mfano wao. Hii itahitaji bidii, tafakari, na maombi ya dhati na bidii. Inahitaji bidii kupata ushindi juu ya ubinafsi na kufanya masilahi ya kusudi la Mungu kuwa ya kwanza. Wengine wamefanya juhudi, na kwa karibu walijizoeza kuwa na nidhamu, na wamepata ushindi wa thamani. Wale ambao wamezingatia masilahi yao kuwa ya msingi, wakiishina ubinafsi. Tabia yao mbele za Mungu ni kama taka isiyofaa. {2T 637sw.1}

Ndugu D amekuwa na watu zaidi ya mmoja anapaswa kufanya kazi kwa masilahi ya kanisa katika mahali pake. Ikiwa angejiondoa kwa muda mfupi ili kufanya kazi kwaajili ya wengine, mizigo mizito na mikubwa yote ilikuwa tayari kuwekwa juu yake wakati arudipo nyumbani. Amewaruhusu kupumzika juu ya mabega yake, na ameinama kwa kuugua chini ya mzigo. Ndugu wakina D wamekuwa katika hatari ya kuwa wakali na kutaka kila kitu kiwe namna wanavyotaka, wamewasilisha maisha yao wenyewe na mfano kama kigezo. Ubinafsi haujazama katika Kristo. Ndugu hawa hawapaswi kuzungumza hata kidogo juu ya ubinafsi, lakini wanapaswa wamwinue Kristo. Wao wanapaswa kujificha nyuma ya Yesu na kumwacha Yeye peke Yake aonekane kama Mfano kamili, ambao wote wanapaswa kuutafuta na kuuiga. {2Tsw 637.2}

Wako wapi wanaume ambao wangetegemewa wakati wa majaribu na hatari? Wako wapi Wanaume wanaomcha Mungu ambao wako tayari kukusanyika ili kuinua kiwango wakati adui alikuwa akitafuta faida? Wengine ambao walipaswa kuwa katika nafasi zao za ulinzi hawakuwa waaminifu wakati msaada wao ulihitajika zaidi. Mwenendo wao ulionyesha kuwa walikuwa hawana shauku maalum katika kuendeleza kazi ya Mungu. Wengine walidhani kwamba mengi yalikuwa yanatarajiwa kutoka kwao; na, badala ya kusonga mbele kwa ucheshi ili kufanya kile ambacho wangeweza kufanya, wakakaa kwa starehe katika kiti cha Shetani kinachobembea, na kugoma kufanya chochote. {2Tsw 638.1}

Wengine daima walikuwa na kawivu/wivu. Ndugu E alikuwa wa tabaka hili. Ana ukaidi wa kipekee kwenye tabia yake ambao unamwongoza kuendelea katika njia mbaya kwa sababu anafikiria atawapa faida

nduguze ikiwa atabadilika na hivyo huchukua njia kinyume na wenzake. Wakati mwingine anajisikia kufanya hivyo basi atakuwa tayari kufanya chochote katika uwezo wake wa kuendeleza kazi ya Mungu. Lakini anapendelea sana kujichukulia njia yake mwenyewe kiasi cha kutojali kwamba kazi ya Mungu ya thamani inapata shida, alimradi tu awe mshindi kwa kufanya anachokitaka mwenyewe. Ndugu E sio mtu ambaye anaweza kutegemewa. Yeye yuko chini ya majaribu ya Shetani na mara nyingi yuko chini ya udhibiti wake. Yeye ana moyo wa ubinafsi, usiotawaliwa. Ni mwenye kigeugeu, harara, akichukia saa hii na mara tena kupenda. Wakati mwingine ni mwema, na mwenye fadhila. wakati mwingine ni mwenye wivu, husuda, na mbinafsi sana. Hawezi kukamilisha tabia ya Kikristo mpaka atakapopinga majaribu, kuselimisha nia ya ukaidi wake mwenyewe, na kuthamini roho ya unyenyekevu, nia ya kuona na kukiri makosa yake. Amekuwa, wakati mwingine, mkweli, dhati na mwenye bidii. Kisha wimbi lingemchukua kinyume cha mwelekeo wake, na angethamini wivu, husuda, na kutoamini wengine. Masilahi ya kibinafsi na ubinafsi yalikuwa kipaumbele kwake, alikuwa amejaa kutafuta makosa, na tuhuma kwamba wengine hawakumthamini, yeye, lakini walitaka kumjeruhi. Ndugu E anahitaji uongofu kamili. Haitoshi kwa binadamu kuukiri Ukweli. Wanaweza kuukiri Ukweli wote, na bado wasijue chochote - hawana ujuzi wenye utendaji/majaribio katika maisha yao ya kila siku - juu ya ushawishi wa utakaso wa Ukweli juu ya moyo na maisha, au ya nguvu ya utauwa wa Kweli. {2Tsw 638.2}

Ukweli ni mtakatifu na wenye nguvu, na utafanya matengenezo kamili katika mioyo na maisha ya hao ambao wametakaswa nao. Ndugu E ana uwezo wa kutoa ushawishi mzuri. Ikiwa atajitiisha mwenyewe na kunyenyekeza moyo wake mbele za Mungu, anaweza kuwa mbebaji wa Kweli wa nira ya Kristo. Anaweza kuwa msaada badala ya kikwazo kwa familia yake na kwa wengine. Yeye hudhoofisha kusudi la Mungu huko Bordoville, kwa sababu ya kasoro katika tabia yake ya Kikristo. Ikiwa Ndugu E anaishi kulingana na nuru aliyopokea, atafanyia kazi wokovu wake kwa hofu na kutetemeka, na, kwa kufanya hivyo, ataruhusu mwangaza mkali wa Bwana utawaangazia njia wengine na watamtukuza Mungu. Kesi ya Ndugu E inawakilisha ile ya wengine

kanisani ambao wanahitaji kazi ile ile ya mabadiliko katika mioyo yao ili kuwa sawa/sahihi. {2Tsw 639.1}

Ndugu F anaweza kuwa mwenye manufaa zaidi katika maisha yake kuliko alivyo sasa au alivyowahi kuwa. Mungu hajamwita yeye hasa kuhudumu kwa Neno na mafundisho. Hana stahiki kwa nafasi hii, lakini anaweza kufanya shuguli zingine kwa ajili ya Bwana na kuwa msaada katika mikutano. Ikiwa anaishi kwenye nuru mwenyewe anaweza kuakisi/kuonyesha nuru kwa wengine. Yeye anaweza kuwa baraka kwa wengine; anaweza kusema maneno ya faraja na kutia moyo kwa wanadamu waliokata tamaa. Lakini ili kufanya hivyo, anapaswa kuhimiza roho ya matumaini zaidi, roho yenye ucheshi kwake mwenyewe, akikataa kutazama upande wa giza au kuzungumza kutokuamini. Anapaswa kuelezea furaha, matumaini, na ujasiri katika maneno yake na hata kwa sauti yake. {2Tsw 639.2}

Dada G ana udhaifu, lakini hachukuliani na hali yake vyema. Anaruhusu adui kudhibiti akili yake na kujiongezea ugumu kwa roho isiyosalimu amri. Anateseka na udhaifu wa mwili na anapaswa kuhurumiwa; lakini kutotulia, kukasirishwa na mambo madogo-madogo, kulalamika, kunung'unika, na majuto yasiyo na maana hayapunguzi mateso yake au kumletea furaha, bali huongeza ugumu tu. {2Tsw 639.3}

Ulimwengu umejaa roho zisizoridhika ambazo zinapuuza furaha na baraka zinazoweza kupatikana karibu nao, na daima wanaendelea kutafuta furaha na kuridhika ambako hawakutambui. Wao daima wanaangalia mbele na sio walipo, wakijinyumbulisha kwa kuangalia mbali wakiwa na matarajio ya kupata vitu vikubwa zaidi kuliko walivyo navyo sasa, na daima huwa katika hali ya kuvunjika moyo. Wanathamini kutoamini na kukosa shukrani, kwa kuwa wanapuuza baraka zilizo ndani ya njia yao. Baraka za kawaida, za kila siku za maisha hazikaribishwi/hazifurahwi kwao, kama ilivyokuwa Mana kwa wana wa Israeli. {2Tsw 640.1}

Kristo anamwambia Dada G: "Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa, na mizigo ya dhambi Nami nitawapa pumziko. Chukueni nira Yangu, na mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na

mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi. "Maneno, mwenendo, na mfano wa jumla wa Dada G hufundisha somo tofauti kabisa na lile lililofundishwa na Bwana wetu. Dada huyu hupoteza sana kwa kutotilia maanani baraka za sasa anazoweka kuzishika ndani ya uelewa wake na kwa ugumu hutafuta furaha. Jitihada zake ni bure, na utafutaji wake ambao hauna matunda humfanya kutokuwa na furaha mwenyewe na kwa wale wote wanaoshirikiana naye. Kutokutulia kwake, wasiwasi wake, roho yenye shida, vimeonyeshwa katika uso wake na kutupa kivuli. Utusitusi huu, huzuni, kutokuamini, na kutokuridhika kunahamasisha vishawishi vya adui. Kwa kutoamini kwake kila wakati, na kujikopesha shida za kesho, hutoa kivuli badala ya kuakisi miale ya jua. {2Tsw 640.2}

Ndugu G anapaswa kuwa mstahimilivu na mvumilivu, na kumlinda dada G kwa uangalifu kutoka kwa mizigo isiyo ya lazima; kwa kuwa Dada G hayuko tayari kuibeba. Yeye, kwa upande wake, anapaswa kuangalia dhidi ya adui anayekuja, anapaswa kuchukua mzigo wa maisha yake bila manung'uniko na kuibeba kwa furaha, akiyafurahia yote shukrani kwa kwasababu sio mizito. Ndugu G ameelekea kutazama upande wa giza. Anapaswa ajishikilie tayari kufanya mapenzi ya Mungu na kutumia kwa faida nzuri, ushawishi ambao Mungu amempa. Anapaswa kutekeleza kwa uchangamfu majukumu ya leo na sio kukopa shida za kesho ili kumfanya awe mnyonge. Hawezi kutekeleza majukumu ya wiki ijayo, bali kazi na majukumu ambayo siku husika inaleta. {2Tsw 640.3}

Ndugu na Dada G wanapaswa kuunganisha ushawishi wao kwa kusema: "Inatosha kwa siku uovu wake "Ni huzuni kukopa shida za wiki ijayo ili kuudhi wiki ya sasa. Wakati shida halisia zinapokuja, Mungu atamuimarisha, na kumstahilisha kila mpole na mnyonge kuzivumilia. Neema Yake inaporuhusu shida kuja, Yeye Atatoa msaada wa kustahimili. Ukiweka wingu la wasiwasi, kuudhika na kunung'unika na kuitia doa nafsi, basi utafunga nje mwanga wa jua ang'avu kutoka kwa njia ya wengine. {2Tsw 641.1}



Ndugu G angeweza kufuata njia ya kumsaidia Ndugu H na wakati huo huo ajisaidie mwenyewe; lakini ubinafsi ulimnyima Ndugu H faida, na Ndugu G mwenyewe alidharauliwa/hakufaidishwa kwa hofu kwamba angeweza kunufaisha wengine. Ndugu G hajampenda jirani yake kama yeye mwenyewe, na ubinafsi wake mkuu katika mambo mengi umemnyima mema na kumfungia baraka za Mungu. Mwishoni, hakumfaidishi mtu yeyote kwa kuwa mbinafsi; kwa maana Mungu huweka alama wote na atamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake. "Chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." "Yeye apandaye haba atavuna atavuna haba. "{2Tsw 641.2}

Nimetaja watu hawa, kuwakilisha hali halisi ya wengi katika kanisa huko Bordoville ambao kesi zao zinafanana. Watu wengi waliokusanyika mahali pale wameleta mizigo, masumbufu na mashaka juu ya Ndugu D ili awaweke sawa. Kama wangukuwa huru mbali na wivu, na kujiweka katika upendo wa Mungu, wangeweza kuinua mikono yake, kuufariji moyo wake, na kumtuma afanye kazi kwa ajili ya wokovu wa roho, wakati sala zao zingemfuata yeye kama mundu mkali katika shamba la mavuno. Ukosefu wao wa kujitolea na uchaji wa Mungu umedhoofisha imani yao wenyewe, umedhoofisha mikono ya Ndugu D, umeharibu ujasiri wake, na kuifanya kazi yake katika uwanja wa injili kuwa karibu na bure/sifuri. Majaribu kwa kanisa la nyumbani yamelemaza juhudi zake nyumbani na nje ya nchi, na kuacha kazi zake ziwe sehemu moja (mahalia), kwa kiwango kikubwa, kwa eneo lake mahalia. Kufungiwa kwa kazi katika eneo moja kuna athari ya kunyauka kwa maslahi ya kiroho na bidii/ari ya mtumishi wa Kristo. {2Tsw 641.3}

Ili kukua katika neema na katika ujuzi wa Ukweli, watendakazi lazima wawe na uzoefu anuwai. Hii itapatikana vizuri katika kupanua kazi katika uwanja mpya, katika maeneo tofauti, ambapo wataingia na kukutana na tabaka zote za watu na aina zote za akili, na mahali ambapo kazi anuwai itakuwa inahitajika ili kukidhi matakwa ya akili nyingi na anuwai. Hii itampeleka mfanyakazi wa Kweli kwa Mungu na Biblia kwa ajili ya nuru, nguvu, na maarifa, ili aweze kuhitimu kikamilifu kukidhi matakwa ya watu. Anapaswa kuzingatia mawaidha aliyopewa Timotheo: "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu,

mtendakazi ambaye hahitaji aibu, akigawanya Neno la Ukweli." "Ni nani basi aliye wakili mwaminifu na mwenye busara, ambaye bwana wake atamweka msimamizi juu ya nyumba yake, na kuwapa sehemu yao ya chakula kwa malipo "Hekima inahitajika kutambua mada inayofaa zaidi kwa tukio hilo. {2Tsw 642.1}

Ndugu D hajaendelea kukua, na kuwa mtendakazi aliyefanikiwa. Amekuwa mbilikimo. Akili yake imepungua, na nguvu zake za kiroho zimekuwa zikipungua. Anapaswa sasa kuwa mfanyakazi aliyefanikiwa, mtendakazi aliye kamili. Badala ya kujitolea kabisa kwa kazi hiyo, amekuwa akihudumia meza (Matendo 6:2 kufanya kazi chache, za kawaida, wakati angeweza kutumika kwa ufanisi zaidi katika injili na maombi). Paulo alimhimiza Timotheo: "Uwe mfano wa waaminio, katika maneno, na katika mazungumzo, na katika upendo, na katika roho, katika imani, na katika usafi. Mpaka nitakapokuja, jihudhurisha kusoma, kutii, na mafundisho. Usidharau karama iliyo ndani yako, uliyopewa kwa unabii, na kuwekewa na Bwana mikono ya uwakili. Tafakari juu ya mambo haya; jitoe kabisa kwayo; ili faida yako ipate kuonekana kwa wote. Jihadhari mwenyewe na mafundisho; endelea kwayo: kwa kufanya hivi wewe utajiokoa mwenyewe na wale wanaokusikia. "{2Tsw 642.2}

Ndugu D ni mtendaji mwenye bidii na yuko tayari kufanya mambo, yuko tayari kubeba mizigo ambayo haijaunganishwa na wito wake; na anayo akili ambayo kwa muda imeshugulishwa sana na vitu vya kidunia. Watumishi/wachungaji wengine hudumisha hadhi fulani sio kulingana na maisha ya Kristo, na hawataki kuwa watumishi na kujihusisha na kazi ya mikono, kama inavyoweza kuhitajika, kupunguza mzigo wa wale ambao ni wenyeji wao, wanaposhiriki ukarimu wao, na kuwapunguzia masumbufu. Mazoezi ya mwili yangethibitisha baraka kwao, badala ya majeraha. Katika kusaidia wengine na wao wangepaidika. Lakini wengine huenda kwa kupitiliza upande mwingine. Wakati nguvu zao zote zinahitajika katika kazi ya Mungu, wanakuwa wako tayari kushiriki katika kazi na kuwa watumishi wa wote, hata katika vitu vya muda; na hakika humwibia Mungu huduma anayotaka kwao. Kwa hivyo mambo yasiyo na maana huchukua muda wa

thamani ambao unapaswa kutolewa kwa masilahi ya kazi ya Mungu. {2Tsw 643.1}

Ndugu J. N. Andrews amepotoka hapa. Muda na nguvu ambazo amejitolea kwa mawasiliano na ndugu zake, kujibu barua zao binafsi zenye maswali, alipaswa kuuweka kwenye maslahi maalumu ya kazi ya Mungu kwa ujumla. Lakini ni watu wachache wanaotambua majukumu yaliyo juu ya watumishi wachache wanaobeba mizigo katika kazi hii. Ndugu huwaita mara kwa mara watu hawa kutoka kazini ili kushughulikia maswala yao madogo-madogo, au kusuluhisha kesi ya kanisa, ambavyo wanaweza na wanapaswa kushughulikia wenyewe."

"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yoyote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, likapeperushwa huku na huko." " Lazima awe na bidii na mstahimilivu. Ikiwa hana msimamo, na anayumba-yumba, ni mwenye mashaka daima kwamba Bwana atafanya kama alivyoahidi, basi hatapokea chochote. {2Tsw 643.2}

Wengi hutazamia wachungaji wao kuwaletea nuru kutoka kwa Mungu, wakionekana kufikiria hii ni njia rahisi kuliko kujipa shida ya kwenda kwa Mungu moja kwa moja kwa ajili yao wenyewe. Hao hupoteza sana. Ikiwa wangemfuata kila siku Kristo na kumfanya kuwa kiongozi na mshauri wao, wangeweza kupata ufahamu bora wa mapenzi Yake, na hivyo kupata uzoefu wa thamani. Kwa kukosa uzoefu huu, ndugu hawa wanaokiri Kweli wanaota mioto ambayo wengine wamewasha; hawamjui Roho wa Mungu na hawana ujuzi wa Mapenzi yake, na kwa hivyo huhamishwa kwa urahisi kutoka kwa imani yao. Hawana msimamo, kwa sababu waliamini wengine kupata uzoefu kwa niaba yao. Mpango/majaliwa bora na toshelevu umewekwa kwa kila kwa kila mwana na binti ya Adamu kupata kujua wao binafsi mapenzi ya Mungu, kuikamilisha tabia ya Kikristo na kutakaswa kupitia Ukweli. Mungu huvunjiwa heshima na tabaka hilo la watu, ambalo linadai kuwa wafuasi wa Kristo na bado hawana ujuzi wa majaribio wa mapenzi ya Mungu au siri ya utauwa. {2Tsw 644.1}

Ndugu D amekuwa na masumbufu mengi ya kazi za nyumbani. Ongezeko la idadi ya watu kanisani halijapunguza mizigo yake.

Ongezeko la idadi katika familia yake limekuwa jukumu zito sana kwake na familia yake, na mambo haya yamekuwa kikwazo cha kumfanya mtendakazi asiye na mafanikio. Amekula kutu katika kazi ya Mungu na anahitaji kuchomwa ili kutu itoke. Ushuhuda wake unahitaji kupewa nguvu na Roho na nguvu ya Mungu. Ndugu zake huko Bordoville, ambao hawana kazi maalum ya kufanya katika kufanya kazi kwa Neno na Mafundisho, wanapaswa kuwa macho ili kuona pale ambapo wengine wanahitaji msaada, na wanapaswa kuwasaidia. Wengi hufumbia macho mema ambayo wana fursa kufanya kwa wengine mema, na kwa kupuuzia hilo wanapoteza mibaraka **ambayo wangeweza kuipata. Ndugu D ameachwa kubeba mizigo ambayo ndugu zake wangeihesabu kuwa ni wajibu na upendeleo kwao kuibeba. Kazi yetu katika** ulimwengu huu ni kuishi kwa faida ya wengine, kubariki wengine, kuwa wakarimu; na mara kwa mara inaweza kuwa kwa usumbufu tu, kwamba tunaweza kuwaburudisha wale ambao wanahitaji sana utunzaji wetu na faida ya jamii yetu na majumba yetu. Wengine huepuka mizigo hii ya lazima. Lakini mtu fulani ni lazima aibebe; na kwa sababu ndugu kwa ujumla hawapendi kukaribisha wageni, na hawashiriki kwa usawa katika majukumu haya ya Kikristo, wale wachache ambao wana mioyo iliyo tayari, na ambao kwa furaha hufanya kesi za wale ambao wanahitaji msaada kuwa yao wenyewe, hutingwa na mizigo. Kanisa linapaswa kuchukua utunzaji maalumu ili kuwapunguzia wahudumu wake mizigo ya ziada **katika mwelekeo huu. Watumishi/wachungaji ambao wanajishughulisha kikamilifu na kazi ya Mungu, wakifanya kazi kwa bidii kwa wokovu wa roho, wana dhabihu (kujitolea) za daima za kufanya. {2Tsw 645.1}**

Ushuhuda wa Ndugu D unahitaji kuimarishwa na neema ya Mungu. Anahitaji upako mpya, ili kwamba aweza kuwa na uwezo wa kuelewa ukubwa wa kazi na kujitolea nafsi yake yote kwa kuendeleza kazi ya Mungu. Bwana ana kazi ya kutosha hata kuajiri wafuasi Wake wote. Wote wanaweza kuonyesha utukufu Wake ikiwa wataifanya. Lakini wengi wanakataa kufanya hivyo. Wanakiri imani, lakini hawana matendo. Imani yao imekufa, kwa kuwa wenyewe. Wanaepuka majukumu na mizigo, na watalipwa kama kazi zao zilivyokuwa. Kwa sababu wengine hawakuinua mizigo ambayo wangeweza kuiinua, au kufanya kazi ambayo wangeweza kuifanya, kazi hiyo ni nzito zaidi kwa

wachache watakojijhusisha nayo. Wanaona mengi ya kufanya, nao hufanya kazi zinazozidi nguvu zao, nao huchakaa haraka. {2Tsw 645.2}

Wakati huu Mungu huita watendakazi ambao shauku/maslahi yao yanajihusisha kabisa na kazi Yake na kusudi Lake. Wahudumu/wachungaji wanaoshiriki katika kazi hii lazima wahuishwe na nguvu, roho na uwezo wa Kweli wanazozihubiri, na ndipo watakuwa na mvuto. Kwa nadra sana watu watanyanyuka juu kuliko wachungaji wao. Roho ya kupenda ulimwengu ndani yake ina nguvu kubwa kushawishi wengine. Watu hutumia mapungufu yake kuwa udhuru wa kufunika roho yao ya kupenda ulimwengu. Wao hunyamazisha dhamiri zao, wakidhani wanaweza kuwa huru kupenda mambo ya maisha haya na kuwa wasiojali mambo ya kiroho, kwa sababu wachungaji wao wako hivyo. Wanadanganya nafsi zao na kubaki katika urafiki na ulimwengu, ambao mtume anatangaza kuwa ni uadui na Mungu. {2Tsw 645.3}

Wachungaji/watumishi wanapaswa kuwa mifano kwa kundi. Wanapaswa kuonyesha upendo usiokufa, kwa roho ya kujitolea sawa na ile wanayotamanikuiona kwa watu katika kusudi la kazi ya Mungu. Watumishi huko Vermont wamefanya makosa katika kazi yao. Wamepita juu ya uwanja huo tena na tena kusaidia makanisa, wakati mara kwa mara walihitaji kazi ifanywe kwao wenyewe, kuwaleta katika nafasi ambapo Mungu angeweza kubariki kazi zao na kuwafanya wazae matunda. Hakukuwa na hata mmoja aliyekuwa na ufanisi katika kusudi huko Vermont, aliyekuwa na sifa kamilifu katika kuendeleza sehemu zote za kazi, huko Vermont. {2Tsw 646.1}

Ndugu na Dada I ni wagonjwa/dhaifu/vilema. Mungu hakuwawekea majukumu mazito sana juu yao. Wanahitaji kuangalia kwa ukaribu, ili wasije wakupunguza ushawishi wao. Hawana watoto wao wenyewe wa kuwapa uzoefu wa utunzaji na upendo wa mzazi, na wako katika hatari ya kuwa finyu, wabinafsi, na wenye nadharia za mtazamo na hisia zao. Vitu hivi vyote vina ushawishi mbaya juu ya kusudi la Mungu. Wanapaswa kufanya kazi kwa kuweka akili zao zisijiinue juu yao wenyewe na hawapaswi kujifanya kigezo kwa wengine. Wale ambao hawana watoto wa kushiriki mawazo na kazi zao, wanahitaji zoezi hilo

ili kupata ustahimilivu, uvumilivu, na upendo, wanapaswa kujilinda, wasije wakafanya mawazo yao na kazi yao kuwa kiini juu yao wenyewe. Hawana sifa ya kufundisha wazazi juu ya mafunzo ya watoto wao, kwani wao hawajapata uzoefu katika kazi hii. Walakini katika hali nyingi wale ambao hawana watoto ndio walio tayari zaidi kuwafundisha wale ambao wana watoto, wakati ambapo wale wasio na watoto, katika mambo mengi wao hujifanya kuwa kama watoto. Hawawezi kutolewa nje ya msimamo fulani, na uvumilivu unahitajika zaidi kwao kuliko kwa watoto. Ni ubinafsi kuwa na sababu fulani iliyowekwa alama na kufuata sababu hii kwa kusumbua wengine. {2Tsw 646.2}

Ni vitu vidogo ambavyo huijaribu tabia. Ni matendo yasiyo bandia/feki ya kujikana nafsi kila siku, kwa ucheshi na upole ndiyo ambayo Mungu hutabasamu juu yake. Hatupaswi kuishi kwa ajili yetu wenyewe, bali kwa ajili ya wengine. Sisi tunapaswa kuwa baraka kwa kujisahau kwetu na kuwaza wengine. Tunapaswa kuthamini upendo, uvumilivu, na ujasiri. {2Tsw 647.1}

Ni wachache sana wanaotambua faida za utunzaji, uwajibikaji, na uzoefu ambao watoto huleta kwa familia. Wengi wana familia kubwa zinazokua bila nidhamu; wazazi wanapuuza amana yenye thamani na jukumu takatifu, ambalo ikiwa lingefanywa kwa uaminifu kwa kumcha Mungu, lingetoa faida, sio tu kwa Watoto wao, bali hata kwao wenyewe, ustahili wa ufalme wa mbinguni. Lakini nyumba isiyo na watoto ni mahali pa ukiwa. Mioyo ya wakazi iko katika hatari ya kuwa na ubinafsi, ya kupenda starehe kwaajili yao mtelekemko kwao wenyewe, na kushauriana na matamania yao, na furaha zao tu. Wanajikusanyia huruma kwao wenyewe, lakini wana huruma chache sana za kuwapa wengine. Utunzaji na mapenzi kwa Watoto ambao bado ni tegemezi, unatoa mikwaruzo ya asili kutoka kwetu, hutufanya kuwa wenye upendo mwanana, kujali na wenye huruma nyororo, na ina ushawishi wa kukuza mambo bora ya tabia yetu. Wengi ni wagonjwa kimwili, kiakili, na kimaadili, kwa sababu umakini wao karibu wote umegeuzwa kwao peke yao. Wanaweza kuokolewa kutoka katika kudumaa kwa uhai mdogo wa afya na nguvu za vijana na akili anuwai isiyopumzika ya watoto. {2Tsw 647.2}

Ndugu J ni mzee. Hakuna jukumu zito ambalo linapaswa kuwa juu yake sasa. Amemchukiza Mungu katika matumizi yake mabaya ya upendo kwa watoto wake. Amekuwa na wasiwasi mwingi sana katika kuwasaidia kwa upekee ili asiwaudhi. Badala ya kuwafurahisha, amewajeruhi. Sio wenye busara na waaminifu katika usimamizi wa njia zao, hata kwa mtazamo wa ulimwengu. Wakitazamwa katika mtazamo wa kidini, wamekuwa pungufu sana. Hawana ufahamu wa kuona haya kuhusu mambo ya kidini. Hawaipambi jamii kwa nafasi na ushawishi wao ulimwenguni, wala hawalipambi kusudi la Mungu kwa maadili safi ya Kikristo na matendo mema katika utumishi wa Kristo. Hawajafundishwa tabia ya kujikana na kujitegemea kama kinga yao maishani. Hapa kuna dhambi kubwa inayokaa juu ya wazazi. hawawaadabishi watoto wao na kuwalea kwa Mungu. Hawawafundishi kuwa na serikali ya kujitawala vyema, uimara wa tabia, na umuhimu wa kuazimia, na kuelekeza nia kuzuri. Watoto wengi katika umri huu, wameachwa kujikuza wenyewe katika tabia hizo. Hawafundishwi umuhimu wa kukuza na kupalilia mwili na akili kwa makusudi mazuri, ili kubariki jamii kwa ushawishi wao, kuwa wenye kustahili vizuri kupamba maisha ya Kikristo, na kukamilisha utakatifu katika hofu na uchaji wa Mungu. {2Tsw 647.3}

Ndugu J amekosea kukabidhi mali zake kwa watoto wake. Amewapa majukumu ambayo hawakuwa na sifa ya kuyabeba. Aliweka mali zake nje ya udhibiti wake na amekusanya mali kwa ndugu zake kwa kazi yake dhaifu. Mungu hajatukuzwa kwa njia ambayo ameichukua kuhusiana na mali yake. Ametoa udhuru kwa mwenendo mbaya inayofuatwa na watoto wake, ambayo haiendi na imani yetu au kiwango cha Biblia. Amesema kwa waovu, itakuwa heri kwako wewe; Wakati Mungu ametangaza wazi kuwa itakuwa mbaya kwake. {2Tsw 648.1}

Makosa haya kwa Ndugu J yanaonyesha ukosefu mkubwa wa hekima ya mbinguni na, kwa kiwango kikubwa, inamwondolea sifa ya kazi nzito iliyo juu ya mtumishi mwaminifu wa Kristo. Ni kitu gani Ndugu J anaweza kusihi mbele za Mungu wakati Bwana atamwomba atoe hesabu ya uwakili wake? Ameongozwa na akili zisizowekwa wakfu za watoto wake, na hahisi umuhimu wa kutafuta ushauri na mawaidha

kutoka kwa watumishi wa Mungu ambao walikuwa wamesimama kwenye nuru. Ameongozwa na huruma potovu na ameshindwa katika hukumu. Amekuwa akisogea kama mtu kipofu. Njia yake imemjeruhi mwenyewe na kusudi la Mungu. {2Tsw 648.2}

Sio wahubiri tu, wa kwenda kati ya makanisa kuomba na kuhimiza mara kwa mara ndiyo ambavyo Vermont inahitaji. Kilio cha kupata watendakazi kinaweza kuletwa mfululizo kati ya watu wa Mungu huko Vermont. Ila ni watenda kazi wenye bidii na ari ndiyo wanaohitajika ili kuimarisha vitu ambavyo vinasalia kwa kuhudumia mahitaji ya kiroho ya watu. Kusudi la Mungu kila mahali, haswa huko Vermont, linahitaji wabeba/wachukuaji mizigo. Watu huenda tena na tena katika uwanja huo huo mmoja, lakini hufanya kidogo sana, ikiwa kuna chochote. Wanatalii vizuri kwa ndugu zao (ziara), na hili mara kwa mara ndilo tu linatimizwa; na bado wanatarajia kulipwa kwa wakati wao. {2Tsw 649.1}

Kesi ya Ndugu na Dada K inakuja mbele yangu ninapoandika. Hawajafanya mazoezi ya kutunza na kujali wengine. Hawajahisi jukumu lililopo juu yao kama wachukuaji wa mizigo. Ndugu K alionyeshwa kwangu kati miongoni mwa wengine ambao wamejihisi kuwa walikuwa na kazi ya kufanya kwa ajili ya Bwana. Hakika anayo, ndivyo ilivyo wengine wengi pia, ikiwa wataifanya. Kuna watendakazi wafanyao kazi kikamilifu katika kazi ya Mungu, ambao wana uzoefu katika kazi na ambao wanajitolea wakati na nguvu zao kwa huduma ya Mungu. Hawa wanapaswa kusaidiwa kwa ukarimu. Lakini wale ambao wanaanza kutembelea makanisa hapa na pale, haswa wale ambao hawana familia za kusaidiana ambao wana uwezo wao wenyewe -- hawapaswi kuchota kutoka katika hazina ya Bwana. {2Tsw 649.2}

Ndugu J na Dada K hawana uzoefu wa kujitoa mhanga kwa ajili ya Ukweli, hawana utajiri wa matendo mema, hawajiwekei hazina zao mbinguni. Huruma yao, kujali kwao, na uvumilivu wao havijaitwa katika zoezi la kulea Watoto wanaowategemea na kuwapenda. Wamejishugulisha na mashauri yao binafsi, yahusuyo raha zao. Mioyo yao haikuwa chemchemi hai inayo peleka mikondo hai ya huruma nyororo, kujali na upendo. Katika kuwabariki wengine kwa maneno



mazuri ya upendo na matendo ya huruma na ukarimu, wangelitambua na kujipatia baraka kwao wenyewe. Wamekuwa finyu sana katika duara la ufanisi wa manufaa kwa wengine. Isipokuwa hapo watakapobadilishwa katika akili, na kufanywa upya kwa Roho ya Kristo, hawawezi kuwa wafanyakazi kamili, wenye ufanisi katika kusudi la Mkombozi. Maisha Yake ni mfano kwa Wakristo. Kujitolea nafsi na ukarimu usio na ubinafsi vinapaswa kuwa tabia ya maisha yao. Masilahi binafsi yamekuwa na kipaumbele sana. Ah, ni kwa udogo kiasi gani Ndugu K anafahamu ni nini maana ya kufanya kazi ya Mungu, kuinua msalaba wa Kristo na kutembea katika nyayo za Mkombozi aliyejikana Mwenyewe! {2Tsw 649.3}

Mtumishi wa Kristo, mwalimu wa Kweli, mchungaji wa Kweli, kwa maana moja ni mtumishi wa wote, akiangalia mahitaji ya wale wanaohitaji msaada, na kujua jinsi ya kutumika hapa na pale katika kazi kubwa ya kuokoa roho. Mtu anayedai kufundisha Kweli, na huenda tu mahali anapopapenda, na hufanya kazi wakati na jinsi apendavyo, na bado anaepuka majukumu, haubebi msalaba wa Kristo, wala hautimizi utume wa mhudumu wa injili. Ni wachache wanajua kwa uzoefu nini maana ya kuteseka kwa ajili ya Kristo. Wanatamani kuwa kama Kristo, lakini wanatamani kuepuka umaskini na msalaba/mateso. Wangefurahi kuwa pamoja na Kristo katika utukufu, lakini hawapendi kuja Kwake kwa kupitia kujikana nafsi na mateso. {2Tsw 650.1}

Haikumgharimu Ndugu K kutafuta Ukweli; kwa maana wateule wa Mungu wameandaa hoja mikononi mwake, zilizo safi, wazi, na za kusadikisha. Hoja ngumu za Ukweli wa sasa zimefikiwa kwa juhudi na bidii za wachache ambao walikuwa wamejitolea kwa kazi hiyo. Kufunga na kuomba kwa bidii kwa Mungu kulimchochea Bwana kufungua hazina Zake za Ukweli katika uelewa wao. Ilibidi wakabiliane na wapinzani wenye ujanja na MaGoliati wanaojisifu, wakati mwingine ana kwa ana, lakini mara nyingi zaidi kwa kutumia kalamu. Shetani amewahimiza watu kufanya upinzani mkali, kupofusha macho na kuweka giza ufahamu wa watu. Wachache ambao walikuwa na shauku na kusudi na Ukweli wa Mungu moyoni waliamshwa kwa utetezi wake. Hawakutafuta raha, lakini walikuwa tayari kujitosa hata kwa kupoteza maisha yao kwa ajili ya Ukweli. {2Tsw 650.2}

Hawa watafutao Kweli wenye bidii na dhati, walihatarisha mtaji wa nguvu zao na vyote walivyokuwa navyo katika kazi ya kutetea ukweli na kueneza nuru. Kiungo baada ya kiungo cha mnyororo wa Kweli kimekuwa kikitafutwa, hadi kisimame kwa upatanifu mzuri, kikiungana katika mnyororo kamili. Hawa wanaume/watu wenye akili za uchunguzi wameleta hoja na kuzifanya ziwe wazi sana, kiasi kwamba mtoto wa shule anaweza kuelewa. Ni rahisi kiasi gani sasa kwa watu kuwa waalimu wa kufundisha Kweli, wakati wanaepuka kujitoa na kujikana nafsi. {2Tsw 651.1}

Watafutaji hawa wa Ukweli wameteseka kwa ajili a hiyo na wanajua inagharimu kiasi gani. Wanaithamini na wanahisi shauku kubwa zaidi katika muendelezo wake. Kujikana-nafsi na kuubeba msalaba vipo pamoja katika kila njia ya mfuasi wa Kristo. Msalaba ni kile kinachopinga upendo wetu wa asili na nia yetu. Ikiwa moyo haukutakaswa kabisa kwa Mungu, ikiwa upendo na matakwa na mawazo hayatawekwa chini ya mapenzi ya Bwana Mungu, kutakuwa na kushindwa kutekeleza kanuni za dini ya Kweli na kushindwa kuwa mfano wa maisha ya Kristo. Hakutakuwa na hamu ya Kweli ya kutupilia mbali anasa na kujipenda wenyewe, na matendo ya mwili hayatasulubiwa ili kufanya kazi za Kristo. {2Tsw 651.2}

Kuna kazi ya kukamilishwa kwa wengi wanaoishi Bordoville. Niliona kwamba adui alikuwa anashugulika kazini kubeba ajenda zake. Wanaume ambao Mungu amewapa talanta ya mali wamehamishia jukumu hilo kwa watoto wao, jukumu ambalo Mbingu imewateua wao kuwa mawakili wa Mungu. Badala ya kumrudisia Mungu vitu ambavyo ni Vyake, wanadai kwamba kila kitu walicho nacho ni chao, kana kwamba ni kwa nguvu zao wenyewe na kwa hekima zao wamezipata hizi mali. Je, ni nani mbaye aliwapa nguvu na hekima kwa kupata hazina ya kidunia? Ni nani aliyenyweshea mashamba yao kwa umande wa mbinguni na kwa manyunyuyu ya mvua? Ni nani mbaye aliwapa jua ili kupasha joto dunia na kuamsha maisha ya vitu vya asili, na kusababisha kushamiri kwa faida ya mwanadamu? Wanaume ambao Mungu amewabariki kwa fadhila Zake, hukunja mikononi mwao hazina ya kidunia na hufanya fadhila na baraka hizi ambazo Mungu kwa

neema Yake amewapa kwa ukarimu, kuwa laana ya kujaza mioyo yao kwa ubinafsi na kutomwamini Yeye. Wanakubali kupokea mema/mazuri kutoka kwa Mungu, lakini bado wanadai kwamba ni vyao/zao wenyewe, wakisahau kwamba Mwalimu ana madai juu yao, na wanakataa hata kutoa riba anayodai. Utajiri husababisha wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo kuwa na wasiwasi na kuwachoma kwa huzuni nyingi kwa sababu wanamsahau Mungu, na wanapenda kuabudu fedha. Wanaruhusu hazina za kidunia kuwafanya wawe na hasira kama vile wameonewa na hili linawazuia kukamilisha tabia ya Kikristo. Na, kana kwamba hii haitoshi, wanasambaza kwa watoto wao mali, ili kuwalaani, kile ambacho kimethibitisha chanzo cha uharibifu wa maisha yao wenyewe. Mungu amewakabidhi wanadamu mali ili kuwathibitisha, kuona ikiwa wako tayari kukiri kwamba hizi ni karama Zake, na kuzitumia kukuza utukufu wa Bwana juu ya dunia. {2Tsw 651.3}

Dunia ni mali ya Bwana, na hazina zote zilizomo. Mifugo juu ya elfu za milima ni Yake. Dhahabu na fedha vyote ni mali Yake Bwana. Amekabidhi hazina Zake kwa mawakili, ili na wao wapate kuendeleza hoja Yake na kulitukuza Jina Lake. Yeye Hakukabidhi hazina hizi kwa wanadamu ambao wangezitumia wao kujiinua na kujitukuza, na kuwa na nguvu ya kuwakandamiza wale ambao walikuwa masikini katika hazina za ulimwengu huu. Mungu hapokei matoleo ya yeyote kwa sababu ni mhitaji na kwamba hawezi kuwa na utukufu na utajiri bila ya wao, lakini ni kwa sababu ya masilahi ya waja Wake, kumlipa Mungu vitu ambavyo ni Vyake. Sadaka za hiari za mnyenyekevu, aliye na moyo uliopondeka Bwana atazipokea, na atamlipa mtoaji kwa wingi wa utajiri wa baraka Zake. Anavipokea kama dhabihu ya utii wa shukrani. Anahitaji na anakubali dhahabu na fedha zetu kama uthibitisho kwamba yote tuliyo nayo ni mali Yake. Yeye Anadai na anakubali uboreshaji wa wakati wetu na talanta zetu kama tunda la upendo Wake uliopo mioyoni mwetu. Kwani utii ni bora kuliko dhabihu. Bila ya upendo ulio safi, sadaka za gharama kubwa zaidi ni masikini/hafifu sana kwa Mungu kuzikubali. {2Tsw 652.1}

Wengi wameweka mioyo yao kwenye hazina za kidunia kiasi kwamba hawatambui faida ya kujiwekea hazina mbinguni. Hawatambui kuwa

sadaka zao za hiari hazimtajirishi Mungu, bali wao wenyewe. Kristo anatushauri tuweke hazina zetu mbinguni. Je, ni kwaajili ya nani? Ni ili Mungu, apate kutajirika? La, hashia! Hazina za ulimwengu wote ni Zake, na utukufu usioweza kuelezewa wa hazina za thamani za mbinguni ni Zake Yeye mwenyewe, kumpa amtakaye. Jiwekeeni akiba katika hazina ya mbinguni. "Wanaume ambao Mungu amewafanya mawakili wanadanganywa sana na utajiri wa ulimwengu huu na hawatambui kwamba kwa ubinafsi wao na tamaa yao, sio tu wanamwibia Bwana katika zaka na sadaka, lakini wanajiibia wenyewe utajiri wa milele. Wanaweza kuongeza kila siku hazina yao ya mbinguni kwa kufanya kazi ambayo Bwana amewaachia waifanye, na wakitumia mali aliyowakabidhi. Mwalimu angewataka watazame fursa za kufanya mema na wakati wanapoishi, watumie mali zao wenyewe kusaidia katika wokovu wa wenzao na katika maendeleo ya makusudi Yake katika matawi yake mbali mbali. Kwa kufanya hivyo wanafanya tu kile ambacho Mungu anataka wakifanye; humtolea Mungu yaliyo Yake. Wengi kwa hiari hufunga macho na mioyo yao, ili wasije kuona na kuhisi mahitaji ya kusudi la Bwana, na kwa kusaidia katika maendeleo yake wapunguze riba au mtaji. Wengine wanahisi kwamba kile wanachotoa kuendeleza kusudi la Mungu hakika kimepotea. Wanafikiria kuwa pesa nyingi zimekwenda na wanahisi kutoridhika isipokuwa wanaweza kurudisha hazina yao pale walipotoa haraka ili mali yao ya kidunia isipunguke. Wanatumia uzoefu wa ubahili, uchoyo na hata ukali katika biashara na ndugu zao na walimwengu pia. Hawasiti kudhulumu kwenye dili (uchuuzi) ili wapate kupata kupita kiasi ili kujinufaisha wenyewe na kupata visenti vichache. {2Tsw 653.1}

Wengine, wakiogopa kuwa watapoteza hazina ya kidunia, wanapuuza maombi na kujikusanya kwa pamoja kwa ajili ya kumwabudu Mungu, ili wapate muda zaidi wa kujitolea kwenye mashamba yao au biashara zao. Wanaonyesha kwa matendo yao kuwa ni katika ulimwengu gani wameweka matarajio ya juu zaidi. Wanatoa kafara ya fursa kidini, ambayo ni muhimu kwa maendeleo yao ya kiroho, kwa mambo ya maisha haya na kushindwa kupata ujuzi wa mapenzi ya Mungu. Wanakosa kukamilisha tabia ya Kikristo na hawakifikii kipimo cha Mungu. Wanafanya masilahi yao ya muda ya kidunia kuwa ya kwanza, na kumwibia Mungu wakati ambao wangepaswa kutumia kwa huduma

Yake. Watu kama hao Mungu huwawekea alama, na watapokea laana badala ya baraka. Wengine huweka mali zao nje ya usimamizi wao kwa kuiweka mikononi mwao watoto. Nia yao ya siri ni kujiweka katika nafasi ambayo hawatahisi kuwajibika kutoa mali zao kueneza Ukweli. Hawa wanapenda kwa maneno, lakini sio kwa matendo na kwa Kweli. Hawatambui kuwa ni pesa za Bwana wanazoshughulikia, na wala sio zao. {2Tsw 654.1}

Wengi wangependa kuona roho zikiongoka na kubadilika ikiwa ingefanywa bila ya gharama/kujitoa kwao; lakini ikiwa mali zao zinaguswa, wanarudi nyuma, kwani ni za thamani zaidi kwao kuliko roho za wanaume na wanawake ambao Kristo alikufa kwa ajili yao. Ikiwa wale ambao Mungu amewapa dhamana ya mali na wameelewa majukumu yao kama mawakili Wake, wangebakisha mikononi mwao wenyewe ile mali ambayo Mungu amewakopesha, ili waweze kutekeleza kwa uaminifu wajibu ambao wamepewa kufanya sehemu yao katika kusaidia kuiendeleza kazi ya Mungu. Ikiwa wote wangeweza kuelewa mpango wa wokovu, na thamani ya hata nafsi moja [mtu mmoja] iliyonunuliwa kwa damu ya Kristo, wangefanya maslahi mengine yoyote kuwa ya matokeo madogo. {2Tsw 654.2}

Wazazi wanapaswa kuwa na hofu kubwa katika kuwakabidhi watoto talanta za mali ambazo Mungu ameweka mikononi mwao, isipokuwa tu wana ushahidi wenye uhakika kwamba watoto wao wanapendezwa zaidi na maslahi ya kazi ya Mungu, wanapenda, na kujitolea kwa, kusudi la Mungu kuliko wao wenyewe, na kwamba watoto hawa watakuwa wenye ari zaidi na bidii katika kupeleka mbele kazi ya Mungu katika taasisi/shuguli mbalimbali ambazo zinahitaji mali kuziendeleza. Lakini wengi wanaweka mamlaka/mali/uwezo wao mikononi mwa watoto wao, na hivyo kuwatupia jukumu lao la uwakili wao wenyewe watoto, kwa sababu Shetani huwahimiza kufanya hivyo. Kwa kufanya hivyo wanaweka mali hiyo katika safu ya adui kwa ufanisi. Shetani anafanyia kazi jambo hili kuhudumia kusudi lake mwenyewe na anazuia kwa kusudi la Mungu mali ambayo anahitaji, ili kwamba kazi iweze kudumishwa. Jitihada zilizofanywa kutoa ukweli mbele ya watu hazifikii nusu au upana kamili kama zinavyopaswa kuwa. Sio sehemu ya hamsini inayofanyika sasa kupanua Ukweli kwamba inaweza

kufanywa kwa kutawanya machapisho na kuleta sauti ya Ukweli kwa wote ambao wanaweza kuwa kishawishi kwa kuja. {2Tsw 655.1}

Mlango wa rehema wa wengi unafungwa. Shetani kila siku anakusanya mavuno yake ya roho. Baadhi wanafanya maamuzi ya mwisho dhidi ya Ukweli, na wengi wanakufa bila kuwa na uelewa. Akili zao hazijaangazwa kwa nuru, na dhambi zao hazijatubiwa; na bado watu wanaodai kuwa watauwa wanajilimbikizia hazina za kidunia na kuelekeza juhudi zao kupata zaidi. Hawajali hali ya wanaume na wanawake ambao huja katika uwanja wa ushawishi wao na ambao wanaangamia kwa kukosa maarifa. Kazi iliyoelekezwa vizuri, iliyovikwa upendo na unyenyekevu, itafanya mengi kuelimisha na kuwaongoa binadamu wenzao; lakini mfano wa wengi ambao wanaweza kufanya mema mazuri unasema: Roho yako haina thamani kwangu kuliko masilahi yangu ya kidunia. {2Tsw 655.2}

Wengi wanapenda Ukweli kidogo, lakini wanaupenda ulimwengu huu zaidi. "Mtawajua kwa matunda yao." Mambo ya kiroho hutolewa dhabihu kwa vitu vya muda mfupi. Matunda ambayo wanabeba sio kwa utakatifu, na mfano wao hautakuwa wa usadikisho na kuwaongoa wale wenye dhambi kutoka kwa makosa ya njia zao na kwenda kwenye Ukweli. Wanaruhusu watu/roho kwenda kwenye uharibifu, wakati wanaweza kuwaokoa ikiwa wangepanya bidii za dhati kwa niaba yao, kama walivyofanya kupata hazina za maisha haya. Ili kupata zaidi vitu vya ulimwengu, ambavyo havihitajiki sana na ambavyo vinaongeza tu majukumu yao na hukumu, wengi hufanya kazi nyingi chini ya mpango wenye shinikizo kubwa, na kuhatarisha afya na furaha ya kiroho, na amani, faraja, na furaha ya familia zao. Wanaacha roho ziende kwenye uharibifu miongoni mwao kwa sababu wana hofu kwamba muda wao mdogo na mali zitahitajika kuokoa roho. Pesa ni muungu yao. Wameamua kwamba haitalipa kutoa mhanga mali zao katika kuongoa roho. {2Tsw 656.1}

Yule ambaye amekabidhiwa talanta moja hatawajibika kwa talanta tano, au kwa mbili, lakini kwa talanta moja. Wengi wamepuuza kujiwekea hazina mbinguni kwa kufanya mema na mali ambazo Mungu amewaazima. Hawamwamini Mungu na wana maelfu ya hofu kuhusu

siku zijazo. Kama wana wa Israeli, wana mioyo miovu ya kutoamini. Mungu aliwapatia watu hawa mahitaji yao kwa wingi, kadiri ilivyohitajika; lakini waliazima taabu kwa siku zijazo. Walilalamika na kunung'unika katika safari yao ambayo Musa alikuwa nao kuwaongoza kwamba alikuwa na mpango wa kuwaua na watoto wao kwa njaa. Mahitaji ya kufikirika yalifunga macho na mioyo yao katika kuona wema na rehema za Mungu katika safari yao, na hawakuwa na shukrani kwa fadhila Zake zote. Ndivyo ilivyo pia kwa watu wasioamini, wanaodai kuwa watu wa Mungu katika zama hizi za wasioamini za upotovu. Wanaogopa kuwa watakuja kuwa na upungufu/dhiki na mahitaji, au watoto wao watakuwa wahitaji, au kwamba wajukuu wao watakuwa fukara. Hawathubutu kumtumaini Mungu. Hawana imani ya kweli Kwake Yeye aliyewakabidhi baraka na neema za maisha, na ambaye amewapa talanta kuzitumia kwa utukufu Wake katika kuendeleza kusudi Lake. {2Tsw 656.2}

Wengi wana kawaida hiyo ya kujisumbua kwa fadhaa hivyo kwamba hawampatii Mungu nafasi ya kuwatunza. Kama wangekuwa na upungufu kwa muda mfupi mara zingine, na kuletwa katika maeneo yenye dhiki, ingelikuwa jambo bora zaidi kwa imani yao. Ikiwa wangemtegemea Mungu kwa utulivu, na kumngojea Yeye awafanyie kazi, haja zao zingekuwa fursa kwa Mungu; basi baraka Zake katika dharura zao zingengeza upendo wao Kwake na kuwaongoza kuthamini mibaraka yao ya kidunia kwa namna ya juu zaidi kuliko walivyowahi kufanya hapo awali. Imani yao ingeongezeka, tumaini lao lingeingaza, na uchangamfu ungechukua mahali pa kiza na mashaka na manung'uniko. Imani ya wengi sana haikui kwa kukosa mazoezi. {2Tsw 657.1}

Kile kinachotafuna nguvu ya watu wa Mungu ni kupenda pesa na kufanya urafiki na ulimwengu. Ni fursa ya watu wa Mungu kuwa taa ang'avu na nuru ulimwenguni, kuongezeka katika maarifa ya Mungu, na kuwa na ufahamu dhahiri wa mapenzi Yake. Lakini masumbufu ya maisha haya na udanganyifu wa utajiri, husonga mbegu iliyopandwa mioyoni mwao, na haizai matunda kwa utukufu Wake. Wanaikiri imani, lakini sio imani hai kwa sababu haitegemezwi na matendo. Imani bila matendo imekufa, ikiwa yenyewe. Wale wanaodai kuwa na imani

kubwa, lakini hawana matendo, hawataokolewa na imani yao. Shetani huamini Kweli na kutetemeka, lakini imani ya aina hii haina ubora. Wengi ambao wameikiri imani wamepungukiwa na matendo mema. Ikiwa wangeonyesha imani yao kwa matendo wangeweza kutoa ushawishi mkubwa juu ya upande wa Ukweli. Lakini hawaendelezi talanta ya mali zao katika kusudi walilopewa na Mungu. Wale wanaofikiria kufurahisha dhamiri zao kwa kuridhia mali zao kwa watoto wao, au kwa kuzuia kuendeleza kusudi la Mungu na kuiacha hiyo mali kupita na kwenda mikononi mwa watoto wasioamini, walio wazembe kwa kutapanya au kujilimbikizia na kuabudu, watalazimika kutoa hesabu kwa Mungu; ni mawakili wasio waaminifu wa pesa za Bwana wao. Wanamruhusu Shetani kuwatoa kwenye uongozi wa hii mali ili, yeye akae kwenye kiti kwa njia ya watoto hawa, ambao akili zao ziko chini ya udhibiti wake. Madhumuni ya Shetani yametimizwa kwa njia nyingi, wakati mawakili wa Mungu wanaonekana kupumbazwa na kupooza; hawatambui jukumu lao kubwa lijalo hivi karibuni na ambalo lazima watatoa hesabu. {2Tsw 657.2}

Wale ambao wana mali na ambao akili zao zimetiba giza na muungu wa ulimwengu huu wanaonekana kudhibitiwa na Shetani katika utendaji wao wa kutoa mali zao. Ikiwa wana watoto wanaopenda Kweli, na wanaoamini. Lakini pia wana watoto ambao mapenzi yao ni juu ya mambo yote ya ulimwengu, katika kuhamisha mali kwa watoto wao, kwa ujumla huwapa kwa kiasi kikubwa wale watoto wasiompanda Mungu, na ambao wanamtumikia adui wa haki yote, kuliko wale wanaomtumikia Mungu. {2Tsw 658.1}

Wanaweka mikononi mwa watoto wasio waaminifu mambo yale ambayo yatathibitisha mtego kwao na hivyo itakuwa ni kizuizi katika njia ya kujisalimisha kwa Mungu. Wakati wanatoa zawadi kubwa kwa watoto wasioamini, huwa wanawapatia zawadi za ubahili sana na zisizo na ukarimu, wale watoto ambao wana imani moja nao wenyewe. Ukweli huu unapaswa kuwashtua kwa hofu watu ambao wametumia mali zao kutimiza kusudi hili. Wataona udanganyifu wa utajiri umepotosha hukumu yao. Ikiwa wangeweza kuona ushawishi ukifanyika kwenye akili zao wangeelewa kwamba Shetani alikuwa ameshikilia mambo haya kwa kiasi kikubwa kulingana na makusudi na



mipango yake mwenyewe. Badala ya Mungu kudhibiti akili zao na kutakasa maamuzi yao, imedhibitiwa nguvu kinyume kabisa na ile ya Mungu. Wale ambao wamekuwa pamoja nao katika imani wakati mwingine hata huwapuuza, na mara nyingi huwadhulumu na kuwafanyia uchoyo/ubahili na ukali katika kuchuuza nao (dili); wakati wana mikono mikarimu kwa watoto wasioamini, wanaoupenda ulimwengu huu, ambao wanajua hawatatumia mali ambayo imewekwa mikononi mwao, ili kuendeleza kazi ya Mungu. Bwana anahitaji wale ambao Amewapatia talanta za mali kuzitumia vizuri/sawa, wakiwa na muendelezo wa kazi Yake kama kipaumbele. Kila uzingatiaji mwingine unapaswa kuwa duni kuliko hii. {2Tsw 658.2}

Kusudi la talanta, ziwe ni tano, mbili, au moja, zinapaswa ziboreshwe. Wale ambao wana mali kubwa wanawajibika kwa idadi kubwa ya talanta. Lakini wale waliokuwa na kidogo au masikini hawakuachwa huru kutoka katika majukumu. Wale ambao wana karama ndogo tu kwa ulimwengu huu wanawakilishwa na yule mwenye talanta moja. Walakini wapo katika hatari kubwa ya kuwa na upendo mkubwa sana kwa hiyo talanta ndogo, na kwa ubinafsi kuiweka mbali na kusudi la Mungu, kama ilivyo kwa wale matajiri ila tu hawatambui hatari yao. Wanatumia makaripio yenye kutibua moyo yaliyoelekezwa katika Neno la Mungu kwa wapenzi wa ulimwengu huu, kwa matajiri peke yao, wakati wao wenyewe wanaweza kuwa katika hatari kubwa zaidi kuliko watu matajiri sana. Ikiwa wana vingi au vichache, wote wanahitajika kuweka talanta zao kwa watoa riba, ili wakati Bwana akija, aweze kupokea Mwenyewe kilicho Chake pamoja na riba. Wanahitajika pia kudumisha wakfu kwa Mungu na kutokuwa na maslahi binafsi katika kusudi la kazi Yake. Kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake, wanapaswa kuamini ahadi Yake kwamba vitu vyote vitaongezwa. Katika kulinganisha na kila mazingatio mengine, wokovu wa roho za binadamu wenzao unapaswa kuwa kipaumbele, lakini hii sio desturi kwao. Ikiwa kuna upuuzwaji popote, kusudi la Mungu ndilo litapuuzwa au kusahauliwa. Mungu amewakopesha wanaume talanta, sio kwaajili ya kuchochea au kulea viburi vyao, au kuchochea wivu ndani yao, lakini zitumike kwa utukufu Wake. Yeye Amewafanya waume hawa kuwa mawakala wa kusambaza mali Yake, ili kuendeleza kazi ya wokovu wa wanadamu. Kristo amewapa mfano katika maisha Yake. Yeye Aliacha

utajiri Wake wote wa mbinguni na utukufu, na kwa ajili yetu, akawa masikini, kwamba kupitia umaskini Wake sisi tuweze kutajirika. Sio mpango wa Mungu kushusha mvua ya mali/pesa kutoka mbinguni ili kwamba kusudi la kazi Yake lidumishwe. Yeye Amekabidhi, au kuweka, mali nyingi kwa binadamu, ili kusiwe na upungufu katika idara yoyote ya kazi Yake. Mungu huwathibitisha wale wanaodai kumpenda kwa mdomo, kwa kuweka mali mikononi mwao, na kisha huwajaribu kuona ikiwa wazinapenda karama zaidi kuliko Mtoaji karama. Mungu atafunua, kwa wakati, hisia za Kweli za moyo. {2Tsw 659.1}

Ili kuendeleza kusudi la Mungu, mali ni muhimu. Mungu alitoa mahitaji haya kwa kuweka kwa wingi mikononi mwa mawakala Wake kuzitumia katika idara yoyote ya kazi, ambapo inaweza kuwa inahitajika, katika kazi ya kuokoa roho. Kila roho iliyoोकolewa ni talanta inayopatikana na iliyoongezwa. Ikiwa ameongoka Kweli, mmoja aliyeletwa katika ujuzi wa Ukweli, kwa upande wake, atatumia talanta ya ushawishi na mali ambayo Mungu amempa, kwa kufanya kazi kwa wokovu wa wanadamu wenzake. Yeye Atafanya kwa dhati na bidii kazi kubwa ya kuwaangazia nuru wale walio katika giza na makosa. Atakuwa chombo na mhusika katika kuokoa roho. Kwa hivyo talanta za ushawishi na mali zitakuwa zinachuuzwa na kuongezeka kila wakati. Wakati Bwana atakapokuja, mtumishi mwaminifu yuko tayari kumrudishia Yeye mtaji pamoja na riba. Kwa matunda yake anaweza kuonyesha ongezeko la talanta ambazo amechuma ili kurudisha kwa Bwana wake. Mtumishi mwaminifu aliyeifanya kazi yake, na Bwana, ambaye thawabu Yake ipo Naye kumlipa kila mtu sawasawa na kazi yake, atamrudishia mtumishi huyo mwaminifu vyote, mtaji pamoja na riba. {2Tsw 660.1}

Katika Neno Lake Bwana, amefunua wazi mapenzi Yake kwa wale walio na mali-utajiri. Lakini kwa sababu amri Zake moja kwa moja zimepuuzwa, rehema Zake zinawasilisha hatari iliyo mbele zao kupitia Shuhuda. Yeye Hatoi nuru mpya, lakini anawaelekeza kwenye nuru ambayo tayari imefunuliwa katika Neno Lake. Ikiwa wale wanaodai kupenda Kweli wanashikilia utajiri wao na, wanashindwa kutii Neno la Mungu, hawatafuti fursa kufanya mema kwa yale ambayo amewakabidhi (amana), Yeye Atakuja karibu na atatapanya mali zao. Atawajia kwa karibu nao pamoja na hukumu. Atatawanya sanamu zao

kwa njia mbali mbali. Hasara nyingi zitafanywa kuwa endelevu. Nafsi za watu wenye ubinafsi hazitakuwa na mibaraka. Lakini "roho ya ukarimu itanenepeshwa/itawandishwa." Wale wamheshimuo Mungu, Naye Mungu atawaheshimu. {2Tsw 660.2}

Bwana alifanya Agano na Israeli kwamba, ikiwa wangetii amri Zake, Angewanyeshea mvua kwa majira yake, na nchi itoe mazao yake, na miti ya kondeni itoe mazao yake ya matunda. Aliahidi kwamba kupura kwao kutafikia msimu wa zabibu na msimu wa zabibu hadi wakati wa kupanda, na kwamba watakula mkate wao kwa kushiba na kukaa katika nchi yao salama. Yeye Angewafanya maadui zao kuangamia. Hangewachukia, lakini angeweza kutembea nao na angekuwa Mungu wao, na wangekuwa watu Wake. Lakini ikiwa wangepuuza matakwa Yake, Yeye angewashughulikia kinyume kabisa na haya yote. Laana Yake ingekaa juu yao badala ya baraka. Yeye Angevunja kiburi chao cha nguvu na ingefanya mbingu juu yao kama chuma na dunia kama shaba. "Nguvu zako zitatumika bure; kwa maana nchi yenu haitatoa mazao yake, wala miti ya ardhi haitatoa matunda yao. Na ikiwa mtatembea kinyume Changu, basi Mimi pia nitakwenda kinyume nanyi." {2T 661.1}

Wale ambao kwa ubinafsi wanashikilia mali zao, hawapaswi kushangaa ikiwa mkono wa Mungu utatapanya. Kwamba walipaswa kujitolea kwa maendeleo ya kazi na kusudi la Mungu, lakini ambazo zimezuiliwa, labda anaweza kukabidhiwa mwana mzembe, na anaweza kuipoteza. Farasi mzuri, ambaye kiburi chao cha moyo wa ubatili, aweza kupatikana amekufa katika zizi. Wakati mwingine ng'ombe anaweza kufa. Kupoteza matunda au mazao mengine kwaweza kukaja. Mungu anaweza kutawanya karama ambazo amewakopesha mawakili Wake, ikiwa watakataa kuzitumia kwa utukufu Wake. Nilioneshwa, baadhi yao, wanaweza wasiwe na hasara yoyote ya kuwakumbusha juu ya ujinga wao katika wajibu, lakini kesi zao zinaweza kutokuwa na matumaini kabisa. {2Tsw 661.2}

Yesu aliwaonya watu hivi: "kuweni makini, na jihadharini na tamaa; kwa maana uzima wa mtu haumo ndani ya wingi wa vitu alivyo navyo. Akawaambia mfano, akisema, shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana; akawaza moyoni mwake, akisema, Nitafanyaje, kwa sababu sina nafasi

ya kutunza matunda yangu? Akasema, Hivi ndivyo nitafanya; nitabomoa ghala yangu, na kujenga kubwa zaidi; na huko nitatoa matunda yangu yote na bidhaa zangu. Nami nitaiambia nafsi yangu, Nafsi, una mali nyingi zilizohifadhiwa kwa miaka mingi; pumzika, kula, kunywa na kufurahi. Lakini Mungu akamwambia, Mpumbavu wewe, usiku huu roho yako itatakiwa kutoka kwako; basi vitu hivyo ulivyovitoa vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu anayejiwekea hazina, lakini hana utajiri kwa Mungu." Kisha akawaambia wanafunzi Wake: "Kwa hivyo nawaambia, Msisumbukie maisha yenu, mtakula nini; wala mtavaa nini mwilini. Maisha ni zaidi ya nyama, na mwili ni zaidi ya mavazi." {2Tsw 662.1}

Maonyo haya yametolewa kwa faida ya wote. Je! Watazingatia maonyo yaliyotolewa? Je! Watanufaika? Je! Watazingatia mifano hii ya kushangaza ya Mwokozi wetu na kuachana na mfano wa tajiri mpumbavu? Tajiri alikuwa navyo tele; ndivyo ilivyo na wengi wanaodai kuamini Ukweli, hao ndio kuchukua hatua mbaya kwa kesi za maskini, matajiri wapumbavu. Laiti wangukuwa wenye busara na kuhisi majukumu yaliyowekwa juu yao kutumia baraka ambazo Mungu amewapa katika kuwabariki wengine, badala ya kugeuka kuwa laana. Mungu atawaambia hao wote, kama yule tajiri mpumbavu: "Mpumbavu wewe." {2Tsw 662.2}

Wanadamu hujifanya kana kwamba hawatumii akili au busara zao. Wamechukuliwa/wamezama na shughuli za maisha haya. Hawana muda wa kujitoa wakfu kwa Mungu, hakuna muda wa kumtumikia Bwana. Kazi, kazi, kazi, ndio wanachowaza kila siku. Kote wanahitajika kufanya kazi kwa ratiba isiyo na muda wa kupumzika, yenye kushinikiza, kusimamia mashamba makubwa. Wanabomoa njozi zao zenye matamano ya ukuu na kuzijenga zingine kwa uimara zaidi, ndio shauku yao, ili kwamba wapate mahali pa kuhifadhi bidhaa zao. Na bado watu hawa hawa ambao wameelemewa na tamaa ya utajiri wanaoneka na watu kuwa ni wafuasi wa Kristo. Wana jina linaloamini kuwa Kristo anakuja upesi (Waadventista), na kwamba mwisho wa mambo yote u karibu; na bado hawana roho ya kujikana nafasi. Wanazama zaidi na zaidi ndani ya ulimwengu. Wanatenga muda kidogo sana, wa kujifunza Neno la uzima na kutafakari na kuomba.

Wala hawatoi fursa hii ya kusikia Neno la uzima kwa wengine katika familia, ama wale wanaowahudumia. Na bado watu hawa wanao ujasiri wa kuamini kuwa dunia hii sio nyumbani kwao, na kwamba wao ni wasafiri na wageni tu, hapa duniani, wakijiandaa kuhamia katika dunia iliyo bora zaidi. Mfano na mivuto ya watu kama hawa ni laana katika kazi ya Mungu. Unafiki mtupu ndio sifa inayoweza kuelezea maisha yao ya kujiita Wakristo. Wanampenda Mungu na Ukweli kadri tu matendo yao yanavyoonesha na wala sio zaidi. Mwanadamu hutenda kwa kadri ya imani aliyo nayo. "Kwa matunda yao mtawajua" Moyo wako ulipo ndipo hazina yako ilipo. Hazina zao zipo katika dunia hii, na mioyo na shauku zao pia zipo hapa. {2Tsw 662.3}

Je, "Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa? "Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake." Wakati wale wanaodai kuwa na imani wanapoonesha mtindo wa maisha yao unaoendana na imani yao, ndipo tutakapoona uwezo ukidhihirika katika utendaji wa imani, uwezo ambao utamuongoa mdhambi na kuzivuta roho kwa Kristo. {2Tsw 663.1}

Imani thabithi/isiyoyumbayumba na ya dhati, ni jambo adimu kwa watu matajiri. Imani halisi, inayodhihirika kwa matendo, ni adimu kuipata. Lakini wote ambao wana imani hii, watakuwa watu ambao hawatakosa ushawishi. Watafanana na Kristo-watachukua nakala yake; watamiliki moyo wa kutoa kwa ukarimu bila ya ubinafsi, ambao faida yake ni katika kuokoa roho, kama alivyokuwa Yesu. Mfuasi wa Kristo atathamini roho kama Yeye alivyozithamini. Huruma zao zitakuwa sawa na huruma za Mwokozi wao mpendwa, na watafanya kazi kuokoa ununuzi/gharama ya watu walionunuliwa kwa damu Yake, kwa gharama yeyote. Pesa, nyumba, na ardhi ni nini ukilinganisha na roho hata moja tu? {2Tsw 663.2}

Kristo alilipa dhabihu na gharama kamili na timilifu, gharama na dhabihu inayotosha kumuokoa kila mtoto wa kike na wa kiume wa Adamu ambaye ataonesha toba/ungamo kwa Mungu kwa kukiuka sheria Yake na kudhihirisha imani katika Bwana wetu Yesu Kristo. Pamoja na kwamba gharama ilikuwa kubwa, bali ni wachache tu

wanaojitoa kwa maisha ya utii ili kuupokea wokovu mkuu huu. Wachache tu, ndio wapo tayari kuiga kielelezo Chake cha ajabu, kuvumilia dhiki na mateso, na kushiriki kazi Yake inayochosha ili kuwaleta wengine kwenye nuru. Lakini ni wachache watakaofuata mfano Wake kwa dhati, maombi ya daima kwa Mungu kwa ajili ya nguvu kustahimili majaribu ya maisha haya na kutenda kazi zako za kila siku. Kristo ni Nahodha wa wokovu wetu, na kwa mateso na kafara Yake, Ametoa kielelezo kwa wafuasi Wake wote kwamba kukesha na kuomba, na juhudi katika kustahimili mateso, ni jambo la muhimu katika fungu lao, ikiwa wataakisi upendo ule ambao ulikaa Kifuani Mwake, kwa jamii ya wanadamu iliyoasi. {2Tsw 664.1}

Wanadamu wenye mali wanakufa kiroho kwa sababu ya kupuuza kutumia mali ambazo Mungu ameweka mikononi mwao kusaidia katika kuokoa wanadamu wenzao. Wengine huamka wakati mwingine na kuamua kuwa watajifanyia marafiki na mali ya udhalimu, ili mwishowe wapokelewe katika makao ya milele. Lakini juhudi zao katika mwelekeo huu sio kamili. Wanaanza, lakini, bila kuwa na moyo wa dhati na wenye bidii kabisa katika kazi, wanashindwa. Sio matajiri katika matendo mema. Wakati wanakawia kuzuia upendo wao na kushikilia hazina zao za kidunia, Shetani anawatoa kwenye utawala, na kisha anakuwa ndiyo kamanda wao. {2Tsw 664.2}

Pendekezo lenye danganyifu kuhusu uwezekano wa kuwekeza katika biashara zenye hati miliki au katika kampuni nyingine inayodhaniwa kuwa nzuri ambayo Shetani ameweka mitego ya kuvutia na kuloga watu, laweza kutolewa. Matarajio ya kupata pesa zaidi, haraka na kwa urahisi, huwapumbaza wanadamu. Wanafikiri kwamba, ingawa walikuwa wameamua kuweka pesa hizi kwenye hazina ya Mungu, watazitumia katika uwekezaji huu, na wataongeza faida kubwa, na kisha watatoa kiasi kikubwa kwa kazi ya Mungu. Hawawezi kuona uwezekano wa kushindwa. Bahati mbaya mambo huenda tofauti, na mali inapotea, baadaye wanagundua, kwa masikitiko yao, kwamba wamefanya makosa. Matarajio angavu, yaliyokuwa mazuri yamepotea. Matarajio yao hayatimizwi. Walidanganywa. Shetani aliwalaghai zaidi akawa kamanda/generali wa mchakato ote. Alikuwa mwerevu kuliko wao, na aliweza kuingiza kipato chao katika jeshi/himaya yake na kwa

hivyo kuhafifisha kazi ya Mungu kile ambacho kilipaswa kutumiwa kuiendeleza katika kupanua Ukweli na kuokoa roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake. Walipoteza yote waliyowekeza, na wakampora Mungu kile ambacho walipaswa kumpa Yeye.{2Tsw 665.1}

Wengine ambao wamepewa talanta moja tu, hutoa visingizio kwa sababu hawana idadi kubwa ya talanta kama wale ambao wamepewa talanta nyingi. Kama mtumwa asiye mwaminifu wanaficha talanta moja ardhini. Wanaogopa kumpa Mungu yale ambayo ameyaweka chini ya uangalizi wao. Wanajihusisha na biashara za ulimwengu, lakini wanawekeza kidogo tu, ikiwa kuna chochote, kwa kazi ya Mungu. Wanatarajia kuwa wale ambao wana talanta kubwa watabeba mzigo wa kazi, wakati ambapo wao wanajihisi kuwa hawawajibiki kwa kusonga mbele kwa kazi ya Bwana ya injili na kufanikiwa kwakwe. {2Tsw 665.2}

Wakati Bwana anakuja kufanya mahesabu na watumwa wake, watumwa wasio na hekima watakiri kwa kuchanganyikiwa: "Nilijua Wewe ni mtu mgumu, huvuna usipopanda, na unakusanya mahali ambapo haukutawanya; na niliogopa [Je, Alikuwa na hofu ya nini? Kwamba Bwana angedai sehemu ya talanta ndogo Aliyokabidhiwa Yeye Mwenyewe], akaenda na kuificha talanta yake katika nchi; tazama, unayo iliyo yako. "Bwana Wake atajibu: akamwambia, Wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoao riba; Nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alichu nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiye faa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. {2Tsw 665.3}

Wengi ambao wana utajiri kidogo tu wa ulimwengu huu wanawakilishwa na mtu aliye na talanta moja. Wanaogopa kumtumaini Mungu. Wanaogopa kwamba Yeye atahitaji kitu ambacho wanadai ni chao wenyewe. Wanaficha talanta yao ardhini, wakiogopa kuwekeza mahali popote, wasije wakaitwa ili kumrudishia Mungu sehemu ya

faida. Badala ya kuweka talanta kwa wabadilishaji/wachuuzi, kama Mungu alivyotaka, wanaizika, au kuificha, ambapo Mungu wala mwanadamu hawataweza kufaidika nayo. Wengi wanaodai kuipenda Kweli wanafanya kazi kama hii. Wanajidanganya nafsi zao wenyewe, kwani Shetani ameyapofusha macho yao. Kwa kumuibia Mungu, wamejinyang'anya wenyewe zaidi. Kwa sababu ya tamaa na moyo mwovu wa kutokuamini, wamejinyima wenyewe hazina ya mbinguni. Kwa sababu wana talanta moja tu, wanaogopa kumtumaini Mungu kwa ajili yake, kwa hivyo wanaificha ardhini. Wanahisi wameondolewa jukumu. Wanapenda kuona Ukweli unaendelea, lakini hawafikiri kwamba wanahitajika kujinyima na kusaidia kazi hiyo kwa juhudi zao binafsi, mali na kwa vipato vyao, ingawa hawana kiasi kikubwa sana. {2Tsw 666.1}

Wote wanapaswa kufanya kitu. Kesi ya mjane ambaye alitoa senti zake mbili imewekwa kuwa rekodi/kumbukumbu kwa manufaa ya wengine. Kristo alimpongeza kwa kafara aliyoitoa na aliwaagiza wanafunzi Wake kumsikiliza kwa ajili ya tendo hilo: "Kweli nawambia, huyu mjane maskini ametoa zaidi kuliko wale wote waliotia katika mfuko wa hazina; kwa kuwa wote walitoa kwa wingi wa mali zao, lakini yeye katika uhaba wake ametia vyote alivyo navyo, hata mali yake yote." Kristo aliiheshimu sadaka yake na kuona kuwa ya thamani kuliko sadaka kubwa za matajiri wengi. Walitoa katika wingi wao. Hawangehisi kupungukiwa kidogo kwa sababu ya matoleo yao. Lakini mjane alikuwa amejinyima mwenyewe hata mahitaji ya maisha ili kutoa sadaka yake ndogo. Hakuweza kuona jinsi mahitaji yake ya baadaye yatakavyoweza kutimizwa (kutegemezwa). Hakuwa na mume wa kumsaidia katika mahitaji. Alimtumaini Mungu kwa kesho yake. Thamani ya sadaka haikadiriwi sana na kiwango ambacho hutolewa bali kwa uwiano na kwa nia inayosababisha sadaka hiyo kutoka. Wakati Kristo atakapokuja, na ujira Wake Utakuwa pamoja Naye, Atamlipa kila mtu kwa kadiri ya kazi yake ilivyo. {2Tsw 666.2}

Wote, wa juu na wa chini, matajiri na maskini, wamekabidhiwa talanta na Bwana; wengine zaidi, wengine kidogo, kulingana na tofauti katika uwezo wao. Baraka ya Mungu itakaa juu ya watendakazi dhati na wenye bidii, wenye upendo na waadilifu. Uwekezaji wao utafanikiwa na



utavuna roho kwa ajili ya ufalme wa Mungu, nazo zitakuwa salama na kwao wataavuna hazina isiyoweza kufa. Wote ni wasimamizi wa maadili, na wote wamepewa dhamana ya mali za mbinguni. Vipaji vimegawanywa kulingana na uwezo ambao kila mmoja anao {2Tsw 667.1}

Mungu humpa kila mtu kazi yake, Naye Anatarajia kupata faida kulingana na amana mbali mbali alizowapa. Yeye Hategemei kupata talanta kumi zaidi kutoka kwa yule mtu ambaye amempa talanta moja tu. Hatarajii mtu maskini atoe sadaka kama mtu aliye na utajiri. Hatarajii kwa mtu dhaifu na anayeteseka kutoa sawa ambavyo mtu mwenye afya na nguvu atakavyotoa. Talanta moja, iliyotumika vizuri, Mungu ataikubali, "Kulingana na kile mtu alichona, na sio kulingana na kile asichona" {2Tsw 667.2}

Mungu anaitua sisi tu watumishi, ambayo inamaanisha kuwa tumeajiriwa Naye kufanya kazi fulani na kubeba majukumu fulani. Yeye Ametukopesha mtaji kwa ajili ya uwekezaji. Sio mali yetu, na hatumpendezi Mungu ikiwa tunajilimbikizia bidhaa za Bwana wetu au kuzitumia kama tupendavyo. Tunawajibika kwa namna tunavyotumia au kuharibu kile ambacho Mungu ametukopesha. Ikiwa mtaji huu ambao Bwana ameuweka mikononi mwetu umelala bila kuingiza faida, au tunauzika ardhini, hata ikiwa ni talanta moja tu, tutahitajika kutoa hesabu mbele ya Bwana. Yeye Anahitaji tutoe hesabu, kwani mali hiyo sio yetu, bali Yake Mwenyewe na riba pia. {2Tsw 668.1}

Kila talanta ambayo inarudi kwa Bwana itachunguzwa kinagaubaga. Matendo na amana za watumishi wa Mungu havitachukuliwa kama jambo lisilo muhimu. Kila mtu atashughulikiwa kibinafsi na atahitajika kutoa hesabu ya talanta alizokabidhiwa, ikiwa ameziboresha au kuzitumia vibaya. Thawabu itakayotolewa italingana na uboreshaji wa talanta. Adhabu itakayotolewa itakuwa kulingana na namna talanta zilivyotumiwa vibaya. {2Tsw 668.2}

Swali la kujiuliza kwa kila mmoja wetu linapaswa kuwa: Je! Nina nini ambacho kimetoka kwa Bwana wangu, na napaswa kukitumiaje kwa ajili ya utukufu Wake? "Zitumieni talanta kufanyia biashara mpaka,"

asema Kristo, "nitakapokuja." Mfalme wa mbinguni yu njiani. Fursa yetu ya pekee ni sasa. Talanta ziko mikononi mwetu. Je! Tuzitumie kwa ajili ya utukufu wa Mungu, au tuziharibu? Tunaweza kuzifanyia kazi leo, maana kesho rehema yetu yaweza kufika ukomo na kazi yetu ikawa imefungwa milele. {2Tsw 668.3}

Kama talanta zetu zinatumiwa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzetu, Mungu atatukuzwa. Kiburi, nafasi na cheo hutumiwa kama kisingizio cha kutumia mali bila kujali uchumi, ubatili wa kujionyesha, tamaa za ukuu, na kuendeleza wenda-wazimu wa ubaradhifu wenye ubinafsi na maadili machafu yenye kuleta aibu, na kutapanya mali [profligate selfishnes]. Talanta za Bwana, zilizokopeshwa kwa mwanadamu kama mibaraka ya thamani, kama zitatumiwa vibaya, vitamletea mtu laana mbaya. Utajiri unaweza kutumiwa nasi kuendeleza kazi ya Mungu na kupunguza uhitaji wa wajane na yatima. Kwa kufanya hivyo, tunajikusanyia baraka nyingi. Sio tu tutapokea maneno ya shukrani kutoka kwa wapokeaji wa neema zetu na ukarimu wetu, lakini Bwana Mwenyewe, ambaye ameweka mali hizi mikononi mwetu kwa kusudi hili mahsusi, atafanya nyoyo zetu kuwa kama bustani iliyotiwa maji, ambayo maji yake hayakauki kamwe. Wakati wa mavuno utakapofika, ni nani kati yetu atakayekosa kuwa na furaha isiyoelezeka ya kuona mavuno ambayo tumekusanya, kama malipo ya uadilifu na matumizi yetu yasiyo na ubinafsi ya talanta ambazo Bwana ametia mikononi mwetu kuzitumia kwa utukufu Wake? {2Tsw 668.4}

Wengi huko Vermont wameamua kushindwa kuishi na kufikia mahitaji ya Mungu. Wengine wameanguka kiroho katika hali ya ubaridi na isiyo na uhai kwa sababu wao ni watumishi wasio waaminifu. Upendo kwa ulimwengu huu umejaza mioyo yao kiasi kwamba wamepoteza raha yao ya vitu vya kimbangu na wamekuwa mbilikimo katika mafanikio ya kiroho. Jimbo hili limenyimwa kazi sahihi ya kufanya. Bordoville imekuwa kituo cha kuvutia wengi. Mikusanyiko yote mikubwa imekuwa ikifanyika katika eneo moja, ambayo imekuwa kama kuweka taa chini ya uvungu wa kitanda; miale yake haijawanufaisha watu wa jimbo hilo kwa ujumla. Wengi bado wako gizani ambao wangekuwa wanafurahi katika kuijua Kweli. Talanta na juhudi kubwa zimeelekezwa katika eneo moja. Hii sio kama Bwana apendavyo. Yeye Anakusudia kwamba

maonyo, ujumbe wa tahadhari upelekwe ulimwenguni kote, na kwamba watu Wake, ambao ni nuru ya ulimwengu, wanapaswa kutawanyika kama mashahidi katikati ya giza la mmomonyoko wa maadili ya ulimwengu; ili kwamba maisha yao, ushuhuda wao, na mfano wao uwe harufu ya uzima ielekeayop uzimani, au ya kifo iendayo mautini-2 Wakorintho 2:16. {2Tsw 669.1}

Ndugu D watahitaji kuchukuliwa kwa tahadhari (pengine ni mtu na mkewe), ili wasizuie malengo ya Mungu kwa mipango yao wenyewe. Wamo katika hatari ya kuibinya kazi ya Mungu, na kuifanya iwe finyu, ambayo ni ya kina na pana. {2Tsw 669.2}

Ndugu D atakuwa katika hatari ya kuchukua mtazamo finyu sana kuhusu kazi. Mungu amempa uzoefu ambao utakuwa wa thamani akiutumia vizuri. Lakini kuna hatari kwamba sifa zake za kipekee italeta uzoefu huo na kwamba akili zingine zitaathiriwa. Umuhimu wa Manufaa ya ndugu D kama mtendakazi sio ambavyo ingekuwa, kama asingekuwa mwepesi sana kuweka nguvu za akili yake juu ya wazo moja tu. Anatafakari zaidi juu ya matukio na juu ya mawazo ambayo amekuwa nayo, na kuyarudia kwa muda mrefu, wakati sio muhimu kwa wengine. {2Tsw 669.3}

Akili yake iliamshwa kwa habari ya afya yake. Alikaza nguvu za akili yake juu ya jambo hili. Yeye na dalili za ugonjwa wake vilikuwa ndiyo mada kuu ya mazungumzo. Alikuwa mahsusi kuendeleza uelekeo aliounzisha akilini mwake; na, wakati anatafuta fadhila yake binafsi, alishindwa kuzingatia anavyofanya usumbufu kwa wengine. Akili yake imefungwa, kwa kiwango kikubwa, katika hali yake mwenyewe. Huu ulikuwa mzigo wa mawazo yake na mada mazungumzo yake. Katika uelekeo huu sahihi, wa hatua kwa hatua ameshindwa kupata faida, katika hali ya afya, kwamba angeweza kugundua ikiwa angejisahau nafsi yake zaidi, siku kwa siku, na kufanya mazoezi ya mwili, hayo yangegeuza mawazo yake kutoka kwake. {2Tsw 670.1}

Mapungufu yale yale yanaoneka katika kazi yake katika eneo la injili. Katika kuzungumza na watu, anatoa “Samahani” nyingi na mambo mengi ya utambulisho wa awali, au utangulizi ambayo hurudia-rudia, na

mkutano unachoka kabla hata hajaifikia mada yake halisi anayoihubiri siku hiyo. Kwa kadiri inavyowezekana, wahubiri wanapaswa kuepuka kutoa udhuru na maelezo ya awali (apologies and preliminaries). {2Tsw 670.2}

Ndugu D ni tofauti sana. Anatafakari zaidi juu ya mambo madogo madogo. Anachukua muda kuelezea hoja ambazo kwa kweli sio muhimu na zingechukuliwa kwa urahisi kuwa ni kweli bila hata kutoa uthibitisho, kwani zinajidhihirisha zenyewe. Lakini hoja halisi za Kweli, na muhimu zinapaswa kusisitizwa kwa kadri ambavyo lugha na uthibitisho vinavyoweza kuzifanya. Zinapaswa kuonekana wazi kama mabango ya maili. Anapaswa kuepuka maneno mengi juu ya mambo madogo, ambayo yatawachosha wasikilizaji kabla hata hoja muhimu kufikiwa. {2Tsw 670.3}

Ndugu D ana hali ya kukaza fikra sana katika jambo. Wakati anapoelekeza akili yake katika mwelekeo fulani, ni vigumu kwake kuielekeza mahali pengine; anadumu kwa kujishugulisha kupindukia katika hoja moja na anaenda taratibu. Katika mazungumzo yuko katika hatari ya kumchosha msikilizaji. Maandishi yake hayana mtindo huru, rahisi. Tabia ya kukaza fikra juu ya jambo moja, kwa kuacha mambo mengine, ni jambo baya. Hili anapaswa kulielewa, na anapaswa kufanya kazi kuzuia na kudhibiti nguvu hii ya akili, ambayo ina utendaji mwingi. Shughuli kubwa sana ya kiungo kimoja cha akili huimarisha kiungo hicho kwa kudhoofisha viungo vingine. Ikiwa Ndugu D angekuwa mtendakazi mwenye mafanikio katika shamba la injili, anapaswa kuielimisha akili yake. Ukuaji mkubwa wa kiungo (ogani) hiki unadhoofisha afya na manufaa yake. Kuna ukosefu wa upatanifu katika mpangilio wa akili yake, na mwili wake unaathiriwa na matokeo. {2Tsw 670.4}

Ingefaa sana kwa maslahi ya Ndugu D kukuza na kupalia uhalisi na pumziko/utulivu kidogo katika uandishi wake. Anahitaji kuepuka kutumia muda mrefu katika hoja yoyote ambayo sio ya muhimu sana; na hata Kweli muhimu zaidi, zilizo wazi, ambazo kwa zenyewe ziko wazi na dhahiri, zinaweza kufunikwa sana kwa maneno kama kutanda kwa mawingu na kutokuwa wazi. {2Tsw 671.1}

Ndugu D anaweza kuwa bora na mwenye hekima katika mambo yote yanayohusu Ukweli wa sasa na bado asiwe na sifa katika kila jambo kutoa sababu za tumaini letu kwa watu wa Ufaransa kwa maandishi. Anaweza kusaidia katika kazi hii. Lakini jambo hili linapaswa kuandaliwa na zaidi ya mawazo ya mtu moja au wawili, ili lisiweze kuwa na muhuri wa sifa ya mtu mmoja. Ukweli uliofikiwa na kutayarishwa na akili kadhaa, na ambao katika wakati wa Mungu uliletwa kwa kiungo baada ya kiungo katika mnyororo uliunganishwa na watafutaji wa Kweli, unapaswa kupewa watu, na utaratibiwa ili kukidhi mahitaji ya wengi. Ufupi wa makala unapaswa kuzingatiwa ili kumvutia msomaji. Makala ndefu zenye maneno mengi huleta maumivu kwa kuharibu Ukweli ambao mwandishi analenga kuuwasilisha. {2Tsw 671.2}

Ndugu D anapaswa asiwaze sana kuhusu yeye mwenyewe na kutojizungumzia sana yeye mwenyewe. Ajiondoe machoni pa watu kwa kutojizungumza sana kuhusu mwenyewe saa yote (out of sight), aepuke kujitaja mwenyewe na kufanya upekee wake wa maisha kuwa mfano kwa wengine kuiga. Anapaswa kuhimiza unyenyekevu wa kweli. Yuko katika hatari ya kufikiria maisha na uzoefu wake ndiyo bora kuliko ule wa wengine. {2Tsw 671.3}

Ndugu D anaweza kuwa wa thamani kwa kazi ya Mungu ikiwa kuna maelewano katika tabia ya kazi yake. Ikiwa anaweza kuona na kurekebisha kasoro za muundo wake wa kipekee, ambao una tabia ya kuharibu kufaa kwake, Mungu anaweza kumtumia kwa kukubalika. Anapaswa kuepuka mahubiri marefu na maombi marefu. Haya hayana faida kwake au kwa wengine. Mazoezi marefu na ya nguvu ambayo ni ukatili kwa viungo vya sauti yamechoma koo na mapafu yake, na kujeruhi afya yake kwa jumla, zaidi ya vile ambavyo sheria zake sahihi za kula na kupumzika zilivyomnufaisha. Hata utumiaji mmoja mbaya wa viungo vya sauti kwaweza kuleta ugonjwa ambao hatuapona haraka na hata kugharimu maisha ya mhubiri/msemaji. Kuzungumza kwa namna tulivu, isiyo na haraka, lakini kwa dhati na bidii, kutakuwa na ushawishi bora juu ya kusanyiko kuliko kuruhusu hisia zichochewe na kutawala sauti na ishara na hulka/tabia (manners). Kwa kadiri

inavyowezekana mzungumzaji anatakiwa kulinda asili ya kupanda na kushuka kwa sauti-toni ya sauti. Ukweli unaowasilishwa, ndio ambao huathiri moyo. Ikiwa msemaji anazifanya Kweli hizi kuwa uhalisi, ataweza, kwa msaada wa Roho wa Mungu, kugusa mioyo ya wasikilizaji kwa ukweli kwamba yu dhati na mwenye ari, bila hata ya kuchosha viungo laini vya koo au mapafu. {2Tsw 672.1}

Ndugu D anapendezwa sana na maisha yake ya nyumbani; lakini kuna hatari katika mazungumzo, ya kukuza tabia ya kukaza akili yake yote juu ya vitu ambavyo humvutia yeye hasa, lakini ambavyo haviwezi kuwavutia au kuwafaidi wengine. Anajaribu kudumisha mfumo ambao, kwa wenyewe, ni sahihi; lakini hapa tena itaonekana kwamba mambo ambayo yanafaa kwa yenyewe yanaweza kuchosha na kuwa mzigo kwa kuyatafakari sana, na kwa kutafuta kushughulika nayo kwa hali yoyote. Kuna hatari ya kupuuza mambo yaliyo mazito zaidi. {2Tsw 672.2}

Ndugu D (wawili) wanapaswa kuepuka kuchosha watu katika kazi yao. Ushawishi wao umekuwa mzuri kwa kiasi kikubwa. Ndugu D kwa kawaida ni meneja mzuri katika mambo ya muda mfupi. Maagizo yake na mfano katika mwelekeo huu vimemewasaidia wale ambao walikuwa wanyenyekevu sana kushauriwa. Lakini wivu, kutokuamini, uasi, kulalamika, na manung'uniko ambavyo vimekuwepo kanisani vimekuwa vikivunja moyo. Ndugu hawa wanapaswa kujilinda dhidi ya kuwa wakali sana (exacting). {2Tsw 673.1}

Ili kuwa na tabia kamilifu ya Kikristo, hatupaswi kukuza maisha ya utulivu tu, ya kuomba tu au kushughulikia yale yenye ari na msisimko mwingi, wakati uchaji Mungu binafsi unapuuzwa. Lakini wakati wa sasa tunahitaji kungojea kuja kwa Bwana na kufanya kazi kwa uangalifu kwa ajili ya wokovu wa wenzetu. "Si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana." Mungu hata kubali huduma za juu kabisa isipokuwa kwanza zimewekwa wakfu kwa kujitoa roho Kwake na kwa upendo Wake. Kwa tabaka fulani la akili kuna hatari ya kumwondoa nje ya mfumo Roho wa Mungu na uhai wa dini ya Kristo, na kuhifadhi duru kamili ya majukumu na sherehe za kuchosha. {2Tsw 673.2}

Tunaishi katikati ya kizazi kilichopinda na kilichopotoka, na mipango yetu mizuri na halisi, haiwezi daima kutekelezwa kwa faida ya wote. Ikiwa tutasimama kwa kuangalia hadhi yetu tutashindwa kuwasaidia wale wanaohitaji msaada zaidi. Watumishi wa Kristo wanapaswa kuchukuliana na hali mbalimbali za watu. Hawawezi kutekeleza sheria halisi ikiwa watakutana na hali za watu wote. Kazi itapaswa kuwa na utofauti ili kuwafikia watu mahali walipo. “Wahurumieni wengine walio na shaka, na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.” {2Tsw 673.3}

Mtume anawashauri ndugu zake wa Korintho: “Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu, vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa.” 1 Wakorintho 10: 31-33. “Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi.” 1 Wakorintho 9:19. “Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu.” Fungu la 22. “Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe. Kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema, akajengwe. Kwa maana Kristo Naye hakujipendeza Mwenyewe; bali kama ilivyoandikwa, Malaumu yao waliokulaumu wewe yalinipata Mimi.” Warumi 15: 1-3. {2Tsw 673.4}

Ndugu na Dada L wa Canada wamekuwa wakishuka polepole katika kumshikilia kwao Mungu na upendo wao kwa mambo ya kimbingu na Bwana kwa ambavyo wamekuwa wakishikilia kwa bidii zaidi hazina za ulimwengu. Wamekuwa wakilegeza ushikiliaji wao wa mbingu na kuukaza kwa nguvu zaidi katika ulimwengu huu. Miaka michache iliyopita walipenda kuvutiwa na maendeleo ya Kweli na kazi ya Mungu. Hivi karibuni upendo wao kwa mali umeongezeka, na hawajahisi kuvutiwa kufanya sehemu yao kuokoa wanadamu wenzao. Kujikana nafsi na ukarimu kwa ajili ya Kristo sio sifa za maisha yao. Wamefanya

kidogo tu kwa ajili ya kazi ya Mungu. Je, wamekuwa wakifanya nini na talanta zao? Wamekuwa wakizizika katika nchi, wakiziwekeza katika ardhi. Hawakuwa wakiziweka kwa watoao riba, ili Bwana ajapo, aweze kupokea iliyo Yake pamoja na faida. {2Tsw 674.1}

Wana kazi ya kufanya ili kutengeneza mambo ya mioyo na nyumba zao kwa kuyaweka sawa, “Jiwekeeni hazina mbinguni.” Mioyo yao imekuwa katika vitu vya maisha haya, na mambo ya milele yamefanywa kuwa ya pili. Wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuondoa upendo wa ulimwengu katika mioyo yao, na wanapaswa kuweka mapenzi yao katika vitu vilivyo juu, sio katika vitu vya duniani. Ikiwa watumishi wa Mungu wangekumbuka kuwa kazi yao ni kufanya yote katika uwezo wao, na ushawishi wao na mali zao, kuokoa roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yao, kungekuwa na bidii zaidi isiyo ya ubinafsi, na wasioamini wangeamshwa; wangeshawishika kuwa kuna uhalisi katika Kweli uliowasilishwa na hivyo kuungwa mkono kwa mfano wao. {2Tsw 674.2}

Ndugu na Dada L wanapaswa kuwa na ujasiri katika kazi kwa siku hizi za mwisho na wanapaswa kukamilisha tabia ya Kikristo, ili waweze kupata thawabu ya milele, Yesu anapokuja. Ndugu L anashindwa katika nguvu ya mwili na akili. Anashindwa kubeba jukumu zaidi. Anapaswa kushauriana pamoja na ndugu zake ambao ni wenye busara na waaminifu. {2Tsw 675.1}

Ndugu L ni wakili wa Mungu. Amekabidhiwa mali na anapaswa kuwa macho kwa jukumu lake na kumpa Mungu yaliyo ya Mungu. Hapaswi kushindwa kuelewa madai Mungu aliyonayo juu yake. Wakati anapoishi, na ana nguvu zake za kufikiri, anapaswa kuboresha fursa ya kutenga mali ambayo Mungu amempatia, badala ya kuwaachia wengine watumie na kujitwalia baada ya kufungwa kwa maisha yake. {2Tsw 675.2}

Shetani yuko tayari siku zote kutumia mapungufu na madhaifu ya watu ili kukidhi makusudi yake mwenyewe. Yeye ni adui mpinzani mjanja, na amewazidi wengi kwa uhodari kama kamanda, ambao makusudi yao yalikuwa mazuri kunufaisha kazi ya Mungu na mali zao. Wengine wamepuuza kazi ambayo Mungu amewapa wafanye, katika kutenga



mali zao. Na wakati wamekuwa wazembe kwa kujipatia katika kazi ya Mungu mali ambazo amewaazima, Shetani huja na kugeuza hiyo mali kuwa kwenye safu yake mwenyewe. {2Tsw 675.3}

Ndugu L anapaswa kwenda kwa uangalifu zaidi. Watu wasio wa imani yetu wanapata mali kwake kwa namna mbalimbali za udanganyifu na kujifanya. Anawaamini, akiamini kuwa ni waaminifu. Haitawezekana kwake kurudisha mali zote alizoziacha zitoke mikononi mwake kwenda kwa safu ya adui. Angeweza kufanya uwekezaji salama wa mali zake kwa kusaidia kazi ya Mungu na hivyo kujiwekea hazina mbinguni. Mara kwa mara hawezi kusaidia wakati angeweza kwa sababu ni mlemavu na hawezi kuamuru mali kufanya hivyo. Wakati Bwana anapohitaji mali Zake, mara kwa mara zipo mikononi mwa wale ambao amewakopesha, baadhi ambao hawapangi kulipa, na wengine hawahisi wasiwasi katika jambo hilo. Shetani atatimiza kusudi lake kikamilifu kupitia wakopaji wasio waaminifu kwa njia nyingine yoyote. Yote ambayo mpinzani wa Kweli na haki anafanyia kazi ni kuzuia maendeleo ya ufalme wa Mkombozi wetu. Adui anatenda kazi kupitia mawakala kutekeleza makusudi yake. Ikiwa anaweza kuzuia mali kwenda kwenye hazina ya Mungu amefanikiwa katika tawi moja la kazi yake. Hiyo mali ambayo ingetumiwa kusaidia katika mpango mkubwa wa kuokoa roho ameizuilia kwenye jeshi lake ili kumsaidia katika kazi yake. {2Tsw 675.4}

Ndugu L anapaswa kuiweka biashara yake sawa na sio kuachwa bila malengo, ikilegealegea. Ni fursa yake kutajirika katika matendo mema, na kujiwekea msingi mzuri kwa wakati ujao, ili aweze kushikilia uzima wa milele. Sio salama kwake kufuata uamuzi wake ulioshindwa (unaofeli). Anapaswa kushaurina na ndugu wenye uzoefu, na kutafuta hekima ya Mungu, ili afanye kazi yake vizuri. Sasa anapaswa kuwa mwenye bidii, akijipatia “mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu.” {2Tsw 676.1}

Ndugu M amefanya makosa katika maisha yake ya nyumbani. Kwa maneno, hajaonesha mapenzi yale kwa mkewe ambayo ilikuwa ni jukumu lake kuyaonesha. Ameshindwa kukuza, uungwana na adabu ya kweli na upole wa Kikristo. Ameshindwa kuwa mwema kila wakati na

mwenye kujali matakwa na faraja yake mkewe, kama ilivyokuwa jukumu lake. Kutokuungana pamoja katika imani kumesababisha kutokuwa na furaha kwa wote wawili. Ndugu M hajaheshimu maoni na ushauri wa mke wake kama anavyopaswa. Kwa namna nyingi uamuzi wake na utambuzi ni bora kuliko wake. Akimwomba shauri, anaweza, kwa mtazamo wake wa utambuzi wa wazi na mzuri, kumsaidia kimsingi katika masuala yake ya biashara, katika kushughulika na majirani zake. Hapaswi kusimamia katika hadhi yake, akihisi kuwa anaelewa yote mwenyewe. Ikiwa angeshauriwa na mkewe, na kwa matendo yake mazuri angeonesha kumjali, na shauku ya kumpendeza, angekuwa anafanya wajibu wake kikamilifu. Ikiwa ushauri wake unapingana na wajibu wake kwa Mungu na madai Yake juu yake, basi anaweza kuchagua kutofautiana, na kwa namna tulivu zaidi iwezekanavyo, akitoa sababu yake kwamba hawezi kuitoa kafara imani yake au kanuni zake. Ingekuwa ni faida kwa Ndugu M katika mambo ya muda mfupi ya ulimwengu, kuchukua maoni na ushauri wa mkewe. {2Tsw 676.2}

Wakati yeye ni mkali, mwonevu, mwenye mikwaruzo na asiye na hisani, hawezi kuwa na ushawishi wa kumwongoa mkewe katika Kweli. Anapaswa kufanya matengenezo. Anahitaji kupunguza ukali, kuwa mwema, mpole, na mwenye upendo mwanana/laini. Anapaswa kuruhusu mwanga wa uchangamfu na kuridhika kwa furaha ndani ya moyo wake, na kisha kuruhusu miali yake iangaze ndani ya familia. Ameleta ndani ya familia yake wale ambao mvuto wao ungeleta laana kwa mkewe kuliko baraka. Kwa kufanya hivyo, amelea mizigo juu yake ambao ungeweza kuepukwa. Anapaswa kuombwa ushauri, na matakwa yake kuzingatiwa, kwa kadri inavyowezekana bila kuhatarisha imani yake. {2Tsw 677.1}

Ndugu M amechagua njia yake mwenyewe, na amekuwa na dhamira yenye ladha ya ukaidi-mapenzi yake yanaganda hapo pamoja. Mara nyingi amekuwa asiyekubali kushindwa. Hii haipaswi kuwa. Anakiri kuiamini Kweli ambayo ina mvuto unaotakasa, kulainisha, na kusafisha; mkewe hana hiyo. Anapaswa kuonyesha kwamba Ukweli unatoa nguvu juu ya asili yake potovu, kwamba unamfanya kuwa mvumilivu, mwenye fadhili, mwenye huruma nyororo, mwenye kujali, mwenye upendo

mwanadana mstahimilivu, mpole, mwenye upendo, na mwenye kusamehe. Njia bora ya Ndugu M kuwa mmishenari aliye hai katika familia yake ni kwa yeye kuonesha mfano wa Mwokozi wetu mpendwa katika maisha yake {2Tsw 677.2}

## SURA YA 79

### KUHAMISHA HAZINA YA KIDUNIA

Ndugu Mpendwa N: Nimehisi mzigo mzito sana kwa habari yako tangu tulipokutana nawe kwenye mkutano wa makambi ya Tipton. Kwa nisi`ngeweza kujizuia kuzungumza nawe kibinafsi wakati ninazungumza na watu juu ya Maneno ya Kristo: “Msijiwekee hazina hapa duniani ambako nondo na kutu hugaribu, na wezi huingia na kuiba. Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuharibu, wala wezi hawaingii wakaiba. Maana pale ilipo hazina yako, ndipo pia utakapokuwa moyo wako.” {2Tsw 678.1}

Niliikumbuka sura yako kama ile niliyooneshwa katika njozi wakati uliopita. Ulikuwa unadhani una jukumu la kuhubiria wengine Neno; lakini mfano wako, kama ulivyo sasa, ungewazuia wengi zaidi kuikubali Kweli kuliko ambavyo mahubiri yako yangewabadili watu katika imani . Unakiri kuamini ujumbe makini, unaopima; lakini imani yako haijaimarishwa kwa matendo. Unayo Kweli katika nadharia, lakini haujaongolewa nayo. Ukweli haujaushika kabisa moyo wako na kudhihirishwa katika maisha yako ya kila siku. {2Tsw 678.2}

Unahitaji kuongoka, kubadilishwa na kufanywa upya nia yako. Wakati Ukweli unapokuwa unashikilia moyo wako, itafanya matengenezo katika maisha. Kisha ulimwengu usioamini utashawishiwa kwamba kuna nguvu katika Kweli iliyoleta mabadiliko makubwa sana kwa mtu

anayeupenda ulimwengu kama wewe ulivyokuwa. Wewe unaupenda ulimwengu huu. Hazina zako ziko hapa, na moyo wako uko katika hazina zako. Na nguvu ya Kweli isipotenganisha mapenzi yako na muungu wako, ambaye ni ulimwengu huu, utapotea pamoja na hazina zako. {2Tsw 678.3}

Una utambuzi kidogo tu juu ya tabia iliyoinuliwa ya kazi kwa siku hizi za mwisho. Haujatoa kafara kwa ajili ya ile Kweli. Una roho ya uchoyo, ya ubahili, na umeyafumba macho yako kwa mahitaji ya wenye shida na mhitaji. Huruma yako haijaamshwa kupooza mahitaji ya wanaodhulumiwa, wala hukuwa na moyo wa kusaidia kazi ya Mungu kwa mali zako au kusaidia mahitaji ya wanaoteseka. Moyo wako uko katika hazina zako duniani. Usiposhinda kupenda kwako vitu vya ulimwengu hautakuwa na nafasi katika ufalme wa mbinguni. {2Tsw 678.4}

Mwanasheria alimuuliza Yesu afanye nini ili apate kuurithi uzima wa milele. Yesu alimwelekeza katika amri za Baba Yake, akimwambia kwamba kuzitii kulikuwa muhimu kwa wokovu wake. Kristo alimwambia kwamba anajua amri, na ikiwa alizitii, atakuwa na uzima. Zingatia jibu lake: “Mwalimu, haya yote nimeshika tangu utoto wangu.” Yesu alimtazama kijana huyu aliyedanganywa kwa huruma nyororo, kujali na upendo mwanana. Yuko karibu kumfunulia kwamba kuna kushindwa kwake kutunza kutoka moyoni amri ambazo alisisitiza kwa ujasiri kuwa anazitii. Yesu akamwambia, “Umepungukiwa na Neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuata.” {2Tsw 679.1}

Yesu anaelekeza umakini wa kijana huyu moja kwa moja katika kasoro ya tabia yake. Anatoa mfano wa maisha Yake Mwenyewe ya kujikana nafsi na kubeba msalaba. Kristo Aliacha vyote kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu, Naye alimsihi kijana kuja kuuiga mfano Wake, na akamhakikishia kwamba atakuwa na hazina mbinguni. Je, moyo wa kijana huyu ulilipuka auuliruka kwa furaha kwa hakikisho hili kwamba Kweli atakuwa na hazina mbinguni? Lo, hapana! Hazina zake za kidunia zilikuwa sanamu yake; zilifunika thamani ya urithi wa milele. Anageuka toka msalabani, anageuka kutoka katika maisha ya kujitoa kafara ya

Mkombozi, na kwenda katika ulimwengu huu. Ana shauku ya muda mrefu kwa ajili urithi wa mbinguni, lakini kwa kusita anageuka kutoka katika matarajio. Inagharimu kupambana kuamua ni nini anapaswa kuchagua, lakini mwishowe aliamua kuendelea na mapenzi yake kwa hazina zake za kidunia. {2Tsw 679.2}

Kijana huyu alikuwa na mali nyingi, na moyo wake ulikuwa juu yake. Hakuweza kukubali kuzihamishia hazina zake mbinguni kwa kuondoa mapenzi yake toka kwazo na kutenda mema nazo—kuwabariki mjane na yatima, na hivyo kuwa tajiri katika matendo mema. Upendo wa kijana huyu kwa hazina zake za kidunia ulikuwa na nguvu kuliko upendo wake kwa wanadamu wenzake na urithi usioharibika. Uchaguzi wake ulifanywa. Ushawishi uliowasilishwa na Kristo, wa kuwapatia hazina mbinguni, ulikataliwa, kwa kuwa asingekubali kufuata masharti. Nguvu ya mapenzi Yake kwa utajiri Wake wa kidunia ilishinda, na mbingu, pamoja na utukufu Wake wote wa kupendeza, na kuvutia vilitolewa kafara kwa hazina za ulimwengu. Kijana huyu alikuwa na huzuni sana, kwani aliyataka malimwengu yote; lakini alitoa kafara wa mbinguni kwa ajili wa kidunia. {2Tsw 680.1}

Lakini ni wachache wanaotambua nguvu ya upendo wao kwa utajiri hadi jaribu linapoletwa kwao. Wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanaonesha kuwa hawajajiandaa kwa ajili ya kwenda mbinguni. Kazi zao zinashuhudia kwamba wanapenda utajiri kuliko jirani yao au Mungu wao. Kama yule kijana tajiri, wanaulizia njia ya uzima; lakini wanapoelekezwa njia, na gharama kukadiriwa, na wanashawishiwa kwamba ni lazima watoe kafara utajiri wao wa kidunia na kuwa matajiri kwa matendo mema, wanaamua kwamba gharama ya mbingu ni kubwa mno. Kadiri hazina kubwa zinavyowekwa duniani, ndivyo inavyokuwa vigumu kwa mmiliki kutambua kuwa sio zake mwenyewe, bali amekopeshwa kutumia kwa utukufu wa Mungu. {2Tsw 680.2}

Hapa Yesu anaboresha nafasi ya kuwapa wanafunzi Wake somo la kugusa moyo: “Yesu akawaambia wanafunzi Wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa shida kwa tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni.” Ni rahisi zaidi ngamia kupenya tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.” Hapa nguvu ya utajiri

inaonekana. Nguvu ya kupenda utajiri katika akili ya mwanadamu karibia inaduwaza na kupumbuza. Utajiri unawapumbaza wengi, na kuwafanya watende kama wendawazimu. Kadiri wanavyokuwa na vya dunia hii, ndivyo wanavyotamani zaidi. Hofu yao ya kupungukiwa, huongezeka na utajiri wao. Wana tabia ya kujilimbikiza mali kwa ajili ya siku zijazo. Ni wachoyo na wenye ubinafsi, wakiogopa kwamba Mungu hatawapatia mahitaji yao ya wakati ujao. Watu kama hawa ni masikini kwa Mungu. Kadiri mali zao zilivyoongezeka, wameweka tumaini lao kwazo, na hawajawa na imani kwa Mungu au ahadi Zake. {2Tsw 680.4}

Mtu maskini ambaye ana imani na ujasiri kwa Mungu, anayetumainia upendo na utunzaji Wake, na atendaye kwa wingi, matendo mema, kwa busara akitumia kidogo alichonacho katika kuwabariki wengine kwa mali yake, ni tajiri kwa Mungu. Anahisi kwamba jirani yake analo dai juu yake ambalo hawezi kulipuuza na huku akitii amri ya Mungu: "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Masikini ambao ni matajiri kwa Mungu huchukulia wokovu wa wanadamu wenzao kuwa na umuhimu mkubwa kuliko dhahabu na fedha zote ambazo ulimwengu unazo. {2Tsw 681.1}

Kristo anaonesha njia ambayo wale wenye utajiri wa ulimwengu bali si matajiri kwa Mungu wanaweza kupata utajiri wa Kweli. Anasema: Uza ulivyo navyo, uwagawie maskini, nawe ujiwekee hazina mbinguni. Dawa/Tiba anayoipendekeza kwa matajiri ni kuhamisha mapenzi yao kutoka kwa utajiri wa kidunia kwenda katika urithi wa milele. Kwa kuwekeza mali zao katika kazi ya Mungu kusaidia katika wokovu wa roho, na kwa kuwabariki wahitaji kwa mali zao, wanakuwa matajiri katika matendo mema nao: "wanajiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli." Hii itathibitisha uwekezaji salama. Lakini wengi huonesha kwa matendo yao kwamba hawadiriki kuamini benki ya mbinguni. Wanachagua kuziamini mali zao duniani badala ya kuzipeleka mbinguni, ili mioyo yao iwe katika hazina yao ya mbinguni. {2Tsw 681.2}

Ndugu yangu, unayo kazi mbele yako, ya kujitahidi kushinda tamaa na kupenda utajiri wa kidunia, na hasa kujiamini binafsi kwa sababu umekuwa na mafanikio ya wazi katika kupata vitu vya ulimwengu huu. Matajiri walio masikini moyoni, wanaodai kumtumikia Mungu, ni watu

wa kuhurumiwa. Japo wanadai kumjua Mungu, kwa matendo wanamkana. Ni giza kubwa kiasi gani kwa watu kama hao! Wanakiri imani katika Kweli, lakini kazi zao haziendani na kukiri kwao. Upendo wa utajiri huwafanya wanadamu kuwa wabinafsi, wakali, na wadhalimu. Utajiri ni nguvu; na mara kwa mara mapenzi yake hupotosha na kupoozesha yote yaliyo mazuri na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu. {2Tsw 681.3}

Utajiri huleta majukumu makubwa. Kupata utajiri kwa njia isivyo haki, kwa hila katika biashara, kwa kumwonea mjane na yatima, au kwa kujilimbikizia mali na kupuuza mahitaji ya mhitaji, mwishowe italeta adhabu ya haki iliyoelezewa na mtume aliyevuviwa: “Haya basi, enyi matajiri! Lieni, mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia. Mali zenu zimeoza, na mavazi yenu yameliwa na nondo. Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto. Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho. Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi.” {2Tsw 682.1}

Wanyenyekevu na maskini zaidi wa wanafunzi wa Kweli wa Kristo, ambao ni matajiri wa matendo mema, wamebarikiwa zaidi na ni wa thamani mbele za Mungu kuliko watu wanaojivunia utajiri wao mwingi. Wao ni wenye heshima zaidi katika nyua za mbinguni kuliko wafalme waliotukuka sana na wakuu wasio matajiri kwa Mungu. {2Tsw 682.2}

Mtume Paulo alimhimiza Timotheo kuwaagiza matajiri: “Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.” Mausia haya yanafaa kwako, Ndugu N, na kwa watu wengi sana ambao wanadai kuiamini Kweli kwa siku hizi za mwisho. {2Tsw 682.3}

Wale wanaojilimbikizia mali au kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika ardhi, wakati wakinyima familia zao faraja ya maisha, wanatenda kama watu wenye wazimu. Hawaziruhusu familia zao kufurahia vitu ambavyo Mungu amewapatia tele. Pamoja na kwamba wana mali nyingi, familia zao hulazimishwa mara kwa mara kufanya kazi zaidi ya nguvu zao, kutunza mali zaidi za kujilimbikizia. Ubongo, mfupa, na misuli hutumikishwa kwa kiasi kikubwa kujilimbikizia, na majukumu ya dini na ya Kikristo yanapuzwa. Kazi, kazi, kazi, ni tamaa toka asubuhi hadi usiku. {2Tsw 683.1}

Wengi hawaoneshi shauku ya dhati ya kujifunza mapenzi ya Mungu na kuelewa madai Yake kwao. Wengine wanaojaribu kuifundisha Kweli kwa wengine, wao wenyewe hawalitii Neno la Mungu. Zaidi kazi ya Mungu inavyokuwa na waalimu kama hao, ndivyo itakavyosonga mbele kwa mafanikio madogo sana. {2Tsw 683.2}

Wengi ambao Mungu amewakabidhi utajiri hawafikirii kuwa wanafanya kazi dhidi ya maslahi yao ya milele kwa kujilimbikizia/kujizuilia kwa ubinafsi utajiri wao. Mtume anawaonesha kwamba kwa kuwa matajiri katika kazi njema wanajifanyia kazi wenyewe. Wanajiwekea akiba kwaajili yao wenyewe, wanaipia mbingu hazina ya kudumu, ili wapate kushikilia uzima wa milele. Katika kutoa kwa ajili ya kazi ya Mungu, na kuwasaidia wahitaji, wanafanya kwa uaminifu kazi ambayo Mungu amewapa; na kumbukumbu ya kujikana nafsi kwao na ukarimu, na matendo ya upendo yataandikwa katika kitabu cha mbinguni. Kila tendo la haki litadumu milele, ingawa mtendaji anaweza asihisi kwamba amefanya chochote kinachostahili kutambuliwa. Ikiwa kutembea kila siku kwa wale wanaoikiri kweli kungekuwa mfano hai wa maisha ya Kristo, nuru ingeng'aa kutoka kwao ambayo ingewaongoza wengine kwa Mkombozi. Ni Mbinguni pekee yake tu, ndipo yatawekwa makadirio kamili ya matokeo yaliyobarikiwa, katika wokovu wa wengine, ya maisha thabiti, patanifu, na ya utauwa. {2Tsw 683.3}

Ndugu yangu, una mengi ya kufanya katika familia yako kuwaonesha kuwa Kweli imefanya kazi nzuri kwako na kwamba imekuwa na mvuto unaolainisha, kusafisha, na kuinua katika maisha na tabia yako. Unakiri kuamini kwamba tunaishi katika siku za mwisho na kwamba ujumbe



unaotoa onyo, unaopima ulimwengu; Je, unaonesha hili kwa matendo yako? Mungu anakujaribu wewe, na atafunua hisia za Kweli za moyo wako. {2Tsw 684.1}

Bwana amekupa talanta za mali za kutumia ili kuendeleza kazi Yake, kuwabariki wahitaji, na kuwasaidia walio maskini. Unaweza kutenda wema mkubwa zaidi na mali zako, kuliko unavyoweza kufanya kwa kuhubiri huku ukizuia mali zako. Je, umeweka talanta zako za mali kwa watoao riba, ili Bwana atakapokuja, aseme, "Toa hesabu ya uwakili wako," unaweza, bila kuchanganyikiwa, kumtolea talanta maradufu, yaani yote mtaji na riba pamoja, kwa sababu hujajilimbikizia, haujazizika kwa ubinafsi katika ardhi, lakini umeziweka kazini? Angalia katika historia ya maisha yako ya zamani. Je, umebariki wangapi kwa mali zako? Je, ni mioyo mingapi umeifanya iwe na shukrani kwa ukarimu wako? Tafadhali soma sura ya hamsini na nane ya Isaya. Je, umefungua vifungo vya uovu? Je, umetafuta kutua mizigo mizito, kuwaweka huru wanaoteseka, na kuvunja kila nira? Je, umewagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Je, umewavika walio uchi? {2Tsw 684.2}

Ikiwa umekuwa tajiri katika haya matendo mema, unaweza kudai ahadi zilizotolewa katika sura hii: "Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, Naye atasema, Mimi hapa." "Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui." Lakini sasa huna sifa ya kupata baraka hizi zilizoahidiwa. Hujajishughulisha katika kazi hii. Angalia nyuma katika maisha yako ya zamani na fikiria jinsi yanavyokosa matendo mema, bora, ya uungwana na maadilifu ya ukarimu. Umezungumza kuhusu Kweli, lakini haujaiishi. Maisha yako hayajainuliwa na kutakaswa, lakini yamekuwa na sifa ya ubinafsi na ubahili. Umeitumikia nafsi kwa uaminifu. Sasa ni wakati

ambao unaopaswa kubadili mwendo wako na kufanya kazi kwa bidii kupata hazina ya mbinguni. {2Tsw 684.3}

Umepoteza mengi ambayo huwezi kupata tena. Hujaboresha fursa zako za kutenda mema, na kukosa kwako uaminifu kumeandikwa kwenye vitabu vya mbinguni. Maisha ya Kristo yalikuwa na sifa ya kujikana nafsi, kujitoa kafara, na ukarimu usio na ubinafsi. Hauchukui mtazamo sahihi wa maandalizi muhimu kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Mawazo yako ni finyu sana. Ni rahisi kubwatika maneno matupu yasiyo na matendo (talk is cheap); hayo maneo hayana gharama kubwa. Kazi, na matunda, vitaamua tabia ya mti. Je, umezaa matunda gani? Mtume Yakobo anawahimiza ndugu zake: “Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa? Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?” Kuwatakia mema kwako tu ndugu yangu, hayakutaleta mahitaji yao. Matendo lazima yashuhudie Ukweli wa huruma na upendo wako. Je, ni mara ngapi umebeba kilichowakilishwa hapo juu katika waraka? {2Tsw 685.1}

Una ukadiriaji mzuri sana kuhusu mwenyewe, lakini unayo kazi ya kufanya ambayo hakuna mtu mwingine anayeweza kukufanyia. Asili yako lazima ibadilishwe, na lazima kuwe na badiliko la nafsi yote kwa ujumla. Wewe unaipenda ile Kweli kwa Neno, lakini si kwa tendo. Unampenda Bwana kidogo, lakini utajiri wako zaidi. Je, Bwana angeweza kukwambia wewe, ikawa atakukuta kama ulivyo kwa wakati huu. “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ..... ingia katika furaha ya Bwana wako?” Je, ni furaha gani imetajwa hapa? “Ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.” Furaha iliyowekwa mbele ya Yesu ilikuwa ile ya kuona roho zikikombolewa kwa dhabihu ya utukufu Wake, heshima Yake, utajiri Wake, na maisha Yake Mwenyewe. Wokovu wa mwanadamu ulikuwa furaha Yake. Wakati wote waliokombolewa watakapokusanyika katika ufalme wa Mungu, Yeye ataona mazao ya uchungu/tabu ya nafsi Yake na kuridhika. {2Tsw 686.1}

Wale ambao ni watendakazi pamoja na Kristo, washirika pamoja Naye katika kujikana nafsi na dhabihu Yake, wanaweza kuwa chombo cha a kuleta roho kwa Kristo, na kuwaona wakiokolewa, wakiokolewa milele, na kumsifu Mungu, na Mwana-Kondoo aliyewakomboa.

Pleasanton, Kansas,  
Oktoba 15, 1870.-{2Tsw 686.2}

## SURA YA 80

### HAKUNA REHEMA BAADA YA KRISTO KUJA

Ndugu O: Wakati ninaandika hatari za wengine, habari yako inazisonga akili zangu. Kwa miezi kadhaa nimekuwa nikitafuta nafasi ya kukuandikia wewe na wengine; lakini kazi ya kudumu imenizuia kuandika shuhuda zote nilizopewa kwa watu binafsi. {2Tsw 686.3}

Habari yako mara nyingi imelemea akili yangu, lakini sijahisi wazi kukuandikia. Nimeandika shuhuda nyingi sana ambazo zimetolewa kwa wengine, ambazo zingine, kwa namna nyingi, zingeweza kutumika kwako. Lengo la kuchapisha Shuhuda ni kwamba wale ambao hawajazungumziwa kwa ubinafsi, lakini ambao wana makosa kama wale wanaokemewa, waweze kuonywa kupitia makaripio waliyopewa wengine. Nilidhani lisingekuwa jukumu langu kukuandikia wewe binafsi. Walakini, ninapoandika Shuhuda za mtu binafsi kwa wale walio katika hatari ya kupuuza wajibu wao kwa kazi ya Mungu, na hivyo kupata jeraha, na hasara, kwa roho zao wenyewe, sijisikii amani kuacha kesi yako bila kukuandika wewe. {2Tsw 687.1}

Mtazamo wa mwisho niliopewa ulikuwa juu ya miaka miwili iliyopita. Kisha niliagizwa kuleta kanuni za jumla, kwa kusema na kwa maandishi, na wakati kuzizungumzia hatari, makosa, na dhambi za watu binafsi, ili wote wapate kuonywa, kukemewa, na kushauriwa. Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao binafsi. {2Tsw 687.2}

Wale ambao wana mapenzi ya asili kwa ulimwengu na ambao wamepuuzia jukumu lao wanaweza kuona wao wenyewe makosa yaliyoainishwa katika kesi za wengine ambao wamekemewa. Mungu hupanga kujaribu imani ya wote ambao wanadai kuwa wafuasi wa Kristo. Yeye Atajaribu uaminifu wa maombi ya wale wote wanaodai kwa bidii hamu ya kujua wajibu wao. Atafanya kazi iwe wazi. Atawapa wote nafasi ya kutosha kukuza kilicho mioyoni mwao. Mgogoro utakuwa karibu kati ya nafsi yako na neema ya Mungu. Ubinafsi utajitahidi kuinua mapembe na utapingwa na kazi ya kuleta maisha na mawazo, mapenzi na nia, chini ya mapenzi ya Kristo. Kujikana mwenyewe na msalaba husimama wakati wote katika njia ya uzima wa milele, na, kwa sababu ya hii, "ni wachache tu ambao wanaipata." {2Tsw 687.3}

Mungu anajaribu taibia za wote. Anathibithisha upendo wao kwa kusudi Lake na kwa kutangaza kwa Ukweli ambao wanadai kuwa wanauzingatia kwamba una thamani isiyo na kifani. Mtafuta mioyo anahukumu, kwa matunda wanayozaa, kwamba ni nani ambao ni Kweli wafuasi wa Kristo; ni nani ambao kama Mfano wao wa Mbinguni, watakataa heshima na hazina za ulimwengu, na wakiridhia kutokuwa na hadhi yoyote, wakichagua upendeleo wa Mungu na msalaba wa Kristo, ili hatimaye, wapate utajiri wa Kweli, hazina iliyowekwa mbinguni, malipo ya thawabu - utukufu wa milele. {2Tsw 688.1}

Wale ambao hawataki kabisa kujitambua wenyewe, wataruhusu maonyo na makaripio kutolewa na kwenda kwa wengine, na hawatatambua kuwa kesi zao wenyewe zimekwishashughulikiwa, makosa yao na kwamba hatari yameonyeshwa tayari. U dunia na ubinafsi umezipofusha akili na kwa hivyo hufanya kazi kwa nafsi kiasi kwamba hawawezi kufanywa upya katika sura ya Mungu. Wale ambao kwa tabia zao mbaya za asili na hawapingi mapenzi Yake, hawataachwa gizani, lakini watafanywa upya katika maarifa na utakatifu wa Kweli, na hata watautukuza msalaba wa Kristo. {2Tsw 688.2}

Nimeonyeshwa kuwa, kwa wakati unaofaa, Mungu angeshinikiza mzigo juu yangu kusema kwa watu binafsi, kama vile Nathani alivyomwambia Daudi: "Wewe ndiye mtu huyo." Wengi inaonekana wanaamini Shuhuda unaoletewa wengine na, kama Daudi, wanatoa hukumu wakijirejelea wenyewe, wakati wanapaswa kuchunguza mioyo yao wenyewe kwa kuchambua maisha yao wenyewe, na kufanya matumizi kwa vitendo, kwa yale maonyo na makaripio wanayopewa wengine kwa ukaribu. {2Tsw 688.3}

Ndugu O, nimeonyeshwa kuwa mapenzi yako yapo juu ya hazina yako ya kidunia kuliko busara yako inavyofikiri. Umechanganyikiwa katika maoni yako ya wajibu. Na wakati Roho wa Mungu anafanya kazi juu ya akili yako na kukuongoza wewe kufanya kile ambacho kinaendana na mapenzi na matakwa ya Mungu, ushawishi mwingine ambao hauna mapatano na kazi ya Mungu kwa wakati huu unakuzuia kutii mapenzi ya Mungu; matokeo ni kwamba, imani yako haikamilishwi kwa matendo. Mapenzi yako yanapaswa kuondolewa kutoka kwa hazina ya kidunia. Wakati mwingine, kinyume cha matakwa yako, mali zilikuwa zikitoka kwako na kwenda kwa safu ya adui, na kwa hivyo kusudi la Mungu lilipoteza mali hizo, umeonekana kufadhaika sana na kusumbuka. Vipaji vya mali vimekabidhiwa kwako na Mwalimu ili kuviboresha kwa utukufu Wake. Wewe ni msimamizi/wakili Wake na unapaswa kuwa mwangalifu, usije ukapuuza wajibu wako. Kwa asili wewe ni mtu wa kupenda ulimwengu na utakuwa na mwelekeo wa kudai kwamba talanta ya mali ni zako mwenyewe japo ulipewa utunze.

Lakini, sauti ya "Toa hesabu ya uwakili wako " itasikika kwako siku ya mwisho ya hukumu. {2Tsw 688.4}

Watoto wa Mungu wana hekima wakati wanaitumainia hiyo hekima Yake peke yake ambayo hutoka juu, na hawana nguvu zaidi ya ile inayotoka kwa Mungu. Kujitenga na urafiki na roho ya Ulimwengu ni lazima kwetu ikiwa tutaunganishwa na Bwana na kukaa ndani Yake. Nguvu zetu na mafanikio yetu uhusika na kushikamana na Bwana, kuchaguliwa na kukubaliwa Naye. Hakuwezi kuwa na muungano kati ya nuru na giza. Mungu anakusudia kwamba watu Wake wawe wa kipekee, waliojitenga na ulimwengu, na kuwa mifano hai ya utakatifu, ili ulimwengu upate kuangazwa, kusadikishwa, au kuhukumiwa, kwa kadiri wanavyoshughulika na nuru waliyopewa. Ukweli ambao umeletwa mbele ya uelewa wao, nuru ambayo imeangaza juu ya roho, utahukumu na kulaani ikiwa utapuuzwa au kuuachwa. {2Tsw 689.1}

Katika zama hizi zilizopotoka, makosa na giza hupendelewa kuliko nuru na Kweli. Kazi za wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, hazitastahimili jaribio wakati zitakapochunguzwa na nuru ambayo sasa inawaangazia. Kwa sababu hii, wengi hawaji kwenye nuru, isije kudhihirika kwamba kazi zao hazifanywi ndani ya Mungu. Nuru hugundua, hufunua, uovu uliofichwa chini ya giza. Watu wa dunia na watu walio watumishi wa Kristo kwa kweli, wanaweza kuwa sawa kwa mwonekano wa nje; lakini ni watumishi wa mabwana wawili ambao masilahi yao yanapingana kwa kuazimia. Ulimwengu hauelewi wala kutambua tofauti; lakini kuna umbali mkubwa, utengano mkubwa, kati yao. {2Tsw 689.2}

Anasema Kristo: "Ninyi si wa ulimwengu, bali Mimi naliwachagua katika ulimwengu." Wafuasi wa Kweli wa Kristo hawezi kufurahia urafiki wa ulimwengu na wakati huo huo maisha yao yamefichwa pamoja na Kristo. Mapenzi, lazima yaondolewe kutoka hazina za dunia na kuhamishiwa kwenye hazina ya mbinguni. Ilikuwa vigumu kiasi gani kwa yule kijana aliyekuwa na mali nyingi, kuondoa mapenzi yake kwa hazina yake ya kidunia, hata kwa ahadi ya uzima wa milele mbele yake kama thawabu yake! {2Tsw 690.1}

Wakati vyote tulivyo navyo haviwekwi wakfu kwa Mungu, masilahi ya ubinafsi hutufumba macho ili tusione umuhimu wa kazi, na mali Mungu anazotaka zinazuiliwa. Lakini Yeye ambaye ametukopesha mali hizi kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake, mara nyingi ataondoa mkono Wake unaostawisha na kwa njia fulani atapanya mali zilizozuiliwa, na zitapotea toka kwa anayezimiliki na kupotelea kutoka kwa kazi ya Mungu. Hazihifadhiwi katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao. Mungu anaibiwa, na Shetani anashinda. Bwana angependa wewe uchunguze kwa karibu moyo wako mwenyewe, Ndugu O, na kuondoa upendo wa ulimwengu ndani yake. Ifie nafsi yako, na kuishi kwa ajili ya Mungu. Ndipo utakuwa katika idadi ya wale ambao ni nuru ya ulimwengu. {2Tsw 690.2}

Nimeoneshwa kuwa ulikuwa unapendelea maoni yenye makosa kwa habari ya siku za usoni, maoni yanayoashiria fikra zilizo danganyifu kuhusiana na zama zinazokuja. Wakati mwingine unayatoa maoni haya kwa wengine. Lakini hayapatani na mwili [wa Kristo]. Hautumii kwa usahihi Maandiko. Wakati Yesu anapoinuka katika Patakatifu sana, na kuweka kando mavazi Yake ya kikuhani, na kuyavaa mavazi ya kisasi, badala ya mavazi ya kikuhani, kazi kwa ajili wenye dhambi itakuwa imemalizika. Kipindi cha wakati kitakuwa kimewadia ambapo agizo litatolewa: Yule “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; . . . na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Tazama, Naja upesi, na ujira Wangu U pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.” {2Tsw 690.3}

Mungu ametoa Neno Lake kwa wote kuchunguza, ili wapate kujifunza njia ya uzima. Hakuna anayehitaji kukosea ikiwa atajitiisha kwa masharti ya wokovu yaliyowekwa katika Neno la Mungu. Rehema imetolewa kwa wote, ili wote waweze kujenga tabia kwa uzima wa milele. Fursa itatolewa kwa wote ili kuamua kwa ajili uzima au mauti. Wanadamu watahukumiwa kulingana na kipimo cha nuru waliyopewa. Hakuna atakayewajibika kwa giza lao na makosa yao ikiwa nuru haikuletwa kwao. Hawakutenda dhambi kwa kutokupokea kile ambacho hawakupewa. Wote watajaribiwa kabla Yesu hajaacha nafasi Yake katika Patakatifu pa Patakatifu. Mlango wa rehema unafungwa

wakati maombezi kwa wenye dhambi unamalizika na mavazi ya kisasi yanavaliwa. {2Tsw 691.1}

Wengi wanapokea wazo kwamba rehema inatolewa baada ya Yesu kuacha kazi Yake kama mpatanishi katika chumba cha Patakatifu pa Patakatifu. Haya ni madanganyo ya Shetani. Mungu hujaribu na kuuthibitisha ulimwengu kwa nuru ambayo anapendezwa kuwapa kabla ya kuja kwa Kristo. Ndipo tabia zinajengwa kwa uzima au mauti. Lakini rehema kwa wale wanaochagua kuishi maisha ya dhambi, na kupuuza wokovu mkubwa uliotolewa, huisha wakati huduma ya Kristo inapokoma, kabla tu ya kuonekana Kwake katika mawingu ya mbinguni. {2Tsw 691.2}

Wale wanaoupanda ulimwengu, na ambao mawazo yao ni ya tamaa za kimwili na wana uadui dhidi ya Mungu, watajidanganya kwamba kipindi cha rehema kitatolewa baada ya Kristo kuonekana katika mawingu ya mbinguni. Moyo wenye matendo ya kimwili, unaochukia sana kujisalimisha na kutii, hudanganywa na wazo hili la kupendeza. Wengi watabaki katika usalama wa matendo ya kimwili na kuendelea katika uasi dhidi ya Mungu, wakijidanganya kwamba kutakuwa na wakati wa kutubu dhambi na fursa kwa ajili yao kuipokea Kweli ambayo sasa haipendwi na inaenda dhidi ya mwelekeo na tamaa zao za asili. Wakati watakapokuwa hawana chochote cha kuhatarisha, na hakuna cha kupoteza, kwa kutoa utii kwa Kristo na Kweli, ndipo wanadhani watachukua nafasi yao kwa ajili ya wokovu. {2Tsw 691.3}

Katika Maandiko kuna mambo ambayo ni magumu kueleweka na ambayo, kulingana na lugha ya Petro, wale wasiojifunza na wasio imara huyapotoa kwa uharibifu wao wenyewe. Inawezekana katika maisha haya, tusiweze kuelezea maana ya kila kifungu cha Maandiko; lakini hakuna hoja muhimu za Kweli na halisia ambao zitafunikwa na fumbo. Wakati utakapofika, katika majaliwa ya Mungu, ili ulimwengu ujaribiwe katika Kweli kwa wakati huo, akili zitatumiwa na Roho Wake kuchunguza Maandiko, hata kwa kufunga na kwa kuomba, hata kiunganisha baada ya kiunganishi kitafutwe na kuunganishwa kikamilifu. Kila jambo linalohusu wokovu wa roho mara moja



litawekwa wazi kabisa ili asiwepo hata mmoja atayekosea au kutembea gizani. {2Tsw 692.1}

Kama tulivyofuata mnyororo wa unabii, Ukweli uliofunuliwa kwa wakati wetu umeonekana wazi na kuelezewa. Tunawajibika kwa upendeleo tunaoufurahia na kwa nuru inayoangazia njia yetu. Wale walioishi katika vizazi vilivyopita waliwajibika kwa nuru iliyoruhusiwa iangaze juu yao. Akili zao zilitendewa kazi kwa hoja tofauti-tofauti za Maandiko ambazo ziliwajaribu na kuwapa changamoto. Lakini hawakuzielewa Kweli tulizonazo sasa. Hawakuwajibika kwa nuru ambayo hawakuwa nayo. Walikuwa na Biblia, kama sisi; lakini wakati wa kufunuliwa kwa Kweli za pekee kuhusiana na matukio ya kufunga ya historia ya dunia, hizi ni za wakati wa vizazi vya mwisho vitakavyoishi juu ya nchi. {2Tsw 692.2}

Kweli maalum zimepokelewa na kuratibiwa kulingana na hali za vizazi kama vilivyokuwepo. Ukweli wa sasa, ambao ni kipimo/jaribu kwa watu wa kizazi hiki, haukuwa kipimo/jaribu kwa watu wa vizazi vya nyuma sana. Ikiwa nuru ambayo sasa inatuangazia kuhusu Sabato ya amri ya nne, wangepewa vizazi vya zamani, Mungu angewataka watoe hesabu kwa nuru hiyo. {2Tsw 693.1}

Wakati hekalu la Mungu lilipofunguliwa mbinguni, Yohana aliona katika njozi takatifu daraja la watu ambao usikivu wao ulivutwa na ambao walikuwa wakitazama kwa kicho kwenye Sanduku la Agano, ambalo lilikuwa na sheria ya Mungu. Kipimo maalum juu ya Amri ya Nne hakikuja mpaka baada ya hekalu la Mungu lilipofunguliwa mbinguni. {2Tsw 693.2}

Wale ambao walikufa kabla ya nuru kutolewa juu ya sheria ya Mungu na madai ya amri ya nne, hawakuwa na hatia ya dhambi ya kukiuka Sabato ya siku ya saba. Hekima na rehema ya Mungu katika kutoa nuru na maarifa kwa wakati unaofaa, kama watu wanavyohitaji, haichunguziki. Kabla ya kuja Kwake, kuhukumu ulimwengu kwa haki, Yeye anatuma onyo la kuwaamsha watu na kuwaita wazingatie kupuuza kwao amri ya nne, ili waweze kuangaziwa nuru, na kutubu uasi wao wa sheria Yake, na kuthibitisha utii wao kwa Mtoa sheria Mkuu.

Bwana Ametoa majaliwa ili wote wawe watakatifu na wenye furaha wakichagua. Nuru ya kutosha ambayo imepewa kizazi hiki, ili tuweze kujifunza na kujua majukumu na upendeleo wetu ni nini, na kufurahia Kweli za thamani na dhati katika usahili wake na nguvu. {2Tsw 693.3}

Tunawajibika tu kwa nuru inayotuangazia. Amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu vinatujaribu. Ikiwa tu waaminifu na watiifu, Mungu atatufurahia, na kutubariki kama watu Wake wa pekee waliochaguliwa. Imani kamilifu na upendo kamili na utii vikidumu, vikitenda kazi katika mioyo ya wale ambao ni wafuasi Kristo, watakuwa na mvuto wenye nguvu. Nuru itatokea kwao, ikifukuza giza karibu nao, ikisafisha na kuwainua wote wanaokuja katika eneo lao la mvuto, na kuwaleta katika ujuzi wa Kweli wale wote walio tayari kuangaziwa nuru na kufuata njia ya unyenyekevu ya utiifu. {2Tsw 693.4}

Wale ambao wana mawazo ya tamaa za kimwili hawawezi kuelewa nguvu takatifu ya Kweli muhimu, ambayo wokovu wao hutegemea, kwa sababu wanapenda kiburi cha moyo, kupenda ulimwengu, kupenda raha, ubinafsi, maisha rahisi, tamaa, wivu, husuda, tamaa, chuki, na kila uovu. Ikiwa wangeyashinda haya wanaweza kuwa washiriki wa asili ya Kiungu. Wengi huacha Kweli iliyo wazi ya Neno la Mungu na kupuuza kufuata nuru ambayo inaangazia kwa wazi njia yao; wanajaribu kuchunguza siri ambazo hazijafunuliwa wazi na kubahatisha, kuzungumza na kulumbana juu ya maswali ambayo hawatakiwi kuelewa, kwa kuwa hayana rejea maalum kwa ajili ya wokovu wao. Maelfu wamedanganywa katika njia hii na Shetani. Wamepuuza imani ya sasa na wajibu wa sasa ambavyo viko wazi na vyenye maarifa mengi kwa wote wenye nguvu zao za fikira, na hueleweka kirahisi; wametafakari nadharia zenye mashaka na Maandiko ambayo hawajaweza kuelewa, nao wamekosea kuhusu imani; wana imani yenye michanganyiko (unitarian nk). {2Tsw 694.1}

Mungu angetaka wote watumie kwa vitendo mafundisho dhahiri ya Neno Lake kuhusiana na wokovu wa mwanadamu. Ikiwa wao ni watendaji wa Neno, ambalo liko wazi na lenye nguvu katika usahili wake, hawatashindwa kukamilisha tabia ya Kikristo. Watatakaswa kupitia Kweli, na kwa utii mnyenyekevu kwayo, itawapatia uzima wa

milele. Mungu anataka watumishi walio wa Kweli, sio kwa maneno tu, bali kwa matendo. Matunda yao yataonesha Ukweli wa imani yao. {2Tsw 694.2}

Ndugu O, utakuwa chini ya majaribu vya Shetani ikiwa utaendelea kupenda mawazo yako potofu na yenye makosa. Imani yako itakuwa imani mchanganyiko (mixed faith), na utakuwa katika hatari ya kuchanganya akili za wengine. Mungu anataka watu Wake wawe kitu kimoja-umoja. Maoni yako ya kipekee yataleta maaumivu katika ushawishi wako; na ikiwa utaendelea kuyathamini na kuyazungumzia hayo, mwishowe yatatumikia kukutenga na ndugu zako. Ikiwa Mungu ana nuru ambayo ni muhimu kwa wokovu wa watu Wake, atawapa kama vile alivyotoa Kweli zingine kuu na muhimu. Hapa unapaswa kuachana na mawazo yako-yapumzishe mawazo yako. Acha Mungu afanye kazi kwa njia Yake Mwenyewe kutimiza makusudi Yake kwa muda na njia Yake Mwenyewe. Hebu Mungu akuwezeshe kutembea katika nuru kama Yeye alivyo katika nuru. {2Tsw 694.3}

## **SURA YA 81**

### **UWAJIBIKAJI KWA NURU ILIYOPOKELEWA**

Nimeoneshwa habari ya Ndugu P. Alikuwa amesimama kwa muda akiipinga Kweli. Dhambi yake haikuwa kwamba hakupokea kile ambacho alichوامini kwa dhati kuwa ni makosa, lakini kwamba hakuchunguza kwa bidii na kupata maarifa ya kile alichokuwa anakipinga. Alichukulia kirahisi bila uchunguzi kuwa Waadventista wanaoitunza Sabato, kama kanisa, walikuwa na makosa. Wazo hili lilikuwa katika mapatano na hisia zake, naye hakuona umuhimu wa

kujitafutia mwenyewe kwa kutafuta kwa uadilifu/bidii Maandiko kwa maombi ya dhati. Ikiwa angefuata mwendo huu sasa angeweza kuwa mbele sana ya mahali alipo sasa. Amekuwa mzito sana kupokea ushahidi na mwenye kupuuza sana katika kuyachunguza Maandiko ili kuona ikiwa mambo haya ndivyo yalivyo. Paulo hakuona watu wana namna hii wanastahili kupongezwa, wale ambao walipinga mafundisho yake kwa kadri walivyoweza mpaka kulazimishwa kwa ushahidi mwingi kuamua kukubaliana mafundisho aliyofundisha na ambayo alikuwa amepokea kutoka kwa Mungu. {2Tsw 695.1}

Paulo na Sila walifanya kazi katika sinagogi la Wayahudi huko Thesalonike kwa mafanikio ya kiasi fulani; lakini Wayahudi wasioamini hawakufurahia sana, na kusababisha usumbufu, na wakafanya ghasia kubwa dhidi yao. Mitume hawa waliojitolea walilazimika kuondoka Thesalonike wakati wa usiku na kwenda Beroia, ambapo walikaribishwa kwa furaha. Wanazungumza wakimpongeza Waberoya hivi: “Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile Neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza Maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo. Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini.”{2Tsw 695.2}

Ndugu P ameshindwa kuona umuhimu wa swali hilo. Hajahisi mzigo unaomsonga ili achunguze kwa bidii, bila kumtegemea mtu yeyote, ili kujua Kweli ni nini.

Amemwazia sana Mzee P, na hajahisi umuhimu wa kujifunza kwa Yeye ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo. Amekuwa mtu asiyefundishika, lakini mwenye kujiamini mwenyewe. Mwokozi wetu hana maneno ya kuwapongeza wale ambao ni wazito wa moyo kuamini katika siku hizi za mwisho, zaidi ya yale aliyokuwa nayo kwa Tomaso mwenye kuona shaka, aliyejigamba kwamba hataamini juu ya ushahidi ambao wanafunzi waliousimulia, na ambao walisema, kwamba Kristo alikuwa amefufuka Kweli na kuwatokea. Tomaso alisema: “Mimi nisipoziona mikononi Mwake kovu za misumari,” “na kutia kidole changu katika mahali pa misumari, na kutia mkono wangu katika ubavu Wake, mimi sisadiki hata kidogo.” Kristo alimpatia Tomaso ushahidi alioutangaza kwamba ni lazima aupate; lakini

alimwambia kwa kumkemea: “Wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye.” Tomaso alikubali kusadikishwa. Yesu akamwambia: “Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki.” {2Tsw 696.1}

Msimamo wa Ndugu P umemfanya kuwa mtu dhaifu. Alidumu kwa muda mrefu kabisa, akipigana dhidi ya kila kitu isipokuwa Sabato. Wakati huo huo alikuwa akishirikiana na wavunja amri, akiwa bado anatajwa na Waadventista ambao walikuwa wanapinga vikali Sabato ya amri ya nne. Hakuwa katika hali yoyote ya kuwasaidia kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa katika hali ya kusita. Mvuto wake umewathibitisha wengi katika kutokuamini kwao. Pamoja na msaada wote, ushahidi, na kutiwa moyo alivyovipata, kusimama kwake nyuma hakujampendeza Bwana, wakati ambapo kumeimarisha mikono ya wale waliokuwa wanapigana dhidi ya Mungu, kwa kuipinga Kweli. {2Tsw 696.2}

Ndugu P sasa anaweza kuwa mtu hodari mwenye ushawishi kwa watu wa Mungu huko Maine na mwenye kuheshimiwa katika upendo kwa ajili ya kazi zake. Lakini anaelekea katika wazo kwamba kurudi nyuma kwake kuna jambo jema maalumu, badala ya kuiona ni dhambi ambayo ni lazima aitubu. Amekuwa mzito sana kujifunza masomo ambayo Mungu amekusudia kumfundisha. Hajawa msomi/mwanafunzi mwepesi, na hajawa na ukuaji na uzoefu katika Ukweli wa sasa, ambao ungemstahilisha kubeba uzito wa jukumu ambalo angeweza kulibeba sasa kwa uadilifu na bidii kama angepiga hatua katika nuru yote iliyotolewa. Nilioneshwa wakati ambapo Ndugu P alianza kufanya juhudi za kujitiisha na kuuzuia uchu wake; ndipo angeweza kuwa mvumilivu kwa urahisi zaidi. Alisisimshwa kwa urahisi, mwenye harara, mwepesi hasira, na mwenye huzuni moyoni. Kula na kunywa kwake kulimfanya awe katika hali hii. Tamaa za mwili zilikuwa na nguvu, zikitawala juu ya nguvu za juu za akili. Kuwa na kiasi kungemsaidia sana Ndugu P; na mazoezi zaidi ya mwili na kazi za mikono, ni muhimu kwa afya yake. Alipofanya juhudi za kujidhibiti, alianza kukua, lakini hakupokea baraka hiyo katika juhudi zake za kupiga hatua ambayo angepata ikiwa zingefanywa katika kipindi cha nyuma. {2Tsw 697.1}

Badala ya kukusanya pamoja na Kristo katika Kweli, kwa muda mrefu sana alirudi nyuma; alikuwa hapigi hatua za kwenda mbele zaidi na alisimama moja kwa moja katika njia ya maendeleo ya wengine, na hivyo kutapanya mbali. Mvuto wake umesimama moja kwa moja katika maendeleo ya kazi ambayo Mungu aliwatuma watumishi Wake kuifanya. {2Tsw 697.2}

Mawazo ya Ndugu P ya utaratibu na mpangilio yamekuwa yakipingana moja kwa moja na mpango wa Mungu wa utaratibu. Kuna utaratibu mbinguni, na unapaswa kuigwa na wale walio duniani, ambao ni warithi wa wokovu. Kadri wanadamu wanavyofikia kwa karibu zaidi utaratibu na mpangilio wa mbingu, ndivyo karibu zaidi wanavyoletwa katika hali ile inayokubalika mbele za Mungu itakayowafanya kuwa raia wa ufalme wa mbinguni na kuwapa kule kufaa kwa kutwaliwa toka duniani kwenda mbinguni, ambayo Henoka alikuwa nayo kabla ya kutwaliwa yake. {2Tsw 697.3}

Ndugu P anapaswa kulindwa. Kuna ukosefu wa utaratibu katika utaratibu wake. Hayuko katika mapatano na huko kujizuia, huko kujali na bidii, ambavyo ni muhimu ili kuhifadhi mapatano na umoja wa tendo. Uzoefu wake, elimu yake katika mambo ya kidini kwa miaka iliyopita, vimekuwa na athari kubwa kwa watoto wake wapendwa na hasa kwa watu wa Mungu. Majukumu ambayo Mbingu imeweka juu ya baba, na hasa juu ya mchungaji, yeye hajayatambua. Mtu ambaye ana udhaifu katika kuyatambua majukumu yake kama baba la kuhimiza, kutia moyo na kusimamia utaratibu, nidhamu, na utii, atashindwa kama mhudumu na kama mchungaji wa kundi. Upungufu huo huo ulio katika usimamizi wake nyumbani katika familia yake utaonekana katika nafasi ya umma/hadhara zaidi katika kanisa la Mungu. Makosa yatadumu bila kusahihishwa kwa sababu ya matokeo mabaya yanayohitaji karipio na wito wa dhati. {2Tsw 698.1}

Matengenezo makubwa yanahitajika katika familia ya Ndugu P. Mungu hapendezwi na hali yao ya sasa ya machafuko, wana njia yao wenyewe, wakifuata mwenendo wao wenyewe. Hali hii ya mambo katika familia yake husababisha ukinzani wa ushawishi wake popote anapojulikana. Pia ina athari ya kuwavunja moyo wale wenye nia ya kumsaidia katika

kutegemeza familia yake. Ukosefu huu ni jeraha katika kazi. Ndugu P hawazuii watoto wake. Mungu hapendezwi na njia zao zisizo na utaratibu, zenye machafuko, na mwenendo wao ambao haujatakaswa. Yote haya ni matokeo ya, au laana inayofuata, uhuru usio na mipaka ambao Waadventista wamedai kuwa ilikuwa upendeleo wao uliobarikiwa, kufurahia. Ndugu na Dada P wametamani wokovu wa watoto wao, lakini nikaona kwamba Mungu hatafanya muujiza katika uongofu wao wakati kulikuwa na majukumu yaliyokuwa juu ya wazazi ambayo walikuwa wanatambua kwa kiasi kidogo. Mungu amewaachia wazazi hawa kazi ya kufanya ambayo wamemrudishia Yeye ili awafanyie. Wakati Ndugu na Dada P wanahisi mzigo wanaopaswa kuhisi kwa ajili ya watoto wao, wataunganisha juhudi zao ili kuweka utaratibu, nidhamu, na kujizuia kamili, kunakoleta afya katika familia zao. {2Tsw 698.2}

Ndugu P, umekuwa mvivu katika kubeba mizigo ambayo kila baba anapaswa kuibeba katika familia yake; na, kama matokeo, mzigo ambao ameachiwa mama kubeba umekuwa mzito sana. Umekuwa tayari sana kutoa udhuru kutoka katika wajibu na mizigo nyumbani na nje ya nyumbani. Kwa hofu ya Mungu, kwa umakini wa akili, kwa kuzingatia hukumu, pokea mzigo ambao mbingu imepanga uuchukue, na unapokuwa umefanya yote unayoweza kwa upande wako, basi unaweza kuomba kwa kuelewa, kwa Roho, na kwa imani, ili Mungu afanye kazi hiyo kwa watoto wako ambayo ni zaidi ya uwezo wa mwanadamu kufanya. {2Tsw 699.1}

Ndugu P hajatumia mali kwa busara. Maamuzi ya busara hayajamshawishi kama vile sauti na matakwa ya watoto wake. Hawekei makadirio anayopaswa juu ya fedha/mali iliyo mikono mwake na kuitumia kwa uangalifu katika vile/vikorokoro vinavyohitajika zaidi, kwa mambo ambayo lazima awe nayo kwa faraja na afya. Familia nzima inahitaji kupiga hatua katika suala hili. Vitu vingi vinahitajika katika familia kwa ajili ya kurahisisha mambo na faraja. Ukosefu wa kutopenda utaratibu na mfumo katika mpangilio wa masuala ya familia husababisha uharibifu na kuleta hasara kubwa. Kila mwanafamilia anapaswa kutambua kuwa jukumu liko juu yake binafsi, kufanya sehemu yake ili kuongezea faraja, utulivu, na utaratibu wa familia (na

kupunguza usumbufu). Mtu hapaswi kutenda kinyume cha mwenzake. Wote kwa umoja wanapaswa kushiriki katika kazi njema ya kutiana moyo; wanapaswa kuonesha upole, ustahimilivu, na uvumilivu, kuzungumza kwa sauti ya chini, tulivu, kuepuka machafuko, na kila mmoja akifanya kila awezalo kupunguza mzigo wa mama. Mambo hayapaswi kuachwa bila kushughulikiwa, au kuachwa kiholela, wote wakitoa udhuru kutotimiza wajibu, na kuwaachia wengine wafanye kile wanachoweza na wanachopaswa kufanya wenyewe. Mambo haya yanaweza kuwa madogo; lakini yote yakiwekwa pamoja, huleta machafuko makubwa na kumhuzunisha Mungu (kuleta hasira ya Mungu). Ni kupuuzwa kwa mambo madogo sana, kunakoharibu furaha ya maisha. Utendaji kwa uaminifu wa mambo madogo hutengeneza jumla ya furaha inayopatikana katika maisha haya. Yeye aliye mwaminifu katika madogo ni mwaminifu pia katika mengi. Yeye ambaye si mwaminifu au dhalimu katika mambo madogo, atakuwa hivyo katika mambo makubwa zaidi. Kila mwanafamilia anapaswa kuelewa tu sehemu anayotarajiwa kutenda kwa kuungana na wengine. Wote, kuanzia mtoto wa miaka sita na zaidi, wanapaswa kuelewa kuwa wanatakiwa kubeba sehemu yao ya wajibu katika maisha. {2Tsw 699.2}

Kuna masomo muhimu kwa watoto hawa kujifunza, na wanaweza kujifunza vizuri zaidi sasa kuliko wakati wa baadaye. Mungu atafanya kazi kwa watoto hawa wapendwa kwa umoja na juhudi zilizoелеkezwa kwa busara za wazazi wao na atawaleta kuwa wanafunzi katika shule ya Kristo. Yesu angependa watoto hawa kujitenga na ubatili wa ulimwengu, kuacha anasa za dhambi, na kuchagua njia ya utiifu mnyenyekevu. Ikiwa sasa watautii mwaliko wa neema, wakampokea Yesu kama Mwokozi wao, na kufuata kumjua Bwana, atawasafisha toka dhambi zao na kuwapa neema na nguvu. {2Tsw 700.1}

Mpendwa Ndugu P, masomo uliyojifunza katikati ya mivuto inayovuruga ambayo imekuwepo huko Maine imekuwa yenye madhara sana katika familia yako. Haujawa mwenye tahadhari katika mazungumzo yako vile Mungu anavyotaka uwe. Haujadumu katika Kweli katika familia yako, kufundisha kwa bidii kanuni zake na amri za Mungu kwa watoto wako unapoamka na uketipo, utokapo na uingiapo.



Haujaithamini kazi yako kama baba au kama mchungaji/mhudumu.  
{2Tsw 700.2}

Haujatimiza wajibu wako kwa bidii kwa watoto wako. Haujatoa muda wa kutosha kwa ajili maombi ya familia, na haujataka uwepo wa nyumba nzima. Maana ya "mume" ni kamba ya kufungia nyumba Pamoja (house-band/husband). Kwa wanafamilia wote, bada ndiye kiini. Yeye ndiye mtunga sheria, akionesha kielelezo katika uwezo wake wa kiume akibeba tabia kali za wema, nguvu, uadilifu, uaminifu, uvumilivu, ujasiri, bidii, na kuwa wa manufaa kwa vitendo. Baba kwa maana moja ni kuhani wa nyumba, akiweka juu ya madhabahu ya Mungu dhabihu ya asubuhi na jioni. Mke na watoto wanapaswa kuhimizwa kuungana katika dhabihu hii na pia kushiriki katika wimbo wa sifa. Asubuhi na jioni baba, kama kuhani wa nyumba, anapaswa kuungama kwa Mungu dhambi zilizofanywa na yeye mwenyewe na watoto wake kwa siku nzima. Zile dhambi alizozijua, na pia zile za siri, ambazo jicho la Mungu pekee limezitambua, zinapaswa kuungamwa. Utawala huu wa vitendo, ukitekelezwa kwa ari na bidii na baba wakati yupo, au na mama wakati hayupo, utaleta baraka kwa familia [The meaning of "husband" is house band. All members of the family center in the father. He is the lawmaker, illustrating in his own manly bearing the sterner virtues, energy, integrity, honesty, patience, courage, diligence, and practical usefulness]. {2Tsw 701.1}

Sababu kwa nini vijana wa wakati huu hawana mwelekeo wa kidini zaidi ni kwamba elimu yao ina kasoro. Upendo wa kweli hautekelezwi kwa watoto wanaporuhusiwa kuendekeza tamaa/passion, au wakati ukiukaji wa sheria zako unaachwa bila kuadhibiwa. Tawi linapopindishwa, basi mti unaelekea huko (mkunje Samaki angali mbichi). Unapenda raha sana. Wewe si mwangalifu sana. Jitihada za kudumu zinahitajika, kukesha kwa kudumu maombi ya kina, ya bidii. Weka akili yako katika hali ya kuomba, ukiinua kwa Mungu; usiwe mvivu katika biashara, lakini mwenye bidii rohoni, ukimtumikia Bwana.  
{2Tsw 701.2}

Umeshindwa katika familia yako kuthamini utakatifu wa Sabato na kuifundisha kwa watoto wako na kuamuru juu yao umuhimu wa kuitunza kulingana na amri. Hisia zako haziko wazi na tayari kutambua

viwango vya juu ambavyo tunapaswa kuvifikia ili kuwa watunza amri. Lakini Mungu atakusaidia wewe katika juhudi zako unapoishikilia kazi hiyo kwa dhati na bidii. Unapaswa kuitawala nafsi yako kikamilifu; kisha unaweza kuwa na mafanikio bora katika kuwadhiti watoto wako wanapokuwa wakaidi au wajeuri. Kuna kazi kubwa mbele yako ya kurekebisha upuuzaji wa wakati uliopita; lakini hauhitajiki kuifanya kwa nguvu zako mwenyewe. Malaika wanaohudumia watakusaidia katika kazi hiyo. Usikate tamaa ya kazi au kuweka kando mzigo, bali ushikilie kwa nia na kurekebisha upuuzaji kwako wa muda mrefu. Ni lazima uwe na mawazo ya juu kuhusu madai ya Mungu kwako kwa habari ya siku Yake takatifu. Kila kitu kinachoweza kufanywa kwa siku sita ambazo Mungu amekupa, kinapaswa kufanywa. Haupaswi kumwibia Mungu hata saa moja ya wakati mtakatifu. Baraka kuu zimeahidiwa kwa wale ambao wanaweka makadirio ya juu katika Sabato na kutambua majukumu yaliyo juu yao kwa kuzingatia utunzaji wake: “Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.” {2Tsw 701.3}

Pale Sabato inapoanza, tunapaswa kuweka ulinzi juu yetu wenyewe, juu ya matendo yetu na maneno yetu, tusije tukamwibia Mungu kwa kuichukua kwa matumizi yetu wakati huo ambao ni wa Bwana kabisa. Tusifanye wenyewe, wala kuwaruhusu watoto wetu kufanya, aina yoyote ya kazi yetu wenyewe inayoleta riziki, au kitu chochote ambacho kingeweza kufanywa katika siku sita za kazi. Ijumaa ni siku ya maandalizi. Muda hapo unaweza kutolewa kufanya maandalizi muhimu kwa Sabato na kufikiria na kuzungumza juu Yake. Hakuna kitu ambacho mbele ya Mbingu kitachukuliwa kama ukiukaji wa Sabato takatifu, kinachopaswa kuachwa ambacho bila kusemwa au kufanywa siku ya Sabato. Mungu hahitaji tu kwamba tujiepushe nayo kazi ya kimwili siku ya Sabato, lakini akili inidhamishwe kukaa juu ya mada takatifu. Amri ya nne ni karibu kukiukwa kwa kuzungumza juu ya

mambo ya kidunia au kwa kujihusisha mazungumzo dunia yenye upuuzi. Kuzungumza juu ya chochote au kila kitu ambacho kinaweza kuja akilini ni kuzungumza maneno yetu wenyewe. Kila kupotoka kutoka kilicho sawa hutuleta katika utumwa, hatia na laana. {2Tsw 702.1}

Ndugu P, unapaswa kujinidhamisha mwenyewe ili kutambua utakatifu wa Sabato ya amri ya nne, na unapaswa kufanya kazi ili kuinua kiwango katika familia yako na mahali popote ulipokishusha, kwa mfano wako, kati ya watu wa Mungu. Unapaswa kukabiliana na mvuto ulioweka katika suala hili, kwa kubadilisha maneno na matendo yako. Umeshindwa mara kwa mara "kuikumbuka siku ya Sabato, na kuitakasa;" umesahau mara nyingi, na umenena maneno yako mwenyewe siku ya Mungu iliyotakaswa. Haujawa na tahadhari, na umejiunga katika siku ya Sabato na wasiojitoa wakfu katika mazungumzo juu ya mada za kawaida wakati huu, kama vile faida na hasara, hisa, mazao, na mahitaji. Katika hili mfano wako unadhuru mvuto wako. Unapaswa kufanya matengenezo {2Tsw 703.1}

Wale ambao hawaongoka kikamilifu katika Kweli mara nyingi huacha akili zao zitafakari kwa uhuru juu ya mambo ya kidunia, na, ingawa wanaweza kupumzika kutokana na taabu ya kimwili katika siku ya Sabato, ndimi zao huzungumza yale yaliyo katika akili zao; Hivyo maneno haya kuhusu mifugo, mazao, hasara, na faida huja akilini. Yote hii ni uvunjaji wa Sabato. Ikiwa akili inajishughulisha au kukimbia katika mambo ya kidunia, ulimi utaifunua, maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake. {2Tsw 703.2}

Mfano wa wahubiri/wachungaji unapaswa hasa kuwa wenye tahadhari katika suala hili. Siku ya Sabato wanapaswa kujikita kwa umakini na kudhamiria, katika mazungumzo yenye mada za kidini—katika Ukweli wa sasa, wajibu wa sasa, matumaini na hofu ya Mkristo, majaribu, migogoro, na mateso; kushinda hatimaye, na thawabu itakayopokelewa. {2Tsw 703.3}

Wahudumu wa Yesu wanapaswa kusimama kama wakaripiaji kwa wale ambao wanashindwa kukumbuka Sabato na kuitakasa.

Wanapaswa kuwakemea kwa upole na kwa dhati wale wanaoshiriki katika mazungumzo ya kidunia katika siku ya Sabato na wakati huo huo wanadai kuwa watunza Sabato. Wanapaswa kuhamasisha kujitoa kwa Mungu katika siku Yake takatifu. {2Tsw 704.1}

Hakuna mtu anayepaswa kujisikia yuko huru kutumia muda uliotakaswa kwa njia isiyofaa/isiyo na manufaa. Haimpendezi Mungu kwa watunza Sabato kulala wakati mwingi wa Sabato. Hawamheshimu Muumba wao kwa kufanya hivyo, na, kwa mfano wao, husema kwamba siku sita ni za thamani sana kwao kuzitumia katika kupumzika. Lazima watafute pesa, ingawa ni kwa kujinyima usingizi unaohitajika, na kisha kufidia usingizi au masaa kwa kulala masaa matakatifu. Kisha wanatoa udhuru kwa kusema: “Sabato ilitolewa kuwa siku ya kupumzika. Sitaki kujinyima pumziko ili kuhudhuria mkutano, kwa kuwa ninahitaji kupumzika.” Watu kama hao hutumia vibaya siku iliyotakaswa. Lazima, siku hiyo, wazivutie familia zao katika utunzaji/ushikaji wake kwa kukusanyika katika nyumba ya sala pamoja na wachache au na wengi, kwa jinsi itakavyokuwa. Wanapaswa kutumia muda wao na nguvu kwa mazoezi ya kiroho, ili mvuto wa Kiungu uliopo kwenye Sabato uweze kuwa nao kwa juma zima. Kati ya siku zote za juma, hakuna hata moja inayofaa sana kwa mawazo ya ibada na hisia kama Sabato. {2Tsw 704.2}

Mbingu yote iliwasilishwa kwangu kama inayotazama na kuwaangalia watu katika Sabato, wale ambao wanaoyakukubali madai ya amri ya nne na wanashika Sabato. Malaika walikuwa wanafuatilia shauku yao, na kuheshimu sana, taasisi hii takatifu. Wale waliomtakasa Bwana Mungu mioyoni mwao kwa ibada katika akili, na waliotafuta kuboresha masaa matakatifu katika kuitunza Sabato kwa kadiri ya uwezo wao, na kumheshimu Mungu kwa kuita Sabato siku ya furaha—hawa malaika walikuwa wakiwabariki haswa kwa nuru na afya, na walipewa nguvu maalum. Lakini, kwa upande mwingine, malaika walikuwa wakigeuka kutoka kwa wale ambao walishindwa kuthamini utakatifu wa siku ya Mungu iliyotakaswa, na walikuwa wakiondoa kwao nuru na nguvu zao. Niliwaona wamefunikwa na wingu, wakikata tamaa, na wakiwa na huzuni mara kwa mara. Walihisi ukosefu wa Roho wa Mungu. {2Tsw 704.3}

Ndugu Ndugu P, wakati wote unapaswa kuwa mwangalifu katika mazungumzo yako. Je, Mungu amekuita wewe uwe mwakilishi wa Kristo duniani, katika kuwasihi Kwake kwa bidii watenda dhambi wapatanishwe na Mungu? Hii ni kazi nzito, adhimu na iliyotukuka. Unapoacha kuzungumza kwenye mimbari, kazi hiyo ni mwanzo tu. Haujaondolewa katika majukumu unapokuwa nje ya mkutano, lakini bado unapaswa kudumisha kujitoa kwako kwa kazi ya kuokoa roho. Unapaswa kuwa barua iliyo hai, inayojulikana na kusomwa na watu wote. Haupaswi kufanya shauri na starehe. Raha haifai kufikiriwa. Wokovu wa roho ndio mada ya muhimu zaidi. Ni kwa kazi hii mhudumu wa injili ya Kristo anaitwa. Ni lazima adumishe kazi njema nje ya mkutano na kupamba taaluma yake kwa mazungumzo yake ya Kimbingu na mwenendo wake wenye tahadhari. Mara kwa mara, baada ya kazi yako ya mimbari kwisha na umeketi na wengine kando ili kuota moto, kwa mazungumzo yasiyo safi, umezipinga juhudi zako kwenye mimbari. Ni lazima uyaishi yale unayohubiri kama wajibu kwa wengine, na lazima ubebe, kuliko hapo kabla, mzigo wa kazi, uzito wa jukumu unaopaswa kuwa juu ya kila mhudumu/mchungaji wa Kristo. Thibitisha kazi iliyotolewa kwa mhudumu, kwa kuifuatilia kwa juhudi za kibinafsi. Shiriki kwenye mazungumzo ya busara yanayohusu Ukweli wa sasa, ukihakikisha kwa wazi hali ya akili ya wale waliopo, na kwa hofu ya Mungu ukifanya matumizi ya kivitendo ya Kweli muhimu kwa habari za wale unaohusiana nao. Umeshindwa kuwa tayari, kwa wakati ukufaa na wakati usiokufaa, kukaripia, kukemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. {2Tsw 705.1}

Kama mlinzi juu ya kuta za Sayuni, kukesha kwa kila wakati ni muhimu. Kukesha kwako hakupaswi kupungua. Jifunze mwenyewe kuweza kuzikatisha shauri familia mnapokuwa kando ya moto. Unaweza kukamilisha kufanya zaidi sana katika mwelekeo huu kuliko kazi yako ya mimbarini peke yake. Linda roho kama ambaye anapaswa kutoa hesabu. Usitoe nafasi kwa wasioamini kukushtaki kwa uvivu katika jukumu hili, kwa kupuuza kuwakatisha shauri kibinafsi. Zungumza nao kwa uaminifu, na uwasihi waikubali Kweli. “Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaokolewa, na katika wao wanaopotea; katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo

mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima.” Kama mtume anavyouona ukubwa wa kazi na majukumu mazito yanayomkabili mhubiri, anasema: “Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo? Kwa maana sisi si kama walio wengi, walighushio Neno la Mungu; bali kama kwa weupe wa moyo, kama kutoka kwa Mungu, mbele za Mungu, twanena katika Kristo.” {2Tsw 706.1}

Wale wanaoliharibu Neno, wakitoa ngano na makapi, au kitu chochote tu wanachokiona ndiyo injili, huku wakizipinga amri za Mungu, hawawezi kuzithamini hisia za mtume kama alivyotetemeka chini ya uzito wa kazi hiyo adhimu, na jukumu lake kama mhudumu wa Kristo, akiwa na hatima ya roho juu yake, ambazo Kristo alikufa juu Yake. Katika makadirio ya wahudumu wa kujitengeneza wenyewe [self made ministers] itahitaji mfano/kielelezo mdogo tu kufaa kuwa mhubiri. Lakini mtume aliweka makadirio makubwa juu ya sifa zinazohitajika ili kuwa mhudumu. {2Tsw 706.2}

Mwenendo wa mhubiri kwenye mimbari, unapaswa kuwa na umakini, usio wa hovy hovy. Hapaswi kuwa mzembe kwa Habari za mtazamo wake. Anapaswa kuwa na utaratibu na utakaso wa hali ya juu. Mungu anataka hili kwa wale walio na kazi inayowajibisha sana, ile ya kupokea Maneno kutoka katika kinywa Chake, na kuyazungumza kwa watu, kuonya na kukaripia, kusahihisha na kufariji, kama inavyoweza kuhitajika. Wawakilishi wa Mungu duniani wanapaswa kuwa katika ushirika wa kila siku Naye. Maneno yao yanapaswa kuchaguliwa, usemi wao wenye busara na uangalifu. Maneno yanayozungumzwa kwa kuborongwa mara kwa mara na wahubiri ambao hawahubiri injili kwa unyofu yanapaswa kuachwa milele. {2Tsw 706.3}

Nilioneshwa, Ndugu P, kwamba wewe kwa kawaida ni mwenye hasira, unaudhika kwa urahisi, na kwamba ulipungukiwa uvumilivu na ustahimilivu. Ikiwa uliulizwa maswali kuhusu mwenendo wako au ulihimizwa kuchukua nafasi yako katika Kweli, ulihisi kwamba haifai watu kukuharakisha. Usingesogea hata hatua moja kwa sababu tu wengine walihitaji ufanye hivyo. Ungetumia muda wako na kujichelewesha. Kama wasikilizaji wako watafuata mwendo huo huo, ungewachukulia kama wanaostahili kulaumiwa. Ikiwa wote

wangefanya kama ulivyofanya, watu wa Mungu wangehitaji miaka elfu ya duniani ili kufanya maandalizi yanayohitajika kwa ajili ya hukumu. Mungu amevumilia kwa rehema na kurudi nyuma kwako; lakini haitasaidia jibu kwa wengine kufuata mfano wako, kwa maana wewe sasa ni dhaifu na mwenye upungufu ambapo ungeweza kuwa na nguvu na sifa nzuri kwa kazi hiyo. {2Tsw 707.1}

Ndugu R angeweza kukufaa lakini kidogo. Kazi zake zilielekezwa bila busara. Alikosea hasa kwa kuvutiwa na wale waliodhani wanapaswa kuwa walimu. Kama asingegusa habari ya mhubiri huko Maine, na ikiwa angefanya kazi katika eneo jipya ambapo hakukuwa na Waadventista, wengi wangeletwa katika ujuzi wa ile Kweli. Ndugu S amekuwa akisonga mbele taratibu na akichukua nafasi ya kumpendeza Mungu zaidi kwa uvumilivu, ustahimilivu, na uthabiti; na bado kuna kazi kubwa zaidi ya kufanywa kwake, kabla ya kumfanya awe mhubiri mwenye mafanikio katika kusudi la Bwana, na kuendeleza kazi ya Mungu.

Ndugu R alivutiwa sana kwa habari yako akiwa na ari kubwa, lakini ulikataa kusaidiwa naye. Wakati na nguvu zilitolewa kwako; na mambo yalipangwa vizuri kwa faida yako maalum, ili kuondoa ubaguzi wako na kukuongoa uikubali Kweli, hadi uvivu wako na kutokuamini vikachosha uvumilivu wa Ndugu R. Kisha sifa ya kazi yake ikabadilika, na kukuhimiza ufikie uamuzi na kwenda kulingana na nuru na ushahidi uliyopokea. Juhudi hii ya dhati kwa upande wake uliuchukulia kama yenye kukunyima nafasi na kukusonga. Tabia yako ya ushupavu ilidhihirishwa; uliinuka kinyume cha mpango huu na ukakataa juhudi alizofanya kukusaidia. Hapa ulijiumiza mwenyewe, na kumvunja moyo Ndugu R, na hii ilimchukiza Mungu. Hisia zako kwa Ndugu R hazikuwa za Kikristo. Uiona fahari katika upinzani wako kwa juhudi zake kwa ajili yako. Bwana alibariki kazi ya Ndugu R katika kuwainua watu katika Jimbo la Maine. Kazi hii ilikuwa ngumu na ya kuchosha, na ulifanya sehemu yako, kuifanya iwe hivyo. Hukutambua jinsi ulivyofanya kazi kuwa ngumu kwa wale ambao Mungu alikuwa amewatuma kuiwasilisha Kweli kwa watu. Walikuwa wakizitumia nguvu zao na kuchoka katika kuwaleta watu kwenye hatua ya uamuzi kuhusu Kweli, wakati wewe na wahubiri wengine moja kwa moja mlipingana nao.

Mungu alikuwa akifanya kazi kupitia wahubiri Wake kuvuta katika Kweli, na Shetani alikuwa akifanya kazi kupitia kwako na wahubiri wengine kuwavunja moyo na kuzipinga kazi zao. Watu wale wale waolidai kuwa walinzi, na ambao, ikiwa wangesimama katika shauri la Mungu, wangukuwa wa kwanza kupokea Neno la onyo na kuwapa watu, walikuwa miongoni mwa watu wa mwisho kuikubali Kweli. Walei walikuwa mbele ya waalimu wao. Walilipokea onyo hata kabla ya walinzi kwa sababu walinzi hawakuwa waaminifu na walikuwa wakilala kwenye lindo lao. {2Tsw 707.3}

Ndugu P, unapaswa kuwa na hisia za huruma ya kindugu na upendo kwa Ndugu R, kwa kuwa alistahili hili toka kwako kuliko neno moja la kukosoa. Unapaswa kukosoa vikali mwenendo wako mwenyewe kwa sababu ulikuwa ukipambana na Mungu. Lakini umejifurahisha mwenyewe na wengine kwa gharama ya Ndugu R kwa kuhusinisha juhudi zake kwako na upinzani wako kwa kazi zake, nwea umefurahia kicheko cha furaha na nguvu, kuhusu jambo hilo. {2Tsw 708.1}

Inakuwa jukumu la kila mhudumu wa Kristo kutumia usemi mzuri, wenye busara, ambao hauwezi kushutumiwa. Nilioneshwa kwamba kazi nzito inapaswa kutekelezwa kwa wahudumu wa Kristo. Hii haiwezi kufanywa bila juhudi kwa upande wao. Ni lazima wahisi kuwa wana kazi ya kufanya kwa upande wao ambayo hakuna mtu mwingine anayeweza kuwafanyia. Ni lazima watafute kupata sifa zinazohitajika, ili kuwa wahudumu wa Kristo wenye uwezo, ili katika siku ya Mungu wasimame wakiwa huru, wakiwa hawadaiwi damu ya roho, wakiwa wametimiza wajibu wao wote kwa kumcha Mungu. Kama thawabu yao, wachungaji chini ya Mchungaji Mkuu walio waaminifu watasikia toka kwa Mchungaji Mkuu: “vema, mtumwa mwema na mwaminifu.” Kisha ataweka taji ya utukufu juu ya vichwa vyao na kuwaamuru kuingia katika furaha ya Bwana wao. Je, ni furaha gani hiyo? Ni kuangalia pamoja na Kristo, watakatifu waliokombolewa, watakapoangalia nyuma pamoja mazao ya taabu ya nafsi, kujikana nafsi kwao na kujitoa kafara kwao, kuacha kwao raha, faida ya kidunia, na kila mvuto wa kidunia, na kuchagua aibu, mateso, kudhalilisha nafsi, kazi ya kuchosha, na uchungu wa moyo/roho kwani watu watapinga shauri la Mungu dhidi ya nafsi zao wenyewe; inawakumbusha juu ya kuzitesa roho zao



mbele za Mungu, kulia kwao kati ya Patakatifu na madhabahu, na kuwa kwao tamasha kwa ulimwengu, na malaika, na kwa wanadamu. Kisha haya yote yanakoma, na matunda ya kazi zao yanaonekana; roho zinaokolewa kwa juhudi zao katika Kristo. Wahubiri ambao wamekuwa watendakazi pamoja na Kristo wanaingia katika furaha ya Bwana wao, na wameridhika. {2Tsw 709.1}

“Tukimtazama Yesu, Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu; Ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana Yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu. Hamjafanya vita hata kumwagika damu, mkishindana na dhambi.” Wahubiri wanamsahau sana Mwenye kuanzisha wokovu wao. Wanadhani wanavumilia sana, wakati wanastahimili na kuteseka kidogo tu. Mungu atatenda kazi kwa wachungaji/wahudumu ikiwa watamruhusu atende kazi kwao. Lakini ikiwa wanahisi kuwa wako sawa na hawahitaji uongofu kamili, na hawatajiona wenyewe na kufikia kipimo cha Mungu, anaweza kufanya vizuri zaidi bila kazi zao kuliko wao. {2Tsw 709.2}

Mungu anahitaji wahubiri, wapande juu na wafikie kiwango, kuonesha kuwa wamekubaliwa na Mungu, watendakazi wasiokuwa na sababu ya kutahayari. Ikiwa watakataa nidhamu hii kali, Mungu atawaachilia na kuchagua watu ambao hawatapumzika mpaka watakapokuwa kamili wakiwa na nyenzo zote za kutenda kila jambo jema. Mioyo yetu ina asili ya dhambi, na yenye uvivu katika utumishi wa Kristo; na tunahitaji kulindwa kila wakati, la sivyo tutashindwa kuvumilia ugumu kama askari wema wa Kristo; na hatutahisi umuhimu wa kulenga masumbwi/makonde yenye nguvu dhidi ya dhambi zinazotusonga, lakini bila kusita tutayakubali maoni ya Shetani kwa urahisi na kujipandishia wenyewe kiwango, badala ya kukubali kiwango safi na kilichoinuliwa ambacho Mungu amekipandisha kwa ajili yetu. {2Tsw 710.1}

Niliona kwamba wahubiri wanaoitunza Sabato wa Maine wameshindwa kuwa wanafunzi wa Biblia. Hawajahisi umuhimu wa

kujifunza kwa uadilifu na bidii Neno la Mungu kwa ajili yao wenyewe, ili waweze kufanywa kamili wakiwa na nyenzo zote za kutenda kila jambo jema.; wala hawajahisi ulazima wa kusesitiza kuchunguza Maandiko kwa karibu kwa wasikilizaji wao. Ikiwa asingekuwapo mhubiri mmoja Mwadventista wa Sabato huko Maine kupinga shauri la Mungu, yote yaliyotimizwa yangeweza kufanywa na nusu tu ya juhudi iliyotumiwa, na watu wangeweza kutolewa toka katika hali ya wasiwasi, na ya kuchanganyikiwa, na kwenda katika utaratibu, na sasa wangukuwa na nguvu ya kutosha kusimama dhidi ya mivuto pinzani. Maeneo mengi ambayo ni mapya yangekuwa yametembelewa na kazi yenye mafanikio ingefanyika, ambayo ingewaletea wengi katika ujuzi wa ile Kweli. {2Tsw 710.2}

Kazi kubwa iliyofanyika Maine imekuwa kwa wachungaji Waadventista Wasabato, kuwaleta katika nafasi sahihi. Imehitaji kazi ngumu ili kukabiliana na mvuto walioutoa wakati wanapinga shauri la Mungu dhidi ya nafsi zao wenyewe na kusimama katika njia ya wenye dhambi. Wasingeingia wenyewe, na wale ambao wangeweza kuingia, huwazuia kwa sheria na mfano. Kosa limefanywa kwa kuingia kwenye uwanja ambao kuna Wasabato, ambao kama jambo la jumla hawahisi umuhimu wowote wa kusaidiwa, lakini ambao wanaojidhania wapo katika hali nzuri na wanaoweza kuwafundisha wengine. Watendakazi ni wachache, na nguvu zao ni lazima zitumiwe kwa faida kubwa zaidi. Kazi kubwa zaidi inaweza kufanyika katika Jimbo la Maine, kama jambo la jumla, ambapo hakuna hata Mwadventista hata mmoja. Mashamba mapya yanapaswa kuingiwa; na wakati ambao mpaka sasa umetumika katika kazi ya kuchosha kwa Waadventista ambao hawataki kujifunza, unapaswa kutolewa kwa maeneo haya mapya, kwa kwenda kwenye njia kuu na vichochoro, na kufanya kazi kwa ajili uongofu wa wanadamu wasioamini. Ikiwa Waadventista watakuja na kusikia, waje. Iache njia wazi kwa ajili yao kuja ikiwa watachagua. {2Tsw 711.1}

## KIAMBATISHO

Kwenye Ukurasa 400

Maagizo Kwenye Ushuhuda Binafsi uliolekezwa Ndugu Na Dada E, Kwamba "Mayai Hayapaswi Kuwekwa Juu Ya Meza Yako," Wengine Wamechukulia kwamba Matumizi Yake ni ya Ujumla Maishani Mwa Kila Mtu. Kwamba Hili Halikukusudiwa Kuwa Fundisho La Jumla Kwa Familia Za Mazingira Ya Kawaida Inawekwa Wazi Sio Tu Kwa Mazingira Ya Kauli Yenyewe, Lakini Pia Kwa Matamko Maalumu, Yasiyopungua Matatu Yaliyochapishwa Ya Ellen G. White Ambayo Yangesahihisha Kuhusu Kutumiwa Vibaya KoKote Kwa Shuhuda Binafsi. Haya Yanapatikana Katika Shuhuda Kwa Kanisa, Gombo La 7, Ukurasa Wa 135 (1902), Huduma Ya Uponyaji, Ukurasa Wa 320 (1905), Na Shuhuda Kwa Kanisa, La 9, Ukurasa Wa 162 (1909). Tunanukuu Kauli Mbili Za Mwisho: {2Tsw 712.1}

"Ni Kweli Kwamba Watu Wenye Mwili Halisi wa Mwanadamu Na Ambao Tamaa Zake Zina Nguvu Sana Kama za Wanyama, Wanahitaji Kuepuka Matumizi Ya Vyakula Vinavyochochea Mwili. Hasa Katika Familia Za Watoto Walio Na Mazoea Ya Anasa, na Ngono Chafu, Mayai Hayapaswi Kutumiwa."—Huduma Ya Uponyaji, Ukurasa Wa 320. {2Tsw 712.2}

"Wakati Maonyo Yametolewa Kuhusu Hatari Za Ugonjwa Unaosababishwa Na Siagi, Na Uovu Wa Matumizi Huru Ya Mayai Kwa Watoto Wadogo, Lakini Tusiichukulie Hii Kama Ukiukaji Wa Kanuni Ya Kutumia Mayai Toka Kwa Kuku Ambao Wemetunzwa Vyema Na Kulisha Vyema. Mayai Yana Viini Ambavyo Ni Wakala Wa Uponyaji Katika Kukabiliana Na Kuzuia Aina Fulani Ya Sumu."—Shuhuda Kwa Kanisa, La 9, Uk. 162. {2Tsw 712.3}